

# FASIRI HURU YA BIBLIA

**UNAWWEZA KUIELEWA BIBLIA!**

***Kitabu cha Kwanza cha Ukristo:Mathayo***

NA BOB UTLEY,  
PROFESA MSTAAFU WA KANUNI ZA UFASIRI  
(UTAFASILI WA BIBLIA)

MWONGOZO WA USOMAJI WA FASIRI MFUATANO  
AGANO LA KALE, VOL.01

BIBLE LESSONS INTERNATIONAL, MARSHAL, TEXAS  
2013

# ORODHA YA YALIYOMO

Neno Toka kwa Mwandishi:Ni kwa namna gani fasiri hii inaweza kukusaidia!.....	i
Mwongozo Mzuri wa Usomaji wa Biblia: Utafiti Binafsi kwa Ukweli Uliothibitika.....	iv
Fasiri	
Utangulizi wa Mathayo.....	01
Mathayo 1.....	05
Mathayo 2.....	18
Mathayo 3.....	30
Mathayo 4.....	41
Mathayo 5.....	55
Mathayo 6.....	87
Mathayo 7.....	107
Mathayo 8.....	120
Mathayo 9.....	132
Mathayo 10.....	144
Mathayo 11.....	165
Mathayo 12.....	178
Mathayo 13.....	193
Mathayo 14.....	211
Mathayo 15.....	221
Mathayo 16.....	231
Mathayo 17.....	243
Mathayo 18.....	253
Mathayo 19.....	263
Mathayo 20.....	283
Mathayo 21.....	293
Mathayo 22.....	306
Mathayo 23.....	318
Mathayo 24.....	328
Mathayo 25.....	348
Mathayo 26.....	356
Mathayo 27.....	378
Mathayo 28.....	394

Viambatisho:

Jedwali la Tarehe na Watawala Wenye Kuhusiana na Palestina .....	402
Maelezo Fasaha ya Muundo Wa Sarufi Za Kiyunani.....	408
Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi .....	417
Kauli ya Mafundisho .....	421

# MADA MAALUM: ORODHA YA YALIYOMO

Majina Ya Uungu, 1:21.....	13
Familia ya Herode Mkuu, 2:1 .....	19
Miujiza, 2:1.....	21
Masadukayo, 2:4.....	22
Maangamizi ( <i>Apollumi</i> ), 2:13 .....	26
Yesu Mnazareti, 2:23 .....	28
Toba katika Agano la Kale, 3:2 .....	32
Moto, 3:12 .....	36
Utatu, 3:17 .....	38
Maneno ya Kiyunani kwa Majaribu na Visawe Vyake, 4:1 .....	43
Uwakilishi wa Hesabu katika Maandiko, 4:2.....	44
Uovu Binafsi, 4:5 .....	47
Ufalme wa Mungu, 4:17.....	52
Haki, 5:6 .....	60
Moyo, 5:8.....	63
Amani na Vita, 5:9.....	64
Viwango vya thawabu na Adhabu, 5:12 .....	67
Baba, 5:16 .....	69
Amina, 5:18.....	71
Mauaji (Kutoka 20:13), 5:21.....	74
Wapumbavu, 5:22.....	76
Wafu wako wapi, 5:22 .....	77
Uzinzi (Kutoka 20:14), 5:27 .....	80
Utakatifu/Utakaso wa Agano Jipya, 5:46.....	85
Kusaidia Wahitaji, 6:1 .....	88
Wanafiki, 6:2 .....	90
Mungu Akielezewa kwa Lugha ya Kibinadamu, 6:4.....	91
Matumizi ya neno “mlango” katika Agano Jipya, 6:6 .....	93
Kufunga, 6:16 .....	98
Mkarimu/Mkweli ( <i>Haplotēs</i> ), 6:22.....	100
Mali, 6:24 .....	101

Hukumu (Je Wakristo wanaweza kuhukumiana?), 7:1 .....	109
Ukanaji wa Imani ( <i>Aphistem</i> ), 7:21 .....	114
Mapenzi ( <i>thelema</i> ) ya Mungu, 7:21 .....	116
Majina ya Agano la Kale la Yule Maalumu Ajaye, 8:20 .....	127
Wokovu (Neno la Agano la Kale), .....	129
Wokovu (Njeo za Vitenzi vya Kiyunani), 10:1 .....	145
Upungaji Pepo, 10:1 .....	146
Pepo (Roho Wachafu), 10:1 .....	147
Jedwali la Majina ya Mitume, 10:1 .....	149
Israeli (Jina), 10:6 .....	151
Kwanini Wakristo Wanateseka, 10:22 .....	156
Ustahimilivu, 10:21 .....	156
Mwili na Roho, 10:28 .....	159
Ukiri, 10:32 .....	160
Kutumwa ( <i>Apostello</i> ), 10:40 .....	163
Unabii wa Agano Jipya, 11:9 .....	168
Kanoni ya Kiebrania, 11:13 .....	171
Ibada ya Wenye Huzuni, 11:21 .....	174
Utakatifu/Utakaso wa Agano Jipya, 11:28 .....	176
Sabato, 12:1 .....	180
Yesu na Roho, 12:18 .....	184
Tumaini, 12:21 .....	185
Utu wa Roho, 12:31 .....	187
Enzi Hii na Enzi Ijaye, 12:31 .....	188
Waandishi, 12:38 .....	189
Kuitafsiri Mifano, 13 .....	195
Uzito na Ujazo wa Mashariki ya Karibu ya Kale (Upimaji wa Hali ya Hewa), 13:32 .....	203
“Mwana wa.....”, 13:38 .....	205
Hesabu ya Kumi na Mbili, 14:20 .....	216
Kauli ya kibinadamu, 15:19 .....	226
Chachu, 16:6 .....	233
Kanisa ( <i>Ekklesia</i> ), 16:18 .....	235
Ile “Miji” miwili ya Isaya, 16:18 .....	236

Baraza la Wakuu wa Masinagogi, 16:21 .....	238
Sarafu Zitumikazo katika Palestina katika siku za Yesu, 17:24.....	250
Milele, 18:8 .....	256
Maombi Yasiyo na Ukomo lakini Yaliyo na Ukomo, 18:19.....	259
Jina la Bwana, 18:20.....	260
Je Uponyaji ni Mpango wa Mungu kwa kila Kizazi?, 19:2.....	265
Maelezo juu ya Kutoka 20, 19:18.....	270
Kutawala katika Ufalme wa Mungu, 19:28 .....	279
Urithi wa Mwamini, 19:29 .....	281
Fidia/Komboa, 20:28.....	290
Milele, ( <i>O'lam</i> ), 21:19 .....	299
Jiwe Kuu la Pembeni, 21:42 .....	304
Farisayo, 22:15 .....	311
Utoaji Zaka, 23:23 .....	323
Kumiminwa, 23:35 .....	325
Kivuli kama sitiari kwa Ulinzi na Kujali, 23:37 .....	326
Fasihi ya Siku za Mwisho, 24 .....	329
Majibu ya Maswali Mawili ya Wanafunzi ya Mathayo, 24:3 .....	331
Ujio wa Mara ya Pili, 24:3 .....	332
Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH, 24:14 .....	335
Chukizo la Uharibifu, 24:15 .....	337
Uchaguzi/Kuamriwa Kabla na Hitaji kwa ajili ya Uwino wa Kithiolojia, 24:22 .....	339
Miezi arobaini na Mbili, 24:22 .....	339
Kurudi kwa Yesu kwa Wakati Wowote dhidi ya Kukawia (Ukinzani ya Agano Jipya),24:27 .....	340
Mwana wa Adamu (kutoka katika malezo ya Danieli 7:13), 24:30.....	342
Kuja Mawinguni, 24:30 .....	342
Pembe zitumikazo na Israeli, 24:31 .....	343
Saa, 24:36.....	345
Mitazamo ya Kibiblia juu ya Pombe na Ulevi, 26:29.....	364
Kukosekana kwa Mashitaka ya Kisheria kwa Usiku wa Baraza la Wakuu wa Masinagogi, 26:57-68 .....	372
Pontio Pilato, 27:2.....	378
Iskarioti, 27:5 .....	380
Mlinzi wa Mfalme, 27:27 .....	384

Watakatifu, 27:52 .....	388
Mwana wa Mungu, 27:54 .....	389
Wanawake waliosafiri pamoja na Yesu na wanafunzi Wake, 27:55.....	390
Ufufuo, 27:63 .....	393
Kuuonekana Kwa Yesu Mara baada ya Kufufuka, 28:9.....	397
Ubatizo, 28:19.....	399

## VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA KATIKA FASIRI HII

AB	Anchor Bible Commentaries, ed. William Foxwell Albright and David Noel Freedman
ABD	Anchor Bible Dictionary (6 vols.), ed. David Noel Freedman
AKOT	Analytical Key to the Old Testament by John Joseph Owens
ANET	Ancient Near Eastern Texts, James B. Pritchard
BDB A	Hebrew and English Lexicon of the Old Testament by F. Brown, S. R. Driver and C. A. Briggs
IDB	The Interpreter's Dictionary of the Bible (4 vols.), ed. George A. Buttrick
ISBE	International Standard Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. James Orr
JB	Jerusalem Bible
JPSOA	The Holy Scriptures According to the Masoretic Text: A New Translation (The Jewish Publication Society of America)
KB	The Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament by Ludwig Koehler and Walter Baumgartner
LAM	The Holy Bible From Ancient Eastern Manuscripts (the Peshitta) by George M. Lamsa
LXX	Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1 970
MOF	A New Translation of the Bible by James Moffatt
MT	Masoretic Hebrew Text
NAB	New American Bible Text
NASB	New American Standard Bible
NEB	New English Bible
NET	NET Bible: New English Translation, Second Beta Edition
NRSV	New Revised Standard Bible
NIDOTTE	New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis (5 vols.), ed. Willem A. VanGemeren
NIV	New International Version
NJB	New Jerusalem Bible
OTPG	Old Testament Passing Guide by Todd S. Beall, William A. Banks and Colin Smith
REB	Revised English Bible
RSV	Revised Standard Version
SEPT	The Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1 970
TEV	Today's English Version from United Bible Societies
YLT	Young's Literal Translation of the Holy Bible by Robert Young
ZPBE	Zondervan Pictorial Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. Merrill C. Tenney



# **NENO TOKA KWA MWANDISHI NI KWA NAMNA GANI FASIRI HII ITAKUSAIDIA?**

Kutafasiri Biblia ni uwiano wa wastani na wa kiroho ambao unajaribu kumwelewa mwandishi wa kale aliyevuviwa kuandika ili kuwezesha ujumbe wa Mungu uweze kueleweka na kutumiwa katika zama hizi.

Mchakato wa kiroho ni muhimu sana lakini mugumu sana kuelezea. Unahusisha kujitua na kuwa wazi kwa Mungu. Lazima pawepo na njaa (1) kwa ajili yake (2) ya kumjua yeye na (3) kumtumkia yeye. Mchakato huu unahusisha maombi, ukiri na kuwa tayari kubadili mfumo wa kuishi. Roho Mtakatifu ni wa muhimu sana katika mchakato wa utafasiri, lakini kwa nini wakristo waaminifu, wanaompenda Mungu wanaielewa Biblia tofauti kabisa na kuitafasiri visivyo.

Mchakato wa uwiano huu ni rahisi kuelezea. Lazima tuwe na msimamo na haki kwa maandiko badala ya kuathiriwa na hali ya upendeleo binafsi au wa ki-madhehebu. Sote tumefungamanishwa ki-historia. Hakuna yeyote mtafasiri miongoni mwetu awezae kubisha. Fahiri hii inatoa kwa uangalifu uwiano ulio sahihi wenye kanuni tatu za tafasiri zilizoundwa kusaidia kudhibiti hali zetu za upendeleo.

## **KANUNI YA KWANZA**

Kanuni ya kwanza ni kuona muundo wa kihistoria ambao kwayo Biblia iliandikwa na tukio zima la kihistoria katika uandishi wake. Mwandishi wa mwanzo alikuwa na kusudi, ujumbe wa kuwakilisha. Andiko haliwezi kumaanisha kitu kwetu ambacho hakikumaanishwa na ile asili, na mwandishi aliyevuviwa wa zama hizo. Kusudi lake na wala sio mahitaji yetu ki-historia, ki-musisimko, ki-tamaduni na mapokeo ya ki-madhehebu yetu ni— ufunguo.

Matumizi ni mbia mkubwa wa tafasiri, lakini tafasiri sahihi lazima ipate kipaumbele kwa matumizi. Lazima isisitizwe kwamba, kila andiko la Biblia lina tafasiri moja tu, na si vinginevyo. Maana hii ndiyo mwandishi wa mwanzo wa Biblia alivyokusudia akiongozwa na roho kuiwasilisha katika enzi zake. Maana hii moja yaweza kuwa na matumizi anwai, katika tamaduni na mazingira tofauti. Matumizi haya lazima yaambatane na ukweli halisi wa mwandishi wa awali. Kwa sababu hii, mwongozo wa fasiri hii imetayalishwa kwa namna ya kutoa utangulizi kwa kila kitabu cha Biblia.

## **KANUNI YA PILI**

Kanuni ya pili ni kuibainisha fasihi moja. Kila kitabu cha Biblia ni hati ya kumbukumbu iliyounganishwa. Wafasiri hawana haki ya kutenganisha hoja moja ya ukweli kwa nyingine. Kwa hiyo hatuna budi kujaribu kuelewa kusudi la kitabu kizima cha Biblia kabla ya kutafasiri fasihi ya kitabu kimoja kimoja. Sehemu moja—sura, aya, au mistari haiwezi kumaanisha ambacho kitabu kizima hakimaanishi. Tafsiri sharti iwiane na mtizamo mzima kuelekea mtimzamo wa sehemu ya vifungu vya Biblia. Kwa hiyo mwongozo huu wa fasiri ya mafunzo haya umelenga kuwasaidia wanafunzi kuchambua muundo wa kila andiko ki-aya. Mgawanyo wa ibara na sura havikuvuviwa bali ni kutusaidia tu ili kubaini mawazo.

Kutafasiri katika ngazi ya aya na sio sentesi, ibara, kifungu au ngazi ya neno ndio ufunguo katika kufuata maana ya mwandishi aliyokusudia. Aya zimejengwa kwenye mada iliyounganishwa pamoja, mara nyingi huitwa sentesi yenye dhamira au mada. Kila neno, kifungu, ibara na sentesi katika aya kwa kiasi fulani vinahusiana na dhamira iliyo pamoja. Aidha haya huweka ukomo, inapanua, kueleza na/ au kuihoji. Maelekezo sahihi (ufunguo) kwa tafsiri sahihi ni kufuata wazo la mwandishi wa awali aya kwa aya kufuatana na fasihi binafsi ambayo inatengeneza Biblia nzima. Tafsiri hizi zimechaguliwa kwa sababu zinatamia nadharia mbalimbali za tafsiri.

1. Andiko la Kiyunani la United Bible Society ni rekebisho la chapisho la Nne la (UBS<sup>4</sup>). Andiko hili liliandikwa ki-aya na wasomi wa maandiko ya kisasa.

2. Toleo la New King James Version (NKJV) ni utafsiri wa fasihi wa neno kwa neno uliosimamia kwenye mapokeo ya machapisho ya Kiyunani yaliyojulikana kama “Upokeaji wa Maandishi”. Mgawanyo wa aya zake ni mrefu kuliko tafasiri zinginezo. Urefu wa aya hizi unamwezesha wasomi kuona mada zilizo pamoja.
3. Toleo la New Revised English Version(NRSV) ni tafsiri ya neno kwa neno lililoboreshwa. Inatengeneza pointi ya kati baina ya matoleo mawili ya kisasa yanayofuata. Mgawanyo wa aya zake ni wa msaada mkubwa katika kubainisha masomo.
4. Toleo Today’s English Version(TEV) ni utafsiri sawia wenye nguvu uliyochapishwa na muungano wa vyama vya Biblia. Unajaribu kutafasiri Biblia kwa njia ya kumwezesha msomaji au mnenaji wa kiingereza cha kisasa kuelewa maana iliyomo katika andiko la Kigiriki. Mara nyingi, hasa hasa katika injili, inagawanya aya kufuatana na mnenaji hata kuliko somo lenyewe, sawa na NIV. Kwa kusudi la mtafasiri, hili halina msaada. Inapendeza kuona kuwa vitabu vya UBS<sup>4</sup> na TEV vimechapishwa na mtu yule yule lakini aya zake zinatofautiana.
5. The Jerusalem Bible(JB) ni tafsiri sawia yenye mlinganyo wa nguvu iliyosimamia kwenye tafasiri ya Katoliki ya Ufaransa. Ni nzuri mno katika kufanya ulinganifu wa aya kutoka katika mtizamo wa ki-Ulaya.
6. Chapisho la andiko ni uboreshaji wa mwaka 1995 wa toleo la Biblia New American Standard Bible (NASB) ambalo ni tafasili ya neno kwa neno. Pia maoni ya mstari kwa mstari yanafuata aya hizi.

## **KANUNI YA TATU**

Kanuni ya tatu ni kusoma Biblia tofauti tofauti ili kupata uwezekano mpana wa maana (somo la maana ya maneno) kwamba maneno ya Kibiblia au vifungu yanaweza kuwa nayo. Daima, neno au fungu la maneno katika Kiyunani yanaweza kueleweka kwa njia mbalimbali. Tafsiri hizi tofauti husaidia kubaini na kuelezea utofauti uliopo katika maandiko ya awali ya Kiyunani. Lakini haya hayaathiri mafundisho, bali husaidia katika kujaribu kurejelea maandiko asili yaliyoandikwa na mwandishi wa kwanza aliyevuviwa.

Fasiri hii humpa mwanafunzi njia ya haraka ya kuchunguza fasiri zake. Hii haina maana kuwa ni ya kumalizia, bali ni ya utoaji taarifa na udadisi kimawazo. Mara nyingi tafsiri nyingine hutusaidia tusiwe ving’ang’anizi na wafinyu wa mawazo na mapokeo ya kimadhehebu. Watafasili wanapaswa kuwa na upana mkubwa wa kuelewa tafasiri tofauti tofauti na kuweza kubaini ni kwa ugumu upi maandiko ya kale yanaweza kuwa. Inashangaza kuona ni kwa kiasi kidogo kilioje cha makubaliano yaliopo kati ya Wakristo ambao wanadai kuamini biblia kama chanzo chao pekee cha ukweli. Kanuni hizi zimenisaidia kushinda hali yangu ya kufungwa kihistoria na kunifanya nipambane na maandiko ya zama hizo. Ni matumaini yangu kuwa kanuni hizi zitakuwa za Baraka kwako.

Bob Utley

Juni 27, 1996

Haki Miliki © 2013 [Bible Lessons International](#)

# MWONGOZO KWA USOMAJI MZURI WA BIBLIA:

## UTAFITI BINAFSI KWA UKWELI ULIO THIBITIKA

Kinachofuata ni maelezo mafupi ya Dr. Bob Utley mwana falsafa wa kanuni za ufasihi na njia alizotumia katika fasihi yake.

Tunaweza kuufahamu ukweli? Unapatikana wapi? Tunaweza kuuthibitisha kimantiki? Kweli, kuna mamlaka ya kimsingi? Kuna imani kamili inayoweza kulinda maisha yetu, na ulimwengu wetu tuliomo? Kuna maana yeyote katika maisha? Kwa nini tuko hapa? Tunakwenda wapi? Maswali haya yanauliza kwa watu wote wenye tafakuri zenye uwiano—wameyatawala maarifa ya binadamu tangu mwanzoni mwa nyakati (Mhu. 1:13-18; 3:9-11). Naweza kukumbuka utafiti wangu binafsi kwa ajili ya ungamanisho la maisha yangu. Nimekuwa mwamini katika Kristo kwenye umri mdogo, awali kabisa nikizingatia juu ya ushahidi wa watu wengine muhimu kwenye familia yangu. Nilivyokuwa kufikia utu uzima, maswali juu yangu na ulimwengu ninamoishi ulivyokuwa. Tamaduni za kawaida na dini hazikuleta maana yeyote kwenye uzoefu niliokusoma au kukutana nao. Ulikuwa ni muda wa kuchanganyikiwa, kutafuta, kutamani, na mara nyingi fikra zisizokuwa na tumaini katika uso wa ulimwengu mgumu, usiojali nilimoishi.

Wengi walidai kuwa na majibu kwa maswali haya ya msingi, lakini baada ya utafiti na kufikiri nikapata majibu yao yamelenga juu ya (1) falsafa binafsi, (2) hadithi za kubuniwa za kale, (3) uzoefu binafsi, au (4) Saikolojia zilizojichomoza. Nilihita digrii fulani ya uthibitisho, baadhi ya vielelezo, kiasi cha busara ambamo ningelenga mtazamo wangu wa kidunia, kiini cha uzima wangu, sababu yangu ya kuishi. Niliyapata haya katika usomaji wangu wa biblia. Nilianza kutafuta ushahidi wa udhamini nilioupata katika (1) utegemezi wa historia ya biblia kama ulivyothibitishwa na elimu kale, (2) usahihi wa Nabii za Agano la Kale, (3) umoja wa jumbe za Biblia zaidi ya miaka 1600 ya kutolewa kwake na (4) shuhuda binafsi za watu ambao maisha yao yalibadilika moja kwa moja baada ya kusoma biblia. Ukristo, kama mfumo wa imani na kuamini uliunganishwa, una uweo wa kukabiliana na maswali magumu ya maisha ya mwanadamu. Siyo haya tu yanaweza kutoa muundo kazi, lakini mwelekeo unaotokana na uzoefu wa imani za kibiblia uliniletea furaha zenye hisia na ustahimili.

Nilijiridhisha ya kuwa nimepata kiini cha uzima wa maisha yangu—Kristo, kama ninavyoelewa kupitia maandiko. Ulikuwa ni uzoefu mgumu, msukumo wenye kuweka huru. Ingawa, naweza kukumbuka mshituko na maumivu yalipoanza kunifahamisha juu ya tafasiri ngapi tofauti ya kitabu hiki zimetetewa, wakati mwingine hata ndani ya makanisa hayo ya aina moja. Nikithibitisha mwongozo wa Ki-Mungu na uaminifu wa biblia haukuwa mwisho, lakini ni mwanzo pekee. Ni kwa vipi naweza kuthibitisha au kukataa tafsiri zinazotofautiana na kugongana za kurasa nyingi ngumu ndani ya maandiko kwa wale waliokuwa wakidai mamlaka yake na uaminifu?

Kazi hii imekuwa lengo la maisha yangu na hija ya imani. Nilifahamu ya kuwa imani katika Kristo imeniletea furaha na amani kubwa. Mawazo yangu yametamani baadhi ya imani kamili katikati ya nadharia ya utamaduni wangu na mfumo wa imani gonganishi wa dini na majivuno ya kimadhehebu. Katika utafiti wangu wa mitazamo halali kwenye utafsiri wa fasihi ya kale, nilishangaa kuvumbua historia yangu, ya kitamaduni, ya kimadhehebu na uzoefu wa kipendeleo. Kwa kawaida kabisa, mara nyingi, nimesoma Biblia ili kuimarisha mtazamo wangu. Nimeutumia kama chanzo cha mfumo wa imani kuvamia imani nyingine wakati nikijihakikishia usalama wangu na utoshelevu. Ni kwa namna gani utambuzi wa maumivu haya yalikuwa kwangu!

Ingawa siwezi kuwa kipingamizi moja kwa moja, naweza kuwa msomaji mzuri wa biblia. Naweza kuweka ukomo wa upendeleo kwa kutambua na kukubali uwepo wao. Sijawaweka huru, lakini nimeukabiri udhaifu wangu. Mtafsiri mara nyingi ndio adui mbaya wa usomaji mzuri wa biblia! Ngoja

nitaje baadhi ya dhanio nilizoleta kwenye usomaji wa biblia ili, msomaji, aweze kuzichunguza pamoja nami:

## **DHANIO**


1. Ninaamini biblia ni uvuvio wa ki-pekee wa ufunuo binafsi wa Mungu mmoja na aliye wa kweli. Kwa hiyo, ni lazima itafsiriwe katika mwanga wa kusudi la Ki-Ungu la mwandishi wa mwanzo (yaani Roho) kupitia mwandishi wa kibinadamu katika muundo wa historia uliokusudiwa.
  - Wapokeaji wa mwanzo
  - Ujumbe ulioandikwa
  - Kusudi la mwandishi wa mwanzo
2. Ninaamini biblia iliandikwa kwa ajili ya mtu wa kawaida—kwa watu wote! Mungu alilazimika mwenyewe kuongea kwetu waziwazi kupitia historia na tamaduni zilizomo. Mungu hakuuficha ukweli, anatutaka sisi kuelewa! Kwa hiyo, inalazimika kutafsiriwa katika (uwazi) katika siku hizo, na siku hizi tulizomo. Biblia haitakiwi kumaanisha kwetu yale ambayo hayakumaanisha kwa wale wa mwanzo walioisoma au kuisikia. Inaeleweka kwa wastani wa mawazo ya kibinadamu na kutumia aina ya njeo mbadala za kawaida za mawasiliano ya ki-binadamu.
3. Ninaamini Biblia inakusudi na ujumbe uliowekwa pamoja. Haina mkanganyiko ndani yake, ingawa inajumuisha (njia ngumu na zinazokinzana). Hivyo basi, mtafsiri mzuri wa biblia ni biblia yenyewe.
4. Ninaamini kwa kila kurasa (pasipo kujumuisha unabii) ina maana moja iliyosimama kwenye kusudi la mwanzo la mwaandishi aliyevuviwa. Ingawa hatuwezi kutia shaka kutambua kusudi la mwandishi wa mwanzo, viashirio vingi daima vimeelekeza katika uelekeo wake;
  - a. Aina ya fasihi tanzu uliochaguliwa kuelezea ujumbe
  - b. Mtindo wa kihistoria na/au muda maalumu ulioshawishi maandiko kuandikwa
  - c. Muundo wa fasihi wa kitabu husika pamoja na kila fasihi moja
  - d. Muundo wa maandishi (elezewa kwa fasaha) wa fasihi moja kama zinavyo husiana na ujumbe
  - e. Umbo la kisarufi husika lililowekwa kuwasilisha ujumbe
  - f. Maana zilizochaguliwa kuwakilisha ujumbe

Mafunzo ya kila eneo hili liwe chanzo cha mafunzo yetu katika aya. Kabla sijaelezea njia zangu za usomaji mzuri wa biblia, hebu nielezee angalau njia zisizosahihi zinazotumiwa siku hizi zilizopelekea kuwepo kwa tafsiri tofauti nyingi na hivyo basi zinatakiwa kuepukika.


## **II. Mbinu zisizofaa**

1. Kutojali mazingira ya fasihi ya vitabu vya Biblia na kutumia kila sentesi, ibara, au maneno binafsi kama maelezo ya kweli yasiyohusiana na kusudi la mwandishi wa mwanzo au mtindo mpana. Hii mara nyingi huitwa “uhakiki wa andiko”
2. Kutoujali muundo wa ki-historia wa vitabu kwa kubadilisha muundo wa ki-historia unaodhaniwa kuwa ni mdogo au usiosaidika kutoka kwenye andiko lenyewe.
3. Kutojali muundo wa kihistoria wa vitabu na kusoma kama gazeti la mtaani lililoandikwa asili kwa wakristo binafsi wa kisasa.
4. Kuupa muundo wa kihistoria wa vitabu kwa kuliistiari andiko ndani ya ujumbe wa falsafa/theolojia isioendana na wasikiaji wa kwanza na kusudi la mwandishi wa mwanzo.
5. Kutojali muundo wa mwanzo kwa kubadilisha mtindo wa theolojia ya mtu, mafundisho yanayopendeka, au mambo ya kisasa yasiyoendana na kusudi la mwandishi wa mwanzo na ujumbe uliotolewa. Tabia hii mara nyingi hufuata usomaji wa mwanzo wa biblia kama kigezo cha kuanzisha mamlaka ya mnenaji. Hii mara nyingi hurejewa kama “mwitikio wa msomaji”

(utafsiri wa-andiko-lililomaanisha-kwangu). Kwa wastani, vitu vitatu vinavyoendana vinaweza kupatikana katika mawasiliano ya binadamu yalioandikwa.



Siku za nyuma, mbinu tofauti za usomaji zimenitazamisha juu ya moja kati ya vitu vitatu. Lakini kweli tunatamka kwa dhati uhuisho wa Biblia wa kipekee na mchora uliofanyiwa mabadiliko unaofaa zaidi:



Kwa kweli vitu hivi nyote vitatu lazima vijumulishwe katika mchakato wa ufasiri. Kwa kusudi la uthibitisho, ufasiri wangu unalenga juu ya moja kati ya vitu viwili: mwandishi wa mwanzo na maandiko. Ninayamkinika kujibu matusi mabaya niliyoyachunguza (1) shutumu au kutakasa maandiko na (2) tafasili ya “mwitikio wa msomaji” (unamaanishwa nini kwangu). Matusi yanaweza kutokea katika kila hatua. Ni lazima kila mara tuchunguze mienendo yetu, upendeleo wetu, mbinu na matumizi. Lakini ni kwa jinsi gani tunaweza kuyachunguza kama hapatakuwepo na mipaka ya ufasih, ukomo au kigezo? Hapa ni pale kusudi la mwandishi na muundo wa maandiko yaliponipa baadhi ya vigezo kuzuia maeneo ya fasiri zilizo halali. Katika kuangazia hizi mbinu za usomaji zisizofaa, zipi ni baadhi ya mitazamo mizuri ya usomaji mzuri wa biblia ambao unatoa digri ya uthibitisho na misimamo?

### III. Mitazamo inayofaa katika usomaji mzuri wa Biblia

Katika hatua hii sijadili mbinu pekee za ufasiri wa namna mahususi lakini kwa pamoja kanuni halali kwa aina yote ya maandiko ya kibiblia. Kitabu kizuri kwa namna ya mitazamo mahususi ni *How To Read The Bible For All Its Worth*, ya Gordon Fee na Douglas Stuart, kilichochapishwa na Zondervan.

Utaratibu wangu mwanzoni ulinitizamisha juu ya msomaji aliyemruhusu Roho Mtakatifu kuangaza biblia kupitia kwa miduara minne ya usomaji binafsi. Hii inamfanya Roho, andiko na msomaji wawe kiwango cha mwanzo, na siyo cha juu. Vile vile hii inamlinda msomaji kutokuwa na mwanya wa kushawishiwa na mtoa maoni. Nimesikia ikisemwa: “Biblia inaangazia zaidi katika fasihi”. Hii haimaanishi kukashifu maoni juu ya msaada wa usomaji lakini ni ombi kwa muda unaofaa kwa matumizi yao. Tunalazimika kuusaidia ufasiri wetu kutoka katika andiko lenyewe. Maeneo matatu yanatoa angalau ukomo wa uthibitisho:

1. muundo wa kihistoria
2. mazingira ya fasihi
3. muundo wa kisarufi (vipashio)
4. matumizi ya maneno ya kisasa
5. milango muhimu iliyo sambamba
6. namna tanzu ya uwasilishaji

Tunahitajika kuweza kutoa sababu na mantiki zilizo nyuma ya ufasihi wetu. Biblia ndiyo chanzo pekee cha imani yetu na mazoezi. Kwa huzuni, mara nyingi wakristo hawakubali juu ya kile

kinachofundishwa au kukiri. Ni kushindwa kudai uhuisho juu ya Biblia na kupelekea waamini washindwe kukubali juu ya kile kinachofundishwa na kutakiwa! Miduara mine ya usomaji imeundwa kutupatia utambuzi wa ufasili ufuatao:

### 1. **Mzunguko wa kwanza wa usomaji**

- a. Soma kitabu katika mkaao mmoja. Soma tena katika fasili tofauti , kwa matumaini kutoka katika fasili tofauti za nadharia
  - 1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
  - 2) Mlinganyo wenye nguvu (TEV, JB)
  - 3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
- b. Angalia kiini cha kusudi la uandishi mzima. Tambua dhamira yake.
- c. Tenga (ikiwezekana) fasihi moja, sura, ibara au sentesi inayoelezea waziwazi Kiini cha kusudi au dhamira
- d. Tambua fasihi tanzu yenye nguvu
  - 1) Agano la kale
    - a) Simulizi za waebrania
    - b) Mashairi ya waebrania (fasihi za hekima, zaburi)
    - c) Unabii wa ki-Ebrania (lugha ya mjazo, shairi)
    - d) Alama za siri za ki-sheria
  - 2) Agano jipya
    - a) Simulizi (Injili, matendo)
    - b) Hadithi za mafumbo (Injili)
    - c) Barua/nyaraka
    - d) Fasihi za mafunuo

### 2. **Mzunguko pili wa usomaji**

- a. Soma kitabu kizima tena, ukitafuta kufahamu mada muhimu au masomo.
- b. Elezea kwa muhtasari wa mada muhimu na elezea kwa kifupi yaliomo kwa maelezo rahisi
- c. Angalia kusudi la maelezo yako na eleza kwa mapana kwa msaada wa usomaji.

### 3. **Mzunguko wa tatu wa usomaji.**

- a. Soma tena kitabu kizima, ukitafuta kutambua muundo wa ki-historia na Matukio lengwa kwa ajili ya uandishi kutoka katika kitabu cha Biblia yenyewe.
- b. Taja vipengele vya ki-historia ambavyo vinatajwa katika kitabu cha Biblia.
  - 1) Mwandishi
  - 2) Tarehe
  - 3) Wapokeaji
  - 4) Kusudu mahsusi la uandishi
  - 5) Mwelekeo muundo wa kitamaduni unaorandana na kusudi la mwandishi
  - 6) Marejeo toka kwenye matukio na watu wa kihistoria/ kale
- c. Panua maelezo yako kwa kiwango cha aya kutoka katika sehemu ya kitabu cha biblia unayotafasiri. Mara nyingi tambua na kuelezea fasihi. Inaweza kuwa na vifungu na aya nyingi. Hii inakuwezesha wewe kufuata wazo na muundo wa maandiko ya mwandishi wa mwanzo.
- d. Angalia muundo wako wa kihistoria kwa kutumia msaada wa usomaji

### 4. **Mzunguko wa nne wa usomaji**

- a. Soma tena bayana fasihi moja katika tafasiri nyinginezo nyingi
  - 1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
  - 2) Mwenendo linganifu (TEV, JB)
  - 3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)

- b. Angalia fasihi au muundo wa kisarufi
  - 1) Misemo ya kujirudia Waefeso.1:6, 12, 14
  - 2) Muundo wa kisarufi unaojirudia Warumi 8:31
  - 3) Mbinjo wa mawazo (dhana zinazoafikiana)
- c. Taja vipengele vifuatavyo:-
  - 1) Istilahi muhimu
  - 2) Istahili zisizo za kawaida
  - 3) Muundo muhimu wa kisarufi
  - 4) Maneno magumu, ibara, na sentesi
- d. Angalia njia muhimu zilizosambamba
  - 1) Angalia njia za wazi za ufundishaji kwenye somo lako kwa kutumia
    - a) Vitabu vya thiolojia
    - b) Biblia za marejeo
    - c) Itifaki
  - 2) Angalia maneno mawili yanayokinzana katika somo lako. Kweli nyingi za ki-Biblia zinatolewa katika rahaja mbili zinazofanana. Migongano mingi ya ki-madhehebu hutokea kutokana nauthibitisho nusu wa maandiko ya Biblia. Biblia zote zimevuviwa. Ni lazima tutafute ujumbe mzima ili kutoa mlinganyo wa ki-maandiko katika tafasiri zetu.
  - 3) Angalia milinganisho ndani ya kitabu, kilekile, mwandishi Yule Yule, au namna ileile, Biblia ina mfasiri wake mzuri kwa sababu ina mwandishi mmoja ambaye ni Roho Mtakatifu.
- e. Tumia misaada ya kusoma kuangalia uchunguzi wako wa muundo wa kihistoria na tukio.
  - 1) Soma biblia
  - 2) Ensaikolopidia za biblia, vitabu vya mkononi na kamusi
  - 3) Tangulizi za biblia
  - 4) Fasihi za biblia (katika hatua hii kwenye usomaji wako ruhusu jamii ya waamini, waliopita na waliopo, kusaidia na kusahihisha usomaji wako binafsi)

#### **iv. Matumizi ya utafasiri wa Biblia.**

Katika hatua hii tunageukia matumizi, umechukua muda kuelewa andiko katika muundo wake, sasa lazima utumie katika maisha yako, utamaduni wako, na elezea mamlaka ya Ki-biblia kama “uelewa ule mwandishi wa ki-biblia wa mwanzo alivyosema katika zama zake na kutumia ukweli huo katika zama hizi”. Matumizi lazima yafuate utafasiri wa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika muda na mantiki.

Hatuwezi kutumia njia ya Biblia katika zama zetu mpaka pale tutakapo fahamu kile alichokuwa akikisema katika zama hizo. Njia ya Biblia isimaanishe kile asicho kimaanisha!

Maelezo yako kwa kirefu, kwa kiwango cha aya (mzunguko wa usomaji #3) yatakuwa mwongozo wako. Matumizi lazima yafanyike katika kiwango cha aya, na sio kiwango cha neno, maneno yana maana pekee katika mazingira, ibara zina maana pekee katika mazingira na sentensi zina maana pekee katika mazingira. Mtu pekee aliyevuviwa ambaye amejumuishwa katika mchakato wa utafsiri ni mwandishi wa mwanzo. Kipekee unafuata utangulizi wake kwa mwanga wa Roho Mtakatifu. Lakini nuru sio uvuvio. Kusema “asema Bwana” lazima, tufungamane na kusudi la mwandishi wa mwanzo. Matumizi lazima yaendane bayana na kusudi lote la uandishi mzima, maandishi bayana, na muendelezo wa kiwango cha aya.

Usiruhusu mambo ya zama hizi yatafasiri Biblia, iruhusu Biblia ijiongee yenyewe. Hii itatuhitaji kuvuta kanuni kutoka kwenye andiko. Hii itakubalika kama andiko litaiwezesha kanuni. Bahati mbaya wakati mwingi kanuni zetu ni “zetu” na si kanuni za ki-maandiko.

Katika kutumia Biblia, ni muhimu kukumbuka kuwa (isipokuwa katika unabii) maana moja na moja pekee itakubalika kwa andiko la Kibiblia pekee. Maana hiyo iendane na kusudi la mwandishi wa mwanzo kama alivyo eleza tatizo au hitaji katika zama zake. Mengi ya matumizi yanayowezekana yanaweza kutolewa kutoka katika maana hii moja. Matumizi yatategemea mahitaji ya wapokeaji lakini ni lazima yaendane na maana ya mwandishi wa mwanzo.

## **v. Sura ya utafasiri wa kiroho.**

Zaidi ya hapo nimejadili mantiki na mchakato wa ki-maandiko uliojumuishwa kwenye utafasiri na matumizi. Sasa ngoja nijadili kwa kinaga ubaga mwelekeo wa kiroho wa utafasiri. Mfuatano ufuatao umekuwa wa msaada sana kwangu.

1. Omba kwa ajili ya msaada wa Roho (kama vile 1 Kor. 1:26-2:16)
2. Omba kwa ajili ya msaada binafsi na kusafishwa kutoka katika dhambi inayojulikana (kama vile 1 Yohana 1:9)
3. Omba kwa ajili ya hamu kubwa ya kumjua Mungu (kama vile Zab. 19:7-14, 42:1, 119:1)
4. Tumia utambuzi wowote mpya mara moja katika maisha yako.
5. Baki mnyenyekevu na anayefundishika.

Ni vigumu kuweka mlinganyo kati ya mchakato wa kimantiki na uongozi wa kiroho wa Roho Mtakatifu. Dondoo zifuatazo zimesaidia kulinganisha hizi mbili:

1. Kutoka kwa mwandishi James W.Sire, *scripture twisting*,kr. 17-18  
“Nuru huja kwenye mawazo ya watu wa Mungu na sio tabaka la watu wa kiroho. Hakuna daraja la ualimu katika ukristo wa kibiblia. Hakuna kuongoza, hapana mtu awaye yote ambaye tafsiri zote nzuri zitoke kwake. Na hivyo, wakati roho mtakatifu anatoa karama maalumu ya hekima, maarifa na utambuzi wa kiroho huwa pamoja. Hakutoa hizi kwa wakristo waliokirimwa kuwa wao ndo pekee watafsiri wenye mamlaka ya Neno lake. Ni juu ya kila watu wake kujifunza, kuamua na kutambua kwa kufanya marejeo kwenye Biblia ambayo inasimama kama yenye mamlaka hata kwa wale ambao Mungu amewapa uwezo pekee. Kwa kufupisha, wazo mnalofanya kupitia kitabu kizima ni kuwa Biblia ni ufunuo wa kweli wa Mungu kwa watu wote, ya kuwa ni mamlaka yetu ya mwisho katika mambo yote ambayo inayaongelea, kuwa sio fumbo lote lakini inaweza kueleweka vya kutosha na watu wa kawaida kwa kila tamaduni.”
2. Juu ya Kierkegaard, inayopatikana toka kwa Benard Ramm, *Protestant Biblical Interpretation(tafsiri ya biblia ya ki-protestanti)* Uk.75:  
Kutokana na Kierkegaard, kisarufi, misamiati na usomaji wa kihistoria wa Biblia ulikuwa ni muhimu lakini utangulizi wa usomaji wa kweli wa Biblia na kusoma Biblia kama neno la Mungu mmoja lazima alisome kwa moyo wake wote mdomoni mwake, kutoka ncha ya kidole, na shauku ya matarajio katika mazungumzo na Mungu. Usomaji wa Biblia pasipo tafakari, kutojali au kielimu, au weledi sio usomaji wa Biblia kama neno la Mungu, kama mmojawapo asomavyo barua ya mapenzi isemavyo, tena mmoja asoma kama neno la Mungu.
3. H.H Rawley katika *The Relevance of the Bible*, Uk.19:  
Hakuna uelewa mdogo wa kisomi wa Biblia, ingawa yote, inaweza kumiliki hazina yote. Haidharau uelewa huo, kwa kuwa ni muhimu kwa uelewa wote. Lakini ni lazima iongeze uelewa wa kiroho wa hazina ya kiroho ya kitabu hiki kwa ujumla. Kwa huo uelewa wa kiroho kitu fulani ambacho ni zaidi ya hadhari ya kiroho ni muhimu. Mambo ya kiroho ni utambuzi wa kiroho, na wanafunzi wa Biblia wanahitaji fikra za upokeaji wa kiroho. Ie hamu ya kumtafuta Mungu ambayo inaweza kumsababisha ajitoe kwake. Ni kama kupita zaidi ya usomaji wa kisayansi kuingia kwenye urithi wa utajiri wa hiki kitabu kikubwa kuliko vyote.

## **VI. Njia hizi za Fasiri**

*Study Guide Commentary (Mwongozo wa usomaji)* wa fasihi umeundwa kusaidia njia zako za utafsiri katika njia zifuatazo:



1. Maelezo fasaha ya kihistoria yanayotambulisha kila kitabu baada ya kufanya “mduara wa usomaji #3” angalia taarifa hizi.
2. Utambuzi wa ki-mazingira unapatikana katika kila kurasa. Hii itakusaidia kuona jinsi gani maandishi/fasihi imeundwa.
3. Katika kila mwanzo wa kifungu au fasihi kubwa inaunganisha mgawawanyo wa aya na maelezo ya kichwa cha makala yanatolewa kutoka katika tafsiri za kisasa.
  - a. United Bible Society Greek Text. Toleo la nne lililobadilishwa (UBC)
  - b. The New American Standard Bible 1995 ya kisasa (NASB)
  - c. The New King James Version (NKJV)
  - d. The New Revised Standard Version (NRSV)
  - e. Today’s English Version (TEV)
  - f. The Jerusalem Bible (JB)

Aya zilizogawanywa hazikuvuviwa. Lazima ziyakinishwe kutoka katika mazingira fulani. Kwa kulinganisha tafsiri nyingi za kisasa kutoka tafsiri nyingi za ki-nadharia na mitizamo ya kitheolojia, tunaweza kuchanganua muundo unaokusudiwa wa mawazo ya mwandishi wa mwanzo, kwani kila aya ina ukweli mmoja mkubwa. Huu uliitwa “mada ya sentensi” au wazo la kati la andiko, hilo wazo lililounganishwa ni ufunguo kwa tafsiri nzuri ya kihistoria na kisarufi. Mmojawapo asitafsiri, kuhubiri au kufundisha chini ya aya, vilevile ukumbuke ya kuwa kila aya inahusiana na aya zingine. Hii ndo maana kiwango cha aya kinachoelezea kitabu kizima ni muhimu. Ni lazima tuweze kufuata mtiririko wa kimantiki wa somo lililotolewa na mwandishi wa mwanzo aliyevuviwa.

4. Muhtasari wa Bob unafuata mtazamo wa kifungu kwa kifungu kwa utafsiri wake. Hii inatulazimisha kufuata mawazo ya mwandishi wa mwanzo. Muhtasari unatoa habari kutoka sehemu nyingi.
  - a. Mazingira ya fasihi
  - b. Utambuzi wa kihistoria na tamaduni
  - c. Habari za kisarufi
  - d. Usomaji wa neno
  - e. Njia muhimu zilizo sambamba
5. Mahali fulani katika fasihi, andiko lililochapishwa toka toleo jipya la Marekani (1995 mpaka sasa hivi) litaongezewa na tafsiri za matoleo mbalimbali ya kisasa.
  - a. New King James Version (NKJV) ambayo unafuata mswada wa “Upokeaji wa Maandiko halisi”.
  - b. The New Revised Standard Version (NRSV) ambayo ni rudio la neno-kwa-neno Kutoka katika Umoja makanisa asili ya Revised Standard Version
  - c. The Today’s English Version (TEV) ambayo ni tafsiri ya mlinganyo wa nguvu Kutoka American Bible Society.
  - d. The Jerusalem Bible (JB) ambayo ni tafsiri ya Kiingereza inayotegemea kutoka tafsiri ya Mlinganyo wa nguvu wa Katoriki ya Ufaransa.
6. Kwa wale wote ambao hawasomi kiyunani, ukilinganisha na tafsiri za kiingereza inaweza kusaidia kutambua matatizo katika andiko:
  - a. Tofauti za mswada
  - b. Maana ya maneno mbadala
  - c. Muundo na maandiko magumu ya kisarufi Ingawa tafsiri za kiingereza haziwezi kuleta suluhu kwenye matatizo hayo yanayalenga kama sehemu ya ndani na usomaji kamili.
  - d. Karibia kila kifungu, maswali muhimu ya majadiliano yanatolewa ambayo yanajaribu kulenga maswala muhimu ya utafsiri wa kifungu hicho

# UTANGULIZI WA MATHAYO

## MAELEZO YA UFUNGUZI

- A. Mpaka muda wa mageuzi ya Mathayo ilikuwa inafikiriwa kuwa injili ya kwanza kuwahi kuandikwa (na bado inafikiriwa hivyo na kanisa Katoliki).
- B. Ilikuwa ni injili iliyonakiliwa na kunukuliwa zaidi kuliko zingine zote katika Katekismusu na katika liturujia ya kwanza ya kanisa kwa karne mbili za kwanza.
- C. William Barclay katika *The First Three Gospels*, kur. 19, alisema "Tunapogeukia Mathayo, tunageukia kwenye kitabu ambacho kwa hakika kinaweza kuitwa nakala moja ya msingi zaidi ya imani ya Ukristo kwa kuwa ndani yake tuna ripoti kamili iliyopangiliwa zaidi ya maisha na mafundisho ya Yesu." Hii ni kwasababu ilikuza mafundisho ya Yesu katika namna ya maudhui. Ilitumika kufundisha waongofu wapya (wote Wayahudi na Mataifa) kuhusu maisha na ujumbe wa Yesu wa Nazareti, Kristo.
- D. Inatengeneza daraja la kimantiki kati ya maagano ya zamani na mapya, kati ya waaminio wa Kiyahudi na waaminio wa Mataifa. Ilitumia Agano la Kale katika mifumo ya ahadi/utimilizwaji kama ilivyofanyika *kerygma (mafundisho ya kanisa la kwanza)*. Agano la Kale limenukuliwa zaidi ya mara hamsini na kuelezewa zaidi sana. Pia majina mengi na simulizi zilizotumika juu ya YHWH zimetumika juu ya Yesu.
- E. Hivyo makusudi ya Injili kulingana na Mathayo yalikuwa uinjilishaji na kufanya wanafunzi, vipengele pacha vya Agizo Kuu (Mt. 28:19-20).
  - 1. Walitakiwa kuwasaidia Wayahudi waongofu wapya kwa kuwataarifu juu ya maisha na mafundisho ya Yesu
  - 2. Walitakiwa kuwafanya wanafunzi wote Wayahudi walioamini na Mataifa katika namna gani wanatakiwa kuishi kama Wakristo.

## UANDISHI

- A. Ingawa nakala za mwanzoni kabisa za Agano Jipya za Kiyunani (mnamo 200-400 B.K) zina maelezo "kulingana na Mathayo," kitabu chenye hakijulikani.
- B. Desturi mfanano ya kanisa la kwanza ni kwamba Mathayo (pia ikijulikana kama Lawi, kama vile Marko 2:14; Luka 5:27,29), mtoza kodi (kama vile Mt. 9:9; 10:3) na mwanafunzi wa Yesu waliandika Injili.
- C. Mathayo, Marko na Luka zina mfanano sawa:
  - 1. wao mara kwa mara katika mfumo wa nukuu wa Agano la Kale kwamba wanapatikana katika andiko la Kimasoteriki wala tafsiri ya Agano la Kale,
  - 2. mara kwa mara wanamnukuu Yesu tungo isiyo ya kawaida, hata kwa kutumia maneno nadra ya Kiyunani
  - 3. wao mara kwa mara wanatumia tungo na hata sentensi ya maneno yaliyosawa ya Kiyunani,
  - 4. kidhahiri ukopwaji wa kifasihi umetokea.
- D. Nadharia kadhaa zimekuzwa kuhusiana na uhusiano kati ya Mathayo, Marko na Luka (Vitabu vya Injili).
  - 1. Desturi mfanano wa kanisa la kwanza ni kwamba Mathayo (Lawi), mtoza ushuru na mwanafunzi wa Yesu, aliandika Injili. Mtume Mathayo hakuwa akikikiri kuwa mwandishi mpaka kuzaliwa upya/mageuzi.
  - 2. Karibia 1776 A. E. Lessing (na baadae Gieseler mnamo 1818), liweka nadharia ngazi ya kinywa katika makuzi ya vitabu vya injili ("kuona pamoja"). Alielezea kwamba walikuwa wakitegemea desturi mza kale kabisa za kinywa:
    - a. Mathayo: Wayahudi

b. Marko: Warumi

c. Luka: Mataifa

Kila mmoja ilikuwa ikihusiana na kituo tofauti cha kijiografia ya Ukristo

a. Mathayo: Antiokia, Shamu

b. Marko: Rumi, Italia

c. Luka: pembeni ya Bahari ya Kaisaria, Palestina

d. Yohana: Efeso, Asia Ndogo

3. Mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa J. J. Griesbach alitoa nadharia kwamba Mathayo na Luka waliandika hadithi tofauti za maisha ya Yesu, tofauti kabisa inayojitegemea. Marko aliandika injili ya kimuhtasari kujaribu kuingilia kati katika hadithi hizi mbili zingine.
4. Mwanzoni mwa karne ya ishirini H. J. Holtzmann alitoa nadharia kwamba Marko alikuwa mtu wa kwanza kuandika Injili na kwamba zote Mathayo na Luka walitumia muundo wa injili yake ikijumuisha nyaraka nyaraka inayojitegemea inayojumuisha misemo ya Yesu iitwayo Q (German *quelleor* "chanzo"). Hii iliitwa nadharia ya "vyanzo viwili" (pia ilipitishwa na Fredrick Schleiermacher mnamo 1832).
5. Baadaye B. H. Streeter alibadili nadharia ya "vyanzo viwili" kuwa nadharia ya "vyanzo vinne" ambayo ilitengeneza "ya kufanana na Luka" ikijumuisha Marko Q.
6. Nadharia za juu za kutengeneza Vitabu vya Injili ni madhanio pekee. Hakuna ushahidi wala ushahidi wa dhahiri wa kimaandiko ya aidha chanzo "Q" chanzo au ya kufanana na Luka." Wanazuoni wa kisasa hawajui namna gani Injili zilivyokuzwa wala aliyeziandika (jambo hilo hilo juu ya sheria ya Agano la Kale na manabii wa kwanza). Hata hivyo huku kukosa taarifa hakuathiri mtazamo wa kanisa juu ya uvuvio au uaminifu kama historian kama nyaraka za imani.
7. Kuna ufanano wa kidhahiri katika muundo na maneno kati ya vitabu vya injili lakini pia kuna tofauti zilizokusanywa. Tofauti ni za kawaida katika hadithi za shuhuda. Kanisa la kwanza halikusumbuka na kutofautiana na hadithi za mahuhuda hawa wa maisha ya Yesu.

Inaweza kuwa kwamba hadhira waliokusudiwa, mbinu ya mwandishi na lugha tofauti zilitumika (Kiaramu na Kiyunani) ambazo yawezekana kuwa zilileteleza utofautiano. Lazima isemwe kwamba waandishi hawa waliovuviwa, wahariri au watungaji walikuwa na uhuru wa kuchagua, kupanga, kufanya na kuweka kimuhtasari matukio na mafundisho ya maisha ya Yesu (kama vile *Howto Read the Bible for All Its Worth* by Fee and Stuart, kur. 113-148).

- E. Kuna desturi za kanisa lka kwanza kutoka kwa Papias, askofu wa Hierapolisi (mnamo 130 B.K), ambayo imeandikwa katika Eusebius'*Historical Ecclesiasticus*3:39:16, kwamba Mathayo aliandika Injili katika Kiaramu.

Hata hivyo wanazuoni wa kisasa wamekataa desturi hii kwa sababu

1. Kiyunani cha Mathayo hakina tabia za fasiri kutoka kwenye Kiaramu

2. kuna mizaha ya Kiyunani (kama vile Mt. 6:16; 21:41; 24:30)

3. Nukuu nyingi zaidi za Agano la Kale zinatoka katika Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani (LXX) na siyo

Maandiko ya Kiebrania ya Kimasoreti

Inawezekana kwamba Mt. 10:3 ni dokezo la uandishi wa Mathayo. Linaongeza "mtoza ushuru" baada ya jina lake. Maoni haya haya ya kushusha hayapatikani katika Marko. Mathayo pia hakuwa mtu anayejulikana sana katika kanisa la kwanza au Agano Jipya. Kwanini desturi nyingi zijengeke na kukua juu ya jina lake na Injili hii ya kwanza ya Kitume?

## TAREHE

- A. Kwa namna nyingi tarehe ya Injili imeunganishwa kwenye tatizo la Vitabu vya Injili. Ni Injili gani iliyoandikwa kwanza na nani alikopa kutoka kwa nani?
1. Eusebius, katika *Historical Ecclesiasticus*, 3:39:15 alisema Mathayo alitumia Marko kama mwongozo wa kimuundo
  2. Augustine, hata hivyo alimuita Marko "mfuasi wa kambi" na mweka kifupisho cha Mathayo.

- B. Mbinu bora zaidi ingekuwa kujaribu kuweka mipaka ya tarehe zinazosemekana
1. Lazima ilikuwa imeandikwa kabla ya mwaka 96 au 115 B.K
    - a. Clement wa Rumi (96 B.K) alitoa maelezo ya Injili ya Mathayo katika barua yake kwa Wakorintho.
    - b. Ignatius (110-115B.K), Askofu wa Antiokia, alinukuu Mt. 3:15 katika barua yake *To the Smyrneans*, 1:1
  2. Swali gumu zaidi ni kwa namna gani ingekuwa mapema kuandikwa?
    - a. Kidhahiri baada ya matukio kuandikwa ambayo ingekuwa kati kati ya miaka ya 30
    - b. wakati mwingine ilitakiwa kupita kwa mahitaji yake, utungaji na mzunguko
    - c. Kuna uhusiano gani wa Mt. 24 kwenye uharibifu wa Yerusalemu mnamo miaka ya 70 B.K? Sehemu ya Mathayo inamaanisha mfumo wa kidhabihu ilikuwa bado ikitenda kazi (Mt. 5:23-24; 12:5-7; 17:24-27; 26:60-61). Hii inamaanisha tarehe kabla ya mwaka 70 B.K.
    - d. Ikiwa Mathayo na Marko ziliandikwa wakati wa huduma ya Paulo (mnamo 48-68 B.K), kwanini hakuwahi kuwarejerea? Irenaeus ananukuliwa na Eusebius katika *Historical Ecclesiasticus* 5:8:2, kusema kwamba Mathayo aliandika Injili yake wakati Petro na Paulo walikuwa Rumi. Petro na Paulo wote waliuwawa wakati wa utawala wa Nero ambao uliisha mnamo mwaka 68 B.K
    - e. dhanio la mwanzoni kabisa la wanazuoni wa kisasa ni mnamo mwaka 50 B.K
- C. Wanazuoni wengi wanaamini kwamba Injili nne zinahusiana zaidi na vituo vya kijiografia vya Ukristo kuliko waandishi wa kidebuti. Mathayo inaweza kuwa iliandikwa kutokea Antiokia ya Shamu kwasababu ya mambo ya kikanisa ya Uyahudi/Mataifa, yawezekana mnamo mwaka 60 B.K au angalau kabla ya 70 B.K.

## WAPOKEAJI

- A. Kama uandishi na tarehe ya Injili haijulikani, hivyo wapokeaji pia. Inaonekana bora kuhusisha hili kwa wote Wayahudi waaminio na Mataifa. Kanisa Antiokia ya Shamu ya karne ya Kwanza inashabihiana na wasifu huu zaidi sana.
- B. Origen ananukuliwa na Eusebius katika *Historical Ecclesiasticus* 6:25:4, kwamba ilikuwa imeandikwa kwa ajili ya Wayahudi waaminio.

## UANISHAJI WA KIMUUNDO

- A. Ni kwa namna gani Injili hii imeundwa? Mtu mmoja anaweza kutafta kusudio la asili la mwandishi aliyevuviwa kwa kuchambua muundo wa kitabu kizima.
- B. Wanazuoni wamependekeza miundo kadhaa
1. Safari za kijiografia za Yesu
    - a. Galilaya
    - b. kaskazini mwa Galilaya
    - c. Peroya na Yudea (wakati akisafiri kwenda Yerusalemu)
    - d. ndani ya Yerusalemu
  2. Vipengele vitano vya kimaudhui vya Mathayo. Vinaweza kutambuliwa kwa tungo inayojirudia rudia, "na wakati Yesu alipokuwa amemaliza mambo haya"(kama vile Mt. 7:28; 11:1; 13:53; 19:1; 26:1). Wanazuoni wengi wanaona vipengele hivi vitano kama jaribio la Mathayo kumuonesha Yesu kama "Musa mpya," kwa kila kipengele kikipewa maelezo kwa moja ya vitabu vitano vya Musa (Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu na Kumbu kumbu la Torati)
    - a. muundo tofauti tofauti ambao unaenda mbadala kati ya masimulizi na vipengele vya
    - b. muundo wa kithiolojia na maisha ambayo inachukua tungo inayojirudia rudia, "kutokea muda ule Yesu alianza. . ." (kama vile Mt. 4:17; 16:21), hivyo kugawanya kitabu katika vipengele vitatu (Mt. 1:1-4:16; 4:17-16:20; na Mt. 16:21-28:20)
    - c. Msisitizo wa Mathayo juu ya vifungu vya habari vya unabii kwa kutumia maneno ya msingi "utimilizwaji"(kama vile Mt. 1:22; 2:15,17,23; 4:14; 8:17; 12:17; 13:35; 21:4; 27:9 and 27:35)

- C. Ile "injili" ni aina ya uandishi wa kipekee ya fasihi. Hayaelezei masimulizi ya maisha. Sio masimulizi ya kihistoria. Ni aina ya kifasihi inayoweka uchaguzi wa kithiolojia yenye muundo mkali wa kimaana. Kila waandishi wa injili walichagua kutokea katika matukio ya maisha na mafundisho ya Yesu kwa kipekee kumwasilisha kwa kusudio kwa hadhira iliyokusudiwa. Injili zilikuwa ukanda wa kiinjili.

### **MZUNGUKO WA KWANZA WA USOMAJI (Kutoka "[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)")**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Dhamira ya kitabu kizima
2. Aina ya fasihi iliyotumika (uwasilishaji)

### **MZUNGUKO WA PILI WA USOMAJI (Kutoka "[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)")**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Mada ya sehemu ya kwanza ya fasihi
2. Mada ya sehemu ya pili ya fasihi
3. Mada ya sehemu ya tatu ya fasihi
4. Mada ya sehemu ya nne ya fasihi
5. N.k.

# MATHAYO 1

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA*				
UBS <sup>4</sup>	NKJV	NRSV	TEV	NJB
Ukoo wa Yesu	Ukoo wa Yesu	Kuchipuka kwa Yesu	Rekodi ya Familia ya	Ukoo wa Yesu
Kristo	Kristo	Kifalme	Yesu	(2-6)
1:1	1:1-7	1:1	1:1	1:1-16
1:2-6a		1:2-6a	1:2-6a	(2-6)
1:6b-11		1:6b-11	1:6b-11	(6b-11)
1:12-16		1:12-16	1:12-16	(12-16)
1:17		1:17	1:17	1:17
Kuzaliwa kwa	Kristo anazaliwa	Kuzaliwa kwa	Kuzaliwa kwa Yesu	Yesu anamfanya Yesu
Yesu Kristo	na Mariamu	Yesu	Kristo	kuwa mwanawe
1:18-25	1:18-25	1:18-25	1:18-21	1:18-25
			1:22-23	(23)
			1:24-25	

\* Ingawa hazijavuviwa, migawanyo ya aya ndiyo ufunguo wa kuelewa na kufuatilia kusudio la asili la mwandishi. Kila tafsiri ya kisasa imegawanya na kufanya muhtasari wa aya. Kila aya ina mada kuu, kweli au wazo. Kila toleo limebeba hiyo mada kwa namna yake ya pekee. Unaposoma maandiko ya mwandishi jiulize ni tafsiri ipi inawiana na uelewa wako wa somo na mgawanyo wa mistari.

Katika kila sura lazima tusome Biblia kwanza na kujaribu kutambua somo (aya), kisha tulinganisha na matoleo ya kisasa. Ni pale tunapoelewa kusudi la asili la mwandishi kwa kufuata mantiki yake na jinsi alivyojieleza tunaielewa kwa Biblia kiukweli. Ni mwandishi wa asili tu aliyevuviwa —wasomaji hawana haki ya kurekebisha ujumbe. Wasomaji wa biblia wana wajibu wa kutumia ukweli uliovuviwa kwenye siku na maisha yao.

Fahamu kwamba maneno yote ya kiufundi na vifupisho vimefafanuliwa kwa kirefu kwenye nyaraka zifuatazo: [Maelezo Fasaha Ya Muundo Wa Sarufi Za Kiyunani\(Brief Definitions of Greek Grammatical Structure\)](#), [Uhakiki Wa Tofauti Za Kiandishi\(Textual Criticism\)](#), [Ufafanuzi na Maelezo ya Kimaandiko\(Glossary\)](#).

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia"](#))

### KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembele katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA MISTARI 1-25

A. Orodha ya watu wa kale inayopatikana katika Mt. 1:1-17 na Luka 3:23-38 hazina ufanano. Kuna dhana kubwa mbili kwa utofautiano:

1. Mathayo aliandika kimsingi kwa hadhira wa kiyahudi na kuandikwa katika uzao wa Yusufu kuridhisha matakwa na shughuli za kisheria za Kiyahudi , wakati Luka aliandika kwa Mataifa na kuandika katika ukoo wa Mariamu (Luther). Rekodi zote mbili zinamtazama Yesu zikirudi nyuma wakati wa Daudi,

lakini Luka anakwenda mbali zaidi akirudi nyuma zaidi mpaka wakati wa Adamu (yaweze kana alikuwa anaandika kwa ajili ya mataifa).

2. Mathayo aliandika ndani ya ukoo wa wafalme wa Yuda waliomfuatia baada ya Daudi (au baada ya uhamishoni, wale ambao waliweza kuwa katika utawala baada yake), wakati Luka aliandika ukoo wenyewe halisia.

B. Ukoo huu ungeweza kutumikia makusudi ya kutoa utambulisho wa kikabila wa Yesu na kuonesha utimilizwaji wa unabii (kama vile Mwa. 49:8-12 and 2 Samweli 7). Unabii uliotimilizwa (kama vile Mt. 1:22; 2:15,17,23; 4:14; 8:17; 12:17; 13:35; 21:4; 27:9,35) ni ushahidi wa nguvu kwa Biblia ya juu zaidi na mamlaka ya Kimungu ya Historian a muda.

C. Mstari wa 17 unatoa uelewa wa msingi kwanini baadhi ya wazao/mababu hawatajwi. Mwandishi alikuwa akitumia muundo wa kimahesabu wa mfungo wa utatu "kizazi cha kumi na nne" kuelezea ukoo wa Yesu.

D. Katika ufunguzi huu wa masimulizi ya uzao kuna nukuu nne za Agano la Kale (kama vile Mt. 1:23; 2:6,15,18) ambayo inajuuhiha ain mbali mbali za unabii.

1. Mt. 1:23 — Isa. 7:14 ni aina nyingi a utimilizwaji wa unabii. Mtoto alizaliwa katika siku ya Isaya, kama vile Mt. 1:15-16; hata hivyo neno la Kiebrania katika Mt. 1:14 sio "bikra" (*bethoolah*, kama vile BDB 143), bali "binti wa umri wa kuolewa" (*almah*, kama vile BDB 761 II). Namini katika uzao wa Yesu wa kuzaliwa na bikra tu!
2. Mt. 2:6 — Mika 5:2 inashangaza sana, unabii hasa ulioandikwa miaka 750 kabla ya tukio unaelezea. Eneo la kuzaliwa kwa Yesu si kitu ambacho angeweza kurekebisha au kuondoa. Aina hii ya unabii wa mambo yajayo unathibitisha (a) maarifa ya Mungu (uweza wake wa kutawala) historia na (b) uvuvio na upekee wa Biblia. Hakuna kitabu kingine chochote katika dini zote zilizomo ulimwenguni zene unabii wa mambo yajayo!
3. Mt. 2:15 — Hosea 11:1 na Mt. 2:18 — Yeremia 31:15 zote ni nabii zenye muundo unaofanana. Kitu kilichotokea katika maisha ya Israeli kinatokea tena katika maisha ya Yesu na mwandishi wa Agano Jipya analielewa kama ishara ya kinabii.

E. Raymond E. Brown, *An Introduction to the New Testament* (ukur. 175), anatoa maoni makubwa kuhusu muundo wa ukoo wa Mathayo.

1. mababa wa imani - majina ya kwanza kumi na nne
2. wafalme wa Kiisraeli - majina ya pili kumi na nne
3. mababu wasiojulikana - majina ya tatu kumi na nne

Ukoo huu una muundo mkali sana na una ubaguzi. Haijulikani kwa nini.

1. mbinu ya kifasihi (kumbusho)
2. muwakilishi wa kihesabu/namba
  - a. 7 x 2; Luka inaorodhesha mababu 77
  - b. barua za jina la Kiebrania la Daudi linaongeza mpaka 14
3. mashuhuri au mababu wacha Mungu
4. wanawake/wanaume: Mataifa/Wayahudi (ujumuishwaji wa kimakusudi)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB(LILOBORESHWA) MATHAYO 1:1

<sup>1</sup> Kitabu cha ukoo wa Yesu Kristo, mwana wa Daudi, mwana wa Ibrahimu.

1:1

NASB "maandiko ya ukoo wa Yesu Masihi,"

NKJV "kitabu cha ukoo wa Yesu Kristo"

NRSV "masimulizi ya ukoo wa Yesu Masihi"

TEV "Hii ni rekodi ya familia ya Yesu Kristo"

NJB "andiko ya ukoo wa Yesu Kristo"

Ukoo (kama vile Mwa. 5:1 au "rekodi," kama vile Mwa. 2:4) inaelezea mkono wa Mungu katika utimilizwaji wa ahadi Zake. Agano Jipya ni utimilizwaji wa Agano la Kale. Katika baadhi ya desturi matumizi ya ukoo ni ushahidi kwa historia yenye kuaminiwa na kuwa na mashiko.

☐"**mwana wa Daudi**" Hiki kilikuwa ni cheo kwa Masihi aliyehaidiwa ambacho kilihamisha ukoo wake wa kiyahudi wa kifalme (kama vile Mwa. 49:8-12). Alikuwa uzao wa mwanamke, Mwa. 3:15; uzao wa Ibrahimu, Mwa. 22:18; uzao wa Yuda, Mwa. 49:10 na uzao wa Daudi, 2 Sam. 7:12-14, 16. Tungo hii ilikuwa maelezo ya kimasihhi yanayojitokeza mara kwa mara (kama vile Mt. 9:27; 12:33; 15:22; 20:30-31; 21:9,15; 22:42).

☐"**mwana wa Ibrahimu**" Ukoo wa Luka unaelezea ukoo kuanzia mbali zaidi. Luka ilikuwa imeandikwa kwa Mataifa, hivyo iliweka msisitizo uzao wa kibinadamu uliozoeleka (kama vile Mwa. 12:3; 22:18). Mathayo iliandikwa kwa ajili ya Wayahudi, hivyo ilijikita juu ya mwanzo wa familia ya Kiyahudi, Ibrahimu. Katika ukoo wa Mathayo "Ibrahimu" na "Daudi" wanaainishwa kwa muundo wake wa kimahesabu (yaani makundi matatu ya 14)

### ANDIKO LA NASB (LILLOBORESHWA) MATHAYO 1:2-6a

<sup>2</sup> Ibrahimu alimzaa Isaka; Isaka akamzaa Yakobo; Yakobo akamzaa Yuda na ndugu zake; <sup>3</sup> Yuda akamzaa Peresi na Zera kwa Tamari; Peresi akamzaa Esromu; Esromu akamzaa Aramu; <sup>4</sup> Aramu akamzaa Aminadabu; Aminadabu akamzaa Nashoni; Nashoni akamzaa Salmoni; <sup>5</sup> Salmoni akamzaa Boazi kwa Rahabu; Boazi akamzaa Obedi kwa Ruthu; Obedi akamzaa Yese; <sup>6</sup> Yese akamzaa

1:2 "**Yuda**" Yuda alikuwa mmoja wa watoto wa Yakobo (kama vile Mwa. 49:10; Kumb. 33:7). Mistari 2-6 inafuata ukoo wa 1 Nyak. 1-3 katika namna ya ukomo.

1:3 "**Peresi na Zera**" Peresi na Zera walikuwa mapacha (kama vile Mwa. 38:27-30). Ukoo wa Kimasihhi ulikuja kupitia Peresi. Hiki kipengele cha ukoo (Mt. 1:3-5) kinafuata Ruthu 4:18-22.

☐"**Tamari**" Tamari alikuwa mkamwana wa Yuda aliyepata ujauzito kwa yeye (kama vile. 38:12 na kuendelea). Halikuwa jambo la kawaida kuwajumuisha wanawake katika orodha ya ukoo wa Kiyahudi. Kadhaa wanajumuishwa hapa katika Mathayo kusisitiza kwamba ukoo wa Masihi haukuwa umejikita katika utaifa au juhudi za kutimiza vigezo. Wanawake watatu walio-orodheshwa – Tamari, Rahabu, na Ruthu walikuwa wa Mataifa na wanne, Bethsheba alikuwa ameolewa na Mhiti. Mataifa, hata wanawake wanajumuishwa kwa ajili ya mguso wa ujumuishi wa kithiolojia!



**1:5 "Rahabu"** Rahabu alikuwa kahaba wa Kikanaani aliyewasaidia wapelelezi (kama vile Yos. 2:13; 6:17,23,25). Katika desturi za Kiyahudi na Ukristo Rahabu alikuwa mfano wa nguvu ya toba (kama vile Ebr. 11:31; Yakobo 2:25).

☐**"Ruthu"** Ruthu alikuwa Mmoabu (kama vile Ruthu 1). Wamoabu walikuwa wamekatazwa kuingia katika kusanyiko la Israeli (kama vile Kumb. 23:3). Alikuza imani ya Mataifa na wanawake upendo jumuisho wa Mungu. Alikuwa bibi wa Mfalme Daudi.

**1:6 "alikuwa mke wa Uria"** Hii inarejerea kwa Bethsheba, mama wa Suleimani (kama vile 2 Samweli 11 na 12), ambaye kama Rahabu na Ruthu hakuwa Myahudi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 1:6b-11**

**mfalme Daudi. <sup>7</sup> Sulemani akamzaa Rehoboamu; Rehoboamu akamzaa Abiya; Abiya akamzaa Asa; <sup>8</sup> Asa akamzaa Yehoshafati; Yehoshafati akamzaa Yoram; Yoram akamzaa Uzia; <sup>9</sup> Uzia akamzaa Yothamu; Yothamu akamzaa Ahazi; Ahazi akamzaa Hezekia; <sup>10</sup> Hezekia akamzaa Manase; Manase akamzaa Amoni; Amoni akamzaa Yosia; <sup>11</sup> Yosia akamzaa Yekonia na ndugu zake, wakati wa ule uhamisho wa Babeli.**

**1:7-11** Sehemu hii (ikiwa na baadhi ya tofauti) inafuatia 1 Nyak. 3:10-15.

**1:7**

**NASB, NKJV,**

**TEV, NJB** "Asa"

**NRSV** "Asafu"

Mfalme huyu Myudea aliitwa Asa katika 1 Wafalme. 15:9 na 1 Nyak. 3:10. "Asa" inapatikana katika MSS L na W na inashabihiana na muktadha. Maandiko ya kale ya Kiyunani, α, B, na C kwa kushangaza "Asafu." Hili lilikuwa jina la mkurugenzi wa kwaya wa Daudi (kama vile Zab. 50, 73,83). Wakosoaji wengi wa kimaandiko wanadhania kwamba hili ni kosa la mnakili wa kale, au ni toleo tu la herufi ya jina la mfalme.

**1:8** Wafalme watatu wa Yuda kati ya Yoram na Uzia wameondolewa (1) Ahazia (kama vile 2 Wafalme. 8,9; 2 Nyak. 22); (2) Yoashi (kama vile. 2 Wafalme. 11:2; 12:19-21; 2 Nyak. 24); na (3) Amazia (kama vile 2 Wafalme. 14; 2 Nyak. 25).

Sababu ya kuondolewa haijulikani. Nadharia mbili ni: (1) Yoram alikuwa ameo na kushawishiwa na mkewe, Athalia, binti wa Yezebeli na hivyo dhambi zake za kuabudu miungu mingine zilihamishwa kwa kizazi cha tatu (kama vile Kumb. 5:9) au (2) Mathayo inaweka muundo wa ukoo katika sehemu tatu za mababu 14 kila moja (Mt. 1:17). Hii ingekuwa sehemu ya tatu.

**1:9 "Yothamu akamzaa Uzia"** Katika 2 Wafalme. 15:1-7 na 1 Nyak. 3:12 Uzia anaitwa Azaria. Alikuwa ni mchamungu aliyepigwa na ukoma kwasababu alitoa sadaka kwa namna mbaya.

**1:10 "Hezekia"** Hezekia alikuwa mmoja wa wafalme wa Yuda (Asa, Yehoshaphat, Uzia, Hezekia, na Yosia). Maisha yake yanaandikwa katika 2 Wafalme. 18-20, 2 Nyak. 29-32, na Isa. 36-39.

☐**"Manase"** Alikuwa mmoja wa watoto wa Hezekia. Manase alikuwa anasemekana kuwa mfalme muovu zaidi

katika historia ya Yuda (kama vile 2 Wafalme 21:2-7). Pia alitawala kwa muda mrefu zaidi, miaka hamsini na tano (kama vile 2 Wafalme. 21; 2 Nyak. 33).

☐ **"Amoni"** Alikuwa mwana wa Manase na baba wa Yosia (kama vile 2 Wafalme. 21:18-19,23-25; 1 Nyak. 3:14; 2 Nyak. 33:20-25). Baadhi ya maandiko ya Kiyani, א, ב<sup>c</sup>, na C, yana jina, "Amosi." Tatizo hili la maandiko haya ni kama la Mt. 1:7.

☐ **"Yosia"** Mfalme mwingine mcha Mungu wa Yuda, Yosia alikuwa na miaka minane alipofanywa kuwa mfalme (kama vile 2 Wafalme. 22-23; 2 Nyak. 34,35). Wanazuoni wengi wanaamini kwamba baba mwenye haki, mtoto mbaya wa baba mwenye haki na mwana mwenye haki wa baba mbaya katika Ezekieli (kama vile Ezek. 18:5-9, 10-13, 14-18) zilikuwa rejea za moja kwa moja kwa Hezekia, Manase na Yosia.

**1:11 "Yekonia"** Pia alikuwa akiitwa Konia (kama vile Yer. 22:24) na Yehokiamu (kama vile 2 Wafalme 24-25). Aliyefuata kutoka mwisho kwa Daudi Mfalme kabla ya mateka wa Babeli, Yekonia alikuwa aidha na miaka 8 alipokalika kiti cha utawala (kama vile 2 Nyak. 36:9) au miaka 18 (kama vile 2 Wafalme 24:8) na alitawala miezi mitatu tu (kama vile 1 Nyak. 3:16-17; Yer. 24:1; 29:2). Ezekieli anaweka tarehe ya unabii wake kutoka mwaka wa uhamishoni mwa mfalme huyu kwa Nebukadreza II mnamo 597 B.K. (kama vile Ezek. 1:1,2; 8:1; 20:1; 24:1; 26:1; 29:1; 30:20; 31:1; 32:1,17; 33:21; 40:1).

☐ **"Kuchukuliwa kwenda Babeli"** Kuchukuliwa huku kulitokea chini ya Nebukadreza II. Yerusalemu ilikuwa imekamatwa na jeshi la Babeli mara kadhaa-mnamo 605, 597, 586, na 582 K.K. kuchukuliwa kadhaa tofauti kulitokea.

1. Kuchukuliwa kwa Danieli na marafiki zake watatu mnamo mwaka 605 K.K.
2. kuchukuliwa kwa Yehokiam, Ezekieli, na askari makumi elfu na wafua vyuma mnamo 597 K.K. (kama vile 1 Wafalme 24:10-17)
3. kuchukuliwa sehemu kubwa ya watu waliobaki (jiji la Yerusalemu liliharibiwa) mnamo 587/586 K.K., 2 Wafalme 25
4. Uvamizi wa mwisho na kuchukuliwa kwa Yuda mnamo mwaka 582 K.K. Kama malipizi ya kuuawa kwa gavana mteule wa Nebukadreza, Gedelia na mlinzi wake wa heshima wa Kibabeli

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 1:12-16**

<sup>12</sup> Na baada ya ule uhamisho wa Babeli, Yekonia akamzaa Shealtieli; Shealtieli akamzaa Zerubabeli; <sup>13</sup> Zerubabeli akamzaa Abihudi; Abihudi akamzaa Eliakimu; Eliakimu akamzaa Azori; <sup>14</sup> Azori akamzaa Sadoki; Sadoki akamzaa Akimu; Akimu akamzaa Eliudi; <sup>15</sup> Eliudi akamzaa Eleazari; Eleazari akamzaa Matani; Matani akamzaa Yakobo; <sup>16</sup> Yakobo akamzaa Yusufu mumewe Mariamu aliyemzaa YESU aitwaye Kristo.

**1:12 "na Shealtieli baba wa Zerubabeli"** Zerubabeli alikuwa kiongozi wa Wayahudi katika kurudi mara ya pili kutoka uhamisho wa Babeli, kurudi kwa kwanza kukiwa chini ya Sheshbazzar (kama vile Ezra 1:8; 5:14). Alikuwa ukoo wa Daudi (kama vile Ezra 2-6). Katika 1 Nyak. 3:16-19, Baba yake anaorodheshwa kama Pedaiya na babu yake kama Shealtieli. Maneno yanayojulikana ya Kiebrania yalikuwa ya kawida na yangeweza kurejerea vipengele tofauti kadhaa vya ndugu. Kwa namna hiyo Shealtieli alikuwa ni mjomba. Mkanganyiko huu unaweza ukaelezewa ikiwa Shealtieli alimchukua Zerubabeli baada ya baba yake Pedaiya kufariki (kama vile Ezra 3:8; 5:2; Neh. 12:1; Hag. 1:1).

Majina haya mawili pia yanatokea katika ukoo wa Luka lakini katika kipindi cha baadaye.

**1:13-15** Majina kutoka kwa mwana wa Zerubbabel Abihudi kwenda kwa Yakobo hayajulikani kutoka katika vyanzo vya Agano la Kale.

**1:14 "Zadoki"** Huyu hakuwa kuhani mwaminifu wa siku za Daudi (kama vile 2 Sam. 20:25; 1 Nyak. 16:39) kwasababu Zadoki wa Mathayo ni wa kabila la Yuda na sio Mlawi.

**1:16 "Yusufu mume wa Mariamu"** "kuposwa," ambayo inatokea sana katika orodha hii ya mababa wengine, inaachwa! Yusufu anatajwa kama baba halali na ukoo wake unatajwa kwasababu hii ilikuwa kile Wayahudi wa karne ya kwanza walikitaka kisheria. Lakini hakuwa baba yake wa ukweli wa kibaiyolojia. Yesu alizaliwa na bikra kwa uwezo wa Roho wa Mungu (kama vile Mt. 1:23-25; Luka 1:34-35).

☐ **"aitwaye Masihi"** "Kristo" (NKJV) ilikuwa fasiri ya Kiyunani ya neno la Kiebrania *Masihi* (BDB 603, kama vile 1 Sam. 2:10,35; 2 Sam. 22:51; Zab. 2:2 18:51; 89:38,51; 132:10,17; Dan. 9:24,25), ikiwa na maana "mpakwa mafuta." Yesu alikuwa Mtumishi maalumu wa YHWH (kama vile Isa. 7:14; 9:1-7; 11:1-5; 52:13-53:12), Yule ajaye ambaye angeanzisha kizazi kipya cha haki (kama vile Isaya 61, 65-66). Angalia Mada Maalumu katika Mt. 8:20.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 1:17**

<sup>17</sup> Basi vizazi vyote tangu Ibrahimu hata Daudi ni vizazi kumi na vinne; na tangu Daudi hata ule uhamisho wa Babeli ni vizazi kumi na vinne; na tangu ule uhamisho wa Babeli hata Kristo ni vizazi kumi na vinne.

**1:17 "vizazi"** Hii haikuwa historia kamili ya ukoo. Neno la Kiebrania "vizazi" lilikuwa tata na linaweza kuwa lingemaanisha babu wa babu wa babu wa babu au muhenga.

☐ **"kutoka katika ule uhamisho wa Babeli hata Masihi, vizazi kumi na nne"** Kuna sehemu tatu za vizazi kumi na nne zinazoorodhesha (1) Ibrahimu mpaka kwa Daudi, (2) Daudi mpaka uhamishoni, na (3) Uhamishoni mpaka Yesu. Majina kumi na tatu tu yanatajwa. Utaratibu wa namba unamaanisha kwamba baadhi ya majina yaliachwa nje (kama vile 1 Nyak. 1-3). Baadhi ya Wafasiri wanaamini kwamba orodha hizi zilizo katika muundo wa kumi na nne zimejikita katika thamani ya kihesabu ya Konsonanti ya jina la Daudi katika Kiebrania (*daleth*, 4 + *waw*, 6 + *daleth*, 4 = 14).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 1:18-25**

<sup>18</sup> Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi. Mariamu mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu. <sup>19</sup> Naye Yusufu, mumewe, kwa vile alivyokuwa mtu wa haki, asitake kumwaibisha, aliazimu kumwacha kwa siri. <sup>20</sup> Basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu. <sup>21</sup> Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao. <sup>22</sup> Hayo yote yamekuwa, ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii akisema, <sup>23</sup> Tazama, bikira atachukua mimba, Naye atazaa mwana; Nao watamwita jina lake Imanueli; Yaani, Mungu pamoja nasi. <sup>24</sup> Naye Yusufu alipoamka katika usingizi, alifanya kama malaika wa Bwana alivyomwagiza; akamchukua mkewe; <sup>25</sup> asimjue kamwe hata alipomzaa mwanawe; akamwita jina lake YESU.

**1:18 "kuzaliwa"** Kuna matoleo tofauti ya maandiko ya Kiyunani "mwanzo" [*mwanzo*] na "kuzaliwa" [*gennasis*]. Neno *mwanzo* yawezekana lilikuwa la asili (kama vile MSS P<sup>1</sup>,  $\alpha$ , B, C; UBS<sup>4</sup> ililiwekea alama ya B). Wakati maneno yote mawili yanamaanisha "kuzaliwa," la kwanza lina uwanja mpana wa visawe (uumbaji, ukoo, yaani, "mwanzo

mpya katika Yesu kama Adamu wa pili, kama vile Rum. 5:12-21) na lingeweza kumaanisha "kuposwa." Imekuwa imependekezwa kwamba waandishi wa baadaye walibadili neno la kwanza kwenda "kuzaliwa" na kupelekea kubadilishwa kwa elimu ya Kristo (wajuzi) vumi (kama vile *The Orthodox Corruption of Scripture* na Bart P. Ehrman, kur. 75-77).

☐ **"aliyeposwa na Yusufu"** Kuposwa kulikuwa desturi ya kuunganisha ya kisheria ya Kiyahudi. Wawili waliishi mbali mbali lakini wakihesabiwa kimkatiba kuwa wameoana. Ni kifo tu au talaka ndiyo ingeweza kuvunja utaratibu wa uchumba.

<b>NASB</b>	<b>"alionekana ana mimba kwa Roho Mtakatifu"</b>
<b>NKJV</b>	<b>"alionekana ana mtoto kwa Roho Mtakatifu"</b>
<b>NRSV</b>	<b>"alionekana kuwa na mimba ya mtoto kwa Roho Mtakatifu"</b>
<b>TEV</b>	<b>"alionekana kama mwenye kutegemea kuzaa mtoto kwa Roho Mtakatifu"</b>
<b>NJB</b>	<b>"alionekana kuwa na mtoto kwa Roho Mtakatifu"</b>

Hii inarejerea kuzaliwa na bikra ambalo halikuwa na tendo la kingono kwa Mariamu au Roho Mtakatifu. Hii ilikuwa ni utimilizwaji wa unabii wa Mwa. 3:15 (" Nami nitaweka uadui kati yako na mwanamke na kati ya uzao wako na uzao wake; Atakuponda kichwa, nawe utamponda kisigino"), katika namna ya utimizwaji kadhaa, wa Isa. 7:14 ("Hivyo Bwana mwenyewe atakupa ishara: Tazama Bikra atazaa mwana wa kiume naye atamwita jina lake Immanueli"). Cha kushangaza, hakuna mahubiri ya kitume katika Matendo ya Mitume au Nyaraka yanayotaja hili, yawezekana kwasababu ingeweza kuchanganywa na hadithi za uungu za Wayunani-Warumi (miungu ya mlima Olympus mara kwa mara ilichukua wanawake wa kibinadamu na kupata watoto pamoja nao).

**1:19 "akiwa mtu mtauwa"** Yule "mtu mtauwa" ilimaanisha mtu wa sheria kwa namna za Sheria za Musa na desturi za Kinywa za wakati wake. Haimaanishi kwamba hakuwa na dhambi; Nuhu na Ayubu walikuwa watauwa kwa namna hii hii inayofanana (kama vile Mwa. 6:9 na Ayubu 1:1).

☐ **"kumuacha kwa siri"** Yusufu angeweza kukamilisha hili kupitia taratibu mbili za kisheria: (1) kumkana wazi mbele ya mahakama au (2) uwasilishaji wa mswaada ulioandikwa wa talaka mbele ya mashahidi wawili (kama vile Kumbu kumbu la Torati 24). Mariamu hakuwa ameshirikisha maono juu ya ujauzito wake na Yusufu. Sheria ya Agano la Kale ilidai hukumu ya kifo kwa kukosa uaminifu wa kingono (kama vile Kumb. 22:20-21,23-24).

**1:20** Yusufu alikuwa anajua kuhusu ujauzito wa mke wake aliyemposa kwa kupitia mjumbe wa kimalaika. Katika Luka 1:26 malaika anatambuliwa kama Gabrieli (kama vile Mt. 1:19; Dan. 8:16; 9:21).

Neno "ndoto" (*onar*) inatokea mara tano katika sura mbili za kwanza za Mathayo (kama vile Mt. 1:20; 2:12,13,19,22), lakini haitokei tena mpaka 27:19 na hakuna tena katika Agano Jipya.

☐ **"malaika wa Bwana"** Tungo hii inatumika katika njia mbili katika Agano la Kale.

1. malaika (kama vile Mwa. 24:7,40; Kut. 23:20-23; 32:34; Hes. 22:22; Waamuzi. 5:23; 1 Sam. 24:16; 1 Nyak. 21:15ff; Zek. 1:28)
2. Ni njia ya kurejerea kwa YHWH (kama vile Mwa. 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16; Kut. 3:2,4; 13:21; 14:19; Waamuzi. 2:1; 6:22-24; 13:3-23; Zek. 3:1-2)

Mathayo anatumia tungo mara kwa mara (kama vile Mt. 1:20,24; 2:13,19; 28:2), lakini siku zote kwa namna ya #1 juu. Agano Jipya halitumii namna #2 isipokuwa Mdo. 8:26 na 29, ambapo, "malaika wa Bwana" anapewa usambamba wa kimaana wa Roho Mtakatifu.

**1:21 "utamwita jina lake Yesu"** Jina hili (Kiebrania, Yoshua) lilimaanisha "YHWH anaokoa," "YHWH analeta wokovu," au "YHWH ni Mkombozi" (baadhi ya vitenzi vinaweza kuwekwa, kama vile Luka 1:31). Angalia [MADA MAALUM: JINA LA BWANA](#) katika Mt. 18:20.

Jina YHWH humaanisha

1. Hili ni jina ambalo linaaksi uungu kama Mungu atengenezaye maagano; Mungu kama Mwokozi, mkombozi! Wanadamu huvunja maagano, bali Mungu ni mwaminifu kwa neno lake, ahadi, agano (kama vile Zab. 103).

Jina hili linatajwa kwa mara ya kwanza katika muunganiko na *Elohim* katika Mwa. 2:4. Hakuna hadithi mbili za uumbaji katika Mwanzo 1-2, bali misisitizo miwili: (1) Mungu kama muumbaji wa ulimwengu (wa mwili unaoonekana) na (2) Mungu kama muumbaji maalumu wa mwanadamu. Mwanzo 2:4 inaanza na ufunuo maalumu kuhusu nafasi za upendeleo na kusudi la mwanadamu, pamoja na tatizo la dhambi na uasi unaohusianishwa na nafasi ya kipekee.

2. Katika Mwa. 4:26 inasemwa "*watu wakaanza kuliitia jina la Bwana*" (YHWH). Hata hivyo, Kut. 6:3 inamaanisha kwamba watu wa kimaagano wa kale (mababa wa imani na familia zao) walimjua Mungu tu kama *El-Shaddai*.

Jina YHWH ilinaelezwa mara moja tu katika Kut. 3:13-16, haswa Mt. 1:14. Hata hivyo maandiko ya Musa mara kwa mara yanafasiri maneno kwa mizaha inayojulikana na sio asili (kama vile Mwa. 17:5; 27:36; 29:13-35).

Kumekuwa na nadharia kadhaa juu ya jina hili (ikichukuliwa kutoka IDB, vol. 2, kur. 409-11).

- a. kutoka katika mzizi wa kiarabu, "kuonesha upendo wa dhati"
- b. kutoka katika mzizi wa Kiarabu "kupuliza" (YHWH kama Mungu wa dhoruba)
- c. kutoka katika mzizi wa Ugaritiki (Kikanaani) "kuzungumza"
- d. kufuatia maelezo ya Kifoenike, kisababishi cha wakati endelevu "Yeye atoshelezaye," au "Yule athibitishaye"
- e. kutoka katika muundo wa Kiebrania *Qal* "yeye aliye," au "yeye aliyepo" (katika namna ya ubaadaye, "yeye atakayekuwepo")
- f. kutoka katika muundo wa Kiebrania *Hiphil* "Yeye asababishaye kuwa"
- g. kutoka katika mzizi wa Kiebrania "kuishi" (mfano Mwa. 3:20), ikimaanisha "Aishiye milele, yule Aishiye tu"
- h. kutoka katika muktadha wa Kut. 3:13-16 mzaha katika muundo wa kauli isiyotimilifu ikitumika katika namna ya utimilifu, "nitaendelea kuwa vile nilivyo zoea kuwa" au "nitaendelea kuwa vile ambavyo nimekuwa" (kama vile J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Old Testament*, ukur. 67)

Jina kamili YHWH mara kwa mara inaelezwa katika ufupisho au yawezekana katika muundo wa asili.

- (1) *Yah* (mfano, Hallelu - yah)
- (2) *Yahu* (majina, mfano, Isaya)
- (3) *Yo* (majina, mfano Yoeli)

3. Katika Uyahudi wa baadaye jina hili la kiagano lilikuwa takatifu sana (ile kipimo cha kisarufi) kwamba Wayahudi waliuwa na hofu kulisema isije wakavunja amri ya Kut. 20:7; Kumb. 5:11; 6:13. Hivyo walitafuta neno mbadala la Kiebrania kuwa "mmiliki," "bwana," "mume," "bwana" -*adon* au *adonai* (bwana wangu). Wakati walipokuja kwa YHWH katika kusoma kwao maandiko ya Agano la Kale walitaja "bwana." Hii ndiyo sababu YHWH inaandikwa Bwana katika Tafsiri ya Kingereza.
4. Kama ilivyo *El*, mara kwa mara YHWH inaunganishwa na maneno mengine ili kutilia mkazo tabia fulani za Mungu wa Agano wa Israeli. Wakati kuna muunganiko mwingi sana wa maneno, haya hapa ni baadhi.
  - a. *YHWH - Yireh* (YHWH atatoa), Mwa. 22:14
  - b. *YHWH - Rophekha* (YHWH ni mponyaji wako), Kut. 15:26

- c. *YHWH - Nissi* (YHWH bendera yangu), Kut. 17:15
- d. *YHWH - Meqaddishkem* (YHWH ni yule awatakasaye), Kut. 31:13
- e. *YHWH - Shalom* (YHWH ni amani), Waamuzi. 6:24
- f. *YHWH - Sabbaoth* (YHWH wa majeshi), 1 Sam. 1:3,11; 4:4; 15:2; mara kwa mara katika manabii)
- g. *YHWH - Ro'i* (YHWH ni mchungaji wangu), Zab. 23:1
- h. *YHWH - Sidqenu* (YHWH ni haki yetu), Yer. 23:6
- i. *YHWH - Shammah* (YHWH yuko pale), Ezek. 48:35

## MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU

- A. *El* (BDB 42, KB 48)
1. maana ya asili ya jina la jumla la kale kwa ajili ya Uungu haijulikani, ingawa wanataaluma wengi wanaamini linatoka katika mzizi wao wa lugha ya Akkadia, “kuwa shupavu” au “kuwa mwenye nguvu” (kama vile Mwanzo 17:1; Hesabu 23:19; Kumb 7:21; Zab. 50:1).
  2. Katika hekalu la miungu ya Wakanaanani mungu mkuu ni *El* (maandiko ya Ras Shamra), akaitwa “baba wa miungu” na “bwana wa mbinguni”
  3. Kalika Biblia *El* mara nyingi huwa haliambatani na maneno mengine. Miunganiko hii ilifanyika njia ya kuainisha tabia za Mungu.
    - a. *El-Elyon* (Mungu aliye Mkuu sana BDB 42 & 751 II), Mwanzo 14:18-22; Kumb. 32:8; Isa. 14:14
    - b. *El-Roi* (“Mungu aonaye” au “Mungu ajifunuaeye Mwenyewe” BDB 42 & 909), Mwanzo 16:13
    - c. *El-Shaddai* (“Mungu Mkuu” au “Mungu mwenye huruma zote” au “Mungu wa mlima”), BDB 42 & 994) Mwanzo 17:1; 35:11; 43:14; 49:25; Kutoka 6:3
    - d. *El-Olam* (Mungu wa milele yote), Mwanzo 21:33. Neno hili linaunganishwa na ahadi ya Mungu kwa Daudi, II Sam. 7:13,16
    - e. *El-Berit* (Mungu wa Agano”), BDB 42 & 136), Waamuzi 9:46
  4. *El* inalinganishwa na
    - a. YHWH katika Zaburi. 16:1-2; 85:8; Isa. 42:5, Hes. 23:8
    - b. *Elohim* katika Mwanzo 46:3; Ayubu 5:8, “Mimi ni *El, Elohim* wa baba yako
    - c. *Shaddai* katika Mwanzo. 49:25
    - d. “wivu” katika Kut. 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15
    - e. “reheema” katika Kumb. 4:31; Neh. 9:31
    - f. “mkuu na mzuri” katika Kumb. 7:21; 10:17; Neh. 1:5; 9:32; Dan. 9:4
    - g. “maarifa” katika I Sam. 2:3
    - h. “kimbilio langu” katika II Sam. 22:33
    - i. “mlipa kisasi wangu” katika II Sam. 22:48
    - j. “mtakatifu” katika Isa. 5:16
    - k. “muweza” katika Isa. 10:21
    - l. “wokovu wangu” katika Isa. 12:2
    - m. “mkuu na mwenye nguvu” katika Yer. 32:18
    - n. “anayepatiliza: katika Yer. 51:56
  5. Muunganiko wa majina yote makubwa ya Agano la Kale yanapatikana katika Joshua 22:22 (*El, Elohim, YHWH*, kurudiwa)
- B. *Elyon* (BDB 751, KB 832)
1. Maana yake ya msingi ni “juu,” “aliyetukuzwa,” au “kuinuliwa” (kama vile Mwanzo 40:17; I Wafalme. 9:8; II Wafalme. 18:17; Neh. 3:25; Yer. 20:2; 36:10; Zab. 18:13).
  2. Inatumika katika namna ya usambamba wa majina mengine/vyeo vya Mungu.
    - a. *Elohim* – Zab. 47:1-2; 73:11; 107:11
    - b. *YHWH* - Mwanzo 14:22; II am. 22:14

- c. *El-Shaddai* - Zab. 91:1,9
  - d. *El* - Hes. 24:16
  - e. *Elah* - iliyotumika mara kwa mara katika Danieli 2-6 na Ezra 4-7, inaunganishwa pamoja na *illair* (Kiaramaiki kwa ajili ya “Mungu aliye Juu”) katika Dan. 3:26; 4:2; 5:18,21
3. Mara kwa mara inatumika kwa wasio waisraeli.
- a. Melkizedeki, Mwanzo 14:18-22
  - b. Balaamu, Hes. 24:15
  - c. Musa akizungumzia Mataifa katika Kumb. 32:8
  - d. Injili ya Luka katika Agano Jipya, akiandika kwa Mataifa, pia akitumia maneno ya kufanana na Kiyunani *Hupsistos* (kama vile 1:32,35,76; 6:35; 8:28; Mdo 7:48; 16:17)
- C. *Elohim* (wingi), *Eloah* (umoja), inatumika kimsingi katika ushairi (BDB 43, KB 52)
1. Neno hili halipatikani nje ya Agano la Kale.
  2. Neno hili linaweza kumaanisha Mungu wa Israeli au miungu wa Mataifa (kama vile Kut. 12:12; 20:3). Familia ya Ibrahimu walikuwa Waabudu miungu wengi (kama vile Josh. 24:2).
  3. Inaweza kumaanisha waamuzi wa kibinadamu (kama vile Kut. 21:6; Zab. 82:6)
  4. Neno *elohim* pia linatumika juu ya viumbe vingine vya kiroho (malaika na mapepo) kama ilivyo katika Kumb. 32:8 (LXX); Zab. 8:5; Ayubu 1:6; 38:7.
  5. Katika Biblia cheo cha kwanza, jina kwa ajili ya Uungu (kama vile Mwanzo. 1:1). Linatumika bila mjumuisho mpaka Mwanzo. 2:4, ambapo linaunganishwa na YHWH. Kimsingi (kithiolojia) linamaanisha muumbaji, mtoshelevu na mpaji wa uhai wote juu ya sayari hii (kama vile Zab. 104). Ni sawa na kisawe *El* (kama vile Kumb. 32:15-19). Pia linaweza kuwa likifanana na YHWH kama Zab. 14 (*Elohim* KUR. 1,2,5; YHWH, kur. 2,6; hata *Adoni*, uk. 4) ni sawasawa kabisa na Zab. 53 (YHWH), isipokuwa kwa mabadiliko katika majina ya kiungu.
  6. Ingawa wingi unatumika juu ya miungu mingine, neno hili mara kwa mara linamaanisha Mungu wa Israeli lakini siku zote lina kitenzi cha umoja kuelezea matumizi ya imani juu ya Mungu mmoja kama mtawala juu ya dunia nzima.
  7. Inashangaza kwamba jina lililozoeleka kwa imani juu ya Mungu mmoja wa Israeli liko katika Wingi! Ingawa hakuna uhakika, hapa zipo nadharia.
    - a. Lugha ya Kiebrania ina maneno mengi yenye wingi, mara kwa mara hunatumika kuonesha msisitizo. Kwa ukaribu yanayohusiana na hili ni tabia ya kisarufi cha Kiebrania kinachoitwa “wingi wa ukuu,” mahali ambapo wingi unatumika kukuza dhana.
    - b. Hii inaweza kumaanisha baraza la kimalaika, ambalo Mungu hukutana nalo mbinguni na ambalo linafanya kazi za utekelezaji (kama vile I Wafalme. 22:19-23; Ayubu 1:6; Zab. 82:1; 89:5,7).
    - c. Inawezekana hata inaaksi ufunuo wa Agano Jipya wa Mungu mmoja katika nafsi tatu. Katika Mwanzo. 1:1 Mungu anaumba; Mwanzo 1:2 Roho anachepusha na kutoka katika Agano Jipya Yesu ni wakala wa Baba katika Uumbaji (kama vile Yohana 1:3,10; Rum. 11:36; I Kor. 8:6; Kol. 1:15; Ebr. 1:2; 2:10).
- D. YHWH (BDB 217, KB 394)
1. Hili ni jina ambalo linaaksi Uungu kama Mungu afanyaye maagano: Mungu kama mwokozi, mkombozi! Wanadamu wanavunja agano, lakini Mungu ni mwaminifu kwa neno lake, ahadi, agano (kama vile Zab. 103). Jina hili kwanza linatajwa katika munganiko pamoja na *Elohim* katika Mwanzo. 2:4. Hakuna masimulizi mawili ya uumbaji katika Mwanzo. 1-2, lakini msisitizo
    - a. Mungu kama muumbaji wa ulimwengu (wa kimwili, Zaburi 104)
    - b. Mungu kama muumbaji maalum wa uanadamu (Zaburi 103).
 Mwanzo 2:4-3:24 inaanza na ufunuo maalum kuhusu nafasi ya upendeleo na kusudi la mwanadamu, pia tatizo la dhambi na uasi unaohusianishwa na nafasi ya upekee.
  2. Katika Mwanzo 4:26 inasema “wanadamu wakaanza kuliitia jina la BWANA” (YHWH). Hata hivyo Kutoka. 6:3 inamaanisha kwamba watu wa kwanza wa agano (wahudumu wa uzao wa kiume na familia zao) walimfahamu Mungu tu kama *El-Shaddai*. Jina YHWH linaelezewa kwa mara moja tu katika Kut. 3:13-16, hasa mstari wa 14. Hata hivyo, maandiko ya Musa mara kwa mara yanafasiri

maneno kwa utani maarufu na sio kwa asili na chanzo chake (kama vile Mwanzo. 17:5; 27:36; 29:13-35). Kumekuwa na nadharia kadhaa juu ya maana ya jina hili (likichukuliwa kutoka IDB, vol. 2, kur. 409-11).

- a. kutoka katika mzizi wa kiarabu, “kuonesha upendo wa dhati”
  - b. kutoka katika mzizi wa kiarabu “kupuliza” (YHWH kama Mungu wa dhoruba)
  - c. kutoka katika mzizi wa lugha ya Ugariti (ya Wakanaani) “kuzungumza”
  - d. kufuatia maandiko ya Ki-Foenike, KAULI SABABISHI ENDELEVI ikimaanisha “Yeye anayetoshela,” au “yeye anaye anzisha”
  - e. kutoka katika muundo wa Kiebrania *Qal* “Yeye ambaye yupo,” au “Yeye aliyepo sasa” (katika namna ya wakati ujao, “Yeye atakayekuwako”)
  - f. kutoka katika muundo wa kiebrania *Hiphil* “yeye asababishaye kuwa”
  - g. kutoka katika mzizi wa Kiebrania “kuishi” (mfano Mwanzo. 3:20), maana “Mungu mmoja tu aishiye milele”
  - h. kutoka katika muktadha wa Kut. 3:13-16 mbadilishano juu ya muundo wa KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU iliyotumika katika namna ya KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU, “nitaendelea kuwa vile nilivyokuwa” au “nitaendelea kuwa vile ambavyo siku zote nimekuwa” (kama vile J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Old Testament*, ukurasa wa 67 Jina kamili la YHWH mara kwa mara linaelezwa katika vifupisho au yawezekana katika muundo wa asili
    - (1) *Yah* (mfano Hallelu – yah, BDB 219, kama vile Kut. 15:2; 17:16; Zab. 89:8; 104:35)
    - (2) *Yahu* (majina mfano Isaya)
    - (3) *Yo* (majina mfano Joeli)
3. Katika Dini ya Kiyahudi ya baadaye jina la kiagano lilifanyika kuwa takatifu sana (Ni jina la kiebrania la Mungu lililofasiriwa kwa herufi nne) kwamba Wayahudi walikuwa na hofu kusema ili wasije wakavunja amri ya Kut. 20:7; Kum. 5:11; 6:13. Hivyo, alitafta mbadala wa neno la Kiebrania “mmiliki,” “Mkuu,” “mume,” “bwana”—*adon* au *adonai* (bwana wangu). Walipofika kwa YHWH katika kusoma kwao maandiko ya Agano la Kale walitamka “bwana.” Hii ndio maana YHWH inaandikwa BWANA katika fasiri za Kiingereza.
4. Kama ilivyo kwa *El*, mara kwa mara YHWH inaunganishwa na maneno mengine kusisitiza tabia fulani za Mungu wa Agano wa Israeli. Wakati kuna muunganiko mwingi wa maneno, hapa ni baadhi.
- a. *YHWH - Yireh* (YHWH atatoa), Mwanzo. 22:14
  - b. *YHWH - Rophekha* (YHWH ni mponyaji wako), BDB 217 & 950, *Qal* HALI YA KUENDELEA), Kutoka. 15:26
  - c. *YHWH - Nissi* (YHWH ni bendera yangu), BDB 217 & 651, Kutoka. 17:15
  - d. *YHWH - Meqaddishkem* (YHWH yeye awatakasaye, BDB 217 & 872, *Piel* HALI YA KUENDELEA), Kut. 31:13
  - e. *YHWH - Shalom* (YHWH ni amani BDB 217 & 1022), Waamuzi. 6:24
  - f. *YHWH - Sabbaoth* (YHWH wa majeshi, BDB 217 & 878), I Sam. 1:3,11; 4:4; 15:2; mara kwa mara katika manabii)
  - g. *YHWH - Ro’l* (YHWH ni mchungaji wangu, BDB 217 & 944, *Qal* HALI YA KUENDELEA), Zab. 23:1
  - h. *YHWH - Sidqenu* (YHWH ni haki yetu, BDB 217 & 841), Yer. 23:6
  - i. *YHWH - Shammah* (YHWH yupo hapa, BDB 217 & 1027), Ezek. 48

☐ "kwa maana atawaokoa watu wake na dhambi zao" Yesu alikuja kwa makusudi matatu tofauti.

1. kumfunua Baba kiukamilifu
2. kuwapa wanadamu mfano wa kuufuata
3. kumkomboa mwanadamu kutoka katika dhambi

Mwanzo 3 iliyoathiri maisha yote juu ya sayari hii (kama vile Rum. 8:20-23). Yesu alikuja kufa katika nafasi yetu (kama vile Marko 10:45; Yohana 1:29; 2 Kor. 5:21; Flp. 2:6-11; Isaya 53). Ahadi ya mwa. 3:15 inatimilizwa katika Yeye!



**1:23** Mathayo anatumia utimilizwaji wa unabii wa Agano la Kale kama ushahidi mkuu kwa watu wa Kiyahudi kumuamini Yesu kama Masihi aliyehaidiwa.

1. Mt. 1:22 — Isa. 7:14
2. Mt. 2:15 — Hos. 11:1 na Kut. 4:22-23
3. Mt. 2:23 — yawezekana Isa. 11:1
4. Mt. 3:15 — "kutimiza haki yote"
5. Mt. 4:14 — Isa. 9:1,2
6. Mt. 5:17 — ". . .bali kutimiliza"
7. Mt. 8:17 — Isa. 53:4
8. Mt. 12:17 — Isa. 42:1,2,3,4
9. Mt. 13:14 — Isa. 6:9,10
10. Mt. 13:35 — Zab. 78:2
11. Mt. 21:4 — Isa. 62:11 au Zek. 9:9
12. Mt. 27:9 — Zek. 11:12,13

☐"**bikra**" Hii ni nukuu ya Isa. 7:14 kutoka katika Tafsiri ya Agano la Kale ya Kiyahudi. Katika Isaya neno la Kiebrania lililotumika lilikuwa *almah* (BDB 761 II), likimaanisha "binti wa umri wa kuolewa asiye na doa." Kulikuwa na uzao maalum katika siku za Ahazi (kama vile Isa. 7:15-16). Ni uzao wa mara moja tu wa kibikra uliowahi kutokea wala sio miwili; hivyo kutimilizwa kwa kihistoria katika siku za Isaya ilikuwa ishara kwa Ahazi lakini sio kwamba alipewa mimba na Roho Mtakatifu. Huu ni mfano wa utimilizwaji zaidi ya mmoja wa unabii. Ishara ya Ahazi ilikuwa ni jina la mtoto. Angalia fasiri yangu ya Isaya 1-39 katika mtandao wa wavuti katika [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org).

#### **NASB, NKJV**

<b>NJB</b>	"Immanueli"
<b>NRSV, TEV</b>	"Emmanueli"
<b>NJB</b>	"Mungu pamoja nasi"

Immanuel lilimaanisha "Mungu pamoja nasi" (BDB 769). Hii inaonesha kwamba kifungu cha Agano la Kale kilikuwa kikionesha zaidi ya siku zake chenyewe. Isaya 7-12 (Vita vya Shamu-Waefraimu) kwa kilele ilirejerea kuvaa mwili kwa Uungu, Yesu wa Nazareti (kama vile Yohana 1:1; 5:18; 10:33; 14:9-10; Flp. 2:6). Hata hivyo, lazima ikumbukwe kwamba Wayahudi hawakutarajia Masihi kuwa na Uungu. Wangeweza kuwa wameona majina makubwa kutoka Isa. 9:6 kama Sitiari. Haikutokea mpaka Agano Jipya ambapo Masihi kama Mungu aliyevaa mwili kwa uhalisia alifunuliwa.

**1:24-25** Mistari hii inathibitisha kuzaliwa kwa kiungu na bikra. Pia inamaanisha kwamba wanandoa walikuwa na maisha ya kawaida kabisa ya ndoa mara baada ya kuzaliwa kwa Yesu. Toleo la Textus Receptus, likifuatia maandiko ya Kiyunani ya C na D\*, K, W linaongeza "mwana wake wa kwanza," likimaanisha kulikuwa na watoto wengine.

#### **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini Mathayo ana ukoo mrefu kiasi hicho?
2. Kwanini ukoo wa Luka una tofauti na ule wa Mathayo?
3. Je Isaya alitabiri bikra kuzaa katika siku zake mwenyewe?

## MATHAYO 2

MIGAWANYO YA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA				
UBS <sup>4</sup>	NKJV	NRSV	TEV	NJB
Ujio wa mamajusi 2:1-6	Mamajusi toka Mashariki 2:1-12	Mamajusi 2:1-6	Wageni toka mashariki 2:1-2 2:3-4 2:5-6	Ujio wa mamajusi 2:1-12 (6)
2:7-12		2:7-12	2:7-8 2:9-11 2:12	
Kukimbilia Misri 2:13-15	Kukimbilia Misri 2:13-15	Kukimbilia Misri na Kurudi 2:13-15	Kukimbilia Misri 2:13 2:14-15a 2:15b	Kukimbilia Misri, mauaji kwa wasio Na hatia 2:13-15 (15b)
Mauaji ya watoto Wachanga 2:16-18	Mauaji kwa wasio na hatia 2:16-18	2:16-18	Mauaji ya watoto 2:16 2:17-18	2:16-18 (18)
Kurudo toka Misri 2:19-23	Nyumbani Nazareti 2:19-23	2:19-23	2:19-21	Toka Misri hadi Nazareti 2:19-23 (23c)

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka “[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)”)**

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembe katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 2:1-6**

<sup>1</sup> Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi zamani za mfalme Herode, tazama, mamajusi wa mashariki walifika Yerusalemu, wakisema, <sup>2</sup> Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliiona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia. <sup>3</sup> Basi mfalme Herode aliposikia hayo, alifadhaika, na Yerusalemu pia pamoja naye. <sup>4</sup> Akakusanya wakuu wa makuhani wote na waandishi wa watu, akatafuta

habari kwao, Kristo azaliwa wapi? <sup>5</sup> Nao wakamwambia, Katika Bethlehemu ya Uyahudi; kwa maana ndivyo ilivyoandikwa na nabii,

<sup>6</sup> Nawe Bethlehemu, katika nchi ya Yuda,  
Hu mdogo kamwe katika majumbe wa Yuda;  
Kwa kuwa kwako atatoka mtawala  
Atakayewachunga watu wangu Israeli.

**2:1 "Bethlehemu"** jina hili linamaanisha "nyumba ya mkate." Hapa ni mahali alipozaliwa Boazi, na baadae, mfalme Daudi (tazama Ruthu 1:1 na 4:18-22). Kilikuwa ni kijiji kidogo chenye idadi ya wakaazi 300, kilichokuwa umbali wa maili 4-5 kusini mwa Yerusalemu. Kuna vijiji viwili vinavyotumia jina hili; kimoja kinapatikana Yuda (kama vile Mika 5:2) na kingine katika Zabuloni (kama vile Yos.19:15).

☐ **"mfalme Herode"** Herode mkuu alikuwa na wivu, mwendu asiyeaminika (Mwendu) mtawala aliyewekwa na Warumi. Alipanua ujenzi wa hekalu la pili ili kuwaridhisha wayahudi waliokuwa na mashaka juu ya kutawaliwa na mtawala asiyekuwa myahudi. Alikufa mwaka wa 4 b.k.; hivyo, lazima Yesu alikuwa ameshazaliwa mapema, inawezekana kati ya mwaka wa 6 – 4 b.k.

## MADA MAALUM: FAMILIA YA HERODE MKUU

### A. Herode Mkuu

1. Mfalme wa Yudea (37-4 k.k.), Idumean (kutoka Edom), ambao kupitia ujanja wa kisiasa na msaada wa Marko Antoni, waliweza kuteuliwa mtawala wa sehemu kubwa ya Palestina (Kanaani) kwa seneti ya kirumi katika 40 k.k.
2. Anatajwa katika Mt. 2:1-19 na Luka 1:5
3. Watoto wake
  - a. Herode Filipo (mwana wa Mariamne wa Simoni)
    - (1) mume wa Herodia (4 k.k. – 34 b.k)
    - (2) Anatajwa katika Mt. 14:3; Marko 6:17
  - b. Herode Filipo I (mwana wa Cleopatra)
    - (1) Mtawala wa eneo kaskazini na Magharibi ya bahari ya Galilaya (4 k.k. – 34B. k)
    - (2) anatajwa katika Luka 3:1
  - c. Herode Antipa
    - (1) mtawala wa Galilaya na Perea (4 k.k. – 39 b.k)
    - (2) Anatajwa katika Mt. 14:1-12; Marko 6:14,29; Luka 3:1,19; 9:7-9; 13:31; 23:6-12,15; Mdo. 4:27; 13:1
  - d. Archelaus, Herode wa Ethnarch
    - (1) Mtawala wa Yudea, Samaria, na Idumea (4 k.k. – 6 b.k)
    - (2) anatajwa katika Mt. 2:22
  - e. Aristobulus (mwana wa Mariamne)
    - (1) ametajwa kama Baba wa Herode Agrippa I aliyekuwa
      - (a) Mfalme wa Yudea (37-44 B.K)
      - (b) anatajwa katika Mdo. 12:1-24; 23:35
        - (i) mwana wa Herode wa Agrippa II  
– Mtawala ngome ya kaskazini (50-70 B.K)
        - (ii) mtoto wake wakike alitwa Bernice  
– mwenza wa kaka yake  
– anatajwa katika Mdo. 25:13-26:32
        - (iii) mtoto wake Drucilla  
– mke wa Felix

–anatajwa katika Mdo.24:24

B. Rejea za kibiblia kuhusu Herode

1. Herode Mtawala inanatajwa katika Mathayo 14:1 na kuendelea.; Luka 3:1; 9:7; 13:31, na 23:7, alikuwa mtoto wa Herode Mkuu . Wakati wa kifo cha Herode Mkuu, ufalme wake uligawanywa kwa watoto wake wa kiume. Neno "Tetrarch (Mtawala)" lilimaanisha "kiongozi wa sehemu ya nne." Herode huyu alijulikana kama Herode Antipa, ambalo limefupishwa kutoka katika Antipater. Alikuwa akitawala Galilaya na Perea. Hii ilimaanisha kiasi hiki katika huduma ya Yesu iliyokuwa katika mipaka ya kizazi hiki cha pili cha Mtawala Idumean.
  2. Herodia alikuwa mtoto wa kike wa kaka wa Herode Antipa aliyetwa Aristobulus. Lakini kabla alikuwa ameolewa na Filipo ambaye ni ndugu ayekuwa wa ukoo wa Herode Antipa. Huyu hakuwa Filipo mtawala aliyeongoza eneo tu la kaskazini ya Galilaya, lakini ndugu mwingine alikuwa Filipo, aliyeishi katika Rumi. Herodia alikuwa na binti mmoja na Filipo. Katika safari ya Herode Antipa kutembelea Rumi alikutana na alitongozwa na Herodita, aliyekuwa akitafta kutanuka kisiasa. Hivyo, Herode Antipa alimtaliki mkewe aliyekuwa Malkia wa Nabatean, na Herodia alimtaliki Filipo ili kwamba Herode Antipa aweze kuolewa. Yeye alikuwa pia ni dada wa Herode Agrippa I (kama vile Mdo. 12).
  3. Tunajifunza juu ya jina la mtoto wa kike wa Herodia , Salome, kutoka katika kitabu cha Flavius Josephus, Mabaki ya kale ya Wayahudi 8:5:4. Yawezekana lazima alikuwa na umri kati ya kumi na mbili na kumi na saba kwa wakati huu. Kwa dhahiri alikuwa akiongozwa na kurubuniwa vibaya na mama yake. Baadaye aliolewa na Filipo mtawala, lakini baadae alikuwa mjane.
  4. Kama miaka kumi baada ya kukamatwa kwa Yohana Mbatizaji, Herod Antipa alikwenda Rumi katika sherehe ya mke wake Herodia, kutafuta cheo cha mfalme kwakuwa Agrippa I kaka yake alikuwa hapo mwanzo amepewa cheo hicho. Lakini Agrippa I aliwaandikia Rumi na kuwashutumu Antipa kwa kushirikiana na Wa-Parthian, adui wa Rumi mwenye kuchukiwa kutoka katika Crescent ya rutuba (Mesopotamia). Mtawala kidhahiri aliamini Agrippa I na Herode Antipa, pamoja na mkewe Herodia, walikuwa wameenda uhamishoni Uhispania.
  5. Inaweza ikawa rahisi kukumbuka hawa wakina Herode tofauti tofauti kama wanavyowasilishwa katika Agano Jipya kwa kukumbuka kwamba Herode Mkuu aliuwa watoto katika Betlehemu; Herod Antipa aliuwa Yohana Mbatizaji; Herode Agrippa I aliuwa Mtume Yakobo; na Herode Agrippa II alisikia rufaa ya Paulo iliyowekwa katika kumbukumbu katika kitabu cha Matendo ya Mitume.
- C. Kwa ajili ya usuli wa taarifa juu ya familia ya Herode Mkuu, tazama kielelezo cha Flavius Josephus katika Mabaki ya kale ya Wayahudi.

2:1

NASB

"mamajusi"

NKJV, NRSV,

NJB

"wenye busara"

TEV

"watalamu wa nyota"

Aina hii ya hekima inawezekana asili yake ni Umedi, lakini walikuja kufahamika kuwa kundi la watu wenye hekima, washauri, na wanajimu juu ya Mesopotamia yote. Herodotus aliwaita makuhani wa Umedi (Herodotus I, 101). Wakati mwingine wanarejelewa katika fasihi za Babeli kama "Wakaldayo" (kama vile. Dan. 2:2-13).

Mmojawapo anaetajwa kwenye andiko hili inawezekana ni Zoroastrians kutoka Uajemi, lakini inawezekana ni myahudi aliyechukuliwa uhamishoni kama Daniel. Sio jambo la kawaida kwamba Mathayo aliwaandikia wayahudi, akihusisha habari ya wenye hekima (mataifa) kutoka mashariki ambapo Luka, aliwaandikia mataifa, akihusisha habari ya wachungaji wayahudi (wayahudi wa nje).

## MADA MAALUM:MIUJIZA

Katika zama za kale palitokea kuwepo na aina mbali mbali ya watu binafsi na makundi yaliyojijhusisha na aina tofauti ya miujiza. Miujiza ni muundo wa utendaji wa kidini.

1. Kutokea kwa muujiza wa kwanza kunapatikana katika tamaduni za awali zilizoandikwa (yaani., sumeri) katika uwepo wake wa kuundwa.
  - a. mkuu wa miungu, *Ea-enki*, anaitwa “Bwana mwenye umbo la binadamu” kwa sababu alimua *Apsu* kwa msaada wa uchawi
  - b. mwanae, *Marduk*, akamushinda *Tiamat* kwa sababu ya nguvu na uchawi wa baba yake
  - c. angalia Erica Reiner, *Surpu: A Collection of Sumerian and Akkadian Incantations*
2. miujiza ilikuwa ni ya muhimu sana huko Misri, ikiwahusisha *Thoth* na *Isis*. Hapakuwepo na utofauti kati ya miujiza mizuri na mibaya, kama ilivyo katika #1 na #3. Mara nyingi ulihusiana na
  - a. uponyaji
  - b. ufasiri wa ndoto
  - c. masuala ya kisiasa
  - d. ulimwengu wa vifo
3. miujiza huko Anatolia (kwenye tamaduni za Wahiti) ilifanana na #1. Palikuwepo na miujiza mizuri na mibaya. Ya kwanza ilikubaliwa na pili ilikataliwa. Mara nyingi wabibi vizee walitumika sambamba na makuhani. Kama ilivyokuwa watu wa ANE, waliiona miujiza kama sehemu iliyokubalika kwa kampeni za kijeshi.
4. Pana kundi la kijamii ya kikuhani toka Medea waliojijhusisha katika utabiri wa nyota walioitwa “Wakalidayo” (kama vile Dan. 1:20; 2:2,10,27; 4:7,9; 5:11; Mt. 2:1,7,16). Herodotus aliwaita “makuhani wa Kimidiani.” Walijijhusisha na utabiri na kudhibiti matukio ya mbeleni yaliyohusiana na mienendo na ushirikiano wa miungu nyota (yaani., sayari, kundi, vimondo).
5. Kuna simulizi chache zilizopo kuhusiana na miujiza ya Kaanani (yaani., lugha ya kisemitiki iliyoongelewa na watu wa Ugarit). Kwa wazi kabisa *El* alikuwa na nguvu nyingi na aliponya Mfalme wa Ugarit kwa miujiza (angalia “Hekaya za Mfalme Keret” ANET. 148b).
6. Makundi mengi ya kimiujiza yaliundwa na watu waliodai kuwa na uwezo wa kuhadaa nguvu za miujiza (Yaani. Mwa. 41:8,24; Kut. 7:11,22; 8:7,19; 9:11). Mara nyingi hizi nguvu (au miungu) ilionekana kuwa na mtafaruku na wanadamu na ukichukulia upande wa hizi nguvu au mwenye maarifa ya kuzimiliki anaweza kuzidhibiti hizo nguvu kwa matumizi binafsi( kama vile mafunjo ya kimiujiza ya karne ya tatu na ya nne b.k). hawa watu binafsi wangaliweza:
  - a. Kutabiri mambo ya mbeleni
  - b. Kuweza kudhibiti mambo yanayokuja
  - c. Kutabairi mambo yajayo na ndoto
  - d. Kulaani au kumlinda mtu, mji, taifa, jeshi n.k
7. Watenda miujiza, kama katika Mdo. 8:9,11 walidai kuwa na uwezo wa kuhadaa kwa nguvu za asili au za kimapepo kutenda matakwa yao. Hii mara nyingi ilihusiana na ibada ya kimiujiza. Watenda miujiza wa “kweli” mara nyingi waliwashambulia wenzao ambao hawakuweza kutenda ibada na litulujia kiusahihi. Hawa waliitwa wapotoshaji au wenye kuigiza.
8. Nguvu ya injili inaonekana kwenye huduma ya Paulo huko Efeso ambapo wale watenda miujiza wa mwanzo walipo ongoka, na mbele za watu wakavichoma vitabu vyao vya kimiujiza (yaani., ni kwa namna gani unaweza kutenda ibada za matambiko, liturujia na kuwa na mwili wa kibinadamu, kama vile Mdo. 19:19) badala ya kiviua.
9. Kwa usomaji zaidi angalia
  - a. Susan Garrett, *The Demise of the Devil*, Fortress Press, 1989
  - b. Merrill Unger, *Biblical Demonology*, Scripture Press, 1967
  - c. Hendrik Berkhof, *Christ and the Powers*, Herald Press, 1977
  - d. Waller Wink, *Naming the Powers*, Fortress Press, 1984
  - e. Clinton Arnold, *Three Crucial Questions About Spiritual Warfare*, Baker, 1997

10. Miujiza yote hii, utendaji wa mambo ya siri ni chukizo mbele ya YHWH na imekatazwa kwa watu wake (angalia maelezo katika Kumb. 18:10-14, kwenye mtandao)

■ **"wa mashariki"** tamaduni zinajaribu kuangalia ni wapi walitoka na walikuwa wangapi, kama vile asili yao na aina ya jamii yao, lakini Biblia haijasema chochote juu ya mambo haya.

**2:2 "mfalme wa Wayahudi"** hiki kilikuwa ni cheo cha Herode mkuu. Hili ni sawa na lile jina lililowekwa kwenye msalaba wa Yesu (kama vile Mt. 27:37). Ni njia ya kumrejelea Masihi (kama vile. 1 Sam. 8:7; Zab. 10:16; 29:10; 98:6).

**NASB, NKJV** "Kwa maana tuliiona nyota yake mashariki"

**NRSV** "tuliiona nyota yake katika mng'ao wake"

**TEV** "tuliiona nyota yake ikitokea mashariki"

**NJB** "tuliiona nyota yake iking'aa"

Hii ni dhahiri "kutoka mapambazuko ya jua." Hii inaweza kumaanisha: (1) "tuliiona nyota yake tulipokuwa mashariki," au (2) "tuliiona nyota yake ilipong'aa angani usiku." Haimanishi kwamba iling'aa mashariki kwa sababu nyota ingewangoza wao katika mwelekeo tofauti, ingawa iling'aa mashariki lakini ilienda upande wa magharibi mwa anga.

Ulimwengu wa kale ulihusisha kuzaliwa kwa mtu maalumu au matukio na tukio la unajimu. Mungu alijifunua kwao kwa njia ambayo wangeelewa kwa maana ya wao kuwakilisha ulimwengu unaomtafuta na kumwona Masihi myahudi. Hii "nyota" yamkini ilirejelea kwa unabii wa Hes. 24:17: " Namwona, lakini si sasa; Namtazama, lakini si karibu; Nyota itatokea katika Yakobo Na fimbo ya enzi itainuka katika Israeli."

**2:3 "alifadhaika, na Yerusalemu pia pamoja naye"** Herode mkuu alikuwa katili na mwenye kubadilika alipofadhaika, kila mmoja aliogopa! mfano muhimu wa ukatili wake ni alipokaribia kufa, alihofu kwamba hakuna hata mmoja ambaye angeomboleza juu yake, hivyo aliwafunga gerezani mafarisayo wengi ambao walisurubiwa walipokufa. Hii ilithibitisha kwamba siku ya kifo chake itakuwa siku ya kuhuzunisha. Amri haikutekelezwa, lakini hii ni taswira iliyoonyesha tabia yake.

**2:4 "wakuu wa makuhani wote na waandishi wa watu"** hili linarejelea kwa baraza kuu la wayahudi, wakuu wa sheria na mahakama ya kidini ya taifa la Kiyahudi, lilioundwa na viongozi 70 kutoka eneo la Yerusalemu. Liliikuwa linaongozwa na kuhani mkuu (Masadukayo, tazama mada maalumu katika Mt. 22:23), ambaye kwa muda huo nafasi hiyo ilimilikiwa na mamlaka ya Warumi. Baraza kuu la wayahudi kwa mara zote lilirejelewa kwa tungo "makuhani wakuu, waandishi (Mafarisayo, tazama mada maalumu katika Mt. 22:15), na wazee" (kama vile Mt. 26:57; 27:41; Marko 11:27; 14:43,53; Mdo. 4:5). Herode aliwakamata na kuwaua viongozi wengi wa Yerusalemu mapema miaka kadhaa hivyo inatia shaka ikiwa hii inarejelea viongozi wa baraza kuu la wayahudi.

## MADA MAALUM: MASADUKAYO

- I. Chimbuko la Kundi
  - A. Wasomi wengi wanaamini kuwa jina hili linatokana na Sadoki, mmoja wa makuhani wakuu wa Daudi (kama vile 2 Sam. 8:17; 15:24). Baadaye, Suleimani alimhamisha Abiathari kwa kuunga mkono uasi wa Adonia (kama vile 1 Flp. 2:26-27) na alimtambua Sadoki kama Kuhani Mkuu pekee (kama vile 1 Flp. 2:35). Baada ya uhamisho wa Babeli huu mpangilio wa kikuhani uliimarishwa tena katika Yoshua (kama vile Hag. 1:1). Hii familia ya Kilawi ilichaguliwa kwa ajili ya kusimamia hekalu. Baadaye wale waliokuwa miongoni mwa haya mapokeo ya kikuhani na wale wasaidizi wao waliitwa Wasadoki au Masadukayo.
  - B. Ile karne ya tisa B. K. mapokeo ya Walimu wa Kisheria kwa Dini ya Kiyahudi neno (*Aboth* Mwalimu wa Sheria) anasema Sadoki alikuwa mwanafunzi wa Antigonos wa Sokho (karne ya pili K.K.). Sadoki hakuelewa usemi maarufu wa mshauri wake, "baada ya kifo thawabu," na kuiendeleza thiolojia ambayo

ilipingwa hapo nyuma na, ambapo pia ufufuo wa mwili ulipingwa.

- C. Baadaye ndani ya Dini ya Kiyahudi Masadukato walitambuliwa na wafuasi wa Boethus. Boethus pia alikuwa mwanafunzi wa Antigonus wa Sokho. Huyu alikuwa theolojia ile ile ya Sadoki, ambayo ilipingwa hapo nyuma.
  - D. Hili jina Masadukayo halikuonekana hadi siku za Yohana Hyrcanus (135-104 B.K.), ambapo liliinukuliwa Josephus (kama vile *Antiquities* 13.10.5-6). Katika *Antiquities* 13.5.9 Josephus anasema hawa wanaishi "shule tatu za," Mafarisayo, Masadukayo, na Wa-Essene.
  - E. Kuna nadharia za uamsho ambazo zilitokana na kile kipindi cha juhudi za utawala wa Selucid kuwafanya wawe wayunani ukuhani uliokuwa chini ya Antiokio IV Epiphanes (175-163 K.K.). Wamakabayo walipoasi ukuhani mpya ulianza katika Simoni Makabayo (142-135 K.K.) na uzao wake (kama vile I Mak. 14:41). Hawa makuhani wakuu wapya wa Hasmonia bila shaka walikuwa mwanzo wa makuhani wakuu yawezekana ulikuwa mwanzo wa utawala wa Masadukayo wa kimakabila. Mafarisayo walihimarika katika kipindi hiki kutoka Hasidim (yaani, "waliotengwa," kama vile I Mak. 2:42; 7:5-23).
  - F. Kuna nadharia mpya (yaani, T. W. Manson) ambayo "Sadukayo" ni tafsiri ya neno la Kiyunani *sundikoi*. Hili neno lilirejea juu ya mamlaka za mahali pale pale ambazo zilijitokeza pamoja mamlaka ya Kirumi. Hili linaweza kueleza kwanini baadhi ya Masadukayo hawakuwa makuhani wa utawala wa kimakabila, bali walikuwa mojawapo ya Wakuu wa baraza la Sinagogi.
- II. Upekee wa Imani
- A. Haya yalikuwa makundi madogo madogo ya kikuhanu yasiyobadili msimamo (hawa walikubali kuwa Torati pekee kama iliyovuviwa) wa madhehebu ya maisha ya Kiyahudi wakati Hasmonean na vipindi vya Kirumi.
  - B. Hawa hasa walihusika na matukio ya hekalu, hitifaki, taratibu za dini, na liturujia.
  - C. Hawa walishikilia Torati iliyoandikwa yaani, Mwanzo – Kumbukumbu la Torati) kama utawala wa kikabila, lakini waliipinga desturi ya Orad (yaani, Buku la Sheria za Kiyahudi).
  - D. Hawa, kwa hiyo, walipinga mafundisho mengi yaliyotunzwa na kuendelezwa Mafarisayo
    1. ufufuo wa mwili (kama vile Mt. 22:23; Marko. 12:18; Luka 20:27; Matendo ya Mitume 4:1-2; 23:8)
    2. kufa kwa nafsi (kama vile *Antiquities* 18.1.3-4; *Wars* 2.8.14)
    3. uwepo wa kueleza mpangilio wa malaika (kama vile Matendo ya Mitume 23:8)
    4. hawa walichukulia "jino kwa jino" (yaani, *lex talionis*) kiuhalisi na waliunga mkono adhabu ya kimwili na adhabu za kifo (badala ya mapatano ya kifedha)
  - E. Eneo lingine la kithiolojia ilikuwa ni upinzani dhidi ya wazo la awali dhidi ya mapenzi huru. Ni makundi matatu yaliyotajwa na Josephus
    1. Wa-Essene walikubali aina ya nadharia ya maamuzi
    2. Masadukayo waliuondoa ule msisitizo juu ya mapenzi huru ya mwanadamu (kama vile *Antiquities* 13.5.9; *Wars* 2.8.14)
    3. Mafarisayo walishikilia namna fulani ya usawa wa uelekeo kati ya haya mawili
  - F. Katika maana moja ya migogoro kati ya makundi mawili (yaani, Masadukayo – Mafarisayo) yaliyoangalia mvutano kati ya makuhani na manabii wa Kitabu cha Agano la Kale. Mvutano mwingine ulizuka kutokana na ukweli kwamba Masadukayo waliwakilisha daraja la kijamii na umiliki wa ardhi. Hawa walikuwa wenye mamlaka (kama vile Josephus' *Antiquities* 13.10.6; 18.1.4-5; 20.9.1), ambapo Mafarisayo na waandishi walikuwa wasomi na wacha Mungu miongoni mwa watu wa mahali pale. Mvutano huu ungeweza kubainishwa kama hekalu humo Yerusalemu dhidi masinagogi ya maeneo yote.

Mvutano mwingine unaweza kuwakilisha ule ukaidi wa Masadukayo wa ushawishi wa mafundisho ya Zorostra juu ya thiolojia ya kifarisayo. Mifano ya thiolojia yao ni (1) elimu ya juu ya kimalaika iliyokuzwa sana; (2) ule uwili kati ya HWH na Shetani; na (3) maelekezo mapendekezo ya maisha ya nyuma katika kukua kwa maneno ya wazi. Haya mazidi ya wa-Essene na Mafarisayo walisababisha mwtikio wa kithiolojia wa Masadukayo. Walirudi kwenye kushikiria nafasi yao ya thiolojia yao ya Musa tu katika kujaribu kuzuia mawazo mengine ya makundi mengine ya kiyahudi.



III. Chimbuko la Taarifa

- A. Josephus ndiye chimbuko kuu la taarifa kuhusu Masadukayo. Alikuwa mbaguzi wa kujitoa kwake kwa Mafarisayo na nia katika kuweka wazi taswira chanya ya maisha ya kiyahudi ya Warumi.
- B. vyanzo vingine vya taarifa ni fasihi ya kiuahidi. Hata hivyo, hapa, pia, ubaguzi wa nguvu ni dhahiri. Masadukayo walikataa uhusiano na mamlaka ya desturi ya kinywa cha Wazee (yaani, Talmud). Maandiko haya ya Kifarisayo kwa uwazi yanafunua upinzani wao katika hali hasi, yawezekana ikiwa imetiwa chumvi (yaani mpinzani wa kubuni, mbinu) njia.
- C. Hakuna maandiko yanayojulikana ya Kisdakayo yenyewe ambayo yamedumu. Pamoja na uharibifu wa Yerusalemu na hekalu katika miaka ya 70 B.K nyaraka zote na ushawishi wa usomi wa kikuhani uliharibiwa.

Walitaka kuendeleza amani ya kimkoa na njia pekee ya kufanya hivyo katika karne ya kwanza ilikuwa ni kushirikiana na Rumi (kama vile Yohana 11:48-50).

☐ "akatafuta habari kwao" hii ni njeo ya wakati usiotimilifu yenye maana ya (1) alirudia kuuliza au (2) alianza kuuliza.

2:6 hili ni dokezo kwa Mika 5:2. Sio dondoo la kweli kutoka katika maandiko ya kimasoreti au tafsiri ya maandiko ya kale ya kiebrania. Unabii huu wa muhimu unaupatia ushahidi imara uvuvio wa Biblia. Mika aliandika yapata miaka 750 kabla ya kuzaliwa Kristo na bado akatabiri juu ya kijiji kidogo ambapo Masihi asingetarajiwa kuzaliwa. Ushahidi mkubwa wa majaribio kwa ajili ya uvuvio wa Biblia utabiri wa unabii ambao ni wa kipekee katika maandiko!

☐ "Atakayewachunga watu wangu Israeli" hii ni dondoo iliyochanganywa na mstari ulioongezwa kutoka 2 Sam.5:2.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 2:7-12**

<sup>7</sup> Kisha Herode akawaita wale mamajusi faragani, akapata kwao hakika ya muda tangu ilipoonekana ile nyota. <sup>8</sup> Akawapeleka Bethlehemu, akasema, Shikeni njia, mkaulize sana mambo ya mtoto; na mkiisha kumwona, nileteeni habari, ili mimi nami niende nimsujudie. <sup>9</sup> Nao waliposikia maneno ya mfalme, walishika njia; na tazama, ile nyota waliyoiona mashariki ikawatangulia, hata ikaenda ikasimama juu ya mahali alipokuwapo mtoto. <sup>10</sup> Nao walipoiona ile nyota, walifurahi furaha kubwa mno. <sup>11</sup> Wakaingia nyumbani, wakamwona mtoto pamoja na Mariamu mamaye, wakaanguka wakamsujudia; nao walipokwisha kufungua hazina zao, wakamtolea tunu; dhahabu na uvumba na manemane. <sup>12</sup> Nao wakiisha kuonywa na Mungu katika ndoto wasimrudie Herode, wakaenda zao kwao kwa njia nyingine.

2:7

NASB	" akapata kwao hakika ya muda tangu ilipoonekana ile nyota"
NKJV	"akapata kwao muda ilipoonekana nyota"
NRSV	"akajifunza kwao hakika ya muda tangu ilipoonekana nyota"
TEV	"na akapata toka kwao hakika ya muda tangu ilipoonekana ile nyota"
NJB	"akauliza kwao hakika ya muda gani ilipoonekana ile nyota"

Herode alikuwa na shauku ya umri wa mtoto. Iliwachukua miezi mingi sana mamajusi kusafiri kutoka Uajemi, Yesu alikuwa na kama umri wa mwaka mmoja au miwili wakati huu.

2:9

NASB	" ile nyota waliyoiona mashariki ikawatangulia, hata ikaenda ikasimama juu ya mahali alipokuwapo mtoto"
NKJV	"ile nyota walioiona mashariki ikawatangulia, hata ikaenda ikasimama juu ya mahali alipokuwapo mtoto mchanga"

<b>NRSV</b>	<b>"na kule, mbele yao, ikawatangulia nyota iliyong'aa, hata ikaenda ikasimama juu ya mahali alipowapo mtoto"</b>
<b>TEV</b>	<b>"na ikawatangulia mbele yao, hata ikaenda ikasimama juu ya mahali alipokuwapo mtoto"</b>
<b>NJB</b>	<b>"nyota waliyoiona iking'aa ikawatangulia, na kusimama juu ya mahali alipokuwapo mtoto"</b>

Kupata madhanio ya tafsiri. Naamini katika nguvu za Mungu, ingawa mara kwa mara siwezi kuelezea kwa namna gani au kwa nini. Nyota iliwatangulia na kusimama! Haistajabishi kwamba wengi baadhi waliiona au kutambua muhimu wake. Watu hawa walifunzwa ni nini watarajie katika anga nyakati za usiku. Tukio hili halifai katika mfano wa kawaida. Hivyo basi, sio tukio pekee la la asili. Huu mchanganyiko wa asili na nguvu za Mungu unafanana na mapigo juu Misri.

Mamajusi hawakuja muda sawa kama wachungaji. Mara zote inanishangaza mimi kwamba Mathayo, aliwaandikia wayahudi, wanatajwa ujio wa mataifa (waliona nyota) na Luka, anawaandikia mataifa, wanatajwa ujio wa wachungaji wa kiyahudi (waliosikia malaika). Ukweli wa theolojia ni dhahili kwa kila mtu anakaribishwa (mataifa, wayahudi waliokataruwa)!

**2:10 "walifurahi furaha kubwa mno" kwa nini walifurahi?**

1. kutafuta kwao kulitimilika
2. nyota iliendelea kuwaongoza
3. kulikuwa na sehemu ya kiroho kwenye utafiti wao (kama vile Mt. 2:11); walimpata Bwana na mfalme wao mpya!

Umakini wa tungo hii asili yake inatuongoza kwenye chaguo moja #3.

**2:11 "nyumbani"** ni dhahili wakati mwingine (kama miaka miwili) walipitia kutoka wakati wa kuzaa. Yusufu, Mariamu, na Yesu waliishi kwenye nyumba yao wenyewe.

☐ **"mtoto"** neno la kiyunani (*paidion*) limetumika hapa sio neno la kawaida kwa ajili ya "mtoto mchanga" (*brephos*, kama vile Luka 1:41,44; 2:12,16), lakini "mtoto anaanza kutembea" (kama vile. Luka 2:40; Mt. 18:2). Kuna muda mrefu wa nyakati kati ya ujio wa Wachungaji na mamajusi.

☐ **"dhahabu, uvumba na manemane"** Kwa sababu ya zawadi tatu zilizotolewa, utamaduni unadai kwamba walikuwa mamajusi watatu. Tertullian anaenda mbali zaidi hata anadai kwamba ni wafalme waliotajwa kwenye Isa. 60:3. Juhudi zaidi zimehitajika kutafsiri umuhimu wa zawadi, lakini ufafanuzi unaoeleweka ni kwamba zawadi hizi zilikuwa ghali sana na zilitumiwa na watu wa jamii ya Kifalme. Inawezekana walikuwa watimiza unabii wa Isa. 49:23 au Zab. 72:10-12.

**2:12 "Nao wakiisha kuonywa na Mungu katika ndoto"** Mungu aliongea na hawa mamajusi kama alivyojifunua kwa Mariam na Yusufu katika ndoto (kama vile Mt. 1:13,19). Walikuwa watu makini wa kiroho.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 2:13**

<sup>13</sup> Na hao walipokwisha kwenda zao, tazama, malaika wa Bwana alimtokea Yusufu katika ndoto, akasema, Ondoka, umchukue mtoto na mama yake, ukimbilie Misri, ukae huko hata nikuambie; kwa maana Herode anataka kumtafuta mtoto amwangamize.

**2:13 "malaika wa Bwana"** tazama muhtasari katika Mat. 1:20.

☐ **"Herode anataka kumtafuta mtoto amwangamize"** ujinga wa watu waovu unaweza kuonekana wazi katika kujaribu kwao kuzuia mapenzi ya Mungu.

## MADA MAALUMU: MAANGAMIZI (*apollumi*)

Neno hili lina elimu-maana pana, ambayo imesababisha mkanganyiko mkubwa katika kuhusianisha na dhana ya kithiolojia juu ya hukumu ya milele dhidi ya maangamizo. Maana halisi ya msingi inatoka kwenye neno *apo* pamoja na *ollumi*, likimaanisha kuharibu/angamiza.

Tatizo linalokuja kwenye matumizi ya neno hili kitamathari. Hili laweza kuonekana wazi katika toleo la Louw na Nida's *Greek-English Lexicon of the New Testament, Based On Semantic Domains*, juzuu. 2, uk. 30. Inaorodhesha maana nyingi za neno.

1. Angamiza (mfano Mt. 10:28; Luka 5:37; Yohana 10:10; 17:12; Mdo. 5:37; Rum. 9:22 toka juzuu. 1, uk. 232)
2. Kushindwa kupata (mfano Mt. 10:42, juzuu. 1, uk. 566)
3. kupoteza (mfano Luka 15:8, juzuu. 1, uk. 566)
4. Kutokufahamu eneo (mfano Luka 15:4, juzuu. 1, uk. 330)
5. kufa (mfano Mt. 10:39, juzuu. 1, uk. 266)

Gerhard Kittel, *Theological Dictionary of the New Testament*, vol. 1, ukurasa 394, anajaribu kuonyesha matumizi tofauti kwa kuorodhesha maana Nne:

1. kuangamiza au kuuwa (mfano Mt. 2:13; 27:20; Marko 3:6; 9:22; Luka 6:9; 1 Kor. 1:19)
2. Kupoteza au kupata hasara (mfano Marko 9:41; Luka 15:4,8)
3. kuangamia (mfano Mt. 26:52; Marko 4:38; Luka 11:51; 13:3,5,33; 15:17; Yohana 6:12,27; 1 Kor. 10:9-10)
4. kupotea (mfano Mt. 5:29-30; Marko 2:22; Luka 15: 4,6,24,32; 21:18; Mdo. 27:34)

baadaye alisema, "kwa ujumla tunaweza kusema kuwa mstari wa #2 na #4 inayaweka chini maelezo yanayohusiana na ulimwengu huu katika mihitasari ya injili, wakati mstari wa #1 na #3 inayashusha chini maelezo yanayohusiana na ulimwengu ujao, kama ilivyo katika kitabu cha Paulo na Yohana" (uk. 394).

Ukiangalia ndani humu kuna mkanganyiko. Neno lina elimu-maana pana ya utumiaji ambayo waandishi tofauti wa Agano Jipya wanaitumia katika maana tofauti. Nampenda Robert B. Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, ukurasa 275-277. Alihusianisha neno kwa watu wale kimaadili walikuwa wamekwisha haribika na wakisubiri utengano wa milele toka kwa Mungu dhidi ya wale watu wanaomjua Kristo na wana uzima wa milele ndani yao. Kundi la awali ni lile "lililookolewa" na kundi la kwanza ni lile "lililoangamizwa."

Robert B. Girdlestone, katika maaandishi yake yenye maneno yaliyokaribiana maana ya Agano la Kale, uk. 276, anaelekeza kuwa kuna sehemu nyingi ambazo neno hili laweza lisitafasiliwe kama maangamizi, "maumivu kama hayo yanakifanya kitu kiutendaji kionekana kutokuwa na maana kwa kusudi lake la awali."

1. Upotevu wa marhamu, Mt. 26:8
2. Uharibifu wa kutia divai katika viriba vikuukuu, Mt. 9:17
3. Uharibifu wa nywele, Luka 21:18
4. Uharibifu wa chakula, Yohana 6:27
5. Uharibifu wa dhahabu ipoteayo, 1 Pet. 1:7
6. Uharibifu wa ulmwengu, 2 Pet. 3:6
7. Uharibifu wa kimwili, Mt. 2:13; 8:25; 12:14; 21:41; 22:7; 26:52; 27:20; Rum. 2:12; 14:15; na 1 Kor. 8:11

Neno hili kamwe halirejerei maangamizi ya mtu, lakini mwisho wa uwepo wa kimwili. Pia mara nyingi linatumika katika maana iliyo sawa. "watu wote wanahesabika kuharibika kimaadili, yaani, wameshindwa kuchukuliana na kusudi ambalo kizazi kilifanywa kuwa viumbe hai" (uk. 276). Ukubarifu wa Mungu kwenye tatizo ya dhambi hii alikuwa ni Yesu Kristo (kama vile Yohana 3:15-16 na 2 Pet. 3:9). Wale wote walioikataa injili sasa wametizamishwa kwenye uharibifu mwingine, unaojumuisha mwili na roho (kama vile 1 Kor. 1:18; 2 Kor. 2:15; 4:3; 2 The. 2:10). kwa hoja nyingine iliyokinyume angalifu, moto ulao.

Binafsi (kama vile R. B. Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, uk. 276) hafikirii kuwa neno hili linadokeza maangamizi (kama vile E. Fudge, *The Fire That Consumes*). Neno "milele" linatumika pote kwa adhabu ya milele na uzima wa milele katika Mt. 25:46. Kulishusha thamani moja ni kuyashusha yote!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 2:14-15**

<sup>14</sup> Akaondoka akamchukua mtoto na mama yake usiku, akaenda zake Misri; <sup>15</sup> akakaa huko hata alipokufa Herode; ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii, akisema, Kutoka Misri nalimwita mwanangu.

**2:15 "kutoka Misri nalimwita mwanangu"** Hosea 11:1 ni chanzo cha dondoo hii ya Kinabii. Kwenye Agano la kale "mwanangu" linarejelea sawa kwa Israeli, mfalme, au Masihi. Wingi wa "wanangu" kwa dhahili unarejelea kwa malaika.

Hosea 11:1 katika muktadha inarejelea safari ya kutoka Misri. Hivyo huu ni mchezo wa neno "mwanangu," kiasili inarejelea Israeli. Mathayo peke yake ameandika tukio hili. Haiwezekani kuunda ukweli wa kupanga miaka na matukio ya maisha ya awali ya Yesu kutoka kwenye injili. Misri ilikuwa ni makazi ya jamii kubwa ya Kiyahudi. Yumkini hii ni alama ya safari ya pili au ukombozi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 2:16-18**

<sup>16</sup> Ndipo Herode, alipoona ya kuwa amedhihakiwa na wale mamajusi, alighadhabika sana, akatuma watu akawaua watoto wote wanaume waliokuwako huko Bethlehemu na viungani mwake mwote, tangu wenye miaka miwili na waliopungua, kwa muda ule aliouhakikisha kwa wale mamajusi. <sup>17</sup> Ndipo lilipotimia neno lililonenwa na nabii Yerima, akisema,

<sup>18</sup> Sauti ilisikiwa Rama,  
Kilio, na maombolezo mengi,  
Raheli akiwalilia watoto wake,  
Asikubali kufarijiwa,  
kwa kuwa hawako.

**2:16 "akawaua watoto wote wanaume .... miaka miwili na waliopungua"** Bethlehemu ulikuwa mji mdogo, hivyo basi inawezekana waliuawa watoto wachache waliohusika. Tungo hii "miaka miwili na waliopungua" iliimarisha umri wa Yesu kama mtoto anaeanza kutembea, sio mtoto mchanga, wakati wa ujio wa mamajusi.

**2:18 "Rama"** mstari wa 18 ni dondoo kutoka Yer. 31:15, lakini inasimuliwa katika Mwa. 48:7. Raheli, mama yake Yusufu, ana uhusiano na makabila kumi ya kaskazini, ambapo mwana wake mwingine, Benjamini, anahusiana na Yuda. Katika mama huyu mmoja jamii zote za Israeli zinaunganishwa. Mji wa Rama (maili 6 kaskazini mwa Yerusalemu) ulikua ni kituo cha usafirishaji wa makabila kumi ya kaskazini chini ya mtawala Sargon II wa Ashuru kwenye mwaka wa 722 b.k. Alama ya Raheli akiwalilia watoto wake.

<b>NASB</b>	"Kilio, na maombolezo mengi"
<b>NKJV</b>	"Kilio, na maombolezo mengi"
<b>NRSV</b>	"kilio na maombolezo makuu"
<b>TEV</b>	"sauti ya kilio kichungu"
<b>NJB</b>	"maombolezo na kilio kichungu"

Hili ni dokezo la mke kipenzi cha Yakobo, Raheli, aliyekuwa na watoto, ambao mmojawapo atakuwa sehemu ya makabila kumi ya kaskazini (baada ya muungano wa kifalme kugawanyika mwaka wa 922 k.k.) na mmoja atakuwa sehemu ya makabila ya kusini. Alionyesha kilio kama juu ya uhamisho wa watoto wake (kama vile. Yer. 31:15, inarejelea kuchukuliwa uhamishoni kwa Israeli mwaka wa 722 k.k. na Yuda mwaka wa 586 k.k.). Katika muktadha huu huzuni yake ni sitiari kwa ajili ya kifo cha watoto wa Bethlehemu kwa mkono wa Herode.

Baadhi ya machapisho ya Kiyunani yana kitenzi kimoja, "kilio" (yaani., κ, B, Z); mengine yameongeza "maombolezo," ambayo yametoka kwenye toleo la LXX la Yer. 31:15 (yaani, C, D, L, W). kama vile na baadhi ya machapisho mbalimbali mengi, yanafanya tofauti ndogo kwenye utambuzi wa maana ya mstari.

## ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 2:19-23

<sup>19</sup> Hata alipofariki Herode, tazama, malaika wa Bwana alimtokea Yusufu katika ndoto huko Misri, <sup>20</sup> akasema, Ondoka, umchukue mtoto na mamaye, ushike njia kwenda nchi ya Israeli; kwa maana wamekufa walioitafuta roho ya mtoto. <sup>21</sup> Akaondoka akamchukua mtoto na mamaye, akafika nchi ya Israeli. <sup>22</sup> Lakini aliposikia ya kwamba Arkelao anamiliki huko Uyahudi mahali pa Herode babaye, aliogopa kwenda huko; naye akiisha kuonywa katika ndoto, akasafiri pande za Galilaya, <sup>23</sup> akaenda, akakaa katika mji ulioitwa Nazareti; ili litimie neno lililonenwa na manabii, Ataitwa Mnazorayo.

**2:19 "malaika wa Bwana"** tazama muhtasari katika Mt. 1:20.

**2:22 "Arkelao"** Arkelao alikuwa katiri mmoja wa familia ya Herode ambaye Yusufu hakumwamini. Alitawala kusini mwa eneo la himaya ya Herode mkuu (Yuda, Samaria, na Edomu) kutoka mwaka wa 4 k.k. – 6 b.k. alipofukuzwa na Warumi kwenda Gaul kwa sababu ya ukatili wake.

**2:23 "Ataitwa Mnazorayo"** kijiji alichokulia Yesu kilitwa Nazareti. Hakikutajwa kwenye Agano la kale, kitabu cha maadili na sheria za wayahudi, au kwenye Joseph. Ni dhahili hayakuwa makazi hadi wakati wa Yohana Hyrcanus (yaani., Hasmonaen), aliyetawala kutoka mwaka wa 134-104 k.k. Uwepo wa Yusufu na Mariam kutoka kwenye kijiji hiki unadokeza kwamba ukoo wa Daudi uliishi hapa.

Yumkini kuna muunganiko wa elimu ya asili na historia ya maneno kati ya majina Nazareti na jina la Masihi "tawi," ambalo ni *netser* kwa kiebrania (kama vile. Isa. 11:1; Yer. 23:5; 33:15; Zak. 3:8; 6:12; Ufu. 5:5; 22:16). Huu ni ushahidi unaotafasiriwa na jambo hili kwamba hakuna nabii aliyetabiri kuwa Yesu alizaliwa au kukulia Nazareti, lakini walitabiri ujio wa mpakwa mafuta wa nasaba ya mfalme Daudi (yaani., Isa. 7:14; 9:1-7; 11:1-5; Dan. 2:44; 7:13-14, tazama mada maalumu katika Mt. 8:20).

Ni dhahili neno fedheha kwa sababu ya eneo lake la mataifa kuwa mbali kutoka Yerusalemu (kama vile. Yh 1:46 na Mdo. 24:5, hata kama ni hii, pia, ni unabii kama vile Isa. 9:1). Hii yumkini ni kwa nini inahusika na kuweka ubao juu ya msalaba wa Yesu (yaani., Yesu wa Nazareti, mfalme wa Wayahudi).

## MADA MAALUMU: YESU MNAZARETI

Kuna maneno mbalimbali ya Kiyunani ambayo Agano Jipya hutumia kumzungumzia Yesu.

### A. Haya ni maneno ya Agano Jipya

1. Nazarethi – mji katika Galilaya (kama vile Luka 1:26; 2:4,39,51; 4:16; Mdo. 10:38). Mji huu hautajwi katika vyanzo vya wakati huu, bali umekutwa katika kumbukumbu ya maandishi ya baadaye. Kwa upande wa Yesu kuwa alitoka Nazarethi haikujitosheleza (kama vile Yohana 1:46). Alama ya msalaba wa Yesu ambayo imeliweka jina la eneo hili ilikuwa alama ya aibu kwa Wayahudi.
2. Nazarēnos – pia inataja maeneo ya kijiografia (kama vile Luka 4:34; 24:19).
3. Nazōraios – inaweza kuurejea juu ya mji, lakini pia ingeweza kuwa mwaminifu na mtenda haki Masihi wa Kiebrania "Utanzu" (*netzer*, BDB 666, KB 718 II, kama vile Isa. 11:1; maana zinazokaribiana, BDB 855, Yer. 23:5; 33:15; Zek. 3:8; 6:12; iliyodokezwa katika Ufu. 22:16). Luka akilitumia hili kumhusu Yesu katika 18:37 na Mdo. 2:22; 3:6; 4:10; 6:14; 22:8; 24:5; 26:9.
4. Iliyohusiana na #3 nāzir (BDB 634, KB 684), ambalo linamaanisha "aliyewakifishwa kwa maana ya nadhiri."

### B. matumizi ya Kihistoria ya neno nje ya Agano Jipya.

1. Lilimaanisha kundi la ausi la Kiyahudi (Mkristo wa awali) (*nāsōrayyā* ya Kiaramu).
2. Lilitumika katika mzunguko wa Kiyahudi kuwatambulisha waamini katika Kristo (kama vile Matendo 24:5,14; 28:22, nosri).
3. Lilikuja kuwa neno la kawaida katika kumaanisha waamini katika makanisa ya Kisiria (Kiaramu). "Mkristo" lilitumika katika makanisa ya Kyunani kumaanisha waamini.
4. Wakati mwingine baada ya kuanguka kwa Yerusalemu, Wafarisayo walikusanyika huko huko

Jamnia na walichochea utengano rasmi kati ya sinagogi na kanisa. Mfano wa aina ya maapizo ya mazungumzo dhidi ya Wakristo unapatikana katika "*the Eighteen Benedictions*" from Berakoth 28b-29a, ambayo "Wanazarethi." "Wanazareti na awaasi waliweza kutoweka kwa muda mfupi; walifutwa kutoka katika kitabu cha uzima na kutoandikwa kuwa walikuwa na imani."

5. Ilitumiwiwa na Justin Martyr, Dial. 126:1, ambaye alitumia netzer ya (Isa. 11:1) kumhusu Yesu.

#### C. Maoni ya Mwandishi

Nashangazwa sana na herufi za maneno, Ingawa nafahamu kwamba hili ni jambo geni kusikika katika Agano la Kale "Yoshua" ina herufi mbalimbali katika Kiebrania. Maelezo yafuatayo yananisababisha kubaki na mashaka kama maana yake dhahiri :

1. kama vile maana yake ya karibu na neno la Kimasihi "tawi" (*netzer*) au neno lililo sawa *nāzir* (aliyekwa mafuta kwa maana ya nadhiri)
2. vidokezo hasi vya eneo la Galilaya kuyahusu mataifa
3. uchache au kutokuwepo kwa uthibitisho wa fasili za sasa kukusu mji wa Nazarethi katika Galilaya
4. inatoka katika kinywa cha pepo katika maana ya hukumu (yaani, "Umekuja kutuamamiza?").

Kwa wasifu kamili wa masomo ya kundi la neno hili, tazama Colin Brown (ed.), *New International Dictionary of New Testament Theology*, juzuu. 2, uk. 346 au Raymond E. Brown, *Birth of the Messiah*, kur. 209-213, 223-225.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Hawa mamajusi walikuwa akina nani? Je walikuwa wayahudi?
2. Hii nyota ilikuwa ya aina gani?
3. Yesu alikuwa na umri wa miaka mingapi walipokua mamajusi?
4. Ni kwa namna gani Mika 5:2-6 inasimulia mamlaka ya Biblia kama kitabu cha nguvu za Mungu?
5. Dondoo za maandiko ya Agano la Kale zinaonekana ziko mbali na muktadha, kwa nini?

## MATHAYO 3

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Mahubiri ya Yohana Mbatizaji	Yohana Mbatizaji Anaandaa Njia	Kazi ya Yohana Mbatizaji	Mahubiri ya Yohana Mbatizaji	Mbiu ya Yohana Mbatizaji
3:1-6	3:1-12	3:1-6	3:1-3 3:4-6	3:1-12 (3b)
3:7-17		3:7-10 3:11-12	3:12	
Ubatizo wa Yesu	Yohana Anambatiza Yesu	Ubatizo wa Yesu	Ubatizo wa Yesu	Yesu Anabatizwa
3:13-17	3:13-17	3:13-17	3:13-14 3:15a 3:15a-17	3:13-15 3:16-17

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka [“Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia”](#))** **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA ZA MATHAYO 3:1-17**

- A. Kati ya Mathayo 2 na 3 ni miaka ya ukimya wa utoto wa Yesu. Isipokuwa lilie tendo la lililofanyika katika umri wa miaka kumi na miwili, maelezo ya undani yahasuyo utoto wa Yesu hayajulikani. Kumekuwa na shauku na madhahanio mengi kwa waamini. Injili nyingine za kanuni za kujitungia zinayanukuu matukio mahususi, ambayo yalipaswa kuwa yametokea wakati wa ujana wake, lakini miaka hii haikunukuliwa katika Biblia.
- B. Vifungu vyenye kufanana na Mt. 3:1-12 ni Marko 1:3-8, Luka 3:1-17, na Yohana. 1:6-8, 19-28.

C. Vifungu vyeye kufanana vya Mt. 3:13-17 ni Marko 1:9-11, Luka 3:21-22, na Yohana. 1:31-34.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 3:1-6

<sup>1</sup> Siku zile aliondokea Yohana Mbatizaji akihubiri katika nyika ya Uyahudi, na kusema, <sup>2</sup> Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia. <sup>3</sup> Kwa sababu huyo ndiye aliyenenwa na nabii Isaya, akisema, "Sauti ya mtu aliaye nyikani, Itengenezeni njia ya Bwana, Yanyosheni mapito yake. <sup>4</sup> Naye Yohana mwenyewe alikuwa na vazi lake la singa za ngamia, na mshipi wa ngozi kiunoni mwake; na chakula chake kilikuwa nzige na asali ya mwitu. <sup>5</sup> Ndipo walipomwendea Yerusalemu, na Uyahudi wote, na nchi zote za kandokando ya Yordani; <sup>6</sup> naye akawabatiza katika mto wa Yordani, huku wakiziungama dhambi zao.

**3:1 "Siku zile"** Hii ni nahau ya mabadiliko. Hii haina maana ya kutoa ufafanuzi wa wakati maalum.

☐ **"Yohana"** Huu ni muundo uliofupishwa wa jina "Johanan," lililomaanisha "YHWH ni wa neema" au "zawadi ya YHWH." Jina lake lilikuwa nuhimu kwa sababu, kama yalivyo majina yote ya kibiblia, hili lililigusia kusudi la Mungu moja kwa moja kwa ajili ya maisha yake. Yohana alikuwa wa mwisho niongoni mwa manabii wa Ag ano la Kale. Hapakuwa na nabii katika Israeli tangu kipindi cha Malaki, yapata miaka 430 k.k. Kuwepo kwake kulisababisha furaha kubwa ya kiroho miongoni nwa watu.

☐ **"Mbatizaji"** Ubatizo ulikuwa desturi ya kawaida miongoni mwa Wayahudi wa karne ya kwanza na ya pili.

1. kwa ajili ya maandalizi ya kufanya ibada hekaluni (yaani., utaratibu wa kujisafisha)
2. kujitolea katika ubatizo kwa ajili ya kuwashawishi wengine

Ikiwa mtu mwenye historia ya kutoka Mtaifa nengine ilimpasa kuwa mwana kamili wa Israeli, ilimpasa kutimiza matakwa matatu:

- (a) tohara, ikiwa ni mwanamume
- (b) ubatizo wa kujitolea, mbele ya mashahidi watatu
- (c) kujidhabihu ndani ya Hekalu

Katika makundi ya kimadhehebu ya karne ya kwanza ya Kipalestina, kama walivyo Waesene, kwa hali iliyo dhahiri ubatizo ulikuwa jambo la kawaida, zoezi lililorudiwa rudiwa. Hata hivyo, kwa dini ya Kiyahudi iliyotawala, ubatizo wa Yohana uliohusu tobungekuwa wa fedheha kwa wana wa asili ya Ibrahimu kuzifuata taratibu za Mataifa.

1. kama ishara ya kujiosha kiroho (kama vile Isa. 1:16)
2. kama utaratibu wa kawaida uliofanywa na makuhani kama vile Kutoka. 19:10; Law. 15)

Yapaswa kueleweka kwamba aina nyingine zote za ubatizo zilizo katika karne ya ya kwanza ya utamaduni wa Kiyahudi zilikuwa za kujiendesha zenyewe. Ni Yohana pekee aliyelitwa kuundesha utaratibu huu. Kwa namna iliyo dhahiri Yohana alifanya tathmini ya sifa za kiroho ambazo zilidokeza toba binafsi (kama vile Mt. 3:7-10).

☐ **"akihubiri katika nyika ya Uyahudi"** "Nyika" ilikuwa nchi yenye majani na isiyo kalika, si nchi ya jangwa. Yohana hakuvaa kama Eliya (kama vile 2 Wafalme. 1:8), pia aliishi katika mazingira yale yale ya jangwa. Yohana alikuwa akieleza katika nafasi ya kinabii (kama vile Zek. 13:4). Maisha yake ya kuhama hama yalifanana na yale ya kipindi cha kutanga tanga nyikani cha wana wa Israeli, ambacho kiliutimiza uhusiano wa karibu kati ya YHWH na Israeli. Vifungu vyenye kufanana vinaeleza kuwa eneo la kijiografia la kuhubiri kwa Yohana lilikuwa karibu na mji wa Yeriko kaskazini mwa Bahari ya Chumvi, karibu na Mto Yordani.

**3:2 "Tubuni"** Hii ni kauli shurutishi ya wakati uliopo yenye amri endelevu. Pasipo toba, haiwezekani kuokolewa (kama vile Luka 13:3). Ulinganifu wa Kiebrania ulimaanisha "kuyabadili matendo ya mtu," ambapo neno la



Kiyunani lilimaanisha "kuzibadili fikra za mtu." Hii inamaanisha uhiari wa kubadilika. Wokovu huitaji imani katika Kristo na toba (kama vile Marko 1:15; Matendo 3:16, 19; 20:21). Huduma ya Yohana ilikuwa moja ya maandalizi ya kiroho kwa ajili ya ujio wa Yesu Masihi na ujumbe wake.

Yesu pia anatoa wito kwa wale wanaomsikia kutubu (kama vile Mt. 4:17; Marko 1:15).

## MADA MAALUM : TOBA KATIKA AGANO LA KALE

Dhana hii ni ya muhimu sana lakini ni vigumu kuitolea ufafanuzi. Wengi wetu tunao ufafanuzi ambao unatokana na ushirikishwaji wa kimadhehebu. Hata hivyo, mara nyingi huu "mwelekeo" wa ufafanuzi wa kithiolojia unalazimisha maneno kadhaa ya Kiebrania (na Kiyunani) ambayo kwa upekee wake hayamaanishi "elekea" ufafanuzi huu. Lazima ikumbukwe kwamba maandishi wa kitabu cha Agano la Kale (isipokuwa Luka) walikuwa wanafikra wa Kiebrania waliotumia maneno ya lugha ya Koine ya Kiyunani, hivyo sehemu ya kuanzia ni ile ya maneno yenyewe ya Kiebrania, ambayo kimsingi ni mawili.

1. *nacham* ( BDB 636, KB 688)
2. *shub* ( BDB 996, KB 1427)

Neno la kwanza, *nacham*, kiuhalisia linaonekana kumaanisha "kueleza pumzi ya ndani" linatumika katika maana kadhaa.

- a. "kupunzika" au "kufariji" (m.f. Mwa. 5:29; 24:67; 27:42; 37:35; 38:12; 50:21; mara nyingi linatumika katika majina, kama vile 2 Fal. 15:14; 1 Nya. 4:19; Neh. 1:1; 7:7; Nahumu 1:1)
- b. "kuhuzuka" (m.f. Mwa. 6:6,7)
- c. "kughairi" (m.f. Kut. 13:17; 32:12,14; Num. 23:19; Ayubu 42:5-6)
- d. "huruma" (m.f. Kut. 32:36)

Tambua kwamba haya yote yanahusisha hisia za ndani! Hapa ndipo palipo na ufubuzi: hisia za ndani ambazo huelekea katika tendo. Badiliko hili la tendo mara kwa mara huelekezwa kwa watu wengine, lakini pia kuelekea kwa Mungu. Ni hili badiliko la mtazamo na tendo kumwelekea Mungu ambalo hukazia neno hili kwa umuhimu huu wa kithiolojia. Lakini hapa ungalifu lazima ufanyiwe kazi. Mungu anasemekana "kutubu" (kama vile Mwa. 6:6, 7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:11, 35; Zab. 106:45), lakini hili si matokeo ya sononeko juu ya dhambi au makosa, bali ni njia ya kiaandiko ya kuonyesha huruma ya Mungu na uangalifu (kama vile Hes. 23:19; 1 Sam. 15:29; Zab. 110:4; Yer. 4:27-28; Eze.24:14). Adhabu istahiliyo dhambi na uasi inasamehewa ikiwa mtenda dhambi ameamua kwa usahihi kuongoka kutoka dhambini kwake/kwao na kurudi kwa Mungu. Huu ni uthamanisho mpya wa maisha.

Neno la pili, *shub*, linamaanisha "kurudi" (kurudi kutoka, kurejea, kurudi kwa). KITENZI *shub* (BDB 996, KB 1427) kimsingi kinamaanisha "kugeuka" au "kurejea tena" Kitenzi hiki kinaweza kutumika kwa

1. kumuelekea Mungu, Hes. 14:43; Yos. 22:16,18,23,29; Amu. 2:19; 8:33; 1 Sam. 15:11; 1 Fal. 9:6; Yer. 3:19; 8:4
2. kumrudia Mungu, 1 Fal. 8:33,48; 2 Nya. 7:14; 15:4; 30:9; Zab. 51:13; 116:7; Isa. 6:10; 10:21,22; 31:6; Yn. 4:6,8-11 (tambua hasa Yeremia 7 na Amosi 4)
3. YHWH anamwambia Isaya hapo awali kwamba Yuda haitaweza/isingeweza kutubu (kamavile Isa. 6:10), lakini si mara ya kwanza katika kitabu hiki, Yeye anawahita warudi Kwake.

Toba si hisia nyingi sana kama ulivyo mtazamo kumwelekea Mungu. Huu uthamani mpya wa maisha kutoka upekee kuelekea Kwake. Hii inadokeza utayari wa kubadilika na kubadilishwa. Si ukomavu kamili kuihusu dhambi, bali ukomavu wa uasi unaojulikana! Huu ni ukinyume wa matokeo yaliyo kitovu Anguko la Mwanzo 3. Hiii inadokeza kwamba sura na ufanano wa Mungu (Mwa. 1:26-27), ingawa iliharibika, umerejeshwa! Ushirika pamojana Mungu kupitia mwanadamu aliyeanguka inawezakana kurejeshwa tena.

Toba katika Agano la Kale kimsingi inamaanisha "badiliko la tendo," ambapo "toba" katika Agano Jipya inamaanisha "badiliko la fikra" (tazama Mada Maalum: Toba [AJ]). Yote haya ni muhimu kwa ajili ya toba ya kweli ya kibiblia. Pia ni muhimu kutambua kwamba toba ni vyote tendo la awali na hatua endelevu. Tendo la awali linawezakuonekana katika Marko 1:15; Matendo ya Mitume 3:16 na 19; 20:21, ambapo hatua endelevu

inaweza kuonekana katika 1 Yohana 1:9; Ufunuo 2 na 3. Toba si uchaguzi (kama vile Luka 13:3,5)!

Ikiwa ni kweli kwamba mahitaji ya maagano mawili ni "toba" na "imani" (m.f. Mt. 3:2; 4:17; Maro 1:4,15; 2:17; Luka 3:3,8; 5:32; 13:3,5; 15:7; 17:3), kisha neno *nachamr* linarejea juu ya hisia zenye nguvu za kutambaua dhambi ya mtu na kugeuka kutoka ndani ya hiyo dhambi, ambapo neno *shub* lingaliweza kurejea juu ya kurudi toka dhambini na kumwelekea Mungu (moja ya mfano wa haya matendo ya kiroho uko katika Amosi 4:6-11, "hamkunirudia mimi" [mara tano] ana Amosi 5:4,6,14, "Nitafuteni mimi. . .Mtafuteni Bwana. . .Tafuteni mema, wala si mabaya").

Mfano wa kwanza ulio mkuu wa nguvu ya toba ni ile dhambi ya Daudi's sin with Bathsheba (kama vile 2 Samuel 12; Zaburi 32,51). Kulikuwa na matokeo endelevu kwa Daudi, familia yake, na Israeli, lakini Daudi alirejeshwa katika ushirika pamoja na Mungu! Hata Manase aliyekuwa dhalimu aliweza kutubu na kusamehewa (kama vile 2 Nya. 33:12-13).

Maneno yote haya yanatumika kwa usawa katika Zab. 90:13. Lazima kuwepo na utambuzi wa dhambi na nia iliyokusudiwa, kurudi kwa mtu binafsi kuto dhambini, pamoja na shauku ya kumtafuta Mungu na haki Yake (kama vile Isa. 1:16-20). Toba ni hatua tambuzi, hatua binafsi, na hatua ya kimaadili. Haya yote yanahiajika, yote ni kwa ajili ya kuanza uhusiano mpya pamoja na Mungu na kuushikilia uhusiano huo mpya. Hisia za ndani za majuto hurejeshwa ndani ya utele wa uaminifu kwa Mungu na kwa ajili ya Mungu!

☐ **"kwa maana ufalme wa mbinguni"** Mathayo, akiwaandikia Wayahudi, yu makini juu ya matunizi yao mabaya ya jina la Mungu, hivyo anatumia maneno yenye kuzunguka, "ufalme wa mbinguni" (kama vile Mt. 4:17), ambapo Vidokezo vingine vya Kiinjili vinatumia "ufalme wa Mungu" (Mathayo anatumia "ufalme wa mbinguni" mara 32 na " ufalme wa Mungu" mara 4 tu).

Katika maana ya Agano la Kale, Ufalme wa Mungu unarejelea, juu ya kutawala kwa Mungu, si eneo la kijiografia. Mungu ni Mfalme wa uumbaji! Tazama Mada Maalum katika Mt. 4:17.

<b>NASB, NKJV</b>	<b>"umekaribia"</b>
<b>NRSV</b>	<b>"umekuja karibu"</b>
<b>TEV</b>	<b>"u kaibu!"</b>
<b>NJB</b>	<b>"umekaribia"</b>

Hiki ni kitenzi cha wakati timilifu chenye kueleza hitimisho na matokeo endelevu ya tendo lililoanza awali. Ukaribu wa ufalme unakaziwa katika Injili (kama vile Mt. 4:17; 10:7; Marko 1:15; Luka 10:9-11; 11:20; 21:31). Neno "Umekaribia" linaweza kueleweka katika namna mbili: (1) uelekeo wa karibu au (2) ukaribu katika wakati (kama vile Mt. 12:28). Huu nimvutano wa "umekwisha kutimia" na "ungali bado" wa Enzi za Agano Jipya. Hili linaeleza kipindi kati ya jio mbili za Kristo. Hili linazifunika zama mbili za Kiyahudi.

**3:3 "Sauti ya mtu aliaye nyikani"** Hii ni nukuu toka Isa. 40:3 katika Agano la Kale la Kiebrania (LXX). Wazo hili hili pia liliakisiwa katika Isa. 57:14 na 62:10, ma Mal. 3:1. Yohana alijiona kama mwenye kuuandaa ujio wa Masihi (kama vile Yohana. 1:23). Huu ni utimilifu wa tabiri kuhusu Eliya zinazopatikana katika Mal. 3:1 na 4:5. Injili zote nne zinayanukuu maneno haya ya Yohana (kama vile Marko 1:3; Luka 3:4; Yohana 1:23).

☐ **"Itengenezeni njia ya Bwana, Yanyosheni mapito yake"** Vifungu hivi vinaufanano wa kiushairi. Kifungu cha pili mara nyingi ilikuwa stiari ya kujiandaa kwa ajili ya ujio wa kiufalme. Ni muhimu kutambua kwamba katika Isa. 40:3 hili neno "Bwana" lilimrejelea YHWH, ambapo katika nukuu hii lilimrejelea Yesu Mnazareti. Waandishi wa Agano Jipya walitumia mbinu kadhaa za kiuandishi kueleza Uungu wa Yesu.

1. majina ya Agano la Kale ya YHWH kuyatumia kwa Yesu
2. matendo ya Agano la Kale ya YHWH yaliyoonekana katika Yesu
3. nukuu za Agano la Kale zilizohusiana na YHWH sasa zinatatumika kwa Yesu

4. wote Mungu na Yesu kama kiarifu cha kisarufi cha kitenzi mojawapo au kihisishi Neno "Yanyosheni" mara nyingi lilitumika kistiari kueleza sifa ya Mungu (sawa na " haki," "mwenye haki," " usawa," "sawazisha"). Maneno nengi ya Kiebrania panoja na ya Kiyunani yenye kuzungumzia dhambi yanaakisi ukengefu toka kiwango fulani au "kipino." Kiwango ni Mungu mwenyewe (kama ile Law. 11:44; 19:2; Mt. 5:48; 20:7,26; 1 Pet. 1:16).

**3:4** Linganisha tendo hili na uvaaji na maisha ya Eliya yaliyoandikwa katika 2 Fal. 1:8 na ilivyoakisiwa katika Mal. 4:5. Vazi lake la singa za ngamia lilipatikana kwa urahisi sana. Yohana alikuwa na uzoefu wa kuishi jangwani na kula chakula kilichopatikana mahali pale. Nzige kilikuwa chakula kilichoruhusiwa na sheria ya Musa (kama vile Law. 11:22). Hili neno pia lilitumika kumaanisha nyuki aina ya nzige, au karuba, aina fulani ya mti.

**3:5** Wayahudi walioishi Uyahudi walimwona Yohana kama nabii (kama vile Mt. 21:26). Mstari huu unaonyesha njaa kubwa kwa ajili ya Mungu katika karne ya kwanza ya Wayahudi. Hata viongozi wa kidini walikuja. Mstari huu kwa uwazi ni kichochezi, lakini unaeleza juu ya shauku ya kidini iliyosababishwa na Yohana.

**3:6 "huku wakiziungama dhambi zao"** Hili neno la Kiyunani "waiziungama" [*homologeō*] lilimaanisha "kuzungumza kitu kile kile." Hili lilimaanisha vyote ungamo la adharani na ungamo la imani (kama vile Matendo 19:18; Yakobo 5:16). Watu walilitambua hitaji la kujirudi kiroho. Vielelezo vya Agano la Kale vinapatikana katika Mambo ya Walawi.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 3:7-10**

<sup>7</sup> Hata alipoona wengi miongoni mwa Mafarisayo na Masadukayo wakiujia ubatizo wake, aliwaambia, Enyi wazao wa nyoka, ni nani aliyewaonya ninyi kuikimbia hasira itakayokuja? <sup>8</sup> Basi zaeni matunda yapasayo toba; <sup>9</sup> wala msiwaze mioyoni mwenu kwamba, Tunaye baba, ndiye Ibrahimu; kwa maana nawaambia ya kwamba Mungu aweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. <sup>10</sup> Na shoka limekwisha kuwekwa penye mashina ya miti; basi kila mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa motoni.

**3:7 "Hata alipoona wengi miongoni mwa Mafarisayo na Masadukayo wakiujia ubatizo wake, aliwaambia"** Semi za Yohana kwa hawa viongozi wa kidini zinatisha katika uweza wao (yaani., "Enyi wazao wa nyoka," kama vile Luka 3:7; na zinatumiwa na Yesu katika Mt. 12:34; 23:33). Nadharia kadhaa zimekuzwa kuhusu sababu zilizomfanya atende hivyo kwa nguvu.

1. kwa kuwa aliwaona kama mawakala wa ki-Shetani
2. kwa kuwa aliwaona kama wafu kiroho tofauti na imani ya kweli
3. kwa kuwa aliwaona kama waigaji
4. kwa kuwa aliwaona kama viongozi watawalao wenye ungamo za hadhara zisizoendana na mitazomo na shauku zao.

Ni muhimu kwamba hawa viongozi walidhani kwamba ubatizo ulikuwa kwa ajili yao. Huenda walihitaji kujitambulisha mbele ya makutano na ambapo tendo hili lingekuwa hadhi yao ya uongozi. Yohana alizitambua shauku zao. Kwa mjadala kamili wa asili na theolojia ya Mafarisayo tazama Mada Maalum katika Mt. 22:15 na Masadukayo tazama Mada Maalum katika Mt. 22:23.

☐ **"kuikimbia hasira itakayokuja"** Kutokana na ufanano wa Mal. 3:2-3, ni dhahiri kwamba hukumu juu ya Israeli ilikuwa karibu kwa sababu ya kulivunja Agano la sheria ya Musa (kama vile Kumbukumbu 27-28). Amosi anaiita hii "siku ya YHWH" (yaani., Amosi 5:18), ambayo inaiatika Enzi Mpya ya Haki au Ufalme wa Kimasihi. Hapa Yohana anaithibitisha dhana ya hukumu ya Malaki. Tambua kuwa ujumbe wa Yohana haukuwa wa kitaifa au wa kiushirika kama ilivyo ule wa Malaki, bali ulikuwa wa binafsi (kama vile Eze. 18; 33; Yer. 31:31-34).

**3:8**

**NASB** "zaeni matunda yapasayo toba"

**NKJV, NRSV** "zaeni matenda yaliyo sawa na toba"

**TEV** "Fanyeni mambo yatakayoonyesha kuwa mnegeuka toka dhambini"

## NJB "Bali ikiwa mmetubu, zaeni matunda yapasayo"

Hata katika Agano la Kale, imani ilikuwa bora kuliko taratibu au ushirika katika kundi la kitaifa (kama vile Kumb. 10:12, 16; Mt. 7:15-23; Rum. 2:28-29). Imani ilikuwa na ni vyote ya ushirika na binafsi, vyote imani na kazi (kama vile Yakobo 2:14-26)! Maisha yao lazima yaonyeshe uhusiano wao mpya pamoja na Mungu (kama vile Mt. 7:16-20; 12:33; Luka 6:43-44; Matendo 26:20). Kwa neno "toba" tazama maelezo kamili katika Mt. 4:17.

**3:9 "wala msiwaze mioyoni mwenu kwamba, Tunaye baba, ndiye Ibrahimu"** Huu utegemezi juu ya uzao wa kitaifa wenye ufanano unaweza kuonekana katika Yohana 8:3 na kuendelea na Buku la sheria za Kiyahudi "Wakuu wa masinagogi" 10:1. Wayahudi waliamini kwamba manufaa ya imani ya Ibrahimu yalitumika kwao. Hata hivyo, Mal. 3:2 na kuendelea na 4:1 inaonyesha kwamba hukumu ngelikuja juu ya Wayahudi kwa sababu ya wao kulivunja Agano (pia nukuu Mt. 8:11-12). Maisha ya imani, si uzao, ndiyo njia ya kumtambua mtoto wa kweli wa Ibrahimu (kama vile Rum. 2:28-29).

☐ **"mawe. . . watoto"** Hii ilikuwa kejeli iliyotumia maneno ya Kiaramu "mawe" (*'ebnayya*) na "watoto" (*benyya*), ambalo lilitamkika kwa kufanana. Tazama G. B. Caird, *The Language and Imagery of The Bible*, uk.48.

**3:10 "shoka limekwisha kuwekwa penye mashina ya miti"** Huu muundo wa hukumu ni sawa na ule wa Malaki. Ufanano huu unaweza kuonekana katika Isa. 10:33-34. Moja ya sababu iliyomshangaza Yohana Mbatizaji ilikuwa aidha Yesu alikuwa Masihi kweli kwa sababu ujumbe wake hauanza kwa kuzungumzia hukumu kama Yohana alivyotarajia.

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 3: 11-12

<sup>11</sup> Kweli mimi nawabatiza kwa maji kwa ajili ya toba; bali yeye ajaye nyuma yangu ana nguvu kuliko mimi, wala sistahili hata kuvichukua viatu vyake; yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto. <sup>12</sup> Ambaye pepeto lake li mkononi mwake, naye atausafisha sana uwanda wake; na kuikusanya ngano yake ghalani, bali makapi atayateketeza kwa moto usiozimika.

### 3:11

NASB "sistahili hata kuvichukua viatu vyake"

NKJV, NRSV "ambaye hainipasi kuvibeba viatu vyake"

TEV "sijafikia kuvichukua viatu vyake"

Hili neno linaweza kutafsiriwa katika namna mbili (1) kwa kufuata matumizi yaliyo katika mafunjo ya Misri, "kuondoa na kuvibeba viatu vya wageni hadi eneo la utunzaji" au (2) "kuvifungua na kuondoa." Matendo yote haya kiutanadauni yalifanywa na watumwa. Si wanafunzi wa walimu wa sheria za Kiyahudi pekee waliohitajika kulifanya takwa hili. Huu ni usemi wa kinahau wa fahamu wa Yohana kuhusu ukuu wa Yesu.

☐ **"yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto"** Ni kihisishi kimoja tu na kibainishi kimoja tu katika andiko la Kiyunani chenye kuunganisha kifungu kwa Roho Mtakatifu na kwa moto, kinamaanisha kwamba hivi vyote vinafanana (tambua Isa. 4:4). Hata hivyo, kama ilivyo katika Luka 3:17, moto unaweza kurejelea hukumu, ambapo Roho Mtakatifu anarejelewa kama kujisafisha au utakaso. Inawezekana kwamba vyote hivi vinalirejelea tendo la siku ya Pentekoste la Matendo 2. Wengine wameliona hili kama mambo mawili fungamano ya ubatizo: ubatizo mmoja kwa wenye haki na mmoja kwa wale walio dharimu, au Yesu akibatiza kama Mwokozi au Mwamuzi. Wengine wamelihusianisha hili ule uongofu wa kabla ya siku ya Pentekoste na kujaliwa karama maalum siku ya Pentekoste. 1 Wakorintho 12:13 inamaanisha kwamba Yesu ndiye mbatizaji "katika," "pamoja na," au "kwa" Roho (kama vile Marko 1:8; Luka 3:16; Yohana. 1:33; Mdo. 1:5; 2:33).

**3:12 "naye atausafisha sana uwanda wake; na kuikusanya ngano yake ghalani, bali makapi atayateketeza kwa moto usiozimika"** Hii stiari aliyoitumia Yesu kueleza hukumu ya Mungu ya milele (kama vile Isa. 66:24) ilikuwa *Gehenna* (mkaganyiko wa "bonde la wana wa Hinomu"), jalala la taka lililokuwa kusini mwa Yerusalemu (kama vile

Marko 9:48; Mt. 18:8; 24:41; Yuda 7). Huyu ni mungu wa moto na ustawi wa Kikanaani alikuwa akiabudiwa (tendo lililojulikana kama *molech*) huko Gehenna katika siku za Israeli zilizopita kwa kutoa kafara ya watoto wao (kama vile Law. 18:21; 20:2-5; 1 Fal. 11:7; 2 Fal. 21:6; 23:10). Kipengele hiki cha hukumu ya milele ni cha kutisha kwa wasoaji wa sasa, lakini kinajishuhudia (mafundisho ya walimu wa Sheria za Kiyahudi) na kinajieleza kwa Wayahudi wa karne ya kwanza. Yesu hakija kama mwenye kuhukumu, bali wote waliomkataa watahukumu (kama vile Luka 3:16-17, Yohana. 3:17-21). Vielelezo vya Agano la Kale vya stiari hii ilikuwa Isaya 34 ambayo inatoa maelezo ya hukumu ya Mungu juu ya Edomu.

## **MADA MAALUM: MOTO (BDB 77, KB 92)**

Moto unavyo vidokezo chanya na hasi katika maandiko.

### A. Chanya

1. Husisimua (kama vile Isaya 44:15; Yohana 18:18)
2. Huwasha nuru (kama vile Isaya 50:11; Mt. 25:1-13)
3. Hupikia (kama vile Kutok 12:8; Isaya 44:15:16; Yohana 21:9)
4. Husafisha (kama vile Hes 31:22-23; Mit. 17:3; Isaya 1:25; 6:6-8; Yer. 6:29; Malaki 3:2-3)
5. Utakatifu wa Mungu (kama vile Mwa. 15:17; Kutoka 3:2; 19:18; Eze 1:27; Waebrania 12:29)
6. Uongozi wa Mungu (kama vile Kutoka 13:21; Hes. 14:14; Wafalme 1. 18:24)
7. Uwezeshaji wa Mungu (kama vile Matendo 2:3)
8. Ulinzi wa Mungu (kama vile Zekaria 2:5)

### B. Hasi

1. Huunguza (kama vile Yos 6:24; 8:8; 11:11; Mt. 22:7)
2. Huangamiza (kama vile. Mwz 19:24; Walawi 10:1-2)
3. Hasira (kama vile. Hes. 21:28; Isaya 10:16; Zek 123:6)
4. Adhabu (kama vile Mwa. 38:24; Walawi 20:14; 21:9; Yoshua 7:17)
5. Ishara ya mbaya ya siku ya mwisho (kama vile. Ufunuo 13:13)

### C. Hasira ya Mungu dhidi ya dhambi mara nyingi hudhihirishwa kwa tanuru ya moto.

1. Hasira yake huunguza (Kama vile Hos. 8:5; Sefania 3:8)
2. Humimina moto (kama vile Nah 1:6)
3. Moto wa milele (kama vile Yer. 15:14; 17:4; Mt. 25:41; Yuda aya ya 7)
4. Hukumu ya siku ya mwisho (kama vile Mt.3:10; 5:22; 13:40; Yohana 15:5; The. 2. 1:7; Petro 2. 3:7-10; Ufu. 8:7; 16:8; 20:14-15)

### D. Moto mara nyingi huonekana katika tanuru

1. Mwa. 15:17
2. Kutoka 3:2
3. Kutoka 19:18
4. Zaburi 18:7-15; 29:7
5. Eze. 1:4, 27; 10:2
6. Ebr. 1:7; 12:29

### E. Kama sitiari yingi katika Biblia (yaani., chachu, simba) moto unaweza kuwa Baraka au kufuatana na mazingira au muktadha.

## **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 3: 13-17**

<sup>13</sup> Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Yordani kwa Yohana ili abatizwe. <sup>14</sup> Lakini Yohana alitaka kumzuia, akisema, Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? <sup>15</sup> Yesu akajibu akamwambia, Kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. <sup>16</sup> Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; <sup>17</sup> na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.

**3:13 "Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Yordani kwa Yohana ili abatizwe"** Injili inatofautiana katika mtiririko wao wa awali wa huduma za Yesu huko Galilaya na Yudea. Inaonekana kwamba kulikuwa a huduma ya mwanzo ya Yudea na baadaye, lakini mtiririko wa Injili zote nne lazima uhusianishwe ili kuitazama safari hii ya mwanzo ya Yudea (kama vile Yohana. 2:13-4:3).

Sababu iliyomfanya Yesu abatizwe mara nyingi imekuwa ikihusishwa kwa waamini kwa sababu ubatizo wa Yohana ulikuwa ubatizo wa toba. Yesu hakuhitaji msanaha kwa kuwa hakuwa na dhambi (kama vile Yohana 8:46; Matendo 3:14; Rum. 8:3; 2 Kor. 5:21; Ebr. 4:15; 7:26; 1 Pet. 2:22; 1 Yohana 3:5). Dhana hizi zimekuwa kama ifuatavyo:

1. ulikuwa mfano wa kufuatishwa na waamini
2. ulikuwa utambulisho wake wa hitaji la waamini
3. ulikuwa uwakifisho na kutengwa kwa ajili ya huduma
4. ilikuwa ishara ya takwa la ukombozi wake
5. ulikuwa uhakikisho wa huduma na ujumbe wa Yohana Mbatizaji
6. ulikuwa unabii wa kifo chake, maziko, na ufufuo (kama vile Rum. 6:4; Kol. 2:12).

Kwa namna ilivyo sababu hiyo, huu ulikuwa wasaa wa umaelezo katika maisha ya Yesu. Ingawa haimaanishi kwamba Yesu alikuwa Masihi kwa wakati huu (uasilishaji, kama vile *The Orthodox Corruption of Scripture* na Bart D. Ehrman, kr. 47-118), huu ulifanyika kuwa umuhimu mkubwa kwake.

**3:14 "Lakini Yohana alitaka kumzuia"** Hiki ni kitenzi cha wakati usio timilifu. Watoa maoni wengi wamepambana kujua sababu iliyomfanya Yohana kujaribu tena na tena kumzuia Yesu kubatizwa. Baadhi ya nadharia ni :

1. wengine wanaliona hili kuwa Yohana alikuwa na ufahanu wa kabla kumhusu Yesu, lakini hili linakinzana na Yohana 1:31,33
2. wengine wanaliona hili kuwa Yohana anakukubali kuwa Yesu alikuwa Myahudi mwenye haki, lakini si kwamba alikuwa Masihi
3. katika utamaduni wa Mashariki ya Karibu ya sasa inampasa mtu kula kiapo mara tatu ili kufikiriwa kama mtiifu.

**3:15 "Yesu akajibu akamwambia"** Mistari 14-15 inapatikana katika Injili ya Mathayo. Hii haitoi aeleezo ya kutosha kwa jibu kamili la swali la mistari wa 14. Hii ni dhahiri, hata hivyo, kwamba ubatizo ulikuwa na maana kwa wote Yesu na Yohana na yale mapenzi ya Mungu kwa maisha yao wote.

**3:16**

**NASB "Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini"**

**NKJV "alitoka majini upesi"**

**NRSV "kama alivyoondoka majini"**

**TEV "Yesu aliondoka majini"**

**NJB "kisha akaondoka majini"**

Mstari huu umekuwa ukitumiwa na wale wanaouunga mkono ubatizo wa kujitolea kama ulivyo mtazamo wa kibiblia kuhusu ubatizo ili kuthibitisha kwamba Yesu alibatizwa kwa hiari. Hata hivyo, ingeweza kueleweka kumaanisha kwamba alienda ukingoni mwa mto (tazama Michael Magill, *NewTestament TransLine*, uk. 9, #35 na 36).

☐ **"mbingu zikamfunukia"** Hii ni njia ya kisitari ya kuonyesha mapenzi ya Mungu (kama vile Isa. 22:22; Ufu. 3:7). Ni Mungu pekee awezaye kuzifungua mbingu (kama vile Mal. 3:10; Ufu. 4:1). Mungu aliyafungua macho ya upofu (yaani., Mt. 9:27-31; 12:22-23; 20:29-34; nukuu Isa. 29:18; 35:5; 42:7,16) na kujibu maombi (kama vile Mt. 7:7,8). Kwa hakika inawezekana kwamba sitari hii inatokana na Isa. 64:1.

☐ **"akamwona"** Andiko la Kiyunani lina kiwakilishi "yeye," pekee ambacho kingeweza kurejelea aidha kwa Yohana au Yesu. Baadhi ni herufi kubwa za machapisho ya Kiyunani (Χ<sup>1</sup>, C, D, L, na W), baadhi ni tafsiri za kale (Vulgate na Koptiki), na maandiko ya Kiyunani yaliyotumiwa na makasisis wa kanisa la mwanzo (Irenaeus, Eusebius,

Chrysostom, Jerome, na Augustine) yanamaanisha kwamba Yesu alimuona hua akija, katika kifungu "mbingu zilifunguka kwa ajili yake." Hata hivyo, hua pia alikuwa ishara ya Yohana kumgusia Masihi (kama vile Yohana. 1:32).

☑ **"Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake"** Kifungu hiki kimeandikwa katika Injili zote nne (Marko 1:10; Luka 3:22; Yohana 1:32). Je! alikuwa hua au hua halisi? Swali haliwezi kujibiwa kwa ukamilifu (kama vile Luka 3:22). Hili linahusiana na Isa. 11:2; 42:1; 48:16; 61:1. Muundo halisi wa Roho si muhimu kama Roho Mwenyewe juu ya Yesu. Hili halimaanishi kwamba kabla ya wakati huu Yesu alikuwa na Roho Mtakatifu, bali huu ulikuwa usimikwaji maalum wa kazi yake ya ki-Masihi. Ishara ya njiwa inekuwa ikijadiliwa kwa mapana sana kama chimbuko lake na kusudi lake.

1. hii inakirejelea kitabu cha Mwanzo 1, ambapo Roho alikuwa ametulia juu ya maji
2. hii inakirejelea kitabu cha Mwanzo 8, ambapo Nuhu alimtuma njiwa kutoka ndani ya safina.
3. walimu wa sheria wanasema kwamba yule njiwa ni ishara ya Israeli (kama vile Zab. 68:13; Hos. 7:11; 11:11; Buku la Kiyahudi *San.* 95A na *Ber. R.* 39; II Esdras 5.26)
4. Tasker, katika *Tyndale New Testament Commentary Series*, anasema kwamba huyu anaurejelea unyenyekevu, ambapo inatofautishwa na moto katika mstari wa 11 (kama vile Rum 11:22; Mt. 11:29; 25:40).

**3:17 "na tazama, sauti kutoka mbinguni"** Kifungu hiki ni cha muhimu sana kutokana na sababu kadhaa. Katika kipindi cha ukimya kati ya Agano la Kale na Agano Jipya, ambao hapakuwa na mnabii wa kweli, walimu wa sheria wanasema kwamba Mungu aliuthibitisha uchaguzi wake na naamuzi yake kwa maana ya *bath kol*, ambayo ndiyo sauti uliyotoka mbinguni. Pia, sauti hii ilikuwa ishara iliyotoka kwa Mungu katika namna ya utamaduni wa karne ya kwanza ambapo Wayahudi wangeelewa (kama vile Matendo 10:9-16; 11:7-9; Ufu. 1:10; 4:1; 10:8; 11:12). Hii ilikuwa wazi kwa namna ilivyokuwa na maana kwa Yesu kama ilivyokuwa kwa Yohana na huenda kwa wingu ambalo liliutambulisha ubatizo wake.

Mkusanyiko wa nukuu "Mwanangu niliyependezwa naye" unaunganisha ufalme wa ki-Masihi, Msistizo wa Daudi wa Zab. 2:7 pamoja na mfano wa Mtumishi Ateswaye wa Isa. 42:1. Hapa, katika nukuu hii, ufalme wa ki-Masihi unaunganishwa na Mtumishi Ateswaye wa Isaya.

Kifungu hiki, "Mwanangu Mpendwa" (pia tazama 17:5) ni chimbuko la kifungu "Mwana wa Mungu," ambacho kinapatikana katika Mt. 4:3, 6. Ni muhimu kutambua kwamba katika Marko 1:11 hiki kinatafsiriwa "Wewe ni Mwanangu Mpendwa," ambapo kinaonyesha kwamba Baba aliyaelekeza maneno yake kwa Yesu, ambapo katika Mathayo 3, hiki kinatafsiriwa katika namna hii kama Mungu alivyozungumza na Yohana na wingu. Tazama Mada Maalum: Mwana wa Mungu katika Mt. 27:54.

Mstari wa 16-17 unazijumuisha nafsi zote tatu za Uungu. Hili neno "uungu" halipo katika Biblia, lakini dhana hii ni ya kiroho. Hii dhana kwamba Biblia inaeleza juu ya Mungu kuwa mmoja (Imani ya Mungu mmoja, Kumb. 6:4) lazima iwekwe sawa na Uungu wa Yesu na utu wa Roho. Kuna uthahirisho wa asili moja ya Uungu na nafsi tatu za milele. Nafsi tatu za nara yingi zinatajwa katika muktadha ule ule (yaani., Mt. 3:16-17; 28:19; Matendo 2:33-34; Rum. 8:9-10; 1 Kor. 12:4-6; 2 Kor. 1:21-22; 13:14; Efe. 1:3-14; 4:4-6; Tito 3:4-6; 1 Pet. 1:2).

## **MADA MAALUMU: UTATU**

Angalia kazi za watu hawa wote watatu katika mazingira ya pamoja. Neno "utatu," kwanza lilibuniwa na Tertallian, sio neno la Kibiblia, lakini dhana yake imesambaa sana.

- A. Injili
  1. Mt. 3:16-17; 28:19 (na nyingine zinazoendana nazo)
  2. Yohana 14:26
- B. Matendo-Mdo. 2:32-33, 38-39
- C. Paulo
  1. Rum. 1:4-5; 5:1,5; 8:1-4,8-10
  2. 1 Kor. 2:8-10; 12:4-6

3. 2 Kor. 1:21-22; 13:14
4. Gal. 4:4-6
5. Efe. 1:3-14,17; 2:18; 3:14-17; 4:4-6
6. 1 The. 1:2-5
7. 2 The. 2:13
8. Tit. 3:4-6

- D. Petro – 1 Pet. 1:2  
E. Yuda-kur. 20-21

Uwingi wa Mungu umedokezwa katika Agano la Kale

- A. Matumizi ya uwingi kumhusu Mungu
  1. Jina Elohim liko katika wingi (angalia mada maalumu: majina ya Uungu), lakini linapotumika kumhusu Mungu mara zote unakuta lina kitenzi kilichoko katika umoja.
  2. “Sisi” katika Mwa. 1:26-27; 3:22; 11:7
- B. “Malaika wa Bwana” (angalia mada maalumu: Malaika wa Bwana) alikuwa mwakilishi wa Uungu aliyeonekana
  1. Mwanzo 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16
  2. Kutoka 3:2,4; 13:21; 14:19
  3. Waamuzi 2:1; 6:22-23; 13:3-22
  4. Zakaria 3:1-2
- C. Mungu na Roho wake ni nafsi tofauti, Mwa. 1:1-2; Zab. 104:30; Isa. 63:9-11; Ezek. 37:13-14
- D. Mungu (YHWH) na Masihi (Adonai) nao ni nafsi tofauti, Zab. 45:6-7; 110:1; Zak. 2:8-11; 10:9-12
- E. Masiha na Roho Mtakatifu ni nafsi tofauti, Zak. 12:10
- F. Wote watatu wametajwa katika Isa. 48:16; 61:1

Uungu wa Yesu na nafsi/haiba ya Roho vimesababisha matatizo kwa uhalisia, kwa wale wanaamini uwepo wa Mungu mmoja (angalia mada maalumu: wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja), kwa waumini wa awali

1. Tertellian-ilimshusha Mwana kwa Babaye
2. Origin-aliishusha nafsi ya Uungu wa Mwana na Roho
3. Arius-anaukana Uungu wa Mwana na Roho
4. Watawa-waliamini katika ufanisi wa udhahirisho wa matukio ya Mungu mmoja kama Baba, Mwana, na Roho

Utatu ni kanuni anzilishi ya kihistoria iliyoelezewa na maneno ya Kibiblia.

1. Uungu kamili wa Yesu, ambao ni sawa na wa Baba, ulithibitishwa katika mwaka wa 325 B.K na baraza la Nicea (kama vile Yoh.1:1; Fil. 2:6; Tit. 2:13)
2. Nafsi kamili na Uungu wa Roho ambao ni sawa na wa Baba na Mwana ulithibitishwa katika mwaka 381 B.K na baraza la Constantino
3. Mafundisho ya Uungu yameelezwa kiundani katika kazi ya Augustine De Trinitate

Hakika kuna muujiza hapa. Lakini Agano Jipya linathibitisha nafsi moja ya Kiuungu (wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja) ikiwa na udhahirisho wa nafsi tatu za umilele (Baba, Mwana, na Roho)

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni nabii gani ambaye Yohana Mbatizaji anakukumbusha? Kwa nini?
2. Fafanua maana ya toba.



3. Kwa nini Mathayo anakitumia kifungu "ufalme wa mbinguni" na Marko na Luka amatumia "ufalme wa Mungu"
4. Nini umuhimu wa nukuu ya Isaya 40 (Mt. 3:3)?
5. Kwa nini viongozi wa kidini walitaka kubatizwa? Katika siku hizo ubatizo uliashiria nini?
6. Kwa nini msistizo wa ujumbe wa Yohana Mbatizaji u juu ya hukumu na si katika wokovu?
7. Kwa nini Yesu alibatizwa panoja na ubatizo wa toba?
8. Nini umuhimu wa Mungu kuzungumza akiwa nje ya bingu? Tambulisha vyazo viwili vya nukuu ya Baba na eleza umuhimu wake.

## MATHAYO 4

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Jaribu la Yesu 4:1-11	shetani anamjaribu Yesu 4:1-11	Kujaribiwa kwa Yesu 4:1-4 4:5-7 4:8-11	Majaribu ya Yesu 4:1-3 4:4 4:5-6 (4:7) 4:8-9 4:10 4:11	Jaribu katika Nyika 4:1-11 (4b) (6b) (7b)
Mwanzo wa Huduma ya Galilaya 4:12-16 4:17	Yesu anaanza Huduma ya Galilaya 4:12-17	Yesu anaanza shughuli Galilaya 4:12-17	Yesu anaanza kazi Yake Galilaya 4:12-16 4:17	Kurudi Galilaya 4:12-17 (15-16)
Wito wa Wavuvi Wanne 4:18-22	Wavuvi wane Waitwa kama Wanafunzi 4:18-22	4:18-22	Yesu anaita wavuvi wanne 4:18-20 4:21-22	Wanafunzi wa kwanza Wanaitwa 4:18-20 4:21-22
Kuhudumia Makutano Makubwa 4:23-25	Yesu anaponya Umati Mkuu 4:23-25	4:23-25	Yesu anafundisha anahubiri na Kuponya 4:23-25	Yesu anatangaza Ujumbe na kuponya wagonjwa 4:23-25

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia"](#))**

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA MISTARI 1-25**

- A. Ni umuhimu sana kwamba mara baada ya kufuata ukiri wa Mungu wa Umasihi wa wana wa Yesu, Roho "anaongoza" Yesu kuelekea jangwani kujaribiwa (kama vile Marko 1:12). Majaribu yalikuwa katika mapenzi ya Yangu kwa ajili ya Mwana. Majaribu yanaweza yakasemwa kama kuyateka shauku iliyotolewa na Mungu zaidi ya mipaka ya Mungu. Majaribu sio dhambi. Majaribu haya yalianzishwa na Mungu. Wakala alikuwa Shetani (kama vile 2 Wafalme. 22:13-23; Ayubu 1-2; Zek. 3)

- B. Pia ni muhimu kwamba katika hii sura Israeli/uanishi wa Kristo. Yesu anaonekana kama "Waisraeli wanaokubali" anayetimiliza jukumu ambalo taifa kiasili lilitolewa (kama vile Isa. 41:8-9; 42:1,19; 43:10). Wote wanaitwa "Mwana" (kama vile Hos. 11:1). Hii inaelezea baadhi ya utata ambao unapatikana katika wimbo wa Mtumishi wa Isa.41-53 katika mabadiliko kutoka katika wingi kwenda katika umoja (Isa. 52:13-15 katika LXX). Israeli hii/Uainishaji wa elimu ya Kristo unafanana na wa Adamu unapatikana katika Rum. 5:12-21.
- C. Je yawezekana Kristo alitenda dhambi? Hii hakika ni siri ya asili mbili za Kristo. Majaribu yalikuwa hakika. Yesu katika asili yake ya ubinadamu yawezekana alikana mapenzi ya Mungu. Haya hayakuwa maonesho. Yesu kweli mwanadamu ingawa hana asili ya kuanguka (kama vile Ebr. 4:15; 7:26). Kwa namna hii alikuwa kama Adamu. Tunaona asili hii hii ya kibinadamu katika bustani ya Gethsemane ambapo Yesu aliomba mara tatu kwa ajili ya njia nyingine ya Ukombozi ipatikane kuacha msalaba (kama vile Mt. 26:36-46; Marko 14:32-42). Hali hii ni kuwepo kwa kila jaribu la shetani katika Mathayo 4. Ni kwa namna gani Yesu atatumia karama zake za Kimasihi kumkomboa mwanadamu? Hata hivyo kuacha upatanisho wa mbadala lilikuwepo jaribu!
- D. Yesu lazima alikuwa amewaambia jambo hili wanafunzi wake kwa maana Yeye alikuwa peke yake huko nyikani. Hii inamaansa kwamba hadithi hii sio tu kwamba inatufundisha sisi kuhusu majaribu ya Kristo bali pia inatusaidi katika majaribu yetu.
- E. Lazima ikumbukwe kwamba Biblia sio historia ya magharibi yenye mpangilio wa matukio, tukio na madhara yake. Historia ya Mashariki ya Karibu ina ubaguzi lakini si kwamba imekosewa. Injili sio hadithi za maisha ya watu bali nyaraka za kiinjili zilizoandikwa kwa makundi tofauti tofauti ya watu kwa makusudi ya uinjilisti na kuwafanya wanafunzi, sio tu historia. Mara kwa mara waandishi wa Injili walichagua, wakaasilisha na kupangilia maandiko kwa ajili ya makusudi yao ya kithiolojia na kifasihi (kama vile Gordon Fee na Douglas Stuart's *Howto Read the Bible for All Its Worth*, Kur. 94-112, 113-134). Kuna maelezo mazuri kadhaa ya mwelekeo wa Mathayo kutengeneza muundo wa Injili yake.
1. Anaweka mafundisho ya ayaesu kwa pamoja katika mahubiri ya ya aina moja (Mathayo 5-7), kama anavyofanya miujiza Yake na mifano yake.
  2. Ana mwelekeo wa kihesabu kwa (kama vile NIDOTTE, vol. 3, kur. 657)
    - a. Tatu
      - (1) majaribu matatu, Mt. 4:1-11
      - (2) matendo matatu ya haki ya kiyahudi, Mt. 6:1-18
      - (3) uponyaji wa iana tatu, Mt. 8:1-15
      - (4) "msiogope," tatu Mt. 10:26,28,31
      - (5) siku tatu, Mt. 12:40
      - (6) maswali matatu, Mt. 22:15-40
      - (7) maombi matatu ya Yesu kwa Baba wakati akiwa Gethsemane, Mt. 26:39-44
      - (8) siku tatu za kulijenga hekalu, Mt. 27:40 (#5)
      - (9) Yesu anafufuka ndai ya siku tatu, Mt. 27:63 (#5,8)
    - b. Saba
      - (1) mapepo, Mt. 12:45
      - (2) vipande vya mikate, Mt. 15:34,36
      - (3) vikapu, Mt. 15:37
      - (4) msamaha kwa ndugu, Mt. 18:21,22 (saba mara sabini)
      - (5) ndugu saba, Mt. 22:25
      - (6) ole saba, Mt. 23:13,15,16,23,25,27,29

Marko (Injili ya kwanza kuandikwa, ikitumiwa na Mathayo na Luka) ina "saba" kwa #2, #3, na #5, ambalo linaonesha hesabu haikuwa muundo wa kipekee wa Mathayo. Ni ngumu kujua nini

kilikuwa sehemu ya desturi na sehemu gani ya mwelekeo wa Mathayo kwa hesabu hizi kulisababisha muundo wake.

Hii haimaanishi waandishi wa Injili walidanganya u walidanganya matukio au maneno. Tofauti katika Injili haikani uvuvio. Inakiri ushuhuda wa hadithi.

F. Ufanano wa majaribu wa Yesu inapatikana katika Marko 1:12-13 na Luka 4:1-13.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 4:1-4

<sup>1</sup> Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi. <sup>2</sup> Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa. <sup>3</sup> Mjaribu akamjia akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate. <sup>4</sup> Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.

**4:1 "Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi"** Huu ni mstari wa muhimu sana ikiwa na maana kwamba inaonesha mapenzi ya Mungu kwa maisha ya Yesu ilikuwa akabiliane na majaribu (Ebr. 5:8). Tukio la Jaribu hili likihusiana na namna gani Yesu angetumia nguvu zake za kimasihiki kukomboa mwanadamu (matumizi ya sentensi daraja la kwanza yenye masharti katika Mt. 4:3, 6).

☑ **"aliongozwa"** Katika Marko 1:12 ufanano wake tunakuta tungo "aliongozwa na Roho." Jambo hili lilikuwa muhimu kwa Yesu (kama vile Ebr. 5:8).

☑ **"nyikani"** Hii inarejerea sehemu ya ardhi ya malisho isiyokaliwa na watu karibu na Yeriko. Hii ingekuwa sehemu ya mipaka ambayo Musa (kama vile Kut. 34:28), Eliya (kama vile 1 Wafalme. 19:8) alipoishi Yohana Mbatizaji (kama vile Mt. 3:1).

☑ **"ajaribiwe"** Maneno mawili katika lugha ya Kiyunani inaelezea majaribu au jaribu. Moja lina maana ya "kujaribu kwa mtazamo wa kuelekea kuimarisha" [*dokimazo*] na ingine "kujaribu kwenye lengo la uharibifu" [*peirasmo*]. Neno litumikalo hapa ni moja kwa uharibifu (kama vile Mt. 6:13; Yakobo 1:13-14). Mungu hatowahi kutujaribu sisi kuelekea kwenye uharibifu, lakini mara kwa mara anatupa majaribu kwa lengo la kuimarisha (kama vile Mwa. 22:1; Kut. 16:4; 20:20; Kumb. 8:2,16; 13:3; Amu. 2:22; 2 Nyak. 32:31; 1 Thes. 2:4; 1 Pet. 1:7; 4:12-16). Shetani hujaribu ili kuharibu!

### MADA MAALUMU: MANENO YA KIYUNANI YAHUSUYO JARIBU NA VIDOKEZO VYAKE VINGINE

Kuna manaeno mawili ya Kiyunani ambayo yana kidokezo kwa ajili ya kumjaribu mtu kwa kusudi fulani.

1. *Dokimazō, Dokimion, Dokimasia*

Neno hili ni neno la mtu yule afuaye vyuma kwa ajili ya kujaribu uhalisia wa kitu fulani (yaani, kistiari mtu fulani) kwa moto (tazana Mada Maalumu: Moto). Moto hudhilihisha chuma halisi na huteketeza (yaani, husafisha) dongo la chuma. Kitendo hiki cha kifizikia kinakuwa nahau yenye nguvu kwa Mungu na/au Ibilisi na/au binadamu kuwajaribu wengine. Neno hili linatumika tu katika maana chanya ya kujaribu kwa kuangalia hadi kuufikia ukubalifu (tazama Mada Maalumu: Mungu Huwajaribu Watu Wake [Agano la Kale]).

Linatumika katika Agano la Kale kwa ajili ya

- a. Madume ya ng'ombe – Luka 14:19
- b. sisi wenyewe – 1 Kor. 11:28

- c. imani yetu – Yakobo 1:3
- d. hata Mungu –Ebr. 3:9

Matokeo ya majaribu hayajafikiwa kuwa chanya (kama vile. Rum. 2:18; 14:22; 16:10; 2 Kor. 10:18; 13:3,7; Flp. 2:27; 1 Pet. 1:7), hivyo, neno husilisha wazo la mtu aliyepimwa na kuhakikishwa

- a. kuwa wa thamani
- b. kuwa wazuri
- c. kuwa halisi
- d. kuwa wa maana
- e. kuwa wa kuheshimiwa

## 2. Peirazō, Peirasmus

Neno hili mara nyingi lina maana nyingine ya kupimwa kwa kusudi la utafutaji au ukataaji. Linatumika katika maana nyingine kwa majaribu ya Yesu nyikani.

- a. Linabeba jaribio la kumtega Yesu (kama vile Mt. 4:1; 16:1; 19:3; 22:18, 35; Marko 1:13; Luka 4:2; Ebr. 2:18).
- b. Neno hili (*peirazōn*) linatumika kama wadhifa kwa Ibilisi katika Mt. 4:3; 1 The. 3:5 (yaani, "mjaribu").
- c. Matumizi
  - 1) Lilitumiwa na Yesu alipokuwa akiwaonya wanadamu kutomjaribu Mungu (kama vile Mat. 4:7; Luka 4:12, [au Kristo kama vile 1 Kor 10:9]).
  - 2) Pia linamaanisha jaribio la kufanya kitu fulani ambacho kimeshindikana (kama vile Ebr.11:29).
  - 3) Linatumika katika maana nyingine kwa majaribu na masumbufu ya waamini (kama vile 1 Kor. 7:5; 10:9, 13; Gal. 6:1; 1 The. 3:5; Ebr. 2:18; Yakobo. 1:2, 13, 14; 1 Pet. 4:12; 2 Pet 2:9).

☐"**ibilisi**" Katika Agano la Kale jina la viumb vya kimalaika watoao kwa mwanadamu uchaguzi ni shetani (BDB 966), mshitaki (kama vile Marko 1:13). Katika Agano Jipya anafanyika *diabulos* (ukifuatia LXX) au shetani ambalo linamaanisha mdanganyi, mpinzani au mjaribu. Katika Agano la Kale alikuwa mtumishi wa Mungu (kama vile Ayubu 1-2; 2 Wafalme 22:13-23; 1 Nyakt. 21:1; Zek. 3:1,2). Hata hivyo kwa muda wa Agano Jipya kulikuwa na ukuaji wa uovu na amekuwa adui mkubwa wa Mungu. Moja ya vitabu bora zaidi juu ya ukuaji wa uovu katika Biblia ni A. B. Davidson's *Old Testament Theology*, published by T. na T. Clark, kur. 300-06. Angalia Mada Maalum katika Mt. 4:5.

**4:2 "baada ya kuwa amefunga"** Angalia [MADA MAALUM: KUFUNGA](#) katika Mt. 6:16.

☐"**siku arobaini mchana na usiku**" Hapa tena Mathayo alichagua maudhui kutoka katika Agano la Kale ya (1) Siku arobaini mchana na usiku katika Mlima Sinai kwa Musa (kama vile Kut. 24:18; 34:28; Kumb. 9:9; 10:10) na (2) Israeli wakizagaa jangwani kwa miaka arobaini (kama vile Hes. 14:26-35). Mathayo alimuona Yesu kama mtoa sheria na mkombozi (yaani kutoka mpya).

Neno "arobaini" lilitumika mara kwa mara katika Biblia likimaanisha lingweza kufanya kazi vyote kibayana (miaka 40 kutoka Misri mpaka Kanaani) na kwa kimafumbo (gharika). Waebrania walitumia Kalenda ya Lunar. "Arobaini" ilimaanisha kipindi kirefu zaidi kisichojulikana cha muda mrefu zaidi wa mzunguko wa mwezi, sio hakika arobaini ya vipindi vya ishirini na nne.

## MADA MAALUM:UWAKILISHI WA NAMBA KATIKA MAANDIKO

- A. Namba fulani zilitenda kazi maeneo yote kama tarakimu na ishara.
  1. Moja – Mungu (yaani, Kumb. 6:4; Efe. 4:4-6)
  2. Nne – dunia nzima (yaani, pembe nne, nchinne za dunia, yaani, Isa. 11:12; Yer. 49:36; Dan. 7:2; 11:4;

Zek. 2:6; Mt. 24:31; Marko 13:27; Ufu. 7:1)

3. Sita – kutokamilika kwa mwanadamu (moja chini ya 7, m.f, Ufu. 13:18)
4. Saba – itimilifu wa Kiungu (siku saba za uumbaji). Tambua matumizi ya kiishara katika Ufunuo:
  - a. vinara vya taa saba, Ufu. 1:12,20; 2:1
  - b. nyota saba, Ufu. 1:16,20; 2:1
  - c. makanisa saba, Ufu. 1:20
  - d. Roho saba za Mungu, Ufu. 3:1; 4:5; 5:6
  - e. taa saba, Ufu. 4:5
  - f. Mihuri saba, Ufu. 5:1,5
  - g. pembe saba na macho saba, Ufu. 5:6
  - h. malaika saba, Ufu. 8:2,6; 15:1,6,7,8; 16:1; 17:1
  - i. baragumu saba, Ufu. 8:2,6
  - j. nghurumo saba, Ufu. 10:3,4
  - k. elfu saba, Ufu. 11:13
  - l. vichwa saba, Ufu. 13:1; 17:3,7,9
  - m. mapigo saba, Ufu. 15:1,6,8; 21:9
  - n. vitasa saba, Ufu. 15:7; 21:9
  - o. wafalme saba, Ufu. 17:10

5. Kumi– ukamilifu

- a. matumizi katika Injili
    - 1) Mt. 20:24; 25:1,28
    - 2) Marko 10:41
    - 3) Luka 14:31; 15:8; 17:12,17; 19:13,16,17,24,25
  - b. matumizi katika Ufunuo
    - 1) Ufu. 2:10, siku kumi dhiki
    - 2) Ufu. 12:3; 17:3,7,12,16, pembe kumi
    - 3) Ufu. 13:1, vilemba kumi
  - c. Vigawe vya kumi katika Ufunuo
    - 1)  $144,000 = 12 \times 12 \times 1000$ , kama vile Ufu. 7:4; 14:1,3
    - 2)  $1,000 = 10 \times 10 \times 10$ , kama vile Ufu. 20:2,3,6
6. Kumi na Mbili – ushirika wa mwanadamu
- a. Wana kujmi na wawili wa Yakobo (yaani, makabila kumina mbili ya Israeli, Mwa. 35:22; 49:28)
  - b. nguzo kumi na mbili, Kut. 24:4
  - c. mawe kumi mawili katika juu ya kifua cha Kuhani Mkuu, Kut. 28:21; 39:14
  - d. mikate kumina miwili, ju ya meza Mahali Patakatifu (ishara ya utoaji wa Mungu wa kwa makabila kumi na mawili), Law. 24:5; Kut. 25:30
  - e. Watu kumina wawili, Kumb. 1:23;
  - f. mawe kum na mawili, Jos. 4:2,3,4,8,9,20
  - g. mitume kumi na wawili, Mt. 10:1

matumizi katika Ufunuo

- 1) makabila kumi na mbili elfu waliotiwa mhuri, Ufu. 7:5-8
- 2) nyota kumi na mbili, Ufu. 12:1
- 3) milango kumi na miwili, malaika kumi na wawili, makabila akumi na mawili, Ufu. 21:12
- 4) misingi ya mawe kumi na mawili, majina ya Mitume kumi na mawili, Ufu. 21:14
- 5) Yerusalemu mpya ilikuwa Yerusalemu ilikuwa vipimo vya mraba elfu kumi na mbili, Ufunuo 21:16
- 6) milango kumi na miwili ilitotengenezwa kwa lulu kumi na mbili Ufu. 21:21

7) mti wa uzima uzaao matunda, aima kumi na mbili, Ufu. 22:2

7. Arobaini –namba za nyakati

- a. wakati mwingine ni halisi (kuhamishwa na kutangatanga nyikani, m.f. Kut. 16:35); Kumb. 2:7; 8:2
- b. inaweza kuwa halisi au ya kiishara
  - 1) mafuriko, Mwa. 7:4,17; 8:6
  - 2) Musa juu ya Mlima Sinai, Kut. 24:18; 34:28; Kumb. 9:9,11,18,25
  - 3) mgawanyo wa maisha ya Musa:
    - a) miaka arobaini ndani ya Misri
    - b) miaka arobaini jangwani
    - c) miaka arobaini ya kuiongoza Israeli
  - 4) Yesu alifunga siku arobaini, Mt. 4:2; Marko 1:13; Luka 4:2
- c. Tambua (kwa maana ya Upatanisho) tarakimu za wakati hii tarakimu inajitokeza katika wakati wa uteuzi ndani ya Bibia!

8. Sabini – namba ya jumla ya watu

- a. Israeli, Kut. 1:5
- b. wazee sabini, Kut. 24:1,9
- c. matukio ya siku za mwisho, Dan. 9:2,24
- d. kundi la huduma, Luka 10:1,17
- e. msamaha (70x7), Mt. 18:22

B. Marejeo mazuri

1. John J. Davis, *Biblical Numerology*
2. D. Brent Sandy, *Plowshares and Pruning Hooks*

☑"**akaona njaa**" Kufunga kulihusisha kujinyim chakula na sio maji. Baadhi ya Wafasiri wanaona hili kama shetani akisuribi mpaka mwisho wa mfungo wa Yesu alipokuwa dhaifu na mwenye kuchoka kabla hajakabiliwa naye. Wengine wanaamini kwamba Shetani alikuja wakati wa mfungo mzima. Uchaguzi wa kwanza unashabihiana na muktadha vizuri zaidi.

Hii pia inaonesha ubinadamu kamili wa kujazwa na Roho, Roho aliyemtuma Yesu.

**4:3 "mjaribu"** Hii ni kauli endelevu ya wakati uliopo inayotumika kama ujazilizo wa "kumjaribu" kama katika Mt. 4:1.

☑"**akamjia akamwambia**" Majaribu haya yangeweza kuwa aidha ya kiakili au ya kimwili. Yakijikita katika ukweli kwamba shetani atampeleka juu ya mlima mrefu kuona fahari zote za ufalme wa duniani kwa mara moja (ufanano wa Luka), hii yawezekana ikawa maono lakini ukabiliano wa kibinafsi kati ya Yesu na shetani.

☑"**Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu**" Kama mstari wa 6, hii ni sentensi ya daraja la kwanza yenye masharti ambayo inadhaniwa kuwa kweli kuanzia katika mtazamo wa mwandishi; hivyo ilitakiwa ifasiriwe "kwakuwa" (badala ya "ikiwa") kwa wasoamaji wa Kingereza. Shetani si kwamba ana mashaka na U-masihi wa Yesu (yaani ukiri wa Mungu katika Mt. 3:17), bali alikuwa akimjaribu ilikuweza kumtumia vibaya au kutukanisha nguvu zake za Ki-Masihi. Muundo huu wa kisarufi unatengeneza uzuri wa ufasiri wa uzoefu wote wa jaribu lote (kama vile James Stewart's *The Life and Teachings of Jesus Christ*).

☑"**amuru kwamba mawe haya yawe mikate**" Inavyoonekana miamba hii katika jangwa la Yudea ilikuwa imechongoka kama vipande vya mkate vilivyookwa na kuliwa katika karne ya kwanza. Shetani alikuwa anamjaribu Yesu kwa kutumia nguvu zake za ki-masihi ili vyote kupata mahitaji yake binafsi na kupata kuaminiwa na

wanadamu kwa kuwalisha. Katika Agano la Kale Masihi alielezwa kama kuwalisha masikini (kama vile. Isa. 58:6-7,10). Matukio ya majaribu haya kwa kiasi Fulani yaliendelea kutokea kipindi cha huduma za Yesu. Kuwalisha watu elfu tano (Mt. 14:13-21) na elfu nne (Mt. 15:29-33) kulionesha kiasi gani wanadamu wange na walivyofanya kwa kutukana msaada wa Mungu wa chakula cha mwilini. Hii tena inafanana na matatizo ya jangwani kwa Waisraelijangwani. Wayahudi walikuwa wakitegemea Masihi kutenda mambo mengi ya Musa.

Majaribu ya shetani yalitenda kazi katika viwango viwili. Ya kwanza ilikuwa matarajio ya kiyahudi ya Masihi kutoa chakula kama Musa (yaani Yohana 6). Ya pili ilikuwa ni maana kwamba ikiwa alikuwa kweli Mwana wa Mungu, Masihi, athibitise kwa "kuzungumza" mapenzi Yake. Hii kidhahiri inarejerea kwa uumbaji kwa neno la kuzungumza (Mwanzo 1). Jaribio la Shetani lilikuwa

1. kutoa chakula cha kibinadamu kama Musa alivyofanya
2. oneshwa nguvu zako kwa kuzungumza tukio la kimiujiza (tazama nukuu katika Mt. 4:4b)

**4:4 "Imeandikwa"** Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati timilifu. Hii ilikuwa njia ya kinahau iliyozoeleka ya kutambulisha nukuu ya uvuvio kutoka Agano la Kale (kama vile Mt. 4:4,7,10), kwa namna hii kutoka Kumb. 8:3 kutoka Tafsihi ya Agano la Kale la Kiyunani (LXX). Hii nukuu hasa inahusiana na Mungu kutoa manna kwa wana wa Israeli wakati wa kipindi cha jangwani:

Miitikio yote ya Yesu kwa majaribu ya shetani yalikuwa nukuu kutoka Kumb. Hii lazima ilikuwa moja ya vitabu vyake avipendavyo sana.

1. Alinukuu kwa kurudia rudia kutoka katika hiyo wakati wa majaribu yake, Mt. 4:1-16; Luka 4:1-13.
2. Yawezekana ni uainisho nyuma ya Nahubiri Juu ya Mlima, Mt. 5-7.
3. Yesu alinukuu Kumb. 6:5 kama sheria iliyo kuu zaidi, Mt. 22:34-40; Marko 12:28-34; Luka 10:25-28.
4. Yesu alinukuu sehemu hii ya Agano la Kale (Mwanzo – Kumbu kumbu la Torati) zaidi mara kwa mara kwasababu Wayahudi wa siku zake walilichukulia kuwa na mamlaka zaidi.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 4:5-7**

<sup>5</sup> Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mji mtakatifu, akamweka juu ya kinara cha hekalu, <sup>6</sup> akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu jitupe chini; kwa maana imeandikwa,

Atakuagizia malaika zake;

Na mikononi mwao watakuchukua; Usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.

<sup>7</sup> Yesu akamwambia, Tena imeandikwa, Usimjaribu Bwana Mungu wako.

**4:5 "Ibilisi"** Neno la Kiyunani, *Diabolos*, limetumika hapa katika Agano Jipya mara 37, wakati *Satanas* limetumika mara 36; zote zikirejerea kwa yule ashitakiye ambalo ndilo lilikuwa jukumu lake la Agano la Kale. Mathayo na Luka wanatumia *diabolos* kwa matukio ya kujaribiwa, wakati Marko anatumia *Satanos*. Kwanini mabadiliko hayo hayajulikani. Angalia [MADA MAALUMU: UOVU BINAFSI](#) inayofuata

#### **MADA MAALUMU: UOVU BINAFSI**

- I. SOMO KUHUSU SHETANI NI GUMU SANA
  - A. Agano la Kale halibainishi adui mkubwa wa (Mungu), bali mtumishi wa YHWH ambaye anawapa wanadamu mbadala na kutuhumu huyu mwanadamu kwa kutokuwa na haki (A. B. Davidson, *A Theology of the OT*, kur. 300-306).
  - B. Dhana ya adui mkubwa wa Mungu ulianza wakati wa fasili kati ya Biblia (zisizo na taratibu za kikanisa) katika kipindi cha dini ya kiislamu iliyoanzishwa na Zoroaster huko Uajemi. Hii kwa namna nyingine, kwa kiwango kikubwa ilisababisha sheria ya dini ya Kiyahudi (yaani, waliokuwa wametengwa na kuishi nje ya Israel yaani Babiloni, na Uajemi).
  - C. Agano Jipya linaunda dharura ya Agano la Kale katika ugumu wa ajabu lakini makundi yaliyochaguliwa



kama mtu anaanza kusoma habari za uovu katika mtizamo wa thiolojia ya biblia (kila kitabu au mwandishi au michoro alisoma na kuandika kwa kifupi kwa kutenganisha) basi mawazo mbalimbali kuhusu uovu yangeibuliwa. hata hivyo, mtu ataanza kusoma kuhusu uovu lakini kwa njia isiyo ya kibiblia au nje zaidi ya biblia mfano dini za kiulimwengu au dini za mashariki, basi sehemu kubwa ya mambo mengi ya maendeleo ya agano jipya yalionyeshwa katika pande mbili za uajemi na tabia za uyunani na kiroma.

Kama mtu alidhaniwa kujitoa kwa uwezo wa kiungu neno la Mungu (kama nilivyo!),kwa hiyo mambo ya Agano Jipya lazima yaonekane kama ufunuo endelevu. Wakristo yawapasa wajilinde dhidi ya kuruhusu simulizi za Kiyahudi au fasihi za Kiingereza (yaani, Dante, Milton) kufafanua zaidi dhana hiyo bila shaka miujiza na maana tofauti tofauti katika eneo hili la wokovu. Mungu amechagua kutobainisha mambo yote ya uovu, asili yake (tazama Mada Maalumu: Lusifa),kusudi lake,lakini amebainisha kushindwa kwake!

## II. SHETANI KATIKA AGANO LA KALE

Katika Agano la kale neno "Shetani" (BDB 966, KB 1317) au "mshitaki" linaonekana kuhusiana na makundi matatu tofauti.

- A. Washtaki wa wanadamu (1 Sam. 29:4; 2 Sam. 19:22; 1 Fal. 5:4, 11:14,23,25; Zab. 109:6,20,29)
- B. Washtaki wa kimalaika (Hes. 22:22-23; Zak. 3:1)
  1. Malaika wa Bwana – Hes. 22:22-23
  2. Shetani – 1 Nya. 21:1; Ayubu 1-2; Zak. 3:1
- C. Washtaki wa kimapepo (bila shaka shetani) (1 Fal. 22:21; Zak. 13:2)

Baadaye katika kipindi cha kuingia agano jipya ibilisi wa Mwanzo 3 alijulikana ni shetani (kama vile.Kitabu cha Hekima 2:23-24; II Enoch 31:3), na hata baadaye ambapo anakuja kuwa chaguo la viongozi wa kidini wa Uyahudi (kama vile. Sot 9b na Sanh. 29a). "wana wa Mungu" wa Mwanzo 6 wanakuwa malaika wa uovu katika I Enoch 54:6. Wanakuwa waanzilishi wa uovu katika thiolojia ya viongozi wa kidini wa Kiyahudi. Nalitaja hili sio kwa kuonyesha usahihi wake wa kithiolojia, bali kuonyesha maendeleo yake katika Agano Jipya, shuguli hizi za Agano la Kale zinachangia katika uovu wa malaika wa nuru (yaani shetani,)katika 2 Kor. 11:3; Ufu. 12:9.

Asili ya uovu wa yule aliyejigeuza kuwa malaika wa nuru ni mgumu au haiwezekani (kutegemea maoni yako) kuupima toka katika Agano la Kale. Sababu moja wapo ni ile imani ya nguvu juu ya uwepo wa Mungu mmoja tu. (kama vile Kumb. 6:4-6; 1 Fal. 22:20-22; Mhu. 7:14; Isa. 45:7; Amosi 3:6). Majeruhi wote walipelekea YHWH kuonyesha kwa vitendo alivyo wa pekee na mkuu (kama vile. Isa. 43:11; 44:6,8,24; 45:5-6,14,18,21,22).

Uwezekano wa vyanzo vya habari ni (1) Ayubu 1-2, ambapo shetani ni mojawapo wa wana wa Mungu "mwana wa Mungu" (yaani, malaika) au (2) Isaya 14; Ezeieli 28, ambapo ujivuni karibu na wafalme wa mashariki (Babiloni na Uturuki) wamekuwa wakielezea sifa au ujivuni wa shetani (kama vile. 1 Tim. 3:6). Nimechanganya mihemko kuhusu kuliendea suala hili. Ezeieli anatumia bustani ya Edeni kama neno mbadala sio tu kwa mfalme wa Uturuki kama shetani (kama vile. Ezek. 28:12-16), lakini pia kwa ufalme wa Misri kama mti wa maarifa wa mema na mabaya (Ezeieli 31). Hata hivyo, Isaya 14, hasa kurasa 12-14, anaonekana kuelezea uasi wa malaika kupitia majivuno kama Mungu alivyotaka kubainisha kwetu jinsi alivyo hasa na asili ya shetani hii ni njia isiyo elezea moja kwa moja na mahali pa kuifanya (tazama Mada Mada Maalumu: Lusifa). Lazima tujilinde dhidi ya mwenendo wa Theolojia wa kuchukua sehemu ndogo ndogo, tata toka kwenye maeneo yenye maana mbalimbali ya waandishi, vitabu, na kuviunganisha kama vipande vipande vya fumbo la Kiungu.

## III. SHETANI KATIKA AGANO JIPYA

Alfred Edersheim (*The Life and Times of Jesus the Messiah*, juzuu. 2, kiambatisho XIII [kur.. 748-763] na XVI [kur. 770-776]) anasema mafundisho ya sheria za Kiyahudi yameathiriwa wazi kabisa na umiliki wa pande mbili za Uajemi na mtizamo wa kimapepo. Viongozi hawa wa kidini sio vyanzo vizuri vya ukweli katika eneo. Yesu kimsingi anakwepa kutoka kwenye mafundisho ya sinagogi. Nafikiri kuwa dhana ya viongozi wa dini ya kiyahudi ya upatanisho wa kimalaika (kama vile Matendo 7:53) na upinzani katika kutoa sheria za Musa kwenye mlima Sinai ilifungua mlango kwa dhana ya adui mkuu wa YHWH kadhalika na mwanadamu. Palikuwa na Mungu wawili wa pande mbili za Iran (ufuasi wa Zoroaster).

1. *Ahura Mazda*, baadaye akaitwa *Ohrmazd*, aliyekuwa mungu muumbaji, mungu mwema

2. *Angra Mainyu*, baadaye aliitwa *Ahriman*, roho aangamizaye, mungu mwovu, Vita juu ya ukuu na dunia ikawa kama uwanja wa vita. Umiliki wa pande mbili ukajengeka ndani ya pande mbili za Kiyahudi zenye ukomo kati ya YHWH na shetani. Hakika kuna mafunuo endelevu katika agano Jipya kama ilivyo kwenye uovu, lakini sio kama ilivyoelezewa kama walimu wa dini ya Kiyahudi wanavyodai. Mfano mzuri wa utofauti huu ni "vita vya mbinguni." Kuanguka kwa shetani (Mwovu) ni mantiki yenye umuhimu, lakini sehemu husika haikutolewa (Tazama Mada Maalumu: Kuanguka kwa shetani na malaika wake). Hata hivyo kile kilichotolewa kimefichika kwenye mafunuo tanzu (k.v. Ufu. 12:4,7,12-13). Ingawa shetani ameshindwa na kutupwa duniani, bado anatenda kazi kama mtumishi wa YHWH (kama vile. Mt. 4:1; Luka 22:31-32; 1 Kor. 5:5; 1 Tim. 1:20). Lazima tuthibiti kiu yetu katika eneo hili. Kuna nguvu binafsi ya majaribu na uovu lakini bado kuna Mungu mmoja tu na mwanadamu bado anawajibika kwa uchaguzi wake. kuna vita ya kiroho kabla na baada ya wokovu. Ushindi wawezakuja tu na kubakia ndani na kupitia Mungu wa Utatu. Uovu umekwisha shindwa na utaondolewa (kama vile. Ufu. 20:10)!

☉ "**akamchukua mpaka mji mtakatifu**" Tungo hii "jiji takatifu" ni ya kipekee na yalikuwa maelezo maalumu kwa ajili ya Yerusalemu (kama vile Mt. 27:53; Dan. 9:24; Neh. 11:1,18; Ufu. 11:2). Mathayo alijua Wayahudi wangeelewa hili mapema kama maelezo kutoka Agano la Kale (kama vile Isa. 48:2; 52:10; 64:10). Utaratibu wa matukio ya majaribu katika Mathayo na Luka ni tofauti. Sababu kwa ajili ya hili haijulikani. Yawezekana hadithi ya Mathayo ina mfuatano (" kisha"), wakati hadithi ya Luka inaanzisha muundo upya na utaratibu wa madhara ya kimazingira ("tena").

**NASB, NKJV,**

**NRSV**

**"akamsimamisha juu ya kilele cha hekalu'**

**TEV**

**"akamweka juu ya kilele cha hekalu"**

**NJB**

**"akamwek juu ya kilele cha hekalu"**

"Sehemu ya juu" au "kilele" inaweza kibayana kufasiriwa kama "sehemu." Neno hili lingemaanisha (1) sehemu ya nje kabisa ya hekalu upande wa kusini mashariki katika kona ya ukuta wa nje ambayo ilitazama kwa juu bonde la Kidron (2) sehemu ya Hekalu la Herode ambayo ilitazama upande wa ndani wa mahakama. Kwasababu ya desturi za Kiyahudi kwamba Masihi alitakiwa kutokea ghafla katika Hekalu (kama vile Mal. 3:1), desturi hii ilifanyika kuwa moja ya majaribu ya shetani ya namna gani ya kuwapata watu kwa kutenda miujiza ya kujirusha juu na kuelea juu ya eneo la Hekalu, yawezekana wakati wa siku ya sherehe.

**4:6 "Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu jitupe chini"** Hii ni sentensi nyingine ya daraja la kwanza lenye masharti ambalo linachukuliwa kuwa kweli kulingana na matazamo wa mwandishi au kwa amakusudi yake mwenyewe (kama vile Mt. 4:3). Shetani ananukuu Zab. 91:11-12. Baadhi wamekuwa wanaelezea kwa shetani alinukuu vibaya mstar huu. Ingawa aliacha "katika njia zako zote," nukuu hii inafanana na matumizi ya Mitume walipotumia maandiko ya Agano la Kale. Tatizo halikuw kwa shetani kunukuu vibaya andiko bali kutaka kulitumia vibaya pasipotakikana.

**4:7 "Yesu akamwambia"** Mstari wa 7 ni nukuu kutoka Kumb. 6:16, ambayo ilirejerea Waisraeli kumjaribu Mungu pale Massah wakati wa kipindi cha kutembea Jangwani (kama vile Kut. 17:1-7). Israeli kwa wakati huu hawakumwamini Mungu kuwapatia mahitaji yao ya kila siku bali walitaka miujiza. Kiwakilishi "ninyi" katika nukuu inahusiana na Israeli, sio shetani (kama vile Mt. 4:10).

☐ **"Usimjaribu Bwana Mungu wako"** Jambo la msukumo kwa "jaribu" kama vile 1 Kor. 10:9 [Hesabu 21]; Mdo. 5:9; 15:10). Waamini wanaitwa kiutendaji kutumaini ahadi za Mungu (yaani, Yos. 1:56; Isa. 7:10-13; Mal. 3:10).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 4:8-11**

<sup>8</sup> Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonyesha milki zote za ulimwengu, na fahari yake, <sup>9</sup> akamwambia, Haya yote nitakupa, ukianguka kunisujudia. <sup>10</sup> Ndipo Yesu alipomwambia, Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake. <sup>11</sup> Kisha Ibilisi akamwacha; na tazama, wakaja malaika wakamtumikia.

**4:8-9** Jaribu hili linamaanisha maono badala ya tukio halisi lenyewe. Linganisha Luka 4:5 ambayo inasema "baada ya muda." Katika namna yoyote, lilikuwa ni jaribu halisi na la kibinafsi lililomkabili Yesu.

Kumekuwepo na mjadala mkubwa juu ya nini shetani alimaanisha na madai yake katika Mt. 4:9: (1) Je inamaanisha kwamba alikuwa mmiliki wa wa falme zote za nchi? au (2) je inamaanisha kwamba alikuwa tu hajali dhambi za ulimwengu kwa kumuonesha Yesu fahari yake? Shetani anaitwa "mungu wa dunia hii" (kama vile Yohana 12:31; 2 Kor. 4:4) na mtawala wa ulimwengu huu (kama vile Efe. 2:2; 1 Yohana 5:19) ina bado ulimwengu huu unamilikiwa na Mungu aliyeuumba na kuutunza! Kiwango kamili cha ushawishi wa shetani, umiliki wake (kama vile Luka 4:6), na utashi huru (kama vile Ayubu 1-2; Zekaria 3) haijulikani, lakini nguvu zake na uovu wake ni wa umeenea (kama vile 1 Pet. 5:8).

**4:9 "ikiwa"** Hii ni sentensi ya daraja la kwanza yenye masharti ambayo ilimaanisha tendo linalowezezana kufanywa baadaye. Mstari huu unaonesha shauku ya kweli ya shetani kuwa mbadala wa YHWH!

**4:10 "Yesu alipomwambia"** Hii nukuu huru katika Kumb. 6:13. Haitokei katika maandiko ya Kimasoreti (MT) au katika Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani (LXX). Yesu aliongeza neno "tu." Mstari huu na Kumb. 6:5 inakiri kujitoa kunakohitajika kwa Mungu katika moyo, akili na maisha. Ukweli kwamba Yesu kwa uhuru ananukuu maandiko inatakiwa itutie moyo sisi kukariri na kuyajua maandiko (yaani Zab. 119:11; 37:31; 40:8), kusudi ni kujua maana yake kubwa na kuliishi kila siku sio sana juu ya kunukuu kwa ukamilifu hasa katika nyakati za majaribu na mapito (kama vile Efe. 6:17).

☐ **"Nenda zako, Shetani"** Hii inafanana kama pacha ya Mt. 16:23. Baadhi ya maandiko ya Kale ya Kiyunani, C<sup>2</sup>, D, L, na Z, yanaongeza "nenda nyuma yangu shetani." Inavyoonekana waandishi wa mwanzo waliongeza tungo hii ambayo inatoka Mt. 16:23. Toleo la UBS<sup>4</sup> alinatoa andiko fupi alama ya "B" (karibu na hakika).

**4:11 "Kisha Ibilisi akamwacha"** Luka 4:13 inaongeza tungo "mpaka wakati ulipowadia." Jaribu halitokei mara moja na alafu lipotee kimoja bali ni endelevu. Yesu alipitia majaribu tena. Maneno ya Petro pale Kaisarea Philipi yalikuwa ya kujaribu na ya kukata kama maneno ya shetani katika nyika (kama vile Mt. 16:21-23).

☐ **"malaika wakaja na kuanza kumtumikia"** Neno la Kiyunani "muhudumu" mara kwa mara linahusianishwa na chakula cha mwili (kama vile Mt. 8:15; 25:44; 27:55; Mdo. 2:6). Hii inakumbusha 1 Wafalme. 19:6-7, ambapo kimiujiza Mungu alimpatia chakula Eliya. Malaika wa Mungu walianza kumuhudumia Mwanawe wa Pekee. Mungu alitoa yote ambayo shetani alikuwa amezimia atatoa.

Kwanini Mwana wa Mungu aliyevikwa mwili angehitaji huduma ya malaika bado ni siri. Malaika wanawahudumia roho kwa aliookoka (kama vile Ebr. 2:14). Mara mbili katika maisha ya Yesu walimsaidia katika nyakati za udhaifu wa mwili, hapa katika Gethsemane (kama vile Luka 22:43 katika MSS, \*κ, D na L na Vulgate).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 4:12-17**

<sup>12</sup> Basi Yesu aliposikia ya kwamba Yohana amefungwa, alikwenda zake mpaka Galilaya; <sup>13</sup> akatoka Nazareti, akaja akakaa Kapernaumu, mji ulioko pwani, mipakani mwa Zabuloni na Naftali; <sup>14</sup> ili litimie neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema, <sup>15</sup> Nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali, Njia ya bahari, ng'ambo ya Yordani, Galilaya ya mataifa, <sup>16</sup> Watu wale waliokaa katika giza Wameona mwanga mkuu, Nao waliokaa katika nchi na uvuli wa mauti Mwanga umewazukia. <sup>17</sup> Tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri, na kusema, Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.

**4:12** Hizi sababu za kibayana kwa kukamatwa kwa Yohana kunatolewa katika Mt. 14:3-5.

**4:13 "akatoka Nazareti"** Yesu alibadilisha makazi yake ya kuishi kwasababu ya kutokuamini kwa jiji (kama vile Luka 4:16-31). Angalia Mada Maalum: Yesu Mnazareti katika Mt. 2:23.

☐ **"akakaa Kapernaumu"** Huu ulikuwa mji wa nyumbani wa Petro na Yohana. "Kapernaumu" ulimaanisha "kijiji cha Nahumu." Hivyo inaweza kuwa ilikuwa nji wa nyumbani wa kdesturi wa nabii wa Agano la Kale. Ilikuwa katika eneo na pwani ya kaskazini mwa bahari ya Galilaya.

**4:13c-16** Kwasababu ya tungo inayohitimishwa ya Mt. 4:13, Hii ilitimiliza unabii (kama vile Isa. 9:1-2). Kila mmoja alitarajia Masihi kuhudumu kimsing kabisa kuelekea Yudea na Yerusalemu lakini unabii wa kale wa Isaya ulitimilizwa kiupekee katika maish na huduma ya Yesu (kama vile Yohana. 7:41). Nchi ya Zebuloni na Naftali zilikuwa za kwanza kuanguka kwa wavamizi wa Ki-Ashuru na ya kwanza kusikia habari njema.

**4:15 "ng'ambo ya Yordani"** Nahau hii siku zote ilirejerea upande wa mashariki wa Yordani (kupita Yordani) lakini hapa inarejerewa kama magharibi (nchi ya ahadi). Yote inategemea juu ya wapi mtu anayezungumza alikuwa amesimama (au akifikiria).

☐ **"Galilaya ya Mataifa"** Galilaya ulikuwa mchanganyiko wa wote Wayahudi na Mataifa (*ethnē*, LXX Isa. 9:1), sehemu kubwa walikuwa mataifa. Mataifa hawa walidharauliwa na Wayahudi wa Yudea. Moyo wa Mungu umekuwa siku zote kwa ajili ya wokovu juu ya ulimwengu wote (yaani Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Isa. 2:24; 25:6-9; Yohana 3:16; Efe. 2:11-3:13).

**4:16 "Watu wale waliokaa katika giza"** Hii ilikuwa aidha (1) rejea kwa dhambi zao, (2) rejea kwa ujinga wao, au (3) nahau kwa kejeli kwasababu ya tofauti zao.

☐ **"nchi na uvuli wa mauti"** Hii ilikuwa ni sitiari kwa ajili ya hatari kuu (kama vile Ayubu 38:17; Zab. 23:4; Yer. 2:6).

**4:17 "Tokea wakati huo"** Tungo hii imetumika mara tatu katika Mathayo (kama vile Mt. 4:17; 16:21; 26:16) na kuonekana kuwa kiashiria cha kimakusudi cha kifasihi cha mgawanyiko mkuu wa uwasilishaji wa Yesu unaofanywa na Mathayo.

☐ **"Yesu alianza kuhubiri, na kusema, Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia"** Hii ni sawasawa na Injili ya Yohana Mbatizaji (kama vile Mt. 3:2). Katika kinywa cha Yesu ilimchukua umuhiu mpya. Ufalme ni vyote sasa na baadaye. Hii ni "tayari" lakini bado" uvutano wa zama mpya (angalia Robert Stein, *The Method and Message of Jesus' Teachings*, kur. 75-79).

## MADA MAALUMU: UFALME WA MUNGU

Katika Agano la Kale Mungu alifikiriwa kama mfalme wa Israel (kama vile 1 Sam. 8:7; Zab. 10:16; 24:7-9; 29:10; 44:4; 89:18; 95:3; Isa. 43:15; 44:6) na Masihi akawepo kama mfalme aliyedhaniwa/kutegemewa (kama vile Zab. 2:6; Isa. 9:6-7; 11:1-5). Na kuzaliwa kwa Yesu pale Bethlehemu (mwaka wa 6-4 K.K) ufalme wa Mungu ukavunjiliwa ndani ya historia ya mwanadamu kwa nguvu mpya na ukombozi ("Agano Jipya," kama vile Yer. 31:31-34; Ezek. 36:27-36).

1. Yohana Mbatizaji akatangaza kukaribia kwa ufalme (kama vile Mt. 3:2; Mk 1:15).
2. Yesu wazi wazi akafundisha kwamba ufalme ulikuwa tayari ndani yake mwenyewe na mafundisho yake teachings (kama vile Mt. 4:17,23; 10:7; 12:28; Luke 10:9,11; 11:20; 17:21; 21:31-32). Na bado ufalme unakuja (kama vile Mt. 16:28; 24:14; 26:29; Mark 9:1; Luk 21:31; 22:16,18).

Katika usambamba wa mihitasari kwenye Marko na Luka tunakipata kifungu, "ufalme wa Mungu." Hii ilikuwa mada ya kawaida katika mafundisho ya Yesu yakijumisha utawala wa Mungu uliopo kiatika mioyo wa watu, ambao siku moja utakamilishwa katika ulimwengu wote. Huu unaakishwa kwenye maombi ya Yesu katika Mat.6:10. Mathayo, akiwaandikia Wayahudi, alipendelea kifungu kile ambacho hakitumii jina la Mungu (yaani., Ufalme wa Mbinguni), wakati Marko na Luka, akiwaandikia watu wa mataifa, anatumia usanifu wa kawaida, akiweka jina la Uungu.

Hiki ni kile kifungu cha mfano katika mihitasari ya injili. Hotuba za kwanza na za mwisho za Yesu, na zaidi mafumbo yake, yanashughulika na mada. Zinarejerea utawala wa Mungu katika mioyo ya wanadamu sasa! Inashangaza kuona kwamba Yohana anatumia kifungu hiki mara mbili tu (na kamwe sio kwenye mafumbo ya Yesu). Katika injili ya Yohana "uzima wa milele" ni sitiari muhimu.

Mvutano na kifungu hiki unasababishwa na ujio mara mbili wa Kristo, Agano la Kale linatazamisha kwenye ujio mmoja wa Masiha wa Mungu kama afisa wa kijeshi, ujio wa kitukufu-lakini Agano Jipya linaonyesha kuwa alikuja kwanza kama mtumishi mwenye mateso katika Isaya 53 na mfalme mnyenyekevu katika Zak. 9:9. Enzi mbili za Kiyahudi (angalia mada maalumu: Enzi hii na Enzi inayokuja), enzi ya uovu na enzi mpya ya haki, zimeingiliana. Kwa sasa Yesu anatawala ndani ya mioyo ya waumini, lakini siku moja atatawala juu ya uumbaji wote. Atakuja kama Agano la Kale lilivyotabiri (kama vile Ufunuo 19)! Waamini wanaishi ndani ya ulimwengu wa Mungu "uliotayari" dhidi ya "ule ambao bado" (kama vile Gordon D. Fee na Douglas Stuart's *How to Read The Bible For All Its Worth*, kurasa za. 131-134).

☐**"tubuni"** Toba ni muhimu kwa ajili ya imani ya mahusiano pamoja na Mungu (kama vile Mt. 3:2; 4:17; Marko 1:15; 6:12; Luka 13:3,5; Mdo. 2:38; 3:19; 20:21). Neno kaika Kiebrania lilimaanisha kubadili kitendo (BDB 996), wakati katika Kiyunani lilimaanisha kubadili nia. Toba ni utayari wa kubadilika kutoka kwenye ubinafsi kwenda kwenye maisha yenye taarifa na yanayoongozwa na Mungu. Inahitaji mgeuko kutoka katika kipaumbele na kifungo cha ubinafsi (kama vile Mwanzo 3). Kimsingi ni matazamo mpya, mtazamo mpya wa kiulimwengu, mtawala mpya. Toba ni mapenzi ya kila mwanadamu aliyefanywa kwa sura yake (kama vile Ezek. 18:21,23,32 na 2 Pet. 3:9).

Kifungu cha Agano Jipya ambacho kinaaksi vizuri zaidi maneno tofauti ya Kiyunani kwa ajili ya Toba ni 2 Kor. 7:8-12.

1. *lupē*, "simanzi" au "huzuni" 2 Kor. 7:8 (mara mbili), 2 Kor. 7:9 (mara tatu), 2 Kor. 7:10 (mara mbili), 2 Kor. 7:11
2. *metamelomai*, "baada ya matunzo," 2 Kor. 7:8 (mara mbili), 2 Kor. 7:9
3. *metanoēō*, "tubu," "baada ya nia," 2 Kor. 7:9, 10

Tofauti ni toba ya uongo [*metamelomai*] (kama vile Yuda, Mt. 27:3 na Esau, Ebr. 12:16-17) dhidi ya toba ya kweli [*metanoēō*].

Toba ya kweli kithioloji inaunganishwa na

1. Mahubiri ya Yesu (kama vile Mt. 4:17; Marko 1:15; Luka 13:3,5)
2. mahubiri ya kitume katika Mdo. [*kerygma*] (kama vile Mdo. 3:16,19; 20:21)
3. kipawa cha Mungu altawalaye (kama vile Mdo. 5:31; 11:18 na 2 Tim. 2:25)
4. upotevu (kama vile 2 Pet. 3:9)

Toba sio suala la kuchagua!

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 4:18-22**

<sup>18</sup> Naye alipokuwa akitembea kando ya bahari ya Galilaya, aliona ndugu wawili, Simoni aitwaye Petro, na Andrea nduguye, wakitupa jarife baharini; kwa maana walikuwa wavuvi. <sup>19</sup> Akawaambia, Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu. <sup>20</sup> Mara wakaziacha nyavu zao, wakamfuata. <sup>21</sup> Akaendelea mbele, akaona ndugu wengine wawili, Yakobo wa Zebedayo, na Yohana nduguye, ambao walikuwamo chomboni pamoja na Zebedayo baba yao, wakizitengeneza nyavu zao; akawaita. <sup>22</sup> Mara wakakiacha chombo na baba yao, wakamfuata.

**4:18 "bahari ya Galilaya"** Maji masafi ya ziwa ni kama maili 12 kwa maili 8. Ilikuwa inajulikana katika Biblia kwa majina manne.

1. bahari ya Kinerethi (kama vile Hes. 34:11)
2. ziwa la Genesareti, (kama vile Luka 5:1)
3. Bahari ya Tiberia (kama vile Yohana 6:1; 21:1)
4. hapa bahari ya Galilaya

☑ **"aliona ndugu wawili"** Haifahamki ikiwa hii ilikuwa mara ya kwanza kwa watu hawa kukutana na kumsikia Yesu. Inavyoonekana mwitikio wao wa haraka uliaksi kukutana mapema zaidi yawezekana imeandikwa katika Yohana 1:45- 51. Lazima ikumbukwe kwamba Yohana aliandika mapema juu ya huduma za Galilaya na Yudea. Mfululizo wa Yohana wa maish ya Yesu na matukio katika: Galilaya, Yudea, Galilaya, na Yudea.

☑ **"jarife"** Hii inarejerea jarife la mviringo la kurusha kwa mkono japo neno "jarife" katika Mt. 4:20 na 21 ni neno tofauti na inarejerea jarife kubwa inayovutwa na boti.

1. nyuma ya boti au kati ya boti
2. katika upande wa mwishoni ana kupigwa nanga mwambaoni, upande mwingine kunyooshwa zaidi na boti kwa kama nusu duara.

**4:19 "Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu"** Katika mazingira ya kiyahudi Yesu alikuwa kirasmi akiwaita watu hawa kuwa wanafunzi. Kulikuwa na kanuni na taratibu juu ya namna gani mwalimu angefanya hivi. Msamiati ni mbinu ya kazi yao ya sasa ya uvuvi na wale wapya wao kama ushuda na mwnjilisti.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 4:23**

<sup>23</sup> Naye alikuwa akizunguka katika Galilaya yote, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri Habari Njema ya ufalme, na kuponya ugonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu.

**4:23 "Yesu naye alikuwa akizunguka katika Galilaya yote"** Hii ilihusiana huduma za kibayana tatu: (1) kufundisha; (2) kuhubiri; na (3) kuponya. Inashangaza kujua kwamba waliitikia huduma ya tatu bali mara nyingi ya kwanza na ya pili ziliachwa. Huduma ya tatu ilikuwa tu kama uthibitisho wa ustawi na nguvu ya mbili za kwanza. Ilikuwa inawezekana mtu kupona bila kuokoka (kama vile Yohana. 5).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 4:24-25**

<sup>24</sup> Na habari zake zikaenea katika Shamu yote; wakamletea wote waliokuwa hawawezi, walioshikwa na maradhi mbalimbali na mateso, wenye pepo, na wenye kifafa, na wenye kupooza; akawaponya. <sup>25</sup> Na makutano mengi wakamfuata, kutoka Galilaya, na Dekapoli, na Yerusalemu, na Uyahudi, na ng'ambo ya Yordani

**4:24 "Na habari zake zikaenea katika Shamu yote"** Shamu ilikuwa jimbo la Kirumi ambalo lilijumuisha Palestina Kaskazini. Hata hivyo katika muktadha huu inaweza kurejerea eneo lote ambalo lilionesha umaarufu ulioenea la mponyaji huyu kutoka Nazareti.

☑️**"akamletea wote waliokuwa hawawezi, walioshikwa na maradhi mbalimbali na mateso, wenye pepo, na wenye kifafa, na wenye kupooza"** Katika Injili Utofauti unatengenezwa kati ya udhaifu wa mwili na kupagawa na pepo. Ingawa nguvu za mapepo zinaweza kusababisha dalili za kimwili, tiba ya kila kimoja ni tofauti. Yesu aliwaponya wote walioletwa Kwake (Angalia Mada Maalumu katika Mt. 19:2). Tunajua kutoka katika hadithi zingine kwa habari ya uponyaji wakati mwingine ulijikita katika imani ya mtu au imani ya rafiki wa mtu anayeumwa; na wakati mwingine ilikuja bila hata imani sana kabisa. Uponyaji wa mwili siku zote haukumaanisha au kuashiria kwamba kuna wokovu wa kiroho (kama vile Yohana. 9).

☑️**"mapepo"** Angalia Mada Maalum katika Mt. 10:1.

☑️**"kifafa"** Angalia dokezo katika Mt. 17:15.

**4:25 "makutano makubwa yakamfuata"** Mstari wa 25 ni maelezo ya kimahesabu ya kiwango cha umaarufu wa Yesu (kama vile Marko 3:7-8; Luka 6:17). Umaarufu huu ulisababisa viongozi kuwa na wivu na makutano kumuelewa vibaya.

### **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Nini makusudi ya kujaribiwa kwa Yesu?
2. Shetani ni nani na nini kusudi lake?
3. Je majaribu haya yalikuwa ya kisaikolojia, kimwili au kimaono?
4. Kwanini Injili zinasisitiza huduma ya Yesu ya Galilaya?
5. Wakati Yesu alipoita wanafunzi, je walikuwa wamekwisha kukutana nae au kumsikia kabla ya muda huo?
6. Je Agano Jipya linaweza utofauti katika kupagawa na pepo na udhaifu wa mwili? Ikiwa ndivyo, kwanini?

## MATHAYO 5

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Mahubiri juu ya Mlima	Heri	Mahubiri juu ya Mlima (5:1-7:27)	Mahubiri juu ya Mlima	Heri
5:1-2	5:1-12	5:1-2	5:1-2	5:1-12
Heri		Heri	Furaha ya Kweli	
5:3-12		5:3	5:3-10	(3-10)
		5:4		
		5:5		
		5:6		
		5:7		
		5:8		
		5:9		
		5:10		
		5:11-12	5:11-12	
Chumvi na nuru	Waamini ni Chumvi na nuru	Ushuhuda wa Wanafunzi	Chumvi na nuru	Chumvi kwa nchi na Nuru kwa Ulimwengu
5:13-16	5:13-16	5:13	5:13	5:13
		5:14-16	5:14-16	5:14-16
Kufundisha Juu ya Sheria	Kristo Kutimiza Sheria	Uhusiano wa Ujumbe wa Yesu Kwa sheria ya Wayahudi	Kufundisha Kuhusu sheria	Kutimilizwa kwa Sheria
5:17-20	5:17-20	5:17-20	5:17-20	5:17-19
Kufundisha juu Ya Hasira	Mauaji huanza Katika Moyo	Kielelezo cha Uelewa wa Kweli Wa Sheria	Kufundisha juu ya Hasira	Viwango vipya vya juu Kuliko vya Zamani
				5:20
5:21-26	5:21-26	5:21-26	5:21-24 5:25-26	5:21-26
Fundisho juu Ya Uzinzi	Uzinzi katika Moyo		Fundisho kuhusu Uzinzi	
5:27-30	5:27-30	5:27-30	5:27-20	5:27-30
Fundisho juu Ya Talaka	Ndoa ni Takatifu na ya Kudumu		Fundisho juu ya Talaka	
5:31-32	5:31-32	5:31-32	5:31-32	5:31-32
Fundisho juu Ya Viapo	Yesu anakataa Viapo		Fundisho juu ya Viapo	
5:33-37	5:33-37	5:33-37	5:33-37	5:33-37
Fundisho juu ya Visasi	Nenda maili mbili		Fundisho juu ya Visasi	
5:38-42	5:38-42	5:38-42	5:38-42	5:38-42
Upendo kwa Adui	Wapende Adui Zako		Upendo kwa Adui	
5:43-48	5:43-48	5:43-48	5:43-48	5:43-48



## **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)")**

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA SURA YA 5-7**

A. Mahubiri haya yamekuwa yakiitwa

1. "Mahubiri ya kuwekwa Wakfu kwa Mitume Kumi na Wawili"
2. "Mkusanyo wa Mafundisho ya Ukristo"
3. "Kanuni za Ufalme"
4. "Itifaki ya Mfalme"

Neno "Mahubiri ya Mlimani" lilitumika kwa mara ya kwanza na Augustine (354-430 B.K) katika Fasiri yake ya Kilatini juu ya Mathayo. Neno hili lilikuja katika Biblia zetu za Kingereza kupitia Biblia ya Coverdale ya mnamo mwaka 1535 B.K.

B. "Mahubiri ya Mlimani" katika Mathayo 5-7 yawezekana ni sawasawa na "Mahubiri juu ya Mambo ya Msingi" katika Luka 6. Tofauti katika maudhui inaweza kuelezewa kwa kulinganisha hadhira iliyokusudiwa ya waandishi wa Injili; Wasomaji wa Mathayo walikuwa Wayahudi wa Kipalestina na wasomaji wa Luka walikuwa Mataifa. Hata hivyo kwasababu tofauti ni kubwa sana, wengi huamini kwamba si mahubiri ya aina moja. Yanaweza kuwa mfano mara kwa mara ya maudhui yanayorudiwa kwa kutumiwa na Yesu katika sehemu nyingi yakiwa na hadhira tofauti. Mfano wa hili ni mafano wa kondoo aliyepotea. Katika Mathayo 18 ilikusudiwa kwa wanafunzi lakini katika Luka 15 kwa wenye dhambi.

C. Chini ya uvuvio wa Mungu, waandishi wa Injili walikuwa huru kuchagua kutoka katika mafundisho ya Yesu na matendo na kuyaunganisha katika namna isiyo ya mfuatano kuzungumzia ukweli wa kithiolojia. Tazama Fee na Stuart's *Howto Read the Bible for All Its Worth*, kur. 127-148. Injili sio hadithi za maisha ya watu, ni machapisho ya kiinjalisti na miongozo ya kutengeneza wanafunzi. Mathayo inaunganisha mafundisho ya Yesu na miujiza kwenda katika vipengele vya kimaudhui wakati Luka anaandika mafundisho haya katika muktadha mbali mbali katika Injili yake.

D. Muundo wa kwanza wa Mathayo (kati ya tano, yaani, 5-7; 10-13; 18; 24-25) na muktadha mrefu wa Yesu ni wa Kiyahudi, yawezekana ufanano unaoeleweka wa kimuundo na Amri Kumi. Kauli zinaelekeza sentensi fupi na tata. Kimaudhui hazina uhusiano wa ukaribu lakini kisarufi zikijitenga.

E. Mafundisho haya ni kilele cha maadili ya Ufalme kuwashuhudia waliopotea na kuwatia hamasa waliokoka. Hadhira ilikuwa imejumuishia makundi kadhaa tofauti tofauti: wanafunzi, wenye shauku, watazamaji na wasomi wa kidini. Maandiko tofauti yalikuwa yamekusudiwa kwa makundi tofauti.

- F. Mafundisho haya kimsingi ni mtazamo wa maisha au "mtazamo wa kiulimwengu" mbao kimsimamo umejikita upya katika imani na utii kwa Mungu. Kuna hadithi ya dhahiri katika Kutoka 20 na Kumb. 5.
- G. Kitabu kizuri ambacho kinaelezea mafundisho ya Yesu na mbinu za kuhubiri ni Robert H. Stein's, *The Methods and Message of Jesus' Teaching*, Westminster Press, 1978, ISBN 0-664-24216-2.
- H. Kusudi sio kuonesha waliopotea namna gani ya kuokolewa lakini namna gani Mungu anatarajia waliokoka kuishi. Maadili ya Ufalme upya ni ya kimsimamo kwamba hata wajihesabiao haki waliojitoa zaidi hujihisi kukosa utoshelevu. Neema ni tumaini pekee kwa ajili ya wokovu (yaani, Isa 55:1-3) na nguvu ya Roho tumaini pekee kwa ajili ya kuishi katika ufalme (yaani, Isa. 55:6-7).

### TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA 5:3-12 (HERI)

- A. Heri zinatengeneza ngazi ya Kiroho (1) kutoka katika wokovu mpaka kufanana na Kristo au (2) Kutoka katika namna ya hitaji la kiroho la mwanadamu kwa maisha mapya ya mwanadamu katika Kristo.
- B. Hesabu zake zimekuwa zikieleweka tofauti tofauti kama 7, 8, 9, na hata 10.
- C. Heri inadai mwitikio kutoka kwa msomaji/msikilizaji! Hazijakusudiwa kuwa taarifa bali kuleta hamasa!
- D. Nukuu tatu za Muhimu:
  1. Kila mfumo wa kimaadili ni barabara ambayo kwa kujikana kibinafsi, nidhamu na juhudi, wanadamu wanatafta kufikia lengo. Kristo anaanza kwa lengo hili na kuwaweka wanafunzi wake mara moja katika nafasi ambayo wanafunzi wengine wote wanamwelekeza kama hitaji. . .Wanaanza kwa kuamuru: kwasababu analeta mafungu mema ya msamaha na rehema." *The Life and Times of Jesus the Messiah* na Alfred Edersheim, kur. 528-529.
  2. "Mahubiri ya mlimani sio mwongozo usio tekelezeka wala taratibu za kisheria zilizowekwa kwa kuafikinishwa. Badala yake ni kauli ya kanuni za maisha zilizo za msingi katika jamii ya kawaida. . . Misemo mingi ya mahubiri ni ya kisitiari au kauli za kimithali na hazitakiwi kueleweka. Ndani yake Yesu alikuwa akifafanua kanuni katika kanuni katika makubaliano yaliyowazi." *The International Standard Bible Encyclopedia*. vol. 4 p. 2735.
  3. "Kanuni za Msingi:
    - a. tabia ni siri ya furaha.
    - b. Haki imejikita katika maisha ya ndani. Tabia sio kitu cha kushurutishwa kutoka nje bali maisha yanayotoka ndani.
    - c. Maisha ya ndani ni umoja.
    - d. Upendo wa kiujumla ni msingi wa kanuni ya kijamii.
    - e. Tabia na maisha yanakuwepo na kwa ajili ya ushirika na Baba. Ibada zote na mwenendo unamueleza kwa Mungu.
    - f. Utimilizwaji ni jaribu la mwisho la maisha.
    - g. Matendo na tabia ni vitu pekee ambavyo vinadumu na uvumilivu ni jaribio la mwisho." *The International Standard Bible Encyclopedia*. vol. 4 kur. 2735.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 5:1-2

<sup>1</sup> Naye alipowaona makutano, alipanda mlimani; na alipokwisha kuketi, wanafunzi wake walimjia; <sup>2</sup> akafumbua kinywa chake, akawafundisha, akisema,

**5:1 "Naye alipowaona makutano"** Watu kutoka kila eneo la jamii walimkimbilia Yesu. Makutano haya makubwa yalikuwa pia katika Mt. 4:23-25 na Luka 6:17. Yawezekana wanafunzi na wale waliokuwa hasa wakitamani, walitengeneza mzunguko wa ndani uliokaribu zaidi na Yesu pamoja na wengine (kama vile Mt. 7:28).

☐ **"mlimani"** Katika Luka 6:17 mazingira ya kimwili yako wazi lakini maushui ya ujumbe kimsingi ni ule ule. Mazingira ya kihistoria ya Luka yanaonekana kuwa bora zaidi kabisa. Yesu alikuwa akiomba juu ya mlima kuhusu uchaguzi wake wa Wanafunzi Kumi na Mbili lakini alishuka chini mpaka bondeni ili kupokea makutano na alafu akapanda juu ya mlima mwendo mfupi ili kwamba wote wapate kusikia na kuona. Neno la Kiyunani katika Mathayo linaweza kurejerea mji wa juu na neno katika Luka linaweza kurejerea katika uwanda unaolingana katika sehemu ya mlima. Hivyo labda kutofautiana kwa dhahiri ni tatizo la ufasiri wa kingereza.

Hata hivyo jumbe mbili ni tofauti kwa namna nyingi. Mathayo anaweza kuwa ameelezea mazingira ya mlima kwa ufanano wa kutolewa kwa sheria juu ya Mlima Sinai. Yesu ni mtoa sheria (kama vile Mt. 5:21-48). Mwandishi wa Injili kwa makusudi anatengeneza muundo wa maisha ya Yesu kwa namna ya kuigilizia maisha ya Musa (hapa, Kut. 19:3; 24:12). Yesu ni "Mtoa sheria" mpya na mkuu! Yeye ni nabii ambaye Musa alisema kuwa atakuja baada yake (kama vile Kumb. 18:14-22). Wanadamu walioanguka (wote Wayahudi na Mataifa) wanapata wokovu wao katika Yeye, sio katika utendaji kazi wao wa kidini (kama vile Yer. 31:31-34; Ezek. 36:22-38, "agano jipya")!

☐ **"alika chini"** Hii ilikuwa nahau ya kiyahudi kwa ajili ya kufundishia kirasmi (26:55; Marko 9:35; Luka 4:20; 5:3; Yohana 8:2), kama alivyokuwa "alifungua kinywa chake" (Mt. 5:2). Tungo hizi sambamba na ufungaji ulioyakinishwa wa Mt. 7:28, "Wakati Yesu alipofunga mahubiri haya," ikimaanisha kwamba hii iliwasilishwa na Mathayo kama moja ya mahubiri. Haya ni moja ya mahubiri marefu kati ya matano yaliyofanywa na Yesu yakibandikwa katika Mathayo (Mathayo 10, 13, 18, & 24-25).

☐ **"wanafunzi wake wakamwendea"** Baadhi wanadhania kwamba Mathayo na Luka ni mahubiri tofauti, wanaeleza kwamba ni wanafunzi tu waliokuwepo hapa. Walikuwa ndio vyombo na wapokeaji wa mahubiri haya, lakini watu wa kawaida na viongozi wa kidini walikuwa wakisimama kando wakisikiliza (kama vile Mt. 7:28). Inawezekana kwamba Yesu alizungumza na kundi moja alafu pia akazungumza na lingine.

**5:2 "akaanza kuwafundisha"** Hii ni njeo ya wakati usio timilifu, ambayo naweza kumaanisha (1) Alianza kufundisha au (2) aliendelea kurudia rudia mambo haya sehemu mbali mbali. Injili ya Mathayo inapewa sifa ya kuunganisha mafundisho ya Yesu katika mada. Maudhui ya Mathayo 5-7 yametawanyika katika sura nyingi nyingi katika Luka.

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 5:3

<sup>3</sup> Heri walio maskini wa roho; Maana ufalme wa mbinguni ni wao.

**5:3 "Heri"** Neno hili lilimaanisha "kuwa na furaha" au "kuheshimishwa" (kama vile Mt. 5:3-11). Neno la Kingereza "furaha" linatoka katika kingereza cha zamani "kipindi kati ya kutokea." Furaha inayotolewa na Mungu kwa ajili ya waamini haijikiti juu ya mazingira ya nje bali furaha ya ndani. Hakuna vitenzi katika kauli hizi. Ni zenye kuuliza (kama vile Ufu. 1:3) katika muundo kama Kiaramu au Waebrania (kama vile Zab.1:1). Kubarikiwa huku ni vyote

mtazamo wa sasa kumuelekea Mungu na maisha na pia tumaini la siku za mwisho. Mtu aliyebarikiwa alikuwa ni mwenye haki (kama vile Zab. 119:1-2).

☐ **"masikini wa roho"** Maneno mawili katika Kiyunani yalitumika kuelezea umasikini; moja ya iliyotumika hapa ilikuwa kali zaidi kuliko nyingine. Ilikuwa mara kwa mara ikitumika juu ya masikini aliyekuwa akimtegemea mtoaji. Katika Agano la Kale hii ilimaanisha tumaini katika Mungu pekee! Mathayo anaweka wazi kwamba hii hairejerei umasikini wa mwilini bali hali ya kutojitosheleza kiroho. Mwanadamu lazima atambue utoshelevu wa Mungu na kutojitosheleza kwake yeye mwenyewe (kama vile Yohana. 15:5; 2 Kor. 12:9). Huu ni mwanzo wa injili (kama vile Rum. 1:18-3:31). Yawezekana heri hizi chache za kwanza zina-aksi Isa. 61:1-3, ambayo ilitabiri Baraka za Kimasihi kwa Zama Mpya Ijaye.

☐ **"ufalme wa mbinguni"** Tungo hii, "Ufalme wa Mbinguni" au "Ufalme wa Mungu," linatumika mara 100 katika Injili. Katika Luka 6:20 ni "Ufalme wa Mungu." Mathayo alikuwa anaandika kwa ajili ya watu walio na historia ya Kiyahudi waliokuwa na hofu ya kutaja jina la Mungu kwasababu ya Kutoka 20:7. Lakini Injili ya Marko (kama vile Mt. 10:14) na Luka kiliandikwa ajili ya Mataifa. Tungo mbili zina ufanano. Angalia Mada Maalum katika Mt. 4:17. Tungo inarejerea kwenye utawala wa Mungu katika mioyo ya watu sasa kwamba utatimilizwa juu ya nchi (kama vile Mt. 6:10). Hii yawezekana inathibitishwa na Mathayo ikika kati ya njeo ya wakati uliopo "ni" katika Mt. 5:3 na 10, njeo ya wakati ujao "uta.." katika Mt. 5:4-9.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 5:4**

<sup>4</sup> Heri wenye huzuni; Maana hao watafarijika.

**5:4 "huzuni"** Hii inarejerea kwa "kuomboleza kwa sauti ya juu," ambalo lilikuwa neno lenye nguvu zaidi kwa kuomboleza katika lugha ya Kiyunani. Mukadha unamaanisha kwamba maombolezo yalikuwa kwa ajili ya dhambi zetu. Matokeo ya kuona dhambi ya mtu (Mt. 5:3) lazima kuwe na toba (Mt. 5:4). Inawezekana ikiwa Agano la Kale rejea yake ni Isa. 61:1-3, kwamba yalikuwa ni maombolezo ya jamii moja kwa namna ya kijamii.

☐ **"watafarijiwa"** Angalia Isa. 12:1; 40:1; 49:13; 51:3,12; 52:9; 66:13. Zama mpya imeanza katika Kristo. Mungu anafariji sio tu watu wa Mungu bali wote waaminio/wamtumainio Yesu. Ahadi za Agano la Kale kwa Israeli zimekuwa za kiulimwengu wote (kama vile Yohana 3:16).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 5:5**

<sup>5</sup> Heri wenye upole; Maana hao watairithi nchi.

**5:5 "wenye upole"** Hii kibayana "upole" au "mwenye kujinyenyekeza." Yesu alilitumia neno hili kwa ajili yake Mwenyewe (kama vile Mt. 11:29; 21:5). Asili yake inamaanisha nguvu inayofugwa kama farasi mwenye mafunzo. Kutambua hitaji letu kwa ajili ya Mungu na utoaji Wake katika Kristo unafanya waaminio wapole na wenye kufundishika (kama vile 1 Pet. 3:4). Mungu anataka kuongoza nguvu zetu kwa ajili ya makusudi yake (Aliwapa, kama vile Zab. 139; 1 Wakorintho 12), sio kuwavunja.

☐ **"watairithi nchi"** Hii mara kwa mara ilikuwa ikihusianishwa na Nchi ya Ahadi (kama vile Zab. 37:11), lakini inaweza kuwa rejea ya siku za mwisho kwa ajili ya nchi yote (kama vile Isa. 11:6-9). Hii inaaksi utata wa neno la kiebrania *erets* (BDB 75). Tena Ahadi za Mungu za Agano la Kale zimefanywa kuwa za ulimwengu wote.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 5:6**

**5:6 "wenye njaa na kiu"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo (kama vile Yohana. 4:10-15). Sitiari hii inaaksi mtazamo wa mtu unaoendelea kumuelekea Mungu (kama vile Zab. 42:2; 63:1-5; Isa. 55:1; Amosi 8:11-12). Hii ni ishara kwamba sura ya Mungu ilipotea wakati wa anguko, imerejeshwa kupitia Kristo.

**NASB, NKJV**

**NRSV**

**"kwa ajili ya haki"**

**TEV**

**"kufanya kile Mungu akitakacho"**

**NJB**

**"kwa ukamilifu"**

Kimsingi neno hili kithiolojia linaweza kumaanisha (1) kutangazwa (kisheria) au kukatwa (kibenki) kwa ukamilifu (kama vile Warumi 4) au (2) maadili ya ufalme wa kibinafsi ambayo ni matumizi ya Mathayo ya neno (kama vile Mt. 6:1 matumizi ya hekalu). Ilihusisha vyote kuhesabiwa haki na haki; vyote kutakaswa na maisha yaliyotakaswa! Huu ni mfano mwingine wa mzunguko wa Mathayo, kuweka mbadala wa neno lingine au tungo kwa ajili ya jina la Mungu (kama vile Mt. 5:7-8).

## **MADA MAALUM:HAKI**

"Haki"ni mada muhimu ambayo mwanafunzi wa Biblia yampasa kufanya ni upanuzi binafsi wa kusoma juu ya dhana yenyewe.

Katika Agano la Kale sifa za Mungu zinaelezwa kama "halali" au "haki" (KITENZI, BDB 842, KB 1003; NOMINO JINSI YA KIUME, BDB 841, KB 1004; NOMINO JINSI YA KIKE, BDB 842, KB 1006). Neno la Mesopotamia lenyewe linatokana na "mafunjo ya mto" ambayo yalitumika kama chombo cha matengenezo ya utaalamu wa mlalo ulionyooka na uelekeo wa ukuta na ua. Mungu alilichagua neno lililotakiwa kutumika kistiari juu ya asili Yake mwenyewe. Yeye ni ukingo ulionyooka (kiongozi) ambapo vitu vyote vinatathiminiwa toka kwake. Dhana hii inatetea haki ya Mungu pamoja na Haki Yake ya kuhukumu.

Mwanadamu aliumbwa katika mfano wa Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1,3; 9:6). Mwanadamu aliumbwa kwa ushirika wa Mungu (yaani, Mwa. 3:8). Uumbaji wote ni hatua au mrejesho kwa Mungu na mwingiliano wa wanadamu. Mungu aliutaka uumbaji Wake mkuu, mwanadamu, kumjua Yeye, kumpenda Yeye, kumtumikia Yeye, na kuwa kama Yeye! Uaminifu wa mwanadamu ulipimwa (kama vile Mwanzo 3) na watu hawa wanadoa wa mwanzo walishindwa jaribio. Hii ilileta matokeo ya kuvunjika kwa uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu (kama vile Rum. 5:12-21).

Mungu aliahidi kufanya marekebisho na kurejesha ushirika (kama vile Mwa. 3:15; tazama Mada Maalumu: Mpango wa Wokovu wa Milele wa YHWH). Alifanya hivi kupitia mapenzi Yake mwenyewe na Mwanee . Wanadamu hawawezi kurejesha ahadi iliyovunjwa (kama vile Rum. 1:18-3:20; Ufunuo 5).

Baada ya Anguko,hatua ya kwanza ya Mungu kuelekea urejesho ilikuwa dhana ya agano lililojikita katika mwaliko Wake na toba ya mwanadamu, imani, mwitikio wa utii (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38). Kwa sababu ya Maanguko yote, wanadamu huwakuweza kujitenga na tendo (kama vile Rum. 3:21-31; Wagalatia 3).

Mungu Pekee ilimbidi kuanzisha upya agano lililokuwa limevunjwa na wanadamu. Alifanya hivi kwa

1. kutangaza haki ya mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya mahakama)
2. kwa kutoa haki huru kwa mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya kuzuliwa)
3. kumtoa Roho akaaye ndani ambaye huleta haki (yaani, Ufanano na Kristo, urejeshaji wa mfano wa Mungu) ndani ya mwanadamu
4. kurejesha ushirika wa Bustani ya Edeni (linganisha Mwanzo 1-2 na Ufunuo 21-22)

Hata hivyo, Mungu anahitaji mwitikio wa kimaagano. Mungu hutoa maagizo (yaani, hutoa kwa uhuru, Warumi 5:8; 6:23) lakini yawapasa wanadamu kuitikia na kuendelea kuitika katika

1. Toba
2. Imani
3. Utii kwenye stadi ya maisha

#### 4. Ustahimilivu

Haki, kwa hiyo, ni agano, ni makubaliano kati ya Mungu na uumbaji Wake wa juu, uliyojikita juu ya sifa za Mungu, kazi ya Kristo, na Roho mwezeshaji, ambapo kila mtu kibinafsi anapaswa kuitikia kwa namna ifaavyo. Dhana inaitwa "haki kwa neema kupitia imani" (yaani, Efe. 2:8-9). Dhana inafunuliwa katika Injili, lakini si katika maneno haya. Kimsingi ilielezwa na Paulo, ambaye anatumia neno la Kiyunani "mwenye haki" katika miundo yake mbalimbali zaidi ya mara 100.

Paulo, akiwa mwalimu wa sheria aliyefundishwa, anatumia neno *dikaio sunē* katika maana yake ya Kiebrania ya neno *tsaddiq* lililotumika katika Tafsiri za Maandiko ya Kale ya Kiebrania, na si kutoka katika fasiri ya Kiyunani. Katika maandishi ya Kiyunani neno linamhusu yule ambaye amethibitisha matarajio ya Mungu na jamii (yaani, Nuhu, Ayubu). Katika maana ya Kiebrania mara nyingi limendwa katika maneno ya kimaagano (tazama Mada Maalumu: Agano). YHWH ni haki, maadili, Mungu mwema. Anawataka watu Wake kuwa viumbe vipya ili kwendana na sifa zake. Mwanadamu aliyekombolewa anakuwa kiumbe kipya (kama vile 2 Kor. 5:17; Gal. 6:15). Upya huu unaleta matokeo katika mtindo mpya wa maisha ya Kimungu (kama vile Mathayo 5-7; Gal. 5:22-24; Yakobo; 1 Yohana). Tangu Israeli ilipokuwa katika mfumo wa utawala wa kidini hapakuwepo na maelezo sahihi na ya kinagaubaga kati ya ulimwengu (kanuni za kijamii) na Mungu (mapenzi ya Mungu). Utofauti huu unaeleza katika maneno ya Kiebrania na Kiyunani kuwa ya kutafsirika katika Kiingereza kama "haki" (yakihusiana na jamii) na "mwenye haki" (ikihusiana na dini).

Injili (habari njema) juu ya Yesu ni kwamba wanadamu walioanguka wamerejesha ushirika na Mungu. Hii limetimizwa kupitia pendo la Baba, huruma, na neema; maisha ya Mwana, kifo, na ufufuo; na kuugua kwa Roho na kielelezo cha injili. Haki ni tendo huru la Mungu, lakini linapaswa kuwa jambo la kimungu (Mtazamo wa Augustine, ambao unaakisi vyote msistizo wa Mabadiliko mapya juu ya uhuru wa injili na msisitizo wa Kanisa Katoriki juu ya maisha yaliyobadilishwa ya upendo na uaminifu). Kwa waleta mabadiliko neno "haki ya Mungu" ni shamilisho milikishi (yaani, tendo la mwanadamu aliyetenda dhambi kukubaliwa na Mungu [utakaso wa mahali], ambapo kwa Wakatoliki ni kiima milikishi, ambapo ni tendo la kuimarika zaidi kama Mungu [utakaso endelevu na uliozoeleka]).

Katika mtazamo wangu, Biblia nzima kutoka Mwanzo 4 – Ufunuo 20 ni maandiko yenye kuonyesha urejesho wa ushirika wa Mungu pale Edeni. Biblia inaanza kati ya Mungu na mwanadamu kuleta ushirika na mpangilio wa dunia (kama vile Mwanzo 1-2) na Biblia inaridhia mpangilio huo huo (kama vile Ufunuo 21-22). Mfano wa Mungu na kusudi lake vitarejeshwa!

Ili kuthibitisha mjadala wa hapo juu andika vifungu vilivyochguliwa vya Agano Jipya vyenye vielelezo vya kundi la neno la Kiyunani.

1. Mungu ni haki (mara kwa mara imeunganishwa kwa Mungu kama Hakimu)
  - a. Warumi 3:26
  - b. 2 Wathesalonike 1:5-6
  - c. 2 Timotheo 4:8
  - d. Ufunuo 16:5
2. Yesu ni haki
  - a. Matendo 3:14; 7:52; 22:14 (jina la Masihi)
  - b. Mathayo 27:19
  - c. 1 Yohana 2:1,29; 3:7
3. Mapenzi ya Mungu kwa uumbaji Wakeni ya haki.
  - a. Mambo ya Walawi 19:2
  - b. Mathayo 5:48 (kama vile 5:17-20)
4. Kusudi la Mungu kutoa na kutoa haki
  - a. Warumi 3:21-31
  - b. Warumi 4
  - c. Warumi 5:6-11
  - d. Wagalatia 3:6-14
  - e. Iliyotolewa na Mungu
    - a. Warumi 3:24; 6:23

- b. 1 Wakorintho 1:30
- c. Waefeso 2:8-9
- f. Iliyopokelewa kwa imani
  - a. Warumi 1:17; 3:22,26; 4:3,5,13; 9:30; 10:4,6,10
  - b. 2 Wakorintho 5:7,21
- g. kupitia matendo ya Mwana
  - a. Warumi 5:21
  - b. 2 Wakorintho 5:21
  - c. Wafilipi 2:6-11
- 5. Mapenzi ya Mungu ni kwamba wafuasi Wake wawe wenye haki
  - a. Mathayo 5:3-48; 7:24-27
  - b. Warumi 2:13; 5:1-5; 6:1-23
  - c. Waefeso 1:4; 2:10
  - d. 1 Timotheo 6:11
  - e. 2 Timotheo 2:22; 3:16
  - f. 1 Yohana 3:7
  - g. 1 Petro 2:24
- 6. Mungu ataihukumu dunia kwa haki
  - a. Matendo 17:31
  - b. 2 Timotheo 4:8
- 7. Kupitia matendo ya Mwana
  - a. Warumi 5:21
  - b. 2 Wakorintho 5:21
  - c. Wafilipi 2:6-11
- 8. Mapenzi ya Mungu ni kwamba wafuasi wake wawe watakatifu
  - a. Mathayo 5:3-48; 7:24-27
  - b. Warumi 2:13; 5:1-5; 6:1-23
  - c. Waefeso 1:4; 2:10
  - d. 1 Timotheo 6:11
  - e. 2 Timotheo 2:22; 3:16
  - f. 1 Yohana 3:7
  - g. 1 Petro 2:24
- 9. Mungu atauhukumu ulimwengu kwa haki
  - a. Matendo 17:31
  - b. 2 Timotheo 4:8

Haki ni tabia ya Mungu, iliyotolewa huru kwa wanadamu wenye dhambi kupitia Kristo. Hilo ni

1. agizo la Mungu
2. zawadi ya Mungu
3. tendo la Kristo
4. ni maisha yapaswayo kuishi

Lakini pia ni tendo la kuwa mwenye haki ambapo ni lazima kuwa na juhudi, uaminifu na kuishikilia, kwamba siku moja itatimizwa katika Ujio wa Pili. Ushirika na Mungu unarejeshwa katika wokovu lakini unaendelea katika maisha mazima ili kukutana naye ana kwa ana (kama vile 1 Yohana 3:2) katika kifo au ujio wa pili!

Hapa kuna dondoo nzuri ya kuhitimisha mjadala huu. Imechukuliwa kutoka Kamusi ya Paulo na barua zake kutoka IVP "Calvin, zaidi sana kuliko Luther, inasistiza kipengele cha uhusiano wa haki ya Mungu. Mtazamo wa Luther juu ya haki ya Mungu unaonekana kuwa dhana ya kuwa huru. Calvin anasisitiza asili ya ajabu ya mawasiliano au kutuarifu juu ya haki ya Mungu" (uk. 834).

Kwangu mimi uhusiano wa waumini na Mungu una vipengele vitatu.

1. injili ni mtu (msistizo wa Kanisa la Mashariki na Calvin)

2. injili ni ukweli (msisitizo wa Augustine na Luther)
3. injili ni maisha yaliobadilishwa (msisitizo wa Katoliki)

Yote ni sawa na yanapaswa kuungamanishwa kwa pamoja kwa ajili ya afya, sauti, Ukristo wa kibiblia. Ikiwa ye yote anasisitizwa sana au anapunguza thamani, matatizo yanatokea.

Yatupasa kumkaribisha Yesu!

Yatupasa kuiamini injili!

Yatupasa kuwa na ushawishi juu ya ufanano wa Kristo

☐ **"watashibishwa"** Kibayana "kuridhishwa," neno hili lilitumika juu ya kunenepesha mifugo kwa ajili ya kupeleka sokoni.

#### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 5:7

<sup>7</sup> Heri wenye rehema; Maana hao watapata rehema.

**5:7 "wenye rehema"** Rehema ni matokeo sio msingi wa kumjua Mungu. Ni uwezo wa kujiweka mwenyewe katika hali ya mtu mwingine na kutenda kwa huruma (kama ile Mt. 6:12,14-15; 18:21-35; Luka 6:36-38; Yakobo 2:13). Mabadiliko yanatokea hapa katika heri. Zile heri za kwanza zilizopita zimejikita katika namna ya mtu Ufalme ya hitaji la kiroho; Zinazofuata hata hivyo zinajikita katika mtazamo ambao unahamasisha matendo ya mtu. Hii iikuwa kile ambacho kilikosekana kwa mafarisayo alafu sheria sasa.

☐ **"watapata rehema"** Hii ni kauli tendwa elekezi a wakati ujao ambao kibayana inafasiriwa "watapata rehema" Maana ya njeo hii ni: (1) njeo ya wakati ujao ilitumika katika namna iliyotumika ya uhakika sasa, katika enzi hii au (2) baraka IJAYO na msamaha katika tukio Siku ya Mwisho ya Hukumu (siku za mwisho). Sauti irabu inaweza kuwa mzunguko mwingine kama "ufalme wa mbinguni," kukwepa kutumia jina la Mungu.

#### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) 5:8

<sup>8</sup> Heri wenye moyo safi; Maana hao watamwona Mungu.

**5:8 "wasafi wa moyo"** Mitazamo wetu ni wa msingi (kama vile Tito 1:15). Vipaumbele navyo kwa uzito huo huo ni muhimu (kama vile Ebr. 12:14). Kutoka Zab. 24:4 na 73:1, "safi" inaweza kumaanisha (1) nia moja, (2) inajikita, au (3) kusafishwa (kama vile Ebr.12:14). Neno hili lilitumika katika Agano la Kale kwa ajili ya ibada ya kuoshwa. Tazama mkazo upo moyoni, kituo cha utu wa mtu, sio akili au matendo ya kiibada. Kipengele cha kati cha utu ni utu katika Agano la Kale lilikuwa "moyo," wakati katika Kiyunani wazo liimaanisha "nia."

#### MADA MAALUMU: MOYO (AGANO JIPYA)

Neno la Kiyunani *kardia* limetumika katika maandiko ya kale ya Kiyunani na Agano Jipya kuashiria neno la Kiebrania *lēb* (BDB 523, KB 513). Limetumika kwa njia tofauti kadhaa (kama vile Bauer, Arndt, Gingrich na Danker, *A Greek-English Lexicon*, 2nd ed. kur. 403-404).

1. Kitovu/Kituo cha maisha ya kimwili, neno mbadala kwa mtu (kama vile. Matendo 14:17; 2 Kor. 3:2-3; Yakobo 5:5)
2. Kitovu cha maisha ya kiroho (yaani, adilifu)
  - a. Mungu anatumia moyo (kama vile. Luka 16:15; Rum. 8:27; 1 Kor. 14:25; 1 The. 2:4; Ufu. 2:23)
  - b. Imetumika kwa maisha ya kiroho ya mwanadamu (kama vile. Mt. 15:18-19; 18:35; Rum. 6:17; 1 Tim. 1:5; 2 Tim. 2:22; 1 Pet. 1:22)
3. Kitovu cha maisha ya kifikra (yaani, uwezo wa kufikiri, kama vile. Mt. 13:15; 24:48; Matendo 7:23; 16:14; 28:27; Rum. 1:21; 10:6; 16:18; 2 Kor. 4:6; Efe. 1:18; 4:18; Yakobo 1:26; 2 Pet. 1:19; Ufu. 18:7; moyo ni sawa na mawazo katika 2 Kor. 3:14-15 na Flp. 4:7)



4. kitovu cha maamuzi binafsi (yaani, matakwa, kama vile. Matendo 5:4; 11:23; 1 Kor. 4:5; 7:37; 2 Kor. 9:7)
5. Kitovu cha hisia za ndani (kama vile. Mt. 5:28; Matendo 2:26,37; 7:54; 21:13; Rum. 1:24; 2 Kor. 2:4; 7:3; Efe. 6:22; Flp. 1:7)
6. Mahali pa pekee kwa shughuli za kiroho (kama vile. Rum. 5:5; 2 Kor. 1:22; Gal. 4:6 [yaani, Kristo katika mioyo yetu, Efe. 3:17])
7. Moyo ni njia mbadala ya ki-sitiari ya kumrejerea mtu (kama vile. Mt. 22:37, kwa kunukuu Kumb. 6:5). Mawazo, sababu, na matendo vikichangia kikamilifu kwenye moyo kubainisha kikamilifu mtu alivyo. Agano la Kale lina baadhi ya matumizi ya maneno ya kushangaza.
  - a. Mwa. 6:6; 8:21, "Mungu alihuzunishwa katika moyo," pia tazama Hosea 11:8-9
  - b. Kumb. 4:29; 6:5; 10:12, "kwa moyo wako wote na nafsi yako yote"
  - c. Kumb. 10:16; Yer. 9:26, "Roho zisizo na tohara" na Rum. 2:29
  - d. Ezek. 18:31-32, "moyo mpya"
  - e. Ezek. 36:26, "moyo mpya" dhidi ya "moyo wa jiwe" (kama vile Ezek. 11:19; Zak. 7:12)

☑ **"watumwona Mungu"** Kwa walio safi wa moyo Mungu anaweza kuonekana katika uumbaji wote na katika kila hali. Usafi unafungua macho ya rohani. Katika Agano la Kale kumuona Mungu kulimaanisha kufa (kama vile Mwa. 16:13; 32:30; Kut. 20:19; 33:20; Waamuzi. 6:22, 23; 13:22; Isa. 6:5). Kauli hii hivyo yawezekana inarejerea mazingira ya matukio ya siku za mwisho.

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 5:9**

<sup>9</sup> Heri wapatanishi; Maana hao wataitwa wana wa Mungu.

**5:9 "wapatanishi"** Hili neno ambatani linatokea tu hapa. Linarejerea upatanisho kati ya Mungu na mwanadamu ambacho kinapelekea amani kati ya watu. Hata hivyo hii sio amani kwa gharama yoyote lakini amani kupitia toba na imana (kama vile Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21; Rum. 5:1). Mungu hajabadilika, mwanadamu ndiye kabadilika (yaani Mwanzo 3; Rum. 3:9-19; Gal. 3:22), lakini katika Kristo nia ya asili imerejeshwa.

#### **MADA MAALUM: AMANI NA VITA**

##### I. Utangulizi

- A. Biblia, chanzo chetu pekee cha imani na matendo, hakina ibara za kutosha kuhusiana na amani (tazama Mada Maalum: Amani [Agano la Kale] na Mada Maalum: Amani [Agano Jipya]). Kwa uhalisia, hili ni fumbo katika uwasilishaji wake. Agano la Kale linaweza kudokezwa kama mtazamo wa amani wenye kumaanisha kutokuwepo kwa vita. Agano Jipya, hata hivyo, linaweka mgogoro katika maneno ya kiroho ya ndani ya nuru na giza (yaani., Efe. 2:2; 6:10-17).
- B. Imani ya kibiblia, pamoja na dini za ulimwengu wa wakati uliopita na uliopo, zihitajikazo na bado zinategemewa, kipindi cha usawa wa mali ambapo hapakuwa na vita.
  1. Isaya 2:2-4; 11:6-9; 32:15-18; 51:3; Hosea 2:18; Mika 4:3
  2. Nabii za imani ya kibiblia za mwakilishi binafsi wa Masihi, Isa. 9:6-7
- C. Hata hivyo, ni kwa namna gani tunaishi katika ulimwengu wa sasa wenye migogoro? Kumekuwa na mitikio kadhaa ya Kikristo iliyokuzwa kwa mtiririko kati ya kifo cha Mitume na Zama za Kati.
  1. Upinzani vita – ingawa hii ni adimu katika nyakati za kale, huu ulikuwa mwitikio wa kanisa la mwanzo kwa jamii ya jeshi la Kirumi.
  2. Vita ya Haki – baada ya mabadiliko ya Constantine (313 B.K) kanisa lilianza kupata fikra mpya juu ya kuungwa mkono kwa jeshi la "serikali ya Kikristo" katika mwitikio wa mafanikio ya uvamizi wa Barbaria. Kimsingi hii ilikuwa nafasi ya kisasa ya Kiyunani. Nafasi hii kwa mara ya

kwanza ilitamkwa na Ambrose na kufanyiwa upanuzi na kukuzwa na Augustine.

3. Vita vya Kidini – hii ni sawa na dhana ya Vita Takatifu ya Agano la Kale. Hii ilishamiri katika Zama za Kati katika mwitikio wa mwndelegeo wa Uislamu katika "Nchi Takatifu" na tawala za kale za Kikristo kama vile Afrika ya Kaskazini, Asia Ndogo, na Dora ya Kirumi ya Mashariki. Hii haiku fanywa kwa mbadala wa utawala, bali kwa mbadala wa Kanisa na chini ya ufadhili.
4. Hii mitazamo yote mitatu iliendelezwa katika muktadha wa Kikristo kwa kutofautiana kimawazo juu ya namna Wakristo wanavyopaswa kuhusiana na mfumo wa ulimwengu ulioanguka. Kila mmoja ulisisitiza maandiko fulani ya Biblia katika utengefu wa wengine. Upinzani vita ulikuwa na mwelekeo wa kujitenga wenyewe na ulimwengu. Huu mwitikio wa "Vita ya Haki" umeiunga mkono nguvu ya utawala ili kuuendesha ulimwengu wa uovu (Martin Luther). Nafasi ya Vita vya Kidini imedia kwamba Kanisa limeushambulia mfumo wa ulimwengu ulioanguka ili kuutawala.
5. Roland H. Bainton, katika kitabu chake, *Christian Attitudes Toward War and Peace, published by Abingdon*, ukurasa 15, anasema "Huu Uundaji Mpya umehimiza vita vya kidini, ambapo nafasi tatu za kihistoria zimeonekana tena: hii vita ya haki miongoni mwa Walutherani na Waanglikana, vita ya kididi katika Makanisa Yaliyoundwa Upya, na upinzanivita miongoni mwa Wanabaptisti na baadaye Kundi la Wanachama wa jamii ya Kikristo. Karne ya kumi na nane katika dhana na katika tendo lililochochea misingi ya ufuasi wa amani ya kibinadamu ya Kuzaliwa Upya. Karne ya kumi na tisa kilikuwa kipindi cha ushirika wa amani na mwamko mkubwa wa kuitokomeza vita. Katika karne ya ishirini kumi na nane kulionekana kuwa na vita ya ulimwengu ya aina mbili. Katika kipindi hiki tena, zile nafasi tatu za kihistoria zilikuwa zimejitokeza tena. Makanisa yaliyoko Marekani kwa upekee yalibeba mtazamo wa vita ya kidini kuihusu Vita ya Kwanza ya Dunia; upinzani vita ulienea kati ya vita ya aina mbili; hali ya Vita ya Pili ya Dunia iliyokadiriwa kuwa kama vita ya haki."

D. Ufafanuzi halisi wa neno "amani" umetiliwa mashaka.

1. Kwa Wayunani hili linaonekana kuirejelea jamii ya utulivu na umoja.
2. Kwa Warumi hili lilikuwa tendo la kutokuwepo migogoro iletwa na nguvu ya utawala.
3. Kwa Waebrania amani ilikuwa neema ya YHWH iliyojikita katika mwitikio sahihi wa mwitikio kwake. Mara nyingi linawekwa katika maneno ya kilimo (kama vile Mambo ya Walawi 26; Kumbukumbu la Torati 27-28). Si mafanikio tu, bali usalama na ulinzi wa Kiungu unahusishwa.

II. Nyenzo za Kibiblia

A. Agano la Kale

1. Vita Takatifu ni dhana ya msingi ya Agano la Kale. Hiki kifungu "usiu" cha Kut. 20:13 na Kumb. 5:17 kilicho katika Waebrania kinarejelea mauaji ya kukusudia (BDB 953; tazama Mada Maalum: Mauaji), si kifo kitokanacho na ajali au hamaki au vita. Hata YHWH naonekana kama shujaa kwa niaba ya watu wake (kama vile Yoshua, Waamuzi na Isa. 59:17, kama ilivodokezwa katika Efe. 6:14).
2. Mungu anatumia vita kama njia ya kuadibisha watu wake walizikiuka njia zake – Ashuru inaipeleka Israeli uhamishoni (722 B.K); Babeli ya Sasa inaipeleka uhamishoni Yuda (586 k.k.).
3. Inatishisha, katika mazingira haya ya kijeshi, kukisoma kifungu "mtumishi ateswaye" cha Isaya 53, ambacho kinaweza kuainishwa kama vita pinzani ya kiukombozi.

B. Agano Jiya

1. Katika Injili askari wanatajwa pasipo malalamiko. Wale "maakida" wa Kirumi mara nyingi wanatajwa na kwa namna fulani mara kadhaa katika maana ya kundi tawala.
2. Hata askari walioamini hawakuamrisha kuziacha kazi zao (kanisa la mwanzo).

3. Agano Jipya halidai majibu ya undani kwa uovu wa kijamii katika maana ya dhana ya kisiasa au tendo, bali katika ukombozi wa kiroho. Tazamio haliko katika mapambano ya kimwili, bali li juu ya mapambano ya kiroho kati ya nuru na mwanga, jema na uovu, upendo na chuki, Mungu na Shetani (Efe. 6:10-17).
4. Amani ni mtazamo wa moyo katikati ya matatizo ya ulimwengu. Hii inahusiana tu na uhusiano wetu na Kristo (Rom. 5:1; Yohana 14:27), si utawala. Waleta amani wa Mt. 5:9 ni wa kisiasa, lakini ni wahubiri wa injili! Ushirika, si migongano, ipasayo kuyabainisha maisha ya Kanisa, vyote kwa hii na kwa ulimwengu uliopotea.

☛ **"wana wa Mungu"** Katika Agano la Kale tungo hii siku zote inarejerea kwa malaika. Ni nahau ya Kiebrania ikiakisi tabia ya Mungu. Lengo la Ukristo ni kufanana na Kristo (kama vile Rum. 8:28-29; Gal. 4:19), ambayo ni urejesho wa taswira ya Mungu kwa mawanadamu iliyopotea katika Aguko la Mwanzo 3. Angalia Mada Maalum katika Mt. 27:54.

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 5:10**

<sup>10</sup> Heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki; Maana ufalme wa mbinguni ni wao.

**5:10 "wenye kuudhiwa"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati timilifu. Inazungumzia kwa wale waliokuwa na wanaendelea kuteseka na msababish wa nje (yaani shetani, mapepo na wasioamini). Mateso ya waaminio ni ukweli uwezekanao na hat ukweli unaotegemewa kwa ajili ya watu wa Mungu katika ulimwengu ulioanguka (kama vile Mdo. 14:22; Rum. 5:3-4; 8:17; Flp. 1:29; 1 Thes. 3:3; 2 Tim. 3:12; Yakobo 1:2-4; 1 Pet.3:14; 4:12-19; Ufu. 11:7; 13:7). Tazama mateso yanayotokea ni kwasababu ya mtindo wa maisha wa kumcha Mungu na ushuhuda wa waaminio. Mungu analitumia kuwafanya waaminio wawe kama Kristo (kama vile Ebr. 5:8). Mstari huu ni uwiano unaoitajika kwa Mmarekani wa kisasa (afya, mali na mafanikio, angalia Gordon Fee, *The Disease of the Health Wealth Gospel*) msisitizo uliopitiliza juu ya ahadi za kiagano za Kumbu kumbu la Torati 27-29 zikitukimika moja kwa moja (yaani kupuuzia laana kwa ajili ya kutotii) kwa waaminio wote. Afya, mali na ahadi za mafanikio lazima ziwianishwe kwa kurudia kutambua kwa waaminio watesekao kwasababu ni watu wa imani katika ulimwengu usio na usiomcha Mungu na ulioanguka. Yesu aliteseka, Mitume walieseka na wakristo wa kwanza waliteseka, hivyo pia waamini wa kila kizazi! Pamoja na ukweli huu katika ufahamu pia kuna uwezekano kwamba kanisa litapita katika kipindi cha dhiki (hakuna kutwaliwa kwa siri)!

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 5:11-12**

<sup>11</sup> Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu. <sup>12</sup> Furahini, na kushangilia; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu.

**5:11-12** Aya mpya inatakiwa ianze na Mt. 5:11 (kama vile NRSV & TEV). Viwakilishi katika mistari hii inabadilika kutoka nafsi ya utatu kwenda ya pili. Luka 6:22-23 ina kifungu cha maneno chenye nguvu zaidi.

**5:11 "kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya"** Hizi zote mbii ni kauli za wakati uliopita usiotimilifu tegemezi ambazo zinaashiria kupelekea muundo wa daraja la tatu lenye masharti (kama vile Rum. 5:3-5; Yakobo 1:2-4; 1 Pet. 4:12-19). Mateso yanaweza kuwa ya kawaida lakini hayatarajiwi wala kutafutwa (kama walivyofanya mababa wengi wa kanisa la kwanza). Katika Agano la Kale matatizo na mateso yalikuwa mara kwa mara yakifasiriwa kama ishara ya Mungu ya kutopendezwa na dhambi (kama vile Ayubu, Zab. 73, na Habakuki vinajishughulisha na somo). Wenye haki wanapata mateso. Lakini Yesu alienda hatua moja zaidi. Wale waishio na kushuhudia kwa ajili yake watapitia mateso ya kukataliwa kutoka katika ulimwengu ulioanguka kama alivyofanya (kama Yohana. 15:20; Mdo. 14:22; 2 Tim. 3:12).

**NASB, NKJV**

<b>NRSV</b>	<b>"na kwa uongo wakisema kila aina ya ubaya dhidi yako"</b>
<b>TEV</b>	<b>"na kusema kila uongo na aina ya uovu dhidi yako "</b>
<b>NJB</b>	<b>"na kuzungumza aina zote za ubaya dhidi yako"</b>

Kuna baadhi ya mashaka ya kimaandiko juu ya wakati uliopo endelevu "kwa uongo." Yanakosekana katika maandiko ya kimagharibi D, the Diatesseron, na maandiko ya Kiyunani yatumikayo na Origen, Tertullian, na Eusebius. Inajumuishwa katika maandiko ya kale ya Kiyunani,  $\alpha$ , B, C, W, na Vulgate na Fasiri za Kikoptiki. Inaaksi hali ya kihistoria ya kanisa la kwanza. Wakristo wa kwanza walishitakiwa kwa uchochezi, ulaji wa nyama ma kutomwabudu Mungu. Mashitaka yote haya yalikuwa yakihusiana na kutoeleweka juu ya maneno ya Wakristo na matendo ya ibada (kama vile 1 Pet. 2:12,15; 3:16). Toleo la UBS<sup>4</sup> linatoa ujumuishi wake alama ya C (ngumu katika kuamua).

☐ **"kwa ajili yangu"** Hii inaunganishwa na Mt. 5:10. Mateso yaliyoandaliwa kibayana yanahusiana na kuwa mfuasi mtendaji wa Kristo (kama vile 1 Pet. 4:12-16).

**5:12 "furahini"** Hizi mbili ni kauli shurutishi za wakati uliopo (kama vile Mdo. 5:41; 16:25). Kufurahia kunatokana na kule kuhesabiwa kustahili kuteseka kwa/pamoja na Kristo na kutunukiwa (kama vile Rum. 8:17). Kuwa mwangalifu juu ya kujihurumia. Hakuna kitu "kinachojikuta kimetokea tu" kwa wana wa Mungu (kama vile Rum. 5:2-5; Yakobo 1:2-4, Angalia Hannah Whithall Smith's *The Christian's Secret of a Happy Life*). Mteso yana kusudi katika mpango wa Mungu.

☐ **"kwa kuwa thawabu yenu mbinguni ni kubwa"** Angalia Mada Maalum inayofuata.

### **MADA MAALUMU: VIWANGO VYA THAWABU NA ADHABU**

- A. Mwitikio unaofaa na usiofaa kwa Mungu umeegemea juu ya kiwango cha maarifa ya mtu. Kiwango kidogo cha maarifa alichu nacho mtu, ndio mwitikio mdogo alionao mtu. Pia kinyume chake ni kweli (yaani. Luka 12:45).
- B. Maarifa ya Mungu huja katika njia mbili za msingi
  1. uumbaji (yaani Zaburi 19; Warumi 1-2)
  2. Andiko (yaani Zaburi 19; 119; Yesu, kama alivyofunuliwa katika Agano la Kale)
- C. Ushahidi wa Agano la Kale
  1. thawabu
    - a. Mwa. 15:1 (mara nyingi hii inahusiana na thawabu ya kidunia, pamoja na wana)
    - b. Law. 26:1-13; Kumb. 28:1-14,58-68 (utii wa agano huleta baraka)
    - c. Dan. 12:3
  2. adhabu – Law. 26:14-39; Kumb. 27:15-26; 28:15-37 (kutolitii agano huleta ulaanifu)
 

Mpangilio wa Agano la Kale wa thawabu kwa mtu, haki ya kimaagano imerekebishwa kwa sababu ya dhambi mwanadamu. Marekebisho haya yanaonekana katika Yakobo na Zaburi 73 (yaani, "njia mbili," yaani Kumb. 30:15,19; Zaburi 1). Agano Jipya linachochea mitazamo kutoka katokana na tendola fikra (kama vile ile Hotuba ya huko Mlimani, Mathayo 5-7).
- D. Ushahidi wa Agano Jipya
  1. thawabu (nyuma ya wokovu)
    - a. Marko 9:41
    - b. Mt. 5:12,46; 6:1-4,5-6,6-18; 10:41-42; 16:27; 25:14-23
    - c. Luka 6:23,35; 19:11-19,25-26
  2. adhabu
    - a. Marko 12:38-40
    - b. Luka 10:12; 12:47-48; 19:20-24; 20:47
    - c. Mathayo 5:22,29,30; 7:19; 10:15,28; 11:22-24; 13:49-50; 18:6; 25:14-30

d. Yakobo 3:1

E. Kwangu mimi ufanano huu wa kipekee ambao anaunda maana inatoka katikajumba la maonesho ya burudani. Mimi sishughuliki uwasilishaji hivyo huo siuelewi. Kadri nilivyo ufahamu ugumu huu na utata wa mtiririko huu, muziki, na dansi, Kadri ambavyo ningeweza kuukubali utendaji. Naamini kuwa mbingu itavijaza vikombe vyetu, lakini naamini huduma zetu za kidunia zitabainisha saizi ya kikombe.

Kwa hiyo, maarifa na mwitikio wa maarifa hayo huleta matokeo ya thawabu na adhabu (yaani Mt. 16:7; Luka 12:48; 1 Kor. 3:8,14; 9:17,18; Gal. 6:7; 2 Tim. 4:14). Kuna kanuni ya kiroho—tunavuna kile tulichokopanda! Wengine hupanda vingi na kuvuna vingi (kama vile Mt. 13:8,23).

F. "Lile taji la haki" ni letu katika kazi ya Kristo iliyomalizika (kama vile 2 Tim. 4:8), lakini tambua kwamba "taji la uzima" inahusiana na uvumilivu katika majaribu (yaani Yakobo 1:12; Ufu. 2:10; 3:10-11). Lile "taji la utukufu" kwa viongozi wa ki-Kristo linahusiana na namna walivyoyaishi maisha yao (kama vile 1 Pet. 5:1-4). Paulo alifahamu kuwa ana taji isiyoharibika, lina lakini zoezi la ziada la kujitawala mweyewe (kama vile 1 Kor. 9:24-27).

Siri ya maisha ya Mkristo ni kwamba ni ya huru kweli kweli katika kazi ya Kristo iliyomalizika, lakini yatupasa kuiitikia neema ya bure katika Kristo, pia yatupasa kuitikia nguvu ya Mungu kwa maisha ya Kristo. Maisha ya Mkristo ya kimiujiza kama ulivyo wokovu, bado yatupasa kuupokea na kuutunza. Ni wa bure lakini uliogharamikia fumbo la kila kitu na pia ni siri ya thawabu na upandaji/ uvunaji.

Hatuokolewi na kazi njema, bali kwa kazi njema (yaani Efe. 2:8-10). Kazi njema ni ushahidi wa kwama tumekutana naye (yani Mathayo 7). Manufaa ya mwanadamu katika eneo la wokovu huelekea katika uharibifu, bali maisha ya Uungu yana thawabu.

☐ **"manabii"** Hii ilikuwa ni rejea iliyofunikwa kwa Uungu Ukristo. Kama Manabii wa Agano la Kale walivyoteseka kwasababu ya mahusiano yao na huduma zao kwa YHWH, hivyo pia Mkristo watateseka kwasababu ya uhusiano wake na huduma yake kwa Kristo.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 5:13**

<sup>13</sup> Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini chumvi ikiwa imeharibika itatiwa nini hata ikolee? Haifai tena kabisa, ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu.

**5:13 "Ninyi ni chumvi ya dunia"** Kwasababu ya uthamani sana wa chumvi katika ulimwengu wa kale (1) kwa ajili ya uponyaji na utakasaji; (2) kwa ajili ya utunzaji wa chakula; (3) kwa ajili ya kuweka ladha kwenye chakula; na (4) kwa ajili ya kutunza unyevu kwa binadamu katika kila majira ya ukame. Mara kwa mara ilitumika kuipa wanajeshi kama mishahara. Wakristo wanaitwa "chumvi ya ulimwengu" kwasababu ya nguvu yao ipenyayo na uwezo wa kutunza ndani ya ulimwengu uliopotea. "Ninyi" ni wingi na yenye huruma kama Mt. 5:14. Waaminio ni chumvi (kama vile Marko 9:50). Sio jambo la kuchagua. Uchaguzi pekee ni kuwa aina gani ya chumvi wataamua kuwa. Chumvi ikaharibiwa na kuwa haifai (kama vile Luka 14:34-35). Watu waliopotea wanatazama.

☐ **"chumvi ikiwa imeharibika"** Hii ni sentensi ya daraja la tatu lenye masharti ambayo inamaanisha kitendo kinachoweza kufanyika. Kibayana Chumvi haiwezi kupoteza nguvu yake mpaka inapochanganya na uchafu chumvi hufufia na hivyo kile kilichomo kwenye chumvi kinapotea. Wakristo wanaweza kupoteza na au kuharibu shuhuda zao! Neno "kukosa ladha" kawaida lilitumika katika namna ya "wapumbavu" (kama vile Rum. 1:27; 1 Kor. 1:20).

☐ **"Haifai tena kabisa, ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu"** Chumvi ambayo ilikuwa haitumiki kama kihifadhio au kitia ladha hakika ilikuwa haifai. Ilitupwa katika njia au juu ya paa kutengeneza sehemu ya juu ngumu ya bahari. Chumvi iliyochukuliwa kutoka Bahari ya Chumvi ilikuwa na uchafu mwingi. Watu katika sehemu hii ya ulimwengu walikuwa wakizoelea chumvi isiyotumika.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 5:14-16**

<sup>14</sup> Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima. <sup>15</sup> Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani. <sup>16</sup> Vivyo hivyo nuru

**yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.**

**5:14 "Ninyi ni nuru ya ulimwengu"** Nuru siku zote imekuwa sitiari ya kibiblia kwa ajili ya ukweli na uponyaji. Ilitumika na Yesu kumuelezea mwenyewe (kama vile Yohana 9:5). Swali sio, "Je mtakuwa nuru ya ulimwengu?" Kama mwamini, ninyi ni nuru ya ulimwengu (kama vile Flp. 2:15). Swali pekee ni hili, "Ni aina gani ya nuru unataka kuwa?" Vile watu wanavyojua kuhusu Mungu, wanajua kutoka kwako na maisha yako! "Ninyi" ni wingi na yenye hisia za huruma Mt. 5:13.

☐**"mji"** Hii ni rejea ya jumla aidha kwa (1) mahali pa mji katika utazamio wa uwanda (2) rangi yake ya chaki nyeupe ilig'aa wakati wa jua. Wale wanaojaribu kuweka uhusiano wa hili na matukio ya siku za mwisho wa Yerusalemu ni magumu kuyaelezea kukosekana kwa kibainishi cha wazi. Miji kama nuru haikutengeza au kukusudiwa kufichwa.

**5:15**

**NASB, NKJV** "kikapu"

**NRSV** "kiango"

**TEV** "kiango"

**NJB** "kiango"

Hii inarejerewa kama bakuli litumikalo kupimia ngano.

☐**"kiango"** Kulikuwa na kutokeza kidogo wa sehemu ndogo kutoka katika ukuta katika nyumba za kale za wapalestina ambazo taa na ndogo za mafuta ziliwekwa ili kuweza kutoa mwanga kwenye chumba chote (kama vile Marko 4:21-22; Luka 8:16-17).

**5:16** Mitindo ya maisha ya waaminio lazima ilete utukufu na heshima kwa Mungu (yaani, "wana wa Mungu" katika Mt. 5:9, kama vile Efe. 1:4; 2:8-10). Inawezekana nia ya mstari huu unahusiana na kutojumuishwa na kujitenga kwa makundi kama Waesene. Waamini lazima wakae katika hali ya kujihusisha na kushughulikia jamii zenye uovu lakini wasiwe sehemu yake (kama ile Yohana. 17:15-18).

☐**"Baba"** Mkao wa kawaida kwa maombi ya Kiyahudi ilikuwa ni kusimama macho yakiwa yamefunguka huku kichwa na mikono ikiwa imeinuliwa juu. Waliomba kama vile wako katika mazungumzo na Mungu. Matumizi ya Yesu ya jina la Baba kumuelezea YHWH ni moja ya kipengele che upekee wa mafundisho Yake. Mathayo anaandika juu ya matumizi ya jina hili kwa ajili ya Mungu mara arobaini.

## **MADA MAALUMU: BABA**

Agano la Kale linaanzisha neno mbadala la ndani la Mungu kama Baba. (tazama Mada Maalum: Ubaba wa Mungu):

1. Taifa la Israeli daima linaelezwa kama "mwana" wa YHWH (kama vile Hos. 11:1; Mal. 3:17)
2. Hata mwanzoni kabisa mwa kitabu cha Kumbukumbu la torati mfanano wa Mungu kama Baba umetumika (1:31)
3. Katika kumbukumbu la torati 32 Israeli inaitwa "Mwana wake" na Mungu anaitwa "Baba yako"
4. Ufananisho huu unatajwa katika Zab. 103:13 na kuendelea katika Zab. 68:5 (baba wa yatima)
5. Lilikuwa la kawaida katika manabii (kama vile Isa. 1:2; 63:8; Israeli kama mwana, Mungu kama Baba, 63:16; 64:8; Yer. 3:4, 19; 31:9).

Yesu alizungumza Kiaramu, ikimaanisha kuwa kuna sehemu nyingi ambapo "Baba" anaonekana, ni *Pater* yule wa Kiyunani, na linaweza kuwa linaakisi neno *Abba* la Kiaramu (kama vile. Marko 14:36). Neno hili la kawaida "Baba" au "Papa" linaonyesha ukaribu uliopo wa Yesu na Baba. Udhahilisho wake huu kwa wafuasi wake pia

kunahamasisha ukaribu wetu na Baba. Neno "Baba" lilitumika kidogo sana katika Agano la Kale kwa YHWH, lakini Yesu analitumia daima na kwa kulieneza. Ni uthibitisho mkubwa wa uhusiano mpya wa Waamini na Mungu kupitia kwa Kristo (kama vile Mathayo 6:9)

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. kauli hizi zimeelekezwa kwa nani?
2. Je kuna mtu anaweza kufikia viwango hivi?
3. Kwa nini Mathayo na Luka wanaandika juu ya mahubiri ya aina moja kwa aina tofauti?
4. Kwanini kauli hizi zinakinzana?
5. Je ni kwa namna gani heri zina husiana zenyewe kwa zenyewe?
6. Nini kusudi la Mahubiri ya Mlimani?
7. Andika ukweli mkuu wa kila aya kwa maneno yako mwenyewe alafu uyaweke kwa muhtasari yote.

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA MISTARI YA 5:17-48

- A. Ili kuweza kuelewa 5:17-20 mtu lazima atambue kwamba Yesu alikataliwa na desturi za kina za desturi za Kiyahudi (Talmud) ambazo zilijaribu kufasiri Agano la Kale lililoandikwa. Yesu alikuza Agano la Kale katika nguvu na maelezo yaliyo dhahiri (yaani, 5:17-19), alafu alijionesha mwenyewe kuwa mtimilizaji wake wa kweli na mfasiri wake wa mwisho (yaani, 5:21-48). Hii inaweza kuonekana katika ukweli kwamba Yesu alitumia tungo "mmesikia" sio "imeandikwa." Hii ni kifungu cha habari cha elimu ya Kristo chenye nguvu katika ufahamu wa heshima ya wayahudi kwa sheria iliyoandikwa na sheria ya kinywa.
- B. Sehemu hii haitoi kila kitu juu ya makosa ya ufasiri Dini ya Kiyahudi ya karne ya kwanza bali kiwakilishi. Mahubiri yote, Mathayo 5-7, ni matazamo wa kuweza kutambua waaminio wapole na wauwaji wa wa majivuno kwa wasomi wa sheria wajihebiao haki. Yesu aliweka ufahamu pamoja na mikono kama chanzo cha dhambi na uasi dhidi ya sheria ya Mungu. Alizungumzia mtu wa ndani na pia yule wa nje. Dhambi huanzia katika maisha ya wazo.
- C. Namna ya viwango vya Mungu vya hukumu inavyotofautiana na vya mwanadamu (kama vile Isa. 55:8-9). Haki ya mwamini ni vyote ni karama ya kuanzia na kukuza kufanana na Kristo vyote kisheria, nafasi ya kisheria na utakaso endelevu unaoongozwa na Roho. Sehemu hii itajikita katika kilichosemwa mwishoni.
- D. Ikiwa mistari hii ingezungumzwa katika muktadha wa kihistoria wa Ukristo wa kisasa wenye msimamo, sote tungekuwa tunashangazwa na namna gani Mungu anatazama udini wetu+!

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 5:17-19

<sup>17</sup> Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza. <sup>18</sup> Kwa maana, amin, nawaambia ,Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka,yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka ,hata yote yatimie. <sup>19</sup> Basi mtu ye yote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; bali mtu atakayezitenda na kuzifundisha, huyo

**5:17 "Msidhani"** Hii ni kauli tendaji kanushi ya wakati uliopita usiotimilifu tegemezi ambayo ilikuwa tungo ya kisarufi iliyomaanisha "hata msianze!"

☑ **"nalikuja kuitangua torati"** Muktadha wa Mt. 5:17-20 ni kauli ya kukiri uvuvio na umilele wa Agano la Kale. Yesu alitenda kazi kama mtoa sheria mpya, kama Musa wa pili. Yesu mwenyewe alikuwa utimizwaji wa Agano la Kale. Agano Jipya ni mtu sio jozi za sheria zinazohitajika. Maagano mawili kimsimamo ni tofauti sio katika kusudi bali katika namna ya kutimiliza kusudi hilo. Msukumo hapa haupo katika kukosa uwezo kwa Agano la Kale kumfanya mwanadamu atembea sawa na Mungu kama katika Wagalatia 3, hasa katika fasiri ya mwalimu isiyokamili na isiyosahihi ya maandiko ya kibiblia kwa namna ya mbinu za Kisokratiki na ki-lahaja. Yesu kwa kuangalia hili alitambua upeo wa sheria kutoka katika matendo yasiyosawa kwenda katika fikra za kiakili. Hii inaangalia ugumu wa haki ya kweli kupitia Agano Jipya kwa kiwango kwa kutowezekanika kabisa (kama vile Gal. 3:10,21-22). Kutowezekanika huku kutakutana na Kristo mwenyewe na kurudishwa kwa jamii ya imani yenye toba kupitia kukatwa kwa haki au kuhesaniwa kwa imani (kama vile Rum. 4:6; 10:4). Maisha ya mwanadamu ya kidini ni matokeo ya mahusiano na Mungu na sio namna ya kuelekea kwenye hayo mahusiano.

☑ **"torati au manabii"** Hii ilikuwa nahau inayorejerea mgawanyiko wa mbili ya tatu ya Kanoni ya Kiebrania: Sheria, Manabii na Maandiko. Ilikuwa ni njia ya kuelezea Agano lote la Kale. Pia ilionesha kwamba uelewa wa Yesu wa maandiko ulikuwa karibu na thiolojia ya Mafarisayo kuliko Masadukayo (Mwanzo-Kumbukumbu la Torati) kama mwenye mamlaka.

**NASB, NKJV**

**NRSV**

**"lakini kutimiliza"**

**TEV**

**"bali kufanya mafundisho yao kuwa kweli"**

**NJB**

**"kukamilisha"**

Hili lilikuwa ni neno lililozoeleka (*pleroō*) ambalo lilitumika katika namna kadhaa. Katika muktadha huu ilimaanisha kutimilizika au kuja kwenye ukamilifu ulioelezwa (kama vile. Rum. 10:4). Agano la Musa limetimilizwa kupitiliza kwa Agano Jipya. Hii ni kweli kuu ya kitabu cha Waebrania na Wagalatia 3!

**5:18 "hakika"** Hii ni kibayana "Amina." Angalia Mada Maalum hapa chini.

## **MADA MAALUMU: AMINA**

### **I. AGANO LA KALE**

A. Neno "Amina" linatoka kwenye neno la Kiebrania lenye maana ya

1. "ukweli" (emun, emunah, BDB53)
2. "Uaminifu" (emun, emunah, BDB 53)
3. "imani" au "uaminifu"
4. "amini" (dmn, BDB 52)

B. Asili yake ya neno inadokeza mkao wa mwili wa mtu ulivyo imara. Kinyume cha hili kinaonyesha mwili wa mtu Yule asio imara, unaotereza (kama vile. Zab. 35:6; 40:2; 73:18; Yereemia 23:12) au kizuizi (kama vile. Zab. 73:2). Kutokana na utumiaji huu wa fasihi unatengeneza upanuzi wa kiisitiari wa imani, uaminifu, utiifu na wa kutegemewa (kama vile. Hab. 2:4)

C. Utumiaji maalumu (angalia mada maalumu: kuamini, amini, imani na uaminifu katika agano la kale)

1. Nguzo, 2 Fal. 18:16 (1 Tim. 3:15)
2. Kuthibitika, Kut 17:12
3. Uimalifu, Kut. 17:12
4. Uthabiti, Isa. 33:6



5. Ukweli, 1 Fal. 10:6; 17:24; 22:16; Mith. 12:22
6. Thabiti, 2 Nya. 20:20; Isa. 7:9
7. Stahili (sheria alizopewa Musa), Zab. 119:43,142,151,160

D. Katika Agano la Kale maneno mawili ya Kiebrania yanatumika kwa ajili ya imani thabiti

1. Bathach(BDB 105), imani
2. Yra (BDB 431), hofu, heshima, abudu (kama vile. Mwa. 22:12)

E. Kwa maana ya kuamini au uaminifu ulioanzishwa kwa matumizi ya liturujia ambao ulitumika kuthibitisha maelezo ya kweli ya mtu mwingine (kama vile. Hes. 5:22; Kumb. 27:15-26; 1 Fal. 1:36; 1 Nya. 16:36; Neh. 5:13; 8:6; Zab. 41:13; 72:19; 89:52; 106:48; Yer. 11:5; 28:6).

F. Kiongozi cha kithiolojia kwenye neno hili sio uaminifu wa mwanadamu, bali ni wa Mungu mwenyewe (kama vile Kut. 34:6; Kumb. 32:4; Zab. 108:4; 115:1; 117:2; 138:2). Tumaini la mwanadamu aliyeanguka ni neema, uaminifu, kutii Agano la Mungu na ahadi zake. Wale wanaomfahamu Mungu wanahitajika kufanana naye (kama vile. Hab. 2:4). Biblia ni historian na kumbu kumbu ya Mungu kurejesha taswira yake (kama vile. Mwa. 1:26-27) kwa mwanadamu. Wokovu unarejesha uwezo wa mwanadamu kuwa na ushirika wa ndani na Mungu. Hii ndio sababu ya kuumbwa kwetu.

## II. AGANO JIPYA

- A. Utumiaji wa neno "amina" kama hitimisho la kiliturujia kwa minajili ya kuthibitisha ukweli wa maelezo/taarifa ni la kawaida katika Agano Jipya (kama vile. 1 Kor. 14:16; Ufu. 1:7; 5:14; 7:12).
- B. Utumiaji wa neno kama kifungio cha maombi ni wa kawaida kwenye Agano Jipya (kama vile. Rum. 1:25; 9:5; 11:36; 16:27; Gal. 1:5; 6:18; Efe. 3:21; Flp. 4:20; 2 Thes. 3:18; 1 Tim. 1:17; 6:16; 2 Tim. 4:18).
- C. Yesu ndiye yeye aliyelitumia hili neno (limezidishwa mara 25 katika Yohana, yaani., Yohana 1:51; 3:3,5,11; n.k.) kuyatambulisha maelezo muhimu (kama vile. Luka 4:24; 12:37; 18:17,29; 21:32; 23:43).
- D. Linatumika kama cheo kwa Yesu katika Ufu 3:14 ( pia angalia 2 Kor 1:20, yamkini jina la heshima la Mungu kutoka Isa. 65:16)
- E. Dhana ya kusadiki au sadiki, au kuamini au amini inaelezewa katika neno la Kiyunani *pistos* au *pistis*, ambalo linatafasiliwa katika Kiingereza kama "imani", "sadiki", "kuamini" (angalia mada maalumu: Sadiki, Kuamini au Imani).

☐"mbingu na nchi" Katika Agano la Kale namna hizi mbili zilitumika kama mbili zinazotakiwa kuwa shuhuda kuthibitisha kauli za YHWH (kama vile Hes. 35:30; Kumb. 17:6; 19:15). Ni vipengele vya ulimwengu wetu kwamba utabaki kadiri zama hizi zinabaki. Kauli hii iko kama kiapo kutoka kwa YHWH.

<b>NASB</b>	<b>"hata herufi moja au nukta"</b>
<b>NKJV</b>	<b>"nukta moja au jina moja"</b>
<b>NRSV</b>	<b>"sio herufi moja, wala nukta moja ya herufi"</b>
<b>TEV</b>	<b>"sio herufi, wala nukta"</b>
<b>NJB</b>	<b>"sio nukta moja,wala herufi ndogo"</b>

Hii inarejerea kwa

1. herufi ndogo ya herufi za kiebrania, *yodh*, ilikuwa na ufanano katika herufi ndogo katika herufi za Kiyunani, *iota*
2. Nyongeza ya upendezeshaji ili kuumba maandiko ya Kiebrania, sawasawa na kuandika kwa kupitiliza kidogo katika mashine za kuandika zinazotumika kutambua ukweli za kisasa
3. herufi ndogo ambayo inatofautisha kati ya hizi mbili zinazofanana herufi za Kiebrania

Suala ni kwamba Agano La Kale katika sehemu zake zote; hata sehemuzake zingine zote ziznazoonekana kama zisizo na msingi. Bado Agano la Kale kwa ukamilifu lilitimilizwa ndani ya mtu, kazi na mafundisho ya Kristo.

<b>NASB</b>	<b>"ya torati haitaondoka ,hata yote yatimie"</b>
<b>NKJV</b>	<b>"kwa namna yoyote .....haitaondoka ,hata yote yatimie"</b>
<b>NRSV</b>	<b>"haitaondoka ,hata yote yatimie"</b>
<b>TEV</b>	<b>"haitaondoka ,hata yote yatimie "</b>
<b>NJB</b>	<b>"haitaondoka. . .mpaka makusudi yake yametimia"</b>

Neno la kwanza siku zote lilimaanisha kuharibu kitu kwa kukiangusha chini kama ukuta. Neno la pili lilitumika katika Mt. 1:22 kutimiliza kama katika kukamilisha kazi yake iliyotangazwa. Ingawa neno hili lilikuwa na maana zingine kadha katika sehemu zingine za Agano Jipya,hapa inazungumzia juu ya Agano la Kale kutimiza ukamilifu wake katika Kristo. Mafundisho ya Yesu ni kama mvinyo mpya ambao hauwezi kuwekwa katika kiriba kikuu kuu (kama vile Mt. 9:16-17). Kutimilizwa huku kunarejerea maisha ya Yesu, kifo, ufufuo, kuja kwa mara ya pili, hukumu na utawala wa milele ambao ni kwa namna baadhi kuchomoza kwa Agano la Kale. Agano la Kale linaelekeza kwa Kristo na kazi Zake. Mitume walilifasiri katika namna ya uanishi au namna ya elimu ya Kristo!

**5:19** Mstari huu sio tishio kuelekea wafasiri wa kisasa na walimu bali kukataliwa kwa nadharia za kidhiria za desturi za Kiyahudi. Yesu Mwenyewe kwa uwazi aliweka kando desturi za kinywa (Talmud), lakini pia sehemu ya sheria zilizoandikwa! Mifano miwili ingekuwa (1) mifano ya talaka katika Kumb. 24:1-4 ikikataliwa katika Mt. 5:31-32 (kama vile Marko 7:15,19-23) na (2) sheria za vyakula katika Mambo ya Walawi 11 ikikataliwa katika Marko 7:15-23. Matumizi ya "udogo" na "ukubwa" inaweza kuwa ushahidi kwa baadhi ya aina za upangaji wa viwango ndani ya ufalme (kama vile Mt. 20:20-28; Luka 12:47-48; 1 Kor. 3:10-15).

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 5:20**

<sup>20</sup> Maana nawaambia ya kwamba, Haki yenu isipozidi hiyo haki ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni.

**5:20** Hii ilikuwa kauli ya kushangaza kwa watu wa dini wenye dhati wa sheria. Kujihesabia haki ni pigo lililozoeleka la mwanadamu mwenye udini (kama vile Isa. 29:13; Kol. 2:16-23). Si mafundisho yaliyo sahihi (Yakobo 2:19) wala matendo ya kidini (Mt. 7:21-23) inaweza kuchukua hitaji la toba binafsi/uhusiano wa ki-imani (kama vile Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21; Flp. 3:8-9; Rum. 10:3-4). Mstari huu na mstari wa 48, ni msingi kufasiri Mahubiri yote ya mlimani. Kwa ajili ya mjadala kamili wa asili na thiolojia ya Mafarisayo, angalia Mada maalumu katika Mt. 22:15.

<b>NASB</b>	<b>"hamtaingia"</b>
<b>NKJV</b>	<b>"kwa namna yoyote hamta"</b>
<b>NRSV, NJB</b>	<b>"kamwe hamtakuja"</b>

Huku kufululizamaneno mawili ya Kiyunani kwa ukanushi. Kazi mojawapo yenye hali ya uelekezi na ya pili nyingine ya hali ya Kiyunani. Ilikuwa namna ya ujasiri zaidi ya kauli ya ukanushi (kama vile Mt. 5:18,26; 10:23,42; 13:14; 15:6; 16:22,28; 18:3; 23:39; 24:2,21,34,35; 25:9; 26:29,35).

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 5:21-26**

<sup>21</sup> Mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, Usiue, na mtu akiua, itampasa hukumu. <sup>22</sup> Bali mimi nawaambieni, Kila amwoneaye ndugu yake hasira itampasa hukumu; na mtu akimfyolea ndugu yake, itampasa baraza; na mtu akimwapiza, itampasa jehanum ya moto. <sup>23</sup> Basi ukileta sadaka yako madhabahuni, na huku ukikumbuka ya kuwa ndugu yako ana neno juu yako, <sup>24</sup> iache sadaka yako mbele ya madhabahu, uende zako, upatane kwanza na ndugu yako, kisha urudi uitoe sadaka yako. <sup>25</sup> Patana na mshitaki wako upesi, wakati uwapo pamoja naye njiani; yule mshitaki asije akakupeleka kwa kadhi, na kadhi akakupeleka kwa askari, ukatupwa

**5:21 "Mmesikia watu wa kale walivyoambiwa"** Hii ingeweza kueleweka kama "kwenda kwa watu wa kale" kwa watu wa kale." Sehemu ya kwanza ya mstari huu inatoka katika Amri Kumi lakini sehemu ya pili ni ngumu kubainisha a inaweza kuwa nukuu kutoka kwa shule za Kiyahudi (Shammai, wenye msimamo mkali, au Hillel, waliberali). Hii ilimaanisha kukataliwa kwa wafasiri wa kimaandiko wa Mafarisayo wakati huohuo ikielezea uvuvio wa Agano la Kale.

☐ **"mauaji"** Hii ni nukuu kutoka katika Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyahudi (LXX) ya Kut. 20:13 au Kumb. 5:12. Ni kauli tendaji elekezi ya wakati ujao kama shurutishi. Toleo la KJV lina "kuua," lakini katika kutoa huku ni dhana pana sana. Toleo la NKJV lina "mauaji." Fasiri sahihi zaidi ingekuwa "kuua kwa kukusudia kusiko kwa kisheria." Katika Agano la Kale kulikuwa na mauaji ya kukusudia kuliko kwa kisheria "mlipaji kisasi wa damu" (kama vile Kumbu kumbu la Torati 19; Hesabu 35; Yoshua 20).

## MADA MAALUM: MAUAJI (KUTOKA 20:13, BDB 953, KB 1283)

### I. Mukstadha

- A. Inahitajika kukumbukwa kwamba hata amri zinayoonekana kuwa na asili ya kijamii kiukweli ni za kidini. Ukuu wa Mungu juu ya viumbe na ukombozi vinafichwa katika amri. Amri ya usiue ii, katika tazamio sahihi, neno kuhusu sura ya Mungu katika kila mwandamu na uangalizi wa Mungu na uhusika wake katika maisha ya mwandamu.
- B. Inahitajika kukumbukwa kwamba kila amri inaimulika jamii ya waaminio. Maana zake ni kama pana kama alivyo mwanadamu!

### II. Neno la Kujifunza la Maneno Muhimu

#### A. "Mauaji"

1. Neno hili *rasah*, BDB 953, KB 1283 linamaanisha kukatisha maisha. Hili limetumika mara sita tu katika Agano la Kale. Kuna maneno mengine kadhaa ya Kiebrania yanayopishana yaliyotumika mara miamoja.
2. Hili neno (*rasah*) linaonekana kuwa na maana halisi yenye kuwekewa mipaka na maana iliyopanuliwa.
  - a. Kiuhalisia hii ilihusiana na kuuondoa uhai wa mwenzu wa agano katika sheria, katika namna iliyokusudiwa, mara nyingi inahusiana na kifungu "mkombozi wa kidugu" au *go'el*. Matumizi haya yalikusudia, lakini katika maana ya malipizi ya kisheria (kama vile Hes. 35:30-34; Law. 24:13-23). Katika uhalisia Talionis, "jicho kwa jicho," (kama vile Mwa. 9:5-6) ilikuwa njia ya kuthibiti kisasi. Baadaye, miji ya wakimbizi (Kut. 4:41; Yos. 20:3) ilihimarishwa ili washiriki wa agano waliowaua wanajamii wengine kwa bahati mbaya au kwa hamaki waweze kuikwepa ghadhabu ya wanafamilia walioathiliwa na matukio hayo.
  - b. Baadaye hili neno lilikuja kurejelea shauku au mtazamo ulio nyuma ya kuuondoa uhai. Hii dhana ya "makusudi" inakuwa ya juu zaidi (kama vile Kut. 21:12-14; Hes. 35:11,22; Kumb. 28:24).
  - c. Tofauti hii inakuwa ya muhimu katika amri hii. Katika mukstadha huu hili linaonekana kurejelea wengine tu walio katika jumuiya ya agano. Hili lilihusiana na mkombozi wa kidugu, au kisasi cha damu. Hata hivyo, hili neno linatumika katika vifungu vinavyofuatia vyenye kuziakisi Amri Kumi za Mungu Hosea 4:2 na Yer. 8:9, kumrejerea muuaji. Neno hili linahusiana na sheria tu, lakini kwa shauku. Hii inapanuka toka jirani hadi mwandamu.
3. Neno hili kwa uhakika halihusiani na mambo yetu ya sasa yahusuyo maadili adhabu za mali au vita. Kamwe Wayahudi hawakuwa na na tatizo kuhusu utekelezaji wa kijamii au vita takatifu

(au, kwa ajili hiyo, vita isiyo takatifu!).

4. Tafsiri bora zaidi kwa utamaduni wetu ingeweza kuwa "mauaji ya kukusudia."

III. Tambuzi za Kimuktadha

- A. Amri za sita, saba, na nane zinaundwa na maneno mawili tu ya Kiebrania. Haya ni mafupi sana na yenye kuelekea hoja moja kwa moja.
- B. Maisha, kama yote yahusuyo uumbaji, yanahusiana na Mungu. Namna tunavyowatenda wengine inaziakisi fikra zetu kumhusu Mungu.

IV. Ufanano wa Agano Jipya

A. Yesu

- 1. Upanuzi wake wa amri hii katika Mt. 5:21-26 unatupa mwelekeo sahihi wa mjadala wetu wa sasa kuhusu namna ya kulitumia andiko hili katika nyakati zetu.
- 2. Kwa uwazi kabisa Yesu alizihamasisha Amri Kumi za Mungu kutokana na kweli wa matendo katika ukweli wa shauku. Tuko kama tunavyofikiri! "Awazavyo mtu moyoni mwake, ndivyo alivyo." Wazo la maisha ni sawa na umuhimu ni bora kuliko tulitambuavyo mara nyingi.

B. Yohana

- 1. Katika Yohana 3:5, dhana hii ya chuki yenye kufanana na yenye kufikiriwa kama mauaji inaelezwa.
- 2. Maneno ya Kiyunani yaliyotumika katika Mt. 5:21 na kuendelea na 1 Yohana 3:5 ni tofauti, bali maana zake kimsingi zinafanana.
- 3. Kitambue kipengele yakinifu katika 1 Yohana 4:19-21.

V. Matumizi

- A. Hata kama kesi za kinataifa zihuszo mauaji zinaweza kumnusulisha mlipa kisasi wa damu kwa kukimbilia mji wa wakimbizi (Hesabu 35; Yohana 20), inampasa kulipa fidia ya kifungo katika mji huo hadi kifo cha Kuhani Mkuu. Matokeo ya tendo hili bado yapo.
- B. Ingawa mstari huu moja kwa moja haurejelei tendo la kujiua, kama ambavyo huenda watu wa kale hawakuweza kufikiri juu ya tukio hili, bado andiko linatupa msingi wa kiroho kuhusu utakaso wa maisha ya mwanadamu.
- C. Andiko hili, hata hivyo, halilizungumzii neno muhimu la swali la sasa la (1) adhabu ya kifedha au (2) vita. Kwa Israeli, haya hayakuwa mambo ya uovu kwao. Waisraeli walijihusisha katika matendo haya yote. Bado, kanuni ya umuhimu wa uhai uliombwa katika sura ya Mungu chini ya utawala wake ni kweli muhimu katika eneo hili.
- D. Andiko hili linazungumzia uhitaji wa neno kuhusu utu na utakatifu wa maisha ya mwanadamu! Sisi tulio katika jumuiya ya waaminio tu watumishi, si kwa matendo yetu tu, bali jamii yetu. Zawadi ya uhai ni vyote binafsi na ushirika.

Tunawajibika kimwili, kijamii, matumizi ya miili yetu kisaikolojia kama tulivyo kimwili, kijamii, na matumizi ya vitu vingine katika jumuiya. Hili ni la kweli katika utamaduni kama letu ambapo tunaruhusiwa kuzungumza na, hivyo, kubadili mfumo. Sisi ni walinzi wa ndugu zetu!

**5:22 "bali nawaambieni"** Mafundisho ya Yesu kulikuwa kimsimamo kutoka kwa walimu wa siku Zake ambae mamlaka yalikuwa yanapatikana katika kunukuu walimu wa Kiyahudi kama mamlaka yao (kama vile Mt. 7:28-29; Marko 1:22). Mamlaka ya Yesu yako katika Yeye mwenyewe. Yeye ndiye mfunuaji wa kweli wa maana ya Agano la

Kale. Yesu ni Bwana wa maandiko. Ile "Mimi" yenye nguvu ni ya -"Mimi mwenyewe na hakuna mwingine" au "mimi mwenyewe (kama Mwana wa Mungu ajuaye ufahamu wa Mungu.)"

☑️"**yeyote aonaye hasira**" Hii ni kauli ya kati endelevu ya wakati uliopo. Hii ilikuwa neno la Kiyunani kwa hasira iliyotulizwa, isiyosamehe ya muda mrefu. Mtu huyu aliendelea kugubikwa na hasira kali.

☑️"**ndugu yake**" Toleo la KJV linaongeza "bila sababu." Hii ni aina tofauti ya maandiko ya Kiyunani. Nyongeza haipo katika maandiko ya kale ya Kiyunani P<sup>67</sup>, \*κ, B, au Vulgate. Hata hivyo lipo katika maandiko κ<sup>c</sup>, D, K, L, W, Diatesseron, na fasiri za kale za kishamu na kikoptiki. Toleo UBS<sup>4</sup> linatoa maandiko mafupi zaidi alama ya B (karibia na hakika). Nyongeza inaweka udhaifu wa msukumo mkubwa wa kifungu cha habari. Inaweza kuwa msaada kwa wakati huu kuelezea andiko la juu: ile \* ilimaanisha nakala ya kale kabisa ya aina ya maandiko ambayo inapatikana; ile c inamaanisha wasahihishaji wa baadaye wa wanakili. Hii mara kwa mara inawakilishwa na 1, 2, 3, n.k, ikiwa kuna mfululizo wa wasahihishaji; hesabu baada ya P inarejerea maandiko ya mafunjo. Maandiko ya Kiyunani yanaelezea kwa herufi kubwa wakati maandiko ya mafunjo yanaelezewa kwa hesabu. Kwa taarifa ya nyongeza, angalia [Uhakiki wa Kimaandiko](#)

<b>NASB</b>	"enyi wapumbavu"
<b>NKJV</b>	"mtafyolea"
<b>NRSV</b>	"ikiwa mtatukana"
<b>TEV</b>	"Yenyi msio faa"
<b>NJB</b>	"wapumbavu"

*Raca* kilikuwa kiaramu kwa ajli ya "mtu mjinga asiye na uwezo wa kimaisha." Sehemu hii haijishughulishi na majina Fulani ambayo mtu anaweza au hawezi kuita mwingine bali mtazamo wa mwamini kwa wengine na hasa ndugu wa kiagano.

Neno la Kiyunani, *mōros*, inayofasiriwa "mpumbavu," lilimaanisha kuaksi neno la Kiaramu *raca*. Hata hivyo matumizi ya maneno ya Yesu hayakuwa kwa neno la Kiyunani *mōros*, bali kimsingi neno la Kiebrania *mōreh*, BDB 598, ambalo lilimaanisha "uasi dhidi ya Mungu" (kama vile Hes. 20:10; Kumb. 21:18,20; angalia F. F. Bruce, *Answers to Questions*, ukr. 42). Yesu aliita Mafarisayo kwa neno hili katika Mt. 23:17. Sio tu kwa matendo yetu bali misukumo yetu, mitazamo na makusudi kujua dhambi dhidi ya mwanadamu mwenzetu. Mauaji kadiri Mungu inavyomuhusu inaweza kuwa kwa mawazo! Chuki dhidi ya ndugu zetu au dada kwa uwazi inaonesha kwamba hatumjui Mungu (kama vile 1 Yohana. 2:9-11; 3:15, na 4:20). Tukizungumza kijamii, mawazo ya chuki ni zaidi kuliko mauti lakini kumbuka kwamba sehemu hii ya maandiko inakusudiwa kuvunja kujihesabia haki kote na kiburi juu ya matendo ya mtu mwenyewe. Inawezekana kwamba maelezo haya yaliyofunganishwa katika utatu ilikuwa mbinu ya kejeli juu ya ufasiri wa kiuandishi.

## MADA MAALUM: WAPUMBAVU

Mtazamo huu/Mtu huyu anaelezea kwa maneno kadhaa ya Agano la Kale.

1. "mpumbavu," "mtu mpumbavu" (BDB 17, KB 21) – kama vile Ayubu 5:2,3; Zab. 107:17; Mith. 1:7 (na mengine mengi); Isa. 19:11; 35:8; Yer. 4:22; Hos. 9:7
2. "yule mwenye ujasiri wake" (BDB 493, KB 489) – kama vile Zab. 49:10; 92:6; 94:8; Mith. 1:22,32 (na nyingine nyingi); Muh. 2:14-16; 5:1,3,4 (na mengine mengi)
3. "mtu mtupu" (BDB 614, KB 663) – kama vile Kumb. 32:6,21; 2 Sam. 3:33; 13:13; Ayubu 2:10; 30:8; Zab. 14:1; 39:8; 53:1; 74:18,22; Mith. 17:7,21; 30:22; Yer. 17:11
4. "mwenye kichwa kizito" (BDB 698, KB 754) – kama vile Mwa. 31:28; 1 Sam. 13:13; 2 Sam. 15:31; 24:10; 1 Nyak. 21:8; 2 Nyak. 16:9; Mh. 2:19; 10:3,14; Isa. 44:25; Yer. 5:21

Yesu alitumia maneno matatu kuelezea watu wapumbavu.

1. *aphrōn*, Luka 11:40; 12:20
2. *anoētos*, Luka 24:25

3. mōros, Mt. 5:22; 23:17,19

Kauli ya nguvu zaidi iliyotolewa na Yesu kutumia tabia ya sifa hii ya mtu mmoja kwa mwingine katika Mt. 5:22, ambapo mōros inaaksi neno la Kiaramu raca, ambalo linamaanisha kushindwa maisha. Kipengele hiki hakishughulikii majina gani unaweza au huwezi kumuita mtu mwingine lakini kwa mtazamo wa mwamini kwa wengine hasa ndugu wa agano.

Neno la Kiyunani, mōros, linafasiriwa "mpumbavu," lilimaanisha kuaksi neno la Kiaramu raca. Hata hivyo maneno ya Yesu hayakuwa kwa maneno ya Kiyunani mōros, bali kimsingi neno la Kiebrania mōreh, BDB 598, ambalo lilimaanisha "uasi dhidi ya Mungu" (kama vile Hes. 20:10; Kumb. 21:18,20; angalia F. F. Bruce, Answers to Questions, ukur. 42). Yesu aliwaita Mafarisayo kwa jina hili katika Mt. 23:17. Si tu matendo yetu, bali msukumo, mtazamo na makusudi yanaamua dhambi dhidi ya binadamu wenzetu. Mauaji inavyoonekana kwa Mungu, linaweza hata likawa wazo! Chuki dhidi ya ndugu yetu wa kike au wa kiume inaonesha kwa uwazi kwamba hatumjui Mungu (kama vile 1 Yohana. 2:9-11; 3:15, na 4:20). Tukizungumza kijamii, mawazo ya chuki ni mazuri zaidi ya mauti lakini kumbuka kwamba sehemu hii ya maandiko imekusudiwa kuvunja hali yote ya kujihesabia haki na kiburi katika wema wetu wenyewe.

Paulo anafuata Agano la Kale na Yesu katika kutumia maneno kadhaa kuelezea watu wapumbavu.

1. aphrōn, 1 Kor. 15:36; 2 Kor. 11:16,19; 12:6,11

2. mōros, 1 Kor. 3:18; 4:10 na hali inayofanana na hiyo katika Rum. 1:22

Watu wanaodai kumjua Mungu bali wanafikiri na kutenda katika njia zisizofaa, mara kwa mara wanapewa sifa kama fukara wa mawazo! Maoni ya kejeli ya Paulo, yanajirudia rudia katika 1 na 2 Wakorintho, inafunua aina hii ya mtu. Walikuwa na ujasiri wote kwamba walikuwa na na maarifa kiasi kwamba hawakuweza kuona wala kutambua maarifa ya kweli!

NASB	"moto uwakao wa kuzimu"
NKJV, NJB	"moto wa kuzimu"
NRSV	"kuzimu ya moto"
TEV	"moto wa kuzimu"

Huu ni ubananishaji wa Kiyunani *Gehenna*. Angalia Mada Maalum hapa chini, II. D.

## **MADA MAALUMU: WALIOKUFA, WAKO WAPI? (SHEOL/HADES, GEHENNA, TARTARUS)**

I. Agano la Kale

- A. Watu wote wanakwenda shimoni (*sheol*) (hakuna mizizi yenye chanzo kimoja cha neno na asili ya neno lenyewe haijulikani, BDB 982, KB 1368), ambayo ndiyo ilikuwa njia ya kurejerea mahali pale wafu wanaishi au kaburi, hasa hasa katika kitabu cha Ayubu na Isaya. Katika Agano la Kale ilikuwa ni kivuri, utambuzi, lakini maisha yasiyo na furaha (kama vile Ayubu 10:21-22; 38:17)
- B. Tabia za shimoni (*sheol*)
1. Inahusiana na hukumu ya Mungu (moto), kumb.32:22
  2. Gereza lenye viziwi, Ayubu 38:17; Zab. 9:13; 107:18
  3. eneo ambalo huwezi rudi tena, Ayu. 7:9 (sifa ya mkazi wa Akkad kwa ajili ya umauti)
  4. Eneo/ulimwengu wa giza, Ayu. 10:21-22; 17:13; 18:18
  5. Mahali penye utulivu, Zab.. 28:1; 31:17; 94:17; 115:17; Isa. 47:5
  6. panahusiana na mateso hata kabla ya siku ya hukumu, Zab. 18:4-5
  7. panahusiana na *utelekezaji* (maangamizo; angalia Mada Maalum: *Kutelekezwa. . Apollyon*), ambapo pia Mungu yupo, Ayu. 26:6; Zab.. 139:8; Amo. 9:2
  8. panahusiana na "shimo lefu" (kaburi), Zab.16:10; 88:3-4; Isa. 14:15; Ezek. 31:15-17
  9. waovu hushuka ndani ya shimo la *sheol*, Hes. 16:30,33; Ayu. 7:9; Zab.. 55:15
  10. mara nyingi hujibadilisha kama mnyama mwenye mdomo mkubwa, Hes. 16:30; Mith. 1:12; Isa. 5:14; Hab. 2:5

11. kule watu huitwa *Repha'im* (yaani., "roho za mauti"), Ayu. 26:5; Mith. 2:18; 21:16; 26:14 Isa. 14:9-11)
  12. Hata hivyo, YHWH yupo hata hapa, Ayu. 26:6; Zab.. 139:8; Mithali. 15:11
- II. Agano Jipya
- A. Kwa Kiebrania *Sheol* limetafasiliwa kwa Kiyunani kama Kuzimu (ulimwengu usio onekana)
  - B. Tabia za kuzimu (nyingi zinafanana kama za *Sheol*)
    1. Anarejerea mauti, Mt. 16:18
    2. imehusianishwa na mauti, Ufu. 1:18; 6:8; 20:13-14
    3. mara nyingi panafanana na mahali pa mateso ya milele (Gehenna), Mt. 11:23 (nukuu toka agano la kale); Lk. 10:15; 16:23-24
    4. mara nyingi inafanana na kuwekwa kaburini, Lk. 16:23
  - C. Yumkini imegawanywa na (walimu wa dini ya Kiyahudi)
    1. Sehemu ya watakatifu iitwayo Paradiso (ki-ukweli ni jina lingine la Mbinguni, kama vile. 2 Kor. 12:4; Ufu. 2:7), Lk. 23:43
    2. Sehemu ya waovu iitwayo "kwenye vifungo vya giza", iliyoko chini kabisa ya kuzimu, 2 Petr 2:4, mahali palipowekwa kwa ajili ya malaika waovu (k.v Mwanzo 6; I Enoch). Inahusiana na kutupwa "shimoni" Luk. 8:31; Rum. 10:7; Ufu. 9:1-2,11; 11:7; 17:18; 20:1,3
  - D. *Gehenna*
    1. Inaangazia kwenye kifungu cha agano la kale, "bonde la wana wa Hinnom (kusini mwa Yerusalemu). Palikuwa ni mahali Wafoenike walipoichoma miungu ya , Molech (BDB 574, KB 591), ilikuwa inaabudiwa wakati wa kuwadhabihu watoto (kama vile 2 Fal. 16:3; 21:6; 2 Nya. 28:3; 33:6), ambavyo ilikuwa imekataliwa katika Law. 18:21; 20:2-5.
    2. Yeremia alibadili toka sehemu ya ibada ya wapagani kuwa mahali pa hukumu ya YHWH (Kama vile Yer. 7:32; 19:6-7). Ikajakuwa mahali pa hukumu kali, ya milele katika I Enoch 90:26-27 na Sib. 1:103.
    3. Wayahudi wa enzi ya Yesu waliogopeshwa na ushiriki wa wazee wao katika ibada ya kipagani kwa kuwadhabihu watoto, kwamba waliigeuza sehemu hii kuwa sehemu ya kutupa takataka kwa ajili ya Jerusalemu. Mingi ya misemo ya Yesu kwa ajili ya hukumu ya milele ilitokana na sehemu hii iliyojaza (moto, moshi, minyoo, funza, kama vile Mk 9:44,46). Neno Gehenna limetumiwa na Yesu tu (hasa katika Yakobo 3:6).
    4. Matumizi ya Yesu juu ya neno Gehenna
      - a. Moto, Mt. 5:22; 18:9; Mk 9:43
      - b. Mahali pa milele, Mk. 9:48 (Mt. 25:46)
      - c. mahali pa maangamizo (kwa mwili na roho), Mt. 10:28
      - d. panafanana na *Sheol*, Mt. 5:29-30; 18:9
      - e. Panaainisha waovu kama "wana wa Jehanamu" Mt. 23:15
      - f. Ni matokeo ya hukumu ya kimahakama, Mt. 23:33; Luk 12:5
      - g. Dhana ya Gehenna inafanana na mauti ya pili (kama vile Ufu. 2:11; 20:6,14) au ziwa la moto (k.v. Mt. 13:42,50; Ufu. 19:20; 20:10,14-15; 21:8). Yawezekana ziwa la moto pakawando mahali pa watu kuishi milele (wanaotoka kuzimu) na malaika waovu (waliotoka shimoni, 2 Petr. 2:4; Yuda 1:6 au shimoni, kama vile Luk 8:31; Ufu. 9:1-11; 20:1,3).
      - h. ilikuwa haikusanifiwa kwa ajili ya binadamu, lakini ilikuwa ni kwa ajili ya shetani na malaika wake, Mt. 25:41
  - E. yawezekana, kwa sababu ya kupishana kwa maneno shimoni (*sheol*), kuzimu(*hades*) na Jehanamu(*Gehenna*) kuwa
    1. kiasili watu wote walikwenda shimoni/kuzimu
    2. uzoefu wao wa (mema/mabaya) utazidishwa kwenye siku ya hukumu ya mwisho, lakini sehemu ya watenda maovu itabaki kuwa ile ile (hi indo kwa sababu toleo la KJV linaitafasili kama kuzimu (kaburi) kama Jehanamu .
    3. Andiko katika agano jipya linalotaja kuhusu mateso kabla ya hukumu ni pale penye mfano

katika Luka 16:19-31(Lazaro na mtu tajiri). Sheol pia pameelezwa kama mahali pa mateso (kama vile Kumb. 32:22; Zab. 18:1-5). Hata hivyo, mtu hawezi kutengeneza andiko juu ya mfano.

III. Hali ya mwingiliano kati ya mauti na ufufuo

- A. Agano jipya halifundishi juu ya “zinaa ya nafsi,” ambacho ni moja ya kitu kati ya mitazamo mingi ya kale juu ya maisha baada ya kufa , ambapo panadaiwa kuwa
1. nafsi ya mwanadamu huwepo hata kabla ya maisha haya ya kimwili
  2. nafsi ya mwanadamu ni ya milele kabla na baada ya kifo cha kimwili
  3. mara nyingi mwili unaonekana kuwa gereza na mauti inaurudisha kwenye hali uliokuwanayo kabla
- B. Agano Jipya linadokeza juu ya hali ya kutoungana kati ya mauti na ufufuo
1. Yesu anaongelea juu ya utengano wa mwili na roho, Mt. 10:28
  2. Ibrahimu angeweza tayari kuwa na mwili, Mk. 12:26-27; Lk. 16:23
  3. Musa na Eliya walikuwa na mwili wa nyama kipindi Yesu anageuka sura, Mathayo 17
  4. Paulo anadai kuwa kipindi cha Yesu kurudi mara ya pili, waamini watakuwa na mwili mpya, 1 The. 4:13-18
  5. Paulo anadai kuwa waamini watapata mili mipya ya kiroho siku ya kufufuka, 1 Kor. 15:23,52
  6. Paulo anadai kuwa waumini hawaendi kuzimu, lakini huwa wamekufa huwa na Yesu, 2 Kor. 5:6,8; Fil. 1:23. Yesu aliyashinda mauti na kuwachukuwa watakatifu akaenda nao mbinguni, 1 Pet. 3:18-22.

IV. Mbinguni

- A. Neno hili limetumika kwa maana tatu katika Biblia.
1. kwa maana ya anga juu ya dunia, Mwa. 1:1,8; Isa. 42:5; 45:18
  2. Mbingu yenye nyota, Mwa. 1:14; Kumb. 10:14; Zab. 148:4; Ebr. 4:14; 7:26
  3. Mahali pa kiti cha Enzi cha Mungu, Kumb. 10:14; 1 Fal. 8:27; Zab. 148:4; Efe. 4:10; Ebr. 9:24 (Mbingu ya tatu, 2 Kor. 12:2)
- B. Biblia haifunui mengi kuhusu maisha baada ya kifo, yumkini kwa sababu ya mwanadamu aliyeanguka hana njia au uwezo wa kuelewa (kama vile 1 Kor. 2:9).
- C. Mbinguni kumesimama kwa yote ni mahali (kama vile Yn. 14:2-3) na mtu kamili (kama vile 2 Kor. 5:6,8). Mbinguni paweza kuwa ni bustani ya Edeni iliyorejeshwa (Mwanzo 1-2; Ufunuo 21-22). Dunia itatakaswa na kurejeshwa (k.v. Mdo.3:21; Rum. 8:21; 2 Pet. 3:10). Taswira ya Mungu (Mwa. 1:26-27) imerejeshwa katika Kristo. Sasa ushirika ule wa ndani kwenye bustani ya Edeni yawezekana ukarejea tena. Hata hivyo, huu wawezakuwa ni msemu (mbinguni kama mji mkubwa Ufu. 21:9-27) na sio halisi. 1 Korintho 15 inaelezea tofauti kati ya mwili halisi na mwili wa kiroho kama mbegu ya mti uliokomaa. Tena, 1 Kor. 2:9 (nukuu toka Isaya 64:4 na 65:17) ni ahadi kubwa na tumaini! Nafahamu kuwa tutakapomwona Yeye tutafanana naye (kama vile 1 Yoh.3:2).

V. Vyanzo vya kusaidia

- A. William Hendriksen, *The Bible On the Life Hereafter*  
B. Maurice Rawlings, *Beyond Death's Door*

**5:23** Hii ni sentensi ya daraja la tatu lenye masharti inayomaanisha kitendo kinachoweza kutokea.

☑"**ukileta sadaka yako madhabuni**" Hii kwa nguvu inamaanisha kwamba Mathayo aliandika kabla ya kuharibiwa kwa Hekalu na Kamanda wa Kirumi Tito mnamo mwaka 70 B.K. Mtindo wa maisha ya upendo unatangulia matendo ya kidini! Mahusiano yanatawala juu ya ibada. Watu ndio kipaumbele pamoja kwa Mungu.Ni watu ndio wa milele.

**5:24 “upatane na nduguyo"** Hii ni kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu. Mahusiano ya kibinafsi ni muhimu zaidi kuliko (1) ibada za vipindi (Mt. 5:24) au (2) maamuzi ya kimahakama (Mt. 5:25).



5:26 "hakika" Angalia Mada maalumu katika Mt. 5:18.

☑ "hata uishe kulipa senti ya mwisho" "Senti" ni sarafu ndogo zaidi ya Kirumi, *quadrans* (angalia Mada Maalum katika Mt. 17:24). Hukumu inaondoa adhabu kamili. Rehema na upendo husamehe vyote!

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 5:27-30**

<sup>27</sup> Mmesikia kwamba imenenwa, Usizini; <sup>28</sup> lakini mimi nawaambia, Kila mtu atazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake. <sup>29</sup> Jicho lako la kuume likikukosesha, ling'oe ulitupe mbali nawe; kwa maana yakufaa kiungo chako kimoja kipotee wala mwili wako mzima usitupwe katika jehanum. <sup>30</sup> Na mkono wako wa kuume ukikukosesha, ukate uutupe mbali nawe; kwa maana yakufaa kiungo chako kimoja kipotee wala mwili wako mzima usitupwe katika jehanum.

5:27 "uzinzi" Hapa ni neno *moichaomai*. Ni nukuu kutoka Amri Kumi inayopatikana katika Kut. 20:14 na Kumb. 5:18. Neno la Kiyunani kutoka Tafsiri ya neno la Kiyunani *porneia*. Neno hili siku zote lilirejerea kwa mahusiano ya kindoa ya ziada lakini pia lilikuwa na nyongeza ya kisawe cha shughuli za kimahusiano ndoa zaidi kama vile mahusiano ya jinsia moja au ukatili. Katika Agano la Kale uzinzi ulikuwa tendo la kingono linalojumuisha watu waliooana. Yesu alifafanua upya dhambi ya kingono kama mtazamo wa moyo. Tendo la ndoa ni zawadi kutoka kwa Mungu, njema na jambo kamili. Lakini Mungu pia ameweka mipaka juu ya kulifanya kwa ajili ya ustawi wetu wenyewe na furaha ya kudumu. Wanadamu wenye viburi, wenye kujipenda wenyewe tu siku zote wanataka kwenda zaidi ya mipaka waliyowekewa na Mungu. Maneno haya ya Yesu kwa kuyarejea pia yangeweza kumaanisha matendo ya kingono kabla muda wa ndoa.

**MADA MAALUM: UZINZI (KUTOKA 20:14, BDB 610, KB 658)**

I. Muktadha

- A. Ni dhahiri kwamba amri hii inahusiana na heshima ya mtu kwa Mungu ambayo inaonekana katika heshima ya maisha ya majirani wa mtu, mke, ma mali (kama vile Yer. 5:8). Hili linathibitishwa na mtiririko tofauti wa amri hizi katika Agano la Kale la Kiebrania.
- B. Ufanano wa Kitabu cha Kutoka unaonyesha ufanano wa kufaa kwa kuasilisha kweli hii ya kale katika utamaduni wetu.
- C. Kama tendo la kuwaheshimu wazazi lilivyoonekana kama msingi kwa jamii imara, ndivyo ilivyo, amri hii.
- D. Pia amri hii inadokeza umiliki wa Mungu na utawala wa tendo la kujamiiana na maisha ya familia zetu.

II. Neno la Kujifunza

Neno kuu katika andiko hili ni "uzinzi" (גַּזְזִי, BDB 610). Ni muhimu kwamba mtu hulielewa neno hili katika nuru ya utamaduni wa kale wa Kiebrania.

- A. Neno hili ni tofauti na muktadha wa Agano la Kale wa neno "uasherati." Uzinzi unahusiana na sehemu ndogo sana katika uhusiano wa tendo la kujamiiana kwa mtu aliye katika ndoa. Hili neno "uasherati" leye kudokeza pande zote si kwa walio katika ndoa (kama vile Mit. 29:3; 31:3). Tofauti hii inapotea katika maneno ya Agano Jipya la Kiyunani.
- B. Uwezekano huu unaeleza sababu za mkazo wa ndoa kwa sababu unahusiana na umuhimu wa haki za kurithi, ambazo zilihusishwa katika ahadi ya Mungu ya kifungu "nchi." Kila baada ya miaka hamsini (jubilei) kila kitu kinareshwa kwa makabila yao wenyewe (kama vile Law. 25:8-17).
- C. Uzinzi ulishutumiwa hata kabla ya Torati ya Musa (kama vile Mwa. 12:10 na kuendelea; 26:7 na kuendelea; 39:9).
- D. Uzinzi ulionekana kama ishara ya dhambi dhidi ya
  - 1. jirani – Kut. 20:14; Kumb. 5:18

2. ndoa – Law. 18:20
  3. Mungu – Mwa. 20:2-13; 26:7-11
- E. Adhabu yake ilikuwa kifo kwa pande zote mbili
1. Law. 20:10
  2. Kumb. 22:22-24
  3. Eze. 16:40 (stiaari)
  4. Maonyo makali yanapatikana katika Mithali 1-9

III. Uhusiano wake na Agano Jipya

- A. Yesu alikitumia kitabu cha Law. 19:18 kama muhtasari wa Agano la Kale (kama vile Luka 10:27). Hili linathibitisha kuwa Amri Kumi zinahusiana na namna tunavyowatendea wengine.
- B. Yesu anazichochea amri hizi katika Mt. 5:28. Anaondoa mkazo uhusuo shauku kuliko tendo. Wayahudi wanazona fikra kama kiini cha nafsi. Alichokiwaza mtu ndicho/ndivyo alivyokuwa (Mit. 23:7). Hili linayafanya Amri Kumi kwa namna fulani yasiwe ma uwezekano wa kutunzwa—hii ndiyo sababu! (kama vile Gal. 2:15-3:29).

IV. Matumizi yake ya Sasa

- A. Ndoa ni kitu ufanano pekee ulio bora wa maisha ya imani ya kujitolea katika jina la Mungu. Ni nafasi yetu bora sana kuzielewa kweli za dhana za maagano ya Agano la Kale (Mal. 2:14). Kuwaheshimu wenza wetu katika nyanja zote, ikiwemo kujamiiana kwa mwanadamu, hutusaidia kuelewa msukumo wa mstari huu.
- B. Utulivu wa ndoa na uaminifu, kama heshima kwa wazazi, ndiyo msingi mkuu wa nguvu ya kijamii na kudumu kwake.
- C. Inahitajika kusistizwa kwamba kujamiiana kwa mwanadamu ni zawadi toka kwa Mungu (kama vile Mwa.1:27,28; 9:1,7). Hili lilikuwa wazo lake na mapenzi yake kwa mwanadamu. Masharti hayamaanishi kuingilia uhuru au furaha ya mwanadamu, bali kutoa agizo la baadhi ya masharti ya Kimungu kwa mwadamu aliyeanguka. Mipaka hii inafumuliwa kwa ajili ya manufaa yetu na furaha ya muda mrefu. Ingawa mwadamu amelitumia vibaya tendo hili la kujamiiana, kama alivyokuwa na zawadi zote toka kwa Mungu, bado kuna hamu kubwa ndani ya mwanadamu ambayo lazima iwe chini ya utawala na mwongozo wa Mungu.
- D. Miongozo ya tendo la kujamiiana lazima iwekewe maelekezo ili utakatifu wa nafsi ya mwanadamu (mume au mke) uheshimiwe kwa sababu yeye ameumbwa katika sura ya Mungu (Mwa. 1:27). Tazamio letu lililoanguka lililo juu ya "mimi" li dhahiri sana katika eneo hili.

**5:28 "moyo"** Angalia Mada maalum katika Mt. 5:8.

**5:29-30** Hii kidhahiri ni utiaji chumvi kwa ajili mguso wa kihisia! Dhambi ni hatari na madhara yake ni ya milele!

**5:29 "ikiwa"** Hizi ni sentenzi za daraja la kwanza zenye masharti ambazo zilikuwa zinahisiwa kuwa kweli kutoka katika mtazamo wa mwandishi au kwa ajili ya makusudi ya kifasihi. Wanadamu wameathiriwa na Mwanzo 3. Hatuko kama tulivyoumbwa tuwe.

<b>NASB</b>	<b>"kuwafanya mjikwae"</b>
<b>NKJV, NRSV</b>	
<b>TEV</b>	<b>"kuwafanya mtende dhambi"</b>
<b>NJB</b>	<b>"litakuwa ndiyo anguko lenu"</b>

Neno hili lilitumika juu ya kuwekewa chambo, likichochea mbinu ya mtego wa mnyama. Angalia ufanano katika Marko 9:43- 48 na kutajwa kwa Yesu mara ya pili katika somo hili katika Mt. 18:8-9. Kwakuwa wanadamu wote wameathiriwa na dhambi (tofauti tofauti kwa watu tofauti tofauti), lazima sisi tuchukue jukumu binafsi kujiondoa wenyewe kutoka katika maeneo/vitu na mazingira yaletayo uharibifu (yaani Mithali 1-9; Efe. 4:27; 6:10-18;

Yakobo 4:7; 1 Pet. 5:8-9). Hatutaweza kumlaumu shetani au hali ya kurithi au mazingira kwa ajili ya dhambi zetu pale sisi sote tutakaposimama mbele za Mungu na kutoa hesabu ya kipawa cha uzima (kama vile Mt. 25:31-46; Ufu. 20:11-15). Sisi ni mawakala wa kimaadili tulio huru tuliofanywa kwa sura ya Mungu, tunaowajibika kwake kwa ajili ya maisha yetu!

☐ **"kupoteza"** Neno hili katika zote mbili katika Mt. 5:29 na 30. Angalia Mada Maalum: *Apollumi* katika Mt. 2:13.

**5:29,30 "kuzimu"** Kuna kuzimu ya milele na dhambi ni tiketi ya kuingia! Angalia Mada Maalum katika Mt. 5:22.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 5:31-32**

<sup>31</sup> Imenenwa pia, Mtu akimwacha mkewe, na ampe hati ya talaka; <sup>32</sup> lakini mimi nawaambia, Kila mtu amwachaye mkewe, isipokuwa kwa habari ya uasherati, amfanya kuwa mzinzi; na mtu akimwoa yule aliyeachwa, azini.

**5:31 "Mtu akimwacha mkewe"** Mistari 27-32 na 19:3-12 inashughulikia jambo lile lile. Kuwa mwangalifu usije kusoma dhana za kidesturi zilizo katika ufahamu katika vifungu hivi! Katika muktadha, Yesu alikuwa anaonesha njia ambazo mtu anafanya uzinzi kuliko zile zilizofundishwa na waandishi: (1) tamaa za kifikra (2) kumuacha mke isipokuwa kwa kukosa uaminifu kwa kuzini nje (kama vile Kumb. 24:1). Yesu anaonesha yeye Mwenyewe kuwa mfasiri sahihi wa maandiko (yaani, 5:17-19,21-48).

**NASB, NKJV**

**NRSV** "talaka ya kuachana"  
**TEV** "hati ya kutalikiana"  
**NJB** "hati ya kuachana"

Hii ni nukuu kutoka Kumb. 24:1-4. Musa alifanya hivi kumlinda mke wake aliyekuwa hana haki au mali kabisa kwa siku hizo na desturi zao. Kuoia tena kuliruhusiwa. Hata hivyo Yesu alielezea kwamba hayo yalikuwa mapatano kwa ajili ya anguko, sio mapenzi ya Mungu. Kutalikiana sio dhambi isiyosameheka bali ni kushindwa ambako kunaathiri uthabiti wa kijamii.

**5:32**

**NASB, NRSV** "isipokuwa kwa habari ya uasherati "  
**NKJV** "kwa sababu yoyote isipokuwa kwa habari ya uasherati "  
**TEV** "ikiwa amekuwa si mwaminifu"  
**NJB** "isipokuwa kwa habari ya uasherati ndani ya ndoa"

Hii "tungo ya isipokuwa" ni ya kipekee katika Injili ya Mathayo. Yawezekana kwasababu ilihusiana na maono ya Kiyahudi ya haki ya urithi itolewayo na Mungu ambayo Mataifa wasingeweza kuelewa. "kukosa uaminifu" ni neno la *porneia*, kama katika Mt. 5:27. Hii inarejerea kwa ukosefu wa maadili wa aina yoyote ya kingono. Hii mara kwa mara ilifasiriwa kama "uasherati" au "ukosefu wa uaminifu." Kulikuwa na shule mbili za Kiyahudi kwa ajili ya ufasiri: (1) Shammai, aliye ruhusu talaka kwasababu ya matendo ya kingono yaliyokuwa sio sawa ("baadhi walikosa nidhamu," Kumb. 24:1) na (2) Hillel, walioruusu talaka kwa sababu yoyote (yaani, "hakupata kibali katika macho yake," Kumb. 24:1). Talaka ilikuwa imefanyika tatizo kubwa ndani ya dini ya Kiyahudi. Baadhi ya wanazuoni wanaona neno hili likihusiana na kujamiiana kingono lakini kusiko kwa uaminifu (Kama vile Mambo ya Walawi 18; 1 Kor. 5:1). Bado wengine wanafikiri inahusiana na jambo la ubikra unaojadiliwa katika Kumb. 22:13-21. Katika Agano la Kale uzinzi uliathiri urithi wa familia ambayo ilikuwa takatifu na iliyotolewa na Mungu (Yoshua 12-24). Ule "Mwaka wa Jubilee" ni kielelezo cha jambo hili.

☐ **"amfanya kuwa mzinzi"** Hii ni kauli tendwa yenye kitenzi jina ya wakati uliopita usio timilifu. Sauti irabu ni muhimu katika ufasiri sahihi wa "kumsababisha azini." Kitendo chenyewe kabisa cha kutaliki mke kilimsababisha mke kunyanyapaliwa na jamii kama mzinifu ikiwa anayo hatia au hana. Yule anayemuoa pia alikuwa

akinyanyapaliwa. Hii sio kauli ya kimafundisho inayorejere kuolewa tena kama kuwa mzinifu (kama vile A. T. Robertson katika *Word Pictures in the New Testament*, vol. 1 kur. 155). Inahitajika kusemwa kwamba somo hili gumu la talaka lazima ishughulikiwe katika muktadha. Hapa ni ujumbe kwa wanafunzi wakati katika Mt. 19:1-9 na Marko 10:2-12 mazingira ni ya kimaswali ya kifarisayo ya kimtego. Lazima tujilinde dhidi ya kutengeneza thioloji yetu wenyewe ya kutalikiana kwa kuunganisha muktadha hizi na kudai kuwa na maoni ya kati ya thiolojia ya Yesu juu ya somo.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 5:33-37**

<sup>33</sup> Tena mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, Usiape uongo, ila mtimizie Bwana nyapo zako; <sup>34</sup> lakini mimi nawaambia, Usiape kabisa; hata kwa mbingu, kwa maana ndicho kiti cha enzi cha Mungu; <sup>35</sup> wala kwa nchi, kwa maana ndiyo pa kuwekea miguu yake; wala kwa Yerusalemu, kwa maana ndio mji wa Mfalme mkuu. <sup>36</sup> Wala usiape kwa kichwa chako, maana huwezi kufanya unywele mmoja kuwa mweupe au mweusi. <sup>37</sup> Bali maneno yenu yawe Ndiyo, ndiyo; Siyo, siyo; kwa kuwa yazidiyo hayo yatoka kwa yule mwovu.

**5:33 "viapo"** Hii ilikuwa maelezo ya maandiko kadhaa ya Agano la Kale. Hii haikumaanisha kulaani lakini jina la Mungu likiletwa katika mazungumzo kuhakikishia ukweli wa kauli ya mtu (kama vile Mt. 23:16-22; Yakobo 5:12). Viapo au nadhiri katika Agano la Kale vingeweza kumaanisha (1) kuabudu (kama vile Kumb. 6:15); (2) taratibu za kisheria (kama vile Kut. 20:7; Law. 19:12); au (3) ukiri wa kufanya jambo fulani (kama vile Law. 27; Hes. 30:2; Kumb. 23:21-22). Yesu alihusishwa katika kiapo katika Mt. 26:63-64. Paulo alifanya kiapo katika 2 Kor. 1:23, Gal. 1:20, Flp. 1:8, na 1 Thes. 2:5. Kiapo kingine kinapatikana katika Ebr. 6:16. Shabaha haipo katika kufanya kiapo bali katika kushindwa kutimiza kiapo!

**5:34-36** Hii ilionesha kwa kuelezea walimu walikuwa wamekuza kuweka na kuondoa nadhiri (kama vile Mt. 23:16-22). Ilikuwa ni njia ya kutokea kusema ukweli kwa kuhusianisha na kauli ya mtu ya Uungu lakini muda wote tukijua kwamba nadhiri ya mtu inatolewa kwa njia fulani haikuwa inamfunga kisheria.

**5:34 "usiape"** Yesu alitoa ushuhuda chini ya kiapo katika Mt. 26:63-64. Paulo mara kwa mara alithibitisha maneno yake ka kuapa kwa jina la Mungu (kama vile 2 Kor. 1:23; Gal. 1:20; Flp. 1:8; 1 Thes. 2:5,10). Jambo ni ukweli na sio sio kuweka vikwazo vya kuapa (kama vile Yakobo 5:12).

**5:37 "maneno yenu yawe Ndiyo, ndiyo; Siyo, siyo"** Yesu alikuwa anashughulika na ukweli sio muundo! Wengine wanaodai kumjua Mungu lazima wawe wakweli na wanaoaminika sio wajanja wajanja.

<b>NASB</b>	"muovu"
<b>NKJV, NRSV</b>	"Yule muovu"
<b>TEV, NJB</b>	"Yule Muovu"

Muundo ulioaksiwa wa neno katika Kiyunani inaweza kuwa aidha isiyo na jinsi, "muovu" au ya kiume, "yule muovu" (angalia Mada Maalum katika Mt. 4:5). Tungo tata ile ile inatokea katika Mt. 6:13; 13:19,38; Yohana 17:15; 2 Thes. 3:3; 1 Yohana. 2:13,14; 3:12; 5:18-19.

Uovu una miundo kadhaa.

1. mfumo wa ulimwengu ulioanguka, Mwanzo 3; Efe. 2:2; Yakobo 4:4
2. uovu binafsi, Efe. 2:2
3. watu binafsi walioanguka, Efe. 2:3; Yakobo 4:1-2

Uovu unatazma fursa ili kuweza kuua, kuiba na kuharibu. Ni rehema za Mungu tu, Mwana Wake na Roho Yake inaweza kutusababisha kuishi kwa furaha, kwa kusudi na maisha ya kuridhisha!

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 5:38-42**

<sup>38</sup> Mmesikia kwamba imenenwa, Jicho kwa jicho, na jino kwa jino; <sup>39</sup> Lakini mimi nawaambia, Msishindane na mtu mwovu; lakini mtu akupigaye shavu la kuume, mgeuzie na la pili. <sup>40</sup> Na mtu atakaye kukushitaki na

**kuitwaa kanzu yako, mwachie na joho pia.<sup>41</sup> Na mtu atakayekulazimisha mwendo wa maili moja, nenda naye mbili.<sup>42</sup> Akuombaye, mpe; naye atakaye kukopa kwako, usimpe kisogo.**

**5:38 "jicho kwa jicho"** Haya ni maelezo ya Kut. 21:24, Law. 24:20, na Kumb. 19:21. Sheria hii kama hati za talaka kiasili ilikusudiwa kushughulikia tatizo la kijamii kwa kujaribu kudhibiti visasi binafsi. Haikuruhusu watu mmoja mmoja au familia kufanya kisasi bali ilikuwa ni mwongozo kwa ajili ya mahakama. Ilikuwa mara kwa mara ikipunguzwa ampaka kiwango cha kifedha na mahakimu wa Kiyahudi. Hata hivyo kanuni ya kudhibitiwa kwa visasi binafsi inadumu.

**5:39-42** Hii ilikuwa ni mfululizo wa mifano itano ya maadili mapya ya Yesu kuhusiana na mitazamo wetu juu ya wengine kwa wote waliopo ndani na walioko nje. Hizi historia ni mifano yenye masharti. Inafanya kazi mtazamo sio sheria ngumu na za haraka kwa kila jamii au kizazi. Ni roho upande uliokwazwa wa waaminio ambao unatakiwa kutoa matendo mazuri ya upendo. Hii haitakiwi kufasiriwa kama kufunika maombi yasiyofaa au yanayorudiwa rudiwa kutoka kwa watu wajanja wajanja au watu wavivu.

**5:39 "mtu muovu"** Hii inaweza kwa muktadha irejeree mfumo wa kisheria wa karne ya kwanza katika namna kwamba ni bora kuvumilia matukano yanayozidi kuliko kumpeleka nduguyo wa kiagano kwa hakimuasiyeamini. Ikiwa "uovu" unahusiana na Mt. 5:37, inaweza kurejerea kwa Yule Muovu. Fasiri ya Charles B. Williams, *The New Testament in the Language of the People*, inatoa chaguzi ya tatu, "yeye anayekujeruhi wewe."

**5:40 "shati. . .koti"** Kitu cha kwanza cha mavazi kinaangukia mavazi ya ndani na kipengele cha pili mavazi ya nje. Hii ni kauli ya utiaji chumvi. Yesu hajaribu kupiga chepuo hali ya kubaki uchi! Haya ni maelezo ya Kut. 22:26- 27; Kumb. 24:10-13. Ukweli wa msingi wa sehemu hii yote ni kwamba Wakristo lazima waende zaidi ya vile wanavyotegemewa na wengine. Kusudi ni kutia moyo wasioamini kuvutwa kwa Mungu kwa matendo ya watu Wake (kama vile Mt. 5:16; 1 Pet. 2:12).

**5:41** Hii kihistoria imewekewa masharti ya muda wakati taifa moja kijeshi linatawala juu ya jingine. Neno "nguvu" lilikuwa limetoholewa kutoka kiajemi, kwa asili likirejerea kubebwa kwa kifurushi. Ilikuwa kuwa neno lilitumika kwa kazi ya nguvu ya namna yoyote kwa kukaliwa kijeshi au serikali ya kiraia. Mfano wa hii ni Mt. 27:32. Wakristo wanatakiwa kwenda zaidi hata ya kile kinachotakiwa au kutegemewa.

**5:42** Hii haikumaansa kuchukuliwa kama sheria ngumu na ya haraka juu ya kukopesha bali mtazamo wa upendo na uwazi kwa wengine hasa masikini, wahitaji na wageni (kama vile Kut. 22:25; Kumb. 15:7-11; Mith. 19:17).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 5:43-48**

<sup>43</sup> Mmesikia kwamba imenenwa, Umpende jirani yako, na, Umchukie adui yako; <sup>44</sup> lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi, <sup>45</sup> ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki. <sup>46</sup> Maana mkiwapenda wanaowapenda ninyi mwapata thawabu gani? Hata watoza ushuru, je! Nao hawafanyi yayo hayo? <sup>47</sup> Tena mkiwaamkia ndugu zenu tu, mnatenda tendo gani la ziada? Hata watu wa mataifa, je! Nao hawafanyi kama hayo? <sup>48</sup> Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.

**5:43** Nukuu inayorejerewa na Yesu ni mujumuisho wa.

1. "Utampenda jirani yako" kutoka Law. 19:18. Yesu anaonekana kuona andiko hili muhimu, hata likiorodheshwa katika Amri Kumi katika Mt. 19:18-19. Katika Marko 12:31, ni amri ya pili kubwa baada ya Kumb. 6:4-5 na katika njia ile ile katika Luka 10:25-28. Paulo anatomia andiko hili kama muhtasari wa sheria nzima katika Rum. 13:8-10.
2. "na wachukie adui zako" sio nukuu itokayo katika Agano la Kale bali ikitoka kwa wayahudi watu wa dini wajitengao (yaani Masadukayo, Mafarisayo, wa-esene). Ni kwa namna gani maadili ya ufalme mpya

kutoka kwa limwengu ulioanguka unatengenezwa na "u-mimi," " zaidi kwa ajili yangu kwa gharama yoyote," "nitapata nini kwa ajili yangu"! Kumjua Mungu kunabadilisha kila kitu (kama vile Mt. 5:20,48)!

**5:44** Toleo la KJV linaongeza tungo kutoka Luka 6:27-28. Haitokei katika maandiko ya kale ya Kiyunani  $\kappa$  au B au maandiko ya kale ya kijiografia kadhaa yaliyotenganishwa. Katika mstari wa 44 kuna kauli shurutishi mbili: "endelea kupenda na kuomba" na kauli endelevu ya wakati uliopo moja, "yule aendeleaye kuleta mateso." Hizi kauli za wakati uliopo zinazungumzia amri zinazoendelea zote za kupenda na kusamehe upande wa mwamini na pia uwezekano wa mateso kuendelea. Ufalme kimsimamo unatofautiana na utaratibu wa ulimwengu wa kisasa!

**5:45** "ili kwamba muwe wana wa Baba yenu aliye mbinguni" Mtindo wa maisha wa waamini kwa uwazi unafunua ni familia ya nani wanamomilikiwa: ya Mungu au ya shetani. Watoto hutenda kama baba yao (kama vile Law. 19:2).

**5:46-47** Matendo ya waaminio lazima yaende zaidi ya matendo yategemewayo ya kijamii ya wasioamini. Mistari hii inahusisha sentensi mbili za daraja la tatu lenye masharti ambayo inamaanisha matendo ya baadaye yanayowezekana kutendwa.

**5:46 "thawabu"** Haya yalikuwa maudhui yanayojitokeza katika mahubiri ya Mlimani (kama vile Mt. 6:1,2,4,6). Angalia Mada Maalum katika Mt. 5:12.

**5:48**

<b>NASB</b>	"ninyi ni wakamilifu,"
<b>NKJV</b>	"mtakuwa wakamilifu"
<b>NRSV</b>	"kuweni wakamilifu"
<b>TEV, NJB</b>	"lazima muwe wakamilifu"

Haya ni maelezo ya Law. 11:44,45; 19:2; 20:7,26. Neno hili kibayana lilimaanisha "kupevuka" au "kuwezesha kikamilifu." Hii ni kauli yenye nguvu kwamba kilele cha viwango vya Mungu vya haki ni yeye Mwenyewe (kama vile Kumb. 18:13). Wanadamu hawawezi kuwa wakamilifu isipokuwa katika Kristo (kama vile 2 Kor. 5:21). Hata hivyo waamini lazima wahangaika kila siku kwa ajili ya maisha ya kila siku. Lazima kuwe na uwiano wa kithiolojia kati (1) wokovu kukubaliwa kama karama ya bure ya Mungu kupitia Kristo ambayo inaitwa utakaso wa kinafasi na (2) kuuchuchumilia kufanana na Kristo ambako kunaitwa utakaso endelevu. Baadhi ya wafasiri wanaona mstari huu kama muhtasari wa aya iliyomalizika. Ikiwa hivyo ndivyo ingekuwa shabaha kwenye upendo jumuishi wa Mungu kwamba watoto Wake wanatakiwa wamuige.

## **MADA MAALUM: UTAKATIFU WA AGANO JIPYA/UTAKASO**

Agano Jipya linadai kwamba pindi mwenye dhambi anapomgeukia Yesu katika toba na imani (kama vile Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21), mara moja anahesabiwa haki na kutakaswa. Hii ni nafasi yao mpya katika Kristo. Haki yake imewekwa ndani yao (kama vile Mwa. 15:6; Warumi 4). Wanahesabiwa haki na utakatifu (mambo ya kimahakama ya Mungu)

Lakini Agano Jipya pia linataka waamini wote kuwa katika utakatifu na utakaso. Hii yote ni nafasi ya kithiolojia katika kazi aliyoimaliza Kristo na kuwaita wote kufanana na Kristo katika mienendo na matendo katika maisha ya kila siku. Kama ilivyo wokovu ni zawadi ya bure na kuyaghalimia maisha, vile vile pia, utakaso.

### Mwitikio wa awali

Matendo 26:18

Warumi 15:16

1 Wakorinto 1:2-3; 6:11

### Mwendelezo wa kufanana na Kristo

Warumi 6:19

2 Kor. 7:1

Waefeso 1:4; 2:10

2 Wathesalonike 2:13

Waebrania 2:11; 10:10,14; 13:12

2 Petro 1:2

1 The. 3:13; 4:3-4,7; 5:2

1 Timotheo 2:15

2 Timotheo 2:21

1 Petro 1:15-16

Waebrania 12:14

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je Yesu alifasiri upya Agano la Kale au alibadilisha?
2. Nini maana ya "kutimiliza" katika Mt. 5:17 na 18?
3. Je mtu anaweza kupoteza wokovu wake kwa kumwita mtu mwingine au jina la kushusha hadhi (mstari wa 22)?
4. Je Mt. 5:23-24 anasema kwa ibada yetu ya matendo ya kisasa?
5. Je kuolewa tena ni uzinzi?
6. Je kuapa katika mahakama ni dhambi?
7. Elezea ni kwa namna gani Mt. 5:17-20 na 48 inaweka mistari mingine inayobaki.

## MATHAYO 6

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Fundisho juu ya Kusaidia wahitaji	tenda wema ili kumpendeza Mungu	Fundisho juu ya Heshima itendayo Kazi	Fundisho juu ya Ukarimu	Kusaidia wahitaji kwa Siri
6:1	6:1-4	6:1	6:1	6:1-4
6:2-4		6:2-4	6:2-4	
Fundisho juu ya Maombi	Maombi ya Mfano		Fundisho kuhusu Maombi	Maombi ya Siri
6:5-15	6:1-15	6:5-6	6:5-6	6:5-6
		6:7-8	6:7-13	Namna ya Kuomba Sala Ya Bwana
		6:9-15		6:7-15 (9-13)
			6:14-15	
Fundisho kuhusu Kufunga	Kufunga ili kuonwa Na Bwana tu		Fundisho kuhusu Kufunga	Kufunga kwa Siri
6:16-18	6:16-18	6:16-18	6:16-18	6:16-18
Hazina Mbinguni	Weka hazina Mbinguni		Utajiri Mbinguni	Hazina za Kweli
6:19-21	6:19-21	6:19-21	6:19-21	6:19-21
Nuru ya Mwili	Nuru ya Mwili	Taa ya mwili	Nuru ya Mwili	Macho, taa ya mwili
6:22-23	6:22-23	6:22-23	6:22-23	6:22-23
Mungu na Sanamu	Huwezi mtumikia Mungu na Mali		Mungu na mali	Mungu na Fedha
6:24	6:24	6:24	6:24	6:24
Kujali na Hofu	Msiogope			Tumaini katika kukidhiwa
6:25-34	6:25-34	6:25-33	6:25-27	6:25-34
		6:34	6:28-34	

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia"](#))**

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

#### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA MISTARI YA 1-8 NA 16-18**



- A. Mathayo 5 inaelezea tabia za watu wapya wa Mungu na mtazamo wa Mungu wa haki ya kweli. Mathayo 6 inaweka mahusiano ya matazamo wa desturi za Kiyahudi juu ya kile kinachotengeneza haki (yaani kusaidia wahitaji, maombi na kufunga).
- B. Hakuna kanuni za dhahiri bali kipimo cha mtazamo kwa waamini. Kwa maana halizi ya haki, tazama Mt 5:20, 48. Hii inaweza kuwa zawadi yetu aliyotupa Mungu katika Kristo (kama vile 2 Kor. 5:21). Hata hivyo shukrani zetu zinatembea kuelekea kufanana na Kristo.
- C. Kujitoea kusikobadilika kunakotakiwa kwa wanafunzi kuwawekwa wazi, sio kwa kanuni za wazi bali kwa kanuni za kiroho.
- D. Kuna vyote kusudi hasi na chanya katika Mahubiri ya Mlimani.
  - 1. Kutuonesha aina ya maisha ambayo Mungu anatarajia watu wake wayaishi, utaratibu kwa maisha ya ujazo wa Roho
  - 2. kuonesha namna mwanadamu asivyo na uwezo wa kutunza Amri za Mungu. Inatuonesha hali yetu ya dhambi, zaidi kama Amri Kumi (kama vile Gal. 3:15-29). Hakuna anayeweza kusimama akikaguliwa na nuru yake.
- E. Inawezekana kwamba Mt. 6:5, 6 inazungumzia matatizo ya Kiyahudi katika maombi wakati 6:7, 8 inazungumzia matatizo ya wapagani katika maombi.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 6:1-4

<sup>1</sup> Angalieni msifanye wema wenu machoni pa watu, kusudi mtazamwe na wao; kwa maana mkifanya kama hayo, hampati thawabu kwa Baba yenu aliye mbinguni. <sup>2</sup>Basi wewe utoapo sadaka, usipige panda mbele yako, kama wanafiki wafanyavyo katika masinagogi na njiani, ili watukuzwe na watu. <sup>3</sup>Amin, nawaambieni, Wamekwisha kupata thawabu yao. Bali wewe utoapo sadaka, hata mkono wako wa kushoto usijue ufanyalo mkono wako wa kuume; <sup>4</sup>sadaka yako iwe kwa siri; na Baba yako aonaye sirini atakujazi.

6:1

NASB, NRSV "Angalieni msifanye"  
 NKJV "kuweni waangalifu kwamba msifanye"  
 TEV "kuweni waangalifu kwamba msifanye"  
 NJB "kuweni waangalifu kwamba msifanye"

"angalieni" ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Hii ni kibayana "kuweni makini katika kufikiria." Mungu anaangalia moyo (msukumo) kabla ya chochote (kitendo)!

☛ **"haki yenu"** Kifungu hiki kinashugulikia sehemu tatu za karne ya kwanza ya shughuli za kidini za kiyahudi ambazo zilifikiriwa kumfanya mtu awe katika upatanisho na YHWH: (1) usaidaji wahitaji (Mt. 6:2-4); (2) maombi (Mt. 6:5-15); na (3) kufunga (Mt. 6:16-18). Kuweni makini na tabia za kidini (kama vile Mt. 5:20). Vitu vingi vinaweza kuwa vizuri au viovu kutegemea mtazamo wetu, msukumo na kusudi!

"Haki" ikisimama kwa ajili ya utoaji wa msaada katika siku za Yesu. Utoaji wa sadaka ulikuwa mfumo wa kila wiki wa kiyahudi wa utoaji wa kutitolea kusaidia maskini na wahitaji.

### MADA MAALUM: KUWASAIKIA WAHITAJI

- I. Neno lenyewe

- A. Neno hili lilikuwa ndani ya Uyahudi.
- B. Ili linarejelea kuwapa wahitaji na/ama maskini.
- C. Neno la Kiyunani, kuwasaidia wahitaji, linatokana na ufupisho wa neno la Kiyunani *eleēmosunē*.

II. Dhana ya Agano la Kale

- A. Dhana ya kuwasaidia wahitaji ilihidhinishwa katika torati ya kale
  - 1. muktadha unaofanana, Kumb. 15:7-11
  - 2. kusaza," kubakiza sehemu ya mavuno kwa wahitaji, Law. 19:9; 23:22; Kumb. 24:20
  - 3. "mwaka wa Sabato," kuwaruhusu masikini kula mazao ya saba, mwaka wa kutopanda,
- B. Dhana hii iliendelezwa katika Hekima ya Fasihi (mifano iliyoteuliwa)
  - 1. Ayubu 5:8-16; 29:12-17 (yule dhalimu anaelezwa katika 24:1-12)
  - 2. Zaburi, 11:7
  - 3. Mithali 11:4; 14:21,31; 16:6; 21:3,13

III. Uendelezwaji katika Uyahudi

- A. Mgawanyo wa kwanza Mishnah unashughulika na kuwatunza wahitaji, maskini, na Walawi wa mahali palepale.
- B. Nukuu zilizoteuliwa
  - 1. Kitabu cha Mhubiri (pia kinajulikana kama Hekima ya Bin Sira) 3:30, "kama maji yazimishavyo ndimi za moto, ndivyo kuwasaidia wahitaji kulipiavyo dhambi" (NRSV)
  - 2. Tobiti 4:6-11, <sup>6</sup>"Maana ukitenda vitu kwa uaminifu utafanikiwa katika mambo yako yote. <sup>7</sup>Toa sehemu ya mali yako kuwapa maskini. Kamwe usimpe kisogo mtu maskini naye Mungu hatakupa kisogo. <sup>8</sup>Toa ulicho nacho. Ukiwa na zaidi, toa zaidi. Hata kama unacho kidogo tu, toa sehemu yake <sup>9</sup>Kwa kufanya hivyo utajiwekea hazina bara kwa wakati wa shida. <sup>10</sup>Kwa maana kusaidia maskini huokoa mtu kifoni na kumkinga asiingie katika makao ya giza. <sup>11</sup>Naam! Kusaidia maskini, kwa wale wanaofanya hivyo, ini sadaka bora mbele ya Mungu Mkuu." (NRSV)
  - 3. Tobiti 12:8-9, <sup>8</sup>"Afadhali sala pamoja na ukweli na kusaidia maskini pamoja na kutenda haki kuliko kuwa tajiri na kukosa uaminifu. <sup>9</sup>Sadaka kwa maskini humwokoza mtu na kifo na kumtakasa dhambi zake. Wale wanaowasaidia maskini watajaliwa uhai." (NRSV)
    - A. Nukuu ya mwisho kutoka Tobiti 12:8-9 inaonyesha uendelevu wa tatizo. Matendo ya mwanadamu/ faida za mwanadamu zilionekana kama utaratibu kwa misamaha yote na utele.
    - B. Dhana hii iliendelea baadaye katika Maandiko ya Kale ya Kiyunani amabapo nenola Kiyunani la "kuwasaidia wahitaji" (*eleēmosunē*) lilikuja kuwa kisawe cha "mwenye haki" (*dikaikosunē*). Haya yangeweza kubadili kila kitu katika kutafsiri Kiebrania "mwenye haki" (BDB 842, agano la upendo wa Mungu na uaminifu, kama vile Kumb. 6:25; 24:13; Isa. 1:27; 28:17; 59:16; Dan. 4:27).
    - C. Matendo ya mwanadamu ya huruma huwa kusudi ndani yake ili kufanikisha utele wa mtu binafsi hapa na wokovu wakati wa kifo. Tendo lenyewe, badala ya nia iliyo nyuma ya tendo, huwa sifa ya kitheolojia. Mungu huangalia mioyo, kisha hupima kazi ya mikono. Hili lilikuwa fundisho la Walimu wa sheria za Kiyahudi, lakini kwa kiasi fulani hii imepotezwa katika haki binafsi (kama vile Mika 6:8).

IV. Agano Jipya

- A. Neno hili linapatikana katika
  - 1. Mt. 6:1-4
  - 2. Luka 11:41; 12:33
  - 3. Matendo ya Mitume 3:2-3,10; 10:2,4,31; 24:17
- B. Yesu anaelezea uelewa wa kitamaduni kuhusu haki kama (kama vile II Clement 16:4)

☐ "mbele za watu" Kuna baadhi ya mambo ambayo waamini wanatakiwa kuyafanya "mbele za watu."

1. kufanya nuru yako iangaze, Mt. 5:16
2. kumkiri Kristo, Mt. 10:32

☐ "ili kutambuliwa nao" Neno la Kingereza "theatrical (uigizaji)" linatokana na neno la Kiyunani (*theamai*), ambalo linamaanisha "kutazama kwa umakini." Neno "wanafiki" katika Mt. 6:2 pia lina asili ya "theatrical (uigizaji)". Mafarisayo walikuwa wakiigiza mchezo wa kidini (kama vile Mt. 5:20).

☐ "thawabu" Neno hili linapatikana katika Mt. 6:1,2,5,16 na maana "kupokea malipo kamili" (kama vile Flp. 4:18). Biblia inafundisha thawabu lakini katika msingi wa mtazamo wa mwamini, sio matendo yao peke yake (yaani Mt. 7:21-23). Mfanano wa tungo hiyo hiyo katika Mt. 6:2 ilikuwa ni nahau kwa "risiti iliyosainiwa na kupokelewa." Angalia mada maalum katika Mt. 5:12.

**6:2 "kuwapa maskini"** Utoaji ilikuwa namna ya kuwasaidia masikini kwa wiki. Walimu hata wao walifikiria kuwa na sifa za kuokoa (kama vile Tobit 12:8-9; Ecclesiasticus 3:30; 29:11-12).

☐ "usipige panda mbele yako" Hii mara kwa mara imekuwa ikifasiriwa kama kuelezea baragumu lenye vyuma kumi na tatu vya kupulizia katika Hekalu ambapo fedha ziliwekwa (kama vile Luka 21:2). Kila kibakuli kilikuwa na makusudi yake tofauti tofauti yaliyoelezewa. Hata hivyo hakuna ushahidi wa wazi uliopatikana katika fasihi ya Kiyahudi kwa hizi. Hata hivyo inawezekana kuwa mbinu ya mtu kutaka usikivu kwa matendo ya kidini.

☐ "wanafiki" Angalia Mada Maalum inayofuata.

### **MADA MAALUM: WANAFIKI (katika Mathayo)**

Hili neno ambatani (*hupokritēs*) kwa maana iliyo wazi linatafasiriwa "kuhukumu chini ya." Ingalimaanisha (1) kidokezo kwenye neno la kitamthilia kwa ajili ya kuzungumza toka nyuma ya pazia (yaani kuigiza) au (2) matumizi yake ya mwanzo yalikuwa ni "kuhitimisha ufasiri."

Mafarisayo walitenda nje ya utaratibu wa kidini na ibada (mara nyingi hadharani) ili wapate kusifiwa na watu, na sio kumpendeza Mungu (ingawa nina uhakika kuwa ilikuwa ni moja ya sababu):

1. kutoa misaada, sio tu kuwasaidia wahitaji, bali ili wapate kusifiwa na watu, Mt. 6:2
2. wakiomba kwenye Masinagogi na kuomba hadharani ili waonekane mbele za watu, Mt. 6:5
3. walipofunga walionekana kuwa wasio nadhifu ili wengine wapate kuvutiwa na namna walivyo wa kiroho, Mt. 6:16
4. walisema kitu hiki lakini wakitenda kitu kingine (kama vile Mt. 15:7-9; Marko 7:1-7; Isa. 29:13)
5. walijaribu kumkamata Yesu kwa maswali ya mitego, na sio kutafuta hekima ya kweli, Mt. 22:15-22
6. waliwazuia wengine wasiweze kuingia kwenye ufalme, Mt. 23:13-15
7. hulipa zaka za bizari na jira na kuacha mambo makuu ya sheria, Mt. 23:23
8. walisafisha kikombe kwa nje, na sio ndani, Mt. 23:25
9. walikuwa ni makaburi matupu yasiyosafishwa, Mt. 23:27-28 (kama vile *Dictionary of Biblical Imagery*, uk. 415)
10. walikuwa wenye kujihesabia haki, Mt. 23:29-30
11. walikuwa na sehemu maalum huko jehanamu, Mt. 24:51

**NASB** "ili kwamba waheshimiwe na wanadamu"

**NKJV** "kwamba wapewe utukufu kutoka kwa wanadamu"

**NRSV** "ili kwamba wasifiwe na wengine"  
**TEV** "ili kwamba watu wawasifu"  
**NJB** "ili kupata kupendwa na wanadamu"

Mungu anaangalia moyo (kama vile 1 Sam. 16:7; Mith. 21:2; Luka 16:15; Yohana. 12:43; Mdo. 1:24; 15:8; Rum. 8:27; Ufu. 2:23).

**NASB** "hakika nawaambieni,"  
**NKJV** "hakika nakwambieni"  
**NRSV** "hakika, nawaambieni"  
**TEV** "kumbuka hili"  
**JB** "nawaambieni kwa hakika"  
**NJB** "Kwa ukweli nakwambieni"

Kibayana "amina, amina" (kama vile Mt. 6:2, 5, 16), hii ilitumika na Yesu kutambulisha kauli muhimu. Mzizi wa Agano la Kale wa "amina" ni uaminifu, uadilifu au kutegemewa. Hii ilikuwa na kisawe cha, "Ninatoa kauli za uaminifu, sikiliza kiumakini." Angalia Mada Maalum katika Mt. 5:18.

☐ **"wamekwisha pata thawabu yao"** Neno hili "thawabu" linapatikana katika mafunjo ya Kimisri (angalia James Moulton na George Milligan, *The Vocabulary of the Greek Testament*, ukur. 413) ikiashiria posho au mapato. Neno hili linatokea katika Mt. 5:12,46; 6:1,2,5,16.

**6:3** Hii ilikuwa ni nahau ya faragha/usiri. Hii haikukusudiwa iwe kibayana. Ilikuwa ni mwitikio na ulinzi dhidi ya za kidini.

**6:4 "Baba yenu aonaye sirini"** Umuhimu waimani binafsi ya kujitegemea inapatikana katika tumaini binafsi la mwamini katika Mungu. Waamini wanaonesha uhusiano wao binafsi kwa Mungu katika shughuli zisizotazamwa zaidi kuliko zingine (kama vile Mt. 6:6, 18). Mtazamo, sio faragha ni msingi (kama vile Mt. 5:16). Mara kwa mara uwakala wa kifedha inaweza kuwa ushuhuda mkuu, mfano., J. C. Penney na R. G. Letourneau.

## **MADA MAALUMU: LUGHA YA WANADAMU KUELEZEA UUNGU**

- I. Aina hii ya lugha (yaani., Uungu kuelezewa katika maneno ya kibinadamu) ni wa kawaida katika Agano la Kale (baadhi ya mifano)
  - A. Viungo vya mwili
    1. Macho - Mwa. 1:4,31; 6:8; Kut. 33:17; Hes. 14:14; Kumb. 11:12; Zak. 4:10
    2. Mikono – Kut. 15:17; Hes. 11:23; Kumb. 2:15
    3. Viganja – Kut. 6:6; 15:16; Kumb. 4:34; 5:15
    4. Masikio – Hes. 11:18; 1 Sam. 8:21; 2 Fal. 19:16; Zab. 5:1; 10:17; 18:6
    5. Uso – Kut. 33:11; Law. 20:3,5,6; Hes. 6:25; 12:8; Kumb. 31:17; 32:20; 34:10
    6. Vidole – Kut. 8:19; 31:18; Kumb. 9:10; Zab. 8:3
    7. Sauti – Mwa. 3:9,11,13; Kut. 15:26; 19:19; Kumb. 26:17; 27:10
    8. Miguu – Kut. 24:10; Ezek. 43:7
    9. Umbo la mtu – Kut. 24:9-11; Zaburi 47; Isa. 6:1; Ezek. 1:26
    10. Malaika wa Bwana – Mwa. 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16; Kut. 3:4,13-21; 14:19; Amu. 2:1; 6:22-23; 13:3-22

B. Matendo ya mwili (angalia mifano)

1. Kuongea kama moja ya mfumo wa uumbaji- Mwa. 1:3,6,9,11,14,20,24,26
2. Kutembea (yaani., sauti ya)- Mwa. 3:8; Law.26:12; Kumb. 23:14; Hab. 23:14
3. Kufunga mlango wa safina ya Nuhu – Mwa. 7:16
4. kunukia dhabihu – Mwa. 8:21; Law. 26:31; Amo. 5:21
5. kurudi chini – Mwa. 11:5; 18:21; Kut. 3:8; 19:11,18,20
6. maziko ya Musa – Kumb. 34:6

C. Mihemuko ya kibinadamu (baadhi ya mifano)

1. Majuto/toba- Mwa. 6:6,7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:29,35; Amo. 7:3,6
2. Hasira- Kut. 4:14; 15:7; Hes. 11:10; 12:9; 22:22; 25:3,4; 32:10,13,14; Kumb. 6:15; 7:4; 29:20
3. Wivu - Kut. 20:5; 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15; 32:16,21; Yosh. 24:19
4. Karaha/chuki- Law. 20:23; 26:30; Kumb. 32:19

D. Maneno ya kifamilia (baadhi ya mifano)

1. Baba
  - a. Wa Israeli- Kut. 4:22; Kumb. 14:1; Isa. 1:2; 63:16; 64:8; Yer. 31:9; Hos. 11:1
  - b. Wa Wafalme- 2 Sam. 7:11-16; Zab. 2:7
  - c. Sitiari za vitendo vya kibaba- Kumb. 1:31; 8:5; 32:6-14; Zab. 27:10; Mith. 3:12; Yer. 3:4,22; 31:20; Hosea 11:1-4; Mal. 3:17
2. Mzazi – Hosea 11:1-4
3. Mama- Isa. 49:15; 66:9-13 (mshabihiano wa unyonyeshaji wa mama)
4. Kijana mpendwa mwaminifu-Hosea 1-3

II. Sababu za kutumia aina hii ya lugha

- A. Ni muhimu kwa Mungu kujidhihirisha mwenyewe kwa mwanadamu. Hakuna misamiati mingine kuliko ile ya maneno ya kiulimwengu, ulioanguka. Dhana iliyosambaa ya Mungu kuwa wa jinsia ya kiume ni mfano mmoja wa lugha ya kumwelezea binadamu kwa sababu Mungu ni Roho!
- B. Mungu anachukulia dhana ya maana halisi ya maisha ya mwanadamu na kuwatumia ili kujidhihilisha mwenyewe kwa mwanadamu aliyeanguka (Baba, Mama, Wazazi, Wapendwa)
- C. Ingawa ni muhimu kwa wakati mwingine (yaani., Mwa. 3:8), Mungu hahitaji kuwekewa pingamizi kwa aina yeyote juu ya umbo la kibinadamu (kama vile Kut. 20; Kumbu. 5)
- D. Hatima ya Mungu kuelezewa kama mtu ni kubadilika kwa Yesu katika umbo la kibinadamu! Mungu akawa mtu, mwenye kugusika (kama vile Yohana 1:1-18).

III. kwa umakinika wa maelezo, angalia G. B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible*, ukurasa 10, "Tabia ya mwanadamu kwa Mungu," katika *The International Standard Bible Encyclopaedia*, kurasa za. 152-154

☑"atawajzeni" Neno la Kiyunani "kwa uwazi" linapatikana katika toleo la NKJV katika Mt. 6:4,6, na 18. Maandiko ya kale ya Kiyunani ya K, L, & W, na maandiko ya Kiyunani yaliyotumika na Chrisostom inaongeza "kwa uwazi" hapa katika Mt. 6:6 na 18. Neno hili halitokei katika maandiko makubwa ya kale ya Kiyunani, α, B, D, Z; wala maandiko ya Kiyunani yatumikayo na Origen, Cyprian, Jerome, au Augustine. Toleo la UBS<sup>4</sup> inatoa maandiko mafupi alama ya "B" (karibia na hakika).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 6:5-15**

<sup>5</sup>Tena msalipo, msiwe kama wanafiki; kwa maana wao wapenda kusali hali wamesimama katika masinagogi na katika pembe za njia, ili waonekane na watu. Amin, nawaambia, Wamekwisha kupata thawabu yao.

<sup>6</sup>Bali wewe usalipo, ingia katika chumba chako cha ndani, na ukiisha kufunga mlango wako, usali mbele za Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi. <sup>7</sup>Nanyi mkiwa katika kusali, msipayuke-payuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi.

<sup>8</sup>Basi msifanane na hao; maana Baba yenu anajua mnyohitaji kabla ninyi hamjamwomba. <sup>9</sup>Basi ninyi

salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni,  
 Jina lako litukuzwe,  
 Ufalme wako uje,  
<sup>10</sup>Mapenzi yako yatimizwe,  
 hapa duniani kama huko mbinguni.  
<sup>11</sup>Utupe leo riziki yetu. <sup>12</sup>Utusamehe deni zetu,  
 kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu.  
<sup>13</sup>Na usitutie majaribuni,  
 lakini utuokoe na yule mwovu.  
 [Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu,  
 hata milele. Amina.] <sup>1</sup>  
<sup>4</sup>Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao,  
 na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi.  
**15 Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu.**

**6:5 "wao wapenda kusali hali wamesimama katika masinagogi"** Mkao wa kawaida uliozoeleka kwa maombi ya Wayahudi ilikuwa ni kusimama mikono na sura ikiwa imeinuliwa mbinguni na macho yakiwa wazi. Jambo sio nafasi ya mwili bali mtazamo wa moyo wa kidini.

☐**"katika pembe za njia"** Wayahudi wa Yerusalemu wakati wa Yesu waliomba mara tatu kwa wakati fulani wakati wa mchana. Muda wa pili kati ya muda huu ulikuwa ni wa saa 3 na saa 9 mchana. Wakati dhabihu fulani (kwa kuendelea) zikitolewa katika hekalu; kwa nyakati hizi waliongeza mchana uliosogea zaidi. Baadhi ya viongozi wajihebiao haki walipanga kujikuta wenyewe hadharani, sehemu zilizobanana kwa nyakati hizi zilizowekwa ili kwamba wote waweze kuona kujitoa kwao.

☐**"ili waonekane na watu"** Hii kibayana ni "kuangaza mbele za watu." Waamini wanaonywa kuacha nuru zao kuangaza mbele za watu lakini kusudi ni kwamba Mungu na sio wao wenyewe watukuzwe (kama vile Mt. 6:2; 5:16 na Yohana. 12:43; Flp.2:15). Angalia [MADA MAALUM: WANAFIKI](#) katika Mt. 6:2.

☐**"Hakika"** Angalia Mada Maalum katika Mt. 5:18.

6:6

NASB	"ingia katika chumba chako cha ndani"
NKJV, NRSV	"nenda chumbani mwako"
TEV	"nenda chumbani mwako"
NJB	"nenda katika chumba chako cha ndani"

Hii inarejerewa kama chumba cha kuhifadhia vitu (kama vile Luka 12:24). Hii ilikuwa ni kutoka katika neno la Kiyunani ambayo kiasili ilimaanisha "kukata," ambayo ilimaanisha kutenganisha au kukata sehemu (kama vile Mt. 24:26; Luka 12:3). Hiki kingekuwa chumba pekee chenye mlango.

## **MADA MAALUM: "MLANGO" KATIKA AGANO JIPYA**

Agano Jipya linatumia "mlango" katika namna kadhaa.

1. kibayana
  - a. ya nyumba, Mt. 6:6; Marko 1:33; 2:2; 11:7, chumba cha juu, Yohana 20:19,26

- b. ya hekalu, Mdo. 3:2; 21:30
  - c. ya gereza, Mdo. 5:19,23; 12:6; 16:26-27
  - d. ya kaburi, Mt. 27:60; 28:2; Marko 15:46; 16:3
  - e. ya zizi la kondoo, Yohana 10:1,2
  - f. ya mahakama, Yohana 18:16; Mdo. 12:13
2. kisitari
    - a. ukaribu wa muda, Mt. 24:33; Marko 13:29; Mdo. 5:9; Yakobo 5:9
    - b. vikwazo kwa kuingia katikia imani ya kweli, Mt. 7:13-14; Luka 13:24; Ufu. 3:20
    - c. nafasi ya imani iokoayo waliopotea, Mt. 25:10; Luka 13:25; Ufu. 3:7
    - d. nafasi ya imani iokoayo, Mdo. 14:27; Ufu. 3:7
    - e. nafasi kwa ajili ya huduma, 1 Kor. 16:9; 2 Kor.2:12; Kol. 4:3; Ufu. 3:8
    - f. ufunuo, Ufu. 4:1; 19:11
  3. cheo kwa Yesu, Yohana 10:7,9

**6:7**

**NASB** "marudio rudio yasiyo na maana"

**NKJV** "marudio marudio matupu"

**NRSV** "kuwa na marudio rudio matupu yasiyo na maana"

**TEV** "maneno mengi yasiyo na maana"

**NJB** "kuongea bila kutoa maana"

Neno hili linatumika hapa tu katika Agano Jipya. Maana yake haijulikani. Tazama utofauti katika matoleo ya Kingereza yalivyofasiri hili! Yesu na Paulo walirudia rudia maombi (kama vile Mt. 26:44; 2 Kor. 12:8). Yawezekana fasiri "maneno yasiyoikuwa na maana" ni bora zaidi. Kwa mifano inayowezekeka ya kibiblia ya matumizi ya maombi ya kiruturujia, angalia 1 Wafalme. 8:26 na Mdo. 19:34. Suala sio mara ngapi mtu anarudia maneno bali moyo unaoamini mwaminifu/unaotumaini wa mwaminio.

**6:8 "ninyi"** Katika muktadha hiiki kiwakilishi cha huruma kinakinzana na makundi mawili: (1) wapagani wa Mt. 6:7 au (2) wanasheria wa kifarisayo wa Mt. 6:5.

## **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA MISTARI YA 9-15**

- A. Mfano huu ulikuwa wa kwanza kupewa jina "Sala ya Bwana" na Cyprian, 250 B.K. Hata hivyo maombi yalikuwa kwa ajili ya wanafunzi wa Yesu, "Maombi ya Mfano," ni sifa za kitabia nzuri zaidi.
- B. Maombi ya Mfano yanaundwa na tungo saba. Za kwanza tatu zinahusiana na Mungu. Za mwisho nne zinahusiana na hitaji la mtu.
- C. Maombi haya yawezekana yalikuwa kufanyia kazi upya kwa Yesu Amri Kumi kwa siku zake. Heri pia yawezekana pia zilihusiana na Amri Kumi (Amri Kumi). Mathayo alimchukulia Yesu kama Musa wa pili. Paulo alitumia aina ile ile ya masimulizi ya Agano la Kale kwa kumrejerea Yesu kama Adamu wa pili (kama vile Rum. 5:12-21; 1 Wakorintho 15; Flp. 2:6-11).
- D. Maombi ya mfano yanaelezwa katika kauli shurutishi. Ni mifano ya kauli shurutishi za kusihhi. Hatumwamuru Mungu.
- E. Toleo la Luka ni fupi zaidi. Linapatikana katika Mt. 11:2-4 na sio Mahubiri ya Mlimani, Mathayo 6, ambayo yanafanana na Mathayo 5-7. Wimbo wa kumsifu Mungu ambao una mkanganyiko kimaandiko wa Mt. 6:13b pia unakosekana katika toleo la Luka.

6:9

**NASB, NRSV** "Ombeni sasa kwa namna hii"  
**NKJV** "kwa namna hii, ombeni"  
**TEV** "hivi ni namna mnavyotakiwa kuomba"  
**NJB** "hivyo muombe hivi"

"Omba" ni kauli shurutishi ya wakati uliopo ambayo ni amri ya mtindo wa maisha ambayo inaashiria kitendo cha kitabia kinachoendelea. Maombi haya yalimaanisha kuwa mfano, sio lazima kuweka muundo. Upana na mtazamo wa maombi yana umuhimu zaidi sana kuliko maneno ya kawaida. Hii inaweza kufafanuliwa kwa ukweli kwamba toleo la Luka katika Mt. 11:2-4 ni tofauti. Yesu inawezekana kuwa alikuwa amefundisha maombi haya mara kwa mara lakini kwa utofauti kidogo.

☐ **"yetu"** Maombi haya kwa kusanyiko lililokusanyika, na pia maombi binafsi. Tu familia ya *Abba* mmoja, Baba! Kwa ufahamu huu, Mt. 6:14-15 inaleta maana zaidi.

☐ **"Baba"** Baba hairejerei kuzaliwa kwa njia ya ngono au mfuatano wa namna hiyo bali uhusiano wa karibu sana katika nyumba ya Kiyahudi. Historia ya Nyuma ya Agano la Kale ni Kumb. 32:6, Zab. 103:13, Isa. 63:16, Mal. 2:10, na 3:17. Dhana hii ya Mungu kama Baba haikuwa maudhui kubwa katika Agano la Kale wala katika maandiko ya walimu wa Kiyahudi. Inashangaza kwamba waaminio wanaweza kumuita YHWH "Baba" (kama vile Rum. 8:15) Katika uhusiano wao wa kiimani na Yesu! Angalia Mada Maalum katika Mt. 5:16.

**6:9-10 "utukuzwe. . . uje. . . yafanyike"** Hizi zote ni kauli shurutishi za wakati uliopita usio timilifu. Pia zinawekwa zote katika sentensi ya Kiyunani kwa ajili ya msisitizo. Kuweka, njeo na hali vyote vinazungumzia juu ya uharaka na msisitizo. Hii ni namna waamini wanatakiwa kumuheshimu Mungu. Tungo "hapa duniani kama mbinguni" inarejerea vitenzi hivi vyote vitatu.

☐ **"utukuzwe"** Neno linatokea katika mzizi "takatifu" (kama vile Ebr. 10:29) na kumaanisha "kuheshimu," "kuheshimika," au "kuchukuliwa kwa heshima kubwa." Kitenzi kinatoka katika sentensi ya Kiyunani kwa ajili ya msisitizo. Kitenzi hiki kinapatikana katika Vitabu vyta injili mara nne tu (kama vile Mt. 6:9; 23:17,19; Luka 11:2).

**6:9 "jina"** Hii ilisimama kwa ajili ya tabia na hulka ya Mungu (kama vile Ezek. 36:22; Yoeli 2:32). Jina lake linatakiwa kufanywa lijulikane katika ulimwengu huu ulioanguka kwa utii wa watoto wa Mungu (kama vile Isa. 29:23).

**6:10 "ufalme wako uje"** Mungu alikuwa anaalikwa katika wadhifa wake kama mfalme. Haya yalikuwa ni maombi kwa ajili ya Mungu kushughulikia mambo ya duniani kama anavyoshughulikia mambo ya mbinguni. Ufalme wa Mungu ulielezwa katika Agano Jipya kama vyote (1) ukweli wa sasa (kama vile Mt. 4:17; 12:28; Luka 17:21) na (2) kuhitimishwa kunakokuja (kama vile Mt. 6:10; 13:2 na kuendelea; Luka 11:2; Yohana.18:36). Kauli hii inaelezea ukinzani wa utawala wa Mungu ambao utahitimishwa kwa ujio wa mara ya pili lakini kwa sasa katika maisha ya wanafunzi wa kweli. Angalia Mada maalum katika Mt. 4:17.

**6:11 "utupe"** Kama marudio matatu ya kwanza yanashughulikia namna gani waamini wanatakiwa kumuheshimu Mungu, yale mengine manne yanashughulikia namna anataka kumtendea Mungu.



☐ **"leo"** Mungu anataka watoto Wake waishi kwa imani katika Yeye kila siku. Mfano mmoja wa Agano la Kale ulikuwa kwamba Manna ilitolewa kila siku (kama vile Kut. 16:13-21). Katika Mashariki ya Kati mkate uliokuwa mapema sana kila siku na aidha uliwe au uanikwe uwe mgumu uliwe jioni. Mikate ya leo haiwezi ikawa na maana kwa kesho.

☐ **"kila siku"** Hili lilikuwa ni neno nadra la Kiyunani. Lilitumika

1. Katika mafunjo ya misri ya Bwana akimpa mtumwa chakula cha kutosha ili aweze kutimiza jukumu lake alilopangiwa
2. yawezekana nahau ya Kiyunani "kwa ajili ya chakula muhimu kwa leo" ("mkate kwa uhitaji wetu")
3. toleo la Tyndale *Commentary on Matthew* lina "Tupatie nguvu muhimu ili kwamba majaribu ya maisha yasituchukue katika majaribu ya kiroho," ukur. 74.

Tertullian alifasiri hili "kila siku." Neno lilitumika katika Agano Jipya na katika ufanano katika Luka 11:3.

☐ **"mkate"** uwezekano kadhaa wa namna gani "mkate" inavyotakiwa kueleweka.

1. mkate wa kawaida
2. Karamu ya Bwana (kama vile Mdo. 2:46)
3. Neno la Mungu, Biblia (kama vile Mt. 4:4; Luka 4:4)
4. Neno linaloishi, Yesu (kama vile Yohana 6:41,48,51,55)
5. karamu ya Kimasihi (kama vile 14:15)

Uchaguzi mmoja unashabihiana zaidi na muktadha. Hata hivyo inawakilisha utoaji wa Mungu kwa mahitaji yote ya maisha.

## 6:12

NASB, NRSV,

NJB "msamehe"

NKJV, TEV "samehe"

Kuna maandiko ya Kiyunani tofauti kwa sehemu hii yanayohusiana na njeo ya matumizi ya pili ya kitenzi, "sameheni." Kauli ya wakati uliopita usiotimilifu inapatikana katika MSS,  $\alpha^*$ , B, Z, Vulgate, na Peshitta. Matoleo mengine yote ya MSS ya Kiyunani na matoleo ya kale yana wakati uliopo. Neno lilimaanisha "kutoa" au "kuondoa," vyote ambavyo vinaelezea sitiari za Agano la Kale zinazohusiana na msamaha.

☐ **"deni"** Ufanano katika Luka 11:4 una "dhambi." Dini ya Kiyahudi ya Karne ya kwanza walitumia "makosa" (*opheilēmata*) kama nahau kwa ajili ya "dhambi" (*hamartias*). Katika Mt. 6:14-15 neno lingine linatumika, "makosa" (*paraptōmata*). Vyote hivi vinarejerea uasi dhidi ya Mungu. Dhambi zinatuweka katika uasi dhidi ya Mungu wa haki na utakatifu. Kuna gharama ya kulipwa kwenye uasi!

☐ **"kama tunavyowasamehe wadeni zetu"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliopita usio timilifu. Kama Mungu anavyowasamehe waamini nao wanaweza kusamehe wengine (kama vile Mt. 18:35)! Ishara moja ya uhusiano wetu pamoja na Mungu kupitia Kristo ni kwamba tunaanza kuyaiga matendo Yetu.

## 6:13

NASB, NKJV "usitutie majaribuni"

NRSV "usitufikishe katika majira ya majaribu"

**TEV** "usitulete katika majaribu magumu"  
**NJB** "usitutie majaribuni"

Hii ni kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopita usio timilifu. Hii tungo ya kinahau ilimaanisha "hata usijaribu kuanza kitendo." Kumekuweko na mjadala mkubwa kuhusu mstari huu ukilinganishwa na Yakobo 1:13, juu ya usaidizi wa Mungu katika majaribu. Kuna mbinu juu ya visawe vya maneno ya Kiyunani ikifasiriwa "jaribu" au "jaribu." Hii hapa na katika Yakobo 1:13 ina kisawe cha majaribu kwa ajili ya kusudi la kuharibu [*peirasmo*]; kingine kina kisawe kwa ajili ya majaribu kwa ajili ya makusudi ya kuimarisha [*dokimazo*]. Mungu hajaribu waaminio ili kwamba awaharibu bali kuwaimarisha. Angalia Mada maalum katika Mt. 4:1.

Yawezekana hii ilirejerea majaribu makali sana ya kupita kiasi ya kisheria yaliyoletwa na serikali kipindi hicho (kama vile Mt. 26:41; Marko 13:8). C. C. Torrey katika *The Four Gospels*, ukur. 12, 143. Inafasiriwa kama "tulinde na kuangukia katika majaribu" (kama vile Luka 22:40).

**NASB** "kutoka maovuni"  
**NKJV, NRSV,**  
**JB** "mbali na yule muovu"  
**TEV, NJ** "mbali na Yule muovu"

Haiwezekani kisarufi kuamua ikiwa neno hili lilikuwa na jinsi ya kiume (angalia Mada Maalum katika Mt. 4:5) au isiyo na jinsi. Muundo huu huu unarejerea kwa shetani katika Mt. 5:37, 13:38, na Yohana. 17:15. Muundo wa utata huu huu unaonekana katika Mt. 5:37; 6:13; 13:19,38; Yohana. 17:15; 2 Thes. 3:3; 1 Yohana. 2:13,14; 3:12; 5:18-19.

■ Wimbo wa kumsifu Mungu wa mstari wa 13b haupatikani katika (1) ufanano wa Luka 11:2-4; (2) maandiko ya kale ya Kiyunani,  $\alpha$ , B, D, au (3) fasiri za Origen, Cyprian, Jerome, au Augustine. Kuna miundo kadhaa ya nyimbo hizi za kumsifu Mungu za Mathayo. Inawezekana iliongezwa kutoka 1 Nyak. 29:11-13 kama Sala ya Bwana ilivyoanza kutumika katika njia za kiruturujia na kanisa la Kwanza. Haikuwa halisi. Liturujia ya Wakatoliki wa Rumi inaliondoa kwasababu halipo katika Vulgate. A. T. Robertson aliweka maoni yake katika andiko hili katika *Word Pictures in the New Testament*, "Wimbo wa kumsifu Mungu unawekwa pembezoni mwa toleo lililorejerewa. Linatakikana katika maandiko ya kale na yaliyo bora ya Kiyunani. Miundo ya kale inatofautiana sana, baadhi ni fupi, ingine ni ndefu kuliko ingine katika toleo lililoidhinishwa. Matumizi ya wimbo wa kumsifu Mungu yaliinuka wakati maombi haya yalipoanza kutumika kama liturujia kurudiwa rudiwa au kuimbwa hadharani. Haikuwa sehemu asili ya Sala ya Mfano kama ilivyotolewa na Yesu," ukur 55. Toleo la UBS<sup>4</sup> inaweka alama ya uondaji kama "A" (hakika).

**6:14-15** Mistari 14-15 ni hitimisho la Maombi ya mfano. Hayaelezei kwamba matendo yetu yanatuletea wokovu wetu bali wanatakiwa kutoa ushahidi wa wokovu wetu (sehemu ya pili ya sentensi ya daraja la tatu lenye masharti). Sio msingi bali matokeo (kama vile Mt. 5:7; 18:35; Marko 11:25; Luka 6:36-37; Yakobo 2:13; 5:9) Tunapokuwa tukiomba maombi haya, "Baba yetu," lazima tuishi ukweli huu tunaoujua katika kuhusiana na ndugu zetu wa kiagano.

**6:14 "makosa"** Hii ni kibayana "kuanguka upande mmoja." Hii ilimaanisha kama ilivyo kwa maneno mengi kwa ajili ya dhambi katika Kiebrania na Kiyunani, kutoka nje kidogo ya toleo usanifishwaji ambayo ni tabia ya Mungu. Iliimaanisha tendo lililofanywa kwa hali ya kujitambua la kuvuka mipaka iliyowekwa.

## ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 6:16-18

<sup>16</sup>Tena mfungapo, msiwe kama wanafiki wenye uso wa kukunjamana; maana hujiumbua nyuso zao, ili waonekane na watu kuwa wanafunga. Amin, nawaambia, wamekwisha kupata thawabu yao. <sup>17</sup>Bali wewe ufungapo, jipake mafuta kichwani, unawe uso; <sup>18</sup>ili usionekane na watu kuwa unafunga, ila na Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi.

**6:16-18** Kuna mifano iliyoongezwa ya maonesho ya kidini. Angalia [MADA MAALUM: WANAFIKI](#) katika Mt. 6:2.

**6:16 "mfungapo"** Kulikuwa na siku moja tu ya Upatanisho ambayo inatajwa kidhahiri katika Agano la Kale (kama vile Law. 16), ambalo lilikuwa likiangaliwa katika mwezi wa 7. Viongozi wa Kiyahudi waliteua siku za nyongeza za kufunga kwa ajili ya kufunga nyakati fulani za hatari katika historia ya kitaifa ya Israeli (kama vile Zek. 7:3-5; 8:19). Kwa nyongeza walimu wa kiyahudi waliongeza nyakati za kufunga mara mbili kwa wiki, Jumatatu na Alhamisi (Luka 18:12); Alhamisi kwasababu hiyo ilikuwa ni siku walisema Musa alikwenda Mlima Sinai, Jumatatu. Walitumia mifungo hii kama namna ya kuonesha kiroho chao.

## MADA MAALUM: KUFUNGA

Kufunga, ingawa hakujaamriwa katika Agano Jipya, kulitarajiwa katika wakati muafaka kwa ajili ya wanafunzi wa Yesu (kama vile Mt. 6:16,17; 9:15; Marko 2:19; Luka 5:35). Kufunga kunakostahili kunapatikana katika Isaya 58. Yesu alijiweka mwenyewe kuwa wa mfano (kama vile Mt. 4:2). Kanisa la mwanzo lilifunga (kama vile Mdo. 13:2-3; 14:23; 2 Kor. 6:5; 11:27). Mienendo na tabia ni vya muhimu; kwenda na wakati; umbali na jambo kutokea ni la kiuchaguzi. Kufunga katika agano la kale sio sharti la waamini wa Agano Jipya (kama vile Mdo. 15:19-29). Kufunga sio njia ya ya kuonyesha u-kiroho cha mtu (kama vile Isaya 58; Mt. 6:16-18), lakini ni njia ya kumsogeza mtu karibu na Mungu na kuhitaji mwongozo wake (yaani., Yesu, Mt. 4:2). Yaweza kuwa ni msaada wa kiroho.

Tabia ya kanisa la mwanzo dhidi ya uwazi ulisababishwa na waandishi walioingiza neno "kufunga" katika sura mbali mbali (yaani., Mt. 17:21; Marko 9:29; Mdo. 10:30; 1 Kor. 7:5). Kwa ajili ya maelezo zaidi juu ya ya maandiko haya yenye maswali mwone Bruce Metzger's *A Textual Commentary on the Greek New Testament*, kilichochapishwa na United Bible Societies.

☐ **"uso mg'avu"** Neno hili linatokea hapa tu na Luka 24:17.

☐ **"hakika"** Angalia Mada Maalum katika Mt. 5:18.

**6:17** Huu ni ukweli ule ule wa mstari wa 6. Mukstadha ni maonesho ya kidini. Maisha yetu ya kiroho kimsingi yanatakiwa kuonekana na Mungu! Tunatafuta kutambuliwa nae wala sio kutambuliwa na wanadamu.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini Yesu alichagua maeneo haya matatu ya uharibifu (kusaidia wahitaji, maombi, na kufunga) ili ayahukumu?

2. Ni maeneo gani tunayoyatumia katika siku zetu kwa namna ile ile?
3. Kwanini mtazamo wa mtu ni muhimu zaidi kuliko matendo yake?

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA MISTARI YA 19-24

- A. Kweli za sehemu hii zinarudiwa katika Injili ya Luka lakini katika mazingira tofauti tofauti.
  1. wanadamu lazima watunze hazina zao mbinguni (Luka 12:33-34)
  2. jicho ni taa ya mwili (Luka 11:34-36)
  3. wanadamu hawawezi kuwatumikia mabwana wawili (Luka 16:13)
  4. Utoshelevu wa Mungu kwa asili unafanyika kama mfano wa utoaji wa Mungu kwa watu (Luka 12:22-31)

Yesu alirudia mafundisho Yake kwa makundi tofauti tofauti na akitumia masimulizi yale yale kwa mazingira tofauti tofauti.
- B. Yesu alitumia asili kufundisha kuhusu Mungu: (1) vitu vyote vi vya Mungu na (2) wanadamu ni muhimu zaidi kuliko vitu au wanyama.
- C. Sehemu hii lazima ieleweke kwa namna ya kiubayana. Kumiliki mali za duniani sio kuwa muovu bali ni kukosea kwa vipaumbele vya umiliki kitu kinachoweza kupelekea uovu (kama vile 1 Tim. 6:10). Mashaka yasiyozaa faida kuhusu mahitaji ya kawaida ya maisha yanaonesha kukosekana kwa imani katika kujali na utoaji wa Mungu (kama vile Flp. 4:6). Kutumaini ni jambo la msingi.
- D. Sehemu hii ya maandiko inaweza kugawanywa katika muktadha tatu zilizo na uhusiano: (1) Mt. 6:19-21; (2) Mt. 6:22-24; na (3) Mt. 6:25-34. Ufanano huu wa sawa na kile walimu wa kiyahudi wanachoita "lulu katika kamba," ambacho kilimaanisha masomo kadhaa yasiyohusiana yanashughulikiwa kwa ukaribu sana.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 6:19-23

<sup>19</sup>Msijiwekee hazina duniani, nondo na kutu viharibupo, na wevi huvunja na kuiba; <sup>20</sup>bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusikoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wevi hawavunji wala hawaibi; <sup>21</sup>kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako. <sup>22</sup>Taa ya mwili ni jicho; basi jicho lako likiwa safi, mwili wako wote utakuwa na nuru. <sup>23</sup>Lakini jicho lako likiwa bovu, mwili wako wote utakuwa na giza. Basi ile nuru iliyomo ndani yako ikiwa giza; si giza hilo!

**6:19 "msijiwekee hazina"** Hii ni kibayana "acha kuweka hazina." Matumizi haya haya pia yanapatikana katika Mt. 6:20. Hii ni kauli shurutishi ya wakati uliopo ikiwa na kiambata kanushi. Shauku ya mwanadamu aliyeanguka ni kujaribu kuzalisha kwa namna yoyote ya mali zalke mwenyewe kwa mambo yote yanayohitajika kwa ajili ya furaha yake. Tungo za kisarufi hapa inaonesha kwamba hii pia ni jaribu kwa mwanadamu aliyeanguka. Furaha ya kweli na mafanikio yanapatikana tu katika kumtegemea Mungu na kuridhika katika kile anachotupatia (kama vile Muh. 1-2; 2:24-25; 3:12,22; 5:18; 8:15; 9:7-9; Flp. 4:11-12).

☐ **"hazina"** Katika ulimwengu wa kale mali ilipanda kutoka katika vyanzo vitatu: (1) nguo, (2) chakula, na (3) madini na vito vya thamani. Kila moja ya vitu hivi vinaweza kuharibiwa au kuibiwa. Wadudu watashambulia mavazi. Kutu inatoka katika mzizi "kula" au kisitari "kumaliza kwa kula" au "kuteketea" na ilitumika na wadudu walao chakula. Kimsingi vyote hivi vinamaanisha kwamba umiliki wetu wote wa duniani upo hatarini. Ikiwa furaha ya mtu inategemea umiliki wa mali, mtu anaweza kupoteza wakati wowote. Dhana ya uongo kwamba kuridhika na furaha vinapatikana katika vitu vya mwilini inatajwa katika Luka 12:15.

☉"**huharibu**" Neno hili lilimaanisha "kutoa katika umbo lake" (Mt. 6:16), "kusababisha kupotea" (kama vile Mt. 6:20, Mdo. 13:41; Yakobo 4:14).

☉"**wezi huvunja na kuiba**" Neno "kuvunja" kibayana ilimaanisha "kuchimba ndani. Nyumba nyingi wakati wa kipindi hiki zilikuwa ni za tope katika kuta zake. Katika lugha ya Kiyunani, neno kwa "mwizi" lilikuwa linatoka katika neno ambatani "mchimba tope."

**6:20 "bali jivekeeni hazina mbinguni"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo kimsingi ikirejerea mtazamo wa kiroho na matendo. 1 Timotheo 6:17-19 kwa uzuri inaelezea dhana hii hii. Mungu mwenyewe analinda hazina zetu za mbinguni (kama vile. 1 Pet. 1:4-5).

Kitenzi katika mstari wa 20 unatoka katika mzizi ule ule kama nomino (shamirisho kihusishi). Kibayana hii mbinu ya maneno ingekuwa "jivekeeni hazina zenu mbinguni."

**6:21 "kwakuwa hazina zenu zilipo ndipo moyo wako utakapokuwepo"** Ni muhimu kwamba kiwakilishi cha wingi ambacho kimetumika katika mistari iliyopita sasa kinabadilika kuwa umoja. Sehemu hii inafundisha mabadiliko ya vitu vya duniani na umilele wa vitu vya kiroho. Pia inahamasisha kwamba ambapo mtu anaweka mapenzi yake na mali na nguvu kiukweli anafunua vipaumbele vyake. Moyo (nahau ya Kiebrania) ni kituo cha mtu. Kinaelezea ujumla wa mtu.

**6:22 "jicho ni taa ya mwili"** Historia ya nyuma ya kauli hii ilikuwa ni dhana ya Kiyahudi ya jicho kuwa dirisha au mlango wa nafsi. Kile ambacho mtu anaruhusu katika maisha yake ya mawazo kinaamuru yeye alivyo. Mawazo yanazalisha shauku, shauku inazalisha matendo, matendo yanamfunua mtu.

**6:22-23** Mistari hii miwili ni kwa dhahiri inazungumza ukinzani. Ukinzani ulielezwa kwa maneno: "wema" dhidi ya "ubaya"; "umoja" dhidi ya "mara dufu"; "ukarimu" dhidi ya "uchoyo"; au "afya" dhidi ya "kapatwa na ugonjwa." Jicho lilitumika kwasababu ya umuhimu pekee wa utoaji wa nuru kiafya dhidi ya kupoteza uono au uono hafifu wa macho unaoletwa na magonjwa ("ikiwa"). Mbili za kwanza ni sentensi daraja la kwanza yenye masharti ambayo inazungumzia juu ya kitendo kinachowezekana kutendeka. Kuna wale ambao kwa uwazi wanaona kweli za kiroho na wale ambao kwa habari za mambo ya kiroho wamepofuka.

Ile "ikiwa" ya mwisho ni sentensi daraja la kwanza yenye masharti ambayo inaweka sifa ya vipofu wanaodhani wanaona!

### **MADA MAALUM: UKARIMU/UKWELI (*haplotēs*)**

Neno hili (*haplotēs*) lina vidokezo viwili, "ukarimu" au "ukweli." Ni sitiari iliyohusiana na maono. Katika Agano la Kale jicho lilitumika kama sitiari kwa ajili ya kusudi katika njia mbili.

1. Jicho baya (bahili, kama vile Kumb. 15:9 na Mith. 23:6; 28:22)
2. Jicho jema (wema, kama vile Mith. 22:9)

Yesu alifuatisha matumizi haya (kama vile Mt. 6:22-23; 20:15).

Paulo alilitumia neno hili kwa maana mbili.

1. "urahisi, uaminifu, usafi" (kama vile 2 Kor. 1:12; 11:3; Efe. 6:5; Kol. 3:22)
2. "ukarimu" (kama vile Rum. 12:8; 2 Kor. 8:2; 9:11,13)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 6:24**

<sup>24</sup> Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia huyu, na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu, na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali.

**6:24 "Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili"** Hii inaweka ulimwengu katika uharaka wa uhalisia. Huku ni kupunguza maisha ya ukweli kuwa uamuzi tu wa kawaida. Wanadamu si kwamba wako huru tu. Wanatumikia bwana mmoja kati ya wawili (kama vile 1 Yohana. 2:15-17).

☐ **"atamchukia huyu, na kumpenda huyu; ama"** Haya yako katika uhusiano wa ufanano. Maneno ya Kiebrania "chuki" na "upendo" yalikuwa nahau kwa ulinganifu (kama vile Mwa. 29:30, 31, 33; Mal. 1:2-3; Mt. 21:15; Luka 14:26; Yohana. 12:25, na Rum. 9:13). Hairejerei kwa chuki katika namma ya kiasili lakini katika kuweka vipaumbele.

**NASB, NRSV** "huwezi ukamtumikia Mungu na mali"  
**NKJV** "huwezi ukamtumikia Mungu na mali"  
**TEV** "huwezi ukamtumikia Mungu na mali kwa pamoja"  
**NJB** "huwezi ukawa mtumwa wa Mungu na mali kwa pamoja"

Neno "mali" lilitoka katika mzizi wa Kiebrania "kuweka hazina" au kuweka tumaini." Kiasili ilikuwa ikitumika kuashiria mtu kuweka tumaini lake kwa mwingine kwa kuwekeza fedha yake kwake. Ilikuwa kuwa na maana "kile ambacho mtu alikutumaini." Inaonekana kuweka mkazo wa kitu ambacho mtu anakiona usalama wake wa mbeleni. A. T. Robertson alielezea kwamba neno hili lilitumika na Washamu kwa jina la mungu wa fedha. Ingawa hii ingekataliwa na wanazuoni hivi karibuni, bado inaonekana kuwa na mantiki kimasimulizi. William Barclay, katika chapisho lake *Daily Study Bible*, juu ya Mathayo, vol. 1 ukr. 252, anaelezea kwamba katika ulimwengu wa mediterania ya kale fedha ilikuja kutamkwa na herufi kubwa ya "M," kama njia ya kuelezea uungu.

Fedha yenyewe sio tatizo bali kipaumbele cha fedha (kama vile 1 Tim. 6:10). Janga la fedha ni kwamba hatujawahi kuwa nayo ya kutosha na mara huwa yenyewe ndio inatumiliki badala ya sisi kuimiliki. Kadiri tunavyokuwa nayo, ndivyo tunavyozidi kuhofu juu ya kuipoteza na hivyo tinamalizwa na kuilinda kwetu. Angalia Mada Maalum hapa chini.

**MADA MAALUM: WINGI WA MALI**

- I. Mtazamo wa kitabu cha Agano la Kale kwa ujumla
  - A. Mungu ndiye mmiliki wa vitu vyote
    1. Mwanzo 1-2
    2. 1 Nyakati 29:11
    3. Zaburi 24:1; 50:12; 89:11
    4. Isaya 66:2
  - B. Wanadamu ni wasimamizi wa mali kwa ajili ya makusudi ya Mungu
    1. Kumbukumbu 8:11-20
    2. Mambo ya Walawi 19:9-18
    3. Ayubu 31:16-33
    4. Isaya 58:6-10
  - C. Wingi wa mali ni sehemu ya ibada
    1. zaka za aina mbili
      - a. Hesabu 18:21-29; Kumb. 12:6-7; 14:22-27

- b. Kumb. 14:28-29; 26:12-15
    - 2. Mithali 3:9
  - D. Wingi wa mali huonekana kama zawadi kutoka kwa Mungu kwa ajiri ya agano la uaminifu
    - 1. Kumbukumbu 27-28
    - 2. Mithali 3:10; 8:20-21; 10:22; 15:6
  - E. Onyo dhidi ya mali katika kuwagharimikia wengine
    - 1. Mithali 21:6
    - 2. Yereimia 5:26-29
    - 3. Hosea 12:6-8
    - 4. Mika 6:9-12
  - F. Wingi wa mali sio dhambi kuwa nayo isipokuwa ikiwekwa kama kipaumbele
    - 1. Zaburi 52:7; 62:10; 73:3-9
    - 2. Mithali 11:28; 23:4-5; 27:24; 28:20-22
    - 3. Ayubu 31:24-28
- II. Mtazamo wa kipekee wa kitabu cha Mithali
  - A. Mali imewekwa katika nafasi ya juhudi ya mtu binafsi
    - 1. uzembe na uvivu umelaaniwa – Mithali 6:6-11; 10:4-5,26; 12:24,27; 13:4; 15:19; 18:9; 19:15,24; 20:4, 13; 21:25; 22:13; 24:30-34; 26:13-16
    - 2. kufanya kazi kwa bidii kumeungwa mkono – Mithali 12:11,14; 13:11
  - B. Umaskini dhidi ya mali umetumika kueleza juu ya haki dhidi ya unyonge – Mithali 10:1na kuendelea; 11:27-28; 13:7; 15:16-17; 28:6,19-20
  - C. Hekima (kumjua Mungu na nenp lake na kuishi katika maarifa haya) ni bora kuliko utajiri- Mithali 3:13-15; 8:9-11,18-21; 13:18
  - D. Maonyo na makaripio
    - 1. Maonyo
      - a. jiidhari na kudhamini deni la jirani yako (dhamana) –Mithali 6:1-5; 11:15; 17:18; 20:16; 22:26-27; 27:13
      - b. jiidhari na kupata utajiri kwa njia ya uovu – Mithali 1:19; 10:2,15; 11:1; 13:11; 16:11; 20:10,23; 21:6; 22:16,22; 28:8
      - c. jiidhari na mkopo – Mithali 22:7
      - d. jiidhari na utajiri wa muda mfupi – Mithali 23:4-5
      - e. mali hazifaidii kitu siku ya ghadhabu – Mithali 11:4
      - f. utajiri una "marafiki" wengi– Mithali 14:20; 19:4
    - 2. makaripio
      - a. ukarimu huungwa mkono – Mithali 11:24-26; 14:31; 17:5; 19:17; 22:9,22-23; 23:10-11; 28:27
      - b. afadhali haki kuliko utajiri – Mithali 16:8; 28:6,8,20-22
      - c. maombi kwa ajili ya uhitaji, na sio utoshelevu – Mithali 30:7-9
      - d. kumpa mhitaji ni kumpa Mungu – Mithali 14:31
- III. Mtazamo wa kitabu cha Agano Jipya
  - A. Yesu
    - 1. mali hutengeneza jaribu pekee la imani ndani yetu wenyewewe rasilimali na zetu badala ya Mungu na rasilimali Zake
      - a. Mathayo 6:24; 13:22; 19:23
      - b. Marko 10:23-31
      - c. Luka 12:15-21,33-34
      - d. Ufunuo 3:17-19
    - 2. Mungu atatupa mahitaji yetu ya kimwili
      - a. Mathayo 6:19-34
      - b. Luka 12:29-32

3. kupanda kunahusiana na kuvuna (kiroho pamoja na kimwili)
  - a. Marko 4:24
  - b. Luka 6:36-38
  - c. Mathayo 6:14; 18:35
4. toba huithiri mali
  - a. Luka 19:2-10
  - b. Mambo ya Walawi 5:16
5. unyanyasaji wa kiuchumi umelaaniwa
  - a. Mathayo 23:25
  - b. Marko 12:38-40
6. Humu ya nyakati za mwisho inahusiana na matumizi yetu ya mali – Mathayo 25:31-46

B. Paulo

1. Maoni ya kiutendaji kama ule wa Mithali (kazi)
  - a. Waefeso 4:28
  - b. 1 Wathesalonike 4:11-12
  - c. 2 Wathesalonike 3:8,11-12
  - d. 1 Timotheo 5:8
2. Maoni ya kiroho kama yale ya Yesu (mambo ni ya muda mfupi, iweni na utoshevu)
  - a. 1 Timotheo 6:6-10 (kuridhika)
  - b. Wafilipi 4:11-12 (kuridhika)
  - c. Waebrania 13:5 (kuridhika)
  - d. 1 Timotheo 6:17-19 (ukarimu na kuamini Mungu, si utajiri)
  - e. 1 Wakorintho 7:30-31 (kubadikika badilika kwa mambo)

IV. Hitimisho

- A. Hakuna thiojia ya kimfumo iliyo ya kibiblia kuhusiana na mali.
- B. Hakuna kifungu cheye uhakika kuhusiana na suala hili, hivyo, mitazamo ya kiundani lazima ikusanywe kutokana na vifungu mbalimbali. Jihadhari na kutokutumia maoni yako katika maandiko haya yaliyojitenga.
- C. Kitabu cha Mithali, ambacho kiliandikwa na watu wenye hekima (busara), wana mtazamo tofauti kuliko aina nyingine za miundo ya kibiblia. Kitabu cha Mithali ni cha kiutendaji na kina tazamio binafsi. Hiki kina ulinganifu na lazima kiwe na ulinganifu na Maandiko mengine (kama vile Yer. 18:18)
- D. Katika hizi siku tulizonazo tunahitaji kuchambua maoni na utendaji wake kuhusiana na mali katika nuru ya Biblia. Vipaumbele vyetu vimepotea ikiwa ubepari au ukomonisti ni mwongozo wetu wa pekee. Ni kwa nini na ni kwa namna gani kufanikiwa kwa mtu ni maswali muhimu sana kuliko kuliko kile mtu alichojilimbikizia.
- E. Kujilimbikizia mali lazima kuwe na ulinganifu na ibada ya kweli na utumishi unaostahili kama vile 2 Wakorintho 8-9).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 6:25-33**

<sup>25</sup>Kwa sababu hiyo nawaambieni, Msisumbukie maisha yenu, mle nini au mnywe nini; wala miili yenu, mvae nini. Maisha je! Si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi? <sup>26</sup>Waangalieni ndege wa angani, ya kwamba hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi ghalani; na Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao. Ninyi je! Si bora kupita hao? <sup>27</sup>Ni yupi kwenu ambaye akijisumbua aweza kujiongeza kimo chake hata mkono mmoja? <sup>28</sup>Na mavazi, ya nini kuyasumbukia? Fikirini maua ya mashamba, jinsi yameavyo; hayafanyi kazi, wala hayasokoti <sup>29</sup>nami nawaambia, ya kwamba hata Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo la hayo. <sup>30</sup>Basi, ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo, na kesho hutupwa kalibuni, je! Hatazidi sana kuwavika ninyi, enyi wa imani haba? <sup>31</sup>Msisumbuke, basi, mkisema, Tule nini? Au Tunywe nini? Au Tuvae nini? <sup>32</sup>Kwa maana hayo yote Mataifa huyatafuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote. <sup>33</sup>Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.



**6:25 "kwasababu hiyo nawaambieni"** Hii inaonesha muunganiko wa kimantiki na Mt. 6:19-24.

☑️**"msisumbukie maisha yenu"** Hii ni kauli shurutishi ya wakati uliopo ukiwa na kiambata hasi. Kwa ufanano wa kifungu, angalia angalia Flp. 4:6. Mstari wa 25 unazungumzia kanuni ya jumla katika ufahamu wa mistari iliyopita. Toleo la fasiri ya KJV, "msiwaze," ni bahati mbaya kwasababu inamaanisha katika siku zetu kwamba kutokuwa na mpango wowote juu ya siku za usoni si sahihi. Hii hakika sio jambo hasa (kama vile 1 Tim. 5:8). Wazo la msingi ni "shaka" (kama vile Mt. 6:25, 27, 28, 31, na 34).

☑️**"Maisha je! Si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi?"** Maisha ya kimwili ni muhimu lakini si kilele. Ulimwengu huu ni uwanja wa kujifunzia tu kwa ajili ya uhusiano kamili na zaidi wa karibu na Mungu. Ukweli wa Kibiblia ni kwamba Mungu anajali watoto Wake na kwamba atawapa mahitaji yao ya msingi.

**6:26,28 "ndege wa angani. . .majani ya kondeni"** Fasiri "ndege wa angani" na "mimea ya kondeni" ni sawa kwasababu andiko haliweki wazi kibayana aina fulani ya ndege au mmea lakini ile iliyozoeleka. Kwasababu mazingira yalikuwa ya mlimani, yawezekana Yesu alisonta kundi la ndege wa angani au mimea ya kondeni iliyokuwa karibu. Hii ilikuwa ni hoja ya kiutafsiri ya walimu wa kiyahudi kutoka wadogo mpaka wakubwa.

**6:26 "je ninyi si bora kuliko hivyo"** Huu ulikuwa ni ulinganifu wa kiaina wa kiuahimu wa kiyahudi juu ya mdogo kwenda kwa mkubwa. Biblia iko wazi kwamba Mungu ndiye aliyeeumba wanyama na anawapenda. Lakini wanyama hawawezi kuwa na ushirika na Mungu kama wanadamu aliowafanya kwa sura na mfano wake. Kuwa makini katika kujali sana wanyama kuliko maisha ya wanadamu. Wanyama walitolewa kama chakula na huduma baada ya anguko. Wanyama hawana umilele ila wanadamu wanao! Uinjilisti ni zaidi kuliko "haki za wanyama"! Maisha mengi ya wanyama walioumbwa wametoka katika kuishi.! Mtazamo mbaya wa namna gani huu. Makundi ya Haki za Wanyama yanajali sana wadudu kuliko wanadamu wasiozaliwa bado!  
Neno lingine zaidi tu, ukatili kwa wanyama unazungumza zaidi juu ya kutojali na juu ya mtu asiye na hisia. Mungu aliwaumba wanyama kuwa na pembe za hisia kama sisi. Wanyama walikuwa sehemu ya uumbaji wa asili wa Mwanzo 1 na watakuwa sehemu ya uumbaji upya (kama vile Isa. 11:6-9).

**6:27**

**NASB "anaweza kuongeza saa moja katika maisha yake"**

**NKJV "anaweza kuongeza kimo katika urefu wake"**

**NRSV "anaweza kuongeza saa moja katika umri wa maisha yake"**

**TEV "kuishi zaidi kidogo"**

**NJB "kuongeza kipimo kidogo cha umri wake"**

Hili kibayana ni neno la Kiebrania "kipimo." Yodi ilirejerea urefu kati ya kiwiko cha mwanadamu na kidole chake kirefu zaidi cha mkononi. Ilikuwa ni kipimo cha Agano la Kale kilichotumika katika ujenzi na kawaida ilikuwa inchi kumi na nane. Hata hivyo kulikuwa na yodi ya kuaminika iliyotumika katika hekalu ambayo ilikuwa na kipimo cha inchi ishirini na moja. Katika Agano Jipya ilitumika aidha kwa ajili ya urefu au muda: juu ya urefu katika Luka 19:3 (pia LXX ya Ezek. 13:18) na ya muda katika Yohana. 9:21,23 and na Ebr. 11:11. Kwasabu inachekesha kwa mtu kuwa na uwezo wa kukua kimwili urefu wa fupi, aidha ni (1) sitiari kwa ajili ya umri (2) au ni utiaji chumvi wa mazingira yale ya tamaduni za kimashariki (utiaji chumvi).

**6:30 "lakini ikiwa Mungu"** Hii ni sentensi daraja la kwanza yenye masharti ambayo inadhaniwa kuwa kweli kutoka katika mtazamo wa mzungumzaji au kwa ajili ya makusudi ya kifasihi. Mungu anatoa kwa ajili ya uumbaji wake.

☑️**"yaliyopo leo, na kesho hutupwa kalibuni"** Matumizi ya kawaida ya nyasi kavu ilikuwa ni kuanzisha moto katika jiko dogo lililotumika kuokea mikate. Hii ilikuwa ni stiari kwa mapito ya maisha na sio hukumu ya siku za mwisho. Waaminio ni wenye thamani sana kuliko majani mazuri ya kondeni.

☑️**"enye wenye imani haba"** Tungo hii inatokea mara kwa mara katika injili ya Mathayo (kama vile Mt. 8:26; 14:31;16:8). Mafundisho ya Yesu yalikuwa yanaelezea kuongeza imani ya waaminio.

**6:31 "msiwe na shaka"** Hii ni kauli tegemezi ya wakati uliopita usio timilifu yenye ukanushi, iliyomaanisha "msianze kuwa na mashaka" (kama vile Flp. 4:6). Mkazo usio kuwa na afya wa namna gani mtu atajipatia mahitaji yake ya kimsingi kunaonesha kupoteza kwa tumaini katika Mungu aliyehaidi kuwapatia waaminio.

**6:32**

**NASB** "kwa maana mataifa kwa bidii wanatafuta vitu hivi"  
**NKJV** "kwa maana vitu hivi mataifa wanavitafuta"  
**NRSV** "kwa maana mataifa wanag'ag'ana kwa vitu hivi"  
**TEV** "hivi ni vitu ambavyo wapagani siku zote wanavitazama"  
**NJB** "ni mataifa ambao wameweka mioyo yao katika hivi vitu"

Moja ya tabia ya mwanadamu aliyeanguka ni kiu yake isiyoweza kuongozwa kwa ajili ya vitu. Mungu anajua waamini wanahitaji ya vitu ili waweze kuishi duniani. Atashughulikia kwa ajili ya mahitaji yao, sio sio zote kile wanachotaka.

**6:33**

**NASB, NKJV** "Bali utafuteni kwamnza ufalme wa Mungu na haki Yake"  
**NRSV** "Bali kwanza utafute ufalme wa Mungu na haki yake"  
**TEV** "shughulikia kwanza ufalme wa Mungu na haki yake"  
**NJB** "weka moyo wako kwanza katika ufalmwe wa Mungu na katika kutenda haki"

Hii ni kali shurutishi ya wakati uliopo ambayo inazungumzia tabia ya kila siku ya kuamriwa. Ukweli ni kwamba Mungu lazima awe kipaumbele katika maisha ya mwamini. Tungo "haki Yake" lilitumika hapa katika namna ya kimaadili na sio kwa kisheria (kimahakama) kwa namna ya maandiko ya Paulo. Hii namna ya kimaandiko inaweza kuonekana katika Mt. 5:6,10,20, 6:1, Kum. 6:25, Isa. 1:27-28, na Dan. 4:27. Huu sio wito wa matendo ya haki; bali inapendekeza kwamba mara mtu anapomjua maisha yake yatatawaliwa na matendo mema (kama vile Efe. 2:10). Kinafasi, haki iliyokataliwa lazima iaksiwe katika kuishi kama Kristo. Angalia Mada Maalum: Ufalme wa Mungu katika Mt. 4:17 na Haki katika Mt. 5:6.

Tungo "Ufalme wake" ilikuwa ni dhana ya utawala wa sasa wa Mungu katika mioyo ya wanadamu kwamba siku moja dunia yote itahitimishwa (kama vile Mt. 6:10). Ilikuwa ni kusudio kuu la mahubiri ya Yesu. Maadili ya Ufalme lazima yawe kipaumbele kikubwa. Maandiko ya kale ya Kiyunani (α & Β) hayana tungo ya jinsi "ya Mungu" (kama vile matoleo ya NRSV na TEV).

Neno "kwanza" linatumika na Yesu mara kadhaa kufafanua upya usio badilika wa "zama mpya" ya Roho, ambayo alianzisha.

1. Mt. 5:24, upatanishwe na ndugu yako kabla ya kuabudu
2. Mt. 6:33, utafute ufalme wa Mungu kabla ya mahitaji yako binafsi/shauku
3. Mt. 7:5, kabla ya kuwahukumu wengine jitazame kwanza mapungufu yako na makosa yako
4. Mt. 23:26, safisha maisha yote ya ndani na nje

☛ **"na mengine yote haya mtazidishiwa"** Hii inarejerea mahitaji ya kawaida ya kimwili na ya kawaida ya kimaisha. Mungu hatatuacha katika hali ya njia panda. Hii ni kanuni ya jumla ambayo haiwezi kuleta majibu maswali ya kidhahiri kwanini mtu huyu ama yule anapata hasara au yuko katika uhitaji. Wakati mwingine Mungu atatupatia muda wa uhitaji ili waamini waweze kumtumainia, kumgeukia au kuboresha tabia zao. Kauli hii ni zaidi kama kitabu cha Mithali katika namna kwamba kinataja kanuni za jumla. Hazikusudiwi kumuelezea kila mtu, au tukio fulani.

#### **ANDIKO LA NASB(LILOBORESHWA) MATHAYO 6:34**

<sup>34</sup> **Basi msisumbukie ya kesho; kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe. Yatosha kwa siku maovu yake.**

**6:34** Mstari huu unakatiza mtiririko wa fikra. Maisha ya Mkristo ni ya kutembea kila siku. Vitu vibaya vinavyotokea kwa watu wasioamini mara kwa mara vinatokea kwa mtu anayeamini. Hii haimaanishi kwamba Mungu hajali. Inamaanisha kwamba mwamini anakutwa na mfumo wa kiulimwengu ulioanguka. Usiruhusu matatizo ya maisha yakufanye kufikiria kwamba Mungu hakujali. Angalia Hannah Whithall Smith, *The Christian's Secret of a Happy Life*.

### **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembe katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa namna gani mistari 19-34 inahusiana na uwasilishaji wote wa mahubiri juu ya Mlima?
2. Je watu waliokuwa wakimsikiliza Yesu walikuwa wakijiwekea hazina duniani? Je inahusiana vipi na msisitizo wa kisasa wa akauti za kujiwekea fedha, bima au mipango juu ya kustaafu?
3. Mtu anawezaje kujiwekea akiba mbinguni? Je hazina hizi za mbinguni zinajumuisha nini?
4. Elezea ukweli wa kiroho wa Mt. 6:22-24 kwa maneno yako mwenyewe na kutokana na uzoefu wako.
5. Je fedha ni uovu?
6. Je wasiwasi ni dhambi (Mt. 6:31)?
7. Je mstari wa 33 unatufundisha matendo ya haki?
8. Elezea kwanini Wakristo huteseka.

## MATHAYO 7

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Kuhukumu wengine 7:1-6	Usihukumu 7:1-6	Maana ya mifano ya Ujumbe wa Yesu 7:1-5	Kuhukumu wengine 7:1-5	Usihukumu 7:1-5
Ombeni, tafuteni, maombi Bisheni 7:7-12	Endelea kuomba, kutafuta, kubisha 7:7-12	7:6 7:7-11 7:12	7:6 Ombeni, tafuteni, bisheni 7:7-11 7:12	Usikufuru vitu vitakatifu 7:6 Matokeo ya 7:7-11 Sheria ya shaba 7:12
Mlango ulio Mwembamba 7:13-14	Njia iliyo nyembamba 7:13-14	7:13-14	Njia iliyo nyembamba 7:13-14	Njia mbili 7:13-14
Mti hutambulika Kwa matunda yake 7:15-20	Utawatambua kwa matunda yao 7:15-20	7:15-20	Mti na matunda yake 7:15-20	Manabii wa uongo 7:15-20
Sijakuelewa kamwe 7:21-23	Sijakuelewa kamwe 7:21-23	7:21-23	Sijakuelewa kamwe 7:21-23	Wanafunzi wa kweli 7:21-23
Misingi miwili 7:24-27	Kujenga juu ya Mwamba 7:24-27	7:24-27	Wajenzi wawili wa nyumba 7:24-25	7:24-27
7:28-29	7:28-29	7:28-29	Mamlaka ya Yesu 7:28-29	Mshangao wa makutano 7:28-29

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka “[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)”)**

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuwiwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## HISTORIA YA NYUMA YA MATHAYO 7:1-29

- A. Usambamba wa toleo la Lucan unaanza na sehemu sawa na maelezo chanya "kuwa huruma kama. . ." Luka 6:36- 38, 41-42. Kwa kawaida Luka anatumia mahubiri ya Yesu kwa ufupi zaidi kuliko Mathayo, lakini hapa Luka anaandika zaidi maneno ya Yesu.
- B. Sura hii ina *asyndetons* (ukosefu wa chembe zinazoshikamana, ambazo sio za kawaida kwa kiyunani), Mt. 7:1,6,7,13,15. Ni njia ya kisarufi ya nuru kuu ya kweli kwa kila mmoja. Ni dhanio la uhakika kwamba mahubiri ya Yesu yanaunganisha dhana au muundo wa muhtasari. Yumkini alifuata mtindo wa mafundisho ya walimu wa sheria ya kiyahudi uliozoeleka uitwao "lulu zilizo kwenye gidamu," ambao unaunganika pamoja na mada zisizo na uhusiano. Ingawa baadhi ya tabia zenye uelekeo kwanza zinazonekana hazina uhusiano na muktadha wao unaozunguka vipengele, ni mfasiri wa fasihi bora zaidi anaekaribia kuwatafsiria katika nuru ya (1) muktadha na (2) na matumizi yao ya injili zifananazo. Mwandishi wa Mathayo aliunganisha dhana na muundo wa muhtasari ili kupata mafundisho ya Yesu yaliyoandikwa na nini hasa cha kuandika.
- C. Inawezekana kusimulia mistari ya 1-12 katika muktadha uliotangulia kwenye njia ifuatayo:
1. Mt. 7:1-5 inaonyesha hatari ya Mt. 5:20 na 48
  2. Mt. 7:6 inaonyesha hatari ya kuvutwa na upendo, upendo usio na utambuzi
  3. Mt. 7:7-11, maombi ni ufunguo wa utambuzi ufaao kwa waaminio
  4. Mt. 7:12 ni maelezo ya ukweli mkuu ambao unaelezea ufalme wa watu wote
- D. Sehemu hii, kama mahubiri yote ya mlimani, yanatia maisha rangi nyeusi na nyeupe. Mjadala bora zaidi wa uhusiano kati ya Mt. 7:1-5 na 6 unapatikana kwenye fasiri ya William Hendricksen katika Mathayo, "Bwana anawaonya wasikilizaji wake wajihami kuhuwakumu wengine (Mt.7:1-5), bado pia wanahukumu (Mt. 7:6); wawe na kiasi, bado ni wakosoaji; kuwa wanyenyekevu na wastahimilivu, bado pia hawastahimili," uk. 360.
- E. Kumbuka huu sio uwasilishaji wa injili, lakini ni ujumbe wa maadili juu ya maisha katika ufalme wa Masihi. Kweli zake tatu kuu ni
1. Dhambi za udini
  2. Mafundisho makuu ya Yesu juu ya Mungu
  3. Mwitikio wetu kwa Yesu na mafundisho yake na hukumu ya Mungu kwa mwitikio wetu
- F. Mahubiri ya mlimani yanamalizia na mialiko mitatu au minne na maonyo yanasimuliwa kwa chaguzi mbili kwa wanadamu (Mt. 7:13-27): (1) njia mbili, (2) matunda mawili, (3) maungamo mawili, na (4) misingi miwili. Yote yanasimulia mwisho wa hukumu ambao msingi wake ni matendo.
- G. Mstari wa 28 ni maelezo ya Mathayo. Mathayo alihusisha sehemu ya mafundisho yote matano ya Yesu na maelezo. Yumkini yakafanya muundo wake wa injili.
1. Mt. 7:28
  2. Mt. 11:1
  3. Mt. 13:53
  4. Mt. 19:1
  5. Mt. 26:1
- H. Ni lazima ikumbukwe kwamba mwanzo wa hatua ya mahubiri/mafundisho ya Yesu haukufahamika bado. Wasikilizaji, na hata wanafunzi, hawakumjua Yesu ni nani na thamani ya ushirika wa uanafunzi ilitakiwa iambatane nae kwenye mateso, kukataliwa na hadi kifo.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 7:1-5

<sup>1</sup> Msihukumu, msije mkahukumiwa ninyi. <sup>2</sup> Kwa kuwa hukumu ile mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa; na kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakachopimiwa. <sup>3</sup> Basi, mbona wakitazama kibanzi kilicho ndani ya jicho la ndugu yako, na boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe huiangalii? <sup>4</sup> Au utamwambiaje nduguyo, Niache nikitoe kibanzi katika jicho lako; na kumbe! Mna boriti ndani ya jicho lako mwenyewe? <sup>5</sup> Mnafiki wewe, itoe kwanza ile boriti katika jicho lako mwenyewe; ndipo utakapoona vema kukitoe kile kibanzi katika jicho la ndugu yako.

**7:1 "msije"** hii ni kauli shurutishi ya wakati uliopo na kiambata hasi yenye maana ya kuzuia tendo lililo tayari. Wakristo wanajifunza kuwa makini na wengine. Mstari huu mara nyingi unadokeza kwamba wakristo hawatakiwi kuhukumiana kwa yeyote yule. Lakini, Mt. 7:5,6,15, 1 Kor. 5:1-12, na 1 Yn. 4:1-6 inaonyesha kwamba Yesu anawahakikishia waaminio kwamba wathaminiane kiroho. Mtizamo mmoja na shauku ndio ufunguo (kama vile Gal. 6:1; Rum. 2:1-11; 14:1-23; Yakobo 4:11-12).

☐ **"msihukumu"** neno hili la kiyunani ni chanzo cha maelezo ya asili na historia ya maneno kwa ajili ya neno la kiingereza "critic" (mkosoaji). Muundo wa asili ile ile kwenye Mt. 7:5 uliotafsiriwa "mnafiki." Inaonekana inadokeza ukosoaji, hukumu, haki ya kiroho ambayo uhukumu wengine kwa ukali zaidi kuliko atendavyo yeye. Inatilia mkazo wa utaratibu wa dhambi juu dhambi nyingine. Anakubali makosa yake kwa mwingine, lakini hakubali msamaha wa makosa ya wengine (kama vile 2 Sam. 12:1-9).

### MADA MAALUM: KUHUKUMU (JE! YAWAPASA WAKRISTO KUHUKUMIANA?)

Hukumu ni hakika (kama vile Mt. 12:36; Ebr. 9:27; 10:27; 2 Pet. 2:4,9; 3:7).

A. Yeye anayehukumu ni

1. Mungu (kama vile Rum. 2:2-3; 14:10,12; 1 Pet. 1:17; 2:23; Ufu. 20:11-15)
2. Kristo (kama vile Yohana 9:39; Mt. 16:27; 25:31-46; Mdo. 10:42; 17:31; 2 Kor. 5:10; 2 Tim. 4:1)
3. Baba kupitia Mwana (kama vile Yohana 5:22-27; Mdo. 17:31; Rum. 2:16)

Hukumu sio somo zuri, lakini ni maudhui ya sasa katika Biblia. Imejikita katika misingi au miamba za kweli kibiblia.

1. Huu ni ulimwengu wa kimaadili uliombwa na Mungu mwadilifu (tunavuna tunachopanda, kama vile Gal. 6:7).
  2. Uanadamu umeanguka; tumeasi.
  3. Huu si ulimwengu ambao Mungu alikusudia uwepo.
  4. Uumbwaji wote unaojielewa (malaika na wanadamu) tutatoa hesabu kwa muumbaji wao kwa zawadi ya uzima. Sisi ni mawakili.
  5. Milele itaamuliwa kwa kudumu na matendo yetu na chaguzi tulizozifanya katika haya maisha.
- B. Je Wakristo wahukumiane wao kwa wao? Jambo hili lazima lishughulikiwe katika namna mbili.
1. waamini wanaonywa wasije wakahukumiana wao kwa wao (kama vile Mt. 7:1-5; Luka 6:37,42; Rum. 2:1-11; Yakobo 4:11-12)
  2. waamini waanaonywa kuwatathmini viongozi wao (kama vile Mt. 7:6,15-16; 1 Kor. 14:29; 1 The. 5:21; 1 Tim. 3:1-13; na 1 Yohana 4:1-6)

Baadhi ya vigezo kwa ajili ya tathmini sahihi inaweza kusaidia

1. tathmini lazima iwe kwa kusudi la kukiri (kama vile 1 Yohana 4:1 – "jaribu" ikiwa na mtizamo wa kuthibitisha; angalia Mada Maalum: Kujaribiwa [*peirazō* na *dokimazō*])

2. tathmini lazima ifanyike katika upole na unyenyekevu (kama vile Gal. 6:1)
3. tathmini lazima iweke shabaha kwenye upendeleo wa mambo ya kibinafsi (kama vile Rum. 14:1-23; 1 Kor. 8:1-13; 10:23-33)

Tathmini lazima itambue wale viongozi walio na "sio weza kuvumilia kukosolewa" kutoka ndani ya kanisa au katika jamii (kama vile 1 Timotheo 3).

**7:2** andiko la kiyunani la Mt. 7:2 limejitokeza katika mahadhi, muundo wa kishairi. Hii yumkini ikafamika zaidi kama mithali. Jambo ambalo limetumika kwenye maelezo haya ni utaratibu wa tafsiri tofauti katika baadhi ya injili.

Mstari huu una ukweli wa muhimu ambao umerudiwa mara nyingi kwenye Agano Jipya (kama vile Mt. 5:7; 6:14-15; 18:35; Marko 11:25; Yakobo 2:13, na 5:9). Namna waaminio wanawatendea wengine ni kuaksi namna Mungu anavyowatendea wao. Hii haimanishi kuharibu ukweli wa kibiblia wa haki kupatikana kwa imani. Inamaanisha kutilia mkazo mtizamo ufaao na mtindo wa maisha ya wale waliosamehewa.

**7:3 "mbona wakitazama kibanzi kilicho ndani ya jicho la ndugu yako"** hiki "kibanzi" kilitumiwa na waandishi wa kiyunani kama kifaa kilichotengeneza kiota cha ndege. Hivyo basi, tunaongelea vipande vya mti visivyo na maana vinavyofanana, vitu vidogo.

■ **"na boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe huiangalii"** haya ni maelezo yaliyotiwa chumvi. Hii "boriti" Inarejelea kipande kikubwa cha ubao, ubao wa kujengea au paa. Mara nyingi Yesu alitumia muundo wa fasihi wa kutia chumvi ili kuwasilisha ukweli wa kiroho (kama vile Mt. 5:29-30; 19:24 na 23:24).

**7:5 "mnafiki wewe"** mchanganyo huu wa neno unatoka katika ulimwengu wa maonyesho na hutumiwa na waigizaji kuonyesha uhalisia. Linatokana na maneno mawili ya kiyunani, "kuhukumu" na "chini ya." Inaelezea mtu kuigiza kwa njia nyingine lakini akiwa ni mtu mwingine (Luka 18:9). Mfano mzuri wa matendo ya aina hii unaweza kuonekana katika maisha ya Daudi (kama vile 2 Sam. 12:1-9). Yesu alitumia neno hili kwa ajili ya Mafarisayo waliojihesabia haki kwenye Mt. 5:20; 6:2,5,16; 15:1,7; 23:13.

Mstari huu unadokeza umuhimu wa waaminio kuthaminiana na wakristo wengine hakutendewa wema, njia ya kujihesabia haki. Wagalatia 6:1 unasaidia kuangalia mtizamo ufaao na shauku kwa ajili ya kumshawishi mkristo na kuwakusanya wengine. Kanisa mara zote linatakiwa kuwa na uchunguzi wa kiroho na ushawishi wa uongozi na ushirika.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 7:6**

**<sup>6</sup> Msiwape mbwa kilicho kitakatifu, wala msitupe lulu zenu mbele ya nguruwe, wasije wakazikanyaga chini ya miguu yao, wakageuka na kuwararua.**

**7:6 " Msiwape mbwa kilicho kitakatifu "** Hii ni kauli tegemezi ya wakati uliopita usiotimilifu na kiambata hasi ambayo inadokeza "usifikilie kutenda jambo hili kamwe." kitabu *Didache*, kilichowakifishwa zaidi kilichotumiwa na kanisa la mwanzo, kinatumia mstari huu kutowabatiza watu waliojitenga na meza ya Bwana (*Didache* 9:5 na Tertullian, *Depraesc.* 41). Swali la uhakika mara zote ni: (1) "vitu vitakatifu" ni nini? na (2) neno "mbwa" na "nguruwe linarejelea akina nani? "vitu vitakatifu" lazima vimechukuliwa kwenye muktadha wa mahubiri yote ya mlimani, ambayo yalikuwa ni mafundisho juu Mungu kuunganika kwenye huduma na maisha ya Yesu wa Nazareti. au, kuweka njia nyingine, injili.

Marejeo ya Yesu kwa baadhi ya wanadamu kama "mbwa" (kama vile Mt. 15:26, 27) au "nguruwe" yamesababisha hofu kuu kati ya wafasiri. Wanyama wote hawa aliowazungumzia walikua na tabia mbaya na wasiovutia katika jamii. Kuna mjadala mwingi kama maneno haya yanamrejelea nani. Katika maisha ya Yesu, inaweza kurejelea kwa viongozi wa kiyahudi waliojihesabia haki, kama kutojali na wasiojali chochote kuhusu watu wa Palestina. Hii yumkini ikawa ni rejeleo la kinabii la kukataliwa na kifo cha Yesu toka kwa uongozi wa kiyahudi na umati wa Yerusalemu. Hata hivyo, katika maisha ya kanisa, sio dhahili kwa akina nani maneno haya yalirejelewa. Mwandishi William Hendricksen, aliandika fasiri yake ya Mathayo, "hii inamaanisha, kwa mfano,

kwamba wanafunzi wa Kristo waendeleo kupeleka ujumbe wa injili kwa wale waliowadhihaki" (uk. 359). Mfano huu umeandikwa katika Mt. 10:14, "kung'uteni mavumbi ya miguuni mwenu" (kama vile Mdo. 13:51 na 18:5-6.) imetumika kwa wayahudi kwenye Fil. 3:2-3. Imetumika kwenye Ufu. 22:15 kwa ajili ya wasioamini waliojitenga kutoka mbinguni.

☐ "lulu" hizi zilikuwa na thamani sana katika ulimwengu wa kale.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 7:7-11**

<sup>7</sup> Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa; <sup>8</sup> kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa. <sup>9</sup> Au kuna mtu yupi kwenu, ambaye, mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe? <sup>10</sup> Au akiomba samaki, atampa nyoka? <sup>11</sup> Basi ikiwa ninyi, mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Si zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wao wamwombao?

**7:7 "ombeni. . tafuteni. . bisheni"** hizi zote ni kauli shurutishi za wakati uliopo ambazo zinaongelea amri za mtindo wa maisha, ya kawaida (kama vile Kumb. 4:29; Yer. 29:13). Ni muhimu kwamba uwiano wa uvumilivu wa mwanadamu na tabia ya wajibu wa Mungu. Waamino hawawezi kumlazimisha Mungu asitende jambo lisilo zuri kwao. Hata hivyo, wakati mwingine wanaweza kupeleka mahitaji yao yoyote kwa Baba yao wa mbinguni. Yesu aliomba maombi yale yale Gethsemane mara tatu (kama vile Marko 15:36,39,41; Mt. 26:39,42,44). Paulo pia aliomba mara tatu juu ya mwiba kwenye mwili wake (kama vile 2 Kor. 12:8). Lakini jambo kubwa juu ya maombi sio kwamba mtu Fulani amepokea majibu ya maombi yake, lakini ni kwamba amechukua muda wa kukaa na Baba. Tazama [MADA MAALUM: MAOMBI YENYE UKOMO ILA YASIYO NA UKOMO](#) katika Mt. 18:19.

**7:8-10** uvumilivu ni wa muhimu (kama vile Luka 18:2-8). Hata hivyo, sio kulazimisha ukaidi kwa Mungu lakini ufunua kiwango cha shauku na mtu aliye na hofu. Mmoja ana maneno mengi wala maombi yake ya kurudia yatampa Mungu shauku ya kumpatia kile kisichokua tarajio lake kubwa. Jambo la pekee ambalo waaminio hupata kwenye maombi ni ukuaji wa ushirika na mshikamano ndani ya Mungu.

**7:9-10** Yesu alitumia ulinganifu wa baba na mwana kuelezea siri ya maombi. Mathayo anatupatia mifano miwili ambapo Luka anatupatia mifano mitatu (kama vile. Luka 11:12). Taswira yote inalenga kwamba Mungu huwapatia waaminio "mema." Luka anafafanua haya "mema" kama "Roho mtakatifu" (kama vile Luka 11:13). Mara nyingi jambo kuu ambalo Baba yetu anaweza kulitenda ni kujibu maombi yetu, binafsi yasiyofaa! Mifano yote mitatu inacheza kwenye mambo yanayofanana: jiwe kama mkate, samaki kama nyoka, na yai kama nge.

Maswali ya Mt. 7:9 na 10 yanatalajia majibu "hapana" (kama Mt. 7:16).

**7:11 "Basi ikiwa ninyi "** hii ni sentensi amrishi daraja la kwanza, ambayo ni uthibitisho wa kweli kutoka katika taswira ya mwandishi au kwa ajili ya makusudi ya fasihi. Katika hali ya njia ya kukingamana huu ni uthibitisho wa watu wote kutenda dhambi (kama vile. Rum. 3:9,23). Tofauti ni kati ya wanadamu watenda maovu na Mungu mwenye upendo. Mungu anaonyesha tabia yake kwa kufananisha na familia ya mwanadamu.

☐ **"atawapa mema wao wamwombao"** mfanano upo katika Luka 11:13 una "Roho mtakatifu" mahali pa "mema." Hakuna kifungu kwenye Luka; hivyo basi, inaweza kumaanisha "vipawa" vitolewavyo na Roho mtakatifu. Hili haliwezi kutumika kama ushahidi wa andiko kwamba mtu ni lazima amuombe Mungu kwa ajili ya Roho mtakatifu, kwa msukumo wa maandiko ni kwamba Roho mtakatifu anaishi ndani ya waaminio katika wokovu (kama vile. Rum. 8:9 na Gal. 3:2,3,5,14). Bado kuna maana ambayo ujazo wa Roho umerudiwa katika msingi wa hiari ya waaminio (kama vile. Efe. 5:18).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 7:12**

<sup>12</sup> Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii.



**7:12** Hii mara nyingi inaitwa sheria ya shaba (kama vile. Luka 6:31). Msingi huu wa maelezo uko kwenye uhakika wa waaminio kwamba ufalme wa wanadamu na moyo mpya. Hili sio anguko binafsi la mwitikio wa mwanadamu.

Yesu pekee ndiye aliyeweka mfano huu halisi katika muundo chanya, ingawa muundo hasi unafahamika kutoka maandiko ya waalimu wa dini ya kiyahudi (kama vile *Tobit* 4:15 na mwalimu Hillel, yanayopatikana kwenye kitabu cha sheria na maadili ya kiyahudi, *b Shabbath* 31a, na Philo ya Alexandria). Hii haitilii mkazo heshima binafsi isiyofaa, lakini ni neno jema juu ya kuwatambua waaminio walio katika Kristo na wenye mpango wa maana wa amani na wema kwa mshirika katika jina la Yesu. Inahitajika kwamba watu watende mema na haki, ambao uko mbali zaidi ya kujizuia kutenda mabaya.

☐ **"maana hiyo ndiyo torati na manabii"** torati na manabii ni majina mawili yaliyogawanywa mara tatu kwenye kitabu kilichowakifishwa cha kiebrania. Huu ni ufupisho wa nahau ya kiebrania unaorejelea Agano la kale lote (kama vile Mt. 5:17).

Ina umuhimu kwamba Yesu alifanya yote yaliyohitajika kwenye Agano la kale (kama vile Mt. 22:34-40; Marko 12:28-34). Haya yalikuwa ni mabishano makubwa ya wayahudi wa karne ya kwanza (kama vile Rum. 13:9).

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 7:13-14**

<sup>13</sup> **Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo.** <sup>14</sup> **Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache.**

**7:13** Je mstari huu unadokeza (1) kuingia katika mlango na kutembea juu ya njia; au (2) kutembea juu ya njia inayokuelekeza katika mlango; au (3) ni mfano wa kiebrania unaofanana? Jambo ni kwamba mlango umejitokeza kwanza na kisha njia hii inarejelea kwamba mtu binafsi anakuja kumtambua Mungu kupitia mafundisho ya Yesu na kuishi maisha mapya ya kifalme. Baadhi ya utata hapa unaweza kufikiliwa kuwa ni vipengele vitatu vya wokovu wa Kibiblia: (1) imani ya mwanzo na toba; (2) mtindo wa maisha unaofanana na Kristo; na (3) upeo wa matukio ya siku za mwisho. Mfano huu unafanana na wa kwenye Luka 13:23-27. Tazama mada maalumu: matumizi ya "mlango" kwenye Agano Jipya katika Mt. 6:6.

☐ **"mlango ulio mwembamba"** huu ni ukweli wa aina ya mithali unaofahamika kwa desturi kama "njia mbili" (kama vile Kumb.30:15, 19; Zab. 1; Mit.4:10-19; Isa. 1:19-20 na Yer. 21:8). Ni vigumu kutambua Yesu alikua anamwongelea nani: (1) wanafunzi, (2) mafarisayo, au (3) makutano. Mukstadha mzima unaweza kudokeza kwamba mstari unasimulia katika 5:20 na 5:48. Ikiwa ni hivyo, basi hii inadokeza kwamba inawekea mipaka ya asili ya mlango na sio sheria, kama mafarisayo walioshikilia sheria, lakini umejaa upendo wa ushirika na mtindo wa maisha na Kristo. Kristo ana sheria (kama vile Mt. 11:29-30), lakini umejaa kutoka katika moyo uliobadilika! Ikiwa tutaweka mstari huu na uhusiano wa mukstadha wa wayahudi wa mataifa (kama vile Mt. 6:7, 32), basi itasimulia imani katika Yesu kama mwokozi (mlango) na Bwana (njia).

Inaanza na Mt. 7:13-27 kuna mfuatano tofautishi unaosimulia watu wa kidini.

1. njia mbili za kutekeleza wajibu wa kidini (Mt. 7:13-14)
2. aina mbili za viongozi wa kidini (Mt. 7:15-23)
3. misingi miwili ya maisha ya kidini (Mt. 7:24-27)

Swali sio kundi lipi la watu wa kidini ambalo Yesu alirejelea, lakini ni kwa namna gani watu wa kidini wanaitikia ufahamu wa mapenzi ya Mungu. Baadhi wanatumia dini kama mwongozo wa kuwa karibu na watu ili kupata zawadi na sifa. Ni "mimi" na "sasa" wanalenga mtindo wa maisha (kama vile Isa.29:13; Kol. 2:16-23). Wanafunzi wa kweli wanapangilia maisha yao kwenye nuru ya maneno ya kristo juu ya uwepo na ujio wa ufalme wa Mungu.

☐ **"maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni"** "njia" inaweza kuwa (1) sitiari ya mtindo wa maisha na (2) jina la awali la kanisa (kama vile Mdo. 9:2; 19:9,23; 22:4; 24:14,22; 18:25-26). Mstari huu unadokeza kwamba wokovu sio maamuzi rahisi ambayo yatafaa kwenye mwelekeo wa desturi, lakini ni

mabadiliko ya maamuzi yanayoonyesha wale waishio maisha ya uhuru wa Mungu. Mara nyingi walionekana wa kidini sana (kama vile Isa. 29:13; Mt. 7:21-23; Kol. 2:23)!

Tungo hii ina aina ya machapisho ya kiyunani yanayobadilika. Mwanzo wa mstari huu unasema, "ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba," lakini sehemu ya pili nusu yake "mlango" umerukwa kwenye machapisho ya  $\kappa^*$ , baadhi ya machapisho ya kale ya kilatini, baadhi ya machapisho ya Vulgate, Diatessaron, na maandiko ya kiyunani yaliyotumiwa na Clement na Eusebius. Yapo kwenye matoleo ya  $\kappa^1$ , B, C, L, W, na baadhi kilatini cha kale, Vulgate, Shamu, na machapisho ya Koptiki. Hivyo swali ni, "je yamewekwa ajili ya uwiano" au "ni kwa bahati mbaya?" toleo la UBS<sup>4</sup> linatupatia andiko refu (yaani, mjumuisho wake) alama "B" (yenye uhakika). Hata hivyo, mjumuisho wake au pasipo haiwezi kubadili maana ya aandiko. Huu ni ukweli mpana wa mabadiliko kwenye maagano mapya ya kiyunani kiasi cha 5,300 kwenye Agano Jipya uliopo leo! Tazama Bruce Metzger, *A Textual Commentary on the Greek New Testament*, uk. 19.

**7:14** katika siku ya "tumainifu rahisi" inahitaji uwiano! Hii haisemi kwamba Ukristo unategemea juhudi ya mwanadamu, lakini zaidi kwamba maisha ya imani yatajawa na mateso. "Mwembamba" kwenye mstari huu unashiriki asili moja ile ile kama "dhiki" au "mateso" kwenye vifungu vingine vya Agano jipya. Mkazo huu huu kinyume halisi cha Mt. 11:29-30. Mistari hii miwili inaelezewa kama "mlango" na "njia." Tunamwendea Mungu kupitia kwa Yesu kama kipawa cha bure toka kwa Mungu (kama vile Rum. 3:24; 5:15-17; 6:23; Efe. 2:8-9), lakini tangu tunapomfahamu yeye, ni lulu ya thamani ambayo tunauza vyote tulivyonavyo ili tumfate yeye. Wokovu thabiti ni huru, lakini unagarimu kila kitu tulichonacho.

Tungo hii "nao waionao ni wachache" inaweza kulinganishwa na Mt. 7:13 na Luka 13:23-24. Swali ni "je wengi wataangamia zaidi badala ya kuokolewa?" je mstari huu unafundisha tofauti ya idadi?

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 7:15-20**

<sup>15</sup> Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa-mwitu wakali. <sup>16</sup> Mtawatambua kwa matunda yao. Je! Watu huchuma zabibu katika miiba, au tini katika mibaruti? <sup>17</sup> Vivyo hivyo kila mti mwema huzaa matunda mazuri; na mti mwovu huzaa matunda mabaya. <sup>18</sup> Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mwovu kuzaa matunda mazuri. <sup>19</sup> Kila mti usiozaa tunda zuri hukatwa ukatupwa motoni. <sup>20</sup> Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua.

**7:15 "Jihadharini na manabii wa uongo"** Hii ni kauli shurutishi ya wakati uliopo. Yesu mara nyingi aliongelea juu ya manabii wa uongo (kama vile Mt. 24:4, 5, 11, 23-24; Marko 13:22). Mara zote ni vigumu kuwatambua wahubiri wa uongo kwa sababu kwa kawaida wanakua na chembe za ukweli kwenye ujumbe wao, na mtu anaweza asiwe na shaka na shauku zao. Hivyo basi, linakuwa swali la msingi sana kwa namna gani waaminio wahakikishe akina nani ni wahubiri wa uongo. Kuna vipengele kadhaa ambavyo ni lazima viwekwe kwenye tathmini.

1. Kumb. 13:1-3 na 18:22
2. Tito 1:16 na 1 Yn. 4:7-11
3. 1 Yn. 4:1-3, inahusika kwenye uhakiki huu, wakristo wanaweza kufanya tathmini yao.

Mistari ya 15-20 inahusika na jambo la kutazama matunda, ambapo Mt. 7:21-23 inahusika na watu wazaao matunda yaonekanayo kuwa mema, lakini hawana ushirika binafsi na Mungu. Kuna "mlango" na "njia" yote ni imani ya awali na maisha ya imani!

☑ **"watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa-mwitu wakali"** mbwa-mwitu kiutamaduni ni adui wa kondoo (kama vile Mt. 10:16; Mdo. 20:29). Hii inamaanisha kwamba moja ya vipengele vigumu katika njia iongozayo uzimani ni kwamba kuna watu wanaojaribu kutudanganya kwa ujumbe wa uongo (kama vile Efe. 4:14). Kwa kawaida ujumbe huu unakuwa na baadhi ya faida binafsi kwa ajili ya manabii wa uongo. Wanaonekana wa kidini sana! Mistari 21-23 unaonyesha namna mbwa-mwitu anavyoweza kufanana kama kondoo!

**7:16 "Mtawatambua kwa matunda yao"** mfano huu ni wa kipee katika Mathayo. Hii ni dalili ya wakati ujawo iliyotumika kama kauli shurutishi ya wakati uliopo (tazama pia Mt. 7:20). Swali linalotalajiwa ni jibu "hapana" (kama Mt. 7:10). "tambua" ni muundo wa huruma, udokezo kwamba waaminio lazima wanaweza na

kuwatambua wahubiri wa uongo. Tunaweza kuwatambua wao kwa kipaumbele cha maisha na mafundisho yao. Mara nyingi lilikua ni swali kama hawa wanaweza kuzaa tunda japo moja, kwa kweli, nao huzaa pia matunda.

1. Mafundisho yao (kama vile Kumb. 13:1-3; 18:22; Luka 6:45; 1 Yn. 4:1-3)

2. Matendo yao (kama vile Luka 3:8-14; 6:43-46; Yn 15:8-10; Efe. 5:9-12; Kol. 1:10; Tit. 1:16; Yakobo 3:17-18; 1 Yn. 4:7-11)

Kwa namna gani watu wanaaksi maisha

1. Ukweli wao binafsi

2. Ushirika wao na Mungu

Ni vigumu kuzishikilia kweli hizi mbili pamoja mwaliko huru wa wokovu, na matakwa ya kufanana na Kristo. Bado zote ni kweli! Mjadala huu mzuri mfupi ni kwenye Manfred T. Brauch, *Abusing Scripture*, uk. 104-116.

**7:19** Kwa sababu Yohana mbatizaji alitumia tungo sawa sawa na hii kwenye Mt. 3:10, wengi wanaamini hii ni mithali iliyozeleka kusemwa.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 7:21-23**

<sup>21</sup> Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. <sup>22</sup> Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? <sup>23</sup> Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu.

**7:21** "Si kila mtu aniambiaye" Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo ambayo inaongelea tendo la kuendelea. Aliyasema maneno haya tena na tena.

■ **"Bwana, Bwana"** waalimu wa sheria ya kiyahudi wanasema kwamba majina mawili yanaonyesha upendo (kama vile Mwa. 22:11). Neno la kiyunani *kurios* limetumika mara kadhaa kwa njia tofauti kwenye karne ya kwanza. Ni dhahili inaweza kumaanisha (1) "bwana"; (2) "Bwana"; (3) "mmiliki"; au (4) "mme." lakini, kwenye muktadha wa kitheolojia, inatafsiriwa na maana yake kamili iliyotolewa katika tafsiri ya Agano la kale ya jina YHWH (kama vile. Kut. 3:14). Katika muktadha huu watu hawa walifanya semi juu ya Yesu, lakini hawakuwa na uhusiano binafsi naye. Ilikuwa ni vigumu katika hatua hii ya awali kwenye huduma ya Yesu kutambua ni kwa kiasi gani uzito wa kitheolojia kwa kuunganisha neno hili.

Petro pia alilitumia awali kama thiolojia kwa ajili Yesu (kama vile. Luka 5:8), kama alivyotumia Luka 6:46, ambapo Yesu aliunganisha kitenzi thibitisho kimoja na utii. Hata hivyo, katika muktadha huu ni taswira ya ujio wa pili wa hukumu ya manabii wa uongo katika matukio ya siku za mwisho.

Wataokolewa na kuangamia kabisa au wasiokolewe daima?

#### **MADA MAALUMU: UKANAJI WA IMANI (APHISTĒMI)**

Neno la Kiyunani *aphistēmi* lina uwanja mpana wa elimu-maana. Hata hivyo, Neno la Kiingereza "uasi" limetokana na neno hili na athari za matumizi yake kwa wasomaji wa sasa. Muktadha, kama iliyo kawaida, ndio ufunguo, sio maelezo ya wakati uliopo.

Hili ni neno lililounganishwa kutokana na KIHUSISHI *apo*, ambacho kinamaanisha "kutokana na" au "mbali na" and *histēmi*, "kukaa," "kusimama," au "kupachika." Angalia matumizi yafuatayo (yasiyo ya kithiolojia):

1. kuondoa kimwili

a. kutoka Hekaluni, Luka 2:37

b. kutoka katika nyumba, Marko 13:34

c. kutoka kwa mtu, Marko 12:12; 14:50; Matendo 5:38

d. kutoka katika vitu vyote, Mt. 19:27,29

2. kuondoa kisiasa, Matendo 5:37

3. kuondoa kimahusiano, Matendo 5:38; 15:38; 19:9; 22:29

4. kuondoa kisheria (tarakisha), Kumb. 24:1,3 (LXX) na Agano Jipya, Mat. 5:31; 19:7; Marko 10:4; 1 Cor.

7:11

5. kuondao deni, Mt. 18:7
6. kuonyesha kutokuhusika kwa kuondoka, Mat. 4:20; Yohana 4:28; 16:32
7. kuonyesha kutokuhusika kwa kutoondoka, Yohana 8:29; 14:18
8. kuruhsu au kutoa kibali, Mt. 13:30; 19:14; Marko 14:6; Luka 13:8

Katika maana ya kitheolojia KITENZI pia kina matumizi mapana:

1. kufuta, kusamehe, kuifuta hatia ya dhambi, Kut.32:32 (70) (LXX); Hes. 14:19; Yak. 42:10 na Agano Jipya, Mt. 6:12,14-15; Marko 11:25-26
2. kujiondoa toka dhambini, 2 Tim. 2:1
3. kukataa kwa kujiondoa toka kwenye
  - a. Sheria, Mat. 23:23; Matendo 21:21
  - b. imani, Ezek. 20:8 (LXX); Luka 8:13; 2 The. 2:3; 1 Tim. 4:1; Ebr. 3:12

Waamini wa sasa wanauliza maswali mengi ya kitheolojia ambayo waandishi wengi wa Agano Jipya wasingalifikiri kuyahusu. Moja ya haya yangeliweza kuhusiana na uelekeo wa sasa wa kuitenga imani (uthibitisho) kutoka kwenye imani (utakaso).

Kuna watu katika Biblia walihusishwa miongoni mwa watu wa Mungu na jambo lililotokea na kusababisha wao kuondoka.

- I. Agano la Kale
  - A. Wale walioisikia taarifa ya wale wapelelezi kumi na wawili (kumi), Namba 14 (kama vile Heb. 3:16-19)
  - B. Kora, Namba 16
  - C. Wana wa Eli, 1 Samueli 2, 4
  - D. Sauli, 1 Samueli 11-31
  - E. Manabii wa uongo (mifano)
    1. Kumb. 13:1-5 18:19-22 (nji za kumtambau nabii wa uongo)
    2. Yeremia 28
    3. Ezekieli 13:1-7
  - F. Manabii wa uongo
    1. Ezekieli 13:17
    2. Nehemia 6:14
  - G. Uovu wa viongozi wa Israeli (mifano)
    1. Yeremia 5:30-31; 8:1-2; 23:1-4
    2. Ezekieli 22:23-31
    3. Mika 3:5-12

II. Agano Jipya

- A. Hili neno la Kiyunani kifasihi linamaanisha "kuasi." Vitabu vyote vya Agano la Kale na Agano Jipya vinathibitisha uchochezi wa uovu na mafundisho ya uongo kabla ya Ujio wa Pili (kama vile Mt. 24:24; Marko 13:22;

Matendo 20:29,30; 2 The. 2:9-12; 2 Tim. 4:4). Neno hili la Kiyunani linaweza kuyaaakisi maneno ya Yesu katika Mfano wa Udongo unaopatikana katika Mathayo 13; Marko 4; na Luka 8. Kwa kudhaniwa walimu hawa wa uongo si Wakristo, bali waamini wachanga (kama vile Ebr. 3:12).

Swali la kitheolojia ni hili walimu wa uongo wanawapeleka wapi waamini? Hili ni vigumu kulijibu kwa kuwa kulikuwa na walimu wa uongo katika makanisa anzilishi (kama vile 1 Yohana 2:18-19). Mara nyingi tamaduni au madhehebu yetu yanajibu swali hili pasipokuwa na marejeo ya maandiko ya Biblia mahususi (isipokuwa njia ya kuhakiki kwa nukuu mstari ulio nje ya muktadha ili kwa uangalifu kuhakiki madhara yaliyomo).

B. Imani Thabiti

1. Yuda, Yohana 17:1
2. Simoni mchawi, Matendo 8
3. Wale waliozungumziwa katika Mt. 7:13-2
4. Wale waliozungumziwa katika Mathayo 13; Marko 4; Luka
5. Wayahudi wa Yohana 8:31-59

6. Alexanda na Himenayo, 1 Tim. 1:19-20
  7. Wale wa 1 Tim. 6:21
  8. Himanayo na Fileto, 2 Tim. 2:16-18
  9. Dema, 2 Tim. 4:10
  10. Walimu wa uongo, 2 Petro 2:19-22; Yuda 1:12-19
  11. wapinga Kristo, 1 Yohana 2:18-19
- C. mani isiyo kuwa na matunda
1. 1 Wakorintho 3:10-15
  2. 2 Petro 1:8-11

Mara chache tunafikiri juu ya haya maandiko kwa kuwa mfumo wa injili yetu (Ufuatao mtazamo wa Calvin, Arminian, n.k.) unaamuru mwendaji wa kimamlaka. Tafadhari usinihukumu kabla kwa kuwa nafundisha somo langu. Shauku yangu ni hatua ya kiufasiri. Tunapaswa kuipa nafasi Biblia ili izungumze nasi na si kuiumba katika mpangilio wa thiolojia iliyopita. Mara nyingi hii inaumiza na kushtua kwa kuwa thiolojia zetu zilizo nyingi ni za kimadhehebu, kitamaduni, kimahusiano (mzazi, rafiki, mchungaji), si za kibiblia (tazama [Mada Maalumu: Nini maana ya neno "Kupokea," "Kuamini," "Kiri/Ungama," na "Itisha"?](#)). Wengine walio miongoni mwa watu wa Mungu wanarudi nyuma na kutokuwa miongoni mwa watu wa Mungu (m.f. Rum. 9:6).

☐ **"atakayeingia katika ufalme wa mbinguni"** hii ni ishara ya wakati ujao. Ufalme ndio lengo kuu la mahubiri ya Yesu. Inafanana na tungo "ufalme wa Mungu" iliyotumika kwenye Marko na Luka. Mathayo, aliyewaandikia Wayahudi, alitumia "mbinguni" kama maneno ya kuzungusha kwa ajili ya "Mungu." Mara nyingi mstari huu unadokeza wakati ujao, ambapo Mt. 3:2 inadokeza wakati wa sasa uliopo. Ufalme wa mbinguni ni utawala wa Mungu kwenye miyo ya wanadamu sasa ambao siku moja utatimilizwa kwa ulimwengu wote. Yesu, kwenye mtindo wake wa maombi ya Mt. 6:10, aliomba kwa ajili ujio wa ufalme wa Mungu ulimwenguni.

☐ **"bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni"** hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo. Malengo halisi ya mistari michache ifuatayo ni kwa watu ambao husema wao ni ufalme lakini wanaishi katika njia ambazo hazifunui maisha ya ufalme. Hili linaweza kuonekana kwenye kifungu cha hitimisho katika Mt. 7:23, na katika Mt. 7:24 na 26. Mapenzi ya Mungu yanaelea kwamba kila mmoja amwamini mwana wake (kama vile Yn. 6:29, 39-40). Uhusiano huu binafsi ndio ambao hawa wenye dini, manabii wa uongo hawakuwa nao (kama vile Mt. 7:23).

Muundo huu wa ukweli kinzani au upembuzi ni tabia ya ukweli kibiblia. Mapenzi ya Mungu ni maamuzi yote ya awali (mlango) na kuendeleza mtindo wa maisha (njia).

## **MADA MAALUM: MAPENZI (*thelēma*) YA MUNGU**

"Mapenzi" ya Mungu yamejikita katika namna mbalimbali.

### **INJILI YA YOHANA**

- Yesu alikuja kuyatenda mapenzi ya Baba yake (kama vile Yohana 4:34; 5:30; 6:38)
- Kuwafufua siku ya mwisho wote Baba aliowampa Mwana (kama vile Yohana 6:39)
- Kwamba wote waamini katika Mwana (kama vile Yn. 6:29; 40)
- Maombi yaliyojibiwa kuhusiana na kuyatenda mapenzi ya Mungu (kama vile Yn 9:31 na Yn 5:14)

### **VIDOKEZO VYA INJILI**

- Kuyatenda mapenzi ya Mungu ni jambo la muhimu (kama vile Mt. 7:21)
- Kuyatenda mapenzi ya Mungu hutufanya kuwa kaka na dada pamoja na Yesu (kama vile Mt. 12:50; Marko 3:35)
- Sio mapenzi ya Mungu kwa yeyote kuangamia (kama vile Mt.18:14; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9)
- Kalvari ilikuwa ni mapenzi ya Mungu kwa Yesu (kama vile Mt. 26:42; Luka 22:42)

#### NYARAKA ZA PAULO

- ukomavu na huduma ya waamini wote (kama vile Rum. 12:1-2)
- waamini waliondolewa kutoka katika enzi hii ya maovu (kama vile Gal. 1:4)
- mapenzi ya mungu ulikuwa ni mpango wake wa ukombozi (kama vile. Efe.1:5, 9,15)
- waamini wanapitia na kuishi maisha yaliyojazwa na Roho (kama vile 5:17-18)
- waamini wamejazwa na maarifa ya Mungu (kama vile Kol. 1:9)
- waamini wanafanywa kuwa imara na wakamilifu (Kol. 4:12)
- waamini wanatakaswa (kama vile 1 The. 4:3)
- waamini watoa shukrani katika vitu vyote (kama vile The.5:18)

#### NYARAKA ZA PETRO

- Waamini wanatenda haki (yaani, kunyenyekea kwenye mamlaka ya chini) na, kwa hiyo wanawanyamazisha watu wajinga, hivyo kuwapa fursa kwa kuijua injili/matendo mema (kama vile 1 Pet. 2:15)
- Mateso ya waamini (kama vile 1 Pet. 3:17; 4:19)
- Waamini hawapaswi kuishi maisha ya ubinafsi (kama vile 1 Pet. 4:2)

#### NYARAKA ZA YOHANA

- waamini kuendelea kudumu milele (kama vile Yohana 2:17)
- waamini ni kielelezo kwa maombi yaliyojibiwa (kama vile 1 Yohana 5:14)

**7:22 "Wengi wataniambia siku ile"** muundo wa swali hili la kiyunani unatalajiwa "ndio" jibu lake.

Tungo hii "siku ile" inarejelea ujio wa pili wa Yesu Kristo. Hii mara nyingi huitwa siku ya ufufuo au siku ya hukumu, inategemea na unavyomjua binafsi au hapana.

☑ **"kwa jina lako. . .kwa jina lako. . .kwa jina lako"** tungo hii inadokeza "kwa mamlaka yako" au "kama mwanafunzi wako." Ni dhahili kutoka Mt. 7:23 kwamba hawakumjua Yesu kwa njia sahihi. Tambua kwamba kazi walizofanya ni vipawa vya kiungu. Lakini matunda bila uhusiano ni chukizo sana kama uhusiano bila matunda. Aina hii ya miujiza inafanana na ile iliyotendwa na wanafunzi wa kweli wa Kristo (kama vile Mt. 10:1-4), pamoja na Yuda Iskariote! Miujiza sio ishara ya moja kwa moja toka kwa Mungu (kama vile Mt. 24:24 na 2 Thes. 2:9-10). Kujilinda binafsi kwa viongozi wa kidini ni masikitiko.

☑ **"kutoa pepo"** tazama mada maalum: Upungaji pepo katika Mt. 10:1 na pepo wachafu katika Mt. 10:1.

**7:23 "Ndipo nitawaambia dhahiri"** neno hili la kiyunani linamaanisha "sema wazi" au "kukiri" kwa watu wote (tazama mada maalum katika Mt. 10:32). Dokezo la maelezo haya ni kwamba Yesu ana sehemu na mamlaka ya kuhukumu na kwamba hukumu ni ya kwenye mahusiano ya imani binafsi kwake.

☑ **"Sikuwajua ninyi kamwe"** huu ni muundo imara wa kisarufi kwa Kiyunani. Neno "kumjua" lina utambuzi katika Agano la kale likimaanisha "uhusiano binafsi, wa moyoni" (kama vile Mwa. 4:1 na Yer.1:5). Inatuogopesha kufikilia kwamba ni matendo ya wenye dini katika Mt. 7:22 waliweza kutenda kwa njia ya kujidanganya (kama vile 1 Kor. 13:1-3).

☑ **"ondokeni kwangu"** hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo, amri endelevu inayoonyesha wazi kama "endelea kutoka kwangu" dokezo hilo linamaanisha "unaendelea kupotelea mbali –endelea kwenda!" ni taswira ya Zab. 6:8.

☐ "ninyi mtendao maovu" inashangaza kuwa ni dhahili iliwaathiri hawa viongozi wa kidini waliokuwa na uhuru wa nguvu na ubinafsi wa Kristo.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 7:24-27**

<sup>24</sup> Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba; <sup>25</sup> mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba. <sup>26</sup> Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyaafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga; <sup>27</sup> mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, ikaanguka; nalo anguko lake likawa kubwa.

**7:24 "Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya"** huu ni mfano wa kipekee katika Mathayo na Luka (6:47-49). Hii inafanana na fikra ya kwenye neno la kiebrania *Shema* ya Kumb. 6:1 ambapo neno linadokeza "kutenda kama ulivyosikia." Wakristo wanahusika (1) ufahamu; (2) mwitikio binafsi; na (3) huduma ya mtindo wa maisha. Inatia shauku kote kwamba wajenzi walisema walisikia maneno ya Yesu. Tena, inaonekana kama muktadha wa maonyo haya ni ya wenye dini ambao walisikia na kuitikia kwa kiwango sawa.

**7:24-27** mistari hii inafanana na ukweli wa Mathayo 13, mfano wa udongo. Ni kwa kupitia mateso pekee na hatari kwamba tabia ya kweli ya "kudhania" kwa waaminio imefunuliwa. Maisha ya mateso ni kitu kinachowezekana kwa wakristo (kama vile Yn. 15:20; 16:33; Mdo 14:22; Rum. 8:17; 1 Thes. 3:3; 2 Tim. 3:12; 1 Pet. 2:21; 4:12-16).

**7:26** inatia shauku kwamba wajenzi wote walisema walisikia maneno ya Yesu. Tena, inaonekana kama muktadha wa maonyo haya ni ya wenye dini ambao walisikia na kuitikia kwa daraja sawa. A.T. Robertson anasema kwenye *Word Pictures in the New Testament*, "kusikia mahubiri ni jambo la hatari sana kama hautaweka katika matendo," uk. 63, na ningependa kuongeza, kama yalivyoandikwa na uyatekeleze (yaani mahubiri).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 7:28-29**

<sup>28</sup> Ikawa, Yesu alipoyamaliza maneno hayo, makutano walishangaa mno kwa mafundisho yake; <sup>29</sup> kwa maana alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi wao.

**7:28 "Ikawa, Yesu alipoyamaliza maneno hayo"** Mathayo ametumia tungo hii kufunga sehemu kadhaa muhimu kwenye injili yake (kama vile Mt. 7:28; 11:1; 13:53; 19:1; 26:1). Inawezekana ni moja ya mstari unaonyesha umbo la kitabu.

☐ "makutano walishangaa mno kwa mafundisho yake" mafundisho ya Yesu yalikuwa tofauti ya waandishi. Msingi wa mamlaka yake haukuwa kwa waalimu waliomtangulia, lakini kwake yeye mwenyewe. Kipengele hiki cha cha mamlaka ya Yesu ni sifa ya injili ya Mathayo (kama vile Mt. 8:9; 9:6, 8; 10:1; 21:23-24, 27; 28:18). Yesu alitangaza sehemu zote za masihi aliyeahidiwa (yaani Musa mpya au mtoaji wa sheria mpya) na hakimu wa matukio ya siku za mwisho.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je ni kosa kwa wakristo kuwahukumu wengine?
2. Je ni nini mstari wa 6 unamaanisha?
3. Je mstari wa 7 unadokeza kwamba uvumilivu wa mwanadamu unaweza kumsaidia katika maombi?
4. Je mstari wa 13 unadokeza kwamba ni vigumu kuokolewa? Ni nini hasa hizi njia mbili?

5. Ni kwa namna gani wewe unamtambua nabii wa uongo?
6. Je neno “tunda” linamaanisha nini?
7. Je inawezekana kwa huduma kufanikiwa kuwa mamlaka mbali na uhusiano binafsi na Kristo?
8. Kuna uhusiano gani kati ya kusikia na kutenda kwenye imani ya Mkristo?
9. Je mateso yanahitajika kwenye maisha ya mkristo?



## MATHAYO 8

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Kumtakasa mwenye Ukoma	Yesu Anantakasa Mwenye Ukoma	Matukio yaliyofanyika katika Galiya  (8:1-9:38)	Yesu Ananfanya Mwenye Ukoma Kutakasika	Tiba kwa Mtu Mwenye Ugonjwa wa Ngozi
8:1-4	8:1-4	8:1-4	8:1-2  8:3-4	8:1-4
Uponyaji wa Mtumishi Wa Akida	Yesu anamponya Mtumishi wa Akida	8:5-13	Yesu Anamponya Mtumishi wa Akida Wa Kirumi  8:5-6  8:7  8:8-9  8:10-13b  8:13c	Tiba ya Mtumishi wa Akida  8:5-13
8:5-13	8:5-13	8:5-13	8:5-6  8:7  8:8-9  8:10-13b  8:13c	8:5-13
Uponyaji wa Watu Wengi	Mkwe wa Petro Anaponywa  Wengi Waponywa Baada ya Jioni ya Sabato	8:14-17	Yesu Anawaponywa Watu Wengi wa  8:14-15  8:16-17	Tiba kwa Mkwe Petro  Idadi ya Tiba  8:16-17 (17b)
8:14-17	8:14-15  8:16-17	8:14-17	8:14-15  8:16-17	8:14-15  8:16-17 (17b)
Tutakuwa Wafuasi Wa Yesu	Gharama ya Uanafunzi	8:18-22	Kuwa Wafuasi wa Yesu  8:18-19  8:20  8:21  8:22	Kujitoka kwa Hiari  8:18-20  8:21-22
8:18-22	8:18-22	8:18-22	8:18-19  8:20  8:21  8:22	8:18-20  8:21-22

Kimbunga Kinakoshwa	Upepo na Mawimbi yanamtii Yesu		Yesu Anayakemea Mawimbi	Kuyakemea ya Bahari
8:23-27	8:23-27	8:23-27	8:23-27	8:23-27
Uponyaji wa Watu Wenye pepo katika waliokuwa Kambi ya Wagerasi	Mtu mwenye pepo Anaponywa		Yesu Anawaponya Watu Wawili	Watu wenye pepo  katika kambi ya Wagerasi
8:28-34	8:28-34	8:28-34	8:28-29  8:30-31  8:32  8:33-34	8:28-34

## **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka [“Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia”](#)) KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembe katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## **HISTORIA YA NYUMA YA MATHAYO 8:1-34**

A. Mathayo 8 na 9 inaunda muungano wa kimaandishi wa miujiza kumi yenye kueleza uwezana mamlaka ya Yesu kwa wanadamu, lakini magonjwa na asili. Si kwa bahati mbaya kwamba uweza miujiza ya uweza huu unafuatisha Hotuba ya Mlimani. Miujiza hii ilimaanisha (1) kuuthibitisha ujumbe wa Kristo, (2) kuonyesha ukweli wa mpangilio wa siku za mwisho, na (3) kuonyesha uhuru wa Uhungu.

- B. Katika sura hii makundi kadhaa yalipingwa na jamii ya Kiyahudi yaliyohudumiwa na Yesu.
1. mkoma - Mt. 8:2,4 (Mt. 10:8; 11:5; 26:6; Luka 5:12-14; 17:11-14)
  2. Mataifa (yaani., akida wa Kirumi) - Mt. 8:5-13 (kama vile Marko 7:26-30,31-37)
  3. wanawake - Mt. 8:14-15 (kama vile Luka 8:2,43-48; 7:36-50; 13:10-12)
  4. Mwenye pepo, Mt. 8:16,28

Orodha hii inaweza kupanuliwa kwa urahisi.

1. watoto - 18:2 (katika muktadha huu hii ni stiari ya waamini wapya); Marko 10:13-16; Luka 18:15-17
2. maskini –

3. Wasamaria - Luka 10:30-37; 17:15-19; Yohana 4:1-54
4. Watoza ushuru- Marko 2:15-17; Luka 5:27-32; 15:1na kuendelea; 19:1-10
5. Watenda dhambi (wale waliyoyakiuka mapokeo) - Mt. 9:10-11; 11:19; Luka 15:2; 18:13; Yohana 9:16,24,25,31 Umakini wa Yesu kwa uponyaji na uponyaji wa watu hawa ulikuwa ukamilifu wa unabii wa Agano la Kale (kama vile Mt. 11:5, ambao unanukuu Isa. 35:5-6; na 61:1, pia uangalie ufanano ulio katika Luka 7:22).

C. Kuna tofauti zinazohusiana na wakati, mahali, na maelezo yayohusishwa katika ufafanuzi huu kama ilivyonyukuliwa katika Vidokezo vya Injili. Tofauti hizi zinazungumzia (1) uwezo wa kila mwandishi wa Injili chini ya uvuvio ili kuuumba uinjilishaji wake/uwasilishaji wa kikatekisimu wa Yesu kwa hadhira fulani na (2) uhalisia wa maelezo ya ushahidi wa macho. Hatuwezi kulieleza neno "kwa nini" na "kwa namna gani" la muunganiko wa Injili, bali tunaweza kuukubali uaminifu wao, uvuvio, na mamlaka yao kwa ajili ya maisha yetu!

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 8:1-4

<sup>1</sup> Naye aliposhuka mlimani, makutano mengi walimfuata. <sup>2</sup> Na tazama, akaja mtu mwenye ukoma akamsujudia, akisema, Bwana, ukitaka, waweza kunitakasa. <sup>3</sup> Yesu akanyosha mkono, akamgusa, akisema Nataka; takasika. Na mara ukoma wake ukatakasika. <sup>4</sup> Yesu akamwambia, Angalia, usimwambie mtu; ila enenda zako, ukajionyeshe kwa kuhani, ukaitoe sadaka kama alivyoamuru Musa, iwe ushuhuda kwao.

**8:1 "Naye aliposhuka mlimani"** Usemi huu na 5:1 inaunda sura ya kiuandishi. Kwa uwazi kabisa Mathayo alikuwa akilirejelea hitimisho la Hotuba ya Mlimani, Mathayo 5-7. Wengine wanalifasiri hili kama Yesu mleta sheria wa pili, akiufuatisha mlima kama Musa alivyofanya, Yesu aliileta Sheria mpya, hakuipokea!

☐ **"makutano mengi walimfuata"** Sababu za kufanya miujiza zilikuwa ni kuleta uthabiti wa ujumbe. Mwanadamu aliyeanguka mara nyingi huvutiwa na mambo ya muda mfupi, shauku yake binafsi, mambo mbalimbali badala ya umilele, ushirika, na yale ya kiroho!

**8:2 "akaja mtu mwenye ukoma akamsujudia"** Neno letu la Kiingereza "mwenye ukoma" linatokana na neno la Kiyunani "magamba." Neno la kale lilimaanisha ugojwa ulioenea katika ngozi nzima kuliko istilahi yetu ya sasa. Mambo ya Walawi 13 na 14 inashughulika na mifano ya ukoma ulio katika Agano la Kale. Hii dhana kwamba mtu mwenye ukoma alimkaribia Yesu kijamii na kithiolojia haikuwa sahihi kwa kuwa ukoma ulitazamwa kama ugonjwa ulioachiliw kama hukumu toka kwa Mungu. Misingi ya Agano la Kale na ile ya kithiolojia ya hili ilikuwa ya Mfalme Uzia, 2 Nyak. 26:16-23.

☐ **"Bwana"** Neno hili *kurios*. Hili linaweza kutumika kama wadhifa kama "Bwana" au kama wadhifa wa kithiolojia wa Uungu wa Yesu wa Kimasihi. Muktaadha ndiyo wenyekutambulisha ni matumizi yaliyokusudiwa. Mara nyingi hili halifahamiki, kama ilivyo katika muktaadha huu.

☐ **"ukitaka"** Hii ni sentensi amrishi daraja la tatu, yenye kumaanisha kuwepo kwa uwezekano wa tendo lijalo. Mtu huyu alikuwa amesikia juu ya miujiza ya Yesu na kuamini kuwa angempatia tiba ikiwa angekua na uwezo.

**8:3 "Yesu akanyosha mkono, akamgusa"** Tendo la kumgusa mtu mwenye ukoma lilikuwa kinyume na utamaduni wa siku zile utamaduni uliojikita katika amrishi la Agano la Kale (kama vile Law. 13:45-46). Tendo hili lilionyesha huruma ya Yesu, kutokuwa na woga, na hiari ya kuzivunja desturi za Kiyahudi (kama vile Mt. 5:21-48).

☑ **"Nataka"** Mtu huyu alikuwa na imani katika uwezo wa Yesu uliojikita katika kile alichokisikia, lakini hakuwa na uhakika wa hiari ya Yesu!

**8:4 "Angalia, usimwambie mtu"** Aina hii ya usemi mara nyingi inaitwa siri ya Kimasihi ya Kividokezo (kama vile Mt. 8:4; 9:30; 12:16; 16:20; 17:9; Marko 1:44; 3:12; 5:43; 7:36; 8:30; 9:9; Luka 4:41; 5:14; 8:56; 9:21). Hii inahusiana na hiari ya Yesu yenye kujulikana baada kama msikilizaji. Ujumbe wa Injili ulikuwa haujatimia (kama vile Mt. 17:9; Marko 9:9). Alifahamu kwamba wanadamu wagekuwa na mwitikio kwake kwa nakusudi yasiyo sahihi.

☑ **"ila enenda zako, ukajionyeshe kwa kuhani. . . iwe ushuhuda kwao"** Hii ni jitihada iliyofanywa na Yesu ilikuithibitisha sheria ya Musa ya Mambo ya Walawi 13-14. Pia ilikuwa jitihada ya kuonyesha uweza wake kwa makuhani waliokuwa Yerusalemu (kama vile Marko 1:44; Luka 5:14; 17:14). Hapo mwanzo katika kitabu cha Matendo ya Mitume maelfu mengi ya watu hao yalimkiri Yesu na ujumbe wake (kama vile Matendo 6:7).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 8:5-13**

<sup>5</sup> Hata alipoingia Kapernaumu, akida mmoja alimjia, <sup>6</sup> akamsihi, akisema, Bwana, mtumishi wangu amelala nyumbani, mgonjwa wa kupooza, anaumwa sana. <sup>7</sup> Yesu akamwambia, Nitakuja, nimponye. <sup>8</sup> Yule akida akamjibu, akasema, Bwana, mimi sistahili wewe uingie chini ya dari yangu; lakini sema neno tu, na mtumishi wangu atapona. <sup>9</sup> Kwa maana mimi nami ni mtu niliyewekwa chini ya mamlaka, mwenye askari chini yangu; nikimwambia huyu, Nenda, huenda; na huyu, Njoo, huja; na mtumwa wangu, Fanya hivi, hufanya. <sup>10</sup> Yesu aliposikia hayo, alistaajabu, akawaambia wale waliomfuata, Amin, nawaambieni, Sijaona imani kubwa namna hii, kwa ye yote katika Israeli. <sup>11</sup> Nami nawaambieni, ya kwamba wengi watakuja kutoka mashariki na magharibi, nao wataketi pamoja na Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo katika ufalme wa mbinguni; <sup>12</sup> bali wana wa ufalme watatupwa katika giza la nje, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno. <sup>13</sup> Naye Yesu akamwambia yule akida, Nenda zako; na iwe kwako kama ulivyoamini. Mtumishi wake akapona saa ile ile.

**8:5 "Kapernaumu"** Mji huu baadaye ulikuwa makao makuu ya Yesu Mgalilaya baada ya kukatalliwa kwake huko Nazareti (kama vile Mt. 4:13). Hili ni eneo lililo kati. Petro na Andrea walikuwa na makazi mahali pale.

☑ **"akida"** Hakuna watu waliochukiwa sana katika jamii ya Kiyahudi kama wenye ukoma (Mt. 8:2) na najemedari wa Kirumi. Hii ni dhana yenye kueleza upendo wa Yesu kwa wanadanu wote, kama alivyowahudumia watu wenye pepo katika kambi ya Wagerasi. Mt. 8:28, 34; na mwanamke Mkananayo (Mt.15:21-28). Maelezo haya haya yanafananishwa na yale yaliyo katika Luka 7:1-10, lakini yako katika mpangilio tofauti.

**8:6 "mtumishi wangu"** Maelezo haya yaliyo katika Luka yananukuu kwamba mtu huyu alikuwa na upendo mkubwa kwa watu wa Kiyahudi (kama alivyofanya Kornelio wa Matendo 10). Maelezo yaliyo katika Mathayo yanaonyesha kwamba huyu alikuwa na upendo mkubwa kwa mtumishi wake. Katika Agano Jipya mara nyingi Maakida wa naelezwa katika namna chanya.

**8:7 "Nitakuja, nimponye"** Haya ni matmizi yeye msistizo ya neno "ni," ambalo linaelezwa katika Mt. 8:8 tendo la Yesu kuingia kwa hiari katika myumba ya mtu wa Mataifa tendo ambalo halikuwahi kusikika, na tendo ambalo lilikuwa mwiko kitamadauni/kidini.

**8:8 "sistahili"** Neno hili linatumika katika usemi wa

1. Yohana Mbatizaji -3:11; Marko 1:7; Luka 3:16

## 2. Akida wa Kirumi - 8:8; Luka 7:6

Katika maana ya kithiolojia neno hili linaeleza hali ya dhambi za wanadamu wote pamoja na upendo na huruma ya Mungu ya kustaaajabisha. Yawapasa wanadamu kutambua hitaji lao la kiroho (kama vile Mt. 5:3-6) kabla ya kuwa na uwezo wa kuupokea msanaha na ukubalifu wa Mungu.

■ **"sema neno tu, na mtumishi wangu atapona"** Mtu huyu, aliyekuwa wa kijeshi, aliielewa mamlaka na hakuwa na dai la kimila, au mawazo ya kishirikina, au hata uwepo wa Yesu kwa ajili ya uponyaji. Katika Luka akida huyu hakuja kwa Yesu kibinafsi, bali aliwatuma wawakilishi: (1) wazee wa Kiyahudi (kama vile Luka 7:3-5) na (2) narafiiki zake (kama vile Luka 7:6). Huu ni mfano mzuri wenye kuonyesha namna Injili zinavyoyanukuu matukio yale yale katika namna tofauti. Swali haliulizi ni maelezo gani yaliyo sahihi bulini kwa nini waandishi walililukuu tukio hili katika namna walivyofanya. Tazama Gordon Fee and Douglas Stuart, *How to Read the Bible for All Its Worth*, kr. 127-148. Waponyaji wa Kiyahudi na Kiyunani walikuwa wakiponya kupiia nyimbo, mazingaonbwe, na matambiko maalum, lakini Yesu aliponya kwa neno lililolenwa. Hii ilikuwa njia ya kuonyesha

1. Uhusiano wake na uumbaji (yaani., Mwanzo 1)
2. Mamlaka yake ya kipekee (kama vile Mt. 8:16)
3. Tofauti yake na waponyaji wengine wa nyakati zake

Hii ndiyo sababu jina *logos* (nneo) linaendana sana na Yohana 1:1! Yesu a ngekuwa na uwezo wa kuponya kwa kugusa (kama vile Mt. 8:3) au kuzungumza neno (kama vile Mt. 8:8), pamoja na kuyafukuza mapepo (kama vile Mt. 8:16). Alizungumza kwa mamlaka (kama vile Mt. 7:28-29); Aliponya kwa mamlaka!

Pia inafurahisha namna alivyotumia maelezo katika Mathayo "kilichonenwa. . .kilitimia" (kama vile Mt. 1:22; 2:15,17,23; 4:14; 8:17; 12:17; 13:35; 21:4; 22:31; 24:15; 27:9) kama njia ya kueleza uaminifu wa Maandiko na utimilifu wake katika Yesu na zama mpya alizozihimarisha.

### 8:10

**NASB "Amin, nawaambieni"**

**NKJV "Hakika nawaambia"**

**NRSV "kwa ukweli nawaambia"**

**TEV "Naawaambieni"**

**JB "Nawaambia kwa yakini"**

**NJB "Katika hakika nawaambia"**

Hii ilikuwa namna tofauti ya Yesu ya kuonyesha msistizo. Kuna mifano mingine katika maandishi ya Kiyunani. Matumizi ya namna moja au mbili ya neno "amin" ya kuanza mazungumzo yalikazia umuhimu wa usemi huo, pamoja na ma mamlaka ya Yesu ya kipekee. Tazama Mada Maalum katika Mt. 5:18.

**8:11 "wengi watakuja kutoka mashariki na magharibi, nao wataketi pamoja na Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo katika ufalme wa mbinguni"** Hili lilikuwa dokezo la jumuisho la Mataifa katika familia ya Mungu (kama vile Isa. 25:6-9; Mal. 1:11; Luka 13:22-30). Imani ya huyu je medari wa Kirumi ilikuwa kubwa kuliko zile alizowai kukumbana nazo miongoni mwa watu wa Kiyahudi. Kukumbana huku pamoja na wat Mataifa (yaani., Mt. 15:28; 21:32; Marko 7:24-30; Luka 10:30-37; 17:11-19), kuliunganisha semi za Yesu zenye nguvu zenye kuhusiana na imani yao ni ushahidi wa asili ya kiulimwengu na shabaha ya uinjilishaji wa injili (kama vile Mt. 15:28; 22:2-14; 28:18-20; Luka 7:9; 24:47; Matendo 1:8). Uwekaji wa vifungu ulitokana na dhana ya karamu ya ki-Masihi nyakati za mwisho (kama vile Isa. 25:6-9; Luka 14:15; Ufu. 19:9). Yesu amnawazungumzia Mababa hawa wa imani kama walio hai katika ufalme wa mbinguni (yaani., zama mpya). Hawa watashiriki kwa ukamilifu katika matukio ya siku za mwisho, pamoja na waamini wengine. Hakika huu ni ushahidi wenye nguvu wa maisha halisi ya uzima baada ya

kifo, pamoja na ahadi za ushirika na Mungu na waamini wengine.

**8:12 "bali wana wa ufalme watatupwa katika giza la nje"** Wayahudi wengi hawakufahamu cho chote kuhusu uhusiano binafsi na Mungu bali rangi tu, sheria, na taratibu za kidini zilizokuwa zilizokuwa zimeshikiliwa (kama vile Isa. 6:9-10; 29:13; Mt. 15:14). Hawa walijivuna na kujihesabia haki hali iliyojikita katika rangi zao na utendaji Agano la Musa (kama vile Mt. 3:9). Yesu analilisistiza hili katika Mt. 8:12 kwamba wengi ambao kihistoria hawakuwa watu wa Mungu watajumuishwa, na wengi ambao walifikiri kuwa wao ni sehemu ya watu wa Mungu watatengwa (kama vile Mt. 21:43; Luka 13:28).

■ **"katika giza la nje, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno"** Stiari hizi pia zilitumika katika Mt.13:42,50; 22:13; 24:51; 25:30 kueleza hofu ya utengano na Mungu hmo jehanamu (*Gehenna*, tazama Mada Maalum katika Mt. 5:22). Tazama wanaume na wanawake walio na Yesu Kristo ambao sasa wanaitambua hatima yao milele (kama vile Mt. 25:31-46). Yesu Mwenyewe ndiye anayetonyesha hofu hofu mbali mbali itakayowapata wale waliokataa kumwamini. Katika Agano la Kale kifungu "kusaga meno" kiliashiria "ghadhabu" (kama vile Ayubu 16:9; Zab. 35:16; 37:12; 112:10; Omb. 2:16), kama liyo katika Matendo 7:54, lakini hapa kinamaanisha uchungu na maumivu wa hukumu ya siku za mwisho (yaani, kutenganishwa na Mungu katika *Gehenna*).

**ADIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 8:14-17**

<sup>14</sup> Hata Yesu alipofika nyumbani kwa Petro, akamwona mkwe wa Petro, mamaye mkewe, amelala kitandani hawezi homa. <sup>15</sup> Akamgusa mkono, homa ikamwacha; naye akaondoka, akawatumikia. <sup>16</sup> Hata kulipokuwa jioni, wakamletea wengi wenye pepo; akawatoa pepo kwa neno lake, akawaponya wote waliokuwa hawawezi, <sup>17</sup> ili litimie lile neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema, Mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu, Na kuyachukua magonjwa yetu.

**8:14 "Petro . . . mkwe"** Petro alikuwa na mke (kama vile 1 Kor. 9:5). Kifungu hiki kinazungumzia desturi ya ndoa miongoni mwa Wayahudi. Walimu wa sheria walikuwa wakisema kwamba ndoa ilikuwa wajibu kwa sababu ya agizo lililo katika Mwa. 2:24. Hatukuwahi kupata maelezo yanayomhusu mkewe; labda kwa wakati huo alikuwa amekwisha kufa. Injili hizi hazikuandikwa kwa ajili ya kutoshereza uchunguzi wetu.

**8:16 "Hata kulipokuwa jioni"** Hitimisho la siku ya Sabato lilikuwa limefika (Marko 1:32) na Wayahudi waliokuwa wamefundishwa ya kuwa uponyaji haukuruhusiwa kufanyika siku ya Sabato sasa walikuwa wakikusanyika mbele ya mlango wa Petro. Siku ya Sabato jioni ya siku ya Ijumaa na kumalizika siku ya Juma mosi jioni. Tendo hili lilifuatisha mtiririko wa siiku za uumbaji zilizo katika Mwa. 1:5,8,13,19,23,31.

■ **"wengi wenye pepo. . . akawaponya wote waliokuwa hawawezi"** Kuna tofati ya mara kwa mara iliyotengenezwa kati ya wenye mapepo na wale wenye magonjwa ya mwili katika Agano Jipya. Wakati mwingine pepo walisababisha matatizo ya kimwili, lakini si mara kwa mara. Naradhi ya kimwili, majeraha, na magonjwa si lazima yasababishwe na pepo. Tazama Mada Maalum: Pepo Wabaya (Roho Chafu) katika Mt. 10:1.

**8:17** Hii ni nukuu toka Isa. 53:4, lakini haitoki katika Maandiko ya Tafsri ya Agano la Kale la (Hebrania) wala Tafsri ya Agano la Kale (Tafsri ya Kiyunani). Hii ndiyo sehemu pekee katika Agano Jipya ambapo mstari huu unanukuliwa. Kifungu hiki kinatumiwa na makundi mengi ya sasa kukiri kwamba uponyaji wa kimwili ni asili ya Upatanisho. Mungu ni Mungu wa roho anayetenda katika maisha ya watu kwa ajili ya mema. Hakuna ushahidi wa kiroho wa kutosha wenye kujikita katika mstari huu kuthibitisha kwamba magonjwa hayo yote ya matukio yote si mapenzi ya Mungu na tatatibiwa ikiwa tutaitikia kwa imani ya kutosha au maombi (kama vile 2 Kor. 12:8-10; 2 Tim. 4:20). Zaburi 103:3b pia inanukuliwa mara yingi katika uhusiano na suala hili. Kuna ufanano wa uhusiano wa ushairi wa

Kiebrania kati ya 103:3a na 3b. Wote unarejelea msamaha wa kiroho. Katika Agano la Kale magonjwa ya kimwili yalitumika kama alama ya matatizo ya kiroho (yaani., Isa. 1:5-6). Walimu wa sheria waliiona dhambi na maradhi kama vitu vyeye kuhusiana (kama vile Yakobo 5:14-16). Tazama F. F. Bruce, *Answers to Questions*, kr. 44-45.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 8:18-22**

<sup>18</sup> Naye Yesu alipoona makutano mengi wakimzunguka, aliamuru kuvuka kwenda ng'ambo. <sup>19</sup> Mwandishi mmoja akamwendea, akamwambia, Mwalimu, nitakufuata ko kote uendako. <sup>20</sup> Yesu akamwambia, Mbweha wana pango, na ndege wa angani wana viota; lakini Mwana wa Adamu hana pa kulaza kichwa chake. <sup>21</sup> Mwingine katika wanafunzi wake akamwambia, Bwana, nipe ruhusa kwanza, niende nikamzike baba yangu. <sup>22</sup> Lakini Yesu akamwambia, Nifuate; waache wafu wazike wafu wao.

**8:19 "Mwandishi"** Huyu alikuwa mahiri katika mapokeo ya sheria (kitabu cha sheria za Kiyahudi) na mapokeo ya Wayahudi (Maandiko) yaliyoandikwa. Hawa walichukua nafasi ya Mlawi wa Agano la Kale katika kuyatafsiri Maandiko. Hawa walirejelea namna ya kuitumia Sheria ya Musa kwa mambo ya kila siku. Tazama Madam Maalum : Waandishi katika Mt.12:38. Katika nyakati za Yesu wengi wao walikuwa Mafarisayo (tazama Mada Maalum katika Mt. 22:15).

☐ **"Mwalimu"** Huu ni muundo wa kauli ya mneni (*didaskale*) ya neno "mwalinu" (*didaskalos*). Uhuu unallitafsiri neno la Kiebrania "mwalimu" (kif. "kuu," kama vile Yohana 1:38; 20:16) na unamrejelea yule aliyejua Sheria ya Musa (yaani., jina la heshima). Huu unatumika katika Agano Jipya juu ya

1. walimu wa Kiyahudi - Luka 2:46
2. Yohana Mbatizaji - Luka 3:12
3. Yesu - Mt. 8:19; 9:11; 17:24; 26:25,49; Marko 9:5,17,38; 11:21; Luka 10:25; Yohana 1:49
4. Nikodemo- Yohana 3:10
5. Paulo - 1 Tim. 2:7; 2 Tim. 1:11
6. Walimu wa ki-Kristo – Matendo 3:1; 1 Kor. 12:28; Efe. 4:11; Yakobo 3:1

Yesu anapinga matumizi ya hili neno/jina lake Mwenyewe (kama vile Mt. 23:7-12; Marko 14:14; Yohana 3:2; 11:27-28; 13:13-14). Kuna neno mwalimu "moja" tu Baba; kuna neno moja tu "mmoja"! Yeye ndiye wa kweli pekee "Aliye Mkuu" !

**8:20 "Yesu akamwambia"** Watu watatu wanahusishwa katika andiko hili. Mmoja alikwa na hiari ya kwenda mahali po pote pale; Yesu alimwambia kustisha na kuhesabu gharama (kama vile Mt. 8:20). Wengine walikaidi kuyafuatisha; Yesu akamwambia, kunfuata kwa gharama yo yote kwa sababu ya kipaumbele cha wito wa Mungu juu ya maisha ya mwanadamu (kama vile Mt. 8:21). Mara nyingi inatengwa katika namna mbili!

☐ **"Mwana wa Adamu"** Hili ni jina la kipekee mbalo Yesu alijichagiliwa. Hiki kilikuwa kifungu cha Kiebrania chenye kumrejelea mwanadamu (kama vile Zab. 8:4; Eze. 2:1). Lakini kwa sababu ya matumizi yake yaliyo katika Dan. 7:13, hiki kilichukuwa viwango vya Uungu. Hivyo, hili neno linaunanisha ubinadamu na Uungu wa Yesu. Jina hili halikutumiwa na walimu wa Sheria za Kiyahudi; hivyo, hiki hakikuwa na dondoo za kiuzalendo au kijeshi. Hapa kuna nukuu inayotokana na maoni yangu juu ya Danieli 7:13.

☐ **"mwana wa adamu akija"** Hiki kifungu cha kiaramu ("ben *enosh*," tungo BDB 1085 na 1081) "mwana wa adamu" ni tofauti na ufanano wa kifungu cha Kiebrania ("ben *adam*") kinachopatikana katika Zaburi na Ezekieli. Vifungu vyote vinatumika katika ufanano ulio katika Ayubu 25:6; Zab. 8:4; 90:3; 144:3; Isa. 13:12. Kwa namna iliyo dhahiri hiki kinamrejelea Masihi na kinaunganisha ubinadamu wake (kama vile Dan. 8:17; Ayubu 25:6; Zab. 8:4;

Eze. 2:1), ambacho ni maana ya vifungu vya Kiaramu na Kiebrania, "mwana wa adamu" pamoja na Uungu wake kwa sababu mawingu ni usafiri wa Uungu (kama vile Mt. 24:30; 26:64; Marko 13:26; 14:62; Ufu. 1:7; 14:14). Yesu anatumia kifungu hiki kujirejelea mwenyewe katika Agano Jipya. Hiki hakikutumika kumaanisha Masihi katika dini ya Kiyahudi. Hiki hakikuwa na utengano, uzalendo, maana nyingine za kijeshi. Kwa namna ya kipekee hiki kinamweleza Masihi kama mwanadamu kamili na Mungu kamili (kama vile 1 Yohana 4:1-3). Matumizi ya Danieli ni ya kwanza yenye kutazamia katika kipengele cha Uungu wake! Yesu anatumia kifungu hiki kwa ajili yake mwenyewe katika maana tatu.

1. Kuteswa kwake na kifo chake (m.f., Marko 8:31; 10:45; 14:21; Luka 9:22,44)
2. Kuja kwake kama Mwamuzi (m.f., Mt. 16:27; 25:31; Yohana 5:27)
3. Kuja kwake katika utukufu kuuhimarisha ufalme wake (m.f., Mt. 16:28; 19:28; Marko 13:26-27; 14:62)

Kutokana na *The Jewish Study Bible*, uk. 1657 (pia tazama George E. Ladd, *A Theology of the New Testament*, kr. 136-139), utamaduni wa Kiyahudi uliofuatia kuhusu andiko hili unaorodheshwa.

1. Muktaba huu ni wa ki-Masihi (kama vile I Enoch 46:1; 48:10; 4 Ezra [2 Esdras] sura ya 13; b. Sanh. 98a)
2. Utabiri wote ulio katika nuktaba huu umekwisha kutimizwa (kama vile b. Sanh. 97b)
3. Muktaba huu haurejelei nyakati za mwisho (kama vile Mwa. Rab. 98:2)
4. Muktaba huu unaiwakilisha Israeli (kama vile Ibn Ezra na Rashi)

## **MADA MAALUM: MAJINA YA AGANO LA KALE KWA YULE PEKEE AJAYE**

- A. Nabii – Kumb. 18:15,18
- B. Mfalme
  1. kutoka kabila la Yuda, Mwa. 49:10; Zab. 60:7; 108:8
  2. kutoka nyumba ya Daudi, 2 Samueli 7 (kutoka kwa Yese, Isa. 11:1)
  3. kutoka maandiko mengine, 1 Sam. 2:10; Zab. 89:3-4; Isa. 9,11; Yer. 30:8-9; Eze. 37:21-22; Zek. 9:9-10
- C. Mfalme /Kuhani
  1. Zaburi 110 (mfalme, mist. 1-3; kuhani, mst. 4)
  2. Zek. 4:14 (miti miwili ya mizeituni, wawili waliotiwa mafuta, Zerubabeli [uzao wa Daudi] na Yoshua [uzao wa Aaroni])
- D. Aliyetiwa Mafuta (tazama Mada Maalum: Masihi)
  1. Mfalme wa Mungu, Zab. 2:2; 45:7
  2. Uwepo wa Roho, Isa. 11:2; 61:1
  3. Yule Ajaye, Dan. 9:26
  4. Viongozi watatu wa Agano la Kale walitiwa mafuta kama alama ya wito a Mungu na nguvu: wafalme (kama vile Amu. 9:8,15; 1 Sam. 2:10; 9:16; 24:10; 2 Sam. 19:21; 23:1; Zab. 18:50), makuhani (kama vile Kut. 28:41; Law. 4:3; 6:22), na manabii (kama vile 1 Fal. 19:16)
- E. Mwana wa Mfalme
  1. Zab. 2:7,12
  2. Mfalme wa Israeli kama alama ya utawala wa Mungu kama vile 1 Samueli 8)
- F. Mwana wa Mtu (Dan. 7:13; tazama Mada Maalum: Mwana wa Mungu)
  1. mwanadamu, Zab. 8:4; Eze. 2:1
  2. Uungu, Dan. 7:13
- G. Nyadhifa Pekee za Wokovu
  1. Mtumishi ateswaye, Isa. 52:13-53:12
  2. Mchungaji ateswaye, Zek. 12-14
  3. Jiwe la kujikwaza, Zab. 118: Isa. 8:14-15; 28:16 (tazama Mada Maalum: Jiwe la Kujikwaa)
  4. Mwana wa Pekee, Isa. 7:14; 9:6-7; Mika 5:2
  5. Chipukizi, Isa. 4:2; 11:1-5; 53:2; Yer. 23:5-6; 33:15; Zek. 3:8; 6:12 (tazama Mada Maalum: Yesu)



Mnazarethi)

Kitabu cha Agano Jipya kinayachukua marejeo mbalimbali kuhusu usuluhisho pekee wa ukombozi wa Mungu na kuyabainisha na kuyakuza katika ufahamu wa Yesu kama Mungu Ajaye Aliyehaidiwa (m.f, Mt. 16:13-20; Yohana 11:25-27). Huu ujio wa Masihi wa mara mbili ni maana ambapo tofauti hizi zinatenda kazi na nyadhifa hizi zinaunganishwa (tazama Mada Maalum: Zama hizi na Zama Zijazo).Kwa mjadala ulio mzuri wa tofauti katika Injili kati ya Mwana wa Adamu kama umbo la mamlaka dhidi ya Mtumishi ateswaye, tazama George E. Ladd, *A Theology of the New Testament*, uk. 149-158.

**8:21 "nipe ruhusa kwanza, niende nikamzike baba yangu"** Katika sura hii kifungu hiki kinaonekana kuwa kama ombi lenye maana. Hata hivyo, hii ilikuwa nahau ya kitamaduni ya kubaki nyumbani na kuwajali wa wazazi wa mtu huyo kama walivyoishi. Hili lilikuwa wajibu wa kijamii (kama vile 1 Fal. 19:20).

**8:22 "waache wafu wazike wafu wao"** Huu ulikuwa mchezo wa neno "wafu." Hiki kinaweza kutumika katika masha ya kiroho kama ilivyo katika Mt. 10:39. Kile alichokisema Yesu kilikuwa cha maisha ya kiroho na utii wa Baba wa mbinguni ni muhimu sana kuliko wajibu wa kijamii kwa maisha ya familia ya mtu wa kidumia.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 8:23-27**

<sup>23</sup> Akapanda chomboni, wanafunzi wake wakamfuata. <sup>24</sup> Kukawa msukosuko mkuu baharini, hata chombo kikafunikizwa na mawimbi; naye alikuwa amelala usingizi. <sup>25</sup> Wanafunzi wake wakamwendea, wakamwamsha, wakisema, Bwana, tuokoe, tunaangamia. <sup>26</sup> Akawaambia, Mbona mmekuwa waoga, enyi wa imani haba? Mara akaondoka, akazikemea pepo na bahari; kukawa shwari kuu. <sup>27</sup> Wale watu wakamaka wakisema, Huyu ni mtu wa namna gani hata pepo na bahari zamtii?

**NASB "Kukawa msukosuko mkuu baharini"**

**NKJV " Na ghafla tufani kubwa ikavuma baharini**

**NRSV "Dhoruba ikatokea baharini"**

**TEV "Kwa ghafla machafuko ya kimbunga yakalivamia ziwa"**

**NJB "Pasipo tahadhari tufani ikalizunguka ziwa"**

Bahari ya Galilaya imezungukwa na vilima na inaathirika kwa ukaribu wake na M. Hermon na bahari ya Mediterranean. Upepo mkubwa uliovuma uliovuma juu ya vilindi vyake vya maji mara nyingi ulitokea ghafla, pasipo kutarajia, na kwa machafuko. Hata wavuvi hawa wenye uzoefu walishikwa na woga.

Toleo la NIDOTTE, juzuu 3, uk. 557,ina naoni yenye kuvutia kuhusu neno *seismos* ("dhoruba"). "Matukio mengine kumi na moja ya neno *seismos* katika Agano la Kale yote yanarejelea tetemeko la ardhi, na mara nyingi kama mwingiliano wa Kiuungu: muda mfupi baada ya kifo cha Yesu (Mt. 27:54); katika ufufuo, ambapo kinaunganishwa na kuliviringisha jiwe; na huko Filipi, kama Paulo na Sila walivyomsifu Mungu katika gereza (Matendo 16:26). Tetemeko la ardhi ni moja ya ishara za siku za mwisho (Mt. 24:7; Marko 13:8; Luka 21:11; Ufu. 6:12; 8:5; 11:13,19; 16:18)."

Hii dhoruba ya bahati mbaya, bali Mungu aliachilia fursa kwa ajili ya

1. kumfunua Yesu
2. kujenga imani ya wanafunzi

**8:25 "Bwana, tuokoe"** Haya yalikuwa matumizi ya Agano la Kale ya neno "tuokoe" yenye kumaanisha uponyaji wa kimwili (kama vile Mt.14:30; Yohana 12:27; Matendo 23:24; 27:20,31,34,43,44; 28:1,4; Yakobo 5:15).

## MADA MAALUM : WOKOVU (NENO LA AGANO LA KALE)

Neno hili (BDB 447, KB 446, zote NOMINO JINSI YA KIKE NA KIUME), ambazo kimsingi humaanisha "pana na yenye nafasi kubwa" au "kuwa huru," lina vidokezo mbalimbali.

1. usalama, 2 Sam. 22:3; Ayubu 5:11; Zab. 12:5
2. ustawi, mafanikio, Ayubu 30:15
3. wokovu wa Kiungu wenye kujumuisha wokovu wa kimwili na kiroho
  - a. Mwa. 49:18
  - b. Kumb. 32:15
  - c. 2 Sam. 23:5
  - d. Zab. 3:2,8; 22:1; 35:3; 62:2; 69:29; 70:5; 78:22; 80:3; 89:26; 91:16; 106:4; 140:7
  - e. Isa. 12:2; 33:2; 51:6,8; 52:7,10; 56:1; 59:11; 60:18; 62:1,11
4. wazo la ukombozi wa kiroho na kimwili kwa wazi unaonekana katika Yona 2:9-10
5. ushindi, Kut. 14:30; 15:2; 1 Sam. 14:45; Zab. 20:6; 21:5; 44:4-5; 68:19-20; 118:14,15,21; Isa. 12:2; Hab. 3:8
6. mara nyingi neno "furahini" linahusiana na wokovu wa YHWH, 1 Sam. 2:1; Isa. 25:9; 26:1; Zab. 9:14; 13:5; 21:1; 35:9; 118:15,21

Wokovu unahusisha uanzishaji wa ushirika wa mwanzo wa YHWH uliokusudiwa na jamii ya wanadamu. Inajumuisha ujumla wa kibinafsi na kijamii!

**8:26-27 "kukawa shwari kuu"** Kwa hakika walikuwa wakishangazwa na uweza wa Yesu na hata yenye kuiondoa asili. Kwa sababu ya Zab. 89:8,9 hili lilikuwa dokezo la Uungu wa Yesu. Ni muumbaji pekee mwenye uwezo wa kuitawala asili (kama vile Zab. 107:23-32).

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 8:28-34

<sup>28</sup> Naye alipofika ng'ambo, katika nchi ya Wagerasi, watu wawili wenye pepo walikutana naye, wanatoka makaburini, wakali mno, hata mtu asiweze kuipitia njia ile. <sup>29</sup> Na tazama, wakapiga kelele, wakisema, Tuna nini nawe, Mwana wa Mungu? Je! Umekuja kututesa kabla ya muhula wetu? <sup>30</sup> Basi, kulikuwako mbali nao kundi la nguruwe wengi wakilisha. <sup>31</sup> Wale pepo wakamsihi, wakisema, Ukitutoa, tuache twende, tukaingie katika lile kundi la nguruwe. <sup>32</sup> Akawaambia, Nendeni. Wakatoka, wakaingia katika nguruwe; na kumbe! Kundi lote wakatelemka kwa kasi gengeni hata baharini, wakafa majini. <sup>33</sup> Lakini wachungaji walikimbia, wakaenda zao mjini, wakazieneza habari zote na habari za wale wenye pepo pia. <sup>34</sup> Na tazama, mji wote ukatoka kwenda kumlaki Yesu; nao walipomwona, walimsihi aondoke mipakani mwao.

8:28

NASB, NKJV, "katika nchi ya Wagerasi"

NRSV, JB "katika nchi ya Wagerasi"

TEV "katika eneo la Wagerasi ng'ambo ya ziwa"

Kumekuwa na mijadala mingi kuhusiana na eneo hili la kijiografia. Eneo hili lilikuwa na maana tatu tofauti katika machapisho tofauti ya Kiyahudi ya Mathayo, kama ilivyo Vidokezo vitatu tofauti vya Injili. Kwa namna iliyo dhahiri eneo hili lilikuwa karibu na mji wa Kersa, lakini mji wa Wagerasi ulichukua eneo fulani la ardhi kandokando ya ziwa na huu mara nyingi uliitwa wilaya ya Wagerasi, japo mji huu ulikuwa na umbali upatao maili sita.

☐ **"watu wawili"** Mara nyingi Mathayo alikuwa na watu wawili waliohusishwa katika maelezo ambapo Marko na Luka wana mtu moja tu (kama vile Marko 5:1; Luko 8:26). Mfano mwingine unaweza kuwa wa yule mtu kipofu/watu wa Yeriko (kama vile Mt. 20:29; Marko 10:46; Luka 18:35). Wengine wamekuwa wakidhani kwamba wale wawili walitajwa kwa sababu Agano la Kale lilihitaji ushahidi wa namna mbili katika baraza (Hes. 35:30;

Kumb. 17:6; Mt. 18:16).

☑ **"wenye pepo . . . wanatoka makaburini"** Hawa walikuwa wametengwa na jamii na hili na hii ilikuwa sehemu ambapo wangepata makazi. Katika kipindi hiki kifupi kilitengenezwa na mwanadamu au maagano ya asili yaliyotumika kama mahala pa maziko. Ikiwa eneo hili lilikuwa limeunganishwa na kupagawa na mapepo haijulikani. Kua maswali mengi mahususi kuhusu pepo na malaika ambayo hayawezi kujibiwa kwa sababu hakuna maelezo ya kibibilia yanayojitosheleza. Ulimwengu wetu umeenea nguvu binafsi ya mwovu pamoja na watenda kazi wake, malaika walioasi, walio nje ya kizuizi cha mapenzi ya Mungu na kwa ajili ya maangamizi ya mwanadamu, hatima ya uumbaji wa Mungu na tazamio la pendo na wema wake. Tazama Mada Maalum: Uovu Binafsi katika Mt. 4:5 na Pepo Wabaya katika Mt. 10:1.

☑ **"hata mtu asiweze kuipitia njia ile"** Tazama Marko 5:2-6 na Luka 8:27.

**8:29 "Mwana wa Mungu"** Pepo hawa walitambua Yesu ni nani (kama vile Yakobo 2:19). Hili jina "Mwana wa Mungu" lilitumika mara kadhaa katika Mt. 4:3; 14:33; 16:16; 27:43,54. Hili lilikuwa bezo la neno "mwana" (kama vile Mt. 2:15); Taifa la Israeli linakitwa "mwana"; Mfalme wa Israeli mwana"; na Masihi wa Israeli anaitwa "mwana." Mara kadhaa katika Injili pepo walimtambua Yesu (kama vile Marko 1:24; Luka 4:34). Yesu hakuukubali ushuhuda wao. Pepo hawa hawakulisema hili kwa ajili ya kumsaidia. Baadaye Yesu anashtakiwa kuwa alikuwa akitumia nguvu za Shetani (12:24). Ushahidi wa pepo hawa ulisababisha uzto wa shtaka hili. Tazama [MADA MAALUM : MWANA WA MUNGU](#) katika Mt. 27:54.

**NASB, NKJV**

**NRSV, JB** "Umekuja kututesa kwa wakati usio faa"

**TEV** "Umekuja kutuadhaisha kabla ya wakati wetu"

Ulimwengu wa roho unatambua kuwa muda umekwisha kuwekwa kwa ajili ya Mungu kuwahukumu walio hai ma waliokufa, wanadamu, na malaika (kama vile Flp. 2:10-11; Ufu. 11:15).

**8:30 "kundi la nguruwe wengi wakilisha"** Hili ilikuwa eneo la Mataifa lililoonyeshwa kwa kuwepo nguruwe hawa. Kwa usahihi sababu iliyowafanya pepo hawa kuingia katika nguruwe ni suala la kimadhanio. Hakuna taarifa za kujitosheleza. Maanganizi ya kundi hili la nguruwe yanaonyesha hatima ya kusudi la kifo cha kipepo kwa nguruwe wao. Pia, naangamizi ya kundi hili yangewasababisha watu wa mji kumsihi Yesu aondoke katikati yao!

☑ **"pepo"** Tazama Mada Maalum katika Mt. 10:1.

☑ **"Ukitutoa"** Hii ni sentensi amrishi daraja la kwanza. Yesu alikuwa anakwenda kuwafukuza pepo!

**8:34 "walimsihi aondoke mipakani mwao"** Huu ulikuwa moja ya mistari ya huzuni sana katika Biblia nzima. Katika uwepo wa historia ya mtu mkubwa, hawa wanakijiji waliguswa na kifo cha nguruwe wachache kuliko kuguswa na ukombozi na matengenezo ya watu wawili waliokuwa na uwezo wa kiroho wa injilio katika eneo lao.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeleze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Vidokezo vya Injili vinatofautiana katika uandishi wao wa maneno na matendo ya Yesu?
2. Kwa nini tendo la kumponya nwemye ukoma lilikuwa tukio la kama vile Mt. 11:5)?
3. Kwa nini Yesu aliwataka wale walioponywa kwenda kwa kujionyesha kwa makuhani?
4. Kwa nini haikuwa kawaida kwa Yesu kutembea na akida wa Kirumi?
5. Nini umuhimu wa mistari ya 11 na 12?
6. Nani au nini maana ya pepo? Nini kusudi lao katika ulimwengu?
7. Je! mstari wa 17 unafundisha kwamba uponyaji wa kimwili ni sehemu ya kama vile Eze. 2:1; Dan. 7:13)?

## MATHAYO 9

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>USB<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Uonyaji wa Mtu Aliyepooza	Yesu anasamehe na Kumponya aliyepooza	Matukio katika Galilaya (anaendelea)  (8:1-9:38)	Yesu Anamponya Mtu nwenye kupooza	Tiba ya mwenye kupooza
9:1-8	9:1-8	9:1  9:2-8	9:1-2  9:3  9:4-6  9:7-8	9:1-8
Kuitwa kwa Mathayo	Mathayo Mtoza ushuru		Yesu Anamwita Mathayo	Kuitwa kwa Mathayo
9:9-13	9:9-13	9:9  9:10-13	9:9a-b  9:9c  9:10-11  9:12-13	9:9  Kula pamoja na wenye dhambi  9:10-13
Swali kuhusu Kufunga	Yesu Anaulizwa Kuhusu Kufunga		Swali Kuhusu Kufunga	Mjadala wa Kufunga
9:14-17	9:14-17	9:14-17	9:14  9:15  9:16-17	9:14-17
Binti wa Mjumbe na Mwanamke Aliyeligusa Pindo la Yesu	Binti Arejeshewa Uhai na Mwanamke Anaponywa		Binti wa jumbe na Mwanamke Aliyegusa Pindo la Yesu	Tiba ya Mwanamke Aliyetoka damu; Binti wa Mjumbe Anafufuliwa
9:18-26	9:18-26	9:18-26	9:18	9:18-19

			9:19	
			9:20-21	9:20-22
			9:22	
			9:23-24a	9:23-26
			9:24b-26	
Uponyaji wa Vipofu Wawili	Vipofu Wawili Waapoywa		Yesu Anawaponya Vipofu Wawili	Tiba ya Vipofu Wawili
9:27-31	9:27-31	9:27-31	9:27	9:27-31
			9:28a-b	
			9:28c	
			9:29-30	
			9:31	
Uponyaji wa Mtu Bubu	Mtu mwenye Pepo Bubu Azungumza		Yesu Anamponya Bubu	Tiba ya mtu Mwnye Pepo Bubu
9:32-34	9:32-34	9:32-34	9:32-33	9:32-34
Huruma ya Yesu			9:34	Mjadala wa Umati
9:35-38	9:35-38	9:35-38	9:35-38	9:35
				9:36-37

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka [“Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia”](#))** **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## HISTORIA YA NYUMA KUHUSU MATHAYO 9:1-38

- A. Mara nyingi Mathayo anayafupisha matukio haya ambayo yameandikwa sana katika maelezo ya undani yaliyo kamili katika vitabu vyote vya Marko na Luka. Haipaswi wafasiri kuzilingalisha Injili nyingine zenye kuhitaji maelezo ya undani yaliyo kamili hadi yatakapobainishwa ni kwa namna gani/kwa nini mwandishi binafsi wa Injili alifanya namna hii. Hatuitafuti historia kamili, bali kwa kusudi la kithiologia la mwandishi aliyevuviwa (kama vile Gordon Fee na Douglas Stuart's *Howto Study the Bible for All Its Worth*, kr. 120-129).
- B. Sura hii inagawanyika katika vipengele kadha tofautitofauti:
1. Mistari ya 1-8, kama vile Marko 2:3-12 na Luka 5:17-26
  2. Mistari ya 9-17, kama vile Marko 2:14-22 na Luka 5:27-38
  3. Mistari ya 18-26, kama vile Marko 5:22-43 na Luka 8:41-56
  4. Mistari ya 27-31, ambayo ni ya kipekee kwa Mathayo
  5. Mistari ya 32-34, ambayo pia ni ya kipekee kwa Mathayo
  6. Mistari ya 35-38, inaweza kuamini kwamba huu ni utangulizi wa agizo la wale Kumi na Wawili ambayo lazima yaendane na Mathayo 10
- C. Mathayo 8 ilionyesha uweza wake juu ya magonjwa, asili, na pepo. Mathayo anakitunia kipengele hiki kuonyesha uweza na mamlaka ya Yesu juu ya nafasi za aina tofautitofauti.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 9:1

<sup>1</sup>Akapanda chomboni, akavuka, akafika mjini kwao.

**9:1** Kimuktadha mstari huu ni lazima uendane na Mathayo 8, kama ilivyo katika mstari wenye mabadiliko wenye kuelekea katika tukio linalofuata. Kwa kuwa nji wa Kapernaum ulikuwa makazi makuu ya huduma ya Yesu (kama vile Marko 2:1; Mt. 4:13) baada ya tendo la kutokuamini na ukanaji lililofanyika humo Nazareti mahali alipokulia.

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 9:2-8

<sup>2</sup>Na tazama, wakamletea mtu mwenye kupooza, amelala kitandani; naye Yesu, alipoiona imani yao, alimwambia yule mwenye kupooza, Jipe moyo mkuu, mwanangu, umesamehewa dhambi zako. <sup>3</sup>Na tazama, baadhi ya waandishi wakasema nafsini mwao, Huyu anakufuru. <sup>4</sup>Naye Yesu, hali akijua mawazo yao, akasema, Mbona mnawaza maovu mioyoni mwenu? <sup>5</sup>Kwa maana rahisi ni lipi, ni kusema, Umesamehewa dhambi zako, au ni kusema, Ondoka, uende? <sup>6</sup>Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi, (amwambia yule mwenye kupooza) Ondoka, ujitwike kitanda chako, uende nyumbani kwako. <sup>7</sup>Akaondoka, akaenda zake nyumbani kwake. <sup>8</sup>Makutano walipomwona, walishikwa na hofu, wakamtukuza Mungu, aliyewapa watu amri ya namna hii.

**9:2 "wakamletea mtu mwenye kupooza"** Maelezo ya undani yanayohusu tukio hili yanapatikana katika Marko 2:1-22. Haya ni sawa na yale maelezo ambayo yanaeleza namna wale marafiki wa yule mtu mwenye kupooza walivyoezua paa na kumshusha yule mtu mwenye kupooza miguuni pa Yesu.

☐ **"alipoiona imani yao"** Katika muktadha huu kifungu "imani yao" hakimrejelei mtu aliyehitaji uponyaji, bali kimsingi kiliwarejelea marafiki zake waliokuwa na werevu na ustahimilivu.

☐ **"alimwambia yule mwenye kupooza, Jipe moyo mkuu, mwanangu, umesamehewa"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo (kama vile Mt. 9:22) na kauli tendwaji elekezi ya wakati uliopo. Mara nyingi Wayahudi

walihusianisha dhambi na nagonjwa (kama vile Yohana 5:14; 9:2; na Yakobo 5:15-16). Ingawa Yesu alitanbua dhahiri uhusiano huu, Pia alionekana kuupinga uhusiano huu (kana vile Yohana. 9:3 na Luka 13:2-3). Huu ni usemi wenye nguvu wa uelewa wa Yesu. Ni Mungu pekee mwenye kusamehe dhambi (yaani., kauli tendwa)!

Yesu anamwelezea mtu huyu kama "mwana" (*teknon*). Hata hivyo, hiki hakikuwa kielelezo cha umri wake, bali ni neno la wema (kama vile Marko 10:24; pia labda Luka 16:25 na Mwa. 43:29 katika LXX).

**9:3 "waandishi"** Tangu kutekwa kwa Babeli, Hekalu kwa namna fulani lilitakwa na Sinagogi kama eneo takatifu katika jamii ya Kiyahudi. Hawa ni wataalamu wa sheria za Kiyahudi, wenye kuufuata utamaduni za Ezra, walikuja kujulikana kama waandishi (tazama Mada Maalum katika Mt. 12:38, Ezra 7:8,10). Hawa walitoka katika historia mbalimbali za kithiolojia, lakini hasa hawa walikuwa Mafarisayo. Haijalishi kuwa walikuwepo kwa sababu ya shauku halisi au walikuwa wakimchunguza Yesu haijulikani. Kwa namna fulani walikuwa na mshangao juu ya yeye kudai kuwa na uweza wa kusamehe dhambi. Waliamini kwamba ni Mungu pekee mwenye uweza wa kusamehe dhambi hii. Katika muktadha huu walimshtumu Yesu kama mwenye kukufuru (kama vile Marko 2:7); katika hali halisi, hawa ndiyo waliokufuru ikiwa Yesu hakuuutwa Mwili huku akiwa Mwana wa Mungu!

**9:4 "hali akijua mawazo yao,"** Kwa vyo vyote vile huu ni mfano wa maarifa ya asili ya Yesu ambayo yalionekana kudokezwa kutokana na muktadha, au kwa vyo vyote mtu aliyekuwa miongoni mwa makutano alipita wakati walipokuwa wakinung'unika haujulikani. Kuna vifungu katika Agano Jipya vyenye kumaanisha kwamba Yesu aliifahamu vema asili ya mwanadamu na vifungu vingine vyenye kumaanisha kwamba aliitumia asili ya nguvu zake.

Kuna tofauti za kimachapisho kati ya

1. kuona (*idōn*) -  $\alpha$ , C, D, L, W, na Kilatini cha kale, Vulgate, na tafsiri za Koptiki
2. kujua (*eidōs*) - B, E<sup>c</sup>, na tafsiri za Shamu na Kiarmeni

Toleo la UBS<sup>4</sup> linaiweka #1 kama daraja "B" (kwa namna fulani kuna ukweli). Uchaguzi wa pili huenda unatokana na Mt. 12:25; Luka 6:8;9:47. Toleo la NASB, NKJV, na NJB linaufuatisha uchaguzi #2.

**9:5 "Kwa maana rahisi ni lipi, ni kusema, Umesamehewa dhambi zako, au ni kusema, Ondoka, uende"** Kuseema, "Umesamehewa dhambi zako" ni vigumu sana, lakini ni dhahiri kama uponyaji wa kimwili. Yote haya hayawezekani kwa wenye dhambi wanaokufa!

**9:6 "Lakini mpate kujua"** Katika Injili zote hakujishughulisha na wahitaji pekee, bali pia na viongozi wa Kiyahudi (kama vile Yohana. 11:42,45). Yesu alikabilia nao kwa kusudi la kuwarejesha katika imani katika yeye. Uponyaji ulikuwa wa muhimu sana hasa kwa waandishi kama ilivyokuwa kwa Yule mtu mwenye kupooza na marafiki zake. Kama ada, hii ni huduma ya Yesu ya uponyaji iliyo ya kweli. Mara nyingi haya matendo yenye nguvu yalikuwa ni kwa ajili ya kuihimarisha imani ya wanfunzi au kuisimika imani kwa watazamaji.

☐ **"Mwana wa Adamu"** Hiki ni kifungu cha kikundi vumishi chenye kutoka Agano la Kale. Hiki kinatumika katika Eze. 2:1 na Zab. 8:4 katika asili yake ya maana ya kifungu "mwana damu." Hata hivyo, hiki kinatumika katika Dan. 7:13 katika muktadha pekee ambao ulimaanisha vyote ubinadamu na Uungu wa mtu aliyeelezewa na jina hili. Kwa kuwa jina hili halikutumiwa na wamlimu wa sheria za dini ya Kiyahudi, hivyo, halikuwa maana ya na kiuzalendo, kiutengefu, kijeshi, Yesu alilichagua hili kama jina kamili la kuifunika na kuifunua asili yake (kama vile 1 Yohana 4:1-6). Huu ulikuwa upendeleo wa kujiimarisha mwenyewe.

☐ **"anayo amri duniani ya kusamehe dhambi"** Hili neno " amri" (*exousia*) lilikuwa neno lenye kumaanisha "haki," "uweza" au "mamlaka." Kwa mkazo wake lilimaanisha Umasihi wa Yesu, kama si Uungu wake. Wayahudi



hawakutegemea kuwa Masihi angekuwa wa ki-Uungu, bali kiongozi mwenye nguvu za asili kijeshi/kisiasa, kama Waamuzi wa Agano la Kale. Ni kupitia ufuo endelevu wa Agano Jipya pekee ambapo waamini wanaitambua asili ya Masihi kuutwaa mwili (yaani., Yohana 1:1; 5:18; 8:58; 10:30,34-38; 14:9-10; 20:28; Rum. 9:5; Flp. 2:6-7; Ebr. 1:8; 2 Pet.1:1).

☑ **"amwambia yule mwenye kupooza, 'Ondoka, ujitwike kitanda chako, uende nyumbani kwako'"** Katika kifungu hiki kuna vitenzi vitatu.

1. "Ondoka" hii ni kauli tendwaji endelevu ya wakati uliopita usio timilifu yenye kutumika kama shurutishi
2. "ujitwike kitanda chako" hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu
3. "uende nyumbani kwako" hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo.

Vidokezo vya nyakati hizi vin gelikuwa kwamba Mungu ndiyee mtawala wa kauli tendwaji, "ondoka." Hizi kauli mbili shurutishi zingeyazungumzia matendo ya mwanadauamu muda mfupi baada ya uponyaji wake. Kujitwika kitanda chake ilikuwa ishara kwamba siku zake za kuombaomba zilikuwa zimeisha na alikuwa akirudi nyumbani. Uponyaji huu ulilithibitisha dai la Yesu la Uungu na Umasihi!

**9:8 "Makutano walipomwona, walishikwa na hofu"** Kuna tatizo la machapisho ya Kiyunani hapa lenye kuhusiana na neno "hofu. Maandiko ya Kiyunani ya kale na yaliyo bora yana kifungu "waliogopa" (MSS,  $\alpha$ , B, D,W). Baadaye maandiko yalililainisha neno "walipatwana mshangao" au NKJV "walistaajabu" (MSS C, L). Maandiko mengine ya Kiyunani yalikiacha kifungu (MS X). Toleo la UBS<sup>4</sup> linaupa uchaguzi #1 daraja "A" (ni wa uhakika).

Makutano hawakuwa na mazoea ya kuwa na mtu mwenye kuzungumza kwa mamlaka ya namna hii. Dini ya kaihahudi ilinaswa kwa desturi na kunukuu semi za kale za walimu wa Kiyahudi. Yesu alizungumza kwa ukweli na mamlaka, ambapo kizazi hiki cha watu wa Kiyahudi hakikiwahi kusikia hivyo. Walimsifu Mungu kwa kuwapa mtu wa aina hii mwenye uweza kwa mtu mwingine. Hili linaweza kuwa dokezo lililofunuliwa juu ya Uungu wa Yesu ambao uliibua maswali kwa kanisa la kale lililikuwa la uasi lililoitwa "Ujuzi wa uongo." Pia lilijitokeza katika maandiko yaliyofuatia ya Agano Jipya kwamba viongozi wa kidini waliona wivu kwa ajili ya wingi wa watu aliokuwa nao Yesu.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 9:9**

<sup>9</sup>Naye Yesu alipokuwa akipita kutoka huko aliona mtu ameketi forodhani, aitwaye Mathayo, akamwambia, Nifuate. Akaondoka, akamfuata.

**9:9 "Naye Yesu alipokuwa akipita kutoka huko"** Mistari ya 9-17 inaelezwa katika maelezo ya undani zaidi katika ufanano wa vidokezo vingine vya Injili, Marko 2 na Luka 5.

☑ **"aliona mtu ameketi forodhani, aitwaye Mathayo"** Kutokana na Marko 2:14 na Luka 5:27 tunajifunza kwamba jina lake linguine lilikuwa Lawi. Hii haimaanishi kuwa alikuwa kuhani au Mlawi. Mara nyingi Wayahudi walikuwa na majina mawili, moja la Kiyahudi na linguine la Kiyunani, mara nyingi waliwapa majina haya wakati wa kuzaliwa. Huyu ni mwanafunzi ambaye mamlaka ya injili hii ni yake. Yesu anaweza kuwa alimchagua kwa sababu ya karama yake ya umakini katika kutunza kumbukumbu au kama njia ya kuonyesha pendo lake kwa watu wote, hata watoza ushuru!

☑ **"ameketi forodhani"** Mji wa Kapernaumu alikuwa kandokando ya Bahari ya Galilaya kati ya utawala wa ngome ya Filipi na ngome ya Herode. Hivyo, ushuru ungekuwa kati ya Shamu na Uyunani. Kazi ya mtoza ushuru aliyoagizwa na mamlaka za Herodia au za Kirumi. Mara nyingi hili lilifanywa kwa mapendekezo kuwa mapato yote ya ziada yaliyokuwa yakikusanywa yangekuwa ujira wa Yule mwenye kazi hiyo. Hili lilijulikana sana na lilitendwa

nyakati za Yesu na, hivyo kazi hii kujulikana kama ya uovu na ya unyonyaji. Watoza ushuru hawakuruhusiwa kuingia katika sinagogi au katika jamii ya Kiyahudi.

☐ **"Nifuate. Akaondoka, akamfuata" Huenda hii haikuwa mara ya kwanza kwa Mathayo kusikia habari zenye kumhusu Yesu. Kwa namna iliyo dhahiri alikuwa amefunuliwa juu ya mafundisho ya Yesu kuhusu matukio mbalimbali na hili lililikuwa hitimisho la wito maalum (kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo) wa mwalimu kwa mfuasi na kuwa mwanafunzi kwa wakati wote (kama vile Mt. 4:19,21).**

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 9:10-13**

**<sup>10</sup>Ikawa alipoketi nyumbani ale chakula, tazama, watoza ushuru wengi na wenye dhambi walikuja wakaketi pamoja na Yesu na wanafunzi wake. <sup>11</sup>Mafarisayo walipoona, waliwaambia wanafunzi wake, Mbona mwalimu wenu anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi? <sup>12</sup>Naye aliposikia, aliwaambia, Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi. <sup>13</sup>Lakini nendeni, mkajifunze maana yake maneno haya, Nataka rehema, wala si sadaka; kwa maana sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi.**

**9:10** Kifungu hiki linairejelea nyumba ya Mathayo, si ya Yesu. Kwa namna iliyo wazi utoaji wa chakula baada ya kufanya maamuzi ya kumaanisha katika maisha lilikuwa tendo la kawaida kwa sababu Zakayo, mtoza ushuru mwingine, alifanya jambo lile lile (kama vile Luka 19). Kifungu wenye dhambi wengi" kimsingi kinaweza kurejelea wale waliokataliwa na jamii ya Kiyahudi ambao hawezi kufanya kazi ya umakini wa kutunza kumbukumbu ya Sheria ya Musa kama ilivyoelezwa zaidi katika desturi za mapokeo ya walimu wa sheria za dini ya Kiyahudi. Suala kwamba baadhi yao walikuwa watu wenye kukiuka maadili linawezekana, lakini kwa mara nyingine, inaweza kuwa kwamba umiliki wao wa biashara haukukubalika kwa viongozi wa Kidini (yaani., wachungaji, wawekaji alama wa mifugo, n.k).

Hiki kifungu "wakaketi" kilimaanisha "wakajinyoosha." Katika kipindi cha kihistoria watu hawa watu hawa waliviegamisha viwako vya mikono ya kushoto wakati wa kula. Ni Misri tu ambamo watu walikuwa wakikaa mezani wakati wa kula.

**9:11 "Mafarisayo walipoona, waliwaambia wanafunzi wake"** Mafarisayo hawa walikuwepo wakati wa kula chakula cha jioni, lakini hawakuwa washiriki wa chakula hiki. Inaonekana kutokuwa kawaida lakini katika ulimwengu wa kale mtu ye yote angekuja na kusimama karibu na kuta au kuchungulia madirishani huku akishiriki katika mazungumzo pasipo kuwa mgeni maalum wa chakula hicho. Kwa namna iliyo wazi kabisa jina "Mafarisayo" lilikuwa jina lingine la "waandishi" waliotajwa mwanzoni katika muktadha huu. Hili lilikuwa kundi la Wawayahudi waliojitoa ambao walizifuata desturi fulani ambazo zilikuwa zinaendena na mapokeo ya desturi za Kiyahudi (Buku la Sheria za Kiyahudi). Tambua kwamba hawa waliwashambulia wanafunzi na si Yesu mwenyewe. Yesu, kwa kula na hawa watenda dhambi maarufu, alikuwa akieleza ushirika na urafiki. Yohana Mbatizaji alikuwa ametangulia mapema kama mtu mwenye kujinyima na viongozi wa Kiyahudi walimpinga na sasa wanampinga Yesu aliyekuja kama zaidi ya mtu wa kijamii (kama vile Mt. 11:19; Luka 7:34). Hawa pia walimshtaki Yesu kuwa "mpenda mvinyo" ambapo inamaanisha "mlafi" au "mtu mwenye kulewa sana." Mara kwa mara ushikiliaji wa mambo ya kale ya kidini haukuwa na mvuto na mambo hayo alikuwa ya kiubinafsi. Kwa mjadala kamili uhusio chimbuko na theolojia ya Mafarisayo, tazama katika Mt. 22:15.

**9:12 "Naye aliposikia, aliwaambia"** Katika tukio hili kwa uwazi kabisa Yesu hakuwa amezisoma fikra za Mafarisayo (kama vile mst.wa 4). Kwa vyo vyote yote walivyokuwa wakizungumza yalikuwa yakimfikia au aliyasikia yeye mwenyewe.

☐ **"Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi"** Kifungu hiki hakimaanishi kuwa Mafarisayo hawakuwa na dhambi; huu ulikuwa mwitikio wa kejeli.

**9:13 "Lakini nendeni, mkajifunze maana yake maneno haya"** Hii ni nukuu toka Hosea 6:6 (kama ilivyo Mt. 12:7). Mstari huu unaanza na kifungu cha kauli shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu ambayo ni nahau ambayo walimu wa sheria za Kiyunani waliitumia kuwaambia wanafunzi wao kujifunza jambo fulani. Mstari wa 13 ni wa kipekee katika Injili ya Mathayo.

☐ **"kwa maana sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi"** Luka 5:32, ambayo ni ufanano wa Kidokezo cha maelezo yake, inaongeza kifungu "wapate kutubu." Maelezo ya Mathayo, ingawa hayakinukuu kifungu hiki kwa upekee, yalimaanisha hili. Mwitikio wa aina mbili wenye umuhimu kwa watu kuwa sawa na Mungu ulikuwa ni toba na imani (kama vile Marko 1:15; Matendo 3:16, 19; 20:21). Hata Yesu anaeleza kwamba mpaka watu watubu la sivyo watapotea (kama vile Luka 13:5). Kimsingi toba ni tendo la kujirudi toka, dhambini, na uasi na kuyarudia matakwa na njia ya Mungu kwa maisha ya mtu huyo. Tendo hili si la kihisia kama yalivyo mabadiliko katika kipaumbela na maisha. Hii ni hiari ya kufanya mabadiliko. Tazama mada Maalum katika Mt. 3:2.

Hiki kitenzi "kuwaita" (*kaleō*) kinaweza kueleweka kama "kalika" (kama vile Mt. 22:2-10 na Luka 14:16-25; Yohana 2:2; Ufunuo. 19:9). Katika maana ya kithiolojia jambo hili linakazia dhana ya agano.

1. Mungu anaalika (wito wa ki-ungu)
2. yawapasa wanadamu kkuhitikia (kwa imani ya awali na endelevu, toba, utii, na ustahimilivu)

Tazama [MADA MAALUM: UCHAGUZI /KUAMRIWA KABLA NA HITAJI LA USAWA WA KITHIOLOJIA](#) katika Mt. 24:22.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 9:14-17**

<sup>14</sup> Wakati ule wanafunzi wake Yohana wakamwendea, wakasema, Kwa nini sisi na Mafarisayo twafunga, bali wanafunzi wako hawafungi? <sup>15</sup> Yesu akawaambia, Walioalikwa arusini wawezaje kuomboleza, muda bwana arusi akiwapo pamoja nao? Lakini siku zitakuja watakapoondolewa bwana arusi; ndipo watakapofunga. <sup>16</sup> Hakuna mtu atiyaye kiraka cha nguo mpya katika vazi kuukuu; maana kile kilichotiwa huondoa kipande cha lile vazi, na pale palipotatuka huzidi. <sup>17</sup> Wala watu hawatii divai mpya katika viriba vikuukuu; na kama wakitia, vile viriba hupasuka, divai ikamwagika, na viriba vikaharibika; bali hutia divai mpya katika viriba vipya, vikahifadhika vyote.

**9:14 "Wakati ule wanafunzi wake Yohana wakamwendea"** Haijulikani kama walikuwa (1) wamemaanisha kiukweli, (2) walikuwa wamechanganya kiukweli, au (3) walikuwa wakijaribu kumtega. Wao, kama Mafarisayo, walikuwa wageni wasio waalikwa, lakini kwa namna iliyo dhahiri walikuwepo katika sikukuu. Kulikuwa na wanafunzi wengi wa Yohana Mbatizaji, kama inavyoweza kuonekana katika Matendo 9:1 na kuendelea.

☐ **"Kwa nini sisi na Mafarisayo twafunga, bali wanafunzi wako hawafungi"** Katika Agano la Kale kulikuwa na siku moja maalum ya kufunga iliyoitwa *Yom Kippur* (Siku ya Upatanisho, kama vile Mambo ya Walawi 16) iliyofanyika kila mwaka. Hata hivyo, walimu wa sheria za Kiyahudi waliweka siku ya pili nay a tatu ya juma kuwa sikukuu pia (kama vile Luka 18:12), kwa ushahidi uliojikita kwao kuhusiana na siku ambayo Musa alikwenda juu ya Ml. Sinai na katika siku ambayo alishuka toka mlimani. Tendo la kufunga ilikuwa njia ya kuhakikisha mtu kujitoa kidini. Yesu hakulipinga tendo hili, bali kwa vyo vyote alikubali kama ilivyotakiwa. Tazama [MADA MAALUM: KUFUNGA](#) katika Mt. 6:16.

Kuna tatizo la machapisho ya Kiyunnani katika mstari huu wenye kuhusiana na neno "mara nyingi" linalopatikana katika matoleo ya NKJV na NRSV, yenye ufanano ulio dhahiri ulio katika Luka 5:33. Marko inafanana na 2:18 yenye neno "kufunga." Kamati ya toleo la UBS<sup>4</sup> inaliweka neno lingine "sana" katika mabano kwa sababu maneno haya

hayajulikani kama ndiyo halisi katika Mathayo au yaliongezwa baadaye na wanuukuu toka Luka.

**9:15** Sarufi ya swali hili inatarajia jibu la " hapana".

☑ **"Lakini siku zitakuja watakapoondolewa bwana arusi; ndipo watakapofunga"** Yesu alidhani kwamba wanafunzi wake wangepunga nbaada ya yeye kusulibiwa. Huu ni wakati wa kwanza kudokezwa kwa tendo la kusulibiwa. Vitenzi viwili *apairo* ("watakapoondolewa"), vilivyotumika katika kifungu hiki, vina maana ya machafuko (kama vile Marko 2:20; Luka 5:35). Ufanano wa Yesu wa kifungu "bwana arusi," una maana nyingine za ki-Masihi. Tazama Mada Maalum: Kufunga katika Mt. 6:16.

**9:16-17** Kumekuwa na mjadala mwingi kuhusu namna ya kuitumia kweli hii. Hii inaonekana kuweka mkazo wa hitaji kuwa na mabadiliko katika maisha ya imani ya mtu. Hata hivyo, yapasa mtu kuwa makini kama ilivyo asili na namna ya mabadiliko haya. Jambo hili liko katika ukweli wa shutma za fasiri za kiuandishi za walimu wa sheria za Kiyahudi za Mapokeo ya Desturi. Ujumbe wa Yesu mar azote ulikuwa mpya na wenye utofauti na nadhehebu ya Kiyahudi ya nyakati zake! Mungu atusaidie, wakati mwingine tunafungwa sana na desturi zetu na sheria kuliko inavyopaswa kutenda, utii, uhusiano na Mungu wa kila siku (kama vile Isa. 6:9-10; 29:13). Fumbo hili linafananishwa katika Marko 2:19-20 na Luka 5:33-39. Jambo jipya limekuja (yaani., injili) na limebadilisha kila kitu!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 9:18-19**

<sup>18</sup>Alipokuwa akiwaambia hayo, tazama, akaja jumbe mmoja, akamsujudia, akisema, Binti yangu sasa hivi amekufa; lakini njoo, uweke mkono wako juu yake, naye ataishi. <sup>19</sup>Akaondoka Yesu, akamfuata, pamoja na wanafunzi wake. <sup>20</sup>Na tazama, mwanamke aliyekuwa na ugonjwa wa kutoka damu muda wa miaka kumi na miwili, alikuja kwa nyuma, akaugusa upindo wa vazi lake.

**9:18 "akaja jumbe mmoja, akamsujudia"** Maelezo yaenye undani zaidi yanapatikana katika Marko 5:22-43 na Luka 8:41-56. Kifasihi mtu huyu alikuwa "mkuu wa sinagogi" (kama vile Marko 5:22; Yohana 3:1). Mtu huyu alikuwa mwangalizi wa sinagogi pamoja na shughuli nyinginezo zilizohusu sinagogi. Huyu alitenda kwa namna isiyo halali kwa kuipotosha misingi ya kibiblia, mwalimu wa sheria asiye fuata sheria hizo kama alivyofanya Yesu na kwa kuanguka miguuni pa Yesu. Hata hivyo, katika hali isiyo ya kawaida alikuwa na hisia kubwa juu ya binti yake, ambaye alimpenda Mtu akilinganishapo kifungu hiki pamoja na Marko 5:21 na Luka 8:42, kuna baadhi ya mkanganyiko kama binti alikuwa katika hali ya kufa au tayari alikuwa amekwisha kufa.

**9:19 "Akaondoka Yesu, akamfuata"** Kwa uwazi kabisa imani ya mu huyu ilikuwa imehusishwa na (1) uwepo wa Yesu unaoonekana, (2) tendo la kuweka mikono, na (3) maombi. Katika Mt. 11:5 kumfufua mtu aliyekufa ilikuwa moja ya ishara zilizotajwa kwa Yohana Mbatizaji ili kuithibitisha huduma ya ki- Masihi ya Yesu. Iwe tendo hili la uamsho ni la kweli au tendo la uonyaji kutokana na hari ya kuzimia haijulikani kutokana na muktadha.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 9: 20-22**

<sup>20</sup>Na tazama, mwanamke aliyekuwa na ugonjwa wa kutoka damu muda wa miaka kumi na miwili, alikuja kwa nyuma, akaugusa upindo wa vazi lake. <sup>21</sup>Kwa maana alisema moyoni mwake, Nikigusa tu upindo wa vazi lake nitapona. <sup>22</sup>Yesu akageuka, akamwona, akamwambia, Jipe moyo mkuu, binti yangu; imani yako imekuponya. Yule mwanamke akapona tangu saa ile.

**9:20 "mwanamke aliyekuwa na ugonjwa wa kutoka damu muda wa miaka kumi na miwili"** Tunajifunza mamobo mengi zaidi kuhusu naelezo haya kutoka Marko 5:26 na Luka 8:43. Kwa uwazi kabisa huyu alikuwa ametumia

fedha nyingi kwa matabibu na hakupata msaada. Tunafahamu baadhi ya tiba za kienyeji katika sheria za Dini ya Kiyahudi kutoka katika Buku la sheria za Kiyahudi, hasa Shabb, 110 A na B. Moja ya tiba ilikuwa ni kubeba mayai ya mbuni au nafaka aina ya shayiri yenye kutokana na kinyesi cha punda mweupe katika shingo ya mtu. Mtu anaweza kuona mshangao juu za aina ya tiba hizi zenye kuchekesha mwanamke huyu alikuwa amezijaribu tiba hizi kwa miaka kumi na miwili. Aina ya ugonjwa huu ulinifanya kuwa najisi kimila na kuruhusiwa kuhudhuria katika huduma za ibada za Kiyahudi (kama vile Law. 15:25). Pia alikuwa akitengwa waziwazi mara zote.

**9:21 "Nikigusa tu upindo wa vazi lake nitapona"** Kulikuwa na dalili za ushirikina katika inami ya mtu huyu nab bado Yesu aliiheshimu hata imani hii dhaifu (sentensi amrishi daraja la tatu). Kwa kujikita katika Law. 15:19 na kuendelea. Kwake ilikuwa mwiko kumgusa mwalimu kwa sababu hali hii ingenfanya Yesu kuwa najisi. Yesu alikuwa akiwajali watu kuliko sheria za kimila!

Vazi lililorefejelewa huenda ni (1) Joho la Yesu alililokuwa akilivaa juu (kama vile Yohana 19:2) au (2) Skafu ya Yesu ya maobi (*talith*), ambayo aliitumia wakati wa kuomba (kama vile Hes. 15:38-40; Kumb. 22:12; Mt. 23:5) na kwa wakati mwingine kuivaa mabegani.

**9:22 "imani yako imekuponya"** Kifasihi hili ni neno "okolewa." Hili lilitumika katika maana yake ya Agano la Kale umaanisha "ukombozi wa kimwili" (kama vile Yakobo 5:15). Hii imani ya mwanamke huyu, iliyokuwa dhaifu kwa sababu ya kujihusisha na ushirikina, bado Yesu aliiheshimu. Katika Agano Jipya ni suala la imani ya mtu ambalo ndilo la msingi.

**ANDIKO LA NASB ( LILILOBORESHWA) MATHAYO 9:23-26**

<sup>23</sup>Yesu alipofika nyumbani kwa yule jumbe, aliona wapiga filimbi, na makutano wakifanya maombolezo, <sup>24</sup>akawaambia, Ondokeni; kwa maana kijana hakufa, amelala tu. Wakamcheka sana. <sup>25</sup>Lakini makutano walipoondoshwa, aliingia, akamshika mkono; yule kijana akasimama. <sup>26</sup>Zikaenea habari hizi katika nchi ile yote.

**9:23 "Yesu alipofika nyumbani kwa yule jumbe, aliona wapiga filimbi, na makutano wakifanya maombolezo."** Katika sheria za dini ya Kiyahudi tendo hili lilikuwa la kawaida (kama vile Yer. 9:17; 48:36) kwamba mtu alipokuwa akifa, hata katika familia maskini sana, angalau wapiga filimbi wawili na mwanamke mmoja mwenye kuomboleza lazima angekodishwa ili kufanikisha msiba. Misiba ilikuwa hali za ndani na kihisia.

**9:24 "Ondokeni; kwa maana kijana hakufa, amelala tu"** Hili neno "amelala" halikutumika katika hali ya kifo mara kwa mara, bali katika muktadha huu ilitumika kutofautisha hali hii na kifo. Iwe ilikuwa hali ya kuzimia sana au kifo, hakika muujiza wa uponyajia ultokea.

**9:25 Lakini makutano walipoondoshwa"** Luka 8:51 inaeleza kwamba wazazi na mkusanyiko wa wanafunzi wake wa karibu, Petro, Yakobo, na Yohana, waliruhusiwa kubaki.

■ **"akamshika mkono"** Kutokana na Marko 5:41 mambo mengi zaidi yameandikwa hasa yale Yesu aliyomwambia kijana huyu. Tendo la kuugusa mwili wa aliyekufa lingemfanya kuwa najisi kwa mujibu wa mila hizo. Bali, mtu anapokuwa na uweza juu ya maisha dhidi ya kifo, hakuna kitu kilicho kama mwili uliokufa!

**9:26 "Zikaenea habari hizi katika nchi ile yote"** Sababu iliyomfanya Yesu kukiacha chumba wazi ilikuwa kwamba pasingekuwepo mtu wa kueneza habari hizi kuhusu uponyaji wa kimuujiza (kama vile Mt. 8:4; 9:30; 12:16; 16:20;

17:9; Marko1:44; 3:12; 5:43; 7:36; 8:30; 9:9; Luka 4:41; 5:14; 8:56; 9:21). Hata hivyo, kadri msiba ulivyokuwa unaendelea, urejesho wa kijana huyu mdogo ulivyozi kutangazwa.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 9: 27-31**

<sup>27</sup>Yesu alipokuwa akipita kutoka huko, vipofu wawili wakamfuata wakipaza sauti, wakisema, Uturehemu, Mwana wa Daudi. <sup>28</sup>Naye alipofika nyumbani, wale vipofu walimwendea; Yesu akawaambia, Mnaamini kwamba naweza kufanya hili? Wakamwambia, Naam, Bwana. <sup>29</sup>Ndipo alipowagusa macho, akasema, Kwa kadiri ya imani yenu mpate. <sup>30</sup>Macho yao yakafumbuka. Naye Yesu akawaagiza kwa nguvu, akisema, Angalieni hata mtu mmoja asijue. <sup>31</sup>Lakini wakatoka, wakaeneza habari zake katika nchi ile yote.

**9:27 "vipofu wawili wakamfuata wakipaza sauti"** Hii ilikuwa sifa bainishi ya naelezo ya Vidokezo vya Injili ambapo Mathayo mara kwa mara anaziandika sababu mbili ambapo Marko na Luka wanaandika sababu moja tu (kama vile Mt. 8:28 na 20:30). Sababu halisi ya hili haijulikani. Imekuwa ikidhahaniwa kwamba Mathayo alihitaji ushahidi wa aina mbili ili kuyakamilisha mahitaji ya Agano la Kale (kama vile Hes. 35:30; Kumb. 17:6; 19:15).

☐ **"Uturehemu, Mwana wa Daudi"** Hili jina la Agano la Kale pia linatumika katika Mt. 1:20. Kwa uwazi hii lilikuwa na vidokezo vya Kinasihi vyenye kurejelea 2 Samweli 7 (kama vile Mt. 1:1; 12:23; 15:22; 20:30; 21:9,15). Kwa kadri fulani watu hawa walielewa kwa kuyasikia majina haya haijulikani, lakini kwa hakika hii ilikuwa ishara ya imani yao, si kutimiza uelewa wa kithiolojia wa mtu wa Kristo. Wayahudi wa siku zile za Yesu walimtarajia Masihi kuwa mponyaji kutokana na Isa. 35:5-6.

**9:28 "Naam, Bwana"** Hili ni jina "*kurios*." Hili lilitumika katika maana ya "bwana" au "mtawala" au linaweza kuwa jina la kithiolojia la Uungu wa Yesu. Hapa inaonekana kutumika zaidi katika maana ya moja kwa moja kupitia vipofu hawa wawili kulitumia jina la "Mwana wa Daudi" ilidokeza uelewa wa kithiolojia. Yesu aliwatenga mbali na makutano kwa sababu hakutaka kuzieneza habari za uponyaji wao (kama vile Mt. 9:26, 30; 8:4).

**9:29 "alipowagusa macho"** Inashangaza ni mara ngapi maelezo ya vipofu hawa yameandikwa katika Injili. Hata hivyo, hawa walitendewa kwa namna tofauti sana. Hapa Yesu anawagusa macho yao, ili kuiongeza imani yao dhahiri. Urejesho wa kuona kwa hawa vipofu ilikuwa moja ya shahidi za kinabii za yule Masihi (kama vile Zab. 146:8; Isa. 29:18; 35:5; 42:7, 16, 18; Mt. 11:5).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA ) MATHAYO 9: 32-34**

<sup>32</sup>Hata hao walipokuwa wakitoka, tazama, walimletea mtu bubu mwenye pepo. <sup>33</sup>Na pepo alipotolewa, yule bubu alinena, makutano wakastajabu, wakasema, Haijaonekana hivi katika Israeli wakati wo wote. <sup>34</sup>Lakini Mafarisayo wakasema, Kwa nguvu za mkuu wa pepo atoa pepo.

**9:32 "mtu bubu mwenye pepo"** Tofauti kubwa ilifanywa katika Injili kati ya mtu mwenye mapepo na uponyaji wa kimwili. Mfano mzuri wa hili unapatikana katika Marko 7:32 na 9:25: mtu mwenye pepo bubu aliponywaji ambapo alimponya dhidi ya pepo haya, ambaye pia alikuwa bubu, aliondolewa pepo. Japokuwa kutoongea kulisabisha ugonjwa, si ugonjwa wote ulio wa pepo. Agano Jipya linakiri uwepo wa pepo katika ulimwengu. Wale waliotumia muda wao mwingi katika nchi za Ulimwengu wa Tatu wanaikiri kweli hii na kuona kuuona udhahirisho zaidi wa mara kwa mara na katika vipengeli vya Agano Jipya. Hii haimaanishi kuwa kuna pepo wengi zaidi katika Ulimwengu wa Tatu. Mtazamo wa sasa wa ulimwengu wa sasa The modern western worldview is uko kinyume na nguvu ya asili. Tazama mada maalum katika Mt.10:1.

Hili neno "bubu" (*kōphos*) linaweza kumaanisha

1. kiziwi (kama vile Mt. 11:5; Marko 7:32,37; Luko 7:22, lililotumiwa sana na Homer)
2. bubu (kama vile Mt. 12:22; 15:30-31; Luka 1:22; 11:14, lililotumiwa sana na Herodotus)

La kwanza linaweza kulielekea la pili. Muktaadha ndiyo ishara bora ambapo maana hii inakusudiwa.

**9:34**

**NASB, NKJV**

**NRSV** "Kwa nguvu za mkuu wa pepo atoa pepo"

**TEV** "Ni mkuu wa pepo ampaye uweza wa kutoa pepo"

**NJB** "Ni kupitia mkuu wa Ibilisi ambaye humwezesha kutoa pepo"

Hii "mtawala wa mapepo" kinamrejelea pepo mkuu aliye katika Mt. 10:25 anayeitwa *Beelzebul*. Majina yote haya yako pamoja katika Mt. 12:24. Tazama maelezo kamili yahasuyo jina hili mahali hapa.

Inashangaza kwamba Mafarisayo alizona nguvu za Yesu na kuyasikia mafundisho yake walimkataa eti kwa sababu alizikiuka desturi zao. Maelezo haya yanayofanana yanapatikana katika Marko 3:22 na Luka 11:15. Hufuru hii ya aina ile ile inaandikwa kama kuja toka mawinguni katika Yohana. 7:20. Hawa wasingeweza kuyapinga matukio haya ya miujiza ya kweli, hivyo waliyageuza kuwa uweza wa Ibilisi.

Yesu anaijibu shutma hii kwa ukamilifu, ambayo mara nyingi inaitwa "dhambi isiyo sameheka" katika Mt. 12:22 na kuendelea. Dhambi hii isiyo sameheka kwa uwazi ni kule kuendelea kuipinga imani katika Yesu katika uwepo wa nuru kuu. Watu hawa walikuwa vipofu sana kwa nawazo yao waliokuwa nayo awali ambapo hawakuwa na uwezo wa kuiona injili ambayo ilikuwa imefunuliwa wazi sana katika maneno na matendo ya Yesu Kristo. Nuru inapokuwa giza, ni giza lililoje (kama vile Mt. 6:23; 2 Kor. 4:4).

Inatia moyo kwamba mstari huu unaondolewa katika machapisho ya Kiyunani D (Bezae) na katika baadhi ya Kilatini cha Kale MSS, lakini yamo katika mtiririko wote wa machapisho ya herufi kubwa. Mstari huu umo katika Mt. 12:24 na Luka 11:15. Toleo la UBS<sup>4</sup> linalipa hitimisho lake kama "B" (kwa kiasi fulani ni yakini).

☐ "mkuu wa pepo atoa pepo" Kifungu hiki kilimrejelea Shetani (kama vile Mt. 12:24-32, Marko 3:22, na Luka 11:15). Mtazamo wa Mafarisayo katika kuipinga nguvu ya Yesu na mamlaka yake uliwapelekea katika kuwa na dhambi isiyosameheka ya kuigeuza nuru ya Mungu katika giza!

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 9:35-38**

<sup>35</sup>Naye Yesu alikuwa akizunguka katika miji yote na vijiji, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri habari njema ya ufalme, na kuponya magonjwa yote na udhaifu wa kila aina. <sup>36</sup>Na alipowaona makutano, aliwahurumia, kwa sababu walikuwa wamechoka na kutawanyika kama kondoo wasio na mchungaji. <sup>37</sup>Ndipo alipowaambia wanafunzi wake, Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache. <sup>38</sup>Basi mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke watenda kazi katika mavuno yake

**9:35-38** Kuna njia mbili tu za kuhusianisha muhtasari huu mfupi (1) kama muhtasari wenye kurejelea 4:23 au (2) Utangulizi wa agizo la wale Kumi na Wawili lililo katika Mathayo 10.

**9:35 "kuihubiri habari njema ya ufalme"** Ufalme wa Mungu ulizielekea hotuba za kwanza na za pili za Yesu na hasa mifano yake. Kwa namna iliyo dhahiri huu ulirejelea utawala wa Mungu ndani ya mioyo ya watu sasa ambao siku moja utakamilishwa juu ya nchi yote (kama vile Mt. 6:10). Tazama Mada Mada Maalum katika Mt. 4:17. Hili neno "habari" (*euangelion*) linatumika katika semi fupi zinazotumiwa na Mathayo katika Mt. 4:23 na 9:35. Hili linatumika na Yesu katika Mt. 24:14 na 26:13. Hili neno linakuwa jia ya kipimo cha kuyarejelea maisha kwa

ujumla, mafundisho, kifo, ufufuo, kuja nara ya pili, na kuutoa wokovu katika Paulo. Ni karne ya pili pekee ambapo neno hili lilianza kudokeza maelezo ya aina nne yahasuyo maisha ya Yesu (yaani., Injili katika Ireneaus na Clement wa Iskandria).

**9:36 "aliwahurumia"** Inatia faraja kujua namna ya kumpokea Yesu Masihi (kama vile Mt. 14:14;15:32; 20:34) kijamii na kumweneza kidini. Huruma yake kwao inaelezwa ndani ya haya maneno yaliyo katika Luka 13:34.

▣ **"kama kondoo wasio na mchungaji"** Neno "Mchungaji" ilikuwa stia tri ya kawaida iliyotumika kwa viongozi wa kidini (kama vile Hes.27:17; 1 Fal. 22:17; Eze. 34:1-16). Kwa wakati mwingine ilitumika katika maana ya wachungaji wa uongo (kama vile Eze. 34; Zek. 11:5). Yesu ndiye nchungaji mwema (kama vile Yohana. 10; Zek. 11:7-14; 13:7-9).

**9:37-38** Mungu hulitazamia neno lake katika maana tofauti kuliko wanadamu (kama vile Isa. 55:8-9). Waamini wwanahitaji kujiandaa kwa ajili ya Mungu kulisukuma au kulisogeza shamba la mavuno yake. Kwa kutazama uhitaji si kuhimarisha agano bali, kuliko Mungu, pale tuombapo, wakati mwingine Mungu hutuachilia! Tambua kwamba ulimwengu unaonekana kama shambala Mungu la mavuno. Huu ni ulimwengu wake. Anaupenda. Anataka kuukomboa (kama vile Yohana. 3:16; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembe katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini mafundisho haya yanaonekana kuwa na mwonekano wa tofauti na mazingira tofauti katika Vidokezo vya Injili?
2. Nini umuhimu wa kusamehe dhambi ya mtu aliyepooza?
3. Nini umuhimu wa kithiolojia wa neno "Mwana wa Adamu"?
4. Kwa nini ni muhimu kwamba Yesu alikula pamoja na wenye dhambi na watoza ushuru?
5. Yesu anasema nini kuhusu kufungu?
6. Kwa nini mwanamke mwenye kutoka damu alitaka kuligusa pindo la Yesu?
7. Eleza juu ya ubobezi uhusuo misiba.
8. Kwa nini Mathayo kwa uhakika anaandika habari za vipofu wawili au malaika ambapo Marko na Luka anaandika habari za mtu mmoja?
9. Eleza tofauti kati ya ugonjwa wa kimwili na ule wa kipepo.
10. Ni kwa namna gani Mafarisayo walitenda dhambi isiyo sanehewa katika Mt. 9:34?
11. Je! mst. wa 37 na 38 wanazungumza kuhusu moyo wa Mungu?



## MATHAYO 10

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Safari ya kumi na Mbili	Mitume Kumi na Mbili	Kuwezesha na Maelekezo kwa kumi Na Mbili (10:1-11:1)	Mitume Kumi na Mbili	Safari ya Kumi na Mbili
10:1-4	10:1-4	10:1-4	10:1-4	10:1 10:2-5a
Kutumwa kwa Kumi na Mbili	Kuwatuma Kumi na Mbili		Safari ya Kumi na Mbili	
10:5-15	10:5-15	10:5-15	10:5-10 10:11-15	10:5b-10 10:11-16
Mateso Yajayo	Mateso yanakuja		Mateso Yajayo	Wamishionari Watateswa
10:16-23	10:16-26	10:16-23	10:16-20	10:17-20 10:21-23
10:24-25		10:24-25	10:21-23 10:24-25	10:21-23 10:24-25
Nni wa kumuogopa	Yesu anafundisha Hofu ya Mungu		Nani wa Kuogopa	Kauli ya uwazi na bila Kuogopa
10:26-31	10:27-31	10:26-31	10:26-31	10:26-27 10:28-31
Kumkiri Kristo Mbele za Watu	Kumkiri Kristo Mbele Za watu		Kumkiri na kumkana Kristo	
10:32-33	10:32-33	10:32-33	10:32-33	10:32-33
Si amani bali Upanga	Kristo analeta Mgawanyiko		Si amani bali Upanga	Yesu sababu ya Mgawanyiko
10:34-39	10:34-39	10:34-39	10:34-36 10:37-39	10:34-36 Kujikana nafsi na Kumfuata Yesu 10:37-39
Thawabu	Kikombe cha maji		Thawabu	Hitimisho la Maelekezo
10:40-11:1	10:40-42	10:40-11:1	10:40-42	10:40 10:41 10:42

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia"](#))**

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembele katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza

2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## HISTORIA YA NYUMA YA MATHAYO 10:1-42

- A. Wanafunzi wapya waliochaguliwa wanatumwa katika safari ambayo inatabiriwa katika Mt. 9:37-38. Yesu pia aliwatuma, kwa baadaye kundi kubwa la wanafunzi sabini (kama vile Luka 10:1 na kuendelea).
- B. Kifungu hiki kinalinganishwa na Marko 3:14-16; 6:7-13; na Luka 9:1-6. Kunaweza kuwa kulikuwa na aina hizi za safari kadhaa.
- C. Ujumbe wa Yesu kwa Kumi na Mbili umegawanyika sehemu tatu zianazotambuliwa kwa tungo inayojirudia rudia "Hakika nawaambieni" Mt. 10:15,23,42.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 10:1

<sup>1</sup> Akawaita wanafunzi wake kumi na wawili, akawapa amri juu ya pepo wachafu, wawatoe, na kupoza magonjwa yote na udhaifu wa kila aina.

**10:1 "kumi na mbili"** Hii ni mara ya kwanza hesabu hii inatajwa, yawezekana ikishabihiana na makabila kumi na mbili ya Israeli. Angalia Mada Maalum:Hesabu ya Kumi na Mbili katika Mt. 14:20.

☐**"Wanafunzi"** Hii kibayana ni "wanaojifunza." Agano la Kale wanasisitiza wanafunzi, sio tu uamuzi (kama vile Mt. 28:19; Mdo. 14:21)! Mada Maalum hapa chini inazungumzia upekee huu wa kithiolojia.

### MADA MAALUM: WOKOVU (NJEO ZA VITENZI VYA KIYUNANI VILIVYOTUMIKA)

Wokovu siyo kitu, bali ni uhusiano. Haiishii hapo mtu anapomwamini Kristo; ndiyo safari imeanza! Siyo Sera ya bima ya moto, wala tiketi ya kwenda mbinguni, bali ni kukua kumfanana Kristo. Tunao usemi katika Amerikaunaosema, kadiri wawili katika ndoa wanavyoendelea kuishi, ndiyo wanaendelea kufanana. Hili ndilo lengo la wokovu!

#### WOKOVU KAMA KITENDO KILICHO KAMILISHWA (WAKATI TIMILIFU)

- Matendo 15:11
- Warumi 8:24
- 2 Timotheo 1:9
- Tito 3:5
- Warumi 13:11(inajumuisha WAKATI TIMILIFU ukiwa na mazingira ya WAKATI UJAO )

#### WOKOVU KAMA HALI YA KUWA (TIMILIFU)

- Waefeso 2:5,8

#### WOKOVU KAMA MCHAKATO UNAOENDELEA (WAKATI ULIOPO)

- 1 Wakorintho 1:18; 15:2
- 2 Wakorintho 2:15
- 1 Petro 3:21

#### WOKOVU KAMA UKAMILISHO UJAO (WAKATI UJAO katika NJEO YA KITENZI au MAZINGIRA)

- Warumi 5:9, 10; 10:9,13

- 1 Wakoritho 3:15; 5:5
- Wafilipi 1:28;
- 1 Wathesalonike 5:8-9
- Waebrania 1:14; 9:28
- 1 Petro 1:5,9

Kwa hivyo, wokovu unaanza na uamuzi wa imani ya awali (kama vile Yohana 1:12; 3:16; Rum 10:9-13), lakini hili lazima liendane na mchakato wa imani katika mtindo ya maisha (kama vile Rum. 8:29; Gal. 3:19; Efe.1:4; 2:10), ambao siku moja utakuja kukamilishwa kwa kuonekana (kama vile 1 Yoh. 3:2). Hatua hii ya mwisho inaitwa utukufu. Hili linaweza kuelezwa kama

1. Utukufu wa awali – udhihirisho (kukombolewa kutoka katika adhabu ya dhambi)
2. Wokovu endelevu – utakaso (kuokolewa toka katika nguvu ya dhambi)
3. Wokovu wa mwisho – utukufu (kuokolewa kutoka katika uwepo wa dhambi)

☑ **"akawapa mamlaka juu ya pepo wa chafu, wawatoe"** Yesu aliwawezesha wafuasi hawa kwa nguvu zake. Walifanyika wawakilishi wake Rasmi (yaani Mitume). Miujiza ya kimwili ilikuwa njia ya kuthibitisha ujumbe mpya wa Yesu.

## **MADA MAALUM : UPUNGAJI PEPO**

Upungaji Pepo yalikuwa mambo ya kawaida katika siku za Yesu, lakini njia za Yesu zilikuwa tofauti sana (kama vile Mt. 8:16; Marko 1:27). Upungaji Pepo Wake ilikuwa ishara ya Zama Mpya (kama vile Luka 9:1). Walimu wa Sheria za Kiyahudi (kama vile Mt. 12:27; Matendo ya Mitume 19:13) walitumia njia za nguvu za giza (tazama Alfred Edersheim, *The Life and Times of Jesus, The Messiah*, juzuu. 2, kiambatisho XIII, uk. 748-763; XVI, kur. 770-776), lakini Yesu alitumia mamlaka yake Mwenyewe. Kuna mkanganyiko mkubwa na habari mbaya zinazoenea kwa sasa kuhusu upungaji pepo na pepo wachafu. Sehemu ya tatizo hili ni kwamba Agano Jipya haijadili juu ya mambo haya. Kama mchungaji natumaini ninayo habari zaidi kuhusu jambo hili. Hapa kuna baadhi ya vitabu ninavyoviamini.

1. Christian Counseling and the Occult, Kurt E. Koch
2. Demons in the World Today, Merrill F. Unger
3. Biblical Demonology, Merrill F. Unger
4. Principalities and Powers, John Warwick Montgomery
5. Christ and the Powers, Hendrik Berkhof
6. Three Crucial Questions About Spiritual Warfare by Clinton Anton

Hii inanishangaza kwamba upungaji pepo haukuorodheshwa kama moja ya karama za kiroho na suala hilo halielezwi ndani ya barua za ki-Utume. Naamini katika mtazamo wa kiulimwengu kibiblia unahusisha ufalme wa kiroho (yaani, mema na mabaya), wakati uliopo na tendaji katika ufalme wa kiroho (yaani, Ayubu 1-2; Danieli 10; Efe. 6:10-18). Hata hivyo, Mungu amechagua kutofunua ule ubaya. Sisi kama waamini habari zote, tunahitaji kuishi ki-Ungu, maisha yenye manufaa Kwake! Lakini mambo mengine hayajafunuliwa kwa ukamilifu au kuimarishwa. Waamini wanahitaji kukumbuka kwamba upungaji pepo ni ushahidi unaonekana juu ya ushindi wa Yesu dhidi ya uovu (kama vile Luka 10:17-20). Kitabu cha Agano Jipya kinaunda tofauti iliyo wazi kati ya upungaji pepo na uonyaji (kama vile Mt. 8:16; Marko 1:32; Luka 4:40-41).

Tazama Mada Maalum:

1. Mada Malum: Shetani
2. Mada Maalum: Uovu Binafsi
3. Mada Maalum: Pepo Wachafu katika Agano la Kale

Mada Maalum: Pepo Wachafu katika Agano Jipya

☐ "pepo wachafu. . .kuponya kila ugonjwa" Tazama utofauti unaotengenezwa kati ya kupagawa na pepo na ugonjwa. mapepo yanaweza kusababisha magonjwa japo sio siku zote.

## MADA MAALUMU: MALAIKA NA MAPEPO

- A. Watu wa kale waliamini kwamba viumbe vyote vina uhai. Walifikiri kwamba sifa za mwanadamu ni sawa na nguvu ya asili, wanyama, na viumbe vya asili. Maisha yalielezeka kupitia mwingiliano wa uwepo wa vitu/viumbe hivi na wanadamu.
- B. Mifano hii wakati mwingine ilileta matokeo ya kuabudu miungu mingi (miungu wengi). Kwa kawaida mapepo (*genii*) ilikuwa miungu midogo au nusu miungu (mizuri au miovu) ambao ilileta matokeo kadha wa kadha katika maisha ya watu binafsi.
1. Machufuko na migogoro huko Mesopotamia,
  2. Mpangilio na kazi huko Misri,
  3. Kanaani, tazama W. F. Albright's *Archaeology and the Religion of Israel*, Toleo la Tano, kur. 67-9
- C. Agano la Kale halielezi sana au kukuza jambo la miungu wadogo, malaika, au pepo, huenda ni kwa sababu ya msistizo wake mkali unaozungumzia Imani ya Mungu mmoja (tazama Mada Maalumu : Mungu mmoja\_ Imani ya Mungu mmoja kama vile Kut. 8:10; 9:14; 15:11; Kumb. 4:35,39; 6:4; 33:26; Zab. 35:10; 71:19; 86:8; Isa. 46:9; Yer. 10:6-7; Mik. 7:18). Haliizungumzii miungu ya uongo ya mataifa ya wapagani (*Shedim*, BDB 993, kama vile Kumb. 32:17; Zab. 106:37) na halitaji majina au kufananisha baadhi yao.
1. *Se'im* (mazimwi au majitu yenye manyoya, BDB 972 III, KB 1341 III, kama vile Law. 17:7; 2 Nya. 11:15; Isa. 13:21; 34:14)
  2. *Lilith* (jike, pepo apotoshaye kizinifu nyakati za usiku, BDB 539, KB 528, kama vile Isa. 34:14)
  3. *Mavet* (neni la Kiebrania liliotumika kumtaja mungu mwovu wa Wakanani, Mot, BDB 560, KB560, kama vile Isa. 28:15,18; Yer. 9:21; na kwa kadri iwezekavyo Kumb. 28:22)
  4. *Resheph* ( mahali, moto, au mawe yenye kutiririsha mvua ya mawe, BDB 958, KB 958, kama vile Kumb. 32:24; Zab. 78:48; Hab. 3:5)
  5. *Dever* (uharibifu, BDB 184, cf. Zab. 91:5-6; Hab. 3:5)
  6. *Az'azel* (jina halina uhakika, lakini huenda akawa pepo wa jangwani au jina la mahali, BDB 736, KB 736, kama vile Law. 16:8,10,26)

(Mifano hii inachukuliwa kutoka *Encyclopedia Judaica*, juzuu I. 5, uk. 1523.).Hata hivyo, hakuna imani ya Mungu wawili au uhuru wa malaika kutoka kwa YHWH katika Agano la Kale. Ibilisi chini ya YHWH (kama vile Ayubu 1-2; Zekaria 3), hayuko huru, ni adui anayejiongoza (kama vile A. B. Davidson, *A Theology of the Old Testament*, kr. 300-306).

- D. Dini ya Kiyahudi iliendelezwa kipindi cha uhamisho wa Babeli (586-538 b.k). Kitheolojia iliathiriwa aina mbili za Kiajemi zilizochukua nafasi kwa wafuasi wa Zoroaster, mungu mkuu na mzuri alitwa Mazda au Ormazd na mpinga uovu aitwaye Ahriman. Huyu aliruhusiwa ndani ya dini ya Kiyahudi baada ya uamisho na kuwa mfano wa aina mbili kati ya YHWH na malaika Zake na Ibilisi malaika zake au pepo.

Theolojia ya dini ya Kiyahudi yenye kutoa mfano wa uovu inaelezwa na kunakiliwa vema katika Edersheim ya Alfred *The Life and Times of Jesus the Messiah*, juzuu. 2, kiambatisho XIII (kur. 749-863) na XVI (kur. 770-776).

Dini ya Kiyahudi ilitoa mifano ya uovu katika njia tatu.

1. Ibilisi au Malaika wa maangamizi
2. kusudi la uovu (yetzer hara) ndani ya mwandamu
3. Malaika wa Mauti

Edersheim anayabainisha haya kama

1. Mshitaki
2. Mjaribu
3. Mwadhishaji (juzuu. 2, uk. 756)

Kuna tofauti zinazodhihirika kitheolojia kati ya dini ya Kiyahudi iliyokuwepo baada ya uhamisho na nanma

uwasilishaji na maelezo ya uovu inavyofanyika ndani ya Agano Jipya.

- E. Agano Jipya, haswaa Injili, linadai uwepo na upinzani wa uovu wa viumbe vya kiroho kwa mwanadamu na kwa YHWH (katika dini ya Kiyahudi, Ibilisi alikuwa adui wa mwanadamu, lakini si kwa Mungu). Hawa wanayapinga mapenzi ya Mungu, amri, na ufalme.

Yesu alikabiliana na kuvifukuza hivi viumbe vya kimapepo, pia vililitwa (1) roho chafu (kama vile. Luka 4:36; 6:18) au (2) roho za uovu kama vile. Luka 7:21; 8:2), kutoka kwa wanadamu. Yesu kwa udhahiri alitengeneza tofauti kati ya maradhi (kimwonekano na kiakili) na hali ya kimapepo. Aliithibitisha nguvu Yake na mtazamo wa ndani wa kiroho kwa kuwatambua na kuwafahamu hawa pepo wabaya. Mara nyingi walimtambua na kumwita, lakini Yesu aliukataa ushuhuda wao, alihitaji wawe kimya, na kuyafukuzia mbali. Utambuzi wa pepo hawa ni ishara ya kuvunja ufalme wa Ibilisi.

Kuna upungufu wa ajabu wa habari ndani ya barua za Kitume za Agano Jipya kuhusiana na somo hili. Utambuzi huu kamwe haukuorodhesha karama za kiroho, wala methodolojia au hatua yake iliyotolewa kwa ajili ya vizazi vijavyo vya huduma au waamini.

- F. Mwovu yu dhahiri; mwovu ni mtu binafsi; mwovu yupo. Si asili yake wala kusudi lake linalofunuliwa. Biblia inatetea ukweli wake na kwa ukali inapinga ushawishi wake yule mwovu. Ndani ya ukweli hakuna hatima yenye mitazamo yenye uwili ndani yake. Mungu yu ndani ya utawala wake mwenyewe; mwovu anaangamizwa na kuhukumiwa na ataondolewa kutoka katika uumbaji.
- G. Watu wa Mungu yawapasa kumpinga mwovu (kama vile Yakobo 4:7). Hawawezi kutawaliwa na naye (kama vile 1 Yohana 5:18), bali wanaweza kujaribiwa na ushuhuda na ushawishi wake kuangamizwa (kama vile Efe. 6:10-18). Mwovu ni sehemu ya mtazamo wa ulimwengu kwa wakristo uliofunuliwa. Wakristo wa sasa hawana haki ya kueleza wazi kwa mara nyingine (kutafasiri upya maandishi ya Rudolf Baltmann); kuyaua maovu (miundo ya kijamii ya Paul Tillich), wala kujaribu kuelezea kwa ukamilifu katika namna ya kisaikolojia (Sigmund Freud). Ushawishi wake umeenea kote, lakini umeangamizwa. Waamini wanahitaji kuenenda ndani ya ushindi wa Kristo!

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 10:2-15**

<sup>2</sup> Na majina ya hao mitume kumi na wawili ni haya; Wa kwanza Simoni aliyeitwa Petro, na Andrea nduguye; Yakobo wa Zebedayo, na Yohana nduguye; <sup>3</sup> Filipo, na Bartholomayo; Tomaso, na Mathayo mtoza ushuru; Yakobo wa Alfayo, na Thadayo; <sup>4</sup> Simoni Mkananayo, na Yuda Iskariote, naye ndiye mwenye kumsaliti. <sup>5</sup> Hao Thenashara Yesu aliwatuma, akawaagiza, akisema, Katika njia ya Mataifa msiende, wala katika mji wo wote wa Wasamaria msiingie. <sup>6</sup> Afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. <sup>7</sup> Na katika kuenenda kwenu, hubirini, mkisema, Ufalme wa mbinguni umekaribia. <sup>8</sup> Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure. <sup>9</sup> Msichukue dhahabu, wala fedha, wala mapesa mishipini mwenu; <sup>10</sup> wala mkoba wa safari, wala kanzu mbili, wala viatu, wala fimbo; maana mtenda kazi astahili posho lake. <sup>11</sup> Na mji wo wote au kijiji cho chote mtakachoingia, tafuteni ni nani humo aliye mtu mwaminifu; mkae kwake hata mtakapotoka. <sup>12</sup> Nanyi mkiingia katika nyumba isalimuni. <sup>13</sup> Na nyumba ile ikistahili, amani yenu na iifikilie; la, kwamba haistahili, amani yenu na iwarudie ninyi. <sup>14</sup> Na mtu asipowakaribisha wala kuyasikiliza maneno yenu, mtokapo katika nyumba ile, au mji ule, kung'uteni mavumbi ya miguuni mwenu. <sup>15</sup> Amin, nawaambia, itakuwa rahisi nchi ya Sodoma na Gomora kustahimili adhabu ya siku ya hukumu, kuliko mji ule.

**10:2 "majina ya mitume kumi na mbili"** Neno "mtume" (angalia dokezo katika Mt. 10:5) ilinatumika hapa tu katika Mathayo (hapa) na Marko (3:14) katika muunganiko na orodha ya majina ya mitume, pia zaidi katika Marko 6:30. Ni zaidi sana katika Luka na Mdo..

1. Luka 6:13; 9:10; 11:49; 17:5; 22:14; 24:10

2. Mdo.

a. kumi na mbili, Mdo. 1:2,26; 2:37,42,43; 4:33,35,36,37; 5:2,12,18,29,40; 6:6; 8:1,14,18; 9:27; 11:1; 15:2,4,6,22,23; 16:4

- b. mitume wengine (matumizi ya baadaye ya neno)  
 (1) Paulo, Mdo. 14:4,14 (mamlaka sawa na kumi na mbili)  
 (2) Barnaba Mdo. 14:14 (mamlaka ya kimasomo)

Orodha ya Mitume inapatikana katika Marko 3:16-19, Luka 6:12-16, na Mdo. 1:13-14. Majina na mpangilio unabadilika kidogo. Hata hivyo siku zote yako katika makundi matatu ya nne. Petro siku zote huwa ni wa kwanza na Yuda Iskarioti huwa ni wa mwisho. Kuwekwa kimakundi huwa kunabaki vile vile. Kuwekwa kimakundi kunawezekana kulikuwa mfumo wa mzunguko ambapo wanafunzi Fulani walikuwa na uwezo wa kwenda nyumbani kwa muda mfupi kuangalia familia zao.

## MADA MAALUMU: CHATI YA MAJINA YA MITUME

	<b>Mathayo 10:2-4</b>	<b>Marko 3:16-19</b>	<b>Luka 6:14-16</b>	<b>Matendo 1:12-18</b>
<b>Kundi la kwanza</b>	Simoni (Petro) Andrea (Petro nduguye) Yakobo (mwana wa Zebedayo) Yohana (nduguye Yakobo)	Simoni (Petro) Yakobo (mwana wa `Zebedayo) Yohana (nduguye Yakobo) Andrea	Simoni (Petro) Andrea (Petro nduguye) Yakobo Yohana	Petro Yohana Yakobo Andrea
<b>Kundi la pili</b>	Filipo Bartholomayo Thomaso Mathayo (mtunza ushuru)	Filipo Bartholomayo Mathayo Thomaso	Filipo Bartholomayo Mathayo Thomaso	Filipo Thomaso Bartholomayo Mathayo
<b>Kundi la tatu</b>	Yakobo (mwana wa Alfayo) Thadayo Simoni (Mkananayo) Yuda (Iskariote)	Yakobo (mwana wa Alfayo) Thadayo Simoni (Mkananayo) Yuda (Iskariote)	Yakobo (mwana wa Alfayo) Simoni (Zelote) Yuda (wa Yakobo) Yuda (Iskariote)	Yakobo (mwana wa Alfayo) Simoni (Zelote) Yuda (wa Yakobo)

Kutoka katika muhtasari wa Luka 6:14:

☐ **“Simoni, aliyemwita jina la pili Petro”** Kuna orodha nyingine tatu za mitume kumi na wawili. Kwa kawaida Petro ni wa kwanza; Yuda Iskariote ni wa mwisho daima. Kuna makundi matatu kati ya manne ambayo yamebaki kwa usawa, hata kama mtiririko wa majina ndani ya makundi unageuzwa mara kwa mara (kama vile Mathayo 10:2-4; Marko 3:16-19; Matendo 1:13).

☐ **“Andrea”** Neno la Kiyunani linamaanisha “mwenye sifa za kiume.” Kutoka Yohana 1:29-42 tunajifunza kwamba Andrea alikuwa mwanafunzi wa Yohana Mbatizaji na kwamba alimtambulisha nduguye, Petro, kwa Yesu.

☐ **“Yakobo”** Hili ni jina la Kiebrania “Jacob” (BDB 784), ambalo linamaanisha “chukua nafasi ya,” kama vile Mwa. 25:26). Kuna wanaume wawili wanaitwa Yakobo katika katika orodha ya wale Kumi na wawili. Ni nduguye Yohana (kama vile Marko 3:17) na sehemu ya mzunguko wa ndani (yaani, Petro, Yakobo, na Yohana). Huyu ni nduguye Yohana.

☐ **"Yohana"** Huyu alikuwa nduguye Yakobo na moja wa mzunguko wa ndani wa wanafunzi. Aliandika vitabu vitano katika Agano Jipya na aliishi kipindi kirefu kuliko mtume ye yote yule.

☐ **"Filipo"** Jina la Kiyunani linamaanisha "mpenda farasi" Wito wake umeandikwa katika Yohana 1:43-51.

☐ **"Bartholomayo"** Jina linamaanisha "mwana wa mtawala wa Misri" Anaweza kuwa Nathanaeli wa Injili ya Yohana (kama vile Yohana 1:45-49; 21:20).

☐ **"Mathayo"** Jina la Kiebrania (kutoka *Mattithiah*, kama vile 1 Nya. 9:31; 15:18,21; 16:5; 25:3,21; Neh. 8:4) linamaanisha "karama ya YHWH." Hii inarejea katika Lawi (kama vile Marko. 2:13-17).

☐ **"Tomaso"** Jina la Kiebrania linamaanisha "pacha" au Didimus (kama vile Yohana 11:16; 20:24; 21:2).

☐ **"Yakobo wa Alfayo"** Hili ni jina la Kiebrania "Yakobo." Kuna wanaume wawili walioitwa kwa jina la Yakobo katika wale Kumi na wawili. Mmoja ni nduguye Yohana (kama vile Luka 6:17) na sehemu ya mzunguko wa ndani (yaani, Petro, Yakobo, na Yohana). Huyu anajulikana kama "Yakobo aliye mdogo" (kama vile Marko 3:17).

☐ **"Simoni aitwaye Zelote"** Maandishi ya Kiyunani ya Marko yana "Mkananayo" (pia Mathayo. 10:4). Marko, ambaye Injili iliandikwa kwa Warumi, asingetakiwa kutumia "maneno makali" ya kisiasa, Zelote, ambalo linarejea juu ya Wapigania Mabadiliko wa Kiyahudi Waishio mstuni walio kinyume na utawala wa Kirumi. Luka anamtaja kwa istirahi hii (kama vile Mdo 1:13). Istirahi ya Mkananayo ina minyumbuo mbali mbali.

1. kutoka eneo la Galilaya lijulikanalo kama Kana
2. kutoka matumizi ya Agano la Kale ya Wakanaani kama mfanyabiashara
3. kutoka jina la jumla kama mwenyeji wa Kanaani.

Kama jina la jumla aliloliumia Luka ni sahihi, basi Zelote linatokana na neno la Kiaramu "*mwenye shauku*" (kama vile Mdo. 1:17). Uchaguzi wa Yesu wa wanafunzi kumi na wawili walikuwa wametoka makundi shindani tofauti na mbalimbali. Simoni alikuwa mmoja wa kundi la kizalendo ambalo lilipigania kupinduliwa kwa ghasia za mamlaka ya Kirumi. Mara nyingi Simoni na Lawi (yaani, Mathayo, mtoza ushuru) na kila mmoja . Wasingekuwa katika chumba kile kile

☐ **"Yuda wa Yakobo"** Pia aliitwa "Lebbeus" (kama vile Mt. 10:3) au "Yuda" (kama vile Yohana 14:22). Wote Thadayo na Lebbeus inamaanisha "mtoto apendwaye."

☐ **"Yuda Iskariote,"** Kuna Simoni wawili, Yakobo wawili, na Yuda wawili. Jina Iskariote lina uwezekano wa minyumbuo miwili:

1. mtu wa Kerioth (mji) katika (kama vile Yos. 15:23, ambapo ingemaanisha yeye alikuwa waYudea pekee)
2. jina la baba yake (kama vile Yohana 6:71; 13:2,26)
3. "mtu wa uadui" au mwaaji, ambapo ingemaanisha yeye pia alikuwa Zelote, kama Simoni

**10:3 "Barthomayo"** Aliitwa pia Nathanieli (kama vile Yohana. 1:45-51).

☐ **"Mathayo"** Aliitwa pia Lawi (kama vile Marko 2:14; Luka 5:27).

☐ **"Thaddeo"** Aliitwa pia Yuda, mwana au kaka wa Yakobo (kama vile Luka 6:16; Mdo. 1:13) au Lebbaeus (andiko la Kiyunani MSS C<sup>2</sup>, L, na W).

**10:4**

**NASB "Simon the Zelote"**

**NRSV "Simoni Mkananayo"**

TEV "Simoni Mkananayo"

NJB "Simoni Mzalendo"

Pia aliitwa "Mkananayo," ambalo likimaanisha kwamba ni mtu atokaye Kana (kama vile Marko 3:18). Hata hivyo Wayunani waliaksi neno la Kiebrania "mwenye wivu." Alikuwa mzalendo wa Kiyahudi na Mtenganishaji (kama vile Luka 6:15; Mdo. 1:13). Kwa Mathayo na Simoni kuwa katika kundi moja kunaonesha mabadiliko ya msingi ambayo Yesu alifanikisha katika maisha ya watu hawa.

☐ "Iskarioti" Neno hili linaweza kumaanisha mtu anayetoka jiji la Yuda, Kerioth (kutoka katika Kiebrania), au kisu cha muuaji alengaye (kutoka katika Kiyunani). Ikiwa alikuwa anatokea Yuda, alikuwa mtume pekee kutokea kusini.

☐ "mtu aliyemsaliti" Kuna kitabu cha kufurahisha ambacho kinajaribu kumfasiri Yuda katika namna chanya zaidi na mpya, *Judas, Betrayer or Friend of Jesus?* cha William Klassen, kilichochapishwa na Fortress Press, 1996. Hata hivyo ili kufanya hivyo kiukamilifu kinapuuzia Injili ya Yohana.

**10:5 "akawatuma"** Huu ulikuwa kutoka mzizi ule ule wa Kiyunani kama "mtume" (*apostello*, linalotoka katika LXX kwa Mungu kutuma manabii kwa ajili ya kuzungumza naye), ambayo ilikuja katika mzunguko wa walimu wa kiyahudi "waliotumwa" ikiwa na maana ya mamlaka ya kiofisi. Marko 6:7 inatwambia Yesu aliwatuma Mitume katika jozi.

☐ "msiende katika njia ya Mataifa na wala kuingia katika miji ya Wasamaria" Hii inawezekana kuwa chanzo cha Paulo "kwa Wayahudi kwanza pia na Wayunani" (kama vile Rum. 1:16). Hii haukuwa unyanyapaa bali kuweka mipaka kwa msisitizo wake ili kuwapa uzao wa Ibrahimu kila nafasi ya kuitikia.

Wayahudi waliwachukia Wasamaria kwasababu walichukuliwa kama machotara. Hii ilirejerea kwa Uhamisho wa Ashuru wa Makabila Kumi ya Kaskazini mwa Israeli katika 722 B.K. Maelfu ya Wayahudi walihamishiwa Media na maelfu ya Mataifa walipelekwa kuchukua nafasi yao katika Israeli. Baada ya miaka mingi ya mchanganyiko wa kidini na desturi za kijamii kutokea (kama vile Ezra na Neh.). Kwa wakati huu wa mapema wa huduma ya Yesu ujumuishi wa makundi haya ungeathiri uwezo Wake wa kuwafikia Wayahudi!

**10:6 "kondoo waliopotea"** Huu ulikuwa muunganiko wa maneno usiokuwa wa kawaida; "kondoo" mara kwa mara ilirejerea watu wa Mungu (kama vile Yohana. 10), wakati "waliopotea" ilimaanisha kutojitosheleza kwao kiroho na kuwepo hatarini (kama vile Mt. 9:36), hasa ikiwa hakuna mchungaji (kama vile Hes. 27:17; 1 Wafalme. 22:17; Zab. 119:176; Isa. 53:6; Zek. 13:7).

☐ "wa nyumba ya Israeli" Hii ilikuwa ni njia ya kurejerea uzao wa mababa wa imani.

Wao pia hujulikana kama

1. nyumba ya Yakobo (yaani Luka 1:33, kama Mt. 15:24; Mdo. 2:36; Ebr. 8:8)
2. nyumba ya Yuda (yaani Ebr. 8:8)
3. watoto wa Ibrahimu (yaani, Mt. 3:9; Yohana 8:33,39)

### MADA MAALUM: ISRAELI (Jina)

- I. Kwa mshangao maana ya jina haijulikani (BDB 975, KB 442).
  - A. *El kug'ag'ania*



- B. Mwache *El* ag'ag'ane (KAULI AMRISHI)
- C. *El* Hulinda
- D. *Mwache El* na apambane
- E. *El* Achuchumilie
- F. Yule apambanaye na Mungu (neni la mzaha la Mwa. 32:28)
- G. Mwenye Kutegemewa (IDB, juzuu ya 2, uk. 765)
- H. Aliye fanikiwa
- I. Furaha

II. Matumizi katika Agano la Kale

- i. Jina la Yakobo (mbadilishaji, mshika kisigino, BDB 784, KB 872, kama vile Mwa. 25:26) linabadilishwa baada ya kushindana mweleka na mtu katika mto Yaboki (kama vile Mwa. 32:22-32; Kut. 32:13). Mara nyingi maana ya majina ya Kiebrania ayanatamkika kama lahaja, si kwa asili zake (kama vile Mwa. 32:28). "Israeli" likawa jina lake la kupewa (kama vile, Mwa. 35:10).
- ii. Hili lilikuja kutumika kama jina la jumla kwa wana wote kumi na wawili wa Yakobo (mf. Mwa. 32:32; 49:16; Kut. 1:7; 4:22; 28:11; Kumb. 3:18; 10:6).
- iii. Hili lilikuja kubeba wadhifa wa taifa lililoundwa kwa makabila kumi na mawili kabla ya kipindi cha kutangatanga jangwani (kama vile Mwa. 47:27; Kut. 4:22; 5:2) na baadaye (kama vile Kut. 1:1; 18:6; 33:10).
- iv. Baada ya muungano wa utawala wa kifalme wa Sauli, Daudi, na Suleimani chini ya waliyatenga makabila Rehoboamu (kama vile 1 Fal. 12).
  - 1. tofauti inaanza hata kabla ya utenganishaji wa kiutawala (mf. II Sam. 3:10; 5:5; 20:1; 24:9; 1 Fal. 1:35; 4:20)
  - 2. hili linabeba wadhifa wa makabila ya kaskazini hadi kufikia kuanguka kwa Samaria hadi Ashuru katika 722 K.K. (kama vile 2 Wafalme 17).
- v. Hili linatumika kumaanisha Yuda katika maeneo machache (mf. Isaya 1; Mika 1:15-16).
- vi. Baada ya kupelekwa utumwani Ashuru na Babeli kwa mara nyingiine jina hili lilikuwa jina la ujumla kwa vizazi vya Yakobo vilivyoishi katika Palestina (mf. Isa. 17:7,9; Yer. 2:4; 50:17,19).
- vii. Hili lilitumika jumuishi la muundo wa kuwatofautisha makuhani (kama vile 1 Nya. 9:2; Ezra 10:25; Neh. 11:3).

**10:7 "mwendapo"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo iliyotumiwa kama kauli shurutishi (kama vile Mt. 28:19).

☐ **"hubirini"** Hii ilikuwa ni kauli shurutishi ya wakati uliopo. Ni kuoneshwa kujacho kwa (1) safari za kimisionari za Kumi na Mbili na Sabini (2) Agizo Kuu la Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8.

☐ **"ufalme. . .umewaijilia"** Haya yalikuwa ni maudhui ambayo walitakiwa kuyahubiri (kama vile Mt. 3:2; 4:17; Marko 1:15; Luka 10:9,11; 11:20; 21:31). Ufalme upo katika utawala wa Mungu katika moyo wa wanadamu sasa ambao siku moja utahitimishwa juu ya dunia yote (kama vile Mt. 6:10). Ingawa wanafunzi hawakuelewa hili bado (yaani Luka 24:16,31), Ilianza na kuvaa mwili kwa Kristo (Masihi) na kutimishwa kwa Ujio wa Pili wa Kristo. Mwanzoni Yesu na wanafunzi walihubiri ujumbe sawa na Yohana Mbatizaji. Angalia [MADA MAALUM: UFALME WA MUNGU](#) katika Mt. 4:17.

**10:8 "ponya. . .fufua. . .takasa. . .toeni"** Hizi zote ni kauli shurutishi (kama vile Mt. 10:1). Walikwenda na kuhudumu kama Yesu alivyo hudumia. Nguvu yake na mamlaka yalikuwa yakitiririka kupitia wao. Ishara hizi zilithibitisha ujumbe wao kuhusu Yeye. Maandiko ya Kiyunani yanajumuisha matoleo tofauti tofauti ya tungo "fufueni wafu." Hii inaweza kuwa kwasababu (1) Kumbukumbu za kibiblia zinakosa kusema kwamba kumi na mbili

walifanya hiki, (2) ni stiari ya kufa mfu kiroho, na (3) Mathayo alitumia vitenzi vingine vitatu mara kwa mara bila kutaja "kufufua wafu." Angalia Bruce Metzger, *A Textual Commentary On the Greek New Testament*, ukur. 27-28. Tungo hii inajumuisha katika matoleo ya MSS,  $\alpha$ , B, C, D, N, na matoleo mengine mengi.

☐ **"viwete"** Katika Agano la Kale magonjwa ya ukoma ilikuwa ni ishara ya kukosa kibali (kama vile 2 Nyakt. 26:16-23).

☐ **"toeni pepo"** Nguvu ya Yesu ni kubwa kuliko ya shetani na mapepo (kama vile 1 Yohana. 4:4). Mapepo yanaelezwa kama "roho," (kama vile Mt. 8:16) "roho wachafu," (kama vile Mt. 10:1). Asili ya pepo haiwekwi wazi. Walimu wa kiyahudi wanataja asili ya uovu katika ulimwengu wa Mwanzo 6 (Paulo anasema ilikuwa Mwanzo 3, kama vile Rum. 5:12-21). Walielezea kwamba "wana wa Mungu" (angalia Mada Maalum katika Mwanzo 1-11 fasiri katika tovuti [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org) inayotajwa katika Mwanzo 6 ilifanyika isiyoshikika wakati wa mauti yake wakati wa gharika la Nuhu na kufanyika pepo wakati wa Agano Jipya ikitafta mwili mwingine.

☐ **"mmepewa bure, toeni bure"** Hiki sio kifungu dhidi ya mishahara kwa wamishonari bali ni kuwatia moyo waamini kumtumaini Mungu wakati wakifanya kazi ya ufalme katika (1) Nguvu zake, (2) utoshelevu wake, na (3) Kusudi lake kutimilizwa. Mistari hii si kanuni za kiulimwengu bali miongozo kwa aina hii ya safari za umisionari (kama vile Luka 22:35-36). Ni ufanyiaji kazi wa kivitendo wa Mt. 6:25-34 mpaka hali ya sasa.

**10:9 "mifuko yenu"** Hii ilikuwa ni namna ya karne ya kwanza ya Wayahudi kubeba fedha zao.

**10:10 "mfuko"** Aina hii ya mfuko ilifanya kazi kama kibebeo. Wanafunzi walitakiwa kuibeba na kubeba kila kitu walichokihitaji lakini wakimwamini Mungu kwa ajili ya utoshelevu wa kila siku.

☐ **"au hata koti mbili, au ndala, au fimbo"** Ulinganifu wa Marko 6:8-9 umesababisha mabishano makubwa. Nadharia ni

1. "fimbo" inaweza kutumia katika namna mbili tofauti: fimbo ya kutembelea au rungu la kujilindia
2. mashati mawili ya Mt. 10:10 inamaanisha "usichukue zaidi ya vitu hivi"
3. Luka 22:35-36 inaonesha uwekwaji pamoja

Injili ziliandikwa kwa ajili yetu ili tuweze kulinganisha maelezo. Msingi wa andiko hili ni kwamba waamini wanatakiwa kumwamini Mungu kwa kukidhiwa kwa mahitaji; kutegemea vyanzo Vyake!

☐ **"kwa maana mtenda kazi anastahili ujira wake"** Yesu yawezekana anaelezea kweli ya Kumb. 25:4 (kama vile 1 Kor. 9:6-7,14; 1 Tim. 5:18), ambayo inaturudisha Kumb. 24:14-15 (kama vile Law. 19:13). Wahubiri wa Injili wanatakiwa wasaidiwe na wasikiaji wao! Miongozo ya Agano Jipya kwa ajili ya utoaji sio utoaji zaka wa Agano la Kale bali utoaji wa kutaka, kwa furaha na kwa kujidhabihu kulingana na uwezo (kama vile 2 Wakorintho 8-9). Angalia [MADA MAALUM: UTOAJI ZAKA](#) katika Mt. 23:23.

**10:11**

**NASB** "tafuteni ni nani humo aliye mtu mwaminifu; mkae kwake hata mtakapotoka "

**NKJV** "tafuteni ni nani humo aliye mtu mwaminifu; mkae kwake hata mtakapotoka "

**TEV** "tafuteni ni nani humo aliye mtu mwaminifu; mkae kwake hata mtakapotoka "

**NJB** " tafuteni ni nani humo aliye mtu mwaminifu; mkae kwake hata mtakapotoka "

Walipofika katika vijiji (1) walikuwa wakitafuta nyumba ya wacha Mungu ambayo ilitamani Baraka za uwepo wao na (2) hawakutakiwa kuondoka tena kutafuta makao bora zaidi. Inawezekana kwamba nyumba ya watauwa ingekuwa ni ile ya kwanza kuiikia mahubiri yao.

**10:12 "wasalimiani"** Hii ilirejerea Baraka ya asili ya Kiyahudi, *shalom*

**10:13 "ikiwa. . ikiwa"** Hizi ni sentensi mbili daraja la tatu zenye masharti zinazorejerea kitendo kinawezekana kutokea mbeleni.

**10:14 "kunguteni mavumbi katika miguu yetu"** Hii ilikuwa ni ishara ya kiyahudi ya kukataliwa (kama vile Mdo. 13:51; 18:6).

**10:15** Hiki ni kifungu kimoja ambacho kinamaanisha kiwango cha hukumu kikijikita katika kiwango cha ufahamu ambacho kimekataliwa (kama vile Mt. 11:22-24). Pia tazama kitabu kile kile ambacho kinafunua upendo wa Mungu usifananishwa pia kufunua ghadhabu ya Mungu na hukumu. Angalia [MADA MAALUM: VIWANGO VYA THAWABU NA ADHABU](#) katika Mt. 5:12.

☑ **"hakika"** Angalia Mada Maalum katika Mt. 5:18

**ANDIKOLA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 10:16-20**

<sup>16</sup> Angalieni, mimi nawatuma kama kondoo kati ya mbwa-mwitu; basi iweni na busara kama nyoka, na kuwa watu wapole kama hua. <sup>17</sup> Jihadharini na wanadamu; kwa maana watawapeleka mabarazani, na katika masinagogi yao watawapiga; <sup>18</sup> nanyi mtachukuliwa mbele ya maliwali na wafalme kwa ajili yangu, kuwa ushuhuda kwao na kwa mataifa. <sup>19</sup> Lakini hapo watakapowapeleka, msifikiri-fikiri jinsi mtakavyosema; maana mtapewa saa ile mtakavyosema. <sup>20</sup> Kwa kuwa si ninyi msemao, bali ni Roho wa Baba yenu asemaye ndani yenu.

**10:16 "nawatuma kama kondoo"** Kondoo ilikuwa ni stiari kwa jamii ya imani mpya lilikowa dhaifu, lisilo na msaada, lenye uhitaji wa kuhudumiwa kila mara na kupewa ulinzi, angalia Luka 10:3 na Yohana. 10. Hii ni mara ya kwanza ya stiari nne kutoka katika ufalme wa wanyama ambayo yanatengeneza tabia ya kibinadamu.

☑ **"katikati ya mbwa mwitu"** Mbwa mwitu waliwakilisha wale walioshambulia jamii mpya ya imani, angalia Mt. 7:15-27; Luka 10:3; Yohana. 10:12; Mdo.20:29; 2 Petro 2.

☑ **"wajanja kama nyoka na wapole kama njiwa"** Waamini lazima wawe wenye hekima lakini wasio na makosa (kama vile Rum. 16:19). Walitakiwa kukwepa migogoro inapobidi lakini watangazaji wa injili.

**10:17 "kwasababu ya. . ."** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo (kama vile Mt. 7:15; 16:6,11). Hata katika kuchomoza kwa nyakati mpya (Warumi 5-6), nyakati mpya inabaki (Warumi 7)! Huu ni uvutano wa "ulio tayari" na "usio tayari" kuingiliana (yaani ujio mbili za Kristo) wa nyakati mbili. Angalia Mada Maalum katika Mt. 12:31.

☑ **"mahakama"** Hii inarejerea mahakama za nyumbani za sinagogi za kiyahudi (kama vile Mt. 23:34). Inafurahisha kutambua kwamba mazingira baadhi ya matukio ya siku za mwisho ya Marko (kama vile Marko 13:9-13) ya Yesu yanarudiwa rudiwa hapa badala ya Mathayo 24. Hivyo jukumu hili la kimisheni la wanafunzi linachukua maana ya kimatukio ya siku za mwisho (kama ilivyokuwa katika Mt. 10:23).

☑️"**dhihaki**" Hii inarejerea upigaji fimbo wa Kiyahudi (kama vile Kumb. 25:3), ambayo ilijumuisha angalau fimbo arobaini, robo sehemu ya mbele ya mwili na zinazobaki katika mgongo (kama vile 2 Kor. 11:24).

☑️"**katika Sinagogi lao**" Angalia ufanano katika katika Mt. 23:34. Hii ilikuwa sehemu ya kuabudu ya nyumbani, elimu na ahueni ya ustawi.

**10:18 "mtapelekwa mbele ya watawala na wafalme"** Hii inarejerea kuenea kwa ulimwengu juu ya injili (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8). Ni muhimu kwamba kutojumuishwa huku kudogo kwa Mt. 10:5 kusawazishwe na mstari huu. Gordon Fee (*How to Read the Bible For All Its Worth*, ukur. 133) kunatoa maelezo kwamba Mt. 10:5-12 kunahusiana na kutumwa kwa Kumi na Mbili kwa mitume wapya, lakini Mt. 10:10-20 ni maelekezo kwa muda wa baadaye (yaani gavana, falme, mataifa) kwasababu kwa mara ya kwanza Yesu alikuja tu kwa kondoo waliopotea wa Israeli. Hii inaelezea namna gani waandishi wa Injili "walichagua, walipanga upya, na kuasilisha" mafundisho ya Yesu ili kukutana na mahitaji ya kanisa la kwanza.

Mfano mwingine wa hii ni Mt. 10:23 "mpaka mwana wa adamu atakapokuja" (angalia dokezo katika Mt. 10:23). Kidhahiri hii inaweza kuwa na maana kadhaa kutegemeana na kipindi cha kihistoria.

☑️"**watawala na wafalme**" Ikiwa hii inarejerea kwa (1) Siku ya Yesu, alafu Pontio Pilato au (2) shughuli za kimisionari za Paulo

1. "watawala" inaweza kuwa watawala wa Kirumi wa Felix (Mdo. 23:24) au Festo (Mdo. 24:27)
2. "wafalme" inaweza kuwa Agrippa I (Mdo. 12:1) au Agrippa II (Mdo. 25:13)

Walikuwa kimsingi wakisimama kama mamlaka ya kiserikali wa kila namna.

**10:19** Hii inazungumzia unurulishwaji na naama kipindi cha mateso (kama vile Marko 13:11; Luka 21:12). Hili sio andiko la uthibitisho kwa wahubiri na walimu kwamba wasisome kabla ya kuanza kutangaza! Mstari huu na mistari ya 26 ni kauli tegemezi ya wakati uliopita usio timilifu ikiwa na kiambata kanushi. Mistari ya 28 na 31, ambayo pia inashughulika na hofu, ni kauli shurutishi ya wakati uliopo ikiwa na kiambata kanushi ambacho kila mara kilimaanisha kuacha kitendo kinachoendelea.

**10:20 "ni Roho wa Baba"** Hapa Roho Mtakatifu anaunganishwa na Baba (kama vile Rum. 8:11,14). Katika Rum. 8:9; 2 Kor. 3:17; Gal. 4:6; na 1 Pet. 1:11 Roho anaunganishwa na Mwana. Kuna sintofahamu kati ya nafsi na Utatu. Wote vinashiriki katika matendo ya ukombozi. Angalia [MADA MAALUM: UTATU](#) katika Mt. 3:17.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 10:21-22**

<sup>21</sup> Na ndugu atamsaliti nduguye ili auawe, na baba atamsaliti mwana, na wana watawainukia wazazi wao, na kuwafisha. <sup>22</sup> Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu; lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayeokoka.

**10:21** Hii inazungumzia kujizatiti kusikobadilika muhimu kwa kufanya wanafunzi ambako kunazidi hata upendo familia na mara kwa mara kusababisha mgogoro ndani ya familia (kama vile Mt. 10:34-39).

**10:22 "utachukiwa na watu wote kwasababu ya jina Langu"** Mateso yalikuwa yakitarajiwa kwa ajili ya wanafunzi wa Yesu (kama vile Mt. 5:10-12; Yohana 15:18-21; 16:1-3; 17:14; Mdo. 14:22; Rum. 5:3-4; 8:17; 2 Kor. 4:16-18; 6:3-10; 11:23-30; Flp. 1:29; 1 Thes. 3:3; 2 Tim. 3:12; Yakobo 1:2-4; na wote wa 1 Petro).

## MADA MAALUM: KWANINI WAKRISTO WANATESEKA?

1. Kwasababu ya dhambi binafsi (hukumu ya muda). Hii haimaanishi kwamba matatizo yote na mazingira magumu ni matokeo ya dhambi (kama vile Ayubu; Zaburi 73; Luka 14:1-5; Nehemia 9; Yohana 9; Mdo. 5:1-11; 1 Kor. 11:29-30; Gal. 6:7).
2. Kukuza hali ya kufanana na Kristo (Ebr. 5:8). Hata Yesu, ukizungumza kibinadamu alitakiwa akomae na ndivyo inavyowapasa wafuasi wake (kama vile Rum. 5:3-4, 8:28-29; 2 Kor. 12:7-10; Flp. 3:10; Ebr. 12:5-12; Yakobo 1:2-4; 1 Pet. 1:7).
3. Kukuza ushuhuda wenye nguvu na wenye uhalisia (kama vile Mt. 5:10-12; Yohana 15:18-22; 1 Pet. 2:18-21, 3:13-17).
4. Kama ishara ya kuzaa kwa uchungu kwa Zama mpya (kama vile Mt. 24:6; Marko 13:8).

Vitabu viwili ambavyo vimenisaidia mimi kushughulikia kutokuwepo na usawa na uovu wa ulimwengu ulioanguka ni Hannah Whithall Smith, *The Christian's Secret of a Happy Life* na John W. Wenham, *The Goodness of God*.

Mwamini lazima akumbuke kwamba matatizo na mateso sio kwamba ni ishara ya hasira ya Mungu au kukataliwa. Vitu vibaya hutokea kwa wafuasi waamiifu katika ulimwengu ulioanguka (kama vile. 1 Pet. 4:12-19). Ahadi za Mungu na kujitoa kwa Kristo ni ishara za upendo wa Mungu (kama vile Rum. 5:8). Maandiko lazima yachukue nafasi juu ya hali za muda!

☐ **"atakayevumilia mpaka mwisho ndiye atakayeokoka"** Mafundisho ya "ustahimilivu" (angalia Mada Maalum hapa chini) ni kama kibiblia "usalama wa waamini!" (kama vile Mt. 24:13; Gal. 6:9; Ufu. 2:7,11,17,26; 3:5,12; 21:7). Lazima tukiri kweli zote hata kama zitasababisha uvutano wa kima fundisho! Mafundisho yanatolewa katika mahusiano ya kujaa ukinzani na mafundisho mengine, sio kweli zilizojitenga. Maelezo mazuri ni kwamba ukweli wa Biblia unafunuliwa kama kusanyiko la nyota, sio nyota moja. Lazima tujikite katika utaratibu wa ufunuo mzima wa kibiblia. "Mwisho" (*telos*) inarejerea mwisho wa kizazi hiki (kama vile Mt. 24:6,13,14). "Kuokolewa" kunaweza kueleweka katika namna yake ya Agano la Kale juu ya ukombozi wa kimwili au namna yake ya Agano Jipya ya wokovu wa kiroho.

## MADA MAALUMU: USTAHIMILIVU

Mafundisho ya kibiblia yaliyohusiana na maisha ya Mkristo ni vigumu kuyaelezea kwa sababu yanawasilishwa katika namna ile ile ya mashariki, milinganyo ya kirahaja (tazama Mada Maalumu: Fasihi ya Mashariki [mafumbo ya kibiblia]). Milinganyo hii inaonekana kuwa na mkanganyiko, bado mihimili yote ni ya kibiblia.

Wakristo wa Mashariki walielekea kuchagua ukweli ulio mmoja na kuachana au kukashifu kweli iliyo kinyume. Baadhi ya Mifano ni:

1. Je! Wokovu ni maamuzi asilia ya kumwamini Kristo au ni maisha yenye wajibu ya kiuwanafunzi?
2. Je! Wokovu ni uchaguzi kwa maana ya neema kutoka katika mamlaka ya Mungu au imani na mawitiko wa toba kwa sehemu ya mwanadamu kwa majitoleo ya Mungu?
3. Je! wokovu, unapopokelewa, haiwezekani kuupoteza, au kuna uhitaji wa jitihada endelevu

Jambo hili la ustahimilivu limekuwa la kibishi katika historia nzima ya kanisa. Tatizo linaanza na muonekano wa mgogoro wa vifungu vya Agano Jipya:

1. maandiko yahasuyo uhakika
  - a. semi za Yesu katika Injili ya Yohana (Yohana 6:37; 10:28-29)
  - b. semi za Paulo (Rum. 8:35-39; Efe. 1:13; 2:5,8-9; Flp. 1:6; 2:13; 2 The. 3:3; 2 Tim. 1:12; 4:18)
  - c. semi za Petro (1 Pet. 1:4-5)
2. maandiko yahasuyo umuhimu wa ustahimilivu
  - a. semi za Yesu katika Injili za Kimuhtasari (Mt. 10:22; 13:1-9,24-30; 24:13; Marko 13:13)
  - b. semi za Yesu katika Injili ya Yohana (Yohana 8:31; 15:4-10)

- c. semi za Paulo (Rum. 11:22; 1 Kor. 15:2; 2 Kor. 13:5; Gal. 1:6; 3:4; 5:4; 6:9; Flp. 2:12; 3:18-20; Kol. 1:23; 2 Tim. 3:2)
- d. semi za mwandishi wa Kiebrania (2:1; 3:6,14; 4:14; 6:11)
- e. semi za Yohana (1 Yohana 2:6; 2 Yohana 9; Ufu. 2:7,17,26; 3:5,12,21; 21:7)

Mambo ya wokovu ndani ya biblia hutoka katika pendo, huruma, na neema ya mamlaka ya Mungu wa Utatu. Hakuna mwanadamu awezaye kuokolewa pasipo kuingiliwa na Roho (kama vile Yohana 6:44,65). Mungu alikuja na kupangilia mambo muhimu, lakini alidai kwamba wanadamu wanapaswa kuitikia katika imani na toba, katika namna zote kwa uanzilishi na kwa uendelevu. Mungu hutenda kazi na wanadamu katika uhusiano wa agano. Kuna upendeleo na majukumu!

Wokovu umetolewa kwa wanadamu wote. Kifo cha Yesu kilihusika na tatizo la dhambi ya uumbaji ulioanguka! Mungu ameleta njia na anahitaji wale wote walioumbwa kwa mfano Wake kuliitikia pendo Lake na utoaji katika Yesu. Kama ungependa kusoma zaidi juu ya somo hili tazama

1. Dale Moody, *The Word of Truth*, Eerdmans, 1981 (kur. 348-365)
2. Howard Marshall, *Kept by the Power of God*, Bethany Fellowship, 1969
3. Robert Shank, *Life in the Son*, Westcott, 1961

Biblia inashughulikia matatizo mawili tofauti katika eneo hili: (1) kuchukulia imani kama msimamo wa kuishi bila kuzaa matunda, maisha ya ubinafsi au (2) kuwatia moyo wale wanaopambana na huduma na dhambi binafsi. Tatizo ni kwamba makundi yasiyo sahihi yana uchukuwa ujumbe usio sahihi na kutengeneza mifumo ya kitheolojia yenye vifungu vya kibiblia vyenye kuwekewa mipaka. Baadhi ya Wakristo wakiwa katika hali ya kukata tamaa wanahitaji ujumbe wa kuwatia moyo, wakati wengine wanahitaji kuonywa kwa ukali kuhusiana na uvumilivu! Wewe uko ndani ya kundi lipi?

Kuna mabishano ya historia ya kitheolojia iliyomuhusisha Augustine dhidi ya Pelagius na Calvin dhidi ya Arminius (semi-Pelagian). Jambo hili lilihusisha swali la wokovu : kama mtu akiokolewa kiukweli, yampasa kustahimili katika imani na uamiifu?

Wafuasi wa Calvin wamesimama nyuma ya maandiko yale ya kibiblia ambayo yanadai kwamba mamlaka ya Mungu na nguvu idumuyo (Yohana 10:27-30; Rum. 8:31-39; 1 Yohana 5:13,18; 1 Pet. 1:3-5) na vitenzi vya nyakati kama kauli tendewa timilifu endelevu ya Efe. 2:5,8.

Wafuasi wa Arminius wamesimamia maandiko yale ya kibiblia ambayo yanamuonya yule aaminiye "kusimama imara," "kudumu," au "kuendelea" (Mt. 10:22; 24:9-13; Marko 13:13; Yohana 15:4-6; 1 Kor. 15:2; Gal. 6:9; Ufu. 2:7,11,17,26; 3:5,12,21; 21:7). Mimi binafsi siamini kwamba Waebrania 6 na 10 zinatumiwa, lakini wafuasi wengi wa Arminius wanazitumia kama onyo dhidi ya uasi. Mfano wa Mpanzi katika Mathayo 13 na Marko 4 inashughulikia suala la imani, kama inavyofanya Yohana 8:31-59. Kama wafuasi wa Calvin wanavyo nukuu vitenzi vya kauli ya wakati uliopo timilifu vilivyotumiwa kueleza wokovu, Wafuasi wa Arminius wana nukuu vifungu vya kauli ya wakati uliopo kama 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15.

- Huu ni mfano kamili wa namna mfumo wa kitheolijia unayotumiwa vibaya njia ya uhakiki wa fasiri za maandiko. Mara nyingi kanuni inayoongoza au andiko kuu linatumika kutengeneza ufito wa kitheolojia ambapo maandiko mengine yote yanatazamiwa. Kuwa makini na mfumo kutoka vyanzo vyo vyote vile. Vitokana na ufafanuzi wa mantiki ya mashariki, si ufunuo. Biblia ni kitabu cha mashariki. Inawakilisha kweli katika mvutano uliokamilishwa, ulinganifu wa mafumbo yaonekanayo. Wakristo wanamaanisha kukubaliana na yote na kuishi ndani ya mvutano huo. Agano Jipya linawasilisha vyote yaani ulinzi wa mwaamini na dai la imani endelevu na uovu. Ukristo ni mwitikio wa mwanzo wa toba na imani inayofatiwa na mwitikio endelevu wa toba na imani. Wokovu si kama matokeo (tiketia ya kwenda mbinguni au sera ya bima ya moto), bali uhusiano. Ni maamuzi na uwanafunzi. Inaelezwa katika Agano Jipya 3:5
- utimilifu (tendo lililokamilishwa na matokeo endelevu), Efe. 2:5,8
- inawasilisha (tendo endelevu), 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15
- wakati ujao (matukio yajayo au matukio fulani), Rum. 5:8,10; 10:9; 1 Kor. 3:15; Flp. 1:28; 1 The. 5:8-9; Ebr. 1:14; 9:28

katika vitenzi vyote vya nyakati:

- kauli (tendo timilifu), Matendo 15:11; Rum. 8:24; 2 Tim. 1:9; Tito

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 10:23**

<sup>23</sup> Lakini watakapowafukuza katika mji huu, kimbilieni mwingine; kwa maana ni kweli nawaambia, Hamtamiliza miji ya Israeli, hata ajapo Mwana wa Adamu.

**10:23 "lakini watakapowatesa"** Hii inakosekana katika Luka lakini ana ufanano katika Marko 9:1. Angalia dokezo na Mada maalum katika Mt. 10:22.

☐ **"kimbilieni mji mwingine"** Waamini lazima waepuke mgogoro na migongano pale inapobidi. Uinjilisti lazima iwe lengo lisilokoma!

☐ **"Hakika"** Angalia Mada Maaalum katika Mt. 5:18.

☐ **"hamtamaliza miji hii ya Israeli kabla ya Mwana wa Adamu hajaja"** Hii yawezekana mwanzoni ikieleweka kama

1. Yesu atajiunga na Kumi na Mbili baada ya safari yao
2. Yesu alielezea mamlaka Yake katika Yerusalemu
3. uanzishwaji wa kanisa (yaani, Pentekoste)
4. Yesu alitimiliza ahadi Yake kwao (yaani tukio la chumba cha juu la Yohana 20:19-23)
5. hukumu juu ya Yerusalemu mnamo mwaka 70 B.K (NASB Study Bible, ukur. 1382)
6. Kuja kwa mara ya Pili kwa Yesu katika nguvu kama Hakimu (yaani, Dan. 7:13-14), kukianzisha ufalme wa milele.

Angalia Mada Maalum: Muda wowote wa Kurudi kwa Yesu dhidi ya Bado (mkanganyiko wa Agano Jipya) katika Mt. 24:27.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 10:24-25**

<sup>24</sup> Mwanafunzi hampiti mwalimu wake, wala mtumwa hampiti bwana wake. <sup>25</sup> Yamtosha mwanafunzi kuwa kama mwalimu wake, na mtumwa kuwa kama bwana wake. Ikiwa wamemwita mwenye nyumba Beelzebuli, je! Si zaidi wale walio wa nyumbani mwake?

**10:25 "ikiwa"** Hii ni daraja la kwanza lenye masharti ambalo linadhaniwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi.

☐ **"Beelzebuli"** Hili lilikuwa neno ambatani kutoka *Ba'al* na *Zebub*. Hili lilikuwa likijulikana kinyumbani *Ba'al* Ekroni (kama vile 2 Wafalme. 1:16). Wayahudi walibadili majina ya watawala wa kipagani na miungu ya kipagani kwa kubadilisha irabu, kuwadhihaki. Neno linaweza kufasiriwa kama "Bwana wa nyumba," "Bwana wa wadudu," au "Bwana wa mavi ya ng'ombe."

Neno la pili mara kwa mara lilitajwa *Zebul*, pepo kuu la desturi za kijadi (kama vile Mt. 12:24; Luka 11:15). Hii inaelezea kwanini matoleo ya NASB na NRSV yana *Beelzebul*, wakati toleo la NKJV na NIV yana *Beelzebub*.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 10:26-27**

<sup>26</sup> Basi, msiwaogope, kwa maana hakuna neno lililositirika, ambalo halitafunuliwa; wala lililofichwa, ambalo halitajulikana. <sup>27</sup> Niwaambialo ninyi katika giza, lisemeni katika nuru; na msikialo kwa siri, lihubirini juu ya nyumba.

**10:26 "msiwaogope"** Hii ni kauli tendwa tegemezi kanushi ya wakati uliopita usio timilifu (wenye ushahidi) kama Mt. 10:19 ikifanya kazi kama kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita kama Mt. 10:28 na 31. Hii tungo ikimaanisha "hata ushithubutu kuanza." Mstari huu unaweka wazi kwamba msukumo na makusudi ya miyo ya wanadamu vyote hasi na chanya itajulikana Siku ya hukumu.

Ni ngumu kuhusianisha ukweli wa mstari huu pamoja na ahadi za kibiblia kwamba wakati Mungu akisamehe, husahau (kama vile Zab. 103:11-14; Isa. 1:18; 38:17; 43:25; 44:22; Mika 7:19). Yawezekana ikiwa bila kukiri (waamini, kama vile 1 Yohana 1:7-9) au dhambi au kutosamehewa (wasioamini) dhambi inarejerewa. Hivyo nafurahia katika "usahaulifu wa Mungu"! Damu ya Yesu inatakasa dhambi zote (kama vile Waebrania 9)!

Waamini hawataiki kuwahofu wanadamu bali kumuheshimu Mungu (kama vile Mt. 10:28; Ebr. 10:31). Kwa ujumla nafikiria mstari huu unarejerea msukumo ana matendo ya

1. nyumba isiyostahili, Mt. 10:13
2. mbwa mwitu, Mt. 10:16
3. watu waovu, Mt. 10:17
4. watawala na wafalme, Mt. 10:18
5. ndugu, Mt. 10:21
6. mtoto, Mt. 10:21
7. "wao" wa Mt. 10:23
8. "wao" wa Mt. 10:26
9. "wale" wa Mt. 10:28

**10:27 "paa za nyumba"** Paa za nyumba imezoeleka katika palestina kuwa sehemu za shughuli za kijamii; hivyo kile kilichozungumzwa kingekuwa kujulikana mbele ya watu. Yesu alitaka ujumbe wake ujulikane na wanadamu wote!

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 10: 28-31**

<sup>28</sup> Msiwaogope wauuao mwili, wasiweze kuiua na roho; afadhali mwogopeni yule awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika jehanim. <sup>29</sup> Je! Mashomoro wawili hawauzwi kwa senti moja? Wala hata mmoja haanguki chini asipojua Baba yenu; <sup>30</sup> lakini ninyi, hata nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa zote. <sup>31</sup> Msiogope basi; bora ninyi kuliko mashomoro wengi.

**10:28 "msiogope"** Angalia dokezo katika Mt. 10:26.

☐ **"kuharibu"** Angalia Mada Maalum: *Apollumi* katika Mt. 2:13.

☐ **"nafsi na mwili"** Mstari huu haurejerei ulinganifu mkali kati ya mwili, nafsi na roho lakini ni uelezo wa uwezekano wa kifo cha kimwili na si kifo cha milele cha waaminio.

#### **MADA MAALUM: MWILI NA ROHO**

Mwili na roho si maisha maradufu katika mwanadamu, bali uwili wa uhusiano huu kwa pande zote yaani hyu mzazi na Mungu. Neno la Kiebrania *nepshesh* (BDB 659, yaani., tazama maelezo katika Mwa. 35:18 mtandaoni) linatumika katika pande zote yaani mwanadamu (kama vile Mwa. 2:7) na wanyama (kama vile Mwa. 1:20,24,30; 9:12,15,16) katika Mwanzo, ambapo "roho" (*ruah*) linatumika kwa upekee kwa mwanadamu. Huku si kuyachunguza maandiko katika asili ya mwanadamu kama pande mbili (uwili, kama vile 1 Kor. 7:34; Ebr. 4:12) au kuwa pande tatu (mwenye pande tatu) (kama vile 1 The. 5:23). Mwanadamu anawasilishwa kwanza katika Biblia kama umoja (kama vile Mwa. 2:7; 2 Kor. 7:1). Kwa muhtasari zuri uhusuo nadharia za



mwanadamu kama mwenye pande tatu, au umoja, tazama Millard J. Erickson's *Christian Theology* (toleo la pili), kr. 538-557 na Frank Stagg's *Polarities of Man's Existence in Biblical Perspective*.

☛ **"kuzimu"** Hili ni neno la Kiebrania "*Gehenna*." Lilikuwa ni ambatani la "bonde" na "(wana wa) Hinnom." Hili lilikuwa ni bonde nje ya Yerusalemu ambapo mungu wa wakaanani wa moto na ustawi (kama vile Law. 18:21) alikuwa akiabudiwa kwa dhabihu za watoto (akiitwa *molech*). Wayahudi waliligeuza katika shimo la taka kwa ajili ya Yerusalemu. Stiari ya Yesu ya adhabu ya milele ilichukuliwa kutoka katika shimo liwakalo, lililojaa minyoo na linalonuka. Angalia Mada Maalum: Wafu wako wapi? Katika Mt. 5:22.

**10:29-30 "ndege. . .nywele"** Mungu anajali na kujua kila sehemu ya maisha ya waaminio (kama vile Luka 12:6; 21:18; 1 Pet. 5:7). Hii ni ahadi ya mtu mmoja mmoja (si ja kujumla) na kujali.

☛ **"senti"** Hii kibayana "*assarion*," ambayo ilikuwa ni sarafu ya shaba ya kirumi. *Assarion* moja ingeweza kununua njiwa kadhaa.

**10:31 "hivyo msihofu"** Angalia dokezo katika Mt. 10:19 na 26.

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 10:32-33

<sup>32</sup> Basi, kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni. <sup>33</sup> Bali mtu ye yote atakayenikana mbele ya watu, nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni.

**10:32 "atakenikiri mbele ya watu"** Hii ilimaanisha "kukiri kumtambua hadharani" (kama vile Marko 8:38; Luka 12:8-9). Mistari ya 32 na 33 ni kauli zinazofanana katika kupingana. Ukristo ni agano lililotolewa na Mungu ambalo lazima lipokelewe kwa mtu mmoja mmoja binafsi na mbele ya watu na kutunzwa.

#### MADA MAALUMU: KUTUBU (AGANO JIPYA)

Toba (sambamba na imani) ni hitaji la pande zote mbili yaani Agano la Kale (Nacham, BDB 636, KB 688, mf., Kut. 13:17; 32:12,14; Shuv, BDB 996, KB 1427, m.f. 1 Flm. 8:47; Eze. 14:6; 18:30; tazama [Mada Maalum: Toba](#) [Agano la Kale]) na Agano Jipya.

1. Yohana Mbatizaji (Mt. 3:2; Marko 1:4; Luka 3:3,8)
2. Yesu (Mt. 4:17; Marko 1:15; Luka 5:32; 13:3,5; 15:7; 17:3)
3. Petro (Matendo 2:38; 3:19; 8:22; 11:18; 2 Petro. 3:9)
4. Paulo (Matendo 13:24; 17:30; 20:21; 26:20; Rum. 2:4; 2 Kor. 2:9-10)

Lakini Toba ni nini? Ni huzuni ya kiroho? Ni kumaanisha kuacha dhambi? Eneo zuri katika Agano la Jipya katika kuelewa maana tofauti ya dhana hii ni 2 Wakorintho 7:8-11, ambapo hizo tatu zinahusiana, lakini ni tofauti, maneno ya Kiyunani yanatumiika.

1. "huzuni" (*lupeō*, kama vile. mst. 8 [mara mbili], 9 [mara tatu], 10 [mara mbili], 11). Inamaanisha kupata maumivu au kutambua na ina maana ya kithiolojia isiyofungamana na upande wo wote.
2. "toba" (*metanoēō*, kama vile mst. 9,10). Ni muunganiko wa neno "baada ya" na "kumbukumbu," ambayo inadokeza akili mpya, njia mpya ya kufikiri, mtazamo mpya kuhusu maisha na Mungu. Hii ni toba ya kweli.
3. "majuto" (*metamelomai*, kama vile mst. 8 [mara mbili], 10). Ni muungano wa "baada ya" na "uangalifu." Linatumika juu ya Yuda katika Mt. 27:3 na Esau katika Ebr. 12:16-17. Linadokeza sikitiko juu ya matokeo, si juu ya matendo. Toba na imani ni matendo ya kimaagano yanayohitajika (kama vile Marko 1:15; Matendo 2:38,41; 3:16,19; 20:21). Kuna baadhi ya maandiko ambayo yanadokeza kwamba

Mungu hutoa toba (kama vile Matendo 5:31; 11:18; 2 Tim. 2:25). Lakini maandiko mengi yanalitazama hili kama mwitikio muhimu wa agano la mwanadamu kwa majitoleo ya Mungu ya wokovu huru. Maelezo ya maneno yote ya Kiebrania na Kiyunani yanahitajika ili kuelewa maana kamili ya toba. Neno la Kiebrania linadai "mabadiliko ya tendo," ambapo neno la Kiyunani linadai "mabadiliko ya akili." Mtu aliyeokolewa anapokea akili na moyo mpya (kama vile Eze. 36:26-27). Anafikiri tofauti na kuishi tofauti. Badala ya "Kilicho ndani ni kwa ajili yangu?" sasa swali ni "Mapenzi ya Mungu ni nini?" Toba si hisia ambazo hufifia au dhambi ya moja kwa moja, bali uhusiano mpya na Aliye Mtakatifu ambaye humbadilisha mwamini kwa uendelevu na kuwa ndni ya utakatifu. Si rahisi mtu akasitisha kufanya kitu au kuachana nacho, bali ni kwa mtazamo na uelekeo mpya katika maisha. Anguko linatusabisha sisi kujitazama wenyewe lakini injili inaturuhusu sisi kumtazama Mungu. Toba ni tendo la kugeuka na imani ni tendo la kugeukia kitu/kifikra!

☐ **"Baba yangu aliye mbinguni"** Kuna viwakilishi kadhaa tofauti tofauti vilivyotumika pamoja na Baba.

1. yenu - Mt. 5:16,45; 6:1; 7:11
2. yetu- Mt. 6:9
3. Yangu - Mt. 7:21; 10:32,33; 12:50

Nafikiria 12:50 ni muhimu, yeye ayatendaye mapenzi ya Baba, kama Yesu alivyofanya ni sehemu ya familia. Yeye akataaye si sehemu ya familia. Lazima ilikuwa inakera hasa kwa viongozi wa kiyahudi wa siku za Yesu kumsikia mwalimu asiye rasmi na mtu wa Galilaya kutumia "Baba" kurejerea YHWH, Aliye Mtakatifu wa Israeli. Hata zaidi kuruhusu mtu wan je kujumuishwa katika familia ya Mungu!

**10:33** Kinyume cha "kukiri" (*homologeō*, kama vile Mt. 10:32 [mara mbili]) ni "kukataa" (*arneomai*, kama vile Mt. 10:33 [mara mbili]; Mt. 26:70,72 [*aparneomai* katika Mt. 26:35,75]). Angalia [MADA MAALUM: UKIRI](#) katika Mt. 10:32 juu. Huu ni mstari wa kushangaza, kama ilivyo katika 2 Tim. 2:12. Lazima ikumbukwe kwamba ukiri wa hadharani kwa maneno (kama vile Rum. 10:9-13) na katika matendo (kama vile Mt. 13:1-23; 25:36-46) ni muhimu. Maamuzi yanayotengenezwa sasa yanahusiana na umilele (kama vile Mt. 25:46)

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 10:34-36**

<sup>34</sup> Msidhani ya kuwa nimekuja kuleta amani duniani; la! Sikuja kuleta amani, bali upanga. <sup>35</sup> Kwa maana nalikuja kumfitini mtu na babaye, na binti na mamaye, na mkwe na mkwe mtu; <sup>36</sup> na adui za mtu ni wale wa nyumbani mwake.

**10:34 "Msifikiri"** Kulingana na *Analytical Greek New Testament* by Barbara na Timothy Friberg, hiki ni kitenzi tendaji tegemezi cha wakati uliopita usio timilifu kinachofanya kazi kama kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu.

Yesu yawezekana alikuwa akizungumza maneno haya dhidi ya matakwa yasiyotimia juu ya Masihi aliyekuwa akiitwa "Mfalme wa Amani" (kama vile Isaya. 9:6). Wayahudi walitegemea Masihi kuleta usaidizi wa kijeshi na utaratibu wa kitaifa kwa niaba ya Wayahudi (kama vile Luka 12:49-53).

☐ **"amani"** Asili hii ya neno ilikuwa "kuleta pamoja kile kilichovunjika" (kama vile Yohana. 14:24).

☐ **"sikuja kuleta amani bali upanga"** Yesu hakuja kuleta vita au migongano bali ukweli kwamba amekuja kwa nguvu kutengeneza maamuzi ya kimsingi "ufuasi" au kukataliwa (kama vile Yohana. 3:17; Luka 12:51-53).

**10:35 "kwa kuwa nalikuja kumfitinisha mtu na babaye"** Angalia Mt. 10:21. Ufanano katika Luka 14:26 una nahau ya kiebrania, "kumchukia baba," ambayo ilikuwa ulinganifu wa kinahau. Lazima tutambue hii ni nahau ya

Kiebrania badala ya kuitafsiri kibayana (kama vile Mwa. 29:31, 33; Kumbu kumbu la Torati. 15; Mal. 1:2-3; Yohana. 12:25). Hii inazungumzia ukipaumbele wa kujizatiti wa Yesu ambayo unapita ushirikiano wote wa kiulimwengu.

**10:35-36** Hii ni nukuu kutoka Mika 7:6. Kifungu hiki mara kwa mara kilinukuliwa katika mazingira ya matukio ya siku za mwisho (kama vile Marko 13:12 na Luka 12:53).

**10:36** "adui wa mtu ni watu wa nyumbani mwake mwenyewe" Mfano mzuri wa aina hii ya shinikizo inayojulikana inaweza kuonekana katika mwitikio wa Petro kwa madai ya ayaesu kwa U-Masihi (kama vile Mt. 16:22).

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 10: 37-39**

<sup>37</sup> Apendaye baba au mama kuliko mimi, hanistahili; wala appendaye mwana au binti kuliko mimi, hanistahili.

<sup>38</sup> Wala mtu asiyechukua msalaba wake akanifuata, hanistahili. <sup>39</sup> Mwenye kuiona nafsi yake ataipoteza; naye mwenye kuipoteza nafsi yake kwa ajili yangu ataiona.

**10:37** "Yeye appendaye. . .zaidi Yangu" Huu ni msingi wa kipaumbele kisichobadilika katika kujizatiti. Kufanyika wanafunzi, tofauti na maamuzi, ni kujitoa kimaisha kwa muda mrefu kwa ufuasi na utii!

☐ "hanifai" Angalia Luka 9:62.

**10:38** "aubebe msalaba wake na anifuata" Huku ni kujizatiti kwa kisitiari za jumla kwa maisha ya Kristo. Yesu anataka kwamba wafuasi wahesabu gharama (kama vile Luka 14:25- 35).

Msalaba ulikuwa mbinu ya Wafoenike ya utekelezaji wa adhabu ambayo ilicukuliwa na Warumi na kukuzwa katika jambo lisilofaa ikihusisha siku kadhaa za kupitia maumivu kabla ya kufa. Kusudi lake lilikuwa kuwakatisha tama watu wasio warumi kutofanya shughuli za kihalifu. Kulikuwa na historia ya matumizi yake hapo kabla katika Palestina:

1. Antiochus IV "Epiphanes" aliwasulubisha Mafarisayo mia nane
2. Varus, kamanda wa Kirumi, alizimisha mgomo na kusulubisha Wayahudi elfu mbili pembezoni mwa njia kuu ya Palestina (kama vile Josephus, *Antiquities of the Jews* 17:10:10)
3. Herode alipanga kusulubisha Mafarisayo wengi wakati wa kifo chake ili kwamba watu waomboleze. Stiaari hii hairejerea aina Fulani ya tatizo katika maisha yako. Inarejerea hali ya ubinafsi (kama vile 2 Kor. 5:14-15; Gal. 2:20; 1 Yohana. 3:16).

**10:39** "uhai. . .uhai" Hili lilikuwa ni neno la Kiyunani *psuche*. Neno hili mara kwa mara lilikuwa ni kisawe pamoja na "roho" [*pneuma*]. Katika muktadha huu hata hivyo inaonekana kurejerea nafsi ya mtu mmoja mmoja au nafsi. Kauli hii ilihusisha usulubishwaji usio na huruma kwa ajili ya ajenda binafsi katika ufahamu wa matakwa ya Yesu (kama vile Mt. 10:39; 16:25; Marko 8:35; Luka 9:24; 17:33; Yohana. 12:25). Wokovu unajumuisha zaidi kuliko maamuzi au maombi. Inadai yote (umiliki wa mali, familia, heshima, muda, na nguvu)! Hakuna kingine zaidi!

☐ "kupoteza" Angalia Mada Maalum: *Apollumi* katika Mt. 2:13.

**ANDIKOLA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 10:40-42**

<sup>40</sup> Awapokeaye ninyi, anipokea mimi; naye anipokeaye mimi, ampokea yeye aliyenituma. <sup>41</sup> Ampokeaye nabii kwa kuwa ni nabii, atapata thawabu ya nabii; naye ampokeaye mwenye haki kwa kuwa ni mwenye haki, atapata thawabu ya mwenye haki. <sup>42</sup> Na mtu awaye yote atakayemnyweshwa mmojawapo wa wadogo hawa

ngaa kikombe cha maji ya baridi, kwa kuwa ni mwanafunzi, amin, nawaambia, haitampotea kamwe thawabu yake.

**10:40,41 "Yoyote awapokeaye ninyi anipokea mimi. . nabii. . mwenye haki"** Mukhadha unaonekana kumaanisha kwamba Yesu anarejerea kibinafsi kwa maneno haya matatu. Neno "nabii" inaelezea katika Kumb. 18:15 na 18. Neno "mwenye haki" ikiwa sawa na "Mwenye Haki" wa Mdo. 7:52 na yawezekana tungo katika magombo ya bahari ya chumvi "mwalimu wa haki." Yesu pamoja na ujumbe wake usioadilika mpya ulikuwa umeelekezwa kwa wale ambao wangeweza kumwamini na Maneno yake. Mtu lazima kwanza atubu na Kumpokea kama mwokozi wao na tumaini. Kwa kufanya hivyo walikuwa wanajitambulisha pamoja na ufalme mpya wa kiroho wa Mungu. Wanafunzi waliwakilisha Yesu mwenyewe na ujumbe wake hivyo yeyote awapokeaye na ujumbe wao, anampokea Yesu na kumpokea Yesu ni kumpokea Baba (kama vile Yohana 8:19; 16:3; 17:3; 1 Yohana 2:23; 4:15; 5:1,10-12; 2 Yohana 9). Mtu hawezi kujua au kuwa na ushirika na Baba mpaka kupitia Mwana (kama vile Yohana 14:6-7,8-11).

☐"kutumwa" Angalia Mada Maalum hapa chini.

### **MADA MAALUMU: KUPELEKWA (*apostellō*)**

Hili ni neno la kiyunanila kawaida kwa "upelekwa" (yaani *apostellō*). Neno hili lina matumizi kadha ya kithiolojia:

1. Katika kiyunani cha sasa na kwa Wayahudi waliokuwa na elimu na viongozi wa dini, neno hili hutumiwa kama moja inayoitwa na kutumwa kama mwakilishi rasmi wa mwingine, kitu kama kiingereza chetu "Balozi". (kama vile. 2 Kor. 5:20).
2. Injili daima zinatumia kitenzi hiki kwa Yesu kutumwa na baba yake, katika Yohana, linasikika zaidi kama Masihi (kama vile Mt. 10:40; 15:24; Marko 9:37; Luka 9:48 na hasa Yohana 5:36, 38; 6:29, 57; 7:26; 8:42; 10:36; 11:42; 17:3, 8, 18, 21,23 25; 20:21 (Yote "*apostellō*" na KISAWA CHAKE *pempō* inayotumika katika mst. 21). Inatumika kwa Yesu kutuma waumini (kama vile. Yn 17:18; 20:21,21 [Yote "*apostellō*" na KISAWA CHAKE ni "*pempō*" katika Yohana 20:21]).
3. Agano Jipya lilituma jina "Mtume" kwa wanafunzi
  - a. Mitume kumi na wawili wa mwanzo kama mzunguko wa kwanza kati ya wanafunzi wake. (Marko 6:30; Luka 6:13; Matendo 1:2; 26)
  - b. Kundi maalumu la msaada la Mitume na watumishi wenzie.
    - 1) Barnabasi (kama vile. Matendo 14:4, 14)
    - 2) Andronicus na Junias (KJV, Junia , kama vile. Rum. 16:7)
    - 3) Appollo (kama vile. 1 Kor. 4:6-9)
    - 4) Yakobondugu wa Bwana (kama vile. Gal. 1:19)
    - 5) Silvanus na Timotheo (kama vile. 1The. 2:6)
    - 6) Bila shaka Tito (kama vile. 2 Kor. 8:23)
    - 7) Bila shaka Epafrodito (kama vile. Waf. 2:25)
  - c. Zawadi inayoendelea katika kanisa (kama vile. 1 Kor. 12:28-29; Efe 4:11)
4. Paulo anatumia cheo hiki kwa ajili yake katika barua zake nyingi kama njia ya kuonesha mamlaka yake aliyopewa na Mungu kama mwakilishi wa Kristo. (kama vile. Rum. 1:1 1 Kor. 1:1; Gal. 1:1; Efe. 1:1; Kol. 1:1; Tim. 1:1 2Tim. 1:1; Tito 1:1).
5. Tatizo tunalokumbana nalo kama waamini wa leo ni kwamba Agano Jipya halitafasiri hii zawadi inayoendelea inahusu nini au vipi inabainishwa kwa waamini. Bila shaka mtu apaswa kutofautisha kati kumi nambaili ya awali (# 3b) na matumizi ya baadaye (# 3b). Tazama Mada Maalum: Msukumo na Mada Maalum: Mwangaza. Kama mitume wa leo hawakusukumwa kuandika maandiko mengi matakatifu (yaani, kitabu cha Wayunani kanoni kimefungwa, kama vile. Yuda mst.

3; tazama. Mada Maalumu: kanuni ya kanisa) kisha kipi wanafanya tofauti na Manabii wa Agano Jipya na Wainjilisti (kama vile. Efe. 4:11) hapa kuna uwezekano wa mambo.

- a. Waanzilishi wa kanisa la wamisionari huanza katika maeneo yasiyo ya uinjilisti (kutumika kama vile katika *Doache*)
- b. Viongozi wa Wachungaji katika eneo Fulani au madhehebu.
- c. ?

Napenda # 1.

**10:42 "awapaye mmoja wa wadogo hawa"** Msaada wa upendo utolewao na Mkristo mmoja unatakiwa utolewe na mwingine kwasababu vyote vinahusiana na Yesu Kristo. "wadogo hawa" sio watoto bali waamini wapya (kama vile Mt. 18:6).

☐ "**Hakika**" Angalia Mada Maalum katika Mt. 5:18.

☐ "**thawabu**" Biblia imejaa na kauli juu ya thawabu za Mkristo. Thawabu hizi zimejikita katika shughuli za Roho kwa waamini na kujitolea kwao kwa shughuli. Hata hivyo katika ujazo wa neema wa Mungu, waamini watapata thawabu kwa kuzaa kwao kwa namna ya Kristo na kazi mahususi za Roho Mtakatifu zitendazo kazi ndani yao kupitia kukirimiwa vipawa vyao kiroho! Angalia Mada Maalum katika Mt. 5:12.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini Yesu anajiwekea mpaka yeye mwenyewe zaidi kwa Wayahudi? Unaweza ukaorodhesha upekee?
2. Kwanini Mathayo, Marko na Luka zinatofautiana hadithi za Yesu za maisha?
3. Je hivi ni viwango vya thawabu na adhabu? Vinajikita katika nini?
4. Nini mstari wa 23 unachomaanisha?
5. Kwanini ukiri wa hadhara ya imani katika Yesu ni muhimu sana?
6. Kwanini Yesu anasababisha mkanganyiko wa namna hii?
7. Je ina maanisha nini kuchukua msalaba wako mwenyewe na kumfuata?

## MATHAYO 11

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Wajumbe wa Yohana Mbatizaji (10:40-11:1)	Yohana Mbatizaji Anatuma wajumbe  11:1-19	Hadithi inafafanua Mamlaka yanayodaiwa Na Yesu (11:2-15:50)	Wajumbe kutoka kwa Yohana Mbatizaji  11:1	11:1 Swali la Mbatizaji: Yesu anamwamuru 11:2-6
11:2-15		11:2-6  11:7-15	11:2-3 11:4-6 11:7-15	11:2-6  11:7-10 (10b) 11:11-15 Yesu analalamikia Alionao
11:16-19		11:16-19	11:16-19	11:16-19 (17)
Ole wa miji Isiyotubu 11:20-24	Ole wa miji Isiyoona aibu 11:20-24	11:20-24	Miji Isiyoamini  11:20-24	Maombolezo juu ya Miji ya ziwani 11:20 11:21-24
Njoni kwangu Mpumzike  11:25-30	Yesu anatoa Pumziko la Kweli  11:25-30	11:25-27  11:28-30	Njoo kwangu na Upumzike  11:25-26 11:27 11:28-30	Habari Njema Inafunuliwa kwa Kwa wanyonge. Baba na Mwana 11:25-27 Utawala wa upole Wa Kristo 11:28-30

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia"](#))**

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembele katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## HISTORIA YA NYUMA YA MATHAYO 11:1-30

- A. Sura hii mara kwa mara imekuwa ikielezwa kama hadithi zisizofanana lakini kinachofanya ziwe na ufanano ni jibu kwa swali, "Kwanini huduma ya Yesu haikufanikiwa zaidi kwa nje?"
- B. Yohana Mbatizaji ni muhusika mkuu katika sura hii (kama vile Yohana 1:6-8, 19-36). Alikuwa nabii wa mwisho wa Agano la Kale (kama vile Mt. 11:9).
- C. Isaya anaorodhesha matendo kadhaa ambayo Wayahudi waliweza kumtambua Masihi ambaye mtangulizi wake alikuwa Yohana Mbatizaji (yaani Isaya 40:3; Marko ulinganifu mkali. 3:1; 4:5b). Haya ndiyo matendo pekee ya Yesu yaliyoandikwa katika Mathayo 8 na 9.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 11:1

<sup>1</sup> Ikawa Yesu alipokwisha kuwaagiza wanafunzi wake kumi na wawili, alitoka huko kwenda kufundisha na kuhubiri katika miji yao.

**11:1 "Yesu alipokwisha kuwaagiza"** Hii ilikuwa ni tungo ambayo Mathayo alitumia kuainisha kitabu chake. Ilitokea mwishoni mwa vipengele vitano vya kifasihi vya Mathayo (kama vile Mt. 7:28; 11:1; 13:53; 19:1; 26:1).

☐ **"huko kwenda kufundisha na kuhubiri katika miji yao"** Hii ni misheni kuu ya Yesu kuzungumzia Injili na sio kuponya (kama vile Mt. 4:23; 9:35). Kuponya kulikusudiwa kuthibitisha injili, sio kufanyika shabaha ya huduma yake. Kuponya ilikuwa ni njia (1) kuonyesha upendo wa Mungu; (2) kuonyesha nguvu ya Yesu; na (3) kutimiliza unabii wa Agano la Kale juu ya Masihi (kama vile Mt. 11:5).

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 11:2-6

<sup>2</sup> Naye Yohana aliposikia huko gerezeni matendo yake Kristo, alituma wanafunzi wake, kumwuliza, <sup>3</sup> Wewe ndiwe yule ajaye, au tumtazamie mwingine? <sup>4</sup> Yesu akajibu akawaambia, Nendeni mkamweleze Yohana mnayoyasikia na kuyaona; <sup>5</sup> vipofu wanapata kuona, viwete wanakwenda, wenye ukoma wanatakaswa, viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa, na maskini wanahubiriwa habari njema. <sup>6</sup> Naye heri awaye yote asiyechukizwa nami.

**11:2 "Naye Yohana huko gerezeni"** Yohana Mbatizaji alifungwa huko Machaerus (Josephus, *Antiquities of the Jews*. 18.5.2), moja ya ngome za Herode Antipa. Iko upande wa mashariki mwa Bahari ya Chumvi. Herode alikuwa amemfunga Yohana kwa kuhubiri kinyume na ndoa yake kwa mke wa zamani wa Herode Philipo aitwaye Herodia. Antipa alipita kuomboleza na kumfariji wakati wa kifo cha Phillip wakati wa safari yake kutokea Rumi (kama vile Josephus' *Antiq.* 18:5:2).

☐ **"Kristo"** Neno "Kristo" ni sawasawa na neno la Agano la Kale *Messiah* ambalo lilimaanisha "Mpakwa Mafuta." Lilitumika katika namna maalum ya Mungu ya wito na kuwezesha. Katika Agano la Kale, manabii, makuhani na wafalme walipakwa mafuta. Yesu alitimiliza kazi zote tatu za kupakwa mafuta (kama vile Ebr. 1:1-3). Mfalme Koreshi wa Ufame wa Uajemi, ambaye hakuwa mwamini, hata yeye alikuwa Mpakwa mafuta wa Bwana (kama vile Isaya. 44:28; 45:1).

**11:3 "Je wewe ndiye au tutarajie Mwingine"** Hiki kilikuwa ni cheo cha kimasih (kama vile Zab. 118:26; kilieleza mara kwa mara, Mt. 21:9; 23:39; Marko 11:9; Luka 13:35; 19:38; Yohana 6:14; 11:27; 12:13; na Ebr. 10:37).

Angalia Mada Maalum katika Mt. 8:20. Katika Luka 1:15 Yohana alikuwa amejazwa na Roho lakini bado alikuwa na mashaka. Nadharia kadhaa zinaelezea mashaka ya Yohana.

1. Yohana alikuwa amekata tama kwa sababu alikuwa gerezani
2. John Calvin anasema kwamba hii ilikuwa ni njia yake ya kurejerea wanafunzi wake kwa Yesu
3. Yesu alikuwa hatendi katika namna iliyokuwa inategemewa (kama vile Mt. 3:7-12) "Mtu mwingine" ni neno la Kiyunani *heteros* lililomaanisha, katika Kiyunani cha wakati ule, "mwingine wa namna tofauti." Yohana alitegemea ujumbe wa hukumu kutoka kwa Masihi badala yake Yesu alitoa wokovu kwa wote.

**11:4-5 "Yesu akawajibu akawaambia"** Mstari wa 5 ni nukuu kutoka Isaya. Inajadiliwa ikiwa ilitoka 26:19; 29:18,19; 35:5-6; au 61:1. Inasisitiza huduma ya Masihi kama huduma ya huruma na uponyaji kwa masikini na watu wa nje.

**11:5 "Injili"** Muundo wa nomino (*euangelion*, zaidi ya mara 60 katika maandiko ya Paulo) inapatikana katika Mt. 4:23; 9:35; 24:14; na 26:13. Muundo wa kitenzi (*euangelizumai*) inapatikana hapa katika Mathayo (sio katika Yohana). Neno hili linaelezea maudhui ya ujumbe wa Yesu, "habari njema." Inajumuisha "habari mbaya" ya dhambi na kutengwa kwa wanadamu wote mbali na Mungu lakini inaendelea kutoa msamaha, urejesho na wokovu wa milele katika imani katika Kristo. Habari njema ya ushindi katika mgogoro wa kiroho!

**11:6** Haya yalikuwa makemeo ya upole kwa sababu ya kukosekana imani kwa Yohana. Biblia inawataja wahusika wake katika hali chanya na hasi. Hii inaonesha sifa yake. Haikuwa Propaganda bali watu wa kweli wa kihistoria na hisia zao na makosa yao! Mathayo alichagua kuandika hili kwasababu inarudi kwenye jambo kubwa la kithiolojia – Yesu ni nani?

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 11:7-15**

<sup>7</sup> Na hao walipokwenda zao, Yesu alianza kuwaambia makutano habari za Yohana, Mlitoka kwenda nyikani kutazama nini? Unyasi ukitikiswa na upepo? <sup>8</sup> Lakini mlitoka kwenda kuona nini? Mtu aliyevikwa mavazi mororo? Tazama, watu wavaao mavazi mororo wamo katika nyumba za wafalme. <sup>9</sup> Lakini kwa nini mlitoka? Ni kuona nabii? Naam, nawaambia, na aliye mkuu zaidi ya nabii. <sup>10</sup> Huyu ndiye aliyeandikiwa haya, Tazama, mimi namtuma mjumbe wangu Mbele ya uso wako, Atakayeitengeneza njia yako mbele yako. <sup>11</sup> Amin, nawaambieni, Hajaonokea mtu katika wazao wa wanawake aliye mkuu kuliko Yohana Mbatizaji; walakini aliye mdogo katika ufalme wa mbinguni ni mkuu kuliko yeye. <sup>12</sup> Tangu siku za Yohana Mbatizaji hata sasa ufalme wa mbinguni hupatikana kwa nguvu, nao wenye nguvu wauteka. <sup>13</sup> Kwa maana manabii wote na torati walitabiri mpaka wakati wa Yohana. <sup>14</sup> Na ikiwa mnataka kukubali, yeye ndiye Eliya atakayekuja. <sup>15</sup> Mwenye masikio, na asikie.

**11:7 "Unyasi ukitikiswa na upepo?"**Tazama ulinganifu wa ufanano wa pande tatu, "je mliona nini?" Yohana alikuwa kama Eliya; alitimizia unabii kwa Marko. 3:1 na Isa. 40:3 (kama vile Marko 1:2-3). Hii inaweza kuhusiana (1) Yohana aliona shaka ambayo ilikuwa imedhihirishwa hadharani katika swali lake (yaani, Mt. 11:3) au (2) tabia ya kug'ag'ania ya Yohana na ujasiri wa kimaadili katika kukemea dhambi (yaani ya mafarisayo na ya Herode).

**11:9 "na aliye mkuu zaidi ya nabii"** Yohana hakuwa muhubiri wa kwanza wa Injili bali nabii wa mwisho wa Agano la Kale aliyetabiriwa na Isaya na Malaki. Ni ngumu kulinganisha manabii wa Agano la Kale na wa Agano Jipya. Manabii wa Agano la Kale waliandika maandiko lakini si manabii wa Agano Jipya. Baadhi ya Mitume kama Paulo walidai kuwa manabii lakini si wote. Sasa ni nini kusudi la karama ya Agano Jipya? Angalia Mada maalum hapa chini.



## MADA MAALUMU: UNABII WA AGANO JIPYA

- I. Sio sawa na Unabii wa Agano la Kale (BDB 611, KB 661; tazama Mada Maalumu:Unabii [Agano la Kale]), ambao una vidokezo vya upokeaji wa sheria za Kiyahudi na kunukuu mafunuo yaliyovuviwa toka kwa YHWH (kama vile Mdo. 3:18, 21; Rum. 16:26). Ni manabii tu waliweza kuandika maandiko.
  - A. Musa aliitwa nabii (kama vile kumb. 18:15-21)
  - B. Vitabu vya historia (Yoshua – Wafalme [isipokuwa Ruthu]) waliitwa “manabii wa mwanzo” (kama vile Matendo. 3:24)
  - C. Manabii wanachukua nafasi ya makuhani wakuu kama chanzo cha habari kutoka kwa Mungu. (kama vile Isaya –Malaki)
  - D. Mgawanyo wa pili wa kanuni za kanisa la Kiebrania ni “Manabii” (kama vile Mt. 5:17; 22:40; Luka 16:16; 24:25, 27; Rum. 3:21).
- II. Katika Agano Jipya dhana ya unabii imetumika katika njia kadhaa tofauti tofauti.
  - A. Kuwarejea manabii wa Agano la Kale na jumbe zao zilizovuviwa (kama vile Mt. 2:23; 5:12 11:13; 13:14; Rum. 1:2).
  - B. Kuurejea ujumbe kwa mtu mmoja badala ya kikundi kichoungana (yaani, manabii wa Agano la Kale kimsingi waliongelea juu ya Israeli).
  - C. Kuwarejea wote wawili Yohana mbatizaji (kama vile Mt. 11:9; 14:5; 21:26 Luka 1:76) na Yesu kama mpiga mbiu wa ufalme wa Mungu (kama vile Mt. 13:57; 21:11, 46; Luka 4:24; 7:16; 13:33; 24:19). Yesu pia alidai kuwa mkuu kuliko manabii (kama vile Mt. 11:9; 12:41; Luka 7:26).
  - D. Manabii wengine katika Agano Jipya
    1. Maisha ya awali ya Yesu kama ilivyoandikwa katika injili ya Luka (yaani., kumbu kumbu za Maria)
      - a. Elizabethi (kama vile Luka 1:41-42)
      - b. Zakaria (kama vile Luka 1:67-79)
      - c. Simoni (kama vile Luka 2:25-35)
      - d. Ana (kama vile Luka 2:36)
    2. Ubashiri wa kejeli (kama vile Kayafa, Yohana 11:51)
  - E. Inarejea juu ya mtu anayeitangaza injili (ikijumuishwa kwenye orodha ya kipawa cha utangazaji katika 1 Kor. 12:28-29; Efe. 14:11)
  - F. Ikirejea juu ya vipawa vinavyoendelea kanisani (kama vile Mt. 23:34; Mdo. 13:1; 15:32; Rum. 12:6; 1 Kor. 12:10, 28-29; 13:2; Efe. 4:11) wakati mwingine hii inaweza kumaanisha kwa wanawake (kama vile Luka 2:36; Mdo. 2:17; 21:9; 1 Kor. 14:4-5).
  - G. Ikirejea kwa sehemu mafunuo ya kitabu cha ufunuo (kama vile Ufu. 1:3; 22:7, 10, 18,19)
- III. Manabii wa Agano Jipya
  - A. Hawatoi ufunuo uliovuviwa kwa maana sawa kama manabii wa Agano la Kale waliofanya (yaani mafundisho ya Biblia). Usemi huu unawezekana kwa sababu ya Matumizi ya kifungu cha neno “Imani” (yaani., kwa maana ya injili iliyokamilika) iliyotumika katika Matendo 6:7; 13:8; 14:22; Gal. 1:23; 3:23; 6:10; Flp. 1:27; Yuda 3, 20.

Dhana hii iko wazi kutokana na fungu kamili la maneno lililotumika katika Yuda 3, “imani ya mara moja pasipo kujirudia imekabidhiwa kwa watakatifu.” Imani ya “jumla pasipo kujirudia” inarejerea kwenye ukweli, mafundisho, dhana, maoni ya dunia juu ya mafundisho ya ukristo. Msisitizo huu unaotolewa mara moja tu ni msingi wa Kibiblia kwa ajili ya kuzuia uvuvio ulio wa kithiolojia wa maandiko ya Agano Jipya na pasipo kuruhusu maandiko mengine kufikirika kimafunuo (angalia Mada Maalumu: Uvuvio). Kuna maeneo mengi yenye utata, yasiojulikana katika agano jipya (Tazama Mada Maalumu: Fasihi za mashariki [mafumbo ya Kibiblia]), lakini waamini wanathibitisha kwa imani kuwa kila kitu “kinachohitajika” kwa ajili ya imani na utendaji inajumuishwa ikiwa na utosherevu wenye uwazi wa kutosha katika Agano Jipya. Dhana hii inaelezwa kama “ufunuo pembe tatu.”

1. Mungu amejidhihirisha mwenyewe katika historia kwa muda muafaka (UFUNUO)
  2. Amechagua baadhi ya waandishi wa kibinadamu kuweka kumbu kumbu na kuelezea matendo yake (UVUVIO).
  3. Alimtoa Roho Wake ili kufungua mawazo na mioyo ya watu wapate kuyaelewa maandishi haya, si kwa ubora tu bali kwa utoshelevu wa wokovu na maisha ya Mkristo yenye kufaa (NURU, tazama Mada Maalumu: nuru). Hoja iliyopo hapa ni kuwa uvuvio umewekewa ukomo kwa waandishi wa neno la Mungu. Hakuna maandiko mengine, maono au mafunuo yenye mamlaka. Sheria za kanisa zimefungwa. Tuna ukweli wote tunaohitaji ili kuitikia vizuri kwa Mungu. Ukweli huu unaonekana vizuri katika makubariano ya waandishi wa Kibiblia dhidi ya waumini watiifu wa ki-Mungu wasiokubali. Hakuna mwandishi au mnenaji wa kisasa aliye na kiwango cha uongozi wa ki-Uungu kama ambao waandishi wa neno la Mungu waliokuwa nacho.
- B. Kwa namna nyingine manabii wa Agano Jipya ni sawa na wale wa Agano la Kale.
1. Utabiri wa matukio yajayo (kama vile Paulo, Mdo. 27:22; Agabo, Mdo. 11:27-28; 21:10-11; manabii wengine wasiotajwa Mdo. 20:23).
    1. Kutangaza hukumu (kama vile Paulo, Mdo. 13:11; 28, 25-28)
    2. Dalili za matendo ambayo dhahili yanaonyesha matukio (kama vile Agabo Matendo 21:11).
- C. Mara zote wananena kweli ya injili, wakati mwingine kwa njia ya utabiri (kama vile Matendo 11:27-28; 20:23; 21:10-11) Lakini kimsingi huu sio mtazamo wenyewe. Unenaji wa unabii katika Wakorinto wa 1 kimsingi unaibainisha injili (kama vile 1 Kor. 14:24,39).
- D. Ni Roho wa wakati ule ule akimaanisha kudhihirika wakati ule ule na utumiaji wa kiutendaji wa kweli ya Mungu kwa kila hali, tamaduni mpya au kipindi cha muda (kama vile 1 Kor. 14:3).
- E. Walikuwa imara katika makanisa ya mwanzo ya Paulo (kama vile 1 Kor. 11:4-5; 12:28, 29; 13:2, 8, 8,9; 14:1 3,4,5,6,22,24,29,31,32,37,39; Efe. 2:20; 3:5; 4:11; 1 The. 5:20) na wametajwa katika *Didache* (iliyoandikwa katika karne ya mwisho au karne ya pili tarehe haijulikani) na wakati wa mienendo ya Kikristo ya karne ya pili na tatu katika Afrika ya kaskazini.

IV. Je karama za Agano Jipya zimekoma?

- A. Swali ni gumu kulijibu. Linasaidia kufafanua jambo kwa kuelezea kusudi la karama. Je wanamaanisha kuthibitisha mafundisho ya awali ya kuhubiri injili au ni njia endelevu ya kanisa kujihudumia lenyewe kwenye ulimwengu ulipotea?
- B. Je mmoja aweza kuangalia kwenye historia ya kanisa kujibu maswali au Agano Jipya lenyewe? Hakuna kiashirio chochote kinachoonyesha katika Agano Jipya kuwa karama za rohoni zilikuwa za muda tu. Wale wote wanaojaribu kutumia 1 Kor 13:8-13 kuelezea habari hii wanatukanisha kusudi la mwandishi wa aya hii, ambayo inadokeza kuwa kila kitu kitatoweka isipokuwa upendo.
- C. Nathubutu kusema kuwa tangu Agano Jipya, si historia ya kanisa, ndiyo yenye mamlaka, waamini wanapaswa kuthibitisha kuwa karama zinaendelea. Hata hivyo ninaamini kuwa mila zinaathiri tafsiri za maandiko. Baadhi ya maandiko yalioko wazi hayatumiki tena (yaani busu takatifu, Baibui, makanisa kukutana nyumbani n.k). kama mila zinaathiri maandiko, hivyo kwa vipi zisiathiri historia ya kanisa?
- D. Hili ni swali ambalo haliwezi kujibiwa. Baadhi ya waumini wanatetea kuwepo na “ukoma” na wengine watetea “kusiwepo na ukomo”. Katika eneo hili, kama ilivyo kwa mambo mengi yaliyo fasiliwa, moyo wa mwamini unabaki kuwa ndo kiini. Agano jipya ni tata na la kitamaduni zaidi. Ugumu unaweza kuamua ni maandiko yapi yanaathiriwa na mila/historia na yapi yanaathiriwa kwa wakati wote na yapi kwa mila (kama vile Fee na Stuart, *How to*

*read the Bible for all its Worth*, kur. 14-19 na 69-77 hapa ndipo pale mjadala wa uhuru na kuwajibika, unaopatikana katika Warumi 14:1-15, 13 na Kor. 8-10 unapokuwa wenye umuhimu mkubwa. Namna tunavyojibu swali ni muhimu katika njia mbili.

1. Kila mwamini anapaswa kutembea katika imani yake kwa mwanga walio nao. Mungu anaona mioyo yetu na nia.
  2. Kila mwamini yampasa aruhusu waamini wengine kutembea katika uelewa wa imani. Lazima pawepo na uvumilivu ndani ya mipaka ya kibiblia. Mungu anatutaka tupendane kama anavyotupenda.
- E. Kwa kuhitimisha suala hili, Ukristo ni maisha ya imani na upendo, na sio tu thiolojia kamili. Uhusiano wetu na Yeye unaosababisha kuwepo na uhusiano na wengine ni muhimu zaidi kuliko habari au imani kamili.

**11:10 "Huyo ndiye aliyeandikiwa haya"** Hii ni nukuu kutoka Marko. 3:1. Ilikuwa ni rejea kwa safari ya kifalme na maandalio ya kupendeza ambayo yalitangulia. Marko 1:2-3 ni nukuu ya uhusishi Marko. 3:1 na Isaya. 40:3. Dhana hii inayofanana katika Isaya. 57:14; 62:10.

Mathayo anakusanya maisha ya mafundisho ya Yesu ili kuwashawishi Wayahudi kwamba ndiye Masihi (Ajaye). Hii inafanyika kwa kunukuu maandiko ya Agano la Kale. Yanatambulishwa katika namna mbali mbali tofauti.

1. nabii hatajwi au kuelezwa kwa
  - a. nabii, Mt. 1:22 (asiyetajwa, Isaya. 7:14)
  - b. nabii, Mt. 2:5 (asiyetajwa, Mika 5:2)
  - c. nabii, Mt. 13:35 (asiyetajwa, Zab. 78:2)
  - d. nabii, Mt. 21:4 (asiyetajwa, Isa. 62:11)
2. nabii anatajwa
  - a. Isaya -- Mt. 3:3; 4:14; 12:17; 13:14; 15:7
  - b. Yeremia -- Mt. 2:18; 27:9
3. Imendikwa (kauli tendwa ya wakati timilifu), Mt. 4:6,10; 11:10; 21:13; 26:24,31
4. Mungu alisema, Mt. 15:4; 22:31
5. je hamjasoma, Mt. 19:4; 21:16,42
6. Musa alisema, Mt. 22:24
7. Daudi katika Roho, Mt. 22:43

Kuzaliwa kwa Yesu, maisha, kifo, ufufuo na kurudi vilikuwa utimilizwaji wa unabii wa Agano la Kale (kama vile Mt. 26:54-56).

**11:11 "Hakika"** Hii kibayana ni "amina," neno la Kiebrania kwa imani (kama vile Hab. 2:4). Asili yake ya sasili ilimaanisha "kuwa thabiti" au "kuwa na hakika." Mara kwa mara ilitumiwa na Yesu kutambulisha kauli za muhimu. Angalia Mada Maalum katika Mt. 5:18.

☐ **"kati yao waliozaliwa na wanawake"** Mstari huu sio kumdharau Yohana Mbatizaji bali ukiri kwamba alikuwa ni nabii wa mwisho wa manabii wa Agano la Kale (kama vile Mt. 13:16, 17). Katika namna hii ilikuwa ni njia ya Yesu ya kukiri umuhimu wa zama mpya (Agano Jipya, Yer. 31:31-34; Ezek. 36:22-38), ikianzishwa na yeye mwenyewe.

**11:12**

**NASB, NKJV,**

**NRSV** "ufalme wa mbinguni hupatikana kwa nguvu, nao wenye nguvu wauteka"

**TEV** "ufalme wa mbinguni hupatikana kwa nguvu, nao wenye nguvu wauteka"

Kumekuwepo na mjadala mkubwa kuhusu mstari huu unachomaanisha na namna gani inatakiwa ifasiriwe. Tungo ya kwanza inaweza kuwa (1) katika namna chanya, inayoashiria ufalme wa mbinguni kwa nguvu unaendelea mbele, au(2) kwa namna hasi, ikirejerea mwitikio wa ktumia nguvu wa viongozi wa Kiyahudi kwa wote mahubiri ya Yohana na Yesu. Tungo ya pili inaonekana kuwa ni mbinu ya maneno "kwa nguvu" na ilitumika juu ya wenye dhambi kwa shauku kutwaa au kupokea injili (kama vile Luka 16:16). Tafsiri ya toleo la Kale la Kiyunani linatumia kitenzi hiki katika namna ya "kualika kwa nguvu" (kama vile Mwa. 33:11; Amu. 19:7). Angalia Mada Maalum: Ufalme wa Mungu katika Mt. 4:17.

**11:13 "kwa kuwa manabii wote na torati"** Kanoni ya Kiebrania ilikuwa imegawanywa katika sehemu tatu, "sheria," "manabii," na "maandiko." Hii ilikuwa ni njia ya Agano la Kale ya kuonesha Agano la Kale lote (kama vile Luka 24:44). Agano la Kale lilielekeza kwa Yesu na injili.

### **MADA MAALUM: KANONI YA KIEBRANIA**

Biblia ya Kiebrania imegawanyika kwenye migawanyo mitatu (Biblia ya Kiingereza inafuata mpangilio wa tafsiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani).

1. Torati (vitabu vitano vya Musa), Mwanzo – Kumbu kumbu la Torati
2. Manabii (Nevi'im)
  - a. Manabii wa mwanzo, Yoshua – Wafalme (isipokuwa kitabu cha Rutu)
  - b. Manabii wa baadaye, Isaya – Malaki (isipokuwa kitabu cha Maombolezo na Daniel)
3. Maaandiko (Kethubim)
  - a. Fasihi za Hekima, Ayubu – Mithali
  - b. Kipindi cha Wayahudi baada ya kutoka uhamishoni, Ezra – Esta
  - c. Vitabu vitano vya Kiebrania (Megilloth) (vile vitabu vitano, vilivyosomwa kwenye sherehe)
    - 1) Kitabu cha Rutu (kilichosomwa siku ya Pentekoste)
    - 2) kitabu cha Mhubiri (kilichosomwa kwenye hema la kukutanikia)
    - 3) kitabu cha Wimbo ulio bora (kilichosomwa siku ya Pasaka)
    - 4) kitabu cha Maombolezo (kilichosomwa kukumbuka kuanguka kwa Yerusalem mwaka wa 586 k.k.)
    - 5) kitabu cha Esta (kilichosomwa wakati wa kupiga kura)
  - d. 1 na 2 Nyakati
  - e. Danieli

Kitabu kipya cha Kanoni ni kile cha 2 Nyakati. Tarehe kamili haijulikani kwa sababu matoleo ya kiuandishi kwa baadhi ya koo.

**11:13 "mpaka Yohana"** Hii inaonekana kumaanisha kwamba agano la kale linaelekea mwisho (kama vile Wagalatia 3 na kitabu cha Waebrania) kwa mahubiri ya Yohana Mbatizaji, aliyekuwa nabii wa mwisho wa agano. Kitu fulani kipya kimekuja pamoja na Yesu. Yohana ni muaandaa njia! Zama mpya ya Roho; agano jipya; ahadi ya Mwa. 3:15; 12:3 imekuja!

**11:14 "ikiwa"** Hii ni sentensi daraja la kwanza lenye masharti ambayo inadhaniwa kuwa kweli kulingana na mtazamo wa mwandishi au kwa makusudi ya kifasihi.

☐**"Yohana mwenyewe ndiye Eliya aliyekuja"** Hii inamaanisha katika Luka 1:17. Katika Yohana. 1:20-25, alikataa kwamba yeye hakuwa Eliya lakini huu ulikuwa muktadha wa maswali bayana ya Mafarisayo. Yohana alikuwa

kikataa kwamba yeye siye Eliya aliyezaliwa upya. Yesu anaelezea kwamba Yohana ameutimiliza unabii wa kurudi kwa Eliya kabla ya Masihi kutoka Mal. 3:1 na 4:5, (kama vile. Mt. 11:10).

**11:15 "Yeye aliye na masikio na asikie"** Nahau hii (ya wakati endelevu uliopo na shurutishi ya wakati uliopo) inamaanisha kwamba mpaka Roho Mtakatifu asaidie uelewa wa mwamini ndio aweze kuufahamu ukweli wa kiroho (kama vile Isaya. 6:9-10; 50:5; Mt. 13:9,43; Marko 4:9,23; Luka 8:8; 14:35; sawasawa na Ufu. 2:7,11,17,29; 3:6,13,22; 13:9). Hata hivyo pia inamaanisha kwamba utayari wa mtu mmoja mmoja kusikia na kuitikia pia ni muhimu. Ufunuo unajumuisha mtumaji wa kiungu (yaani agano)

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 11:16-19**

**<sup>16</sup> Lakini nitakifanana na nini kizazi hiki? Kimefanana na watoto wanaokaa sokoni, wanaowaita wenzao, wakisema, <sup>17</sup> Tuliwapigia filimbi, wala hamkucheza; tuliomboleza, wala hamkulia. <sup>18</sup> Maana Yohana alikuja, hali wala hanywi, wakasema, Yuna pepo. <sup>19</sup> Mwana wa Adamu alikuja, akila na kunywa, wakasema, Mlafi huyu, na mlevi, rafiki yao watoza ushuru na wenye dhambi! Na hekima imejulikana kuwa ina haki kwa kazi zake.**

**11:16 "watoto wanaokaa sokoni"** Hii inafanana na Luka 7:31-32. Hata kama Yohana Mbatizaji alikuja kama mwenye nidhamu ya hali ya juu ya kitabia (yaani nabii wa jangwani kama Eliya), Wayahudi walimkataa. Yesu alikuja kama mtu aliyetayari kuchangamana a kushirikiana na wanadamu wa Nyanja zote za kijamii nab ado walimkataa pia. Aidha walizungumza juu ya kutoeleweka kwa viongozi wa Kiyahudi au kuonesha ubaguzi wao waliokuwa nao hapo kabla.

**11:17 "Tuliwapigia filimbi, wala hamkucheza"** Mbinu hii ya kijamii inarejerea namna Yesu alivyochangamana na watu (kama vile Mt. 11:19). Filimbi ilitumika kwa ajili ya kucheza (Mt. 11:17a) wakati wote wa sherehe na misiba (Mt. 11:17b).

☐ **"tuliomboleza, wala hamkulia"** Mbinu hii ya kujinyima na upole inarejerea huduma ya Yohana Mbatizaji (kama vile Mt. 11:18).

**11:18 "Yuna pepo"** Mashitaka na shutuma hizi zinafanywa dhidi ya Yesu katika Mt. 9:34 and 12:24 (kama vile Yohana 7:20; 8:48-49,52; 10:20). Hili ni andiko pekee ambalo linashitaki Yohana juu ya kuwa na pepo. Wayahudi wasingeweza kumkataa aidha nguvu ya Yohana au Yesu, bali walidai vyanzo vya mamlaka yao ilikuwa ni kwa yule muovu. Hii kwa hakika ni dhambi isiyosameheka.

**11:19 "Mwana wa Adamu"** Hiki n cheo na jina la kujichagulia la Yesu kwa sababu halikuwa na maana ya kijeshi wala utaifa. Liliunganisha sehemu ya ubinadamu na asili ya Kristo (kama vile Ezek. 2:1; Zab. 8:4; Dan. 7:13). Muunganiko wa sehemu ilifanyika kuwa ukweli muhimu wa Agano Jipya (kama vile 1 Yohana 4:13).

☐ **"Mlafi huyu, na mlevi, rafiki yao watoza ushuru na wenye dhambi"** Yesu alitenda katika namna isiyotegemewa (kama vile Mt. 9:11; Luka 5:30; 7:34; 15:2). Hii inatimiliza utabiri wa kimasihwa wa Isaya. Sheria ya kidini na nidhamu ya kitabia imekuwa jitihada ya kiroho na kithiolojia kwa kanisa na ningependa kunukuu kwa muhtsari kutoka New International Dictionary of New Testament Theology, vol. 1, ukur. 495.

"Ikitazamwa kwa ujumla wake, hata hivyo, nidhamu ya kitabia katika namna ya kukataa mali, matendo ya kingono na kujilinda katika vyakula sijambo ambalo linachukuliwa na mafundisho ya Yesu katika Injili. Hii haimaanisha kwamba kujikana kwa mtu husika katika mazingira husika kumwekwa kando (kama vile hadithi ya kijana tajiri, Mt. 19:21). Ni kwamba tu kutoka katika kifungu kama hicho (kama vile Mt. 11:19; 9:14ff; Mk. 2:18f; Lk. 5:33ff.), Mtu hawezi kutoa mapenzi yake kwaujumla wakuwepo kwa maadili ya nimidhamu. Kujikataa kunatakiwa tu ambapo kitu fulani kinasimama katika njia ya kumfuata Yesu."

11:19

NASB, NRSV "Na hekima imejulikana kuwa ina haki kwa kazi zake."

NKJV "Na hekima imehesabiwa kuwa ina haki kwa kazi zake."

TEV "Na hekima imeoneshwa kuwa ina haki kwa kazi zake."

NJB "Na hekima imethibitishwa kuwa ina haki kwa kazi zake."

Kutajwa kwa "hekima" kunaelezea Mithali 8, ambapo inapewa sifa ya kibinadamu. Yesu ni usanifishaji huo. Mfano wa taswira hii inaonekana katika Mt. 12:42, ambapo Yesu ni zaidi ya hekima ya Suleimani (pia tazama yeye ni Mkuu kuliko hekalu, Mt. 12:6 na mkubwa zaidi kuliko Yona, Mt. 12:41). Hata matumizi ya Yesu ya "nira" katika Mt. 11:29 inaweza kuwa rejea kwa hekima ya mafundisho. Kuna utofauti wa maandiko ya Kiyunani hapa. Kwa "matendo" yake inapatikana katika maandiko ya Kiyunani ya kale,  $\alpha$ , B, and W, wakati "watoto" inapatikana katika Corrector ya Vaticanus B<sup>2</sup>, C, D, K, na L. "Watoto" ni ufanano katika Luka 7:35 na inaonekana kuongezwa hapa na waandishi kutengeneza kifungu kukubali. "Matendo" inaweza kurejerea kwa Mt. 11:2. Toleo la UBS<sup>4</sup> linatoa "matendo" alama ya "B" (karibia na hakika). Kweli ile ile inaelezewa katika tungo "kwa matunda yao mtawatambua" (kama vile Mt. 7:16,20; 12:33). Hii ni kweli kwa Yesu na kwa watu wote. Matendo ya Yesu katika Mathayo 8-9 ilifunua wale ambao wangeona kwamba alikuwa ni Masihi aliyehaidiwa Ajaye (kama vile Isa. 29:18-19; 35:5-6; 61:1-2).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 11:20-24**

<sup>20</sup> Ndipo akaanza kuikemea miji ile ambamo ndani yake ilifanyika miujiza yake iliyo mingi, kwa sababu haikutubu. <sup>21</sup> Ole wako, Korazini! Ole wako, Bethsaida! Kwa kuwa kama miujiza iliyofanyika kwenu ingalifanyika katika Tiro na Sidoni, wanalitubu zamani kwa kuvaa magunia na majivu. <sup>22</sup> Walakini nawaambieni, itakuwa rahisi Tiro na Sidoni kustahimili adhabu zao siku ya hukumu kuliko ninyi. <sup>23</sup> Nawe Kapernaumu, je! Utakuzwa mpaka mbinguni? Utashushwa mpaka kuzimu; kwa kuwa kama miujiza iliyofanyika kwako ingalifanyika katika Sodoma, ungalikuwapo mji huo hata leo. <sup>24</sup> Walakini nawaambieni, itakuwa rahisi nchi ya Sodoma kustahimili adhabu yake siku ya hukumu kuliko wewe.

**11:20-24 "Ndipo akaanza kuikemea miji ile ambamo ndani yake ilifanyika miujiza yake iliyo mingi"** Hii ilionesha ukweli wa jumla wa yule aliyepewa vingi kwake vingi vitatakiwa (kama vile Luka 12:48). Miji ya siku za Yesu inalinganishwa na miji ya Agano la Kale. Walikuwa wameona Miujiza Yake na kusikia mafundisho Yake. Ninawi ilitubu wakati wa Mahubiri ya Yona wakati Tiro, Sidoni, Sodoma na Gomora haikutubu, na bado miji ya Galilaya ya siku za Yesu ilikuwa na ufahamu mkubwa wa kuitikia. Wale wenye ufahamu mkubwa watawajibika zaidi! Maoni ya Yesu yalitangulizwa na "ole" (kama vile. Mt. 18:7; 23:13,15,16,23,25,27,29; 24:19; 26:24). Hii ilikuwa ni moja ya miundo ya kifasihi ambayo manabi wa Agano la Kale walizungumza jumbe zao (ahadi za Mungu, maeneo ya kimahakama, na maeneo ya misibani na maombolezo). Muundo huu unawakilishwa na ombolezo la msiba (ombolezo).

☛ **"tubuni"** Toba ni kugeuka kutoka dhambini na ubinafsi, sehemu hasi ya wokovu wakati imani ni kumgeukia Mungu katika Kristo, kipengele hasi cha woovu (kama vile Marko 1:15; Mdo 3:16, 19; 20:21). Kwa kuunganisha maana za Kiyunani na maneno ya kiebrania, maana ya toba ni kubadilisha nia ikifuatiwa na kubadilisha kitendo. Toba ni zaidi ya hisia (kama vile 2 kor. 7:8-11). Lazima ipelekee mabadiliko katika mtindo wa maisha. Angalia dokezo kamili katika Mt. 4:17.

**11:21,23 "ikiwa"** Hii ni sentensi daraja la pili yenye masharti ambayo inaiwa "tofauti na ukweli," kauli ya uongo inawekwa ili kuoneshwa mazingira a uongo iliyotokana nayo.

**11:21 "Korazini"** Hii inaonesha mpaka wa kimaarifa wa kazi za Yesu. Lazima tukumbuke kwamba Injili ni kweli zilizochaguliwa kithiolojia kwa hadhira walio wa aina fulani (yaani Wayahudi, Warumi na Mataifa), na sio historia za kimagharibi (kama vile Yohana. 20:30-31)

☐ **"Bethsaida"** Kulikuwa na Bethsaida mbili. Moja ilikuwa karibu na Kapernaumu na ingine katika sehemu ambapo Mto Yordani ulitiririka Bahari ya Galilaya.

☐ **"ikiwa"** Hii ni sentensi daraja la Pili yenye masharti, angalia dokezo katika Mt. 11:23.

☐ **"Tiro na Sidoni"** Tiro na Sidoni zilikuwa aina za Agano la Kale za mataifa yenye dhambi na yenye viburi. Tungo inayopatikana katika Mt. 11:23 inahusiana nah ii katika Isa. 14:13-15 na Ezek. 28:12-16. Katika mistari hii kiburi cha Mfalme wa Babeli na Tiro vilitumika kama mfano wa kiburi cha shetani.

☐ **"katika magunia na majivu"** Katika muktadha huu inarejerea ishara ya toba (kama vile Yohana 3:5-8).

### **MADA MAALUMU: IBADA KWA WALIO KATIKA HUZUNI**

Waisraeli walieleza huzuni kwa mpendwa wao aliyefariki na toba binafsi, pamoja na makosa ya jinai yaliyofanyika kwa ujumla kwa njia kadhaa:

1. Kurarua mavazi, Mwa. 37:29,34; 44:13; Waamuzi. 11:35; 2 Sam. 1:11; 3:31; 1 Fal. 21:27; Ayubu 1:20
2. Kuvaa gunia, Mwa. 37:34; 2 Sam. 3:31; 1 Fal. 21:27; Yer. 48:37
3. Kuvua viatu, 2 Sam. 15:30; Isa. 20:3
4. Kuweka mikono kichwani, 2 Sam. 13:19; Yer. 2:37
5. Kuweka vumbi kichwani, Yos. 7:6; 1 Sam. 4:12; Neh. 9:1
6. Kuketi sakafuni, Omb. 2:10; Ezek. 26:16 (kulala chini, 2 Sam. 12:16); Isa. 47:1
7. Kupiga kifua, 1 Sam. 25:1; 2 Sam. 11:26; Nah. 2:7
8. Omboleza, 1 Sam. 25:1; 2 Sam. 11:26
9. Kata mwili, Kumb. 14:1; Yer. 16:6; 48:37
10. Kufunga, 2 Sam. 1:12; 12:16,21; 1 Fal. 21:27; 1 Nya. 10:12; Neh. 1:4
11. Kuimba na kusifu katika maombolezo, 2 Sam. 1:17; 3:31; 2 Nya. 35:25
12. Upara (nywele zilikatwa), Yer. 48:37
13. Kunyoa ndevu, Yer. 48:37
14. funika kichwa au uso, 2 Sam. 15:30; 19:4

Hizi zilikuwa ishara za nje kutokana na hisia za ndani

**11:22** Kuna viwango vya vyote thawabu na adhabu vikijikita katika kiwango cha ufahamu ambacho wasikiaji wamepata kuwa nacho (kama vile Luka 12:47, 48; Mt. 10:15). Angalia Mada maalum katika Mt. 5:12.

**11:23 "Nawe Kapernaumu, je! Utakuzwa mpaka mbinguni?"** Hii tungo ya kisarufi inategemea jibu la "hapana". Haya yanaweza kuwa maelezo kwa Isaya. 14:13-14 na Ezek. 28:2,5-6,17, ambayo inakuza kiburi cha wafalme wa Tiro na Babeli.

☐ **"Utashushwa mpaka kuzimu"** Haya yanaweza kuwa maelezo ya Isa. 14:15 au Ezek. 26:20; 28:8; 31:14; 32:18,24. Hii inarejerea kwa ulimwengu wa waliokufa (kama vile Luka 16:23) katika Kiebrania *Sheol*. Kulingana na walimu wa kiyahudi, kulikuwa na sehemu ya wenye haki iitwayo, *Paradise* na sehemu ya wabaya iitwayo *Tartarus*. Hii inawezekana kuwa kweli. Maneno ya Yesu kwa mmoja wa wahalifu aliosulubiwa pamoja naye katika Luka 23:43 yanaonekana kumaanisha sehemu ya wenye haki ya Hades kwasababu hakurudi mbinguni siku ya Pentekoste. Wakati wa Ufufuko wa Yesu alichukua sehemu ya wenye haki ya Hades (*Sheol*) kuwa sehemu yake. Hivyo Paulo

anasema sasa katika 2 Kor. 5:8b kutokuwepo katika mwili ni kuwa pamoja na Bwana. Kuwa makini juu ya dhana za *Hades* na *Gehenna*. Ni tofauti katika Agano Jipya. Angalia [MADA MAALUM: Wafu wako wapi?](#) katika Mt. 5:22.

☑️"**ikiwa**" Hii ni senensi ya darajala pili yenye masharti ambayo inaitwa "kinyume na ukweli" (ilivyokuwa katika Mt. 11:21). Hii inatakiwa ifasiriwe kama, "ikiwa miujiza ilitokea katika Sodoma ambayo ilitokea pia kwenu (lakini haikuwa hivyo), ingewezakudumu mpaka leo, (ambavyo haikuwa hivyo)."

**11:24 "nchi ya Sodoma"** Neno "nchi" inaweza kuwa tungo ya Kiaramu kwa ajili ya "mji." Wanaekolojia wa kisasa wanaamini kwamba huu mji wa Agano la Kale ulikuwa mwishoni mwa kusini mwa bahari ya Chumvi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 11:25-27**

<sup>25</sup> Wakati ule Yesu akajibu, akasema, Nakushukuru, Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa mambo haya uliwaficha wenye hekima na akili, ukawafunulia watoto wachanga. <sup>26</sup> Naam, Baba, kwa kuwa ndivyo ilivyopendeza mbele zako. <sup>27</sup> Akasema, Nimekabidhiwa vyote na baba yangu; wala hakuna amjuaye Mwana, ila Baba; wala hakuna amjuaye Baba, ila Mwana, na ye yote ambaye Mwana appenda kumfunulia.

**11:25** Katika Luka10:21 maneno haya ya Yesu yanazungumzwa baada ya kurudi kwa safari ya sabini. Kumbuka Injili sio lazima kuwa katika mpangilio wa ufuatano! Angalia Gordon Fee na douglas Stuart, *HowTo Read the Bible For All Its Worth*, ukur. 127-148.

☑️"**Nakutukuza**" Hili neno ambatani katika muktadha huu linamaanisha kukiri kwa uwazi (kama vile Mt. 3:6; Flp. 2:11), kusifu, au kusherehekea. Neno hili hili la Kiyunani linafasiri neno la Kiebrania"sifa" katika tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani. Kiaramu yawezekana kilimaanisha "kukubali kwa wazi."

☑️"**Bwana wa mbingu na nchi**" Hii ni nahau ya Kiebrania kwa uumbaji wa kimwili. Hii inakiri Mungu kuwa muumbaji wa vitu vyote. Cha kufurahisha, Yohana, Yohana 1:3,10; Paul, 1 kor. 8:6, Kol. 1:16; na mwandishi wa Waebraia, Ebr. 1:2; 2:10, wanaelezea kwamba Yesu ni chombo cha Baba katika uumbaji.

☑️"**kwa kuwa mambo haya uliwaficha wenye hekima na akili, ukawafunulia watoto wachanga**" Hii ni nahau ya kisemitiki ikimaanisha vitu ambavyo wanadamu wote na sio tu wale wa kidini au wasomi wa kiulimwengu wanaweza kujua kuhusu Mungu. "Watoto wachanga" inamaanisha waamini wapya (kama vile Mt. 18:6). Inashangaza bado kwamba viongozi wa kidini wa Wayahudi waliolijua Agano la Kale lote hawakuweza kumtambua Yesu na kuweka imani yao Kwake (kama vile Warumi 9). Isaya 50:5 lazima itokee kabla ya kupelekea dhambi (Isaya 6:9-10) inaweza kugeuzwa!

**11:26 "Kwakuwa hivi ndivyo ilivyokupendeza machoni pako"** Hii ilikuwa ni nahau ya Kiebrania "lilikuwa ni mapenzi ya Mungu" (kama vile Luka 10:21).

**1:27 "Nimekabidhiwa vyote na baba yangu"** Huu ulikuwa ni ukiri wa nguvu wa uelewa wake mwenyewe Yesu na namna pekee ya mamlaka iliyotolewa katika huduma yake ya mapema (kama vile Mt. 28:18, Yohana 3:35; 13:3; Efe. 1:20-22, Kol. 1:16-19; 2:10, na 1 Pet. 3:22). Yesu anasema kauli kuu juu yake yeye mwenyewe (yaani Yohana 10:1-18; 14:1-24). Hawezi kuwa mwalimu mkuu, mbobezi wa kidini! Yeye ni aidha Mwana wa Mungu au mwendawazimu au muongo! Hakuna sababu nyingine ya kati kati hapa! Agano Jipya ni kweli au Ukristo ni uongo (kama vile 1 Kor. 15:12-19). Lazima uamue!

Mstari huu unaonekana kama injili ya Yohana (kama vile Yohana 3:35; 10:15; 13:3; 17:2). Japo bado kweli hii hii inarudiwa katika Mt. 28:18.



☑️**"wala hakuna amjuaye Baba"** Neno la kwenda ndani zaidi "kumjua," limetumika mara mbili, likimaanisha kikamilifu, kwa kukamilika, na maarifa binafsi (yaani, *epiginoskō*). Hakuna amjuaye Baba isipokuwa Mwana (kama vile Yohana 1:18; 17:25; 1 Yohana 5:1-12)

☑️**"na ye yote ambaye Mwana apenda kumfunulia"** Huu mstari sio andiko la uthibitisho kwa Yesu kuchagua baadhi na kutowachagua wengine. Mstari wa 28 unaonesha kwamba Mungu kwa kumchagua Kristo, alichagua wanadamu wote (kama vile Yohana 3:16; 4:42; 1 Tim. 2:4; Tito 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:1; 4:14). Pia linaelezea kwamba Yesu ni kilele cha ufunuo wa Mungu wa milele asiyeonekana kwa macho ya mwili na nyama (kama vile Yohana 1:1,18; Kol. 1:15; Ebr. 1:3). Yeye ndiye njia pekee (1) ya kumjua Baba (kama vile Yohana 1:18; 3:11) na (2) kwenda kwa Baba (kama vile Yohana 10:1-9; 14:6; Mdo. 4:12; 1 Tim. 2:5)!

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 11:28-30**

<sup>28</sup> Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. <sup>29</sup> Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; <sup>30</sup> kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi.

**11:28-30** Mistari hii ni ya kipekee kwa Mathayo. Mstari wa 28 unakiri fundisho la utakaso, wakati mstari wa 29 unakiri utakaso unaoendelea.

**MADA MAALUMU: UTAKATIFU/ UTAKASO KATIKA AGANO JIPYA**

Kitabu cha Agano jipya kinadai kwamba wenye dhambi wanapomgeukia Yesu kwa toba na imani (kama vile Marko 1:15; Matendo 3:16,19; 20:21), huthibitishwa na kutakaswa papo kwa papo. Hii ni nafasi mpya katika Kristo. Haki yake imewekwa ndani yao (kama vile Mwa. 15:6; Warumi 4). Wametangaziwa haki na utakatifu (tendo la ki-Mungu la kumto mtu hatiani).

Lakini Agano Jipya pia linawasistiza waamini kuwa katika utakatifu au utakaso. Hii ni nafasi ya kitheolojia katika kazi ya Yesu Kristo iliyomalizika na wito wa kufanana na Kristo katika mtazamo na matendo katika maisha ya kila siku. Kwa kuwa wokovu ni neema ya bure na gharama ya kila kitu cha mtindo wa maisha, hivyo hata hii, ni utakaso.

**Mwitikio wa Awali**

Matendo 26:18  
Warumi 15:16  
1 Wakorintho 1:2-3; 6:11  
2 Wathesalonike 2:13  
Waebrania 2:11; 10:10,14; 13:12  
2 Petro 1:2

**Ufanano na Kristo Endelevu**

Warumi 6:19  
2 Kor. 7:1  
Waeieso 1:4; 2:10  
1 Wathesalonike. 3:13; 4:3-4,7; 5:2  
1 Timotheo 2:15  
2 Timotheo 2:21  
1 Petro 1:15-16  
Waebrania 12:14

**11:28 "Njoni kwangu"** "njoo" ni kielezi kilichotumika kama kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu. Inaashiria mwitikio wa imani ya haraka kwa Yesu mwenyewe na ujumbe wake mpya wa agano. Tazama msisitizo ulikuwa katika uhusiano binafsi, sio maudhui ya kimfundisho au ibada tu. Kweli hii hii ilirudiwa mara kwa mara katika Injili ya Yohana.

☑️**"msumbukao"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo. Maneno "kusumbuka" na "kuelemewa" katika mstari huu inaelezea kazi ngumu. Yanafanana.

☑️"**wenye kuelemeza**" Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati timilifu. Maneno haya mawili yanafanana kidesturi juu ya majukumu mazito ya Dini ya Kiyahudi ya walimu wa dini (kama vile Mdo. 15:10). Wazo hili hili linaelezwa kwa nahau ya Kiebrania "nira" (kama vile Mt. 11:29,30; Mt. 23:4; Luka 11:46). Hii kisitiari ilitumika kwa Desturi za kinywa za wayahudi (Talmud), ambayo ilikuwa ni mzigo mzito kiasi cha kumtenganishwa mwanadamu na Mungu kuliko kuwaleta Kwake. Dini ya Kiyahudi ilikuwa kikwazo badala ya kuwa daraja! Agano Jipya katika Yesu lina vigezo kama ilivyo agano la Kale. Hata hivyo hayatuleti kwa Mungu na kutufanya tukubalike. Inakuwa ni matokeo tu ya asili yakumjua Yeye katika Kristo. Mungu bado anataka watu wenye haki wanaoaksi tabia yake kwa ulimwengu. Siku zote huwa nataja matakwa ya Agano Jipya

1. Toba
2. Imani
3. Utii
4. Ustahimilivu

☑️"**nitawapumzisha**" Hii ni Tungo ya mkazo ya kisarufi. Yesu alikuwa nasema "Mimi mwenyewe nitawaongoza kwenye pumziko." "Pumziko" haikumaanisha hali ya kukaa na kutofanya shughuli yoyote ila kupata muda wa kufurahia na kufanya mazoezi ili kuelekea katika huduma yenye manufaa kwa ajili ya Kristo. Dhana hii ya mapumziko inaenda mpaka siku ya Saba ya Mwanzo 1. Kwa ajili ya mjadala mzuri wa njia tofauti tofauti za namna neno hili lilivyotumika katika Agano la Kale angalia Waebrania na Mathayo 3 na4.

**11:29 "jifunzeni"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu. Kiasili inahusiana na neno "wanafunzi" linalopatikana katika Mt. 11:1. Waamini wanaamuliwa kujifunza na kukomaa.

☑️"**mimi ni mpole na mnyenyekevu**" Hizi hazikuwa sifa za ulimwengu wa Kiyunani, lakini Yesu alifanya mtazamo uwe msingi. Unyenyekevu na upole ukafanyika kuwa kivutio kwa ufalme mpya wa Mungu.

**11:30 "kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi"** Kuna majukumu mapya yanayotakiwa kufanyika. Imani na toba katika Jina la Yesu ni hatua za kwanza; ya pili ni utii na makuzi; ya tatu ni ustahimilivu. Yesu alibadili jukumu la mzigo wa mafarisayo (kama vile Mt. 23:4; Luka 11:46) kuwa katika maisha ya shukurani na huduma katika Jina lake (kama vile 1 Yohana 5:3).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini Yohana Mbatizaji anaona mashaka kwamba Yesu alikuwa Masihi aliyehaidiwa kuja?
2. Kwanini Yesu anasema kwamba Yohana Mbatizaji hakuwa katika ufalme mpya wa Mungu?
3. Ni kwa namna gani mstari wa 17 unafanya kazi kwa Yesu na Yohana Mbatizaji?
4. Je kutakuwako viwango vya adhabu?
5. Je Yesu anawaalika watu wote kuja kwake au ni ni wateule fulani tu?
6. Toa maana ya maneno "mzigo" na "nira" katika mazingira yao ya kimila na kidini.

## MATHAYO 12

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Kuvunja masuke siku Ya Sabato 12:1-8	Yesu ni Bwana wa Sabato 12:1-8	Yesu na sheria za Sabato 12:1-8	Swali juu ya Sabato 12:1-2 12:3-8	Uteuzi siku ya Sabato 12:1-8
Mtu mwenye Mkono uliopooza 12:9-14	Uponyaji siku ya Sabato 12:9-14	12:9-14	Mtu mwenye mkono uliopooza 12:9-10 12:11-13a 12:13b-14	Kuponywa mtu aliyepooza mkono 12:9-14
Mtumishi Aliyechaguliwa 12:15-21 (18-21)	Tazama mtumishi wangu 12:15-21	Kazi ya uponyaji 12:15-21	Mtumishi wa Mungu aliyechaguliwa 12:15-21	Yesu mtumishi wa Yahweh 12:15-21 (18-21)
Yesu na Beelzebuli 12:22-32	Nyumba iliyofitinika Haisimami 12:22-30  Dhambi isiyosamehewa 12:31-32	Asili ya nguvu za Yesu 12:22-32	Yesu na Beelzebuli 12:22-23 12:24 12:25-28 12:29 12:30-32	Yesu na Beelzebuli 12:22-24  12:25-28 12:29 12:30-32
Mti na matunda Yake 12:33-37	Mti hufahamika kwa matunda yake 12:33-37	12:33-37	Mti na matunda yake 12:33-35 12:36-37	Maneno huusaliti moyo 12:33-37
Kuhitaji ishara 12:38-42	Waandishi na Mafarisayo wanataka ishara 12:38-42	Wanataka ishara 12:38-42	Kuhitaji miujiza 12:38 12:39-42	Ishara ya Yona 12:38-42
Kurudi kwa pepo Mchafu 12:43-45	Kurudi kwa pepo mchafu 12:43-45	Kurudi kwa pepo mchafu 12:43-45	Kurudi kwa pepo mwovu 12:43-45	Kurudi kwa pepo mchafu 12:43-45
Mama yake na Ndugu zake Yesu 12:46-50	Mama yake Yesu na ndugu wanatumwa kwake 12:46-50	Familia halisi ya Yesu 12:46-50	Mama yake Yesu na ndugu zake 12:46-47 12:48-50	Ukoo halisi wa Yesu 12:46-50

## **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka “[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)”)**

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### **HISTORIA YA NYUMA YA MATHAYO 12:1-50**

- A. Mathayo 12 inaelezea ukuaji wa upinzani (kama vile Mt. 11:12) wa viongozi wa kidini wa kiyahudi, hasa Mafarisayo, kwa Yesu kwa sababu ya kuvunja mapokeo ya fasihi simulizi (yaani, "kitabu cha maadili na sheria za wayahudi") kuna vitabu viwili vya maadili na sheria za kiyahudi vya Babeli na Palestina. Kitabu cha Wapalestina kamwe hakikukamilika, hivyo basi kitabu cha Wababeli kimekuwa chenye mamlaka mawili zaidi.
- B. Mathayo 12 inasimulia 11:28-30 ambayo inaelezea maneno ya mapokeo ya fasihi simulizi kama “mzigo” na “nira.” Nira ya Yesu ni nyepesi na rahisi na inareta pumziko, lakini isichanganywe na tamaduni na sheria halali za Mafarisayo.

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 12:1-8**

<sup>1</sup> Wakati ule Yesu alipita katika mashamba siku ya sabato; wanafunzi wake wakaona njaa, wakaanza kuvunja masuke, wakala. <sup>2</sup> Na Mafarisayo walipoona, walimwambia, Tazama! Wanafunzi wako wanafanya neno ambalo si halali kulifanya siku ya sabato. <sup>3</sup> Akawaambia, Hamkusoma alivyotenda Daudi, alipokuwa na njaa, yeye na wenziwe? <sup>4</sup> jinsi alivyoingia katika nyumba ya Mungu, akaila mikate ile ya wonyesho, ambayo si halali kwake kuila wala kwa wale wenziwe, ila kwa makuhani peke yao? <sup>5</sup> Wala hamkusoma katika torati, kwamba siku ya sabato makuhani hekaluni huinjisi sabato wasipate hatia? <sup>6</sup> Lakini nawaambieni, kwamba hapa yupo aliye mkuu kuliko hekalu. <sup>7</sup> Lakini kama mngalijua maana yake maneno haya, Nataka rehema, wala si sadaka, msingaliwalaumu wasio na hatia. <sup>8</sup> Kwa maana Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa sabato.

**12:1 "wakati ule"** mara nyingi waandishi wa injili walitumia wakati huu (na mwingine) kama njia ya kukusudia kwenda na mada mpya au tukio, sio ishara ya wakati halisi (kama vile Mt. 11:25; 12:1; Luka 10:21; 13:1; Mdo. 7:20; 12:1; 19:23).

☐ **" Yesu alipita katika mashamba siku ya sabato "** kitabu cha maadili na sheria za kiyahudi kinafundisha kwamba hatua zaidi ya 2,000 siku ya Sabato ilihesabiwa kuwa ni kazi na haikuruhusiwa. Inatia shauku kwamba makutano, katikati ya Mafarisayo na waandishi, walimfuata Yesu siku ya Sabato; hivyo basi, wao pia walikuwa na hatia kwa kuvunja sheria hii ya Sabato. Kwa ajili ya mjadala kamili wa asili na theolojia ya Mafarisayo, tazama muhtasari katika Mt. 22:15.

Waandishi wa injili walichagua matukio maalumU na mafundisho ambayo Yesu alitenda na kusema (kama vile. Yn. 20:30-31) kudhihirisha Agano Jipya na Umasihi wake na kazi. Takribani inaonekana kwamba hawa waandishi

walichagua ukabilianaji wa Sabato kama picha ya kuonyesha ni kwa namna gani Yesu anaweza kuikabili na kuhusika na viongozi wa kidini, madhehebu, na tamaduni za kitabu cha maadili na sheria za kiyahudi. Habari njema ya Yesu ilikuwa tofauti kutoka ushikiliaji mno wa sheria na taratibu za kitamaduni za kiyahudi (kama vile. Mt. 5:21-48).

## ▣ "Sabato"

### **MADA MAALUM: SABATO**

Hili linatokana na maana ya kiebrania "pumziko" au "kuacha kwa muda" (BDB 992). Linahusiana na siku ya saba ya uumbaji ambapo Mungu aliacha kazi zake baada ya kumaliza uumbaji wake wa mwanzo (kama vile Mwa. 2:1-3). Mungu hakupumzika kwa sababu alikuwa amechoka, lakini ni kwa sababu (1) uumbaji ulikuwa umekamilika na kuonekana unapendeza machoni pake (kama vile Mwa. 1:31) na (2) kumpa mwanadamu mwongozo kwa ajili ya ibada na pumziko. Utaratibu kama ilivyo siku ya kuabudu ulianza Mwa. 2:2-3, ambapo YHWH alitumia pumziko lake kama utaratibu kwa ajili ya wanyama (kama vile Kut. 23:12) na mwanadamu (binadamu huhitaji utaratibu wa kila mara wa kazi, pumziko, na ibada). Sabato ilianza kama ilivyo siku zote za mwanzo 1, jioni; kwa hiyo, Ijumaa jioni mpaka Jumamosi jioni ulikuwa ni muda rasmi kwa ajili ya sabato. Maelezo yote juu ya kuishika sabato yametolewa katika kitabu cha Kutoka (hasa katika sura 16; 20; 31; na 35) na Mambo ya Walawi (hasa sura ya 23-26). Hasa utumiaji wa kwanza wa siku hii kwa Waisraeli ilikuwa ni katika Kut. 16:25-26 kwenye kusanyiko la manna. Baadaye ikajakuwa sehemu ya "amri kumi" (kama vile Kut. 20:8-11; Kumb. 5:12-15). Huu ni mfano mojawapo ambapo Amri Kumi katika Kutoka 20 kwa kiasi kidogo zimetofautiana na zile zilizoko katika Kumbukumbu la Torati 5. Zile za Kumbukumbu la Torati lilimwandaa Mwisraeli kwa ajili ya makazi, maisha ya kilimo huko Kanaani.

Mafarisayo walizichukua hizi taratibu na, kwa majadiliano yao ya kusimuliana, wakazitafasiri kwa namna ya kuzitumia kwenye sheria nyingi. Yesu mara nyingi alitenda miujiza, akijua wazi anakwenda kinyume na sheria zao ili kwamba waweze kuingia kwenye mjadala. Ilikuwa sio sabato aliyoikataa Yesu, bali kujihesabia kwao haki na kukosekana kwa upendo.

▣ **"wakaanza kuvunja masuke, wakala"** kwa kawaida hili liliruhusiwa kihalali (kama vile Kumb. 23:25). Tatizo ni kwamba lilifanyika siku ya Sabato (kama vile Kut. 34:21). Kutoka baadhi ya ufupisho wa injili tunajifunza kwamba wanafunzi walikuwa na njaa. Kulingana na mbinu za walimu wa sheria ya kiyahudi, walikuwa na hatia kwa kuvunja sheria kadhaa: (1) mavuno, (2) njia, (3) kuandaa chakula siku ya Sabato na (4) yote haya na kufuata utaratibu wa kidini kwa mikono najisi.

**12:3 "Hamkusoma alivyotenda Daudi, alipokuwa na njaa"** tungo hii ya Yesu inathibitisha msukumo wa Agano la kale (kama vile Mt. 5:17-19). Kwa ajili ya tukio la kihistoria tazama 1 Samweli 21:1 na kuendelea.

**12:4 "nyumba ya Mungu"** mstari wa 4 ni dokezo la kihistoria la Hema la kukutania (kama vile Kutoka 25-30) la siku za Daudi akiwa angalia mdogo. Lakini pia inarejelea Hekalu lililojengwa baadae na Suleimani (kama vile Mt. 12:6). Ishara ya YHWH kukaa kati ya mbawa za makeribu juu ya sanduku la Agano. Mwanzo 1 yumkini ikawa ni miale ya YHWH kwenye Hekalu (tazama John L. Walton, *The Lost World of Genesis One*).

<b>NASB</b>	<b>"mkate mtakatifu"</b>
<b>NKJV</b>	<b>"mikate ya wonyesho"</b>
<b>NRSV</b>	<b>"mikate ya ahadi"</b>
<b>TEV</b>	<b>"mikate itolewayo kwa Mungu"</b>
<b>NJB</b>	<b>"mikate ya sadaka"</b>

Hii inarejelea "mikate ya wonyesho" au "mkate wa uwepo" ambao uliwekwa juu ya meza kwenye mahali patakatifu ndani ya Hema la kukutania na baadae Hekalu (kila mmoja ulikua na uzito wa paundi 12). Hii

inaonekana ni uwakilishi wa utoaji chakula wa YHWH na kuwajali watu wake, sio chakula kwa ajili YHWH! Ni mikate isiyotiwa chachu ambayo inayoturidisha nyuma katika Kutoka (kama vile Mwa. 15:12-21). Ulikuwa ni chakula kwa ajili ya makuhani kwa juma moja (kama vile Law. 24:5-9; Kut. 25:30). Mikate hii kumi na mbili ilibadilishwa kila juma moja. Hata hivyo, ikiwa na hali nzuri ya 1 Samweli 21, Daudi aliruhusiwa kula mikate hiyo.

**12:5 "makuhani hekaluni huinajisi sabato wasipate hatia"** Siku ya Sabato ilikuwa ni siku ya kazi kwa ajili ya makuhani (kama vile Hes. 28:9-10). Kitenzi hiki "huinajisi" ni dhahiri "kama walivyozoea kutenda." Inapatikana hapa pekee na Mdo. 24:6. Muundo wa Kiwakilishi nomino ni kwenye 1 Tim. 1:9.

**12:6 "Lakini nawaambieni, kwamba hapa yupo aliye mkuu kuliko hekalu"** baadhi ya machapisho yana kiume "mtu Fulani" (kama vile. Toleo la NKJV), lakini uthibitisho wa usomaji wa kale ni isio kuwa na jinsi, "baadhi ya kitu" (kama vile. Toleo la NASB, NRSV, TEV, JB). Hii inaonekana kurejelea ufalme wa Mungu, inarejea uficho wa Kimasihi (kama vile Mt. 12:28, 41-42). Hii lazima ilikuwa ni semi ya kushangaza kwa Wayahudi hawa.

Yesu alikuwa ni mkuu zaidi ya:

1. Hekalu, Mt. 12:6
2. Yona, Mt. 12:41
3. Suleimani, Mt. 12:42
4. Yakobo, Yn. 4:12
5. Yohana mbatizaji, Yn. 5:36
6. Ibrahimu, Yn. 8:53
7. Maandiko, Mt. 5:21-48; Marko 7:18-19

**12:7 "Lakini kama mngalijua maana yake maneno haya"** hii ni sentensi amrishi daraja la pili iitwayo "jambo la kinyume." Ufahamu wake ni "kama mngalijua (lakini bado hujatambua), hivyo msingewalaumu wasio na hatia (lakini mnalaumu)."

☐ **"Nataka rehema, wala si sadaka"** hii ni dondoo kutoka Hosea 6:6. Ni mfano wa manabii waliohubiri karne ya nane, ambao unatilia mkazo juu ya taratibu za ibada (kama vile. Mika. 6:6-8).

Kuelezea jambo hili kitheolojia nimehusisha mawazo yangu kutoka Hosea 6:6.

☐ **"nafurahia katika uaminifu zaidi ya sadaka"** Mungu anaangalia moyo! Shauku ndio ufunguo (kama vile. Yer. 9:24)! Huu ni ufunguo wa vifungu vya kitheolojia kwenye kitabu (kama vile Hos. 8:7; 11:12). "uaminifu" ulio sawa kama Hos. 6:4, lakini hapa ni maagano ya kweli/uaminifu. Yesu alitumia muktadha huu kwenye mjadala wake na Mafarisayo katika Mt. 9:13; 12:7. Hii haidokezi kwamba Mungu anawataka wasimamishe utowaji wa sadaka za kuteketezwa, lakini wawe makini na shauku ya haki (kama vile. 1 Sam. 15:22; Isa. 1:11-13; Yer. 7:21-23; Amosi 5:21-24; Mika 6:6-8). Kwa ajili ya mjadala bora tazama *Hard Sayings of the Bible*, uk. 207-208, 294-295). Utaratibu wa sadaka za kuteketezwa ulikuwa ni njia ya kuonyesha ukweli wa dhambi na mapenzi ya Mungu kumpokea mwenye dhambi katika uhusiano na yeye mwenyewe. Ilipogeuka kuwa utaratibu wa kidini bila kutubu, ilikuwa kichekesho, kizuizi cha kweli cha uhusiano wa mtu binafsi na Mungu."

**12:8 "Kwa maana Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa sabato"** huu lazima ulikuwa mshangao mkubwa kwa wayahudi ambao walitunza Sabato na tohara kwa ukaribu kabisa (kama vile. Marko 2:27). Yesu alidokeza ukweli huu alioutafsiriwa tena kutoka kwa Musa (kama vile Mt. 5:20-48). Watu wanapoinua kitu au mtu katika sehemu ya uaminifu wa juu kabisa badala ya Mungu mwenyewe (au Masihi wake), wanakuwa waabudu sanamu. Kwa ajili ya jina "mwana wa Adamu" tazama muhtasari katika Mt. 8:20.

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 12:9-14**

<sup>9</sup> Akaondoka huko, akaingia katika sinagogi lao. <sup>10</sup> Na tazama, yumo mtu mwenye mkono umepooza; wakamwuliza, wakisema, Ni halali kuponya watu siku ya sabato? Wapate kumshitaki. <sup>11</sup> Akawaambia, Ni mtu yupi miongoni mwenu mwenye kondoo mmoja, na yule kondoo ametumbukia shimoni siku ya sabato, asiye mshika akamwopoa? <sup>12</sup> Je! Mtu ni bora kuliko kondoo mara ngapi? Basi ni halali kutenda mema siku ya

**sabato.** <sup>13</sup> Kisha akamwambia yule mtu, Nyosha mkono wako; akaunyosha, ukapona, ukawa mzima kama wa pili. <sup>14</sup> Lakini wale Mafarisayo wakatoka wakafanya shauri juu yake jinsi ya kumwagamiza.

**12:10 "Ni halali kuponya watu siku ya sabato"** Swali hili kamwe haliuhusiki kwenye Agano la kale, lakini hatimaye Sabato ilikuwa sehemu ya mapokeo ya fasihi simulizi ambayo walimu wa sheria wa kale iliitafsiri maandiko ya Agano la kale (yaani, kuponya siku ya Sabato ni kwa ajili ya kuokoa maisha pekee). Malengo yalikua katika sheria za mwanadamu (kama vile. Isa. 29:13), sio mahitaji ya mwanadamu!

☑ **"Na tazama, yumo mtu mwenye mkono umepooza"** kutoka katika "injili ya Kiebrania" isiyothibitishwa tunajifunza utamadauni kwamba alikua ni mjenzi na kwamba ulikua ni mkono wa kulia uliopooza. Hivyo hakuweza kufanya kazi.

**12:11 "kondoo"** huu ni mojawapo kati ya mifano mingi ya mapokeo ya fasihi simulizi aliyekuwa mzigo badala ya furaha. Kondoo alikuwa na thamani zaidi kuliko wanadamu (kama vile Mt. 12:12).

☑ **"na"** hii sentensi amrishi daraja la tatu ambayo inaonyesha tendo linalowezekana.

**12:12** Yesu ametumia mazungumzo ya urasimishaji swali/jibu kwa washindani wake (kama vile Mt. 9:5; 12:12; 21:25; hata wanafunzi, Marko 8:17-18).

**12:14 "Mafarisayo wakatoka wakafanya shauri juu yake"** kutoka Marko 3:6 tunajifunza kwamba mashauriano yalifanywa kati ya Waherode na Mafarisayo, ambao kiotamaduni walikua ni maadui (kisiasa na kidini).

☑ **"Mafarisayo wakatoka wakafanya shauri juu yake"** viongozi hawa walijiona wao wenyewe kama walenzi wa YHWH! Inashangaza kwamba viongozi wa kidini waliona hakuna mgogoro kwenye mpango wao wa mauaji waliyodhamiria kwa kulinganisha na Yesu aliyedhaniwa kuvunja utaratibu wa kidini na Sabato (kama vile. Mt. 26:4; Luka 6:11; Yn. 11:53).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 12:15-21**

<sup>15</sup> Naye Yesu hali akiyafahamu hayo akaondoka huko; na watu wengi wakamfuata; akawa ponya wote, <sup>16</sup> akawakataza wasimdhahirisha; <sup>17</sup> ili litimie neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema,

<sup>18</sup> Tazama, mtumishi wangu niliyemteua;

Mpendwa wangu, moyo wangu uliyependezwa naye;

Nitatia roho yangu juu yake,

Naye atawatangazia Mataifa hukumu.

<sup>19</sup> Hatateta wala hatapaza sauti yake;

Wala mtu hasasikia sauti yake njiani.

<sup>20</sup> Mwanzi uliopondeka hatauvunja,

Wala utambi utokao moshi hatauzima,

Hata ailetapo hukumu ikashinda.

<sup>21</sup> Na jina lake Mataifa watalitumainia.

**12:15 "hali akiyafahamu hayo"** ni vigumu kuhakikisha chanzo cha ufahamu wa Yesu.

1. juu ya aliyosikia
2. alijua moyo wa mwanadamu
3. alijulishwa na Roho

Swali hili haliwezi kujibiwa kwa sababu ya muunganiko wa kipekee wa mwanadamu na Uungu wa Yesu (yaani, Kutwaa mwili).

☐ **"akawaponya wote"** kulikua na nguvu, huruma, na utimilifu wa unabii wa Agano la kale unaoelezwa kwenye tungo hii. Yesu aliwajali watu, watu wote. Ni lazima ikumbukwe kwamba uponyaji wa kimwili, hata wapunga pepo, hawakuhusika moja kwa moja kwa urejsho wa kiroho au wokovu.

Mistari inayoongelea huduma ya uponyaji wa Yesu inaeleza kwa mapana zaidi katika njia tofauti.

1. wakati mwingine ilisema "wote," (kama vile Mt. 8:16; 12:15; Luka 4:40; Mdo 10:38)
2. wakati mwingine ilisema kila "namna," sio kila "mmoja" (kama vile Mt. 4:23; 9:23)
3. wakati mwingine ilisema "wengi" sio "wote" (kama vile Marko 1:34; 3:10; Luka 7:21)
4. mara nyingi inadokeza kwamba aliwaponya wote (kama vile Mt. 14:14; 15:30; 19:2; 21:14)

**12:16 "akawakataza wasimdhahirishe"** hii inasimulia siri ya Masihi (hasa injili ya Marko). Yesu aliwasihi watu wasiiseme miujiza yake, lakini wadhahirishe ujumbe wake ambao bado uliokuwa kwenye utaratibu. Injili ilikua bado haijakamilika. Siri hii ya Masihi ni dhana iliyozeleka ya muhtasari (kama vile Mt. 8:4; 9:30; 17:9; Marko 1:44; 3:12; 5:43; 7:36; 8:30; 9:9; Luka 4:41; 8:56; 9:21). Yesu hakutaka ajulikane kama mponyaji mwingine anaезunguk!

**12:17 "nabii Isaya"** mistari ya 18-21 ni dondoo kutoka Isa. 42:1 na kuendelea. Haifuati maandiko ya Kiebrania ya Kimasoreti au tafsiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani kamili. Ni wazi inaonyesha hisia za Yesu masihi.

**12:18-21** hili ni dondoo kutoka Isa. 42:1-4 (lakini sio toleo la LXX), ambalo ni la kwanza katika "nyimbo za mtumishi" Isaya.

Tambua sifa za huyu ajae ambae anaonyeshwa kwa Yesu.

1. Ataitwa
  - a. mtumishi wangu (YHWH)
  - b. niliyemteua
  - c. mpendwa wangu
  - d. moyo wangu uliyependezwa naye (YHWH)
2. roho ya YHWH itatiwa juu yake
3. atawatangazia mataifa hukumu
4. sifa zake binafsi
  - a. hatateta
  - b. hatapaza sauti yake
  - c. wala mtu hatasikia sauti yake njiani
5. matendo yake binafsi
  - a. mwanzo uliopondeka hatauvunja
  - b. wala utambi utokao moshi hatauzim
  - c. hata ailetapo hukumu ikashinda
  - d. na jina lake mataifa watalitumainia

**12:18 "mtumishi wangu"** hiki ni cheo maalumu cha heshima (kama vile Mdo 3:13) walichotumia Musa, Yoshua, na Daudi kwenye Agano la kale. Kwa sababu ya mashairi maalumu kwenye Isa. 42:1-9; 49:1-7; 50:4-11; 52:13-53:12, ikaitwa "nyimbo za mtumishi," imechukua vidokezo vya masihi. Kipengele hiki cha masihi kinafikia kilele kwenye Isa. 52:13-53:12, "mtumishi atesekaye." Wayahudi siku za Yesu hawakumtarajia masihi ateswaye lakini Masihi mwenye nguvu za Uungu na kijeshi. Hii ndio maana inaelezwa ni kwa nini viongozi wa Kiyahudi hawakuupokea ujumbe wa Yesu (hata Yohana mbatizaji hakuelewa, kama vile Mt. 11:3).

Wayahudi mara zote walizitambua hizi nyimbo za mtumishi zilirejelea kwa taifa la Israeli na huu ni ukweli wa uhakika (kama vile Isa. 41:8; 42:1,19; 43:10; 49:3-6). Kwa vyovyote nyimbo hizi zilikuwa zinabainisha haki ya waisraeli (kama vile Isa. 52:14 (toleo la LXX), 15 (toleo la LXX); 53:1-12). Israeli walishindwa (kama vile Isa. 42:19; 53:8) kwenye jukumu lake ulimwenguni (kama vile Mwa. 12:3; Kut. 19:5-6) kwa sababu ya kuendelea kuvunja sheria za maagano ya Musa (kama vile Law. 26; Kumb. 27-28). Hivyo basi, badala ya Baraka, ulimwengu mzima uliiona hukumu ya Mungu. Hivyo basi, YHWH mwenyewe aliandaa maagano mapya yaliyolenga matendo yake na uaminifu (kama vile Ezek. 36:22-38).



☐ **"Mpendwa wangu, moyo wangu uliyependezwa naye"** tungo hii imetumika pia katika ubatizo na kubadilika sura ya Yesu (kama vile Mt. 3:17; 17:5). Baba amependezwa na huduma ya mwana. Jina hili linaunganisha utii unaotiliwa mkazo katika Zaburi 2 na mtumishi atesekaye katika Isaya 40-53.

Kutumika kwa "moyo" kumwelezea Mungu ni sitiari inayofafanua kwamba yeye ni kiumbe hai (kama vile Ebr. 10:38). Ufafanuzi huu wa Mungu kwenye maneno ya mwanadamu unaitwa anthropomorphism (nadharia ya kuelezea uungu kwa lugha ya kibinadamu). Tazama mada maalumu katika Mt. 6:4.

☐ **"Nitatia roho yangu juu yake"** umeona watu watatu katika utatu (Tazama Mada Maalumu katika Mt.3:17) kwenye dondoo kutoka katika Isa. 42:1?

Yesu na Roho wana muunganiko wa uhusiano wa kithiolojia. Tazama Mada Maalumu ifuatayo.

## **MADA MAALUMU: YESU NA ROHO**

Kuna bubujiko kati ya kazi ya Roho na Mwana. G. Campbell Morgan alisema jina zuri la Roho Mtakatifu ni "Yesu mwingine" (hata hivyo, tofauti yao, utu wa milele). Ufuatao ni mlinganisho wa mhutari wa kazi na wadhifa wa Mwana na Roho.

1. Roho aitwaye "Roho wa Yesu" au maelezo yanayofanana (kama vile Rum. 8:9; 2 Kor. 3:17; Gal. 4:6; 1 Pet. 1:11).
2. Wote wanaitwa kwa maneno sawa
  - a. "kweli"
    - 1) Yesu (Yohana 14:6)
    - 2) Roho (Yohana 14:17; 16:13)
  - b. "mwombezi"
    - 1) Yesu (1 Yohana 2:1)
    - 2) Roho (Yohana 14:16,26; 15:26; 16:7)
  - c. "Mtakatifu"
    - 1) Yesu (Marko 1:24; Luka 1:35; Matendo 3:14; 4:27,30)
    - 2) Roho (Luka 1:35)
3. Wote hukaa ndani ya waamini
  - a. Yesu (Mt. 28:20; Yohana 14:20,23; 15:4-5; Rum. 8:10; 2 Kor. 13:5; Gal. 2:20; Efe. 3:17; Kol. 1:27)
  - b. Roho (Yohana 14:16-17; Rum. 8:9,11; 1 Kor. 3:16; 6:19; 2 Tim. 1:14)
  - c. Baba (Yohana 14:23; 2 Kor. 6:16)
4. Kazi ya Roho ni kutoa ushuhuda juu ya Yesu (kama vile Yohana 15:29; 16:13-15)

**12:18,21 "Naye atawatangazia Mataifa hukumu . . . Na jina lake Mataifa watalitumainia"** maelezo kwamba ufalme umefunguliwa kwa waaminio wa mataifa yaliwashangaza sana Wayahudi (kama vile. Isa. 2:1-4; 45:22; 49:6; 60:3; 66:18,23; tazama maelezo ya Paulo katika Efe. 2:11-3:13).

**12:19 "Hatateta, wala hatapaza sauti yake"** hii inafafanua mbinu ya huduma ya Yesu kabla ya viongozi wa utawala wa Palestina (kama vile. Isa. 53:7) kama Pilato na Herode.

**12:20 "Mwanzi uliopondeka hatauvunja,**

**Wala utambi utokao moshi hatauzima,**

**Hata ailetapo hukumu ikashinda"** hii inaweza kumaanisha (1) Yesu anawatendea watenda dhambi na wenye upole au (2) ufalme wa Yesu unaonekana dhaifu na mdogo, lakini bado utaijaza ulimwengu na furaha (kama vile. Mt. 13:31-32).

**12:21 "na jina lake"** tazama mada maalumu katika Mt. 18:20.

☐ **"watalitumainia"** Hili ni shangazo pekee linalojitokeza neno "watalitumainia" kwenye Mathayo na hata hapa ni dondoo la Agano la kale kutoka Isa. 42:4. Limejitokeza mara tatu kwenye Luka (kama vile Luka 6:34; 23:8; 24:21). Neno limelenga katika matukio ya siku za mwisho kwenye maandiko ya Paulo, ambaye ameyatumia mara kumi na tisa.

### **MADA MAALUM: TUMAINI (elpis, kwa Paulo)**

Paulo alilitumia neno hili mara nyingi kwa namna tofauti lakini katika maana zinazoshabihiana. Mara nyingi lilihusiana na utimilifu wa imani ya waamini (mfano., 1 Tim. 1:1). Hili laweza kuellezewa kama utukufu, maisha ya milele, hatma ya wokovu, ujio wa mara ya pili, n.k. Utimilifu huu unajulikana, bali sula la muda ni mbeleni na halijulikani. Tumaini mara nyingi lilihusiana na "imani" na "upendo" (kama vile 1 Kor. 13:13; 1 The. 1:3; 2 The. 2:16). Orodha ya muda ya baadhi ya matumizi ya Paulo ni:

1. Ujio wa mara ya pili, Gal. 5:5; Efe. 1:18; 4:4; Tit. 2:13
2. Yesu ni tumaini letu, 1 Tim. 1:1 (Mungu ni tumaini letu, 1 Tim. 5:5; 1 Pet. 3:5)
3. Waamini kuwasilishwa mbele ya Mungu, Kol. 1:22-23; 1 The. 2:19
4. Tumaini likewekwa mbinguni, Kol. 1:5
5. Imani katika injili, Kol. 1:23; 1 The. 2:19
6. Hatma ya wokovu, Kol. 1:5; 1 The. 4:13; 5:8
7. Utukufu wa Mungu, Rum. 5:2, 2 Kor. 3:12; Kol. 1:27
8. Wokovu wa watu wa mataifa kupitia Kristo, Kol. 1:27
9. Uhakika wa wokovu, 1 The. 5:8
10. Maisha ya milele, Tit. 1:2; 3:7
11. matokeo ya ukomavu wa Mkristo, Rum. 5:2-5
12. ukombozi wa uumbaji wote, Rum. 8:20-22
13. kukubali utimilifu, Rum. 8:23-25
14. wadhifa wa Mungu, Rum. 15:13
15. shauku ya Paulo kwa waamini, 2 Kor. 1:7
16. agano la Kale kama mwongozo wa waamini wa Agano Jipya, Rum. 15:4

### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 12:22-24**

<sup>22</sup> Wakati ule akaletewa mtu mwenye pepo, kipofu, naye ni bubu; akamponya, hata yule bubu akanena na kuona. <sup>23</sup> Makutano wote wakashangaa, wakasema, Huyu siye mwana wa Daudi? <sup>24</sup> Lakini Mafarisayo waliposikia, walisema, Huyu hatoi pepo, ila kwa Beelzebuli mkuu wa pepo.

**12:22** Hii ni moja ya ishara za Kimasihi (kama vile. Isa. 29:18; 35:5; 42:7,16; Mt. 9:27-31; 12:22; 15:30; 21:14). Israeli nae alihitaji hii huduma ya uponyaji (kama vile Isa. 6:9-10 na 42:18-22). Ni ishara kwamba walikataa kuiona!

**12:23 "Huyu siye mwana wa Daudi?"** kwa Kiyunani, swali hili lilitalajiwa jibu la "hapana," lakini kwa uwezekano kwamba yumkini ikawa kweli. Neno hili "mwana wa Daudi" lilikuwa ni jina la Kimasihi kutoka 2 Samweli 7. Limetumika mara kwa mara na Mathayo (kama vile Mt. 1:1; 9:27; 12:23; 15:22; 20:30-31; 21:9,15; 22:42; pia muhtasari wa Ufu. 3:7; 5:5; 22:16).

**12:24 "Mafarisayo waliposikia, walisema"** hiki ni kiini cha dhambi isiyosamehewa, kufikiria kazi ya Mungu kuwa ya shetani na kuuita kwamba ukweli ndio uongo, na kwamba nuru ndio giza. Mafarisayo hawakukana nguvu za ajabu za Yesu walifikiria wao kuwa ni nguvu za mwovu (kama vile Mt. 9:32-34; Marko 3:22-30, Luka 11:14-26).

☐ **"Beelzebuli"** hii inarejelea kwa *Ba'al* (mungu mme wa uzao ya wakanani) wa mji wa *Zebub* (kama vile. 2 Fal. 1). Wayahudi kwa dharau walibadili jina kua *Ba'al wa Zebul* lililomaanisha "bwana wa mavi" au "bwana wa inzi."

Neno hili lina herufi tofauti kwenye maandiko ya kale. *Zebul* ni katika tafsiri za toleo la Vulgate kilatini na toleo la Peshitta, ambapo neno *Zebub* liko kwenye machapisho yote ya Kiyunani. Ni jina kwa ajili ya shetani. Na baadae katika Uyahudi, *Zebul* alikuwa ni mkuu wa pepo wabaya.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 12:25-30**

<sup>25</sup> Basi Yesu akijua mawazo yao, akawaambia, Kila ufalme ukifitinika juu ya nafsi yake, hufanyika ukiwa; tena mji au nyumba yo yote ikifitinika juu ya nafsi yake, haitasimama. <sup>26</sup> Na Shetani akimtoa Shetani, amefitinika juu ya nafsi yake; basi ufalme wake utasimamaje? <sup>27</sup> Na mimi nikitoa pepo kwa Beelzebuli, je! Wana wenu huwatoa kwa nani? Kwa sababu hiyo hao ndio watakaowahukumu. <sup>28</sup> Lakini mimi nikitoa pepo kwa Roho wa Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia. <sup>29</sup> Ama awezaje mtu kuingia ndani ya nyumba ya mtu mwenye nguvu na kuviteka vyombo vyake, asipomfunga kwanza yule mwenye nguvu? Ndipo atakapoiteka nyumba yake. <sup>30</sup> Mtu asiye pamoja nami yu kinyume changu; na mtu asiyekusanya pamoja nami hutapanya.

**12:25-32** Yesu alitumia mantiki, hoja yenye mantiki kuonyesha mzaha uliodaiwa na Mafarisayo (kama vile. Marko 3:23-27; Luka 11:17-22). Kuna mifano minne iliyotumika: (1) Mt. 12:25; (2) Mt. 12:27; (3) Mt. 12:28; na (4) Mat. 12:29. Kuna mfuatano wa sentensi amrishi daraja la kwanza, ambao kwa hakika unasadiki ukweli wa taswira ya mwandishi au kwa ajili ya makusudi ya fasihi, lakini hapa ni waongo (Mt.12:26 na 27). Hata hivyo, sentensi amrishi daraja la kwanza kwenye Mt. 12:28 ni uhalisia wa ukweli! Muktaadha, muktaadha, muktaadha!

**12:25 "akijua mawazo yao"** haina uhakika kama Yesu alitumia uwezo wake wa nguvu za Uungu kujua mawazo ya watu au kama aliwaona wakiongea na kusikia bila kukusudia mawazo yao (kama vile Mt. 9:4). Tazama muhtasari katika Mt. 12:1.

☑ **"Yesu"** machapisho ya kale zaidi ya Kiyunani yameliacha jina hili (yaani, P<sup>21</sup>, α, B, D, na baadhi ya kilatini cha kale, shamu, na machapisho ya Koptiki).

**12:27**

**NASB** "Wana wenu huwatoa kwa nani"

**NRSV** "ninyi wenyewe wapunga pepo huwatoa kwa nani"

**TEV** "nani amewapa nguvu wafuasi wenu kuwatoa"

**NJB** "kupitia nani mnapata ujasiri wa kuwatoa"

Wayahudi (yaani, "wana wako") walizoea upungaji pepo kwa njia ya uchawi na viapo (kama vile Marko 9:38; Mdo. 19:13). Uhusiano usio wa kawaida kwenye Mat. 12:43-45 unaonekana kusimulia upungaji pepo huu wa Kiyahudi ambao ulitoa nje pepo wabaya, lakini hawakuweka imani katika Mungu, wakiuacha utupu wa kiroho.

**12:28 "lakini. . . basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia "** hii ni sentensi amrishi daraja la kwanza, inasadiki kuwa kweli na mwandishi kwa ajili ya makusudi ya fasihi. Hii ni rejea nyingine ya uficho wa kimasihhi. Pia ni jambo kuu lisilo la kawaida kwa Mathayo kutumia tungo "ufalme wa Mungu," ambalo kwa kawaida linapatikana kwenye Marko na Luka. Mathayo kwa kawaida ametumia tungo "ufalme wa mbinguni." Kuna mambo manne ya kipekee: (1) kifungu hiki; (2) Mt. 19:24; (3) Mt. 21:31; na (4) Mt. 21:43. Yesu anatetea kwamba utoaji wake pepo unaelezea wazi kwamba nguvu zake za Kimasihhi zinathibitisha enzi mpya ya Roho! Tazama mjadala mfupi mzuri wa "uelewa wa matukio ya siku za mwisho" kwenye F. F. Bruce, *Answers to Questions*, uk. 198. Tazama [MADA MAALUMU: UFALME WA MUNGU](#) katika Mt. 4:17.

**12:29** mstari huu mara nyingi umetumika kusaidia mazoezi ya kumtoa shetani nje ya huduma ya kuabudu.

Lakini kwenye muktaadha huu hili sio andiko la "ahadi" linalotumika kushirikiana upungaji pepo. Waaminio hawakupewa mamlaka ya kuungana na shetani (yaani, "mtu mwenye nguvu"). Hata malaika mkuu Mikaeli wa Israeli hakuongea dhidi ya shetani kwa ajili hukumu (kama vile. Yuda 9). Mitume na wale sabini walipewa nguvu za kutoa pepo wabaya (kama vile Mt. 10:1; Luka 10:17-20). Hata hivyo, hili halikutajwa kamwe miongoni mwa

vipawa vilivyotolewa na Roho kwa ajili ya kanisa. Mfano huu unafanana na ule wa kwenye Marko 3:22-27 na Luka 11:21-23.

**12:30 "Mtu asiye pamoja nami yu kinyume changu"** kwa uwazi, chaguo la muhimu ni lazima lifanywe (kama vile. Marko 9:40; Luka 9:49, 50; 11:23). Yesu amelea enzi mpya, mwanadamu ni lazima amwitikie yeye. Sio kuitikia ni kuchagua!

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 12:31-32**

<sup>31</sup> Kwa sababu hiyo nawaambia, Kila dhambi na kila neno la kufuru watasamehewa wanadamu, ila kwa kumkufuru Roho hawatasamehewa. <sup>32</sup> Naye mtu ye yote atakayenena neno juu ya Mwana wa Adamu atasamehewa, bali yeye atakayenena neno juu ya Roho Mtakatifu hatasamehewa katika ulimwengu wa sasa, wala katika ule ujao.

**12:31-32** Hii rejea ya kufuru dhidi ya Roho mara nyingi huitwa "dhambi isiyosamehewa." Kutoka mfanano wa kwenye Marko 3:28 ni wazi kwamba "mwana wa Adamu" kwenye muktadha huu halikua jina la Yesu lakini kwa ujumla imetumia nahau ya Kiebrania "wana wa mtu" au "mwanadamu." Hii inasaidiwa na mfanano wa Mt. 12:31 na 32. Dhambi iliyojadiliwa sio dhambi ya ujinga lakini ni ya kutamani kumkataa Mungu na kweli yake katika uwepo wake wa nuru kuu. Watu wengi wana wasiwasi kama wametenda dhambi hii. Watu wanaotamani kumjua Mungu au wana hofu kwamba hawajatenda dhambi hii! Dhambi hii imeendelea kumkataa Yesu kwenye uwepo wa nuru kuu, inalenga uchanga wa kiroho. Hii inafanana na Ebr. 6:4-6 na 10:26-31.

#### **MADA MAALUMU: HULKA YA ROHO**

Kwenye Agano la Kale "Roho wa Mungu" (yaani *ruach*) ilikuwa nguvu iliyotimiza kusudi la YHWH, lakini kuna kidokezo kwamba alikuwa mtu binafsi (yaani Mungu mmoja, tazama Mada Maalumu: U-Mungu mmoja). Hata hivyo kwenye Agano Jipya ukamilifu wa nafsi ya ubinadamu na utu wa Roho umefunuliwa:

1. Anaweza kufanyiwa kufuru (kama vile Mt. 12:31; Marko 3:29)
2. Hufundisha (kama vile. Luka 12:12; Yohana 14:26)
3. Hushuhudia (kama vile Yohana 15:26)
4. Ana hukumu, anaongoza (kama vile Yohana 16:7-15)
5. Anaitwa "ambaye" (yaani, *hos*, kama vile Efe 1:14)
6. Anaweza kuhuzunishwa (kama vile Efe. 4:30)
7. Anaweza kuzimishwa (kama vile 1 The. 5:19)
8. Anaweza kupingwa (kama vile Matendo 7:51)
9. Anawatetea waaminio (kama vile Yohana 14:26; 15:26; 16:7)
10. Humtukua Mwana (kama vile Yohana 16:14)

Maandiko ya utatu (hapa yapo matatu mioongoni mwa mengi, tazama Mada Maalumu: Utatu) pia anazungumza juu ya watu watatu.

1. Mt. 28:19
2. 2 Kor. 13:14
3. 1 Pet. 1:2

Ingawa neno la Kiyunani "roho" (*pneuma*) ni sio na jinsi wakati linapohusika Roho, Agano Jipya kila mara hutumia KIVUMISHI KIONYESHI CHA JINSIA YA KIKE (kama vile Yohana 16:8,13-14).

Roho anahusishwa na shughuli za binadamu.

1. Matendo 15:28
2. Rum. 8:26
3. 1 Kor. 12:11
4. Efe. 4:30

Mwanzoni kabisa mwa matendo, jukumu la roho lina sisitizwa (kama katika injili ya Yohana). Pentekoste haikuwa mwanzo wa kazi ya Roho bali, sura mpya. Yesu kila wakati alikuwa na Roho. Ubatizo wake haukuwa

mwanzo wa kazi ya Roho bali mwanzo wa sura mpya. Roho ndio njia yenye nguvu ya makusudi ya Baba kwa sura yake (tazama Mada Maalumu: Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH)!

☐ "ulimwengu wa sasa, wala katika ule ujao"

## MADA MAALUMU: ENZI HII NA ENZI IJAYO

Manabii wa Agano la Kale waliutazama wakati ujao kama upanuzi wa wakati uliopo. Kwao wakati ujao utakuwa marejesho ya Israeli ya kijiografia. Hata hivyo, hata wao waliuona kama siku mpya (kama vile Isa. 65:17; 66:22). Kwa kwendelea kukataliwa YHWH kwa makusudi na uzao wa Abraham (hata baada ya uhamisho) ni kielelezo kiliicho dhihirika ndani ya hati ya Kiyahudi ya fasili ya mambo ya ufunuo wa matukio ya siku za mwisho (yaani, I Enoch, IV Ezra, II Baruch). Maandishi haya yanatengeneza utofauti kati ya zama hizi mbili: zama za uovu za sasa zinazomilikiwa na Shetani na zama zijazo za haki zinazomilikiwa na Roho na zilizozinduliwa na Masihi (apiganaye mwenyewe mara kwa mara).

Katika eneo hili la theolojia (hukumu, kifo na peponi) kuna maendeleo ya dhairi. Wanatheolojia wanalihita hili "ufunuo endelevu." Agano Jipya linakubaliana na ukweli huu mpya wa kiulimwengu wa zama hizi mbili (yaani, nyakati mbili

Yesu	Paulo	Webrania (Paulo)
Mt. 12:32; 13:22,39	Warumi 12:2	Ebr.1:2; 6:5; 11:3
Marko 10:30	1 Kor. 1:20; 2:6,8; 3:18	
Luka 16:8; 18:30; 20:34-35	2 Kor. 4:4	
	Wagalatia 1:4	
	Efe. 1:21; 2:2,7; 6:12	
	1 Timotheo 6:17	
	2 Timotheo 4:10	
	Tito 2:12	

Katika thiolojia ya Agano Jipya zama hizi za Kiyahudi zimekuwa zikipishana kwa sababu ya tabiri zisizotarajiwa na ambazo hazikutiliwa maanani zilizohusu kuja kwa Masihi. Kuonekana kwa Yesu katika umbile la mwili kulitimiza unabii mwingi wa Agano la Kale uliohusu utambuzi wa zama mpya (Dan. 2:44-45). Hata hivyo, Agano la Kale pia liliutazama ujio Wake kama Hakimu na Mshindi, bado alikuja kwa mara ya kwanza kama Mtumishi Ateswaye (kama vile Isaya 53; Zek. 12:10), mnyenyekevu na mpole (kama vile Zekaria 9:9). Atarudi katika nguvu ile ile kama Agano la Kale lilivyotabiri (kama vile Ufunuo 19). Utimilifu wa zama hizi mbili ulisababisha Ufalme kuwepo (uliotambuliwa), lakini zile zijazo (hazijatimilika ipasavyo). Huu ni mvutano wa Agano Jipya wa uliopo tayari, lakini bado!

## ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 12:33-37

<sup>33</sup> Ufanyeni mti kuwa mzuri na matunda yake kuwa mazuri; au ufanyeni mti kuwa mbaya na matunda yake mabaya, kwa maana kwa matunda yake mti hutambulikana. <sup>34</sup> Enyi wazao wa nyoka, mwawezaje kunena

mema, mkiwa wabaya? Maana, kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake.<sup>35</sup> Mtu mwema katika akiba njema hutoa mema; na mtu mbaya katika akiba mbaya hutoa mabaya.<sup>36</sup> Basi, nawaambia, Kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu.<sup>37</sup> Kwa kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa.

**12:33 "kwa maana kwa matunda yake mti hutambulikana"** anatenda, kama anavyosema, anajifunua mwenyewe. Tazama muhtasari katika Mat. 7:16.

**12:34 "Enyi wazao wa nyoka"** Yesu katika siku zake alitumia lugha kali kwa ajili viongozi wa kidini. Kwa mtazamo huu makini alifuata mahubiri ya Yohana mbatizaji (kama vile. Mat. 3:7). Nyoka wa kwenye kitabu cha Mwanzo 3 anaweza kuwa chanzo cha sitiari hii (kama vile Ufu. 12:9; 20:2).

☐ **"Maana, kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake"** sio kile kimwingiacho mtu, lakini ni kile kintokacho, ndicho najisi (kama vile Marko 7:17-23). Wanadamu hujifunua wenyewe kwa jinsi wanavyoongea. mazungumzo ni sehemu ya sura ya Mungu. Mazungumzo hufunua moyo (kama vile. Mat. 7:116,20; Luka 6:44; Yakobo 3:12). Tazama [MADA MAALUM: KAULI YA MWANADAMU](#) katika Mt. 15:19.

**12:35** Hii "hazina" inarejelea sehemu ya ndani ya mtu binafsi (kama vile Luka 6:45).

**12:36 " watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu "** Yesu alirudia kuongea juu ya hukumu na matokeo yake ya umilele (kama vile. Mathayo 7; 25). Hii inasimulia kwa wale wote wanaomkataa Yesu. Maisha yao, vipaumbele vyao, na maneno huaksi chaguzi zao za kiroho (kama vile Mt. 12:37).

**12:37** tazama [MADA MAALUM: KAULI YA MWANADAMU](#) katika Mt. 15:19.

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 12:38-42

<sup>38</sup> Hapo baadhi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu, wakasema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako.<sup>39</sup> Akajibu, akawaambia, Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara, wala hakitapewa ishara, ila ishara ya nabii Yona.<sup>40</sup> Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.<sup>41</sup> Watu wa Ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, nao watawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona.<sup>42</sup> Malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani, na hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.

**12:38 "waandishi"**

#### MADA MAALUM: WAANDISHI

Hili jina linatokana na nomino ya Kiebrania (BDB 706, KB 767) ambayo inamaanisha "ujumbe uliozungumzwa," "kumbukumbu iliyoandikwa/amri" (KB 766). Tafsihi ya Kiyunani grammateus (Agano la Kale la Kiebrania-LXX) mara nyingi hurejelea ujumbe ulioandikwa. Jina hili linaweza kudokeza

1. mwelimishaji (Nehemia 8)
2. mtawala wa kiserikali (2 Fal 22:3-13)
3. mchukua kumbukumbu/mhazili (1 Nya. 24:6; 2 Nya. 34:13; Yer. 36:22)
4. mkuu wa majeshi (kama vile Amu. 5:14)
5. kiongozi wa kidini (yaani, Ezra, Ezra 7:6; Neh. 12:12-13)

Katika Agano Jipya mara nyingi hawa wanahusiana na Mafarisayo (tazama Mada Maalum: Mafarisayo). Katika maana iliyo dhahiri hawa walikuwa watu waliokuwa wameelimishwa katika Agano la Kale na katika ustadi wa Masimlizi (yaani, Buku la Sheria za Kiyahudi). Hawa walisaidia kufasiri na kutumia desturi za Kiyahudi kila siku (kama vile Sira 39:6). Kwa uwazi kabisa waandishi pia waliitwa "wanasheria" (kama vile Marko 12:28; Luka 7:30; 10:25; 11:45; 14:3). Hata hivyo, haki yao (yaani, ushikiliaji sana wa sheria za Kiyahudi na taratibu) kusikungeleta amani kwa Mungu (kama vile Mt. 5:20; Rum. 3:19-20; 9:1-5,30-32; 10:1-6; Kol. 2:20-22).

Mara nyingi hawa walikuwa wakitabiri katika injili za ki-Muhtasari (Yohana hawataji kamwe, Yohana 8:3 si halisi), kama walivyompinga Yesu, na kwa uwazi kabisa kuja kama wakuu toka Yerusalemu (kama vile Marko 3:22; 7:1). Wengine, hata hivyo, walimtii (kama vile Mt. 8:19).

1. mgogoro kuhusu kula pamoja na watenda dhambi na watoza ushuru, Marko 2:16; Mt. 9:9-13
2. mgogoro kuhusu chimbuko la mamlaka ya Yesu katika upungaji pepo, Marko 3:22
3. mgogoro kuhusu kusamehe dhambi, Mt. 9:3; Luka 5:21
4. dai la ishara zishangazazo Mt. 12:38
5. mgogoro kuhusu kunawia mikono (yaani, taratibu za unawaji), Mt. 15:1-2; Marko 7:1-5
6. mgogoro kuhusu kukubaliwa kwake na umati katika kuingia kwa shangwe humo Yerusalemu, Mt. 21:15
7. sababu mashtaka ya Yesu (yaani, kutafuta heshima na ukuu), Marko 12:38-40
8. shutuma za Yesu kuhusu wao kuwa na miongozo ya kinafikiri na ya kiupofu katika kiti cha Musa, Mt. 23:1-36

Kwa sababu ya ufahamu wao wa Maandiko, kwanza wangetakiwa kuwa wamekwisha mgundua na kumshikilia Yesu, lakini desturi zao (kama vile Isa. 29:13; 6:9-10) zilikuwa zimewapofusha! Nuru ilipogeuka kuwa giza, tazama jinsi giza lilivyo kuu!

☐ **"twataka kuona ishara kwako"** walisikia mafundisho ya Yesu na kuona uponyaji na kuwatoa pepo wabaya aliotenda Yesu, lakini walitaka ishara zaidi ili kuwashawishi wamwamini yeye. Haya ni majaribu ya wazi katika Mt. 4:5-7 ambayo Yesu hakushindwa. Hata hivyo, kwa uwazi, aliwapa ishara baada ya ishara lakini hawakuweza au hawakuona (yaani., Isa. 6:9-10)!

**12:39 "zinaa"** zinaa imekua sitiari kwa ajili ya kutokuwa mwaminifu (kama vile. Law. 20:5; Hes. 25:1; Hos. 1:2; 4:10,18; 5:3; Mt. 16:4; Marko 8:38; Yakobo 4:4).

☐ **"ila ishara ya nabii Yona"** kama vile Yona akivyokuwa siku tatu katika tumbo la Nyangumi, Yesu alikaa siku tatu kaburini (kuzima). Ni lazima tukumbuke kwamba hizi ni siku tatu kwa hesabu ya Kiyahudi, sio nyakati za saa Ishirini- nne. Kila sehemu yoyote ya siku, ambayo kwao ilikuwa ni jioni hata jioni (kama vile Mwanzo 1), ilihesabiwa kama siku nzima. Dokezo la Yesu kwa Yona ni kuthibitisha historia imara ya kitabu cha Yona. Ni kwa usahihi kabisa kwamba ufahamu kwenye tumbo la Nyangumi umetumika kama mfano (kama vile Mt. 16:4).

**12:40 "siku tatu"** tazama muhtasari katika Mt. 16:21.

☐ **"katika moyo wa nchi"** hii inarejelea kushuka *Hades (kuzimu)* (kama vile. Mat. 11:23), ufalme wa kifo, kaburi, au sitiari ya mahali watoto wasiozaliwa (kama vile Zab. 139:15-16). Hii ni lugha ya ajabu: lugha ya kuangalia na maelezo yaliyozoeleka kwa mwanadamu. Wayahudi, kama sisi, walizika watu waliokufa, hivyo basi, "waliishi" kwenye ardhi. Tazama [MADA MAALUM: Wafu wako wapi?](#) Katika Mt. 5:22.

Maneno ya Yesu hayakufahamika kwa wakati ule ule na wasikilizaji wake hata mpaka baada ya ufufuo wake. Mathayo ana muundo wa semi za Yesu kwa ajili ya makusudi ya kitheolojia, sio mfuatano wa umri wa makuzi (kama vile Mt. 7:21-23, pia inaweza isiwe na maana hadi muda wa baadae zaidi).

**12:41 "Watu wa Ninawi "** hii pia inasimuliwa katika Mt. 11:20-24, kama vile Mt. 12:42. Watu wa Ninawi walitubu kwa mahubiri ya Yona na matokeo yake hasira ya hukumu ya Mungu ikazuiliwa juu yao. Hii pia inadokeza kwamba watu wa Ninawi siku za Yona walikua hai baada ya kufa kwao.

☐ **"walitubu"** tazama [MADA MAALUM: TOBA KATIKA AGANO LA KALE](#) katika Mt. 3:2 na tazama muhtasari katika Mt. 4:17.

**12:42 "Malkia wa kusini"** hii inarejelea njia ya Malkia wa Sheba (kama vile. 1 Fal 10:1-15), ambaye bado angali hai na atatokea ili kushudia kwenye matukio ya siku za mwisho.

☐ **"hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani"** hili ni dai jingine la wazi la kimasihhi. Linafunua ufahamu binafsi wa Yesu. Aliona yeye kuwa ni mkuu zaidi kuliko mtu mwenye hekima huko mashariki ya kale (kama vile 1 Fal. 3:12; 4: 19-34). Tazama muhtasari kamili katika Mt. 12:6.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 12:43-45**

<sup>43</sup> Pepo mchafu, amtokapo mtu, hupitia mahali pasipo maji, akitafuta mahali pa kupumzika, asipate. <sup>44</sup> Halafu husema, Nitarudi nyumbani kwangu nilikotoka; hata akija, aiona tupu, imefagiwa, na kupambwa. <sup>45</sup> Mara huenda, akachukua pamoja naye pepo wengine saba walio waovu kuliko yeye mwenyewe, nao huingia na kukaa humo; na mtu yule hali yake ya mwisho huwa mbaya kuliko ya kwanza. Ndivyo itakavyokuwa kwa kizazi hiki kilicho kibaya.

**12:43 "Pepo mchafu"** tazama mada maalumu mbili : pepo wabaya (pepo mchafu) katika Mt. 10:1.

☐ **"mahali pasipo maji"** kwenye Agano la kale jangwa yalikuwa ni makazi ya pepo wabaya (yaani, Azazeli kwenye Law 16 na wanyama wa jangwani kwenye Isa. 13:21; 34:14).

**12:44-45** kifungu hiki kinawezekana kina maana tatu.

1. mpungaji pepo wa Kiyahudi alitoa pepo bila kuwa na imani binafsi, na roho ya pepo mchafu ikarudi
2. ni dokezo kwa taifa la Israeli kwa maana ya kukataa ibada ya sanamu, lakini bila kuweka imani yenye mahusiano kwa YHWH
3. inarejelea mahubiri ya Yohana mbatizaji, wanaompokea kama aliyetoka kwa Mungu, ambapo wanamkataa Yesu

Hali yake ya mwisho huwa mbaya zaidi kuliko ya kwanza (kama vile 2 Pet. 2:20-22).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 12:46-50**

<sup>46</sup> Alipokuwa katika kusema na makutano, tazama, mama yake na ndugu zake walikuwa wakisimama nje, wataka kusema naye. <sup>47</sup> Mtu mmoja akamwambia, Tazama, mama yako na ndugu zako wamesimama nje, wanataka kusema nawe. <sup>48</sup> Akajibu, akamwambia yule aliyempasha habari, Mama yangu ni nani? Na ndugu zangu ni akina nani? <sup>49</sup> Akawanyoshea mkono wanafunzi wake, akasema, Tazama, Mama yangu na ndugu zangu! <sup>50</sup> Kwa maana ye yote atakayeyafanya mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni, huyu ndiye ndugu yangu, na umbu langu, na mama yangu.

**12:46 "mama yake na ndugu zake walikuwa wakisimama nje"** Ni dhahili walifikiria Yesu alifanya kazi sana au amekuwa sio wa utamaduni (kama vile. Marko 3:20-21).

**12:47** Mstari huu hauko pamoja kwenye machapisho ya Kiyunani  $\alpha$ , B, na L au kwenye Kilatini cha kale, Shamu, na machapisho ya Koptiki. Unahusiana kwenye machapisho ya  $\kappa^c$ , C, na D na toleo la Vulgate na toleo la Diatessaron. Unapatikana pia kwenye Marko 3:32 na Luka 8:20. Inaonekana kwamba waandishi waliongeza kwenye huu mstari ili kufanya mistari mitatu. Inahusiana kwenye fafsiri za matoleo ya NASB, NKJV, NRSV, na TEV. Toleo la kamati ya tafsiri la United Bible Societies Fourth Edition agano jipya la kiyunani wanaamini kwamba ni kwa makosa



maandiko yaliachwa kwa sababu ya kosa dogo la macho (*homoloteleuton*) kati ya maneno mawili yanayofanana ("kiongea") kwenye andiko la mwisho la Kiyunani katika Mt. 12:46 na 47. Mstari unahitajika ili kukipatia kifungu maana.

**12:50 "Kwa maana ye yote atakayeyafanya mapenzi ya Baba yangu"** mapenzi ya Mungu ni kutubu na kumwamini yeye aliyetumwa (kama vile Yohana. 6:39-40). Mmoja anapookolewa, Mapenzi ya Mungu pia ni kwa ajili ya kila mwaamini kufanana na Kristo, (kama vile Rum. 8:28-29; Gal. 4:19). Tazama mada maalumu: mapenzi ya Mungu katika Ma. 7:21.

Toleo la NIDOTTE, juzuu. 1, ukr. 488, lina maelezo mazuri juu ya wito wa Yesu kuwa mwanafunzi.

1. Sadaka isiyo na masharti kwa maisha ya mtu mmoja (kama vile Mt. 10:37; Luka 9:59-62; 14:26-27)
2. Sadaka isiyo na masharti kwa ajili maisha yote ya mtu (kama vile Mt. 16:24-25; Yn. 11:16)
3. Kufungamana na Yesu na kuyatenda mapenzi ya Mungu (kama vile Mt. 12:46-50; Marko 3:31-35)

Wito wa kumfata Yesu ni wito wa muhimu kwa kujikana binafsi ambao unathibitisha kurudishwa baada ya matokeo ya anguko! Haya ni maisha marefu, maisha pamoja na wito!

☑ **"aliye mbinguni"** hii ni dhana inayojirudia kwenye Mathayo (kama vile Mt. 5:16,45; 6:1,9; 7:11,21; 10:32-33; 12:50).

☑ **"huyu ndiye ndugu yangu, na umbu langu, na mama yangu"** imani katika Kristo zinafungamanisha familia ulimwenguni (inafanana na kwenye Marko 3:31-35). Ukristo ni familia iliyo na msingi wa Ubaba wa Mungu Udugu wa Yesu (kama vile Rum. 8:15-17).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Yesu alithibitisha sheria za Agano la kale kwenye Mathayo 5:17-21 na bado akayakataa mapokeo ya fasihi simulizi yaliyowaelemea wayahudi?
2. Je alitangaza kuwa Masihi kwenye Mathayo 12?
3. Je Yesu alitenda miujiza hii kwa kuwakabili au kwa kuwajibu Mafarisayo?
4. Ni kwa namna gani Isaya 42:1-4 inaeleza huduma ya Masihi?
5. Fafanua/eleza Mafarisayo kumuita Yesu Beelzebuli.
6. Kuzimu ni nini na iko wapi?
7. Elezea mfano uliopo kwenye mistari ya 43-45.

## MATHAYO 13

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Mfano wa Mpanzi 13:1-9	Mfano wa Mpanzi 13:1-9	Kufundisha kwa Mifano 13:1-9	Mfano wa Mpanzi 13:1-3a 13:3b-9	Utangulizi 13:1-3a  Mfano wa Mpanzi 13:3b-9
Kusudi la Mfano  13:10-17  (14b-15)	Kusudi la Mifano  13:10-17	  13:10-17	Kusudi la Mifano  13:10 13:11-15  13:16-17	Kwanini Yesu Alizungumza kwa Mifano 13:10-15  (14b-15) 13:16-17
Mfano wa Mpanzi Unaelezwa 13:18-23	Mfano wa Mpanzi Unaelezwa 13:18-23	  13:18-23	Yesu anaelezea Mfano wa Mpanzi 13:18-23	Mfano wa Mpanzi unaelezwa 13:18-23
Mfano wa magugu Kati ya Ngano 13:24-30	Mfano wa ngano Na Magugu 13:24-20	Magugu katika Ngano 13:24-30	Mfano wa Magugu 13:24-30	Mfano wa Magugu 13:24-30
Mfano wa Punje Ya haradali na Chachu 13:31-32	Mfano wa Punje ya Haradali  13:31-32 Mfano wa Chachu	Punje ya Haradali  13:31-32 Chachu	Mfano wa Punje Ya haradali  13:31-32 Mfano wa Chachu	Mfano wa Punje Ya Haradali  13:31-32 Mfano wa Chachu
13:33 Matumizi ya  13:34-35 (35b)	13:33 Unabii na Mifano  13:34-35	13:33  13:34-35	13:33 Matumizi ya mifano Ya Yesu  13:34-35	13:33 Watu Wanafundishwa Kwa mifano tu 13:34-35 (35b)
Mifano ya Magugu Inaelezwa 13:36-43	Mfano wa Magugu unaelezwa 13:36-43	  13:36-43	Yesu anaelezea mfano wa magugu 13:36 13:37-43	Mfano wa magugu unaelezwa 13:36-43
Mifano Mitatu  13:44	Mifano ya Hazina Iliyofichwa 13:44 Mfano wa lulu Ya thamani kuu	Hazina Iliyofichwa 13:44 Lulu ya thamani kuu	Mfano wa Hazina iliyofichwa 13:44 Mfano wa lulu	Mfano wa Hazina na lulu 13:44
13:45-46	13:45-46 Mfano wa Javu	13:45-46 Javu	13:45-46 Mfano nyavu	13:45-46 Mfano wa nyavu
13:47-50	13:47-52	13:47-50	13:47-50	13:47-50 Hitimisho
13:51-52		13:51-53	13:51a 13:51b 13:52	13:51-52
Kukataliwa kwa	Yesu anakataliwa	Kukataliwa nyumbani	Yesu anakataliwa	Safari kuelekea

Yesu Nazareti 13:53-58	Nazareti 13:53-58		Nazareti 13:53-57a	Nazareti 13:53-58
		13:54-58		
			13:57b-58	

## **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka “[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)”)**

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuwiwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Ayayapili
3. Ayatatu
4. N.k

## **HISTORIA YA NYUMA YA MATHAYO 13:1-58**

A. Uelewa wa mifano ulikuwa na unahusiana na kutanguliwa na kujitoa kiimani. Hata Mitume mwanzoni hawakuyaelewa mafundisho ya Yesu (na kuendelea Marko 4:13,40; 6:52; 7:18; 8:17,21,33; 9:10,32). Kwa namna Fulani uelewa unategemeana juu ya

1. Uchaguzi
2. uwezo wa nguvu ya nuru ya Roho
3. utayari wa kutubu na kuamini (yaani, Isa. 6:9-10; 30:6)

Uelewa unajumuisha kuwezesha kiungu na mwikio wa imani ya kibinadamu.

B. "mfano" ni neno ambatani katika maana ya Kiyunani "kutupa kando." Kutokea kulikozoeleka kulitumika kuelezea kweli za kiroho. Hata hivyo lazima ikumbukwe kwamba kwa waandishi hawa wa Kiyahudi neno hili la Kiyunani liliaki *mashal* lililomaanisha "fumbo" au "mithali," katika misamiati ya fasihi ya hekima. Mifano inatengeneza aina za mahusiano ya kifasihi sawasawa na ufanano wa ushairi wa Kiebrania.

1. mifano inayoelezea ufanano
2. mifano ambayo inaelezea ulinganifu
3. mifano ambayo inajenga aina fulani za kauli za mazingira ya kweli

Ni muhimu kuamua aina ya kilele cha ulinganifu/ufanano ambacho mfano umekusudiwa kuelezea. Kukosa hili ni kufasiri kimakosa kusudio lililokusudiwa katika mifano. Mtu lazima awe tayari kufikiria upya mambo na matokeo yaliyokusudiwa katika ufahamu wa asili ishangazayo ya *mashal*.

C. Baadhi ya mifano katika Mathayo 13 inatengeneza u-pili. Kweli zile zile kuu zinarudiwa kwa mifano tofauti tofauti.

1. Magugu na Juya
  2. Punje ya haradali na chachu
  3. Hazina zilizofichwa na lulu za thamani kuu
- Inawezekana kwamba Mt. 13:51-52 inatengeneza mfano wa nane

D. Mfano wa Mathayo 13 unapewa usambamba katika vitabu vingine vya Injili

Mathayo	Marko	Luka
Mt. 13:1-9, 18-23	Marko 4:1-9, 13-20	Luka 8:4-8, 11-15
Mt. 13:6-9	-----	-----
Mt. 13:24-30, 36-43	-----	-----
Mt. 13:31-32	Marko 4:30-32	Luka 13:18-19
Mt. 13:33	-----	Luka 13:20-21
Mt. 13:34	-----	-----
Mt. 13:44	-----	-----
Mt. 13:45-46	-----	-----

E. Kati ya mifano saba Mathayo 13, mpanzi na udongo zote pia zipo katika Marko na Luka wakati mfano juu ya chachu unarudiwa katika Luka peke yake. Kama Mathayo alikusanya mafundisho ya Yesu kuyafanya mahubiri marefu ya Mathayo 5-7, hivyo pia alikusanya mifano ya Yesu kwenda katika muktadha mmoja.

F. Inawezekana kwamba Mathayo aliweka injili yake katika muundo ili kwamba mwitikio wa imani wa mahubiri ya Yesu na mafundisho yachanganywe (Mathayo 8-12). Baadhi waliitikia lakini wengine hawakufanya hivyo. Ikiwa Yesu alikuwa Masihi mwa Mungu, kwanini hawakuitikia wote? Hili ni swali ambalo mfululizo huu wa mifano unajibu.

### MADA MAALUM: KUITAFASIRI MIFANO

Madokezo ya injili yaliandikwa miaka mingi baada ya maisha ya Yesu. Wandishi wa injili (kwa kusaidiwa na Roho) kimaadili walijiozea kwenye fasihi simulizi. Walimu wa sheria walifundisha kwa mpangalio wa simulizi. Yesu aliiga huu utaratibu wa simulizi kwenye mafundisho. Kwa ufahamu wetu kamwe hakuandika mafundisho au hotuba zake. Kuongezea katika kumbukumbu, uwasilishaji wa mafundisho ulikuwa wa kujirudia, kufupishwa, na kuelezewa kwa mifano. Wandishi wa injili walizitunza hizi kumbukumbu. Mifano, iliyokuwa migumu kuelezea, ni moja ya hizi mbinu.

"Mifano kwa uzuri zimeelezewa kama hadithi zenye kuwa na maana mbili zinazolingana; kiwango cha habari hutoa taswira ambapo ukweli hudhaniwa na kueleweka," *Dictionary of Jesus and the Gospels*, (uk. 594).

"mfano ni msemu au hadithi ambayo hutafuta kupeleka hoja ambayo mnenaji hupenda kuisisitiza kwa kuelezea kwa mifano kwenye mazingira ya maisha ya kawaida," *The Zondervan Pictorial Bible Encyclopedia* (uk. 590).

Ni vigumu kuelezea kiusahihi ni nini kilichoeleweka kwa neno "mifano" katika siku za Yesu

1. Baadhi wanasema liliaksi neno la Kiebrania *mashal* ambalo lilimaanisha kitendawili cha aina yeyote (Marko 3:23), msemu wa kiujanja (Mithali, Luka 4:23), miseemo mifupi (Marko 7:15), msemu wa kimafumbo ("msemu usioeleweka").
2. Wengine wanashikilia zaidi kwenye maelezo yasio kamili ya hadithi fupi.

Kulingana na kila mtu anavyojaribu kuelezea neno, zaidi ya theruthi moja ya mafundisho ya Yesu yaliyoandikwa yako katika muundo wa mafumbo. Huu ulikuwa ni uwasilishaji mkuu wa fasihi ya Agano Jipya. Hakika mifano ya Yesu ilikuwa ni ya ukweli. Ikiwa mtu atakubaliana na maelezo ya pili, bado pana aina nyingine mbalimbali ya hadithi fupi fupi:

1. hadithi rahisi za kueleweka (Luka 13:6-9)
2. hadithi ngumu zisioeleweka (Luka 15:11-32)
3. hadithi kinzani (Luka 16:1-8; 18:1-8)
4. za uainishaji/kiistiari (Mt. 13:24-30, 47-50; Luka 8:4-8, 11-15; 10:25-37; 14:16-24; 20:9-19; Yohana. 10;

15:1-8)

Katika kushughulika na suala hili la aina ya mafumbo mtu lazima atafasiri misemo hii kwa hoja mbalimbali. Hoja ya kwanza ingalikuwa ni kanuni za ufasiri wa pamoja zenye kutumika kote kwenye uwasilishaji wa kibiblia.

Baadhi ya miongozo:

1. kutambua kusudi la kitabu kizima au kwa kiasi Fulani sehemu ya fasihi
2. kuwatambua wasikilizaji wa mwanzo. Ni muhimu kuwa mara nyingi mfano wa aina ile ile unatolewa kwenye makundi tofauti, mfano:
  - a. kondoo aliyepotea katika Luka 15 uliowalenga wenye dhambi
  - b. kondoo aliyepotea katika Mt. 18 uliolenga kwenye kanuni
3. uwe na uhakika wa kuandika kwa uharaka muktadha wa huo mfano. Mara nyingi Yesu au wandishi wa injili huzungumzia hoja kuu (mara nyingi mwishoni mwa mfano au haraka baada ya kuuzema).
4. kuelezea kiini cha kusudi la mfano katika sentensi yenye habari moja. Mifano huwa na wahusika wawili au watatu. Mara nyingi ni ukweli uliodokezwa, kusudi, au hoja (mpango) kwa kila mhusika (Luka 15:11-22 ina wahusika 3 lakini sio mfano wa msamaria Mwema, Luka 10:25-37).
5. angalia sura zinazofanana katika injili zingine, baadaye tena viatabu vingine vya Agano Jipya na Agano la Kale

Hatua nyingine ya kanuni za utafasiri ni zile zenye kuhusiana hasa na suala la kimafumbo

1. Soma (usikilize ikiwezekana) mfano tena na teana. Hizi zilitolewa kwa ulazima wa kusimuliwa, na sio uchunguzi ulioandikwa.
2. Mingi ya mifano ina kweli kuu moja ambacho huhusiana na muktadha wa kihistoria na kifasihi wa wote Yesu na/ au wainjilisti.
3. Uwe mwangalifu kuyatafasiri maelezo. Mara nyingi huwa tu ni sehemu ya mazingira ya hadithi.
4. Kumbuka kuwa mifano sio kweli yenyewe. Ni mfanano wa maisha halisi, lakini mara nyingi wenye kukuzwa, ili kulazimisha hoja (ukweli).
5. Tambua hoja kuu ya hadithi ambayo umati wa Wayahudi wa karne ya kwanza wangaliweza kuitambua (Kenneth E. Bailey, *Jesus Through Middle Eastern Eyes*). Baadaye angalia angalia mpindisho wa hadithi au mshangao. Mara nyingi huja mwishoni mwa hadithi (kama vile A. Berkeley Mickelsen, *Interpreting the Bible*, kur. 221-224).
6. mifano yote ilitolewa ili kupata mwitikio. Mwitikio huo mara nyingi ulihusiana na dhana ya "ufalme wa Mungu." Yesu ndiye mwanzilishi wa ufalme mpya wa Kimasihi (Mt. 21:31; Luka 17:21). Wale wote waliomsikia lazima wajongee kwake sasa!  
Ufalme pia ulihusu mambo yajayo (Mathayo25). Hatma ya mbele ya mtu ilitegemea namna alivyojongea kwa Yesu kwa wakati. Mifano ya ufalme ilielezea ufalme mpya uliojiri ndani ya Yesu. Waliielezea kwa hitaji la kimaadili na maana kuu ya uanafunzi. Hakuna chochote chawezakuwa kama kilivyokuwa. Kwa umuhimu yote ni mapya na yanamlenga Yesu!
7. Mifano mara nyingi haelezei hoja au kiini cha ukweli. Mfasiri sharti atafute majibu ya kimuktadha yanayodhihilisha kweli kuu halisi yenye kufundisha kwa wapokeaji wa mwanzo lakini sasa ambayo ni tata kwetu.  
Hoja ya tatu ambayo mara nyingi ni yenye mkanganyiko ni ile yenye kuwa na uficho wa ukweli wa kimafumbo. Yesu mara nyingi alizungumza mifano yenye hali isioeleweka (kama vile Mt. 13:9-15; Marko 4:9-13; Luko 8:8-10; Yohana. 10:6; 16:25). Hili lilihusiana na unabii katika Isa. 6:9-10. Moyo wa wasikiaji unaamua kiwango cha uelewa (kama vile Mt. 11:15; 13:9,15,16,43; Marko 4:9,23,33-34; 7:16; 8:18; Luka 8:8; 9:44; 14:35).

Hata hivyo, lazima ielezewe kuwa uati wa watu (Mt. 15:10; Marko 7:14) na Mafarisayo (Mt. 21:45; Marko 12:12; Luka 20:19) walielewa kile Yesu alichokuwa akizungumza lakini wakakataa kuitikia kiusahihi kwa imani na toba. Kwa maana moja huu ndio ukweli wa mfano wa udongo (Mathayo 13; Marko 4; Luka 8). Mifano ilikuwa na maana ya kudhihilisha ukweli (Mt. 13:16-17; 16:12; 17:13; Luka 8:10; 10:23-24).

Grant Osborne, katika kitabu chake cha *Hermeneutical Spiral*, uk. 239, analeta hoja kuwa "mifano ni chombo

chenye kuleta mkabala na hufanya kazi tofauti kutegemeana na wasikilizaji...kila kundi (viongozi, umati wa watu, wanafunzi) linakabiliwa kitofauti na mifano." Mara nyingi wanafunzi hawakuielewa mifano au mafundisho Yake (kama vile Mt. 15:16; Marko 6:52; 8:17-18,21; 9:32; Luka 9:45; 18:34; Yohana. 12:16).

Hoja ya nne pia ni yenye mkanganyiko. Inashughulika na kweli kuu ya mifano. Wengi wa watafasiri wa sasa wametenda ufasiri wa mifano kiistiari. Istiari ilibadili maelezo ya muundo wa ukweli kuwa wenye kufafanuliwa kiundani. Njia hii ya utafasiri hailengi kwenye muundo wa kihistoria, muundo wa kifasihi, au kusudi la kiuandishi, bali kuwasilisha mawazo ya mfasiri, na sio andiko.

Hata hivyo, lazima ikubalike kuwa mifano ambayo Yesu aliitafasiri iko karibu na ile ya kiistiari au uainishaji. Yesu alitumia maelezo kupeleka ujumbe (mpanzi, Mathayo 13; Marko 4; Luka 8 na watumwa waovu, Mathayo 21; Marko 12, Luka 20).

Baadhi ya mifano mingine ina kweli kuu mbalimbali. Mfano mzuri ni ule wa Mwana Mpendwa wa pekee (Luka 15:11-32). Sio tu upendo wa Baba na uasi wa mwana lakini ni mwenendo wa kijana mkubwa ambaye ndiye kiini cha maana kamili ya mfano.

Nukuu ya kukusaidia ni kutoka *Linguistics and Biblical Interpretation* by Peter Cotterell na Max Turner:

"Alikuwa ni Adolf Julicher zaidi ya wengine ambaye alieleza usomaji wa Agano Jipya dhidi ya jaribio lenye maamuzi kuelewa wajibu wa mfano katika mafundisho ya Yesu. Umuhimu wa kuiweka kiistiari mifano iliachwa na utafiti ukaanza kwa ajili ya suluhisho lenye kutuwezesha kupenye kwenye maana ya kweli yao. Lakini kama Yeria alivyoweka sawa, 'bidii zake za kuiweka huru mifano toka kwenye utafasiri usioaminika na usio na mantiki wa kila maelezo ulimsababishia kuangukia kwenye makosa makubwa.' Kosa lilikuwa ni lenye kusisitiza na sio tu huo mfano uweze eleweka kama wenye kupeleka wazo moja, bali kuwa wazo liweze kuwa la pamoja" (uk. 308).

Nukuu nyingine inayoweza kukusaidia *The Hermeneutical Spiral* by Grant Osborne:

"Mpaka sasa nimeweza kutambua viashilia vingi kuwa mifano hakika ni istiari, ingawa inadhibitiwa na kusudio la mwandishi. Blomberg (1990) kiukweli hakubaliani kuwa kuna hoja nyingi kama ilivyo wahusika katika mifano na hakika ni istiari. Wakati hili kwa kiasi fulani limekuzwa, liko karibu na ukweli kuliko mkabiliano wa 'hoja moja'" (uk. 240).

Je mifano inapaswa kutumika kufundisha kweli ya maandiko au kuiangaza kweli ya maandiko? Wengi wa watafasiri wameweza kushawishiwa na utumiaji mbaya wa njia za kiistiari za kuitafasiri mifano iliyowaruhusu kuitumia kuanzisha mafundisho yasiyo na uhusiano na kusudi la mwanzo la Yesu wala lile la mwandishi wa injili. Maana lazima iendane na kusudio la uandishi. Yesu na wandishi wa injili walikuwa katika hali ya uvuvio, lakini watafasiri sio. Hata hivyo, mifano imetumika vibaya nab ado inafanya kazi kama chombo cha kufundishia ukweli, ukweli wa kimafundisho. Msikilize Bernard Ramm juu ya hoja yake.

"Mifano haifundishi mafundisho na madai ya kuwa isitumike kabisa katika uandishi wa kimafundisho sio sahihi. . .lazima tuangalie matokeo kwa uwazi, mafundisho dhahili ya Bwana wetu , nay ale ya Agano Jipya yaliyobaki. Mifano yenye maangalizo sahihi yaweza kutumika kuelezea kwa mifano mafundisho, kuangaza maarifa ya Kikristo na kufundishia masomo kwa vitendo." *Protestant Biblical Interpretation* (uk. 285).

Katika kuhitimisha ngoja nitoe nukuu tatu ambazo zinaaksi maonyo kwenye utafasiri wa mifano:

1. Zilizochukuliwa toka *How to Read the Bible For All Its Worth* cha Gordon Fee na Doug Stuart, "Mifano zimepatwa na matokeo ya kutotafasiriwa kiusahihi katika nafasi ya pili ndani ya kanisa baada ya ufunuo" (uk. 135).
2. Ikichukuliwa toka *Understanding and Applying the Bible* by J. Robertson McQuilkin, "Mifano imekuwa ni chanzo cha baraka zisizo ambilika katika kuwafumbua watu wa Mungu kuhusu ukweli wa kiroho. Kwa wakati ule ule, mifano imekuwa chanzo cha machafuko yasioambilika katika yote mafundisho na utendaji ndani ya kanisa" (uk. 164).

3. Ikichukuliwa toka *The Hermeneutical Spiral* cha Grant Osborne,  
"Mifano imekuwa kati ya maandiko yaliyoandikwa sana lakini mpaka sasa kikanuni za ufasri yametumia vibaya kwenye sehemu za maandiko. . utendaji wake bado ni mgumu kueleweka kwenye uwasilishaji wa kibiblia. Umuhimu wa mifano kwa ajili ya mawasiliano ni mkubwa, pale ambapo huleta ulinganifu au msingi wa hadithi juu ya kila maarifa ya kila siku. Hata hivyo, hadithi yenyewe ina uwezo wa kuwa na maana nyingi, na wasomaji wa sasa wanapata shida ya kuitafasiri kama walivyokuwa wasikilizaji wa kale" (uk. 235).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 13:1-2

<sup>1</sup> Siku ile Yesu akatoka nyumbani, akaketi kando ya bahari. <sup>2</sup> Wakamkusanyikia makutano mengi, hata akapanda chomboni, akaketi; na ule mkutano wote wakasimama pwani.

13:1

NASB, NRSV

NKJV

"siku hiyo"

NRSV, TEV,

"siku hiyo hiyo"

NJB

"siku ile ile"

Hii haikusudiwi kuwa alama ya muda katika mukdhadha huu bali mbinu inayopita. Mfano wake kama kiashiria cha alama cha muda 22:23; Marko 4:35.

☛ **"alika kando ya bahari"** Kukaa ilikuwa fundisho rasmi la mkao wa mwalimu (kama vile Mt. 13:2; 15:29; 24:3; 26:55; Luka 4:20; Mdo. 13:14). Walisimama kusoma Maandiko (kama vile Luka 4:16). Mkao huu na sehemu inaonesha kipindi cha mafundisho. Bahari ilikuwa kama jumba la kiasili la kuoneshea matukio.

**13:2 "aliingia mashuani na kuketi"** Chombo siku zote kilikuwa kinapatikana wakati Yesu alipokuwa akifundisha kwasababu ya kusongwa na makutano (kama vile Luka 5:1-3; Marko 3:9).

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 13:3-9

<sup>3</sup> Akawaambia mambo mengi kwa mifano, akisema, Tazama, mpanzi alitoka kwenda kupanda. <sup>4</sup> Hata alipokuwa akipanda, mbegu nyingine zilianguka karibu na njia, ndege wakaja wakazila; <sup>5</sup> nyingine zikaanguka penye miamba, pasipokuwa na udongo mwingi; mara zikaota, kwa udongo kukosa kina; <sup>6</sup> na jua lilipozuka ziliungua; na kwa kuwa hazina mizizi zikanyauka. <sup>7</sup> Nyingine zikaanguka penye miiba; ile miiba ikamea, ikazisonga; <sup>8</sup> nyingine zikaanguka penye udongo mzuri, zikazaa, moja mia, moja sitini, moja thelathini. <sup>9</sup> Mwenye masikio na asikie.

**13:3 "mpanzi alitoka kwenda kupanda"** Mfano huu (Mt. 13:3-9) ni muhimu sana kwasababu Yesu mwenyewe alitoa ufasiri wake. Mbegu, mpanzi, udongo na mavuno vyote ni muhimu katika ufasiri wa Yesu wa mfano (Mt. 13:18-23).

Ni kwa namna fulani ya kiistiari au angalau uainishwaji. Istiari inatafuta kiwango cha ndani zaidi kilichofichwa cha maana katika andiko. Inachukua maana katika andiko ambalo halina uhusiano kabisa na maana iliyokusudiwa ya mwandishio wa asili au siku zake au hata msukumo wa Maandiko kama kitu kimoja. Uainishaji kwa upande mwingine unatafta kuweka shabaha juu ya umoja wa Biblia ukijikita katika mwandishi wa kiungu na mpango mmoja wa kiungu. Ufanano katika Agano la Kale unaweka kabla kweli za Agano Jipya. Ufanano huu unakua kiasili kutokana na kusoma Biblia nzima (kama vile Rum. 15:4; 1 kor. 10:6, 11).

**13:4-7 "njiani. . .kwenye mawe. . .penye miba"** Siku zote wakulima wa kijiji walifanya kazi kwa pamoja na kulima shamba zima kuzunguka nyumba zao. Katika shamba hili kulikuwa na nyayo za miguu, baadhi ardhi ya juu na sehemu baadhi kulikuwa na vichaka vya miba vilivyokuwa vimejiotea vyenye. Shamba lote lilikuwa limelimwa. Mpanzi alitapanya mbegu bila kuchagua katika shamba kubwa lililolimwa.

**13:8 "Na zingine zilianguka katika udongo mzuri na kuzaa sana, na ziingine mia, zingine sitini na zingine thelathini"** Mimea izaayo matunda, bila kiasi fulani ni shabaha kuu. Lazima tuwe makini tusije kulinganisha ukuaji na wokovu! Yohana 8:31 inasema "wale wayahudi waliokuwa wamemwamini Yeye," lakini bado katika muktadha wa baadaye ni wazi hawajaokolewa (Yohana 8:59). Biblia inatofautisha kati ya mwitikio wa kwanza wa hisia na uanafunzi wa kudumu unaobadilisha maisha. Katika mfano huu wa kuchipua kunarejerea ya kwanza, kuzaa matunda kwa pili.

**13:9** Angalia dokezo katika Mt. 11:15.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 13:10-17**

<sup>10</sup> Wakaja wanafunzi, wakamwambia, Kwa nini wasema nao kwa mifano? <sup>11</sup> Akajibu, akawaambia, Ninyi mmejaliwa kuzijua siri za ufalme wa mbinguni, bali wao hawakujaliwa. <sup>12</sup> Kwa maana ye yote mwenye kitu atapewa, naye atazidishiwa tele; lakini ye yote asiye na kitu, hata kile alichochacho nacho atanyang'anywa. <sup>13</sup> Kwa sababu hii nasema nao kwa mifano;

kwa kuwa wakitazama hawaoni,  
na wakisikia hawasikii, wala kuelewa.

<sup>14</sup> Na neno la nabii Isaya linatumika kwao,  
likisema, Kusikia mtasikia, wala hamtaelewa;  
Kutazama mtatazama, wala hamtaona.

<sup>15</sup> Maana mioyo ya watu hawa imekuwa mizito,  
Na kwa masikio yao hawasikii vema,  
Na macho yao wameyafumba;  
Wasije wakaona kwa macho yao,  
Wakasikia kwa masikio yao,  
Wakaelewa kwa mioyo yao,  
Wakaongoka, nikawaponya

<sup>16</sup> Lakini, heri macho yenu, kwa kuwa yanaona; na masikio yenu, kwa kuwa yanasikia. <sup>17</sup> Kwa maana, amin, nawaambia, Manabii wengi na wenye haki walitamani kuyaona mnayoyaona ninyi, wasiyaone; na kuyasikia mnayoyasikia ninyi, wasiyasikie.

**13:10-13** Ufasiri mzuri wa mifano ya Yesu unajumuisha kujitoka kiimani katika sehemu ya wasikiaji sawasawa na nguvu ya kuangazia ya Roho. Mifano inahitaji mwitikio. Mwitikio huu unaunganisha nguvu ya Mungu na utashi huru wa msikiaji anayeamini. Angalia dokezo za utangulizi mwanzoni mwa sura hii.

**13:11 "siri za ufalme wa mbinguni"** Yesu anatumia neno hili kwa Zama Mpya (kama vile Mathayo 5-7) ikiwa na njia mpya ya kuutazama uhalisia. Siri hizi ni juu Yake na Ufalme wake Mpya. Neno hili linatumika kuelezea mpango wa ukombozi wa milele wa Mungu ambao ndiyo pekee unaofunuliwa na Masihi wa Mungu (kama vile Luka 22:22; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; Efe. 1:11; 1 Pet. 1:12). Kila msikiaji haelewi (kama vile Mt. 13:13,16-17,19,23; Marko 4:11-12).

**13:12** Uongozi wa Kiyahudi na maarifa yao ya maandiko walitakiwa watambue na kuyakumbatia mafundisho ya Yesu na Yesu mwenyewe lakini hawakufanya hivyo. Hivyo wale waliotakliwa na wanaotakiwa kuwa wawajibikaji (kama vile Luka 12:48). Maarifa yao madogo yanapelekea katika hukumu kamalifu (sawasawa na 2 Pet. 2:20-22).

**13:14-15 "unabii wa Isaya unatumizwa"** Hii ni nukuu kutoka Tafsiri ya Agano la Kale ya Kiyunani (LXX). Hii inahusiana na wito wa Isaya na Agizo lake. Mungu alimwambia angezungumza lakini watu wasingemsikiliza na



kumuitikia (kama vile Isaya 6:9-10). Kifungu hiki cha Agano la Kale kinanukuliwa katika Yohana 12:40 na Mdo. 28:25-27. Kwa wale walio na imani, Mungu kwa kuendelea atawafunulia kweli zaidi kadiri wanavyotembea katika nuru waliyonayo bali wale wasio na imani maandiko yanakuwa giza na kimya! Mifano ni kweli iliyowazi kwa wale watakaosikia lakini kweli iliyofichwa kwa wale waliokataa imani katika Kristo. Angalia F. F. Bruce, *Answers to Questions*, ukur. 176-177.

☐ "moyo" Angalia [MADA MAALUM: MOYO](#) katika Mt. 5:8.

**13:16** Linganisha hii na Marko 4:13.

**13:17 "Hakika"** Angalia Mada Maalum katika Mt. 5:18.

☐ "Manabii wengi na wenye haki walitamani kuyaona mnayoyaona ninyi, wasiyaone" Waaminio wa Agano Jipya wanajua zaidi juu ya mpango wa ukombozi wa milele wa Mungu na makusudi kwa wanadamu wote kuliko wahusika wowote walivyowahi kujua katika Agano la Kale (1 Pet. 1:10-12). Hii inatupatia sisi wajibu mzuri sana!

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 13:18-23**

<sup>18</sup> Basi ninyi sikilizeni mfano wa mpanzi. <sup>19</sup> Kila mtu alisikiapo neno la ufalme asielewe nalo, huja yule mwovu, akalinyakua lililopandwa moyoni mwake. Huyu ndiye aliyepandwa karibu na njia. <sup>20</sup> Naye aliyepandwa penye miamba, huyo ndiye alisikiaye lile neno, akalipokea mara kwa furaha; <sup>21</sup> lakini hana mizizi ndani yake, bali hudumu kwa muda; ikitukia dhiki au udhia kwa ajili ya lile neno, mara huchukizwa. <sup>22</sup> Naye aliyepandwa penye miiba, huyo ndiye alisikiaye lile neno; na shughuli za dunia, na udanganyifu wa mali hulisonga lile neno; likawa halizai. <sup>23</sup> Naye aliyepandwa penye udongo mzuri, huyo ndiye alisikiaye lile neno, na kuelewa nalo; yeye ndiye azaaye matunda, huyu mia, na huyu thelathini.

**13:18-23** Ufasiri wa mfano huu wa Yesu walipewa wanafunzi wakiwa faragha nae.

**13:19 "huja yule mwovu akalinyakua lililopandwa moyoni mwake"** Katika ufanano wa Marko 4:15 anaitwa Shetani (angalia Mada Maalum katika Mt. 4:5). 2 Wakorintho 4:4 inaelezea kazi yake kati ya watu. Inashangaza kwamba yule muovu anatokea mara kwa mara katika mifano (kama vile Mt. 13:25, 28, 39). Yesu alielezea uwepo wa nguvu binafsi ya muovu ambaye yuko huko nje kukatisha mapenzi ya Mungu kwa wote mataifa na mtu mmoja mmoja. Kuna rejea iliyofichwa katika hizi mifano kwa maadui watatu wa mwanadamu: (1) Shetani (kama vile Mt. 13:19; Efe. 2:2); (2) mfumo wa ulimwengu (kama vile Mt. 13:22; Efe. 2:2); na (3) asili ya mwanadamu iliyoanguka (kama vile Efe.2:3).

**13:20 "Naye aliyepandwa penye miamba, huyo ndiye alisikiaye lile neno, akalipokea mara kwa furaha"** Hii Kidhahiri ni mwitikio wa hali ya juu kwa Yesu na Ujumbe wake kama muktadha unavyoonesha. Wokovu wa kweli ni mwitikio wa mwanzo kwa toba na imani inayofuatiwa na mwitikio unaoendelea wa toba na imani. Kuna makanisa mengi yanayoonekana yanayotumia maneno ya Kikristo, wanaohudhuria mikutano ya Wakristo na kusoma Biblia ya Kikristo lakini hayana uhusiano binafsi pamoja na Yesu Kristo (kama vile Mt. 7:21-23; 2 Pet. 2).

**13:21-22 "lakini hana mizizi ndani yake, bali hudumu kwa muda; ikitukia dhiki au udhia kwa ajili ya lile neno, mara huchukizwa"** Kufanana na Kristo ni matazamo na mtindo wa maisha ni ushahidi wa ukiri wa dhiti (kama vile Vitabu vya 1 Yohana na Yakobo). Mwitikio wa awali hata wakati umejawa na furaha kuu, siku zote huwa sio wa kudumu au wa kuamini. Angalia [MADA MAALUM: UKANAJI WA IMANI \(APHISTĒMI\)](#) katika Mt. 7:21. Agano Jipya mara kwa mara linazungumzia wale waliosikia wakigeuka.

1. Hakuna mzizi, Mt. 13:21; Marko 4:17; Luka 8:13
2. kuanguka, Mt. 24:10
3. kutokukaa, Yohana 15:6
4. kupotea, 1 Tim. 1:9; 6:21; 2 Tim. 2:18
5. kupata dhoruba, 1 Tim. 1:19

6. kuanguka, 1 Tim. 4:1
7. kukana imani, 2 Thes. 2:3
8. kuanguka, Ebr. 3:12
9. kuanguka, Ebr. 6:6
10. kugeuka, 2 Pet. 2:20-22

Ukristo ni uhusiano ambao lazima uendelezwe! Inahusisha mwitikio wa awali (na kuendelea Yohana 1:12; Rum. 4), mwitikio unaoendelea (Yakobo na 1 Yohana), na hitimisho la uaminifu (Ebr. 11)!

**13:22 "na udanganyifu wa mali"** Angalia Mada Maalum: Mali katika Mt. 6:24.

**13:23 "lisizae matunda"** Kuzaa matunda ni ushahidi wa uongofu wa kweli na sio tu uamuzi wa kuanzia wa kihisia! Ukristo ni muda Fulani mzuri lakini maisha ya uanafunzi.

Manfred T. Brauch, *Abusing Scripture: the Consequences of Misreading the Bible*, ukur. 106, ana maoni mazuri sana ya kufurahisha.

"Katika kuonya dhidi ya manabii wa uongo, Yesu alifundisha kwamba wangejulikana kwa matunda wanayozaa (Mt. 7:15-16). Hiyo ndio tabia yetu, tahamani yetu ya ndani na imani vinafunuliwa katika kilele katika maisha tunayoyaishi (Mt. 7:17-20; Lk. 6:43-45). Hivyo ushiriki katika anga la utawala wa Mungu haiwekewi dhamana wala kulindwa kwa kumkiri Yesu kama Bwana bali wale tu wanaoyatenda mapenzi ya Mungu katika maisha yao ni watoto wa ufalme (Mt. 7:21; Lk. 6:46-48). Katika ufasiri wake wa mfano wa mpanzi (Mt. 13:18-23; Mk. 4:13-29; Lk. 8:11-15), Yesu alieleza sio kusikia wala kupokea "neni la ufalme" inatosheleza. Ni wale tu wazaa matunda ya uwepo wao katika maisha yao wanafunuliwa kama wale wanaoelewa kwa hakika umuhimu wake wa ndani (Mt. 13:23), lipokee (Mk. 4:20) na "hulishika kwa mioyo mizuri na ya wema" (Lk 8:15)

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 13:24-30**

<sup>24</sup> Akawatolea mfano mwingine, akisema, Ufalme wa mbinguni umefanana na mtu aliyepanda mbegu njema katika konde lake; <sup>25</sup> lakini watu walipolala, akaja adui yake akapanda magugu katikati ya ngano, akaenda zake. <sup>26</sup> Baadaye majani ya ngano yalipomea na kuzaa, yakaonekana na magugu. <sup>27</sup> Watumwa wa mwenye nyumba wakaenda wakamwambia, Bwana, hukupanda mbegu njema katika konde lako? Limepata wapi basi magugu? <sup>28</sup> Akawaambia, Adui ndiye aliyetenda hivi. Watumwa wakamwambia, Basi, wataka twende tukayakusanye? <sup>29</sup> Akasema, La; msije mkakusanya magugu, na kuzing'oa ngano pamoja nayo. <sup>30</sup> Viacheni vyote vikue hata wakati wa mavuno; na wakati wa mavuno nitawaambia wavunao, Yakusanyeni kwanza magugu, myafunge matita matita mkayachome; bali ngano ikusanyeni ghalani mwangu

**13:24-30** Mfano wa ngano mwitu ni wa kipekee kwa Mathayo (kama vile Mt. 36-43). Hii hapa ni aya ya kufurahisha kutoka New International Dictionary of New Testament Theology (NIDOTTE), vol. 1, ukur 299.

"Wazo la kanisa lisiloonekana linapatikana katika jarida la Augustine, *City of God*; Wycliffe, *De ecclesia*; Luther, *Preface to Revelation*; Calvin, *Institutes* IV 1 7; na waandishi wengineo wengi (angalia pitio la Calvin's *Institutes*, ed. J. T. McNeill, 1960, II 1022). Wazo kwamba sehemu ya juu sio kupunguza umuhimu wa uanachama wa kanisa bali kutambua uwezekano wa unafiki na dhuluma. Katika uchambuzi wa mwisho, wale wa Mungu wanaonekana kwa Mungu pekee. Ushirika wa kanisa la kweli ni ukweli kwamba halionekani kwa mwanadamu. Wazo linatoa kauli ya 2 Tim. 2:19; 'Bwana huwajua walio wake.' inaongeza kwa kanisa na kile Paulo anachokisema juu ya Israeli kwamba wote si waisraeli walio wa Israeli bali tu "wana wa ahadi" (Rum. 9:6 f.). Linatambua hatari ambayo washirika wa kanisa wanaonywa dhidi ya kuvuna uharibifu kupitia kupanda katika mwili (Gal. 3:7; kama vile Rum. 8:12.). Paulo anatambua hitaji la nidhamu katika maisha yake mwenyewe asije akakataliwa (1 Kor. 10:27; kama vile Flp. 2:12, 19). Uwezekano wa washirika wa kanisa kuanguka ni moja ya maudhui makubwa ya Waebrania (kama vile Ebr. 2:3; 3:7-4:14; 6:1-12; 10:26-39; 12:12-28). Inapendekezwa pia na mfano wa magugu (Mt. 13:24-43) na kondoo na mbuzi (Mt. 25:31-46) na mfano wa Yuda (Mt. 10:4; 26:14, 25, 47 na kuendelea 27:3; Mk. 14:10, 43; Lk. 6:16; 22:3, 47; Yohana 13:2; 17:12; 18:22 na kuendelea Mdo.1:17 na kuendelea 25)."

Maonyo haya hayaharibu usalama, bali yanatoa uwiano kwa ujasiri uliozidi katika maamuzi ya mwanzo na kupuuzia mamlaka ya uanafunzi na ustahimilivu.

**13:25 "adui"** Katika muktadha huu uhusika unarejerea

1. Shetani, Luka 10:19
2. walimu wa uongo, Mathayo 7; 2 Petro 2

Yeyote anayeharibu injili ya ufalme. Ni neema ya Mungu tu inayoweza kusaidia waamini kuelewa kweli (kama vile Mt. 13:13,16-17,23) na kupinga makosa.

☐ **"magugu"** Ngano mwitu (magugu) na ngano ilimwayo vilifana sawasawa kabisa mpaka wakati wa kuzaa matunda. Mbegu mwitu ilikuwa na punje nyeusi wakati ngano halisi ilikuwa na punje ya rangi ya hudhurungi.

**13:27 "Bwana"** Huu ni mfano wa neno *kurios* (Bwana) inayotumika kama kumtaja mtu kwa heshima. Kumbuka muktadha, muktadha, muktadha na sio kamusi au misamiati. Kamusi inaorodhesha njia tu ya neno lilivyotumika katika fasihi inayojulikana au kauli katika lugha husika/desturi.

**13:29 "msije mkakusanya magugu, na kuzing'oa ngano pamoja nayo"** Muktadha unaonekana kuhusiana na viongozi wa dini wa siku za Yesu. Hakuna namna ya wanadamu kujua mioyo ya wanadamu wengine. Mungu atanyoosha kila kitu siku ya Hukumu. Moja ya mbinu bora ya ufanisi ya Shetani ni dini. Watu wanaonekana kuwa wa kiroho lakini si kweli (yaani Mt. 7:21-23). Ngano na magugu yanaonekana kuwa sawa lakini muda unaweka kila kitu sawa. Watu wengi wanapumbazwa na udini (kama vile Isa. 29:13; Kol. 2:16-23) unafiki/kujifanya kama ukiroho (kama vile Mathayo 7)!

**13:30 "Yakusanyeni kwanza magugu, myafunge matita matita mkayachome "** Kilele cha hatima kinahusiana na nini wanadamu wanafanya na ujumbe wa Yesu Kristo na nafsi ya Yesu Kristo (kama vile Mt. 13:42, 50). Inafurahisha kuona kwamba ni Yesu anayesisitiza madhara ya kushangaza ya milele ya kukataa imani binafsi katika Yeye.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 13:31-32**

<sup>31</sup> Akawatolea mfano mwingine, akisema, Ufalme wa mbinguni umefanana na punje ya haradali, aliyoitwaa mtu akaipanda katika shamba lake; <sup>32</sup> nayo ni ndogo kuliko mbegu zote; lakini ikiisha kumea, huwa kubwa kuliko mboga zote, ikawa mti, hata nyuni wa angani huja na kukaa katika matawi yake.

**13:31-32** Mifano ya punje ya haradali na chachu na mistari 31-33, vinafanana. Inarudiwa katika Marko 4:30-32 na Luka 13:18-19. Wale wanaoitikia kwa injili wanaonekana wachache na wasio kuwa na maana lakini wao ni sehemu ya ufalme wa kiroho ambao mwishowe wataijaza nchi.

**13:32 "hata nyuni wa angani huja na kukaa katika matawi yake"** Kuwekewa herufi kubwa katika NASB kunadhaniwa kuwa hii nukuu kutoka Dan. (4:11-12). Hii ingetengeneza tungo kama njia ya kuelezea namna gani punje ya haradali inaweza kuwa kubwa, hapa ni uwakilishi wa kiwango cha ufalme wa kimasihani cha siku za mwisho.

NASB	"kula"
NKJV, NRSV,	
NJB	"kupima"
TEV	"kupima"

Neno hili la Kiyunani *saton* (*kuketi juu ya*) linafasiri kipengele cha Kiebrania cha vipimo *seah*. Ujazo wake kisawia haujulikani lakini ilikuwa ni kiwango kikubwa (kinachofanana na mti mkubwa).

## MADA MAALUM: UZANI NA VIPIMO VYA MASHARIKI YA KARIBU YA KALE (USOMAJI WA VIPIMO)

Uzani na vipimo vilivyotumika katika masuala ya biashara vilikuwa ni vya muhimu katika uchumi wa kilimo hapo kale. Biblia inawasihi Waisraeli kuwa wasiwe na upendeleo kwenye mambo yao wanayoyafanya na wengine (kama vile Law. 19:35-36; Kumb. 25:13-16; Mith. 11:1; 16:11; 20:10). Tatizo kubwa lilikuwa sio tu uaminifu, bali kutokuwepo na istilahi zilizo sawa na muundo uliotumika huko Palestina. Inaonekana kuwa palikuwepo jozi mbili za uzani; moja "nyepesi" na nyingine "nzito" kwa kila idadi (angalia *The Interpreter's Dictionary of the Bible*, juzuu ya 4, uk. 831). Pia muundo wa desimali (ulioegamia kwenye sehemu ya 10) wa Misri umekuwa ukijumuishwa na sehemu ya 6 huko Mesopotamia.

Wingi wa "vipimo" na "idadi" vilivyotumika vilitokana na sehemu ya mwili wa mwanadamu, wanyama, mizigo, vibeeo vya wakulima, hakuna hata kimoja kilichokuwa sawia. Kwa hiyo, chati hapa chini ni makadilio tu na ya majaribio. Njia rahisi ya kuonyesha uzani na vipimo iko katika uwiano.

- I. Istilahi za uzito zilizotumika mara nyingi
  - A. Vipimo vya vitu vikavu
    1. Homeri (BDB 330, yumkini "mzigo wa punda," BDB 331), mf., Law. 27:16; Hosea 3:2
    2. Lateki (AU lethech, BDB 547, yumkini inadokeza katika Hosea 3:2)
    3. Efa (BDB 35), mf., Kut. 16:36; Law. 19:36; Ezek. 45:10-11,13,24
    4. Se'ah (BDB 684), mf., Mwa. 18:6; 1 Sam. 25:18; 1 Fal. 18:32; 2 Fal. 7:1,16,18
    5. Homeri (BDB 771 II, yumkini "mganda" [safu ya mbegu zilizoanguka], BDB 771 I), mf., Kut. 16:16,22,36; Law. 23:10-15
    6. Hini (BDB 798, "sehemu ya kumi" ya efa), mf., Kut. 29:40; Law. 14:21; Hes. 15:4; 28:5,13
    7. Kibaba ( BDB 866), kama vile 2 Fal. 6:25
  - B. Vipimo vya vimiminika
    1. Kori (BDB 499), mf., Ezek. 45:14 (inaweza kuwa kipimi cha vitu vikavu, kama vile II Nya. 2:10; 27:5)
    2. Bathi (BDB 144 II), mf., I Fal. 7:26,38; II Nya. 2:10; 4:5; Isa. 5:10; Ezek. 45:10-11,14
    3. Hini (BDB 228), mf., Kut. 29:40; Law. 19:36; Ezek. 45:24
    4. Logi (BDB 528), kama vile Law. 14:10,12,15,21,24
  - C. Chati (iliyochukuliwa toka kwa Roland deVaux, *Ancient Israel*, juzuu. 1, uk. 201 na *Encyclopedia Judaica*, juzuu. 16, uk. 379)

Homeri (kikavu) =Kori kimiminika au kikavu	1						
Efa (kavu) =bathi (kimiminika)	10	1					
Se'ah (kikavu)	30	3	1				
Hini (kimiminika)	60	6	2	1			
Homeri (kikavu)	100	10	-	-	1		
Kibaba (kikavu)	180	18	6	3	-	1	
Logi (kimiminika)	720	72	24	12	-	4	1

II. Istilahi za uzani zinazotumika mara nyingi

A. Uzani unaotumika mara nyingi, taranta, shekeli, na gera.

1. Kipimo kikubwa katika Agano la Kale ni talanta. Toka Kutoka 38:25-26 tunajifunza kuwa talanta moja ni sawa na shekeli 3,000 (yaani, "uzani wa jumla," BDB 503)
2. Neno shekeli (BDB 1053, "uzani") hutumia mara nyingi kama inavyodhaniwa, lakini hakijaelezewa katika andiko. Kuna thamani mbali mbali za shekeli zilizotajwa katika Agano la Kale.
  - a. "kipimo cha kibiashara" (toleo la NASB la Mwa. 23:16)
  - b. "shekeli ya madhabahuni" (toleo la NASB la Kut. 30:13)
  - c. "kwa uzani wa Mfalme" (toleo la NASB la II Sam. 14:26), pia uliitwa "uzani wa Kifalme" kwenye mafunjo ya Elephantine.
3. Gera (BDB 176 II) ilithaminiwa na shekeli 20 (kama vile Kut. 30:13; Law. 27:25; Hes. 3:47; 18:16; Ezek. 45:12). Uwiano ulitofautiana toka Mesopotamia hadi Misri. Israeli ilifuatisha uthaminishaji uliokuwa ukitumika huko Kaanani (Ugariti)
4. Mina (BDB 584) inathaminishwa na shekeli 50 au 60. Neno hili linapatikana hasa katika vile vitabu vya Agano la Kale (yaani Ezek. 45:12; Ezra 2:69; Neh. 7:71-72). Ezekeili ilitumia uwiano wa 1 ya 60, wakati Wakaanani walitumia uwiano wa 1 ya 50.
5. Beka (BDB 132, "nusu ya shekeli," kama vile Mwa. 24:22) imetumika mara mbili katika Agano la Kale (kama vile Mwa. 24:22; Kut. 38:26) na inathaminishwa na nusu shekeli. Jina lake linamaanisha "kugawanya."

B. Chati

1. Imesimamia juu ya Torati

Taranta	1				
Mina	60	1			
Shekel	3,000	50	1		
Beka	6,000	100	2	1	
Gera	60,000	1,000	20	10	1

2. Ikisimamia juu ya Ezekeili

Taranta	1				
Mina	60	1			
Shekeli	3,600	60	1		
Beka	7,200	120	2	1	
Gera	72,000	1,200	20	10	1

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 13:33**

<sup>33</sup> Akawaambia mfano mwingine; Ufalme wa mbinguni umefanana na chachu aliyoitwaa mwanamke, akaisitiri ndani ya pishi tatu za unga, hata ukachachwa wote pia

**13:33 "chachu"** Katika Agano la Kale chachu mara kwa mara ilitumika kama uwakilishi wa uovu lakini hapa ilikuwa ni dhahiri ishara ya ukawaida na ukuaji wa Ufalme wa Mungu. Kuwa makini juu ya kujiwekea maana yako mwenyewe au visawe kwenye neno bila kuangalia muktadha wake. Muktadha unaamua maana! Angalia Mada Maalum katika Mt. 16:6.

☛ **"akaisitiri"** Katika Muktadha huu inamaanisha mchakato wa kuchanganya. Inaelezea ufichikaji wa Ufalme.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 13:34-35**

<sup>34</sup> Hayo yote Yesu aliwaambia makutano kwa mifano; wala pasipo mfano hakuwaambia neno; <sup>35</sup> ili litimie neno lililonenwa na nabii, akisema, Nitafumbua kinywa changu kwa mifano, Nitayatamka yaliyositirika tangu awali.

**13:35 "ili litimie neno lililonenwa na nabii"** Hii ni nukuu kutoka Zab. 78:2. Maandiko kadhaa ya Kiyunani ya kale ikijumuisha nakala ya asili ya  $\kappa$  na maandiko ya Kiyunani yatumikayo na Eusebius na Jerome yana "kupitia Isaya nabii." Imekuwa ikidhaniwa kwamba maandiko ya asili yalikuwa "kupitia Asafu" ambayo Zab.78 inahusishwa katika maandiko ya Kimasoteriki. Hakuna andiko la Kiyunani hata hivyo lenye jina hili. Mwandishi wa kale (1) hakumtambua kiongozi huyu wa kwaya wa Hekalu la Kilawi "Isaya" au (2) walifikiria rejea kutoka Mt. 13:14-15 kwa namna fulani iliendelea.

Wayahudi waliamini kwamba maandishi wote wa maandiko yaliyovuviwa walikuwa "manabii." Maandiko mapana ya Kiyunani ya kale hayana jina "Isaya" katika andiko.

☐ **"misingi ya ulimwengu"** Tungo ya JINSI "ya ulimwengu" haipatikani katika maandiko ya  $\kappa^1$  na B, na pia badhi ya Kilatini cha Kale na na Maandiko ya Kishamu na maandiko ya Kiyunani yaliyotumiwa na Origen na Jerome. Tungo kamili inatokea katika Mt. 25:34 na maandiko mengi ya Kiyunani (yaani,  $\kappa^2$ ,  $\kappa^*$ , C, D, L, W. Kamati ya toleo la UBS<sup>4</sup> liliamua kujumuisha "*Kosmou*," lakini katika mabano, ikiwa na alama ya "C" (yaani ngumu katika kuamua).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 13:36-43**

<sup>36</sup> Kisha Yesu akawaaga makutano, akaingia nyumbani; wanafunzi wake wakamwendea, wakasema, Tufafanulie mfano wa magugu ya kondeni <sup>37</sup> Akajibu, akasema, Azipandaye zile mbegu njema ni Mwana wa Adamu; <sup>38</sup> lile konde ni ulimwengu; zile mbegu njema ni wana wa ufalme; na yale magugu ni wana wa yule mwovu; <sup>39</sup> yule adui aliyeyapanda ni Ibilisi; mavuno ni mwisho wa dunia; na wale wavunao ni malaika. <sup>40</sup> Basi, kama vile magugu yakusanywavyo na kuchomwa motoni; ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia. <sup>41</sup> Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi, <sup>42</sup> na kuwatupa katika tanuru ya moto, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno. <sup>43</sup> Ndipo wenye haki watakapong'aa kama jua katika ufalme wa Baba yao. Mwenye masikio, na asikie.

**13:36-43** Hii ilikuwa ni tafsiri ya Yesu juu ya mfano wa Mt. 13:24-30 iliyotolewa kwa faragha kwa wanafunzi.

**13:37 "Azipandaye zile mbegu njema ni Mwana wa Adamu"** Mifano hii inahusiana na wote Yesu kama Masihi wa Mungu aletaye uzima na kweli na ujumbe wa injili kama maudhui ya ile kweli. Ukweli wa Mungu ni vyote nafsi (mpanzi) na ujumbe (mbegu).

**13:38 "lile konde ni ulimwengu"** Huu ndio msingi wa uelewa wa mifano hii. Sio kanisa bali ulimwengu (kama vile Mt. 13:47). Ni mfano tu wa mpanzi unaoonekana kushughulikia na wale waliosikia ujumbe wa injili na hata inaweza kurejerea kwa (1) Wapalestina wa siku za Yesu (2) maeneo ambapo injili ilihubiriwa (yaani ulimwengu, kama vile Mt. 28:19; Luka 24:46; Mdo. 1:8).

☐ **"wana wa ufalme. . . wana wa yule muovu"**

**MADA MAALUM: "WANA WA . . ." (BDB 119, KB 137)**

Hili neno "mwana" (au "watoto wa. . .") mara nyingi linatumika kubainisha kundi (au mtu binafsi) au kuwepo kwake katika kundi.

A. Agano la Kale

Neno la Kiebrania la "mwana" (BDB 119, KB 137) bubujiko. Hili neno la Kiebrania *ben* (BDB 119-122) linaweza

## kumaanisha

1. mwana aliyetolewa na baba
2. watoto (hata wana wa baba zao mf. Hes. 36:11)
3. mjukuu (mf. Mwa. 31:28,55)
4. washirika wa utaalumwa umoja fulani
5. wahenga/uzao (vizazi)
6. washirika wa kabila/taifa (mf. "wana wa Israeli")
7. watu wa kawaida (ana wa nchi)
8. washirika wa dini (mwana wa [jina la mungu]. Mfalme wa Kiebrania, Zaburi 2; 2 Sam. 7:14)
9. malaika (kama vile Mwa. 6:2,4; Ayubu 1:6; 2:1)
10. nahau ya ubainishaji (mf. "ana wa Beliali," "wana wa hekima," "wana wa ushujaa")

Katika Yohua 21 hili neno linatumika mara kadhaa:

1. ya mtu binafsi – mwana wa Nuni, Yos. 21:1
2. wa kikabila/kundi la kitaifa – ana wa Israeli, Yos. 21:1,3,8,31
3. wa kundi maalum (yaani., makuhani/ Walawi)
  - a. wana wa Haruni, Yos. 21:4,10,13,19
  - b. wana wa Lawi, Yos. 21:10 (kama vile mst. 27)
4. wa washirika wa makabila binafsi
  - a. wana wa Yuda, Yos. 21:9
  - b. wana wa Simeoni, Yos. 21:9
5. washirika wa makundi ya familia ya
  - a. wana wa Kohathi, Yos. 21:5,20,26
  - b. wana wa Gashoni, Yos. 21:6,27
  - c. wana wa Merari, Yos. 21:34

Aina hii ya sintofahamu unatengeneza jambo lisilo na uwezekano kuongeza tarehe ya wahenga na kupata yarehe ya uumbaji (yaani., Usshur 4004 k.k.). Mara nyingi, hizi tarehe muhimu (kwa vyo vyote wa uovu au wema au baadhi ya matendo yanayokumbukwa) zinaorodheshwa. Mara kadhaa vizazi vinaondolewa mara kwa mara vinaondolewa (mf. Ukoo wa Yesu).

### B. Agano Jipya

Hili neno "mwana" (au "watoto wa . . .") mara nyingi linatumika kutoa sifa bainishi za kundi (au mtu binafsi) au kuonyesha ushiriki nwa mtu katika kundi.

1. Sifa bainishi za kundi
  - a. dhahiri
    - 1) wana wa Ufalme, Mt. 8:12; 13:38
    - 2) wana wa wanadamu, Marko 3:28; Efe. 3:5
    - 3) wana wa nuru, Luka 16:8; Yohana 12:36; Efe. 5:8; 1 The. 5:5
    - 4) ana wa ufufuo, Luka 20:36
    - 5) wana wa Manabii, Matendo 3:25
    - 6) ana wa agano, Matendo 3:25
    - 7) watoto wa Mungu, 1 Yohana 3:10
  - b. kanushi
    - 1) wana wa mwovu, Mt. 13:38; Yohana 8:44; 1 Yohana 3:10
    - 2) wana wa jehanim, Mt. 23:15
    - 3) wana wa wa ulimwengu huu, Luka 16:8; 20:34
    - 4) wana wa Ibilisi, Matendo 13:10; 23:6
    - 5) wana wa kuasi, Efe. 2:2; 5:6
2. Sifa pambanuzi za mtu binafsi

- a. dhahiri
  - 1) mwana wa faraja (yaani., Barnaba), Mtendo 4:36
  - 2) mwana wa Mafarisayo (yaani., Paulo), Matendo 23:6
- b. kanushi
  - 1) wana wa ngurumo (yaani., Yakobo na Yohana), Marko 3:17
  - 2) mwana wa upotevu (yaani., Yuda Iskarioti), Yohana 17:12
  - 3) mwana wa uharibifu (Wapinga Kristo), 2 The. 2:3

**13:39,40 "mwisho wa dunia"** Haya ni mazingira ya kimatukio ya siku za mwisho. Ufalme ni vyote "tayari" lakini "bado," kama ilivyo hukumu.

☐ **"moto"** Angalia Mada Maalum katika Mt. 3:12.

**13:41** Hii ni nukuu ya juu juu kutoka Zek. 1:3. Tazama kwamba katika mstari huu Ufalme unaitwa "ufalme Wake." Kuna maeneo kadhaa ambapo Ufalme unapewa sifa za mwana (kama vile Mt. 16:28; Luka 22:30; 23:42; Yohana 18:36; 2 Tim. 4:1,18).

Pia kuna maeneo kadhaa ambapo ufalme unapewa sifa za wote Baba na Mwana (kama vile Mt. 13:43; Efe. 5:5; Ufu. 11:15). Ufalme wa Mwana sio wa muda (Yohana 18:36), bali milele (Yohana Dan. 7:14; Luka 1:33; 2 Tim. 4:18; 2 Pet. 1:11). Angalia Frank Stagg, *New Testament Theology*, kur. 164-165.

**13:42** Angalia dokezo katika Mt. 8:12. Angalia Mada Maalum katika: Wafu wako wapi? Katika Mt. 5:22.

**13:43 "watakapong'aa kama jua katika ufalme wa Baba yao"** Hii ilikuwa sawasawa na kauli za Dan. 12:3.

☐ **"Yeye aliye na masikio na asikie"** Wale ambao Mungu amewaruhusu kuelewa injili lazima waitikie kwayo sasa! Tungo hii ya siri inatokea mara nyingi katika Agano Jipya (kama vile Mt. 11:15; 13:9,43; Marko 4:9,23; Luka 8:8; 14:35; Ufu. 2:7,11,29; 3:6,13,22; 13:9). Mifano hii inaweka dokezo kuu la uharaka katika uharaka wa kusikia, kuamini na kuitikia sasa!

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 13:44**

<sup>44</sup> Tena ufalme wa mbinguni umefanana na hazina iliyositirika katika shamba; ambayo mtu alipoiona, aliificha; na kwa furaha yake akaenda akauza alivyo navyo vyote, akalinunua shamba lile.

**3:44 "ufalme wa mbinguni"** Angalia Mt. 13:45,47,52. Tungo hii ilikuwa sawasawa na "Ufalme wa Mungu" katika Marko na Luka. Mathayo katika maandiko kwa Wayahudi hawakutumia jina la Mungu bali walizunguka kutafta mbadala wake wa, "kimbingu." Mfano ni wa kipekee kwa Mathayo.

☐ **"hazina iliyositirika katika shamba"** Kuzika vitu vya thamani katika ardhi ilikuwa ni kulinda wao na tabia iliyozoeleka katika Mashariki ya Karibu ya Kale. Hakukuwa na taasisi za kifedha kama benki.

☐ **"akauza vyote. . .akalinunua shamba"** Hii inaonesha asili ya kimsimamo wa kujisimamia ya uanafunzi. Kumjua Yesu ni bora kuliko kila kitu! Ukinzani huu ni (1) wokovu wa bure unakuja kwa neema ya Mungu pekee na hivyo hakika ni bure kabisa (kama vile Yohana. 3:24; 5:15; 6:23; Efe. 2:8-9), lakini (2) inawagharimu wanafunzi kila kitu (kama vile Mt. 10:34-39; 13:44,46)

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 13: 45-46**

<sup>45</sup> Tena ufalme wa mbinguni umefanana na mfanya biashara, mwenye kutafuta lulu nzuri; <sup>46</sup> naye alipoona lulu moja ya thamani kubwa, alikwenda akauza alivyo navyo vyote, akainunua.



**13:45-46** Mfano wa lulu ya gharama kubwa ni ya kipekee kwa Mathayo.

**13:45 "lulu"** Lulu zilikuwa za thamani sana katika ulimwengu wa kale na wenye thamani sawasa na dhahabu kama njia ya mabadilishano ya kimanunuzi.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 13:47-50**

<sup>47</sup> Tena ufalme wa mbinguni umefanana na juya, lililotupwa baharini, likakusanya samaki wa kila namna; <sup>48</sup> hata lilipojaa, walilivuta pwani; wakaketi, wakakusanya walio wema vyomboni, bali walio wabaya wakawatupa. <sup>49</sup> Ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia; malaika watatokea, watawatenga waovu mbali na wenye haki. <sup>50</sup> na kuwatupa katika tanuru ya moto; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno.

**13:47-50** Mfano wa juya ni wa kipekee katika Mathayo. Maana yake ni sawasawa na mfano wa juya, ambayo ni kile itakuwapo nyakati ya mwisho ya kutenganishwa kwa waaminio na wasio amini (kama vile Mt. 25:31-46).

**13:48** Mstari huu unaelezea mgawanyo wa nyakati za siku ya mwisho ikijikita katika mwitikio wao kwa Yesu na injili (kama vile Mt. 25:31-46; Ufu. 20:11-15).

**13:49 "mwisho wa dunia"** Wayahudi waliona uhalisia katika zama mbili: zama ya sasa ya uovu na zama ijayo (angalia Mada Maalum katika Mt. 12:31). Waliamini kwamba Mungu angewawezesha kiongozi wa kibinadamu kuanzisha zama mpya kwa nguvu. Kutoka Agano Jipya sasa tunajua nyakati hizi zimepandana, kutoka kuvaa mwili katika Bethlehemu mpaka kuja kwa Mara ya Pili. Mstari huu unazungumzia hukumu ya matukio ya siku za mwisho (Kama vile Mt. 25:31-46; Ufunuo 20).

**13:50 "na kuwatupa katika tanuru ya moto; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno"** Angalia Mt. 13:30, 42, 50; 8:12; 25:31 na kuendelea. Yesu mara kwa mara alizungumza juu ya kuzimu!

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 13: 51-52**

<sup>51</sup> Yesu aliwauliza, Mmefafahamu hayo yote? Wakamwambia, Naam. <sup>52</sup> Akawaambia, Kwa sababu hiyo, kila mwandishi mwenye elimu ya ufalme wa mbinguni amefanana na mtu mwenye nyumba atoaye katika hazina yake vitu vipya na vya kale.

**13:52 "kila mwandishi aliyefanyika mwanafunzi"** Mwandishi alikuwa mtaalamu wa kisheria katika sheria ya kuandikwa na ya mdomo (angalia Mada Maalum katika Mt. 12:38). Mwandishi aaminiye hataweza kuchukua kweli kutoka Agano la kale na pia kutazama utimilizwaji wa mafundisho ya Yesu (kama vile Rum. 4:23-24; 15:4; 1 Kor. 10:6,11; 2 Tim. 3:16). Inawezekana Mathayo ana jiwekea sifa za kwake mwenyewe!

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 13: 53-58**

<sup>53</sup> Ikawa Yesu alipoimaliza mifano hiyo, alitoka akaenda zake. <sup>54</sup> Na alipofika nchi yake, akawafundisha katika sinagogi lao, hata wakashangaa, wakasema, Huyu amepata wapi hekima hii na miujiza hii? <sup>55</sup> Huyu si mwana wa seremala? Mamaye si yeye aitwaye Mariamu? Na nduguze si Yakobo, na Yusufu, na Simoni, na Yuda? <sup>56</sup> Na maumbu yake wote hawapo hapa petu? Basi huyu amepata wapi haya yote? <sup>57</sup> Wakachukizwa naye. Yesu akawaambia, Nabii hakosi kupata heshima, isipokuwa katika nchi yake, na nyumbani mwake mwenyewe. <sup>58</sup> Wala hakufanya miujiza mingi huko, kwa sababu ya kutokuamini kwao.

**13:53 "mifano"** Hili ni neno ambatani la Kiyunani ambalo lilimaanisha "kutupa kando." Kule kutokea kuliko zoeleka kilitumika kuelezea kweli za kiroho. Hata hivyo lazima ikumbukwe kwamba waandishi hawa wa Kiyahudi wa neno hili la Kiyunani (*parabola*) liliaksi Kiebrania *mashal*, ambalo lilimaanisha "fumbo" au "mithali." Mtu lazima awe tayari kufikiria mara mbili mambo na kutarajia matokeo katika ufahamu wa asili inayoshangaza ya *mashal*. Kuna sababu kinzani mbili zinazotolewa kwa matumizi ya mifano katika huduma ya mafundisho ya Yesu: (1)

kuzungumza kwa ufasaha kweli za kiroho kwa wale wanaofanyika kazi imani katika Yeye na (2) kuficha kweli za kiroho kutoka kwa wale wasio kuwa na imani ndani Yake.

**13:54 "alikuja nyumbani kwao"** Simulizi inayofanana inatajwa katika Luka 4:16-30. Kumekuwa na mjadala mkubwa kati ya wafasiri ikiwa hii ni safari ile ile au safari ya pili. Kuna hadithi kadhaa katika huduma ya Yesu ambazo zinafanana (kama vile yohana 2:13-22 dhidi Mt. 21:12-16; Marko 11:15-18; Luka 19:45-47), lakini wanazuoni lazima wawe makini, kulingana na madhanio yao ya kimagharib ya kifasihi wasije wakadhani ni tukio lilelile. Kunawezekana pia kuwa kulikuwa na kusafishwa mara mbili kwa Hekalu kwa mfano. Na hadithi ya Luka inaweza kurejerea tukio jingine.

☐ **"akaanza kuwafundisha katika sinagogi lao"** Ilikuwa ni tabia ya Yesu kuhudhuria ibada za Sabato. Yesu alijifunza Agano la Kale wakati wa Siku zake katika shule ya Sinagogi huko Nazareti. Sinagogi ilikuwa taasisi ya Kiyahudi iliyokuzwa wakati wa uhamisho wa Babeli kwa ajili ya kusudi la (1) kutoa mafunzo kwa watoto, (2) kuabudu, (3) kuhudumia jamii ya wayahudi, na (4) kuendeleza desturi za kipekee za Wayahudi wakati wawapo Uhamishoni kwa kuhamasisha mafunzo ya sheria na desturi za mababa.

☐ **"walishangaa"** Walikuwa na mashaka sio tu kwa ufahamu wa mafundisho Yake bali pia mamlaka ya mafundisho Yake. Waandishi walifundisha katika mamlaka ya waalimu maarufu waliopita; Yesu alifundisha kwa mamlaka Yake mwenyewe (kama vile Mt. 7:28-29).

☐ **"mtu huyu kapata wapi hekima hii na nguvu hizi z za kutenda miujiza"** Chanzo cha nguvu ya Yesu kilitengeneza mjadala mkubwa. Alikuwa ni kijana aliyekuwa hajapata mafunzo yaliyo rasmi. Wayahudi hata walimtumumu kwa kuwa katika chama kimoja na Yule muovu. Kwa wao matendo Yake dhidi ya sheria ya desturi za kinywa ilikuwa "dhambi isiyosameheka. Kwa wale walio Nazareth ilikuwa ngumu kuamini kwamba kijana wa mtaani tu alikuwa ni Masihi, Mungu mwenye kuvaa mwili.

**13:55,56 "je huyu si mwana wa seremala"** Kuna maswali matatu katika mistari hii miwili; yote mitatu inategemea jibu la "ndio". Seremala alitumika katika namna ya ufundi. Inaweza kurejerea ufundi wa mawe, vyuma au mbao. Neno la Kingereza "fundu mchoraji" linatoka katika neno hili la Kiyunani. Maswali haya kwa watu wa mjini wa mji wa Yesu inamaanisha Yesu alikuwa na makuzi ya kawaida yaliyozoeleka kama ya watoto wengine (kama vile Luka 2:40,52).

**13:55 "ndugu Zake"** Wanadamu waliorodheshwa

1. Yakobo aliyefanyika kiongozi wa kanisa la Yerusalemu na aliandika kitabu cha Yakobo.
2. Yusufu, anaitwa Yosefu katika Marko 6:3 na maandiko machache ya baadaye ya Kiyunani. Hatujui chochote kingine juu yake.
3. Simoni hatujui kitu kingine cha ziada juu yake.
4. Yuda, pia anaitwa Yuda na aliandika kitabu cha Agano Jipya cha Yuda.

☐ **"ndugu zake. . . maumbu Yake"** Hawa baadaye ni watoto wa Mariamu na Yusufu (kama vile Mt. 1:25; 12:46; Marko 6:3) au yawezekana watoto kutoka kwenye ndoa ya kwanza ya Yusufu (ambayo haiandikwi popote katika Maandiko), hivyo uchaguzi #1 ni mzuri zaidi (angalia F. F. Bruce, *Answers to Questions*, ukur. 47 na 174).

**13:57 "Wakachukizwa naye"** Yeye ni jiwe la mashitaka na jiwe la kujikwalia. Jiwe walilolikataa waashi limekuwa jiwe kuu la pembeni (kama vile Mt. 11:6; Isaya. 8:14; 28:16; Yer. 6:21).

☐ **"nabii"** Hii ilikuwa mithali iliyozoeleka. Kile kinachojulikana kinapoteza umuhimu wake. Angalia Mada Maalum katika Mt. 11:9.

**13:58 "wala hakufanya miujiza huko"** Mungu siku zote alichagua Waamini kushirikiana katika mambo ambayo yanahusiana naye (agano). Si kwamba Yesu asingeweza, aliamua kutofanya hivyo. Tunajifunza kutoka Luka 4:28-29 kwamba walijaribu kumuua kwasababu ya kauli zake.

## **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Orodhesha kweli kuu ya kila mifano kwa maneno yako mwenyewe. Je kuna maudhui inayoleta umoja katika sura hii?
2. Ni kwa namna gani mtu anaweza kuwianisha wokovu huru na ule unaogharimu kila kitu?
3. Je kuzimu ni fundisho la kibiblia kama ilivyo mbingu?
4. Ni kwa namna gani ufundishaji wa Yesu ni tofauti na walimu wa Kiyahudi'?
5. Kwanini Nazareti ilimkataa Yeye?

## MATHAYO 14

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Kifo cha Yohana Mbatizaji	Yohana Mbatizaji Anakatwa Kichwa	Matukio ya Udanganyifu Kukubaliwa au Kukataliwa kwa Yesu  (13:53-17:27)  Kifo cha Yohana	Kifo cha Yohana Mbatizaji	Herode na Yesu
14:1-12	14:1-12	14:1-12	14:1-2	14:1-2
				Yohana Mbatizaji Anakatwa Kichwa
			14:3-5	14:3-12
			14:6-7	
			14:8	
			14:9-12	
Kuwalisha Watu Eflu Tano	Kuwalisha Watu Eflu Tano	Watu Eflu Tano Wanalishwa	Yesu Anawalisha Watu Eflu Tano	Muujiza wa Kwanza wa Mikate
14:13-21	14:13-21	14:13-21	14:13-14	14:13-14
			14:15	14:15-21
			14:16	
			14:17	
			14:18-21	
Kutembea Juu Ya Maji	Yesu Anatembea Juu ya Bahari	Yesu Anatembea Juu ya Maji	Yesu Anatembea juu ya Maji	Yesu Anatembea Juu ya Maji na, Petro panoja Naye
14:22-33	14:22-33	14:22-27	14:22-26	14:22-33
			14:27	
		14:28-33	14:28	

			14:29-30 14:31	
			14:32-33	
Kumponya Mgonjwa Huko Ginesareti	Wengi Wanamgusa na Kuwa Vizuri		Yesu Anaponya Mgonjwa katika Ginesareti	Tiba huko Ginesareti
14:34-36	14:34-36	14:34-36	14:34-36	14:34-36

## **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka “[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)”)** **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## **HISTORIA YA NYUMA YA MATHAYO 14:1:36**

- A. Mfalme Herode anatajwa katika Mathayo 14:1 na kuendelea; Luka 3:1; 9:7; 13:31, na 23:7, alikuwa mwana wa Herode Mkuu. Wakati wa kifo cha Herode Mkuu, ufalme uligawanywa miongoni mwa wanae watatu (Archelaus, Herod Antipas, na Philip). Hili neno "Mtawala" lilimaanisha "kiongozi wa upande wa nne." Huyu Herode alijulikana kama Herode Antipa ambapo ni muundo wa jina Antipater lililofupishwa. Huyu aliitawala Galilaya na Perea (mnamo 4 b.k. – 39 b.k). Hili lilimaanisha kwamba huduma ya Yesu illiyo nyingi ilikuwa katika himaya ya hiki kizazi cha pili cha mtawala wa Idumaya.
- B. Herodia alikuwa binti wa ndugu wa Herode Antipa, Aristobulus, ambaye alimfanya mkewe. Kwa wakati uliopita huyu pia alikuwa ameolewa na Philip, ndugu wa kambo wa Herode Antipa. Huyu hakuwa Philip Mtawala aliyeliongoza eneo la kaskazini wa Galilaya, bali ndugu mwingine wa Philip aliyeishi katika Rumi. Herodias alipata binti mmoja kwa Philip (Salome). Herode Antipa alipoitembelea Rumi alikutana naye na kutongozwa na Heroditas ambaye alikuwa akiangalia maslahi ya kisiasa. Hivyo, Herode Antipa aliachana na mkewe, ambaye alikuwa malkia wa Nabatea na Herodia aliachana na Philip ili yeye na Herode Antipa waweze kuoana. Huyu pia alikuwa dada wa Herode Agrippa I (kama vile Matendo 12).
- C. Tunajifunza juu ya jina la binti wa Herodia, Salome, kutoka kwa Flavius Josephus katika kitabu chake cha *The Antiquities of the Jews* 18:5:4. Lazima huyu alikuwa kati ya umri wa miaka kumi na miwili na kumi na saba kwa wakati huo. Kwa namna iliyo wazi huyu alikuwa akitawaliwa na mamaye na kuongozwa na mamaye. Baadaye aliolewa na Philip yule Mtawala lakini alikuwa mjane kwa muda mfupi.
- D. Miaka ipatayo kumi baada ya kukatwa kichwa kwa Yohana Mbatizaji, Herode Antipa alikwenda Rumi katika kusimikwa kwa mkewe Herodia kuwania cheo cha ufalme kwa sababu ya mfalme Agrippa I, kaka yake, alikuwa amepokea cheo hicho. Lakini Agrippa I aliandika Rumi na kumshtaki Antipa kwa sababu ya

kuungana na wa-Parthia, adui aliyechukiwa na Rumi kutoka Irani (Mesopotamia). Kwa namna iliyo dhahiri Mfalme alimwamini Agrippa I na Herode Antipa, sambamba na mkewe Herodias, aliamishiwa Uhispania.

- E. Inaweza kuwa rahisi kuwakumbuka hawa Ma-Herode tofauti tofauti kama wanavyozungumziwa katika Agano Jipya kwa kukumbuka kwamba Herode Mkuu ndiye aliyewauwa watoto humo Bethlehemu; Herode Antipa ndiye aliyemuua Yohana Mbatizaji; Herode Agrippa I ndiye aliyemuua Mtume Yakobo; na Herode Agrippa II ndiye aliyesikiliza rufani ya Paulo iliyoandikwa katika kitabu cha Matendo ya Mitume

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 14: 1-5

<sup>1</sup>Wakati ule mfalme Herode alisikia habari za Yesu, akawaambia watumishi wake, <sup>2</sup> Huyu ndiye Yohana Mbatizaji; amefufuka katika wafu; na kwa hiyo nguvu hizo zinatenda kazi ndani yake. <sup>3</sup> Maana Herode alikuwa amemkamata Yohana, akamfunga, akamtia gerezani, kwa ajili ya Herodia, mke wa Filipo nduguye. <sup>4</sup> Kwa sababu Yohana alimwa Naye alipotaka kumwua, aliwaogopa watu mbia, Si halali kwako kuwa naye. <sup>5</sup> Naye alipotaka kumwua, aliwaogopa watu, maana walimwona Yohana kuwa nabii.

**14:1 "ule mfalme Herode alisikia habari za Yesu"** Kwa hali dhahiri Mathayo anaweka mabano kati ya Mt. 14:1-2 na Mt. 14:13 inashughulika na kifo cha Yohana Mbatizaji. (Alichokisikia Yesu katika Mt. 14:13 hakikuwa kifo cha Yohana Mbatizaji bali ilikuwa ujumbe kwamba Herode alikuwa amesikia habari kumhusu na kufikiri kuwa Yohana Mbatizaji amefufuka.)

**14:2 "Huyu ndiye Yohana Mbatizaji"** Tazama maelezo katika Luka 9:7-9.

☐ **"na kwa hiyo nguvu hizo zinatenda kazi ndani yake"** Kwa mnamna iliyo wazi Herode alikuwa na nguvu za kishirikina na hili liliongeza kiwango cha hatia yake ya kumkata kichwa Yohana Mbatizaji. Hakuna kumbukumbu za kihistoria za Yohana Mbatizaji kutenda miujiza.

**14:3 "Herode alikuwa amemkamata Yohana, akamfunga, akamtia gerezani"** Tunajifunza kutoka katika kitabu cha Josephus' *Antiquities of the Jews* 18.5.2 kwamba hili lilikuwa gereza la Machaerus (kama vile Mt. 4:12; 11:2). Kwa namna iliyo dhahiri gereza hili lilikuwa refu, lenye kuzungushiwa ngome iliyo himara upande wa kusini mashariki mwa Bahari ya Chumvi mpakani mwa Himaya ya Nabatea. Inafurahisha kuandika kwamba mke wa kwanza wa Herode alifanikiwa kutorokea kwa babaye, Aretas (kama vile 2 Kor.11:32), kwa kuomba kurudi wakati wa mapumziko ya kiangazi. Baadaye, alikuwa na mapigano ya kijeshi na mme wa kwanza wa mke huyu, Herode Antipa, na kumwondosha moja kwa moja. Herode angeondolewa katika utawala endapo mamlaka za Kirumi zisingeingilia.

☐ **"Herodia"** Kitabu cha *The New Testament TransLine* kilichoandikwa na Michal Magill kinao muhtasari mzuri wenye kumzungumzia.

**"Huyu alikuwa mjukuu wa Herode Mkuu, binti wa Aristobulus, dada wa Agrippa I. Tazama 2:1. Aliolewa na Herode Philip I, rafiki wa karibu wa ndugu wa baba yake. Baadaye, alimwacha na kuolewa na Herode Antipas, pia ndugu wa karibu sana na baba yake kwa mwanamke mwingine. Alichagua kwenda uhamishoni akiwa na Antipas wakati alipohamishiwa mnamo 39 b.k " (uk. 49).**

**14:4 "Kwa sababu Yohana alimwambia"** Hiki kitenzi ni kauli ya wakati usio timilifu yenye kumaanisha tendo lililorudiwa rudiwa katika wakati uliopita. Yohana alifanya shutuma za wazi wazi mara kwa mara. Mashtaka haya huenda yalikuwa yakimhusu Herode Antipa na Herodia (mpwa wake) kuona huku wakiwa na uhusiano wa karibu sana (kama vile Law. 18:16), au huenda ni zaidi ya hayo, kwa sababu kila mmoja alikuwa amemtarakisha mwenza wake wa ndoa kinyume na sheria (kama vile Kumb. 24:1-4).

**14:5 "Naye alipotaka kumwua, aliwaogopa watu"** Kifungu hiki kinaonekana kuwa katika mkanganyiko wa moja kwa moja kwa Mt. 14:9. Hata hivyo, kuchanganyikiwa kiakili kwa hawa watawala wa falme za mashariki kulikuwa maarufu sana. Kwa uwazi kulikuwa na hali ya mvuto kwa Yohana kwa sababu mara nyingi Herode alikuwa akimuita Yohana kwa ajili ya kufanya mazungumzo naye (kama vile Marko 6:20), bado kwa wakati mwingine, kulikuwa na woga mkubwa!

☐ **"Naye alipotaka kumwua, aliwaogopa watu"** Katika Mt. 11:7-11 Yesu anaesema kwamba Yohana alikuwa nabii wa mwisho wa Agano la Kale na mtu mkubwa ambaye hakuwa kuzaliwa na mwanamke ye yote chini ya agano la kale. Tazama [MADA MAALUM: UNABII WA AGANO JIPYA](#) katika Mt. 11:9

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 14:6-12**

<sup>6</sup> Hata ilipofika sikukuu ya kuzaliwa kwake Herode, binti Herodia alicheza mbele ya watu, akampendeza Herode. <sup>7</sup> Hata akaahidi kwa kiapo ya kwamba atampa lo lote atakaloliomba. <sup>8</sup> Naye, huku akichochea na mamaye, akasema, Nipe hapa katika kombe kichwa cha Yohana Mbatizaji. <sup>9</sup> Naye mfalme akasikitika; lakini kwa ajili ya viapo vyake, na kwa ajili ya wale walioketi chakulani pamoja naye, akaamuru apewe; <sup>10</sup> akatuma mtu, akamkata kichwa Yohana mle gerezani. <sup>11</sup> Kichwa chake kikaletwa katika kombe, akapewa yule kijana; akakichukua kwa mamaye. <sup>12</sup> Wanafunzi wake wakaenda, wakamchukua yule maiti, wakamzika; kisha wakaenda wakampasha Yesu habari.

**14:6 "Hata ilipofika sikukuu ya kuzaliwa kwake Herode"** Kuna baadhi ya ushahidi wa kale, ushahidi wa kiisimu kwamba kifungu hiki kinaweza kuirejelea siku kuu ya mwaka yenye kutambulisha kusimikwa kwake. Kwa kutoa hukumu yenye kutokana na ushahidi wa kihistoria uliopo, hii ilikuwa sherehe ya kukumbuka siku ya kuzaliwa kwake. Katika matukio haya sikukuu kubwa ilikuwa siku ya utawala.

☐ **"binti Herodia alicheza mbele ya watu"** Kucheza kwa Salome (tazama Josephus, *Antiq.* 18.5.4) lazima kulimshangaza sana kila aliyekuwapo kwa sababu katika siku hizo na wanawake wenye kucheza walifikiriwa kuwa wasio na maadili. Kwa mtoto wa malkia kucheza mbele ya kundi hili la wageni wanywaji, hasa katika umri huu mdogo, lazima ingestaajabisha sana. Dokezo la muktadha huu ni kwamba huku kulikuwa kucheza kwa hisia kulikochochewa na mamaye ili kumshindisha Herode katika kinyang'anyiro cha kusimikwa kwake.

**14:8 "huku akichochea na mamaye"** Hili neno "akichochea" lilikuwa neno la Kiyunani lenye nguvu "akimsihi." Hiii inaonyesha kwamba binti huyu hakuwa anaendeshwa mamaye tu, bali pia alikuwa akitawaliwa naye katika mpango wake wa makusudi wa kumwokoa Yohana Mbatizaji dhidi ya kifo (kama vile Marko 6:22-25).

**14:9 "akasikitika"** Hakuweza kuomba msamaha kwa sababu alikuwa akienda kufanya mauaji ya mtu asiye na hatia, lakini kwa sababu ya alikuwa amekula kiapo (matumizi kiroho ya neno "akakubali," kama vile Luka 22:6) na alikuwa akilazimishwa kukiondoa kiapo hicho mbele ya wageni wanywaji (kama vile Marko. 6:26).

**14:11 "Kichwa chake kikaletwa katika kombe, akapewa yule kijana; akakichukua kwa mamaye"** Hatufahamu mwanamke huyu alikifanyia nini kichwa hiki. Kuna desturi, iliyotajwa na Jerome kwa mara ya kwanza katika karne ya 4 b. k. kwamba mwanamke huyu aliuondoa ulimi wake na kuufunga kwa pini. Neno la Kiyunani "kijana" katika pande zote za binti wa Yairo (kama vile Marko 5:41-42) ambapo alisemekana kuwa na miaka kumi na miwili) na Salome, hivyo, kwa vyo vyoye vile alikuwa katika umri wa kuvunja ungo.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 14:13-14**

<sup>13</sup> Naye Yesu aliposikia; hayo, aliondoka huko katika chombo, akaenda mahali pasipo watu, faraghani. Na makutano waliposikia, walimfuata kwa miguu kutoka mijini mwao. <sup>14</sup> Yesu akatoka, akaona mkutano mkuu, akawahurumia, akawaponya wagonjwa wao.

**14:13 "Naye Yesu aliposikia; hayo"** Hili linaonekana kuirejelea Mt. 14:1 na 2 na si mabano yaliyoingizwa ya Mt. 14:3-12.

☑ **"aliondoka huko katika chombo, akaenda mahali pasipo watu, faraghani"** Haya maelezo ya Yesu kuwalisha watu elfu tano pia yameandikwa katika Marko 6:32-44, Luka 9:10-17, na Yoh. 6:1-13. Kwa uwazi kabisa alitaka kujitenga kwa ajili ya kuomba. Hii ilikuwa desturi yake ya mara kwa mara ambayo ilimsaidia kujiandaa kwa ajili ya kukabiliana na mambo mbalimbali aliyokumbana nayo. Ikiwa Yesu alijitenga kwa ajili ya kuomba, waamini hulifanya hili mara ngapi?

☑ **"Na makutano waliposikia, walimfuata kwa miguu kutoka mijini mwao"** Kamwe Yesu hakuchoka wala kukerwa na umati wa watu, bali mara nyingi alijawa na huruma (kama vile Mt. 14:14). Hii ndiyo dhima katika Injili ya Mathayo (kama vile Mt. 9:36; 15:32). Ingawa Yesu, alikuwa amechoka na kuhitaji muda wa kujitenga kwa ajili ya maombi, bado alizidi kuwaweka watu kipaumbele. Aliwaponywa wote walioletwa kwake, ingawa mara nyingi hakwenda nje ya uponyaji wake. Kwa mara ya kwanza hakutaka kujulikana kama mponyaji bali huruma yake ilijitokeza pale alipomwona mwanadamu hana raha. Uponyaji wa Yesu ulifanya mambo mawili: (1) ulithibitisha ujumbe wake na (2) ulionyesha sifa na uwepo wa ufalme wa ki-Masihi. Yesu anaandikwa kama mwenye kuponya watu mara kadha katika Injili ya Mathayo (kama vile Mt. 4:23; 8:16; 9:35; 14:14; 15:30; 19:2; 21:14). Bado naamini katika Mungu mwenye nguvu aponyaye. Sielewi ni kwa nini Mungu huwaponya baadhi na kutokuwaponya wengine. Naamini kwamba kulikuwa na mkazo wa kipekee kuhusu uponyaji katika karne ya kwanza ili kuuthibitisha ujumbe wa Yesu kama ulivyojitokeza mlipuko wa pepo wa kipekee katika kipindi cha maisha yake. Mkondo huu wenye kufanana unaweza kurudiwa rudiwa kabla ya Kuja kwa mara ya Pili. Tazama Mada Maalum: Je, Uponyaji ni Mpango wa Mungu kwa Kila Enzi? katika Mt. 19:2

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 14:15-21**

<sup>15</sup> Hata kulipokuwa jioni, wanafunzi wake walimwendea, wakasema, Mahali hapa ni nyika tupu, na saa imekwisha pita; uwaage makutano, waende zao vijijini, wakajinunulie vyakula. <sup>16</sup> Yesu akawaambia, Hawana haja kwenda zao, wapeni ninyi vyakula. <sup>17</sup> Wakamwambia, Hamna kitu hapa ila mikate mitano na samaki wawili. <sup>18</sup> Akasema, Nileteeni hapa. <sup>19</sup> Akawaagiza makutano waketi katika majani; akaitwaa ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama juu mbinguni, akabariki, akaimenga ile mikate, akawapa wanafunzi, wanafunzi wakawapa makutano. <sup>20</sup> Wakala wote wakashiba; wakayaokota masazo ya vipande vya mikate, vikapu kumi na viwili, vimejaa. <sup>21</sup> Nao waliokula walikuwa wanaume wapata elfu tano, bila wanawake na watoto.

**14:15 "Hata kulipokuwa jioni"** Tazama Mt. 14:23. Mathayo anawaiwasilisha sura hii kama siku moja katika maisha ya Yesu (kama vile Mt. 14:23). Inadhaniwa kwamba Wayahudi wa siku za Yesu walikuwa na asubuhi iliyowahi kuingia na jioni yenye kuchelewa. Yenye kuwahi ingeanzia saa 3 aduhuri wakati sadaka za jioni zilipokuwa zinateketezwa Hekaluni. Kwa wakati mwingine nyingine ingeteketuzwa wakati wa machweo ya jua.

☑ **"Mahali hapa ni nyika tupu"** Nahau hii ilimaanisha kwamba hapakuwa na mji mkubwa au kijiji kilichokuwa karibu, si kwamba mahali hapa palikuwa jangwa kiasi cha kutokaliwa na watu.

**14:16** Kwa namna iliyo dhahiri Yesu aliwaambia wanafunzi kuwapa chakula watu hawa (kama vile Marko 6:37). Hiki kifungu "Wapeni ninyi chakula" ni cha msisitizo katika andiko la Kiyunani. Walistaajabu. Hii ilikuwa nafasi ya mafunzo kwao, kama ilivyokuwa wakati wa tufani (kama vile Mt. 14:32).

**14:17 "ila mikate mitano na samaki wawili"** Hiki kilikuwa chakula cha mtoto mmoja (kama vile Yohana 6:9). Wafasiri wenye hofu kuhusu miujiza (William Barclay na wanauyakiniifu wa kimantiki) wanajaribu kusema kwamba kilichotokea ni kwamba mtoto huyu mdogo alishiriki chakula na wengine waliokuwa wameleta vyakula vyao walishiriki, kitu ambacho kilisababisha kila mmoja kupata chakula cha kutosha. Huu ni mfano wa mara kwa mara wa mawazo ya awali ya mtu ya kuifasiri kinyume maana ya kibiblia iliyokusudiwa na mwandishi. Je, hivi vikapu kumi na viwili vilivyojaa vililitoka wapi ikiwa kulikuwa na ushiriki wa vyakula? Pia tambua kwamba Yesu kwa uweza



wake aliigawa mikate; lakini hakupoteza hata mmoja kwa sababu wanafunzi waliokota okota vipande vidogo vidogo kwa ajili ya kula baadaye. Mazidisho haya ya chakula lilikuwa jaribio halisi la Yule mwovu katika Mt. 4:1-4, ili Yesu ajilishe kwa uhitaji la kibinadamu. Moja ya sababu zilizomfanya Yesu kujitega peke yake kwa ajili ya kuomba ilikuwa ni jaribio hili la awali. Watu walitaka kumfanya "mfalme wa mikate" (kama vile Yohana. 6:15).

**14:18 "Nileteeni hapa"** Yesu alilifanya hili si kwa ajili ya kuwalisha watu tu, bali kuwafundisha wanafunzi na kuijenga imani yao. Hii ndiyo sababu halisi ya miujiza yake mingi. Huru kwa kila muhitaji na shauku ya kujenga imani ya wanafunzi wake vilikuwa vivutio pacha vya miujiza.

Tendo hili la kulisha pia lina maana ya Masihi wa Kiyahudi. Wayahudi walimtarajia Masihi kufanya matendo kama ya Musa. Hii mana mpya inaweza kuwa moja ya tendo hili (kama vile Yohana. 6).

**14:19 "Akawaagiza makutano waketi katika majani"** Kifasihi huku ni kusema "kutazamishakatika kioo." Hapa palikuwa mahali pa kulia katika Palestina. Hawa walikuwa makundi ya mamia na maelfu (kama vile Marko 6:39-40). Kuwepo kwa majani haya, yaliyo na hali ya ujani ilimaanisha kwamba huenda ilikuwa wakati wa masika.

☐ **"akatazama juu mbinguni, akabariki"** Ukawaida wa maombi ya Wayahudi ilikuwa ni pamoja na kuinua macho na mikono kuelekea mbinguni. Haikuwa kawaida kwao kupiga magoti wakati wa kuomba. Tendo letu la sasa la kushusha mikono na kuinua macho yetu linatokana na fumbo la Mafarisayo na mtenda dhambi. Ikiwa tunaviinamisha vichwa vyetu na kufumba macho yetu, kuwa kweli kibiblia pia yatupasa kupiga piga vifua vyetu (kama vile Luka 18:9-14)!

**14:20 "vikapu kumi na viwili, vimejaa"** Tazama Mada Maalum hapa chini.

### **MADA MAALUMU: HESABU YA KUMI NA MBILI)**

Kumi na mbili mara nyingi imekuwa ya kiishara (Angalia [Mada Maalum: Namba za Kiishara katika Andiko](#)) namba ya shirika

- A. Nje ya biblia
  1. Ishara kumi na mbili za ukanda
  2. Miezi kumi na miwili ya mwaka
- B. Katika Agano la Kale (BDB 1040 kuongeza 797)
  1. wana wa Yakobo (Makabila ya Kiyunani)
  2. waliotazamishwa kwenye
    - a. Nguzo kumi na mbili za madhabahu katika Kut. 24:
    - b. Vito kumi na viwili juu ya kifua cha kuhani mkuu (ambayo vinasimama kwa niaba ya makabila) katika Kut. 28:21
    - c. unga mwembamba wa mikate kumi na miwili katika sehemu takatifu ya kibanda katika Law. 24:5
    - d. wapelelezi kumi na wawili waliotumwa huko Kanaani katika idadi ya kabila (mmoja kutoka katika kila kabila)
    - e. fimbo kumi na mbili (viwango vya kikabila) katika uasi wa Kora katika Hes. 17:2
    - f. mawe kumi na mawili ya Yoshua katika Yos. 4:3,9,20
    - g. majimbo kumi na mawili ya kiutawala katika utawala wa Suleimani katika 1 Fal. 4:7
    - h. mawe kumi na mawili ya madhabahu ya YHWH katika 1 Fal. 18:31
- C. Katika Agano Jipya
  1. Mitume kumi na wawili waliochagulwa
  2. Vikapu kumi na viwili vya mikate (kimoja kwa kila Mtume) katika Mat. 14:20
  3. Viti kumi na viwili vya enzi ambapo Wanafunzi wa Agano Jipya wamekaa (vinayorejea juu ya makabila 12 ya Israeli) katika Mt. 19:28
  4. majeshi kumi na mawili ya malaika wa kumsaidia Yesu katika Mt. 26:53

5. Ishara ya Ufunuo
  - a. Wazee 24 juu ya viti 24 4:4
  - b. 144,000 (12x12,000) katika 7:4; 14:1,3
  - c. nyota kumi na mbili juu ya taji la mwanamke katika 12:1
  - d. malango kumi na mawili, malaika kumi na wawili wakiakisi makabila kumi na mawili katika 21:12
  - e. Mawe kumi na mawili ya misingi ya Yerusalemu mpya na juu yao majina ya mitume kumi na mawili katika 21:14
  - f. Mianzi kumi na mbili elfu katika 21:16 (kipimo cha mji mpya, Yerusalemu Mpya)
  - g. kuta ni dhira 144 katika 21:17
  - h. malango kumi na mawili ya lulu katika 21:21
  - i. miti mipya katika Yerusalemu yenye aina aina kumi na bili za tunda (moja kwa kila mwezi) katika 22:2

**14:21 "Nao waliokula walikuwa wanaume wapata elfu tano, bila wanawake na watoto"** Kwa namna fulani hili ni eneo lililojitenga, huenda hapakuwa na wanawake wengi sana isipokuwa kuwepo kwa sababu ya kuumwa na kwa hitaji la uponyaji. Idadi kamili imekuwa ipatayo elfu sita au saba lakini hili halijulikani vizuri.

Kwa kuwa Injili ya Mathayo inawaelekea moja kwa moja viongozi wa Kiyahudi, jambo hili linaweza kuwa linazungumzia suala la kitamaduni la wanaume kula peke yao mbali na wanawake na watoto (kama vile NASB Study Bible, tanbihi, uk. 1389).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 14:22-27**

<sup>22</sup>Mara akawalazimisha wanafunzi wake wapande chomboni na kutangulia mbele yake kwenda ng'ambo, wakati yeye alipokuwa akiwaaga mkutano. <sup>23</sup>Naye alipokwisha kuwaaga makutano, alipanda mlimani faraghani, kwenda kuomba. Na kulipokuwa jioni, alikuwako huko peke yake. <sup>24</sup> Na kile chombo kimekwisha kufika katikati ya bahari, kinataabika sana na mawimbi; maana upepo ulikuwa wa mbisho. <sup>25</sup> Hata wakati wa zamu ya nne ya usiku Yesu akawaenda, akienda kwa miguu juu ya bahari. <sup>26</sup> Wanafunzi walipomwona akienda juu ya bahari, wakafadhaika, wakisema, Ni kivuli; wakapiga yowe kwa hofu. <sup>27</sup> Mara Yesu alinena, akawaambia, Jipeni moyo ni mimi; msioope.

**14:22 "Mara akawalazimisha wanafunzi wake wapande chomboni"** Sababu iliyomfanya Yesu kuwalazimisha wanafunzi wake wapande chomboni haikubainishwa. Hii inaweza kuhusisha

1. matendo ya makutano yasiyo faa (kama vile Marko 6:15)
2. mfano mwingine wa nguvu zake za ajabu ilil kujenga imani ya wanafunzi (kama vile Marko 6:45-51; Yohana. 6:15- 21)

☐ **"wakati yeye alipokuwa akiwaaga mkutano"** Walishikwa na mshangao kutokana na muujiza huu wa kulisha watu na kutaka kumfanya kuwa mfalme (kama vile Yohana. 6:15). Hili ndilo jaribu la yule Ibilisi lililo katika Mt. 4:1-4 lenye kuzungumzia kugeuza mawe kuwa mkate. Ni kwa sababu hii iliyomfanya Yesu aondoke upesi, kuomba na kuzungumza na Baba kuhusu huduma yake inayofuatia. Kulikuwa na mkanganyiko mkubwa miongoni mwa watu kuhusiana na uponyaji wake na, hapa, tendo la kulisha makutano.

**14:23 "alipanda mlimani faraghani, kwenda kuomba"** Hili ndilo kusudi halisi lililo katika Mt. 14:13. Kwa kurudia rudia Injili zinanukuu kuwa Yesu alijitenga kwa ajili ya kuomba. Ikiwa Yeye, kuwa Mungu aliyetwaa Mwili, alilhitaji hili, je! Yatupasa sisi mara ngapi?

**14:24 "kile chombo kimekwisha kufika katikati ya bahari"** Marko 6:47 anasema chombo kimekwisha kufika katikati ya bahari.

**14:25**

NASB, NKJV

NJB "wakati wa zamu ya nne ya usiku "

NRSV "asubuhi na mapema"

TEV "kati ya saa tisa na saa kumi na mbili kamili asubuhi"

Hili ni neno la kiufundi la uchaguzi wa muda wa awamu ya nne ya Kirumi ya usiku wa manane, ambayo ilikuwa saa 3 usiku hadi saa 6 alfajiri. (kama vile Marko 13:35). Kiuhalisia Wayahudi walikuwa na vipindi vitatu tu vya wakati katika masaa ya usiku (kama vile Amu. 7:19; Omb. 2:19), bali wakati wa kipindi cha Kirumi walianzisha mgawanyo fungamano wa awamu ya nne. Tambua kwamba Yesu alikuwa katika maombi takribani usiku mzima.

☐ "akawaendea, akienda kwa miguu juu ya bahari" Kwa kuwa mawimbi na upepo vilikuwa vimeinuka, Ilimpasa kuja katika hayo na nje ya mwonekano kadri mawimbi yalivyokuwa yakikiinua chombo. Hapa tena Yesu anaonyesha uweza wake juu ya asili. Tunajifunza kutokana na Injili nyingine kwamba Yesu alimaanisha kutangulia mbele yao lakini, kwa sababu ya woga wao, aliingia chomboni pamoja nao.

**14:26 "Ni kivuli"** Kwa hakika hili ndilo alilo lisema wakiwa Ghorofani katika Luka 24:37. Walishikwa na hofu. Maneno ya Yesu ya mwanzo kwao yalikuwa "msiogope" (kauli shurutishi ya wakati uliopo yenye kiambata hasi. Maneno haya yenye kutia moyo yanarudiwa mara kwa mara katika (kama vile Mt. 14:27; 17:7; 28:19; Marko 6:50; Luka 5:10; 12:32; Yohana. 6:20; Ufu. 1:17)

**14:27** Yesu anawapa wanafunzi wake amri mbili.

1. NASB, "Jipeni moyo"  
NKJV, "iweni na furaha"  
NRSV, "tulizeni mioyo"  
TEV, NJB, "jitieni moyo"

Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Yesu anazungumza maneno haya mara kwa mara kwa

- a. mtu mwenye kupooza, Mt. 9:2
  - b. mwanamke mwenye kutoka damu, Mt. 9:22
  - c. wanafunzi walipokuwa chomboni, Mt. 14:27; Marko 6:50
  - d. mwanamme kipofu Marko 10:49
  - e. wanafunzi akiwa ghorofani, Yohana 16:33
  - f. Paulo, Matendo 23:11
2. "msiogope"— Hii ni kauli ya kati / tendwaji shurutishi yenye ushahhidi ya wakati uliopo. Yesu anazungumza maneno haya kwa
    - a. Wanafunzi wakiwa chomboni, Mt. 14:27; Marko 6:50; Yohana 6:20
    - b. Petro baada ya kuvua samaki wengi, Luka 5:10
    - c. Wanafunzi wakati alipokuwa akiwafundisha, Luka 12:32
    - d. katika kubadilika sura kwake, Mt. 17:7
    - e. wnwake walipokuwa kaburini, Mt. 28:10
    - f. Paulo huko Korintho, Matendo 18:9
    - g. Paulo huko baharini, Matendo 27:24
    - h. Yohana akiwa Patmo, Ufu. 1:17 Haya maneno yenye kufanana yalizungumzwa na malaika kwa
      1. Zakaria, Luka 1:13
      2. Mariamu, Luka 1:30
      3. wachungaji, Luka 2:10
      4. wanawake alipokuwa kaburini, Mt. 28:5

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 14:28-33**

<sup>28</sup> Petro akamjibu, akasema, Bwana, ikiwa ni wewe, niamuru nije kwako juu ya maji. <sup>29</sup> Akasema, Njoo. Petro akashuka chomboni, akaenda kwa miguu juu ya maji, ili kumwendea Yesu. <sup>30</sup> Lakini alipouona upepo, akaogopa; akaanza kuzama, akapiga yowe, akisema, Bwana, niokoe. <sup>31</sup> Mara Yesu akanyosha mkono wake,

**akamshika, akamwambia, Ewe mwenye imani haba, mbona uliona shaka? <sup>32</sup> Nao walipopanda chomboni, upepo ulikoma. <sup>33</sup> Nao waliokuwamo ndani ya chombo wakamsujudia, wakisema, Hakika wewe u Mwana wa Mungu.**

**14:28 "Petro akamjibu"** Tukio hili limeandikwa katika Injili ya Mathayo. Petro alikuwa mtu mtundu sana. Alikuwa na mchanganyiko wa imani na mashaka makubwa.

☐ **"ikiwa ni wewe"** Hii ni sentensi amrishi daraja la kwanza, yenye kufikiwa kuwa ya kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au sababu zake za kiuandishi. Petro alitambua ya kuwa huyo alikuwa Yesu.

**14:30 "Lakini alipouona upepo"** Huyu aliuona na kuusikia upepo na mawimbi na kuanza kupoteza mwelekeo wa imani yake.

☐ **"Bwana, niokoe"** Huu ni mfano mzuri wa neno "kuokolewa" lilitumika katika maana ya Agano la Kale ya kifungu "ukombozi wa kimwili" (kama vile Yakobo 5:15).

**4:31 "Ewe mwenye imani haba"** Hii ni dhima ya mara kwa mara katika Injili ya Mathayo (kama vile Mt. 6:30; 8:26; 16:8). Miujiza mingi ya Yesu alifanyika ili kuongeza kiwango cha mani ya wanafunzi wake. Mungu hutenda kazi pamoja na wale wenye imani haba. Amina!

**14:32 "wakamsujudia, wakisema, Hakika wewe u Mwana wa Mungu"** Yesu alikukubali kusujudiwa huku. Ni mara ngapi walikuwa wakielewa kwa ufasaha neno "Mwana wa Mungu" (tazama Mada Maalum katika Mt. 27:54) na ni kwa namna gani walielewa kwa kuviona na kuvisikia vipengele vya uweza wake wa huduna yake haijulikani. Mara nyingi hili linaanzisha hatua ya ukiri wa kithiolojia wa Mt. 16:16. Injili ya Mathayo haionyeshi kifungu "siri ya ki-Masihi" kwa kadri ilivyofanya Injili ya Marko (yaani., Marko 6:52).

Hili neno "Mwana wa Mungu" lilitumika mara kawa mara hasa katika Injili ya Mathayo (kama vile Mt. 4:3,6; 16:16; 26:63; 27:40,43,54). Hakuna kibainishi cha neno mahali hapa kama ilivyo katika Luka 27:54. Wengi wanadhani kwamba hili lilimaanisha kwamba hawa hawakuwa na dondoo za kutosha kithiolojia, ambazo zilidokeza Uungu. Hili linaweza kuwa sawa. Uelewa wao ulikuwa endelevu na si wa ghafla. Lakini ni hatari sana kuijenga thiolojia ya kiwango cha juu katika uwepo au kutokuwepo kwa kibainishi cha Kiyunani!

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 14:34:36**

<sup>34</sup> Na walipokwisha kuvuka, walifika nchi ya Genesareti. <sup>35</sup> Na watu wa mahali pale walipomtambua, walituma watu kwenda nchi zile zilizo kandokando, wakamletea wote waliokuwa hawawezi; <sup>36</sup> nao wakamsihi waguse hata pindo la vazi lake tu; na wote waliogusa wakaponywa kabisa

**4:34 "Na walipokwisha kuvuka, walifika nchi ya Genesareti"** Kuna utata katika maneno "kuvuka" Katika Marko 6:45 kulikuwa na eneo lililoitwa Bethsaida lenye maana ya "nyumba ya samaki." Lazima kuwepo na Bethsaida za aina mbili au hata kuna baadhi ya mikanganyiko katika jiografia ya maelezo mbalimbali ya Vidokezo vya Injili. Yesu alikuwa akiishi katika himaya ya Mfalme Filipo na si kurudi katika himaya ya Mfalme Herode. Eneo la Gennesareti hapo awali lilikuwa eneo la Mataifa. Huenda hii ilikuwa jia yake ya kuyatoroka makutano ya Kiyahudi kama ambavyo baadaye angelikwenda huko Kaizaria Filipi.

**14:35 "Na watu wa mahali pale walipomtambua"** Jambo halisi lenye kufanana ambalo linatokea katika Mt. 14:13 linatokea tena na Yesu kwa mara nyingine aliuutumia nuda wake kuwahudumia watu walio wahitaji. Hawa walikuwa na imani ya miujiza inayofanana Hawa walikuwa na asili ya nguvu za imani zinazofanana kama ilivyokuwa kwa mwanamke aliyekuwa anatoka damu katika Mt. 9:20- walitaka kuligusa pindo la vazi lake (kama vile Mt. 14:36). Yesu alikubali na kutenda kazi hata na hawa wenye imani haba. Huruma yake inaweza kuonekana dhahiri hata kwa hawa wenye wenye nguvu fulani lakini

wasio Wayahudi.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini mistari ya 3-12 inafikiriwa kuwa mabano?
2. Je! Unaweza kuitambua tofauti ya ma-Herode waliotajwa katika Agano Jipya?
3. Kwa nini Herodia alimkasirikia sana Yohana Mbatizaji?
4. Nini kusudi la miujiza ya Yesu?
5. Kwa nini Yesu aliwalisha makutano mara mbili baada ya kulishinda jaribu la Ibilisi katika Mathayo 4:1-4?
6. Ni kwa namna gani hali ya woga wa Petro na wanafunzi inatusaidia sana katika imani yetu?

## MATHAYO 15

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Mapokeo ya Wazee	Unajisi hutoka Ndani	Mapokeo ya Wazee	Mafundisho ya Wahenga	Mapokeo ya Mafarisayo
15:1-9	15:1-20	15:1-9	15:1-2	15:3-9
15:1-9				
(8-9)				(8-9)
Mambo yawezayo Mtu kuwa najisi	Mtu Aliye safi na Asiye Safi			
15:10-20		15:10-20	15:10-11	15:10-11
			15:12	15:12-14
			15:13-14	
			15:15	15:15-20
Imani ya Mwanamke Mkananayo	Mataifa Yaonyesha Imani Yake	Mwanamke Mkananayo	Imani ya Mwanamke	Binti wa Mwanamke Mkananayo Aponywa
15:21-28	15:21-28	15:21-28	15:21-22	15:21-28
			15:23	
			15:24	
			15:25	
			15:26	
			15:27	
			15:28	
Uponyaji wa Watu Wengi	Yesu Anawaponya Makutano Makubwa	Uponyaji	Yesu Anawaponya Watu Wengi	Tiba kandokando ya Ziwa
15:29-31	15:29-31	15:29-31	15:29-31	15:29-31
Kulisha	Kulisha Watu	Elfu Nne	Yesu Awalisha	Muujiza wa

Elfu Nne	Elfu Nne	Walishwa	Elfu Nne	Mikate
15:32-39	15:32-39	15:32-39	15:32	15:32-39
			15:33	
			15:34a	
			15:34b	
			15:35-38	
			15:39	

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)")** **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 15:1-11**

<sup>1</sup>Ndipo Mafarisayo na waandishi toka Yerusalemu walipomwendea Yesu wakisema, <sup>2</sup> Mbona wanafunzi wako huyahalifu mapokeo ya wazee, kwa maana hawanawi mikono walapo chakula. <sup>3</sup> Akajibu, akawaambia, Mbona ninyi nanyi huihalifu amri ya Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu? <sup>4</sup> Kwa kuwa Mungu alisema, Mheshimu baba yako na mama yako, na Amtukanaye baba yake au mama yake kufa na afe. <sup>5</sup> Bali ninyi husema, Atakayemwambia babaye au mamaye, Cho chote kikupasacho kusaidiwa na mimi ni wakfu, <sup>6</sup> basi asimheshimu baba yake au mama yake. Mkalitangua neno la Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu. <sup>7</sup> Enyi wanafiki, ni vema alivyotabiri Isaya kwa habari zenu, akisema,

<sup>8</sup>Watu hawa huniheshimu kwa midomo;

Ila mioyo yao iko mbali nami.

<sup>9</sup>Nao waniabudu bure,

Wakifundisha mafundisho Yaliyo maagizo ya wanadamu.

<sup>10</sup> Akawaita makutano akawaambia <sup>11</sup> Sikilizeni, mfahamu; Sicho kiingiacho kinywani kimtiacho mtu unajisi; bali kitokacho kinywani ndicho kimtiacho mtu unajisi.

**15:1 "Mafarisayo"** Hawa walikuwa viongozi wa kidini walioonekana kwa nje kidhehebu katika karne ya kwanza ya dini ya Kiyahudi. Hawa walipata umaarufu kipindi cha Kimakabayo. Jina hili inaweza kuwa limemaanisha "waliojitenga." Yesu hakuwatuhumu Mafarisayo wote bali wale walioonekana kuishika sheria kwa nje pasipokuwa wenye haki ndani yao (Isa. 29:13). Walitia mkazo juu ya usawa wa mapokeo ya fasihi ambayo baadaye yaliwekwa

katika kanuni katika Kitabu cha Sheria za Kiyahudi. Kwa mjadala mzima wa chimbuko na thiolojia ya Mafarisayo tazama Mada maalum katika Mt. 22:15.

☐ **"waandishi"** Hili lilikuwa kundi la wanasheria wa kidini lenye weledi, waliochukua mafunzo ya sheria zilizoandikwa na mapokeo ya fasihi simulizi, ambao waliowekwa ili kutoa mapendekezo juu ya sheria za Kiyahudi zilizohusu maisha ya kila siku. Tazama Mada Maalum katika Mt. 12:38.

☐ **"toka Yerusalemu"** Kwa wakati huu Yesu alikuwa Galilaya hivyo watu hawa walitembea mwendo mrefu kwa ajili ya kumsikiliza. Hawa walikuwa, endapo ungeifurahia, mamlaka itokayo makao makuu!

**15:2 "wanafunzi wako"** Wanafunzi hawa toka Galilaya, mahali ambapo Dini ya Kiyahudi haikuwa na makali sana kana ilivyokuwa katika eneo la Yerusalemu.

☐ **"mapokeo ya wazee"** Hii ilikuwa rejea ya kundi kubwa la mapokeo ya fasihi simulizi lililoitwa *Mishnah*, lililokuwa likifasiri Sheria ya Musa na kusidia matumizi yake katika maisha ya kila siku. Hii *Mishnah* iliunganishwa zaidi na kukamilishwa na Rabbi Judah mnamo 200 b.k. na baadaye kuwa sehemu ya Kitabu cha Sheria. Iliaminiwa na walimu wa sheria za kiyahudi kuwa kama ya amri kama ilivyo Torati (Mwa-Kumb.), kwa hiyo, pia, iliaminiwa kuwa hii nayo Mungu alimpa Musa kwa njia ya mapokeo (kama vile Kumb. 4:14).

☐ **"hawanawi mikono walapo chakula"** Tendo la kunawa mikono halikuwa kwa makusudi ya kiafya bali kwa taratibu zihusozo usafi. Agano la Kale lilihitaji tendo la kunawa mikono kwa kila mlo, lakini mapokeo haya yaliendelea (1) kutokana na Kut. 30:19 ambapo makuhani walikuwa wakinawa na (2) Mambo ya Walawi 15, ambapo wale waliokuwa wakitaja kitu kisicho safi iliwapasa kunawa. Kwa kipindi cha Yesu kunawa kabla ya kula ilikuwa sehemu kubwa ya maisha ya dini ya Kiyahudi. Mwalimu mmoja wa sheria za Kiyahudi alitengwa kwa sababu ya kutonawa mikono vema! Si tendo la kunawa mikono kabla ya kula tu lililoagizwa, bali kunawa baada na hata katika utaratibu binafsi jambo hili pia nalo lilifikiriwa kuwa mila ya wajibu wa kidini.

**15:4 "Mungu alisema"** Marko 7:11 ina kifungu "Musa alisema." Hii inaonyesha mtazamo wa Yesu wa mamlaka na uvuvio wa Agano la Kale (kama vile Mt. 5:17-19).

☐ **"Mheshimu baba yako na mama yako"** Yesu ananukuu moja ya Amri Kumi (kama vile Kut. 20:12; Kumb. 5:16). Neno "Mheshimu" lilikuwa neno la kibiashara lililomaanisha "kutoa kulingana na uzito."

☐ Nukuu ya pili ya Agano la Kale iliyo katika Mt. 15:4 inatoka katiika Kut. 21:17 au Law. 20:9. Utulivu wa jamii ulitegemea uharaka na uhimara wa tendo dhidi ya wale waliyoyaiuka mahitaji ya agano. Familiya ilikuwa/ilijikita katika jamii.

☐ **"Amtukanaye baba yake au mama yake kufa na afe."** Tazama Kut. 21:17 na Law. 20:1.

**15:5**

**NASB, NRSV** " na mimi ni wakfu"

**NKJV** "amejitoa kwa ajili ya hekalu"

**TEV** "ni wa Mungu"

**NJB** "amejitoa kwa Mungu"

Hii dhana ya kula kiapo au kujitoa kwa ajili ya isiyohitaji cho chote toka kwa Mungu iliitwa *corban* (kutoka neno la Kiebrania "matoleo" kama vile Law. 1:2; 22:27; 23:14; Hes. 7:25) au "chini ya pishi" (kama vile Marko 7:11).



Kiapo hiki kilivifanya vitu hivi kutopatikana kisheria kutumika katika kuwasaidia wazazi walio wazee (japo vingeweza kutumika kwa makusudi ya mtu mwingine).

**15:6**

**NASB** "asimheshimu"

**NKJV** "amewekwa huru kutomuheshimu"

**TEV** "hawahitaji kumheshimu"

**NJB** "yuko huru kufanya yampasayo"

Ingawa hili halikuelezwa katika Lugha ya Kiingereza kifungu hiki ni

1. ukanushi mara dufu wenye nguvu
2. kinamaanisha swali
3. nukuu inayotokana na maandiko (au maana ya) Mafarisayo/Waandishi

**NASB** "Mkalitangua"

**NKJV** "hakuna matokeo"

**NRSV** "tupu"

**NJB** "hakuna matunda"

Hili ni neno la Kiyunani linalotumika hapa tu na ufanano wake ulio katika Marko 7:13 na katika Gal. 3:17. Kwa shauku zao na matendo yao kusudi la Maandiko lilikuwa kuiomdoa hasira ya kibinadamu! Watu hawa walioonekana kuwa wa kidini, lakini ushahiidi wa Anguko lao ulibakia (yaani., zaidi kwangu kwa gharama yo yote).

☐ **"kwa ajili ya mapokeo yenu"** Neno hili (*pardosis*) linatumika katika maana kadhaa.

1. katika 1 Kor. 11:2,23 kwa ajili ya kweli ya injili
2. katika Mt. 15:6; 23:1 na kuendelea ; Marko 7:8; Gal. 1:14 juu ya tamaduni za Kiyahudi
3. katika Kol. 2:6-8 juu ya madhahanio ya mafunuo ya uongo
4. Kanisa la Katoliki linautumia mstari huu kama uchunguzi wa kibiblia wa Maandiko na mapokeo kuwa sawa katika mamlaka.

Hata hivyo, katika muktadha huu kifungu hiki kinairejelea ile kweli ya Kitume, iwe ni ya kimazungumzo au iliyoandikwa (kama vile 2 Thes. 3:6)

**15:7 "Enyi wanafiki"** Hili lilikuwa neno la kisanaa kifasihi ni "kutoa hukumu" lakini katika maana ya "kucheza nje ya mwonekano."

**15:8-9 "Watu hawa huniheshimu kwa midomo"** Hii ni nukuu toka katika Agano la Kale la Kiebrania la kifungu cha Isa. 29:13. Mstari huu wenye nguvu unaonyesha kwamba imani ya mtu binafsi inafunuliwa dhahiri kwa matendo yake ya nje na maneno yao (kama vile Rum. 4:3-6; Yakobo 2:14-26).

**15:8 "mbali nami"** Kifungu hiki kiazungumzia wazo la kushikilia kitu fulani au mbali na mkono.

**15:10 "Akawaita makutano"** Yesu aliwapinga hadharani hawa viongozi wa kidini toka Yerusalemu.

**15:11 "Sicho kiingiacho kinywani kimtiacho mtu unajisi"** Kimsingi kifungu hiki kilihusiana na swali lililohusu kunawa mikono (kama vile Mt. 15:18,20), lakini Marko 7:19 inaongeza kifungu kinaongeza kifungu kinachohusiana

na usemi wa vyakula vyote (kama vile Matendo 10). Utakaso unatoka ndani na unatoa mwongozo/kuelekeza kazi za nje.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 15:12-14**

<sup>12</sup> Ndipo wanafunzi wake walipomwendea, wakamwambia, Wajua ya kuwa Mafarisayo walipolisikia neno lile walichukizwa? <sup>13</sup> Akajibu, akasema, Kila pando asilolipanda Baba yangu wa mbinguni litang'olewa. <sup>14</sup> Waacheni; hao ni viongozi vipofu wa vipofu. Na kipofu akimwongoza kipofu mwenzake, watatumbukia shimoni wote wawili.

**15:12 "Mafarisayo walipolisikia neno lile walichukizwa"** Wanafunzi walitishwa na usemi huu wa viongozi wa kidini, Usemi wake kuhusu mapokeo ya fasihi simulizi, na kwa maana, upinzani wake kuhusu sheria za vyakula vya Law. 11.

**15:13 "Kila pando asilolipanda Baba yangu wa mbinguni litang'olewa"** Kwa vyo vyote hiki kiliyarejelea mafundisho ya Mafarisayo au kwa Mafarisayo wenyewe. Ilionyesha kwamba haya hayakuwa ya Mungu (kama vile Mt.5:20; 16:6,11). U dini unaweza kuwa jambo la hatari (kama vile Rum. 2:17-29). Amani kwa gharama yo yote haikuwa njia ya Yesu!

Inawezekana kwamba Yesu anaeleza pando hili kwa taswira toka Isa. 60:21; 61:3. Israeli anatoa maelezo katika maneno ya kilimo (kama vile Isaya 5; Yohana 15). Israeli ni mzabibu wa YHWH uliochaguliwa, uliochaguliwa kujifunua wenyewe kwa mataifa! Kama Israeli ilivyoshindwa, ndivyo ilivyokuwa theolojia ya Kithiolojia. Dhambi kubwa karibia na kutokuamini ni kujihesabia haki!

**15:14** Hii ni sentensi amrishi daraja la tatu, yenye kurejelea tendo lenye umuhimu.

☑ **"vipofu"** Neno hili linatumika kistiari kuelezea uelewa wa kiroho wa Mafarisayo na wanafunzi wao (kama vile Mathayo 23, hasa Mt. 15:16,24).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 15:15-20**

<sup>15</sup> Basi Petro akajibu, akamwambia, Tueleze mfano huo. <sup>16</sup> Yesu akasema, Hata sasa ninyi nanyi mngali hamna akili? <sup>17</sup> Hamjafahamu bado ya kuwa kila kiingiacho kinywani hupita tumboni, kikatupwa chooni? <sup>18</sup> Bali vitokavyo kinywani vyatoka moyoni; navyo ndivyo vimtiavyo mtu unajisi. <sup>19</sup> Kwa maana moyoni hutoka mawazo mabaya, uuaji, uzinzi, uasherati; wivi, ushuhuda wa uongo, na matukano; <sup>20</sup> hayo ndiyo yamtiayo mtu unajisi; lakini kula kabla hajanawa mikono hakumtii mtu unajisi.

**15:15-20** Kipengele hiki kinazungumzia hitaji la ulinganifu wa wa kiroho kati ya uhuru katika Kristo na jukumu la kujitawala nje ya upendo wa Kristo na wengine (kama vile Rum. 14:1-15:13; 1 Kor. 8; 10:23-33; 1 Tim. 4:4; Tito 1:15).

**15:16 "ninyi nanyi mngali hamna akili"** Kifungu hiki ni adimu, nahau ya Kiebrania yenye msisitizo. Hata wanafunzi hawakuelewa hadi baada ya ufufuko (kama vile Luka 24:45, pia tazama Luka 24:16,31; Matendo 16:14; 1 Yohana 5:20).

**15:18** Ni chakula cha aina gani awezacho kula mtu au asichoweza kula hiyo si sababu bali moyo wa mtu (kama vile Mt. 12:34; Marko 7:20). Kwa semi hizi Yesu alizipinga sheria za vyakula za Mambo ya Walawi 11! Mara nyingi Yesu anasemekana kuzipinga desturi za mapokeo ya walimu wa sheria, lakini alilikubali Agano la Kale. Hata hivyo, kwa

mfano huu na kwa suluhisho lake kuhusu talaka (kama vile Mt. 5:31-32; 19:8-9) alizibadili sheria za Agano la Kale. Ni vizuri zaidi kuikiri haki ya Yesu na uvuvio ili kuzifasiri tena desturi za mapokeo ya Agano la Kale na mila za walimu washeria za kiyahudi pasipo kuliweka hili katika uvuvio wa kulifasiri katika kanuni ya ufasiri wa kibiblia. Wafasiri wa sasa hawakuvuviwa bali wameangazwa. Tunayakiri mafundisho ya Yesu, lakini tunathubutu kutoifuata mbinu yake ya ufasiri wa biblia!

☐ **"moyoni"** Tazama Mada Maalum katika Mt. 5:8.

**15:19 "uasherati"** Neno la Kiingereza "picha zinazohamasisha ngono" linashiriki mzizi wa neno lile lile kama lilivyo neno hili la Kiyunani. Iliimaanisha tendo la kujamiina kwa usahihi, mapenzi ya nje ya ndoa, ngono za jinsia moja, usagaji, na hata kukiuka majukumu ya kilawi (ndugu kufanya tendo la kujamiiana linalohusiana na mjane wa ndugu yake ili kuuteka urithi).

Katika Agano la Kale kulikuwa na tofauti kati ya kutokuwa na uaminifu wa ndoa (uasherati) na kuanza tendo la kujamiiana mapema (uasherati).

☐ **"wivi"** Neno la Kiingereza "kleptomania" limetoholewa toka mzizi wa Kiyunani.

☐ **"uongo"** Neno hili lote lilirejerea Amri Kumi. Kufuru lilikuwa tendo la kuzungunza kinyume na Mungu.

## MADA MAALUM : LUGHA YA WANADAMU

- I. Aina hii ya lugha (yaani., Uungu kuelezewa katika maneno ya kibinadamu) ni wa kawaida katika Agano la Kale (baadhi ya mifano)
  - A. Viungo vya mwili
    1. Macho - Mwa. 1:4,31; 6:8; Kut. 33:17; Hes. 14:14; Kumb. 11:12; Zak. 4:10
    2. Mikono – Kut. 15:17; Hes. 11:23; Kumb. 2:15
    3. Viganja – Kut. 6:6; 15:16; Kumb. 4:34; 5:15
    4. Masikio – Hes. 11:18; 1 Sam. 8:21; 2 Fal. 19:16; Zab. 5:1; 10:17; 18:6
    5. Uso – Kut. 33:11; Law. 20:3,5,6; Hes. 6:25; 12:8; Kumb. 31:17; 32:20; 34:10
    6. Vidole – Kut. 8:19; 31:18; Kumb. 9:10; Zab. 8:3
    7. Sauti – Mwa. 3:9,11,13; Kut. 15:26; 19:19; Kumb. 26:17; 27:10
    8. Miguu – Kut. 24:10; Ezek. 43:7
    9. Umbo la mtu – Kut. 24:9-11; Zaburi 47; Isa. 6:1; Ezek. 1:26
    10. Malaika wa Bwana – Mwa. 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16; Kut. 3:4,13-21; 14:19; Amu. 2:1; 6:22-23; 13:3-22
  - B. Matendo ya mwili (angalia mifano)
    1. Kuongea kama moja ya mfumo wa uumbaji- Mwa. 1:3,6,9,11,14,20,24,26
    2. Kutembea (yaani., sauti ya)- Mwa. 3:8; Law.26:12; Kumb. 23:14; Hab. 23:14
    3. Kufunga mlango wa safina ya Nuhu – Mwa. 7:16
    4. kunukia dhabihu – Mwa. 8:21; Law. 26:31; Amo. 5:21
    5. kurudi chini – Mwa. 11:5; 18:21; Kut. 3:8; 19:11,18,20
    6. maziko ya Musa – Kumb. 34:6
  - C. Mihemuko ya kibinadamu (baadhi ya mifano)
    1. Majuto/toba- Mwa. 6:6,7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:29,35; Amo. 7:3,6
    2. Hasira- Kut. 4:14; 15:7; Hes. 11:10; 12:9; 22:22; 25:3,4; 32:10,13,14; Kumb. 6:15; 7:4; 29:20
    3. Wivu - Kut. 20:5; 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15; 32:16,21; Yosh. 24:19
    4. Karaha/chuki- Law. 20:23; 26:30; Kumb. 32:19
  - D. Maneno ya kifamilia (baadhi ya mifano)
    1. Baba

- a. Wa Israel- Kut. 4:22; Kumb. 14:1; Isa. 1:2; 63:16; 64:8; Yer. 31:9; Hos. 11:1
  - b. Wa Wafalme- 2 Sam. 7:11-16; Zab. 2:7
  - c. Sitiari za vitendo vya kibaba Kumb. 1:31; 8:5; 32:6-14; Zab. 27:10; Mit. 3:12; Yer. 3:4,22; 31:20; Hosea 11:1-4; Mal. 3:17
2. Mzazi – Hosea 11:1-4
  3. Mama- Isa. 49:15; 66:9-13 (mshabihiano wa unyonyeshaji wa mama)
  4. Kijana mpendwa mwaminifu-Hosea 1-3

II. Sababu za kutumia aina hii ya lugha

- A. Ni muhimu kwa Mungu kujidhihirisha mwenyewe kwa mwanadamu. Hakuna misamiati mingine kuliko ile ya maneno ya kiulimwengu, ulioanguka. Dhana iliyosambaa ya Mungu kuwa wa jinsia ya kiume ni mfano mmoja wa lugha ya kumwelezea binadamu kwa sababu Mungu ni Roho!
  - B. Mungu anachukulia dhana ya maana halisi ya maisha ya mwanadamu na kuwatumia ili kujidhihirisha mwenyewe kwa mwanadamu aliyeanguka (Baba, Mama, Wazazi, Wapendwa)
  - C. Ingawa ni muhimu kwa wakati mwingine (yaani., Mwa. 3:8), Mungu hahitaji kuwekewa pingamizi kwa aina yeyote juu ya umbo la kibinadamu (kama vile Kut. 20; Kumbu. 5)
  - D. Hatima ya Mungu kuelezewa kama mtu ni kubadilika kwa Yesu katika umbo la kibinadamu! Mungu akawa mtu, mwenye kugusika (kama vile Yohana 1:1-18).
- III. kwa umakinika wa maelezo, angalia G. B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible*, ukurasa 10, "Tabia ya mwanadamu kwa Mungu," katika *The International Standard Bible Encyclopaedia*, kurasa za. 152-154.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 15:21-28**

<sup>21</sup>Yesu akaondoka huko, akaenda kando pande za Tiro na Sidoni. <sup>22</sup>Na tazama, mwanamke Mkananayo wa mipaka ile akatokea, akampazia sauti akisema, Unirehemu, Bwana, Mwana wa Daudi; binti yangu amepagawa sana na pepo. <sup>23</sup>Wala yeye hakumjibu neno. Nao wanafunzi wake wakamwendea, wakamwomba, wakisema, Mwache aende zake; kwa maana anapiga kelele nyuma yetu. <sup>24</sup>Akajibu, akasema, Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. <sup>25</sup>Naye akaja akamsujudia, akisema Bwana, unisaidie. <sup>26</sup>Akajibu, akasema, Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa. <sup>27</sup>Akasema, Ndiyo, Bwana, lakini hata mbwa hula makombo yaangukayo mezani pa bwana zao. <sup>28</sup>Ndipo Yesu akajibu, akamwambia, Mama, imani yako ni kubwa; na iwe kwako kama utakavyo. Akapona binti yake tangu saa ile.

**15:21 "Tiro na Sidoni"** Hii ilikuwa miji ya pwani ya Foinike katika Agano la Kale inahusiana zaidi na kumwabudu *Ba'al* na udhaifu, hata hivyo (1) Suleimani haliagiza wasanifu na vifaa vya kulijenga hekulu la Hiram, Mfalme wa Tiro (kama vile 1 Flp. 7); na (2) Eliya alimsaidia mjane katika eneo hili (kama vile Luka 4:25-26.)

**15:22 "mwanamke Mkananayo"** Haya ni matumizi pekee ya neno hili katika Agano Jipya, ingawa muundo unaofanan unapatikana katika jina hili (Mt. 10:4; Marko 3:18). Katika Marko 7:26 huyu alitwa mwanamke wa Msirofoinike ambaye kwa ulimwengu wa sasa angekuwa mwanamke toka Lebaboni ya kusini. Kwa uwazi huyu hakuwa Myahudi. Maelezo haya kama 8:5-13, yalionyesha Yesu kuyajali Mataifa. Uponyaji huu uliowekwa katika muhtasari katika Mt. 15:29-31 ulikuwa maarufu sana katika eneo la Mataifa (kama vile Marko 7:31).

☐ **"akampazia sauti"** Kwa namna iliyo dhahiri hili lilifanyika kwa sauti na kwa kurudiwa rudiwa. Hii kauli ya wakati timilifu inaweza kumaanisha (1) tendo lenye kurudiwa rudiwa katika wakati uliopita au (2) mwanzo wa tendo katika wakati uliopita.

☑ **"Unirehemu"** Rehema na huruma ya Yesu kwa maskini, wagonjwa, na wenye kupagawa ilikuwa ikiachiliwa hata akiwa mbali na kwa ukubwa zaidi. Hata mwanamke asiye wa Kiyahudi alihisi huwa angetenda kwa niaba (kama vile Mt. 9:27; 17:15).

Hii kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu inatumika katika maana ya ombi la kusihi, uamrishi

☑ **"Bwana"** Kwa vyo vyote haya yalikuwa (1) matumizi ya kawaida ya Neno "Bwana" au (2) matumizi ya kithiolojia ya "Mtawal" na "Masihi" ; ni muktadha pekee uwezao kutueleza. Kwa kuwa hapa jina hili limeunganishwa na jina la ki-Masihi, pendekezo la pili ni bora zaidi.

☑ **"Mwana wa Daudi"** Hili lilikuwa jina la ki-Masihi toka 2 Sam. 7. Huyu alifahamu jambo fulani kuihusu imani ya Kiyahudi na tumaini. Tazama Mada Maalum katika Mt. 9:27.

☑ **"binti yangu amepagawa sana na pepo"** Hali ya kupagawa na pepo ilikuwa na ni ukweli kwamba inaweza kuwapata watoto (kama vile Mt. 17:14-18). Hatuwezi kufahamu mwengi kuhusu eneo hili!

Nimepambana katika eneo hili la kupagawa na pepo. Naamini na kukiri mtazamo wa kibiblia wa kiulimwengu. Hata hivyo, inanisumbua kwamba (1) tendo la kuondoa pepo halikuorodheshwa kama moja ya karama za kiroho; (2) hili halikujadiliwa kamwe katika waraka wo wote wa Agano Jipya; (3) Sikuhabarishwa na mwandishi aliyevuviwa kuhusu namna ya kuufanya nutaratibu huu wa kiroho. Nimebaki kuikiri kweli, lakini si kuweza kuitambua au kujua namna ya kuieleza aua kuiondoa! Tazama mada maalumu zihusuzo pepo wachafu katika Mt. 10:1.

**15:23 "Nao wanafunzi wake wakamwendea, wakamwomba"** Hiki kitenzi pia ni cha wakati usio timilifu. Wanafunzi wanaonyesha kiwango chao cha huruma katika utofauti na Yesu (kama vile Mt. 9:36; 14:14; 15:32). Jibu la Yesu lililo katika Mt. 15:24 lilielezwa kwao, si kwa mwanamke yule. Katika Marko kifungu hiki kinaachwa kwa sababu huyu alikuwa akiyaandikia Mataifa ambao wasingeweza kuelewa kukataa kwa wanafunzi kuwasaidia Mataifa.

**15:24 "Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli"** Kumbuka Yesu aliyasaidia Mataifa mengine, lakini ndani ya mipaka ya kijiografia ya Nchi ya Ahadi. Ikiwa Yesu alikuwa ameanza huduma ya uponyaji katika nchi ya Mataifa, angekuwa amekwisha kukataliwa na halaiki ya Kiyahudi kwa ujumla kwa sababu ya ubaguzi wao. Hiki kifungu "kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli" kinaonyesha hali ya kiroho ya watu wa Kiyahudi (kama vile Mt. 10:6; 9:36).

Hili neno "mchungaji" kitaswira lilianza katika Hes. 27:17 (kama vile Zek. 10:2). Zaburi 23; 78:52; Isa. 40:11; Yer.31:10 likimtabiri YHWH kama Mchungaji wa Israeli. Taswira hii ilikuja kuwa ya Kimasihhi katika Mika 5:2; Zek. 11:4-17; na Yohana 10:1-10. Wachungaji wabaya wanatofautishwana wachungaji wema katika Ezekieli 34.

Kondoo wanahitaji uangalizi ulio himara na ulinzi. Hawakuwa na msaada, hawakuwa na ulinzi, na kwa wepesi walikabiliwa na wanyama! Kuwaita watu wa Mungu walio kondoo si hatima bali kweli ya kiroho!

Naweza kutengeneza wazo moja zaidi juu ya hili neno "pekee"! Yesu alilisaidia Taifa hili lenye uhitaji, kama alivyofanya mara zote kwa Mataifa. Hizi ni tabiri za shabaha yake kwa ulimwengu mzima (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Matendo 1:8). Masihi alikuja kwa ajili ya wanadamu wote walioumbwa kwa sura ya Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27). Mwanzo 3:15 si ahadi kwa Israeli, bali kwa wanadamu. Wito wa Ibrahim ulihusisha ulihusisha Mataifa (kama vile Mwa. 12:3). Kupewa Torati juu ya Mt. Sinai ilihusisha uangalizi wa Mungu kwa ulimwengu (kama vile Kut. 19:5)!

**15:26 "mbwa"** Haya ni matumizi pekee ya hili neno lililo katika Agano Jipya. Ukali wake unapunguzwa kwa ukweli kwamba ni mdogo kwa umbo lake, "vitoto" (Toleo la JB, "mbwa wafugwao"). Wayahudi waliwaita watu wa Mataifa kwa jina la "mbwa." Mazungumzo haya yalikusudia kuwasiadia wanafunzi kukushinda kutengwa kwao dhidi ya Mataifa. Yesu alitambua na kwa namna ya hadhara alikiri kwamba imani yake ilikuwa kubwa (kama vile Mt. 15:28)!

**15:27 "makombo"** Mara nyigi watu walikuwa wakitumia mikate kusafisha mikono yao baada ya kula.

**15:28 "Mama, imani yako ni kubwa"** Mara kadhaa Yesu aliwasifia watu wa Mataifa (kama vile Mt. 8:10). Hii ilikuwa ni kwa ajili ya: (1) kuonyesha pendo kwa watu wa Mataifa, au (2) kuusimua mtazamo wa wanafunzi kiulimwengu.

☐ **"Akapona binti yake tangu saa ile"** Tambua kwamba msichana huyu hakuhitaji tambiko au kuwepo kwa Yesu kimwili (kama vile Mt. 8:8-9). Alipomwambia kwamba binti yake ameponywa, aliamini.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 15:29-31**

<sup>29</sup>Yesu akaondoka huko, akafika kando ya bahari ya Galilaya; akapanda mlimani, akaketi huko. <sup>30</sup>Wakamwendea makutano mengi wakimletea viwete, vipofu, mabubu, vilema, na wengine wengi, wakawaweka miguuni pake; akawaponya; <sup>31</sup>hata ule mkutano wakastaajabu, walipowaona mabubu wanasema, vilema wanakuwa wazima, viwete wanakwenda, na vipofu wanaona; wakamtukuza Mungu wa Israeli.

**15:30 "makutano mengi"** Haya makutano mengi yaundwa na wadadisi, waliodhamiria, viongozi wa kidini, wagonjwa.

☐ **"akawaponya"** Hii ilikuwa ishara ya Kimasihi (kama vile Mt. 11:5) ambayo ilionyesha moyo wa Mungu.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 15:32-38**

<sup>32</sup>Yesu akawaita wanafunzi wake, akasema, Nawahurumia mkutano, kwa kuwa yapata siku tatu wamekaa pamoja nami, wala hawana kitu cha kula, tena kuwaaga wakifunga sipendi, wasije wakazimia njiani. <sup>33</sup>Wanafunzi wake wakamwambia, Tupate wapi mikate mingi hapa nyikani, hata kushibisha mkutano mkuu namna hii? <sup>34</sup>Yesu akawaambia, Mnayo mikate mingapi? Wakasema, Saba, na visamaki vichache. <sup>35</sup>Akawaagiza mkutano waketi chini; <sup>36</sup>akaitwaa ile mikate saba na vile visamaki, akashukuru akavimega, akawapa wanafunzi wake, nao wanafunzi wakawapa makutano. <sup>37</sup>Wakala wote wakashiba; wakayaokota masazo ya vipande vya mikate makanda saba, yamejaa. <sup>38</sup>Nao waliokula walikuwa wanaume elfu nne, bila wanawake na watoto.

**15:33 "Wanafunzi wake wakamwambia"** Ni kwa namna gani wanafunzi wamekwisha kusahau lile tendo la kulisha watu 5,000 kwa haraka (kama vile Mt.14:13-21)? Tofauti yake katika idadi, muktadha, na ina vikapu vilivyotumika inaonyesha kwamba kulikuwa na aina mbili tofauti za ulishaji wa makutano, si ile moja iliyonukuliwa mara mbili.

Ingawa semi za Yesu zinaonekana kuweka mipaka ya huduma yake kwa Wayahudi, tendo hili la ulishaji, kama lile la kuiponya nyumba ya Akida katika Mathayo 8, uponyaji wa toto wa mwanmke wa kimataifa ulio katika Mt. 15:21-28 na usemi wa kimuhutari wa Mt. 15:29-30, yote haya yawarejelea watu wa Mataifa.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 15:39**

<sup>39</sup>Akawaaga makutano, akapanda chomboni, akaenda pande za Magadani.

**15:39 "pande za Magadani"** Eneo hili halijulikani. Katika Marko muktadha wenye ufanano una neno "Dalmanatha" (Marko 8:10), lakini pia eneo hili linajulikana. Baadhi ya machapisho ya Kiyunani yaibadili Magadan kuwa Magdala neno ambalo ni la Kisemitiki la neno "mnara."

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Mafarisayo na waandishi walisafiri hadai Mataifa kumwona Yesu?
2. Ni kwa namna gani desturi inaweza kuwa kitu hatari?
3. Je, inawezekana kuwa mtu wa kidini na kutomjua Mungu?
4. Ni kwa namna gani tunaweka usawa wa uhuru wetu kama Wakristo kwa majukumu yetu?
5. Kwa nini orodha za Mathayo na Marko katika mstari wa 19 ni tofauti?
6. Kwa nini Yesu hakuwa tayari kumsaidia binti huyu? Kwa nini alikataa au, alikuwa alikuwa amekwsha kukataa?
7. Ni kwa namna gani watoto wanaweza kupagawa na pepo?

## MATHAYO 16

<b>MIGAWANYO YA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Madai kwa ajili ya Ishara 16:1-4	Mafarisayo na masadukayo wataka ishara 16:1-4	Madai ya ishara 16:1-4	Madai ya miujiza 16:1-4c	Mafarisayo wataka ishara toka mbinguni 16:1-4
Chachu ya Mafarisayo na Masadukayo 16:5-12	Chachu ya mafarisayo na masadukayo 16:5-12	Chachu ya mafarisayo 16:5-12	Chachu ya mafarisayo na masadukayo 16:5-6 16:7 16:8-11 16:12	Chachu ya mafarisayo na masadukayo 16:5-12
Tamko la Petro Juu ya Yesu 16:13-20	Petro anakiri Yesu ndiye Kristo 16:13-20	Ukiri wa Petro 16:13-20	Tamko la Petro juu ya Yesu 16:13 16:14 16:15 16:16 16:17-19 16:20	Umahili wa imani ya Petro, sifa zake 16:13-20
Yesu anazungumza Juu ya kifo chake 16:21-28	Yesu anatabiri kifo na ufufuo wake 16:21-23	16:21-23	Yesu anazungumzia mateso na kifo chake 16:21 16:22	Unabii wa kwanza wa mateso 16:21-23
	Ajitwike msalaba Na amfuata yeye 16:24-28	Katika uanafunzi 16:24-26 16:27-28	16:24-28	Hali ya kumfuata Kristo 16:24-26 16:27-28

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka [“Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia”](#))**

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasisi, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembele katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k



## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 16:1-4

<sup>1</sup> Wakamjia Mafarisayo na Masadukayo, wakamjaribu, wakamwomba awaonyeshe ishara itokayo mbinguni. <sup>2</sup> Akajibu, akawaambia, [Kukiwa jioni, mwasema, Kutakuwa na kianga; kwa maana mbingu ni nyekundu. <sup>3</sup> Na asubuhi, mwasema, Leo kutakuwa na dhoruba; kwa maana mbingu ni nyekundu, tena kumetanda. Enyi wanafiki, mwajua kuutambua uso wa mbingu; lakini, je! Ishara za zamani hizi hamwezi kuzitambua?] <sup>4</sup> Kizazi kibaya na cha zinaa chataka ishara; wala hakitapewa ishara, isipokuwa ishara ya Yona. Akawaacha, akaenda zake.

**16:1 "Mafarisayo na Masadukayo "** Mathayo alifahamu muunganiko wa haya makundi mawili kwa pamoja kama muungano wa uongozi wa waalimu wa sheria wa Kiyahudi (kama vile. Mat. 3:7; 10:1, 6, 11, 12; 22:34). Kwa mjadala kamili wa asili na theolojia ya Mafarisayo, tazama muhtasari katika Mt. 22:15 na kwa Masadukayo tazama mada maalumu katika Mt.22:23.

☉ **"wakamjaribu"** Neno hili (*peirasmos*) limetumika na kidokezo cha "wakimjaribu juu ya uharibifu" (kama vile. Mt. 6:13; Yakobo 1:13).

Tazama mada maalum katika Mt. 4:1.

☉ **"ishara itokayo mbinguni"** "itokayo mbinguni" ni maneno ya kuzungusha kwa ajili ya "Mungu." Waliona miujiza yake lakini walitaka zaidi (kama vile Mt. 12:38-42). Hii ni sawa na jaribu lile lile lililotolewa na shetani kwenye Mt. 4:5-6 juu ya kuushinda uaminifu wa mwanadamu kwa kutumia miujiza.

Ni dhahiri hawa Wayahudi wa kidini walitaka ushahidi kwamba Yesu anatumiwa na YHWH. Waliuita uponyaji kuwa "kazi ya shetani," hivyo walitaka ishara dhahili kwamba ametoka kwa Mungu (yaani, "mbinguni").

Ni kweli kwamba alivyokuwa si walichokijaribu kwa uwazi. Yesu aliwapa ishara, lakini kwa kificho na njia ya wakati ujao (yaani, ufufuo wake).

**16:2b-3** maelezo haya hayapo kwenye machapisho muhimu ya kale ya Kiyunani  $\alpha$ , B, X, na andiko la Kiyunani lililotumiwa na Origen, Machapisho ya Kiyunani yanafamika kwa Jerome, wala baadhi ya Peshitta au matoleo ya Koptiki, lakini yanapatikana kwenye machapisho ya C, D, L na W. Kifungu kili kile kinapatikana kwenye Luka 12:54-56. Andiko la kuhakiki nyuma ya toleo la nne la Agano Jipya la Kiyunani limeachwa na toleo la United Bible Societies halikutoa maamuzi juu ya asili ya mistari hii (kama vile. *A Textual Commentary on the Greek New Testament* na Bruce Metzger, uk. 41.)

**16:3 "Ishara za zamani"** Tambua WINGI "zamani." Hii inarejelea enzi mbili (tazama mada maalumu katika Mt. 12:31). Hawa wayahudi wa kidini waliweza kutabiri na kutambua baadhi ya majira ya ajabu, lakini hawakuweza/wasingeweza kutambua ujio wa enzi mpya wa Roho katika Yesu. Aliwakemea kwa ajili ya ukosefu wa kiroho (kama vile. Isa. 6:9-10). Ishara nyingine/unabii ulitimizwa kwao!

**16:4 "Kizazi kibaya na cha zinaa"** tungo hii imetumika kwa maana ya sitiari ya "wasio waaminifu." sitiari (kama vile Mt. 12:39; Yakobo 4:4) inasimulia matumizi ya ibada ya sanamu na ibada ya uzao iliyopita kwenye Agano la Kale (yaani, Yer. 3:8; 9:2; 23:10; 29:23; Ezekieli 23; Hosea 4:2-3; Mal. 3:5).

☉ **"ishara ya Yona"** hawakuwa na ushahidi wa kile alichokua anazungumzia! Huu ulikuwa ni mfanano wa Yona kuwa ndani ya tumbo la nyangumi kwa siku tatu na Yesu atakuwa katika *Hades (kuzimu)* (kama vile 1 Pet. 3:19). Kumbuka Yesu alikuwa kwenye kaburi kwa masaa thelethini na sita hadi arobaini pekee tu, lakini inahesabiwa kama siku tatu kwenye utaratibu wa Kiyahudi wa kuhesabu siku za Yesu. Sehemu ya siku ilihesabiwa kama siku nzima na ilianza na kumalizika wakati wa jioni (kama vile Mwa. 1). Tazama muhtasari katika Mt. 12:39 na Mt. 16:21.

#### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 16:5-12

<sup>5</sup> Nao wanafunzi wakaenda hata ng'ambo, wakasahau kuchukua mikate. <sup>6</sup> Yesu akawaambia, Angalieni, jilindeni na chachu ya Mafarisayo na Masadukayo. <sup>7</sup> Wakabishana wao kwa wao, wakisema, Ni kwa sababu hatukuchukua mikate. <sup>8</sup> Naye Yesu akafahamu, akawaambia, Mbona mnabishana ninyi kwa ninyi, enyi wa imani chache, kwa sababu hamna mikate? <sup>9</sup> Hamjafahamu bado, wala hamkumbuki ile mikate mitano kwa wale elfu tano, na vikapu vingapi mlivyoviokota? <sup>10</sup> Wala ile mikate saba kwa watu elfu nne, na makanda mangapi mliyoyaokota? <sup>11</sup> Imekuwa hamkufahamu ya kuwa si kwa sababu ya mkate naliwaambia? Ila jilindeni na chachu ya Mafarisayo na Masadukayo. <sup>12</sup> Ndipo walipofahamu ya kuwa hakuwaambia kujilinda na chachu ya mkate, bali na mafundisho ya Mafarisayo na Masadukayo.

**16:6, 11 "chachu"** inawezekana kwamba neno la Kiaramu "ukali ulioruhusiwa" hapa linamaanisha (kumbuka Yesu na Wayahudi katika siku zake walizungumza Kiaramu). Maneno mawili yanafanana katika Kiaramu; hata hivyo, mstari wa 12 unadai neno "hamira" au "chachu."

#### MADA MAALUM: CHACHU

Neno "chachu" (BDB 329, KB 329; Kiyunani, *zumē*) linatumika katika namna mbili katika zote Agano la Kale na Agano Jipya:

1. namna ya uharibifu na hivyo uwakilishi wa uovu
  1. Kut. 12:15,19; 13:3,7; 23:18; 34:25; Law. 2:11; 6:17; Kumb. 16:3
  2. Mt. 16:6,11-12; Marko 8:15; Luka 12:1; Gal. 5:9; 1 Kor. 5:6-8
2. namna ya upenyaji na hivyo taswira ya ushawishi, sio uwakilishi wa uovu
  1. Law. 7:13; 23:17; Amosi 4:5
  2. Mt. 13:33; Luka 13:20-21

Muktadha pekee unaweza kuamua kuamua maana ya neno hili (ambayo ni kweli juu ya maneno yote!).

Kuhusu somo la mikate isiyotiwa chachu, Waisraeli hawakuweza kusubiri asubuhi kwa ajili ya mikate kuchachuka. Maelezo haya ya usiku wa kutoka ulipelekea sherehe ya Kutoka ya Pasaka iunganishwe na sherehe za kilimu (kama vile Kut. 12:15-20; 23:14-17; 34:18).

Chachu mara kwa mara ilitumika kama vitu vya kutolea dhabihu (kama vile Law. 7:13; 23:17), lakini baadaye ilikuwa uwakilishi wa dhambi na uasi. Kuchachua kulionekana katika namna hii ya uwakilishi kama nafasi ya Israeli katika msingi wa mtu mmoja mmoja kuchunguza maisha yao kwa kiashiria chochote cha uasi au kukosa utii kwa YHWH. Kama ilivyo Siku ya Upatanishi (Mambo ya Walawi 16) lilifanya kazi katika ngazi ya taifa, Sikukuu ya Mikate isiyotiwa chachu ilifanya kazi katika ngazi ya mtu mmoja mmoja au familia.

Hii sikukuu ya mwisho wa mwaka ikiunganishwa na sherehe ya Pasaka ilitunza ukombozi wa neema ya YHWH siku zote mbele za akili na mioyo ya Watu wake. Kadiri neema na ahadi ilivyotoa ukombozi kutoka Misri, ndivyo Israeli ilivyotegemea katika tabia za Kiungu zisizobadilika kuokoa kadiri miaka ilivyoenda (kama vile Kut. 13:8,14; Kumb. 4:9; 6:2,7,20-21).

**16:8** Yesu mara kwa mara alirejelea wale kumi na mbili maana walikua na imani haba (kama vile Mt. 6:30; 8:26; 14:31; 16:8). Wale wote waliomsikia na kuishi pamoja nae mara zote hawakumtambua au hawakua na imani. Mstari wa 7-10 walikua kwenye mabano. Yesu alitaka kuongea juu ya imani ya uongo ya Mafarisayo (kama vile Mt. 5:20-48), lakini wanafunzi kwa ufahamu wao mdogo walifikilia juu ya ukosefu wa "mikate."

**16:9** wanafunzi walikua na nafuu ya kumsikiliza Yesu akiongea na kuwahudumia makutano na pia mjadala wa faragha na tafsiri baadae, lakini bado, walikua kama wasikilizaji (kama vile Mt.13:13,14-15 [Isa. 6:9-10,19]), hawakutambua (yaani, Mt. 15:17; 16:11; Luka 2:50; 18:34; Yn. 10:6; 12:16). Ujumbe wa Yesu ulikua wa kipeena wa tofauti sana kulinganisha wa viongozi wa Kiyahudi (yaani, "chachu ya Mafarisayo") walikulia katika hali hiyo ilihitajika kuongozwa na nguvu za Roho ili kufungua ufahamu wao wa utambuzi (yaani., Luka 24:45). Hili lilitokea taratibu wakati Yesu akiwa nao (yaani, Mt. 16:13-28), lakini sio kwa ukamili hadi pale

1. baada ya ufufuo

2. kwenye chumba juu orofani (kama vile Yn 20)
3. kandokando ya bahari kwenye Yohana 21
4. Mdo. 1 alipopaa mbinguni

**16:12** ilikua ni ushikiliaji wao sheria na upungufu wa upendo uliosababisha Yesu awashutumu kwa maneno! Mara nyingi wenye wanaweza kuwa kizuizi badala ya daraja!

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 16:13-20**

<sup>13</sup> Basi Yesu akaenda pande za Kaisaria-Filipi, akawauliza wanafunzi wake akasema, Watu hunena Mwana wa Adamu kuwa ni nani? <sup>14</sup> Wakasema, Wengine hunena u Yohana Mbatizaji, wengine Eliya, wengine Yeremia au mmojawapo wa manabii. <sup>15</sup> Akawaambia, Nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani? <sup>16</sup> Simoni Petro akajibu akasema, Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai. <sup>17</sup> Yesu akajibu, akamwambia, Heri wewe Simoni Bar-yona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni. <sup>18</sup> Nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda. <sup>19</sup> Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lo lote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni. <sup>20</sup> Ndipo alipowakataza sana wanafunzi wake wasimwambie mtu ye yote ya kwamba yeye ndiye Kristo.

**16:13 "Kaisaria-Filipi"** Huu ulikua ni mji yapata maili 20 kusini mwa bahari ya Galilaya kwenye himaya ya Filipi. Hii ilikua ni mara ya pili kwa Yesu kujaribu kujitenga mbali akiwa na wanafunzi wake pekee Mt. 15).

☐ **"mwana wa Adamu"** Tungo hii imetumika mara kadhaa kwenye Agano la kale. Inadokeza mwanadamu (Zab. 8:4; Ezek. 2:1) na Uungu (Dan. 7:13). Tungo haikutumiwa na walimu wa sheria siku za Yesu; hata hivyo, haihusishi uzalendo au mtu anaamini katika nguvu za kijeshi. Hili ni jina alililolichagua Yesu mwenyewe kwa sababu linaunganisha vipengele pacha vyake binafsi, Mungu kamili na Mtu kamili (kama vile Fl. 2:6-8; 1 Yn. 4:1-3). Tazama muhtasari katika Mt. 8:20.

**16:14 "Yohana mbatizaji"** Herode Antipa alifikilia kwamba Yesu ni Yohana mbatizaji (kama vile Mt.14:1-2).

☐ **"Eliya"** hii ni kutoka katika unabii wa Mal. 3:1; 4:5 ambao unasema kwamba Eliya ataandaa mapito kwa ajili ya Masihi. Ni uthibitisho wa mwanzo wa enzi mpya ya Roho.

☐ **"Yeremia"** walimu wa sheria wanashikilia kwamba alificha sanduku la Agano katika mlima Nebo na ataritoa nje muda mfupi kabla ya kuanza enzi mpya.

☐ **"mmojawapo wa manabii"** hii inamfanya Yesu kuwa nabii kama mfano wa wengine kwenye Agano la kale. Inaweza kusimulia unabii wa Kumb. 18:15-22 (kama vile Yn. 2:2). Makisio haya yote yanahusisha uamusho!

☐ **"Nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani"** "nanyi" ni wingi. Yesu aliwauliza wanafunzi wote hili swali. Petro alijibu kwanza. Nafsi yake ilimfanya kuwa msemaji wa kundi.

**16:16 "Wewe ndiwe Kristo"** hili lilielezwa kabla na Andrea kwenye Yn. 1:41, Nathanieli kwenye Yn.1:49, na Petro kwenye Yn. 6:69. Jina la Kiyunani "Kristo" linafanana na Kiebrania "Masihi" au "mpakwa mafuta." Tazama mada maalumu: Majina ya Agano la kale yeye ajae katika Mt. 8:20.

☐ **"Mwana wa Mungu aliye hai"** Petro hakujua kikamilifu umasihi wa Yesu kama ilivyo wazi kwenye mistari ya 21-23. Hivyo basi, Baraka za mstari wa 17 zinasimulia kwa tungo "mwana wa Mungu aliye hai." Tungo "Mungu aliye hai" ilikuwa inatafsiri YHWH ambayo inatoka kwenye kitenzi cha Kiebrania "kitenzi kisaidizi" (kama vile Kut. 3:14). tazama [MADA MAALUMU: MAJINA YA UUNGU](#) katika Mt. 1:21.

16:17

NASB "Simon, Bar-yona"  
NKJV "Simon Bar-Yona"  
NRSV, NJB "Simon mwana wa Yona"  
TEV "Simon mwana wa Yohana"

Neno hili la Kiaramu "*Barjonas*" linamaanisha "mwana wa Yohana."

☐ "**bali Baba yangu aliye mbinguni**" furaha ya ukiri wa Petro (Mt. 16:16) sio kwa ugunduzi wa kibinadamu, lakini ni ufunuo wa kiroho. Roho ni nafsi ya utatu ambaye alilitambua jambo hili, lakini hapa ni Baba, inwezekana kwa sababu ametaja "mwana wa Mungu."

Injili haiwezi kujumuishwa wala kuitikia bila msaada wa kiroho (kama vile Yn 6:44, 65; 10:29). Hii haitoi mamlaka ya mwitikio kwa mwanadamu (kama vile Yn 1:12; 3:16; Rum. 10:9-13), lakini inaonyesha kwamba wanadamu anaitikia mwanzoni tu kutoka katika utawala wa kiroho. Hawawezi/kutenda maamuzi ya awali ya kiroho! Kitenzi njeo kinasimulia "unganisha" na "legeza" ya Mt. 16:19 kinaaksi ukweli mmoja!

**16:18 "Petro"** hili ni neno la Kiyunani "*petros*," nomino ya kiume. Linarejelea mwamba uliotenganishwa. Kwa ajili ya uzima wake zaidi (yaani, Mt. 16:22,23; Marko 14) yeye ni kila kitu lakini "mwamba"!

☐ "**mwamba huu**" hili ni neno la Kiyunani, "*petra*," nomino ya kike. Linarejelea msingi wa mwamba (kama vile Mt. 7:24). Maneno haya mawili (*petros* na *petra*) hayawezi kuunganika kwa kila moja kisarufi kwa sababu ya jinsia zao. Wanafunzi hawakuliona hili kama rejea kwa mamlaka ya Petro kwa sababu waliendelea kubishana juu ya nani alikua mkubwa (kama vile Mt. 18:1, 18; Yn. 20:21). Maneno haya mawili yanasimuliwa lakini kwa utofauti kwenye Kiyunani. Kuna mchezo wa wazi kati ya imani ya Petro na imani ya mitume wote. Hata hivyo, kwenye Kiaramu kuna neno moja pekee, "*kepha*" ("Kefa, Yn. 1:42; 1 Kor. 1:12; 3:22; 9:5; 15:5) kwa ajili ya maneno yote ya Kiyunani kwa ajili ya "mwamba." Yesu aliongea Kiaramu lakini maneno yake yaliandikwa na waandishi waliovuviwa kwa Kiyunani. Hivyo basi, ni lazima tuhusike na andiko la Kiyunani, sio kwa dhani ya maelezo ya Kiaramu.

☐ "**kanisa**" "*Ekklesia*" lilikua ni neno lililotumika kwenye tafsiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania kwa ajili ya "kusanyiko la Israeli" (*Qahal*, BDB 874, kama vile Kumb. 18:16; 23:2). Mmoja anatakiwa kuwa makini asisome kama ufafanuzi wa mhimili wa Upentekosti na katika miundo iliyo wazi kabisa na kifungu cha Kiyahudi. Wanafunzi hawa wa awali walijiona wao kuwa ni uenezi wa watu wa Agano la kale (yaani, *Qahal*) la Mungu. Walikua ni utimilifu wa watu wa Agano la kale. Neno lenyewe linadokeza waliitwa na kukusanywa kwa ajili ya kusudi. Ulikua ni utambuzi wa awali wa Kiyunani ulioitwa kusanyiko la mji (kama vile Mdo. 19:32,39, 41). Neno hili halionekani kwenye Marko, Luka, au Yohana. Limejitokeza mara tatu pekee kwenye Mathayo (kama vile Mt. 16:8; 18:17 [mara mbili]). Katika Mt. 18:17 ni wazi andiko linarejelea kipindi wakati wa baadae. Neno limejitokeza mara kwa mara kwenye Mdo. na maandiko ya Paulo.

### **MADA MAALUM: KANISA (*eklesia*)**

Neno hili la Kiyunana, *eklesia*, linatokana na maneno mawili, "nje ya" na "kuitwa." Neno hili linatumika kidunia (yaani., jamii iliyoitwa kwenye kikao, k.v Mdo. 19:32,39,41) na kwa sababu ya utumiaji wa maandiko ya kale ya Kiyunani ya neno hili kwa ajili ya "kusanyiko" la Israeli (*Qahal*, BDB 874, KB 1078, k.v. Hes. 16:3; 20:4; Kumb. 31:30), na matumizi ya kidini. Kanisa la mwanzo walijiona wao kama mwendelezo wa Agano la Kale la watu wa Mungu. Walikuwa Waisraeli wapya (k.v. Rum. 2:28-29; Gal. 3:29; 6:16; 1 Pet. 2:5,9; Uf. 1:6), utimilizo wa kusudi la Mungu kidunia (k.v. Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Mt. 28:18-20; Luka 24:47; Mdo 1:8; angalia Mada Maalum: Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH

Neno lililotumika kwa maana nyingi katika injili na matendo.

1. Mikusanyiko ya kidunia, Mdo. 19:32,39,41
2. Watu wa Mungu ulimwenguni katika Kristo, Mt. 16:18 na Waefeso

3. Kusanyiko la waumini wa mahali katika Kristo, Mt. 18:17; Mdo. 5:11 (katika aya hii, ni kanisa huko Yerusalem); Mdo. 13:1; Rum. 16:5; 1 Kor. 16:19; Kol. 4:15; Filemoni uk. 2
4. Watu wa Israel kwa ujumla, Mdo. 7:38, katika hotuba ya Stephano
5. Watu wa Mungu kwenye Miji, Mdo. 8:3; Gal. 1:2 (Yuda au Palestina)

Kanisa ni watu waliokusanyika, na sio jengo. Hapakuwepo na majengo ya kanisa kwa muda wa miaka mingi. Katika Yakobo (moja ya kitabu cha mwanzoni kabisa cha Wakristo) kanisa lilitajwa kwa neno "*synagōgē*" (kusanyiko). Neno kanisa limetokea tu kwa Yakobo (k.v. Yakobo 2:2; 5:14)

☐ **"milango ya kuzimu"** "milango" inaweza kurejelea (1) dhana ya mji wa wafu ambapo hakuna awezea kuwa huru, (2) baraza la mji lililokutana katika mlango, au (3) dhana ya matendo maovu dhidi ya kanisa. *Hades* (*kuzimu*) linatokana na neno "kuona" kanusha, hivyo basi haionekani. Ni sawa na neno la kutoka Agano la kale "*Sheol*," ambapo wenye haki na waovu hufa mara moja. Tazama mada maalum: wafu wako wapi? Katika Mt. 5:22.

☐ **"haitalishinda"** neno hili lina kidokezo tendaji cha "kushinda, kutawala." Kifo na uovu hakitashinda wala kujumuishwa (maana mbili ya neno hii) kanisa la Mungu aliye hai.

**16:19 "funguo za ufalme wa mbinguni"** hii ilikua ni sitiari kwa ajili kupata umiliki wa mlango. Tazama Isa. 22:22; Ufu. 1:18; 3:7. Funguo ni tangazo la injili na mwitikio wa mwaliko. Dhana hii ya kuzimu na mbinguni ina milango kama mji iliyokuwako siku za Isaya (tazama mada maalum inayofuata). Mwandishi wa Waebrania pia ametumia sitiari hii kwa ajili ya mbinguni (kama vile Ebr. 11:10,16; 12:22; 13:4), kama alivyofanya Yohana kwenye Ufunuo (kama vile Ufu. 3:12; 21-22).

## MADA MAALUM: "MIJI" MIWILI KATIKA ISAYA

- A. Isaya 24-27 ni kipengele cha kifasihi kilicho katika hitimisho la mfululizo wa hukumu ya Mungu dhidi ya mataifa yaliyozunguka yapatikanayo katika Isaya 13-23. Hukumu siyo neno la mwisho! Mungu wa neema na rehema ana mpango wa milele, jumishi na ukombozi (angalia [Mada Maalum: Mpango wa Milele wa Ukombozi wa YHWH](#))!
- B. Sehemu nzima ni tamthilia ya miji miwili.
  1. Miji iliyotengenezwa na wanadamu watoto wa Kaini aliyeanguka, aliyejaribu kutimiza mahitaji yao kiukamilifu kwa rasilimali zake mwenyewe (yaani Mwanzo 4:10-11).
  2. Mji wa Sayuni, ambapo (yaani juu ya mabawa mawili ya makerubi katika sanduku la agano katika patakatifu pa patakatifu pa hekalu katika Yerusalemu) na ambapo wafuasi wake waaminifu (Wayahudi na Mataifa) huja kwake na kumuabudu Yeye (kama vile Isa. 2:2-4; 19:18-25; Ebr. 11:10; 12:22; 13:14; Ufu. 21:1-2).
- C. Miji inawakilisha makundi ya watu/mataifa.

### Miji ya kibinadamu

Isa. 1:7,8, miji ya Wayudea iliyochomwa  
 Isa. 1:21, mji wa uaminifu umekuwa mji wa kahaba  
 Isa. 6:11, miji ya Wayudea ikiharibiwa  
 Isa. 14:17,21, miji yote ikiharibiwa  
 Isa. 14:31 miji ya Filistia  
 Isa. 17:1-3,9, Miji ya Shamu ikiharibiwa  
 Isa. 19:2, cities of Egypt destroy each other miji ya Misri iharibiana yenyewe kwa yenyewe  
 Isa. 22:2,9, mji wa furaha, Yerusalemu inaanguka

### Mji wa Mungu

Isa. 1:26, mji wa haki, mji wa waaminifu  
 Isa. 19:18-22, miji ya Misri ikimwabudu Mungu  
 Isa. 19:23-25, Misri yote na Ashuru ikijumuishwa katika watu wa Mungu

Isa. 23, Tiro ikiharibiwa	
Isa. 24:1-25:5, uharibifu wa kiujumla wa miji	
Isa. 25:10-12, Moabu na sehemu yake, ikiwekewa ngome	Isa. 25:6-9, karamu katika mlima wa Mungu (yaani, miji ikikanyaga Yerusalemu)
Isa. 26:5, mji usioshindwa, yawezekana Moabu	Isa. 26:1, mji imara, Yerusalemu, unarejeshwa
Isa. 27:10, mji wenye ngome unaanguka	
Isa. 29:1, "Ariel" (Yerusalemu)	
Isa. 33:2,19, mji wa furaha (Yerusalemu)	
	Isa. 45:13, Mji wangu (kama vile Isa. 44:23)
Isa. 48:2, mji mtakatifu, japo kwa jina langu	
	Isa. 52:1-6, mji mtakatifu
	Isa. 60:14, mji wa Bwana
	Isa. 62:12, mji usiosahauliwa
	Isa. 66:6, sauti ya shangwe, sauti ya hekalu

☐ **"ufalme wa mbinguni"** Marko na Luka wana, "ufalme wa Mungu." Tofauti sio moja ya sababu, lakini tofauti ya wapokeaji. Tazama mada maalum ya ufalme wa Mungu katika Mt. 4:17.

**NASB, NKJV,**  
**NRSV, NJB** "utakalolifunga. . . utakalolifungua"  
**TEV** "utakalokataza. . . utakaloruhusu"

Haya ni maneno ya walimu wa sheria yaliyotumika kwa ajili ya maamuzi sahihi yaliyoruhusiwa au kitu kisichoruhusiwa. Kitenzi cha Njeo hii ya kuongea kwa mafumbo mawili ni muhimu. Vyote vinaonyesha ishara ya wakati ujao ya "mimi" na kauli timilifu tendwa endelevu/ya hali ya kuendelea. Kinaweza kutafsiriwa "litakuwa limefungwa" na "litakuwa limefunguliwa" (kama vile Mt. 18:18). Hii inaaksi ukweli kwamba kile ambacho mwanadamu, akiongozwa na Roho Mtakatifu, akiamua Duniani juu ya mambo ya kiroho tayari yatakuwa yameamriwa mbinguni. Kifungu hiki hakielezei maamuzi ya mwanadamu, lakini wanadamu wanafuata mwongozo wa Mungu (kama vile Mt. 18:18; Yn. 20:23).

**16:20 "alipowakataza sana wanafunzi wake wasimwambie mtu ye yote ya kwamba yeye ndiye Kristo"** injili ilikuwa bado haijakamilika. Dhana ya Wayahudi wa sasa ni juu ya kazi ya Masihi haikuwa sahihi. Wanafunzi ni lazima wasubiri (kama vile Mt. 8:4; 9:30; 12:16; 17:9).

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 16:21-23**  
<sup>21</sup> Tangu wakati huo Yesu alianza kuwaonya wanafunzi wake ya kwamba imempasa kwenda Yerusalemu, na kupata mateso mengi kwa wazee na wakuu wa makuhani, na waandishi, na kuuawa, na siku ya tatu kufufuka. <sup>22</sup> Petro akamchukua, akaanza kumkemea, akisema, Hasha, Bwana, hayo hayatakupata. <sup>23</sup> Akageuka, akamwambia Petro, Nenda nyuma yangu, Shetani; u kikwazo kwangu; maana huyawazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu.

**16:21 "imempasa"** hili lilikuwa neno "dei" ambalo linamaanisha maadili yanayotakiwa (Yesu alikuja ili afe, Marko 8:31; 10:45; Yn. 3:14,16). Yesu akitambua kulikua na mpango wa kiroho kwa ajili ya huduma na uzima wake (kama vile Mt. 12:15-21; Luka 22:22; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 10:42; 17:31). Alitambua akiwa na umri wa miaka kumi na miwili (kama vile Luka 2:41-49)!

☐ **"na kupata mateso mengi"** Yohana anadokeza hili kwa kumuita Yesu "mwanakondoo wa Mungu" (kama vile. Yn 1:29), lakini wanafunzi hawakujianda kwa ajili ya ukweli huu. Haikua kwenye karne yao ya kwanza dhana ya

Kiyahudi juu ya Masihi. Walimu wa sheria wanasisitiza ujio wa Masihi kama tendo la hukumu na ushindi wa kijeshi (kama vile Ufu. 19:11-16). Hawakua na makosa kwenye hukumu hii lakini walishindwa kuutambua ujio wake wa kwanza kama mtumishi atesekaye (kama vile Isa. 53), mnyenyekevu aliyepanda mwana punda (kama vile Zek.9:5), yote ambayo yameonekana yakifuata Mwa. 3:15. Tazama mada maalumu: MPANGO WA UKOMBOZI WA MILELE WA YHWH katika Mt. 27:66.

Ufunuo huu wa mateso yake unashangaza kwamba Yesu aliurudia mara kadhaa (kama vile Mt. 17:9, 12, 22-23; 20:18-19). Alifanya hivyo pindi itakapotekea kwa wanafunzi, baada ya huzuni ya mwanzo na mkanganyiko, ataelewa kwamba Yesu alikua ni mmiliki wa hatima yake. Hii itawatia moyo wao kwa ajili ya wito wa umisheni (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8).

☐ **“wazee na wakuu wa makuhani, na waandishi** "Hii ni tungo iliyotumika kuelezea baraza kuu la Wayahudi. Kilikua ni chombo cha utawala wa Wayahudi kilichoundwa na viongozi wapato 70 kutoka maeneo ya Yerusalemu. Katika siku za Yesu kilipotoshwa na siasa za Rumi kwa sababu nafasi ya ukuhani ilinunuliwa.

## MADA MAALUMU: WAKUU WA BARAZA LA SINAGOGI

- I. chanzo cha habari
  - A. Agano Jipya lenyewe
  - B. Flavian Yusufu wa mambo ya kale ya Kiyahudi
  - C. Sehemu ya Mishna juu ya sheria za kiibada za Kiyahudi (yaani eneo la watu wa Sinagogi kuu).

Bahati mbaya Agano Jipya na Yusufu hawakubaliani na maandiko ya sheria za Kiyahudi, ambazo zinaonekana kuwathibitisha watu wawili wa Sinagogi kuu katika Yerusalemu, kuhani mmoja (yaani., Msadukayo), akidhibitiwa na kuhani mkuu na akishughulika na haki za jamii na uhalifu na wa pili ikidhibitiwa na mafarisayo na waandishi, waliohusiana na mambo ya kidini na kitamaduni. Hata hivyo, tarehe za maandiko ya sheria za Kiyahudi toka mwaka 200 B.K na kuangazia hali ya kitamaduni baada ya Yerusalemu kuangukia mikononi mwa kamanda Tito wa Rumi, mwaka wa 70 B.K. wayahudi (yaani., uongozi wa kifarisayo) waliimarisha tena makao makuu yao kwa minajili ya maisha ya kidini katika mji uitwao Jamnia na baadaye (yaani mwaka wa 118 B.K) wakaondoka kwenda Galilaya.

### II. Istilahi

Tatizo la kumtambua mtu wa kimahakama unahusisha majina tofauti yanayojulikana. Kuna maneno mengi yaliyotumika kuelezea watu wa kimahakama ndani ya jamii ya Kiyahudi ya Yerusalemu.

- A. *Gerousia*-“ senati” au “baraza.” Hili ni neno la zamani lililotumika kwenye kipindi cha mwisho cha Uajemi (kama vile vitu vya asili ya kale vya Yusufu 12.3.3 na II Wamakabayo 11:27). Linatumiwa na Luka katika Mdo 5:21 pamoja na “watu wa Sinagogi kuu.” Yaweza kuwa ni njia ya kuelezea neno kwa viongozi wanaoongea Kiyunani (kama vile Wamakabayo 12:35)
- B. *Synedrion*- “watu wa Sinagogi kuu.” Huu ni muunganikano toka *syn* (pamoja na) na *hedra* (nafasi). Cha kushangaza neno hili linatumiwa katika lugha ya Kiarama, lakini likitazamisha neno la Kiyunani mwishoni mwa kipindi cha Wamakabayo hili likajakuwa ni neno linalokubalika kuunda mahakama kuu ya Kiyahudi katika Yerusalemu (kama vile Mt. 26:59; Marko 15:1; Luka. 22:66; Yohana 11:47; Mdo. 5:27). Tatizo hapa linakuja wakati maneno yale yale yanatumika katika mabaraza ya kimahakama ya mahali fulani nje ya Yerusalemu (kama vile Mt. 5:22; 10:17)
- C. *Presbyterion*- “baraza la wazee” (kama vile Luka 22:66). Huu ni mfumo wa Agano la Kale la viongozi wa kikabila. Hata hivyo, ilikuja kurejerea mahakama kuu katika Yerusalemu (kama vile Mdo. 22:5)
- D. *Boulē* –neno hili “baraza”lilitumiwa na Yusufu (yaani vita 2.16.2; 5.4.2, lakini sio agano jipya) kuelezea watu mbali mbali wa kimahakama:
  1. Seneti kwenye mji wa Rumi
  2. Mahakama za kawaida za Rumi
  3. Mahakama kuu ya Kiyahudi katika Yerusalemu
  4. Mahakama za kawaida za Kiyahudi

Yusufu wa Arimataya ameelezewa kama mwanajumuiya ya watu wa Sinagogi kuu kwa muundo wa neno hili

(yaani., *bouleutē*, likimaanisha “mkuu wa baraza” kama vile Marko 15:43; Luka 23:50)

### III. Maendeleo ya kihistoria

Mwanzoni kabisa Ezra alisema kulitengeneza Sinagogi kuu (kama vile Targum katika Wimbo ulio Bora 6:1) katika kipindi cha uhamisho, ambacho kilikuja onekana kuwa watu wa sinagogi kuu katika siku za Yesu.

- A. Mishna (yaani., sheria za kiibada za Kiyahudi) zimeweka kumbu kumbu kwamba palikuwepo mahakama mbili kuu katika Yerusalemu (kama vile Sanh. 7:1)
  1. Moja iliyokuwa imeundwa na wanajumuiya 70 (au 71) (sand. 1:6 hata inaelezewa kuwa Musa alitengeneza hilo baraza la kwanza la watu wa Sinagogi kuu (Sanhedrin) la watu 11, kama vile Hes.11:16-25)
  2. Lingine lililokuwa limeundwa na wanajumuiya 23 (lakini yawezekana inarejerea mabaraza ya Sinagogi ya kawaida).
  3. Baadhi ya wasomi wa Kiyahudi waliamini kuwa palikuwepo na wanajumuiya 23 waliounda sinagogi kuu huko Yerusalemu. Wakati watatu wanaungana, pamoja na viongozi wawili, likiteua wanajumuiya 71 toka “watu wa sinagogi kuu.” (yaani Nasi na Av Bet Din).
    - a. Kuhani mmoja (yaani Sadukayo)
    - b. Mwanasheria mmoja (Farisayo)
    - c. Mtu wa ukoo bora mmoja (yaani., wazee)
- B. Wakati wa ukimbizi toka mahali pao, kizazi cha Daudi kilichorudi ni Zurubabeli na kizazi cha Aroni alikuwa Yoshua. Baada ya kifo cha Zerubabeli, hapakuwepo na kizazi cha Daudi kilichoendelea, kwa hiyo joho la kimahakama lilipitishwa pasipo kuwajumuisha makuhani (kama vile I Macc. 12:6) na wazee wa mahali (cf. Neh. 2:16; 5:7).
- C. Jukumu la kuhani katika mahakama lilithibitishwa na Diodorus 40:3:4-5 wakati wa
- D. Jukumu hili la kuhani katika serikali liliendelea mpaka kipindi cha Selucid. Yusufu anamnukuu Antiokia “mkuu III” (223-187 K.K) katika mambo ya kale 12.138-142.
- E. Mamlaka ya kuhani yaliendelea mpaka kipindi cha Wamakabayo kutokana na mambo ya kale ya Yusufu 13.10.5-6; 13.15.5
- F. Wakati wa kipindi cha utawala wa Warumi gavana wa Syria (yaani Gabinus toka 57-55 K.K) akaanzisha “sinagogi kuu” za Kimikoa (kama vile mambo ya kale ya Yusufu 14.5.4; na Vita 1.8.5), lakini baadaye ilitenguliwa na Rumi (yaani., mwaka wa 47 K.K)
- G. Watu wa Sinagogi kuu walikuwa na mkabiliano wa kisiasa na Herode (yaani mambo ya kale 14.9.3-5) ambao, mwaka 37 K.K, wakalipiza kisasi na watu wengine wa baraza kuu wakauwawa (kama vile mambo ya kale ya Yusufu 14.9.4; 15.1.2)
- H. Chini ya wakili wa Kirumi (yaani., 6-66 B.K) Yusufu anatuambia (kama vile mambo ya kale 20.200,251) kuwa watu wa Sinagogi kuu tena wakapata nguvu na umaarufu (kama vile Marko 14:55). Kuna majaribu matatu yalioandikwa katika Agano Jipya pale watu wa siagogi kuu, chini ya uongozi wa familia ya kuhani mkuu, walitenda haki.
  1. Jaribu la Yesu (kama vile Marko 14:53-15:1; Yohana 18:12-23,28-32)
  2. Petro na Yohana (kama vile Mdo 4:3-6)
  3. Paulo (kama vile Mdo. 22:25-30)
- I. Wakati Wayahudi walipoasi katika mwaka wa 66 K.K, Warumi baadaye wakaiharibu jamii yote ya Kiyahudi na Yerusalemu katika mwaka wa 70 K.K. watu wa sinagogi kuu moja kwa moja wakatenguliwa, ingawa Mfarisayo pale Jamnia wakajaribu kurudisha tena baraza kuu la kisheria (yaani Beth Din) katika maisha ya dini ya Kiyahudi (lakini sio kwenye jamii au siasa)

### IV. Uanachama

- A. La kwanza Kibiblia kutajwa kwenye baraza kuu huku Yerusalemu ni lile la 2Nya. 19:8-11. Liliundwa na
  1. Walawi
  2. Makuhani
  3. Wakuu wa familia (yaani., wazee, kama vile I Wamak. 14:20; II Wamak.4:44)
- B. Wakati wa kipindi cha Wamakabayo lilimilikiwa na (1) familia ya kikuhani ya Masadukayo na (2) familia



ya ukoo bora wa mahali fulani (kama vile I Wamak. 7:33; 11:23; 14:28). Baadaye katika kipindi hiki “waandishi” (wanasheria wa Musa, ambao mara nyingi walikuwa mafarisayo) waliongezwa, inaonekana na mke wa Alexandra Jannaesus, yaani Salome (76-67 B.K). Hata hivyo alisema kuwafanya mafarisayo kuwa kikundi cha maarufu (kama vile Yusufu, vita vya Wayahudi 1.5.2).

C. Wakati wa siku za Yesu baraza liliundwa na

1. Familia ya kuhani mkuu
2. Watu wa kawaida toka kwenye familia ya watu wenye uwezo
3. Waandishi (kama vile Luka 19:47)

V. Vyanzo vya maoni vikatafuta toka

- A. Dictionary of Jesus and the Gospels, IVP, kurasa 728-732
- B. The Zondervan Pictorial Encyclopedia of the Bible, vol. 5, kurasa 268-273
- C. The New Schaff-Herzog Encyclopedia of Religious Knowledge, vol. 10, kurasa 203-204
- D. The Interpreter's Dictionary of the Bible, vol. 4, kurasa 214-218
- E. Encyclopedia Judaica, vol. 14, kurasa 836-839

☐ **"na siku ya tatu"** Yesu kwa kawaida alitaja kipengele hiki mara kadhaa, Mt. 12:40; 16:4, ambapo ilisimuliwa na nabii Yona na kama ishara ya Umasihi wake. Paulo anadokeza kwenye 1 Kor. 15:4 kwamba ni utabiri wa kwenye Agano la kale. Ahadi mbili pekee za kwenye Hos. 6:2 na Yona 1:16. Katika muktadha wa matumizi ya Yesu ni lazima imesimuliwa kwa Yona.

Hata hivyo, hayakua masaa 72 kamili lakini ni juu ya masaa 36-40. Wayahudi walihesabu siku nusu kama siku kamili. Siku zao zilianza jioni. Yesu alikufa muda wa saa 9 jioni siku ya Ijumaa na alizikwa kabla ya saa 12 jioni. Hii ilihesabiwa kama siku moja. Alibakia kuzimu siku yote ya Sabato, kutoka saa 12 jioni siku ya Ijumaa hadi saa 12 jioni siku Jumamosi. Na muda kabla ya mawio ya jua siku ya Jumapili alifufuka (tazama mada maalum: Ufufuo katika Mt. 27:63), kwa namna hiyo, ni siku tatu za Kiyahudi.

**16:22 "Petro akamchukua, akaanza kumkemea"** Petro alikiuka mipaka yake. Yesu alitumia neno “kukemea” kwenye muktadha mingine kadhaa imara (kama vile Mt. 8:26; 12:10; 16:20). Hisia binafsi za Petro kwa ajili ya Yesu zilikuwa juu ya kutawala mpango wa Mungu wa ukombozi.

☐ **"haya hayatakupata"** hii ni wazi “reheba ziwe kwako” ambayo inadokeza “reheba za Mungu ziwe kwako hivyo haya hayawezi kutokea kwako.” Haya ni makanusho imara mawili yaliyotumika kwa ajili ya kusisitiza.

**16:23 "Nenda nyuma yangu, Shetani"** Petro, ambaye muda mfupi baada ya kuongea ufunuo kutoka kwa Mungu, sasa anaongelea majaribu toka kwa shetani. Hili ni sawa na jaribu lile lile ambalo Yesu alikutana nalo jangwani, njia ya kuelekea msalabani (kama vile Mt. 4:1-11). Kwenye muktadha huu, Petro alikuwa msemaji wa shetani!

☐ **"kikwazo kwangu"** hii inarejelea kwa uwazi chambo kwenye mtego wa mnyama. Neno limetumia sitiari ya kizuizi.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 16:24-27**

<sup>24</sup> Wakati huo Yesu aliwaambia wanafunzi wake, Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuata. <sup>25</sup> Kwa kuwa mtu atakaye kuiokoa nafsi yake, ataipoteza; na mtu atakayepoteza nafsi yake kwa ajili yangu, ataiona. <sup>26</sup> Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake? <sup>27</sup> Kwa sababu Mwana wa Adamu atakuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika zake; ndipo atakapomlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake.

**16:24 "wanafunzi"** Hii inamaanisha “wanaojifunza.” Msisitizo wa Yesu haukuwa kwenye maamuzi ya awali pekee bali kuendelea na kufanywa kuwa mwanafunzi zaidi (kama vile Mt. 28:19).

☑ **"akitaka"** hii ni sentensi amrishi daraja la kwanza ambayo inathibitisha ukweli kutoka katika taswira ya mwandishi au makusudi ya fasihi yake. Yesu anathibitisha kwamba watu watataka kumfuata yeye.

☑ **"na ajikane mwenyewe"** hii ni kauli ya kati (ushahidi wa mwandishi) shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu. Ni lazima kuwe na tendo la muhimu. Waaminio ni lazima wageuke kutoka maisha ya ubinafsi (matokeo ya anguko la Mwanzo 3) kwenye maeneo yote. Dhana hii inafanana na kutubu.

**16:24 "ajitwike msalaba wake, anifuate"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu. Msisitizo huu mmoja umeandikwa kwenye Marko 8:35; Luka 9:24; Yn 12:25. Tendo lingine muhimu limeitwa. Wahalifu walioshutumiwa walibeba msalaba wao kuelekea sehemu ya kusulubiwa (kama vile Yn. 12:24). Hii ni sitiari ya kifo cha mateso, kwenye muktadha huu, kifo ni maisha binafsi (kama vile Yn. 12:24; 2 Kor. 5:13-14; Gal. 2:20; 1 Yn. 3:16).

☑ **"anifuate"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Kama katika tungo mbili zilizopita ambapo umuhimu unaamriwa (kauli shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu) hii inaongelea maisha ya kawaida. Ushirika (mwanafunzi wa sheria ya kiyahudi) katika karne ya kwanza muktadha maalumu ulihitajika. Kama vile Yesu alivyowaita wanafunzi watembe nae, aliwaita waaminio wa kila umri. Yesu aliyamimina maisha yake kwa watu hawa na wao wanaitikia kwa kuyamimina maisha yao kwa wengine (kama vile 2 Tim. 2:2; 1 Yn. 3:16). Yesu mara nyingi aliongelea umuhimu wa kuendeleza asili ya ushirika (kama vile Mt. 10:37-39; Marko 8:38-39; Luka 9:23-27; 14:25-27; 17:33; Yn. 12:25).

**16:25** enzi mpya ni tofauti na uovu wa sasa, maisha binafsi. Wanadamu huonyesha kwamba mabadiliko hufanywa kwa namna wanavyoishi (kama vile Mathayo 7 na 13). Kuishi maisha ya haki hakufanyi haki sawa na Mungu (kama vile Efe. 2:8-9); ukiri na imani hutenda (yaani. 16:16), lakini inatupa badiliko la ushahidi lililofanywa!

Neno "nafsi" (*psuchē*) ni sawa na *nephesh* (BDB 659), ambalo linadokeza uzima katika sayari ya Dunia, kwenye jambo hili maisha ya kujiongoza binafsi (yaani, mwanadamu). Wito wa enzi moya ni kwa ajili ya malengo mapya ya msingi. Enzi ya kale inaelezewa kwa msukumo wa mbele binafsi (kama vile Mwanzo 3), lakini enzi mpya inaelezwa kwa kujitoa binafsi. Sura ya Mungu katika mwanadamu (kama vile Mwa. 1:26-27) iliharibiwa na anguko. Wokovu ulirejesha sura hivyo ni ushirika na Mungu (yaani, kusudi la uumbaji) uliorejeshwa! Utu unawekwa tena na utumishi, dhambi kwa utakatifu, mimi kwa huduma, zaidi na zaidi kwa ajili yangu na zaidi katika yeye!

**16:26 "kwani"** hii ni sentensi amrishi daraja la tatu ambalo linamaanisha tendo muhimu la wakati ujao. Wengine wanapata vitu vya ulimwengu lakini kiroho wamepotea, vitu vya umilele.

☑ **"mtu atatoa nini badala ya nafsi yake"** maisha ya ubinafsi mwisho wake ni kifo, lakini maisha yatolewayo kwa ajili Kristo matokeo yake ni katika maisha ya uzima wa umilele (kama vile. Marko 8:34-38). Waaminio wanawajibika kwa kipawa cha utumishi wa maisha ya kimwili na maisha ya kiroho!

**16:27 " Kwa sababu Mwana wa Adamu atakuja . . . pamoja na malaika zake"** hii inarejelea ujio wa pili (kama vile Mt. 10:23; 24:3, 27, 37, 39; 26:64; Mdo. 1:11; 1 Kor. 15:23; 1 Thes. 1:10; 4:16; 2 Thes. 1:7,10; 2:1,8; Yakobo 5:7-8; 2 Pet. 1:16; 3:4,12; 1 Yn. 2:28; Ufu. 1:7). Tambua malaika wa mbinguni wanaweza kuwa wa Baba na /au malaika wa Mwana. Hii ni njia nyingine ya kutetea Uungu wa Yesu. Mara kadhaa katika Mathayo malaika watakusanyika katika matukio ya siku za mwisho watawagawa wanadamu (kama vile Mt. 13:39-41,49; 24:31).

☑ **"katika utukufu wa Baba yake"** katika Agano la kale neno la Kiebrania lililozoeleka kwa ajili ya "utukufu" (*kbd*) lilikua na asili ya neno la manufaa (ambalo linarejelea jozi ya mizani) ambalo humaanisha "kuwa nzito." Kwamba kilicho na uzito ni cha thamani au kina msingi wa muhimu. Mara nyingi dhamira ya utukufu ilikua imeongezwa neno katika kuelezea ukuu wa Mungu (kama vile Kut.15:16; 24:17; Isa. 60:1-2). Yeye pekee ni wa kuheshimiwa na wa thamani. Tazama Yeye pia ni mng'ao kwa ajili ya anguko la mwanadamu (kama vile. Kut 33:17-23; Isa. 6:5).

Mungu anaweza kuwa ukweli unaofahamika kupitia kwa Kristo (kama vile Yer. 1:14; Mt. 17:2; Ebr. 1:3; Yakobo 2:1).

Neno “utukufu” ni kama lina utata: (1) yumkini likafanana na “haki ya Mungu”; (2) yumkini likarejelea “utakatifu” au “ukamilifu” wa Mungu; (3) linaweza kurejea sura ya Mungu ambayo katika hiyo mwanadamu aliumbwa (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1; 9:6), lakini ambalo baadae lilitiwa dosari kupitia uasi (kama vile Mwa. 3:1-22). Kwa mara ya kwanza limetumika kama uwepo wa YHWH na watu wake (kama vile Kut. 16:7,10; Law. 9:23; Hes. 14:10).

☐ "ndipo atakapomlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake" hili ni dokezo la Zab. 62:12 au Mit. 24:12. Hukumu hii ya matendo inaonekana kwenye Ayu 34:11; Zab. 28:4; Mit. 24:12; Mhu. 12:14; Yer. 17:10; 32:19; Mt. 16:27; 25:31-6; Rum. 2:6; 14:12; 1 Kor. 3:8; 2 Kor. 5:10; Gal. 6:7-10; 2 Tim. 4:14; 1 Pet. 1:17; Ufu. 2:23; 20:12; 22:12. Maisha yetu yanaonyesha utii wetu! 1 Yohana na Yakobo wanadai kwamba kwa kadri tuishivyo tunapata ushahidi wa uthabiti wa weledi wa imani yetu. Hakuna matunda-hakuna asili! Yesu alikuja kama mwokozi (kama vile Yn 3:16-21), lakini atarudi kama hakimu (kama vile. Ufunuo 19)!

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 16:28**

**<sup>28</sup> Amin, nawaambieni, Pana watu katika hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika ufalme wake.**

**16:28** huu ni mstari mgumu sana kuutafsiri. Kwenye muktadha inaonekana inarejelea ujio wa pili, lakini Mathayo, Aliandika miaka arobaini na zaidi baada ya kifo cha Yesu, alitambua hii sio sahihi. Inaweza kurejelea kwa

1. kupaa kwa Yesu
2. ufalme ambao tayari umekwisha onekana kwa Yesu
3. Parousia au ujio wa pili
4. ujio wa Roho na matayarisho ya siku ya Pentekoste
5. maangamizi ya Yerusalemu mwaka wa 70 B.K chini ya Jemedari wa Kirumi Tito
6. kubadilika sura kulikoandikwa kwenye sura inayofuata (muhtasari wa karibu kwenye Marko 9:1 na 9:2)

Kwa sababu ya muktadha wa karibu sana wa Mathayo 17, chaguo la sita linafaa zaidi. Tazama mada maalumu ya Ufalme wa Mungu katika Mt. 4:17 na Utawala wa Ufalme wa Mungu katika Mt. 5:3.

☐ "amin" tazama mada maalumu katika Mt. 5:18.

☐ "hawataonja mauti" hii ni Nahau ya Kiebrania kwa ajili ya kufa (kama vile. 1 Sam. 15:32).

## **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. kwa nini Mt. 16:13-20 ni msingi kwa ajili ya kanisa la Romani Katholiki?
2. je wanafunzi waliutambua ukuu wa Petro?
3. je Yesu alimaanisha nini aliporejelea neno “kanisa” ? (Mt. 16:18)
4. je mstari wa 18 unadokeza utendaji au mashambulizi ya kutendwa katika kanisa?
5. ni nini ufunguo wa ufalme? (Mt. 16:19)
6. kwa nini aliwazuia wasimwambie mtu yeyote kuwa ndiye Masihi, mwana wa Mungu?
7. kwa nini wanafunzi walirudi nyuma juu ya ufunuo wake Yesu wa siku zijazo?
8. inamaanisha nini kufa binafsi?
9. ni kwa namna gani unaelewa mstari wa 28?

## MATHAYO 17

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Kugeuka kwa Yesu 17:1-8	Yesu anageuka katika Mlima 17:1-13	Kugeuka 17:1-8	Kugeuka 17:1-4 17:5	Kugeuka 17:1-8
17:9-13		Unabii Juu ya Eliya 17:9-13	17:6-8 17:9 17:10 17:11-12 17:13	Swali juu ya Eliya 17:9-13
Uponyaji wa kijana Mwenye pepo 17:14-20	Kijana anaponywa 17:14-21	Kijana mwenye Kifafa anaponywa 17:14-21	Yesu anaponya Kijana mwenye pepo 17:14-16 17:17-18 17:19 17:20-21	Pepo wa kifafa 17:14-18 17:19-20
17:21 Yesu anatabiri Tena kifo chake Na Ufufuko 17:22-23	Yesu tena anatabiri Kifo chake na Ufufuko 17:22-23	17:21 Mateso yanatabiriwa kwa mara ya pili 17:22-23 17:23c	Yesu anazungumza Tena juu ya kifo Chake 17:22-23b	17:21 (haijumuishwi) Unabii wa Pili juu ya Mateso 17:22-23
Malipo ya kodi Ya Hekalu 17:24-27	Petro na Bwana Wake Wanalipa kodi zao 17:24-27	Fedha kwa ajili ya Kodi ya Hekalu 17:24-27	Malipo kwa ajili ya Kodi ya Hekalu 17:24 17:25a 17:25b 17:25b 17:26a 17:26b-27	Kodi ya Hekalu inalipwa na Yesu na Petro 17:24-27

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka [“Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia”](#))**

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## UAINISHI WA KIMUHTASARI KWA MISTARI YA 1-27

- A. Kugeuzwa, Mt. 17:1-13 (kama vile Mt. 17:1-11; Marko 9:2-13; Luka 9:28-36; 2 Pet. 1:16-18)
- B. Kuponywa kwa kijana aliyekuwa na pepo, Mt. 17:14-23 (kama vile Marko 9:14-29; Luka 9:37-42)
- C. Hekalu kutaka ushuru kwa Petro na Yesu, Mt. 17:24-27 (hii ni pekee kwa Yesu)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 17:1-8

<sup>1</sup>Na baada ya siku sita Yesu akawatwaa Petro, na Yakobo, na Yohana nduguye, akawaleta juu ya mlima mrefu faraghani; <sup>2</sup>akageuka sura yake mbele yao; uso wake ukang'aa kama jua, mavazi yake yakawa meupe kama nuru. <sup>3</sup>Na tazama, wakatokewa na Musa na Eliya, wakizungumza naye. <sup>4</sup>Petro akajibu akamwambia Yesu, Bwana, ni vizuri sisi kuwapo hapa; ukitaka, nitafanya hapa vibanda vitatu, kimoja chako wewe, na kimoja cha Musa, na kimoja cha Eliya. <sup>5</sup>Alipokuwa katika kusema, tazama, wingu jeupe likawatia uvuli; na tazama, sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye. <sup>6</sup>Na wale wanafunzi waliposikia, walianguka kifulifuli, wakaogopa sana. <sup>7</sup>Yesu akaja, akawagusa, akasema, Inukeni, wala msiogope. <sup>8</sup>Wakainua macho yao, wasione mtu ila Yesu peke yake.

**17:1 "siku sita baadaye"** Kifungu cha ufanana katika Marko 9 pia kina siku sita, bali Luka 9:28 kinaandika siku nane. Hii si sana mkanganyiko kama ilivyo kwa njia mbili za kuelezea Wiki.

☑ **"Yesu akawatwaa Petro, na Yakobo, na Yohana nduguye"** Watu hawa walitengeneza kikosi cha ndani zaidi, si watu waliopendwa zaidi na Yesu, bali wale ambao yawezekana walikuwa makini kiroho na wanaofundishika (kama vile Mt. 2:13; 4:5; 12:45). Yakobo alikufa mapema zaidi. Mungu hana upendeleo. Angalia jedwali katika Mt. 10:2.

☑ **"akawaleta juu ya mlima mrefu faraghani"** Mathayo kidhahiri analinganisha Musa Mlimani katika Kut. 19:24; 24:1 na kubadilishwa huku kwa Yesu. Maeneo manne ya ulinganifu yangukuwa

1. wote walikuwa juu mlimani
2. Mungu alizungumza kutoka katika wingu katika matukio yote (kama vile Kut. 24:16)
3. Sura ya Musa ilig'aa, (kama vile kut. 34:29), na mwili wote wa Yesu ulig'aa
4. wale waliokuwa jirani na Musa waliogopa kama wale waliomsindikiza Yesu pia

Kumekuwa na mjadala mkubwa kuhusu mlima huu ulikuwa ni mlima gani. Eneo lililozoeleka ni Mlima Tabori, lakini hii ni mbali kuytoka Kaisaria Filipi. Baadhi wanasema ilikuwa Mlima Hermoni ambao inawezekana ikawa zaidi. Yawezekana zaidi ilikuwa ni Mlima Mironi, mlima mrefu zaidi katika mipaka ya kingo za Nchi ya Ahadi; Pia ipo njia ya kutokea Kaisaria Filipi kuelekea Karpenaumu.

**17:2 "akageuka sura yake mbele yao"** Hili ni neno ambatani la Kiyunani kutoka "baada" (*meta*) na "muundo" (*morphē*). Neno "kugeuzwa" linatoka katika Vulgate ya Kilatini. Tunapata neno la Kingereza metamorphosis kutoka neno ambatani la Kiyunani. Kisawe cha kithiolojia ni kwamba asili ya Uungu ya Yesu ilivunjwa kupitia asili ya uanadamu. Neno linatumika pia juu ya kitu gani kinatokea katika namna ya kiroho kwa waaminio (kama vile Rum. 12:2; 2 Kor. 3:18).

Tunajifunza kutoka Luka 9:28 kwamba hii ilitokea wakati walikuwa wakiomba. Inaweza hata kuwa ilikuwa usiku baada ya mwendo mrefu kuelekea katika mlima huu; hivyo wanafunzi walikuwa wamechoka na wenye usingizi.

Tukio hili lina ufanano na Bustani ya Gethsemane.

☑️"**uso wake ukang'aa kama jua**" Hii inaonekana kuwa sura nyingine ya kitabu cha Injili ya ambacho kinajaribu kumuwasilisha Yesu kama Musa mwingine, Musa ag'aaye sana, Mathayo (kama vile Kut. 34:29-35). Hii isieleweke kama ndio ulinganifu.

1. Mg'ao wa sura ya Musa uliisha
2. Musa alificha kule kuchakaa
3. Musa alilipokea neno la Mungu, Yesu ni neno la Mungu (kama vile Mt. 5:17-48)

☑️"**mavazi yake yakawa meupe kama nuru**" Weupe kipekee unahusianishwa na kutukuzwa kimbingu kwa watakatifu na viumbe.

1. Kugeuka kwa Yesu
2. malaika pale kaburini, Mt. 28:3
3. malaika wakati wa kupaa kwake, Mdo 1:8
4. malaika (kifasihi. "wazee") kuzunguka kiti cha enzi, Law. 4:4
5. jeshi la kimbingu la malaika, Law. 19:14
6. watakatifu kutukuzwa, Law. 3:4-5,18; 6:11; 7:9,13

**17:3 "wakatokewa na Musa na Eliya, wakizungumza naye"** Kumekuwa na mjadala mkubwa juu ya kwanini Musa na Eliya. Baadhi wanasema hii inawakilisha Sheria na Manabii. Wote walikuwa mifano ya siku za mwisho, Musa kutoka Kumbu kumbu la Torati 18 na Eliya kutoka Malaki 4. Wengine wanasema kuwa wote walikutana na vifo visivyokuwa vya kawaida. Wote kwa pamoja wanawakilisha utaratibu wa zamani na walikuwa wakimtia moyo Yesu wakati anaanzisha utaratibu mpya. Ni kwa namna gani wanafunzi walijua kwamba ilikuwa ni Musa na Eliya haijulikani labda walikuwa katika mavazi ya aina fulani yenye sifa, kwa kauli zao, au Yesu aliwaambia.

Kama ilivyo kwa miujiza na utabiri wa Yesu, uzoefu huu ulikuwa zaidi kwa imani za wanafunzi hawa na ukuaji wa imani (kama vile Mt. 17:5) kama milivyokuwa kwa kutiwa moyo kwa Yesu.

Suala lingine la nyongeza, hii ilikuwa ni kuonesha waamini wa Agano la Kale walikuwa bado hai! Inathibitisha kuwa na uhai wa kujitambua baada ya kifo mara baada ya kifo cha mwili.

**17:4 "Petro akamwambia Yesu"** Petro aliingilia na kujibu swali ambalo halikuwahi kuulizwa, hii ilikuwa ni tabia ya Paulo.

☑️"**ukitaka, nitafanya hapa vibanda vitatu**" Maana yake ilikuwa ni "Hebu tuendelee kukaa hapa hapa (sentensi daraja la kwanza yenye masharti). Hii hali ilikuwa ya kupendeza sana na ya kiroho." Kwa namna fulani hii ilifanya kazi kama tukio la jaribu katika Mathayo 4 - njia nyingine ya kukwepa msalaba. Hii yawezekana ilikuwa ni sababu kwanini hadithi hii ilitunzwa kwa ajili yetu-Yesu kujionesha mwenyewe kuwa hakika Mungu kwa wanafunzi na kujuaribu kwao kugeuka mabali nae (kama vile Mt. 16:22-23) kutoka kwenye kifo chake kilichopangwa hapo kabla (kama vile Marko 10:45). Katika muktadha huu huu wa kifasihi (kama vile Mt. 19:16-17), Yesu anasimulia tena juu ya kifo kinachomsabiri (kama vile Mt. 17:9-13, 22-23).

**17:5 "wingu jeupe likawatia uvuli; na tazama, sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema"** Wingu hili lig'aalo lilikuwa likihusiana na *Shekinah* wingu la utukufu wa Agano la Kale ambalo lilikuwa ni ishara ya uwepo binafsi wa Mungu. Wingu hili lilitokea mara moja kabla ya ubatizo wa Yesu (kama vile Mt. 3:17). Petro alilielezea baadaye katika 2 Pet. 1:17-18. Kunawezekana hata kukawa na baadhi ya muunganiko kati ya Mungu kuzungumza kutokea mawinguni na dhana ya kiyahudi *bath kol*, ambalo ilikuwa njia wakati wa kipindi cha kati ya Agano Jipya na Agano la Kale cha kuthibitisha mapenzi ya Mungu kwakuwa kulikuwa hakuna nabii.

Tungo hii "likawakalia" linatokea katika mzizi ule ule wa Kiyunani uliotumika kurejerea kutungwa mimba cha Yesu kwa Roho Mtakatifu kwa Bikra Mariamu katika Luka 1:35.

Kile alichokisema Mungu ni muhimu sana. Ufanano katika Luka inaunganisha nukuu kutoka Zab. 2:7 (Mwanangu) na Isa. 42:1 (Mteule wangu, kama vile Luka 9:35). Zaburi 2 ni zaburi ya kifalme ya Daudi na Isaya 42 ni mwanzo wa Wimbo wa Mtumishi wa Isaya. Hapa tuna uungu kamili wa Yesu ukiunganishwa na huduma ya Mtumishi Atesekaye wa Isaya (kama vile Marko 9:28; Luka 9:28-36). Hii inaaksi unabii wa Mwa. 3:15.

☐ **"msikieni yeye"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo ambayo inaaksi Kumb. 18:15,18-19 na kumaanishwa katika Isaya 42:1. Kuwa mfuasi wa Yesu sio tu kulimaanisha uelewa wa kithiolojia wa Utu Wake na misheni bali pia utii (tazama Kumb. 18:20)!

**17:6 "walianguka kifulifuli, wakaogopa sana"** Watu wa Biblia waliamini kwamba kumuona Mungu kulimaanisha kufa (kama vile Kut. 33:20-23; Waamuzi 6:22-23; 13:22; Yohana 1:18; 6:46; kol. 1:15; 1 Tim. 6:16; 1 Yohana 4:12). Sauti ya Mungu iliwatisha Mitume hawa kama ilivyokuwa imewaogopesha hapo mwanzo watu wa Mungu katika Mlima Sinai (kama vile kut. 19:16). Kumbuka Mathayo alimuwasilisha Yesu kama mtoaji sheria wa pili, au Musa wa pili (kama vile Kumb. 18:15).

**17:7 "Yesu akaja, akawagusa"** Walikuwa wamelala (kama vile Luka 9:32). Hii inawezekana kuwa tukio la muda wa usiku ambapo utukufu wa Yesu ulikuwa umeg'aa kote na mg'ao zidi dhidi ya kiza cha anga la usiku. Mguso huu ulikuwa ishara ya kwamba Yesu anawajali.

☐ **"Inukeni, wala msiogope "** Hizi zote ni kauli shurutishi. Zina zungumzia mambo yanayotokea sasa.

1. hapana hatuwezi kukaa hapa juu mlimani (shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu)
2. msiogope juu ya tukio hili la ukaribu na Mungu (shurutishi ya wakati uliopo)

Hali hii ilikuwa ikihamasisha kitendo, sio hali ya kukaa tu bila hatua, na kutia moyo katika jukumu, sio hofu!

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 17:9-13**

<sup>9</sup>Na walipokuwa wakishuka mlimani, Yesu aliwaagiza, akasema, Msimwambie mtu ye yote habari ya maono hayo, hata Mwana wa Adamu atakapofufuka katika wafu. <sup>10</sup>Wanafunzi wake wakamwuliza, wakisema, Basi kwa nini waandishi hunena ya kwamba imempasa Eliya kuja kwanza? <sup>11</sup>Naye akajibu, akawaambia, Kweli Eliya yuaja kwanza, naye atatengeneza yote, <sup>12</sup>ila nawaambia, ya kwamba Eliya amekwisha kuja, wasimtambue, lakini wakamtenda yote waliyotaka. Vivyo hivyo Mwana wa Adamu naye yuaenda kuteswa kwao. <sup>13</sup>Ndipo wale wanafunzi walipofahamu ya kuwa amesema nao habari za Yohana Mbatizaji.

**17:9 "Yesu aliwaagiza, akasema, Msimwambie mtu ye yote habari ya maono hayo, hata Mwana wa Adamu atakapofufuka katika wafu"** Hii ni siri ya Kimasihi (kama vile Mt. 8:4; 9:30; 12:16; 16:20; Marko 1:44; 3:12; 5:47; 7:36; 8:30; 9:9; Luka 4:41; 5:14; 8:56; 9:21). "Waambie" ni kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopita usio timilifu. Luka 9:30 inasema kwamba hawakumwambia mtu. Tatizo lilikuwa, wangeenda kusimulia nini? Yesu alikuwa tayari ana tatizo la kutojulikanana kama mtenda miujiza na injili ilikuwa bado haijamalizika. Kungetokea wakati kama Yesu alivyotaja katika Mt. 17:9, baada ya Yeye kuwa amefufuka mawinguni kutoka kwa wafu (aliwaambia mara kadhaa hili katika namna nyingi lakini hawakuonekana kulisikiliza au kupata maana yake), kwamba maudhui ya kithiolojia ya tukio hili yangeweza kueleweka.

Mstari wa 9 pia unamaanisha kwamba hii ilikuwa ni rejea kwa mateso ya Yesu (kama vile Mt. 16:21 na kuendelea), ambacho kwamba jaribio la Petro kuwakalisha mlimani lilikuwa ni lengo lingine la shetani.

**17:10 "Wanafunzi wake wakamwuliza, wakisema, Basi kwa nini waandishi hunena ya kwamba imempasa Eliya kuja kwanza?"** Hii ilirejerea kwa unabii wa Mal. 3:1 na 4:5. Kumekuwa na mjadala kuhusu jibu ambalo Yesu alitoa. Alisema kibayana kwamba Eliya alikuwa amekwisha kuja katika huduma ya Yohana Mbatizaji (kama vile Mt. 11:10, 14; Marko 9:11-13; Luka 1:17). Hata hivyo wakati Mafarisayo walimuuliza Yohana katika Injili ya Yohana (1:20-25) ikiwa alikuwa Eliya, alikataa waziwazi. Hii inaonekana kuwa mkanganyiko unaweza kuwezesha na ukweli kwamba Yohana alikataa kwamba alikuwa Eliya aliyefufuka, lakini Yesu alikiri kwamba Yohana kiishara alitimiliza maandalizi ya huduma ya Eliya. Wote walikuwa wamevaa na kutenda kazi katika namna inayofanana, hivyo utambulisho ungekuwa wazi katika ufahamu wa Wayahudi waliojua kuhusu Eliya na waliosikia na mkumuona Yohana Mbatizaji (Luka 1:17).

☑ **"Vivyo hivyo Mwana wa Adamu naye yuaenda kuteswa kwao"** Haya ni maudhui yanayojitokeza tokeza baada ya ukiri wa Petro (kama vile Mt. 16:21; 17:9,12,22-23; 20:18-19). Aliwaambia kuhusu mateso Yake lakini ikiwa walisikia, pia bado aliwaambia juu ya Kufufuka kwake. Masihi Atesekaye alikuwa mgeni sana kwa desturi zao za Kiyahudi kwamba hawakuweza tu kumpokea!

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 17:14-18**

<sup>14</sup>Nao walipoufikia mkutano, mtu mmoja akamjia, akampigia magoti, akisema, <sup>15</sup>Bwana, umrehemu mwanangu, kwa kuwa ana kifafa, na kuteswa vibaya; maana mara nyingi huanguka motoni, na mara nyingi majini. <sup>16</sup>Nikamleta kwa wanafunzi wako, wasiweze kumponya. <sup>17</sup>Yesu akajibu, akasema, Enyi kizazi kisichoamini, kilichopotoka, nitakaa pamoja nanyi hata lini? Nitachukuliana nanyi hata lini? Mleteni huku kwangu. <sup>18</sup>Yesu akamkemea pepo, naye akamtoka; yule kijana akapona tangu saa ile.

**17:15 "Bwana, umrehemu mwanangu"** Neno "Bwana" (*kurios*) inaweza kumaanisha "msheshimiwa" au "mkuu" (kifasihi. *kurie*), bado katika baadhi ya muktadha inachukua visawe vya kithiolojia. Hii yawezekana ni moja yake. Ombi la mtu huyu lilimaanisha swali lililoulizwa. Je Yesu aweza kurehemu (kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu) kama mtu huyu alivyouliza? Hili ni swali ambalo agano la Kale lilitabiri, Masihi angekuwa na Rehema (kama vile Isaya 35:2- 6; 61:1-2). Nguvu ya Yesu na Huruma (kama vile Mt. 9:27; 15:22; Marko 10:47,48; Luka 17:13) zilikuwa ni "ishara" ambazo uongozi wa kiyahudi walikuwa wakitafuta!

**NASB, NJB** "ni mwendawazimu"  
**NKJV, NRSV,**  
**TEV** "anakifafa"  
**NJB** "ni taahira"

Hadithi yenye maelezo ya ziada juu ya ugonjwa huu inatolewa katika Marko 9:18-20. Neno "kifafa" lilikuwa neno la kibayana "kupigwa na mwezi" au "uendawazimu." Aina hii ya ugonjwa ulikuwa umesababishwa na pepo (kama vile Mt. 17:18). Kuna jaribio kubwa katika Agano Jipya kutofautisha kati ya kupagawa na pepo ambayo mara kwa mara inasababisha ugonjwa wa mwili na udhaifu wenyewe (kama vile Mt. 4:24). Hii ilikuwa ni hadithi ya upungaji pepo sio uponyaji.

**17:16 "Nikamleta kwa wanafunzi wako, wasiweze kumponya"** Hii ilikuwa hali ya tofauti sana, kwa 10:1,8 inatwambia walikuwa na nguvu hii waliopewa. Sababu hasa kwa kushindwa kwao katika jambo hili haikuwa imetajwa kama ukosefu wa imani na maombi. Hadithi yenye maelezo ya ndani zaidi ya mazungumzo kati ya Baba na Yesu yanaandikwa katika Marko 9:21-24.



**17:17 " Yesu akajibu, akasema, Enyi kizazi kisichoamini, kilichopotoka,"** Hii ilikuwa maelezo ya Kumb. 32:5, 20. Katika hali ya jaribu la Yesu (na kuendelea Mathayo; Luka 4), Alinukuu Kumbu Kumbu la Torati mara tatu. Lazima alikuwa amejua na kukipenda kitabu hiki.

Swali la kimaandiko ni kwa nani Yesu alikuwa anazungumza

1. wanafunzi (kama vile Mt. 17:19-20)
2. mtu/makutano/kizazi hicho
3. viongozi wa Kiyahudi
4. wanadamu walioanguka kwa ujumla wao

Inafurahisha kwamba "kizazi" mara kwa mara ina maana hasi (kama vile Kut 1:6; Kumb 1:35; 32:5; Zab. 12:7).

Tazama wasioamini hawa walivyokuwa katika makundi ya sifa.

1. waovu na wazinzi, Mt. 12:39
2. wasioamini na waliopotoka, Mt. 17:17
3. wazinzi na wenye dhambi, Marko 8:38
4. wasioamini na wenye imani haba, Marko 9:19
5. waovu, Luka 11:29
6. waliopotoka, Mdo 2:40
7. waliopotoka na kuharibikiwa, Flp. 2:15

**17:18 "yule kijana akapona tangu saa ile"** Kwa ajili ya hadithi ya maelezo zaidi angalia Marko 9:26. Lazima ikumbukwe kwamba kila mwandishi wa injili aliandika hadithi hizi katika namna yake mwenyewe kwa ajili ya makusudi yake ya kipekee na hadhira wake. Hivyo ni muhimu kujaribu kuelewa kila mmoja wao mmoja mmoja kabla ya kuwauliza wengine na kuunganisha taarifa (kama vile Gordon Fee and Douglas Stuart katika *How to Read the Bible For All Its Worth*, ukur. 113-134)

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 17: 19-21**

**19** Kisha wale wanafunzi wakamwendea Yesu kwa faragha wakasema Mbona sisi hatukuweza kumtoa? **20** Yesu akawaambia, Kwa sababu ya upungufu wa imani yenu. Kwa maana, amin, nawaambia, Mkiwa na imani kiasi cha punje ya haradali mtuambia mlima huu, Ondoka hapa uende kule; nao utaondoka; wala halitakuwako neno lisilowezekana kwenu. **21** [Lakini namna hii haitoki ila kwa kusali na kufunga.]

**17:19 "Mbona sisi hatukuweza kumtoa?"** Yesu alijibu swali hili katika Mt. 17:20 ambapo alisema, "enyi wenye imani haba." Hii ilikuwa ni sentensi iliyorudiwa na Yesu (kama vile Mt. 6:30; 8:26; 14:31; 16:8). Mitume walikuwa si malaika wakubwa. Hakuwa watakatifu wakubwa wenye ukamilifu wote!

**17:20**

**NASB** "uhaba wa imani yenu"

**NKJV** "kutoamini kwenu"

**NRSV** "imani yenu haba"

**TEV** "hamna imani ya kutosha"

**NJB** "mna imani kidogo sana"

Maandiko ya kale ya Kiyuani ikiwemo  $\alpha$  na B, yana "imani haba" (*olieopistis*), wakati mengine ikiwemo C, D, L & W, yana "wasioamini" (*apistis*). Kwasabu ya neno la kwanza lilikuwa nadra yawezekana lilikuwa ni la asili. Toleo la UBS<sup>4</sup> linaipa alama ya "A".

☐ "Mkiwa na imani kiasi cha punje ya haradali mtauambia mlima huu, Ondoka hapa uende kule" Mbegu ya haradali ilikuwa punje ndogo kabisa kuliko zote zilizokuwa zikijulikani na watu wa Kiyahudi. Yesu hakuwa anasisitiza nguvu ya imani ya wanadamu wenyewe bali kinachokusudiwa katika imani ile. Yesu hakuwa anawashambulia kutawanyika kwao kwa imani na hitaji lake; ni muhimu (kama vile Ebr. 11:1). Kut 21:21 inaonekana kwamba "imani haba" inawekewa sifa na Yesu kama "mashaka." Hii ni sentensi daraja la tatu yenye masharti; Alifikiria wangukuwa na imani. Dhana ya mlima kuhamishwa ilikuwa ni nji ya mfano ya kurejerea tatizo kubwa zaidi. Hii inaweza kuonekana katika Isaya. 40:4; 49:11; 54:10. Baadhi wanaamini kwamba Yesu aliwasonteshea mlima mahali alipokuwa hasa wakati anageuzwa sura usiku wake uliopita.

**17:21** Mstari wa 21 haupatikani katika andiko la Kiyunani la aidha Siniaticus (κ) au Vaticanus (B). Inaonekana kujumuishwa na wanakili wa mwanzoni kutoka katika hadithi ya ufanano katika Marko 9:29, ambapo ingejumuishwa katika maandiko ya asili. Toleo la UBS<sup>4</sup> haliweki ujumuishi na kutoa alama ya "A".

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 17:22-23**

<sup>22</sup> Nao walipokuwa wakikaa Galilaya, Yesu akawaambia, Mwana wa Adamu anakwenda kutiwa katika mikono ya watu, nao watamwua, na siku ya tatu atafufuka. <sup>23</sup> Wakasikitika sana.

**17:22**

**NASB** "wakati walipokuwa wakikusanyika Galilaya"

**NKJV** "walipokuwa wakikaa Galilaya"

**NRSV** "walipokuwa wakikaa Galilaya"

**TEV** "wakati wanafunzi wote walipokusanyika pamoja Galilaya"

**NJB** "siku moja walikuwa wote huko Galilaya"

Kuna utofautiano wa maandiko ya Kiyunani katika pointi hii. Maandiko ya kale ya κ na B na andiko la Kiyunani lililotumika na Origen yana "yote yalikuja pamoja," wakati C, D, L & W yana "kukaa." Neno la kwanza lilichukuliwa vibaya na wandishi wa kale na kubadilika katika andiko linalojulikana zaidi. Sababu wale Kumi na Mbili waligawanywa katika makundi manne ya watatu ilikuwa ni kwamba walikuwa na zamu katika kusafiri na Yesu na kurudi nyumbani kwa ajili ya vipindi vifupi vya kuangalia familia zao. Mstari huu unazungungumzia wanafunzi na Yesu kukutana sehemu fulani.

**17:22-23** "Mwana wa Adamu anakwenda kutiwa katika mikono ya watu, nao watamwua, na siku ya tatu atafufuka" Yesu alionesha ufahamu wake wa kinabii kuhusu mateso Yake na kifo (kama vile Mt.16:21ff.; 17:9,12; Yohana 10:11,15,17,18). Yesu alikuwa naanza kuweka msingi wa uelewa wa wanafunzi juu ya nini kinakwenda kutokea wakati wa wiki ya mwisho ya Maisha Yake. Kutoka katika kifungu hiki tunajifunza kwamba Yesu angekamatwa na kupelekwa kwa Mataifa (yaani Warumi, kama vile Mt. 20:19).

**17:23** "nao wote walishikwa na huzuni sana" Ufanano wote wa aina mbili wa Injili Marko (9:32) na Luka (9:45) kunaongeza kwamba hawakuelewa lakini walikuwa na hofu ya kuuliza. Inashangaza kwamba Wakuu wa Sinagoga walielewa utabiri wa Yesu kuhusu kufufuka kwake lakini wanafunzi walikuwa katika hali ya kushangazwa tu (kama vile Luka 24:36-38).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 17:24-27**

<sup>24</sup> Hata walipofika Kapernaumu, wale watozao nusu-shekeli walimwendea Petro, wakasema, Je! Mwalimu wenu hatoi nusu-shekeli? Akasema, Hutoa. <sup>25</sup> Naye alipoingia nyumbani, Yesu alitangulia kumwuliza, akisema, Waonaje, Simoni? Wafalme wa dunia hutwaa kodi ama ushuru kwa watu gani? Kwa wana wao au kwa wageni? <sup>26</sup> Naye aliposema, Kwa wageni, Yesu alimwambia, Basi, kama ni hivyo, wana ni

**mahuru.<sup>27</sup> Lakini tusije tukawakwaza, enenda baharini ukatupe ndoana, ukatwae samaki yule azukaye kwanza; na ukifumbua mdomo wake utaona shekeli ichukue hiyo ukawape kwa ajili yangu na kwa ajili yako.**

17:24

NASB "nusu shekeli ya kodi"

NKJV, NRSV

TEV "ushuru a hekalu"

NJB "nusu shekeli"

Hii inarejerea kodi ya nusu shekeli ambayo ilikuwa ikitolewa kwa kujitolea kila mwisho wa mwaka na wanaume wa Kiyahudi kati ya umri wa miaka ishirini na hamsini. Ilikuwa ni ulipaji kwa ajili ya ukarabati wa hekalu. Ilitakikana kutolewa mwezi wa tatu wakati mwingine na hivyo ikiwa uelewa wetu wa nyakati ya mazingira ya kifungu cha habari upo sawa, Yesu alikuwa akilipa kodi hii kwa kuchelewa. Kodi hii ilikuwa yawezekana ikijikita kualimu wa kiyahudi katika wito wa Musa katika Kut. 30:11-16 kwa ajili ya Hema. Ingawa ilikuwa kodi ya kujitolea, ilichukuliwa kuwa muhimu na ya msingi na Wayahudi wa Orthodox. Sarafu iliyopatikana katika mdomo wa samaki ingeweza kulipa kodi ya wote Petro na Yesu.

## MADA MAALUMU: SARAFU ZILIZOTUMIKA PALESTINA ENZI ZA YESU

- I. Sarafu za shaba
  - A. *cherma* – thamani ndogo (kama vile Yohana 2:15)
  - B. *chalchos* – thamani ndogo (kama vile Mt. 10:9; Marko 12:41)
  - C. *assarion* –sarafu ya shaba ya Kirumi yenye thamani ya senti 1/16 ya *a dēnarius* (kama vile Mat. 10:29)
  - D. *kodrantēs* – Sarafu ya shaba ya Kirumi yenye thamani 1/64 ya *dēnarius* (kama vile Mt. 5:26)
  - E. *lepton* – sarafu ya shaba ya Kiyunani yenye thamani ipatayo 1/128 ya *dēnarius* (kama vile Marko 12:42; Luka 21:2)
  - F. *quadrans/robo* – Sarafu ya shaba ya Kirumi yenye thamani ndogo
- II. Sarafu za fedha
  - A. *arguros* ("sarafu ya fedha") – yenye thamani kubwa zaidi kuliko shaba au sarafu za shaba nyeusi (kama vile Mt. 10:9; 26:15)
  - B. *dēnarius* – sarafu ya fedha ya Kirumi yenye thamani na ujira wa siku (kama vile Mt. 18:28; Marko 6:37)
  - C. *drachmē* –sarafu ya fedha ya Kiyunani iliyo na thamani sawa na *dēnarius* (kama vile Luka 15:9)
  - D. *di-drachmon* –sarafu mbili za fedha ya kiyunani ilikuwa sawa na ½ shekeli ya kiyahudi (kama vile Mt. 17:24)
  - E. *statēr* –sarafu ya fedha yenye thamani ipatayo *dēnarii* nne (kama vile Mt. 17:27)
- III. Sarafu za dhahabu – *chrusos* ("sarafu za dhahabu") – zenye thamani zaidi (kama vile Mat. 10:9)
- IV. Maneno ya jumla kwa uzito wa chuma
  - A. *mnaa* – Latini *mina*, uzito wa chuma uliosawa na 100 *dēnarii* (kama vile Luka 19:13)
  - B. *talanton* – Kizio cha Kiyunani cha uzito (kama vile Mt. 18:24; 25:15,16,20,24,25,28)
    1. thamani ya fedha 6,000 *dēnarii*
    2. thamani ya dhahabu 180,000 *dēnarii*
  - A. *sheqel* – uzito wa fedha ya Kiyunani katika agano la kale (yaani, 4 oz., kama ile Mwa. 23:15; 37:28; Kut. 21:32)

1. *pīm* – 2/3 shekeli
2. *beka* – ½ shekeli
3. *gerah* – 1/20 shekeli

Vizio vikubwa

1. *maneh* – 50 shekeli
2. *kikkar* – 3,000 shekeli

**17:25-27** Mstari huu unaonesha kwamba Yesu anadai kuwako na upendeleo katika kodi kwa vile yeye alivyo, lakini bado alilipa kodi ili kuweza kuitimiza haki yote (kama vile Mt. 3:15). Yesu alitaka kuwafikia wayahudi wenye desturi za nyakati zake.

**17:25 "Yesu akazungumza naye kwanza"** Je Yesu alikuwa ameyasikia mazungumzo yao au likuwa anatumia maarifa aliyokuwa kapewa hapo kabla? Swali hili linaulizwa tena na tena katika Injili!

☉"**kodi ama ushuru**" Katika aya hii kuna aina tatu tofauti tofauti za kodi zinazotajwa.

1. kodi ya Wayahudi (drachma mbili, Mt. 17:24)
2. kodi ya kichwa ya maeneo (ushuru, Mt. 17:25)
3. kodi ya uchaguzi (kodi ya ufalme wa Kirumi, kama vile Mt. 22:17)

**17:26 "wana ni mahuru"** Hii ni sentensi yenye nguvu sana juu ya U-Masihi wa kifalme wa Yesu. Yeye ni kweli Mfalme astahiliye wa uzao wa Daudi na Wafuasi wake ni wana wa kifalme wasiolipa kodi! Kinachoshangaza ni kwamba Wayahudi (yaani, makusanyo ya kodi ya hekalu) yanachukuliwa kwa wasiokuwa wana!

**17:27** Wengi wamekosoa hadithi hii kwasababu inaonekana Yesu kutumia nguvu zake za U-Masihi kwa ajili ya makusudi yake mwenyewe. Lilikuwa zoezi linaloendelea la nguvu za miujiza za Yesu ambalo lilitumika kufundisha wanafunzi kuongeza imani zao. Katika hadithi hii Yesu alionesha nguvu Yake juu ya asili na Ufahamu wake wa awali ambao ungeweza kumsaidia Petro katika siku zijazo wakati atakapokuwa anapitia nyakati ngumu katika safari yake yeye mwenyewe ya imani. Iliandikwa kwa ajili yetu sisi wenyewe!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini matukio yale yale yanaandikwa mara tatu katika vitabu vya Injili?
2. Kwanini maelezo wakati mwingine yanatofautiana kati ya hadithi hizi katika Injili zingine?
3. Kwanini Yesu alichangua kundi la wanafunzi wa karibu zaidi katika wengi aliokuwa nao?
4. Kwanini Musa na Eliya wanatokea kwa Yesu juu ya Mlima wa Kugeuzwa?
5. Ni nini umuhimu wa kauli ya Mungu katika kuunganisha Zaburi 2 na Isaya 42?
6. Ni kwa namna gani Mathayo 17 ina mahusiano na Mathayo 16 katika kutabiri mateso ya Yesu na kifo?
7. Kwanini tungo "Mwana wa Adamu" inafanya kazi na kutumiwa na Yesu?
8. Je Yohana Mbatizaji likuwa ni Eliya aliyezaliwa mara ya pili?
9. Ni kwa namna gani Imani inahusiana na upungaji pepo na uponyaji?
10. Mapepo ni nini? Je bado yapo katika ulimwengu wetu?
11. Je neno "mlima" katika Mt. 17:20 inarejerea kuanza kushindana na vitu vya nje vinavyoshikika au kushughulikia matatizo ya maisha?

12. Ikiwa Yesu alitabiri kusalitiwa kwake mwenyewe, kifo na kufufuka mara kwa mara, kwanini matukio haya yanashangaza kwa wanafunzi?

## MATHAYO 18

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Mkubwa zaidi katika Ufalme 18:1-5	Nani aliye mkubwa 18:1-5	Misemo juu ya upole na Msamaha 18:1-5	Nani aliye mkubwa Zaidi 18:1 18:2-5	Nani aliye mkubwa Zaidi 18:1-4
Jaribu ili kutenda Dhambi 18:6-9	Yesu anaonya juu ya Makosa 18:6-9	Maono juu ya kuzimu 18:6-7 18:8-9	Jaribu ili kutenda Dhambi 18:6-7 18:8-9	Juu ya kuwapoteza wengine 18:5-7 18:8-9
Mfano wa Kondoo Aliyepotea 18:10-14	Mfano wa Kondoo aliyepotea 18:10-14	Kondoo aliyepotea 18:10-14	Mfano wa Kondoo Aliyepotea 18:10-11 18:12-14	18:10 18:11 (Haijumuishwi) Kondoo aliyepotea 18:12-14
Ndugu atendaye Dhambi 18:15-17 18:18-20	Kuenenda na ndugu atendaye dhambi 18:15-20	Nidhamu juu ya wafuasi 18:15-20	Ndugu atendaye dhambi 18:15-17 Kukataa na kuruhusu 18:18 18:19-20	Kuonyana kindugu 18:15-17 18:18 Maombi kwa kawaida 18:19-20
Mfano wa Mtumishi asiyesamehe 18:21-35	Mfano wa Mtumishi asiyesamehe 18:2-35	Msamaha 18:21-22 18:23-35	Mfano wa Mtumishi Asiyesamehe 18:21 18:22-27 18:28-34 18:35	Msamaha wa Majeraha 18:21-22 Mfano wa mdeni Asiyesamehe 18:23-35

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka “[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)”)**

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembele katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Mukttadha huu hauelekezwi kwa watoto bali waamini wanya watu wazima hotuba hii ikitumia watoto kwa ajili ya kujenga hoja.
- B. Mukttadha huu haufanani wala kuhusiana na kuvuna waliopotea bali tabia za waamini.
- C. Nidhamu ya kanisa ya mistari ya 15-19 inahusiana na jambo la upendo wetu ju yetu sisi kwa sisi katika Kristo, kama vile Rum. 14:1-15:13; 1 Wakorintho 8; 10:23-33.
- D. Mfano wa mistari ya 21-35 inafanana na namna waamini wanavyowatendea wanyonge au wakristo wanya ikijikita katika namna Mungu anavyowatendea waamini katika Kristo. Msamaha unafanyika katika kusamehe! Si msingi bali matokeo ya tendo la Mungu katika maisha yetu!

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 18: 1-6

<sup>1</sup> Saa ile wanafunzi wakamwendea Yesu wakisema, <sup>2</sup> Ni nani basi aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni? Akaita mtoto mmoja, akamweka katikati yao, <sup>3</sup> akasema, Amin, nawaambia, Msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni. <sup>4</sup> Basi, ye yote ajinyenyekeshaye mwenyewe kama mtoto huyu, huyu ndiye aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni. <sup>5</sup> Na ye yote atakayempokea mtoto mmoja mfano wa huyu kwa jina langu, anipokea mimi; <sup>6</sup> bali atakayemkosesha mmojawapo wa wadogo hawa waniaminio, yamfaa afungiwe shingoni jiwe kubwa la kusagia, na kutoswa katika kilindi cha bahari.

**18:1 "wanafunzi wakamwendea Yesu"** Hii inaonesha kwamba Yesu alikuwa anazungumza na waamini na sio wasioamini!

☑ **"Ni nani basi aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni?"** Swali kinaweka jukwaa kwa ajili ya yaliyofuata. Angalia Marko 9:33-34; Luka 9:46-48. Swali linaonyesha kwamba wanafunzi kwa sehemu kubwa walielewa vibaya asili ya ufalme. Pia inaonesha kwamba wanafunzi hawakumchukulia Petro kuwa mkubwa zaidi kuliko wao wote!

**18:2 "mtoto"** Marko 9:33 inaweka kwamba huyu alikuwa mtoto wa Petro.

**18:3 "hakika"** Angalia Mada Maalum katika Mt. 5:18.

☑ **"Msipoongoka"** "kuongoka" kunaashiria hali ya kuongoka ambapo toba ya ndani inaelezewa katika mabadiliko ya mtindo wa maisha (NRSV, NJB). Katika Yohana 12:40 neno hili linatumika kufasiri Isaya 6:10, ambapo linamaanisha "toba" (Kiebrania *shub*, BDB 996). Tazama hili katika Mt. 18:4 "unyenyekevu" unafananishwa "kuongoka" Watoto bila kujua huamii na kuwategemea wengine. Wako tayari kufundishika na ni watii kwa mamlaka (hapa mamlaka ya kiungu).

Hii ni kauli tendwa tegemezi ya wakati uliopita usio timilifu. Njeo ya wakati uliopita usio timilifu ilimaanisha tendo la kumaanisha wakati hali ya utegemezi ilionyesha hapa kulikuwa na kiashiria cha tukio linalotarajiwa na uchaguzi ukihusishwa. Sauti irabu tendwa ilimaanisha juhudi ya uanzilishi ya Mungu (Kama vile Yohana 6:44,65).

☑ **"hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni"** Hii ni kanushi ya NGUVU YA UPILI inayomaanisha, "haiwezekani kwa namna yoyote." Pia tazama kwamba lango la kuingia katika ufalme ni haraka! Kumwamini Yesu na ujumbe Wake ni sawasawa na kingie katika zama mpya! Ufalme ulikuwa unapatikana kwa wote waliosikia na kuitikia kwa Yesu.

**18:3,4,6 "kama mtoto huyu. . .mtoto. . . mmojawapo wa wadogo hawa"** Kauli hizi zote zinafanana kwa watu wazima wanya, wasio na hatia, walioamini hivi karibuni na sio watoto. Hata hivyo kutumaini kunakojitegemea kwa watoto ni mtazamo sahihi kwa watu wazima.

**18:34 "hamtaingia katika ufalme. . .wa mbinguni"** Katika muktadha hii inarejerea kwa (1) namna gani mtu anakuja kwa Kristo na (2) namna gani anaendelea kwa Kristo.

**18:5** Hii inafanana na msisitizo wa Mt. 10:40. Pia tazama Mt. 25:35-45; Luka 10:16; Mdo 9:4; 1 Kor. 8:12. Yesu anatambuliwa kikamilifu na Wafuasi Wake!

**18:6 "ingemfaa"** Kifo japo cha mateso ni tukio la mara moja bali hukumu ina madhara ya milele (kama vile Mt. 25:31-46). Kauli nyingine ya "ingekuwa vyema" inapatikana katika 2 Pet. 2:20-22.

☞ **"jiwe kubwa la kusagia"** Hii inarejerea jiwe kubwa la juu linalovutwa na wanyama kwa ajili ya kusagia.

☞ **"na kutoswa katika kilindi cha bahari"** Wayahudi walikuwa waoga wa maji, kama ilivyo kwa watu wengi wa jangwani. Hivyo tungo hii inahusiana na kifo kibaya cha mwili ambacho kilikuwa bora kuliko kuwasababishia waamini wapya kuingia katika dhambi (kama vile Mt. 18:8-10; Rum. 14). Angalia [MADA MAALUM: VIWANGO VYA THAWABU NA ADHABU](#) katika Mt. 5:12.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 18:7**

**7 Ole ni wa ulimwengu kwa sababu ya mambo ya kukosesha! Maana hayana budi kuja mambo ya kukosesha; lakini ole wake mtu yule aliletaye jambo la kukosesha!**

**18:7 "Ole ni wa ulimwengu. . . ole wake mtu yule"** Hii iliwekwa katika muundo wa kifasihi wa manabii wa Agano la Kale kama onyo la kifo ambalo liliwakiisha hukumu ya Mungu (kama vile Mt. 11:21; 18:7; 23:13,15,16,23,25,27,29; 24:19; 26:24; Luka 17:1-2). Kuwasababishia waamini wapya kujikwa kuna adhabu na madhara ya milele!

☞ **"mambo ya kukosesha"** Nomino hiyo hiyo (*skandalon*, kama vile Luka 17:1) ilitumika katika Mt. 16:23 kwa kauli za Petro. Inarejerea kifasihi mtego wa mnyama uliowekewa chambo (kama vile LXX of Amosi 3:5). Waamini wapya wako hatarini kuingia katika udanganyifu na mitego (Wayahudi na baadaye walimu wa kikristo wa uongo, kama vile Mt. 7:15-27; 1 Tim. 4:1-5; 2 Tim. 2:14-26; 3:1-9; 2 Petro 2).

Kitenzi kinajirudia rudia katika Injili ya Mathayo (kama vile Mt. 5:29,30; 11:6; 13:21,57; 15:12; 17:27; 18:6,8,9; 24:10; 26:31,33). Matatizo na majaribu siku zote huwa yapo!

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 18:8-9**

**<sup>8</sup> Basi mkono wako au mguu wako ukikukosesha, ukate ukautupe mbali nawe; ni afadhali kuingia katika uzima hali umepungukiwa na mkono au mguu, kuliko kuwa na mikono miwili au miguu miwili, na kutupwa katika moto wa milele. <sup>9</sup> Na jicho lako likikukosesha, ling'oe, ukalitupe mbali nawe; ni afadhali kuingia katika uzima una chongo, kuliko kuwa na macho mawili, na kutupwa katika jehanum ya moto.**

**18:8-9 "Ikiwa. . .ikiwa"** Zote hizi mbili ni sentensi za daraja la kwanza zenye masharti ambazo zinakisiwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa makusudi yake ya kifasihi. Hizi kauli za kushtua za kudhaniwa zinaweka mkazo wa dhambi binafsi na pia watenda dhambi wanaosababisha wengine kutenda pia (kama vile Mt. 18:6,7).

**18:8,9 "ukate....ukautupe"** Hizi hazikukusudiwa kuchukuliwa kama zinavyoonekana bali kuonesha madhara ya dhambi na matokeo yake (kama vile Mt. 5:29-30).

☞ **"moto wa milele"** Angalia Mada Maalum inayofuata.



## MADA MAALUM: UMILELE (*aiōnios*)

Robert B. Girdlestone, katika kitabu chake *Synonyms of the Old Testament*, ana maoni ya kushangaza juu ya neno "umilele":

"Kivumishi *aiōnios* kimetumika zaidi ya mara arobaini katika Agano Jipya. Kwa kuzungumzia uzima wa milele, ambao unachukuliwa kwa sehemu kama zawadi tuliyonayo sasa, kwa sehemu kama ahadi kwa ajili ya ubaadaye. Pia inafanya kazi kwa uwepo wa Mungu usio na ukomo katika Rum. 16.26; kwa thamani ya ondoleo la dhambi lililokuwa na ukomo la Kristo katika Ebr. 9.12; 13.20; na nyakati zilizopita katika Rum. 16.25; 2 Tim. 1.9; Tito 1.2.

Neno hili linatumika kurejerea moto wa milele, Mt. 18.8; 25.41; Yuda 1:7; adhabu ya milele, Mt. 25.46; hukumu ya milele au shutuma, Marko 3.29; Ebr. 6.2; uharibifu wa milele, 2 The. 1:9. Neno katika vifungu hivi inamaanisha hitimisho na kwa dhahiri ikiashiria kwamba wakati hukumu hizi zikitolewa, muda zaidi zwa uangalizi, mabadiliko au nafasi ya kurudisha nafasi ya mtu ya kwanza, vitakuwa vimekwisha ondoka kikamilifu na milele. Tunaelewa kidogo juu ya wakati wa baadaye, kuhusu mahusiano ya maisha ya mwanadamu na maisha mengine. Ikiwa upande mmoja, sio sawa kuongeza neno la Mungu, upande mwingine lazima tusiondoe; na ikiwa tutayumba yumba katika fundisho la adhabu ya milele kama inavyowekwa katika maandiko, lazima tukubaliane kusubiri tukishikiria injili ya upendo wa Mungu katika Kristo wakati tukitambua kwamba kuna historia isiyojulikana ambayo hatuna uwezo wa kuelewa" (kur. 318-319).

**18:9 "jehanum ya moto"** Gehenna linatoka katika maneno mawili ya Kiebrania *ge* ikimaanisha "bonde" na *henna* ikimaanisha "wana wa Hinnom" (kama vile 2 Wafalme. 23:10; 2 Kor. 28:3; 33:6; Yer. 7:31). Hili lilikuwa ni bonde nje ya Yerusalemu ambapo mungu wa moto wa Wafoenike alikuwa akiabudiwa kwa sadaka ya mtoto (tendo liliitwa *molech*). Wayahudi walilibadili kuwa shimo la kutupia taka. Angalia [MADA MAALUM: Wafu wako wapi?](#) katika Mt. 5:22. Yesu mwenyewe alitumia sehemu hii kistiari kuelezea moto. Yesu tu ndiye aliyetumia neno hili (isipokuwa mstari mmoja katika Yakobo 3:6).

Huu ni mstari wa kutisha. Hata hivyo, mtu lazima kukumbuka matumizi ya utiaji chumvi (kutia chumvi) katika mafundisho ya Yesu. Muktdadha unahusiana na wafuasi, waaminio. Bado Yesu anataka kutoa onyo hata kwa wafuasi wake wenyewe juu ya hitaji la kupenda na kuendelea katika imani (kama vile Mt. 5:22).

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 18:10-11

<sup>10</sup> Angalieni msidharau mmojawapo wadogo hawa; kwa maana nawaambia ya kwamba malaika wao mbinguni siku zote huutazama uso wa Baba yangu aliye mbinguni. <sup>11</sup> [Kwa maana Mwana wa Adamu alikuja kukiokoa kilichopotea.]

**18:10 "Angalieni msidharau mmojawapo wadogo hawa"** Sehemu hii yote (yaani, Mt. 18:9, 10-11) inaelezea ukweli ule ule.

☛ **"malaika wao"** Hii inaweza kueleweka kufundisha kwamba waaminio wote wana malaika binafsi anayefanya ulinzi (kama vile Zab. 91:11; Mdo. 12:15; Ebr. 1:14). Hii ni dhana ya kufurahisha lakini kuna ushahidi kidogo sana juu ya kujenga fundisho. Zaburi 24:7 ni ukweli ule ule ila kwa namna ya ujumuishi.

**18:11** Mstari huu haupo katika Maandiko ya Kiyunani ya kale ya  $\alpha$ , B, L, au maandiko ya Kiyunani yaliyotumiwa na Origen, Eusebius, na Jerome. Wala hayapatikani katika matoleo ya Kishamu na Kikoptiki. Inawezekana haikuwa katika sehemu ya asili ya Mathayo. Ni nyongeza kutoka Luka 19:10 kulikofanywa na wanakili wa kale. Toleo la UBS<sup>4</sup> linatoa alama ya kutojumuishwa kwake kama "B" (karibia).

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 18:12-14

<sup>12</sup> Mwaonaje? Mtu akiwa na kondoo mia, mmoja akampotea, je! Hawaachi wale tisa na tisini, akaenda

**milimani, na kumtafuta yule aliyepotea?** <sup>13</sup> Hata akipata kumwona, amin, nawaambia, amfurahia huyo zaidi, kuliko wale tisa na tisini wasiopotea. <sup>14</sup> Vivyo hivyo haipendezi mbele za Baba yenu aliye mbinguni kwamba mmoja wa wadogo hawa apotee.

**18:12-14 "kondoo mia"** Mfano huu unfanana katika muktadha na waamini ambao wamerudi nyuma na baadaye kurudi kwa Mungu. Waaminio wanatakiwa kusaidiana na kurejeshana (kama vile Gal. 6:1-3). Katika Luka 15:4-7 mfano huu unarejerea kupotea kiroho, kujihesabia haki kunakofanywa na Mafarisayo. Hii inaonesha kwamba Yesu alitumia mifano ile ile kwa namna tofauti tofauti kwa hadhira tofauti tofauti.

**18:13 "ikiwa"** Mistari yote miwili ya 12 na 13 ni sentensi za daraja la tatu lenye masharti, kunakomaanisha tendo la baadaye linalotegemea kufanyika.

☐ **"hakika"** Angalia Mada Maalum katika Mt. 5:18.

**18:14 "mapenzi ya Baba yenu aliyeko mbinguni"** Angalia Mada Maalum katika Mt. 7:21.

☐ **"kwamba mmoja wa wadogo hawa apotee"** Kuna Mada Maalum kadhaa ambazo zinafanana au kuhusiana na tungo hii.

1. Uharibifu (*appollumi*) katika Mt. 2:13
2. Ukanaji wa Imani (*aphistami*) katika Mt. 7:21
3. Ustahimilivu katika Mt. 10:22

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 18:15-18**

<sup>15</sup> Na ndugu yako akikukosa, enenda ukamwonye, wewe na yeye peke yenu; akikusikia, umempata nduguyo. <sup>16</sup> La, kama hasikii, chukua pamoja nawe tena mtu mmoja au wawili, ili kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno lithibitike. <sup>17</sup> Na asipowasikiliza wao, liambie kanisa; na asipolisikiliza kanisa pia, na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru. <sup>18</sup> Amin, nawaambieni, yo yote mtakayoyafunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni; na yo yote mtakayoyafungua duniani yatakuwa yamefunguliwa mbinguni.

**18:15-17 "enenda ukamwonye, wewe na yeye peke yenu"** Sentensi hii ya daraja la tatu yenye masharti inafuatiwa na kauli shurutishi mbili.

1. Nenda, kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo
2. Kamuonye, kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu (hapa tu katika Mathayo, japo tazama matumizi yake katika Yohana 3:20; 8:46; 16:8; na Paulo katika Efe. 5:11; 1 Tim. 5:20)  
Hekima hii itendayo kazi juu ya kushughulikia dhambi katika kusanyiko. Inahusiana na kipindi cha baadaye katika historia ya kanisa. Tazama hatua.

1. Mwendee uliyemkosee kwa faragha (Mt. 18:15)
2. chukua mashahidi wawii mwendee tena
3. leta jambo hilo mbele ya kusanyiko
4. mkatae katika kufanya nae ushirika

Miongozo hii haikukusudiwa kwa uongozi tu bali kwa waaminio wote. Sisi tu walenzi wa ndugu zetu (kama vile Luka 17:3; Gal. 6:1-2). Lengo la nidhamu ya kanisa lazima siku zote iwe kukomboa na sio kutoa adhabu. Hata hivyo sifa ya mwili na amani ya mwili pia na pia afya (ya kiroho na kimwili) ya watakatifu watendao dhambi lazima ishughulikiwe.

**18:15 "ikiwa nduguyo atatenda dhambi"** Aya hii inashughulikia nidhamu ya kanisa katika ufahamu wa mistari ya 1-14. Huu ni mfuatano wa sentensi ya daraja la tatu lenye masharti, 15 (mara mbili), 16, 17 (mara mbili). Hii inarejerea juu ya matendo yanayowezekana kutendeka kwa baadaye.

☑️"**dhambi**" Kuna utofautiano wa andiko la Kiyunani hapa. Maagano Mapya yaliyomalizika ya Kiyunani, **κ** na **B**, hayana "kinyume nanyi" baada ya "dhambi." Inatokea katika mandiko ya **D, L, na W**, pia katika Fasiri za Vulgate na Wa-armeni. Toleo la UBS<sup>4</sup> linajumuisha katika mabano yake na kutoa ujumuishi kwa alama ya "**C**".

☑️"**umempata nduguyo**" Tungo hii ina ufanano na Yakobo 5:15,19-20.

**18:16 "ili kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu"** Hii ni nukuu kutoka Kumb. 19:15. Agano la Kale lilihitaji angalau mashahidi wawili kuthibitisha jambo katika mahakama (kama vile Hes. 35:30; Kumb. 17:6).

**18:17 "kanisa"** Kwa ajili ya majadiliano ya asili ya *eklesia* angalia dokezo katika Mt. 16:18. Hii inaonekana kama rejea ya kipindi cha baadaye wakati makundi ya waaminio wanatakiwa kuwatia nidhamu wenzao. Kauli kadhaa za Yesu hazishabihiani na kipindi hiki cha mwanzoni mwa huduma yake lakini ni unabii wa uhitaji wa kanisa wa baadaye. Mathayo akiishi katika kipindi hiki cha baadaye angekumbushwa (kwa Roho) ya kauli za mwanzoni za Yesu, ambazo baada tu ya Pentekoste ndio alianza kuelewa.

Neno "kanisa" linatokea tu katika Injili, mara mbili katika Mathayo. Neno linatokea mara kwa mara katika Mdo, ambalo linaonyesha kwamba Luka alikuwa anatambua mabadiliko baada ya Pentekoste.

☑️"**na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru**" Mathayo kiliandikwa kwa ajili ya Wayahudi. Mataifa walichukuliwa kama watu wasio safi na kutozaji wa ushuru ilikuwa ni kazi iliyokuwa ikidharauliwa na Wayahudi (kama vile Mt. 5:46; 9:10-11; 11:19). Tungo hii pamoja na mifano yake miwili ya maelezo ingeweza kuchukuliwa vibaya na Mataifa, hivyo haipo katika Injili zingine.

**18:18 "Hakika"** Angalia Mada Maalum katika Mt. 5:18.

☑️"**Nawaambieni**" "Ninyi" iko katika wingi. Yesu alikuwa anawahutubia wote Kumi na Mbili na wala sio Petro pekee kama katika Mt. 16:19.

☑️"**mtakayoyafunga. . mtakayoyafungua**" Maneno haya yanaweza kuchukuliwa kama "kukataza" na "kuruhusu." Yote yalikuwa ni maneno ya kiyahudi kwa maamuzi ya kisheria juu ya namna gani sheria inatakiwa ifanye kazi kwa hali zinazokuwepo. Angalia mjadala katika Mt. 16:19. Katika Yohana 20:23 maneno haya pia yanarejerea juu ya msamaha wa dhambi kama inavyokuwa hapa!

☑️"**yatakuwa yamefungwa mbinguni. . . yatakuwa yamefunguliwa mbinguni**"Kauli hizi tendwa endelevu zenye mafumbo za wakati timilifu zilikuwa zinazunguka ili kusema kwamba kitu fulani tayari kimeshakuwa. Kifungu hiki cha habari hakielezei juhudi za mwanadamu katika mambo ya kiroho bali mapenzi ya Mungu kutimimilizwa duniani kwa uongozi wa Roho kwa watu (kama vile Mt. 16:19-20; Yohana 20:23). Nidhamu ya kanisa lazima iwe ya ukombozi (kama vile Gal. 6:1-10), ikifuata namna ya Mungu ya kushughulikia waaminio.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 18:19-20**

<sup>19</sup> Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lo lote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni. <sup>20</sup> Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao.

**18:19 "wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lo lote watakaloliomba"** Hii ni sentensi ya daraja la tatu lenye masharti ambayo inamaanisha tendo la baadaye lenye uwezekano wa kutokea. Mukstadha unahusiana na ahadi hii kwa nidhamu ya kanisa na namna tunavyowatendea waaminio wengine.

**18:19** Mstari huu lazima uchukuliwe katika mukstadha wa mapenzi ya Mungu kufunuliwa kwa Roho kutoka Mt. 18:18. Waaminio wanahaidiwa tu majibu chini ya mazingira fulani ya kiroho. Jambo baya zaidi linaloweza kutokea kwa waaminio wengi wa kisasa ni kwamba Mungu anajibu maombi yao ya kibinafsi ya kutaka vitu.

Biblia inawasilisha mtazamo wake kinzani juu ya maombi. Baadhi ya vifungu vinazungumza juu ya uwanja wake mpana usiokoma na ahadi ya majibu (kama vile Mt. 18:19; Yohana 14:13-14; 15:7,16; 16:23). Vifungu vingine vnazungumzia maombi kukwamishwa na

1. kug'ag'ania kwetu (kama vile Mt. 7:7-8; Luka 11:5-13; 18:1-8)
2. mtazamo wetu (kama vile Mt. 21:22; Marko 11:23-24; Luka 18:9-14; Yakobo 1:6-7; 4:1-10)
3. mapenzi ya Mungu (kama vile 1 Yohana 3:22; 5:14-15)

Kithiolojia waaminio wanakubaliana kwamba

1. Mungu anaguswa na maombi ya Watoto Wake
2. zawadi iliyo kuu zaidi sio jibu bali ushiriki pamoja na Baba
3. maombi yote hujibiwa
4. maombi yanabadilisha maisha yetu na maisha ya wale tunaowaombea

Hata hivyo wakati yote yanasemwa na kufanyika, bado kuna "siri" katika maombi. Inawekwa na kujumlishwa kwa kweli kwamba Mungu amechagua katika utawala Wake kujiwekea mipaka kwenye maombi ya watoto Wake. Hata sasa hatuna kwa sababu hatuombi au tunaomba vibaya.

## **MADA MAALUM: MAOMBI, YASIYO NA UKOMO INGAWA YANA UKOMO**

### **A. Madokezo ya injili**

1. Waamini wanatiwa moyo kustahimili kwenye maombi na Mungu atafanya "mambo mazuri" (Mathayo, Mt. 7:7-11) au Roho wake" (Luka, Luka 11:5-13)
2. Katika mukstadha wa kanisa waamini wenye staha (wawili) wanatiwa moyo kuungana katika maombi (Mt. 18:19)
3. Katika Mukstadha wa hukumu ya dini ya Kiyahudi waamini wanatakiwa kuomba kwa imani pasipo na mashaka (Mt. 21:22; Marko 11:23-24)
4. Katika mukstadha wa ile mifano miwili (Luka 18:1-8, hakimu asiye haki na Luka 18:9-14, Mafarisayo na wenye dhambi) waaminio wanatiwa moyo kutenda kivingine toka kwa hakimu mtauwa na Farisayo mwenye kujihesabia haki. Mungu huwasikia wale wanyenyekevu na moyo wa kutubu (Luka 18:1-14)

### **B. Maandiko ya Yohana**

1. Katika mukstadha mwanamme aliyezaliwa kipofu ambaye Yesu alimponya, upofu wa kweli wa Mafarisayo unafunuliwa. Maombi ya Yesu (kama ya mtu yeyote) yanajibiwa kwa sababu alimfahamu Mungu na kuishi ipasavyo (Yohana 9:31).
2. Mazungumzo ya Yohana ya chumba cha juu (Yohana 13-17)
  - a. Yohana 14:12-14 – maombi ya kuaminika yanachagizwa na
    - 1) Yale yatokayo kwa mwamini
    - 2) yakiombwa katika jina la Yesu
    - 3) akitamani kuwa Baba apate kutukuzwa
    - 4) kuzitunza amri (mst. 15)
  - b. Yohana 15:7-10 – maombi ya mwamini yanachagizwa na
    - 1) kudumu katika Yesu
    - 2) Neno lake lidumu ndani yao

- 3) kutamani Baba apate kutukuzwa
- 4) kuzaa matunda mengi
- 5) kuzitunza amri (mst. 10)
- c. Yohana 15:15-17 – maombi ya mwamini yanachagizwa na
  - 1) uchaguzi wao
  - 2) uzaaji wao wa matunda
  - 3) kuomba kwa jina la Yesu
  - 4) kuitunza amri ile ya kupendana ninyi kwa ninyi
- d. Yohana 16:23-24 – maombi ya mwamini yanachagizwa na
  - 1) kuomba kwa jina la Yesu
  - 2) kutamani kuwa furaha yao ikatimie
3. Barua ya kwanza ya Yohana (1 Yohana)
  - a. 1 Yohana 3:22-24 – maombi ya mwamini yanachagizwa na
    - 1) kuzitunza amri zake (kur. 22,24)
    - 2) kuishi istahilivyo
    - 3) kuamini katika Yesu
    - 4) kupendana ninyi kwa ninyi
    - 5) kudumu katika Yeye na Yeye ndani yetu
    - 6) kuwa na karama za rohoni
  - b. 1 Yohana 5:14-16 – maombi ya mwamini yanachagizwa na
    - 1) kuwa na uhakika ndani yake Mungu
    - 2) kutokana na mapenzi yake
    - 3) waamini kuombeana wao kwa wao

### C. Yakobo

1. Yakobo 1:5-7 – waamini wanaokabiliana na majaribu mbalimbali huhitajika kuomba kwa ajili ya hekima pasipo kuwa na mashaka
2. Yakobo 4:2-3 – waamini wanapaswa kuomba wakiwa na mienendo mizuri
3. Yakobo 5:13-18 – waamini wenye kukabiliwa na matatizo ya kiafya hutwiwa moyo
  - a. kuwaomba wazee waombe
  - b. kuomba kwa imani
  - c. kuomba kuwa dhambi zao zipate kusamehewa
  - d. kuzikiri dhambi wao kwa wao na kuombeana wao kwa wao (sawa na 1 Yohana 5:16)

Jawabu la maombi yenye nguvu ni kumfanana Kristo. Hii ndiyo maana ya kuomba kwa jina la Yesu. Kitu kibaya ambacho Mungu anaweza kukifanya ni kuyajibu maombi yao ya ubinafsi! Kwa maana moja majibu yote hujibiwa. Kitu cha thamani kwenye maombi ni kuwa waamini hutumia muda wao wakiwa na Mungu, wakimwamini Mungu.

**18:20** Mara iliyotajwa ni sawasawa na mstari wa 16. Hii ingekuwa mume na mke (mazingira ya kifamilia) au wawili au waaminio zaidi (mazingira ya kuabudu au kufanyika wanafunzi). Hata hivyo inaweza kufanya kazi (yaani kufanya kazi) kwamba wakati waaminio wanakutana kuomba Yesu anakuwa hapo (yaani, 28:20)!

☛ "kwa Jina langu" Angalia Mada Maalum inayofuata.

### **MADA MAALUM: JINA LA BWANA**

Hiki kilikuwa ni kifungu cha kawaida kwenye Agano la Kale kwa ajili ya uwepo wa Mungu na nguvu za utendaji za Mungu wa Utatu katika kanisa. Ilikuwa sio kanuni ya kimiujiza, lakini ni ombi la tabia ya Mungu kama ilivyoonekana kwa Yesu.

Mara nyingi hiki kifungu kinarejerea kwa Yesu kama Bwana (kama vile Flp. 2:11)

1. Kwenye kipawa cha imani ya mtu ndani ya Yesu (kama vile Rum. 10:9-13; Mdo. 2:21,38; 8:12,16; 10:48; 19:5; 22:16; 1 Kor. 1:13,15; Yakobo 2:7)
2. kwenye upungaji pepo (kama vile Mt. 7:22; Marko 9:38; Luka 9:49; 10:17; Mdo. 19:13)
3. kwenye uponyaji (kama vile Mdo. 3:6,16; 4:10; 9:34; Yakobo 5:14)
4. kwenye tendo la huduma (kama vile Mt. 10:42; 18:5; Luka 9:48)
5. kwenye kipindi cha kulionya kanisa (kama vile Mt. 18:15-20)
6. kipindi cha kuwahubiri watu wa mataifa (kama vile Luka 24:47; Mdo. 9:15; 15:17; Rum. 1:5)
7. katika maombi (kama vile Yn. 14:13-14; 15:7,16; 16:23; 1 Kor. 1:2)
8. njia ya kurejerea Ukristo (kama vile Mdo. 26:9; 1 Kor. 1:10; 2 Tim. 2:19; Yakobo 2:7; 1 Pet. 4:14)

Chochote tukifanyacho kama wapiga mbiu, wahudumu, wasaidizi, waponyaji wenye kutoa pepo, n.k., tunatenda katika tabia yake, nguvu zake, — katika Jina Lake (yaani., Flp. 2:9-10)!

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 18:21-22**

<sup>21</sup> Kisha Petro akamwendea akamwambia, Bwana, ndugu yangu anikose mara ngapi nami nimsamehe? Hata mara saba? <sup>22</sup> Yesu akamwambia, Sikuambii hata mara saba, bali hata saba mara sabini.

**18:21**

**NASB, NKJV**

**TEV** "sabini mara saba"

**NRSV, NJB** "sabini mara saba"

Petro alikuwa najaribu kuwa mkarimu kwa kutumia mara saba (kama vile Luka 17:4)! Lijitabu la Sheria za Wayahudi la Wababeli lilikuwa na mara tatu kama ya juu zaidi (kama vile Amosi 1:3, 6; 2:6). Yesu alichukua msamaha kwa kiwango kingine cha juu zaidi kisitiari cha 7 x 70 (au yawezekana 77). Hii haimaanishi inapofika mara ya 491 mwamini hatakiwi kuendelea kusamehe bali ndugu wa agano lazima siku zote wawe tayari kusamehe ndugu mwingine wa agano (kama vile Luka 17:4) kama Mungu anavyo wasamehe (kama vile Mt. 18:35). Agano Jipya linaweka utaratibu mpya kabisa (kama vile Mt. 18:15).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 18: 23-35**

<sup>23</sup> Kwa sababu hii ufalme wa mbinguni umefanana na mfalme mmoja aliyetaka kufanya hesabu na watumwa wake. <sup>24</sup> Alipoanza kuifanya, aliletewa mtu mmoja awiwaye talanta elfu kumi. <sup>25</sup> Naye alipokosa cha kulipa, bwana wake akaamuru auzwe, yeye na mkewe na watoto wake, na vitu vyote alivyo navyo, ikalipwe ile deni. <sup>26</sup> Basi yule mtumwa akaanguka, akamsujudia akisema, Bwana, nivumilie, nami nitakulipa yote pia. <sup>27</sup> Bwana wa mtumwa yule akamhurumia, akamfungua, akamsamehe ile deni. <sup>28</sup> Mtumwa yule akatoka, akamwona mmoja wa wajoli wake, aliyemwia dinari mia akamkamata, akamshika koo, akisema Nilipe uwiwacho. <sup>29</sup> Basi mjoli wake akaanguka miguuni pake, akamsihi, akisema, Nivumilie, nami nitakulipa yote pia. <sup>30</sup> Lakini hakutaka, akaenda, akamtupa kifungoni, hata atakapoilipa ile deni. <sup>31</sup> Basi wajoli wake walipoyaona yaliyotendeka, walisikitika sana, wakaenda wakamweleza bwana wao yote yaliyotendeka. <sup>32</sup> Ndipo bwana wake akamwita, akamwambia, Ewe mtumwa mwovu, nalikusamehe wewe deni ile yote, uliponisihi; <sup>33</sup> nawe, je! Haikukupasa kumrehemu mjoli wako, kama mimi nilivyokurehemu wewe? <sup>34</sup> Bwana wake akaghadhibika, akampeleka kwa watesaji, hata atakapoilipa deni ile yote. <sup>35</sup> Ndivyo na Baba yangu wa mbinguni atakavyowatenda ninyi, msiposamehe kwa mioyo yenu kila mtu ndugu yake.

**18:23 "mfalme"** Mfano huu ni wa kipekee kwa Mathayo. Katika Kiaramu (Yesu alizungumza Kiaramu, sio Kiebrania) neno hili lingemaanisha "mgeni rasmi wa Mfalme."

**18:24 "talanta elfu kumi"** Hiki kilikuwa kiasi kikubwa sana. Talanta mia sita ilikuwa kodi kila mwaka mzima kwa Palestina Kusini. Mfano huu ni utiaji chumvi wa kimakusudi wa desturi za mashariki ya kati (utiaji chumvi). Mara kwa mara Yesu alitumia mbinu hii ya Kifasihi kuhitimisha na kusakafia Mifano Yake. Angalia Mada Maalum katika Mt. 17:24.

**18:25** Watu (na familia zao) wangeweza kuuzwa kwenda utumwani kwa mkopo (kama vile Law. 25:39; 2 Wafalme 4:1; Neh. 5:5; Isaya 50:1). Tishio la mfalme lilikuwa tishio kweli kweli!

**18:26, 29 "Bwana, nivumilie, nami nitakulipa yote pia"** Haya ni maneno yenyewe hakika ya yote Mt. 18:26 na 29. Huu ndio msingi wa mfano. Katika Mt. 18:30 hana huruma juu ya mwanadamu mwingine anayeitaka!

**18:34 "watesaji"** Katika Kiaramu hii yawezekana ilikuwa "magereza."

**18:35 "Ndivyo na Baba yangu wa mbinguni atakavyowatenda ninyi, msiposomehe kwa mioyo yenu"** Hii ni sentensi ya daraja la tatu lenye masharti ambalo linamaanisha tendo la siku za usoni. Msamaha unatakiwa upelekee katika kusamehe (kama vile Mt. 5:7; 6:14-15; 7:1-2; 10:8; Luka 6:36; Kol. 3:13; Yakobo 2:13; 5:9). Msamaha si msingi wa wokovu wetu bali ushahidi wa hakika wa kwamba tumesamehewa. Hata hivyo Yesu anaacha wazi swali kuhusu wali wanaodai kumjua Yeye, lakini wanakataa kusamehe waaminio wengine! Mifano haiwezi, haina majibu yote ya kithiolojia!

▣ **"moyo"** Angalia Mada Maalum katika Mt. 5:8.

## **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je kifungu hiki kinatoa maana ya uhusiano wa watoto na Mungu?
2. Mifano gani miwili inayotolewa kwetu katika kifungu cha habari kuonesha asili ya dhambi zetu binafsi?
3. Je mfano huu katika mistari ya 12-14 inaelezea ukweli ule ule kama katika Luka 15:4-7?
4. Nini mfano wa mstari wa 23-25 ina sema kwetu juu ya msamaha?

## MATHAYO 19

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Mafundisho Yahusuyo Talaka	Ndoa na Taraka	Ndoa na Talaka	Yesu Anafundisha Kuhusu Talaka	Swali lihusulo Talaka
19:1-2	19:1-10	19:1-2	19:1-2	19:1-2
19:3-12		19:3-9	19:3 19:4-6 19:7 19:8-9 Kujizuia	19:3-6 19:7-9
Yesu Anafundisha Kuhusu Useja		19:10-12	19:10	19:10-12
	19:11-12		19:11-12	
Watoto Wadogo Wanabarikiwa	Yesu Anawabariki Watoto Wadogo	Kuwabariki Watoto	Kuwabariki Watoto Wadogo	Yesu na Watoto
19:13-15	19:13-15	19:13-15	19:13-14 19:15	19:13-15
Kijana Mdogo Tajiri	Yesu Anamshauri Kijana Mdogo Tajiri	Kijana Mdogo Tajiri	Kijana Mdogo	Kijana Mdogo Tajiri Tajiri
19:16-22	19:16-22	19:16-22	19:16 19:17 19:17a 19:18b-19 19:20 19:21 19:22	19:16-22



Kwa Mungu Yote Yanawezekana				Hatari ya Utajiri
19:23-30	19:23-30 1	9:23-26	19:23-24	19:23-26
			19:25	
19:26				Thawabu ya Kijizuia
		19:27-30	19:27	19:27-29
			19:28-30	
				19:30

## **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka [“Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia”](#))**

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

- A. Kiukweli Mafarisayo hawa hawakuwa na dhamira kuhsiana na swali hili bali walikuwa wakijaribu kuupunguza umaarufu wa Yesu kwa kuwaogofya wafuasi wake juu ya jambo lisilo sahihi (kama vile Marko 10:2-12). Jibu la Yesu lazima lifasiriwe katika muktadha wa kimajibizano. Hiki si kifungu cha mafundisho yasiyo na upande.
- B. Mathayo 5:31-32; Marko 10:1-12; Luka 16:18 na 1 Wakorintho 7:12-14 lazima zifikiriwe tujadilipo suala la taraka. Kifungu hiki kinahusiana na misingi ya kisheria na kuoa au kuolewa tena katika maandiko ya Musa.
- C. Tunapolifasiri suala la kijamii lililo gumu kama hili, iweni makini juu ya:
  1. kushawishiwa kwa uzito kupitia tamaduni zake mwenyewe na umri
  2. kushawishiwa na namna fulani za hali zenu na uzoefu
  3. kushawishiwa na madhaanio ya awali (udhehebu)
  4. kutengeneza sheria ngumu na zenye msimamo kwa kila hali

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 19 :1-2**

<sup>1</sup> Ikawa Yesu alipomaliza maneno hayo, akatoka Galilaya akafika mipaka ya Uyahudi, ng'ambo ya Yordani. <sup>2</sup>  
**Makutano mengi wakamfuata, akawaponya huko.**

**19:1 "Ikawa Yesu alipomaliza maneno hayo"** Kifungu hiki kwa uwazi ni alama ya kiuandishi ya Matayo kuyaumba mafundisho ya Yesu (kama vile Mt. 7:28; 11:1; 13:53; 26:1).

☐ **"akatoka Galilaya akafika mipaka ya Uyahudi"** Hiki kipindi cha huduma ya Yesu mara nyingi kinaitwa huduma yake huko Perea. Hiki kina kinaizungumzia Mathayo 19-20 yote. Wayahudi wengi wasingepitia Samaria bali wangezunguka kupitia ng'ambo ya Yordani eneo la Perea, kisha kusini hadi Yerusalemu na kuzunguka Yordani huko Yeriko katika Yudea. Hii ilikuwa ni kwa sababu ya kuchukiwa na Wasamaria. Hawa waliamini kuwa hawa ni nusu Wayahudi, nusu wapagani. Haya yalikuwa matokeo ya uhamisho wa Ashuru chini ya Sargon II wa Kusini mwa Makabila Kumi mnamo 722 b.k. na makazi mapya ya wapagani katika eneo hilo.

**19:2 "Makutano mengi wakamfuata"** Huenda hawa walikuwa wana hija waliokuwa wakienda Yerusalemu, lakini pia wangekuwa watu waliokuwa wakihitaji uponyaji au wachunguzi.

☐ **"akawaponya huko"** Uponyaji wa Yesu ulikusudia kuthibitisha ujumbe wake, kusaidia kuonyesha raha ya mbinguni itakayokuwepo, na moyo wa Mungu. Hapo awali hakuja kuponya, bali kufundisha; hata hivyo, kwa vyo vyote aliwaona watu wakiteseka kwa sababu ya matokeo ya dhambi, Alitenda; na bado anatenda!

## **MADA MAALUM: JE! UPONYAJI NI MPANGO WA MUNGU KWA KILA KIZAZI?**

Inanishangaza kuona kuwa si wote walioponywa katika Agano Jipya "waliokolewa" (yaani, walimwamini Kristo na kuwa na uzima wa milele). Uponyaji wa mwili ni mbadala duni kwa ajili ya wokovu wa kiroho. Miujiza inaonekana kuwa ya msaada zaidi pale tu inapaturejeza mbele za Mungu. Wanadamu wote tunaishi katika ulimwengu ulioanguka. Mambo mabaya hutokea. Mara nyingi Mungu huchagua kutoingilia kati, lakini hili halisemi kitu chochote juu ya pendo na uhusika wake. Uwe mwangalifu pale unapotaka Mungu aingilie kati kutenda kimiujiza kwa kila hitaji unalolitaka katika kizazi hiki cha uovu. Yeye ni Mungu Mkuu na hatujui maana yake kamili kwenye hali fulani inayotolewa.

Kwa maana hiyo ningalipenda kuongeza kumbukumbu za fasiri yangu toka kwa 2 Tim. 4:20 kuhusu Paulo na uponyaji wa kimwili (angalia [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org)):

"kuna maswali mengi ambayo tungepaswa kuwauliza waandishi wa Agano Jipya. Somo moja ambalo waaminio wote wanalifikiria ni kuhusu uponyaji wa kimwili. Katika kitabu cha Matendo (kama vile 19:12; 28:7-9) Paulo anaweza kuponya, lakini hapa na katika 2 Kor. 12:7-10 na Fl. 2:25-30, anaonekana kutoweza. Kwa nini baadhi waponywe na sio wote, na kuna muda ambapo dirisha linalohusiana na mambo ya uponyaji huwa linafungwa? Hakika ninaamini kwenye nguvu ya ajabu, Baba mwenye rehema ambaye Yeye huponya kimwili vile vile kiroho, lakini ni kwa nini hii dhana ya uponyaji inaonekana kuwepo na baadaye tena haionekani? Sifikirii kuwa inahusiana na imani ya mwanadamu, kwa hakika Paulo alikuwa na imani (kama vile 2 Wakorintho 12). Nahisi kuwa uponyaji na kuiamini miujiza huthibitisha ukweli na mamlaka ya injili, ambayo bado inatenda katika maeneo ya ulimwengu ambayo mwanzoni ilitangazwa. Hata hivyo, nahisi kuwa Mungu anatumhitaji tutembe katika imani na sio kwa mtazamo. Pia, uponyaji wa kimwili mara nyingi huruhusiwa katika maisha ya watu:

1. kama adhabu ya muda mfupi kwa ajili ya dhambi
2. kama matokeo ya maisha kwenye ulimwengu ulioanguka
3. kuwasaidia waaminio kukuwa kiroho

Tatizo langu ni kuwa sikuwahi kujua ni yupi anahusika! Ombi langu kwa ajili ya mapenzi ya Mungu yaweze tendeka katika kila jambo sio kuwa na uhaba wa imani bali ni jaribio la uaminifu ili kuruhusu Mungu mwenye rehema na mwingi wa fadhila kutenda mapenzi yake katika kila maisha."

Hapa kuna hitimisho langu:

1. uponyaji ulikuwa ni dhana ya huduma ya Yesu na Mitume.
2. ulikusudia kimsingi kuthibitisha moja kwa moja ujumbe mpya kuhusu Mungu na ufalme Wake.

3. kuonyesha moyo wa Mungu kwa ajili ya watu wanaoumia.
4. Mungu hajawahi kubadilika (Mal. 3:6) na atatenda kwa upendo, katika uponyaji (karama zote za kiroho bado zinaendelea, kama vile 1 Kor. 12:9,28,30).
5. Kuna mifano mingi ambapo uponyaji kwa wale wenye imani kubwa haukutenda kazi (kijitabu kilichonisaidia mimi katika eneo hili ni kile cha Gordon Fee, *The Disease of the Health, Wealth Gospel*).
  - a. Paulo, 2 Kor. 12:7-10
  - b. Trofimo, 2 Tim. 4:20
6. dhambi na magonjwa yalihusianishwa kwenye fikra za walimu wa dini ya Kiyahudi (kama vile Yohana. 9:2; Yakobo 5:13-18).
7. Uponyaji sio ahadi ya Agano Jipya. Sio sehemu ya upatanisho wa Mungu ulioelezewa katika Isa. 53:4-5 na Zab. 103:3, ambapo uponyaji ni taswira kwa ajili ya msamaha (angalia Isa. 1:5-6, ambapo magonjwa ni stiari kwa ajili ya dhambi).
8. kuna fumbo la kweli kuhusu ni kwa nini baadhi wanapona na baadhi hawaponi.
9. yawezekana kuwa ingawa uponyaji upo katika kila kizazi, kulikuwepo na ongezeko lenye umuhimu kipindi cha maisha ya Yesu; hili ongezeko litatokea tena kabla ya kurudi kwake.

Mwandishi wa kisasa ambaye amenisaidia mimi kutambua kuwa tamaduni zangu za kimadhehebu zimeshusha utendaji wa Roho, hasa ile ya kimiujiza, iliyoandikwa na Gordon Fee. Ana vitabu mbalimbali, lakini viwili nivipendavyo ni vile vinavyoshughulika na eneo hili ni

1. *Paul, the Spirit, and the People of God*
2. *God's Empowering Presence: The Holy Spirit and the Letters of Paul*

Kama yalivyo masuala mengi ya Kibiblia, kuna mawili makubwa. Lazima tutembe katika nuru tulio nayo katika upendo, lakini siku zote tukijifungua katika nuru zaidi toka kwenye Biblia na Roho wa Mungu.

#### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 19:3-9

<sup>3</sup> Basi Mafarisayo wakamwendea, wakamjaribu, wakimwambia, Je! Ni halali mtu kumwacha mkewe kwa kila sababu? <sup>4</sup> Akajibu, akawaambia, Hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke, <sup>5</sup> akasema, Kwa sababu hiyo, mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe; na hao wawili watakuwa mwili mmoja? <sup>6</sup> Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe. <sup>7</sup> Wakamwambia, Jinsi gani basi Musa aliamuru kumpa hati ya talaka, na kumwacha? <sup>8</sup> Akawaambia, Musa, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu, aliwapa ruhusa kuwaacha wake zenu; lakini tangu mwanzo haikuwa hivi. <sup>9</sup> Nami nawaambia ninyi, Kila mtu atakayemwacha mkewe, isipokuwa ni kwa sababu ya uasherati, akaoa mwingine, azini; naye amwoaye yule aliyeachwa azini.

19:3 Kwa mjadala kamili wa chimbuko na thiolojia ya Mafarisayo tazama Mada Maalum katika Mt. 22:15.

☐ "**wakamjaribu**" Hili neno (*peirazō*) lina maana kidokezo kanushi cha neno "kujaribu kwa lengo la kuharibu." Tazama Mada Maalum katika Mt. 4:1. Huu haukuwa mjadala wa kithiolojia katika mazingira yasiyo na upande wote!

NASB "kwa kila sababu"  
 NKJV "kwa sababu yo yote"  
 NRSV "kwa kisababishi cho chote"  
 TEV "kwa sababu yo yote aionayo"  
 NJB "kwa chanzo cho chote kile"

Katika Marko 10:2 swali linahusu talaka, lakini hapa swali linahusu misingi ya talaka. Shule ya kiutamaduni ya Sheria za Kiyahudi iitwayo Shammai ilichagua kifungu "neni ovu" toka Kut. 24:1, ambapo shule ya Kimabadiliko ya sheria za Kiyahudi iitwayo Hillel ilikichagua kifungu "asipopata kibali machoni mwake." Hivyo shule ya kwanza

inasema kuwa misingi ya vijana au baadhi yao inazuia tendo la kujamiana; ya pili inazungumzia kisababishi cho chote. Baadaye, Rabbi Akiba, wa shule ya Hillel, naye anasema kwamba mtu angemtarakisha mkewe endapo angekutana na mwingine aliye mzuri zaidi!

Mafarisayo wanamuuliza Yesu swali, si kwa ajili ya kupata ufahamu bali kuwaumiza

1. pamoja na baadhi ya wafuasi wake (makundi madogomadogo yaliyokuwa ndani ya Dini ya Kiyahudi)
2. pamoja na Herode Antipa (Yohana Mbatizaji aliyenshutumu Herode kumtarakisha mkewe na kuoa mke mwingine)

**19:4 "Hamkusoma"** Yesu alitarajia kuwa watu hawa wa Kiyahudi walikuwa wamekwisha kukisoma kitabu cha Mungu (kama vile Mt. 12:3; 19:4; 21:16; 22:31). Maarifa yatokanayo na Maandiko ulikuwa msingi wa kuishi maisha ya Kiungu. Yesu alitarajia waamini wapya "kuwa wamekwisha yasoma" haya pia! Desturi za Kiyahudi ziliyapotosha na kuyabatilisha Maandiko, kama zifanyikavyo desturi za sasa kimadhehebu, mara nyingi zikinukuu andiko moja au kwenda nje ya andiko na kuvikanusha vifungu vyote vyenye ufanano!

☐ **"aliyewaumba"** Hii kauli endelevu (*ktisas*) iko katika machapisho ya herufi kubwa MS B, lakini kitenzi "kufanywa" (*poiēsas*) kiko katika MSS,  $\kappa^c$ , D, L, W, Z. Hiki kinalifuatisha Agano la Kale la Kiebrania la Mwa. 1:27. Hata hivyo, toleo la UBS<sup>4</sup> linafikiri kuwa uchaguzi wa kwanza ndiyo halisi (yaani., daraja "B", maana yake " kwa kiasi fulani ni sahihi").

☐ **"mwanzo"** Nukuu hii inatoka Mwa. 1:27 na 5:2 ya kuumbaji wa Mungu wa mwanamume na mwanamke. Ndoa ni wazo la Mungu la kuwa katika uaminifu (kama vile Mwa. 2:23-24) na kudumu (kama vile Mt. 19:6).

**19:5 "Kwa sababu hiyo. . babaye na mamaye"** Hii ni nukuu toka Mwa. 2:24. Tambua kuwa wazazi wote wanatajwa, lakini pia matengano ya mara kwa mara ya yaliyopelekea familia yenye kuhitaji ndoa. Katika ulimwengu wa kale familia zilikuwa zikiishi na vizazi vingi katika nyumba moja. Kapaumbele na uhuru wa lika kizazi unakubalika.

☐ **"hao wawili watakuwa mwili mmoja"** Muundo wa umoja lakini wenye maana ya wingi pia unapatikana katika Mwa. 2:24, Kumb. 6:4, na Eze. 27:17. Upendo huunganisha watu!

**19:6 "aliowaunganisha Mungu"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliopita usio timilifu, yenye kueleza tendo lililokamilika. Kwa kuanza na neno "alio," asi "walio," msingi wa ndoa ulisistizwa. Hili neno "aliowaunganisha Mungu" lilimaanisha "kufungamanishwa pamoja."

**19:7 "Musa aliamuru kumpa hati ya talaka, na kumwacha"** Kifungu hiki kinatoka Kumb. 24:1-4. Yesu anasema kwamba Musa alifanya vile, si kwa sababu Mungu alitaka iwe hivyo, bali ni kwa sababu ya ugumu wa mioyo ya watu. Musa aliwahirumia wanawake waliokuwa wakikabiliwa na magumu kijamii. Hati hii (1) ilihitaji siku kadhaa, (2) ilihitaji msaada wa kisheria, (3) ingehitaji kurudisha makari, na (4) ilidokeza ndoa.

Kinachonisumbua kuhusu Yesu kuyainga maneno ya Musa ni kwa namna gani nitaitambua tofauti iliyowekwa katika Maandiko ya Agano la Kale ambayo Mungu ameyapinga. Kamwe sikuweza kulijua hili hadi pale Yesu alipolieleza kwa uwazi mahali hapa. Maisha yangu yote nimekuwa nikiyaheshimu Maandiko, nikiyatumia kuyali nda maisha yangu na matendo yangu, lakini Yesu anasema kuwa sehenu ya hili si mapenzi ya Mungu!! Hili lilinipa utulivu na kunilazimisha kujikita sana katika Agano la Jipya na si Agano la Kale. Agano la Kale lazima lifanyiwe japo limetolewa fasiri zake toka kwa Yesu na Mitume wake walio vuviwa! Yesu ni Bwana wa Maandiko (kama vile Mt. 5:17-48)!

**19:9**

**NASB** "kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu"

**NKJV** "kwa sababu ya kuzikiuka taratibu ya ndoa"

**NRSV** "kwa sababu ya kutokuwa safi"

**TEV** "wengine kuliko kukosa uaminifu"

**JB** "Sizungumzii juu ya uzinzi"  
**NJB** "Sizungumzii juu ya ndoa zisizo halali"

Neno la Kiyunani ni *porneia*, lenye kutokana na Kiingereza kama "maandishi aua picha zenye kuansha hisia za kingono." Hili lingerejelea uzinzi (tendo la kujamiiana kabla ya ndoa), uasherati (tendo la kujamiiana nje ya ndoa), au matendo ya kujamiiana pasipo halali kama kujamiiana kinyume na maumbile na ngono za jinsia moja (tendo la kujamiiana lililozuiwa).

☐ **"kuwaacha wake zenu"** Kwa kipindi hicho ni wanaume wa Kiyahudi pekee waliokuwa na haki ya kutoa talaka. Katika Marko na Luka, waliokuwa wakiwaandikia Wagalilaya, wanawake pia wanapewa nasaha (kama vile Marko 10:12).

☐ **"azinzi"** Hii ni kauli tendwa (yenye ushahidi) elekezi ya wakati uliopo (kama vile Marko 10:11-12). Kuna baadhi ya tofauti za kimaandishi katika mstari huu huenda zinasababishwa na maandishi kuirejelea Mt. 5:32. Nyakati za kitenzi zinazotokana na 5:32 zinatoa mwangaza kuhusiana na kifungu hiki. Katika Mt.5:32 tafsiri inatakiwa kuwa "kumsababisha kuwa kahaba." Hii kauli tendwa pia inapatikana katika Mt. 19:9 katika machapisho B na C\*. Huenda kifungu hiki kilirejelea matatizo ya kijamii yaliyowakumba wanawake yaliyowekwa kwa mwanmke aliyetarakishwa kwa utamaduni wake wa Kiyahudi, uliomweleza kama kahaba kwa sababu kwamba ameachwa.

Katika hatua hii mawazo ya F. F. Bruce kuhusiana na andiko katika kitabu chake *Answers to Questions*, uk. 55, ni sawana matumizi ya andiko hili la sasa:

"Hakuwa anawapa wanafunzi wake nafasi ya kuanzisha sheria mpya iliyohusu misingi ya kutawala kwake, kama baadhi yao walivyotaribu kufanya. Kilichozungumziwa kuhusiana na sheria ya Sabato kingeweza kusemekana kama sheria ya ndoa: ilifanywa kwa ajili ya wandamu, na si kinyume na hivyo."

Tazama mafundisho ya Dr. Utley mtandaoni yaliyo katika mfumo wa sauti kuhusiana na suala la "talaka" katika [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org) katika kipengele cha "Difficult and Controversial Texts"

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 19:10-12**

<sup>10</sup> Wanafunzi wake wakamwambia, Mambo ya mtu na mkewe yakiwa hivyo, haifai kuo. <sup>11</sup> Lakini yeye akawaambia, Si wote wawezao kulipokea neno hili, ila wale waliojaliwa. <sup>12</sup> Maana wako matowashi waliojaliwa hali hiyo toka matumboni mwa mama zao; tena wako matowashi waliofanywa na watu kuwa matowashi; tena wako matowashi waliojifanya kuwa matowashi kwa ajili ya ufalme wa mbinguni. Awezaye kulipokea neno hili, na alipokee.

**19:10 "Wanafunzi wake wakamwambi. . . haifai kuo"** Usemi wa Yesu uliwatisha. Hawa walikuwa na matazamo wa utamaduni wao uliokuwa umezikamata akili zao. Hivyo ndivyo tulivyo! Ndoa ni mapango wa Mungu kwa wanadamu wote (hii ni sentensi amrishi daraja la kwanza). Hii ni baraka kubwa lakini pia jukumu kubwa. Katika siku za kutoa taraka za mara kwa mara ushahidi wa nguvu, ndoa ya ki-Mungu ina nguvu sana kwa ulimwengu uliopotea.

**19:10-11** Ndoa ni kanuni (kama vile Mwa. 1:28; 9:17), lakini useja ni uchaguzi wa ki- Ungu (kama vile 1 Kor. 7:7,17). Shauku ya kuomba kwa mwanini itamwongoza katika eneo hili. Ikiwa mtu atachagua kuishi pekee yake, itakuwa kwa ajili ya huduma ya Mungu (kama vile 1 Kor. 7:32).

Wayahudi wa nyakati zile za Yesu waliyapinga maisha ya kuishi pekee kama uchaguzi wa ki-Ungu. Yesu anatia changamoto juu ya maadili ya utamaduni wake katika maeneo kadhaa.

1. mamlaka ya mwanamume kwa ujumla
2. wenza lazima waisha pamoja na kukabiliana na matatizo yao
3. maisha ya upekee ni uchaguzi wa Kiungu

**19:12** Yesu anajadili aina mbalimbli za kuishi pekee.

1. waliojaliwa kwa namna hiyo
  - a. wasiokamilika tangu kuzaliwa kwao

- b. tabia binafsi ya mtu
- 2. waliohasiwa kwa nguvu (matowashi, yaani., Esta 2:3; huenda Danieli na wenzake, Matendo 8:27)
- 3. uchaguzi binafsi wa maisha ya upekee kwa makusudi ya huduma (Sifikiri kama tendo hili linaeleza kuhasiwa kimwili japo viongozi wa makanisa ya kale yalijifanyiwa hivyo, yaani, Origen)

Tambua namna Mt. 19:12 alivyolijengea sura

- 1. mstari wa 11, si wote wawezao kulipokea neno hili
- 2. mstari wa 12c, wengine wanaweza kukubaliana na maisha haya

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA ZA MISTARI YA 13-15

- A. Mistari ya 13-15 inafananishwa katika Marko 10:13-31 na Luka 18:15-30.
- B. Agano Jipya halijadili juu ya uhusiano wa watoto wa kiroho pamoja na Mungu.
- C. Mt. 18 haijadili hadhi ya kiroho ya watoto bali inawatumia kama mfano wa waamini wapya.

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 19:13-15

<sup>13</sup> Ndipo akaletewa watoto wadogo ili aweke mikono yake juu yao na kuwaombea; wanafunzi wake wakawakemea. <sup>14</sup> Lakini Yesu akasema, Waacheni watoto wadogo waje kwangu; wala msiwazuie; kwa maana walio mfano wa hao, ufalme wa mbinguni ni wao. <sup>15</sup> Akaweka mikono yake juu yao, akatoka huko.

**19:13 "watoto"** Yesu alikuwa rafiki wa wale waliotengwa kijamii, wenye kuchukiwa, na/au walioonekana kutokuwa na manufaa. Alikuwa rafiki wa watu wa kawaida, watumwa, maskini, wanawake, na watoto.

☐ **"ili aweke mikono yake juu yao na kuwaombea"** Hizi zilikuwa Baraka za mila za walimuwa sheria kwa watoto. Hapakuwa na lo lote la kufanya kuhusu wokovu. Wazazi wa Kiyahudi waliwaona watoto wao kama waliokwisha kuwa mojawapo wa kusanyiko la Israeli kwa kuzaliwa.

**19:14 "Waacheni watoto wadogo"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu. Yesu alikuwa akilazimisha shauku yake kuwa ndani ya wote.

☐ **"waje kwangu wala msiwazuie"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo yenye Kiambata hasi. Utunzi huu wa kisarufi unadokeza kustisha tendo ambalo tayari liko katika mchakato.

☐ **"ufalme wa mbinguni ni wao"** Kifungu hiki hakirejelei watoto tu, bali wale (1) wenye sifa kama watoto au (2) wale wanaojishusha au waipokeao nafasi ambao hao wataingia katika ufalme wa Mungu (kama vile Mt. 18:2-4). Huu si mstari uhusuo wokovu wa watoto. Kitabu cha Agano Jipya kinaandikwa kwa ajili ya vijana!

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 19: 16-22

<sup>16</sup> Na tazama, mtu mmoja akamwendea akamwambia, Mwalimu, nitende jambo gani jema, ili nipate uzima wa milele? <sup>17</sup> Akamwambia Kwani kuniuliza habari ya wema? Aliye mwema ni mmoja. Lakini ukitaka kuingia katika uzima, zishike amri. <sup>18</sup> Akamwambia, Zipi? Yesu akasema, Ni hizi, Usiue, Usizini, Usiibe, Usishuhudie uongo, <sup>19</sup> Waheshimu baba yako na mama yako, na, Mpende jirani yako kama nafsi yako. <sup>20</sup> Yule kijana akamwambia, Haya yote nimeyashika; nimepungukiwa na nini tena? <sup>21</sup> Yesu akamwambia, Ukitaka kuwa mkamilifu, enenda ukauze ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuata. <sup>22</sup> Yule kijana alipolisikia neno lile, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi.

**19:16 "mtu mmoja akamwendea"** Kutokana na Mt. 19:20 tunajua kwamba huyu alikuwa kijana, kutokana na Mt. 19:22 tunajifunza kwamba huyu alikuwa tajiri, na kutokana na Luka 18:18 tunajifunza kwamba huyu alikuwa kiongozi (kama vile Marko 10:17-22).

☐ **"Mwalimu"** Ufanano ulio katika Marko 10:17 na Luka 18:18 una kifungu "Mwalimu mwema." Machapisho bora ya herufi kubwa MSS (yaani., κ, Β, D, L) hapa yanakiondoa hiki (Toleo la UBS<sup>4</sup> linakipa kifungu hiki daraja "A," maana yake "hakuna mashaka").

☐ **"nitende jambo gani jema, ili nipate uzima wa milele?"** Huyu mtu wa Kiyahudi alikuwa na dhana ya kwaida ihusuyo wokovu iliyoaminiwa na Wayahudi wa siku zake zile, ambayo ilikuwa kazi ya haki iliyojikita katika utamaduni wa mtu kuihusu Torati ya Musa na Desturi za Mapokeo (kama vile Luka 10:25; Rum. 9:30-33). Huyu aliuona uzima wa milele kama matokeo ya tendo la kidini.

☐ **"uzima wa milele"** Hii dhana ya Agano la Kale ihusuyo uzima (zoē) ni ya enzi ijayo (kama vile Dan. 12:2). Neno hili linaeleza yote usawa wa maisha mapya na kipindi chake. Katika muktadha huu mmoja wenye maelezo kadhaa tofauti tofauti unatumika kufafanua uhusiano wa mtu pamoja na Mungu.

1. niupate uzima wa milele, Mt. 19:16
2. kuingia katika uzima wa milele, Mt. 19:17
3. kuwa mkanilifu, Mt. 19:21
4. kuingia katika ufalme wa Mungu, Mt. 19:23,24
5. kuokolewa, Mt. 19:25
6. ili niurithi uzima wa milele, Mt. 19:29

**19:17 "Aliye mwema ni mmoja"** Yesu hakunena kuwa hakuwa mwema, bali alikuwa akimwonyesha mtu huyu kiwango cha wema kilichohitajika ili kuwa na haki ya kuwa pamoja na Mungu. Mstari huu si lazima utumike kama wenye kuyachunguza maandiko kwa kuupinga Uungu wa Yesu au yeye kutokuwa na dhambi.

☐ **"ukitaka"** Hii ni sentensi amrishi daraja la kwanza yenye kudhaaiwa kuwa ya kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au makusudi yake ya kiuandishi. Hakuna jambo lo lote la kudokeza katika muktadha huu kwamba mtu huyu alikuwa akijaribu kumtega, akimjaribu au kumnasa Yesu.

☐ **"zishike amri"** Hii ni kauli shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu (Toleo la Kiyunani la Andiko la Nestle lina kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo). Kwa namna iliyo dhahiri kifungu hiki kilirejelea Amri Kumi za Kutoka 20 na Kumbukumbula Torati 5. Hiki kilikuwa kiini cha Sheria za Kiyahudi.

**19:18-19** Hii ni sehemu ya orodha ya mbili ya kumi ya Amri Kumi yenye kushughulika na uhusiano binafsi wa mtu na ndugu yake wa agano. Orodha hii ni tofauti na andiko la Kiebrania Kimasoretiki na Agano la Kale la Kiebrania. Tazama Mada Maalum katika Mt. 5:21, 5:27, 15:4, na Mada Maalum ifuatayo.

## **MADA MAALUM: TAMBUZI ZA KUTOKA 20:12-17 (AMRI KUMI)**

### **KUTOKA 20:13, MAUAJI (BDB 953, KB 1283)**

#### **I. MUKTADHA**

- A. Inahitajika kukumbukwa kwamba hata amri zinazooonekana kuwa na asili ya kijamii ni za kidini hasa. Ukuu wa Mungu juu ya uumbaji na ukombozi umefichwa ndani ya amri hizi. Amri ya usiue i, katika tazamio sahihi, neno kuhusu sura ya Mungu katika kila mwanadamu na kujali kwa Mungu na uhusika kwa ajili ya maisha ya mwanadamu.
- B. Inahitajika kukumbukwa kwamba kila amri inaikisi yajamii imani. Hili zaidi linazungumzia juu ya kuuondoa uhai wa mtu katika hali ya jinai la la msingi na kiuhalisia linaweka msukumo wa maisha ya jamii iaminio. Vidokezo vyake ni vipana kama ulivyo ubinadamu!

## II. USOMAJI WA NENO WA MANENO MUHIMU

### A. "Mauaji"

1. Hili ni neno adimu (*rasah*, BDB 953, KB 1283) lenye kumaanisha kuuondoa uhai, lililotumika mara 46 atika Agano Jipya. Kuna maneno mengine ya Kiebrania yanayokinana yaliyotumika mara mara mia moja.
  2. Hili neno (*rasah*) linaonekana kuwa na maana halisi iliyowekwa mipaka na yenye kunuliwa.
    - a. Kiuhalisia hili linahusiana na kuondoa uhai wa mwenzwa wa agano katika sheria, kwa njia iliyokusudiwa, mara nyingi inahusiana na "mkombozi wa udugu wa damu" au "*go'el*." Matumizi haya yalilusisha mauaji ya kukusudia lakini katika maana ya Tkulipa kisasi kisheria (kama vile Hes. 35:30-34; Law. 24:13-23). Katika ukweli LexTalionis, ya "jicho kwa jicho," (kama vile Mwa. 9:5-6) ilikuwa njia ya kuzuia kisasi. Baadaye, miji ya wakimbizi (Kumb. 4:41; Yosh. 20:3) ilihimariwa ili kwamba wenza wa agano waliouawa kwa bahati mbaya au walimwua mwanajamii kwa hamaki waweze kuiepuka ghadhabu ya mhanga wa familia.
      - b. Baadaye hili neno lilikuja kurejelea juu ya shauku au mtazamo ulio nyuma ya kuuondoa uhai. Hii dhana ya "kudhamiria" inakuwa kuu zaidi! (kama vile Kut. 21:12-14; Hes. 35:11,22; Kumb. 28:24).
      - c. Tofauti hii inakuwa ya muhimu sana katika amri hii. Katika muktadha hii inaonekana kuwarejelea wengine tu walio ndani ya jamii ya agano. Hii inaonekana kuhusiana na mkombozi wa kidugu, wa kisasi cha damu. Hata hivyo, hili neno linatumika katika vifungu vinavyofuatia vyenye kuziakisi Amri Kumi za Mungu, Hosea 4:2 na Yereemia 7:9, Kumrejerea muuaji. Neno hili linahusiana na sheria tu lakini kwa kuielekea shauku. Hii inapanuka kuanzia kwa jirani hadi kwa rafiki.
  3. Neno hili kwa namna fulani linahusiana na mambo yetu ya sasa yahusuyo maadili ya adhabu za kifedha au vita. Wayahudi walikuwa na tatizo la utekelezaji wa kijamii au vita takatifu (au, wa ajili hiyo, vita isiyo takatifu).
  4. Tafsiri iliyo njema ya utamaduni wetu wa sasa ingekuwa "mauaji ya kudhamiria."

## III. TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Ya sita, ya saba, na amri ya nane zimeundwa na maneno mawili tu ya Kiebrania. Haya ni mafupi sana na yanaenda moja kwa moja katika hoja.
- B. Maisha, kama yalivyo maisha yote, yanahusiana na Mungu. Ni kwa namna gani tunavyowachukulia wengine kunaziakisi fikra zetu kuhusu Mungu.

## IV. UFANANO WA AGANO JIPYA

### A. Yesu



1. Upanuzi wa amri hii (ama vile Mt. 5:21-26) unatupa ubobezi sahihi wa mjadala wetu wa sasa kuhusu namna ya kulitumia andiko hili katika siku zetu.
  2. Kwa uwazi Yesu alizichukua Amri Kumi za Mungu kutoka katika uhalisia wa matendo na kuziweka katika uhalisia wa shauku. Tupo kama tunavyofikiri! "Awazavyo mtu moyoni mwake, ndivyo alivyo." Maisha ya fikra yanahusiana sana na nimuhimu kuliko namna ambavyo huwa tuawachukulia.
- B. Yohana
1. 1 Yohana 3:15, hii dhana ya chuki yenye kufanana inafikiriwa kama mauaji inaelezwa.
  2. Maneno ya Kiyunani yaliyotumika katika Mathayo 5:21 na kuendelea na 1 Yohana 3:15 ni tofauti lakini maana zake kimsingi ni zile zile.
  3. Kitambue kipengele yakini kilicho katika 1 Yohana 4:19-21.

#### V. KWELI ZITUMIKAZO

- A. Ingawa mauaji yasiyokusudiwa yanaweza kumwepusha mlipa kisasi kwa kukimbilia katika mji wa wakimbizi (kama vile Hesabu 35; Yoshua 20), yampasa huyu kulipa fidia ya kifungo katika mji huo hadi mauti yatakapomkuta Kuhani Mkuu. Matokeo ya tendo lake bado yanabaki pale pale!
- B. Ingawa mstari huu hausiani moja kwa moja na tukio kujiua, kama ilivyo ajali huenda tukio hili haliwezi kufikirika kamwe, bado andiko linatoa msingi wa kiroho kuhusu utakaso wa maisha ya mwanadamu na ukuu wa Mungu na makusudi maisha ya mwanadamu kuwa katika sura yake. Andiko hili linazungumza neno lenye nguvu juu ya maisha yetu katika mstari huu!
- C. Hata hivyo, andiko hili, halizungumzii juu ya neno la udanganyifu kwa swali letu la sasa la: (1) adhabu ya kifedha au (2) vita. Kwa Israeli, haya hayakuwa mambo maovu kwao. Waisraeli walihusishwa katika matendo yote haya. Bado, bado kanuni ya umuhimu wa maisha ya kufanywa katika sura ya Mungu na chini ya utawala wake ni kweli muhimu katika eneo hili.
- D. Andiko hili haliuzungumzii juu ya uhitaji wa neno linalohusu utu na utakaso wa maisha ya mwadamu! Sisi tulio katika jamii iaminiyo tu watumishi, si kwa matendo yetu tu, bali kwa jamii yetu. Zawadi ya maisha ni vyote binafsi na ushirika. Tunawajibika kimwili, kijamii, na matumizi ya kisaikolojia ya miili yetu kama tulivyo kimwili, kisiasa, na kisaikolojia kuwahusu wengine katika jamii yetu. Hasa hili ni la kweli katika utamaduni kama wetu ambapo tunaruhusiwa kuzungumzia hili na, ambapo, hubadili mfumo. Sisi ni walenzi wa ndugu zetu!

#### **KUTOKA 20:14, UZINZI (BDB 610, KB 658)**

##### I. MUKTADHA

- A. Ni dhahiri kwamba amri zinahusiana na heshima ya mtu kwa Mungu ambayo inaonekana katika heshima kwa maisha ya jirani, mke, na mali (kama vile Yer. 5:8). Hili lilithibitishwa na mpangilio tofauti wa amri hizi katika Agano la Kale la Kiebrania.
- B. Ufanano wa Kumbukumbu la Torati unaonyesha usahihi wa hii kweli ya kale kwa utamaduni wetu.
- C. Kama kuwaheshimu wazazi kulivyoonekana kuwa msingi wa jamii imara, hivyo hivyo, hii ni amri.
- D. Amri hii pia inadokeza umiliki wa Mungu na utawala wa tendo la ndoa na maisha ya familia.

## II. USOMAJI WA NENO

- A. Neno kuu katika andiko hili ni "uzinzi." Ni muhimu kwamba mtu huielewa neno hili katika mwangaza wa utamaduni wa kale wa Kiebrania.
1. Neno hili ni tofauti na muktadha unaotokana na Agano la Kale "uasherati" uasherati unahusiana na mtu kuwa na mahusiano ya kiuzinifu huku akiwa katika ndoa. Hili neno "uasherati" linadokeza sehemu zote zilizomo katika ndoa (kama vile Zab. 29:3; 31:3). Tofauti inapotea katika maneno ya Kiyunani ya Agano Jipya.
  2. Huenda hili linaeleza sababu ya msisitizo juu ya maelezo ya ndoa kwa sababu hili linahusiana na umuhimu wa haki za kurithi ambazo zilijumuishwa katika ahadi ya Mungu ya "nchi." Kila miaka 50 (Jubilee) ardhi zote zilitakiwa kurudishwa kwa makabila asilia (ama vile Law. 25:8-17).
  3. Kiutamaduni uasherati ulishutumiwa kabla ya utungaji wa sheria ya Musa (kama vile Mwa. 12:10 na kuendelea; 26:7 na kuendelea; 39:9).
  4. Uasherati ulionekana kama dhambi dhidi ya:
    - a. Jirani – Kutoka 20:14; Kumbukumbu la Torati 5:18
    - b. Ndoa – Mambo ya Walawi 18:20
    - c. Mungu – Mwanzo 20:1-13; 26:7-11
  5. Hii ilikuwa na adhabu ya kifo kwa pande zote mbili:
    - a. Mambo ya Walawi 20:10
    - b. Kumbukumbu la Torati 22:22-24
    - c. Ezekieli 16:40 (tiyari)
    - d. Angalizo kali zinazopatikana katika Mithali 1-9

## III. UHUSIANO WAKE NA AGANO JIPYA

- A. Yesu alitumia Mambo ya Walawi 19:18 kama muhtasari wa Ufunuo wa zamani (kama vile Luka 10:27). Hii inahitabisha kwamba Amri Kumi zinahusiana na kuwatendea kwetu wengine.
- B. Yesu anaweda zidisho la amri katika Mathayo 5:28. Anaweka mkazo katika kusudio badala ya kitendo. Wayahudi waliona akili kama kilalio cha nafsi. Kile mtu alichofikiria ndicho kile kilichokuwa (Mith. 23:7). Hii inafanya maneno Kumi yanayokaribia kuwa ngumu kuyatimiza—hili ndilo kusudi! (kama vile Gal. 2:15-3:29).

## IV. UTEKELEZAJI WA KISASA

- A. Ndoa inawezekana kuwa masimulizi mazuri zaidi ya kisasa ya imani ya muda mrefu ya kujizatiti katika jina la Mungu. Ni nafasi yetu nzuri zaidi kuelewa uhalisia wa dhana za agano la Kale (Mal. 2:14). Heshima yetu kwa wenza wetu katika sehemu zote ikijumuisha jinsi ya kujamiiana kibinadamu, kunatusaidia kuelewa dhumuni la mstari huu.
- B. Kusimama kwa ndoa na uaminifu, kama heshima kwa wazazi ni nguzo kuu ya nguvu ya kijamii na kuishi muda mrefu.
- C. Inahitajika kusisitizwa kwamba kujamiiana kibinadamu ni zawadi kutoka kwa Mungu (kama vile Mwa. 1:27,28; 9:1,7). Lilikuwa ni wazo lake na mapenzi kwa ubinadamu. Miongozo haikusudiwi kukandamiza uhuru wa mwanadamu au furaha bali kutoa baadhi ya miongozo ya kiungu kwa ajili ya mwanadamu aliyeanzuka. Mipaka inafunuliwa kwa ajili ya faida zetu za muda mrefu na furaha. Ingawa mwanadamu ametumia vibaya kujamiiana kama walivyofanyia karama zote za Mungu, bado ni msukumo wa nguvu ndani ya mwanadamu ambao lazima uwe chini ya uangalizi wa Mungu na mwongozo.
- D. Kujamiiana lazima kulindwa ili kwamba uungu wa nafsi ya mwanadamu (mwanamke au mwanaume) kuheshimiwe kwasababu wameumbwa kwa sura ya Mungu (Mwa. 1:27). Kuanguka kwetu kunalenga kwenye "mimi" ni wazi sana katika eneo hili.

## **KUTOKA 20:15, KUIBA (BDB 170, KB 198)**

### **I. TAARIFA ZA JUMLA**

- A. Kama ilivyo miongozo mingine katika Amri kumi, imani yetu, upendo na heshima kwa Mungu lazima kuonekane katika vipengele vya uungu na maisha yetu ya kawaida ya kila siku. Ni hasira kwa Mungu kujidai kumjua Yeye alafu kumpunja na kumnyonya mwenza wetu wa kiagano (kama vile 1 Yohana 2:7-11; 4:20-21).
- B. Amri yake imekusudiwa kusaidia kuweka ushirika wa jamii ya agano. Ubora wa ushirika huu wa kiroho utavuta ulimwengu uliochanganyikiwa kwa Mungu wetu ambalo ndilo kusudi la Maandiko.
- C. Kama ilivyo kwa amri zingine zilivyojikita katika umiliki wa Mungu wa maisha yote, ndivyo ilivyo na hili pia! Sisi tu mawakili, sio wamiliki. Msukumo wetu ulioanguka juu ya umiliki wa mali bila gharama uko nyuma ya onyo na katazo hili (kama vile Zab. 50:10-12).

### **II. USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

- A. Hii ni amri ya tatu katika nusu ya pili ya Amri Kumi ambayo inatengenezwa kwa maneno maweli tu.
- B. Kilichofanya upigaji wa marufuku hakipo. Hii mara nyingi inasaidiwa na:
  - 1. Mukstadha wa amri mbili zilizotangulia zinazohusiana na makosa makubwa.
  - 2. Uwepo wa vifungu vya habari vinavyofanana vyote ikiwa ni haraka (Kut. 21:16) vyenye kujitenga (Kumb. 24:7). Pia angalia Mwanzo 37.
- C. Hata hivyo, kifupi pia kinalindwa
  - 1. imeandikwa kwa uvuvio
  - 2. inatanua upana wa ujumuishi
  - 3. Pia kuna kifungu kinachofanana katika muktadha wa ghafla ambacho kinahusiana na kuiba—Kutoka 22:1 na kuendelea (sio kutekwa).
  - 4. Yesu kwa dhahiri ananukuu kifungu hiki katika rejea ya kuiba (kama vile Mt. 19:18).
- D. Wizi pia unashughulikiwa katika Vifungu vingine vya Sheria za Kale lakini siku zote adhabu ni mauti, kukatwa, au kurejesha mara 30.
- E. Kuna baadhi ya vifungu vya muhimu ambavyo vinaweka maana na kuelezea kweli hii:
  - 1. Mambo ya Walawi 19:1-18—"Utakuwa mtakatifu kwa kuwa Mimi Bwana Mungu wako ni Mtakatifu"
    - a. Mtindo wetu wa maisha lazima uaksi tabia za familia ya Baba yetu na Mungu wetu (kama vile Mambo ya Walawi 19:18).
    - b. Imani yetu lazima iathiri maisha yetu kwa namna zote mbili matendo yetu chanya na makatazo hasi kwa vyote misukumo sahihi iliyo na taarifa njema (kama vile Law. 19:17).
    - c. Huruma kwa waliokataliwa na wahitaji, Law. 19:9-10, 13, ni muhimu kama kuwakataa jirani zeu katika kuwahudumia, mstari wa 11.
  - 2. Amosi 8:4-7 – Mungu anachukia unyonywaji!
  - 3. Mika 6:6-8 – Mungu anataka maazimio sahihi katika matendo yetu yote. Kwanini hatuibi hilo nalo ni jambo!
  - 4. Kutoka 22:1 na kuendelea – Mara kwa mara ukweli unaokosekana katika mijadala yetu ya kisasa ya wizi ni urejeshwaji! Dhambi siku zote inagharama!

### **III. UTEKELEZAJI WA KWELI**

- A. Joy Davidman, C. S. mke wa Lewis, ameandika kitabu kizuri sana juu ya Amri Kumi. Anatafsiri "Usijaribu kupata kitu fulani bila gharama." Huu uhakika unapanua uwanja zadi ya umiliki wa mali. Pia anasema kwamba "mali huwa si dhambi wala haki iliyokataliwa bali ni mkopo, kuaminiwa na Mungu."
- B. Kuiba kama dhambi zingine za moyo ulioanguka inashughulikia na moyo mpya (kama vile Yer. 31:31-34; Ezek. 36:26; Efe. 4:28). Inafurahisha namna asili ya zamani ya "kuchukua" zamu katika sili mpya ya "ubia"!
- C. Heshima yetu kwa Mungu inaonekana kwa wazi katika heshima yetu kwa wabia wenzetu wa kiagano! Kweli hii inatabiri Amri kumi.
- D. Watu walioanguka huiba kwa namna nyingi!

### **MASWALI YA MJADALA**

- 1. Ni kwa namna gani mtu mwizi wa kisasa anaiba?
- 2. Je urejeshwaji unahusiana vipi na toba?
- 3. Mstari huu ni kwa namna gani unahusiana na mtazamo wa Kibeberu wa mali?

### **KUTOKA 20:17, TAMAA (BDB 326, KB 328)**

#### **I. UTANGULIZI**

- A. Inawezekana kuona uhusiano kati ya Amri tano za mwisho kama ifuatavyo:
  - 1. Namba 6, 7, na 8 inakataza majeraha ya ndugu wa kiagano katika matendo ya wazi.
  - 2. Namba 9 inakataza majeraha ya ndugu wa kiagano katika lugha.
  - 3. Namba 10 inakataza majeraha ya ndugu wa kiagano katika mawazo.
- B. Ni kweli kwamba tendo la tamaa linamsumbua mtu anayewakwa na tamaa, na sio tama bal jirani. Hata hivyo, inawezekana kwamba amri hii inatarajia kwamba mawazo yataendelea katika matendo.
- C. Wengi wanaona amri hii kama dhana ya kipekee inayopatikana tu katika Vifungu vya Sheria ya kale ya Israeli na ambayo haipo katika vifungu vya sheria zingine vya Mashariki ya Karibu ya Kale. Dhana hii mpya ingekuwa katazo la mawazo. Ni kweli kwamba Israel walichukulia mawazo maisha ya wazo kuwa asili ya matendo machafu (kama vile Mith. 23:7; Yak. 1:14-15). Bado mstari huu unaonekana kuhusiana na mawazo ambayo yanaababisha matendo. Vifungu kadhaa vinatumia neno "tamaa" katika muunganiko na matendo yenye matokeo (kama vile Kumb. 7:25; Yos. 7:21; Mika 2:2).
- D. Ikiwa ni kweli kwamba msisitizo unawekwa juu ya kile kinachoorodheshwa kwanza na mwisho, umuhimu wa kweli wa amri hii inaonekana. Kumwabudu Mungu bila kuacha kunaanza kwanza lakini mitazamo yetu na misukumo kuelekea vitu vya ulimwengu huu unaathiri kujitoka kwetu kwa Mungu. Msisitizo huu pacha pia unaonekana katika mahubiri ya Mlimani ya Yesu, Mt. 6:33 —"Bali utafuteni kwanza ufalme na Haki Yake: na mengine (kama vile mistari ya 19-32) mtazidishiwa."

#### **II. USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

- A. Kutoka 20:17 na Kumb. 5:21, ingawa kimsingi ni yale yale yana tofauti za muhimu:
  - 1. Mke anajumuishwa kwa dhana pana ya "nyumba" au mali ya mtu katika Kut. 20, wakati anawekwa katika kipaumbele kinachoonkana tofauti na sehemu katika Kumb. 5.
  - 2. Kifungu katika Kut. 20 kina neno la Kiebrania "tamaa" ambayo inamaanisha "kutamani kupata," lakini katika Kumb. 5 kuna neno la pili, "shauku" (BDB 16, KB 20), na pia "tamaa." "Tamaa" inazungumzia shauku ambayo imeunganishwa na kitendo cha kupata

kitu kilichokusudiwa na shauku "shauku" inaonekana kulenga katika mtazamo pekee.

3. Pia Kut. 20, imeandikwa kwa wana wa Israeli wakati wa kuzagaa kwao jangwani, hapatajwi "shamba" katika orodha za mali, wakati Kumb. 5 inataja upya amri zile zile kwa jamii iliyothabiti katika Nchi ya Ahadi.
- B. Neno "tamaa" ni neno la kati kati. Linaweza kurejerea kuwa na shauku ya vitu vyema (kama vile Zab. 19:10; 1 Kor. 12:31).
- C. Shauku mbaya ni mzizi wa anguko la shetani, Adamu na Hawa na sisi wengineo wote. Paulo anaweka msisitizo mihangaiko yake ya kushughulikia tamaa katika Warumi 7:7-8. Kutamani kimsingi ni hali ya kutoridhika na kupoteza tumaini katika kujali kwa Mungu na Utoshelevu.
- D. Vifungu vya Agano Jipya kadhaa vinahusiana na tamaa:
  1. Tatizo la mwanadamu ni kutoridhika na uchu (kama vile Luka 12:15; 1 Tim. 6:8-10).
  2. Kutamani kunajumuishwa katika orodha za Yesu za dhambi zinazotia unajisi (kama vile Marko 7:17-23; 1 Kor. 5:10; Efe. 5:5; Kol. 3:5).

### III. UTEKELEZAJI WA KWELI

- A. Majibu ya uchu wa tamaa na kutoridhika ni:
  1. Upendo – Rum. 13:8-10
  2. Kuridhika – Ebr. 13:5; Flp. 4:11-13 (na kushirikishana, Flp. 4:14)
- B. Amri inasema "acha" lakini Kristo anatupa namna ya kuacha! Katika Yeye tunaweza kuyatawala mawazo yetu kwa viwango fulani.
- C. Mungu anajua mioyo yetu na akili zetu
  1. 1 Nyak. 28:9
  2. Mith. 20:27
  3. Zab. 139:1,23
  4. Yer. 17:10
  5. Warumi 8:27
  6. Ufunuo 2:23
- D. Vitu sio viovu bali vinakuwa vinapokuwa kipaumbele. Vitu si kilele au vya kudumu milele; watu walioumbwa kwa sura ya Mungu ndio! Tamaa huathiri Jamii ya kiagano katika njia za ulaghai na uharibifu!

### IV. MAELEZO YA NYONGEZA KUTOKA KUMBU KUMBU LA TORATI 5:21:

Kumb. 5:21, "hutatamani. . . hutamtamani," kunatumika VITENZI viwili ambavyo vinafanana :

- A. "tamaa" – BDB 326, KB 325, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, ikimaanisha "shauku kuu" kwa vitu vinavyoshikika, ambavyo inaweza kuwa hasi au chanya. Katika muktadha huu inaweza kusimamiwa, shauku ya kibinafsi ambayo anakuwa nayo ndugu wa agano.
- B. "shauku" – BDB 16, KB 20, *Hiphrael* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, ikimaanisha "shauku" (kama vile Kumb. 14:26) au "tamaa" (mara kwa mara ina muktadha wa kingono 5:21) kwa ajili ya zaidi na zaidi kwa ajili yangu kwa gharama yoyote (mfano Hes. 11:4; Zab. 106:14; Mith. 13:4; 21:26; 23:3,6; 24:1).

Hii inafanana na tazamo wa ndani wa mtu na misukumo. Ni maelezo ya mwisho kwa amri zingine zote. Hii ni amri pekee ambayo inashughulika na kwanini, sio namna gani. Hii hapa haisemi tu "usifanye" bali "usifikirie hili." Yesu alifundisha kwamba si tu kwamba tusiue, bali pia tusichukie au kuonesha mtazamo ambao unaweza kupelekea katika mauaji. Yesu alichukua amri hii ya mwisho na kuinua zilizobaki kwa kiwango cha makusudio ya ndani na mtazamo kama juu ya matendo yetu ya nje (kama vile Mt. 5:17-48). Kuna tofauti zote katika ulimwengu kwa mtu ambaye haibi kwasababu haimpendezi Mungu na mtu ambaye haibi kwasababu anaogopa kukamatwa. Mmoja anatendea kazi kanuni za Kikristo na mwingine anatendea kazi matakwa yake mwenyewe.

## MASWALI YA MJADALA

1. Kuwakwa na tamaa ni nini?
2. Mtu wa nyakati hizi anatamanije?
3. Je mawazo yetu ni dhambi?
4. Kwanini mawazo yetu ni muhimu sana katika maisha ya Mkristo?
5. Kwanini Amri katika Kut. 20:17 kwa namna fulani ni tofauti na zile katika Kumbu Kumbu la Torati 5:21?

**19:18 "Usiue"** Matoleo la King James (KJV) na Jerusalem Bible (JB) yanakielezea kitenzi hiki kama "kufisha" ambapo hii ni tafsiri isiyotarajiwa ya neno la Kiebrania la "mauaji ya kukusudia yaliyo kinyume na sheria." Toleo la NKJV lina neno "usiue." Mkusanyiko wa sheria ya "jicho kwa jicho" wa Israeli kilisababisha kisasi cha damu kwa kuitafuta haki toka kwa mmoja aliyewa mmoja wa wanafamilia (kama vile Hes. 35:12; Kumb. 19:6,12; Yos. 20:1-9). Kifungu hiki kilisaidia kuzuia visasi visivyokuwa na mwisho. Tazama Mada Maalum katika Mt. 5:21.

**19:20 "Yule kijana"** Katika siku zile za Yesu mtu alifikiliwa kijana hadi alipofikisha umri wa miaka arobaini. Luka 18:18 anaongeza kwamba mtu huyu alikuwa "mkubwa," ambapo inamaanisha kwa kiongozi wa sinagogi la eneo hilo au almashauri ya mji wa eneo hilo.

☐ **"Haya yote nimeyashika"** Katika Flp. 3:6 Paulo anatengeneza maelezo hayo hayo. Huu si mkanganyiko wa Rum. 3:23, bali asili ya kisheria ya fasiri za Kiyahudi za Agano la Kale ambazo Yesu anazizungumzia katika Mt. 5:20-48. Haki ilionekana kama ukamilifu wa mkusanyiko wa kisheria. Mtu huyu alidhani kuwa alikuwa amekwisha kuyakamilisha yote yaliyohusiana na wajibu wa kidini na utamaduni wa siku zile.

☐ Toleo la NKJV linaongeza kifungu "kutoka kinywani mwangu," ambacho kinapatikana katika Marko 10:20 na machapisho ya herufi kubwa MSS C na W na matoleo mengi. Katika jamii ya Kiyahudi mtu hakuwa na wajibu wa kushikilia Sheria hadi baada ya muda wa mafunzo binafsi na kula kiapo (yaani., *Bar Mitzvah* katika umri wa miaka 13 kwa wavulana na *Bat Mitzvah* kwa wasichana katika umri wa miaka 12). Hii ni sawana dhana ya "umri wa kuwajibika" katika dini ya Kikristo.

☐ **"nimepungukiwa na nini tena"** Hii inaonyesha kutoridhika kwa moyo wa mtu huyu. Hata baada ya kuzishika sheria zote za Musa na fasiri zake, bado anaendelea kujisikia mtupu.

**19:21 "Ukitaka"** Hii ni sentensi amrishi daraja la kwanza yenye kufikiriwa kuwa ya kweli kutokana na sababu za mwandishi za indishi.

NASB "mkamilifu"

NKJV, NRSV

TEV, NJB "sahihi"

Neno hili linamaanisha "kujaa," "komavu," "kutengwa ka ukamilifu kwa ajili ya kazi fulani" (kutokana na neno *telosi*). Hili halikumaanisha kutokuwa na dhambi.

☑ **"enenda ukauze ulivyo navyo"** Kipengele hiki kinaonyesha asili muhimu ya imani ya Kristo (kama vile Luka 14:33). Ni kujitolea moja kwa moja. Kwa mtu huyu uchaguzi ulikuwa mgumu katika eneo hili la mali. Mali ya mtu huyu ilimiliki yeye! Hili halihitajiki kwa waamini wote, bali ni la muhinu, hatima ya kujitoa kwa ajili ya Yesu! Kuna mtiririko wa kauli shurutishi.

1. enenda, kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo
2. ukauze, kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu
3. uwape, kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu
4. njoo, kitenzi chenye kutumika kama kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu
5. unifuate, kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo

Ushurutishi huu (yaani., #4, 5) ni sawa na ule wito wa Yesu kwa wale Kumi na Wawili. Yesu alikuwa akimwalika mtu huyu kuwa sehemu ya kiungo chake!

☑ **"uwape maskini"** Kutokana na 1 Kor. 13:1-3, tunaona kwamba mtazamo ndiyo wa msingi!

☑ **"nawe utakuwa na hazina mbinguni"** Tazama maelezo katika Mathayo 6:19-20.

☑ **"kisha njoo unifuate"** Yesu alikubaliana na muundo wa kipaumbele cha mtu huyu na alidai kupata nafasi yake ya kwanza. Utajiri wake haukuwa tatizo, bali kipaumbela chake (kama vile 1 Tim. 6:10). Utambue umuhimu wa mtu kijitolea kwa ajili ya kumfuata Kristo (kama vile Mt. 10:34-39).

**19:22 "akaenda zake kwa huzuni"** Yesu alimpenda mtu huyu lakini hakujishusha kwa ajili ya Ufalme. Biblia imenyamaza kuhusianana wokovu wa mtu huyu. Hili linatisha pale tunapoelewa kwamba (1) alikuja kwa dhamira njema, (2) alikuja kwa mtu sahihi, (3) alikuja kwa maswali sahihi, na (4) Yesu alimpenda (Marko 10:21), alikwenda zake!

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 19:23-26**

<sup>23</sup> Yesu akawaambia wanafunzi wake, Amin, nawaambieni, ya kwamba itakuwa shida tajiri kuingia katika ufalme wa mbinguni. <sup>24</sup> Nawaambia tena, Ni rahisi zaidi ngamia kupenya tundu ya sindano, kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu. <sup>25</sup> Wanafunzi waliposikia, walishangaa mno, wakisema, Ni nani basi awezaye kuokoka? <sup>26</sup> Yesu akawakazia macho, akawaambia, Kwa wanadamu hilo haliwezekani; bali kwa Mungu yote yawezekana.

**19:23 "Amin"** Tazama Mada Maalum katika Matt. 5:18.

**19:24 "ngamia kupenya tundu ya sindano"** Kumekuwa na mjadala mwingi kuhusiana na kifungu hiki. Je! hili ni sahihi au ni taswira? Kamwe hapakuwa kuwa na mlango mdogo katika Yerusalemu ambapo iliwapasa ngamia kuinama ili kuingia ndani! Hili ni neno chochezi lililopitiliza, ambapo isingewezekana kwa watu tajiri kuokolewa! Bali kwa Mungu, mambo yote yanawezekana (Mt. 19:26). Yesu anaeleza hali ya tajiri, kijanamdogo. Anaonekana kubarikiwa na Mungu katika maana ya Agano la Kale, lakini haikuwa sahihi kwa Mungu. Matajiri na vyote walivyo navyo vinaweza kuwa (na mara nyingi ni) laana!

☑ **"itakuwa shida tajiri"** Tazama Mada Maalum: Wingi wa Mali katika Mt. 6:24

☑ **"ufalme wa Mungu"** Haya yalikuwa natumizi adimu ya kifungu hiki kilicho katika Mathayo kwa sababu Wayahudi kuogopa kulitaja Mungu katika bure (kama vile Kut.20:7; Kumb. 5:11). Kifungu hiki kinajitokeza mara

kwa mara katika Injili za Marko na Luka zilizoandikwa kwa ajili ya watu wa Mataifa.

**19:25 "Wanafunzi. . . walishangaa"** Kitabu cha Agano la Kale kilifundisha kwamba Mungu aliwabariki wenye haki na kuwaadhibu kwa uchache wadhalimu (kama vile Kumb. 27-28). Kitabu cha Ayubu, Zaburi 73, na Yer. 12:1-4 kupinga dhidi ya mtazamo huu wa kitamaduni. Mara nyingi wenye haki huteseka na wadhalimu hustawi. Wingi wa mali, nafasi na afya mara nyingi si viashiria vya upendeleo wa Mungu!

**19:26** Usemi huu unaweza kulirejelea Agano la Kale (yaani., Mwa. 18:14; Ayubu 42:2; Yer. 32:17,27). Hii ni mbinu ya kinahau ya udhaifu wa mwanadamu na uweza wa YHWH. Makusudi na mipango ya Mungu haviwezi kuzuiliwa (kama vile Ayubu 42:2; Luka 1:37)!

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 19:27-30**

<sup>27</sup> Ndipo Petro akajibu, akamwambia, Tazama, sisi tumeacha vyote tukakufuata; tutapata nini basi?  
<sup>28</sup> Yesu akawaambia, Amin, nawaambia ya kwamba ninyi mlionifuata mimi, katika ulimwengu mpya, atakapoketi Mwana wa Adamu katika kiti cha utukufu wake, ninyi nanyi mtaketi katika viti kumi na viwili, mkiwahukumu kabila kumi na mbili za Israeli. <sup>29</sup> Na kila mtu aliyeacha nyumba, au ndugu wa kiume au wa kike, au baba, au mama, au watoto, au mashamba, kwa ajili ya jina langu, atapokea mara mia, na kuurithi uzima wa milele. <sup>30</sup> Lakini wengi walio wa kwanza watakuwa wa mwisho, na walio wa mwisho watakuwa wa kwanza.

**19:27 "tutapata nini basi"** Petro alikuwa amecha vyote lakini alikuwa akiendelea kuvifikiria! Wanafunzi hawa bado walikuwa wakiendelea kutarajia ufalme wa kidunia kwa ajili ya thawabu maalum kwa ajili yao (kama vile Mt. 20:21,24).

**19:28 "Mwana wa Adamu"** Tazama maelezo katika Mathayo 8:20.

🔍 **"ninyi mlionifuata mimi . . .mtaketi katika viti kumi na viwili, mkiwahukumu kabila kumi na mbili za Israeli"** Kifungu hiki lazima kirejeele wale Mitume halisi Kumi na Wawili (kama vile Luka 22:30), ambapo Mt. 19:29 inazipanua faida za baraka tele na maisha ya milele kwa waamini wote (kama vile Mt. 20:16; Marko 10:31; Luka 13:30). Je! Kifungu hiki "kabila kumi na mbili za Israeli" kinamrejelea nani?

1. Israeli mpya, kanisa (kama vile. Rum. 2:28,29; Gal. 6:16; 1 Pet. 2:5,9; Ufu. 1:6)
2. Israeli ya siku za mwisho iaminiyo

Kwangu inaonekana kwamba mstari huu unasistiza kwamba wale Kumi na Wawili wataushiriki utukufu na utawala wa Yesu. Mistari yenye kufanana na huu haipaswi kutumika kueleza nadharia zenye kujenga asili ya matukio ya mwisho! Tazama Mada Maalum: Hesabu ya Kumi na Mbili katika Mt. 14:20.

#### **MADA MAALUM : KUTAWALA KATIKA UFALME WA MUNGU**

Dhana ya kutawala tukiwa na Kristo ni sehemu ya namna kubwa ya kithiolojia inayitwa "ufalme wa Mungu." Huu ni mwito toka dhana ya Agano la Kale la Mungu Yeye kama Mfalme wa kweli wa Israel (kama vile 1 Sam .8:7). Kiishara anatawala (1 Sam. 8:7; 10:17-19) kupitia kizazi cha kabila la Yuda (kama vile Mwa. 49:10) na familia ya Yese (kama vile 2 Samweli 7).

Yesu ni ahadi ya utimilifu wa unabii wa Agano la Kale kuhusiana na Masihi. Aliuanzisha Ufalme wa Mungu akiwa na mwili wa kibinadamu pale Bethlehemu. Ufalme wa Mungu ukaja kuwa ni nguzo kuu ya mafundisho ya Yesu. ufalme wa Mungu ukawa kamili ndani yake (kama vile Mt. 10:7; 11:12; 12:28; Mark 1:15; Lk 10:9,11; 11:20; 16:16; 17:20-21).

Hata hivyo, ufalme ulikuwa wa wakati ujao (matukio ya siku za mwisho). Ulikuwapo lakini ukawa haujatimilizwa (kama vile. Mt. 6:10; 8:11; 16:28; 22:1-14; 26:29; Lk 9:27; 11:2; 13:29; 14:10-24; 22:16,18). Kwa mara ya kwanza



Yesu akaja kama mtumwa mwenye mateso (kama vile Isa. 52:13-53:12); mwenye kunyenyekea (kama vile Zek. 9:9), bali atarudi kama Mfalme wa Wafalme (kama vile Mt. 2:2; 21:5; 27:11-14). Dhana ya "kutawala" kwa uhakika ni sehemu ya "Ufalme" wa thiolojia. Mungu amekwisha kuwapatia ufalme wafuasi wa Kristo (angalia Lk 12:32).

Dhana ya kutawala pamoja na Kristo ina mitizamo mbali mbali pamoja na maswali

1. Je sura zile zinazodai kuwa Mungu amewapa waamini "ufalme" kupitia Kristo zinarejea juu ya "kutawala" (kama vile Mt. 5:3,10; Lk. 12:32)?
2. Je maneno ya Yesu kwa wanafunzi wa mwanzo kwenye karne ya kwanza katika mazingira ya Kiyahudi yanarejea kwa waamini wote (kama vile Mt. 19:28; Lk. 22:28-30)?
3. Je misisitizo ya Paulo juu ya kutawala katika maisha haya ya sasa yanakinzana au yanawiana na maandiko ya hapo juu (kama vile Rum. 5:17; 1 Kor. 4:8)?
4. Ni kwa namna gani mateso na utawala vinahusiana (kama vile Rum. 8:17; 2 Tim. 2:11-12; 1 Pet. 4:13; Ufu. 1:9)?
5. Dhana ya kujirudia ya ufunuo unachangia pamoja utawala wa Yesu uliotukuzwa, lakini huo utawala wa
  - a. Kidunia, Ufu. 5:10
  - b. Utawala wa miaka 1000, Ufu. 20:4-6
  - c. Milele, Ufu. 2:26; 3:21; 22:5 na Dan. 7:14,18,27

**NASB, NKJV** "ulimwengu mpya"  
**NRSV** "katika urejesho wa yote"  
**TEV** "katika Enzi Mpya"  
**NJB** "ambapo kila kitu kitafanywa upya"

Neno hili linamaanisha "kuzaliwa upya." Philo analitumia neno hili kuzungumzia kuzaliwa tena baada ya gharika. Hili lilitumiwa na wanafikra wa Kiyunani kueleza mpangilio mpya wa ulimwengu. Hapa hili linarejelea kuzaliwa upya katika Enzi Mpya za utimilifu wa Roho. Wanafunzi bado wanafikiri kuwa hili lingetokea wakati wa uhai wao. Hawa walikuwa wakistaajabishwa na hatua mbili za ujio wa Masihi.

Uumbaji wa awali uliharibiwa; uumbaji mpya baada ya gharika ya Nuhu pia uliharibiwa, bali kuzaliwa upya kwa utimilifu wa ki-Masihi utakuwa safi, kamili (kama vile Isa. 9:6-7; 11:1-10; Mika 5:2-5a; Ufunuo 21-22).

#### 19:29

**NASB** "mara mia"  
**NKJV, NRSV** "mara mia"  
**TEV** "zaidi ya mara mia"  
**NJB** "mara mia sana"

Kuna tofauti za machapisho ya Kiyunani katika kiwango hiki. Hili neno "mara mia" kiko katika machapisho ya herufi kubwa MSS, X C na D, ambapo "fungamana na wanadamu" kiko katika MSS B na C. Uchaguzi wa kwanza unaifuatisha Marko 10:29 na ule wa pili Luka 18:30. Wasomi wengi wanadhani kwamba Mathayo na Luka wanaifuatisha muundo wa Marko. Kujitolea kwa mtu kwa ajili ya Yesu kunahitaji kuiacha nyumba yake, mali zake na hata kuutoa uhai wake (kama vile Mt. 10:34-39; Luka 12:51-53). Hizi enzi mpya za haki zinafafanuliwa katika uchechezi wa kitutamadumi (kama ilivyo kaika Agano la Kale). Biblia haionyeshi dhahiri namna mbingu itakavyokuwa inafanana.

1. kurejeshwa upya Bustani ya Edeni
2. wingi wa mazao
3. mji nzuri
4. ufalme mpya wa kiroho

Kinachofunuliwa na andiko ni kwamba imani binafsi katika Yesu sasa huzistiri baraka za mbinguni kwa kwa ajili ya wakati wa baadaye. Sasa hakuna dhabih binafsi itakayokataliwa au ambayo haitatolewa thawabu! Msingi wa baraka ni "uzima wa milele" pamoja na Mungu katika Kristo! Yote huonekana kuwa muhimu.

Yatupasa kuwa makini juu ya kuishikiria thiolojia ya dhahibu sasa kwa ajili ya utele wa baadaye! Mali ya kweli ni kuwa karibu sana na Mungu. Semi za Yesu ni

1. za kutia chumvi
2. zenye kuelezeka kwa ajili ya uelewa wa mara kwa mara wa wanafunzi
3. zenye kuonyesha umuhimu, maamuzi binafsi yaliyohusishwa katika kifungu " kumfuata" Yeye!

Mafikiri kuwa maneno ya Yesu hapa ni ya kutia chumvi na yanahusiana na sura za uzalishaji wa mazao ya Agano la Kale. Alieleza kwa namna hii kwa sababu ya kutoelewana kwa Mitume juu ya asili ya kiroho ya Ufalme wa Mungu. Kwangu hili halileti maana yo yote kwa waanini kuukataa uyaikinifu katika maisha haya tu na kudai katika wakati ujao ("kuingia angani, kwa na kwa kupitia Ukristo"). Yesu anajaribu kuwatia moyo kwa kiwango ambacho wanaweza kukielewa. Hili si andiko la linalojikita katika mitazamo ya mtu kuihusumbingu! Maisha baada ya kifo, vyote jehnamu na mbinguni, yanafunuliwa. Stiari za kidunia zinatumiwa kutoa ufafanuzi wa yote, lakini ni kwa sababu ya upofu wa mara kwa mara unaosababishwa na na Anguko (yaani., "tunajitazma kupitia kioo chenye giza," 1 Kor. 13:9-12). Yatupasa kujilinda mara zote dhidi ya "kile kilicho ndani yake kwa ajili yangu" Ukristo. Mbingu, sawa na Ufalme, unavyohusiana naye!

## **MADA MAALUM: URITHI WA MWAMINI**

Katika Agano la Kale kila kabila isipokuwa la Walawi lilipokea urithi wa ardhi (kama vile YOSHUA 14-22). Walawi, kama kabila la kikuhani, wahudumu wa hekaluni, na waalimu wa kanisa la mahali, walionekana kuwa na YHWH Mwenyewe kama mrithi wao (kama vile. Zab. 16:5; 73:23-26; 119:57; 142:5; Wimb. 3:24). Waandishi wa Agano Jipya mara nyingi walichukua haki na upendeleo wa Walawi na kuitumia kwa waamini. Hii ilikuwa ni njia yao ya kudai kuwa wafuasi wa Yesu walikuwa watu wa Mungu na kwamba sasa waamini wote wameitwa kutumika kama makuhani mbele za Mungu (kama vile 1 Pet. 2:5,9; Uf. 1:6), kama Agano la Kale linavyo watetea Waisrael wote(kama vile Kut. 19:4-6). Msisitizo wa Agano Jipya sio juu ya mtu binafsi kama kuhani aliye na upendeleo Fulani, bali ni katika kweli kwamba waamini wote ni makuhani, wakihitaji ushirika wa mwenendo wa kitumishi (kama vile 1 Kor. 12:7). Watu wa Mungu wa Agano Jipya wamekwisha pewa majukumu ya Agano la Kale ya kueneza injili ulimwenguni (kama vile Mwa. 12:3; Kut. 19:5b; Mt. 28:18-20; Lk. 24:46-47; Mdo 1:8; angalia Mada Maalum: Mpango wa YHWH wa ukombozi wa Milele).

Hii ni dhana ya Yesu kama mmiliki wa uumbaji kwa sababu alikuwa ni wakala wa Baba kipindi cha uumbaji (kama vile. Yn 1:3,10; 1 Kor. 8:6; Kol. 1:16; Ebr. 1:2-3). Sisi ni warithi wenza kwa vile Yeye ni mrithi (kama vile Rum. 8:17; Gal. 4:7; Kol. 3:24). Maandiko yanazungumza kuhusu kurithi kwa waamini (kama vile Mdo. 20:32; 26:18; Efe. 1:4; Kol. 1:12; 3:24) vitu vingi kwa sababu ya mahusiano yao ya kifamilia na Yesu ambaye ndiye mrithi wa vitu vyote (kama vile Ebr. 1:2). Kwa hiyo, wao pia ni warithi wenza (kama vile Rum. 8:17; Gal. 4:7) wa

1. Ufalme (kama vile Mt. 25:34, 1 Kor. 6:9-10; 15:50; Efe. 5:5)
2. Maisha ya milele (kama vile Mt. 19:29; Ebr. 9:15)
3. Ahadi za Mungu (kama vile Ebr. 6:12)

Ulinzi wa Mungu wa ahadi zake (kama vile 1 Pet. 1:4-5)

**19:30** Mambo si kama yanavyoonekana kwetu (kama vile Mt. 20:16; Marko 10:31; Luka 13:30). Njia za Mungu za kuyatazama mambo ni tofauti na zetu (kama vile Isa. 55:8-11). Kuwa kama watoto wanafunzi walipokelewa, ambapo mali na vipaumbele hawakuwa navyo (yaani., Mt. 8:10-12). Imani ya ki-Bibilia husababisha mkanganyiko wa kiuumbaji usio tarajiwa!

## **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kutoa talaka mara nyingi ni dhambi?
2. Ni msingi gani wa kibiblia ambao Yesu aliuutolea maelezo katika kulijibu swali la Mafarisayo?
3. Kwa nini Musa aliruhusu ndoa nyingine ikiwa Mungu aliipinga? Vipi kuhusu siku hizi?
4. Je! Kiroho useja ni jambo kuu zaidi ya ndoa?
5. Fafanua mafundisho ya Biblia kuhusu watoto na wokovu.
6. Je! Mistari ya 13-15 inashughulika na wokovu?
7. Kwa nini Yesu "wema" katika Mt. 19:17? Je! Hili linayaathiri mafundisho yahasuyo Uungu wa Yesu au kutokuwa na dhambi?
8. Je! Mtu huyu anazitunza amri hizi kwa usahihi? Je! Hakuwa na dhambi? (Mt. 19:20)

## MATHAYO 20

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Wakulima kwenye Shamba la mizabibu 20:1-16	Mfano wa wakulima katika shamba la Mizabibu 20:1-16	Wafanyakazi katika shamba la mizabibu 20:1-16	Wakulima kwenye shamba la mizabibu 20:1-7 20:8-15 20:16	Mfano wa wakulima katika shamba la mizabibu 20:1-16
Mara ya tatu Yesu Anaongelea juu ya Kifo na ufufuo wake 20:17-19	Yesu anatabiri mara tatu juu ya kifo na ufufuo wake 20:17-19	Mateso yanasemwa mara tatu 20:17-19	Yesu anaongea mara tatu juu ya kifo chake 20:17-19	Unabii wa tatu wa mateso 20:17-19
Maombi ya Yakobo Na Yohana 20:20-28	Salome anaulizia upendeleo 20:20-28	Yakobo na Yohana wanataka heshima 20:20-23	Maombi ya mama 20:20 20:21a 20:21b 20:22a,b 20:22c 20:23	Mke wa Zebedayo afanya maombi 20:20-23
huduma		20:24-28	20:24-28	Uongozi na 20:24-28
Uponyaji wa vipofu Wawili 20:29-34	Vipofu wawili wapata kuona 20:29-34	Vipofu wawili wa Yeriko 20:29-34	Yesu anaponya vipofu wawili 20:29-30 20:31 20:32 20:33 20:34	Vipofu wawili wa Yeriko 20:29-34

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka [“Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia”](#))**

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMKUTADHA

- A. Katika kutafsiri mifano (tazama Mada Maalumu kwenye utangulizi wa Mathayo 13) ni muhimu kuangalia historia na muktadha wa fasihi. Katika mfano huu maalumu wa muktadha wa kihistoria unasimulia mwisho wa tungo ya Mt. 19:30, ambayo imerudiwa kwa kuribu sana na Mathayo 20:16. Mfanano huu wa kifasihi unaonyesha kwamba mjadala wa awali unasimulia jambo la utajiri na zawadi. Muktadha mkuu wa fasihi unaonekana kwenye Mt. 18:1 na 20:20-21, 24, ambapo wanafunzi walihofu juu ya nani kuwa mkuu kati yao.
- B. Wengi wametafsiri mfano huu kama rejea ya uhusiano kati ya Wayahudi na Mataifa na kutoka muktadha mkuu wa Agano Jipya lote (au pale injili ilipoandikwa), hii inawezekana. lakini, kutoka muktadha wa karibu sana, mfano huu unafanya uhusiano kati ya wanafunzi wenyewe. Ufalme wa Mungu una tofauti ya kawaida kabisa ya tathmini zaidi ya ulimwengu (kama vile Isa. 55:8-11; Mathayo 5-7). Ufalme mpya wa Mungu (kama vile Yer. 31:31-34; Ezek. 36:22-38) umejikita pekee kwenye rehema na sio matendo mema ya mwanadamu. Hii haimaanishi kupunguza au kuharibu matendo ya kidini ya uanafunzi; kidogo, rehema ni msingi wa wokovu na maisha ya haki (kama vile. Efe.2:8-10). Uanafunzi ni lazima utiwe moyo kwa shukrani, sio kwa matendo mema (kama vile Rum. 3:21-24; 6:23; Efe. 2:8-9).
- C. Tunahitaji kukumbuka tunapotafsiri mifano kwamba, msingi wa ukweli na muktadha ni wa muhimu sana zaidi kuliko kuweka kila kitu kwenye utaratibu wa kitheolojia. Ufunguo wa mifano ni kwa ajili ya kuangalia yasiyotarajiwa, au maelezo ya kushangaza kitamaduni.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 20:1-7

<sup>1</sup> Kwa maana ufalme wa mbinguni umefanana na mtu mwenye nyumba aliyetoka alfajiri kwenda kuajiri wakulima awapeleke katika shamba lake la mizabibu. <sup>2</sup> Naye alipokwisha kupatana na wakulima kuwapa kutwa dinari, aliwapeleka katika shamba lake la mizabibu. <sup>3</sup> Akatoka mnamo saa tatu, akaona wengine wamesimama sokoni wasiokuwa na kazi; <sup>4</sup> na hao nao akawaambia, Enendeni nanyi katika shamba langu la mizabibu, na iliyo haki nitawapa. Wakaenda. <sup>5</sup> Akatoka tena mnamo saa sita na saa kenda, akafanya vile vile. <sup>6</sup> Hata kama saa kumi na moja akatoka, akakuta wengine wamesimama, akawaambia, Mbona mmesimama hapa mchana kutwa bila kazi? <sup>7</sup> Wakamwambia, Kwa sababu hakuna mtu aliyetuajiri. Akawaambia, enendeni nanyi katika shamba la mizabibu.

**20:1 "Kwa maana ufalme wa mbinguni"** Fumbo lililotolewa ni kama mfano wa namna gani thawabu itolewayo na dunia hii ambayo ni tofauti kabisa na thawabu za kiroho za ufalme wa Mungu. Fumbo hili ni la kipekee katika Mathayo. "ufalme wa mbinguni" ilikua ni mada kuu kwenye mafundisho na mahubiri ya huduma ya Yesu. Inarejelea utawala wa Mungu kwenye mioyo ya wanadamu ambao siku moja utakamilishwa juu ya ulimwengu (kama vile Mt. 6:10). Madai ya ufalme wa Mungu ya wakati ujao ni asili ya "kuwa tayali" na "sio bado" hofu na kweli kinzani juu ya ujio wa pili wa Kristo na maisha ya Ukristo.

☐ **"mwenye nyumba"** huu ni mchanganyo wa neno "nyumba" ukijumlisha "bwana" (*despotēs*). Inatafsiriwa kwa tungo ya Kiebrania, "mtu mwenye nyumba." Mathayo amelitumia jina hili mara kwa mara (kama vile Mt. 10:25; 13:27,52; 20:1,11; 21:33; 24:43).

Kwenye kifungu hiki inaaksi rehema za Mungu kuhusika na uumbaji wake kwa mwanadamu. Katika Mt. 10:24-25 Yesu ni "Bwana mwenye nyumba" wa kweli, lakini walimuita "*Beelzebul*" (mkuu wa pepo au shetani). Grant Osborne, *The Hermeneutical Spiral*, ukr. 244 ana mawazo yenye shauku.

"Mungu amejitokeza kwenye fuises mara kadhaa kwenye mifano kama Mfalme, Baba, Mwenye nyumba na Hakimu. Popote, picha ni nani mwenye rehema na neema atoaye msamaha, lakini wakati mwingine anataka

maamuzi. . wokovu ni sasa na kusisitiza mwitikio. Utawala ya Mungu unawakilishwa na neema lakini changamoto za neema zinawafanya wasikilizaji kutambua umuhimu wa kutubu."

▣ **"shamba la mizabibu"** wengi wanathibitisha kwamba hii ilikuwa inarejelea kwa taifa la Israeli. Ni kweli kwamba shamba la mizabibu mara kwa mara lilisimama kwa ajili ya Israeli kwenye Agano la kale (kama vile Isa. 5, Yer. 2:21; Zab. 80:8-13), lakini haimaanishi kwamba inafanyika kwa kila muktadha kwenye Agano jipya. Kwenye muktadha huu, inaonekana ni utaratibu wa mfano na usiokuwa na ishara kuu ya ukweli.

**20:2 "Naye alipokwisha kupatana na wakulima kuwapa kutwa dinari"** kundi hili la kwanza la wakulima ndio pekee alikuwa amejadiliana nao kuwalipa kwa ajili ya kazi ya kutwa. Neno hili "denari," kama thamani ya fedha zote kwenye tafsiri, ina muunganiko sawa wa kihistoria. Itakuwa bora zaidi kuona kiasi hiki cha fedha kwenye mwanga wa matumizi yake katika karne ya kwanza, kama mshahara wa kutwa kwa askari au kwa wakulima. Ilikuwa ni pesa iliyotosheleza kununulia chakula na mahitaji muhimu kwa kutwa kwa ajili ya familia ya Kipalestina.

**20:3**

**NASB, NKJV,**

**NJB** "mnamo saa tatu"

**NRSV, TEV** "saa kenda"

Makusudi yote (Mt. 20:3,5,6) kwa ajili ya muda kwenye mfano yanasisitiza wazo la siku kuanza saa 12 asubuhi (muda wa kirumi); hivyo basi, ilikua ni saa tisa asubuhi. Wayahudi siku zao zilianza saa 12 jioni (yaani, Mwa. 1:5).

Swali moja ni kwa nini mwenye shamba la mizabibu aliajiri watu wengi kwa kutwa. Inathibitishwa na wana zuoni kwamba ilikua inafikia kilele cha mavuno ya zabibu pamoja na sabato; hivyo basi, ilikua inawezekana kukusanya zabibu nyingi haraka kabla hajaharibika.

**20:6 "akakuta wengine wamesimama"** ingawa kwa kiingereza tungo hii inashusha heshima, kama ikiwa mwenye shamba alikuwa anawakemea watu hawa kwa kutofanya kazi kutwa nzima, katika ukweli aliwapata baadhi ya watu ambao hawakuajiliwa mapema kabisa. Hakuna dokezo kwamba walikua wavivu au wakulima wasiojali, lakini walikua hawajaweza kutafuta kazi kwa ajili ya siku hiyo (kama vile Mt. 20:7).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 20:8-16**

<sup>8</sup> Kulipokuchwa, yule bwana wa shamba akamwambia msimamizi wake, Waite wakulima, uwalipe ujira wao, ukianzia wa mwisho hata wa kwanza. <sup>9</sup> Na walipokuja wale wa saa kumi na moja, walipokea kila mtu dinari. <sup>10</sup> Na wale wa kwanza walipokuja, walidhani kwamba watapokea zaidi; na hao pia wakapokea kila mtu dinari. <sup>11</sup> Basi wakiisha kuipokea, wakamnung'unikia mwenye nyumba, <sup>12</sup> wakisema, Hao wa mwisho wametenda kazi saa moja tu, nawe umewasawazisha na sisi tuliostahimili taabu na hari za mchana kutwa. <sup>13</sup> Naye akamjibu mmoja wao, akamwambia, Rafiki, sikudhulumu; hukupatana nami kwa dinari? <sup>14</sup> Chukua iliyo yako, uende zako; napenda kumpa huyu wa mwisho sawa na wewe. <sup>15</sup> Si halali yangu kutumia vilivyo vyangu kama nipendavyo? Au jicho lako limekuwa ovu kwa sababu ya mimi kuwa mwema? <sup>16</sup> Vivyo hivyo wa mwisho watakuwa wa kwanza, na wa kwanza watakuwa wa mwisho.

**20:8 "Kulipokuchwa, yule bwana wa shamba akamwambia msimamizi wake, 'Waite wakulima, uwalipe ujira wao'"**Tunajifunza kutokana na sheria ya Musa kwamba wakulima walikua wanalipwa kwa kazi ya kutwa ili kwamba waweze kujinunulia chalula kwa ajili ya familia zao (kama vile Law. 19:13; Kumb. 24:15; Mal. 3:5). Mara nyingi mwenye mashamba walijaribu kushikilia mshahara mpaka siku inayofuatia ili kuwa na uhakika wa kuwashurutisha wakulima waweze kurudi, lakini hii ilikua kinyume dhidi ya sheria ya Musa.

**20:10 "Na wale wa kwanza walipokuja, walidhani kwamba watapokea zaid"** wakulima wa kwanza walioajiriwa walikuwa na uhakika kwamba walistahili fedha zaidi kwa sababu waliotenda kazi muda mchache walipokea kile ambacho walikuwa wameafikiana (kama vile Mt. 20:2). Mfano huu unaonyesha ni kwa namna gani njia za Mungu ni tofauti kulinganisha na njia za ulimwengu huu. Tunaona kutoka Mt. 20:11 kwamba malalamiko yaliendelea,

pale waliposhindwa kupokea fedha zaidi. Shauku yao ya kufulahia kuajiriwa iligeuka kuwa hasira kwa sababu hawakupata kile chote walichokitarajia. Walilinganisha kwamba kwa sababu walitenda kazi siku nzima kwenye jua, walistahili malipo zaidi. Kuhusisha huku ni ishara ya uhusiano wa watu wa kidini na thawabu za kiroho (kama vile Mt. 19:30; 20:16).

**20:13-15** mwenye shamba anajibu maswali matatu yasiyodai majibu. Mwenye shamba alikua na uhuru wa kutenda atakavyo (kama vile. Warumi 9), lakini alichagua kutenda kwa neema!

**20:15** mstari huu ni mfano wa theolojia ya moyo. Mungu ni mtawala na ana haki ya kutenda (yaani, Warumi 9-10). Alichagua kutenda katika neema isiyostahili (kama vile Warumi 11). Je kuna yeyote amwona kuwa na hatia kwa ajili ya hilo?

Huu ni mfanano wa kitheolojia kwa mwana mpotevu ulioandikwa kwenye Luka 15:11-32. Inawezekana neema ya Mungu kwa baadhi ya waliokosea wale ambao pia wana ufahamu wa neema yake?

**NASB, NRSV** "Au jicho lako limekuwa ovu kwa sababu ya mimi kuwa mwema"  
**NKJV** "Au jicho lako limekuwa kwa sababu mimi mwema"  
**TEV** "Au umekuwa wivu kwa sababu mimi ni mwema"  
**NJB** "kwa nini umekuwa mwovu kwa sababu ya mimi kuwa mwema"

Hii inarejelea sitiari ya Mashariki ya kale ya karibu ya "jicho ovu" (kama vile Kumb. 15:9; 1 Sam. 18:9). Katika muktadha huu inarejelea wivu au kijicho (kama vile Marko 7:22). Tazama mada maalum katika Mt. 6:22-23.

**20:16**

**NASB** " hivyo wa mwisho watakuwa wa kwanza, na wa kwanza watakuwa wa mwisho"  
**NKJV** "wa mwisho watakuwa wa kwanza, na wa kwanza watakuwa wa mwisho.walioitwa ni wengi, lakini wateule ni wachache"  
**NRSV** "hivyo wa mwisho atakuwa wa kwanza na kwanza atakuwa wa mwisho"  
**TEV** "wale wote wa mwisho watakuwa wa kwanza, na wale wote wa kwanza watakuwa wa mwisho"  
**NJB** " hivyo wa mwisho atakuwa wa kwanza, na wa kwanza, wa mwisho"

Kuna tungo mwisho wa mstari huu "walioitwa ni wengi, lakini wateule ni wachache," ambayo inapatikana kwenye toleo la KJV, lakini imeachwa kwenye toleo la NASB, NKJV, TEV, na JB. Inaonekana imeongezwa kutoka katika Mt. 22:14. Haijitokezi kwenye machapisho ya Kiyunani ya  $\alpha$ , B, L, au Z. toleo la UBS<sup>4</sup> linatupatia kuachwa " A" daraja (yaani,uhakika).

Kuna uhusiano wa wazi kati 19:30 na 20:16. Thawabu haisisitizi matendo mema lakini katika rehema. Hili linafahamika kwa njia mbili

1. waamino wote hawatapokea thawabu sawa, lakini hadhi sawa kwenye ufalme. Huu ni utata wa Kibiblia kati ya wokovu huru na uanafunzi unaofanana Kristo.
2. Wayahudi waliopokea ahadi za Mungu kwanza hawatapokea thawabu kubwa au Baraka zaidi ya waamini wa mataifa (kama vile. Luka 13:30).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. ni nini mwongozo kwa ajili kutafsiri mifano? (tazama *How to Read the Bible For All Its Worth*, na Fee na Stuart, uk. 135-148)
2. ni nini muktadha wa fasihi wa mfano huu?

3. mfano huu unazungumzia nini uhusiano kati ya wana wa Mungu na thawabu?
4. unafikiria nini kuhusu uhusiano kati ya mfano huu na ndugu mkubwa kwenye mfano wa mwana mpotevu (Luka 15)?

## UTAMBUZI WA KIMUKTADHA WA 20:17-18

- A. Jambo la kufanana hapa, linapatikana kwenye Marko 10:32 na kuendelea., kunapangilia hatua kwa ajili ya mtizamo na matendo ya wanafunzi.
- B. Ni wazi kutoka katika jambo hili kwamba wanafunzi bado msingi wa kutofahamu ufalme wa kimasihi. Hii inawezekana inasimulia maelezo ya Yesu kwenye Mt. 19:28.
- C. Huu ni unabii watatu muhimu unaotabiri kifo cha Yesu na ufufuo kwa wanafunzi (kama vile Mt. 16:21; 17:9,22-23). Alitambua kwa nini alikuja! Alimiliki historia yake mwenyewe (kama vile Yn. 10:17-18)!

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 20:17-19

<sup>17</sup> Hata Yesu alipokuwa akipanda kwenda Yerusalemu, aliwachukua wale wanafunzi kumi na wawili faraghani; na njiani akawaambia, <sup>18</sup> Angalieni, tunapanda kwenda Yerusalemu; na Mwana wa Adamu atatiwa mikononi mwa wakuu wa makuhani na waandishi; nao watamhukumu afe; <sup>19</sup> kisha watampeleka kwa Mataifa wapate kumdhihaki, na kumpiga mijeledi, na kumsulibisha; na siku ya tatu atafufuka.

**20:17 "Hata Yesu alipokuwa akipanda kwenda Yerusalemu"** Marko 10:32 inasema aliuielekeza uso wake Yerusalemu na akawatangulia mbele wanafunzi wake.

**20:18 "mwana wa Adamu"** tazama muhtasari katika Mt. 8:20.

☐ **"wakuu wa makuhani na waandishi"** hii ni rejea kwa baraza kuu la Kiyahudi. Liliundwa na viongozi wapato 70 wa jamii ya Kiyahudi katika Yerusalemu. Jina kamili lilikua "wakuu wa makuhani, waandishi, na wazee," (kama vile. Mt. 16:21). Hili lilikua na mamlaka ya mwisho kwa jambo la kidini na kisiasa kwa ajili ya Wayahudi, ingawa lilikua linadhibitiwa zaidi kwa kumilikiwa na majeshi ya Kirumi kwa maana ya kisiasa.

Tazama [MADA MAALUM: WAKUU WA SINAGOGI](#) katika Mt. 16:21.

**20:19 "kisha watampeleka kwa Mataifa wapate kumdhihaki, na kumpiga mijeledi, na kumsulibisha"** hii inarejelea fedheha ya Yesu na mateso kutoka kwa mamlaka ya Kirumi. Maaskari walipeleka chuki yao kwa wakazi wa Kiyahudi waliojitenga kwa kuihamishia kwa Yesu.

Kitenzi hiki "watampeleka" (*paradidōmi*) mara nyingi inarejelea Yesu kutolewa kwa kundi lenye mamlaka halali au mtu kwa ajili ya hukumu.

1. kwa wakuu wa makuhani na waandishi, Mt. 20:18
2. kwa watu, Mt. 17:22
3. kwa mataifa (*ethnē*), Mt. 20:19
4. kwa Pilato, Mt. 27:2
5. kwa ajili ya kusulibiwa, Mt. 26:2

Kwa sababu ya maelezo ya Yesu katika Mt. 10:24-25, waaminio pia "watapelekwa" (kama vile Mt. 10:17; 24:9; Luka 21:12).

☐ **"kumsulibisha"** muundo huu wa kutisha wa hukumu ya kifo sio tu ulifanyika hadharani pekee kwa fedheha na maumivu, lakini kwenye uhusiano wake na Kumb. 21:23; kwa mujibu wa walimu wa sheria nyakati za Yesu "laana



ya Mungu" ilikua juu ya wale waliotundikwa juu ya mti. Yesu alifanyika "laana" (Law. 26; Kumb. 27-28; Gal. 3:13; Kol. 2:14) kwa ajili ya dhambi za mwanadamu!

☑ **"siku ya tatu"** kwenye 1 Kor. 15:4 Paulo anataja kwamba hiki kilikua ni kipengele muhimu sana cha injili. Hata hivyo, tunapo angalia katika Agano la kale, ni vigumu kupata dokezo la "siku tatu." Baadhi wamejaribu kutumia Hos. 6:2, lakini hii inaonekana kuwa na wasiwasi kabisa. Kwa sababu ya Mt. 12:38-40 wengi wametumia nyakati za Yona kwenye tumbo la nyangumi (kama vile Yona 1:17). Hii inaonekana kufaa zaidi.

Kwa wayahudi nyakati za Yesu sehemu yeyote ya siku ilihesabiwa kuwa siku kamili. Kumbuka wayahudi huanza siku zao jioni (kama vile Mwa 1:5). Hivyo basi kifo cha Yesu siku ya ijumaa mchana (9 mchana.) na kuzikwa kabla ya saa 12 jioni ilihesabiwa kama siku moja. Ijumaa jioni hadi jumamosi jioni (sabato) ilikua ni siku ya pili; kutoka jumamosi jioni hadi wakati fulani kabla ya mapambazuko ya jua siku ya jumapili ilikua ni siku ya tatu. Tazama muhtasari katika Mt. 16:21.

☑ **"atafufuka"** kwa kawaida ufufuo (tazama mada maalum katika Mt. 27:63) unaongelewa kama tendo la mapenzi ya Baba ambayo yanathibitisha uzima, huduma, na kifo cha Yesu. Hata hivyo, kwenye Yn. 10:17-18 Yesu anatetea mamlaka yake kwenye ufufuo wake. Rum. 8:11 inasema Roho alimfufua Yesu. Hapa ni mfano mwema wa wote utatu kuhusika kwenye tendo la ukombozi.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 20:20-23**

<sup>20</sup> Ndipo mama yao wana wa Zebedayo akamwendea pamoja na wanawe, akamsujudia, na kumwomba neno. <sup>21</sup> Akamwambia, Wataka nini? Akamwambia, Agiza kwamba hawa wanangu wawili waketi mmoja mkono wako wa kuume, na mmoja mkono wako wa kushoto, katika ufalme wako. <sup>22</sup> Yesu akajibu akasema, Hamjui mnaloliomba. Je! Mwaweza kunywea kikombe nitakachonywea mimi? Wakamwambia, Twaweza. <sup>23</sup> Akawaambia, Hakika mtakinywea kikombe changu; lakini kuketi mkono wangu wa kuume na mkono wangu wa kushoto, sina amri kuwapa, bali watapewa waliowekewa tayari na Baba yangu.

**20:20 "mama yao wana wa Zebedayo"** kutoka katika Marko 10:35 tunajifunza kwamba Yakobo na Yohana walikua wana ombi la tendo hili pia. Tunapolinganisha Mt. 27:56 na Marko 15:40 na Yn. 19:25 kwa kiasi fulani inawezekana kwamba Salome, mke wa Zebedayo, alikua dada yake na mama wa Yesu.

☑ **"akamsujudia"** hili sio tendo la kuabudu lakini ni kusudi binafsi la familia. Ni kwa namna gani Wakristo hupiga magoti mbele za Mungu ili kupata wanachokitaka? Wanajaribu kufanya biashara ya imani kwa ajili ya fadhila (kama vile Ayu. 1:9-11)!

☑ **"kumwomba neno"** Marko anaandika "tutendee kile tulichokuuliza." Maneno haya ni kama maombi ya mtoto mdogo.

**20:21 "Agiza kwamba hawa wanangu wawili waketi mmoja mkono wako wa kuume, na mmoja mkono wako wa kushoto, katika ufalme wako"** kila mara Yesu alijaribu kujadili kifo chake, wanafunzi wakaanza kubishana juu ya nani ni mkuu. Hii inaonyesha msingi wa kutofahamu sio tu mtu mmoja pekee na kazi za Kristo, lakini ya ufalme wa kimasihhi (kama vile Luka 18:34).

**20:22 "Yesu akajibu akasema, 'Hamjui'"** neno "hamjui" la Mt. 20:21 ni umoja, unamwelezea mama, lakini kwenye Mt. 20:22 ni wingi, inamwelezea Yakobo na Yohana.

☑ **"Je! Mwaweza kunywea kikombe nitakachonywea mimi"** neno "kikombe" kimetumika kwenye fasihi ya Ugaritiki yenye kumaanisha hatima. Kwenye Biblia, hata hivyo, inaonekana inamaanisha uzoefu wa maisha kama mema au maovu. Ilikua kwa kawaida inatumika kwenye maana ya hukumu (kama vile Zab. 75:8; Isa. 51:17-23; Yer. 25:15-28, 49:12, 51:7; Omb. 4:21-22; Ezek. 22:31-34; Hab. 2:16; Zak. 12: 2; Ufu. 14:10, 16:19, 17:4, 18:6). Hata

hivyo, ilikua pia inatumika kutaja kwenye vifungu vichache kama baraka (kama vile. Zab. 16:5, 23:5, 116:13; Yer. 16:7).

Tungo iliyoongezwa inapatikana kwenye toleo la King James (KJV) inarejelea ubatizo wa Yesu sio sehemu pekee ya andiko asilia la Kiyunani la Mathayo, wala Kilatini cha kale, Kishamu, au tafsiri ya Koptiki. Inatokana na Marko 10:38 na Luka 12:50, ambayo baadae iliingizwa katika Mathayo na mtu anayenakili kama nyongeza ile ile kwenye Mt. 20:23. Toleo la UBS<sup>4</sup> limeondoa kiasi chake kama "A" (halitiliwi mashaka).

**20:23 "Hakika mtakinywea kikombe changu"** Yakobo alikua shahidi wa kwanza kupata mateso katika kundi la kitume (kama vile Mdo. 12:2). Yohana aliishi muda mrefu hadi alichukuliwa uhamishoni kwenda Patmo na utawala wa Kirumi (Ufu. 1:9) na alikufa akiwa mzee huko Efeso (kulingana na desturi za kanisa).

Toleo la KJV limeongeza tungo, "na kubatizwa kwa ubatizo niliobatizwa mimi," lakini ni nyongeza kutoka Marko 10:39. Waandishi wanafanya mwelekeo wa injili kuwa mfanano!

☐ **"bali watapewa waliowekewa tayari na Baba yangu"** hii ni kauli timilifu tendwa elekezi ya hali ya kuendelea. Huu ni mfano mwingine wa utiifu wa Yesu kwa mapenzi ya Baba na kusudi. Baba ni mtawala wa vitu vyote (kama vile. 1 Kor. 15:27-28).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 20:24-28**

<sup>24</sup> Na wale kumi waliposikia, waliwakasirikia wale ndugu wawili. <sup>25</sup> Lakini Yesu akawaita, akasema, Mwajua ya kuwa wakuu wa Mataifa huwatawala kwa nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha. <sup>26</sup> Lakini haitakuwa hivyo kwenu; bali mtu ye yote anayetaka kuwa mkubwa kwenu, na awe mtumishi wenu; <sup>27</sup> na mtu ye yote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu; <sup>28</sup> kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi.

**20:24 "Na wale kumi waliposikia, waliwakasirikia wale ndugu wawili"** walikuwa wamekasilika kwa sababu hawakuuliza wao kwanza! Lakini pia walionyesha hasira kama ingawa walijua swali halikua sahihi lakini kwa siri walitaka kuuliza swali hilo hilo.

**20:26 "bali mtu ye yote anayetaka kuwa mkubwa kwenu, na awe mtumishi wenu"** Yesu hakuwashutumu kwa tamaa ya makuu kwa ajili ya ukubwa, lakini maelezo ni kigezo cha kweli kwenye nuru ya mmoja anapomkiri yeye. Kwenye ufalme wa Yesu uongozi ni utumishi (kama vile Mt. 23:11; Marko 9:35; 10:43)! Waaminio wameokolewa ili watumike! Waaminio wameokolewa kutoka kuitumikia dhambi ili wamtumikie Mungu (kama vile. Warumi 6)!

**20:28 "kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika"** hapa ni utendaji wa kweli wa nani ni mkuu (kama vile Marko 10:45; Luka 19:10). Yesu alitambua kwamba alikuja (1) kumfunua Baba; (2) kutoa mfano wa ubinadamu (yaani, huduma ya kujitoa) unaotakiwa kufuatwa; na (3) kufa kifo cha mbadala

☐ **"na kutoa nafsi yake"** kuna gharama ya kulipa kwa ajili ya ukuu wa kiroho na mwishowe wakati mwingine kwenye huduma, ambayo hutoa maisha yako kwa ajili ya rafiki (kama vile Yn. 15:13; 2 Kor. 5:14-15; 1 Yn. 3:16).

☐ **"fidia"** neno hili (*lytron*) linapatikana mara mbili pekee kwenye Agano Jipya, hapa na Marko 10:45, inadokeza kulipa gharama ili kumnunua mtumwa au mfungwa wa kivita. Limetumika kwenye toleo la LXX kutafsiri *koper* (BDB 497 I), ambalo humaanisha maisha yatolewayo ili kufunika dhambi (yaani, Hes. 35:31,32). Yesu alitenda wakati mwingine kwa ajili ya waaminio kwamba na wao kamwe wasitende kwa ajili yao wenyewe. Gharama hulipwa ili kupatanisha haki ya Mungu na upendo wa Mungu (kama vile Isa. 53; 2 Kor. 5:21).

## MADA MAALUM: FIDIA/KOMBOA

### AGANO LA KALE

- A. Kuna maneno mawili ya kimsingi ya sheria ya Kiebrania yanayoeleza dhana hii.
1. *Ga'al* (BDB 145 I, KB 169 I), ambalo kimsingi linamaanisha "kuwa huru kwa maana ya ile gharama iliyolipwa." Muundo wa neno *go'el* unaongeza dhana ya mpatanishi binafsi, mara nyingi huwa mmoja wa familia (yaani, mkombozi wa ndugu wa damu). Hiki kipengele cha kiutamaduni cha haki ya kununua vitu tena, wanyama, ardhi (kama vile Mambo ya Walawi 25,27), au ndugu na (kama vile Ruthu 4:14; Isa. 29:22) hili linaawilishwa kitheolojia hadi kwa ukombozi wa YHWH kwa Israeli kutoka Misri (kama vile Kut. 6:6; 15:13; Zab. 74:2; 77:15; Yer. 31:11). Huyu amekuwa "Mwokozi" (kama vile Ayubu 19:25; Zab. 19:14; 78:35; Mit. 23:11; Isa. 41:14; 43:14; 44:6,24; 47:4; 48:17; 49:7,26; 54:5,8; 59:20; 60:16; 63:16; Yer. 50:34).
  2. Neno *Padah* (BDB 804, KB 911), ambalo kimsingi linamaanisha "kuokoa" au "kusaidia."
    - a. ukombozi wa mzaliwa wa kwanza (Kut. 13:13-15 na Hes. 18:15-17)
    - b. ukombozi wa kimwili unatofautishwa na ukombozi wa kiroho (Zab. 49:7,8,15)
    - c. YHWH ataikomboa Israeli katoka katika dhambi na uhasi wao (Zab. 130:7-8)
- B. Dhana ya kitheolojia inahusisha mambo kadhaa yanayohusiana.
1. Kuna uhitaji, utumwa, unyanganywaji, kifungo.
    - a. Kimaumbile
    - b. Kijamii
    - c. kiroho (kama vile Zab. 130:8)
  2. Gharama lazima ilipwe kwa ajili uya ukombozi, msamaha, na urejesho.
    - a. Juu ya taifa la Israeli (kama vile Kut. 7:8)
    - b. Juu ya mtu binafsi (kama vile Ayubu 19:25-27; 33:28; Isaya 53)
  3. Lazima mtu atende kama msuluishi na mtenda mema. Ndani ya *ga'al* mara nyingi huyu ni mmoja wa familia au ndugu wa karibu (i.e., *go'el*, BDB 145).
  4. Mara nyingi YHWH anajibainisha katika maneno ya kifamilia.
    - a. Baba
    - b. Mme
    - c. Ndugu wa karibu kama Mkombozi/ Ukombozi wa Mlipa kisasi aliyesalimishwa kupitia nguvu binafsi ya YHWH; gharama ililipwa, na ukombozi ulikamilishwa!

### AGANO JIPYA

- A. Kuna maneno kadhaa yaliyotumika kueleza dhana ya kitheolojia.
1. *Agorazō* (kama vile 1 Kor. 6:20; 7:23; 2 Pet. 2:1; Ufu. 5:9; 14:3-4). Hili ni neno la kibiashara ambalo linaakisi juu ya ile gharama iliyolipwa kwa ajili ya kitu fulani. Sisi ni watu tulionunuliwa kwa damu tusioyandesha maisha yetu wenyewe. Sisi ni wa Kristo.
  2. *Exagorazō* (kama vile Gal. 3:13; 4:5; Efe. 5:16; Kol. 4:5). Hikli pia ni neno la kibiashara. Hili linaakisi juu ya kifo halisi cha Yesu kwa ajili yetu. Yesu aliiondoa ile "laanae" utedaji uliojikita ndani ya sheria yaani, Sheria ya Musa, kama vile Efe. 2:14-16; Kol. 2:14), ambayo wanadamu wenye dhambi wasingaitimiliza. Yeye aliiondoa laana (kama vile Kumb. 21:23) kwa ajili yetu sote (kama vile Marko 10:45; 2 Kor. 5:21)! Katika Yesu, Haki na pendo la Mungu huungana katika msamaha kamili, ukubalifu, na upenyo!
  3. *Luō*, "kuweka huru"
    - a. *Lutron*, "gharama iliyolipwa" (kama vile Mt. 20:28; Marko 10:45). Haya ni maneno yenye nguvu kutoka ndani ya kinywa cha Yesu mwenyewe kuhusiana na kusudi la ujio Wake, kuwa Mwokozi wa ulimwengu kwa kulipa deni la dhambi isiyompasa (kama vile Yohana 1:29)
    - b. *Lutroō*, "kuwekwa huru"
      - 1) kuikomboa Israeli (Luka 24:21)

- 2) kujitoa mwenyewe kwa ajili ya kuwakomboa na kuwatakasa watu (Tito 2:14)
  - 3) Kuwa wasi na dhambi badala yake (1 Pet. 1:18-19)
  - c. *Lutrōsis*, "ukombozi," "wokovu," au "uhuru"
    - 1) Unabii wa Zakaria kumhusu Yesu, Luka 1:68
    - 2) Sifa za Anna kwa Mungu kwa ajili ya Yesu, Luka 2:38
    - 3) Ubora wa Yesu, alipojitoa sadaka, Ebr. 9:12
  4. *Apolytrōsis*
    - a. ukombozi katika Ujio wa Mara ya Pili (kama vile Matendo 3:19-21)
      - 1) Luka 21:28
      - 2) Warumi 8:23
      - 3) Waefeso 1:14; 4:30
      - 4) Waebrania 9:15
    - b. Ukombozi katika kifo cha Kristo
      - 1) Warumi 3:24
      - 2) 1 Wakorintho 1:30
      - 3) Waefeso 1:7
      - 4) Wakolosai 1:14
  5. *Antilytron* (kama vile 1 Tim. 2:6). Hili ni andiko la maana sana (kama ilivyo Tito 2:14) ambayo linahusianisha kujitoa kwa Yesu kwa ajili ya kifo cha msalaba. Yeye ndiye mmoja na dhambi pekee iliyokubaliwa, yeye aliyewafia "wote" (kama vile Yohana 1:29; 3:16-17; 4:42; 1 Tim. 2:4; 4:10; Tito 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14).
- B. Dhana ya kitheolojia katika Agano Jipya.
1. Mwanadamu amefungwa na dhambi (kama vile Yohana 8:34; Rum. 3:10-18,23; 6:23).
  2. Kifungo cha mwanadamu juu ya dhambia kimefunuliwa na Agano la Kale la Sheria ya Musa (kama vile Wagalatia 3) na Hotuba ya Yesu kule Mlimani (kama vile Mathayo 5-7). Matendo ya mwanadamu yamekuwa hati ya kifo (kama vile Kol. 2:14).
  3. Yesu, Mwana-Kondoo asiye na dhambi, amekuja na kufa badala yetu (kama vile Marko 10:45; Yohana 1:29; 2 Kor. 5:21). Tumenuuliwa kutoka dhambini ili tumtumikie Mungu (kama vile Warumi 6).
  4. Kwa maana hiyo wote YHWH na Yesu ni "ndugu wa karibu" wanaotenda kazi badala yetu. Hili linaendeleza zile stiari za kifamilia (yaani, baba, mume, mwana, kaka, ndugu wa karibu).
  5. Ukombozi haukuwa gharama iliyolipwa kwa Shetani (yaani, theolojia ya Enzi za Kati), bali upatanisho wa neno la Mungu na haki ya Mungu pamoja na pendo la Mungu na kujitoa kwa ukamilifu ndani ya Kristo. Pale msalabani amani ilirejeshwa, uasi wa mwandamu ulisamehewa, sura na mfano wa Mungu ndani ya mwanadamu inatenda kazi kwa ukamilifu tena katika ushirika wa karibu!
  6. Bado kuna kipengele kingine cha ukombozi kinachoendelea (kama vile Rum. 8:23; Efe. 1:14; 4:30), ambacho kinahusisha miili yetu ya ufufuo na uhusiano binafsi wa karibu sana pamoja na Mungu wa Utatu (tazama Mada Maalum: Utatu). Miili yetu iliyofufuliwa itakuwa kama mwili Wake (kama vile 1 Yohana 3:2). Yeye ana umbo-mwili, lakini mwenye sifa ya namna nyingine. Ni vigumu kutoa ufafanuzi wa fumbo la 1 Kor. 15:12-19 pamoja na 1 Kor. 15:35-58. Kwa uwazi umbo-mwili, mwili wa kidunia na kutakuwa na ule wa kimbingu, mwili wa kiroho. Yesu alikuwa na yote!

☛ **"ya wengi"** hili ni dokezo la Isa. 53:11-12. Neno "wengi" halikutumika kwenye maana ya onyo la wachache, lakini ni asili ya matokeo ya kazi ya Kristo. Walimu sheria na jamii ya Qumran walitumia neno "wengi" kwa ajili ya imani kwa jamii au kwa kuchaguliwa. Kwa kulinganisha Isa. 53:6c na 53:11d na 12e, tunaweza kuona mchezo mkuu kati ya "wote" na "wengi." Mchezo huu huu umetumiwa na Paulo kwenye Rum. 5:17-19. Mistari ya 18 na 19 ni mfanano, ambao humaanisha "wote" na "wengi" ni sitiari. Hili sio andiko la kuhakiki kwa ajili ya mitazamo mikali ya Calvin! Tazama mjadala kwenye NIDOTTE, juzuu. 1, kr. 96-97.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 20:29-34**

<sup>29</sup> Hata walipokuwa wakitoka Yeriko mkutano mkubwa wakamfuata. <sup>30</sup> Na tazama, vipofu wawili wameketi kando ya njia, nao waliposikia ya kwamba Yesu anapita, walipaza sauti, wakisema, Uturehemu, Bwana, mwana wa Daudi! <sup>31</sup> Mkutano wakawakaripia, wanyamazee. Lakini wao wakazidi kupaza sauti, wakisema, Uturehemu, Bwana, mwana wa Daudi! <sup>32</sup> Yesu akasimama, akawaita, akasema, Mnataka niwafanyie nini? <sup>33</sup> Wakamwambia, Bwana, twataka macho yetu yafumbuliwe. <sup>34</sup> Yesu akawahurumia, akawagusa macho yao; mara wakapata kuona, wakamfuata.

**20:29-34** huu ni muujiza mwingine wa uponyaji ulionyesha huruma na nguvu zake. Mathayo anaelezea tena kuwa kulikuwa na vipofu wawili walioponywa (na sio mmoja pekee kama kwenye Marko 10:46-52 na Luka 18:35-43).

**20:29 "Hata walipokuwa wakitoka Yeriko"** inatia shauku kwamba wote Mathayo na Marko (10:46-52) waliweka uponyaji huu wakati Yesu alipotoka Yeriko, ambapo Luka (18:35-43) anauweka uponyaji huu wakati Yesu anaingia. Kulikua na Yeriko ya kale na Yeriko mpya. Inawezekana mambo yote ni sahihi.

☑ **"vipofu wawili"** uponyaji wa kipofu ilikua ni ishara ya Kimasihi katika Agano la kale (kama vile Isa. 29:18; 35:5; 42:7,16,18). Yesu alikua na huruma kwa wale ambao wengine waliwatazama kama watu "waliotupiliwa mbali" (kama vile Mt. 20:31).

**20:30 "mwana wa Daudi"** tazama muhtasari katika Mt. 9:27. Mathayo ameandika kwa kulitumia jina hili la Kimasihi mara kwa mara (kama vile Mt. 1:1; 9:27; 12:23; 15:22; 20:30; 21:9,15; 22:42,45).

#### **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. katika kila muktadha ambao Yesu alizungumzia kifo chake, wanafunzi wake walijadili nini?
2. ni wapi katika Agano la kale siku ya tatu imetajwa kuhusiana na ufufuo wa Yesu?
3. je mama yake Yakobo na Yohana ana uhusiano na Yesu?
4. ni kwanini mstari wa 28 ni wa muhimu sana?
5. elezea ni kwa namna gani "wote" na "wengi" inaweza kuwa na maana ile ile.

## MATHAYO 21

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Kuingia kwa Ushindi Yerusalemu 21:1-11 (5) (9b)	Kuingia kwa Ushindi 21:1-11	Jumapili ya Matawi 21:1-11	Kuingia kwa Ushindi Yerusalemu 21:1-3 21:4-5 21:6-9 21:10 21:11	Masihi anaingia Yerusalemu 21:1-9 (5) (9b) 21:10-11
Kusafishwa kwa Hekalu 21:12-13 21:14-17	Yesu anasafisha Hekalu 21:12-17	Kusafisha Hekalu 21:12-13 21:14-17	Yesu anakwenda Hekaluni 21:12-13 21:14-15 21:16a 21:16b 21:17	Kuondolewa kwa Wafanyabiashara Kutoka hekaluni 21:12-17  (16b)
Kulaaniwa kwa Mtini 21:18-22	Mtini 21:18-19 Somo la Mtini Ulionyauka 21:20-22	Mtini unalaaniwa 21:18-22	Yesu analaani Mtini 21:18-19  21:20 21:21-22	Mtini tasa unanyauka, Imani na Maombi 21:18-22
Mamlaka ya Yesu yanahojiwa 21:23-27	Mamlaka ya Yesu Yanahojiwa 21:23-27	Mamlaka ya Yesu 21:23-27	Swali juu ya Mamlaka ya Yesu 21:23 21:24-25a 21:25b-27a 21:27b	Mamlaka ya Yesu Yanahojiwa 21:23-27
Mfano wa wana Wawili 21:28-32	Mfano wa wana wawili 21:28-32	21:28-32	Mfano wa wana Wawili 21:28-31a 21:31b 21:31c-32	Mfano wa Wana wawili  21:28-32
Mfano wa Shamba la Mizabibu na Wapangaji 21:33-44  (42b) 21:45-46	Mfano wa Wavunaji wa Zabibu wabaya 21:33-46	Mfano wa shamba la Mizabibu 21:33-41  21:42-44 21:45-46	Mfano wa wapangaji katika shamba la Mzabibu 21:33-39 21:40 21:41 21:42 21:43-44 21:45-46	Mfano wa wasimamizi Wabaya 21:33-43  (42) 21:45-46

## **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka “[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)”)**

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuwiwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA 21:1-17**

- A. Kuingia kwa ushindi kulikuwa ni kitendo cha kinabii chenye umuhimu. Chenyewe pamoja na kusafishwa kwa hekalu kulitangaza Yesu kuwa Masihi aliyehaidiwa. Matukio haya yanafananishwa na
1. Kuingia kwa shangwe, Marko 11:1-10, Luka 19:29-44, na Yohana 12:12-19
  2. kusafishwa kwa hekalu, Marko 11:15-18; Luka 19:45-47
- B. Hiki kipengele cha huu ukinzani wa Kuingia kwa shangwe. Yesu kidhahiri alikuwa anatimiliza unabii wa Zek. 9:9, Kelele za umati wa kusanyiko zilikuwa uthibitisho wa U-Masihi. Hata hivyo lazima ikumbukwe kwamba Zaburi hizi za Hallel (yaani 113-118) zilitumika kukaribishia mahujaji kila mwaka walipokuwa wakija Yerusalemu kwa ajili ya Pasaka. Ukweli kwamba walikuwa walikuwa wakiyatumia kwao lilikuwa jambo la kipekee kwenye tukio hili. Hii inaonekana kidhahiri ilionekana kama hofu ya viongozi wa kidini.
- C. Kusafishwa kwa Hekalu kunaandikwa katika Mt. 21:12-17 yawezekana ilikuwa ni kusafisha kwa mara ya pili kwa Yesu. Ya kwanza iliandikwa katika Yohana 2:13-16. Binafsi sikubaliani na utetezi wa ukosoaji wa kifasihi kwamba unaangalia kwa mbali matukio haya mawili kwa kulifanya kuwa moja. Ingawa kuna tatizo katika kuunganisha mfuatano wa Vitabu vya Injili ya Yohana, Inaonekana kuwa bora kwangu kwasababu ya tofauti kati ya hadithi hizi mbili kuendelea katika kufafisha kuwili, moja ikiwa katika huduma yake ya mapema mwanzoni na nyingine karibu na mwisho. <sup>Hii</sup> (pamoja na mifano ya Yesu ya kukataliwa kwa uongozi) kunaelezea kukua kwa uadui kwa viongozi wa kidini wa Yerusalemu.
- D. Kusafisha kwa hekalu kulikuwa na makusudi kadhaa ya kithiolojia.
1. kuelezea mamlaka ya Yesu na Wafalme
  2. kama tukio la hukumu juu ya viongozi wa Israeli (kutabiriwa kabla mnamo miaka ya 70 B.k)
  3. kama ufafanuzi wa makusudi ya hekalu kuwa nyumba ya maombi kwa watu wote (kama vile Mt. 28:19; Luka 24:46-47; Mdo 1:8)
  4. Kuleta mkabiliano kati yake Mwenyewe na viongozi wa Kiyahudi kwenye kilele ambacho kingepelekea katika kukamatwa na Kifo (kama vile Marko 10:45)
  5. kuonesha kwamba Wayahudi waliona utukufu na kuamini katika hekalu (kama vile Yereemia 7), lakini walihitajika kuchukua utukufu katika Mungu na kuamini katika Umasihi Wake na Ufalme wake (Yesu).
  6. kuandaa jukwaa kwa ajili ya kukataliwa kwa
    - a. Israeli
    - b. uongozi wa Israeli

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 21: 1-11

<sup>1</sup> Hata walipokaribia Yerusalemu, na kufika Bethfage, katika mlima wa Mizeituni, ndipo Yesu alipotuma wanafunzi wawili akiwaambia, <sup>2</sup> Enendeni mpaka kijiji kile kinachowakabili, na mara mtaona punda amefungwa, na mwana-punda pamoja naye; wafungueni mniletee. <sup>3</sup> Na kama mtu akiwaambia neno, semeni, Bwana anawahitaji; na mara huyo atawapeleka. <sup>4</sup> Haya yote yamekuwa, ili litimie neno lililonenwa na nabii, akisema,

<sup>5</sup> Mwambieni binti Sayuni Tazama,  
mfalme wako anakuja kwako,  
Mpole, naye amepanda punda,  
Na mwana-punda, mtoto wa punda.

<sup>6</sup> Wale wanafunzi wakaenda zao,  
wakafanya kama Yesu alivyowaamuru,

<sup>7</sup> wakamleta yule punda na mwana-punda, wakaweka nguo zao juu yao, naye akaketi juu yake.

<sup>8</sup> Watu wengi katika ule mkutano wakatandaza nguo zao njiani; na wengine wakakata matawi ya miti, wakayatandaza njiani. <sup>9</sup> Na makutano waliotangulia, na wale waliofuata, wakapaza sauti, wakisema,

Hosana, Mwana wa Daudi;  
ndiye mbarikiwa, yeye ajaye kwa jina la Bwana;  
Hosana juu mbinguni.

<sup>10</sup> Hata alipoingia Yerusalemu, mji wote ukataharuki, watu wakisema, Ni nani huyu? <sup>11</sup> Makutano wakasema, Huyu ni yule nabii, Yesu, wa Nazareti ya Galilaya.

**21:1 "Bethfage"** Jina hili lilimaanisha "nyumba ya mitini." Kijiji kilikuwa mahali Fulani kati ya Bethania na Yerusalemu pembezoni mwa korongo lililjulikana kama Mlima Mzeituni.

☐ **"mlima wa Mizeituni"** Haijulikani bado wapi ambapo Yesu alienda na kutumia usiku wake katika wiki ya mwisho ya maisha yake. Wengine wanaelezea kwamba alirudi Bethania na kukaa na Lazaro; wengine wanadai kwamba aliweka hema juu ya mlima wa mzeituni, yawezekana katika eneo Fulani katika bustani ya Gethsemane. Uhalisia unawezekana ukawa ni muunganiko ya vyote (kama vile Yohana 12:1-10).

**21:2-3** Hii ni moja ya hadithi zile ambazo ni aidha muujiza wa maarifa ya juu ya Yesu au ya kujua kabla. Kuna hadithi zote katika Agano Jipya. Kimuktadha inaonekana kuwa mkutano ulioandaliwa kabla.

**21:2 "punda amefungwa, na mwana-punda pamoja naye"** Katika Yohana 12:14 Punda anatajwa lakini si mwana-punda. Sababu kwamba mwanapunda ni muhimu ni kwasababu ya uwakilishi wa punda kwa Israeli. Punda lilikuwa pando la mfalme (yaani 2 Sam.18:9). Mfalme alikuwa na punda wa kifalme ambaye hakuna mtu aliyempanda. Ule ukweli kwamba Yesu alikuja akiwa kapanda katika punda hasa katika punda ambaye alikuwa hajawahi kupandwa ni kutimilizwa kwa unabii unaotajwa katika Mt. 21:5, kutoka Zek. 9:9, ikiwa na maelezo ya Isa. 62:11. Baadhi ya Maandiko ya Kiyunani ya baadaye yanaongeza "Zakaria" kabla ya "nabii," wakati maandiko yaliyohaririwa ya Vulgate na fasiri za Koptiki zinaongeza "Isaya." Punda alikuwa sio tu uwakilishi wa uaminifu bali pia mwanapunda uwakilishi wa unyenyekevu na amani.

**21:3 "na kama"** Hii ni sentensi daraja la tatu yenye masharti ambayo inaashiria kitendo kinachoweza kutokea.

**21:5** Hiii ni nukuu kutoka Isa. 62:11 na Zakaria 9:9.

**21:7 "wakamleta yule punda na mwana-punda, wakaweka nguo zao juu yao, naye akaketi juu yake"** Hili tendo la kuweka nguo zao kwa wanyama wawili ni kama sana kufanana kama sherehe zetu za kubebe mizigo wakati wa



gwaride. Ni dhahiri kwamba Yesu alipanda juu ya punda ingawa maandiko ya Kiyunani kwa namna Fulani ni tata. "wao" katika maandiko ya Kiyunani inarejerea kwa nguo kwenye wanyama wote wawili na sio wanyama wenyewe.

**21:8 "wakatandaza nguo zao njiani;"** Huku Kulikuwa ni kipengele kingine cha gwaride la kifalme ambalo linafanana na yale yanayotendeka kwetu juu ya "kutembea katika zulia jekundu" kwa wale wagen wanaopewa hadhi ya juu sana tofauti na wengine. Kuna hata maelezo ya kihistoria kwa kitendo hiki hiki kinachofanywa kwa (1) Yehu katika 2 Wafalme 9:13, na (2) Simon Maccabeus katika I Mac. 13:51 katika II Mac. 10:7.

☞ **"na wengine wakakata matawi ya miti, wakayatandaza njiani"** Ingawa kitendo hiki cha uwakilishi kilikuwa mara kwa mara kikifanyika wakati wa sherehe za Mahema (kama vile Law. 23:13-20), matawi yale yaikuwa makubwa zaidi kuliko haya. Matawi yalitumika yalikuwa madogo na yanafananishwa na desturi za kisasa za kurusha maua mbele ya bibi harusi anapokuwa akitembea katika siku yake ya harusi ukumbini. These three acts Haya matendo matatu: (1) nguo juu ya wanyama, (2) nguo barabarani, na (3) matawi ambayo yalitandazwa katika barabara kuonesha kwamba alikuwa wakiheshimu Yesu kama mfalme wa Ukoo wa Daudi ajaye (Masihi).

**21:9 "Na makutano waliotangulia, na wale waliofuata, wakapaza sauti"** Neno "kupiga kelele" ni njeo ya wakati usio timilifu ambayo inamaanisha kwamba walipaza sauti kwa kurudia rudia. Nukuu inatoka katika Zab. 118:26-27. Ilikuwa ni sehemu ya Liturujia ya Pasaka iliyokuwa ikijulikana kama Zaburi za Hallel (kama vile Zab. 113-118). Hizi zilikuwa zikitumika kila mwaka katika sehemu ambapo njia ilitokezea Yerusalemu kuwakaribisha mahujaji kwenye sherehe za Pasaka lakini kwa mwaka huu kulikuwa na matarajio ya kipekee katika utu wa Yesu. Mistari hii ilitumika kipekee kwa ajili yake!. Alikuwa utimilifu wao!

**NASB, NKJV**

**NRSV, NJB** "Hosanna"  
**TEV** "Sifa kwa"

Neno linaweza kuwa ni nahau ya Kiaramu ikimaanisha "nguvu ya kifalme kwa." Kibayana neno hili katika Kiebrania lilikuwa "*Hosanna*" (BDB 446, kama vile Zab. 118:25), ambayo ilikuja kutumika kama salamu iliyo zoeleka. Kiasili ilimaanisha "tuokoe sasa." Matumizi ya kwanza yalirejerea kwa Yesu na ya pili (Zab. 118:26; Mt. 21:10) kwa Mungu baba, wakimsifu yeye kwa kumtuma Masihi.

☞ **"juu mbinguni"** Hili lilikuwa ni neno la kuzunguka ila likimaanisha mbinguni au uwepo wa Mungu.

☞ **"Mwana wa Daudi"** Cheo hiki kilikuwa cha Kimasihi (kama vile Mt. 9:27; 12:23; 15:22; 20:30,31; 22:42). Haya yalikuwa ni maelezo ya 2 Samwelil 7, ambayo yalitabiri kwamba siku zote kungekuwa na uzao wa Daudi katika kiti cha ufalme. Huku kulikuwa ni kutimiizwa kwa kimakusudi kwa Masihi kutokea katika kabila la Yuda (kama vile Mwa 49:10; Zab. 60:7; 108:8).

☞ **"ndiye mbarikiwa, yeye ajaye kwa jina la Bwana"** Mfanano wa Luka unaongeza "Huyo ambaye ni Mfalme" na hiki ndicho kilichokuwa kinamaanishwa kwa uwazi.

**21:10 "Hata alipoingia Yerusalemu, mji wote ukataharuki, watu wakisema, Ni nani huyu?"** Ni kweli kwamba watu wengi walikuwa wamekwisha kusikia juu ya kazi za ajabu za Yesu na wakimpa sifa za cheo cha nabii (kama vile Mt. 21:11). Lakini ilihitajika kwa uwazi kufunuliwa kwamba hakuwa tu ni nabii bali Masihi aliyetabiriwa. Matukio ambayo yanafuata kwa uwazi yatafunua hili kwa mtu yoyote kwamba hakuwa tu nabii bali nabii aliyetabiriwa.

Katika hili Luka 19:41-44 inaingiza juu ya Yesu kuomboleza juu ya mji wa Yerusalemu; hata hivyo Mathayo haiandiki hili mpaka 23:37-39. Waandishi wa injili walikuwa na uwezo chini ya uvuvio kuchagua, kuasili, kupangilia na kuweka muhtasari maneno ya Yesu na mafundisho. Injili sio historia ya kimitiririko wa kimagharibi bali machapisho ya kithiolojia kuweza kuwapata waliopotea na kuwafundisha waliokolewa.

**21:11 "Makutano wakasema, Huyu ni yule nabii, Yesu"** Kule kutambua uvuvio wa Yesu wa kiungu na nguvu inafanana na unabii wa Kimasihi wa Kumb 18:15-19. Watu kwa bure walikubali kwamba Yesu alikuwa nabii wa Mungu (kama vile Luka 7:16; 24:19; Yohana 4:19; 6:14; 7:40; 9:17). Mukadha huu pia ulielezea Umasihi wake. Angalia [MADA MAALUM: UNABII WA AGANO JIPYA](#) katika Mt. 11:9.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 21:12-13**

<sup>12</sup> Yesu akaingia ndani ya hekalu, akawafukuza wote waliokuwa wakiuza na kununua hekaluni, akazipindua meza za wabadili fedha, na viti vyao waliokuwa wakiuza njiwa; <sup>13</sup> akawaambia, Imeandikwa, Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala; bali ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi.

**21:12 "Yesu akaingia ndani ya hekalu, akawafukuza wote waliokuwa wakiuza na kununua hekaluni, akazipindua meza za wabadili fedha, na viti vyao waliokuwa wakiuza njiwa"** Huku kulikuwa ni kusafisha hekalu kwa mara ya pili (kama vile Yohana 2:15). Kuhani mkuu na familia yake walikuwa wamiliki wa vibanda hivi vya kibiashara. Walinunua haki kutoka kwa mamlaka ya Kirumi. Kwa asili walikuwa wameanzisha msaada kwa wale mahujaji kutoka katika maeneo ya kigeni ambao walikuwa hawana uwezo wa kuja na wanyama wa kutolea dhabihu na kiasi sahihi cha fedha (shekeli) ambacho kilikuwa kinatajikana na hekalu. Vibanda hivi vililiisha gharama za juu sana za kushangaza. Ikiwa mtu ameleta mnyama wake mwenyewe, wakaguzi wa kikuhani wangetafuta madhaifu na makosa ndani yake ili kwamba waweze kununua wanyama kutoka katika waendeshaji wa vibanda kwa gharama iliyopandishwa juu kikweli kweli.

Hekalu ilikuwa inapokea shekeli pekee (kama vile Kut. 30:13). Mpaka kulifikia hatua ambayo kulikuwa hakuna tena shekeli za Kiyahudi zilizokuwa zinapatikana lakini zilikuwapo zile za Tiro. Mahujaji walilipishwa gharama za juu kwa kuweza kupata sarafu hizi. Njiwa walikuwa ni kwa ajili ya masikini wa hali ya chini kabisa ambao hawakuwa na uwezo wa kutoa dhabihu (kama vile Law. 1:14; 5:7,11; 12:8; 14:22; Luka 2:24), Lakini Wakuu wa makuhani walikuwa wanawatoza gharama za kutisha sana hata wao.

Hii ilikuwa ni mfano wa hasira ya Yesu katika unyanyasaji wa kidini uliokuwa unafanywa na viongozi wa Kiyahudi katika Siku zake. Ikiwa dhambi ilikuwa ni dhambi basi Yesu angekuwa ametenda dhambi (kama vile Efe. 4:26).

**21:13 "Imeandikwa, Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala"** Kuuza huku na kununua kulifanyikia katika mahakama ya Mataifa ambayo ilimaanisha kuwa sehemu ya kuvutia mataifa katika ibada za YHWH. Yesu alinukuu Isa. 56:7 na kufanya maelezo kwa Yer. 7:11. Katika ufanano wa Marko (kama vile Mt. 11:17), anaongeza Tungo, itaitwa nyumba ya sala kwa mataifa yote. Mathayo, akiwaandikia Wayahudi, aliacha msisitizo huu wa kijumla wakati Marko akiandika kwa Warumi alijumuisha ndani.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 21:14-17**

<sup>14</sup> Na vipofu na viwete wakamwendea mle hekaluni, akawaonya. <sup>15</sup> Lakini wakuu wa makuhani na waandishi walipoyaona maajabu aliyoyafanya, na watoto waliopaza sauti zao hekaluni, wakisema, Hosana, Mwana wa Daudi! Walikasirika, <sup>16</sup> wakamwambia, Wasikia hawa wasemavyo? Yesu akawaambia, Naam; hamkupata kusoma, Kwa vinywa vya watoto wachanga na wanyonyao umekamilisha sifa? <sup>17</sup> Akawaacha, akatoka nje ya mji mpaka Bethania, akalala huko.

**21:14 "Na vipofu na viwete wakamwendea mle hekaluni, akawaonya"** Mistari ya 14 na 15 ni ya pekee kwa Mathayo, lakini inaonyesha kwamba hata katika nyakati hizi zilizoendelea sana, Yesu alikuwa akijaribu kuthibitisha

ujumbe wake kwa viongozi wa kidini kwa kufanya miujiza kuitia matendo ya upendo na huruma katika maeneo ya hekalu. Hizi zilikuwa ni ishara za Agano la Kale za Masihi.

1. kuwafumbua macho vipofu (kama vile Isa. 29:18; 42:7,16)
2. kuwasaidia viwete (kama vile Isa. 40:11; Mik. 4:6; Sef. 3:19)
3. Dalili zote kwa pamoja katika Yer. 31:8 na Isa. 35:5-6

Ikiwa walikuwa na macho ya kiroho ya kuona, wangukuwa wameona mamlaka yake, huruma, kutimilizwa kwa unabii wa Agano la Kale lakini hawakujua.

**21:15 "Lakini wakuu wa makuhani na waandishi"** Maelezo ya kila siku ya Wakuu wa Sinagogi (angalia Mada Maalum katika Mt. 20:18) ambayo ingejumuisha wakuu wa makuhani, waandishi na wazee (kama vile Mt. 21:23; 16:21). Hii ilikuwa ni njia ya kurejerea kwa wale katika nafasi za uongozi katika siku za Yesu.

☐**"na watoto waliopaza sauti zao hekaluni, wakisema, Hosana, Mwana wa Daudi! Walikansirika"** Inavyonekana watoto (lilitumika na Yesu juu ya Kumi na Mbili, kama vile Luka 2:43) walikuwa wamekwisha sikia Zaburi za Hallel zikitumiwa juu ya Yesu siku moja kabla na walikuwa wanarudia ambacho kilikuwa kimewakwaza hapo kabla.

**21:16 "wakamwambia, Wasikia hawa wasemavyo?"** Katika Luka 19:39 Mafarisayo wengine walilalamikia kuhusu jambo hili hili. Yesu alikubaliana na majina haya kama njia nyingine ya kukiri madai ya Kimasihi.

☐**"Yesu akawaambia, Naam; hamkupata kusoma"** Hii ilikuwa ni kauli ya nguvu sana iliyomaanisha kwamba hawakujua hata kwa kutumia mandiko yao wenyewe. Yesu alizungumza kinyume na kejeli mara kadhaa kwa viongozi wa kidini (kama vile Mt. 12:3; 19:4; 21:42; 22:31). Yesu katika hatua hii alinukuu Zab. 8:2. Hii haikuwa hasa Zaburi ya Kimasihi, bali ilikuwa ni zaburi iliyoelezea kwamba watoto (wale wanaotunzwa bado, yawezekana hata mpaka miaka mitatu au zaidi kidogo) watazungumza kweli mbele ya wakubwa nao wataelewa.

**21:17 "Akawaacha, akatoka nje ya mji mpaka Bethania, akalala huko."** Katika Yohaha. 12:1-10, Yesu alikaa pamoja na Lazaro, Mariamu na Martha kwa usiku kadhaa wakati wa wiki ya mwisho wa maisha wake.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini kuingia kwa Shangwe ni muhimu sana?
2. Kwanini ni muhimu kwamba Yesu alipanda mwana-punda?
3. Elezea umuhimu wa Zaburi 118:26-27. Nini kilikuwa ni upekee wa gwaride la ukaribisho wa mwaka huu?
4. Kwanini Yesu alikansirishwa na wanunuzi na wauzaji katika Hekalu?
5. Kwanini viongozi wa dini hawakufurahia katika miujiza ya Yesu?

## TAMBUZI ZA MUKTADHA KWA 21:18-46

- A. Mathayo 21 inaanza na kuingia kwa shangwe na kufunga na mifano mitatu ya pili. Ilikuwa ni jaribu la kujadili Umasihi wa Yesu na viongozi wa Kiyahudi.
- B. Ni ngumu zaidi sana kuwa na hakika ikiwa Yesu alikuwa anakataa (1) taifa la Uyahudi, (2) viongozi wake, au (3) vyote viwili.
- C. Kusafishwa kwa helaku katika Mt. 21:12-17 lilikuwa ni kitendo cha kukataliwa. Kulaaniwa kwa mtini katika mistari ya 18-22 kilikuwa ni kitendo cha kukataliwa. Mfano wa wana wawili katika Mt. 21:28-32 ilikuwa ni mfano wa kukataliwa. Mfano wa mwangalizi muovu, Mt. 21:33-46, ilikuwa ni mfano wa kukataliwa.

Mfano wa sherehe za harusi za mfalme, Mt. 22:1-14, ilikuwa ni mfano wa kukataliwa. Swali linabakia, je viongozi walikuwa uwakilishi wa mataifa yote au ilikuwa ni desturi za sheria za Kiyahudi na hasa kwamba Yesu alikuwa anakataliwa?

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 21: 18-19

<sup>18</sup> Hata asubuhi alipokuwa akienda mjini, aliona njaa. <sup>19</sup> Akaona mtini mmoja kando ya njia, akauendea, asione kitu juu yake ila majani tu; akauambia, Yasipatikane matunda kwako tangu leo hata milele. Mtini ukanyauka mara.

**21:18 "Hata asubuhi alipokuwa akienda mjini"** Mfuatano wa muda katika Marko unaweka utofautiano kidogo sana (kama vile Marko 11:12-14, 20-21). Inavyoonekana Yesu alikuwa narudi kutokea Bethania ambayo ilikuwa ni maili mbili kutokea Yerusalemu (kama vile Marko 11:12).

**21:19 "Akaona mtini mmoja kando ya njia, akauendea"** Ilikuwa ni sawa kisheria kwa msafiri kupumzika na kula chakula akiwa ameketi chini ya mti wa matunda au shamba na kula vyakula vya mtini na shambani (kama vile Kumb. 23:24-25).

☐ **"asione kitu juu yake ila majani tu"** Marko 11:13 inaongeza "haukuwa msimu wa mtini." Hii inafanya tendo la kinabii la kukataliwa kwa viongozi wa Kiyahudi au wa taifa. Kwa nje walionekana matajiri, kiroho na watu wa dini lakini walikuwa hawana tunda la kiungu (kama vile Kol. 2:21-23; 2 Tim. 3:5; Isa. 29:13).

☐ **"Yasipatikane matunda kwako tangu leo hata milele"** Yesu alizungumza Kiaramu lakini alifikiri kwa namna ya Kiebrania. Angalia Mada Maalum inayofuatia kwa maneno "milele" au "milele yote" niliyochukua kutoka katika fasiri yangu.

### MADA MAALUMU: MILELE ('*olam*)

Maelezo ya asili ya neno la Kiebrania 'olam, עולם (BDB 761, KB 798) hayajulikani (NIDOTTE, juzuu. 3, uk. 345). Yametumika katika maana mbali mbali (mara nyingi yanapimwa na maudhui). Ifuatayo ni mifano iliyochaguliwa tu.

1. vitu vya kale
  - a. watu, Mwa. 6:4; 1 Sam. 27:8; Yer. 5:15; 28:8
  - b. mahari, Isa. 58:12; 61:4
  - c. Mungu, Zab. 93:2; Mith. 8:23; Isa. 63:16
  - d. Vitu, Mwa. 49:26; Ayubu 22:15; Zab. 24:7,9; Isa. 46:9
  - e. muda, Kumb. 32:7; Isa. 51:9; 63:9,11
2. mda/ wakati ujao future time
  - a. maisha ya mtu, Kut. 21:6; Kumb. 15:17; 1 Sam. 1:22; 27:12
  - b. heshima ya hali ya juu kwa mfalme, 1 Fal. 1:31; Zab. 61:7; Neh. 2:3
  - c. uwepo endelevu
    - 1) dunia, Zab. 78:69; 104:5; Mhu. 1:4
    - 2) mbinguni, Zab. 148:5
  - d. uwepo wa Mungu
    - 1) Mwa. 21:33
    - 2) Kut. 15:18
    - 3) Kumb. 32:40
    - 4) Zab. 93:2

- 5) Isa. 40:28
- 6) Yer. 10:10
- 7) Dan. 12:7
- e. Agano
  - 1) Mwa. 9:12,16; 17:7,13,19
  - 2) Kut. 31:16
  - 3) Ufu. 24:8
  - 4) Hes. 18:19
  - 5) 2 Sam. 23:5
  - 6) Zab. 105:10
  - 7) Isa. 24:5; 55:3; 61:8
  - 8) Yer. 32:40; 50:5
- f. Agano maalumu na Daudi
  - 1) 2 Sam. 7:13,16,25,29; 22:51; 23:5
  - 2) 1 Fal. 2:33,45; 9:5
  - 3) 2 Nya. 13:5
  - 4) Zab. 18:50; 89:4,28,36,37
  - 5) Isa. 9:7; 55:3
- g. Masihi wa Mungu
  - 1) Zab. 45:2; 72:17; 89:35-36; 110:4
  - 2) Isa. 9:6
- h. Sheria za Mungu
  - 1) Kut. 29:28; 30:21
  - 2) Ufu. 6:18,22; 7:34; 10:15; 24:9
  - 3) Hes. 18:8,11,19
  - 4) Zab. 119:89,160
- i. Ahadi za Mungu
  - 1) 2 Sam. 7:13,16,25; 22:51
  - 2) 1 Fal. 9:5
  - 3) Zab. 18:50
  - 4) Isa. 40:8
- j. Uzao wa Abrahamu na nchi ya ahadi
  - 1) Mwa. 13:15; 17:19; 48:4
  - 2) Kut. 32:13
  - 3) 1 Nya. 16:17
- k. Sikukuu za ahadi
  - 1) Kut. 12:14,17,24
  - 2) Ufu. 23:14,21,41
  - 3) Hes. 10:8
- l. umilele, kudumu milele
  - 1) 1 Fal. 8:13
  - 2) Zab. 61:7-8; 77:8; 90:2; 103:17; 145:13
  - 3) Isa. 26:4; 45:17
  - 4) Dan. 9:24
- m. Zaburi inasema yapi yanayowapasa kufanya milele
  - 1) kushukuru, Zab. 30:12; 79:13
  - 2) kudumu katika uwepo Wake, Ps. 41:12; 61:4,7
  - 3) amini katika huruma zake, Zab. 52:8
  - 4) kumsifu Bwana, Zab. 52:9
  - 5) imba nyimbo za sifa, Zab. 61:8; 89:1

- 6) tangaza haki zake, Zab. 75:7-9
- 7) tukuza jina lake, Zab. 86:12; 145:2
- 8) baliki jina lake, Zab. 145:1
- n. linatumiwa na Isaya kueleza enzi mpya
  - 1) agano la milele, Isa. 24:5; 55:3; 61:8
  - 2) YHWH kama mwamba wa milele, Isa. 26:4
  - 3) furaha ya milele, Isa. 35:10; 51:11; 61:7
  - 4) Mungu wa Milele, Isa. 40:28
  - 5) Wokovu wa milele, Isa. 45:17
  - 6) Wema wa milele, Isa. 54:8
  - 7) Ishara ya milele, Isa. 55:13
  - 8) Jina la milele, Isa. 56:5; 63:12,16
  - 9) Nuru ya milele, Isa. 60:19,20

Matumizi yenye hali ya ukanushi kuhusiana na adhabu ya milele kwa waharifu inapatikana katika Isa. 33:14, "moto wa milele." Isaya kila wakati anatumia "moto" kuelezea hasira ya Mungu (kama vile. Isa. 9:18,19; 10:16; 47:14), lakini katika Isa. 33:14 "ndipo anasema wa milele"

- 3. Wakati wa kurudi nyuma na kwenda mbele ("toka milele hadi milele")
  - a. Zab. 41:13 (sifa kwa Mungu)
  - b. Zab. 90:2 (Mungu pekee)
  - c. Zab. 103:17 (huruma zake)

Kumbuka, muktadha huamua maudhui ya maana ya neno. Maagano ya ahadi za milele ni ya masharti (yaani, Yeremia 7, tazama Mada Maalumu: Agano). Kuwa mwangalifu unaposoma maoni ya kisasa kuhusu muda au Agano Jipya la theolojia iliyopangwa katika matumizi ya kila siku ya neno hili dhaifu katika Agano la Kale. Kumbuka pia, Agano Jipya linajumuisha ahadi zote za Agano la kale (tazama Mada Maalumu: utabiri wa mambo yajayo ya Agano la Kale dhidi ya utabiri wa mambo yajayo ya Agano Jipya.).

☐ **"Mtini ukanyauka mara"** Marko 11:20 inaandika kwamba kunyauka kulitokea asubuh iliyofuatia. Kuna mfano unaofanana katika Luka 13:6-9. Hili lilikuwa ni somo dhidi ya mitazamo ya kidini isiyosawa ya viongozi wa Kiyahudi na kukosekana kwa upendo kuletako chukizo na kujizatiti kwa Mungu.

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 21: 20-22**

<sup>20</sup> Wanafunzi walipoona, walistaajabu, wakisema, Jinsi gani mtini umenyauka mara? <sup>21</sup> Yesu akajibu, akawaambia, Amin, nawaambia Mkiwa na imani, msipokuwa na shaka, mtafanya si hilo la mtini tu, lakini hata mkiuambia mlima huu, Ng'oka, ukatupwe baharini, litatendeka. <sup>22</sup> Na yo yote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea.

**21:21 "Amini"** Angalia dokezo katika Mt. 5:18.

☐ **"mkiwa"** Hii ni sentensi daraja la tatu yenye masharti ambayo ilimaanisha kitendo kinachowezekana kutukia.

☐ **"Mkiwa na imani, msipokuwa na shaka"** Maudhui haya ni muhimu (kama vile Mt. 17:20; Yakobo 1:6-8) kwasababu ya zama mpya ya Roho ni tofauti na zama ya sasa ya uovu. Ni kizazi cha imani/kumtumaini Mungu, neno Lake na Mwanawe! Mstari huu haufanani na mapenzi binafsi ya waaminio mmoja mmoja bali mapenzi ya Mungu yanayofunuliwa katika maisha! Israeli ilishindwa jaribu la imani! Kulikuwa na madhara kwa kushindwa huku! Tukio hili linaafanana na kusafishwa kwa hekalu mwanzoni katika sura.

☐ **"mlima huu"** Hii inarejerea juu ya Mlima Mzeituni ambao ungeweza kuwa sehemu nzuri ya kutazamia.

☑️**"baharini"** Hii inarejerea Bahari ya Chumvi pia inayoonekana kutoka Mlima Mzeituni. Katika Agano la Kale tendo hilli la kusawazisha mlima na kuinua mabonde ilikuwa inahusianishwa na Mataifa kupewa nafasi ya kukubalika kimwili kwa YHWH katika Yerusalemu. Mukatadha sasa unatakiwa kufasiriwa kama nguvu ya usaidizi wa kimujiza kupitia imani bali ni kinahau juu ya kukubalika kiroho kwa Mungu kwa Mataifa ambacho viongozi wa Kiyahudi kwa matendo yao walikuwa wenye shingo ngumu (yaani, mahakama ya mataifa kimsingi ndio iliyotumika kama vibanda vya wafanyabiashara). Mukatadha huu lazima uonwe kama moja ya mfululizo wa vifungu vinavyokataa (Mt. 21:12-17, 28-32, 33-46; 22:1-14).

**21:22 "Na yo yote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea"** Tazama ahadi isiyokuwa na masharti ikiunganishwa na mwitikio wenye masharti. Hii ilikuwa njia iliyozeleka ya kuelezea ukweli wa kibiblia lakini ni ngumu kwa watu waliojikita kimagharibi wapendao majibu na kauli nyeupe na nyeusi za mkato kushughulikia ukinzani wa kibiblia na kilahaja. Maombi yaliyojibiwa lazima yaunganishwe katika mapenzi ya Mungu na imani ya mwanadamu (linganisha Mt. 18:19; Yohana 14:13-14; 15:7,16; 16:23; 1 Yohana 3:22; 5:14-15 pamoja na Mt. 7:7-8; Luka 11:5-13; 18:1-8; 18:9-14; Marko 11:23-24; na Yakobo 1:6-7; 4:3).

Jambo baya zaidi kuliko yote ambalo Mungu angeweza kulifanya kwa watoto wasio na imani ni kujibu maombi yao ya ubinafsi, yenye maombi ya umiliki wa mali. Wale Waaminio wanaotafuta ufahamu wa Kristo huomba vitu ambavyo vinampendeza Mungu na kupanua ufalme wake. Angalia Mada Maalum juu ya Maombi katika Mt. 18:19.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 21: 23-27**

<sup>23</sup> Hata alipokwisha kuingia hekaluni, wakuu wa makuhani na wazee wa watu wakamwendea alipokuwa akifundisha, wakasema, Ni kwa amri gani unatenda mambo haya? Naye ni nani aliyekupa amri hii? <sup>24</sup> Yesu akajibu akawaambia, Na mimi nitawauliza neno moja; ambalo mkinijibu, nami nitawaambia ni kwa amri gani ninatenda haya. <sup>25</sup> Ubatizo wa Yohana ulitoka wapi? Ulitoka mbinguni, au kwa wanadamu? Wakahojiana wao kwa wao, wakisema, Tukisema, Ulitoka mbinguni, atatuambia, Mbona basi hamkumwamini? <sup>26</sup> Na tukisema, Ulitoka kwa wanadamu, twaogopa mkutano; maana watu wote wamwona Yohana kuwa ni nabii. <sup>27</sup> Wakamjibu Yesu wakasema, Hatujui. Naye akawaambia, Wala mimi siwaambii ninyi ni kwa amri gani ninatenda haya.

**21:23 "wakuu wa makuhani na wazee wa watu"** Tazama katika mistari ya 15 wanaitwa "wakuu wa makuhani" na "waandishi." Haya makundi matatu yanaundwa na wakuu wa baraza la Sinagogi. Ikiwa walikuwa wawakilishi rasmi au wasio rasmi haijulikani, laki waliwakilisha uongozi wa Kiyahudi. The phraseTungo "wazee wa watu" ni ya pekee katika Mathayo (kama vile Mt. 21:23; 26:3,47; 27:1).

☑️**"alipokuwa akifundisha"** Yesu alifundisha chini ya lango la Suleimani (kama vile Mdo 3:11; 5:12) katika ile iliyowahi kuwa mahakama ya Mataifa ndani ya eneo la Hekalu. Alikuwa bado anajaribu kufikia uongozi wa Kiyahudi.

☑️**"Ni kwa amri gani unatenda mambo haya?"** Hili ndilo lilikuwa swali kuu! "Mambo haya" inaweza kurejerea kusafishwa kwa hekalu (kama vile Mt. 21:12-16), Kukataa kwa Yesu desturi za masimulizi ya mdomo au miujiza yake ya hadharani. Walikuwa hawawezi kukataa matendo ya kimujiza, hivyo walianza kushambulia vyanzo vyake vya Mamlaka. Inavyoonekana viongozi wa kidini wa siku za Yesu walifikiri Yesu alikuwa mtu aliyepagawa na pepo mwenye nguvu nyingi sana kupitiliza (kama vile Mt. 12:24; Marko 3:22; Luka 11:15; Yohana 7:20; 8:48,52; 10:20-21).

**21:24-27** Mjadala huu unaweka jukwaa kwa mifano mitatu inayofuata. Inaonyesha nafasi ya kukubaliana ya viongozi wa kidini katika kusalimu amri. Watu hawa wamekuwa wakijaribu kumkanata Yesu juu ya "misingi ya mkanganyiko" kwa miezi kadhaa sasa. Sasa aliisambaratisha mbinu yao.

**21:24, 25, 26** Kuna sentensi tatu za daraja la tatu leye mashari ambalo lilimaanisha matendo ya wakati ujao.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 21: 28-32**

<sup>28</sup> Lakini mwaonaje? Mtu mmoja alikuwa na wana wawili; akamwendea yule wa kwanza, akasema, Mwanangu, leo nenda kafanye kazi katika shamba la mizabibu. <sup>29</sup> Akajibu akasema, Naenda, Bwana; asiende. <sup>30</sup> Akamwendea yule wa pili, akasema vile vile. Naye akajibu akasema, Sitaki; baadaye akatubu, akaenda. <sup>31</sup> Je! Katika hao wawili ni yupi aliyefanya mapenzi ya babaye? Wakamwambia, Ni yule wa pili. Basi Yesu akawaambia, Amin nawaambia, watoza ushuru na makahaba wanatangulia mbele yenu kuingia katika ufalme wa Mungu. <sup>32</sup> Kwa sababu Yohana alikuja kwenu kwa njia ya haki, ninyi msimwamini; lakini watoza ushuru na makahaba walimwamini, nanyi hata mlipoona, hamkutubu baadaye, ili kumwamini.

**21:28 "Mtu mmoja alikuwa na wana wawili"** Mfano huu ni pekee kwa Mathayo. Maandiko ya kale ya Kiyunani yanatofautiana katika hatua za mwitikio wa wana wawili. Hatua hakika si muhimu sana katika kuona uhusiano wa mfano huu kwa Mt. 21:23-27. Ulinganifu unatengenezwa kati ya viongozi wa kidini na watu wa kawaida wa nchi.

**21:31 "watoza ushuru na makahaba wanatangulia mbele yenu kuingia katika ufalme wa Mungu"** Hii ilikuwa ni kauli ya kushangaza kwa viongozi wa Kiyahudi wa siku za Yesu. Lazima ilikuwa imewashangaza wao kama Mt. 5:20; 8:11-12; 19:24-25,30 na 20:16 ilivyowafanya. Viongozi walitambua kwamba Yesu bila utata likuwa akizungumzia kuwakataa kwake na kuwakaribisha wenye dhambi na mtu wa kawaida (na ikimaanisha Mataifa).

Mathayo kwa kukazia alitumia neno "ufalme wa mbinguni," kwasababu alikuwa anawaandikia wasikiaji wa Kiyahudi waliokuwa wamejaa hofu ya kutumia jina la Mungu; hata hivyo katika Mt. 6:33, 12:28, na 21:31, tungo iliyozoeleka sana katika Marko na Luka ilitumika na Mathayo. Yawezekana ilitumika kushangaza Wayahudi ili wamsikilize.

**21:32 "Kwa sababu Yohana alikuja kwenu kwa njia ya haki"** Yesu na Yohana waliwakilisha mbinu mbili. Yohana alikuja na desturi za wazee na alikataliwa (Mt. 21:24-26). Yesu alikuja kama rafiki wa wenye dhambi na alikuwa anashutumwa kwa kuwa mlaghai (kama vile Mt. 11:19; Luka 7:34). Wote wawili walikataliwa!

Neno "njia" lilikuwa nahau ya Agano la Kale ya mtindo wa maisha wa imani (yaani, Kut. 32:8; Kumb. 8:6; 10:12; 11:22,28). Na ilikuwa ni jina la kwanza la kanisa, "Ile Njia" (kama vile Mdo 9:2; 19:9, 23; 22:4; 24:22).

☑"ninyi msimwamini. . . walimwamini" Nyuma ya taswira hii ni hitaji kumwamini Yesu na linawekwa wazi kwa yoyote na wanadamu wote katika sura ya Mungu!

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 21:33-41**

**33** Sikilizeni mfano mwingine. Kulikuwa na mtu mwenye nyumba, naye alipanda shamba la mizabibu, akalizungusha ugo, akachimba shimo la shinikizo ndani yake, akajenga mnara, akapangisha wakulima, akasafiri. **34** Wakati wa matunda ulipokuwa karibu, akawatuma watumwa wake kwa wale wakulima, wapokee matunda yake. **35** Wale wakulima wakawakamata watumwa wake, huyu wakampiga, na huyu wakamwua, na huyu wakampiga kwa mawe. **36** Akawatuma tena watumwa wengine wengi kuliko wa kwanza wakawatenda vile vile. **37** Mwishowe akamtuma mwanawe kwao, akisema, Watamstahi mwanangu. **38** Lakini wale wakulima walipomwona yule mwana, wakasemezana wao kwa wao, Huyu ni mrithi; haya na tumwue, tuutwae urithi wake. **39** Wakamkamata, wakamtupa nje ya shamba la mizabibu, wakamwua. **40** Basi atakapokuja yule bwana wa shamba la mizabibu, atawatendaje wale wakulima? **41** Wakamwambia, Atawaangamiza vibaya wale wabaya; na shamba la mizabibu atawapangisha wakulima wengine, watakaomlipa matunda kwa wakati wake.

**21:33 "Sikilizeni mfano mwingine"** Mfano unafana katika Marko 12:1-12; Luka 20:9-19. Huu ni mfano wa nguvu zaidi juu ya Mungu kukataa Israeli na viongozi wake!



☐ **"naye alipanda shamba la mizabibu"** Hii ina muunganiko wa kipekee wa Isa. 5. Shamba la mizabibu siku zote limekuwa uwakilishi kwa taifa la Israeli. Mfano huu uko kisitari zaidi kati ya hizi tatu. Watumwa wanawakilisha manabii. Mwana anawakilisha Masihi (tazama kuna mwana katika kila mifano katika sura hii lakini inatumika katika namna tofauti). Wapangaji wanawalikisha taifa la Israeli au pia viongozi wake.

Katika muktadha wa ghafla wapangaji wanya inarejerea watu wa kawaida wa ardhi lakini katika muktadha pana inarejerea kwa Mataifa (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46; Mdo 1:8).

**21:41** Makutano wanajibu swali na kujimaliza wenyewe. Kuna mbinu ya utumizi wa maneno ambayo inafasiriwa "wale wasio faa kitu (*kakous*) kwa wasiofaa (*kakōs*) mwishoni."

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 21: 42-44**

<sup>42</sup> Yesu akawaambia, Hamkupata kusoma katika maandiko,

Jiwe walilolikataa waashi,

Hilo limekuwa jiwe kuu la pembeni;

Neno hili limetoka kwa Bwana,

Nalo ni ajabu machoni petu?

<sup>43</sup> Kwa sababu hiyo nawaambia, Ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu, nao watapewa taifa lingine lenye kuzaa matunda yake. <sup>44</sup> Naye aangukaye juu ya jiwe hilo atavunjika-vunjika; naye ye yote ambaye litamwangukia, litamsaga tikitiki.

**21:42 "Hamkupata kusoma katika maandiko"** Hii ilikuwa ni nukuu kutoka Zab. 118:22-23. Kiasili hii ilirejerea kwa taifa la Israeli kukataliwa na Mataifa. Ni kejeli ya namna gani kwamba sasa inarejerea kwa taifa la Israeli kukataliwa na Mungu na Ukubalifu wake wa watu wa kawaida na ikimaanisha Mataifa.

☐ **"jiwe"** Ile "jiwe" lilikuwa ni cheo cha Mungu katika Agano la Kale (kama vile Zab. 18). Lilitumika na Masihi kama msingi pekee katika Isa. 28:16. Lilitumika kama sitari ya kuja kwa Ufalme wa Kimasihi katika Dan. 2:34,44-45. Masihi inaweza ikawa vyote hakika na msingi imara uliotumwa na Mungu au hukumu ya uharibifu iliyotumwa na Mungu! Siku ya Ufufuo pia itakuwa ni siku ya Hukumu! Angalia Mada Maalum hapa chini.

**MADA MAALUM: "JIWE" (BDB 6, KB 7) na "JIWE KUU LA PEMBENI" (BDB 819, KB 944))**

Matumizi ya Agano la Kale

- A. Dhana ya jiwe kama kitu kigumu mkinachodumu ambacho kilitumika kutengeneza msingi kilitumika kuelezea YHWH (kama vile Ayubu 38:6; Zaburi 18:2 inatumia maneno mawili ya "mwamba," BDB 700, 849).
- B. Alafu baadae lilikuzwa kuwa cheo cha Kimasihi (kama vile Mwanzo 49:24; Mwanzo 118:22; Isaya 28:16).
- C. Neno "jiwe" au "mwamba" lilikuja kuwakilisha hukumu kutoka kwa YHWH Masihi (kama vile Isaya 8:16 [BDB 6 KUTENGENEZA BDB 103]; Danieli 2:34-35,44-45 [BDB 1078]).
- D. Hii ilikuzwa mpaka kuwa sitari ya kiujenzi (hasa Isaya 28:16).
  1. linalowekwa la kwanza, ambalo lililuwia linahakikisha usalama na kuweka vipimo vya jengo lote linalosalia lilitwa "jiwe kuu la pembeni"
  2. Ingeweza pia kumaanisha jiwe la mwisho linalowekwa sehemu yake likishikilia kuta pamoja (kama vile Zekaria 4:7; Efe. 2:20, 21), lilitwa "jiwe kifuniko," kutoka katika Kiebrania *rosh* (yaani kichwa)
  3. Linaweza kumaanisha "jiwe la msingi," ambalo linakuwa katikati ya njia ya kuingilia na kushikilia

uzito wa jengo la kuta nzima.

Matumizi ya Agano Jipya

- A. Yesu alinukuu Zaburi 118 mara kadhaa katika kujizungumzia mwenyewe (kama vile Mt. 21:41-46; Marko 12:10-11; Luka 20:17)
- B. Paulo alitumia Zaburi 118 akiunganisha kukataliwa kwa YHWH na Waisraeli wasioamini na wenye kuasi (kama vile Rum. 9:33)
- C. Paulo anatumia dhana ya "jiwe kuu la pembeni" katika Efe. 2:20-22 kama urejereo kwa Kristo
- D. Petro anatumia dhana hii ya Yesu 1 Petro 2:1-10. Yesu ni jiwe kuu la pembeni na waamini ni mawe yaliyo hai (yaani waamini kama mahekalu, kama vile 1 Kor. 6:19), yakijengwa juu yake (yaani Yesu ni Hekelu jipya, kama vile Marko 14:58; Mt. 12:6; Yohana 2:19-20). Wayahudi walikataa msingi wa tumaini lao pale walipomkataa Yesu kama Masihi.

Kauli za Kithiolojia

- A. YHWH alimruhusu Daudi/ Sulemani alijenge hekalu. Aliwaambia kwamba iwapo wangelitunza agano angeliwabariki na kuwa pamoja nao (kama vile 2 Samueli 7), lakini ikiwa wasingelishika agano, hekalu lingeliharibiwa (kama vile 1 Wafalme 9:1-9)!
- B. Walimu wa kiyahudi waliweka mkazo katik muundo na ibada na kuachana na kipengele cha imani binafsi (kama vile Yereimia 31:31-34; Ezekieli 36:22-38). Mungu anatafuta uhusiano wa kila siku, wa binafsi na wa kiungu pamoja na wale walioumbwa kwa sura na mfano wake (kama vile Mwanzo 1:26-27). Luka 20:17-18 inajumuisha maneno ya kutisha ya hukumu kama ilivyo kwa Mathayo 5:20, kuelekezwa kwa uyahudi.
- C. Yesu alitumia dhana ya hekalu kuwakilisha mwili wake mwenyewe (kama vile Yohana 2:19-22). Hii inaendelea na kupanuka kwa dhana ya imani binafsi katika Yesu kama masihi ni msingi wa mahusiano pamoja na YHWH (yaani Yohana 14:6; 1 Yohana 5:10-12).
- D. Wokovu umemaanishwa kurejesha sura ya Mungu iliyoharibika katika wanadamu (Mwanzo 1:26-27 na Mwanzo 3) ili kwamba ushirika pamoja na Mungu uwezekane. Lengo la Ukristo ni kufanana na Kristo kwa sasa. Waamini wanatakiwa kuwa mawe yaliyohai (mahekalu madogo yaliyojengwa/kwa mfano wa Kristo).
- E. Yesu ni msingi wa Imani yetu na jiwe letu la imani (yaani the Alfa na Omega). Bado, pia jiwe la kujikwaa na mwamba wa hatia (Isaya 28:16). Kumkosa Yeye ni kukosa kila kitu. Kunaweza kusiwe na ardhi nyingine ya kati hapa!

**21:43 "watapewa taifa lingine"** Kifungu hiki na mfano kinapatikana katika Mt. 22:1-14 unapelekea mtu kuamini kwamba hizi mifano mitatu inaungana kuzungumzia kukataliwa kwa taifa la Israeli, sio tu viomgozi wake. Angalau ilikuwa kukataliwa kwa Dini ya Kiyahudi ya walimu wa sheria. Neno kwa ajili ya Mataifa kibayana ilikuwa ni "mataifa."

**21:44** Toleo la NASB na NRSV yanajumuisha mstari wa 44 wakati matoleo ya RSV, TEV na JB yanaliweka katika tanbihi tu. Mstari huu ni sawa na Luka 20:18 na matoleo ya RSV, JB na kamati za ufasiri za TEV zilichukulia kwamba lilitolewa kwenda Mathayo na wanakili. Toleo la UBS<sup>4</sup> linaipa alama ya "C". Hata hivyo andiko la Kiyunani katika Luka na Mathayo sio halisi. Mstari huu pia ulijumuishwa katika maandiko mengi ya kale ya Kiyunani:  $\alpha$ , B, C, K, L, W & Z na pia fasiri za Kilatini, Kishamu, Kikoptiki na Ki-Armeni, na pia maandiko yaliyotumiwa na Chrysostom, Cyril, Jerome na Augustine. Ukweli ni kwamba maandiko ya kale kabisa ya Kiyunani ambayo yanaondoa maandiko ya karne ya sita, D (*Bezae*). Linatakiwa kujumuishwa.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 21:45-46**

<sup>45</sup> Wakuu wa makuhani na Mafarisayo, waliposikia mifano yake, walitambua ya kuwa anawanenea wao. <sup>46</sup>  
Nao walipotafuta kumkamata, waliwaogopa makutano, kwa maana wao walimwona kuwa nabii.

**21:45 "Wakuu wa makuhani na Mafarisayo, waliposikia mifano yake, walitambua ya kuwa anawanenea wao"**  
Viongozi wa kidini wa siku za Yesu walitambua kiukamilifu nini Yesu alichokuwa anakisema. Kejeli kuu ya namna gani hii! Wanafunzi hawakuelewa lakini masadukayo na Mafarisayo walielewa!

**21:46 "nabii"** Angalia Mada Maalum katika Mt. 11:9.

## **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kuna uhusiano gani kati ya usafishaji wa Hekalu, kuulaani Mtini na mifano mitatu?
2. Je Yesu alikuwa anakataa Dini ya Kiyahudi ya walimu wa sheria, viongozi wa dini au taifa la Israeli? Kwa nini?
3. Inawezekanaje watu wasio wa dini, waliokataliwa na jamii wenye dhambi kama watoza ushuru na makahaba waweze kuokolewa wakati viongozi washika dini wenye mzigo na viongozi wa wa Kiblia waliojikita katika dini wao wamepotea kiroho? (kama vile Mt. 5:20,48)
4. Elezea namna gani Zaburi 118:22-23 inahusiana na kauli za Yesu kuhusu kukataliwa kwake.
5. Ni kwa namna gani Mt. 21:43-46 inafanana na 8:11-12, 19:30, na 20:16?

## MATHAYO 22

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Mfano wa Sikukuu ya Ndoa	Mithali ya Sikukuu ya Harusi	Sikukuu ya Ndoa	Mithali ya Sikukuu ya Ndoa	Mithali ya Sikukuu ya Harusi
22:1-14	22:1-14	22:1-10 22:11-14	22:1-10 22:11-13 22:14	22:1-14
Kulipa Kodi kwa Kaizari	Mafarisayo : Je, Ni halali Kulipa Kodi kwa Kaizari?	Kulipa Kodi kwa Kaizari	Swali Kuhusu Kulipa Kodi	Tozo kwa Kaizari
22:15-22	22:15-22	22:15-22	22:15-17 22:18-19a 22:19b-20 22:21a 22:21b 2:22	22:15-22
Swali Kuhusu Ufufuo	Masadukayo: Vipi kuhusu Ufufuo	Swali Kuhusu Ufufuo	Swali Kuhusu Kufufuka kutoka Wafu	Ufufuo wa Wafu
22:23-33	22:23-33	22:23-28 22:29-33	22:23-28 22:29-32 22:33	22:23-33
Amri Kuu	Waandishi: Je! Ni amri ipi ya Kwanza kati ya Zote	Agizo Kuu	Amri Kuu	Amri Kuu sana kati ya zote
22:34-40	22:34-40	22:34-40	22:34-36 22:37-40	22:34-40
Swali Kuhusu Mwana wa Daudi	Yesu: Je, Ni kwa namna gani Daudi	Mwana wa Daudi	Swali Kuhusu Masihi	Kristo si Mwana tu bali Pia Bwana

	Anaweza Kuuita Uzao Wake Bwana			wa Daudi
22:41-46	22:41-46	22:41-46	22:41-42b	22:41-46
			22:42c	
			22:43-45	
			22:46	

## **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka “[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)”)** **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA ZA 22:1-14**

- A. Hii ni ya mwisho kati ya mithali tatu ambazo Yesu alizitoa kwa viongozi wa kidini katika Yerusalemu (kaa vile Mt. 21:23). Mithali hizi zinazopatikana katika muktadha wa Yesu kulisafisha Hekalu (kama vile Mt. 21:12- 17) na kuulaani mti wa mkuyu (kama vile Mt. 21:18-22), ambapo zote ni viashiria vya Mungu kuukataa uongozi wa Kiyahudi, sheria za Dini ya Kiyahudi, au taifa.
- B. Moja kati ya maswali makuu yampasayo mtu kuyajibu katika kuzifasiri mithali hizi ni mtu gani anayerejelewa na kutumiwa mithali hizi?
  1. Uongozi wa Kiyahudi Mt. 22: Mtu wa Kiyahudi wa kawaida (kama vile Mt. 21:31)
  2. Wayahudi Mt. 22: Wagalilaya (kama vile Mt. 21:41, 43; 22:3-5, 8, 9, 10)
  3. Watu wasiotubu na wasiojali Mt. 22: wenye kutubu na wanyenyekevu
- C. Kuna mifano miwili katika Mt. 22:1-14. Hii ni kwa sababu:
  1. Neno "mithali" katika mstari wa wingi.
  2. Kunaonekana kuwepo matatizo ya nje na ya ndani na ya kimuktadha kati ya Mt. 22:1-10 na 11-14, hasa yenye kuhusiana na mavazi ya hasusi.
- D. Pia kuna swali lenye kuhusiana na idadi ya wazungunzaji wanaozungumzwa katika mistari ya 1-14:
  1. kwa uwazi, mfalme
  2. kwa uwazi, watumwa wa mfalme
  3. huenda ni mwandishi mwenyewe wa Injili aliye katika Mt. 22:7
  4. huenda Yesu Mwenyewe anatoa mawazo katika Mt. 22:14
- E. Mithali tatu zilizo katika muktadha huu wa kiuandishi kwa namna iliyo dhahiri zinahusiana na:
  - a. Hii mithali ya kwanza ni kumkataa mjumbe wa Mungu, yaani., Yohana Mbatizaji.
  - b. Mithali ya pili ni ya kumkataa Mwana wa Mungu, Masihi.

c. Mithali ya tatu ni kuikataa Neema ya Mungu.

F. Inawezekana kwamba Mistari ya 1-10 inahusiana na kutokuwa na hofu kwa Mungu, neema isiyopimika kwa mwanadamu aliyeanguka, abapo mistari ya 11-13 inahusiana na jukumu la mwanadamu baada ya kuipata neema ya Mungu. Mithali hii ni ya utata sana kuyajenga mafundisho katika kiwango hiki, lakini kweli ile ile inaakiwa katika Efe. 2:8-9, 10. Hii pia ingweza kukazia kwamba wokovu huanza na neema ya Mungu, lakini lazima uendelee na uhalisia na maisha marefu ya toba na imani. Hatuokolewi kwa kazi, bali tunaokolewa kwa kazi mzuri.

G. Mithali hii inafanana katika Luka 14:16-24 katika namna mbalimbali. Wakosoaji wa kisomi wamedai kuwa ni maelezo ya aina mbili za wakati hule ule wa mafundisho. Yesu alitumia simulizi za mafundisho yale yale katika muktadha tofauti tofauti. Waandishi wa Injili hawakuwa na uhuru kuweka maneno katika kinywa cha Yesu. Hawa walikuwa na uhuru wao, chini ya uvuvio, wa kuchagua, kuunganisha, na kuyafupisha mafundisho yake. Mfano mzuri unaweza kuwa "Hotuba Mlimani," ya Mathayo (kama vile Mt. 5-7) inapolinganishwa na "Hotuba Mashambani" ya Luka (kama vile Luka 6).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 22:1-10

<sup>1</sup> Yesu akajibu, akawaambia tena kwa mithali, akisema, <sup>2</sup> Ufalme wa mbinguni umefanana na mfalme mmoja aliyemfanyia mwanawe arusi. <sup>3</sup> Akawatuma watumwa wake wawaite walioalikwa kuja arusini; nao wakakataa kuja. <sup>4</sup> Akatuma tena watu kwa wengine, akisema, Waambieni wale walioalikwa, Tazameni, nimeandaa karamu yangu; ng'ombe zangu na vinono vimekwisha kuchinjwa, na vyote vimekuwa tayari, njoni arusini. <sup>5</sup> Lakini hawakujali, wakaenda zao, mmoja shambani kwake, mmoja kwenye biashara yake; <sup>6</sup> nao waliosalia wakawakamata watumwa wake, wakawatenda jeuri, na kuwaua. <sup>7</sup> Basi yule mfalme akaghadhibika; akapeleka majeshi yake, akawaangamiza wauaji wale, akauteketeza mji wao. <sup>8</sup> Kisha akawaambia watumwa wake, Arusi i tayari, lakini wale walioalikwa hawakustahili. <sup>9</sup> Basi enendeni hata njia panda za barabara, na wote mwaonao waiteni arusini. <sup>10</sup> Watumwa wale wakatoka wakaenda njia kuu, wakakusanya wote waliowaona, waovu kwa wema; arusi ikajaa wageni.

**22:1 "kwa mithali"** Utambue wingi, ambao unaweza kumaanisha moja ya mambo haya matatu

1. Mathayo ameunganisha mithali kadhaa za Yesu
2. Yesu alitumia simulizi zile zile kwa nyakati tofauti tofauti ili kukeleza kweli tofauti tofauti
3. Yesu alikuwa akizungumza nao katika mtindo wa kimithali (kama vile Marko 4:10-12)

**22:2 "Ufalme wa mbinguni"** Mada ndiyo iliyokuwa dhamira ya mara kwa mara katika mafundisho na huduma ya Yesu (tazama Mada Maalum katika Mt. 4:17). Hii yote ni kweli ya sasa na tumaini la baadaye. Kimsingi, huu ni ufalme wa Mungu ndani ya mioyo wa wanadamu na ya kwamba siku moja utathibitika juu ya nchi yote. Kifungu hiki kilikuwa kisawe cha kifungu "ufalme wa Mungu" katika Marko na Luka. Mathayo, akiwaandikia Wayahudi, anapinga sana namna jina la Mungu linavyotumika.

☐ **"mfalme. . . mwanawe"** Ingawa ni sahihi kuziweka mithali hizi katika stiari, inaonekana kwamba hili wazo la kifalme linahusiana na Mungu. Pia inafurahisha kwamba katika mithali zote tatu Mt. 21:28-22:14 kifungu "mwana" kinahusika katika simulizi. Ni kweli kwamba hii ni sehemu kuu katika mithali hii, lakini bado ipo. Mtu anashawishiwa amwone Mungu kama Mfalme na Yesu kama mwana. Siku ya harusi inakuwa kidokezo cha kalamu ya ki-Masihi (kama vile Mt. 8:11; Luka 13:29; 14:15; 22:16; Ufu. 19:9,17).

**22:3 "walioalikwa kuja"** Kifasihi kifungu hiki ni "waiite walialikwa." Katika Mashariki ya Karibu ya Kale huu ulikuwa utaratibu wa mialiko ya aina mbili kutolewa: mwaliko maalum na tangazo kwamba siku ilikuwa imekwisha wadia.

☐ **"nao wakakataa kuja"** Hii kauli ya wakati usio timilifu inadokeza tendo la kukataa lililorudiwa rudiwa.

**22:4 "nimeandaa karamu yangu"** Hili neno mlo wa kwanza kati ya milo ya siku (kama vile Luka 14:12). Katika siku na utamaduni ule ule, kulikuwa na mlo asubuhi (saa 3 asubuhi-saa 6 mchana.) na mmoja jioni (saa 9 mchana- saa 12 jioni.). Mlo huu ungeanza na sikukuu ambayo iliendelea kwa siku kadhaa.

**22:5 "Lakini hawakujali"** Kifungu hiki kilidokeza tafrija au kutokuwepo kwa umuhimu wa mwaliko wa kifalme. Kuna mabadiliko rahisi na ya mara kwa mara kwa mtazamo wa mwanadamu aliyepotoka kuihusu injili.

☐ **"mmoja shambani kwake, mmoja kwenye biashara yake"** Hili ni sawa na Luka 14:18-19. Matendo yao hayakuwa dharimu, bali hawakuona umuhimu wa kuitikia wito wa Mungu katika Kristo na hili ni kosa kubwa.

**22:6** Nguvu ya mstari huu inatisha. Mtu anashangazwa na aina hii ya mwitikio katika kutoa majibu ya mwaliko wa siku ya harusi. Tendo la kuupuzia mwaliko wa mfalme kwa lo lote katika Mashariki ya Kati lilifikiliwa kama chukizo lisilo sameheka. Kwa vyo vyote vile hii ni mbinu ya kiuandishi yenye kuonyesha uhusiano wa mithali ya awali (kama vile Mt. 21:35). Wengine huupuzia wito wa Mungu; wengine wamatumia nguvu katika kukataa kwao (yaani., Sauli wa Tarso).

**22:7** Mwitikio kwa mfalme pia unaonekana kwa kwenda nje ya tukio. Wengi wamedhani kwamba kuupuzia mwaliko wa kifalme kiukweli ulikuwa uasi dhidi ya Mfalme. Watoo maoni wengine wameeleza ufananano wa mistari wa 7 na maangamizi ya kihistoria ya Yerusalemu mnamo 70 b.k na Jenerali wa Kirumi na, na baadaye Mfalme, Tito. Wengine wamekuwa wakidai kwamba Mathayo ameliongeza hili katika mithali ya Yesu. Sijisikii vema juu ya uhuru wa upanuzi huu wa Mathayo katika kuyashulikia maneno ya Yesu. Ingawa ningewaruhusu waandishi wa Injili kuwa na uhuru wa kuchagua, kuasilisha, kupanga upya, na kuyafupisha mafundisho ya Yesu chini ya uvuvio, siwezi kuwaruhusu kuweka maneno katika kinywa chake ambayo kamwe hakuwahi kuyanena.

**22:8** Hili, nalo, linafanana na Luka 14:21-23.

**22:9** Mfalme alihitaji siku ya arusi ya mwanae kuhudhuriwa vema. Wale waliotakiwa kuja walikataa. Kutokana na nuktadha na mstari wa 15, uongozi wa Kiyahudi ulitambua kwawa Yesu alikuwa akinena nao.

**22:10 "wakakusanya wote waliowaona, waovu kwa wema"** Mara nyingi swali limekuwa, Mithali hii inamrejelea nani? Katika muktadha huu kifungu hiki kinaonekana kuwarejelea maskini wa Kiyahudi waliokuwa wakitengwa. Haya naneno "waovu kwa wema" pia wanaweza kurejelea utayari na uwezo wao wa kutunza au kutotunza desturi za mapokeo ya wazee wao (yaani., Mt. 15:2). Kidokezo kilicho dhahiri ni kwamba kwa uhuru kabisa Mungu huwakubali wenye dhambi. Wengine huyatambua mahitaji yao na wengine hawatambui! Mwaliko umekwisha kutolewa, na sasa ni nani atakuwa na mwitikio?

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 22:11-14**

<sup>11</sup> Lakini alipoingia yule mfalme ili kuwatazama wageni wake, akaona mle mtu mmoja asiyevaa vazi la arusi. <sup>12</sup> Akamwambia, Rafiki, uliingiaje humu nawe huna vazi la arusi? Naye akatekewa. <sup>13</sup> Mfalme akawaambia watumishi, Mfunjeni mikono na miguu, mchukueni mkamtupe katika giza la nje; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno. <sup>14</sup> Kwa maana waitwao ni wengi, bali wateule ni wachache.

**22:11 "vazi la arusi"** Ingawa kwa miaka mingi wato maoni wameeleza matatizo yaliyo kati ya Mt. 22:9-10 na 11. Hii haitaji juu ya maandalizi ya karamu yaliyokatika 9-10, bali madai yaliyo katika Mt. 22:11. Augustine, akifuatisha ushahidi wa kihistoria uliwekewa mipaka, anadhani kwamba mwenyeji alitoa vazi maalum la tafrija. Hii inaweza kumaanisha mtu aliyekataa au kuingia kwa namna inayotakiwa. Mtu aliyevalia kwa usahihi anaonekana kutambua nafasi yake kwa bahati yake ya mwitikio ulio katika Mt. 22:12.

**22:13** Kama ilivyo awali katika Mt. 22:6 na 7, Mt. 22:13 ni usemi wa kutisha. Huenda mistari yote hii inamaanisha aya kujikita katika semi kwa undani (mubalagha); hata hivyo, ukali wa adhabu unaendana na kosa la kuikataa

neema ya Mungu (kama vile Mt. 22:6-7) na kukataa kutembea katika neema ya Mungu (kama vile Mt. 22:13).

☐ **"mkamtupe katika giza la nje; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno"** Hii ilikuwa nahau ya kwaida iliyotumika mara kwa mara katika Mathayo kutoa ufafanuzi wa hali ya wanadamu waliomkataa Mungu (kama vile Mt. 8:12; 13:42,50; 22:13; 24:51; 25:30). Hii inadokeza hali iliyopo (kama vile Luka 16:19-31) pamoja na mazingira ya siku za mwisho (kama vile Mt. 24:51).

**22:14** Ni vigumu kuufasiri mstari huu. Wengi wanasema kuwa huu unahusiana na Mt. 22:2-10, lakini si 11-13. Huu unaonekana kuitazamia karama ya utukufu wa Mungu iliyoenea kwa wote (yaani., Yohana 1:12; 3:16; 1 Tim. 2:4; 4:10; Tito 2:11; 2 Pet. 3:9). Hata hivyo, mwanadamu aliyepotoka yampasa kuitikia kwa usahihi. Mungu hachagui, bali amemchagua mwanadamu huyu alazimike kuwa na mwitikio kupitia toba na imani (kama vile Marko 1:15; Matendo 3:16,19; 20:21) juu ya injili ya Yesu iliyopatanishwa kupitia kuugua kwa Roho Mtakatifu (kama vile Yohana. 6:44,65). Mstari huu unaweza kuhusiana na ufunuo wa Mungu kwa watoto wa Ibrahimu (kama vile Matendo 3:26; Rum. 1:16; 2:9). Hawa walikukataa kujitolea kwa Mungu katika Kristo, hivyo injili ilienezwa kwa watu wa Mataifa ambao kwa mapenzi mema waliikumbatia (yaani., Warumi 9-11). Muktadha huu mzima unaeleza kweli ambayo ilitarajiwa kuleta matokeo katika mambo ya kiroho yakuwa yanakwenda kugeuzwa (kama vile Mt. 19:30; 20:16)!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembe katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je! Ni kwa namna gani mithali hii inahusiana na Mathayo 21?
2. Ni mithali ngapi zilizo katika mistari ya 1-14?
3. Je! Kifungu hiki "wawaite walioalikwa" kilicho katika mistari ya 3-5 kinamrejlea nani?
4. Je! Kifungu "waovu kwa wema" cha mstari wa 10 kinamrejlea nani?
5. Ni kwa namna gani unaeleza tendo hili la kuwepo kwa mvutano ulio katika mistari ya 6, 7, na 13?
6. Je! Mstari wa 14 unahusianaje na mistari ya 1-14?

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 22:15-22

<sup>15</sup> Ndipo Mafarisayo wakaenda zao, wakafanya shauri, jinsi ya kumtega kwa maneno. <sup>16</sup> Wakatuma kwake wanafunzi wao pamoja na Maherodi, wakasema, Mwalimu, twajua ya kuwa wewe u mtu wa kweli, na njia ya Mungu waifundisha katika kweli, wala hujali cheo cha mtu awaye yote, kwa maana hutazami sura za watu. <sup>17</sup> Basi utuambie, Waonaje? Ni halali kumpa Kaisari kodi, ama sivyo? <sup>18</sup> Lakini wanafiki Yesu akaufahamu uovu wao, akasema, Mbona mnanjaribu, enyi wanafiki? <sup>19</sup> Nionyesheni fedha ya kodi. Nao wakamletea dinari. <sup>20</sup> Akawaambia, Ni ya nani sanamu hii, na anwani hii? <sup>21</sup> Wakamwambia, Ni ya Kaisari. Akawaambia, Basi, mlipeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, na Mungu yaliyo ya Mungu. <sup>22</sup> Waliposikia, walistaajabu, wakamwacha, wakaenda zao.

**22:15 "Mafarisayo"** Tazama Mada Maalum hapa chini.

### MADA MAALUMU: MAFARISAYO

- I. Neno lilikuwa na uwezekano wa kuwa na asili moja kati ya hizi zifuatazo:
  - A. "Kujitenga." Kundi hili lilianza wakati wa ufuasi wa kiongozi wa Kiyahudi Yuda wa karne ya pili ( huu ni



mtizamo mpana sana unaokubalika), na kujitenga wao wenyewe toka kwenye umma wa watu ili kutunza tamaduni simulizi za sheria ya Musa (yaani., mienendo ya kichini chini ya Kiyahudi iliyopatikana karne ya 18).

- B. “Kugawa” Hii ni maana nyingine toka kwenye kiini kile kile cha lugha ya Kiebrania (BDB 827, BDB 831 I, KB 976); yoye yakimaanisha “kugawanya.” Baadhi ya wasomi wanasema linamaanisha mfasilili (kama vile Neh. 8:8; 2 Tim. 2:15).
- C. “Uajemi.” Hii ni maana nyingine toka kwenye kiini kile kile cha lugha ya Kiarama (BDB 828, KB 970). Baadhi ya mafundisho ya mafarisayo yanaingiliana na wafuasi wa dini za Kiislamu za awali toka Uajemi zilizoanzishwa na Zoroaster (angalia Maada Maalumu Uovu).
- II. Pamekuwepo na nadharia nyingi nani alianzisha Ufarisayo.
  - A. Kikundi cha kithiolojia cha dini ya mwanzo ya Kiyahudi (angalia., Yusufu)
  - B. Kikundi cha kisiasa toka kipindi kile cha Herode
  - C. Kikundi cha kisomi cha wafasiri wa sheria za Musa ambao walitaka kuwasaidia watu wa kawaida kuelewa Agano la Musa na tamaduni simulizi zilizowazunguka.
  - D. Mienendo ya chini kwa chini ya waandishi, kama vile Ezra na Sinagogi kuu, wakigombea uongozi wa ukuhani mkuu katika hekalu.

Yaliundwa nje ya misigishano na

- 1. Makabaila wasiokuwa Wayahudi (hasa Antiokia IV).
- 2. jamii ya watu wakuu dhidi ya watu wa kawaida
- 3. wale waliojifungamanisha kwenye maisha ya agano dhidi ya Wayahudi wa kawaida toka Palestina

III. Habari zetu kuwahusu wao zinatoka

- A. Yusufu, aliyekuwa mfarisayo
  - 1. Vitu vya kale vya Kiyahudi
  - 2. Vita vya Wayahudi

B. Agano Jipya

C. Asili ya awali ya Kiyahudi

IV. Mafundisho yao makuu

- A. Imani ya kuja kwa Masiha, iliyoshawishiwa na waandishi wa Kibiblia wa Kiyahudi wenye fasihi ya kimaono kama vile Enock.
- B. Imani ya kwamba Mungu yu hai katika maisha yetu ya kila siku. Hii moja kwa moja ilikuwa kinyume na Masadukayo (kama vile Mdo. 23:8). Mafundisho mengi ya Kifarisayo yalikuwa ni kijazilizo cha yale ya Masadukayo.
- C. Imani katika maelekezo ya kimwili baada ya maisha yaliyolenga maisha ya duniani, yaliyojumuisha zawadi na adhabu (kama vile Dan.12:2)
- D. Imani katika mamlaka ya Agano la Kale vile vile simulizi za kitamaduni (Talmud). Walitambua kuwa watiifu kwa amri za Mungu za Agano la Kale kama zilivyo tafasiliwa na shule za wasomi wa sheria za Kiyahudi (Shammai, asiyependa mabadiliko na Hillel, anayependa mabadiliko). Watafasiri wa sheria za Kiyahudi walisimamia juu ya mazungumzo kati ya wanasheria/walimu wa falsafa mbili zinazokinzana, mmoja asiyependa mabadiliko na mwingine anayependa mabadiliko. Mazungumzo haya ya kisimulizi juu ya maana ya andiko hatimaye likaandikwa kwa miundo miwili: sheria za kiibada za Wababeli na sheria za kiibada za Wapalestina zisizo kamili. Waliamini kuwa Musa alipokea hizi sheria za mdomo kwenye Mlima Sinai. Mwanzo wa haya mazungumzo ya kihistoria yalianzishwa na Ezra na watu wa “Sinagogi kuu” (baadaye wakaitwa Sanhedrin)
- E. Imani ilioanzishwa juu ya mafundisho ya kithiolojia ya kimalaika. Haya yalijumuisha viumbe wazuri na wabaya. Hili lilianzia huko Uajemi yenye pande mbili na fasihi za Kiyahudi zenye mwingiliano na Biblia.
- F. Imani juu ya mamlaka ya kifalme ya Mungu, lakini pia mazoezi ya utashi huru wa binadamu (yetzer).

V. Nguvu ya mabadiliko ya Kifarisayo.

- A. Walipenda , waliheshimu, kuamini mafunuo ya Mungu (yaani., yote, yakijumuisha sheria, Manabii, Maandiko, na simulizi za kitamaduni)
- B. Walijitolea kuwa wafuasi wenye haki (yaani., maisha ya kila siku na imani) wa mafunuo ya Mungu. Walitaka “Israel yenye haki” kutimiza ahadi ya kinabii ya siku mpya yenye mafanikio.

- C. Walitetea kuwepo usawa na jamii za Kiyuda, ambao unajuisha ngazi zote za watu, kwa maana kuwa, walikataa uongozi wa kikuhani (yaani., masadukayo) na thiolojia(kama vile Mdo. 23:8).
- D. Walipigania kitu halisi cha mtu kwenye agano la sheria za Musa. Walitetea au kudai mamlaka ya Mungu, lakini pia wakashikilia kwenye hitaji la utendaji huru wa mwanadamu
- E. Agano Jipya linataja mafarisayo mbali mbali walioheshimika (yaani., Nikodemu, Mtawala tajili kijana, Yusufu wa Alimataya).

Hawa Walikuwa ni kundi hilo tu la dini ya Kiyahudi ya karne ya kwanza kuhimili uharibifu wa Yerusalem na hekalu toka kwa Warumi mwaka wa 70 B.k. wakawa ni dini ya Kiyahudi ya kisasa.

☐ **"wakafanya shauri"** Meno hili linatumia na Mathayo kuweka idadi na mbinu walizozitumia viongozi wa kidini kukusanyika kwa pamoja ili kuipinga huduma ya Yesu (kama vile Mt. 12:14; 22:15; 26:4; 27:1,7; 28:12).

Katika mfano huu hata Mafarisayo waliwasiliana na Maherodi ili kumtega Yesu. Hawa walikuwa wakichukiana wao kwa wao, lakini wote waliathiriwa na Yesu na mafundisho yake. Chuki hutengeneza mazoea "taabu"!

**22:16 "Maherodi"** Tazama Mada Maalum katika Mt. 2:1.

☐ **"Mwalimu"** Kundi hili la kidini linajaribu kumsifu Yesu ili kumfanyia njama (kama vile Mt. 22:15).

Tambua namna wanavyombainisha.

1. twajua ya kuwa wewe u mtu wa kweli
2. na njia ya Mungu waifundisha katika kweli
3. wala hujali cheo cha mtu awaye yote
4. hutazami sura za watu (kif. "usiangalie sura")

Ikiwa Mafarisayo na Maherodi hawa waliziamini seni hizi, kwa nini waliyapinga mafundisho yake?

**22:17 "Ni halali"** Hili lilikuwa na maana itokanayo na desturi za mapokeo ambazo zilifasiriwa kutokana na Torati ya Musa (yaani., "mapokeo ya wazee," 15:2). Yesu alibadisha swali kutoka "kwa vyo vyote/ama "kwa "yote/na" (kama vile Mt. 22:21).

☐ **"kumpa Kaisari kodi"** Kodi hii ya Kirumi ilikwenda moja kwa moja kwa Mfalme. Hii ilidaiwa kwa kila mwanamme kuanzia umri wa miaka 14-65 na kila mwanamke kuanzia umri wa miaka 12-65 waliyoishi katika majimbo ya kifalme.

**22:18 "mnanijaribu"** Hili neno la Kiyunani lilikuwa na maana nyingine ya "kujaribu kwa makusudi ya maangamizi." Tazama Maalum katika Mt. 4:1. Hawa viongozi wa Kiyahudi walijua kwamba idadi kubwa ya Kiyahudi haikuliunga mkono suala la kodi hii. Ikiwa Yesu angejibu kwa namna nyingine angekuwa katika mvutano na mamlaka za Kirumi; ikiwa wengine, ni alaiki ya Kiyahudi.

☐ **"wanafiki"** Hili ni neno ambatani liliomaanisha "kutoa hukumu chini chini" (kama vile Mt. 6:2,5,16; 7:5; 15:7; 16:3; 23:13,15,25,26,27,29; 24:51). Neno hili liirwaejelea watu waliotenda kwa namna moja ambapo ndiyo maisha ya kweli au kuwahisi wengine.

**22:19 "Nionyeseni fedha ya kodi"** Sarafu hii likuwa "dinari." Hii ilikuwa siku ya ujira kwa wanajeshi na wafanyakazi. Mbele yake kulikuwana sanamu ya Tiberio yenye maandishi, "Tiberio Kaisari Augusto, mwana wa Mtakatifu Augusto." Nyuma yake kulikuwa na sanamu ya Tiberio akiwa amekaa juu ya kiti na maandishi, "Kuhani Mkuu." Tiberio alitawala Dora ya Kirumi toka 14-37 b.k. Utengenezaji sarafu ilikuwa alama ya yule aliye madarakani. Tazama Maalum: Matumizi ya Sarafu katika Palestina Nyakati za Yesu katika Mt. 17:24.

**22:21 "mlipeni Kaisari yaliyo ya Kaisari"** Biblia i wazi kwamba waamini wanapaswa kuomaba na kuiunga mkono serikali mamlaka inayowatawala pasipokujali muundo wake kwa kuwa inasimama kwa nafasi ya Mungu katika maisha ya mwaminii (kama vile Rum. 13:1 na kuendelea.; Tit. 3:1; 1 Pet. 2:13). Yesu alilibadilisha neno "kumpa" la

Mt. 22:17 kuwa "mlipeni."

☐ **"na Mungu yaliyo ya Mungu"** Serikali, japo ilianzishwa na Mungu, haiwezi kuwa na utwala kama wa ki-Ungu. Yawapasa waanini kuyapinga madaia yote ya kimmamlaka, ni kwa Mungu pekee palipo na utimilifu. Yatupasa kuwa makini tujikitapo katika nadharia yetu ya kisiasa ya sasa zihusuyo kuliweka mbali kanisa na utawala inayozungumzwa katika kifungu hiki. Biblia haizungumzi bayana kuhusiana na jambo hili, bali ni historia ya kimagharibi ifanyayo hivyo!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je! unaweza kuorodhesha na kueleza makundi yote ya kisiasa na kidini yaliyo ndani ya Dini ya Kiyahudi ya nyakati za Yesu yaliyotajwa katika Agano Jipya?
2. Kwa nini makundi haya yanajaribu kumlia njama Yesu?
3. Nini dokezo la usemi wa Yesu lililo katika mstari wa 21 kwa nyakati zetu?

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 22:23-33

<sup>23</sup>Siku ile Masadukayo, watu wasemao ya kwamba hakuna kiyama, wakamwendea, wakamwuliza, <sup>24</sup>wakisema, Mwalimu, Musa alisema, Mtu akifa, akiwa hana watoto, ndugu yake na amwoe yule mkewe, ili ampatie nduguye mzao. <sup>25</sup> Basi, kwetu kulikuwa na ndugu saba; wa kwanza akaoa, akafariki, na kwa kuwa hana mzao, akamwachia nduguye mke wake. <sup>26</sup> Vivyo hivyo wa pili naye, na wa tatu, hata wote saba. <sup>27</sup> Mwisho wa wote yule mwanamke akafa naye. <sup>28</sup> Basi, katika kiyama, atakuwa mke wa yupi katika wale saba? Maana wote walikuwa naye. <sup>29</sup> Yesu akajibu, akawaambia, Mwapotea, kwa kuwa hamyajui maandiko wala uweza wa Mungu. <sup>30</sup> Kwa maana katika kiyama hawaoi wala hawaolewi, bali huwa kama malaika mbinguni. <sup>31</sup> Tena kwa habari ya kiyama ya watu, hamjalisoma neno lililonenwa na Mungu, akisema, <sup>32</sup> Mimi ni Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo? Mungu si Mungu wa wafu, bali wa walio hai. <sup>33</sup> Na makutano waliposikia, walishangaa kwa mafunzo yake.

**22:23 "Masadukayo"** Tazama Maalum katika Mt. 2:4.

☐ **"wakamwuliza"** Swali hili pia lilimaanisha kumlazimisha Yesu kulishughulikia suala lenye utata, na ambapo, yeye alijitenga na umati wa Kiyahudi.

**22:24 "Musa alisema"** Hii ni rejea ya Kumb. 25:5-6.

☐ **"akifa"** Hii ni sentensi amrishi daraja la tatu, lenye kumaanisha tendo lijalo lenye uwezekano.

☐ **"ndugu yake na amwoe yule mkewe"** Kipengele hiki kilishughulika na dhana ya "ndoa ya Kilawi" (kama vile Kumb. 25:5-6; Ruthu 4:1-2). Neno hili linatokana na neno la Kilatini "shemeji." Katika Israeli ya kale ardhi ilikuwa na msisitizo mkubwa wa kithiolojia (kama vile Mwa. 12:1-3). Mungu aliigawa ardhi vipande vipande kulingana na makabila chini ya Yoshua. Mtu alipogkufa pasipo mrithi swali lilibuka kuhusu hatima ya ardhi yake. Wayahudi walitafuta mbinu nyingine ya mjane kuwa na mtoto, ikiwezekana, kwa jamaa wa karibu ili mrithi wa mali za marehemu aweze kwenda katika urithi. Huyu angefikiriwa kama mtoto wa ndugu wa marehemu (kama vile Hesabu 27 na Ruthu 4).

**22:25 "ndugu saba"** Hii inaonyesha kwamba Masadukayo kiukweli hawakuutaka ufahamu wa kithiolojia bali walikuwa wakitafuta misingi ya shutuma! Hawakuwa n amshangao pale walipoutumia shutma hizi za kthiolojia nyakati zote kuleta mkanganyiko na kuwapinga Mafarisayo.

**22:29 "Mwapotea, kwa kuwa hamyajui maandiko wala uweza wa Mungu"** shutuma hizi lazima ungewakaganya viongozi wa kidini (kama vile Mt. 21:42)! Hata hivyo, Haijulikani ni andiko gani la Agano la Kale alilolirejelea Yesu kuwafahamisha habari hizi.

**22:30 "Kwa maana katika kiyama"** Yesu alikuwa akieleza juu ya kukubaliana kwake na Mafarisayo kuhusiana na ufufuo ujao (kama vile Dan. 12:1-2 au huenda Ayubu 14:7-15; 19:25-27).

☐ **"hawaoi wala hawaolewi"** Hii ilikuwa kweli mpya isiyofunuliwa popote pale katika Maandiko. Hii inadokeza kwamba tendo la ndoa ni kipengele cha muda tu. Ni sehemu ya mapenzi ya Mungu kwa uumbaji (kama vile Mwa. 1:28; 9:17), lakini si la milele! Hili linaonekana kudokeza kwamba ushirika wa ajabu wa kimwili kati ya mke na mume utachukua nafasi hata mbinguni kwa ushirika wa karibu kati ya watoto wa Mungu katika umilele.

☐ **"bali huwa kama malaika mbinguni"**Kifungu hiki kinaeleza kwamba malaika hawana kipengele cha kufanya tendo la ndoa. Hawaongezeki kwa namna hii. Watoa maoni wengi wameutumia mstari huu kuifasiri Mwa. 6:1-4 kama kipengele kisichorejelea tendo la ndoa kwa malaika, bali kama kundi maalum la malaika lililotajwa katika Yuda 6 na huenda 1 Pet. 3:19-20, waliokuwa wakikaa gerezani (Tartarus, jina lililokuwa la sehemu dhaifu ya jehanamu).

**22:32 "Mimi ni Mungu wa Ibrahimu"** Yesu alikuwa akitumia neno la walimu wa sheria za Kiyahudi kuomba katika wakati uliokuwepo uliodokezwa wa kitenzi cha Kiebrania "Mimi ndiye" cha Kut. 3:6 kueleza kwamba bado Mungu alikuwa na bado ni Mungu wa Ibrahimu Baba wa Imani. Ibrahimu anaishi na Mungu na bado ni Mungu wake! Yesu alilitumia andiko toka Vitabu Vitano vya Musa (Mwanzo – Kumbukumbu la Torati) ambapo Masadukayo walidai kuwa na mamlaka katika hivyo.

**22:33** Hawa walipatwa na mshangao kwa sababu Yesu alikitumia kitabu cha Agano la Kale kuzirejelea desturi za walimu wa sheria za Kiyahudi (kama vile Mt. 7:28; 13:54). Yeye alikuwa na mamlaka yake binafsi (kama vile Mt. 5:21-48).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 22:34-40**

<sup>34</sup> Na Mafarisayo waliposikia ya kwamba amewafumba kinywa wale Masadukayo, walifanya shauri pamoja.  
<sup>35</sup> Mmoja wao, mwana-sheria, akamwuliza, akimjaribu; <sup>36</sup> Mwalimu, katika torati ni amri ipi iliyo kuu?  
<sup>37</sup> Akamwambia, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. <sup>38</sup> Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. <sup>39</sup> Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. <sup>40</sup> Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii. ,

**22:35 "mwana-sheria"** Mara nyingi Mathayo aliwaita hawa wataalamu wa sheria "waandishi." Kamwe hakuwahi kilitumia neno hili "mwanasheria" po pote pale katika Injili. Neno hili linaweza kuwa mwigu wa mnuukuu toka Luka 10:25. Luka alilitumia neno hili mara kwa mara (kama vile Luka 7:30; 10:25; 11:45,46,52; 14:3).Hili halipatikani katika ufanano ulio katika Marko 12:28. Hata hivyo hili liko katika machapisho yote ya kale ya Kiyunani. Wanasheria wa dini ya Kiyahudi waliliboresha neno hili wakati wa uhamisho wa Babeli. Ezra analibainisha kundi hili (kama vile Ezra 7:10). Katika namna nyingi hawa walichukuwa nafasi kama Makuhani wa mahali pale. Kimsingi hawa walikuwa wakijibu maswali ya papo kwa papo yaliyohusiana na Torati iliyoandikwa na torati ya mazungumzo (Bukula Sheria za Kiyahudi) ilivyotumika katika maisha ya kawaida.

☐ **"akimjaribu"** Kitenzi hiki (*peiraze*), lililopanuliwa na kuwa "shawishi," " jaribu," "pima" au "hakikisha," lina maana nyingine ya "kupima kwa maana ya kuangamiza" (tazama Mada Maalum katika Mt. 4:1, kama vile Mt. 4:1;

16:1; 19:3; 22:18, 35; nomino I katika Mt. 6:13; 26:41).

**22:36 "torati ni amri ipi iliyo kuu"** Walimu wa Sheria za Kiyahudi wamekuwa wakieleza kwamba kuna amri 248 zilizo chanya na amri 365 zilizo hasi katika maandiko ya Musa (Mwanzo - Kumbukumbu la Torati) kwa jumla ya amri 613.

**22:37-38** Amri iliyo kuu inaelezwa katika Kumb. 6:5. Kuna tofauti ndogo ndogo kati ya andiko la Kimasoretiki la Kiebrania na nukuu ya Yesu, bali asili ni ile ile. Mstari huu hauhusiani na asili ya pande mbili (kama vile Ebr. 4:12) au pande tatu (kama vile 1 The. 5:23) za mwanadamu bali unashughulika na mtu kama umoja (kama vile Mwa. 2:7; 1 Kor. 15:45): kufikiri na kihisi, kiumbe cha kiroho na kimwili. Ni kweli kwamba kwakuwa wanadamu ni wanyama wa kidunia wanaitegemea sayari hii kwa ajili ya chakula, maji, hewa, na mambo mengine yote ya maisha ya wanyama wanayoyahitaji ili kuishi. Pia wanadamu ni viumbe wa kiroho wanaohusiana na Mungu na ufalme wa Mungu. Hata hivyo, hii si tafsiri sahihi ya kuijenga thiolojia juu ya vibainishi tofauti vya asili ya mwanadamu. Msingi wa swali hili ni kule kurudiwa mara tatu "zote," si tofauti zilizo dhaniwa kati ya "moyo," "nafsi," na "akili." Kwa kunukuu, kukiri huku nukuu kwa upekee wa Mungu, kwa uvuvio Yesu ana uhusianisha uelewa wa Agano la Kale na Agano Jipya kumhusu Mungu. Agano Jipya ni utimilifu wa Agano la Kale. Sasa YHWH anafunuliwa kama Umoja wa Utatu. Upekee wake umeelezwa tena! Waamini wa Agano Jipya kwa ukamilifu wanaeleza juu ya Mungu Mmoja, lakini kwa tanbihi. Kwa uwazi kabisa maandishi wa Agano Jipya hawakuona dokezo la Zab. 110:1 kama mkanganyiko (kama vile 1 Kor. 8:6; Efe. 4:5; Flp. 2:11). Hapa kuna siri ya uhakika! Tazama Mada Maalum: Utatu katika Mt. 3:17.

**22:39** Amri ya pili haikupendekezwa na mwandishi, bali inaonyesha ule ulinganifu kati ya upendo wa waanini kwa Mungu na upendo wao kwa wanadamu wenzao unavyopaswa kuwa. Haiwezekani kumpenda Mungu huku tukiwachukia watu (kama vile 1 Yohana. 2:9, 11; 3:15; 4:20). Hii ni nukuu toka Law. 19:18.

**22:40** Yesu alikuwa akieleza kwamba Agano la Kale lina kiini mchanganyiko (yaani., upendo wa agano, kama vile Mt. 7:12; Marko 12:31; Rum. 13:8-10; Gal. 5:14). Amri mbili za Agano la Kale kwa uwazi zinatumiwa kwa waamini wa Agano Jipya. Upendo kwa Mungu hujieleza wenyewe katika kuwa kama Mungu, kwa sababu Mungu ni pendo (kama vile 1 Yohana 4:7-21).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 22:41-46**

<sup>41</sup>Na Mafarisayo walipokusanyika, Yesu aliwauliza, akisema, Mwaonaje katika habari za Kristo? <sup>42</sup>Ni mwana wa nani? Wakamwambia, Ni wa Daudi. <sup>43</sup>Akawauliza, Imekuwaje basi Daudi katika Roho kumwita Bwana, akisema, <sup>44</sup>Bwana alimwambia Bwana wangu, Uketi mkono wangu wa kuume, Hata niwawekapo adui zako Kuwa chini ya miguu yako? <sup>45</sup>Basi, Daudi akimwita Bwana, amekuwaje ni mwanawe? <sup>46</sup>Wala hakuweza mtu kumjibu neno; wala hakuthubutu mtu ye yote tangu siku ile kumwuliza neno tena.

**22:41-42** Viongozi wa Kiyahudi walimuuliza Yesu maswali kadhaa huku wakijaribu kumtega, na sasa anawauliza swali lililoonyesha ukosefu wao wa uelewa wa kiroho (kama vile Mt. 21:24-27).

**22:42 "Mwaonaje katika habari za Kristo? Ni mwana wa nani?"** Swali hili kimsingi lilijhusisha na mtiririko wa uzaowa Masihi. Yesu lilikubali jina la Agano la Kale la ki-Masihi "mwana wa Daudi." Hili ni jina la ki-Masihi lililozoeleka lililo katika Mathayo (kama vile Mt. 9:27; 12:23; 15:22; 20:30; 21:9,15). Yesu alikuwa akieleza wazi juu ya umasihi wake. Wayahudi wa nyakati za Yesu hawakuutarajia Uungu wenye umbile la kimwili bali Uungu wenye uweza kama Waamuzi. Yesu aliitumia Zab. 110 (kama vile Mt. 22:44) kuonyesha ntiririko wa uzao na mtiririko wa uzao wa Masihi

**22:44** Haya matumizi ya kimasihani yenye kufanana ya Zab. 110 yanapatikana katika Mt. 26:64. Andiko la Kiebrania la Zab. 110:1 lilikuwa la kebehi ya neno YHWH (Bwana) na Adonai (Bwana). La kwanza linawakilisha Mungu wa Israeli; na la pili linamrejelea Masihi.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Nini dhima kuu ya ufanano ulio katika Mt. 22:1-14?
2. Ni kwa namna gani unaeleza maneno makali ya Mt. 22:13?
3. Je! Mistari ya 15-22 inazungumzia suala la sasa la kujitenga na kanisa na utawala?
4. Orodhesha na kuyabainisha makundi ya kisiasa na kidini yaliyo kuwa Palestina nyakati za Yesu.
5. Kwa nini makundi haya yalikuwa yakijaribu "kumtega" Yesu? (Mt. 22:15)

## MATHAYO 23

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Shutuma za wandishi Na mafarisayo	Ole kwa wandishi na mafarisayo	Ole kwa wandishi na mafarisayo	Yesu anaonya dhidi ya mafundisho ya sheria Na mafarisayo	Wandishi na mafarisayo:unafiki wao na majivuno
23:1-12	23:1-36	23:1-12	23:1-12	23:1-7 23:8-12
			Yesu anashutumu Unafiki wao	Mashitaka saba ya walimu na Mafarisayo
23:13		23:13-15	23:13	23:13
23:14			23:14	23:14(haiusiki)
23:15			23:15	23:15
23:16-22		23:16-22	23:16-22	23:16-22
23:23-24		23:23-24	23:23-24	23:23-24
23:25-26		23:25-26	23:25-26	23:25-26
23:27-28		23:27-28	23:27-28	23:27-28
			Yesu anatabiri juu ya Hukumu yao	
23:29-36		23:29-36	23:29-36	23:29-32
				Makosa yao na Kuisogelea hukumu 23:33-36
Maombolezo kwa Ajili ya Yerusalemu	Yesu anaomboleza juu ya Yerusalemu	Maombolezo juu ya Yerusalemu	Upendo wa Yesu kwa ajili ya Yerusalemu	Onyo kwa ajili ya Yerusalemu
23:37-39	23:37-39	23:37-39	23:37-39	23:37-39 (39b)

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka [“Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia”](#))**

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembele katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## UTAMBUZI WA KIMUKTADHA

- A. Nafasi iliyopo kati Yesu na muundo wa nguvu za Kiyahudi katika Yerusalemu ulikua mkali sana.
- B. Yesu mara nyingi alijaribu kuwafikia wao lakini hawakutaka kuziacha tamaduni zao, dhana za utafu. Waliendelea kujaribu kumnasa kwa maswali. Maswali yao yalilenga mabishano (1) kati ya shule ya walimu wa sheria ya Hillel (wenye kupenda mabadiliko) na Shammai (wenye kufuata desturi) au (2) kati ya Warumi na watu wa Kiyahudi. Walitumaini kwamba Yesu atatenganisha kundi moja au jingine.
- C. Yesu alipolisafisha Hekalu (kama vile Yn. 2:15 na Mt. 21:12-17) kulizidisha mgogoro.
- D. Yesu alipoulaani mti wa mtini, kielelezo cha Israeli (kama vile Mt. 21:18-22), na mifano miwili kukataliwa (kama vile Mt. 21:28-46 na 22:1-14) ambayo ilikua ni ncha ya mwisho kuvunjwa.
- E. Sura hii inafikia kilele cha kukataliwa Yesu na viongozi wa kidini. Inatia mashaka ikiwa maneno ya Yesu yanaaksi kukataliwa kwa Israeli yote au kwa viongozi wake wa kidini pekee.
- F. Baadhi ya Biblia mfanano kwa fasihi yake ya viongozi wa kidini ni katika Marko 12:38-40, Luka 11:39-54, 20:45-47. Yesu alitumia lugha kali kuwaelezea hawa viongozi wa kidini.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 23:1-12

<sup>1</sup> Kisha Yesu akawaambia makutano na wanafunzi wake, akasema, <sup>2</sup> Waandishi na Mafarisayo wameketi katika kiti cha Musa; <sup>3</sup> basi, yo yote watakayowaambia, myashike na kuyatenda; lakini kwa mfano wa matendo yao, msitende; maana wao hunena lakini hawatendi. <sup>4</sup> Wao hufunga mizigo mizito na kuwatwika watu mabegani mwao; wasitake wenyewe kuigusa kwa kidole chao. <sup>5</sup> Tena matendo yao yote huyatenda ili kutazamwa na watu; kwa kuwa hupanua hirizi zao, huongeza matamvua yao; <sup>6</sup> hupenda viti vya mbele katika karamu, na kuketi mbele katika masinagogi, <sup>7</sup> na kusalimiwa masokoni, na kuitwa na watu, Rabi. <sup>8</sup> Bali ninyi msiitwe Rabi, maana mwalimu wenu ni mmoja, nanyi nyote ni ndugu. <sup>9</sup> Wala msimwite mtu baba duniani; maana Baba yenu ni mmoja, aliye wa mbinguni. <sup>10</sup> Wala msiitwe viongozi; maana kiongozi wenu ni mmoja, naye ndiye Kristo. <sup>11</sup> Naye aliye mkubwa wenu atakuwa mtumishi wenu. <sup>12</sup> Na ye yote atakayejikweza, atadhiliwa; na ye yote atakayejidhili, atakwezwa.

**23:1 "Yesu akawaambia makutano"** hii ilikua ni shutuma za wazi kwa viongozi wa kidini. Ingawa maneno yafuatayo hayatoi maelezo ya kila Mfarisayo, walikua wanaelezea shauku iliyozealewa na kundi.

**23:2 "waandishi"** hawa walikua stadi kwenye sheria zilizoandikwa (Agano la kale) na mapokeo ya sheria (kitabu cha maadili na sheria) za Israeli na zilizopatikana kwa kutumika mahali pale pale. Matokeo yake waliweka tena kazi ya desturi za Walawi za Agano la kale. Tazama mada maalum katika Mat. 12:38.

☐ **"Mafarisayo"** hili lilikua ni kundi la kamati ya utendaji ya Wayuhudi ambalo lilianzishwa nyakati za Wamakabayo. Waliyakubali maandiko yote ya Agano la kale na mapokeo ya fasihi simulizi kama mfunamano. Sio mafarisayo wote ni waandishi, lakini wengi wao ndio. Kwa ajili ya mjadala kamili wa asili na thiolojia ya Mafarisayo tazama mada maalumu katika Mt.22:15.

☐ **"kiti cha Musa"** hii inarejelea mafundisho ya mahali kwenye sinagogi la mahali au kwenye jamii husika ya Kiyahudi.

**23:3 "basi, yo yote watakayowaambia, myashike na kuyatenda"** Yesu alitumia amri mbili.



1. " kuyatenda" kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu

2. " myashike,"kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo

Yesu alisema kwamba ikiwa wataweza kuwaonyesha ukweli katika sheria, basi unaweza kutenda. Neno la Mungu ni kweli haijalishi ni nani analitangaza!

☐ **"lakini kwa mfano wa matendo yao, msitende "** mtindo wa maisha na shauku yao unafunua tabia zao. Katika maana walikua ni waalimu wa uongo wanaoelezewa kwenye Mt. 7:15-23. Hawakuwa wakitenda katika ukweli wa Mungu (kama vile Mt. 7:24-27), lakini tamaduni za wanadamu (kama vile Isa. 6:9-10; 29:13)!

**23:4 "Wao hufunga mizigo mizito"** hii ilikua ni sitiari ya kiutamaduni ambayo inarejelea kupita kiasi au uwekaji wa mizigo usiofaa kwa wanyama wa kufugwa (kama vile Mt. 11:28-30). Viongozi wa kidini hawakuonyesha huruma yeyote kwa ajili ya watu hali duni (kama vile Luka 11:46; Mdo 15:10). Wao wenyewe hawakuzitii sheria zao (kama vile. Rum. 2:17-24).

Kuna machapisho mbalimbali ya Kiyunani kwenye mstari huu. Inatia shaka kama tungo "ni vigumu kubeba" ni asili au uasilishaji kutoka Luka 11:46.

**23:5 "Tena matendo yao yote huyatenda ili kutazamwa na watu"** walikua ni viongozi wanaojionyesha hadharani (kama vile Mt. 6:2,5,16).

**NASB** kwa kuwa hupanua hirizi zao"

**NKJV, NRSV** "walifanya hirizi zao kuwa pana"

**TEV** "tazama mistari ya maandiko kwenye ukanda waliovaa kichwani na mikononi, na tambua namna ilivyo kubwa"

**JB** "wakivaa hirizi pana"

**NJB** "wakivaa hirizi vichwani"

Visanduku hivi vyeusi vya ngozi vilikua na maandiko ya Agano la kale ya Kut. 13:3-16, Kumb. 6:4-9, au Kumb. 11:13-21. Walivaa kwenye vipaji vya uso juu ya macho kidogo. Hii ilikua ni maana iliyo wazi ya Kut. 13:9 na Kumb. 6:8 na 11:18. Maandiko haya yalikua mwongozo wa nuru ya maisha ya waaminio, sio visanduku vyeusi kwenye vichwa vyao!

**NASB** "huongeza matamvua yao"

**NKJV** "hutanua matamvua yao"

**NRSV** "matamvua yao marefu"

**TEV** "kwa namna gani walivyoongeza matamvua kwenye majoho yao!"

**NJB** "matamvua marefu"

Hivi vilikua ni vishada vya rangi ya samawi kwenye majoho yao au kishada cha maombi ambacho kiliwakumbusha torati (kama vile Hes.15:38 na Kumb. 22:12).

**23:6** haya ni majaribu yale yale anayosimulia Yakobo na Yohana kwenye Mt. 20:20-28.

**23:7 "Rabi"** neno hili la Kiaramu lilikua ni jina la heshima (" mwalimu wangu"). Majina haya (rabi, baba, kiongozi) Yalikosolewa kwa sababu ya kiburi na kujisifu kwao kwenye karne ya kwanza ya Uyahudi. Viongozi walipenda kuitwa kwa majina ya heshima.

Toleo la NKJV linafuata toleo la Textus Receptus linalounganisha neno "Rabbi." Hii ni njia ya kiutamaduni ya (1) kuongeza kuambatana na ibada au (2) kuonyesha kupendwa (kama vile Mt. 23:37). Hata hivyo maandiko ya awali ya Kiyunani (X na B kama vile Vulgate) yana mara moja tu.

**23:8-10** tambua kutumika kulikorudiwa kwa "mmoja." Yesu (na Mathayo) hakuona kujipinga kwa imani ya kumwamini Mungu mmoja.

Tazama kifungu cha pili katika Mt. 22:37-38.

1. mwalimu wenu ni mmoja (anaweza kuwa Baba au Mwana, 22:36)
2. Baba yenu ni mmoja (mara mbili)
3. kiongozi wenu ni mmoja, ndiye Kristo

**23:8 "nanyi nyote ni ndugu"** waaminio wako sawa mbele za macho ya Mungu (yaani, Mwa. 1:26-27), hivyo basi, ni lazima tuwe makini na vipimo au majina! Hakuna tofauti ya mhudumu dhidi ya mtu wa kawaida kwenye Agano Jipya. Pia hakuna tofauti zingine, muhtasari Rum. 3:22; 1 Kor. 12:12-13; Gal. 3:28; Kol. 3:11.

**23:11 "Naye aliye mkubwa wenu atakuwa mtumishi wenu"** hili limejadiliwa kwenye Mt. 20:25-28 na Marko 10:42-44. Ni maelezo ya kushangaza! Hii inaweka alama tofauti kutoka kwenye dhamira ya ulimwengu. Ijapokuwa, hii ni ishara ya ukweli mkuu kwenye enzi mpya.

**23:12 "Na ye yote atakayejikweza, atadhiliwa"** hii ni dhana inayojirudia kibiblia (kama vile Ayu 22:29; Mit. 29:23; Luka 14:11; 18:14; Yakobo 4:6; 1 Pet. 5:5).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 23:13-14**

<sup>13</sup> Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnawafungia watu ufalme wa mbinguni; ninyi wenyewe hamwingii, wala wanaoingia hamwaachi waingie. <sup>14</sup> [Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnakula nyumba za wajane, na kwa unafiki mnasali sala ndefu; kwa hiyo mtapata hukumu iliyo kubwa zaidi.]

**23:13 "Ole wenu"** kifungu hiki (Mt. 23:13-36) kinafahamika kama "ole saba." Mathayo mara nyingi katika injili yake ametumia muundo wa vitu saba. Ole ni kinyume cha baraka. Katika mahubiri ya Yesu mlimani kuna mfanano wa Luka, aliongeza "ole" nne kwa kubarikiwa na Kristo (kama vile Mt. 5:3-11 dhidi ya Luka 6:20-26). Katika Agano la kale neno "ole" linatambulishwa kiunabii "maombolezo" au kilio. Ulikua ni muundo wa (yaani, mdundo wa Kiebrania au kipimo cha alama, msisitizo wa mistari ya mashairi) kama muziki wa maziko kuelezea hukumu ya Mungu.

☐ **"wanafiki"** hili lilikua ni neno la Kiyunani lililochanganywa lenye maana ya "kutoa hukumu." Lilikua neno la maonyesho lililotumika kuelezea anaacheza sehemu ya kuigiza au kuigiza nyuma ya ukweli halisi. Lilikua linatumika awali kwenye Mt. 6:2,5,16; 7:5; 15:7; 16:3; 22:18; na pia 24:51.

☐ **"Kwa kuwa mnawafungia watu ufalme wa mbinguni"** hii ilikua inatumia "funguo za ufalme" (kama vile. Mat. 16:19; Ufu. 1:18; 3:7). Ni wajibu gani wa kushangaza wa kuujua ukweli! Siku hizi, utu wa kidunia haujamkataa sana Yesu kama ulivyowakataa wawakilishi wake wa kanisa la sasa kwa maneno yetu, maisha na vipaumbele! Hiki ndicho viongozi wa kidini nyakati za Yesu walitenda pia. Kuna Mafarisayo wangapi kwenye kanisa la leo?

Hii inashangaza na maelezo ya kuhuzunisha (kejeli).

1. viongozi wa kidini hawakua na haki wao wenyewe na Mungu (kama vile. Mat. 5:20)
2. viongozi wa kidini waliwapotosha wengine na kuwazuia wasiwe wenye haki na Mungu (kama vile. Mat. 15:14; 23:16,24; 24:24; Rum. 2:19)

☐ **"wanaoingia"** kitenzi hiki kinafaa kutumika sehemu mpya ya ufalme wa Mungu wa matukio ya siku za mwisho (yaani, maagano mapya ya Yer. 31:31-34). Kila mmoja anaingia kwa kumpokea Yesu sasa! Wale wanaomkataa hawawezi kuingia (muhtasari Mat. 5:20; 7:21; 18:3; 19:23-24; 23:13).

**Yesu ndiye mlango pekee wa mbinguni (yaani, Yn. 1:12; 10:7-18; 14:6; Rum. 10:9-13).**

**23:14** Mstari wa 14 haumo kwenye machapisho ya Kiyunani A, B, D, au L, wala matoleo yote na, hivyo basi, yumkini ikawa sio asili katika Mathayo. Yumkini uliwekwa hapa na mtu aliyenakili kutoka Marko 12:40 au

Luka 20:47. Umejitokeza baadae kwenye machapisho ya Kiyunani kabla ya Mt. 23:13 na baadhi baada ya Mt. 23:13. Toleo la UBS<sup>4</sup> kwa kiasi limeacha "B" kama (kwa uhakika).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 23:15**

<sup>15</sup> Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnazunguka katika bahari na nchi kavu ili kumfanya mtu mmoja kuwa mwongofu; na akiisha kufanyika, mnamfanya kuwa mwana wa jehanum mara mbili zaidi kuliko ninyi wenyewe.

**23:15 "wanafiki"** tazama mada maalumu katika Mt. 6:2.

☐ "kumfanya mtu mmoja kuwa mwongofu" kuna aina mbili za kubadili dini kwa Kiyahudi: (1) wote walio tahiriwa, walibatizwa na kutoa sadaka y kuteketezwa-walioitwa "mlango wa waongofu" na (2) wale wa kawaida wanaohudhulia katika sinagogi- walioitwa "wacha Mungu."

☐ "mnamfanya kuwa mwana wa jehanum mara mbili zaidi kuliko ninyi wenyewe" haya ni kweli maelezo ya kushangaza. Yesu aliteswa kwa kutoishikilia sheria kwa unyoofo! Hii inaimarisha maelezo yake ya Mt. 5:20. Huu ni upinduaji wa maana sana kwa desturi iliyotarajiwa.

☐ "jehanamu" neno hili *Gehenna* linatokana na maneno mawili ya Kiebrania, "bonde" na "Hinomu." Hapa ndipo mahali miungu ya uzao ya Foinike ilikua inaabudiwa kusini mwa Yerusalemu kwenye bonde la Tofeti, kwa kuwatoa watoto sadaka [*molech*] (kama vile 2 Fal. 16:3; 17:17; 21:6; 2 Nya. 28:3; 33:6). Palikua ni mahali uchafu wa Yerusalemu. Yesu alitumia kama sitiari ya awali ya Jehanum na hukumu ya milele.

Neno hili lilitumiwa pekee na Yesu, isipokuwa kwa ajili ya Yakobo 3:6. Upendo wa Yesu kwa ajili ya anguko la mwanadamu haukumzuia yeye kuelezea matokeo ya kushangaza kwa kuyakataa maneno na kazi zake (kama vile Mt. 25:46). Ikiwa Yesu anadai ukweli wa umilele uliotenganishwa kutoka ushirika na Mungu, ni kweli kwamba wafuasi wake ni lazima wawe makini sana. Jehanum ni sikitiko kwa ajili ya mwanadamu, lakini pia imefungua jeraha linalovuja damu kwenye moyo wa Mungu lisiloweza kuponywa kamwe! Tazama mada maalum: wafu wako wapi? katika Mt. 5:22.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 23:16-22**

<sup>16</sup> Ole wenu viongozi vipofu, ninyi msemao, Mtu atakayeapa kwa hekalu, si kitu; bali mtu atakayeapa kwa dhahabu ya hekalu, amejifunga. <sup>17</sup> Wapumbavu ninyi na vipofu; maana ni ipi iliyo kubwa, ile dhahabu, au lile hekalu liitakasalo dhahabu? <sup>18</sup> Tena, Mtu atakayeapa kwa madhabahu, si kitu; bali mtu atakayeapa kwa sadaka iliyo juu yake, amejifunga. <sup>19</sup> Vipofu ninyi; maana ni ipi iliyo kubwa, ile sadaka, au ile madhabahu iitakasayo sadaka? <sup>20</sup> Basi yeye aapaye kwa madhabahu, huapa kwa hiyo, na kwa vitu vyote vilivyo juu yake. <sup>21</sup> Naye aapaye kwa hekalu, huapa kwa hilo, na kwa yeye akaaye ndani yake. <sup>22</sup> Naye aapaye kwa mbingu, huapa kwa kiti cha enzi cha Mungu, na kwa yeye aketiye juu yake.

**23:16 "viongozi vipofu"** hii ilikua ni sitiari ya kejeli kwa ajili ya viongozi wa kidini (kama vile Mt. 15:14; 23:16, 24).

**23:16-22 "atakiyeapa kwa"** Wayahudi waliimarisha utaratibu wa upanuzi ufaao na usiofaa kwa ajili ya viapo, wakitumia majina ya Mungu (kama vile Mt. 5:33-37; Yakobo 5:12). Ilikua ni njia ya kuruhusu udanganyifu pale wanapojitokeza kidini (kama vile Law.19:12; Kumb. 23:21).

☐ "wapumbavu ninyi" tazama mada maalumu katika Mt. 5:22.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 23:23-24**

<sup>23</sup> Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnalipa zaka za mnanaa na bizari na jira, lakini mmeacha mambo makuu ya sheria, yaani, adili, na rehema, na imani; hayo imewapasa kuyafanya, wala yale

**23:23 "wenu. . .wanafiki"** tazama mada maalumu katika Mt. 6:2.

☐ **"Kwa kuwa mnalipa zaka za mnanaa na bizari na jira "** katika kushikilia kwao sana sheria (kama vile. Law. 27:30-33; Kumb. 14:22-29), walitaja hata kikolezo kidogo hivyo kukusanya sehemu ya kumi kwa ajili ya Mungu, lakini hawakujali haki, upendo, na uaminifu. Agano jipya haliizungumzii zaka isipokuwa hapa. Moyo wa agano jipya tuliopewa haupatikani kwa asilimia (kama vile. 2 Kor. 8-9)!

Waaminio wa Agano jipya ni lazima kuwa makini juu ya kuwageuza Wakristo kuingia kwenye sheria mpya kama desturi (kitabu cha maadili na sheria za wakristo). Walitamani kumfulahisha Mungu kwa sababu walijitahidi kuutafuta mwongozo kwa ajili ya kila eneo la maisha. Hata hivyo, kitheolojia ni hatari kushikilia sheria za maagano ya kale ambazo hazikudhibitishwa tena kwenye Agano jipya na kuyafanya kuwa imani halali, hasa wanapotangaza kuwa itasabisha maafa au ahadi ya kustawi!

### **MADA MAALUMU: UTOAJI WA ZAKA**

Agano Jipya lina rejea chache kuhusu utoaji wa zaka. Siamini kuwa Agano Jipya linafundisha kuhusu utoaji wa Zaka kwasababu mazingira haya yote yako dhidi ya "utaftaji makosa" wa sheria za kiyahudi na kujihesabia haki (yaani Mt. 23:13-36). Ninaamini miongozo ya Agano Jipya kwa ajili ya kutoa mara kwa mara (ikiwa kupo kwa aina yoyote) kunapatikana katika II Wakorintho 8 na 9 (yaani ikirejea zawadi ya mara moja ya makanisa ya Mataifa kwenda kwa maskini wa kanisa mama la Yerusalemu), ambayo inakwenda zaidi ya kulipa zaka! Ikiwa Myahudi aliye na taarifa za Agano la Kale alikuwa ameamriwa kutoa asilimia kumi mpaka thelathini (kuna mbili, yawezekana tatu, aina za zaka zinazotakikana katika Agano la Kale: angalia Mada Maalumu: Zaka katika utungaji wa sheria ya Musa), hivyo wakristo lazima watoe sana zaidi na sio hata kuchukua muda wa kujadiliana kuhusu zaka!

Waamini wa Agano Jipya lazima wawe waangalifu juu ya kugeuza Ukristo katika utaratibu uliojikita katika utendaji wa kisheria (Christian Talmud). Shauku yao ya kumpendezesha Mungu iwasababishe wao kujaribu kutafuta miongozo kwenye kila eneo la maisha. Hata hivyo, kitheolojia ni hatari kuvuta kanuni za agano la kale ambazo hazijathibitishwa tena katika Agano Jipya (yaani Baraza la Yerusalemu la Mdo. 15) na kuzifanya kigezo cha kimafundisho ya madhehebu, na haswa wakati zinapokuwa zinadaiwa (na wahubiri wa kisasa) kuwa sababu ya machafuko au ahadi za utajiri (kama vile Malaki 3).

Hiii hapa ni nukuu nzuri kutoka kwa Frank Stagg, *New Testament Theology*, kurasa za 292-293:

"Agano Jipya kwa mara moja halitambulishi utoaji wa zaka katika neema ya kutoa. Utoaji wa zaka unatajwa mara tatu tu katika Agano Jipya:

1. Kuwakemea Mafarisayo kwa kupuuzia haki, rehema na imani wakati wakijali kwa sana juu ya utoaji wa zaka mpaka wa mazao ya bustani (Mt. 23:23; Luka 11:42);
2. Katika kufunua Farisayo mwenye majivuno ambaye 'alikuwa akijiombea,' akijivuna kuwa alikuwa akifunga mara mbili kwa wiki na kutolea zaka kila mali zake (Luka 18:12);
3. katika kubishania hoja ya ukuu wa Melkizedeki, na hivyo wa Kristo, kwa Walawi (Ebr. 7:6-9).

"Ni wazi kwamba Yesu alikubaliana na utoaji zaka kama sehemu ya mfumo wa hekalu, kama katika kanuni na desturi za jumla za Hekalu na Sinagogi alizoziunga mkono, lakini hauna dalili kwamba alifanya lazima sehemu yoyote ya desturi za hekaluni juu ya wafuasi wake. Zaka kwa sehemu kuu zilikuwa za mazao, hapo kabla zililiwa katika madhabahu na yule anayetoa zaka na baadaye kuliwa na makuhani. Zaka kama inavyoanzishwa baadaye katika Agano la Kale ingeweza kubebwa nje tu katika mfumo wa kidini uliojengwa kuzunguka mfumo mzima wa dhabihu za wanyama."

"Wakristo wengi wanaona zaka kama mpango sawa na unaotekelezeka kwa ajili ya utoaji. Ikiwa haitofanywa kuwa jambo la lazima au mfumu wa kisheria, inaweza kuthibitishwa kuwa mpango mzuri. Hata hivyo mtu anaweza asidai kihaki kwamba utoaji wa zaka unafundishwa katika Agano Jipya. Unatambuliwa kama utaratibu wa kuangaliwa sahihi wa Kiyahudi (Mt. 23:23; Luka 11:42), lakini hauwi wa lazima juu ya Wakristo. Kusema ukweli, sasa haiwezekani kwa Wayahudi au Wakristo kutoa zaka katika namna ya Agano la Kale. Kutoa zaka leo

kwa kufifia tu kunafanana na taratibu za kiibada zilizokuwa zikifanyika juu ya mfumo wa kidhabihu za Wayahudi.”

Stagg anahitimisha:

“Wakati mengi yanaweza kusemwa kwa kuuchukua utoaji wa zaka kama kutoa kwa hiari kama kipimo cha utoaji wa mtu bila kwa mkao wa kulazimisha juu ya wengine kama matakwa ya Kikristo, ni wazi katika kufanya taratibu hizi kwamba mtu habebe utaratibu wa Agano la Kale. Wakati mtu anafanya kitu Fulani kidogo anakuwa anahusianisha na taratibu za utoaji wa Ahgano la Kale, ambayo ilikuwa ni kodi kusaidia hekalu na mfumo wa makuhani, jamii na mfumo wa kidini ambao haupo tena. Zaka zilikuwa ni lazima katika dini ya Kiyahudi kama kodi mpaka uharibifu wa Hekalu katika mwaka wa 70 B.K, lakini hawafunganishi hivyo kwa Wakristo.

“Hii sio kukosoa utoaji wa zaka lakini ni kufafanua uhusiano wake kwa Agano Jipya. Ni kukataa kwamba Agano Jipya linasaidia ulazima, kuwekeana sheria, nia ya kutengeneza faida na maelewano ya kimatoleo ambavyo mara kwa mara vianweka tabia ya ukataji rufaa wa utoaji zaka siku za leo. Kama mfumo huru, utoaji zaka unasaidia mengi; lakini lazima ukombolewe kwa neema ikiwa unataka uwe wa kikristo. Kuomba kwamba ‘unafanya kazi’ ni kufanyika kuwa majaribio ya kinadharia ya kivitendo ya kiulimwengu. ‘Kusumbukiwa’ sana huo sio ukristo. Utoaji zaka, ikiwa unataka uwe wa kupendeza, lazima uwe katika mizizi ya neema na upendo wa Mungu.”

**23:24 "wenye kuchuja mbu na kumeza ngamia"** Mafarisayo wa siku za Yesu waliweza kuchuja maji kwa kutumia nguo ili wasije wakameza wadudu najisi, lakini kwenye ukweli kushikilia sheria kusiko na upendo kulisababisha wao kuwa kielelezo cha kumeza ngamia najisi! Huu ni mchezo wa maneno kati ya maneno ya Kiaramu ya aina ya visubi, "*galma*" na ngamia, "*gamla*." Hii ilikua ni utiaji chumvi sana katika kuelezea kitu. Yesu mara nyingi alitumia Ngamia katika maneno yake ya kutia chumvi (kama vile. Mat. 19:24; Marko 10:25; Luka 18:25).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 23:25-28**

<sup>25</sup> Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnasafisha nje ya kikombe na chano, na ndani yake vimejaa unyang'anyi na kutokuwa na kiasi. <sup>26</sup> Ewe Farisayo kipofu, safisha kwanza ndani ya kikombe, ili nje yake nayo ipate kuwa safi. <sup>27</sup> Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mmefanana na makaburi yaliyopakwa chokaa, nayo kwa nje yaonekana kuwa mazuri, bali ndani yamejaa mifupa ya wafu, na uchafu wote. <sup>28</sup> Vivyo hivyo ninyi nanyi, kwa nje mwaonekana na watu kuwa wenye haki, bali ndani mmejaa unafiki na maasi.

**23:25 "wanafiki"** tazama mada maalumu katika Mat. 6:2.

☑ **"Kwa kuwa mnasafisha nje ya kikombe"** walikua wakihusisha usafi na tamaduni, lakini mtizamo na shauku yao ilikua mbali na Mungu (kama vile. Isa. 29:13). Walikua najisi ndani yao (yaani, moyo, kama vile. Marko 7:15,20). Kiwango kipya cha haki (yaani, maagano mapya, kama vile Yer. 31:31-34; Ezek. 36:22-38) kilikua sio utendaji wa mwanadamu, lakini imani katika haki ya Kristo iliyonunuliwa pale Kalvali na kudhibitishwa jumapili ya pasaka!

**23:27 " makaburi yaliyopakwa chokaa "** wakazi wa Yerusalem walipanga rangi nyeupe makaburi kabla ya siku ya sikukuu ili mahujaji kwa bahati mbaya wasiyaguse na kuwa najisi kwa siku saba kwa utaratibu wa sheria, na kwa maana hiyo hawezi kujumuika kwenye sikukuu hata kama alisafiri kwa umbali mrefu kuja kwenye sikukuu (kama vile Hes. 19:16; 31:19). Upakaji rangi huu mpya wa makaburi ulikua unafanana na mwonekano wan je wa viongozi wa Kiyahudi.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 23:29-33**

<sup>29</sup> Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnayajenga makaburi ya manabii, na kuyapamba maziara ya wenye haki, <sup>30</sup> na kusema, Kama sisi tungalikuwako zamani za baba zetu,

hatungalishirikiana nao katika damu ya manabii. <sup>31</sup> Hivi mwajishuhudia wenyewe, ya kwamba ninyi ni wanao wao waliowaua manabii. <sup>32</sup> Kijazeni basi kipimo cha baba zenu. <sup>33</sup> Enyi nyoka, wana wa majoka, mtaikimbiaje hukumu ya jehanum?

**23:29 "wanafiki"** tazama mada maalumu katika Mt. 6:2.

☐ " **Kwa kuwa mnayajenga makaburi ya manabii** " katika Agano la kale watu wa Mungu waliweza kuwaua manabii wa Mungu na kisha kujenga makaburi makubwa kwa ajili yao. Ujenzi wa kumbukumbu ya mnenaji wa Mungu sio kitu ambacho Mungu alitaka. Alitamani utiifu kwa ujumbe wake (kama vile Mt. 23:34-35). Kama ambavyo viongozi wa Agano la kale waliwaua manabii, viongozi hawa walimuua Yesu na wafuasi wake.

**23:30 "kama"** hii ni sentensi amrishi daraja la pili, ambayo inaitwa "kinyume cha ukweli." Kauli iliyofanywa ni ya uongo na kwamba, hivyo basi, hitimisho la kusambaratika kwake pia ni la uongo.

**23:33 "Enyi nyoka, wana wa majoka"** Yesu mara zote hakuwa mpole na mnyenyekevu, "kumgeuzia shavu lingine" mwanadamu mara nyingi anaelezewa katika taswira (kama vile Mt. 3:7; 12:34). Kujihesabia haki viongozi wanafiki kulivuta hukumu kali na bado inaendelea!

☐ "**jehanum**" tazama mada maalumu katika Mt. 5:22.

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 23:34-36**

<sup>34</sup> Kwa sababu hiyo, angalieni, mimi natuma kwenu manabii na wenye hekima na waandishi; na wengine wao ninyi mtawaua na kuwasulibisha, na wengine wao mtawapiga katika masinagogi yenu, na kuwafukuza mji kwa mji; <sup>35</sup> hivyo ije juu yenu damu yote ya haki iliyomwagika juu ya nchi, tangu damu ya Habili, yule mwenye haki, hata damu ya Zakaria bin Barakia, mliyemwua kati ya patakatifu na madhabahu. <sup>36</sup> Amin, nawaambieni, Mambo hayo yote yatakuja juu ya kizazi hiki.

**23:34 "mimi natuma kwenu manabii na wenye hekima na waandishi "** Mungu (muhtasari Yesu alitumia "mimi") anaendeleza hali ya utendaji wa ufunuo kupitia wanenaji wake aliowachagua (kama vile. Mat. 21:34-36; 23:37). Wayahudi hawakua wajinga wasiojua kweli ya Mungu; walichagua kuikataa kwa ajili ya tamaduni zao (kama vile. Isa. 6:9-13; 29:13; Yer. 5:20-29)! Tazama [MADA MAALUM: UNABII WA AGANO JIPYA](#) katika Mat. 11:9.

☐ "**wengine wao ninyi mtawaua na kuwasulibisha** " utabiri wa mateso makali ulitimia kwenye siku za awali za Ukristo. Wanenaji wa Mungu mara nyingi walikusanya uadui wa anguko la mwanadamu, na hata mwanadamu wa kidini, dhidi ya neno na mapenzi ya Mungu.

**23:35 "damu iliyomwagika"** tazama mada maalumu inayofuata.

#### **MADA MAALUM: ILIYOMWAGIKA (AGANO JIPYA)**

Neno la kitamaduni la Kiyunani *cheō* linamaanisha "kumwaga" (mara nyingi ni kwa maana iliyo wazi). Kwa maana ya iliyokuzwa neno, *ekcheō*, linachukua nafasi yake na kutengeneza madokezo mawili.

1. Damu ilimwagika isiyo na hatia, kama vile Mwa. 9:6; 37:22; Kumb. 19:10; Mt. 23:35; Mdo. 22:20; Rum. 3:15
2. Dhahihu iliyotolewa, kama vile Amu. 6:20; 1 Sam. 7:6; 2 Sam. 23:16; Mt. 26:28; Marko 14:24; Luka 22:20

Kwa Yesu maana hizi mbili zilikutana pale Kalvari (kama vile Colin Brown, ed., *The New International Dictionary of New Testament Theology* juzuu ya 2, kur. 853-855).

Biblia pia inatumia KITENZI hiki katika kuhusianisha na

1. Kumwaga kwa Roho Mtakatifu (kama vile Yoeli 2:28-29; Ezek. 39:29; Zek. 12:10; Mdo. 2:17-18,33; 10:45; Tito 3:6)
2. Upendo wa Mungu (kama vile Rum. 5:5; kumbuka ufanano wa kithiolojia katika Gal. 4:6)
3. Ghadhabu ya Mungu (kama vile Ufunuo 16, KITENZI kimetumika mara nane)

☐ **"Habili"** tazama Mwa. 4:8nakuendelea.

☐ **"Zakaria"** kuna mjadala mkubwa hapa kama ni nabii gani anarejelewa. Anaefahamika kwa mateso ambae kwa jina lake anapatikana kwenye 2 Nya. 24:2-22, lakini jina la baba yake ni tofauti kutokana na rejea hii. Hata hivyo mfanano kwenye Luka 11:51 unaliacha jina la baba, kama lilivyofanya toleo la Kiyunani MSS  $\times$  kwenye Mathayo.

Zakaria, nabii baada ya uhamisho, alikua na hili jina lakini hakuwawa kwa jambo hili. Inawezekana kuna nabii mwingine kwa jina hili hatujui chochote juu yake. Hata hivyo, tangu Habili wa kwanza kufa kwa mateso kwenye Agano la kale kisha Zakaria anatajwa kwenye 2 Nya. 24 anaweza kuwa ni wa mwisho kuteswa kwa sababu Kitabu cha Mambo ya Nyakati ni kitabu cha mwisho cha waebrania kilichowakifshwa.

**23:36 "Mambo hayo yote yatakuja juu ya kizazi hiki"** kwa maana moja hii inaonyesha fahali zaidi ya Yesu (kama vile Mt. 10:23; 23:36; 24:34). Yeye ni mnenaji wa Mungu wa mwisho. Viongozi na watu kwa ujumla walipomkataa yeye, kulikua hakuna tumaini-ila hukumu pekee. Enzi mpya ya Roho imekuja!

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 23:37-39**

<sup>37</sup> Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka! <sup>38</sup> Angalieni, nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa. <sup>39</sup> Kwa maana nawaambia, Hamtaniona kamwe tangu sasa, hata mtakaposema, Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana.

**23:37-39** Yesu ni dhahili alijazwa na mchomo wa moyo (kama vile. Luka 13:34,35). Yeye na Baba wote wanawapenda watu wa maagano. Alivumilia kurejesha ushirika na wao, lakini waliambatana na kushikilia sheria zao (Isa. 29:13). Hukumu pekee ndio inaweza kuanzisha tena mahusiano ya maagano!

Swali linabakia, ni lini Yesu aliyasema maneno haya? Je ni wakati kabla ya kuingia ushindi au je unarejelea kuingia kwa matukio ya siku za mwisho? Jambo moja ni hakika, unabii wa Zak. 12:10 utatimia siku moja! Muunganiko wa watu wa Mungu unaozungumziwa kwenye Warumi 9-11 utarejesha ushirika wa bustani ya Edeni (kama vile Mwa. 3:15).

**23:37 "kuwakusanya"** kitenzi hiki pia kimetumika kuwakusanya waliochaguliwa wakati wa mwisho kwenye Mat. 3:12; 13:20,47; 24:31.

☐ **"kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabawa yake"** YHWH na Yesu mara nyingi wametumia sitiari ya kiume kuelezea kazi na mtizamo yao (kama vile Mwa. 1:2; Kut. 19:5; Kumb. 32:11; Isa. 49:15; 66:9-13). Uungu ni kama kiume si kike, lakini Roho. Aliumba jinsia na ana ubora zaidi kwa zote katika yeye.

#### **MADA MAALUM: KIVULI (kwa kutumia tungo kadhaa zinazofanana)**

Hii ni Nahau ya Kiebrania kwa ajili ya

1. "kivuli" kama ulinzi
  - a. wa YHWH – Isa. 16:3-4
  - b. wa Misri – Isa. 30:2-3
  - c. wa Masihi wa YHWH – Omb. 4:20
2. "kivuli cha mkono," pia ni ulinzi wa YHWH – Zab. 121:5; Isa. 49:2; 51:16; pia muhtasari Kut. 33:22)

3. "kivuli cha juu yangu," Nahau nyingine kwa ajili ya ulinzi – Mwa. 19:8
4. "kivuli cha YHWH wingu maalum wakati wa nyikani kipindi cha kuzunguka" (yaani., wingu mchana , usiku Nuru kuwalinda wao) – Kut. 13:21-22; 14:19,20,24; Isa. 4:6; 25:4-5; 32:1-2
5. "kivuli cha mbawa" –Nahau ya Kiebrania ya Mungu kama Ndege mwenye kifaranga – Zab. 17:8; 36:7; 57:1; 61:4; 91:1,4; Isa. 31:5 (sawa na taswira katika Kumb. 32:10-11; Ruth 2:12; Mt. 23:37; Luka 13:34)
6. "kivuli cha mti"
  - a. mfano wa uhusiano na Abimeleki – Amu. 9:15
  - b. mfano wa Tai na Mzabibu – Ezek. 17:23
  - c. mfano wa Misri – Ezek. 31:6,17
  - d. ndoto ya Nebukadnezza – Dan. 4:12
  - e. taswira ya kutekwa Israeli – Hosea 14:7

kivuli kina nguvu, kuokoa - maisha sitiari kwa ajili wa watu wa jangwani.

**23:38 "nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa"** hili limejitokeza kuwa dokezo kwa Yer. 22:5. Inaweza kurejelea maangamizi ya Yerusalem kwenye mwaka wa 70 K.K. au kwa baadhi ya matukio yajayo. Maagano pekee ya Mungu na Israeli yalikuwa ya mwenzi kwa kutokua na imani! Kuna maagano mapya (kama vile Yer. 31:31-34), ambao hausisitizwi katika jamii iliyodhaifu, lakini katika imani na uaminifu kwa Mungu na Masihi wake.

**23:39 "hata mtakaposema"** hii ni rejea katika Zab. 118:26-27, ambayo imetumika kwenye ushindi (kama vile. Mat. 21:9). Hii inafanana na utabiri wa ajabu wa kimasihwa wa Zak. 12:10 kwamba siku moja wayahudi watamrudia yeye waliyemchoma (kama vile. Warumi 9-11)! Waaminio wote waombe kwa ajili ya uamsho wa Wayahudi!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. kwa nini Yesu alikua hatari kwa viongozi wa kidini katika siku zake?
2. kwa jinsi gani tunafahamu kwamba tunaamini na desturi?
3. je dhamira ni ya maana zaidi kuliko matendo?
4. je zaka imefundishwa kwa wazi katika kanuni za Agano jipya?
5. je Yesu aliwakataa Israeli kabisa?



## MATHAYO 24

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA				
UBS <sup>4</sup>	NKJV	NRSV	TEV	NJB
Kuharibiwa kwa Hekalu kunatabiriwa Kabla	Yesu anatabiri Kuharibiwa kwa Hekalu	Kuharibiwa kwa hekalu Kunatabiriwa kabla	Yesu anazungumzia Kuharibiwa kwa Hekalu	Utangulizi
24:1-2	24:1-2	24:1-2	24:1-2	24:1-3
Mwanzo wa Ole	Ishara za Nyakati	Mwisho wa nyakati	Mateso na Dhiki	Mwanzo wa Huzuni
24:3-14	24:3-14	24:3-8	24:3	
		24:9-14	24:4-8	24:4-8
			24:9-14	24:9-13
				24:14
Dhiki Kuu	Dhiki Kuu		Hofu Kuu	Dhiki Kuu ya Yerusalemu
24:15-28	24:15-28	24:15-28	24:15-22	24:15-22
			24:23-25	24:23-25
Kuja kwa Mwana wa				Adamu
			24:26-27	24:26-28
			24:28	
Kuja kwa Mwana Wa Adamu	Kuja kwa Mwana Wa Adamu		Kuja kwa Mwana Wa Adamu	Umuhimu wa kiujumla Wa Ujio Huu
24:29-31	24:29-31	24:29-31	24:29-31	24:29-31
Somo la Mtini	Mfano wa Mtini		Somo la Mtini	Muda wa Ujio Huu
24:32-35	24:32-35	24:32-35	24:32-35	24:32-36
Siku na Saa	Hakuna aijuaye Siku		Hakuna aijuaye	Kuweni Macho
Isiyojulikana	Wala Saa		Siku wala Saa	
24:36-44	24:36-44	24:36-44	24:36-44	24:37-41
				24:42-44
Mtuma Mwaminifu Au asiyemwaminifu	Mtumwa mwaminifu Au Mtumwa muovu		Mtumwa Mwaminifu Au asiyemwaminifu	Mfano wa Mtumwa Anayejitambua
24:45-51	24:45-51	24:45-51	24:45-51	24:45-51

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka [“Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia”](#))**

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiaya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA 24:1-36 (Inafanana na Marko 13:1-37)

- A. Dokezo langu la ufafanuzi wa maandiko juu ya Marko 13 limekamilishwa zaidi katika fasiri yangu mtandaoni katika Marko na 1 & 2 Petro. Unaweza kuona fasiri zangu zote katika [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org).
- B. Mt. 24, Marko 13, na Luka 21 ni ngumu sana kufasiri kwasababu zinashughulikia maswali kadhaa kwa pamoja (kama vile Mt. 24:3).
1. Je ni lini Hekalu litaharibiwa?
  2. Ni nini itakuwa ishara ya Kurudi kwa Masihi?
  3. Je nyakati hizi zitaisha lini?
- C. Aina ya vifungu vya kimaandiko vilivyobeba aina ya fasihi ya matukio ya siku za mwisho ya Agano Jipya siku zote ni muunganiko siku za mwisho (angalia Mada Maalum hapa chini) na lugha ya kinabii ambayo kimakusudi ni tata na yenye kubeba viwakilishi.
- D. Vifungu kadhaa katika Agano Jipya (kama vile Mt. 24, Marko 13, Luka 17 na 21, 1 na 2 Thes. na Ufunuo) Inashughuliakia na Kuja kwa mara ya Pili. Vifungu hivi vinasisitiza
1. muda halisia wa tukio haujulikani bali tukio lazima litukie
  2. Tunaweza kujua muda wa kawaida lakini si muda halisi wa matukio
  3. itatokea ghafla na bila kutarajia
  4. Lazima tukae kwenye maombi, tuwe tayari na waaminifu kwenye kazi tulizopewa
- E. Kuna uvutano wa ukinzani wa kithiolojia kati ya (1) muda wowote wa kurudi (kama vile Mt. 24:27,44) dhidi ya (2) ukweli kwamba baadhi ya matukio katika historia lazima yatokee.
- F. Agano Jipya linasema kwamba baadhi ya matukio yatatokea kabla ya Kuja kwa Mara ya Pili:
1. Injili itahubiriwa kwa ulimwengu wote (kama vile Mt. 24:14; Marko 13:10)
  2. Ukanaji wa imani mkubwa (kama vile Mt. 24:10-13, 21; 1 Tim. 4:1; 2 Tim. 3:1 na kuendelea.; 2 Thes. 2:3)
  3. Ufunuo wa "mtu wa dhambi" (kama vile Dan. 7:23-26; 9:24-27; 2 Thes. 2:3)
  4. kuondolewa kwa kile na Yule anayekuwa kwazo (kama vile 2 Thes. 2:6-7)
  5. uamsho wa Kiyahudi (kama vile Zek. 12:10; Rum. 11)
- G. Mistari ya 37-44 haifanani na ile ya Marko. Kuna ufanano wa juu juu wa Kivitabu katika Luka 17:26-37.

### **MADA MAALUM: FASIHI YA MATUKIO YA SIKU ZA MWISHO (kutoka Utangulizi wa kitabu cha Ufunuo)**

Kitabu cha Ufunuo ni aina ya kipekee ya fasihi ya Kiyahudi, matukio ya siku za mwisho. Mara nyingi hii ilitumika katika nyakati zilizojaa mvutano uyakini kwamba Mungu alikuwa katika mamlaka ya historia na angeleta ukombozi kwa watu Wake. Hii aina ya fasihi inabainishwa na

1. maana nzito ya ukuu wa Mungu kiulimwengu (Mungu aliye mmoja na kuashiliwa)
2. mapambano kati ya wema na uovu, zama hizi na zama zijazo (dhana ya uwili)
3. matumizi ya mfumo wa maneno ya siri (mara nyingi kutoka Kitabu cha Agano la Kale au fasihi ya Kiyahudi ya matukio ya siku za mwisho katika Kipindi cha Agano la Kale na Agano Jipya)
4. matumizi ya rangi, namba, wanyama, wakati mwingine wanyama/wanadamu
5. matumizi ya upatanisho wa kimalaika kwa maana ya maonona ndoto, lakini mara nyingi kupitia upatanisho wa kimalaika
6. mitazamo ya mwanzo juu ya nyakati za mwisho (zama mpya)
7. matumizi ya muonekano wa ishara, si ukweli, ili kupasha habari ya nyakati za mwisho

8. Baadhi ya mifano ya hii aina hii ya fasihi ni
  - a. Agano la Kale
    - 1) Isaya 24-27, 56-66
    - 2) Ezekieli 37-48
    - 3) Danieli 7-12
    - 4) Joeli 2:28-3:21
    - 5) Zekaria 1-6, 12-14
  - b. Agano Jipya
    - 1) Mathayo 24, Maro 13, Luka 21, na 1 Wakorintho 15 (katika njia nyingine)
    - 2) Ufunuo (sura 4-22)
  - c. isiyo ya umbo- mwili (ilichukiliwa kutoka D. S. Russell, *The Method and Message of Jewish Apocalyptic*, kr. 37-38)
    - 1) I Enoch, II Enoch (the Secrets of Enoch)
    - 2) The Book of Jubilees
    - 3) The Sibylline Oracles III, IV, V
    - 4) The Testament of the Twelve Patriarchs
    - 5) The Psalms of Solomon
    - 6) The Assumption of Moses
    - 7) The Martyrdom of Isaiah
    - 8) The Apocalypse of Moses (Life of Adam and Eve)
    - 9) The Apocalypse of Abraham
    - 10) The Testament of Abraham
    - 11) II Esdras (IV Esdras)
    - 12) Baruch II, III
9. Kuna maana ya uwili katika fasifi hii. Hii inauangalia ukweli kama mtiririko wa uwili, tofauti, au mvutano (ni kawaida sana katika maandiko ya Yohana) kati ya:
  - a. mbingu – dunia
  - b. zama za uovu (wanadamu wa uovu na malaika wa uovu) – zama mpya za wenye haki (watu wa Mungu na malaika wa Mungu)
  - c. Kuwepo kwa sasa – kuwepo kwa baadaye

Hizi zote zinaelekea utimilifu ulioletwa na Mungu kumhusu Mungu. Huu si ulimwengu alioukusudia Mungu kuwa, bali Yeye azidi kutenda kazi na kuonyesha mapenzi yake kwa ajili ya urejesho wa uhusiano wa karibu ulionzia ndani ya Bustani ya Edeni. Tukio la Kristo ni mpango wa Mungu wa umwagaji maji, lakini ujio mbili unasababisha uwili wa sasa.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 24:1-2

<sup>1</sup> Yesu akaenda zake, akatoka hekaluni; wanafunzi wake wakamwendea ili kumwonyesha majengo ya hekalu.

<sup>2</sup> Naye akajibu akawaambia, Hamyaoni haya yote? Amin, nawaambieni, Halitasalia hapa jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomoshwa.

**24:1 "hekaluni"** Hili lilikuwa neno la Kiyunani kwa ajili ya eneo zima la hekalu (*hieron*, kama vile Marko 13:1). Yesu amekuwa akifundisha kule tokea Mt. 21:23. Jengo hili lenyewe (*naos*, kama vile Marko 15:38) lilikuwa limefanyika tumaini kubwa la Wayahudi (kama vile Yereimia 7), ishara ya upendo wa Mungu usio na masharti.

☛ **"majengo"** Yalikuwa yenye kupakwa chokaa nyeupa yakiwa na mkanda wa dhahabu. Jengo hili lilimchukua Herode Mkuu zaidi ya miaka 46 kulijenga na kulikamilisha (kama vile Yohana. 2:20). Mradi huu ulikuwa

umekusudiwa kusuuza mioyo ya Wayahudi waliokuwa na simanzi na hasira kwa sababu ya Idumaya (Edomu) waliokuwa wakiwatawala wao.

**24:2 "jiwe"** Josephus anatwambia kwamba Herode Mkuu alitumia chokaa nyeupe au *mezzeh*, ambayo ilikuwa inapatikana kwa asili katika eneo hili. Msingi wa mawe na ukuta wa mawe ulikuwa mkubwa sana, kipimo cha 25x8x12 cubit (cubit moja ilikuwa sawa na inchi 18- 21; hivyo ujazo kamili ulikuwa cubit futi 3600).

☐"**Halitalia hapa jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomoshwa**" Huu ni muundo wenye nguvu wa kisarufi wa kanushi mbili. Hii inzungumzia uharibifu wa moja kwa moja. Hii lazima ilikuwa imewafanya wanafunzi wafunge midomo yao kama mabubu! Josephus anatwambia kwamba mnamo mwaka 70 B.K. Jeshi la Kirumi liliharibu eneo hili kabisa kabisa kiasi kwamba hakuna mtu angeweza kulima katika ardhi juu ya Mlima Moria (kama vile Mika. 3:12; Yer. 26:18) ambapo hekalu lilikuwa.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 24:3**

<sup>3</sup> **Hata alipokuwa ameketi katika mlima wa Mizeituni, wanafunzi wake wakamwendea kwa faragha, wakisema, Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia?**

**24:3 "ameketi katika mlima wa Mizeituni"** Sehemu hii ya mwinuko ilitazama Yerusalemu na eneo la Hekalu. Injili ya Marko inabainisha wanafunzi waliomuuliza Yesu maswali haya kuwa ni Petro, Yohana, Yakobo na Andrea. Mathayo inasomeka "wanafunzi wakamwendea. . .kwake Yeye" (kama vile Mt. 24:1 na 3).

☐"**mambo hayo yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja kwako**" Marko 13:4 na Luka 21:7 walikuwa na swali moja tu, japo Mt. 24:3 inaonesha upana wa swali. Kulikuwa na matukio kadhaa ambayo wanafunzi walitaka kujua kuhusu: (1) kuharibiwa kwa hekalu, (2) Kuja kwa Mara ya Pili na (3) Mwisho wa Dunia. Wanafunzi yawezekana walifikiria kwamba yote haya yangetokea kwa wakati mmoja. Angalia Mada Maalum inayofuata.

Maneno yaliyotumika hapa "kuja" (kama vile Mt. 24:3,27,37,39; 1 Kor. 15:23; 1 Thes. 2:19; 3:13; 4:15; 5:23; 2 Thes. 2:1,8; Yakobo 5:7,8; 2 Pet. 1:16; 3:4,12; 1 Yohana 2:28) ni *parousia*. Angalia Mada Maalum ya pili hapa chini.

#### **MADA MAALUM: MAJIBU YA MASWALI MAWILI YA WANAFUNZI YAHUSIANAYO NA KURUDI KWA YESU KATIKA MATHAYO 24:3**

(Na F. F. Bruce katika *Answers to Questions*, ukurasa wa 57).

Onyo dhidi ya kupotezwa na manabii wa uongo au majanga makuu kwa kufikiri kuwa huu ndiyo mwisho

1. Mt. 24:4-8

2. Marko 13:5-8

3. Luka 21:8-11

Utabiri wa mateso na ahadi kwa ajili ya msaada

1. Mt. 24:9-14

2. Marko 13:9-13

3. Luka 21:12-19

Majibu kwa swali la kwanza kuhusiana na uharibifu wa Yerusalemu na kutawanyika kwa wakazi wake

1. Mt. 24:15-28

2. Marko 13:14-23

3. Luka 21:20-24

Jibu la swali la pili ilikielezea kuja kwa Kristo

1. Mt. 24:29-31

2. Marko 13:24-27

3. Luka 21:20-24

Onyo juu ya kukesha katika hali inayoweza kupelekea kuanguka kwa Yerusalemu

1. Mt. 24:32-35
2. Marko 13:28-31
3. Luka 21:29-33

Onyo juu ya kukesha kwa ajili ya kuja kwa Kristo

1. Mt. 24:36-44
2. Marko 13:32-37
3. Luka 21:34-36

## MADA MAALUM: MANENO KWA UJIO WA PILI

Kuna maneno na vifungu kadhaa ambavyo vinarejea juu ya kurudi kwa Yesu.

1. *parousia*" yaani, Yakobo 5:7), ambalo linamaanisha "kuwepo," lililotumika kifalme (kama vile Mt. 24:3,27,37,39; 1 Kor. 15:23; 1 The. 2:19; 3:13; 4:15; 5:23; 2 The. 2:1,8; 2 Pet. 1:16; 3:4,12; 1 Yohana 2:28)
2. *epiphaneia*, "mwonekano wa ana kwa ana" (yaani, 1 Tim. 6:14; 2 Tim. 1:10; 4:1,8; Tito 2:13)
3. *apokalupis*, "kufunua" au "kuonyesha" (yaani, 1 Kor. 1:7; 2 The.1:7; 1 Pet. 1:5,13; 4:13; 5:1)
4. "siku ya Bwana" na mabadiliko ya kifungu hiki (angalia Mada Maalum: Siku ya Bwana)

Kitabu cha Agano Jipya kama kilivyo kizima kimeandikwa ndani ya mtazamo wa ulimwengu wa Agano la Kale, ambao unadai kwamba

1. uovu wa sasa, zama za uasi
2. zama mpya za haki zijazo
3. hii ingeletwa na ushirika wa Roho kupitia kazi ya Masihi (Mpakwa Mafuta; tazama Mada Maalum: Masihi)

Dhanio la kithiolojia la uhusiano endelevu linahitajika kwa sababu waandishi wa Agano Jipya kwa uchache wanabadilisha matarajio ya Israeli. Badala ya jeshi, ilitazamiwa kitaifa (Israeli) ujio wa Masihi, kuna ujio wa mara ya pili. Ujio wa mara ya kwanza ulikuwa wa umbo-mwili la Uungu katika kutungungwa mimba na kuzaliwa kwa Yesu Mnazarethi. Yeye alikuja kama mtu asiye na majeshi, si mtu wa sheria "mtumwa ateswaye" wa Isaya 53; pia aliyejifanya mdogo juu ya juu ya mngongo wa punda (si farasi wa vita au nyumbu wa vita), wa Zek. 9:9. Ujio wa kwanza ulizitambulisha Zama Mpya za Kimasihi, ufalme wa Mungu hapa duniani (tazama Mada Maalum: Ufalme wa Mungu). Katika maana moja ufalme wa Mungu uko hapa, lakini kwa jinsi hiyo, katika maana nyingine huu bado u mbali. Huu ni mvutano kati ya ujio wa aina mbili wa Masihi ambao, katika maana, huku ni kupishana kwa zama za Kiyahudi ambazo zilikuwa hazikuonekana, au hata kutokuwa sawa, kutoka Agano la Kale (tazama Mada Maalum: Zama hizi na Zama Zijazo). Katika ukweli, ujio ulio katika uwili unasisitiza juu ya ahadi za YHWH za kuwakomboa watu wote (kama vile Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5 na kuhubiri kwa manabii, hasa Isaya na Yona; tazama Mada Maalum: Mpango wa YHWH wa Ukumbozi wa Milele).

Kanisa halisubirii ule utimilifu wa Agano la Kale kwa sababu unabii ulio mwingi unarejea juu ya ujio wa kwanza (kama vile *How to Read the Bible For All Its Worth*, uk. 165-166). Nini waamini wanakitarajia ndani ya ujio wa utukufu wa Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana, historia ya utimilifu wa zama mpya za haki zilizotarajiwa hapa duniani bado iko mbinguni (kama vile Mt. 6:10). Uwasilishaji wa Agano la Kale haukuwa sahihi, bali haukukamilika. Yeye atakuja tena kama manabii walivyotabiri, katika uweza na mamlaka ya YHWH (tazama Mada Maalum: Kwa nini Ahadi za Kiagano Zinaonekana Tofauti Sana Ahadi za Agano Jipya na Agano Jipya?).

Ujio wa Mara ya Pili si neno la kibiblia, bali ni muundo wa dhana ya matazamo wa ulimwengu na sura ya Agano Jipya lote. Mungu atayaweka mambo yote sawa. Ushirika na kati ya Mungu na mwanadamu aliyeumbwa kwa sura na mfano Wake utajejeshwa (kama vile Ufuunuo 21-22). Waovu watahukumiwa na kuondoshwa (kama vile Ufu. 20:11-15). Makusudi ya Mungu ataweza, hawezi, atashindwa!

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 24:4-8**

<sup>4</sup> Yesu akajibu, akawaambia, Angalieni, mtu asiwadanganye. <sup>5</sup> Kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema, Mimi ni Kristo; nao watadanganya wengi. <sup>6</sup> Nanyi mtasikia habari za vita na matetesi ya vita; angalieni, msitishwe; maana hayo hayana budi kutukia; lakini ule mwisho bado. <sup>7</sup> Kwa maana taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme; kutakuwa na njaa, na matetemeko ya nchi mahali mahali. <sup>8</sup> Hayo yote ndiyo mwanzo wa utungu.

**24:4 "Angalieni, mtu asiwadanganye"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo ikiwa na kiambata kanushi ambacho kinamaanisha kusitisha kitendo ambacho kiko katika mchakato. Kulikuwa na kunaendelea kuwa na ishara nyingi za uongo au "ishara zinazotangulia." Kauli hii inarudiwa mara kwa mara (kama vile Marko 13:5, 9, 23, 33). Kuna mkanganyiko mkubwa wa kithiolojia katika eneo hili. Kanisa halijawahi kufanya mapatano ya kukubaliana katika matukio ya siku za mwisho.

Kila kizazi cha Ukristo kilijaribu na kimekuwa kikijaribu kulazimisha historia yao inayoendelea kuingia katika nabii wa kibiblia. Mpaka leo wote wamekosea. Sehemu ya tatizo ni kwamba waaminio wanatakiwa kuishi majira kwa majira wakitegemea Kurudi kwa Mara ya Pili japo unabii wote umeandikwa kwa kutimia katika kizazi kimoja cha wafuasi wenye kupitia mateso. Furahi kwamba hujui!

**24:5 "wengi watakuja kwa jina langu"** Hii inarejerea kwa Masihi (kama vile Mt. 24:11, 23-24; Marko 13:6). Pia ingeweza kuwa maelezo kwa nyakat za mwisho (1) mpiga Kristo wa 1 Yohana 2:18; (2) "Mtu wa Dhambi" ya 2 Wathesalonike 2; au (3) Mnyama wa Baharini wa Ufunuo. 13:1-10.

☐ **"Mimi ni Kristo"** "Kristo" ni utohoaji wa neno la Kiebrania *messiah*, lililomaanisha "mpakwa mafuta." Hii inaonesha kwamba watu watakao kujifanya Masihi wengi wangekuja (kama vile Mt. 24:11, 24; 1 Yohana. 2:18).

☐ **"nao watadanganya wengi"** Hii inaonesha nguvu ya ushawishi ya masihi wa uongo na ombwe la kiroho la mwanadamu aliyeanguka (kama vile Mt. 24:11,23-26). Pia inaonesha ukosefu wa hatia wa waamni wapya na/au Wakristo wa mwilini (kama vile 1 Kor. 3:1-3; Kol. 2:16-23; Ebr. 5:11-14).

**24:6 "angalieni, msitishwe"** Hii ni kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopo yenye kiambata hasi ambao siku zote inamaanisha kusitisha kitendo kilicho katika mchakato.

☐ **"maana hayo hayana budi kutukia; lakini ule mwisho bado"** Vita (Mt. 24:6, 7), njaa (Mt. 24:7), matetemeko ya ardhi (Mt. 24:7), na masihi wa uongo (Mt. 24:5) sio ishara za mwisho bali ishara tangulizi za kila kizazi (kama vile Mt. 24:8). Uwepo wa aina hii ya matukio sio ishara ya mwisho bali ulimwengu ulioanguka.

**24:8**

<b>NASB, NRSV</b>	"utungu"
<b>NKJV</b>	"ya simanzi"
<b>TEV</b>	"maumivu ya kwanza ya kujifungua"
<b>NJB</b>	"utungu"

Hii inarejerea kwa "utungu wa uzao" wa kizazi kipya (kama vile Isa. 13:8; 26:17; 66:7; Mika 4:9-10; Marko 13:8). Hii iliaksi imani ya Wayahudi katika ukuzaji wa uovu kabla ya kizazi kipya cha haki. Wayahudi waliamini katika nyakati mbili (Angalia mada maalum katika Mt. 12:31); kizazi kilichopo cha uovu kilichowekewa na tabia za dhambi na uasi dhidi ya Mungu, na "kizazi kijacho." Kizazi kipya kingeweza kuanzishwa na kuja kwa Masihi. Ingekuwa muda wa haki na uaminifu kwa Mungu. Ingawa mtazamo wa Kiyahudi ulikuwa kweli kwa sehemu hii,

haukuwa ukiangalia Kuja Mara kwa Mara ya Pili kwa Masihi. Tunaishi katika kupandana kwa nyakati hizi mbili. Ule "ulio tayari" na "ambao bado" wa ufalme wa Mungu!

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 24:9-14**

<sup>9</sup>Wakati huo watawasaliti ninyi mpate dhiki, nao watawaua; nanyi mtakuwa watu wa kuchukiwa na mataifayote kwa ajili ya jina langu. <sup>10</sup>Ndipo wengi watakapojikwaa, nao watasalitiana, na kuchukiana. <sup>11</sup>Na manabii wengi wa uongo watatokea, na kudanganya wengi. <sup>12</sup>Na kwa sababu ya kuongezeka maasi, upendo wa wengi utapoa. <sup>13</sup>Lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayeokoka. <sup>14</sup>Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja.

**24:9 "wakati"** Neno hili limetumika mara kadhaa katika mijadala ya Yesu juu ya nyakati za mwisho (kama vile Mt. 24:9,10,14,16,21,23,30,40; 25:1,7,31,34,37, 41,44,45). Swali ni

1. Je kiashiria cha majira ipitayo?
2. Je inaelezea mfuatano wa muda?
3. Je inaelezea mfuatano wa kimuktadha (kama mfuatano wa *waw* katika Kiebrania)?

☐Marko 13:9 inaweka wazi katika suala hili. "Mahakama na Sinagoga," tungo inapatikana katika Mt. 24:9, inaonesha mateso ya kiserikali na kidini ya Wakristo (kama vile 1 Pet. 4:12-16). "Kupigwa" au kibayana "kuchunwa ngozi," Yesu alipigwa na Wayahudi wake waliomshitaki mara thelathini na tisa mara kumi na tatu (kama vile Kumb. 25:1-3; 2 Kor. 11:24).

☐"**mtakuwa watu wa kuchukiwa na mataifa**" Yesu aliwaandaa wanafunzi kwa ajili ya chuki ya ulimwengu (kama vile Mt. 10:22; 21:35-36; 23:37; Marko 13:13; Luka 21:17; Yohana 15:18,19; 1 Yohana 3:13). Kiwango cha upinzani wa injili kinashangaza (kama vile Efe. 6:10-18). Maana ya tungo hii ni kwamba Ukristo umeeneza kwenye huu ulimwengu (kama vile Mt. 24:14) inayomaanisha Yesu alikuwa anarejerea juu ya wakati ujao.

☐"**kwa ajili ya jina langu**" Sio kwa ajili ya ubaya wao wenyewe au makosa ya kijamii yatakayowafanya waaminio wateswe bali kwasababu wao ni Wakristo (kama vile Mt. 5:10-16; Marko 13:9; 1 Pet. 4:12-16).

**24:10 "wengi watakapojikwaa"** Kupitia mateso na kuchekechwa kiroho wafuasi wengi wa Yesu "wataanguka" (kifasihi. "watasababishwa wajikwae," kama vile Mt. 11:6). Hawa ndio waliongelewa katika mfano wa udongo katika Mt. 13:21 (kama vile Marko 4:17; 8:13). Ni wale ambao "hawakai" katika Yohana 15:6. Ni wale ambao wanaacha ushirika katika 1 Yohana 2:18-19. Wao ni wale wanaolezwa katika Waebrania na 2 Pet. 2:20-22. Angalia [MADA MAALUM: UKANAJI WA IMANI \(APHISTĒMI\)](#) katika Mt. 7:21.

**24:10-11** Hii inamaanisha upinzani uliopangwa (kama vile Marko 13:12). Familia zitatengana kwa ajili ya Kristo (kama vile Mt. 10:35-37). Wale ambao walitakiwa wabadilishwe na injili watatenda kama watu amabao hawajaokolewa (kama vile Tito 3:2-3).

**24:11 "manabii wengi wa uongo"** Haya ni mawazo ya kuogofya. Watu hawa ni mbwa mwitu waliovaa mavazi ya kondoo (kama vile Mt. 7:15-23). Waaminio lazima waeleze injili, wajitoe kwa Roho na kuishi maisha ya utauwa kujilinda wenyewe mbali na watu hawa wanaojifanya wema (kama vile 2 Petro 2; 1 Yohana 2:18-19; Ufunuo 13).

**24:12** Mateso yatawafunua asili ya kweli ya watu wanaojifanya wa kiroho (kama vile Mt. 13:20-22) au dhaifu (kama vile 1 Tim. 6:9-10).

**24:13 "Lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayeokoka"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopita usio timilifu (kuvumilia) ikifuatiwa na kauli tendwa elekezi ya wakati ujao (wakiokolewa kama vile Mt. 10:22. Angalia Mada Maalum: Hitaji la Ustahimilivu katika Mt. 10:22). Hili ni fundisho la ustahimilivu (Ufunuo 2:2, 11, 12, 26; 3:5, 12, 21) na lazima lishikiliwe katika mvutano wa kilahaja pamoja na fundisho la usalama wa waamini. Vyote viweili ni kweli! Vyote ni karama ya Mungu. Neno "waliookolewa" inaweza kueleweka katika namna yake ya Agano la Kale ya ukombozi wa kimwili na namna yake ya ukombozi wa milele. Uvumilivu ni ushahidi wa kukutana na Yesu kunakobadilisha maisha (kuwa na uhakika kusoma Mada Maalum juu ya Ustahimilivu katika Mt. 10:22). Haimaanishi hali ya kutokuwa na dhambi bali ina linganisha matendo ya Mt. 24:10- 12!

**24:14 "habari njema ya ufalme"** Hii ilikuwa imetajwa hapa kabla katika Mt. 4:23; 9:35. Ni sawasawa na "injili." Ilijereka maudhui ya mahubiri ya Yesu.

☐ **"itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote"** Hili ni lengo la Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8! Inaweza ishara ya mgeuko mkubwa mbali na sera ya "Israeli tu". Hii ni moja ya vitu ambavyo lazima vitokee kabla ya Kuja kwa Mara ya Pili. Haiwezekani kujua ni kwa namna gani hasa ya kufasiri tungo hii. Je inamaanisha kila kabila moja moja au watu katika makabila yao na rangi au yawezekana kila mmoja katika ulimwengu wa Kirumi wa siku za Paulo? Uchaguzi huu wa pili unawezekana kwasababu ya tungo "ulimwengu wote" kibayana ni "nchi yote inayokaliwa na watu."

## **MADA MAALUM: MPANGO WA UKOMBOZI WA MILELE WA YHWH**

Nalazimika kukubali kwako kiongozi kuwa ninao upendeleo juu ya hoja hii. Mpangilio wangu wa kithiolojia sio wa ufuasi wa Calvin au mfumo wa kidini, bali ni agizo kuu la kiunjilisti (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8). Naamini Mungu ana mpango wa milele kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu (mf., Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Yer. 31:31-34; Eze. 18; 36:22-39; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29; Rum. 3:9-18,19-20,21-31), wale wote walio umbwa kwa sura na ufanano wake (kama vile Mwa. 1:26-27). Maangano yote yameunganishwa katika Kristo (kama vile Gal. 3:28-29; Kol. 3:11). Yesu ni fumbo la Mungu, lilijificha ambalo halijafunuliwa (kama vile Efe. 2:11-3:13)! Injili ya Agano Jipya, sio Israeli, ni ufunguo wa maandiko.

Huu uelewa wangu wa kabla unanakshi tafasiri zangu zote za maandiko. Nasoma maandiko kwa kuyapitia yote! Hakika ni upendeleo (walionao watafsiri wote), lakini ni dhahanio za utaarifishwaji wa kimaandiko.

Mtizamo wa Mwanzo 1-2 ni YHWH akiandaa mahali ambapo Yeye na Uumbaji wake ulio juu, mwanadamu, waweza kuwa na ushirika (kama vile Mwanzo. 1:26,27; 3:8). Uumbaji wake wa vitu ni hatua kwa ajili ya ajenda ya ki-Ungu kati ya watu wawili.

1. St. Augustine anaunganisha kama tundu lenye muonekano wa ki-Ungu katika kila mtu ambaye anaweza kujazwa tu na Mungu mwenyewe.
2. C.S. Lewis aliita sayari hii "sayari inayoshikika," (yaani., iliyoandaliwa na Mungu kwa ajili ya wanadamu).

Agano la Kale lina vidokezo vingi vya ajenda hii ya ki-Ungu.

1. Mwanzo 3:15 ni ahadi ya kwanza kuwa YHWH hatamwacha mwanadamu katika hali tete ya dhambi na uasi. Hii hairejelei kwa Israel kwa sababu hapakuwepo na Israel, wala watu wa agano, mpaka pale Ibrahimu alipoitwa katika Mwanzo 12
2. Mwanzo 12:1-3 ni wito wa awali wa YHWH na ufunuo kwa Abraham ambao ndio ulikuja kuwa watu wa agano, Israel. Lakini hata katika huu wito wa awali, Mungu alikuwa anaangalia ulimwengu wote. Angalia



Mwanzo 12:3!

3. Katika Kutoka 20 (Kumbu kumbu la Torati 5) YHWH alimpa Musa sheria ili kuwaongoza watu wake maalum. Tambua kuwa katika Kutoka 19:5-6, YHWH alidhihilisha kwa Musa uhusiano wa kipekee ambao Israel itakuwa nao. Lakini pia tambua kuwa wao walichaguliwa, kama Abraham, kuubariki ulimwengu (kama vile Kut. 19:5, “kwa vile vitu vyote vya Dunia ni mali yangu”). Israel ilipaswa kuwa chombo kwa mataifa kumjua YHWH na kuvutwa kwake. Kwa masikitiko makubwa wakashindwa (kama vile Eze. 36:22-38)
4. Katika 1 Wafalme 8 Sulemani aliliwafisha hekalu ili wote waje kwa YHWH (kama vile 1 Fal. 8:43,60).
5. Katika Zaburi– 22:27-28; 66:4; 86:9 (Ufu. 15:4)
6. Kupitia kwa manabii wa YHWH kuendelea kudhihilisha mpango wake wa ukombozi kwa watu wote.
  - a. Isaya – 2:2-4; 12:4-5; 25:6-9; 42:6,10-12; 45:22; 49:5-6; 51:4-5; 56:6-8; 60:1-3; 66:18,23
  - b. Yeremia – 3:17; 4:2; 16:19
  - c. Mika 4:1-3
  - d. Malaki 1:11

Msisitizo huu wa wote umerahisishwa na uwepo wa “agano jipya” (kama vile Yer.31:31-34; Ezek. 36:22-38), ambao unaangazia juu ya huruma ya YHWH, na sio utendaji wa mwanadamu aliyeanguka. Kuna “moyo mpya,” “mawazo mapya,” na “roho mpya.” Utii ni kitu cha muhimu lakini ni cha ndani, na sio mfumo wa nje tu (kama vile Rum. 3:21-31).

Agano Jipya linaimalisha mpango wa ukombozi wa wote kwa njia mbali mbali.

1. Agizo kuu – Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8
2. Mpango wa Mungu wa milele (yaani., ulio amuliwa kabla) – Luka 22:22; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29
3. Mungu anawataka wanadamu wote waokolewe – Yohana 3:16; 4:42; Mdo. 10:34-35; 1 Tim. 2:4-6; Tit. 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yn 2:2; 4:14
4. Kristo anaunganisha Agano la Kale na Agano Jipya – Gal. 3:28-29; Efe. 2:11-3:13; Kol. 3:11. Mipaka yote na tofauti zote za mwanadamu zimeondolewa katika Kristo. Yesu ni “fumbo la Mungu,” lililofichika lakini sasa limesidhihilishwa (Efe. 2:11-3:13).

Agano Jipya linaangazia juu ya Yesu, na sio Israel. Injili, sio utaifa wala eneo la kijiografia, ni kitu cha muhimu. Israel ilikuwa ndio ufunuo wa mwanzo lakini Yesu ni hatma ya ufunuo huo (kama vile Mt. 5:17-48).

Natumai utapata wasaa wa kusoma [Mada Maalum: kwa nini ahadi za Agano la Kale zinaonekana kuwa tofauti toka ahadi za Agano Jipya](#). Waweza kupata katika mtandao [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 24:15-28**

<sup>15</sup>Basi hapo mtakapoliona chukizo la uharibifu, lile lililonenwa na nabii Danieli, limesimama katika patakatifu (asomaye na afahamu), <sup>16</sup>ndipo walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani; <sup>17</sup>naye aliye juu ya dari asishuke kuvichukua vitu vilivyomo nyumbani mwake; <sup>18</sup>wala aliye shambani asirudi nyuma kuichukua nguo yake. <sup>19</sup>Ole wao wenye mimba na wanyonyeshao siku hizo! <sup>20</sup>Ombeni, ili kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi, wala siku ya sabato. <sup>21</sup>Kwa kuwa wakati huo kutakuwapo dhiki kubwa, ambayo haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu hata sasa, wala haitakuwapo kamwe. <sup>22</sup>Na kama siku hizo zisingalifupizwa, asingeokoka mtu ye yote; lakini kwa ajili ya wateule zitafupizwa siku hizo. <sup>23</sup>Wakati huo mtu akiwaambia, Tazama, Kristo yupo hapa, au yuko kule msisadiki. <sup>24</sup>Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule. <sup>25</sup>Tazama, nimekwisha kuwaonya mbele. <sup>26</sup>Basi wakiwaambia, Yuko jangwani, msitoke; yumo nyumbani, msisadiki. <sup>27</sup>Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. <sup>28</sup>Kwa kuwa po pote ulipo mzoga, ndipo watakapokusanyika tai.

24:15

NASB, NKJV "chukizo la uharibifu"  
NRSV "chukizo la uharibifu"  
TEV "Hofu iogofyayo"  
NJB "chukizo liogofyalo"

Neno "uharibifu" lilimaanisha kufuru. Hii ilitumika katika Dan. 9:27, 11:31, na 12:11. Inaonekana kurejerea kwa Antioko IV Epiphanes mamo mwaka 168 K.K. (kama vile Dan. 8:9-14; I Mak. 1:54). Pia katika Dan. 7:7-8 ikifanana na Mpinga Kristo wa nyakati za siku za mwisho (kama vile 2 Thes. 2:4). Luka 21:20 inatusaidia sisi kufasiri hili kama kuja kwa jeshi la Titus mnamo mwaka 70 B.K. Haiwezi kurejerea kutekwa kwa Yerusalemu yenyewe kwasababu ingekuwa kuchelewa sana kwa waaminio kuweza kukwepa.

Huu ni mfano wa tungo ikitumika katika namna tofauti tofauti kadhaa lakini zinazofanana. Huku kunaitwa kutimilizwa kwa unabii kadhaa. Mara kwa mara ni ngumu kufasiri mpaka baada ya matukio kutokea. Alafu tukiangalia nyuma, uanishaji ni dhahiri. Kwa taarifa za dokezo zaidi juu ya Danieli angalia katika fasiri yangu katika [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org).

### MADA MAALUM : CHUKIZO LA UHARIBIFU

M. R. Vincent anaelezea vizuri neno chukizo: "Hiki Kitenzi Mfanano, βδελύσσαι, kimaanisha kujihisi kichefuchefu au kupoteza hamu ya kula na hivyo kuchikizwa kwa ujumla. Katika namna ya kimaadili inaashiria jambo la kimaadili au kinyaa cha kidini (kama vile 2 Nyakati. 15:8; Yer. 13:27; Eze. 11:21; Dan. 9:27; 11:31). Inatumika sawa sawa na kuabudu sanamu katika 1 Wafalme 11:17; Kumb. 7:26; 2 Wafalme 23:13. Inaashiria chochote ambacho kutengwa na Mungu kunadhihirishwa kwenyewe, kama kula wanyawa najisi wasio safi. Law. 11:11; Kumb. 14:3; na miundo ya jumla ya kidunia. Hii namna ya kimaadili lazima isisitizwe katika matumizi ya Agano Jipya (yaani linganisha Luka 16:15; Ufunuo 17:4,5; 21:27). Haiashirii kinyaa tu cha kawaida cha kimwili cha hamu. Rejea hii hapa yawezekana inahusiana na kazi ya eneo la hekalu kutumika kwa ibada ya sanamu chini ya Warumi wakiongozwa na Titus pamoja na viwango vyao na kuweka viashiria. Josephus anasema kwamba baada ya kuchomwa kwa hekalu Warumi walizileta bendera zao na kuzisimika juy la lango la mashariki, na walitoa dhabihu kwao, na kudai Tito, kwa vifijo, kuwa mfalme wao" (*Word Studies in the New Testament*, kr. 74-75).

Neno la Kibrania "uharibifu" (BDB 1055, KB 1640) lilimaanisha kufuru. Kifungu hiki kinatumika kataiaka Dan. 9:27, 11:31, na 12:11.

1. Kiuhalisia neno hili lilimrejelea Antiochus IV Epiphanes, ambaye alimjengea madhabahu Zeus Olympios katika hekalu lililokuwa Yerusalemu mnamo 167 k.k. na kutoa dhabihu ya nguruwe ndani ya hekalu hilo (kama vile Dan. 8:9-14; I Mak. 1:54, 59; II Mak. 6:1-2).
2. Katika Dan. 7:7-8 hili linahusiana na Wapinga Kristo wa nyakatai za mwisho (kama vile 2 The. 2:4).
3. Katika Mt. 24:15; Marko 13:14; Luka 21:20 hili linarejelea kuja kwa Generali wa Kirumi (Mfalme wa baadaye) Jeshi la Tito mnamo 70 b.k. aliyetoa dhabihu kwa majeshi yao ambayo iapoza miungu ya kipagani, iliyoondolewa katika lango la mashariki karibia na hekalu. Hili haliwezi kurejelea kizuizi cha Yerusalemu yenyewe kwa sababu waamini wangekuwa wamechelewa sana kukiepuka.

Huu ni mfano wa kifungu kilichokuwa kikitumika katika maana kadhaa na mbalimbali, lakini che kuhusiana. Hiki kinaitwa "unabii uliotilika maradufu." Haiwezekani kukifasiri mpaka pale matukio yatakapotukia; kwa kurejea nyuma, uanishaji u dhahiri.

NASB, NKJV,  
NRSV "limesimama katika patakatifu"  
TEV " limesimama katika patakatifu"  
NJB "limewekwa katika patakatifu"

Kauli endelevu ya Kiyunani "kusimama" is neutersio isiyo na upande, sio ya kiume. Inatakiwa ifasiriwe "lile," ambayo linaunga mkono ufasiri wa "lile" kuendelea kwa jeshi la Kirumi chini ya Titus mnamo mwaka wa 70 B.K. "Mahali Patakatifu" ikirejerea sehemu ya kwanza ya madhabahu ya hekalu. Titus alianzisha viwango vya Kirumi ikiwakilisha miungu yao ya kipagani katika eneo hili katika eneo hili la hekalu.

**NASB, NRSV,**

**NJB** "(msomaji na afahamu)"

**NKJV** "(yoyote asomaye na afahamu)"

**TEV** "(dokezo kwa msomaji: elewa nini kinamaanishwa hapa)"

Haya yalikuwa ni maoni ya Mathayo kwa wasomaji wake wa Kikristo. Kila mmoja alisoma kwa sauti ya juu katika ulimwengu wa kale wa kimediterania. Muhudhuriaji wa kawaida katika Sinagogi wanatakiwa neno la Mungu. Inahusiana na tungo ya hasa tungo za kibayana "chukizo la uharibifu" katika Dan. 9:27, 11:31, na 12:11.

**24:16 "ndipo walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani"** Eusebius, Mwana historia wa kanisa la kwanza (karne ya 4 B.K.), Anatutaarifu kwamba jamii ya Kikristo kukimbilia jiji ya Pella katika Perea wakati jeshi la Kirumi lilipotokea na kuanza kuuzingira Yerusalemu.

**24:17 "naye aliye juu ya dari "** Nyumba zilikuwa na paa tambarare. Palikuwa pakitumika sehemu ya makutano ya kijamii katika miezi yenye joto. Imesemekana kwamba mtu angeweza kutembea juu ya paa za nyumba kwenda sehemu zingine. Inavyoonekana baadhi ya nyumba zilikuwa zimejengwa pembeni mwa ukuta wa mji. Wakati jeshi lilipoonekana, kuogopa kwa mara moja kulikuwa kunatokea.

**24:18 "asirudi nyuma kuichukua nguo yake."** Hii inarejerea nguo ya nje ya mtu ambayo ilitumika kwa ajili ya kulalia. Walitakiwa kukimbia mara moja na kutorudi nyuma kwa kile kilichokuwa kinachukuliwa kama mahitaji ya msingi ya maisha.

**24:19 "Ole wao wenye mimba na wanyonyeshao siku hizo!"** Angalia Marko 13:17. Hii inarejerea kwa Yerusalemu pekee! Haya maswali ya wanafunzi kwa Yesu yalifanana na mambo matatu tofauti: Uharibifu wa Yerusalemu, Kuja kwake kwa Mara ya Pili, na mwisho wa nyakati. Tatizo ni kwamba maswali haya yalishughulikiwa kwa wakati mmoja huo huo. Hakuna mstari rahisi kuugawanya katika mada.

**24:20 "Ombeni, ili kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi"** Tungo hii ilifanana na magumu yanayowapata wanawake wajawazito katika kukimbia kwa haraka. Hili si onyo kwa wanawake wa leo kwamba wasiwe wenye mimba wakati wa Ujio wa Mara ya Pili. Mathayo ikiandikwa kwa Wayahudi, inaongeza tungo "au katika siku ya Sabato" ambayo inaachwa nje katika Marko 13:18. Waaminio wa Kiyahudi hawakuwa tayari kukimbia siku ya Sabato.

Ninashangazwa na vitu viwili vinavyofanana katika mstari huu.

1. Yesu hakujua wakati hasa wa uharibifu wa Yerusalemu.
2. Maombi ya waaminio yangeweza kuathiri wakati hasa wa uharibifu wa Yerusalemu.

**24:21 "ambayo haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu hata sasa, wala haitakuwapo kamwe"** Hii ni tungo ya kinahau inayofanana na nyingine katika Agano la Kale (kama vile Kut. 10:14; 11:6; Yer. 30:7; Dan. 12:1; Yoeli 2:2).

**24:22** Ikiwa wakristo wote watakimbia kama Eusebius anavyotwambia kwamba walifanya, basi hii inaweza kuwa rejea kwa watu wa Kiyahudi, wateule wa Agano la Kale (Mungu bado ana kusudi na taifa la Israeli kama vile Rum. 9-11). Hata hivyo kwasababu ya matumizi ya neno "mteule" katika Mt. 24:24 na 31, inaonekana kurejerea kwa Wayahudi waaminio. Kwa "mteule" angalia Mada Maalum hapa chini.

## **MADA MAALUM: UCHAGUZI/KUAMRIWA KABLA NA UHITAJI WA USAWA KITHIOLOJIA**

Uchaguzi ni fundisho la ajabu. Hata hiyo, si wito ulio na upendeleo, lakini ni wito kuwa njia, chombo, au njia za ukombozi kwa wengine! Katika Agano la Kale neno hilo lilitumiwa hasa kwa jili ya huduma; katika Agano Jipya linatumika hasa kwa ajili ya wokovu unaohusika katika huduma. Biblia hipatanishi kamwe kupingana kati ya Ufalme wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu, lakini inathibitisha zote mbili! Mfano mzuri wa mvutano wa kibiblia itakuwa Warumi 9 juu ya uchaguzi wa Ufalme na Warumi 10 juu ya majibu muhimu ya wanadamu (kama vile Warumi 10:11,13).

Umuhimu wa huu mvutano wa kithiolojia unaweza kupatikana katika 1:4. Yesu ni mwandamu mchaguzi wa Mungu na wote ni uwezo wa kuchaguliwa ndani yake (Karl Barth). Yesu ni Mungu. Yesu "ndio" kwa mahitaji ya mwanadamu aliyeanguka (Karl Barth). Waefeso 1:4 pia husaidia kufafanua suala hilo kwa kuthibitisha kwamba lengo la maji aliwa si mbinguni tu, lakini utakatifu (mapenzi ya kristo). Mara nyingi sisi huvutiwa na faida za injili na kupuuza majukumu! Wito wa Mungu (uchaguzi) ni kwa wakati pamoja na milelele!

Mafundisho huja kuhusiana na ukweli mwingine, sio mmoja tu, ukweli usiohusiana. Hali au tabia nzuri inakuwa ni kundi dhidi ya nyota moja. Mungu hutoa ukweli katika mashariki na sio magharibi, mtindo. Hatupaswi kuondoa mvutano unaosababishwa na jozi za lahaja (fumbo la maneno) za kweli za mafundisho:

1. Kuamriwa kabla/mchaguzi dhidi ya utashi huru wa mwanadamu
2. Usalama wa wanaoamini dhidi ya mahitaji ya uvumilivu
3. dhambi ya asili dhidi ya dhambi ya hiari
4. kutotenda dhambi dhidi ya kutenda dhambi kidogo
5. udhihili na utakaso wa papo kwa papo dhidi ya utakaso endelevu
6. Uhuru wa Kikristo dhidi ya wajibu wa Kikristo
7. Mungu anayeweza kupita uwezo wa binadamu dhidi ya Munngu wa asili
8. Mungu kama hatimaye isiyojulikana dhidi ya Mungu anayejulikana katika maandiko
9. Ufalme wa Mungu kama sasa dhidi ya kukamilishwa baadaye
10. Kutubu kama zawadi ya Mungu dhidi ya jibu muhimu la Agano la kibinadamu
11. Yesu kama Mungu dhidi ya Yesu kama mwanadamu
12. Yesu ni sawa na Mungu Baba dhidi ya Yesu wa kumtumikia Mungu Baba

Dhana ya kithiolojia ya "agano" inaunganisha Ufalme wa Mungu (ambaye daia huchukua hatua kwa kuweka mswada) pamoja na mamlaka ya mwanzo imani ya kuendelea kutubu kujibiwa kutoka kwa mwanadamu (k.v. Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21). Kuwa mwangalifu wa maandishi ya uthibitisho wa upande mmoja wa fumbo la maeneo na punguza kwa mwingine! Kuwa mwangaliu wa kuthibitisha mafundisho yako ya mapenzi tu au mfumo wa thiolojia!

## **MADA MAALUM : MIEZI AROBAINI NA MIWILI (kutoka DANIELI)**

Hiki kifungu "miezi arobaini na miwili" kinabii ni sifa bainishi za kipindi cha mateso. Kutembea katika ua wa nje ni nahau izungumziayo watu wa Mungu chini ya utawala wa wale wasio amini katika vipindi tofautitofauti katika historia—Antiochus Epiphanes, Warumi wa 70 B.K, na Wapinga-Kristo wa nyakatai za mwisho.

Miezi arobaini na miwili, au usawa wake, inatajwa mara kadhaa katika Biblia. Chimbuko lake linaonekana kuwa kitabu cha Danieli.

1. Danieli 7:25; 12:7 inataja "wakati, nyakati, na nusu wakati" au siku 1277 (dhahania "wakati" sawa na mwaka mmoja), kama vile Ufu. 12:14
2. Danieli 8:14 inataja 2300 asubuhi na jioni
3. Danieli 12:11 inataja siku 1290
4. Danieli 12:12 inataja siku 1335. Uwekaji wa kifungu cha maneno unaofanana unapatikana katika Ufu. 11:3; 12:6 (siku 1260 ) na 11:2; 13:5 (mienzi 42).

Njia nyingine ya kukiangalia kifungu hiki kilichifichika ni kukiangalia kama mfuatano: moja,mbili, lakini si tatu; hivyo, ni kiwango cha wakati kilichowekewa mipaka ki-Ungu chini ya falme za Mataifa ziwatesao watu wa Mungu. Mungu, katika kitabu cha Danieli, yu katika utawala kamili (kama vile Dan. 7:4,6,11,12,18,22,25,26,27)! Matukio haya yanapotolewa ufafanuzi, tofauti zao zinaonekana katika kuzungumzia asili ya uwakilishi wa namba (tazama Mada Maalum: Uwakilishi wa Namba katika Maandiko), ambapo ukaribu wake wa miezi arobaini na miwili unaonekana kuonyesha kwamba ni uwakilishi wa namba wa kipindi cha mateso. Kwa kuwa tatu na nusu na nusu ya saba, inaonekana kuwa rejea ya kipindi kamili cha mateso ambayo yamekatishwa (kama vile Mt. 24:22; Marko 13:20; Luka 21:24). Mateso yamewekewa mipaka upendo wa Mungu kama hukumu.

**24:23,26** Kuja kwa kweli kwa Masihi hakutakuwa kwa kujificha au siri. Haitakuwa kwa kundi fulani la kuchaguliwa bali linalooneka kwa watu wote (Mt. 24:27). Kibiblia hakuna "hakuna kunyakuliwa kisiri siri." Angalia dokezo katika Mt. 24:40-41.

**24:23,26 "ikiwa"** Hizi ni sentensi za daraja la tatu lenye masharti mbili ambazo zinaashiria kitendo kinachoweza kutokea.

**24:24 "nao watatoa ishara kubwa na maajabu"** Hawa makristo wa uongo watafanya miujiza (kama vile Mt. 7:21-23). Kuwa makini siku zote na kujibainisha na miujiza kuwa na Mungu (kama vile Kut. 7:11-12,22; Kumb. 13:1-3; 2 Thes. 2:9-12; Ufu. 13:13; 16:14; 20:20).

**24:27 "kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu"** Angalia Luka 17:24. Marko 13 haina tungo hii. Hii inamaanisha kuja kunakoonekana. Agano Jipya halifundishi kunyakuliwa kwa siri kwa waamini (kama vile Mt. 24:40-41). Lakini haifunui kwamba Waaminio waliokufa na walio hai watakutana na Bwana mawinguni wakati wa Kuja kwa Kwa Mara ya Pili (kama vile 1 Thes. 4:13-18). Anga lilichukuliwa uwanja wa mapepo au shetani (kamavile Efe. 2:2). Waaminio watakutana na Yesu kati kati ya ufalme wa shetani kuonesha kumpindua kwa ujumla wake!

## **MADA MAALUM: KURUDI KWA YESU WAKATI WO WOTE DHIDI YA KUKAWIA (UKINZANI WA AGANO JIPYA)**

- A. Vifungu vya Agano Jipya vya matukio ya siku za mwisho vinauakisi utambuzi wa kinabii wa Agano la Kale uliyozitazamia nyakati za mwisho kupitia matukio ya sasa.
- B. Mathayo 24, Marko 13, na Luka 21 ni ngumu sana kuzifasiri kwa sanbabu zinashughulikia maswali kadhaa kwa mfululizo.
  1. Hekalu litaharibiwa lini?
  2. ni ishara gani itakayoonyesha kurudi kwa Masihi?
  3. Je! Nyakati hizi zitaisha lini (kama vile Mt. 24:3)?
- C. Aina hii ya vifungu vya Agano Jipya vinavyohusu matukio ya siku za mwisho mara nyingi ni muungano wa lugha ya matukio ya siku za mwisho na ya kinabii ambayo ni ya utata wa makusudi na wa viashiria

vya hali ya juu (tazama D. Brent Sandy, *Ploshwares and Pruning Hooks: Rethinking the Language of Biblical Prophecy and Apocalyptic*).

- D. Vifungu kadha a vilivyo katika Agano Jipya (kama vile Mathayo 24, Marko 13, Luka 17 na 21, 1 na 2 Wathesalonike na UJfunuo wa Yohana) vinashughulika na Kuja Mara ya Pili. Vifungu hivi vinasistiza:
  - 1. wakati halisi wa matukio haujulikani, bali matukio yanajulikana
  - 2. twaweza kuujua wakati kwa ujumla, lakini si wakati maalum, wa matukio
  - 3. huu utatokea ghafla na pasipokutarajia
  - 4. yatupasa kuomba, kuwa tayari, na kuwa waaminifu kwa kazi tulizopewa.
- E. Kuna fumbo la mvutano wa kithiolojia kati ya
  - 1. wakati wote wa kurudi kwake (kama vile Luka 12:40,46; 21:36; Mt.24:27,44) na
  - 2. ukweli kwamba matukio mengine katika historia lazima yatukie (F.hapa chini)
- F. Agano Jipya linaeleza kwamba baadhi ya matukio yatatukia kabla ya Kuja Mara ya Pili:
  - 1. injili iliyohubiriwa kwa ulimwengu wote (kama vile Mt. 24:14; Marko 13:10)
  - 2. ukanaji mkuu wa imani (kama vile Mt. 24:10-13, 21; 1 Tim. 4:1; 2 Tim. 3:1 na kuendelea; 2 The. 2:3)
  - 3. ufunuo wa "mwana wa dhambi" (kama vile Dan. 7:23-26; 9:24-27; 2 The. 2:3)
  - 4. kuondolewa kwa /yule azuiaye (kama vile 2 The. 2:6-7)
  - 5. uamsho wa matumaini wa Kiyahudi (kama vile Zek. 12:10; Warumi 11)
- G. Luka 17:26-37 haifananihwa na Marko. Hii ina ufanano usio kamili wa Vidokezovilivyo katika Mt. 24:37-44.
- H. Kwa mjadala unaohusu Kristo kurudi kitambo kidogo, tazama [Mada Maalum: Kurudi Kitambo](#)
- I. Kwa mjadala wa kukawia kurudi, tazama [Mada Maalum: Kukawia kwa Kurudi mara ya Pili](#)

**24:28 "Kwa kuwa po pote ulipo mzoga, ndipo watakapokusanyika tai"** Hii haitokei katika Marko 13 japo inatokea katika Luka 17:37. Ni kauli ya kimithali yawezekana kutoka katika Ayubu 39:30. Ikiwa ikikuwa ni rejea ya kisiri kwa vita vya wakati wa mwisho wa Zaburi 2, hivyo basi inaweza kuwa chanzo chake kinatokea Ezek. 39:17-20. Inaweza kuwa sitiari kwa mateso ya nyakati za mwisho.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 24:29-31**

<sup>29</sup>Lakini mara, baada ya dhiki ya siku zile, jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake, na nyota zitaanguka mbinguni, na nguvu za mbinguni zitatikisika; <sup>30</sup>ndipo itakapoonekana ishara yake Mwana wa Adamu mbinguni; ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza, nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi. <sup>31</sup>Naye atawatuma malaika zake pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule wake toka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu.

**24:29 "lakini"** Huu ni upinzani mkubwa kuonesha kukatisha katika muktadha. Tazama fasiri zote za Kingereza zinazoweka katika mgawanyo wa aya kwa hatua hii.

☐ **"jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake"** Hii ilikuwa ni lugha ya kimatukio ya siku za mwisho juu ya nyakati za mwisho (kama vile Isa. 13:10; 34:4; Ezek. 32:7-8; Yoeli 2:10,31; 3:15; Amosi 8:9). Kutakuwako na migogoro katika asili wakati wa kuja kwa Siku ya Bwana (kama vile 2 Pet. 3:7,10,11,12; Ufu. 6:12-14).

☐ **"na nguvu za mbinguni zitatikisika"** Hii ingekuwa yawezekana kuwa mwendelezo wa lugha ya siku ya mwisho na hivyo rejea kwa mvutano wa asili wakati wa Siku ya Bwana au rejea kwa nguvu za kimalaika zinazoshawishi historia (kama vile Dan. 10; Efe. 6:12; Kol. 2:15; Ufu. 12:4).

**24:30 "ndipo itakapoonekana ishara yake Mwana wa Adamu mbinguni"** Inawezekana kwamba muunganiko huu ni kwa Isa. 60:1-3. Ile "ishara" ingekuwa kwa nuru ya wingu la *Shekinah* la utukufu. Nuru za dunia hushindwa lakini nuru za Mungu (kama vile Mwa. 1:3), nyota ya kweli ig'aa a subuhi, hug'aa siku zote!

Ubinadamu wa Yesu (Zab. 8:4; Ezek. 2:1) na Uungu (Dan. 7:13) unasisitizwa na "Mwana wa Adamu." Mawingu yalikuwa yakionekana kama chombo cha usafiri cha Uungu katika Agano la Kale. Yesu aliyatumia katika Mdo.1:9 na 1 Thes. 4:17 jambo lilimaanisha Uungu wake. Ishara itakuwa Kuja kwa Yesu mawinguni ya mbingu kama wingu kla mashariki "linavyofunguka."

### **MADA MAALUM: MWANA WA ADAMU (kutoka Danieli 7:13)**

Kifungu cha lugha ya Kiaramu ("*ben enosh*," BDB 1085 MUUNDO WA MANENO na 1081) "mwana wa Adamu" ni tofauti kutokana na kifungu kinachofanana na cha Kiebrania ("*ben adam*") kinachopatikana katika Zaburi na Ezekieli. Vifungu vyote vinatumika katika ufanano kwenye Ayubu 25:6; Zab. 8:4; 90:3; 144:3; Isa. 13:12. Hili ni dhahili linarejerea kwa Masihi na kuhusiana na ubinadamu wake (kama vile Dan. 8:17; Ayubu 25:6; Zab. 8:4; Ezek. 2:1 [na vingine vingi] katika Ezekieli), lenye maana ya fungu la maneno ya Kiarama na Kiebrania, "mwana wa Adamu," akiwa na Uungu wake kwa sababu mawingu husafirisha Uungu (kama vile Dan. 7:13; Mt. 24:30; 26:64; Marko 13:26; 14:62; Ufu. 1:7; 14:14).

Yesu anatumia kifungu kujirejerea Mwenyewe katika Agano Jipya. Hakikutumika kumhusu Masihi kwenye sheria za Kiyahudi. Hakina vidokezo vya utenganisho, vidokezo vya utafifa, vidokezo vya kijeshi, kipekee kabisa kinamwelezea Masihi kama mwanadamu kamili na Mungu kamili (kama vile 1 Yohana 4:1-3). Matumizi ya Danieli ni ya kwanza ambayo yanatizamisha juu ya dhana ya Uungu!

Yesu alikutumia kifungu kwa ajili yake katika maana tatu.

1. mateso yake na kifo (mf., Marko 8:31; 10:45; 14:21; Luka 9:22,44)
2. ujio wake kama mwamuzi (mf., Mt. 16:27; 25:31; Yn 5:27)
3. kuja kwake katika utukufu kutengeneza ufalme wake (mf., Mt. 16:28; 19:28; Marko 13:26-27; 14:62)

Kutoka katika The Jewish Study Bible, uk. 1657 (pia angalia George E. Ladd, *A Theology of the New Testament*, kur. 136-139), tamaduni za baadaye za Kiyahudi kuhusiana na andiko hili zimeorodheshwa.

1. Huu muktadha ni wa Kimasihi (kama vile I Enoch 46:1; 48:10; 4 Ezra [2 Esdras] sura 13; b. Sanh. 98a)
2. utabiri wote katika muktadha umekwisha kutimika (kama vile b. Sanh. 97b)
3. Muktadha haurejerei siku za mwisho (kama vile Mwanzo. Rab. 98:2)
4. Muktadha huwakilisha Israeli (kama vile Ibn Ezra and Rashi)

☛"**ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboteza**" Hii inarejerea kurudi kunakoonekana kwa Yesu. Kutaonekana na ulimwengu wote. Wasioamini ghafla watatambua madhara ya kutoamini kwao.

☛"**juu ya mawingu**" Angalia Mada Maalum inayofuata.

### **MADA MAALUM: KUJA MAWINGUNI (Maneno kadhaa ya Kiebrania, hasa *anan*, BDB 777, KB 857)**

Huu ujio wa mawinguni ulikuwa ishara muhimu sana ya matukio ya siku za mwisho. Huu ulitumika katika njia tatu tofauti ndani ya Agano la Kale.

1. kuonyesha mwonekano wa uwepo wa Mungu, *Shekinah* wingu la Utukufu kama vile Kut. 13:21; 14:19,20,24; 16:10; 19:9; Hes. 11:25; Neh. 9:19)
2. kuufunika Utakatifu Wake ili kwa mwanadamu asimuone na kufa (kama vile Kut. 33:20; Isa. 6:5)
3. kuupandisha Uungu (kama vile Zab. 18:9; 104:3; Isa. 19:1; Nah. 1:3; Matendo ya Mitume 1:9; 1 The. 4:17)

Katika Danieli 7:13 mawingu yalitumika kama usafirishaji wa uungu, Masihi aliye mwanadamu (tazama Mada Maalum: Masihi). Unabii huu ulio ndani ya Danieli unadokezwa mara 30 katika Agano Jipya. Uhusiano huu huu wa Masihi pamoja na mawingu ya mbinguni unaweza kuonekana katika Mt. 24:30; 26:64; Marko 13:26; 14:62; Luka 21:27; Matendo ya Mitume 1:9,11; 1 The. 4:17; Ufu. 1:7.

☐ **"pamoja na nguvu na utukufu mwingi"** Hii inaonesha ulinganifu wa ghafla kati ya Kuja kwa Mara ya Kwanza na Kuja kwa Mara ya Pili. Hii ni njia Wayahudi walitarajia Kuja kwa Masihi. Angalia dokezo juu ya "Utukufu" katika Mt. 16:27.

**24:31** "Malaika Zako" Angalia Marko 13:27, 8:38, na 2 Thes. 1:7. Malaika wa Mungu wanaitwa malaika wa Yesu hapa. Hii ilimaanisha Uungu Wake.

☐ **"na sauti kuu ya parapanda"** Hii yawezekana ilirejerea kwa Shophar, pembe ya kushoto ya kondoo, ambayo ilitumika kama ishara ya Sabato ya Kiyahudi katika Siku za Sherehe. Katika Isa. 27:13 kuna baragumu linalopulizwa kuhusiana na siku za mwisho (kama vile 1 Kor. 15:52; 1 Thes. 4:16).

## **MADA MAALUM: PEMBE ZITUMIKAZO NA ISRAELI**

Kuna maneno manne katika Kiebrania yahusianayo na pembe/tarumbeta.

1. "pembe ya mwana kondoo" (BDB 901) – ikigeuzwa kuwa chombo cha sauti, kama vile Yosh. 6:5. Neno hilihili linatumika kwa ajili ya mwanakondoo aliyenaswa na pembe zake ambaye Ibrahimu alimfanya mbadala wa Isaka katika Mwanzo 22:13.
2. "tarumbeta" (BDB 1051) – kutoka katika neno la kiashuru ikimaanisha kondoo wa porini (ibex). Hii ni pembe ambayo ilitumika katika Kutoka 19:16,19 katika Mlima Sinai/Horeb; #1 na #2 zina usambamba na Yosh. 6:5. Ilitumika kuwasiliana wakati wa ibada na wakati wa kupigana (yaani Yeriko ilikuwa vyote, kama vile Yosh. 6:4).
3. "pembe ya mwana kondoo" (BDB 385) – kutoka neno la kifoinike kwa ajili ya mwana kondoo (kama vile Yosh. 6:4,6,8,13). Ilisimama pia kwa ajili ya Mwaka wa Jubilei (kama vile Mambo ya Walawi 25:13,28,40,50,52,54; 27:17,18,23,24).  
(Zote za hizi tatu za kwanza zinaonekana kubadilishana bila kutenganishwa. Toleo Mishnah [RH 3.2] iliruhusu mnyama yoyote—kondoo, mbuzi au paa.)
4. "matarumbeta" (BDB 348) – yawezekana kutoka katika KITENZI VERB "kujinyoosha," ikimaanisha mfupa ulionyooka (sio pembe ya mnyama iliyojikunja). Hizi zilikuwa zimefanywa kwa shaba (baada ya uumbo na muundo wa Misri).  
Hizi zinatumika
  - a. zikiwa na ibada za kuabudu (kama vile Hesabu. 10:2,8,10; Ezra 3:10; Neh. 12:35,41)
  - b. kwa makusudi ya kijeshi (kama vile Hesabu. 10:9; 31:6; Hosea 5:8)
  - c. kwa makusudi ya kifalme (kama vile II Wafalme. 11:14)

Moja ya hizi pembe za chuma zinachukuliwa na msaidizi wa Tito katika Rumi; pia Josephus akiwaelezea katika *Antiq.* 3.12.6.

☐ **"watawakusanya wateule wake"** Hii ni taswira ya Agano la Kale juu ya urejesho kutoka uhamishoni (yaani Kumb. 30:4), hapa ikigeuzwa katika kusanyiko la matukio ya siku za mwisho (kama vile Mt. 13:40-43,47-49). Utaratibu halisi wa nyakati hizi za mwisho hazijulikani. Paulo alifundisha kwamba wakati wa kifo kwamba waaminio wako tayari (kama vile 2 Kor. 5:6,8). 1 Thes. 4:13 na kuendelea. Kunafundisha kwamba inavyoonekana kitu fulani cha miili yetu inayoonekana kiliachwa hapa, itaugana na roho zetu katika Siku ya Bwana. Hii



inamaanisha hali kutenganishwa kati ya kifo na siku ya ufufuo. Kuna mengi sana juu ya matukio ya siku za mwisho na baada ya maisha haya ambayo hayaandikwi katika Biblia.

☐ **"toka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu"** Hii inamaanisha upana wa kiulimwengu ikifuatiwa na Yesu! Pia ikimaanisha muda mrefu kwa injili kusambaa.

Namba nne ni ishara kwa ulimwengu. Inarejerea pande nne za ulimwengu (Isa. 11:12; Ufu. 7:1), pepo nne za dunia (Dan. 7:2; Zek. 2:6), na ncha nne za mbingu (Yer. 49:36). Angalia Mada Maalum: Uwakilishi wa Namba katika Maandiko katika Mt. 4:2.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 24:32-35**

<sup>32</sup>Basi kwa mtini jifunzeni mfano; tawi lake likiisha kuchipuka na kuchanua majani, mwatambua ya kuwa wakati wa mavuno u karibu; <sup>33</sup>nanyi kadhalika, myaonapo hayo yote, tambueni ya kuwa yu karibu, milangoni. <sup>34</sup>Amin, nawaambia, Kizazi hiki hakitapita, hata hayo yote yatakapotimia. <sup>35</sup>Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe.

**24:32 "mtini"** Mfano huu unafananishwa na Marko 13:28-32 na Luka 21:29-33. Mtini katika kifungu cha kimithali ilikuwa inaonekana sio uwakilishi wa Israeli kama katika Mt. 21:18-20 na Marko 11:12-14, lakini kama njia ya kuhakikishia waamini kwamba ingawa hawawezi kujua nyakati hasa za matukio ya siku za mwisho, wanaweza kujua nyakati. Mtini unadondosha majani kwa mapema na kila mtu alijua wakati wa hali uko karibu.

**24:32-33 "mwatambua"** Wakati kizazi cha mwisho kijapo, Vifungu vya kinabii vya ki-Biblia vinashabihiana hasa historia ya siku hilo. Maarifa haya yataimarisha imani ya waaminio katika Mungu katika kati ya mateso ya nyakati za mwisho. Tatizo kwa kila kizazi cha waaminio ni kwamba wanalazimisha Biblia katika historia ya siku zao! Majaribio yote mpaka sasa yamekosewa!

**24:33 "Yeye"** Hiki kiwakilishi cha kiume hakipo katika andiko la Kiyunani. Linatakiwa kuwa "lile" (kama vile Mt. 24:14).

☐ **"myaonapo hayo yote"** Hii ingeweza kurejerea kwa (1) uharibifu wa Yerusalemu; (2) kugeuka (kama vile Marko 9:1; Mt. 16:27); au (3) moja ya ishara hizi za Kuja kwa Mara ya Pili.

**24:34** Mstari huu unarejerea juu ya uharibifu wa Yerusalemu mnamo mwaka wa 70 B.K. na kikosi cha kirumi chini ya Titus. Yesu alikuwa anaunganisha maswali ya Mt. 24:3: (1) uharibifu wa hekalu, (2) ishara ya Kurudi kwake mwisho wa nyakati, na (3) mwisho wa nyakati.

Pia inawezekana kuunganisha Mt. 10:23; 16:28 na 24:34 na kuhitimisha kwamba Yesu alitarajia kurudi kwa haraka, lakini Mathayo akiandika mlongo baadaye kwamba, alitambua "kurudi kukochelewa" maudhui katika mafundisho ya Yesu.

**24:25** Ni kauli ya nguvu namna gani ya Yesu ya kujitambua. Hakika inahusiana na Mt. 5:17-19 au Isa. 40:8; 55:11. Yesu ni ufunuo kamili wa Mungu asiyeonekana (yaani, Kol. 1:15)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 24:36-41**

<sup>36</sup>Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna ajiuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake. <sup>37</sup>Kwa maana kama vile ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. <sup>38</sup>Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya Gharika watu walivyokuwa wakila, na kunywa,

wakioa na kuolewa, hata siku ile aliyoingia Nuhu katika safina, <sup>39</sup>wasitambue, hata Gharika ikaja, ikawachukua wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. <sup>40</sup>Wakati ule watu wawili watakuwako kondeni; mmoja atwaliwa, mmoja aachwa; <sup>41</sup>wanawake wawili watakuwa wakisaga; mmoja atwaliwa, mmoja aachwa.

**24:36 "Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake"** Kwa "saa" angalia Mada Maalum hapa chini. Huu ni mstari wa nguvu kuwakatisha tamaa Wakristo kuweka tarehe rasmi za Kuja kwa Mara ya Pili. Tungo "wala si mwana" haijumuishi katika Mt. 24:36 katika baadhi ya maandiko ya Kiyunani ᵐ, K, L, W. Inajumuishwa katika fasiri nyingi zaidi kwasababu haitokei katika maandiko ᵐ, B na D, Diatesseron, na Maandiko ya Kiyunani yajulikanayo kwa Irenaeus, Origen, Chrysostom, na maandiko ya Kilatini ya zamani yanayotumiwa na Jerome. Hii inaweza kuwa moja ya andiko lililorekebishwa na waandishi wa Ki-Orthodoxy kupelekea uungu wa Kristo dhidi ya walimu wa uongo (Angalia *The Orthodox Corruption of Scripture*, Bart D. Ehrman, kur. 91-92, ikichapishwa na Oxford University Press, 1993).

### **MADA MAALUM: SAA (hōra)**

Neno "saa" limetumika kwa namna tofauti mbalimbali katika injili, kama

1. Rejea ya wakati (kama vile Mt. 8:13; 26:40; Luka 7:21; Yohana 11:9)
2. Stiari kwa ajili ya wakati wa kujaribiwa na majaribu (kama vile Mt. 10:19; Marko 13:11; Luka 12:12)
3. Stiari kwa ajili ya Yesu kuanza huduma Yake (kama vile Yohana 2:4; 4:23)
4. Stiari kwa ajili ya siku ya hukumu (yaani., ujio wa mara ya pili, kama vile Mt. 24:36,44; 25:13; Marko 13:32; Yohana 5:25,28)
5. Stiari kwa ajili ya wiki ya mateso ya Yesu (kama vile Mt. 26:45; Marko 14:35,41; Yohana 7:30; 8:20; 12:23,27; 13:1; 16:32; 17:1)

**24:37 "Kuja"** Angalia Mada Maalum katika Mt. 24:3.

☑️**"kama vile ilivyokuwa siku za Nuhu"** Hii ni nahau ambayo ilimaanisha kwamba maisha ya kawaida yalikuwa yanaendelea kama katika siku za nyuma (kama vile Mt. 24:38).

**24:39** Hii ni hukumu ya Mungu kwa wasioamini wote kwa muda na kimatukio ya siku za mwisho.

**24:40-41 "Wakati ule watu wawili watakuwako kondeni; mmoja atwaliwa, mmoja aachwa; wanawake wawili watakuwa wakisaga; mmoja atwaliwa, mmoja aachwa"**Wengi wanajaribu kuhusianisha hili na kunyakuliwa kwa siri. Hata hivyo muktadha unamaanisha Baraka kwa baadhi na hukumu kwa wengine katika siku isiyotarajiwa ya Kurudi kwa Bwana. Haijulikani kundi gani linabarikiwa. Je "kuchukuliwa" au "kuachwa" inarejerea kwa Nuhu na familia yake aliyeachwa hai baada ya Gharika, au wale waliokutana na Bwana katika anga (Mt. 24:31)? Mfano wa baadhi ya watu kubarikiwa na baadhi wakihukumiwa ni Gharika la Nuhu (kama vile Mt. 24:39). Katika Luka mfano wa Agano la Kale wa Sodoma ilitumika (kama vile Luka 17:29). Ukweli ni kwamba, Mt. 24:27 ilimaanisha kuja kwa Bwana kunakoonekana kimwili! Sababu pekee baadhi wanataka kunyakuliwa kwa siri wkwa waamini kwanza kujaribu kuelezea uvutano wa kilahaja katika Agano Jipya (1) kurudi kwa muda wowote kwa Bwana (2) ukweli ni kwamba baadhi ya vitu vingine lazima vitokee kwanza.

Yesu anatoa mifano kadhaa kuashiria ughafla na kutotarajiwa kwa Ujio wake.

1. Gharika la Nuhu, Mt. 24:37-38
2. Mwizi wakati wa usiku, Mt. 24:43

3. kurudi kwa Bwana, Mt. 24:45-46
4. Bibi harusi kuchelewa, 25:5-6
5. yawezekana "nuru" katika Mt. 24:27

Uchaguzi pekee wa Waaminio ni kuwa tayari wakati wote (kama vile Mt. 24:44; 25:10,13)!

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 24:42-44**

<sup>42</sup>Kesheni basi; kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu. <sup>43</sup>Lakini fahamuni neno hili; kama mwenye nyumba angalijua ile zamu mwivi atakayokuja, angalikesha, wala asingaliacha nyumba yake kuvunjwa. <sup>44</sup>Kwa sababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari; kwa kuwa katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu yuaja.

**24:42 "Kesheni basi; kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu"** Mfano huu unafanana na Luka 12:39-40. Msisitizo upo katika kuwa tayari (kama vile Mt. 24:43, 44) na kutojulikana kwa wakati (kama vile Mt. 24:39,47,49,50; 25:5,13) ni maudhui maudhui inayojirudia rudia katika maudhui katika sura. Kutojulikana kwa nyakati kunatoa motisha kwa kutoendelea kwa utayari wa kila kizazi cha waaminio.

**24:43 "mkiwa"** Hii ni sentensi daraja la pili lenye masharti "kinyume na ukweli." Kauli inafanywa ambayo ni ya uongo hivyo hitimisho ni hitimisho inayofanywa pia ni ya uongo.

**24:44 "ninyi nanyi jiwekeni tayari"** Tungo hii ni shurutishi (yenye ushahidi) ya wakati uliopo (kama vile Marko 13:5,9,23). Huu ni ufunguo kwa waaminio sio madhanio na fundisho kuhusu wakati namna gani! Ukweli ni kwamba wengi wanategemea Kuja Kwake hivi karibuni kama ushahidi!

☉"saa" Angalia [MADA MAALUM: SAA](#) katika Mt. 24:36.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 24:45-51**

<sup>45</sup>Ni nani basi yule mtumwa mwaminifu mwenye akili, ambaye bwana wake alimweka juu ya nyumba yake, awape watu chakula kwa wakati wake? <sup>46</sup>Heri mtumwa yule, ambaye bwana wake ajapo atamkuta akifanya hivyo. <sup>47</sup>Amin, nawaambieni, atamweka juu ya vitu vyake vyote. <sup>48</sup>Lakini mtumwa yule mbaya akisema moyoni mwake, Bwana wangu anakawia; <sup>49</sup>akaanza kuwapiga wajoli wake, na kula na kunywa pamoja na walevi; <sup>50</sup>bwana wake mtumwa huyo atakuja siku asiyodhani, na saa asiyojua, <sup>51</sup>atamkata vipande viwili, na kumweka fungu lake pamoja na wanafiki; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno.

**24:45 "ambaye bwana wake alimweka juu ya nyumba yake"** Baadhi wanaona hili kama kuhusiana na mifano hii na viongozi wa Kikristo (kama vile Luka 12:40-48). Katika Muktaadha huu unahusina na kuendelea na mgogoro na viongozi wa Kiyahudi katika siku zake.

**24:46** Waaminio lazima waendeleo kuwa watendaji, tayari na waaminifu (kama vile 12:37-38; Yakobo 1:12; Ufu. 16:15). Wakati gani na namna ya Kuja kwa Mara ya Pili sio jambo kubwa!

**24:47 "atamweka juu ya vitu vyake vyote"** Angalia Mt. 13:12, 25:29, na Luka 19:17.

**24:48 "ikiwa"** Hii ni sentensi daraja la tatu lenye masharti ambayo inamaanisha tendo linaloweza kutokea kwa baadaye.

☉"moyo" Angalia Mada maalum katika Mt. 5:8.

☑ "**Bwana wangu anakawia**" Hii inawakilisha dhana ya kuchelewa katika Ujio wa Mara ya Pili (kama vile Mt. 25:5; 2 Thes. 2; 2 Pet. 3:4).

**24:50 "bwana wake mtumwa huyo atakuja siku asiyodhani, na saa asiyojua"** Angalia Mt. 24:27,44; 25:6, 13. Hii inaaksi "muda wowote" kurudi kwa Bwana.

**24:51 "atamkata vipande viwili"** Kuna kutojulikana juu ya hii sitiari au kibayana (kama vile 2 Sam. 12:31; Ebr. 11:37). Ni hakika maelezo ya hukumu ya Agano la Kale.

☑ "**pamoja na wanafiki**" Ufanano upo katika Luka 12:46 una "wasioamini." Mathayo anawaita Mafarisayo "wanafiki" mara kadhaa. Angalia Mada Maaluma katika Mt. 6:2.

☑ "**kilio**" Vitu viwili vya mwisho ni sitiari za hukumu. Kulia ilikuwa ni ishara za huzuni kubwa (kama vile Mt. 25:30).

☑ "**kusaga meno**" Hii inawakilisha hasira au maumivu (kama vile Mt. 8:12; 13:42,50; 22:13; 25:30).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni nini kusudio la msingi la Sura hii?
2. Je mistari ya 4-7 inaelezea juu ya nyakati za mwisho?
3. Ni kwa namna gani unabii wa Danieli (7:23-28; 9:24-27; 11:26-29) unahusiana na sura hii?
4. Kwa nini Yesu anatumia lugha kama ya mstari wa 24?
5. Je twaweza kujua ni lini Bwana atakuja tena?
6. Je muda wa Kuja kwa mara ya Pili kumetimia, kumechelewa au hakujulikani?
7. Ni kwa namna gani Yesu hakujua muda (Mt. 24:36)?
8. Ni nini msistizo mkubwa wa sehemu hii (Mt. 24:45-51)?
9. Je katika maisha yanko bado unatarajia kurudi kwa Yesu ukiwa hai? Kwanini?

## MATHAYO 25

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA				
UBS <sup>4</sup>	NKJV	NRSV	TEV	NJB
Mfano wa wanawali Kumi 25:1-13	Mfano wa wanawali Wenye hekima na Wapumbavu 25:1-13	Mfano wa wanawali Wenye Hekima na Wapumbavu 25:1-13	Mfano wa wanawali Kumi 25:1-5 25:6-12 25:13	Mfano wa Wanawali Kumi 25:1-13
Mfano wa Talanta Kumi 25:14-30	Mfano wa Talanta Kumi 25:14-30	Mfano wa Talanta 25:14-30	Mfano wa Watumishi Watatu 25:14-18 25:19-30	Mfano wa Talanta 25:14-30
Hukumu ya Mataifa 25:31-40 25:41-46	Mwana wa Adamu Atahukumu Mataifa 25:31-46	Hukumu Kuu 25:31-46	Hukumu ya Mwisho 25:31-40 25:41-46	Hukumu ya Mwisho 25:31-46

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka “[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)”)**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA MUKTADHA**

- A. Tazama kwa umakini muktadha wa kifasihi. Kwa namna hii muktadha ni Mathayo 24-25, inayoangalizwa kwa kurudi kusikotarajiwa kwa ghafla kwa Kristo na angalizo la "kuwa tayari" kwa kuwa mwaminifu katika kutenda mapenzi ya Mungu hata katikati ya dhiki.
- B. Kwa mjadala kamili katika kuitafsiri mifano angalia utangulizi wa Mathayo 13.
- C. Andika kwa maneno yako mwenyewe ukweli mkuu wa kila mfano (kama vile Mt. 24: 45-51; 25:1-13; 25:14-30). Mifano imekusudiwa kuelezea ukweli kutoka katika matukio ya kila siku yanayotokea katika maisha (kama vile Mt. 13:10-17). Siku zote tazamia mgeuko usiotarajiwa au kushangazwa!
- D. Mistari ya 37-44 haipo katika Marko. Ina ulinganifu nusu wa Vitabu vya Kiinjili katika Luka 17:26-37.

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 25:1-13**

<sup>1</sup> Ndipo ufalme wa mbinguni utakapofanana na wanawali kumi, waliotwaa taa zao, wakatoka kwenda

kumlaki bwana arusi.<sup>2</sup> Watano wao walikuwa wapumbavu, na watano wenye busara.<sup>3</sup> Wale waliokuwa wapumbavu walizitwaa taa zao, wasitwae na mafuta pamoja nao;<sup>4</sup> bali wale wenye busara walitwaa mafuta katika vyombo vyao pamoja na taa zao.<sup>5</sup> Hata bwana arusi alipokawia, wote wakasinzia wakalala usingizi.<sup>6</sup> Lakini usiku wa manane, pakawa na kelele, Haya, bwana arusi; tokeni mwende kumlaki.<sup>7</sup> Mara wakaondoka wanawali wale wote, wakazitengeneza taa zao.<sup>8</sup> Wale wapumbavu wakawaambia wenye busara, Tupeni mafuta yenu kidogo; maana taa zetu zinazimika.<sup>9</sup> Lakini wale wenye busara wakawajibu, wakisema, Sivyo; hayatatutosha sisi na ninyi; afadhali shikeni njia mwende kwa wauzao, mkajinunulie.<sup>10</sup> Na hao walipokuwa wakienda kununua, bwana arusi akaja, nao waliokuwa tayari wakaingia pamoja naye arusini; mlango ukafungwa.<sup>11</sup> Halafu wakaja na wale wanawali wengine, wakasema, Bwana, Bwana, utufungulie.<sup>12</sup> Akajibu akasema, Amin, nawaambia, siwajui ninyi.<sup>13</sup> Basi kesheni, kwa sababu hamwijui siku wala saa.

**25:1 "ufalme wa Mungu"** Utawala wa Mungu wa sasa juu ya maisha ya watu waliokombolewa siku moja utahitimishwa katika utawala Wake juu ya dunia nzima (kama vile Mt. 6:10). Angalia Mada Maalum katika Mt. 4:17.

☐ **"kumi"** Angalia Mada Maalum: Uwakilishi wa Hesabu katika Maandiko katika Mt. 24:31.

☐ **"wakatoka kwenda kumlaki bwana arusi"** Historia ya kimila ya mfano huu (ambayo ni ya kipekee katika Mathayo) inahusu desturi za ndoa za Kiyahudi za karne ya kwanza katika Palestina (angalia James Freeman, *Manners and Customs of the Bible*). Baada kama ya mwaka mmoja wa makubaliano ya kuchumbiwa, bwana harusi alikwenda katika nyumba ya bibi harusi kwa siku aliyopangiwa ili amchukue ampeleke nyumbani kwake kwa ajili ya sherehe ya siku saba.

Kuna utofautiano wa Maandiko ya Kiyunani hapa ambayo yanahusiana na maandiko ya kale ya desturi za Kiebrania. Maandiko bora zaidi ya Kiyunani ya kale yana "alitoka kwenda kumlaki bwana harusi." Maandiko ya Kiyunani ya Bezae (D) na ya Kilatini, Kishamu, Kikoptiki, na Fasiri za Ki-Armeni, pia kama maandiko ya kiyunani yaliyotumiwa na Origen, Athanasius, Chrysostom, Jerome, na Augustine linaongeza "na bibi harusi." Hii hivyo ingerejerea wakati alipoungana na sherehe ya harusi. Toleo la UBS<sup>4</sup> linatoa andiko fupi alama ya "B" (karibia na hakika).

**25:5 "Hata bwana arusi alipokawia"** Hii inaweza kurejerea kuchelewa kurudi kwa Yesu. Mathayo 24:14 na 43-44 inarejerea kuchelewa kati ya kuharibiwa kwa Yerusalemu na Kurudi kwa mara ya Pili. Kuchelewa huku kulilishangaza kanisa la kwanza (kama vile 2 Wathesalonike 2). Mifano kifasihi ni taswira ambayo ina kusudi kuu. Kuwa mwangalifu kugeuza maelezo kuwa mafundisho!

☐ **"wote wakasinzia wakalala usingizi"** Hakuna hukumu iliyokusudiwa kwa hili. Inaweka jukwaa kwa ajili ya msisitizo wa kujiandaa.

**25:9** Kila mtu lazima ajiandae yeye mwenyewe katika Ufalme!

**25:10 "mlango ukafungwa"** Luka 13:25 inafanana na mfano huu kwa Israeli na Mataifa, lakini muktadha unataka uhusiano kwa Kuja Mara ya Pili. Hii inaelezea namna gani Wainjilisti waliovuviwa walivyotumia mafundisho ya Yesu kwa mazingira tofauti tofauti na kwa makusudi mbali mbali (kama vile Gordon Fee na Douglas Stuart *How to Read the Bible for All Its Worth*, Ukr. 113-134). Angalia Mada Maalum: Matumizi ya "mlango" katika Agano Jipya katika Mt. 6:6.

**25:11 "Bwana, bwana"** Marudio yalikuwa ni jaribu la kuonesha ukaribu wa upendo (kama vile Luka 6:46), lakini uhusiano unakosekana (kama vile Mt. 7:21,22). Sehemu inayoshangaza ya mifano hii ni kwamba hii ilikuwa inaonekana kuwa sehemu ya wafuasi wa Yesu japo kwwa sehemu fulani siyo (kama vile Mathayo 13, mfano wa udongo na mfano wa magugu). Kama Paulo anavyosema katika Rum. 9:6, "Si Waisraeli wale wote watokao

Israeli," ndivyo ilivyo pia, si wale wafuasi wa nje wa Yesu wamekombolewa (kama vile 2 Pet.2:20-22; 1 Yohana 2:18-19 hata yawezekana baadhi maonyo ya Waebrania [yaani Waebrania 2:1-4; 3:7-13; 4:1-13; 5:11-6:12; 10:26-39; 12:14-17]). Angalia [MADA MAALUM: UKANAJI WA IMANI \(APHISTĒMI\)](#) katika Mt. 7:21.

**25:12 "siwajui ninyi"** Kukosa maandalizi kuna madhara ya milele. Hii inafanana na Mt. 24:50-51; 25:29-30; na Mt. 25:41-44. Mtu lazima awianishe sehemu tofauti za waovu zinazowasilishwa katika Agano Jipya.

1. ni maamuzi, ukiri wa wazi (yaani mtu anayekaribishwa)
2. ni uanafunzi, mtindo wa maisha ya utauwa(kuishi kama mtu huyo)
3. ni uelewa wa kibiblia uliohabarishwa (yaani kukubali ukwelikuhusu mtu huyo)

Vyote vitatu ni muhimu kwa ajili ya upevukaji.

Neno "kujua" lilitumika katika maana yake ya Agano la Kale la mahusiano ya kibinafsi ya upendo wa ukaribu (kama vile Mwa. 4:1; Yer. 1:5). Ukristo unaunganisha namna ya Kiebrania (uhusiano binafsi) na namna ya Kiyunani (taarifa). Injili ni nafsi, mtindo wa maisha na ujumbe!

### 25:13

**NASB** "Basi kesheni, kwa sababu hamwijui siku wala saa"

**NKJV** "Basi kesheni, kwa sababu hamwijui siku wala saa Mwana wa Adamu ajapo"

**NRSV** "Basi kesheni, kwa sababu hamwijui siku wala saa"

**TEV** "Basi kesheni, kwa sababu hamwijui siku wala saa"

**NJB** "Basi kesheni, kwa sababu hamwijui siku wala saa"

Ukweli huu ni makusudi ya mfano. Angalia dokezo kamili katika Mt. 24:40-41. Saa ya Kurudi kwa Mara ya Pili ni hakika lakini hakujulikani (kama vile Mt. 24:36,42,44,50; Marko 13:32). Waaminio wanatakiwa kuwa macho na tayari kwa ajili ya Ujio wa Yesu ambao ni hakika lakini ghafla (kama vile Mt. 24:36).

Kuna utofauti wa maandiko katika suala hili. Inavyoonekana wanakili waliongeza "ambamo ndani yake Mwana wa Adamu anakuja" kutoka 24:44. Tungo inayoongezeka haipo katika maandiko ya kale ya Kiyunani P<sup>35</sup>,  $\alpha$ , A, B, C\*, D, L, W, X, na Y, na pia Kilatini, Kishamu, Kikoptiki, na fasiri za Ki-Armeni. Ni dhahiri kuwa hii haina uasili katika Mathayo. Toleo la UBS<sup>4</sup> linatoa andiko fupi zaidi alama ya "A" (hakika).

☐"saa" Angalia Mada Maalum katika Mt. 24:36

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 25:14-18

<sup>14</sup> Maana ni mfano wa mtu atakaye kusafiri, aliwaita watumwa wake, akaweka kwao mali zake. <sup>15</sup> Akampa mmoja talanta tano, na mmoja talanta mbili, na mmoja talanta moja; kila mtu kwa kadiri ya uwezo wake; akasafiri. <sup>16</sup> Mara yule aliyepokea talanta tano akaenda, akafanya biashara nazo, akachuma faida talanta nyingine tano. <sup>17</sup> Vile vile na yule mwenye mbili, yeye naye akachuma nyingine mbili faida. <sup>18</sup> Lakini yule aliyepokea moja alikwenda akafukua chini, akaificha fedha ya bwana wake.

**25:16 "Mara yule aliyepokea talanta tano"** Mfano huu unafanana na ule katika Luka 19:11-27. Kuna utofautiano wa kimaandiko ya Kiyunani juu ya namna gani "mara/ghafla" inahusiana na Mt. 25:15: (1) Je inamfunua mmiliki wa mtumwa au (2) mtumwa? Ingawa maandiko ya Kiyunani yanatofautiana, muktadha na matumizi ya Mathayo ya "mara/ghafla" yanalazimisha maamuzi ya pili.

☐"talanta tano" Talanta moja ni sawasawa na Dinari 6,000. Dinari ilikuwa ni posho ya kila siku ya maskari na wafanyakazi. Tanbihi ya toleo la RSV inasema "zaidi ya posho ya miaka kumi na mitanoya mfanyakazi." Angalia Mada Maalum katika Mt. 17:24.

☐"kila mtu kwa kadiri ya uwezo wake" Hii inazungumza kanuni ya kibiblia (kama vile Mt. 13:8; 2 Kor. 8:3,11)

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 25:19-23**

<sup>19</sup> Baada ya siku nyingi akaja bwana wa watumwa wale, akafanya hesabu nao. <sup>20</sup> Akaja yule aliyepokea talanta tano, akaleta talanta nyingine tano, akisema, Bwana, uliweka kwangu talanta tano; tazama, talanta nyingine tano nilizopata faida. <sup>21</sup> Bwana wake akamwambia, Vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako. <sup>22</sup> Akaja na yule aliyepokea talanta mbili, akasema, Bwana, uliweka kwangu talanta mbili; tazama, talanta nyingine mbili nilizopata faida. <sup>23</sup> Bwana wake akamwambia, Vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako.

**25:21-23 "Vema, mtumwa mwema na mwaminifu"** Uwakili mzuri sio kiasi ndisho kinachozungumzwa hapa. Angalia Mada Maalum: Viwango vya thawabu na adhabu katika Mt. 5:12.

☐ **"ingia katika furaha ya bwana wako"** Tungo hii inayorudiwa ni nahau kwa kuingia katika Ufalme. Huduma kwa ajili ya Kristo ni huduma kwa ajili ya familia. Furaha ni ushirika.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 25: 24-25**

<sup>24</sup> Akaja na yule aliyepokea talanta moja, akasema, Bwana, nalitambua ya kuwa wewe u mtu mgumu, wavuna usipopanda, wakusanya usipotawanya; <sup>25</sup> basi nikaogopa, nikaenda nikaificha talanta yako katika ardhi; tazama, unayo iliyo yako.

**25:24-25** Tabia na sifa za mtumwa kwa usahihi hazimuelezei Mungu. Mtu hatakiwi kulazimisha maelezo ya mifano hii kuwa ki-istiari. Agano Jipya lina mifano yote ya ulinganifu na utofauti.

**ANDIKO LA NAB (LILIBORESHWA) MATHAYO 25:26-28**

<sup>26</sup> Bwana wake akajibu, akamwambia, Wewe mtumwa mbaya na mlegevu, ulijua ya kuwa navuna nisipopanda, nakusanya nisipotawanya; <sup>27</sup> basi, ilikupasa kuiweka fedha yangu kwa watoao riba; nami nikija ningalipata iliyo yangu na faida yake. <sup>28</sup> Basi, mnyang'anyeni talanta hiyo, mpeni yule aliye nazo talanta kumi.

**25:27 "riba"** Neno hili lilikuwa ni nahau ikiyochukuliwa kutoka katika kuzaa mtoto. Miongozo ya Agano la Kale kwa ajili ya riba inapatikana katika Kumb. 23:19-20. Myahudi alikuwa anaweza tu kukusanya riba kutoka kwa mataifa.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 25:29-30**

<sup>29</sup> Kwa maana kila mwenye kitu atapewa, na kuongezewa tele; lakini asiye na kitu, hata kile alichochacho atayang'anywa. <sup>30</sup> Na mtumwa yule asiyefaa, mtupeni mbali katika giza la nje; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno.

**25:29 "Kwa maana kila mwenye kitu atapewa"** Angalia Mt. 13:12; Marko 4:25; Luka 8:18; 19:26. "kuongezewa" haipo katika maandiko bali inamaanishwa kihakika.

**25:30 "mtupeni mbali katika giza la nje; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno"** Wasomaji wa kimagharibi hawajisikii vizuri na utiaji chumvi wa Mashariki na lugha za ulingafu wa vitu kisitiani (kama vile Mt. 8:12; 13:42,50; 22:13; 24:51). Mfano huu unaonesha uhitaji sio tu wa wokovu wa kuanzia bali jukumu linaloendelea. Ukiri unathibitishwa na mtindo wa maisha. Hakuna matunda-hakuna mzizi!

**MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele



katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kweli kuu gani ya mifano yote hii?
2. Ni kwa namna gani mifano hii inafanana na muktadha mwingine mkubwa wa Mathayo 24 na 25?
3. Elezea kauli kwamba Injili ilikuwa na haki chini ya uvuvio kushagua, kuasilisha na kupangilia mafundisho ya Yesu.

## TAMBUZI ZA MUKTADHA KWA 25:31-46

- A. Ni Yesu mwenyewe anayezungumza mara kwa mara juu ya madhara mabaya ya kutisha ya dhambi ya mwanadamu. Ni Yesu na Yesu pekee anayesisitiza sio tu hukumu ya mwisho bali kuzimu ya milele.
- B. Kifungu hiki kinaonekana kuwa ukuzwaji wa Mt. 16:27. Kifungu kizuri kinachofanana juu ya siku ya hukumu ni Ufunuo 20:11-15.
- C. Yesu anakuja tena kama Mfalme wa Mbingu aliyetukuzwa. Hii ni sawasawa na Wayahudi bado kuendelea kumtegemea Yeyekuja kwa mara ya kwanza.
- D. Biblia inazungumza juu ya uhakika wa hukumu lakini mara kwa mara inaathiriwa kwa usababishi tofauti.
  1. Mungu kama Hakimu (kama vile Rum. 14:2; 1 Petro 1:17)
  2. Kristo kama Hakimu (kama vile Yohana. 5:22, 27; Mt. 16:27; Mdo. 10:42; 2 Kor. 5:10; 2 Tim. 4:1)
  3. Mungu kupitia Kristo (kama vile Mdo. 17:31; Rum. 2:16)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 25:31-33

<sup>31</sup> Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake; <sup>32</sup> na mataifa yote watakusanyika mbele zake; naye atawabagua kama vile mchungaji abaguavyo kondoo na mbuzi; <sup>33</sup> atawaweka kondoo mkono wake wa kuume, na mbuzi mkono wake wa kushoto.

**25:31 "Mwana wa Adamu"** Hili lilikuwa ni neno lililotumika katika Agano la Kale kumaanisha kuashiria mwanadamu kama katika Zaburi 8:4 na Ezek. 2:1. Hata hivyo katika Dan. 7:13 mwanadamu anaitwa "mwana wa adamu," anayekuja katika mawingu ya kimbingu-aina ya usafiri kwa ajili ya uungu na inatolewa kwa ufalme wa milele. Cheo "Mwana wa Adamu" halikutumika katika dini ya Kiyahudi ya walimu wa sheria. Yesu alilitumia neno hili kujieleza mwenyewe kwa kujumuisha dhana za kibinadamu na uungu na halikuwa na ufanano mwembamba wa Kiyahudi, wa kizalendo na kijeshi. Kama Mwana wa Adamu alivyotembea mawinguni ya mbingu katika Dan. 7:13, sasa Anakuja na malaika watakatifu wote kuhukumu wanadamu (kama vile Mt. 25:31; 1 Thes. 4:13-18).

☐ **"katika utukufu Wake"** Angalia dokezo katika "utukufu" katika Mt. 16:27.

☐ **"na malaika wote pamoja naye"** Malaika watafanya kazi ya kukusanya na kutenga. Walikuwa mara kwa mara wakihusianishwa na kuja kwa Kristo (kama vile Mt. 16:27; Marko 8:38; 2 Thes. 1:7; Yuda 14; na Dan. 7:10).

☐ **"atakaa katika kiti Chake cha utukufu"** Atakaa katika kiti chake cha enzi ya Mungu (kama vile Zab. 110:1) sio tu kama Bwana na Mfalme bali kama Hakimu (kama vile Mt. 19:28). Kumkataa Yesu kuna kipengele cha muda mfupi (kama vile Yohana 3:18) na kipengele cha matukio ya siku za mwisho. Hukumu kwa muda itahitimishwa katika umilele.

**25:32 "Mataifa yote yatakusanyika mbele zake"** Kifungu hiki kinaweza kuwa mfano lakini ni uwasilishaji wa kitamthiliya ya pekee kwa Mathayo. Maswali yote juu ya nyakati za mwisho hayashughulikiwi. Mtu anaweza kushangaa ikiwa mataifa yote kunajumuisha wanadamu wote waliohai na wale waliokufa au wale tu walio hai. Kifungu cha maneno "mataifa yote" kulimaanisha kusambaa kiujumla kwa injili kwa watu wote (kama vile Ufunuo 5) kilichojumuisha Waisraeli. Hili ndilo lengo la Mwanzo. 3:15, 12:3, na Kutoka 19:4-6. Wito wa Israeli ilikuwa ni kuwa wamishonari kwa mataifa! Ni ngumu kubainisha kwa uhakika "mbuzi" ni watu gani: (1) wale waliokataa injili au (2) wale walio na ukiri wa nje tu? Makundi yote yanamuita Yesu "Bwana" (kama vile Mt. 7:21-23). Hukumu hii inaonekana kuwa na ukomo kwa wale ambao angalau kwa nje waliitikia injili. Hivyo ni sawasawa katika maana na mfano wa udongo (kama vile Mathayo 13). Shinikizo la matukio ya siku za mwisho na kukosekana kwa upendo kwa WAAMINIO wengine (kama vile 1 Yohana. 2:9,11; 3:15; 4:7-21) itaonyesha kwa uwazi ukiri wa uongo (kama vile Mt. 13:21,22; 1 Yohana 2:19).

☐ **"naye atawabagua"** Kwa mfanano kabisa kama wa ngano na magugu (kama vile Mt. 13:24-30, 36-43) haviwezi kutenganishwa maka siku ya hukumu, hivyo kondoo na mbuzi wasubiri mpaka siku ya mwisho kwa ajili ya wote kuona matunda ya maisha yao. Pia tazama kuna vipengele viwili.

☐ **"kama vile mchungaji abaguavyo kondoo na mbuzi"** Mungu kama mchungaji ilikuwa ni ulinganifu uliozoeleka katika Agano la Kale (kama vile Zaburi 23). "Mchungaji" lilikuwa likitumika katika Ezekieli 34 kuelezea wachungaji wa uongo wa Israeli kama Mchungaji Mkuu na Hakimu. Neno hilo hilo linamzungumzia Yesu katika Zek. 11:4-14; Yohana 10.

**25:33 "mkono wake wa kuume"** Hii ni tungo ya kibiblia ya lugha ya wanadamu kuelezea nafasi ya Mamlaka yasiyohamishika, heshima, nguvu na amri.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 25:34-40**

<sup>34</sup> Kisha Mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu; <sup>35</sup> kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninyweshwa; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; <sup>36</sup> nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia. <sup>37</sup> Ndipo wenye haki watakapomjibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona una njaa, tukakulisha, au una kiu tukakunyweshwa? <sup>38</sup> Tena ni lini tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha, au u uchi, tukakuvika? <sup>39</sup> Ni lini tena tulipokuona u mgonjwa, au kifungoni, tukakujia? <sup>40</sup> Na Mfalme atajibu, akiwaambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi.

**25:34 "Mfalme"** Yesu mara kwa mara alizungumzwa kama Mfalme ajaye (kama vile Ufu. 17:14; 19:16). YHWH pia alizungumzwa kama Mfalme, ambacho kinaleta umuhimu wa nyongeza kwa neno hili linapotumiwa kwa ajili ya Yesu (kama vile Kumb. 10:17; 1 Tim. 6:15). Huku kuhamishwa kwa jina ilikuwa mbinu iliyozoeleka ya maandishi wa Agano Jipya kuelezea uungu kamili wa Yesu wa Nazareti.

☐ **"mliobarikiwa na Baba yangu"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati timilifu. Wamekuwa wanabarikiwa kipindi chote cha nyuma na wanaendelea kubarikiwa. Mungu yuko kazini katika utendaji.

☐ **"urithini"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu. Hukumu ya Waaminio (kama vile 2 Kor. 5:10) haitajikita juu ya dhambi zetu (kama vile Tito 2:14; 1 Yohana. 1:7), bali juu ya matumizi yetu ya karama za rohoni na upatikanaji kwa Mungu (kama vile 1 Kor. 3:10-15). Angalia Mada Maalum: Urithi wa Mwamini katika Mt. 19:29.

☑️"**ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu**" Kauli tendwa endelevu la wakati timilifu. Tungo hii ya Agano Jipya mara kadhaa kuelezea vitu ambavyo Mungu alifanya kwa waaminio hata kabla ya uumbaji (kama vile Yohana. 17:24; Efe. 1:4, 11; 1 Pet. 1:19-20; Ufu. 13:8). Utatu ulikuwa ukifanya kazi hata katika ukombozi kabla ya Mwanzo 1:1! Kazi ya Mungu haijawahi kushindwa!

**25:35-39** Matendo yetu mema na mtindo wetu wa maisha unapenda kufunua na kuthibitisha kujizatiti kwetu katika imani ya kuanzia kwa Yesu Kristo (kama vile Efe. 2:8-9,10; 2 Tim. 2:21; 3:17; Tito 3:1; Ebr. 13:21). Imani bila matendo imekufa (kama vile Yakobo 2:14-26). Matendo haya mema kwa wengine yanafanana na matendo mema ya Yesu mwenyewe (kama vile Isa. 58:6-7). Waaminio wanaendeleza Huduma Yake (kama vile Tito 2:14).

**25:40 "mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi"** Neno "ndugu" linarejerea kwa jirani. Ni kwa waamini kujali wanadamu walioumbwa kwa sura na mfano wa Mungu ambako kunasisitizwa. Uhusiano wa karibu kati ya Yesu na Wafuasi wake unaweza kuonekana katika Matendo 9:4, 22:7, 26:14, na 1 Kor. 8:12. Kumuumiza mmoja ni kuwaumiza wote. Yesu anataka waaminio kuishi kwa namna hiyo ili kwamba Kazi yake duniani iendeleo (yaani kusaidia wanadamu walioanguka kutafuta ushirika pamoja na Muumbaji wao, kama vile Mt. 20:28; Marko 10:45; 1 Yohana 3:16).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 25:41-46**

<sup>41</sup> Kisha atawaambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake; <sup>42</sup> kwa maana nalikuwa na njaa, msinipe chakula; nalikuwa na kiu, msininyweshe; <sup>43</sup> nalikuwa mgeni, msinikaribishe; nalikuwa uchi, msinivike; nalikuwa mgonjwa, na kifungoni, msije kunitazama. <sup>44</sup> Ndipo hao pia watajibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona wewe una njaa, au una kiu, au u mgeni, au u uchi, au u mgonjwa, au u kifungoni, tusikuhudumie? <sup>45</sup> Naye atawajibu, akisema, Amin, nawaambia, Kadiri msivyomtendea mmojawapo wa hao walio wadogo, hamkunitendea mimi. <sup>46</sup> Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele.

**25:41 "Kisha atawaambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, Ondokeni kwangu"** Ubaya kuliko vyote juu ya kuzimu ni kuwa kunakutenganishwa kutoka katika ushirika na Mungu (kama vile Mt. 7:23; Luka 13:27). Mungu hapeleki watu kuzimu; wanajipeleka wenyewe kwa maamuzi ya mtindo wao wa maisha.

☑️"**mliolaaniwa**" Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati timilifu. Tungo hii ya kisarufi iltumika mara kadhaa katika muktadha huu. Inazungumzia kile kilichotokea katika siku zilizopita na matokeo ambayo yameendelea mpaka sasa. Kitendo kimetendeka na mtendaji wa nje. Kumkataa huku Mungu kwa watu na Kristo Wake kwa wakati uliopita kumehitimishwa katika upofu wa kudumu na kukataa! Kukataa huku kunajifunua kwenyewe katika kukosekana kwa wanadamu wengine (Mt. 25:42-43).

☑️"**mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake**" Kuzimu hakutengenezwa kwa ajili ya wanadamu bali kwa viumbe vya kimalaika walio katika kuasi. Shetani ana malaika wanaomtumikia, yawezekana ikielezewa katika Dan. 8:10 na Ufu. 12:4. Mathayo 25 inachanganya sitiari za giza katika Mt. 25:30, na moto katika Mt. 25:41. Hofu na mateso ya kuzimu yanazidi sana misamiati ya kibinadamu na mwanzo wenye ukomo kwamba Biblia inatumia taswira sahihi zaidi inayowezezana. Sitiari nyingi zaidi zinatoka katika taka ya uchafu nje ya Yerusalemu katika bonde la wana wa Hinnom liitwalo "*Gehenna*." Yesu mara kwa mara alilizungumzia (kama vile Isa. 33:14; 66:24; Mt. 3:10, 12; 5:22; 7:19; 13:40, 42, 50; 18:8, 9; Yuda 7; Ufu. 14:10; 19:20; 20:10, 14, 15; 21:8). Angalia [MADA MAALUM: MILELE](#) katika Mt. 18:8.

**25:45 "Amin, nawaambia"** Kibayana "*amen*," lilikuwa ni neno la Kiebrania "kuwa imara." Lilikuwa likitumika na waandishi wa Kibiblia kukiri uhalisia na ukweli wa maneno, dhana na mafundisho. Yesu kipekee alilitumia kuanza

sentensi. Mara kwa mara alilitumia mara mbili hata zaidi kwa ajili ya msisitizo zaidi. Angalia Mada Maalum: katika Mt. 5:1.

**25:46 "Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele"** Neno hilo hilo [*aiōnos*] ambalo linaelezea mbingu kama yenye kudumu linatumiwa kwa kuzimu kama lenye kudumu (kama vile Mt. 18:8; 19:16; Marko 3:29; 9:48; 10:17; Luka 18:18; Yuda 7; Ufu. 20:10; pia pamoja na "hukumu ya milele 2 Thes. 1:9 na Ebr. 6:2). Danieli 12:2; Yohana 5:29; na Mdo. 24:15 inaelezea ufufuo wa wote wenye haki na wabaya. Josephus anasema kwamba Mafarisayo waliamini katika kutokufa kwa wote wenye "nafsi" (kama vile *Antiq.* 18.1,3), lakini tu ufufuo wa wenye haki kupata mwili mpya wakati wabaya wana adhabu ya milele (kama vile *Jewish Wars* 2.8,14). Umilele na mwisho ni mwanzo wa uharaka wa kuhubiri injili, kufundisha na kushuhudia!

Kuzimu ya milele sio tu janga kwa wanadamu wenye uasi lakini pia kwa Mungu! Mungu aliwaumba wanadamu kama kilele cha tukio lake la uumbaji. Tumeumbwa kwa Sura na mfano ili tuwe na ushirika pamoja naye (kama vile Mwa. 1:26-27). Uchaguzi wa Mungu kumruhusu mwanadamu kufanya uchaguzi ulipelekea kiwango fulani cha uumbaji wa Mungu kutenganishwa na Yeye mwenyewe! Kuzimu iko wazi, kidonda kinachovuja katika moyo wa Mungu ambacho hakitawahi kupona.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa namna gani kuzimu inaweza ikawa na vyote giza na moto?
2. Je kifungu hiki kinafundisha kwamba baadhi wataokolewa kwa matendo yao mema kwa wanadamu wengine?
3. Kwa maneno yako mwenyewe, ni kweli kuu gani iliyopo katika kifungu hiki?
4. Je Wakristo watahukumiwa?
5. Je Kuzimu inamgharimu nini Mungu?

## MATHAYO 26

<b>MIGAWANYO YA AYA KATIKA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Njama za Kuumua Yesu	Njama za kumuua Yesu Yesu	Kifo cha Yesu Yesu	Njama dhidi Yesu Yesu	Mpango dhidi ya Yesu
26:1-5	26:1-5	26:1-2	26:1-2	26:1-2
26:3-5	26:3-5	26:3-5		
Utiwaji wa Mafuta huko Bethania	Utiwaji Mafuta huko Bethania		Yesu Anatiwa Mafuta huko Bethania	Utiwaji Mafuta huko Bethania
26:6-13	26:6-13	26:6-13	26:6-9 26:10-13	26:6-13
Makubaliano ya Yudas juu ya Yesu	Yuda Anafanya makubaliano ya Kumsaliti Yesu		Yudas anakubaliana Kumsaliti Yesu	Yuda Anamsaliti Yesu
26:14-16	26:14-16	26:14-16	26:14-16	26:14-16
Paska pamoja na Wanafunzi	Yesu Anasherekea Pasaka pamoja na Wanafunzi wake	Karamu ya Mwisho	Yesu Ankula Karamu ya Pasaka pamoja na Wanafunzi wake	Maandalizi ya Karamu ya Pasaka
26:17-25	26:17-30	26:17-19	26:17 26:18 26:19	26:17-19  Njama za Yuda Zinatabiriwa
		26:20-25	26:20-21 26:22 26:23-24 26:25a,b 26:25c	26:20-25
Karamu ya Ushirika			Karamu ya Bwana	Ushirika wa Ekaristi

26:26-30		26:26-29	26:26 26: 26:27-29	26:26-29
		Gethsemane		
		26:30	26:30	26:30-35
Kukana kwa Petro Kunatabiriwa	Yesu Anatabiri juu ya Kukana Kwa Ptro	Yesu Anatabiri juu ya Kukana kwa Petro	Yesu Anatabiri juu ya Kukana kwa Peto	
26:31-35	26:31-35	26:31-35	26:31-32 26:33 26:34 26:35a 26:35b	
Maombi katika Gethsemane	Maombi ndani ya Bustani		Yesu Anaomba Ndani ya Gethsemane	Gethsemane
26:36-46	26:36-46	26:36-46	26:36-38 26:39 26:40-41 26:42-43 26:44-46	26:36-37 26:38-46
Usaliti na Kukamatwa kwa Yesu	Usaliti na Kukamatwa ndani ya Gethsemane		Kukamatwa kwa Yesu	Kukamatwa
26:47-56	26:47-56	26:47-56	26:47-48 26:49 26:50a 26:50b-54 26:55-56a	26:47-56

		26:56b		
Yesu Mbele ya Baraza	Yesu Anakutana na Waku wa Sinagogi	Yesu Mbele ya Kayafa	Yesu Mble ya Baraza	Yesu Mbele ya Wakuu wa Sinagogi
26:57-68	26:57-68	26:57-68	26:57-61	26:57-58
			26:62-63	26:59-66
			26:64	
			26:65-66a	
			26:66b	
			26:67-68	
			26:67-68	
Petro Kumkana Yesu Petro	Kumkana Yesu, na Kuomboleza kwa Uchungu sana		Petro Anakana	Petro Anakana
26:69-75	26:69-75	26:69-75	26:69	26:69-75
			26:70-71	
			26:72	
			26:73	
			26:74a	
			26:74b-75	

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka “[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)”)**

***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO LA 26:1-35

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 26:1-2

<sup>1</sup> Ikawa Yesu alipomaliza maneno hayo yote, aliwaambia wanafunzi wake, <sup>2</sup> Mnajua ya kuwa baada ya siku mbili itakuwa Pasaka, na Mwana wa Adamu atasalitiwa asulibiwe.

**26:1 "Ikawa Yesu alipomaliza maneno hayo yote"** Kifungu hiki kinayarejelea mazungumzo ya Yesu yahasuyo matukionya siku za mwisho yaliyo katika Mathayo 24-25. Kifungu hiki ni kiashiria cha kifasihi kilichotumiwa na Mathayo kuonyesha mazungumzo ya Yesu (kama vile Mt. 7:28; 11:1; 13:53; 19:1; 26:1).

**26:2 "baada ya siku mbili itakuwa Pasaka, na Mwana wa Adamu atasalitiwa asulibiwe"** Kuna mkanganyiko mwingi kuhusu siku barabara ya Karamu ya Bwana na, kwa sababu hiyo, hili lilikuwa juma la mwisho la safari ya huduma ya Yesu. Kwa uwazi Karamu ya Bwana ilihusianishwa na viashiria vya Pasaka (kama vile Yohana 1:29). Vidokezo vya Injili vinaeleza kuwa huu ulikuwa mlo wa Pasaka, lakini Yohana anasema kuwa hii ilikuwa siku ya kabla ya tukio. Kuna baadhi ya ushahidi kwamba kwakuwa kuhani mkuu alikuwa amepotoka kwa shushwa kwa kulipwa na wamiliki wa Kirumi ya kwamba madhehebu kadhaa ya Kiyahudi yalikuwa na Pasaka yao siku tofauti na hiyo (yaani., Waesene wa Magombo ya Bahari ya Chumvi waliotumia kalenda ya jua na walikuwa na Pasaka iliyotangulia siku moja kabla) kuliko sikukuu maalumu.

Njia ya Yohana ya kuweka tarehe ya Karamu inamsistiza Yesu kama wanakondoo wa Pasaka aliyechinjwa kwa ajili ya familia. Ikiwa ni hivyo, Yohana anaweza kuwa kuwa amebadili tarehe kwa sababu za kithiolojia, kama alivyoligeuza tendo la kusafisha hekalu hapo awali kwa ajili ya uwasilishaji wa kithiolojia wa maisha ya Yesu. Waandishi wa Injili chini ya uvuvio walikuwa na haki ya kuchagua, kuasilisha, na kupanga maneno na mahitaji ya Yesu ili kumwakilisha katika makundi mbalimbali (Gordon Fee, Doug Stuart, *How To Read the Bible For All Its Worth*).

▣ **"Mwana wa Adamu"** Tazama maelezo katika Mt. 8:24:30.

▣ **"atasalitiwa asulibiwe"** Yesu aliwafahamisha wanafunzi juu ya hili mara kadhaa (kama vile Mt. 16:21; 17:9,12,22-23; 20:18-19; 27:63). Tabiri hizi zingewatia moyo wafuasi wake katika siku hizi za juma la Mateso. Yesu aliyajua matukio yajayo. Yesu aliyasalimisha maisha yake mwenyewe (kama vile Marko 10:45; Yohana. 10:11,15,18). Mara nyingi alikuwa akiendana na wakati na matukio yenyewe.

▣ **"asulibiwe"** Huu ni mfumo wa unyanyasaji wa hadharani. Kwa vyo vyote vile uliendelezwa na Wafonisti au katika Mesopotamia kwa ajili yha kuuondoa maasi na uhalifu lakini ulikamilisha wa (yaani., mahali ulipoendelezwa kwa siku kadhaa) na Warumi. Hakuna raia wa Kirumi ambaye angesulibiwa. Huu ulihusisha upigwaji wa hadharani na kupigiliwa misumari msalabani. Umbo la msalaba lilikuwa kama herufi kuwa "T" au herufi ndogo "t" au herufi "X." Pia inawezekana kwamba jukwa la kunyongea wahalifu lilitumika pale watu kadhaa waliposulibiwa kwa pamoja. Hatimaye kifo kilimkumba ntu baada ya kukosa hewa. Ilimpasa mtuhumiwa kusukumwa miiguu yake iliyopigwa misunari kwa ajili ya kupumua. Ndiyo maana tendo la kuvunja miguu ya wahalirifu waliosulibiwa pamoja na Yesu lilisababisha kifo chao cha haraka (kama vile Yohana. 19:32).

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 26:3-5

<sup>3</sup> Wakati ule wakuu wa makuhani, na wazee wa watu, wakakusanyika katika behewa ya Kuhani Mkuu, jina lake Kayafa; <sup>4</sup> wakafanya shauri pamoja, ili wamkamate Yesu kwa hila na kumwua. <sup>5</sup> Lakini wakasema, Isiwe wakati wa sikukuu, isije ikatokea ghasia katika watu.



**26:3 "wakuu wa makuhani, na wazee"** Hili liikuwa jina fupi la Wakuu wa Sinagogi. Tazama Mada Maalum katika Mt. 20:18.

☐ **"katika behewa ya Kuhani Mkuu"** Hili eneo linarejelea uwanja mkuu wa Kayafa na huenda ndiyo kasri la Anasi.

☐ **"Kayafa"** Kayafa alikuwa Kuhani Mkuu, liyeteuliwa na Rumi, katika mabadilishano ya thamani ya fedha, kutoka b.k. 18- 36. Huyu alikuwa mwewe Anasi, Kuhani Mkuu toka b.k. 6-15. Nyumba hii yenye nguvu ilivutia sana kisiasa na kiutajiri kuliko kiroho. Si sawa kuwahukumu Masadukayo wote au, kwa sababu hiyo, Wakuu wa Sinagogi, kwa sababu yao.

**26:4"ili wamkamate Yesu kwa hila na kumwua"** Uamuzi huu wa kumuu ulikuwa umefanywa mapema tangu wakati wa huduma yake, lakini walikuwa wakitegeshea wakati watu hawapo (kama vile Mt. 12:14; Marko 14:1; Luka 22:2; Yohana 5:18; 7:1,19,25; 8:37,40; 11:53). Walimuonea wivu kwa sababu ya umaarufu wake na woga wa mafundisho na matendo yake.

**26:5"wakati wa sikukuu"** Pasaka ilikuwa imeunganishwa na Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu ili kuunda sikukuu ya nane (kama vile Kutoka 12 na Josephus' *Antiquities of the Jews* 3.10.5).

☐ **"isije ikatokea ghasia katika watu"** Wanahija wengi toka Galilaya na sehemu mbalimbali zilizokaliwa na Wayahudi walikuwepo Yerusalemu kwa ajili ya kuisherehekea Pasaka. Pasaka ilikuwa ya muhimu kwa wanaume wote wa Kiyahudi wenye umri upatao miaka ishirini na kuendelea (kama vile Law. 23:2, 4, 17, 44; Hes. 29:39). Yerusalemu ilifurika mara tatu ya idadi ya kawaida wakati wa sikukuu muhimu za mwaka. Mara nyingi Warumi walileta wanajeshi wa ziada wakati wa sikukuu hizi (kama vile Mt. 27:24).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 26:6-13**

<sup>6</sup> Naye Yesu alipokuwapo Bethania katika nyumba ya Simoni mkoma, <sup>7</sup> mwanamke mwenye kibweta cha marhamu ya thamani kubwa alimkaribia akaimimina kichwani pake alipoketi chakulani. <sup>8</sup> Wanafunzi wake walipoona, wakachukiwa, wakasema, Ni wa nini upotevu huu? <sup>9</sup> Maana marhamu hii ingaliweza kuuzwa kwa fedha nyingi wakapewa maskini. <sup>10</sup> Yesu akatambua akawaambia, Mbona mnamtaabisha mwanamke? Maana ni kazi njema aliyonitendea mimi. <sup>11</sup> Kwa maana siku zote mnao maskini pamoja nanyi; lakini mimi hamnami siku zote. <sup>12</sup> Maana kwa kunimwagia mwili wangu marhamu hiyo, ametenda hivyo ili kuniweka tayari kwa maziko yangu. <sup>13</sup> Amin, nawaambieni, Kila patakapohubiriwa Injili hii katika ulimwengu wote, tendo hilo alilolitenda huyu litatajwa pia kwa kumbukumbu lake.

**26:6 "nyumba ya Simoni mkoma"** Maria na Martha waliandaa chakula (kama vile Yohana 12:1 na kuendelea), lakini hapa hapakuwa nyumbani kwao (kama vile Marko 14:3). Inawezekana kwa kiasi fulani walihusiana, wote walitoka katika kijiji kidogo kiitwacho, Bethania. Kwa hali iliyo dhahiri huyu ndiye Simoni (japo haikuandikwa) aliyeponywa na Yesu.

**26:7 "mwanamke"** Yohana. 12:3 inaesma huyu alikuwa Maria, dada wa Lazaro. Maelezo haya hayapaswi kukuchanganywa na ya yule kahaba wa Luka 7:37-39.

☐ **"kibweta cha marhamu ya thamani kubwa"** Hiki kilikuwa kiliba cheupe kilichotengenezwa kwa jiwe/cha njano stone toka Misri. Yaliyokuwa ndani yake manukato ya mmea wa kihindi uitwao "nardo" au "mwiba wa nardo" (kama vile Wimbo Ulio Bora 1:12; 4:13-14; Marko 14:3; Yohana. 12:3). hiki kilikuwa cha gharama sana na yawezekana hiki kilitolewa kama mahari ya harusi ya Maria.

☐ **"akaimimina kichwani pake"** Yohana 12:3 anasema kwamba aliiweka nardo yake "miguuni." Kwa kuwa kilikuwa na aushi 12, au paundi moja ya Kirumi, kulikuwa na marhamu ya kuutosha mwili wake. Kibweta hiki kilipofunguliwa kisingefungwa tena.

**26:8 "Wanafunzi wake walipoona, wakachukiwa"** Yohana 12:4 anasema huyu alikuwa Yuda Iskarioti aliyepata mshutuko.

**26:9 "fedha nyingi"** Gharama hii kubwa ilikuwa dinari ipatayo mia tatu (kama vile Yohana. 12:5). Dinari ulikuwa ujira wa siku kwa wanajeshi au vibarua. Dokezo ni kwamba Yuda alikuwa akifikiri juu ya mahitaji ya maskini. Hata hivyo, huyu alitaka kiasi fulani cha fedha kwa ajili yake mwenyewe (kama vile Yohana 12:6).

**26:10"Kazi njema aliyonitendea mimi"** Hii nomino "tendo" na kitendo vinatokana na asili ile ile. Hii inauchochea usemi huu au ilikuwa nahau (kama vile Yohana 3:21; 6:28; 9:4; Matendo 13:41; 1 Kor. 16:10).

**26:11"Kwa maana siku zote mnao maskini pamoja nanyi"** Huu haukuwa usemi mgumu kuuhusu umaskini, bali ni utambuzi wa upekee wa kuwepo Iwa Yesu.

**26:12"ili kuniweka tayari kwa maziko yangu"** Maria alikuwa mwanafunzi; huenda alikuwa na uelewa zaidi ya Mitume! Marhamu yalitumika kupaka mwili wa mtu aliyekufa kabla ya maziko (kama vile Yohana 19:40).

**26:13 "katika ulimwengu wote"** Yesu alidhani kuwa Injili (Mathayo analitumia neno hili kwa ajili ya mmatendo ya Yesu yaliyo katika Mt. 4:23; 9:35; na kulitumia neno hili katika Mt. 24:14; 26:13) ingehubiriwa kila mahali (kama vile Mt. 24:9,14,32; 28:19-20). Hili linakamlisha tabiri za kiulimwengu za Agano la Kale (hasa Isaya, yaani, 2:1-4; 42:6; 49:6;51:4-5; 56:7)!

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 26:14-16**

<sup>14</sup> Wakati huo mmoja wa wale Thenashara, jina lake Yuda Iskariote, aliwaendea wakuu wa makuhani, <sup>15</sup> akasema, Ni nini mtakachonipa, nami nitamsaliti kwenu? Wakampimia vipande thelathini vya fedha. <sup>16</sup> Tokea wakati huo akawa akitafuta nafasi apate kumsaliti.

**26:14 "Iskarioti"** Kuna nadharia kadhaa kuhusiana na neno hili (neno linaandikwa tofauti katika machapisho ya Kiyunani). Hili lingeweza kurejelea

1. Mtu wa Keriothi, mji wa Yuda
2. Mtu wa Kartani, mji wa Galilaya
3. Mkoba wa ngozi uliotumika tunzia fedha
4. Neno la Kiebrania lenye maana ya "kunyonga"
5. Neno la Kiyunani lenye maana ya kisu cha kuulia

Ikiwa #1 ni kweli huyu alikuwa Myunani pekee miongoni mwa wale Kumi na Wawili. Ikiwa #5 ni kweli huyu alikuwa alikuwa mkereketwa kama Simoni.

Kumekuwa na kitabu kilichoandikwa hivi karibuni kinaitwa *Judas, Betrayer or Friend of Jesus?* Kilichoandikwa na William Klassen, Fortress Press, 1996. Matatizo mengi katika hiki ni kwamba hakikwendana na mawazo yatokanayo na Injili ya Yohana kwa umakini.

**26:15"Ni nini mtakachonipa, nami nitamsaliti kwenu"** Shauku yake inaonekana dhahiri (kama vile Yohana. 12:6). Huzuni ya Yuda haielezeki. Nadharia nyingi za sasa zinamfikiria kama mwenye kujaribu kumlazimisha Yesu kuwa masihi wa Kiyahudi mwenye kutarajiwa kijeshi. Injili ya Yohana inamweleza kama mwizi.

▣ **"vipande thelathini vya fedha"** Hili lilikamilisha unabii wa Zek. 11:12-13 (kama vile Mt. 27:9-10). Yesu alikuwa mchungaji aliyekataliwa. Hii ni gharama iliyolipwa katika Agano la Kale kwa ajili ya mtumwa aliyetumbuliwa (kama vile Kut. 21:32). Sura za 9-14 ya Zekaria zinanukuliwa mara kadhaa kama chimbuko la kinabii katika uhusiano na huduma ya Yesu.

1. Mt. 21:4-5 inainukuu Zek. 9:9
2. Mt. 24:3 inainukuu Zek. 12:10
3. Mt. 26:15 inainukuu Zek. 11:12-13

4. Mt. 26:31 inainukuu Zek. 13:7
5. Mt. 27:9-10 inainukuu Zek. 11:12-13

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 26:17-19**

<sup>17</sup> Hata siku ya kwanza ya mikate isiyotiwa chachu, wanafunzi wake wakamwendea Yesu, wakamwambia, Ni wapi utakapo tukuandalie uile Pasaka? <sup>18</sup> Akasema, Enendeni mjini kwa mtu fulani, mkamwambie, Mwalimu asema, Majira yangu ni karibu; kwako nitafanya Pasaka pamoja na wanafunzi wangu. <sup>19</sup> Wanafunzi wakafanya kama Yesu alivyowaagiza, wakaiandaa Pasaka.

**26:17 "siku ya kwanza ya mikate isiyotiwa chachu"** Mtiririko halisi wa juma lililopita unaleta mkanganyiko. Mara nyingi Vidokezo vya Injili (Mathayo, Marko na Luka) na Yohana (13:1; 19:14,31,42) havikubaliani na hili. Hii siku ya nane ilihusisha Sabato mbili, Pasaka kama ya kwanza (kama vile Law. 23:4-8; Kumb. 16:8).

☐ **"wanafunzi"** Luka 22:8 inawatambua Petro na Yohana kama wanafunzi hawa.

☐ **"Pasaka"** Hii ililiwa katika Nisani mnamo saa 12:00 jioni. Siku kamili ya juma ilitotautiana mwaka hadi mwaka kwa sababu ya kalenda ya mzunguko wa jua la Kiyahudi (kama vile Mt. 26:20).

**26:18 "kwa mtu fulani"** Luka 22:10 inasema huyu alipaswa kutambuliwa kwa "mwenye kubeba mtungi wa maji," kiutamaduni tendo hili lilifikiriwa kama kazi ya wanawake.

**NASB, NRSV,**

**NJB** "Wakati wangu u karibu"

**NKJV** "Wakati wangu u mkononi"

**TEV** "Saa yangu imwewadia"

Hiki kilikuwa kifungu chenye uficho kilichotumiwa na Yesu kwa ajili ya wakati wake wa kukataliwa, kusalitiwa, na kusulibiwa (kama vile Yohana. 2:4; 7:6, 8, 30; 8:20; 12:23; 13:1; 17:1).

☐ **"kwako nitafanya Pasaka pamoja na wanafunzi wangu"** Wengi wanaweza kuamini kuwa hapa palikuwa nyumbani kwa Yohana Marko ambaye alikuwa

1. mjomba wake Barnaba (Kol. 4:10)
2. msaidizi wa huduma ya kimisheni (Matendo ya Mitume 12:25; 13:5,13; 15:37,39)
3. mwandishi wa kumbukumbu za Petro, Injili ya Marko (1 Pet. 5:13)

Pia inafikiriwa kwamba hili lilikuwa eneo la ghorofani (kama vile Matendo ya Mitume 1:13; 12:12), mahali ambapo wanafunzi walikuwa wakiungojea ujio wa Roho (Matendo 1:5; 2:1).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 26: 20-25**

<sup>20</sup> Basi kulipokuwa jioni aliketi chakulani pamoja na wale Thenashara. <sup>21</sup> Nao walipokuwa wakila, alisema, Amin, nawaambia, Mmoja wenu atanisaliti. <sup>22</sup> Wakahuzunika sana, wakaanza kumwuliza mmoja mmoja, Ni mimi, Bwana? <sup>23</sup> Akajibu akasema, Yeye aliyetia mkono wake pamoja nami katika kombe, ndiye atakayenisaliti. <sup>24</sup> Mwana wa Adamu aenda zake, kama alivyoandikiwa; lakini ole wake mtu yule ambaye amsaliti Mwana wa Adamu! Ingekuwa heri kwake mtu yule kama asingalizaliwa. <sup>25</sup> Yuda, yule mwenye kumsaliti, akajibu, akasema, Ni mimi, Rabi? Akamwambia, Wewe umesema.

**26:20 "aliketi chakulani"** Meza na viti vilikuwa vikitumika huko Misri tu katika kipindi cha wakati huu. Katika Palestina walikuwa wakiegemea kiwiko cha kushoto katika meza ndogo na kuweka miguu nyuma yao (kama vile Marko 14:18). Hivi ndivyo namna Maria alivyoweza kuipaka mafuta miguu yake kwa urahisi (kama vile Yohana. 12:3).

**26:21 "atanisaliti"** Hili ni neno la Kiyunani "kuacha" (*paradidōmi*). Mara nyingi hili linatafsiri na Biblia za Kiingereza kama "fichua", lakini hii si maana iliyodumishwa. Hili linaweza kumaanisha

1. kwa maana iliyo chanya ya kufunua (kama vile Mt. 11:27)
2. kurejesha au kuweka mikononi mwa (kama vile Matendo 14:26; 15:40)
3. maana hasi ya kumweka mtu mikononi mwa wenye nguvu
4. kumweka mtu mikononi mwa Shetani (kama vile 1 Kor. 5:5; 1 Tim. 1:20)
5. kwa Mungu ni mtu kuicha njia hiyo na kuigeukia sanamu (kama vile Matendo 7:42)

Ni dhahiri kwamba muktadha ndiyo upasao kuitambulisha maana ya kitenzi cha kawaida.

**26:22 "Ni mimi, Bwana"** Kila mwanafunzi aliuliza swali. Tungo ya sarufi ya Kiyunani inatarajia jibu kanushi. Kuuliza kwao maswali kunaonyesha taharuki yao.

**26:23 "Yeye aliyetia mkono wake pamoja nami katika kombe, ndiye atakayenisaliti"** Mtu kumsaliti mwenyeji wake ilikuwa aibu kubwa katika Mashariki (kama vile Zab. 41:9). Yuda alikuwa na kiti cha heshima baadaye katika mkono wa kushoto wa Yesu. Yesu alikuwa akimnyoshea kidole Yuda!

☐ **"kombe"** Hili lilikuwa la jadi la kuwekea karanga wakati wa Pasaka, zabibu kavu, cha kisasa, tini, na siki.

**26:24** Yesu alijijua yeye ni nani na nini alichopaswa kufanya (kama vile Yohana 13:1). Yesu alikuja kumfunua Mungu, kuwapa wanadamu mfano wa kufuata, na kufa kwa ajili ya dhambi zao (kama vile Marko 10:45; Matendo ya Mitume 2:23-24; 2 Kor. 5:21). Maisha yake yalifunuliwa katika unabii wa Agano la Kale (kama vile Mt. 26:31,54,56; 11:10; 21:42).

☐ **"kama"** Hii ni sentensi amrishi daraja la pili. Kusaliti kwa Yuda kulikuwa muhimu, tendo lililotabiriwa kuwa atayatumikia mateso. Hii ndiyo siri ya uchaguzi na mapenzi huru!

**26:25 "Ni mimi, Rabii"** Elewa kuwa Yuda alitumia jina "rabi" (yaani., mwalimu wangu) si "Bwana" kama wanafunzi wengine walivyokuwa wakitamka.

☐ **"Wewe umesema"** Yesu alikuwa akijaribu kumnyoshea kidole Yuda. Kifungu cha kinahau pia kinatumika katika Mt. 26:64 na 27:11.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) MATHAYO 26:26-29**

<sup>26</sup> Nao walipokuwa wakila Yesu alitwaa mkate, akabariki, akaumega, akawapa wanafunzi wake, akasema, Twaeni, mle; huu ndio mwili wangu <sup>27</sup> Akakitwaa kikombe, akashukuru, akawapa, akisema, Nyweni nyote katika hiki; <sup>28</sup> kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi. <sup>29</sup> Lakini nawaambieni, Sitakunywa kabisa tangu sasa uzao huu wa mzabibu, hata siku ile nitakapokunywa mpya pamoja nanyi katika ufalme wa Baba yangu.

**26:26 "walipokuwa wakila"** Tazamio la mlo huu wa *seder*, unaodokezwa na kifungu hiki, kilikuwa kikombe cha tatu cha Baraka baada yam lo wenyewe. Yesu alitaka halitaka kuitambulisha hili kwa ushahidi wa Kutoka. Yeye alikuwa mwana-kondoo wa Mungu, lakini alichagua mkate na divai, si mwana-kondoo wa Pasaka, kama ishara ya agano jipya.

**Mathayo anamtabiri Yesu mara kwa mara kama Musa wa pili, mleta torati mpya. Yesu analeta torati mpya toka dhambini.**

☐ **"mkate"** Neno hili linairejelea mikate ya keki isiyotiwa chachu yenye umbo bapa, iliyotumika kama mlo wa Pasaka (kama vile Kut. 12).

**26:26-28 "huu ndio mwili wangu. . . hii ndiyo damu yangu"** Karamu ya Bwana iliyoandikwa ni maelezo ya Paulo yaliyo katika 1 Kor. 11:17-34. Vidokezo vya Injili viliandikwa baada ya waandishi wa Agano Jipya. Tarehe kamili haijulikani lakini haya hayakuwa maandishi ya kanisa la kwanza (kama vile William L. Blevins'book *Birth of a New Testament*, personal publication, Carson-Newman College).

**26:28 "hii ndiyo damu yangu ya agano"** Hili linaweza kuwa dokezo la Kut. 24:8. Machapisho mengine ya herufi kubwa za Kiyunani yanaongeza "mpya" kabla ya neno agano: MSS A, C, D, na W. Hili linaweza kuiakisi Yer. 31:31-34. Hata hivyo, machapisho mengine mazuri ya kale (MSS P<sup>37</sup>,  $\kappa$ , B, and L) hayaliweki ongezeko hili. Hili linaweza kuwa limechukuliwa toka katika Luka 22:20. Halipatikani katika Marko 14:24. Toleo la UBS<sup>4</sup> linaupa usomaji huu mfupi daraja "B" (kwa kiasi fulani ni halisi).

☑ **"imwagikayo kwa ajili ya wengi"** Hili ni dokezo la Isa. 53:11-12. Tazama [MADA MAALUM: ILIYOMWAGIKA](#) katika Mt. 23:35. Kumekuwa na mjadala mkubwa kuhusianana uhusiano kati ya kifungu "wengi" cha Isa. 53:11,12 na "sisi sote" cha Isa. 53:6. Ufanano huu wa Rum. 5:17-19 unaweza kutoa jibu la swali hili. Kifungu "watu wote" cha Mt. 5:18 ni sawa na "wengi" cha Mt. 5:19. Yesu alikufa kwa ajili ya wanadamu wote (kama vile Yohana. 3:16); kwa uweza wote wameokolewa katika yeye!

☑ **"kwa ondoleo la dhambi"** Hii ni nguvu ya Agano Jipya (kama vile Yer. 31:31-34) na umuhimu wa jina la Yesu ("YHWH yeye ndiye atakayewaokoa," kama vile Mt. 1:21).

**26:29 "Sitakunywa . . . hata . . . ufalme wa Baba yangu"** Hii ilikuwa rejea ya karamu ya mwisho ya ki-Masihi (kama vile Mt. 8:11; Luka 13:28-30; si Mal. 1:11). Mara nyingi kifungu hiki kilikuwa kikihusianishwa na Sikukuu ya Harusi ya Yesu na Kanisa (kama vile Efe. 5:23-29; Ufu. 19:7). Tazama [MADA MAALUM: UFALME WA MUNGU](#) katika Mt. 4:17.

## **MADA MAALUM: MTAZAMO WA KIBIBLIA KUHUSIANA NA KILEVI NA MATUMIZI MABAYA YA KILEVI**

### I. Maneno ya Kibiblia

#### A. Agano la Kale

1. *Yayin* – Hili ni neno la jumla la divai (BDB 406, KB 409), ambalo limetumika mara 141. Asili ya neno hili si yumkini kwa sababu haitokani na mzizi wa Kiebrania. Hii mara nyingi inamaanisha juisi ya matunda iliyochacha, mara nyingi tunda aina ya balungi. Baadhi ya vifungu bainishi ni Mwa. 9:21; Kut. 29:40; Hes. 15:5,10.
2. *Tirosh* – Hii ni "divai mpya" (BDB 440, KB 1727). Kwa sababu ya tabia ya nchi ya Mashariki ya Karibu, uchachu unianza ndani ya masaa sita baada ya kutengeneza juisi. Neno hili hurejerea juu ya divai katika hatua ya kuchachusha. Kwa vifungu vibainishi tazama Kut. 12:17; 18:4; Isa. 62:8-9; Hos. 4:11.
3. *Asis* – Kwa uhalisia hiki ni kinywaji aina ya kileo ("divai mpya," BDB 779, KB 860, m.f. Yoeli 1:5; Isa. 49:26).
4. *Sekar* – Hili ni neno "kinywaji kikali" (BDB 1016, KB 1500). Mziziz wa Kiebrania unatumika ndani ya neno "kulewa" au "mlevi." Mara nyingi huu unaongezwa katika ndani yake ili kukifanya kileweshe zaidi. Hiki ni sawa na *yayin* (kama vile Mit. 20:1; 31:6; Isa. 28:7).

#### B. Agano Jipya

1. Oinos – neno lililo sawa kimaana na *yayin*
2. Neos oinos (divai mpya) – neno linalofanana la Kiyunani sawa na *tirosh* (kama vile Marko 2:22).
3. Gleuchos vinos (divai mpya, *asis*) – ni ile divai inayotengenezwa katika hatua za mwanzo kabla

ya kuchachushwa (kama vile Matendo ya Mitume 2:13).

## II. Matumizi ya Kibiblia

### A. Agano la Kale

1. Mvinyo ni zawadi ya Mungu (Mwa. 27:28; Zab 104:14-15; Mhu. 9:7; Hos. 2:8-9; Yoeli 2:19,24; Amosi 9:13; Zek. 10:7).
2. Divai ni swehemu ya sadaka ya kuteketeza (Kut. 29:40; Law. 23:13; Hes. 15:7,10; 28:14; Kumb. 14:26; Amu. 9:13).
3. Divai inatumika kama tiba (2 Sam. 16:2; Mit. 31:6-7).
4. Divai inaweza kuwa chanzo cha tatizo (Nuhu –Mwa. 9:21; Lutu – Mwa. 19:33,35; Samsoni – Waamuzi 16; Nabali – 1 Sam. 25:36; Uria– 2 Sam. 11:13; Amnoni– 2 Sam. 13:28; Ela– 1 Fal. 16:9; Ben-hadad i– 1 Fal. 20:12; Watawala – Amosi 6:6; na Wanawake – Amosi 4).
5. Divai inaweza kutumika vibaya (Mit. 20:1; 23:29-35; 31:4-5; Isa. 5:11,22; 19:14; 28:7-8; Hosea 4:11).
6. Divai ilizuiliwa kwa makundi fulani (makuhani waliokuwa katika zamu, Law. 10:9; Eze. 44:21; Wanazareti, Hesabu 6; na watawala, Mit. 31:4-5; Isa. 56:11-12; Hosea 7:5).
7. Divai ilitumika katika mpangilio wa matukio ya siku za mwisho (Amosi 9:13; Yoeli 3:18; Zek. 9:17).
  1. Kipindi cha uwazi kati ya Agano laKale na Agano Jipya
  2. Divai katika upatanisho ina msaada (Ecclesiasticus 31:27-33).
  3. Walimu wa Sheria za Kiyahudi wanasema, "Divai kuu kuliko tiba zote, mahali palipo na uhaba wa divai, madawa yalevyayo yanahitajika." (BB 58b).

### C. Agano Jipya

1. Yesu alikibadili kiwango kikubwa cha maji katika divai (Yohana 2:1-11).
2. Yesu alikunywa divai (Mt. 11:18-19; Luka 7:33-34; 22:17 na kuendelea)
3. Petro alidhihakiwa kwa ulevi "mvinyo mpya" siku ya Pentekoste (Mdo. 2:13).
4. Divai inaweza kutumika kama matibabu (Marko 15:23; Luka 10:34; 1 Tim. 5:23).
5. Watawala hawatakiwi kuwa watumiaji wabaya. Hii haimaanishi kujinyima molja kwa moja (1 Tim. 3:3,8; Tito 1:7; 2:3; 1 Pet. 4:3).
6. Divai ilitumika katika kupangili matukio ya siku za mwisho (Mathayo 22:1na kuendelea; Ufu. 19:9).
7. Divai ililaaniwa (Mt. 24:49; Luka 12:45; 21:34; 1 Kor. 5:11-13; 6:10; Gal. 5:21; 1 Pet. 4:3; Rum. 13:13-14).

## III. Utambuzi wa ndani wa Kithiolojia

### A. Mkazo wa Kiupembuzi

1. Divai ni zawadi kutoka kwa Mungu.
2. Ulevi ni tatizo kubwa.
3. Waamini katika baadhi ta tamaduni yawapasa kuweka uhuru wa mipaka yao kwa ajili ya injili (Mt. 15:1-20; Marko 7:1- 23; 1 Wakorintho 8-10; Warumi 14).

### B. Mwelekeo wa kwenda nje ya mipaka

1. Mungu ndiye mwanzilishi wa mambo yote.
  - a. chakula– Marko 7:19; Luka 11:44; 1 Kor. 10:25-26
  - b. mambo yote yasiyo najisi – Rum. 14:14,20; 1 Tim. 4:4
  - c. mambo yote ya halali – 1 Kor. 6:12; 10:23
  - d. mambo yote yaliyo safi– Tito 1:15
2. Mwanadamu aliyeanguka ametumia vibaya zawadi ya Mungu kwa kuzitumia nje ya mipaka ya Mungu aliyoitoa.

### C. Matumizi mabaya yako ndani yetu, si ndani ya vitu. Hakuna kilicho kiovu ndani ya uuumbaji wa vitu

vinanyoonekana (tazama B. 1. Hapo juu).

- IV. Utamaduni wa Karne ya kwanza ya Kiyahudi na Chachu
- A. Chachu hunza ndani ya muda mfupi, takribani ndani ya masaa 6 baada ya barungi kusagwa
  - B. Desturi ya Kiyahudi inasema kwamba povu linapoonekana juu yake (dalili ya uchachu), hii huelekea kuwa sehemu ya divai iliyo na uchachu (Ma aseroth 1:7). Hii iliitwa "divai mpya" au "divai tamu."
  - C. Chachu ya kwanza iliyo kali uilikamilishwa baada ya juma moja.
  - D. Chachu ya pili ilichukuwa sku zipatazo 40 . Katika hatua hii tendo hili lilifikiriwa kama "divai kukuu" na ingweza kutolewa madhabahuni (Edhuyoth 6:1).
  - E. Divai ambayo iliyobakizwa ndani ya machicha (divai kongwe) ilifikiriwa kuwa nzuri, lakini ilitakiwa kuchujwa vizuri kabla ya kutumiwa.
  - F. Divai ilifikiriwa kuwa kuukuu kwa usahihi baada ya kutunzwa vema kwa ajili ya kuchachushwa. Miaka mitatu kilikuwa kipindi cha muda mrefu ambapo divai ingetunzwa kwa usalama. Hii iliitwa "divai kukuu" na ilitakiwa kuchanganywa na maji.
  - G. Ni katika miaka 100 ya mwisho pekee ya ukame wa mazingira na ongezeko la madawa uchachu umetoweka. Ulimwengu wa kale usingeweza kustisha tendo la asili la kuchachusha.
- V. Maelezo ya Kiufungaji
- A. Hakikisha uzoefu wako, thiolojia, na fasiri ya kibiblia havimkashifu Yesu na ile karne ya kwanza ya Kiyahudi/Utamaduni wa ki- Kristo! Hawa kwa uwazi hawakujinyima moja kwa moja.
  - B. Mimi sitetei matumizi haya ya kilevi kwa jamii. Hata hivyo, wengi huchochea nafasi ya Biblia juu ya somo hili na sasa wanadai keki kuu iliyojikita katika utamaduni/ubaguzi wa kimadhehebu.
  - C. Kwangu mimi, Warumi 14 na 1 Wakorintho 8-10 zimetoa utambuzi na mwongozo uliojikita katika upendo na heshima kwa waamini wenetu na kuieneza injili ndani ya utamaduni wetu, si uhuru binafsi au ukosoaji wa hukumu. Ikiwa Biblia ni chanzo pekee cha imani na matendo, bila shaka yatupasa wote kufikiria upya juu ya jambo hili.
  - D. Ikiwa tunahimiza kujinyima moja kwa moja kama mapenzi ya Mungu, nini tunachokimaanisha juu ya Yesu, pamoja na zile tamaduni za sasa ambazo kwa hali ya mazoea hutumia divai (m.f. Ulaya, Israeli, Argentina).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 26:30**

<sup>30</sup> Nao walipokwisha kuimba, wakatoka nje kwenda mlima wa Mizeituni.

**26:30 "walipokwisha kuimba"** Wimbo huu huenda ulikuwa mmoja aua zaidi ya Zaburi za Hallel 113-118, au 146-150, katika namna ya jadi wimbo huu ulitumika katika sherehe za kukaribia kwa Pasaka au ingekuwa Hallel Kuu (kama vile Zaburi 136).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 26: 31-35**

<sup>31</sup> Ndipo Yesu akawaambia, Ninyi nyote mtachukizwa kwa ajili yangu usiku huu kwa kuwa imeandikwa, Nitampiga mchungaji, na kondoo wa kundi watatawanyika. <sup>32</sup> Lakini baada ya kufufuka kwangu, nitawatangulia kwenda Galilaya. <sup>33</sup> Petro akajibu, akamwambia, Wajapochukizwa wote kwa ajili yako, mimi sitachukizwa kamwe. <sup>34</sup> Yesu akamwambia, Amin, nakuambia wewe, usiku huu kabla ya kuwika jogoo, utanikana mara tatu. <sup>35</sup> Petro akamwambia, Ijaponipasa kufa nawe, sitakukana kamwe. Na wanafunzi wote wakasema vivyo hivyo.

**26:31 "Ninyi nyote mtachukizwa"** Kipengele hiki kinaeleza dhahiri kwamba wanafunzi wa Yesu watamwacha katika saa ya kuhitaji kwake (kama vile Mt. 26:56.) Ni Yohana pekee aliyebaki naye Petro alikuwa akimfuata kwa mbali. Weliobaki walikimbia!

☑ **"kwa kuwa imeandikwa"** Hii ni nukuu toka Zek. 13:7. Inatia shauku kwamba sura nane za kwanza za Zekaria zinanukuliwa toka katika kitabu cha Ufunuo wa Yohana, ambapo sita za mwisho zinanukuliwa mara kwa mara katika Injili. Ni YHWH ampigaye Mchungaji (kama vile Isa. 53:6,10; Rum. 8:32). Huu ulikuwa mpango wa Mungu wa mara kwa mara wa ukombozi (kama vile Matendo ya Mitume 2:23; 3:18; 4:28; 13:29). Tazama [MADA MAALUM: MPANGO WA YHWH WA UKOMBOZI WA MILELE](#) katika Mt. 24:14.

☑ **"kondoo"** Neno Kondoo lilikuja kuwa stiari ya mnyama iliyotumika kumaanisha wafuasi wa Kristo.

1. Mt. 7:15 (kondoo wa uongo)
2. Mt. 9:36; 26:3; Marko 14:27 (kundi lililotawanyika)
3. Mt. 10:6; 15:24 (kondoo wa Israeli waliopotea)
4. Mt. 10:16; Luka 10:3 (kondoo kati ya mbwa-mwitu)
5. Mt. 18:12; Luka 15:6 (mithali)
6. Mt. 25:32-33 (abaguavyo kondoo na mbuzi)
7. Marko 6:34 (kondoo wasio na wachungaji)
8. Yohana 10:1-18 (Yesu kama Mungu Mchungaji)
9. Yohana 21:16-17 (Petro, lisha kondoo na mbuzi wangu)
10. Pet. 2:25 (Isa. 53:6, kondoo tumepotea)

**26:32 "baada ya kufufuka kwangu"** Tazama Mada Maalum katika Mt. 27:63.

☑ **"nitawatangulia kwenda Galilaya"** Huku kukutana kwa baada ya ufufuo kunatajwa mara kadhaa (kama vile Mt. 26:32; 28:7,10,16-20; 1 Kor. 15:6; na Yohana 21). Huu lazima uwe utiwaji moyo mkuu kwa wanafunzi, lakini hawakuelewa.

**26:33 "Wajapochukizwa wote"** Dhahanio la awali la Petro linaonekana dhahiri. Hili linafanana sana na Mt. 16:22-23, ambapo Petro anaukana utabiri wa Bwana.

**26:34 "Amin, nakuambia wewe"** Kiuhalisia hili ni neno *"amen,"* ambalo kiuhalisia lilimaanisha "kukubalika" lakini baadauye lilikuja kumaanisha "na iwe hivyo" au "nakiri." Yesu alilitumia neno hili kwa upekee pale alipotaka kuisisitiza usemi muhimu. Tazama Mada Maalum katika Mt. 5:1.

☑ **"kuwika jogoo"** Hili lilitukia kati ya 6:00 usiku na 9:00 usiku. Lazima hili liwe jogoo la Kirumi kwa sababu Wayahudi hawakuwaruhusu kuwika katika mji mtakatifu. Kumekuwa na madhahanio mengine kwamba kulikuwa na ishara ya baragumu la Kirumi iliyoitwa "Kuwika kwa Jogoo," ambayo ilipigwa mwishoni mwa saa 3 usiku. Hata hivyo, hili bado halijulikani vema.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini viongozi wa kidini walitaka kumuua Yesu?
2. Vipi kuhusu mfuatano wa matatizo miongoni mwa Injili nne? Je, ni kosa lililo katika biblia?
3. Je! Yuda anawajibika kwa ajili ya matendo yake? Je! Nini alilichokifanya? Kwa nini alifanya hivyo?
4. Nini umuhimu wa Karamu ya Bwana?
5. Je! Yuda alishiriki Karamu ya Bwana?
6. Kwa nini utabiri wa ukanaji wa imani wa wanafunzi uliandikwa?



## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO LA 26:36-75

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 26:36-38

<sup>36</sup> Kisha Yesu akaenda pamoja nao mpaka bustani itwayo Gethsemane, akawaambia wanafunzi wake, Ketini hapa, hata niende kule nikaombe. <sup>37</sup> Akamchukua Petro na wale wana wawili wa Zebedayo, akaanza kuhuzunika na kusononeka. <sup>38</sup> Ndipo akawaambia, Roho yangu ina huzuni nyingi kiasi cha kufa; kaeni hapa, mkeshe pamoja nami.

**26:36 "Kisha Yesu akaenda pamoja nao mpaka bustani itwayo Gethsemane"** Jina "Gethsemane" katika Kiebrania lilimaanisha "eneo la mafuta". Kwa hali iliyo dhahiri hii ilikuwa bustani binafsi iliyokuwa nje ya mji mpakani mwa Yerusalemu juu ya Mlima wa Mizeituni. Ilikuwa haramu kuwa na bustani ndani ya mji kwa sababu mbolea iliyohitajika kwa ajili ya mimea ilikuwa ikiunajisi mji. Kwa namna iliyo dhahiri Yesu aliingia katika bustani hii mara nyingi. Pia inawezekana kwamba wakati wa Juma la Mateso aliweka kambi hapa pamoja na wanafunzi wake. Yuda alilifhamu vema eneo hili.

**26:37 "Akamchukua Petro na wale wana wawili wa Zebedayo"** Kutokana na Marko 14:33 na Yohana 4:21 tunafahamu kuwa wale wengine wawili walikuwa Yakobo na Yohana. Huu ulikuwa mzunguko wa ndani kabisa wa uhusiano kati ya wanafunzi (kama vile Mt. 17:1; Marko 5:37). Hawa walikuwa pamoja na Yesu katika matokeo kadhaa muhimu wakati pindi wanafunzi wengine walipokuwa hawapo. Kwa uwazi hili lilipelekea kuwa na mafunzo maalum au wivu ndani ya mioyo ya wanafunzi wengine. Sababu halisi ya Yesu kuwa na mzunguko wa ndani kabisa haijulikani. Orodha ya Wale Kumi na Wawili mara nyingi iko katika makundi manne ya watu watatu watatu. Makundi haya kamwe hayakuwai kubadilika. Inawezekana kwamba makundi haya yaliweka utarabu kwa ajili ya wanafunzi kwenda majumbani kwao kwa muda na kuzitazama nyumba zao.

☐ **"akaanza kuhuzunika na kusononeka"** Haya yalikuwa maneno yenye nguvu katika Kiyunani (kama vile Marko 14:33). Tuko katika eneo takatifu sana hapa katika bustani kama tunavyomuona Mwana wa Mungu kama tulivyokwisha kuona hivi punde. Lazima Yesu angeyahusianisha maelezo haya na wanafunzi wake baada ya ufufuo wake. Kwa hali iliyo dhahiri hili lilimaanisha kuwa msaada kwa wale wanaokumbana na majaribu na wale wanaotafuta kuyaelewa mateso na gharama ya tukio la Kalvari.

**26:38 "Roho yangu ina huzuni nyingi kiasi cha kufa"** Hii ilikuwa nahau ya Agano la Kale (kama vile Zab. 42:5; Yonaha 6:9), yenye kueleza nguvu za maajabu iliyohusishwa katika ukombozi wa mwanadamu mwenye dhambi. Jambo la mapambano linaweza kuonekana katika ufanano wa Luka 22:43-44, ambayo inanukuu kwamba malaika walikuja kumtumikia na kudondosha matone makubwa ya damu. Ushindi dhidi ya yule mwovu ulipatikana hapa ndani ya bustani. Madhara ya majaribu ya shetani yaliyojificha yaliyo katika Mt. 4 na ya kwa namna fulani yalisaidia, bali maangamizi yaliyopita kiasi, maoni yaliyo katika Mt. 16:22, yanafunuliwa kwa ukamilifu katika kifungu hiki .

### ANDIKO LA NASB(LILIBORESHWA) MATHAYO 26:39-41

<sup>39</sup> Akaendelea mbele kidogo, akaanguka kifulifuli, akaomba, akisema, Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke; walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe. <sup>40</sup> Akawajia wale wanafunzi, akawakuta wamelala, akamwambia Petro, Je! Hamkuweza kukesha pamoja nami hata saa moja? <sup>41</sup> Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni; roho i radhi, lakini mwili ni dhaifu.

**26:39 "Akaendelea mbele kidogo, akaanguka kifulifuli, akaomba"** Picha nzuri kabisa ya Yesu akiwa amepiga magoti ndani ya bustani ya kwa mshtuko inanijia, lakini si sahihi. Andiko la Kiyunani hapa linadaia kwamba alikuwa dhaifu sana katika mfadhaiko na mateso, hata kiasi cha kufa, katika nyakati hizi. Mara nyingi limekuwa likiulizwa swali kwamba kitu gani kilichomtia hofu sana Yesu. Wengine wamekuwa wakidhani kwamba huu ulikuwa hofu ya kifo cha kimwili, au alihofu kwamba wanafunzi wasingeliongoza Kanisa. Yesu, aliyejulikana kwa Baba kwa ukaribu sana na kwa kila wakati, alikuwa katika hatua ya mwisho ya kuona namna mwanadamu anavyozidi kuupoteza

ushirika wake na Mungu. Ni katika udhaifu huu wa ushirika na kuubeba mzigo wa dhambi kwa ajili ya watu wote wa nyakati zote ambazo zilimwogopesha Mwana. Kama tunaweza kuona aina hii ya mateso ya ndani kwa upande wa Yesu Mnazareti, mwana wa pekee wa Mungu, ni mshangao na maangamizi ya namna gani yapasayo kututenga na ushirika na Mungu yatakavyokuwa!

■ **"ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke"** Kuna vipengele kadhaa muhimu sana kupita kiasi katika kifungu hiki. Kutokana na ufanano wa Marko tunaewa kwamba alitumia neno la Kiaramu "*Abba*," lililorejelea ukaribu, uhusiano wa kifamilia. Mara nyingi hili linatafsiriwa kama "Baba." Katika masaa machache hili litabadilika na kuwa "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" (kama vile Mt. 27:46). Hiki kifungu "ikiwezekana" (sentensi amrishi daraja la kwanza) kinapatikana katika ufanano wa Marko (kama vile Marko 14:36) katika kifungu "mambo yote yanawezekana." Tofauti ndogo kati ya Mt. 26:35 na 42 na tofauti kati ya Injili na Injili haipunguzi ukweli kwamba, kutokana na Mt. 26:44, tunatambua kwamba Yesu aliomba maombi yale yale mara tatu.

Hii dhana ya "kikombe" katika matumizi ya kibiblia inaakisi ishara ya Agano la Kale ya hatima ya mtu, mara nyingi katika maana ya hukumu ya Mungu (kama vile Zab. 75:8; Isa. 51:17,22; Yer. 25:15,16,27,28). Kikombe cha hukumu kilicholandaliwa na Mungu kwa ajili ya uasi wa mwandamu kilikamilishwa kwa kukokotwa na Mwana wa Mungu asiye na hatia (kama vile 2 Kor. 5:21; Gal. 3:13).

■ **"walakini si kama nitakavyo mimi"** Hiki kiwakilishi "mimi" na "wewe" ki katika hali ya msistizo katika Kiyunani. Hili, lenye kuunganishwa na matumizi ya sentensi amrishi daraja la kwanza na la Tatu zilizo katika Mt. 26:42, linatuonyesha kusudio la Mwana katika maombi yake. Ingawa kwa asili yake ya kibinadamu alilia kwa ajili kuomba msaada, Moyo wake unaendelea kuyatimiza mapenzi ya Baba katika upatanisho mbadala (kama vile Marko 10:45).

**26:40 "Akawajia wale wanafunzi, akawakuta wamelala"** Kabla hatujawashtumu wanafunzi kwa haraka, hebu tuliangalie hili katika Luka 22:45 kifungu, "wamelala usingizi kwa huzuni." kinaeleza kwamba hawakuwa na uwezo wa kuihimili huzuni ya unabii wa Yesu uliohusu kifo chake mwenyewe na utengano wa baadaye. Ingawa Yesu alitumia muda mrefu katika kuwa na ushirika wa mwanadamu na sala kwa wakati huu wa magumu katika maisha yake, Ilimpasa kukabiriana na kipindi hiki yeye mwenyewe, na alikabiriana na hili kwa waamini wote!

**26:41 "Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni"** Hizi zote ni ni kauli shurutishi za wakati uliopo. Lazima kuwepo kukesha kuliko thabiti! Majaribu ni kweli endelevu (kama vile Mt. 4:11; Luka 4:13; Warumi 7). Kume kuwa na nadharia kadhaa ambapo neno "majaribu" linarejelea katika muktadha huu

1. kwa wanafunzi kulala badala ya kuomba
2. kwa wanafunzi kumwacha Yesu katika Mt. 26:56
3. kwa ukanaji wa Petro katika Mt. 26:69-75
4. kwa majaribu ya kiutawala au ya kidini (kama vile Mt. 5:10-12; Yohana 9:22; 16:2)

Hili neno "majaribu" (*peirasmos*) lilikuwa na maana nyingine ya "ili ajaribiwe na Ibilisi" (tazama Mada Maalum katika Mt. 4:1, kama vile Mt. 6:13; Luka 11:4; Yakobo 1:13). Mara nyingi kifungu hiki kinatofautishwa na neno lingine la Kiyunani la kupima (*dokimazo*) lenye maana nyinginezo za "kujaribu au kupima kwa ajili ya kuhimarisha." Hata hivyo, maana hizi mara nyingi hazimo katika kila muktadha. Kithiolojia inaweza kusemwa kwamba Mungu hawajaribu watoto wake kwa ajili ya kuwaangamiza bali hutoa nafasi kwa ajili ya ukuaji wa kiroho kupitia majaribu (kama Mwa. 22:1; Kut. 16:4; 20:20; Kumb. 8:2,16; Mt. 4; Luka 4; Ebr. 5:8). Harta hivyo, Yeye hutoa njia (kama vile 1 Kor. 10:13).

■ **"roho i radhi, lakini mwili ni dhaifu"** Huu ulikuwa ukiri binafsi wa Yesu aliyejua vema ubinadamu wetu na udhaifu wetu (kama vile Ebr. 4:15). Na, kutujua, alitupenda na kutufia (kama vile Rum. 5:8) na kuomba kwa ajili yetu (kama vile Rum. 8:34; Ebr. 7:25; 9:24; 1 Yohana 2:1). Halleluya!

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 26:42-46**

<sup>42</sup> Akaenda tena mara ya pili, akaomba, akisema, Baba yangu, ikiwa haiwezekani kikombe hiki kiniepuke

nisipokunywa, mapenzi yako yatimizwe. <sup>43</sup> Akaja tena, akawakuta wamelala; maana macho yao yamekuwa mazito. <sup>44</sup> Akawaacha tena, akaenda, akaomba mara ya tatu, akisema maneno yale yale. <sup>45</sup> Kisha akawajia wanafunzi wake, akawaambia, Lalen sasa, mpumzike tazama, saa imekaribia, na Mwana wa Adamu anatiwa katika mikono ya wenye dhambi. <sup>46</sup> Ondokeni, twende zetuni! Tazama, yule anayenisaliti amekaribia.

**26:42 "ikiwa haiwezekani kikombe hiki kiniepuke nisipokunywa"** Huu ni muungano wa sentensi amrishi daraja la kwanza na na daraja la tatu. Huu unadokeza kwamba Yesu Alifahamu kuwa yalikuwa mapenzi ya Mungu yeye kuangikwa msalabani, akini alikuwa akionyesha kujali kwake kwa Baba. Ni vema kufahamu kwamba Mungu hatutukataa kwa ajili ya hofu zetu na maangaiko yetu, bali atetenda nasi katika upendo na imani kama alivyotenda pamoja na Yesu. Hatuwezi kujiombea nje ya mapenzi ya Mungu.

**26:44 "akaomba mara ya tatu, akisema maneno yale yale"** Yesu aliomba mara tatu. Jambo hili li sawa na kuomba kwa Paulo mara tatu kuhusu mwiba huu uliokuwa ndani ya mwili wake (2 Kor. 12:8). Kuna jambo fulani la nahau ya Kiebrania ya msistizo katika marudio matatu yaloyofungamanishwa (kama vile Isa. 6:3; Yer. 7:4). Tunaweza kumtwika Mungu fadhaa zetu kwa wakati wa wote, kama tupatapo mahitaji yetu mara kwa mara

**26:45**

**NASB, NKJV**

**TEV** "bado mmelala na kupumzika?"

**NRSV** "bado mmelala na kupumzika?"

**NJB** "mwaweza kulala sasa na kupumzika."

Ni vigumu kuifasiri nahau hii ya Kiyahudi. Je! Hili ni swali? Ni kebehi? Ni usemi? Ni amri? Ijapokuwa maana yake haijulikani, ni dhahiri kwamba Yesu ameshinda na sasa anasimama wima, tayari kwa kukabiriana na mashtaka ya usiku, mapigo ya asubuhi na usulibishwaji.

☐ **"saa imekaribia"** Neno "Saa" ilikuwa nahau muhimu iliyotumika katika Injili zote, hasa ya Yohana (kama vile Mt. 12:23;13:1,32; 17:1), kwa ajili ya kueleza wasaa huu (kama vile Marko 14:35,41). Tazama [MADA MAALUM: SAA](#) katika Mt. 24:36.

☐ **"anatiwa katika mikono ya wenye dhambi"** Huu ni unabii uliotimizwa wa Mt. 16:21.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 26:47-50**

<sup>47</sup> Basi alipokuwa katika kusema, tazama, Yuda, mmoja wa wale Thenashara akaja, na pamoja naye kundi kubwa wenye panga na marungu, wametoka kwa wakuu wa makuhani na wazee wa watu. <sup>48</sup> Na yule mwenye kumsaliti alikuwa amewapa ishara, akisema, Nitakayembusu, huyo ndiye; mkamateni. <sup>49</sup> Mara akamwendea Yesu, akasema, Salamu, Rabi, akambusu. <sup>50</sup> Yesu akamwambia, Rafiki, fanya ulilolijia. Wakaenda, wakanyosha mikono yao wakamkamata Yesu.

**26:47 "Yuda, mmoja wa wale Thenashara akaja, na pamoja naye kundi kubwa wenye panga na marungu"** Kumekuwa na mjadala mkubwa kuhusu nia ya Yuda. Lazima isemekane kwamba hili linabaki vilevile bila kujulikana. Kumbusu Yesu katika Mt. 26:49 kwa vyo vyote (1) ilikuwa ishara kwa askali kwamba huyu ndiye mtu wa kukamata (kama vile Mt. 26:48) au (2) waliazima nguvu za nadhari ya sasa kwamba alikuwa akijaribu kuulazimisha mkono wa Yesu kutenda, (kama vile Mt. 27:4). Vifungu vingine vyua Injili vinaeleza kwamba alikuwa mnyang'anyi na asiyeamini toka mwanzo (kama vile Yohana 12:6).

Kutoka Luka 22:52 tunajua kazi ya umati huu. Kulikuwa na askari wa Kirumi waliojumuishwa kwa sababu wao ndiyo pekee ambao kisheria walikuwa na uwezo wa kubeba panga. Pia, askari wa Hekalu walijumuishwa kwa sababu mara nyingi walikuwa wakibeba marungu. Wawakilishi toka baraza la wazee wa Sinagogi kuu pia walikuwepo katika ukamataji (kama vile Mt. 26:47, 51).

**26:48 "akambusu"** Hii ilikuwa ishara ya heshima na salamu miongoni mwa walimu wa sheria za Kiyahudi. Katika Mt. 26:49 Yuda alimwita Yesu "Rabi" (" mwalimu wangu").

**26:50**

**NASB "Rafiki, fanya ulilolijia"**

**NKJV "Rafiki, kwa umeijia nini"**

**NRSV "Rafiki, fanya lililokuleta kufanya"**

**TEV "Harakisha, rafiki"**

**NJB "Rafiki, fanya lililokuleta kufanya"**

Kumekuwa na baadhi ya kutokukubaliana juu ya nahau hii ya Kiyunani. Hii inaweza kuwa

1. swali (NKJV)
2. shutuma (TEV)
3. nahau ya "fanya ulilolijia" (NASB, NRSV, JB)

Toleo la American Standard na tafsiri ya Williams inakiri kwamba huu ni usemi wa kebehi au maelezo mafupi ya makusudi. Hata hivyo, toleo la King James na Revised Standard linaliona hili kama swali, pia kama nahau iliyojificha. Matumizi ya neno "rafiki" yanaweza kuwa juhudi za kumkumbusha Yuda juu ya mazungumzo yao yaliyofanyika Ghorofani (kama vile Mt. 26:23) au nahau ya kebehi (kama vile Mt. 20:13; 22:12).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 26:51-54**

<sup>51</sup> Na tazama, mmoja wao waliokuwa pamoja na Yesu akanyosha mkono wake, akaufuta upanga wake, akampiga mtumwa wa Kuhani Mkuu, akamkata sikio. <sup>52</sup> Ndipo Yesu akamwambia, Rudisha upanga wako mahali pake, maana wote waushikao upanga, wataangamia kwa upanga. <sup>53</sup> Ama wadhani ya kuwa mimi siwezi kumsihi Baba yangu, naye ataniletea sasa hivi zaidi ya majeshi kumi na mawili ya malaika? <sup>54</sup> Yatatimizwaje basi maandiko, ya kwamba hivyo ndivyo vilivyopasa kujiri?

**26:51** Kutokana na ufanano ulio katika Yohana 18:10 na Luka 22:50-51, tunajua kwamba huyu alikuwa Petro na mtumwa wa Malkusi. Hapo awali wanafunzi walikuwa wamekwisha pewa angalizo juu ya kununua panga (kama vile Luka 22:36-38), lakini kwa uwazi kabisa, hawakuielewa maana kamili ya Yesu kuhusu jambo hili. Lazima isemekane kwa niaba ya Petro kwamba alikuwa tayari kufa kwa ajili ya Bwana kwa wakati huu. Katika sura ya nafasi kubwa, aliuchukua upanga mmoja panga mbili. Lakini, kwa mara nyingine, kutokuwa sahihi kwake na haraka za matendo yake kulionyesha utu wake.

**26:52 "wote waushikao upanga, wataangamia kwa upanga"** Hii ilikuwa mithali ya kitamaduni (kama vile Ufu. 13:10). Hii haikumaanisha kuchukuliwa kama kweli halisi katika kila mfano binafsi, bali kweli bainishi katika hiyo. Hii pia ni kama kitabu cha Mithali za kibiblia. Hii inaweza kuhusiana na ukweli kwamba Yesu alikamatwa kama mharifu wa kawaida. Wanafunzi wake pia wanaonekana kama wanyang'anyi na waporaji, wenye kubeba panga! Tazama Mada Maalum: *Apollumi* katika Mt. 2:13.

**26:53** Yesu alijitambua yeye ni nani (kama vile Yohana 13:1). Aliijua asili ya Babaye, lakini aliazimia kufa (kama vile Yohana 10:17-18)!

🔍 **"zaidi ya majeshi kumi na mawili ya malaika"** Kikosi cha Kirumi kilikuwa na wanaume askari 6,000, lakini neno lilikuwa nahau ya maelfu kadhaa.

Tazama [MADA MAALUM: HESABU YA KUMI NA MBILI](#) katika Mt. 14:20.

**26:54, 56 "basi maandiko"** Ikiwa kifungu hiki kilicho katika Mt. 26:54 kinahusiana na vifungu vingine vilivyokuwa katika Mt. 26:56, huu ni usemi wa moja kwa moja kwamba kila kitu kimetokea kulingana na mpango wa awali wa kiungu ulioamriwa kabla (kama vile Luka 22:22; Matendo 2:23; 3:18; 4:28). Tunajua kwamba Yohana aliambatana na Yesu kupitia mashtaka na kwamba Petro alikuwa akimfuata kwa mbali (kama vile Mt. 26:58). Kwa hiyo, hii ni

rejea ya jumla yenye kuigeukia Isa. 53:6. Yesu alifahamu kwamba matukio yalikuwa yakiendelea kufanyika kama ilivyopaswa ili kulitimiza kusudi la Baba.

Inawezekana kwamba hili linayarejelea mateso aliyowatabiria wanafunzi wake mara kadhaa (kwanza katika Mt.16:21-28), kukiwemo kuteswa, Masihi aliyekataliwa (yaani, Mwa. 3:15; Zab 22; Isaya 53; Zek. 9; 12).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 26:55-56**

<sup>55</sup> Saa ile Yesu akawaambia makutano, Je, mmetoka kama kumkamata mnyang'anyi, wenye panga na marungu, ili kunishika? Kila siku naliketi hekaluni nikifundisha, msinikamate. <sup>56</sup> Lakini haya yote yamekuwa, ili maandiko ya manabii yatimizwe. Ndipo wanafunzi wote wakamwacha, wakakimbia

**26:55** Yesu analeta mwanga dhahiri wa mbinu za viongozi wa kidini (kama vile Mt. 12:14; Yohana 11:53). Hawa walikuwa wakitafuta nafasi ya kumkamata kutokana na umati wa wanahija na wafuasi (kama vile Mt. 26:4; Luka 22:2).

**NASB, NKJV** "mnyang'anyi"

**NJB** "mwivi"

Neno hili linadokeza machafuko, mtu asiye wa sheria (kama vile Luka 10:30). Baadaye lilitumika katika Josephus mwasi, kama Baraba (kama vile Mt. 27:16-17).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 26:57-58**

<sup>57</sup> Nao waliomkamata Yesu wakampeleka kwa Kayafa, Kuhani Mkuu, walikokuwa wamekutanika waandishi na wazee. <sup>58</sup> Na Petro akamfuata kwa mbali mpaka behewa ya Kuhani Mkuu, akaingia ndani, akaketi pamoja na watumishi, auone mwisho.

**26:57** "Nao waliomkamata Yesu wakampeleka kwa Kayafa, Kuhani Mkuu" Kutokana na ufanano ulio katika Yohana 18:12, tunatambua kwamba kwanza alipelekwa kwa Anasi, aliyekuwa na mamlaka nje ya ofisi. Kwa uwazi kabisa Anasi na Kayafa walikuwa wakiishi katika nyumba moja. Watumishi wa baraza la wazee wa Sinagogi waliochaguliwa tayari walikuwa wamekwisha kuwasili hapa. Hiki kifungu, "waandishi na wazee," kandokando ya Kuhani Mkuu, kinaeleza jina kamili la Baraza la wazee wa Sinagogi kuu.

**MADA MAALUM: MASHTAKA MBELE YA WAKUU WA SINAGOGI (Mt. 26:57-68)**

- A. Hakuna hadhabu kunbwa zilizopaswa kutolewa wakati wa usiku.
- B. Mashtaka makubwa na adhabu hayakupaswa kuendeshwa kwa siku hiyo hiyo.
- C. Hakuna mashtaka yaliyopaswa kuendeshwa siku ya sikukuu au wakati wa mkasha.
- D. Asubuhi ya kipekee ilitunzwa kwa ajili ya kuwa ishara (kama vile Kut. 6:8; 11:18).
- E. Asubuhi hii pia ulikuwa wakati wa kugawa karama ndani ya Hekalu (kama vile Mt. 23:

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 26:59-64**

<sup>59</sup> Basi wakuu wa makuhani na baraza yote wakatafuta ushuhuda wa uongo juu ya Yesu, wapate kumwua; <sup>60</sup> wasiuone wangawa walitokea mashahidi wa uongo wengi. <sup>61</sup> Hata baadaye wawili wakatokea, wakasema, Huyu alisema, Naweza kulivunja hekalu la Mungu, na kulijenga kwa siku tatu. <sup>62</sup> Kisha Kuhani Mkuu akasimama akamwambia, Hujibu neno? Hawa wanakushuhudia nini? <sup>63</sup> Lakini, Yesu akanyamaza. Kuhani Mkuu akamwambia, Nakuapisha kwa Mungu aliye hai, utuambie kama wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu. <sup>64</sup> Yesu akamwambia, Wewe umesema; lakini nawaambieni, Tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija juu ya mawingu ya mbinguni.

**26:59 "wakatafuta ushuhuda wa uongo juu ya Yesu"** Kifungu kinaonekana kudokeza kwamba hawa walikuwa wakatafuta mashahidi ambao wangekubaliana na shitaka hili kwa sababu mifano ya sheria za Agano la Kale ilihitaji mashahidi wawaili ili kumshtaki mtu (kama vile Hes. 35:30; Kumb. 17:6; 19:15).

Baraza la Wakuu wa Sinagogi wasingetafuta shuhuda mbili za kuaminika dhidi ya Yesu (Mt. 26:60-61). Mwishowe walipata shuhuda mbili zinazofanana (kama vile Marko 14:59) zilizohusianishwa na usemi wa Yesu kuhusu kuliharibu hekalu (kama vile Yohana 2:19).

Kulikuwana mambo mengi yaliyo kinyume katika usiku huu wa mashtaka (tazama Mada Maalum katika Mt. 26:57). Viongozi wa Kiyahudi wangelifikiria hili kwa kumtoa kafara mtu huyu mmoja kinyume ili kuliokoa taifa dhidi ya kisasi cha Kirumi.

**26:61** Hili ni dokezo la usemi wa Yesu ulioandikwa katika Yohana 2:19, ingawa alikuwa akiutoa usemi huu mara kwa mara. Huyu alikuwa akirejelea maangamizi ya hekalu yajayo mnamo 70 b.k kwa yaliyofanywa na Tito na ufufuo mpya wa mwili wake (kama vile Mt. 16:21; 17:23; 20:19), ambao utakuwa tazamio jipya kwa watu wa YHWH kumwabudu. Mfumo wa utoaji dhabihu unaondolewa mara mmoja na kwa dhabihu zote za Kristo (kama vile Waebrania). Kiini cha tazamio la makubaliano na namna ya kuabudu kimebadilika! Yesu ndiye hekalu jipya (kama vile Yohana 2:19-21), kama walivyo wafuasi wake (kama vile 1 Kor. 3:16-17; 2 Kor. 6:19).

**26:63 "Lakini, Yesu akanyamaza"** Hili pia lilikuwa la kweli wakati wa mashtaka yake yaliyofuatia yaliyoandikwa katika Mt. 27:12, 14. Hili lilitimiza unabii wa Isa. 53:7.

☐ **"Kuhani Mkuu akamwambia, Nakuapisha kwa Mungu aliye hai, utuambie kama wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu"** Kujitolea kwa kula kiapo ilikuwa kinyume lakini ilisaidia, Yesu asingekuwa kimya katika kula kiapo katika jina la YHWH. Hili jina "YHWH," kutoka Kutoka 3:14, lilitokana na kitenzi cha Kiebrania "kuwa," chenye kumaanisha "Mungu wa milele, Mungu wa pekee aishiye" (kamavile Mt. 16:16). Hili lilikuwa jina la agano la Mungu wa Israeli. Viongozi hawa walitambua Yesu, hata kwa maneno yake na matendo yake, alipokuwa akieleza yeye kuwa Masihi aliyehaidiwa (tambua namna majina "Masihi" na "Mwana wa Mungu" yanavyohusiana). Hawa wanamwona kama mmoja wa Masihi wengi wa uongo kwa sababu hakujikita katika desturi za mapokeo na mamlaka yao.

**26:64**

**NASB "Wewe umesema"**

**NKJV "ni kama ulivyosema"**

**NRSV "umesema hivyo"**

**TEV "ndivyo ulivyo sema"**

**JB "haya maneno ni yako mwenyewe"**

**NJB "ni wewe uliyelisema hili"**

Hii nahau ya ukiri yenye kufanana inapatikana katika Mt. 26:25. Kwa kiasi fulani ilikuwa tata. Huenda Yesu alikuwa akisema, "Ndiyo, mimi ni Masihi, lakini si katika maana ya kufikiri kwako" (kama vile Marko 14:62).

☐ **"nawaambieni, Tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija juu ya mawingu ya mbinguni"** Hizi nahau za maandiko ya Kiebrania zinakukiri kujifahamu kwake. Kuwa na haki na nguvu (yaani, YHWH) lilikuwa dokezo la Zab. 110:1. Kuja juu ya mawinguni lilikuwa dokezo la Dan. 7:13 (kama vile Marko 13:26; Mt. 24:30; na Ufu. 1:7). Kwa vifungu hivi vya Agano la Kale, Yesu alikuwa akieleza kwa namna ya utata kuhusu Uungu wake na Umasihi wake. Yeye alifahamu kuwa hili lingepolekeleka kifo chake ni kama kufuru (yaani, kudai kuwa sawa na Mungu).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 26:65-66**

<sup>65</sup> Ndipo Kuhani Mkuu akararua mavazi yake, akisema, Amekufuru; mna haja gani tena ya mashahidi?

**Tazameni, sasa mmesikia hiyo kufuru yake; <sup>66</sup> mwaonaje ninyi? Wakajibu, wakasema, Imempasa kuuawa.**

**26:65 "Ndipo Kuhani Mkuu akararua mavazi yake"** Hii ilikuwa ishara ya roho ya kughadhabika kwa undani iliyosababishwa na kukufuru (kama vile Matendo ya Mitume 14:14). Adhabu ya kukufuru inayotokana na Law. 24:15 ilikuwa kifo. Yesu alijithamanisha kufa kwa misingi ya Kut. 13:1-3 na 18:22 kama asingekuwa Yule Ajaye, Masihi, Mwana wa Mungu, Mkombozi wa ulimwengu. Hapa hakuna mzunguko. Kwa vyo vyote yeye ndiye aliyedaiwa kuwa ama yeye ni mwenye kufuru aliyejithamanisha kufa (kama vile Josh McDowell's, *Evidence That Demands a Verdict*).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 26: 67-68**

**<sup>67</sup> Ndipo wakamtemea mate ya uso, wakampiga makonde; wengine wakampiga makofi, <sup>68</sup> wakisema, Ewe Kristo, tufumbulie; ni nani aliyekupiga?**

**26:67-68** Haijulikani kama matendo haya yalifanywa na mojawapo ya baraza la wazee wa Sinagoga lenyewe na wahudhuriaji wao. Marko 14:65 inasema wakaanza kumtemea mate, wakamfunika uso, na kumpiga makonde, na kumwambia, tabiri! Huu unaweza kuwa utimilifu wa Isa. 53:3.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 26:69-75**

**<sup>68</sup> wakisema, Ewe Kristo, tufumbulie; ni nani aliyekupiga? <sup>69</sup> Na Petro alikuwa ameketi nje behewani; kijakazi mmoja akamwendea, akasema, Wewe nawe ulikuwapo pamoja na Yesu wa Galilaya. <sup>70</sup> Akakana mbele ya wote, akisema, Sijui usemalo. <sup>71</sup> Naye alipotoka nje hata ukumbini, mwanamke mwingine alimwona, akawaambia watu waliokuwako huko, Huyu alikuwapo pamoja na Yesu Mnazareti. <sup>72</sup> Akakana tena kwa kiapo, Simjui mtu huyu. <sup>73</sup> Punde kidogo, wale waliohudhuria wakamwendea, wakamwambia Petro, Hakika wewe nawe u mmoja wao; kwa sababu hata usemi wako wakutambulisha. <sup>74</sup> Ndipo akaanza kulaani na kuapa akisema, Simjui mtu huyu. Na mara akawika jogoo. <sup>75</sup> Petro akalikumbuka lile neno la Yesu alilolisema, Kabla ya kuwika jogoo, utanikana mara tatu. Akatoka nje, akalia kwa majonzi.**

**26:69-73** Mririko kamili wa haya mastaka matatu unatofautiana Injili hadi Injili. Huu ukweli kwamba Petro alimkana Yesu mara tatu kwa msisizo uliofanikiwa ni wa kawaida kwa maelezo yote. Huu ukweli kwamba walitofautisha maelezo ya ushahidi wa macho, si ithibitisho wa kihistoria.

**26:71 "Yesu Mnazareti"** Tazama Mada Maalum katika Mt. 2:23.

**26:72 "Simjui mtu huyu"** Hii nahau ya Kiebrania ulikuwa usemi wa dharau iliyofichika.

**26:73 "hata usemi wako wakutambulisha"** Wale waliokuwa wakiishi Galilaya wangetambuliwa kwa tofauti zilizokuwa katika lafudhi na matamshi ya sauti za kooni za lugha ya Kiaramu.

**26:74 "Ndipo akaanza kulaani na kuapa akisema, Simjui mtu huyu"** Tena hii ni nahau yenye kuakisi dharau na huzuni katika kulitumia jina la Mungu katika kukiri uongo. Ikiwa mtu yo yote anajithamanisha kwa kiwango cha kupoteza, ni Petro, mbele ya upendo kama huo, msamaha, unabii na miujiza, alikana, mara tatu kwa ghadhabu na kiapo, Aliyedaiwa kukupenda. Ikiwa Petro anaweza kuokolewa, mtu yo yote anaweza kuokolewa! Tofauti pekee iliyopo kati ya Petro na Yuda ilikuwa kwamba Yuda hakumwongokea Yesu kwa imani.

■ **"Na mara akawika jogoo"** Lazima hili liwe jogoo la Kirumi kwa Wayahudi haikuruhusiwa kufuga kuku katika Yerusalemu kwa sababu hawa walisababisha eneo hili kutokuwa takatifu (tazama maelezo katika 26:34). Kutokana na Luka 22:61, tunajua kwamba Yesu alimtazama Petro. Hili linadokeza kwamba Anasi na Kayafa walikuwa wakiishi katika nyumba ile ile na kwamba Yesu angeuona uwanja wa hukumu au alikuwa akihamishiwa katika maeneo hayo mawili.

**26:75 "Akatoka nje, akalia kwa majonzi"** Petro alikuwa akikamilisha unabii katika kukana kwake na kutoa tumaini kwa waamini wote waliomkataa Yesu kwa ndimi zao, kwa maisha yao na kwa mali zao. Kuna tumaini kwa ye yote anayemgeukia yeye katika imani (kama vile Yohana 21).

## **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Yesu alikwenda mahali alipofahamu Yuda?
2. Ni kitu gani kilichomwogofya Yesu ndani ya bustani ambacho kilichomfanya ahisi kwamba anakwenda kufa?
3. Yesu anamuaomba Mungu afanye nini katika maombi ya maraya tatu?
4. Kwa nini Yuda aliuleta umati mkubwa kama ule kwa ajili ya kumkamata Yesu?
5. Kwa nini Yesu alijishtumu mwenyewe kwa usemi wake wa mara kwa mara katika mstari wa 64?
6. Kwa nini maelezo ya Injili yanatofautiana na mtiririko wa ukanaji wa Petro?



## MATHAYO 27

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Yesu analetwa mbele Ya Pilato 27:1-2 Kifo cha Yuda 27:3-10	Yesu anakabidhiwa kwa Pilato 27:1-2 Yuda anajinyonga 27:3-10	Yesu mbele ya Pilato 27:1-2 27:3-10	Yesu anapelekwa kwa Pilato 27:1-2 Kifo cha Yuda 27:3-4a 27:4b 27:5 27:6-8 27:9-10 Pilato anamhoji Yesu 27:11a 27:11b-12 27:13 27:14 Yesu anahukumiwa Kifo 27:15-18 27:19 27:20-21a 27:21b 27:22a 27:22b 27:22a 27:22b 27:24-26 27:25 27:26 Wanajeshi Wanamdhihaki Yesu 27:27-31 Usulubishwaji Wa Yesu 27:32-44	Yesu anapelekwa Mbele ya Pilato 27:1-2 Kifo cha Yuda 27:3-10 Yesu mbele ya Pilato 27:11-14 27:15-18 27:19 27:20-26 Yesu anavikwa taji ya Miba 27:27-31 Usulubishwaji 27:32-36 27:37-38 Kristo Msulubishwaji Anadhihakiwa 27:39-44 Kifo cha Yesu 27:45-50
Yesu anahojiwa na Pilato 27:11-14	Yesu anamkabili Pilato 27:11-14	27:11-14		
Yesu anahukumiwa Kifo 27:15-26	Kuchukua sehemu Ya Baraba 27:15-26	27:15-23		
27:22a				
Wanajeshi Wanamdhihaki Yesu 27:27-31 Usulubishwaji Wa Yesu 27:32-44	Wanajeshi Wanamdhihaki Yesu 27:27-31 Mfalme Msalabani 27:32-44	Usulubishwaji 27:27-31 27:32-37 27:38-44		
Kifo cha Yesu 27:45-56	Yesu anakufa Msalabani 27:45-56	Kifo cha Yesu 27:45-54	Kifo cha Yesu 27:45-46 27:47-48	

			27:49	
			27:50	
			27:51-53	27:51-54
			27:54	
		27:55-56	27:55-56	27:55-56
Kuzikwa kwa Yesu anazikwa			Mazishi ya Yesu	Maziko
Yesukatika kaburi la Yusufu				
27:57-61	27:57-61	27:57-61	27:57-61	27:57-61
Mlinzi katika Kaburi	Pilato anaweka Walinzi		Walinzi Kaburini	Mlinzi Kaburini
27:62-66	27:62-66	27:62-66	27:62-64	27:62-66
			27:65	
			27:66	

## **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka “[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)”)**

### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiyaya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 27:1-2**

<sup>1</sup> Na ilipokuwa asubuhi, wakuu wa makuhani wote na wazee wa watu wakafanya shauri juu ya Yesu, wapate kumwua; <sup>2</sup>wakamfunga, wakamchukua, wakampeleka kwa Pilato aliyekuwa liwali.

**27:1 "Na ilipokuwa asubuhi"** Warumi waliendesha mahakama zao mapema zaidi kila siku yawezekana kwa sababu ya joto. Mhujaji wengi zaidi na wananchi wa Yerusalemu walikuwa hawajaamka bado. Lazima ilifanyika saa 12 asubuhi.

☑️**"wakuu wa makuhani wote"** Wengi unarejerea familia ya Kikuhani ya Annas, aliekuwa ameinunua hii ofisi kutoka kwa Warumi. Alikuwa ametanguliwa na wanawe wa kiume na mashemeji zake kadhaa.

☑️**"wakafanya shauri"** Kauli za Yesu katika Mt. 26:64 ziliwahukumu katika fahamu zao juu ya kukufuru ambalo lilikuwa ni kosa lilinalostahili kupewa adhabu ya kupigwa mawe lakini walitaka abebeshwe laana ya kusulubiwa (kama vile Kumb. 21:23). Hivyo wakaja na mashitaka ambayo Warumi wangeweza kuyafanyia kazi. Hapa ndipo mashitaka ambayo alidai kuwa mfalme wa Wayahudi yalitumika kama tishio la kisiasa dhidi ya utawala wa Kirumi

**27:2 "wakamfungwa"** Yesu alifungwa wakati wa mashitaka haya yawezekana kwasababu (1) walikuwa na hofu ya uweze wake wa kufanya miujiza ili kuweza kujifungua mwenyewe; (2) ilikuwa nai namana ya kumfedhehesha; au (3) utaratibu uliozoeleka kwa Wahalifu.

☐ **"Pilato aliyekuwa liwali"** Yawezekana haya yalitendeka katika ngome ya Kirumi ya Antonia ambayo ilikuwa imejengwa jirani na Hekalu, inagawa ingeweza kuwa pia katika jumba la kifalme la Herode ambalo lingeweza kutumika kwa viongozi wa Kirumi. Warumi walikuwa na vikosi vya ziada kutoka Bahari ya Kaisaria huko Yerusalemu wakati wa sherehe za Kiyahudi iwapo kungetokea maandamano na ghasia (kama vile Mt. 27:24). Pilato aliteuliwa kuwa Liwali kutokea mnamo mwaka 26-36 B.K. Historia inamtaja yeye kama katili na mtu asiyejali.

Imekuwa ikidhaniwa kuwa uongozi wa kiyahudi ulimleta Yesu kwa Pilato

1. kutimiliza unabii wa Yesu juu ya kuuawa na Mataifa
2. Kuwapa nafasi Warumi kwasababu katika sikuzake wakuu wa sinagogi hawakuwa na mamlaka ya adhabu za vifo

Hata hivyo Yesu alikuwa anashitakiwa kwa kukufuru na hivyo alitakiwa apigwe mawe. Wayahudi walifanya jambo hili kwa Stefano katika Mdo. 7 na hawakutaka kibali kutoka kwa Warumi. Nafikiria kwamba viongozi hawa wa Kiyahudi walitaka Yesu asulubishwe ili abebe laana ya kiungu ya Kumb. 21:23 ipitishwe juu yake. Walitaka mtu huyu aliyejifanya Masihi alaaniwe na Mungu. Yesu aliibeba "laana" (kama vile Gal. 3:13; Kol. 2:14) kwa ajili yetu!

Kuna utofautiano wa maandiko ya Kiyunani hapa. Katika maandiko kadhaa mazuri jina la kwanza la Pilato Pontio lipo, (kama vile MSS A, C, W, na Vulgate). Pia inatokea katika Luka 3:1; Mdo. 4:27 na 1 Tim.6:13. Majina mawili ni utaratibu katika fasihi ya kwanza ya kanisa. Hata hivyo halipo katika MSS, α, B, na L, pia katika Marko 15:1 na Luka 23:1.

## MADA MAALUMU: PONTIO PILATO

- I. Mtu
  - A. Mahali na wakati alipozaliwa havijulikani
  - B. Wa daraja au tabaka la Equestrian (daraja la juu ngazi ya kati la jamii ya Warumi)
  - C. Aliaoa, lakini watoto hawajulikani
  - D. Teuzi za kiutawala wa awali (ambazo lazima zilikuwa nyingi) hazijulikani
- II. Nafsi ya mtu
  - A. Mitazamo miwili tofauti
    1. Philo (Legatio na Gaium, 299-305) na Josephus (Antiq. 18.3.1 na Jewish Wars 2.9.2-4) wanamwelezea mtawala wa ..... asiye na huruma na katili.
    2. Agano Jipya (Injili, Matendo) linamtoa kama wakili wa Kirumi dhaifu ambaye anaweza kuendeshwa kwa urahisi.
  - B. Paul Barnett, *Jesus and the Rise of Early Christianity*, kur. 143-148, kinatoa maelezo yenye kukubalika kuhusu mitazamo hii miwili.
    1. Pilato aliteuliwa kuwa wakili mwaka 26 b.k chini ya Tiberia ambaye alikuwa anaunga mkono Wayahudi (kama vile. Philo, Legatio na Gaium, 160-161).
    2. Tiberius alipatwa mateso ya kupotesa nafasi yake ya kisiasa kwa L. Aelius Sejanus, Kiranja wake wa walinzi wa jumba la kifalme aliyefanyika ngu halisi nyuma ya kiti cha kifalme na aliyewachukia Wayahudi (Philo, Legatio na Gaium, 159-160).
    3. Pilato alikuwa mfuasi wa Sejanus na alijaribu kumvutia
      - a. Kuleta viwango vya kirumi kwenye mji wa Yerusalemu (26 B.K), ambavyo mawakiri wengine hawakuwa wamefanya. Hizi alama za Miungu wa Kirumi iliwachochea Wayahudi (kama vile. Josephus' Antiq. 18.3.1; Jewish Wars 2.9.2-3).

- b. Kuchapa sarafu (29-31 b.k) ambayo ilikuwa na picha za Warumi wakiabudu zimechongwa juu yake. Josephus anasema alikuwa kwa makusudi kabisa anajaribu kupindua sheria za kiyahudi na desturi (kama vile Josephus, Antiq. 18.4.1-2).
  - c. Kuchukua fedha kutoka hazina ya hekalu kujenga mfereji Yerusalemu (kama vile Josephus, Antiq. 18.3.2; Jewish Wars 2.9.3).
  - d. kupata Wagalilaya baadhi na kuwaua wa kutoa dhabihu siku ya pasaka mjini Yerusalemu.
  - e. Kuleta ngao za Kirumi mjini Yerusalemu katika mwaka 31 b.k. ,mwana wa Herode mkuu aliyempelekea ombi kwake waondolewe. Lakini asingefanya hivyo walimwandikia Tiberia ambaye aliwataka warejeshwe kaisaria kwa bahari (kama vile. Philo, Legatio na Gaium, 299-305).
  - f. Kupata Wasamaria wengi wachinjwe juu ya mlima Gerizim (mwaka 36/37 b.k) walipokuwa wanalifuta vifaa vyao vitakatifu vya dini yao, ambavyo vilikuwa vimekwisha potea. Jambo hili lilimsababisha mkuu wake Pilato wa mahali pale (Vitellius, Kiranja wa Ashuru) amwondoe kutoka ofisini na kumtuma Roma (kama vile Josephus, Antiq. 18.4.1-2).
4. Sejanus alihukumiwa katika mwaka 31 b.k na Tiberia alirejeshwa kwenye mamlaka ya kisiasa kwahiyo , #a, b, c, na d pengine zilifanywa na Pilato kupata imani kwa Sejanus' ; #e zingeweza kuwa ni majaribio ya kupata imani kwa Tiberia lakini yawezekana yakawa yamelipuka na kuharibika.
  5. Ni dhahiri kwa amiri jeshi mfalme anayeunga mkono Wayahudi aliyerejeshwa pamoja na barua rasmi kwa mawakili kutoka Tiberia kuwa mwema kwa Wayahudi (kama vile Philo, Legatio na Gaium, 160-161), kwamba uongozi wa Kiyahudi katika Yerusalemu walichukua fursa ya udhaifu wa kisiasa wa Pilato na Tiberia na wakamrubuni ili amsababisha Yesu kusulubiwa. Nadharia ya Barnett inaleta pamoja mitazamo hiyo miwili ya Pilato katika njia inayoonekana kuwa yenye mantiki.
- III. Hatma yake
- A. Aliitwa tena na alifika Roma mara tu baada ya kifo cha Tiberia (mwaka 37b.k).
  - B. Hakuteuliwa tena.
  - C. Mke wake hajulikani baada ya hili. Kuna nadharia nyingi za baadaye, lakini hakuna kweli zilizo salama.

#### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 27:3-10

<sup>3</sup>Kisha Yuda, yule mwenye kumsaliti, alipoona ya kuwa amekwisha kuhukumiwa, alijuta, akawarudishia wakuu wa makuhani na wazee vile vipande thelathini vya fedha, akasema, Nalikosa nilipoisaliti damu isiyo na hatia. <sup>4</sup>Wakasema, Basi, haya yatupasani sisi? Yaangalie haya wewe mwenyewe. <sup>5</sup>Akavitupa vile vipande vya fedha katika hekalu, akaondoka; akaenda, akajinyonga. <sup>6</sup>Wakuu wa makuhani wakavitwaa vile vipande vya fedha, wakasema, Si halali kuviweka katika sanduku ya sadaka, kwa kuwa ni kima cha damu. <sup>7</sup>Wakafanya shauri, wakavitumia kwa kununua konde la mfinyanzi liwe mahali pa kuzika wageni. <sup>8</sup>Kwa hiyo konde lile huitwa konde la damu hata leo. <sup>9</sup>Ndipo likatimia neno lililonenwa na nabii Yemia, akisema, Wakavitwaa vipande thelathini vya fedha, kima chake aliyetiwa kima, ambaye baadhi ya Waisraeli walimtia kima; <sup>10</sup>wakavitumia kwa kununua konde la mfinyanzi, kama Bwana alivyoniagiza.

**27:3 "Kisha Yuda, yule mwenye kumsaliti, alipoona ya kuwa amekwisha kuhukumiwa"** Tungo hii inahusiana kiwakilishi tata tangulizi, Yeye. Fasiri za Williams na Phillips za Agano Jipya zinadhania kwamba inarejerea kwa Yuda lakini fasiri zingine zote za kisasa zinarejerea hii kama kiwakilishi cha Yesu. Tazama kuanza kwa herufi kubwa "Yeye" katika NASB. NIV, TEV, JB, na NRSV na hata ingiza jina "Yesu" katika kiwakilishi.

☐ **"alijuta"** Kuna maneno mawili katika Kiyunani yanayofasiri "toba." Moja lililotumika hapa halikuwa neno la kawaida lililotumika katika Mt. 3:2, ambalo lilimaanisha "kubadilisha kwa mawazo na matendo." Hapa neno lilimaanisha "huzuni ya baadaye" lakini likiwa na maana ya kutokuwepo na mabadiliko ya uhalisia (kama vile Mt.

21:29; 2 Kor. 7:8). Mukstadha bora zaidi katika Agano Jipya kulinganisha na visawe vya maneno haya ni 2 Kor. 7:8-10. Angalia [MADA MAALUMU: TOBA KATIKA AGANO LA KALE](#) katika Mt. 3:2.

▣"vipande thelathini" Haya ni maelezo ya Zek. 11:12. Hii ilikuwa ni gharama ya mtumwa aliyechinjwa (kama vile Mt. 26:15;Kut. 21:32).

**27:4 "damu isiyo na hatia"** Kuna utofautiano wa maandiko ya Kiyunani katika ngazi hii. Matoleo yote ya Kingereza ambayo yanalinganishwa katika fasiri hii yana "isiyo na hatia." Hata hivyo maandiko ya kale B, kiasili yalikuwa na "bila hatia," lakini baadaye wanakili waliweka "mwenye haki" kutoka Mt. 23:35. Hii ilifuatiwa na Vulgate na Diatessaron. Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale linatumia vivumishi vyote kuelezea nomino "damu" ; "isiyo na hatia" inatokea mara kumi na nne na "mwenye haki" inatokea mara nne katika LXX. Toleo la UBS<sup>4</sup> linatoa "isiyo na hatia" kipimo cha "B" (karibu na hakika).

**27:5 "katika hekalu"** Neno hili las Kiyunani siku zote linarejerea Madhabahu Kuu inayotengenezwa na Mahali Patakatifu na Patakatifu kama kutenganisha kutoka eneo Hekalu kamili (kama vile Yohana 2:9).

▣"akajinyonga" Hii ilikuwa si maandiko ya uthibitisho ya kithiologia juu ya kujinyonga na kuleta hukumu. Kuna kujinyonga kadhaa kaunakotajwa katika Agano la Kale: Amu. 9:54; 16:30; 1 Sam. 31:4,5; 2 Sam. 17:23; 1 Wafalme 16:18. Hakuna chochote hasi ambacho kilishawahi kusemwa juu ya matendo haya. Ilikuwa ni kukosekana kwa toba ya kweli kwa Yuda kulikosababisha upotevu wake kugongwa muhuri, wala sio kujinyonga mwenyewe.

Hii hadithi ya kifo cha Yuda katika Mdo. 1:18 haitofautiani wala kupingana na ile ya Mathayo bali inaiongeza na kuiunga mkono. Inavyoonekana Yuda alijinyonga mwenyewe juu ya mwinuko na baadaye kamba ilikatika na mwili wake kuanguka na kuvunjika kwa kupasuka wazi.

## MADA MAALUMU: YUDA ISKARIOTI

Yuda alikwisha sikia, akachunguza, na kufanya ushirika na Bwana Yesu kwa karibu sana kwa miaka mingi, lakini dhahili kabisa hakuwa na ushirika binafsi na Yeye katika imani (k.v.. Mt. 7:21-23). Petro naye alipitia uzito ule ule wa jaribu kama alilolipitia Yuda, lakini yakiwa na matokeo yenye athari kubwa (k.v.Mt.26:75). Majadiliano mengi yalifanyika juu ya mwenendo wa usaliti wa Yuda:

1. Kimsingi yalikuwa ni mambo ya fedha (k.v.Yoh.12:6)
2. Kimsingi yalikuwa ni mambo ya kisiasa (k.v William Klassen, *Judas Betrayer or Friend of Jesus?*)
3. Yalikuwa ni mambo ya kiroho (kama vile Luka 22:3; Yoh. 6:70; 13:2,27)

Juu ya somo la ushawishi wa kishetani au kumilikiwa na pepo (angalia Mada Maalumu: hali ya kimapepo katika agano jipya) kuna vyanzo mbali mbali vya kimapato (vilivyo oredheshwa katika mpangilio wa wale ninao waamini)

1. Merrill F. Unger, *Biblical Demonology, Demons in the World Today*
2. Clinton E. Arnold, *Three Crucial Questions About Spiritual Warfare*
3. Kurt Koch, *Christian Counseling and Occultism, Demonology Past and Present*
4. C. Fred Dickason, *Demon Possession and the Christian*
5. John P. Newport, *Demons, Demons, Demons*
6. John Warwick Montgomery, *Principalities and Powers*

Uwe mwangalifu juu ya udanganyifu wa kitamaduni na miiko. Shetani anamwathuri Petro katika Mt. 16:23 kumjaribu Yesu katika njia zile zile-kifo chake mbadala. Shetani anaendelea. Anajaribu kutumia kila liwezekanalo kuzuia kazi ya Yesu ya ukombozi kwa niaba yetu.

1. Jaribu la Yesu, Luka 4
2. Akamtumia Petro
3. Akamtumia Yuda Iskarioti na wakuu wa Sinagogi

Yesu hata anamweleza Yuda kama shetani katika Yohana 6:70. Biblia haizungumzii somo la kushawishiwa na kumilikiwa na shetani kama inahusiana na waumini. Lakini, waumini wazi kabisa wanaathiriwa na maamuzi

binafsi na uovu binafsi (angalia Mada Maalumu: Uovu Binafsi)

Asili ya "Yuda Iskarioti" kwa kiasi Fulani haieleweki; hata hivyo, kuna uwezekano mbali mbali:

1. *Kerioth*, mji wa Yuda (k.v. Yosh. 15:25)
2. *Kartan*, mji wa Galilaya (k.v. Yosh. 21:32)
3. *Karōides*, walipomlaki na matawi ya mitende huko Yerusalemu au Yeriko
4. *scortea*, aproni au begi la ngozi (k.v. Yoh. 13:29)
5. *ascara*, kujinyonga (Waebrania) toka Mt. 27:5
6. kisu cha kujiulia (Kiyunani), ikimaanisha alikuwa mkereketwa kama simion (k.v. Luka 6:15)

**27:6 "ni kima cha damu"** Hawakuwa na hofu juu ya kutumia fedha zilizokuwa zimetolewa kumsaliti Yesu lakini hawakujiskia vizuri kuichukua tena! Kejeli ya namna gani hii!

**27:7 "wao. . . kununua konde la mfinyanzi"** Hii yawezekana ilikuwa ni shamba la mfinyanzi ambalo halina rutuba na hivyo lilikuwa lenye thamani kidogo. Inaweza kuwa maelezo ya Yer. 18-19. Kutoka katika nyakati za Jerome (karne ya 4 B.K.) ilikuwa inasemekana kuwa ni bonde la Hinnom jirani na Yerusalemu.

**27:8 "konde la damu"** Hii inafasiri neno la Kiaramu *Hakeldama*, linalopatikana katika Mdo. 1:19. Toleo la Vulgate la Jerome linaweka neno la Kiaramu katika mstari huu.

**27:9 "lililonenwa na nabii Yereimia"** Hii ilikuwa ni nukuu ya moja kwa moja kutoka Zek. 11:12-13. Yereimia 18:119 pia kuzungumzia mfinyanzi na Yer. 32:7-9 inataja kununua shamba. Hii iliwasababisha wafasiri matatizo makubwa

1. Augustine, Beza, Luther, na Keil wanasema kwamba Mathayo alinukuu jina la Yereimia kimakosa
2. The Peshitta, Fasiri ya kishamu ya karne ya 5 B.K. na Diatessaron viliondoa jina la nabii kutoka katika andiko
3. Origen na Eusebius wanasema mnakili alisababisha tatizo
4. Jerome na Ewald walisema ni nukuu kutoka kwa maandiko yasiyo ya kweli anayopewa Yereimia
5. Mede alisema kwamba Yereimia aliandika Zekaria, sura za 9-11
6. Lightfoot na Scofield wanasema Yereimia aliwekwa kwenye orodha kwanza katika mgawanyo wa Kiebrania wa Kanoni ijulikanayo kama "manabii" na hivyo jina lake linasimama kwa sehemu hiyo ya Kanoni
7. Hengstenberg alisema kwamba Zekaria alinukuu Yereimia
8. Calvin alisema kwamba makosa yaliingia katika andiko
9. F. F. Bruce na tanbihi ya inasema kwamba ulikuwa ni muunganiko wa nukuu kutoka Zekaria na Yereimia.

Nafikiria #6 ni maelezo mazuri zaidi.

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 27:11-14**

<sup>11</sup>Naye Yesu akasimama mbele ya liwali; liwali akamwuliza, akasema, **Wewe ndiwe mfalme wa Wayahudi? Yesu akamwambia, Wewe wasema.** <sup>12</sup>Lakini aliposhitakiwa na wakuu wa makuhani na wazee, hakujibu hata neno. **13** Ndipo Pilato akamwambia, **Husikii ni mambo mangapi wanayokushuhudia?** <sup>14</sup>Asimjibu hata neno moja, hata liwali akastaajabu sana.

**27:11 "Wewe ndiwe mfalme wa Wayahudi?"** Hili lilikuwa ni swali ambalo lilimaanisha uhaini dhidi ya Rumi. Lilikuwa ni jambo la Kisiasa lililomuhusu Pilato.

**27:11**

**NASB, NKJV**

**"ni kama usemavyo"**

**NRSV**

**"wewe wasema"**

TEV "wewe wasema"  
NJB "ni wewe usemaye"

Jibu la Yesu lilikuwa ni tungo ya kimafumbo, "Ndio!" lakini ikiwa na sifa (kama vile Yohana 18:33-37), ambacho kinaonesha kwamba ufalme wake haukuwa wa kidunia.

**27:12 "aliposhitakiwa"** Angalia Luka 23:2.

☐ **"hakujibu"** Hii inahusiana na unabii wa kimasihwa wa Isa. 53:7. Alimjibu Pilato kwa faragha lakini asingeweza kutaja mashitaka mbele ya viongozi wa Kiyahudi au Herode.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 27:15-18**

<sup>15</sup>Basi wakati wa siku kuu, liwali desturi yake huwafungulia mkutano mfungwa mmoja waliyemtaka. <sup>16</sup>Basi palikuwa na mfungwa mashuhuri siku zile, aitwaye Baraba. <sup>17</sup> Basi walipokutanika, Pilato akawaambia, Mnataka niwafungulie yupi? Yule Baraba, au Yesu aitwaye Kristo? <sup>18</sup> Kwa maana alijua ya kuwa wamemtoa kwa husuda.

**27:15 "siku kuu"** Hii inarejerea kwenye Paska, moja ya sherehe za mwisho wa mwaka kati ya tatu ambapo wanaume wote wa Kiyahudi walio na umri zaidi ya miaka ishirini walitakiwa kuhudhuria (kama vile Law. 23).

☐ **"hata liwali akastaajabu"** Hakuna uthibitisho wa kihistoria kwa hili isipokuwa katika Josephus, *Antiquities of the Jews* 20.9.3.

**27:16, 17 "Barabba"** Baadhi ya matoleo yaliyofuata baadaye yana "Yesu Barabba," lakini hili si sana kama uchaguzi wa kimaandiko kama ilivyo desturi. Mjadala mzuri upo kwa Bruce Metzger's *A Textual Commentary on the Greek New Testament*, ukur. 67-68, kutoka United Bible Societies. "Barabba" iilimaanisha kijana wa baba au mwalimu. Kiukweli alikuwa amepatikana na hatia za kiuahuni ambazo aliyekuwa anashitakiwa nazo ni Yesu.

**27:18 "Kwa maana alijua ya kuwa wamemtoa kwa husuda"** Pilato alijaribu njia kadhaa kumwachia Yesu kwaababu ya chuki yake kwa viongozi wa kiyahudi na njama zao za kilaghai.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 27:19-23**

<sup>19</sup>Na alipokuwa ameketi juu ya kiti cha hukumu, mkewe alimpelekea mjumbe, kumwambia, Usiwe na neno na yule mwenye haki; kwa sababu nimeteswa mengi leo katika ndoto kwa ajili yake. <sup>20</sup>Nao wakuu wa makuhani na wazee wakawashawishi makutano ili wamtake Baraba, na kumwangamiza Yesu. <sup>21</sup>Basi liwali akajibu, akawaambia, Mnataka niwafungulie yupi katika hawa wawili? Wakasema, Baraba. <sup>22</sup> Pilato akawaambia, Basi, nimtendeje Yesu aitwaye Kristo? Wakasema wote, Asulibiwe. <sup>23</sup>Akasema, Kwani? Ni ubaya gani alioutenda? Wakazidi sana kupiga kelele, wakisema, Na asulibiwe.

**27:19 "mkewe alimpelekea mjumbe, kumwambia, Usiwe na neno na yule mwenye haki; kwa sababu nimeteswa mengi leo katika ndoto kwa ajili yake"** Taarifa hizi ni za kipekee katika Mathayo. Lazima walikuwa wamemwongelea Yesu. Alitumia jina lake la kimasihwa kumrejerea Yesu, japo ni kiasi gani alijua haijulikani! Kejeli ni kwamba mwanamke wa kipagani aliona kile ambacho viongozi wa kiyahudi hawakuona (kama vile Mt. 27:54; Yohana 1:11).

**27:20 "kumwangamiza"** Angalia Mada Maalum: *Apollumi* katika Mt. 2:13.

**27:23 "Kwani? Ni ubaya gani alioutenda?"** Pilato halikuwa hashawishiki ikiwa Pilato ana hatia. Andiko hili lilikuwa ni nia kwa kanisa la kwanza (pia mapito katika Mdo) kuonesha kwamba Ukristo haukuwa tishio kwa utawala wa Kirumi.

☐ **"Wakazidi sana kupiga kelele"** Tungo ya njeo ya wakati usio timilifu, hii inaweza kuchukuliwa "walianza kupiga kelele" au "walipiga kelele tena na tena." Kusanyiko hili halikuwa kama lile lililowahusisha mahujaji katika Kuingia kwa shangwe. Hawa yawezekana walikuwa marafiki za Barabba waliokuwa wamekusanyika kwa lengo la kujaribu kumpigia debe achiwe! Baadhi wameona hili kama kusanyiko lililokuwa limepangwa na wazee wa sinagogi.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 27:24-26**

**24**Basi Pilato alipoona ya kuwa hafai lo lote, bali ghasia inazidi tu, akatwaa maji, akanawa mikono yake mbele ya mkutano, akasema, Mimi sina hatia katika damu ya mtu huyu mwenye haki; yaangalieni haya ninyi wenyewe. **25** Watu wote wakajibu wakasema, Damu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu. **26**Ndipo akawafungulia Baraba; na baada ya kumpiga Yesu mijeledi, akamtoa ili asulibiwe.

**27:24 "ghasia inazidi tu"**Hii siku zote ilikuwa inawezekana wakati wa sherehe kwa kuwa Yerusalemu ilijawa na watu wengi hasa mahujaji wenye mihemko. Rumi siku zote iliweka vikosi vya ziada kutokea Kaisaria katika ngome ya Antonio wakati wa siku za sherehe.

☐ **"akatwaa maji, akanawa mikono yake mbele ya mkutano"** Hizi zilikuwa ni desturi za Kiyahudi na sio za Kirumi (kama vile Kumb.21:6-7; Zab. 26:6; 73:13).

**27:25 "Damu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu"** Hiki kilikuwa ni kiapo kibaya sana cha kimakosa, hasa kwa ufahamu wa mtazamo wa Agano la Kale katika kuingia hatia ya kijumuiya (kama vile Kut. 20:5-6; 2 Sam. 3:29). Hii ilikuwa ni kujivutia laana wenyewe! Ilitimizika mnamo mwaka 70 B.K.

**27:26 "wakamtesa"** Hii ilikuwa ni adhabu kali sana! Mara kwa mara ilipelekea kifo. Siku zote ilitangulia kabla ya kusulubiwa lakini inaonekana kimapema kutokea Yohana 19:1, 12 kwamba hii yawezekana lilikuwa ni jaribio lingine la Pilato kumfanya watu wamuhurumie Yesu.

Injili zinatumiya maneno tofauti tofauti kuelezea kupigwa huku kunakopelekea kifo.

1. *phragelloō* katika Mt. 27:26; Marko 15:15, imefasiliwa na toleo la NASB kama "kuteswa"
2. *derō* katika Luka 22:63, likifasiriwa na toleo la NASB kama "kupigwa"
3. *mastigoō* katika Yohana 19:1, kunafasiriwa na toleo la NASB kama "kuteswa" (kama vile Mt. 20:19; Marko 10:34; Luka 18:33)

Kupigwa huku kwa namna mbaya kulitangulia kabla ya kusulubiwa. Ilikuwa ni maumivu makali sana kiasi kwamba wengi walikuwa wamekufa kutokana nayo. Mtu alikuwa amevuliwa nguo zote na mikono yao ikifungwa nyama kwenye ardhi. Fimbo yenye ngozi na vyuma vyenye kama miiba na miamba au mifupa mwishoni vikiwa tisa ilipigwa katika mgongo na kufanya nyama ya mgongo kubaki inaonekana wazi. Imeandikwa kwamba vyuma hivyo kama miiba

1. vilimfanya mtu awe haoni
2. vilifunua nyama na kuacha mbavu na mifupa yake kuonekana
3. vilitoa na kugonga meno

Hakukuwa na kiwango gani cha mwisho wa uchapwaji wa fimbo uliokuwa ukitolewa na wanajeshi wawili, mmoja kila pande.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 27:27-31**

<sup>27</sup>Ndipo askari wa liwali wakamchukua Yesu ndani ya Praitorio, wakamkusanyikia kikosi kizima. <sup>28</sup>Wakamvua nguo, wakamvika vazi jekundu. <sup>29</sup>Wakasokota taji ya miiba, wakaiweka juu ya kichwa chake, na mwanzi katika mkono wake wa kuume; wakapiga magoti mbele yake, wakamdhihaki, wakisema, Salamu, Mfalme wa Wayahudi! <sup>30</sup>Kisha wakamtemea mate, wakautwaa ule mwanzi, wakampiga-piga kichwani. **31** Walipokwisha kumdhhihaki, wakalivua lile vazi, wakamvika mavazi yake, wakamchukua kumsulibisha.



27:27

NASB, NKJV,

NJB "Praetorio"

NRSV, TEV "makao makuu ya liwali"

Hili eneo lilikuwa katika ngome ya Antonio au katika jumla la kifalme la Herode ambalo lilikuja kuwa makazi ya Liwali wa Kirumi akiwa Yerusalemu. Baadhi wamefiiria kuwa ilikuwa ni eneo la vikosi vya wanajeshi.

### **MADA MAALUM: MLINZI WA MFALME**

Kwa asili yake neno, "praetoria," linahusu hema la majeshi ya Kirumi ("hakimu"), lakini baada ya kipindi cha kuangushwa kwa mtawala wa Rumi lilitumika katika dhana ya utawala kuonesha makao makuu ama maskani ya siasa (kama vile Mt. 27:27; Yohana 18:28,33; 19:9; Matendo 23:35; Flp. 1:13).

Hata hivyo kwenye ulimwengu wa kirumi wa karne ya kwanza lilitumika kwa watumishi ambao waliunda kikosi maalumu cha ulinzi wa ufalme. Kundi hili la maaskari waliopewa heshima maalumu lilianziswha na Augustino (27 k.k) lakini mwishowe lilitiwa mkazo katika Rumi na Tiberia.

1. Kuwa wenye cheo kimoja, kamanda wa karne
2. pokea mshahara mara mbili ya kiwango
3. Kuwa na upendeleo maalumu (yaani, walistaajabu baada ya miaka 16 badala ya miaka 25)
4. kuwa wenye nguvu kiasi kwamba uchaguzi wao kwa amiri jeshi mkuu wa ufalme wa Rumi aliyeheshimiwa

Ulipofika muda wa Konstantine ndipo kikundi hiki kilichokuwa kimepewa heshima maalumu chenye nguvu kisiasa mwishowe kilivunjika

☐ **"kikosi kizima"** Hiki kilikuwa na watu kama 600, lakini kiukweli ni baadhi yao tu walikuwa katika malindo yao kwa wakati mmoja.

**27:28 "vazi jekundu"** Neno hili linatokea katika mdudu ambaye alitumika kubadili nguo kuwa na uwekundu mweusi. Marko 15:17 na Yohana 19:2 zina "Zambarau." Hii yawezekana lilikuwa vazi jekundu la Afisa wa Kirumi lililofifia rangi yake. Zambarau lilikuwa vazi na rangi ya kifalme. Kanisa la mwanzoni lililiona hili kama uwakilishi wa nafasi ya kifalme ya Yesu (kama walivyomfanyia stephano kwa kumvika taji ya miiba). Watu wa kale hawakuwa vizuri kwenye kutoa majina ya rangi kama wat wa kisasa.

**27:29-30** Wanajeshi wanachukua uadui wao kwenda kwa watu wa kiyahudi juu ya Yesu katika kejeli zao Kwake. Ie "taji ya miiba" inaweza kuelezea (1) dhahaka juu ya madai ya Yesu ya kuwa mfalme au (2) laana ya Mwanzo 3:18 (kama vile Gal. 3:13). Miiba ni uwakilishi wa kuikataa injili (kama vile Ebr. 6:8).

### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 27:32**

<sup>32</sup>Hata walipokuwa wakitoka, wakamwona mtu Mkirene, jina lake Simoni; huyu wakamshurutisha auchukue msalaba wake.

**27:32 "mtu Mkirene, jina lake Simoni"** Kirene ni Libya ya sasa, lakini jina la bwana huyu ni la Kiyahudi. Ukweli ni kwamba alikuwa Yerusalemu kwa wakati huu inaashiri kwamba alikuwa ni Myahudi au chotara. Kulikuwa na Sinagogi katika Yerusalemu kwa ajili ya Wayahudi Wakirene (kama vile Mdo. 6:9). Utaifa wa rangi yake au historia yake ya kikabila haifahamiki, lakini kuna uwezekano kwamba alikuwa ni Myahudi aishiye nje.

☐ **"wakamshurutisha"** Hili ni neno la Kiajemi linalotumika katika Mt. 5:41. Majeshi walikuwa na uwezo wa kuamuru wakazi wa kawaida kufanya shughuli fulani.

☐ **"auchukue msalaba wake"** Ikiwa ni vipande vya mbau vya kutengenezea msala au msalaba mzima ulibebwa kuelekea Golgota haijulikani. Umbo la msalaba inaweza kuwa ulikuwa na umbo la herufi kubwa ya "T," herufi ndogo ya "t," na "X," au miimo kadhaa inayoweza kubeba watu wengi kadhaa.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 27:33-34**

<sup>33</sup>Na walipofika mahali paitwapo Golgotha, yaani, Fuvu la kichwa, <sup>34</sup>wakampa kunywa divai iliyochanganyika na nyongo; lakini yeye alipoionja hakutaka kunywa.

**27:33 "Golgotha"** Hili neno la Kiebrania lililomaanisha "fuvu." "Kalvari" linatoka katika Kilatini. Neno linarejerea mlima ulio chini, usio na uoto wowote, sio fuvu kamili kabisa.

**27:34 "wakampa kunywa divai iliyochanganyika na nyongo"** Lijitabu la Sheria za Kiyahudi za Kibabeli linasema kwamba wanawake wa Yerusalemu walitoa kinywaji hiki kwa wahalifu waliohukumiwa ili kuwapunguzia maumivu yao (kama vile Marko 15:23, ambapo "nyongo" inamaanisha "manukato"). Hii yawezekana ilikuwa ni rejea ya kinabii ya Zab.69:21.

☐ **"hakutaka kunywa"** Hii haihusiani na majadiliano ya kidini ya kisasa ya kuacha kabisa kutumia (angalia Mada Maalum katika Mt. 26:29). Yesu baadaye anakuja kukubali mvinyo wa kawaida wa maaskari (kama vile Mt. 27:48). Anakataa kunywa chochote kupooza maumivu au fahamu zake.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 27:35-37**

<sup>35</sup>Walipokwisha kumsulibisha, waligawa mavazi yake, wakipiga kura; [ili litimie neno lililonenwa na nabii, Waligawa nguo zangu kati yao, na juu ya vazi langu walipiga kura.] <sup>36</sup>Wakaketi, wakamlinda huko. <sup>37</sup>Wakaweka juu ya kichwa chake mashitaka yake, yaliyoandikwa HUYU NI YESU, MFALME WA WAYAHUDI.

**27:35 "Walipokwisha kumsulibisha"** Injili haikai katika vipengele vya kimwili vya kifo cha Yesu (kama vile Zab.22:16). Aina hizi za vifo zilianzishwa huko Mesopotamia na kuchukuliwa na Wayunani na Warumi. Ilikusudiwa kuongeza na kurefusha muda wa kuishi kabla ya kifo ili kupata siku kadhaa. Kusudi lake ilikuwa ni kufedhehesha na kusababisha hofu ili kusitokee uasi dhiri ya Warumi. Makala ya kina zaidi inapatikana katika Zondervan Pictorial Bible Encyclopedia, Vol. 1, ukur. 1040-42.

☐ **"waligawa mavazi yake, wakipiga kura"** Haya ni maelezo kwa Zab.22:18. Yesu yawezekana likuwa uchi na yawezekana zaidi akifungwa kiunoni kitamba tu. Toleo la maandiko ya Textus Receptus linaongeza kwenye andiko tungo kadhaa zitokazo katika Yohana 19:24, ambayo ilinukuu Zab. 22:18; Hizi hata hivyo sio maandiko ya Kiyunani. Matoleo ya uhariri huu haupo katika maandiko ya Kiyunani, α, A, B, D, L, au W, wala katika Kilatini au fasiri za Kishamu. "Kupiga Kura" kunatumika katika Agano Jipya kama nani atakayepata bahati hapa, na kama njia ya kujua mapenzi ya Mungu kama katika Mdo. 1:26. Mfano huu unaofutia wa Agano la Kale ni wa Urim na Thummim. Hii ni njia ya kimwili ya kujua mapenzi ya Mungu imepitwa na wakati. Hii inaonesha kwamba Biblia inaandika vitu ambavyo sio lazima ivitetee. Mfano mwingine mzuri wa wazo hili hili ingekuwa ni ulaghai wa Gideoni (cf. Jdgs kama vile Amu. 6:36-40).

**27:37 "mashitaka yake"** Kutoka Yohana 19:20 tunajifunza kwamba mashitaka yalikuwa yameandikwa katika lugha tatu (Kiaramu, Kilatini na Kiyunani). Pilato aliweka katika maneno kwa kusudi kwa namna kwamba isiwape hasira viongozi wa Kiyahudi. Mashitaka yanatolewa tofauti tofauti katika injili nne:

Mathayo: "Huyu ndiye Yesu mfalme wa Wayahudi"

Marko: "Mfalme wa Wayahudi" (kama vile Marko 15:26)

Luka: "Huyu ndiye Mfalme wa Wayahudi" (kama vile Luka 23:38)

Yohana: "Yesu Mnazareti, Mfalme wa Wayahudi" (kama vile Yohana 19:19)

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 27:38-44**

<sup>38</sup>Wakati uo huo wanyang'anyi wawili wakasulibiwa pamoja naye, mmoja mkono wake wa kuume, na mmoja mkono wake wa kushoto. <sup>39</sup>Nao waliokuwa wakipita njiani wakamtukana, wakitikisa-tikisa vichwa vyao, wakisema, <sup>40</sup>Ewe mwenye kulivunja hekalu na kulijenga kwa siku tatu, jikoe nafsi yako; ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, shuka msalabani. <sup>41</sup>Kadhalika na wale wakuu wa makuhani wakamdhihaki pamoja na waandishi na wazee, wakisema, Aliokoa wengine, hawezi kujiokoa mwenyewe. <sup>42</sup>Yeye ni mfalme wa Israeli; na ashuke sasa msalabani, nasi tutamwamini. <sup>43</sup>Amemtegemea Mungu; na amwokoe sasa, kama anamtaka; kwa maana alisema, Mimi ni Mwana wa Mungu. <sup>44</sup>Pia wale wanyang'anyi waliosulibiwa pamoja naye walimshutumu vile vile.

**27:38 "wanyang'anyi wawili wakasulibiwa pamoja naye"** Haya ni maelezo kwisa. 53:12. Matumizi ya Josephus ya neno "wanyang'anyi" inamaanisha hawa walikuwa "wafia dini," kama Barabba.

**27:39 "Nao waliokuwa wakipita njiani wakamtukana, wakitikisa-tikisa vichwa vyao"** Haya ni maelezo kwa Zab.22:7. Golgotha lazima ilikuwa karibu na njia kuu kuelekea Yerusalemu. Kusudio la kusulubishwa lilikuwa ni kupunguza uhalifu na mapinduzi.

**27:40 "ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu"** Hii ni sentensi daraja la kwanza yenye masharti ambayo mzungumzaji anadhania kuwa kweli kwa kusudi la kueleweshwa jambo (kama vile Mt. 4:3). Viongozi hawa hawakuwa na mashaka juu ya vile Yesu alivyodai kuwa!

**27:41 "wakuu wa makuhani. . .waandishi na wazee"** Haya yalikuwa maelezo kamili ya Wakuuwa baraza la sinagogi.

**27:43 "Amemtegemea Mungu; na amwokoe sasa, kama anamtaka"** Hii ni nukuu kutoka Zab.22:8. Zaburi hii ya Daudi inaelezea usulubishwaji wa Yesu katika maelezo ya kushangaza.

**27:44** Mathayo anasema kwamba wafia dini waliosulubishwa na Yesu walimtukana kwanza lakini Luka 23:39 inasema ni mhalifu mmoja tu ndiye aliyemkebehi na kumtusi. Ieleweke hii sio pointi ya kuonesha ukinzani bali maelezo ya ujaziliaji. Wote walikuwa na hasira na wasio na heshima hapo mwanzo lakini mmoja akatuli na kutubu.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 27: 45-54**

<sup>45</sup>Basi tangu saa sita palikuwa na giza juu ya nchi yote hata saa tisa. <sup>46</sup>Na kama saa tisa, Yesu akapaza sauti yake kwa nguvu akisema, Eloi, Eloi, lama sabakthani? Yaani, Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha? <sup>47</sup>Na baadhi yao waliohudhuria, waliposikia, walisema, Huyu anamwita Eliya. <sup>48</sup>Mara mmoja wao akaenda mbio, akatwaa sifongo, akaijaza siki, akaitia juu ya mwanzi, akamnyweshwa. <sup>49</sup>Wale wengine wakasema, Acha; na tuone kama Eliya anakuja kumwoko. <sup>50</sup>Naye Yesu akiisha kupaza sauti tena kwa nguvu, akaitoa roho yake. <sup>51</sup>Na tazama, pazia la hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini; nchi ikatetemeka; miamba ikapasuka; <sup>52</sup>makaburi yakafunuka; ikainuka miili mingi ya watakatifu waliolala; <sup>53</sup>nao wakiisha kutoka makaburini mwao, baada ya kufufuka kwake, wakauingia mji mtakatifu, wakawatokea wengi. <sup>54</sup>Basi yule akida, na hao waliokuwa pamoja naye wakimlinda Yesu, walipoliona tetemeko la nchi na mambo yaliyofanyika, wakaogopa sana, wakisema, Hakika huyu alikuwa Mwana wa Mungu.

**27:45 "tangu saa sita. . .hata saa tisa"** Hii inarejerea muda wa Kirumi (yaani, mchana wa saa 6-saa 9). Mara kwa mara ni ngumu kujua na hasa katika injili ya Yohana ikiwa maelezo ya muda yanarejerea muda wa Kirumi. Hapa ni dhahiri.

☐ **"giza"** Giza lilikuwa ni moja la pigo juu ya Misri katika laana za kiagano ikiwa amri za Mungu hazifuatwi (kama vile Kut. 10:21 na kuendelea; Kumb. 28:29; Yoeli 2:10; na Amosi 8:9). Kithiolojia ilikuwa ni uwakilisho wa Mungu

kugeuka mbali na Mwanawe pale aipochukua dhambi za ulimwengu. Huku kutengwa kibinafsi na pia mzigo wa dhambi zote za mwanadamu lilikuwa ni jambo ambalo Yesu aliliogopa kupita kiasi.

**27:46 "Eloi, Eloi, lama sabakthani?"** Yesu anaunganisha maneno ya kiebrania na Kiaramu kutoka Zab. 22:1. Mathayo na Marko (Marko 15:34) vinatumia maneno yenye utofauti kidogo. Mathayo anawafasiria wao kwa wasomaji wao waliozungumza Kiaramu tu. Kutoka Mt. 27:47 ni dhahiri maneno ya Yesu yalieleweka vibaya bna kusanyiko lililokuwa limekusanyika kuangalia usulubishwaji.

☛ **"Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?"** Haya ni maneno ya kwanza ya Zab. 22. Kwa kuyanukuu Yesu alitaka kuurejereza ufahamu wa wasikilizaji wake kwenda katika Zaburi nzima. Yesu alikuwa anapitia kutengwa na Mungu, patio la mwisho kubwa la asili ya dhambi ya mwanadamu (kama vile Gal. 3:13; 2 Kor. 5:21). Hata hivyo, Zaburi pia inaelezea imani katika uaminifu wa YHWH!

**27:47 "Huyu anamwita Eliya"** Eliya alitakiwa awe mtangulizi wa Masihi (kama vile Mal. 4:5). Inawezekana kwamba Kiaramu cha Yesu "*Eloi*" (kama vile Marko 15:34) au Yawezekana "*Eliya*" ilionekana kama jina la nabii.

**27:48**

**NASB, NKJV,**

**NRSV** "sifongo"

**TEV** "mvinyo"

**NJB** "sifongo"

Huu ulikuwa mvinyo wa kawaida wa bei ndogo ambao askari walikunywa. Kutolewa kwa mvinyo huu haikuwa kitendo cha huruma kwa askari bali namna ya kuongeza maumivu ya usulubishwaji. Yesu alichukua kidogo kwenye kinywa chake kwakuwa kinywa Chake kilikuwa kikavu sana kiasi kwamba alikuwa hawezi kuzungumza (kama vile Zab. 22:15). Hii inaweza kuwa kutimilizwa kwa Zab. 69:21

**27:49** Kwa hatua hii tungo ingine inayoongezwa kutoka kwa Yohana 19:34. Haipo katika maandiko ya Kiyunani ya kale ya A, D, K, na maandiko ya Kiyunani ya Origen, Jerome, na Augustine, lakini yapo katika  $\alpha$ , B, C, na L. Ni ngumu kuamua juu ya uasili wake wa kifungu hiki kwasababu (1) inaonekana kuwa kufanywa kwa kuigilizwa kutoka Yohana; (2) Inaonekana kuwa nje ya mfuatano wa kihatua; ila bado (3) ipo katika maandiko kadhaa mazuri. Je Yesu alichomwa mkuki kabla ya Kufa? Toleo la UBS<sup>4</sup> linatoa andiko fupi zaidi alama ya "B" (karibu na hakika). Katika muktadha wa Mathayo, Yesu alikuwa bado hajafa!

**27:50 "Naye Yesu akiisha kupaza sauti tena kwa nguvu"** Linganisha na Yohana 19:30; Zab. 22:15; Luka 23:46; Zab. 31:5.

**27:51 "Na tazama, pazia la hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini"** Hili lilikuwa ni pazia ambalo lilitenganisha Mahali Patakatifu na Patakatifu pa Patakatifu, paitwapo pazia la ndani (kama vile Kut. 26:31-35). Tendo hili la Mungu liliashiria kwamba njia sasa ilikuwa wazi kwa watu wote kumuendea Mungu! Lilichanwa kutokea juu ambacho kiliwakilisha tendo la Mungu kuondoa vikwazo vyote kwenda katika uwepo wake na akajitoa mwenyewe kutosogelea na kupatikana kwa watu wote.

**27:52 "makaburi yakafunuka"** Hilli lilisababisha tetemeko la ardhi (kama vile Mt. 27:54). Hasa wakati gani watu walipata kuwa hai haijulikani. Huku kupea uhai mpya kunaonekana kunganishwa na ufufuo wa Yesu (kama vile Mt. 27:53). Lakini andiko linaonekana kuweka tukio katika kifo cha Yesu. Kuna utata hapa juu ya nani, lini, wapi na kwa nini. Taarifa hii ni ya kipekee kwa Mathayo.

## **MADA MAALUM: WATAKATIFU** (*hagios*)

Huu ni usawa wa Kiyunani wa neno la Kiebrania *kadosh* (NOMINO, BDB 871; KITENZI, BDB 872, KB 1066-1067; tazama Mada Maalum: Takatifu), lililo na maana ya msingi ya kumweka mtu katia usawa, kitu fulani, au baadhi ya sehemu tofauti na matumizi ya YHWH yaliyojitenga. Hili linadokeza dhana ya Kiingereza ya "wekwa wakfu." Israeli lilikuwa "taifa takatifu" la YHWH (kama vile 1 Pet. 2:9, ambayo inanukuu Kut. 19:6). YHWH anaweka mbali na ubinadamu kwa kutumia asili Yake (milele, Utatakatifu usiombwa) na sifa Yake (ukamilifu wa maadili). Yeye ni kipimo ambapo vitu vyote vinapimwa na kuhukumiwa. Yeye yu kila mahali, Mtakatifu, Mtakatifu wa Watakatifu.

Mungu aliwaumba wanadamu kwa ushirika, lakini anguko (Mwanzo 3) lilisababisha kikwazo cha mahusiano na maadili kati ya Mungu Mtakatifu na mwanadamu mdhambi. Mungu alichagua kuurejesha ufahamu Wake wa uumbaji; hivyo, Anawaita watu Wake kuwa "watakatifu" (kama vile Law. 11:44; 19:2; 20:7,26; 21:8). Kwa imani uhusiano wa YHWH na watu Wake ukawa mtakatifu kwa nafasi zao za kiagano ndani Yake, lakini pia wanaitwa kuishi maisha matakatifu (tazama Mada Maalum: Utakaso, kama vile Mt. 5:48; Efe. 4:1,17; 5:2-3,15; 1 Pet. 1:15). Huku kuishi kitakatifu kunawezekana kwa sababu waamini wamekubaliwa kwa utimilifu na kusamehewa kupitia (1) Maisha ya Yesu na (2) kazi na uwepo wa Roho Mtakatifu ndani ya fikra na mioyo yao. Hili linahimarisha hali ya ukinzani kwa waamini:

1. kuwa watakatifu kwa sababu ya haki ya Kristo iliyowekwa ndani yao (kama vile Warumi 4)
2. walioitwa kuishi kitakatifu kwa sababu ya uwepo wa Roho (tazama Mada Maalum: Utakaso)

Waamini ni "watakatifu" (*hagios*) kwa sababu ya

1. mapenzi ya yule Aliye Mtakatifu (Baba, kama vile Yohana 6:29,40; 1 Pet. 1:15-16)
2. kazi ya Mwana aliye Mtakatifu (Yesu, kama vile 2 Kor. 5:21; 1 Pet. 1:18-21)

uwepo wa Roho Mtakatifu akaaye ndani (kama vile Rum. 8:9-11,27)

Mara nyingi katabu cha Agano Jipya kinawarejelea watakatifu kama WINGI (isipokuwa mara moja katika Flp. 4:21, lajini muktadha unalifanya neno hili kuwa WINGI). Kuokolewa ni kuwa sehemu ya familia, mwili, ujenzi! Imani ya kibiblia huanza na mapokezi binafsi, bali suala li ndani ya ushirika wa pamoja. Kila mmoja wetu amekirimiwa kama vile 1 Kor. 12:11) kwa ajili ya afaya, ukuaji, na manufaa ya Mwili wa Kristo—kanisa (kama vikile 1 Kor. 12:7). Tumeokolewa ili kutumika! Utakatifu ni sifa ya familia!

Hili linakuwa adimu kwa waamini (kama vile Matendo ya Mitume 9:13,32,41; 26:10; Rum. 1:7; 1 Kor. 1:2; 2 Kor. 1:1; Efe. 1:1; Flp. 1:1; Kol. 1:2) na njia ya kuonyesha huduma kwa wengine (kama vile Rum. 12:13; 16:2; Efe. 1:15; Kol. 1:4; 1 Tim. 5:10; Ebr. 6:10). Paulo alichukua wakati wa kipekee wa kujitoka kwa makanisa Mataifa kwa watu whitaji waliokuwa ndani ya Kanisa Mama ndani ya Yerusalemu (kama vile Rum. 15:25-26; 1 Kor. 16:1; 2 Kor. 8:4; 9:1).

☐ "waliolala" Kulala ilikuwa ni mbinu ya upunguzaji makali wa maneno juu ya kufa (yaani ilitumika zaidi kwa Wafalme na Mambo ya Nyakati). Hili si andiko linalohibitisha kwa nadharia ya "kulala kwa nafsi." Maandiko lazima yafasiriwe kwa ufahamu wa maana ya maneno kwa wasilizaji/wasomaji wa kwanza!

**27:54**

**NASB, NKJV**

**"Hakika huyu alikuwa Mwana wa Mungu"**

**NRSV**

**"Kiukweli Mtu huyu alikuwa Mwana wa Mungu!"**

**TEV**

**" Hakika huyu alikuwa Mwana wa Mungu!"**

**NJB**

**" Hakika huyu alikuwa Mwana wa Mungu!"**

Hakuna kiambata pale "mwana" inapotumika. Askari huyu alikuwa ameshangzwa sana na yote ambayo yametokea. Anaeleza kwamba Yesu "ni mwana wa Mungu." Hata hivyo, katika ufanano na Luka 23:47 anamtaja

Yesu kama "mwenye haki" au "asiye na hatia." Cha kushangaza ni kwamba askari huyu wa Kirumi aliona kile ambacho vingozi wa Kiyahudi hawakuona (kama vile Mt. 27:19; Yohana 1:11).

Hii kibayana ni "mtu huyu alikuwa mwana wa Mungu." Taswira ya Mungu inarejeshwa kwa mwanadamu! Ushirika wa mahusiano ya karibu zaidi tena unawezekana. Hata hivyo kukosekana kwa kiambata tambulishi hakimaanishi kwamba si huyu anayesemwa (kama vile Mt. 4:3,6; 14:33; 27:43; na Luka 4:3,9). Huyu alikuwa askari wa Kirumi mwenye roho ngumu aliyeimarishwa. Alikuwa ameona wanaume wengi wakifa (kama vile Mt. 27:54). Hii inaweza kuwa "ujumbe kusudiwa" wa Marko kwasababu injili hii hasa iliandikwa kwa Warumi. Injili ya Marko ina maneno mengi ya Kilatini na nukuu chache sana za Agano la Kale. Pia desturi za Kiyahudi na tungo za Kiaramu zinafasiriwa na kuelezewa. Huyu hapa ni akida wa Kirumi akikiri imani kwa mfitinishaji wa Kiyahudi aliyesulubishwa!

Inawezekana kwamba kimakusudi wapitaji wa njiani, wakuu wa makuhani na hata wafungwa wenza walimbeza Yesu lakini akida wa Kirumi anaitikia katika ukiri na mshangao!

### **MADA MAALUMU: MWANA WA MUNGU**

Hii ni moja kati ya nyadhifa kubwa alizopewa Yesu katika Agano Jipya. Ni wazi kabisa ina kidokezo cha Uungu. Inamjumuisha Yesu kama "Mwana" au "Mwana wangu," pia Mungu anaelezewa kama "Baba" (angalia Mada Maalumu: Ubaba wa Mungu). Linatokea mara 124 katika Agano Jipya. Hata usanifu wa Yesu mwenyewe kama "Mwana wa Adamu" ina kidokezo cha Uungu toka Dan. 7:13-14

Katika Agano la Kale usanifu wa neno "Mwana" ingalirejea kwenye makundi maalumu manne (angalia Mada Maalumu: "Wana wa.....")

- A. Malaika (mara nyingi iko katika hali ya WINGI, kama vile Mwa. 6:2; Ay. 1:6; 2:1)
- B. Mfalme wa Israeli (kama vile 2 Sam. 7:14; Zab. 2:7; 89:26-27)
- C. Taifa la Israeli kwa pamoja (kama vile Kut. 4:22-23; Kumb. 14:1; Hos. 11:1; Mal. 2:10)
- D. Waamuzi wa Israeli (kama vile Zab. 82:6)

Ni utumiaji wa mara ya pili ambao unahusianishwa na Yesu. kwa njia hii "Mwana wa Daudi" na "Mwana wa Mungu" semi zote zinahusianishwa na 2 Samwel 17; Zaburi 2 na 89. Katika Agano la Kale neno "Mwana wa Mungu" kamwe halitumiki hasa kwa Masihi, isipokuwa kama ni mfalme wa siku za kiama kama mmoja wa "wapakwa mafuta" wa Israeli. Hata hivyo, katika magombo ya bahari ya chumvi wadhifa unaohusiana na Masihi ni wa kawaida (angalia nukuu maalumu katika *Dictionary of Jesus and the Gospels*, uk. 770). Pia "Mwana wa Mungu" ni wadhifa wa Kimasihi katika miingiliano miwili ya kazi za mafunuo ya Kiyahudi (kama vile II Esdras 7:28; 13:32,37,52; 14:9 na I Enoch 105:2)

Mazingira ya nyuma ya Agano Jipya kama inavyorejereka kwa Yesu kwa uzuri imefupishwa kwa namna mbali mbali.

1. Uwepo wake kabla (kama vile Yohana 1:15-30; 8:56-59; 16:28; 17:5; 2 Kor. 8:9; Flp. 2:6-7; Kol. 1:17; Ebr. 1:3; 10:5-8)
2. Kuzaliwa kwake kwa njia ya pekee (kama vile Isa. 7:14; Mt. 1:23; Luk. 1:31-35)
3. Ubatizo wake (kama vile Mt. 3:17; Mk. 1:11; Luk. 3:22. Sauti ya Mungu toka mbinguni ikiunganisha ufalme wa kifahari wa Zaburi 2 na mtumishi mwenye mateso wa Isaya)
4. Majaribu ya shetani (kama vile Mt. 4:1-11; Mk 1:12,13; Luk 4:1-13. Anajaribiwa kuuwekea mashaka uwana wake au kutimiliza kusudi lake kwa njia tofauti na ile ya msalaba.
5. Uthibitisho wake na wale wakiri wasiokubalika
  - a. Mapepo (kama vile Mk 1:23-25; Luk. 4:31-37,41; Mk. 3:11-12; 5:7; angalia Mada Maalumu: Pepo [roho wachafu])
  - b. Wasioamini (kama vile Mt. 27:43; Mk. 14:61; Yohana 19:7)
6. Uthibitisho wake kupitia wanafunzi wake
  - a. Mt. 14:33; 16:16

- b. Yohana 1:34,49; 6:69; 11:27
- 7. Uthibitisho wake mwenyewe
  - a. Mt. 11:25-27
  - b. Yohana 10:36
- 8. Utumiaji wake wa stiari ya kawaida ya Mungu kama Baba
  - a. Utumiaji wake wa neno *abba* kwa ajili ya Mungu
    - 1) Mk. 14:36
    - 2) Rum. 8:15
    - 3) Gal. 4:6
  - b. Utumiaji wake wa sasa wa jina Baba (*patēr*) kuelezea uhusiano wake na Uungu.

Kwa ufupi, wadhifa wa neno "Mwana wa Mungu" una maana kubwa ya kithiolojia kwa wale waliolifahamu Agano la Kale na ahadi zake, lakini waandishi wa Agano Jipya waliogopeshwa kuhusu utumiaji wao na watu wa mataifa kwa sababu ya mazingira ya nyuma ya wapagani ya "miungu" ikiwachukulia wanawake na matokea ya watoto kuwa "majitu."

#### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 27:55-56

<sup>55</sup>Palikuwa na wanawake wengi pale wakitazama kwa mbali, hao ndio waliomfuata Yesu toka Galilaya, na kumtumikia. <sup>56</sup>Miongoni mwao alikuwamo Mariamu Magdalene, na Mariamu mama yao Yakobo na Yusufu, na mama yao wana wa Zebedayo.

**27:55 "wanawake wengi"** Marko 15:40 ina orodha inayofanana. Wanawake hawa walikuwa wakisafiri na waliokuwa wakifuatana na Yesu na Kumi na Mbili. Wanaweza kuwa hata walimuunga mkono Yesu na Wanafunzi kifedha na pia kuwapikia na kukutana na mahitaji ya wanawake wengine ambao Yesu na Mitume walwahudumia. Angalia Mada Maalum inayofuata.

#### MADA MAALUM: WANAWAKE WALIOFUATANA NA YESU NA WANAFUNZI WAKE

##### Mathayo 27:55-56

Maria Magdalene  
Mariamu, mama yao  
Yakobo na Yusufu  
Mama wa wana  
wa Zebedayo (Yakobo na  
Yohana)

##### Marko 15:40-41

Maria Magdalene  
Mariamu, mama wa  
Yakobo Mdogo na, Yose  
Salome

##### Luka 8:2-3; 23:49

Maria Magdalene  
Yoana, mkewe Kuza  
(wakili wa Herode)  
Susana na wengine wengi

##### Yohana 19:25

Mariamu, mama wa Yesu  
Umbu la mamaye  
Mariamu, wa Klopa

Mariamu Magdalene

Yafuatayo ni maelezo yahusuyo hawa wanawake kutokana na maoni yangu kuhusu Marko 15:40-41: "Palikuwepo na wanawake wakitazama kwa mbali." Kundi la kimitume lilisaidiwa na wanawake kadhaa wanawake waliohudumia kwa vyote kiuchumi na kimwili (yaani, kupika, kusafisha, nk. Kama vile Marko 15:41; Mt. 27:55; Luka 8:3).

"Mariamu Magdalene." Magdala ulikuwa mji mdogo katika fukwe za Bahari ya Galilaya, umbali wa maili tatu kaskazini mwa Tiberia. Mariamu alimfuata Yesu kutoka Galilaya baada ya Yeye kumkomboa kutoka katika pepo kadhaa waliokuwa wachafu (kama vile Luka 8:2). Pasipokuwa na usawa huyu alitambuliwa kama kahaba lakini hakuna ushahidi wa Agano Jipya wa jambo hili.

"Mariamu, mama yao Yakobo na Yusufu." Katika Mt. 27:56 huyu anaitwa "mama yao Yakobo na Yusufu." Katika Mt. 28:1 huyu anaitwa "Mariamu yule wa pili." Swali la muhimu ni hili, huyu alikuwa mke wa nani? Katika Yohana 19:25 bila shaka huyu alikuwa mke wa Klopa, bado mwanaye Yakobo, aliyesemekana kuwa "mwana wa Alfayo" (kama vile Mt. 10:3; Marko 3:18; Luka 6:15).

"Salome." Huyu alikuwa mama wa Yakobo na Yohana, ambao walikuwa sehemu ya mzunguko wa ndani wa mwanafunzi wa Yesu, na mke wa Zebedayo (kama vile Mt. 27:56; Marko 15:40; 16:1-2).

Yafuatayo ni maelezo yangu kuhusu wanawake hawa kutokana na maoni yangu ya Yohana 19:25:  
"Na penye msalaba wake Yesu walikua wamesimama mamaye, na umbu la mamaye, Mariamu wa Klopa, na Mariamu Magdalene" Kuna mjadala mwingi kuhusu kwa vyovyote kuna majina mane hapa au majina matatu. Inawezekana kwamba kuna majina matatu kwa sababu hapawezi kuwa na maumbu mawili wanaoitwa Mariamu. Umbu la Mariamu, Salome, limetajwa katika Marko 15:40 na Mt. 27:56. Ikiwa ndivyo ilivyo, hii ingemaanisha Yakobo, Yohana na Yesu walikuwa jamaa wa karibu. Karne ya pili ya desturi (Hegesippus) inasema kwamba Klopas alikuwa ndugu wa Yusufu. Mariamu wa Magdala alikuwa mmoja wa wale ambao Yesu aliwaondolea pepo saba, na wa kwanza aliyemchagua kujionyesha kwake baada ya ubatizo Wake (kama vile Yohana 20:1-2; 11-18; Marko 16:1; Luka 24:1-10).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini wakuu wa sinagogi walienda kwa Pilato? Kwanini hawakutaka kumuua Yesu kwa kumpiga mawe?
2. Ni kwa namna gani toba ya Yuda ni tofauti na ya Petro?
3. Kwanini Pilato alijaribu kumuachilia Yesu?
4. Nini makusudi ya kutafuta maelezo mengi ya Agano la Kale juu ya kifo cha Kristo?
5. Kwanini kuligeuka giza wakati Yesu alipowa pale msalabani? Kwanini Yesu alijiona kuwa ameachwa?
6. Orodhesha ishara ambazo zilifuatia baada ya Kifo cha Yesu. Nini yalikuwa makusudi yake?

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO (Muktadha unajumuisha 27:57-28:20)

(Ufanano wa Injili Hii ni Marko 15:42-16:8, Luka 23:50-24:12, Yohana 19:30-20:10)

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 27:57-61

<sup>57</sup>Hata ilipokuwa jioni akafika mtu tajiri wa Arimathaya, jina lake Yusufu, naye mwenyewe alikuwa mwanafunzi wa Yesu; <sup>58</sup>mtu huyu alimwendea Pilato akauomba mwili wa Yesu. Ndipo Pilato akaamuru apewe. <sup>59</sup>Yusufu akautwaa mwili, akauzonga-zonga katika sanda ya kitani safi, <sup>60</sup>akauweka katika kaburi lake jipya, alilokuwa amelichonga mwambani; akavingirisha jiwe kubwa mbele ya mlango wa kaburi, akaenda zake. <sup>61</sup>Na pale walikuwapo Mariamu Magdalene, na Mariamu yule wa pili, wameketi kulielekea kaburi.

**27:57 "ilipokuwa jioni"** Tungo hii inamaanisha ilikuwa mwanzo wa Pasaka ambayo ilianza saa 12 asubuhi au mapambazukoni. Wayahudi walikuwa na jioni mbili. Ya kwanza saa 9 na ya pili saa 12 jioni ambapo wanaanza siku nyingine mpya.

☛ **"mtu tajiri wa Arimathaya, jina lake Yusufu"** vifungu kadhaa vinamuelezea mtu huyu.

1. alikuwa mtu tajiri na mwanafunzi wa Yesu (kama vile Mt. 27:57)
2. Alikuwa mshirika mwenye kuheshimiwa sana wa baraza la wazee wa sinagogi (kama vile Marko 15:43)



3. alikuwa mtu mwema na mtauwa (kama vile Luka 23:50)
4. alikuwa mwanafunzi wa siri wa Yesu kwa hofu ya Wayahudi (kama vile Yohana 19:38)

**27:57-58** Hiki kilikuwa ni kitendo cha ujasiri kwasababu kadhaa.

1. Alikuwa akijitambulisha hadharani kuwa na ushirika na mtu aliyehukumiwa kwa uhaini
2. alikuwa tayari kuwa najisi kwa asiku ya Pasaka
3. kitendo hiki kiukweli kingemuongdoa katika baraza la wazee wa sinagogi

**27:59** Yusufu alienda haraka kuandaa mwili kabla ya saa 12 jioni ambapo Pasaka ingeanza. Muda halisi kabisa wa kuviringishwa jiwe pale kaburini hakujulikani. Ilikuwa kabla ya saa 12 jioni. Haijalishi kwa haraka kiasi gani, ilihesabiwa kama siku moja katika siku tatu ambazo Yesu alikuwa kaburini.

**27:60 "akauweka katika kaburi lake jipya, alilokuwa amelichonga mwambani"** Huku ni kutimilizwa kwa unabii wa Isa. 53:9.

**27:61 "Mariamu Magdalene"** Angalia Mt. 27:55-56 kwa orodha ya wanawake watatu.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 27:62-66**

<sup>62</sup>Hata siku ya pili, ndiyo iliyo baada ya Maandalio, wakuu wa makuhani, na Mafarisayo wakamkusanyikia Pilato, <sup>63</sup>wakasema, Bwana, tumekumbuka kwamba yule mjanja alisema, alipokuwa akali hai, Baada ya siku tatu nitafufuka. <sup>64</sup>Basi amuru kwamba kaburi lilindwe salama hata siku ya tatu; wasije wanafunzi wake wakamwiba, na kuwaambia watu, Amefufuka katika wafu; na udanganyifu wa mwisho utapita ule wa kwanza. <sup>65</sup>Pilato akawaambia, Mna askari; nendeni mkalilinde salama kadiri mjuavyo. <sup>66</sup>Wakaenda, wakalilinda kaburi salama, kwa kulitia lile jiwe muhuri, pamoja na wale askari walinzi.

**27:62-66** Hii hadithi ni ya kipekee kwa Mathayo (kama vile Mt. 28:2-4,11-15).

**27:62 "Hata siku ya pili, ndiyo iliyo baada ya Maandalio"**Hii kwa dhahiri ni rejea juu ya Sabato. Kwa kuwa katika uwepo wa Pilato na mahakama kungewafanya viongozi wa Kiyahudi najisi na hivyo kushindwa kushiriki katika Pasaka. Tendo hili linaonyesha ni kwa kiasi gani walikuwa wamejaa hofu juu ya Yesu na Nguvu zake na utabiri wake.

☐**"wakuu wa makuhani, na Mafarisayo wakamkusanyikia"** Hii inashangaza (1) kwamba walikusanyika; (2) kwamba ilikuwa ni Wiki ya Sabato ya Pasaka; (3) kwamba Masadukayo hata hawakuamini katika ufufuo; na (4) walikuwa wenye nguvu licha ya kutokuwa tayari kuwa mashuhda kwa ufufuo!

**27:63** Inashangaza kwamba Pilato anaitwa *Kurie* (ikitafsiriwa kama "mheshimiwa") na viongozi hawa wa Kiyahudi na Yesu, Bwana anaitwa "yule muongo."

NASB, NKJV	"yule muongo"
NRSV, NJB	"yule mpotoshaji"
TEV	"yule muongo"

Neno hili (*planos*) linaweza kibayana likatafsiriwa kama "mtangaji,"likielezea mgeuzo wa maneno yetu ya kiingezewa "sayari" kutoka katika neno lile lile "kutanga tanga" mianga ya anga. Kiasili ilirejeea mzunguko wa sayari ambao haukufuata utaratibu wa kawaida wa mfumo wa sayari zingine. Ilikuwa na maana hasi katika Kiyunani. Lilitumika juu ya watenda makosa au waongo.

NASB	"Baada ya siku tatu nitafufuka"
NKJV	"Baada ya siku tatu nitafufuka"

Kibayana, "baada ya siku tatu nitafufuliwa." Hii ni kauli tendwa ya wakati uliopo. Mukatadha unamaanisha kwamba Pilato aliwapa jukumu askari wa Kirumi kulinda kaburi. Viongozi wa Kiyahudi walijua juu ya utabiri wa Yesu (kama vile Mt.12:40; 16:4) na waliogopa. Wanafunzi walishangazwa na ufufuo-mshangao wa namna gani huu!

## MADA MAALUM: UFUFUO

Katika Biblia hali ya kulejeshwa toka mautini ina maana tatu.

- A. Wale wote ambao hawakufa lakini wakaenda kukaa pamoja na Mungu (yaani., Enoko, kama vile Mwa. 5:24; Eliya, kama vile 2 Fal.. 2:11), ambao huitwa "utafasiri."
- B. Baadhi, kupitia nguvu ya Mungu, hurejeshwa toka kwenye lango la mauti hadi kuwa na uhai. Hii huitwa "kurudi uzimani." Watakufa kwa kiasi Fulani huko mbeleni.
- C. Pamekuwepo na ufufuo mmoja tu (yaani., Yesu). Alikufa lakini akafufuka toka katika wafu (yaani., *kuzimu*) na kupewa mwili mpya ulioandaliwa kwa ajili ya uzima wa milele wakiwa na Mungu (kama vile 1 Kor. 15:20,23; "mzaliwa wa kwanza katika wafu," kama vile Kol. 1:15,17). Kwa sababu ya Yeye, waamini watafufuliwa kwenye ujio wake wa pili (kama vile Zab. 49:15; 73:24; Isa. 26:19; Dan. 12:2; Mt. 22:31-32; Marko 12:26-27; Yohana 5:25,28-29; 6:39-40,44,54; Rum. 8:11; 1 Wakorintho 15; 1 The. 4:13-18; 1 Yohana 3:2).

Ushuhuda kwa ajili ya ufufuo

- A. Baada ya siku (50) baadaye kwenye Pentekoste, ufufuko ukajakuwa ujumbe muhimu wa hotuba za Petro (kama vile Matendo 2). Maelfu walioishi kwenye maeneo tukio lilipotokea waliamini!
- B. Maisha ya wanafunzi yalibadilika moja kwa moja toka kwenye kukatishwa tamaa (hawakutarajia ufufuko) kwa ujasiri, hata kifo.
- C. Paulo anaorodhesha mashuhuda wa macho katika 1 Kor. 15:5-8, ikimjumuisha yeye mwenyewe (kama vile Matendo 9).

Umuhimu wa ufufuo

- A. Inavyoonyesha Yesu alikuwa ni waliyedai ndiye (kama vile Mt. 12:38-40, utabiri wa kifo na ufufuo)
- B. Mungu aliweka kibali chake juu ya maisha ya Yesu, mafundisho, na kifo mbadala! (kama vile Rum. 4:25)
- C. Inatonyesha ahadi kwa Wakristo wote (yaani., ufufuko wa miili, kama vile 1 Wakorintho 15)

Madai ya Yesu kuwa atafufuka kutoka katika wafu

- A. Mt. 12:38-40; 16:21; 17:9,22, 23; 20:18-19; 26:32; 27:63
- B. Marko 8:31; 9:1-10,31; 14:28,58
- C. Luka 9:22-27
- D. Yohana 2:19-22; 12:34; sura ya 14-16

Wote Petro na Paulo wanadai kuwa Zaburi 16 inamrejelea Yesu, Masihi

- A. Petro katika Matendo 2:24-32
- B. Paulo katika Matendo 13:32-37

Usomaji zaidi

- A. *Evidence That Demands a Verdict* by Josh McDowell
- B. *Who Moved the Stone?* by Frank Morrison
- C. *The Zondervan Pictorial Encyclopedia of the Bible*, "Resurrection," "Resurrection of Jesus Christ"

**27:65 "Mna askari"** Hii ni nahau (yaani shurutishi sio elekezi) kwa ruhusa ya ujumbe wa kiyahudi kwenda kwa askari wa Kirumi kulinda kaburi.

☐ **"nendeni mkalilinde salama kadiri mjuavyo"** "nendeni" ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo inayofuatiwa na kauli shurutishi ya kati (yenye ushahidi) ya wakati uliopita usio timilifu. Kuna kiasi cha kejeli hapa (yaani "kadiri

mjuavyo"). Viongozi hawa wa kikuhani hawakuwa marafiki wa Pilato lakini walishirikishana shauku ya kusaidiana na kufaana kisiasa.

**27:66 "Wakaenda"** Hii inarejerea wawakilishi wa uongozi wa Kiyahudi na askari wa Kirumi. Viongozi hawa hata yawezekana walihakikisha kaburi lilikuwa limefunikwa na kulindwa! Wawakilishi wao hata wanaweza kuwa wamesaida kulifunika kaburi wao wenyewe!

Tungo "Mungu aliye hai" ni mbinu ya utumizi wa maneno juu ya jina la YHWH (kama vile Kut. 3:14; Zab. 42:2; 84:2; Mt. 16:16). Matumizi ya maneno mara kwa mara kunapatikana katika viapo vya kibiblia, "kadiri Bwana Aishivyo."

☑️**"wakalilinda kaburi salama"** Hii inarejerea kufunga rasmi ambako kulitumia makopo ya nta kuweka katika mzunguko wa jiwe n kuta za kaburi kwa kugongwa muhuri wa Kirumi ikiawa na vikamba kati yake.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je Yusufu Armathaya alikuwepo siku ya usiku wa mashitaka?
2. Kwanini Pilato alikuwa anakusudia kuona miili imetupwa?
3. Orodhesha utabiri wa nabii katika sehemu hii.
4. Ni kazi gani wanawake waliomfuatana na kundi la Kitume walifanya?
5. Elezea mambo ya kushangaza ya Mt. 27:64 na kejeli ya Mt. 27:65.

## MATHAYO 28

MIGAWANYO YA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA				
UBS <sup>4</sup>	NKJV	NRSV	TEV	NJB
Ufufuo wa Yesu 28:1-10	Amefufuka 28:1-8  Wanawake Wanamwabudu Bwana aliyefufuka 28:9-10	Pasaka ya kwanza 28:1-10	Ufufuo 28:1-4 28:5-7 28:8  28:9-10	Kaburi tupu:Ujumbe Wa malaika 28:1-8  Kujitokeza mbele ya wanawake 28:9-10
Taarifa ya walinzi 28:11-15	Walinzi wapewa Rushwa 28:11-15	Rushwa kwa walinzi 28:11-15	Taarifa ya walinzi 28:11-15 28:15	Tahadhali inatolewa na viongozi wa watu 28:11-15
Maagizo kwa Wanafunzi 28:16-20	Agizo kuu 28:16-20	Agizo la Yesu kwa wanafunzi wake 28:16-20	Yesu anajitokeza kwa wanafunzi wake 28:16-20	Kujitokeza Galilaya; Agizo kuu kwa ulimwengu 28:16-20

### MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka [“Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia”](#))

#### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

### USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

#### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 28:1-7

<sup>1</sup> Hata sabato ilipokwisha, ikipambazuka siku ya kwanza ya juma, Mariamu Magdalene, na Mariamu yule wa pili, walikwenda kulitazama kaburi. <sup>2</sup> Na tazama, palikuwa na tetemeko kubwa la nchi; kwa sababu malaika wa Bwana alishuka kutoka mbinguni, akaja akalivingirisha lile jive akalikalia. <sup>3</sup> Na sura yake ilikuwa kama umeme, na mavazi yake meupe kama theluji. <sup>4</sup> Na kwa kumwogopa, wale walinzi wakatetemeka, wakawa kama wafu. <sup>5</sup> Malaika akajibu, akawaambia wale wanawake, Msiogope ninyi; kwa maana najua ya kuwa mnamtafuta Yesu aliyesulibiwa. <sup>6</sup> Hayupo hapa; kwani amefufuka kama alivyosema. Njoni, mpatazame mahali alipolazwa. <sup>7</sup> Nanyi nendeni upesi, mkawaambie wanafunzi wake, Amefufuka katika wafu. Tazama, awatangulia kwenda Galilaya; ndiko mtakakomwona. Haya, nimekwisha waambia.

**28:1 "Hata sabato ilipokwisha"** tungo hii ya Kigiriki inarejelea kuzama kwa jua siku ya Jumamosi (kama vile Toleo la Vulgate "jioni ya Sabato"). Kwenye Marko tungo ya Kigiriki inarejelea mapambazuko ya siku Jumapili. Kuna utata mwingi kwenye utaratibu wa kupanga miaka na matukio ya juma la mwisho la maisha ya Yesu, hasa matukio yanazunguka ufufuo. Limetajwa neno "mapambazuko" kwamba mmoja anafikilia kwamba inarejelea yumkini kwa nyakati za Warumi, sio nyakati za Kiyahudi. Kuna mifano miwili iliyotumika kwenye injili.

☐ **"Mariamu Magdalene, na Mariamu Yule wa pili"** zote Marko 16:1 na Luka 24:10 wametajwa wanawake wengine, ambapo Yn. 20:1 ametajwa Mariamu Magdalene pekee.

**28:2 "palikuwa na tetemeko kubwa la nchi; kwa sababu malaika wa Bwana alishuka kutoka mbinguni, akaja akalivingirisha lile jiwe"** hii ni ya pekee kwa Mathayo. Maelezo mawili kwa ajili ya jinsi gani jiwe liliondolewa na kuwekwa pembeni. Ni lazima kulikuwa na matetemeko makubwa mawili (1) moja wakati wa kifo cha Yesu kwenye Mt.27:54, na (2) na lingine la kuondoa jiwe na kuwaruhusu wafuasi wa Yesu kuingia ndani ya kaburi tupu. Tazama muhtasari "malaika wa Bwana" katika Mt. 1:20.

**28:3 "Na sura yake ilikuwa kama umeme"** hii inarejelea kwa malaika ambaye huvaa nguo ya kitani, kielelezo cha utakatifu. Luka 24:4 na Yn 20:12 wametajwa malaika wawili. Aina hii mbalimbali kati mmoja au watu wawili au malaika imezoeleka miongoni mwa injili, lakini idadi imerudishwa, kwa kawaida ni injili ya Mathayo kwamba ina "mbili." Mifano mingine ni: (1) mgerasi mwenye pepo mchafu (Marko 5:1; Luka 8:26) na pepo wachafu wawili (Mat. 8:28); na (2) mwanaume kipofu (Marko 10:46; Luka 18:35) na vipofu wawili (Mt. 20:30).

**28:5 "Msiogope ninyi"** huu ni ukweli wa wazi ambao Yesu aliwaambia kwenye mstari wa 10. Yalikua ni maelezo ambayo nguvu za utawala wa kimungu zilivunja asili.

1. maneno ya Yesu kwenye Mt. 14:27; 17:7; 28:10; Marko 6:50; Luka 5:10; 12:32; Yn. 6:20; Ufu. 1:17
2. malaika kwenye Mt. 28:5; Luka 1:13, 30; 2:10

**28:6 "amefufuka"** katika muktadha huu ukubalifu wa Baba na uthibitisho wa maneno ya mwana na kazi unaelezewa katika matukio makuu mawili.

1. ufufuo wa Yesu kutoka kwa wafu
2. kupaa kwa Yesu na kuketi mkono wa kuume wa Baba

Tazama [MADA MAALUM: UTUKUFU \(DOXA\)](#) katika Marko 10:37b.

**28:7 "awatangulia kwenda Galilaya"** Yesu alikuwa amewaambia ya kuwa atakutana nao kwenye mlima huko Galilaya (kama vile Mt. 26:32, 28:7, 10; 1 Kor. 15:6). Hii ni njia ya kuutetea ufufuo wake na kuwapatia matumaini. Alikuwa na ujumbe wa mwisho kwa ajili yao (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8).

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATHAYO 28:8-10**

<sup>8</sup> Wakaondoka upesi kutoka kaburini, kwa hofu na furaha nyingi, wakaenda mbio kuwapasha wanafunzi wake habari. <sup>9</sup> Na tazama, Yesu akakutana nao, akisema, Salamu! Wakakaribia wakamshika miguu, wakamsujudia. <sup>10</sup> Kisha Yesu akawaambia, Msiogope; enendeni, mkawaambie ndugu zangu waende Galilaya, ndiko watakakoniona.

**28:8** Hofu na furaha nyingi unaelezewa kama mwanzo wa ufufuo wa kukabiliana wa maadui. Utawala wa kiroho unaovunja ukweli wa kimwili pia unasababisha hofu (ambao unapaswa kusimamishwa, kama vile Mt. 28:10, lakini furaha kuu itaendelea), lakini wakati huu ulikua ni ujumbe wa ufufuo wa Kristo ambao huleta "furaha nyingi" nab ado unaendelea kufanya hivyo!

Walienda mbio ili kupasha habari. Hii ni nguvu sawa na ile ya kama Mt. 28:19-20. Ni lazima wafuasi waende na kupasha habari!

28:9	
NASB	"Salamu"
NKJV	"wakafurahi"
NRSV, NJB	"salamu"
TEV	"amani iwe kwenu"

Hii ilikua ni salamu iliyozoeleka kwa Yesu. Linatokana na neno linalomaanisha "furahi."

### MADA MAALUMU: KUONEKANA KWA YESU BAADA YA UFUFUO

Yesu alijionesha kwa watu kadhaa kuthibitisha kufufuka kwake.

1. Wanawake kaburini, Mt. 28:9
2. Wanafunzi kumi na moja kwenye mkutano ulioandaliwa Galilaya, Mt. 28:16
3. Simoni, Luka 24:34
4. Wale wawili njiani kuelekea Emau, Luka 24:15
5. Wanafunzi gorofani, Luka 24:36
6. Maria Magdalena, Yohana 20:15
7. Wanafunzi kumi ghorofani, Yohana 20:20
8. Wanafunzi kumi na moja ghorofani, Yohana 20:26
9. Wanafunzi saba kwenye bahari ya Galilaya, Yohana 21:1
10. Kefa (Petro), 1 Kor. 15:5
11. (Mitume) kumi na wawili, 1 Kor. 15:5
12. Ndugu 500, 1 Kor. 15:6 pamoja na mathayo Mt. 28:16-17
13. Yakobo (mtu wa familia yake), 1 Kor. 15:7
14. Mitume wote, 1 Kor. 15:7
15. Paulo, 1 Kor. 15:8 (Matendo 9)

Bila shaka baadhi ya haya mengine yanarejelea kuonekana kulekule. Yesu alitaka wao wajue kwa hakika kwamba alikuwa hai!

☐ **"waka"** inaelezea sifa, Marko na Luka anatajwa mwanamke mmoja, ambapo Mathayo anataja wawili.

☐ **"wakamshika miguu"** Yn. 20:17 imeandikwa Maria peke yake alimshika Yesu miguu yake. Hii ni njia ya kawaida ya kuonyesha unyenyekevu, heshima, na hata kuabudu.

**28:10 "ndugu zangu"** Ni jina gani kwa ajili ya hawa wanafunzi wenye hofu (kama vile Mt. 12:15)!

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 28:11-15

<sup>11</sup> Nao wale walipokuwa wakienda, tazama, baadhi ya askari waliingia mjini, wakawapasha wakuu wa makuhani habari za mambo yote yaliyotendeka. <sup>12</sup> Wakakusanyika pamoja na wazee, wakafanya shauri, wakawapa askari fedha nyingi, <sup>13</sup> wakisema, Semeni, ya kwamba wanafunzi wake walikuja usiku, wakamwiba, sisi tulipokuwa tumelala. <sup>14</sup> Na neno hili likisikilikana kwa liwali, sisi tutasema naye, nanyi tutawaondolea wasiwasi. <sup>15</sup> Basi wakazitwaa zile fedha, wakafanya kama walivyofundishwa. Na neno hilo likaenea kati ya Wayahudi hata leo.

**28:11** inashangaza kwamba walenzi wa Kirumi wanawapasha habari makuhani wa Kiyahudi! Baadhi ya haya lazima Mathayo ameyasema!

**28:12 "wakawapa askari fedha nyingi"** ni nini ambacho hawa maaskari walifikilia, kuujuu ukweli na kusema uongo!

Hawa viongozi wa Kiyahudi (yaani, baraza kuu la wayahudi) walitenda kila kinachowezezana kumuangamiza Yesu. Wali

1. walitumia usaliti kumpata na kumkamata Yesu
2. walimshikilia usiku kinyume cha sheria kwa kumshitaki
3. walitumia mashahidi wa uongo ili kumshitaki
4. mwishowe wakatumia rushwa kuwanyamazisha mashahidi

**28:13 "wanafunzi wake walikuja usiku, wakamwiba, sisi tulipokuwa tumelala"** ikiwa walikua wamelala, walitambua kuwa wanafunzi wake waliuiba mwili wake? Hata hivyo, jambo hili linatiliwa mkazo kwamba kwa taarifa ya maaskari wa Kirumi, wanawake, na wanafunzi, kaburi lilikua tupu.

**28:14 "nanyi tutawaondolea wasiwasi "** maaskari wa Kirumi kulala mahali pa kazi ilikua ni kosa kubwa, na wakati mwingine adhabu yake ni kifo.

**28:15 "neni hilo likaenea kati ya Wayahudi hata leo"** kumbuka kwamba Mathayo alikua anaandika kwa ajili ya wasikilizaji wa kiyahudi. Jambo linalofanana lilitolewa kwenye ushahidi wa Justin (114-115 B.K) *Dialogue with Trytho* (yaani, 108). Walikua ni Masadukayo na Warumi walizuia mwili wa Yesu usiibiwe.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATHAYO 28:16-20**

<sup>16</sup> Na wale wanafunzi kumi na mmoja wakaenda Galilaya mpaka mlima ule aliowaagiza Yesu. <sup>17</sup> Nao walipomwona, walimsujudia; lakini baadhi yao waliona shaka. <sup>18</sup> Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. <sup>19</sup> Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; <sup>20</sup> na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.

**28:16 "Na wale wanafunzi kumi na mmoja wakaenda Galilaya mpaka mlima ule aliowaagiza Yesu"** Yesu alikua amekwisha waeleza wanafunzi mapema (kama vile Mt. 26:32; 27:7,10) kwamba atakutana nao hapo. Ikiwa wangemsikiliza kwa makini wangetarajia ufufuo, lakini hawakufanya hivyo. Huu haukua mlima ule aliotumia kupaa. Kupaa kwa Yesu kulitokea katika mlima wa Mizeituni siku arobaini baada ya kufufuka (kama vile. Luka 24:50-51; Mdo. 1:4-11).

**28:17**

<b>NASB</b>	"lakini baadhi yao waliona shaka"
<b>NKJV, NRSV</b>	"lakini baadhi waliona mashaka"
<b>TEV</b>	"baadhi yao walikua na mashaka"
<b>NJB</b>	"baadhi walikua na wasiwasi"

Hii hairejelei kwa wanafunzi 120 waliomwona mara tatu huko Yerusalemu kwenye ghorofa. Inawezekana inarejelea idadi kubwa ya wafuasi (zaidi ya 500) ambao Paulo amewataja kwenye 1 Kor. 15:6. Ni dhahili Yesu alijitokeza kwa umbali na kutembea akiwakaribia. Kulikuwa na baadhi ya utofauti wa kimwili wa mwonekano wa Yesu baada ya kufufuka (kama vile Yn. 20:14; 21:4; Luka 24:13,31).

Umuhimu wa hili ni kwamba agizo kuu hawakupewa mitume pekee, wala sio wanafunzi mia moja na ishirini wa ghorofani, lakini kwa kanisa zima. Ni kwa ajili ya Wakristo wote, na sio kwa uongozi wa kanisa! Lilitolewa kidogo kwa maeneo matatu tofauti.

1. ghorofani, jioni ya ufufuo (kama vile Luka 24:46-47; Yn. 20:21)
2. kwenye mlima huko Galilaya (kama vile Mathayo 28)
3. kwenye mlima wa Mizeitumi kabla ya kupaa (kama vile Mdo 1:8).

**28:18 "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani"** haya ni maelezo ya kushangaza (kama vile Mt. 11:27; Luka 10:22; Yn. 3:35; 13:3; Efe. 1:20-22; Kol. 1:16-19; 2:10; 1 Pet. 3:22)! Yesu ni lazima awe Masihi au mwongo. Ufufuo wake unathibitisha madai yake!

**28:19 "enendeni"** hii ni kauli tendwa (shahidi wa maandishi) endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu iliyotumika kama shurutishi. Hii haitafsiriwi "kama ukienda" kwasababu hii inaweza kutafsiriwa kama kauli shurutishi ya wakati uliopo, sio wakati uliopita usiotimilifu. "Nendeni" yumkini ikawa ni chaguzi sahihi zaidi. Wakristo wote wanaamuriwa kuishi maisha yenye ushahidi (kama vile. 1 Pet. 3:15 na inawezekana Kol. 4:2-6). Ni kipaumbele. Hili ni agizo kuu-sio uchaguzi mkuu.

☐ **"mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi"** hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu. Neno "wanafunzi" linamaanisha "wanaojifunza." Biblia haitilii mkazo maamuzi, lakini maisha ya imani. Ufunguo wa uinjilisti ni uanafunzi. Hata hivyo, uanafunzi ni lazima uanze na kazi ya imani ya kutubu na kuendelea kwenye njia ile ile ya utiifu na uvumilivu.

☐ **"mataifa yote"** haya maelezo ni lazima yaliwashangaza wayahudi, lakini kufuatana na Dan. 7:14 ambayo inaongelea ulimwengu, ufalme wa milele (Ufunuo 5). Haya ni marudio ya nyuma ya maagizo ya Yesu (kama vile. Mat. 10:5-6). Tambua idadi ya nyakati ambazo zimehusishwa "wote" zimejitokeza kwenye kifungu hiki. Tazama [MADA MAALUM: MPANGO WA UKOMBOZI WA MILELE WA YHWH](#) katika Mt. 24:14.

☐ **"mkiwabatiza"** hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo iliyotumika kama shurutishi. Huu ni uwiano na "fundisha" (mstr.20). Makusudi mawili ya kanisa ni uinjilisti na uanafunzi. Ni pande mbili katika sarafu moja. Hayawezi kamwe kutenganishwa!

## **MADA MAALUM: UBATIZO**

- I. Ubatizo katika maisha ya Kiyahudi
- II. Ubatizo ulikuwa utaratibu wa kawaida miongoni mwa Wayahudi wa karne ya kwanza na ya pili.
  1. maandalizi ya kuabudu hekaluni (yaani, utaratibu wa kujitakasa)
  2. ubatizo wa kujibatiza mwenyewe kwa kubadili dini  
Ikiwa mtu aikuwa na histori ya kuwa mtu wa Mataifa ilimlazimu kuwa mtoto kamili wa Israeli, huyu ilimpasa kutimiza majukumu matatu:
    - a. tohara, ikiwa ni mwanamume
    - b. kujibatiza mwenyewe kwa kuzama majini, katika uwepo wa mashahidi watatu
    - c. dhabihu ndani ya Hekalu
  3. Tendo la utakaso (kama vile Mambo ya Walawi 15)  
Makundi ya kimadhehebu ya karne ya kwanza ya ki- Palestina, kama vile Essene, kwa uwazi kabisa ubatizo lilikuwa jambo la kawaida, zoezi lililorudiwa rudiwa. Hata hivyo, kuipa kipaumbele dini ya Kiyahudi, Ubatizo wa Yohana wa toba ungeweza kuwa wa kumnyenyekeza mtoto wa asili kuyafanya Mataifa kuzikubali taratibu hizi.
    1. baadhi ya vigezo vya kitabu cha Agano la kale vinavyoweza kunukuliwa vinaweza kuonekana kupitia sikuu ya kutawazwa
    2. Kama taratibu zilivyofanywa na makuhani kwa ukawaida (kama vile Kutoka 19:10; Mambo ya Walawi 16)  
Lazima itambuliwe kwamba batizo nyingine zote katika karne ya kwanza ya utamaduni wa Kiyahudi zilikuwa ni za kujijendesha zenyewe. Wito pekee wa Yohana Mbatizaji kwa ajili ya ubatizo ndiyo uliomhusisha yeye kama mtathimini (kama vile Mt. 3:7-12) na mwendeshaji wa tendo hili la toba (kama vile Mt. 3:6).
- III. Ubatizo ndani ya Kanisa
  - A. Sababu za Kithiolojia
    1. msamaha wa dhambi – ya Mitume 2:38; 22:16
    2. upokeaji wa Roho Mtakatifu – Matendo ya Mitume 2:38 (Matendo ya Mitume 10:44-48)



3. ushirika pamoja na Kristo – Gal. 3:26-27
  4. ushirika ndani ya kanisa – 1 Kor. 12:13
  5. dalili za kurudi kwa roho – 1 Pet. 3:20-21
  6. dalili za kifo cha kiroho na ufufuo – Rum. 6:1-5
- B. Ubatizo ulikuwa fursa ya kanisa la kale kwa ajili ya ukiri wa umati wa watu (au ungamo). Huiu haukuwa/si kwa maana ya wokovu, bali tukio la ukili kwa maneno ya imani (yaani, bila shaka, "Yesu ni Bwana"). Kumbuka kanisa la kale halikuwa na majengo na hawa walikutana majumbani au walikutana katika maeneo ya maficho mara kwa mara kwa sababu ya kuteswa.
- C. Watoa maoni wengi wamekuwa wakidai kuwa 1 Petro ni hotuba ya kiubatizo. Ijapokuwa hili linawezekana, huu si uchaguzi wa kipekee. Ni kweli kuwa Petro mara nyingi alitumia ubatizo kama tendo muhimu la imani (kama vile Matendo ya Mitume 2:38, 41;10:47). Hata hivyo, hili lilikuwa/ ni tukio la kisakramenti, lakini tukio la imani, linaashiria mauti kuzikwa, na ufufuo kama mwamini atambuavyo kwa uzoefu wa mara kwa mara (kama vile Rum. 6:7-9; Kol. 2:12). Tendo ni la kiishara, si la kisakramenti; tendo ni tukio la ukiri, si kwa maana ya wokovu.
- IV. Ubatizo na Toba katika Matendo ya Mitume 2:38
- Curtis Vaughan, Kitabu cha Matendo ya Mitume kina tanbihi inayoshawishi katika ukr. 28 unahusiana na Matendo ya Mitume 2:38.
- "Neno la Kiyunani la 'kubatizwa' ni nafsi ya tatu shurutishi; neno la 'kutubu,'ni nafsi ya pili shurutishi. Hii inabadilika moja kwa moja kutoka nafsi ya pili shurutishi hadi nafsi ya tatu ya chini ya moja kwa moja ya neno 'kubatizwa' linalomaanisha kwamba dai la msingi la Petro ni kwa ajili ya toba."
- Hili linafuata ule msisitizo wa Yohana Mbatizaji (kama vile Mt. 3:2) na Yesu (kama vile Mt. 4:17). Toba inaonekana kuwa ufunguzi wa kiroho na ubatizo uko nje ya sura ya madiliko hili la kiroho. Kitabu cha Agano Jipya hakifahamu lolote juu ya waamini wasiobatizwa! Kwa kanisa la kale ubatizo ulikuwa ungamo la imani ya wengi. Hili ni tukio la ungamo la imani ya walio wengi katika Kristo, si kwa maana ya wokovu! Inahitajika kukumbuka kwamba ubatizo hautajwi ndani ya hotuba ya pili ya Petro, ijapokuwa toba ipo (kama vile Matendo ya Mitume 3:19; Luka 24:17). Ubatizo ulikuwa mfano uliowekwa na Yesu (kama vile Mt. 3:13-18). Ubatizo uliamriwa na Yesu (kama vile Mt. 28:19). Swali la sasa la umuhimu wa ubatizo kwa ajili ya wokovu hauelezwi katika kitabu cha Agano Jipya; waamini wote wanatarajiwa kubatizwa. Hata hivyo, mtu lazima pia ajilinde dhidi ya sifa ya kisakramenti! Wokovu ni suala la imani, si sehemu ya haki, haki ya maneno, haki ya suala la utaratibu!

☐ **"kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu"** kanuni hizi za nafsi-tatu yumkini zinaaksi Isa. 42:1. Tambua "kwa jina" ni umoja. Jina la Mungu ni nafsi tatu kwa umoja (kama vile. Mat. 3:16-17; Yn 14:26; Mdo. 2:32-33, 38-39; Rum. 1:4-5; 5:1,5; 8:1-4, 8-10; 1 Kor. 12:4-6; 2 Kor. 1:21; 13:14; Gal. 4:4-6; Efe. 1:3-14,17; 2:18; 3:14-17; 4:4-6; 1 Thes. 1:2-5; 2 Thes. 2:13; Tito 3:4-6; 1 Pet. 1:2; Yuda 20-21). Tazama mada maalumu: Utatu katika Mt. 3:17 na ushupavu binafsi wa Roho katika Mat. 12:31.

Kanuni ya ubatizo ya Mdo. 2:38, "kwa jina la Yesu," sio ya kipekee kwa kanuni hii ya kwenye agizo kuu. Wokovu ni mfuatano wa matendo yote ya awali na yanayoendelea: kutubu, imani, utiifu, na uvumilivu. Sio kanuni ya kawaida ya ibada na sala ya dini au utaratibu wa sakramenti. Ni wa moyoni sana, kila siku, ukuaji, uhusiano binafsi na Mungu. Hili ndilo lilikua kusudi la uumbaji.

**28:20 "kuwafundisha"** hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo iliyotumika kama shurutishi. Tambua kwamba "tunafundisha nini" sio jambo la kipekee juu ya Yesu, lakini utiifu kwa mafundisho yote. Wakristo waliokomaa wanahusika na

1. kutubu kwa imani
2. kuishi maisha ya kumfanana kristo
3. ukuaji wa ufahamu katika mafundisho

☐ **"mimi nipo pamoja nanyi siku zote"** huu ni mkazo. Uwepo binafsi wa Yesu mara zote upo na waaminio.

Mungu pamoja nasi amekuja (kama vile Mt. 1:23) na kukaa! Kuna ugeukaji wa wazi kati kukaa ndani ya Roho mtakatifu na kukaa katika mwana (kama vile Rum. 8:9-10; 2 Kor. 3:17; Gal. 4:6; Flp. 1:19; Kol. 1:27). Katika Yohana 14:23 wote Baba na mwana wanakaa ndani kwa waaminio. Katika ukweli utatu wote wa kiroho umehusika kwenye matukio ya ukombozi. Mmoja mwenye “mamlaka yote” na aliye “pamoja nasi siku zote” ametuamrisha kuhubiri injili na kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi (muhtasari wa matumizi manne ya “wote” kwenye agizo kuu). Na uwepo wake na nguvu tunaweza kutenda hivyo!

☑ **"hata ukamilifu wa dahari"** hii inarejelea nyakati mbili za kiyahudi na ilikua ni rejea ya ujio wa pili au utimilifu wa ufalme wa Mungu. Tazama [MADA MAALUM: ENZI HII NA ENZI IJAYO](#) katika Mt. 12:31.

## **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembele katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. kwa nini mambo ya matukio ya ufufuo ni tofauti sana kati ya injili nne?
2. kwa nini Mungu aliliondoa jiwe wakati tayali Yesu alikwisha toka?
3. kwa nini wanawake walilitembelea kaburi? Mara ngapi? Walikua wanawake wangapi?
4. kwa nini Yesu alikutana na wanafunzi wake katika Galilaya?
5. ni nini kinahusishwa na agizo kuu lililotolewa kwa kanisa zima, na sio kwa uongozi?

# JEDWALI LA TAREHE NA WATAWALA WENYE KUHUSIANA NA PALESTINA WAKATI WA KIPINDI CHA KATI CHA KIBIBLIA

## UFALME WA KIAJEMI

Koreshi II .....	538-529 K.K
Cambyses II .....	529-522
Dario I (Hystaspes) .....	522-486
Ahasuero I .....	485-465
Artashasta I (Longimanus) .....	464-424
Ahasuero II (Miezi michache tu) .....	424-423
Dario II (Nothus).....	423-404
Artashasta II (Mnemon).....	404-359
Artashasta III (Ochus).....	359-338
Dario III (Codomannus).....	338-331

## UFALME WA KI-PTOLEMY (MISRI)

Ptolemy I (Soter I) .....	311-283/2
Ptolemy II (Philadelphos).....	285-246
Ptolemy III (Euegetes I) .....	246-221
Ptolemy IV (Philopator) .....	221-203
Ptolemy V (Epiphanes).....	203-181/0
Ptolemy VI (Philometor) .....	181/0-145
Ptolemy VII (Euergetes II, Physcon) .....	145-116
Ptolemy VIII (Soter II, Lathyros) .....	116-108/7 & 88-89
Ptolemy IX (Iskanda I) .....	108/7-88
Ptolemy X (Iskanda II) .....	80
Ptolemy XI (Auletes) .....	80-51
Ptolemy XII & Cleopatra VII .....	51-48
Ptolemy XIII & Cleopatra VII .....	47-44
Ptolemy XIV (Kaisari) & Cleopatra VII .....	44-30

## UFALME WA KI-SELEUKO

Seleuko I (Nicator) .....	311-281/0
Antioko I (Soter).....	280-262/1
Antioko II (Theos).....	261/0-247/6
Seleuko II (Callinicos) .....	246/5-226/5
Seleuko III (Ceraunus) .....	225/4-223
Antioko III (Mkuu).....	223-187
Seleuko IV (Philopator) .....	187-175
Antioko IV (Epiphanes.....	175-163
Antioko V (Eupator) .....	163-162
Demetrio I (Soter).....	162-150
Iskanda Balas.....	150-145
Demetrio II (Nicator).....	145-139/8
Antioko VI (Epiphanes) .....	145-142/1
Tryphon.....	142/1-138
Antiochus VII (Euergetes, Sidetes).....	139/8-129
Demetrio II (Nicator).....	129-126/5
Antioko VIII (Grypos).....	125-96
Antioko IX (Kyzikenos) .....	115-95
(Mkanganyiko na wadai wa kiuhasama kwa miaka ijayo 30)	

## WAHASMONI

Yuda Makabayo .....	166/5-160
Yonathan (Kuhani Mkuu).....	160/59-142/1
Simoni (Kuhani Mkuu) .....	142/1-135/4
Yohana Hyrcanus I (Kuhani Mkuu, Mfalme) .....	134/3-104/3
Aristobulus I (Kuhani Mkuu, Mfalme).....	103/2
Iskanda Jannaeus (Kuhani Mkuu, Mfalme).....	102/1-76/5
Alexadra Salome .....	75/4-67/6
Hyrcanus II (Kuhani Mkuu,Mfalme).....	75/4-66/5 & 63/40
Aristobulus II (Kuhani Mkuu, Mfalme).....	66/5-63
Antigonos (Kuhani Mkuu, Mfalme).....	40-37
Herode Mkuu .....	37-4

## WATAWALA WA YUDA TOKEA MNAMO MWAKA WA 4 K.K MPAKA KUANGUKA KWA YERUSALEMU MNAMO MWAKA 70 B.K

Archelaus ..... 4 K.K – 6 B.K

### WAENDESHA MASHTAKA WA KIRUMI

Coponius .....	6-9
Marcus Ambibulus .....	c9-12
Annus Rufus .....	c12-15
Valerius Gratus.....	15-26
Pontio Pilato.....	26-36
Marcellus .....	36
Marullus .....	37
Merennius Capito .....	?41
Herode Agrippa I.....	41- 44
Cuspius Fadus .....	44-?
Tiberio Iskanda.....	?
Cumanus .....	?48-52
Felix.....	52-?60
Porcius .....	?60-62
Albino.....	63-64
Gessius Florus .....	64-

Kipindi cha kati cha Mpito cha Biblia (400-5 K.K.)

- A. Utawala wa Uajemi (539/538-332 K.K.)
- B. Utawala wa Kiyunani (322-167 K.K.)
  1. Iskanda Mkuu (332-323 K.K.) aliyemtangulia Philipo wa Makedonia, baba yake mnamo mwaka 336 K.K. wakati wa kifo chake Ufalme wa Iskanda uligawanywa kati ya Makamanda wake—wawili kati yao wanatuhusu: Ptolemy na Seleuko
  2. Utawala wa Ki-Ptolemy (232-198 K.K.) Ptolemy na ufalme wake walitawala Palestina kutokea Misri
    - a. Ptolemy I (“Soter,” 323-285 K.K.) Alijenga Mnara wa Nuru (LightHouse) katika kisiwa kule Paphos
    - b. Ptolemy II (“Philadelphus,” 285-245 K.K.) Alijenga au alijenga upya na kuboresha miji mingi katika Palestina kama vituo vya utamaduni wa Kiyunani: Ashdodi, Ashkeloni, Gaza na Joppa, Gaza, Mnara wa Strato, Sidoni, Ptolemais, Samaria, Beth-shani, ambao sasa unaitwa Scythopolis.

- c. Ptolemy V (mtoto) Aliipoteza Palestina kwa Wa-Seleuko mnamo 198 K.K.
3. Utawala wa Seleuko (198-167 K.K.)  
 Seleuko I (“Nicator,” 281 K.K.)  
 Antioko I (mwana wa kiume wa Seleuko, 281-261 K.K.)  
 Antioko II (alimuoa Bernice, binti wa Ptolemy II, 261-246 K.K.)  
 Antioko III (kaka wa Seleuko III, 223-187 K.K.)  
 Seleuko II (246-226 K.K.)  
 Seleuko III (226-223 K.K.)  
 Antioko III (aitwaye “Antioko Mkuu”) Aliitwaa Palestina kutoka katika mikono ya wa-Ptolemy.  
 Kuhani Mkuu wa Kiyahudi na Simoni II (Familia Yake mara kwa mara walikuwa wenye kuomba misaada) walikuwa kinyume na kufanya ushawishi wa Kiyunani.  
 Familia nyingine ya Kiyahudi Tobiad, ilikuwa ikisimamia uenezwaji wa Desturi za Kiyunani.  
 Mfuasi wa Mabadiliko ya Kiyahudi “watu watauwa” wa Yerusalemu waliokana na kukataa kueneza desturi za Kiyunani.  
 Rumi ilimshinda Antioko mnamo mwaka 188 K.K. na kumtoa kodi kubwa.  
 Seleuko IV — 187-175 K.K.  
 Antioko IV — 175-163 K.K. “Epiphanes” (Kaka wa Seleuko IV) Antioko Epiphanes alimuondoa kuhani mkuu, Onias III, na kuteuwa kaka yake katika nafasi yake — Jason, Myahudi aliyemfuasi wa desturi za Kiyunani. Wafuasi wa Mabadiliko ya Kiyahudi walimpinga kwa Nguvu. Baadaye alimuweka Jason pamoja na Menelaus kuhani Mkuu (na kwa kutumia msaada Antioko baadaye aliliibia Hekalu talanta 1800 za dhahabu!) Baada ya kueneza uvumi huko Yerusalemu kwamba ameuwawa kulikosababisha ghasia za Kiyahudi, Antioko alisitisha ibada za hekalu kaamuru maandiko yao yaharihiwe na Sabato isifuatwe. Akaamuru mungu Zeus aabudiwe. Madhabahu ya Zeus ikatengenezwa katika hekalu! Wayahudi walikuwa hawaruhusiwi kutahiri watoto wao na walikuwa wakilazimishwa kula nguruwe.
- C. Utawala wa Makabayo au Uhuru wa Waebrania 167-63 K.K.
1. Mattathias — kuhani wa Modin; baba wa wana watano — Familia yake iliitwa wa-Hasmoni, kutoka kwa Hasmoni muhenga wa Mattathias.
  2. Yuda — aitwaye “Makabayo” au “The Hammer (Nyundo)” walipata uhuru wa kidini kwa ajili ya Wayahudi kwa namna ya vita ya msituni. Walisafisha hekalu na kuliweka wakfu upya, Disemba 25— aidha mnamo mwaka 165 au 164 K.K. (Hanukkah au Sherehe ya Mianga); Onias IV (wana wa Kuhani Mkuu wa Kiyahudi aliyehalali aliyekwisha fariki) alijenga Hekalu la Kiyahudi katika Misri huko Leontopolis na kuzidisha ibada za Yerusalemu. Ukoo huu wa Kikuhani ulifikia mwisho miaka 230.
  3. Yonathana alimtangulia Yuda katika utawala — 160 K.K. - 143 K.K.
  4. Simoni alipata nguvu wakati wa kifo cha Yonathani na ni aidha mnamo mwaka 143 au 142 K.K. aliwapatia Waseleuko kutambuliwa kwa uhuru wa kisiasa. Alirithishwa kuwa kuhani mkuu na aliuwawa na shemeji yake mnamo mwaka 134 K.K. au 135 K.K.
  5. Yohana Hyrcanus (Kijana wa kiume wa Simoni) alichukua kiti cha utawala — mnamo miaka ya 135-105 K.K. aliharibu Hekalu la Kisamaria. Masadukayo na Mafarisayo sasa wanatokea katika historia kulingana na Josephus.
  6. Aristobulus I — mnamo miaka ya 105-104 K.K. Kwa mwaka mmoja, mwana wa Yohana alijiita mwenyewe “mfalme.” Aliungwa mkono na Mafarisayo.
  7. Iskanda Jannaeus, 104-103 K.K. — 78-77 K.K or 76 ndugu wa nje wa Aristobulus. Alifanyika mfalme na kuhani mkuu baada ya kuoja mjane Salome Alexandra. Aliungwa mkono na Masadukayo. Alimteua Antipata kama Liwali wa Idumaya. Hiki kilikuwa ni kilele cha nguvu na ukuu wa ufalme wa Kimakabayo.

8. Salome Alexandra — alitawala miaka tisa kama malkia, akimfanya mwanawe wa kiume, Hyrcanus II (aliyekuwwa Mfarisayo), kuhani mkuu na mwanawe mwingine, Aristobulus II (aliyekuwa Sadukayo), kamanda wa Kijeshi. Hii ilisababisha vita kati yao. Antipata wa Idumaya na Artas, Mfalme wa Nabatea katika Petra, alimsaidia Hyrcanus II. Pompey, kamanda wa Kirumi aliwasili huko Dameski mnamo mwaka 63 K.K. na wote Hyrcanus na Aristobulus II walikata rufaa kwa ajili ya kuungwa mkono.
- D. Utawala wa Kirumi — 63 K.K.
1. Pompey — alimuunga mkono Hyrcanus II akiwa na Antipata kama mshauri.
  2. Julius Kaisari — alimpatia Antipata nguvu kubwa kama mwendesha mashitaka wa Yuda na Antipata akawafanya wanawe wawili Herode Phasael, wasimamizi wa kijeshi juu ya Galilaya na Yudea hasa.
  3. Marko Anthony alimteua Herode na Phasael “watawala” kwa umoja juu ya Yudea mnamo mwaka 41 K.K.
  4. Parthia waliendesha na kutawala Yudea kutokea mnamo mwaka 40-39 K.K. kuhani mkuu aliyetawala kama mfalme. Phasael alijiua lakini Herode alikimbilia Rumi na kwa msaada wa Antony na Octavius, Baraza la Seneti lilimfanya kuwa mfalme wa Wayahudi. Ilimchukua miaka miwili au mitatu ya vita ili kuuchukua kikamilifu Palestina. Wakati Octavius na Antony (na Cleopatra) mjadiliano ya kumaliza migogoro mnamo mwaka 31 K.K. huko Actium, Octavius aliinuka kama mtawala wa ulimwengu wa Kirumi na Herode aliendelea kuungwa mkono.
  5. Utawala wa Herode — 37-4 K.K. : kinadharia, mfalme huru kwa kushirikiana na Rumi.
    - a. Idumaya (au mtu kutoka Edomu)
    - b. Alikuwa amempindua mtawala wa ki-Hasmoni — hivyo alimuoa binti wa mfalme wa kihasmoni, Marianne. Kuibuka kwa shauku ya kutaka kujua mauaji, n.k. kulifuatia.
    - c. Kulipanua mipaka yake kwa kiwango alichokitaka
    - d. Mjenzi Mkubwa
      - (1) Kaisaria kando ya Bahari
      - (2) Hekalu lilianza mnamo mwaka 20 au 19 K.K. na ilichukua mpaka mwaka 64 B.K. mpaka kukamilika
      - (3) Samaria ilifanyika Sebaste kwa kumuheshimu Augustus.
      - (4) Hivyo pia, Antipatris kaskazini mashariki mwa Joppa
      - (5) Hivyo pia, Phasaelis kaskazini mwa Yeriko
      - (6) na ngome zilizengwa zilikuwa kama zile za Machaerus na Masada
    - e. Familia yake iliyotawala:
      - (1) Archelaus — 4 K.K. - 6 B.K. waltawala Yudea, lakini aliondolewa na waendesha mashitaka waliwekwa katika nafasi yake (kama vile Mt. 2:20-22)
      - (2) Herode Antipa — alitawala Perea na Galilaya; alimuua Yohana Mbatizaji. Alijenga mji wa Tiberio katika Bahari ya Galilaya mnamo.. 22 B.K. Kilifanyika kituo cha kujifunzia cha Kiyahudi baada ya Yerusalemu kuharibiwa mnamo mwaka 70 B.K.
      - (3) Mtawala Philipo — alitawala Kaskazini mashariki mwa Palestina. Mji Mkuu wa Panioni ukijengwa upya. (Sio mume wa Herodia.) Aliita Mji Mkuu wa Kaisaria, hivyo Kaisaria Philipo. Alijenga upya Bethsaida na kuuita Bethsaida Julius kwa kumuheshimu Julia, binti wa Kaisari Augustus.
      - (4) Antioko IV — 175-163 K.K. “Epiphanes” (kaka wa Seleuko IV). Antioko Epiphanes alimuondoa kama kuhani mkuu, Onias III, na kumteua kaka yake katika nafasi yake — Jason, Myahudi mwenye desturi za Kiyunani. Wafuasi wa mabadiliko ya Kiyahudi walimpinga kwa nguvu sana. Baadaye alimbadilisha Jason na kuuweka Menelaus kama kuhani (na kwa kutumia msaada Antioko baadaye alilibia Hekalu talanta 1800 za dhahabu!) Baada ya kueneza uvumi huko

Yerusalemu kwamba ameuwawa kulikosababisha ghasia za Kiyahudi, Antioko alisitisha ibada za hekalu kaamuru maandiko yao yaharibiwe na Sabato isifuatwe. Akaamuru mungu Zeus aabudiwe. Madhabahu ya Zeus ikatengenezwa katika hekalu! Wayahudi walikuwa hawaruhusiwi kutahiri watoto wao na walikuwa wakilazimishwa kula nguruwe.



# TAFASIRI SAHIHI ZA ISTILAHU ZA VISARUFU VYA KIYUNANI

Lugha ya kawaida ya Koine mara nyingi inafahamika kama Kiyunani kilichobobea, ilikuwa ni lugha ya kawaida ya ulimwengu wa Mediterania ilianzishwa na Alexandra mkuu (336-323 B.K) na ikadumu mpaka miaka ya (300 K.K-B.K 500). Haikuwa rahisi, Kiyunani kuwa cha daraja la juu, lakini kwa njia nyingi ni dhana ya Kiyunani ambayo ilikuja kuwa lugha ya pili karibu na mashariki ya kale na ulimwengu wa Mediterania.

Kiyunani cha Agano Jipya kilikuwa ni cha kipekee kwa njia kadhaa kwa watumiaji wake, isipokuwa Luka mwandishi wa kitabu cha Waebrania, yamkini alitumia lugha ya Kiarama kama lugha ya msingi. Kwa hiyo, uandishi wao uliathiliwa na dhana ya muundo wa Kiarama. Pia, walisoma na kunukuu wandishi wa maandiko ya kale (tafasiri ya Kiyunani ya maandiko ya kale) ambayo pia yaliandikwa kwa lugha ya Koine. Lakini maandiko ya kale pia yaliandikwa kwa wasomi wa Kiyahudi ambao lugha yao ya asili ilikuwa sio ya Kiyunani.

Hii ilisaidia kuwa kama kumbukumbu ambayo haiwezi kulipeleka Agano Jipya kwenye muundo mgumu wa kisarufi. Ni wa kipekee na bado una mambo mengi yaliyo pamoja na (1) maandiko ya kale (2) maandiko ya kale kama yale ya Yusufu na (3) mafunjo yaliyopatikana Misri. Kwa hiyo tunakabilianaje na uchambuzi wa visarufi vya Agano Jipya.

Muundo wa kisarufi wa lugha ya Koine na Agano Jipya la lugha ya Koine ulibadilika. Kwa njia tofauti ulikuwa ni urahisishaji wa sarufi. Mazingira ndio yatakuwa mwongozo wetu mkuu. Maneno pekee yana maana katika upanuzi wa mazingira, kwa hiyo, muundo wa kisarufi unaweza tu kueleweka katika mwanga wa (1) aina mahsusi ya mwandishi, na (2) mazingira mahsusi

Hapana hitimisho la fasiri ya dhana na muundo wa Kiyunani unaowezekana. Kimsingi lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ya maneno tu. Mara nyingi msingi wa utafasiri ni aina na dhana ya maneno. Mara nyingi vishazi vikuu hutokea kwanza, vikionyesha kushinda vingine vyote. Katika kueleza kitenzi cha Kiyunani, vipande vitatu vya habari lazima vizingatiwe (1) kiini cha msisitizo wa njeo, sauti na dhamira (tukio au umbo); (2) kiini cha maana husika ya kitenzi (usawidi kamusi); na (3) mtiririko wa mazingira yenyewe (isimu ya mpangilio wa maneno)

## I. NJEO

- A. NJEO au sura inajumuisha uhusiano wa VITENZI ili kukamilisha kitendo au kutokamilisha kitendo. Mara nyingi huitwa “utimilifu” au “utoutimilifu”
  1. Njeo timilifu zinaangazia juu ya utoaji wa kitendo. Hakuna taarifa nyingine zilizotolewa isipokuwa ya kile kilichotokea! Kuanza kwake, mwendelezo au ukomo wake haukuelezwa.
  2. Njeo zisizo timilifu zinaangazia juu ya mchakato endelevu wa kitendo. Zinaweza kuelezewa dhidi ya unasaba wa kitendo, kudumu kwa kitendo, mwendelezo wa kitendo, n.k.
- B. Njeo zaweza kugawanywa kwa jinsi mwandishi anavyoona kitendo kinavyoendelea.
  1. Kimetokea-KITENZI TIMILIFU
  2. Kilivyotokea au matokeo yake-KITENZI CHA WAKATI ULIOPIA
  3. Kilivyokuwa kikitokea nyuma na matokeo yake yakastahimili, lakini sio sasa-KITENZI CHA WAKATI ULIOPIA TIMILIFU
  4. Kinatokea –WAKATI ULIOPO
  5. Kilikuwa kikitokea- WAKATI USIOTIMILIFU
  6. Kitatokea –WAKATI UJAO

Mfano thabiti wa jinsi njeo hizi zinasaidia katika utafasiri ungalikuwa wa neno “okoa.” Lilitumika katika NJEO nyingi tofauti kuonyesha kwa pamoja mchakato na ukomo.

1. KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU- “okolewa” (Rum 8:24)

2. KITENZI CHA WAKATI ULIOPIITA- “ameokolewa na matokeo yake yanaendelea” (Efe 2:5,8)
  3. KITENZI CHA WAKATI ULIOPO- “anaokolewa” (kama vile 1Kor 1:18; 15:2)
  4. KITENZI CHA WAKATI UJAO- “ataokolewa” (kama vile Rum 5:9,10; 10:9)
- C. Katika kuzingatia juu ya VITENZI VYA NJEO, mfasiri huangalia sababu za mwandishi wa kwanza alichagua kuelezea yeye binafsi NJEO fulani. Tarajio la NJEO “hakuna madoido” lilikuwa ni la KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU. Kilikuwa ni muundo wa KITENZI cha kawaida “kisichoainishwa” “kisichotambulika” “kisichochoka.” Chaweza tumika katika Nyanja pana ambamo mazingira lazima yaelezee. Kwa kawaida kilikuwa kinaelezea kuwa kitu fulani kimetendeka. Sura ya muda uliopita ulikusudia tu katika DHAMIRA ELEKEZI. Kama pana NJEO nyingine zilizotumika, uainishaji wa kitu fulani ulikuwa unasisitizwa. Lakini ni nini?
1. NJEO YA WAKATI ULIOPIITA. Hii inaongelea juu ya tendo lililokwisha tendeka na matokeo yakiendelea kuwepo. Katika namna fulani ilikuwa ni muunganikano wa NJEO ZA WAKATI TIMILIFU na ZA WAKATI ULIOPIITA. Mara kwa mara mlengo ulikuwa juu ya matokeo yalioendelea kuwepo au kumalizika kwa kitendo. Mfano: Efe 2:5 & 8, “umekuwa na unaendelea kuokolewa.”
  2. NJEO YA WAKATI ULIOPIITA AINISHI. Hii ilikuwa kama njee ya WAKATI ULIOPIITA isipokuwa matokeo yalishakoma. Mfano: “Petro alikuwa akisimama nje mlangoni” (Yoh 18:16)
  3. NJEO YA WAKATI ULIOPO. Hii inazungumzia juu ya kitendo kisichokiwisha au kisichotimilifu. Mtizamo mara nyingi ni juu ya uendelezaji wa tukio. Mfano: “kila mmoja ashikamanae ndani yake haendelei kutenda dhambi”, “kila mmoja aliyesamehewa na Mungu haendelei kutenda dhambi” (1Yoh 3:6 & 9).
  4. NJEO YA WAKATI USIOTIMILIFU. Katika njee hii uhusiano na NJEO YA WAKATI ULIOPO ni mwendelezo wa uhusiano kati ya WAKATI ULIOPIITA na WAKATI ULIOPIITA AINISHI. WAKATI USIOTIMILIFU unaongelea juu ya kitendo ambacho hakijaisha kutendeka ambacho kilikuwa kinatokea lakini sasa kimekoma au mwanzo wa kitendo awali. Mfano: “kwa hiyo Yerusalemu yote waliendelea kumwacha” au “Yerusalemu yote wakaanza kumwacha”(Mt3:5)
  5. NJEO YA WAKATI UJAO. Hii inaongelea juu ya kitendo ambacho kawaida kilijitokeza ndani ya muda mwafaka. Inaangazia juu ya umuhimu wa jambo kutokea kuliko utokeaji wa uhalisia. Mara nyingi unazungumzia juu ya ualakini wa tukio. Mfano: “Heri wale....wata...”(Mt 5:4-9).

## II IRABU

- A. Irabu inaelezea mahusiano kati ya kitendo cha KITENZI na KIIMA
- B. IRABU TENDAJI ilikuwa ni njia ya kawaida, tarajiwa, isiosisitiza utetezi wa kwamba kiima kilikuwa kikitenda kitendo cha KITENZI.
- C. IRABU TENDEWA ina maana kuwa KIIMA kilikuwa kikipokea kitendo cha KITENZI kilichotolewa na mtu wan je. Mtu wa nje anayetoa kitendo alionyeshwa katika Agano Jipya la Kiyunani kwa mambo na VIHUSISHI vifuatavyo:
  1. Mtu binafsi wa moja kwa moja wa *hupo* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (cf. Mt 1:22; Mdo 22:30)
  2. Mtu binafsi wa kati na *dia* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (cf. Mt 1:22)
  3. Mtu wa kawaida asiyehusika na *en* kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO
  4. Wakati mwingine ni mtu binafsi au asiyehusika kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO pekee.
- D. IRABU YA KATI inamaanisha kuwa KIIMA kinatoa tendo la KITENZI na pia moja kwa moja kinahusishwa katika kitendo cha KITENZI. Mara nyingi huitwa irabu ya kurefusha matakwa binafsi. Muundo huu unasisitiza KIIMA cha kishazi au sentesi kwa namna nyingine. Muunganikano huu haupatikani katika Kiingereza. Una uwezekano mpana wa maana na ufasiri katika Kiyunani. Baadhi ya mifano ya dhana hizi ni;

1. YENYE KUJIREJEA – kitendo cha moja kwa moja cha kiima chenye. Mfano: “kajiangika mwenyewe” (Mt 27:5)
2. YENYE KUTIA MKAZO- kiima kinazaa kitendo chake chenye. Mfano: “shetani mwenyewe anajifanya kama malaika wa nuru” ( 2Kor 11:14)
3. Kukubaliana – mwingiliano wa viima viwili. Mfano: “walishauliana wao kwa wao” (Mt 26:4)

### III. DHAMIRA (au “NAMNA”)

- A. Kuna namna nne za DHAMIRA katika lugha ya Koine. Zinaashiria uhusiano wa KITENZI kuwa kweli, haswa ndani ya wazo la mwandishi mwenyewe. DHAMIRA hizi zinagawanyika katika namna pana mbili: ile inayoonyesha ukweli (ELEKEZI) na ile inayoonyesha umuhimu (UTEGEMEZI, KUAMURU/KUSHURUTISHA na HALI YA UCHAGUZI).
- B. DHAMIRA ELEKEZI ilikuwa ni NAMNA ya kawaida ya kuelekeza kitendo ambacho kimekwisha tokea au kilikuwa kinatokea, haswa kwenye wazo la mwandishi. Ilikuwa namna pekee ya Kiyunani ya kueleza ukomo wa muda na hata hapa sura hii ilikuwa daraja la pili.
- C. DHAMIRA TEGEMEZI kinaelekeza yumkini kitendo kitakachotokea mbeleni. Kitu fulani ambacho hakijawahi tokea lakini nafasi ya kutokea ingaliwezekana. Ina vitu vingi vinavyofanana na KITENZI CHA WAKATI UJAO ELEKEZI. Utofauti ni kuwa UTEGEMEZI unaelezea kiwango fulani cha mashaka. Katika Kiingereza hii mara nyingi inaelezewa na neno “ingalikuwa”, “ingaliweza”, “yawezezana” au “yenye uwezo”.
- D. DHAMIRA YA UCHAGUZI inaelezea utashi ambao kinadharia unawezezana. Ilifikiliwa ni hatua moja mbele kutoka katika ukweli kuliko HALI YA UTEGEMEZI. HALI YA UCHAGUZI inaelezea uwezekano chini ya hali fulani. HALI YA UCHAGUZI ilikuwa ni nadra katika Agano Jipya. Utumikaji wake mara nyingi kilikuwa ni kifungu maarufu cha Paulo. “yawezezana isiwe” (KJV, Mungu anakataza), kimetumika mara kumi na tano (kama vile Rum 3:4,6,31; 6:2,15; 7:7,13; 9:14; 11:1,11; 1Kor 6:15; Gal 2:17; 3:21; 6:14) mfano mwingine unapatikana katika Thes 1:38, 20:16, Mdo. 8:20 na 1Thes 3:11
- E. DHAMIRA SHURUTISHI inasisitiza juu ya amri ambayo iliwezekana, lakini msisitizo ulikuwa juu ya dhamira ya mnenaji. Inatetea juu ya uwezekano wa hiari na ilishurutishwa juu ya chaguzi za wengine. Kulikuwa na matumizi ya kipekee ya HALI YA KUSHURUTISHA katika maombi na hitaji la mtu wa tatu. Amri hizi zinapatikana tu katika WAKATI ULIOPO na njeo ya WAKATI TIMILIFU katika Agano Jipya.
- F. Baadhi ya visarufi vinabainisha VIAMBATA kama moja aina ya NAMNA. Ni vya kawaida katika Agano Jipya la Kiyunani, mara nyingi vikielezwa kama KIVUMISHI CHA TENDO. Vinatafasiriwa kama muunganiko wa VITENZI vikuu ambavyo vinafanana. Tofauti pana iliwezekana katika utafasiri wa viambata. Ni vizuri kuzirejea tafasiri nyingi za Kiingereza. *The Bible in Twenty Six Translation* kilichochapishwa na Baker ni msaada mkubwa hapa.
- G. KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni njia ya kawaida au “kisichotambulika” cha Kuingiza matokeo. Njeo nyingine, irabu au zilikuwa na ufasiri mahususi ambao mwandishi wa kwanza alihitaji kuwasilisha.

### IV. Kwa mtu ambaye hayuko na uzoefu na lugha ya kiyunani, msaada wa usomaji unaofuata utatoa taarifa inayohitajika;

- A. Friberg, Barbara na Timothy. *Analytical Greek New Testament*. Grand Rapids: Baker 1988
- B. Marshall, Alfred. *Interlinear Greek-English New Testament*. Grand Rapids: Zondervan 1976
- C. Mounce, William D. *The Analytical Lexicon to the Greek New Testament*. Grand Rapids: Zondervan 1993
- D. Summer Ray. *Essential of the New Testament Greek* Nashville: Broadman 1950
- E. Kitaaluma mtangamano wa kozi ya lugha ya Koine unapatikana kupitia taasisi ya Moody Bible iliyoko Chikago II

## V. NOMINO

- A. Ki-isimu, NOMINO zinaainishwa kwa jambo. Jambo ni lile lililoshurutisha dhana ya NOMINO ambayo ilionyesha kuwa na uhusiano na KITENZI na sehemu nyingine ya sentesi. Katika lugha ya Koine kazi nyingi za uhusika zilionyeshwa na VIHUSISHI. Tangu dhana ya uhusika iliweza kutambua tofauti ya mahusiano mbali mbali, VIHUSISHI vilitokea kutoa utengano mzuri wa kazi hizo.
- B. Uhusika wa Kiyunani uliainishwa kwa njia nane zifuatazo;
1. UHUSIKA WA KIIMA ulitumika kwa ajili ya kutaja na kawaida kilikuwa ni kiima cha sentesi au kishazi. Pia ilitumika kwa NOMINO ARIFU na VIVUMISHI vikiunganishwa na VITENZI “kuwa” au “kufaa”
  2. UHUSIKA MILIKISHI ulitumika kwa ajili ya kuelezea na kawaida ulitoa kivumishi au thamani ya nenolililofanana nalo. Ulijibu swali, “aina gani?” mara nyingi ulielezwa na utumiaji wa KIHUSISHI cha Kiingereza “ya/za”
  3. UHUSIKA WA KUONDOA ulitumia dhana ile ile ya kushurutisha kama ya UMILIKISHI, lakini ulitumika kuelezea utenganifu. Kawaida ulidokeza utengano wa alama kwenye muda, nafasi, kiini, chanzo au degrii. Mara nyingi ulielezwa na matumizi ya KIHUSISHI cha Kiingereza “kutoka”.
  4. UHUSIKA WA WAKATI ulitumika kuelezea matwaka ya mtu binafsi. Hii ingalidokeza mtizamo chanya au hasi. Mara nyingi hiki kilikuwa si kitu cha moja kwa moja. Mara nyingi ulielezwa na KIHUSISHI cha Kiingereza “ya”.
  5. UHUSIKA WA MAHALI ilikuwa dhana shurutishi ya WAKATI, lakini ilielezea mahali au eneo kwenye nafasi, muda au ukomo. Mara nyingi ulielezwa na KIHUSISHI cha Kiingereza “ndani, juu, ni, kati, kwa, juu ya na mbali na”
  6. UHUSIKA WA KUTUMIKA ilikuwa ni dhana shurutishi kama uhusika wa WAKATI na MAHALI. Unaelezea namna au uhusiano. Mara nyingi ulielezwa na KIHUSISHI cha Kiingereza cha neno “kwa” au “enye”
  7. UHUSIKA WA KUSHUTUMU ulihusika kuelezea hitimisho la kitendo. Unaelwzea ukomo. Haswa utumikaji wake ulikuwa kwenye dhana ya moja kwa moja. Ulijibu maswali “kwa umbali gani” au “kwa namna gani”
  8. UHUSIKA WA KAULI ulitumika kuelezea moja kwa moja.

## VI. VIUNGO NA VIUNGANISHO

- A. Kiyunani ni lugha sahihi kwa sababu ina viunganishi vingi. Viunganisho fikra ( vishazi, sentesi na aya). Ni vya kawaida kwamba utouwepo wao mara nyingi unakuzwa. Kama jambo la uhakika, viunganisho na viungo hivi vinaonyesha muelekeo wa fikra za mwandishi. Mara nyingi ni vya maana kupima ni kipi haswa anajaribu kukiwakilisha.
- B. Hapa pan orodha ya baadhi ya viunganishi na viungo na maana zake (taarifa hizi zimekusanywa haswa toka kwa H.E Dana na Julius K. Mantery. A Manual Grammar of the Greek New Testament
1. Viunganishi vya wakati
    - (a) *epei, epedē, hopote, hōs, hote, hotan* (TEGEMEZI)- “lini”
    - (b) *heōs*- “wakati”
    - (c) *hotan, epan* (TEGEMEZI)- “kila, wakati wowote”
    - (d) *heōs, achri, mechri* (Tegemezi)- “mpaka”
      - a. *priv* (kitenzijina)- “kabla”
      - b. *hōs*- “tangu”, “lini”, “kama”.
  2. Viunganishi venye mantiki
    - a. Kusudi/dhumuni
      - 1) *hina* (TEGEMEZI) *hopōs* (TEGEMEZI) *hōs*- “ya kwamba”, “kuwa”
      - 2) *hōste*(KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- “kuwa”

- 3) *pros*(KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO) au *eis* (KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- “kuwa”
- b. Tokeo (kuna uhusiano wa karibu kati ya kusudio la dhana ya kisarufi na tokeo)
- (1) *hōste*(ISIYO NA KIKOMO, hasa hiki ni cha kawaida)- “ili kwamba”, “hivyo”
  - (2) *hiva*(TEGEMEZI)- “ya kwamba”
  - (3) *ara*- “kwa kiasi hicho”
- c. Chanzo au sababu
- 1) *gar*(chanzo/athari au sababu/hitimisho)- “kwa”, “kwa sababu ya”
  - 2) *dioti, hotiy*- “kwa sababu ya”
  - 3) *epei, epeidē, hōs*- “tangu”
  - 4) *dia*(ikiwa na SHUTUMA) na (ikiwa na KIUNGO KISICHO NA UKOMO)- “kwa sababu ya”
- d. Maamuzi
- (1) *ara, poinun, hōste*- “kwa hiyo”
  - (2) *dio*(KIUNGO HITIMISHO chenye nguvu)- “kwa sababu ipi”, “kwa nini”, “kwa hiyo basi”
  - (3) *oun*- “kwa hiyo basi”, “kwa kiasi hicho”, “hatimaye”, “hivyo basi”
  - (4) *tinoun*- “kufuatana na”
- e. –a kinyume au tofauti
- (1) *alla*( yenye KINYUME thabiti)-“lakini”, “isipokuwa”
  - (2) *de*- “lakini”, “ingawa”, “bado”, “kwa upande mwingine”
  - (3) *kai*- “lakini”
  - (4) *mentoi, oun*- “ingawa”
  - (5) *plēn*- “hata hivyo” (haswa katika Luka)
  - (6) *oun*- “ingawa”
- f. Ulinganifu
- (1) *hōs, kathōs* (ingiza vishazi linganifu)
  - (2) *kata*(kwa muunganiko, *katho, kathoti, kathōsper, kathaper*)
  - (3) *hasos*(katika Kiebrania)
  - (4) *ē*- “kuliko”
- g. Enye mlolongo au mtiririko
- (1) *de*- “na”, “sasa”
  - (2) *kai*- “na”
  - (3) *tei*- “na”
  - (4) *hina, oun*- “kile”
  - (5) *oun*- “kasha”(katika Yohana)
3. Matumizi yenye mkazo
- a. *alla*- “kwa hakika”, “naam”, “kwa kweli”
  - b. *ara*- “hakika”, agharabu”, “kweli”
  - c. *gar*- “lakini kweli”, “agharabu”, “hakika”
  - d. *de*- “hakika”
  - e. *ean*- “hata”
  - f. *kai*- “hata”, “hakika”, “kweli”
  - g. *mentoi*- “hakika”
  - h. *oun*- “kweli”, “kwa hali zote”

- A. SENTESI SHURUTISHI ni ile iliyo na kishazi kimoja au zaidi. Muundo huu wa kisarufi unaongeza utafasiri kwa sababu unatoa amri, sababu au chanzo kwa nini kitendo cha KITENZI kikuu kimetokea au hakikutokea. Palikuwa na aina nne za sentesi shurutishi. Zilitoka kwa zile zilizofikiwa kuwa kweli toka kwa mtizamo wa mwandishi au kwa kusudio lake kwa lile alilokuwa na utashi nalo.
- B. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA ilielezea kitendo au kile kilichofikiwa kuwa kweli toka kwa mtimamo wa mwandishi au kusudio lake. Ingawa ilielezewa kwa neno “kama.” Katika mazingira tofauti lingeweza kutafasiriwa “tangu”(cf. Mt 4:3, Rum 8:31). Ingawa hii haimaanishi kudokeza kuwa MADARAJA YA KWANZA yote ni ya kweli. Mara nyingi yalitumika kuweka alama kwenye hoja au kuangazia kosa(cf. Mt 12:27)
- C. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA PILI mara nyingi huitwa “inayopingana na ukweli”. Inaelezea kitu ambacho kilikuwa ni cha uongo kwenye ukweli wa kufanya jambo. Mfano:
1. “kama kweli alikuwa nabii, ambapo sio, alikuwa sasa nani na mwanamke wa tabia gani anaye mng’ang’ania yeye, lakini hawezi (Thess 7:39)
  2. Kama kweli Musa, lakini hamkumwamini, mngaliniamini na mimi lakini hamkuniamini (Yoh 5:46)
  3. Kama ningalitaka kuwapendezesha wanadamu lakini sivyo, nisingalikuwa mtumwa wa Christo hata sasa(Gal 1:10)
- D. DARAJA LA TATU linaongelea juu ya tukio lijalo ambalo laweza kutokea. Mara nyingi unafikirika uwezekanao wa kitendo kutokea. Kawaida inaashiria tahadhari. Kitendo cha KITENZI kikuu ni tahadhari juu ya tendo la kishazi “hiki”. Mfano toka 1Yoh 1:6-10; 2:4,6,9,15,20,21,24,29; 4:20; 5:14,16
- E. DARAJA LA NNE ni daraja la mbali lililoondolewa kwenye uhakika. Ni adimu katika Agano Jipya. Kama jambo la kweli, hakuna SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA NNE lililokamilika ambamo pande zote za jambo zinastahili maelezo. Mfano wa DARAJA LA NNE ni ufunguzi wa kishazi katika 1Pet 3:14. Mfano wa sehemu DARAJA LA NNE ni katika kuhitimisha kishazi katika Mdo 8:31.

#### VIII. VIZUIZI

- A. KITENZI CHA KUAMURU CHA WAKATI ULIOPO kikiwa na KIAMBATA MĒ mara nyingi (lakini hakitengwi) kina msisitizo wa kusimamisha tendo ambalo liko kwenye mchakato. Baadhi ya mifano: “msijiwekee hazina yenu duniani.....”(Mt 6:19); “msisumbukie maisha yenu.....” ( Mt 6:25); “wala msiendeele kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi.....”(Rum 6:13); “wala msimhuzunishe Yule Roho Mtakatifu wa Mungu (Efe 4:30) na “tena msilewe kwa mvinyo.....”(Ef 5:18)
- B. KITENZI TEGEMEZI TIMILIFU kina mkazo wa “udhahanifu au mwanzo wa kutenda kitendo” baadhi ya mifano: “msidhani ya kuwa.....”(Mt 5:17); “msisumbuke.....”(Mt 6:31); “msiuonee haya.....”(2Tim 1:8)
- C. KITENZI HASI CHENYE JOZI kikiwa na DHAMIRA TEGEMEZI ni chenye msisitizo hasi. “kamwe, katu” au “kwa hali yeyote ile”. Baadhi ya mifano: “kamwe, hataonja mauti.....”(Yoh 8:51); “hakika, kamwe.....”(1Kor 8:13)

#### XI

- A. Katika lugha ya Koine, KIBAINISHI CHA WAZI cha neno “wale, Yule,ile” kina matumizi mfanano na kwenye Kiingereza. Kazi yake kuu ilikuwa ni ya “muonyeshwaji”, ni njia ya kukamata hisia ya neno, jina au kirai. Utumiaji unatofautiana kati ya mwandishi na mwandishi kwenye Agano Jipya. KIBAINISHI CHA WAZI pia chaweza kutenda
1. Kama chombo cha kutofautisha mfano cha kuonyesha
  2. Kama alama ya kurejea KIIMA kilichowekwa awali au mtu
  3. Kama njia ya kutambua kiima kwenye sentesi kikiwa na KITENZI kinchounganisha. Mfano: “Mungu ni Roho” Yoh 4:24, “Mungu ni nuru” 1Yoh 1:5; “Mungu ni upendo” 4:8,16

B. Lugha ya Koine haina KIBAINISHI KISICHO CHA WAZI kama ilivyo kwenye Kiingereza cha neno “a” herufi ya kwanza ya alfabeti au “an” mbadala wa “a” kwenye irabu zinazoanza na herufi kama “e”, “h”. Kutokuwepo na KIBAINISHI CHA WAZI chaweza kumaanisha;

1. Mlengo juu ya tabia au thamani ya kitu
2. Mlengo juu ya aina ya kitu

C. Waandishi wa Agano Jipya walitofautiana sana kwa jinsi KIBAINISHI kilivyotumiwa.

X NJIA ZA KUONYESHA MKAZO KWENYE AGANO JIPYA LA KIYUNANI

A. Mbinu za kuonyesha msisitizo zinatofautiana toka kwa mwandishi mmoja hadi mwingine kwenye Agano Jipya. Waandishi waendelezaji na warasimishaji walikuwa ni Luka na mwandishi wa Waebrania.

B. Mwanzo kabisa tumesema ya kuwa KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni kipimo na kisichoangaliwa kwenye msisitizo, lakini njeo nyingine, irabu au dhamira zina umuhimu wa ufasiri. Hii sio kumaanisha kuwa KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI mara nyingi hakikutumika kwenye umakinishaji wa kisarufi. Mfano: Rum 6:10 (mara mbili)

C. Upangiliaji wa neno kwenye lugha ya Koine.

1. Lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ngumu isiyo tegemezi, kama vile Kiingereza, kwenye mpangilio wa maneno. Kwa hiyo mwandishi angaliweza kutofautiana kwenye mpangilio wa kawaida aliotegemea kuonyesha.

- a. Kile mwandishi alihitaji kusisitiza kwa viongozi
- b. Kile mwandishi angalikishangaza kwa viongozi
- c. Kile mwandishi alichosikia toka ndani

2. Mpangilio wa kawaida wa neno kwenye Kiyunani bado ni jambo ambalo halijatulia ingawa mpangilio wa kawaida unaokusudiwa ni

a. Kiunganishi cha VITENZI/Vitenzi unganishi

- (1) KITENZI
- (2) KIIMA
- (3) SIFA

b. VITENZI elekezi

- (1) KITENZI
- (2) KIIMA
- (3) KISHAMILISHI
- (4) KISHAMILISHI KISICHO DHAHIRI
- (5) KIRAI HUSISHI

c. Virai vya NOMINO

- (1) NOMINO
- (2) KIVUMISHI
- (3) KIRAI HUSISHI

3. Mpangilio wa neno waweza kuwa muhimu mno kwenye upangiliaji wake. Mfano:

- a. “walinipa mimi na Barnaba mkono wa kuume wa shirika” (Gal 2:9) kirai “mkono wa kuume wa shirika” imegawanyika na kuwekwa mbele kuonyesha umuhimu wake.
- b. Pamoja na Kristo (Gal 2:20), iliwekwa kwanza kifo chake kilikuwa kiini.
- c. “ni sehemu nyingi na kwa njia nyingi” (Ebr 1:1), iliwekwa kwanza. Ilikuwa ni kwa namna Mungu alivyojidhihilisha mwenyewe kwa tofauti na sio ukweli wa mafunuo.

D. Kawaida kwa kiasi fulani cha degrii ya msisitizo ulionyeshwa na

1. Urudiaji wa KIWAKILISHI ambacho tayari kilikuwepo katika KITENZI kilichonyambulika. Mfano: “mimi mwenyewe, hakika nitakuwa nawe.....”(Mt 28:20)
  2. Ukosekanaji wa KIUNGO tarajiwa, au kitu kingine cha kuunganisha maneno, virai, vishazi au sentesi. Hii inaitwa (isiofungamana). Kitu unganishi kilikuwa ni
    - a. Ibada ya kubarikiwa kwa Kristo, Mt 5:3 ff(ikisisitizia orodha)
    - b. Yohana 14:1 (maada mpya)
    - c. Rumi 9:1 (kifungu kipya)
    - d. 2Kor 12:20 ( inasisitizia orodha)
  3. Urudiaji wa maneno au virai vilivyomo katika mazingira tajwa. Mfano: “usifiwe utukufu wa neema yake” (Efe 1:6, 12 & 14). Kiraiki hiki kilitumika kuonyesha kazi ya kila mtu wa utatu.
  4. Utumiaji wa nahau au neno (sauti) unakaa kati ya istilahi.
    - a. Tasifida- maneno mbadala kwa viima vyenye miiko kama “lala” kwa kifo (Yoh 11:11-14) au “nyayo” kwa viungo vya uzazi vya kiume (Ruth 3:7-8; 1Sam 24:3)
    - b. Maneno ya kuzunguka- mbadala wa maneno kwa jina la Mungu, kama “ufalme wa mbingu” (Mt 3:21) au “sauti toka mbinguni” (Mt 3:17)
    - c. Maumbo ya hotuba
      - (1) Kutowezekana kuyakuza (Mt 3:9; 5:29-30; 19:24)
      - (2) Upole wa maelezo (Mt 3:5; Mdo 2:36)
      - (3) Mfano halisi wa (1Kor 15:55)
      - (4) Kejeli (Gal 5:12)
      - (5) Dondoo za kishairi (Flp 2:6-11)
      - (6) Mvumo unaokaa kati ya maneno
        - (a) “kanisa”
          - i. “kanisa” (Efe 3:21)
          - ii. “Kuitwa” (Efe 4:1,4)
          - iii. “Kuitwa” (Efe 4:1,4)
        - (b) “huru “
          - i. “Mwanamke huru” (Gal 4:31)
          - ii. “uhuru” (Gal 5:1)
          - iii. “huru” (Gal 5:1)
    - d. Lugha ya kinahau- ni lugha ambayo mara nyingi ni ya kitamaduni na lugha bayana
      - (1) Hii ilikuwa ni matumizi ya kistiari ya neno “chakula” (Yoh 4:31-34)
      - (2) Hii ilikuwa ni matumizi ya kiistiari ya neno “hekalu” (Yoh 2:19; Mt 26:61)
      - (3) Hii ilikuwa ni nahau ya Kiebrania ya kuonyesha huruma, ya neno “chukia” (Mwa. 29:31; Kumb.21:15; Thess 14:36; Yoh 12:25; Rum 9:13)
      - (4) “wote” dhidi ya “wengi”. Linganisha Isa. 53:6 (“wote”) na 53:11 & 12 (“wengi”). Istilahi hizi zina maneno sawa kama Rum 5:18 na 19 kama inavyoonyesha.
  5. Utumiaji wa kifungu cha isimu moja kwa moja badala ya neno moja. Mfano: “Bwana Yesu Kristo”.
  6. Utumiaji maalumu wa neno *autos*
    - a. Wakati likiwa na KIFUNGU (nafasi ya kivumishi angama) kilichofasiliwa “sawa”
    - b. Wakati bila KIFUNGU (nafasi ya kuarifu) kilitafasiliwa kama KIWAKILISHI CHENYE MKAZO CHA KUIJIREJEA- “mwenyewe jinsia ya ME” “mwenyewe jinsia ya KE” au “yenyewe/chenyewe”
- E. Wanafunzi wa Biblia wasio weza soma Kiyunani waweza kutambua mkazo katika Nyanja tofauti:
1. Utumiaji wa misamiati ya kichambuzi na andiko nasaba la Kiyunani/ Kiingereza.



2. Mlinganyo wa fasili za Kiingereza, hasa toka kwa nadharia za fasiri zinazotofautiana. Mfano: ufasiri mlinganyo wa “neno kwa neno” (KJV, NKJV, ASV, NASB, RSV, NRSV) na “mfanano wa karibu” (William, NIV, NEB, REB, JB, NJB, TEV)  
Msaada mzuri hapa ungalikuwa ni ule toka *The Bible in Twenty-Six Translation* kilichochapishwa na Baker.
3. Utumiaji wa *The Emphasized Bible* cha Joseph Bryant Rotherham (Kregel, 1994).
4. Utumiaji wa tafasiri yenyewe.
  - a. *The American Standard Version* ya mwaka 1901
  - b. *Young’s Lateral Translation of the Bible* cha Robert Young (Guardian Press, 1976)

Usomaji wa kisarufi unachosha lakini unafaa kwa ufasiri mzuri. Maelezo hasa sahihi, maoni na mifano inahamasisha na kuwaamusha watu wasiojua Kiyunani kutumia mihitasari ya kisarufi iliyotumiwa kwenye juzuu hii. Hakika maana hizi zimerahisishwa zaidi. Zisingaliweza kutumika katika hali madhubuti nay a kulazimisha, lakini kama ngazi ya kupandia kwenda kwenye uelewa mkubwa wa isimu za Agano Jipya. Kimatumaini maana hizi zitawawezesha wasomaji kuelewa maoni ya msaada mwingine wa usomaji kama vile maoni ya kiufundi juu ya Agano Jipya.

Ni lazima tuweze kuthibitisha ufasiri wetu uliolenga kwenye habari iliyopatikana kwenye maandishi ya Biblia. Sarufi ni moja ya msaada mkubwa wa vipengere hivi, vipengere vingine vingalijumuisha muundo wa kihistoria, maandishi ya kifasihi, utumiaji wa neno la wakati ule ule na dondoo zinazorandana.

# Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi

Somo hili litajikita kwa namna moja kutoa maelezo yanayopatikana katika maoni haya.

Mhutasari ufuatao utahusika

- I. Vyanzo vya maelezo ya Biblia zetu za Kiingereza
    - A. Agano la Kale
    - B. Agano Jipya
  - II. Maelezo mafupi ya matatizo na nadharia ya “maoni dhaifu” pia yanaitwa “uhakiki wa maandiko”
  - III. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya usomaji wa badaye
- I. Vyanzo vya maandiko ya Biblia yetu ya Kiingereza

A. Agano la Kale

1. Machapisho ya kale ya Kiebrania ya karne ya kumi na tisa (MT)-maandiko ya konsonanti za Kiebrania yalipangwa na Rabbi Aquiba miaka 100 Baada ya Kristo. Nukta za irabu na lafudhinukuu za pembeni, vituo vya uandishi na alama za nukta zilizoongezwa katika karne ya sita Baada ya Kristo na vilihitimishwa katika karne ya tisa Baada ya Kristo. Yalifanywa na familia ya wasomi wa Kiyahudi wajulikanao kama Wana-maandiko ya Kale ya Kiebrania. Muundo wa maandiko walioutumia ulikuwa sawa na ule katika Mishnah, Talmud, Targums, Peshitta, na Vulgate.
2. Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania (LXX) –Utamaduni unasema Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania ilitengenezwa na wasomi wa Kiyahudi 70 katika siku 70 katika maktaba ya Alexandria chini ya ufadhili wa Mfalme Ptolemy wa II (285-246 K.K). Tafsiri ilidhaniwa kuwa matakwa ya kiongozi wa Kiyahudi aliyeishi katika Alexandria. Utamaduni huu unatokana na “Herufi Aristeas.” Mara kwa mara Tafsiri ya Agano Kale(LXX) ilijikita katika kutofautiana kwa utamaduni wa maandishi ya Kiebrania kutoka katika maandishi ya Rabbi Aquiba (MT).
3. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (MBC)-Michoro ya Bahari ya Chumvi -iliandikwa huko Ruma kipindi cha K.K(200 Kabla ya Kristo hadi Baada ya Kristo 70) na madhehebu ya Kiyahudi waliojitenga waitwao “ Esene”. Machapisho ya Kiebrania, yalikutwa katika sehemu nyingi kandokando ya Bahari ya Chumvi yakionyesha baadhi ya zile tofauti za machapisho ya familia za Kiebrania nyuma ya Machapisho ya Kale ya Kiebrania (MKK)na Tafsiri za Kale za Kiebrania (70).
4. Baadhi ya mifano ya mahususi ni kwa namna gani ulinganifu wa maandishi haya imewasaidia wakalimani kulielewa Agano la Kale.
  - a. Tafsiri za Kale za Kiebrania zimewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa maandishi ya Kale ya Kiebrania.
    - (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania za Isa. 52:14, “Kama vile wengi watakavyo shangazwa Naye.”
    - (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania ya Isa. 52:14, “Bado kama vile wengi walivyo staaabishwa Nawe.”
    - (3) Katika Isa. 52:15 tofauti ya kiwakilishi cha Tafsiri za Kale za Kiebrania imehakikishwa
      - (a) Tafsiri za Kale za Kiebrania, “hivyo mataifa mengi yatashangazwa naye”
      - (b) Maandishi ya Kale ya Kiebrania, “hivyo yeye ameyatapakaza mataifa mengi”
  - b. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) yamewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa Maandishi ya Kale ya Kiebrania
    - (1) Mafunjo ya Bahari ya Chumvi ya Isa. 21:8, “ndipo akalia Karibu na mlinzi wa mnara nilipo simama.”
    - (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania (MT) ya Isa. 21:8, “ndipo akalia kama simba, Ee Bwana, mimi nasimama daima juu ya mnara wakati wa mchana.....”
  - c. Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) zote zilisaidia kuichuja Isa. 53:11
    - (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari Chumvi (DSS), “Baada ya kutaabika sana, mtumishi wangu atafurahi. Kwa kuwajibika kwake kikimilifu, atatosheka na matokeo hayo.”

- (2) Maandishi ya Kale ya Kale ya Kiebrania (MT), “Ataona ..... ya taabu ya nafsi yake, na kuridhika. Kwa maarifa yake mtumishi wangu mwenye haki Atawafanya wengi kuwa wenye haki.”

#### B. Agano Jipya

1. Maandishi yapatayo 5,300 yote au sehemu za Agano Jipya la Kiyunani yapo hadi leo. Yapatayo 85 yameandikwa katika karatasi za mafunjo na 268 ni maandishi yaliyoandikwa yote kwa herufi kubwa (maandiko adimu) Baadaye, mnamo karne ya tisa B.K., maandishi yaliyo somwa (madogo sana) yalikuswa. Maandishi ya Kiyunani yaliandikwa kutoka namba zipatazo 2,700. Pia tunazo nakala zipatazo 2,100 za orodha ya Machapisho ya maandiko Matakatifu yalitumika katika kuabudu ambayo tunaita misale ya waumini.
2. Machapisho ya Kiyunani yapatayo 85 yaliyokuwa na sehemu za Agano Jipya zilizoandikwa katika karatasi za mafunjo yamejengewa katika makumbusho. Baadhi yao yamewekwa katika kipindi maalumu kutoka karne ya pili B.K., yaliyo mengi ni kuanzia karne za tatu na nne A.D. Hakuna kati ya machapisho ya kale. Hizi zilizo na Agano Jipya Kamili. Hii ni kwa sababu hizi ni nakala za kale za Agano Jipya hazimaanishi kuwa sio ya kujiendesha yenyewe zina tofauti chache. Zilizo nyingizilinuuliwa kwa kasi kwa matumizi ya kawaida. Utunzaji haukuzingatiwa katika utendaji. Hivyo, zina utofauti mwingi.
3. Kitabu cha miswada ya kale chenye maandishi ya Kale ya Kiyunani ya karne ya nne B.K. kinachojulikana kwa herufi ya Kiebrania  $\aleph$  (aleph) au (01), iliyokutwa katika nyumba ya Mt. Katarina juu ya Mlima Sinai na Tischendorf. Tarehe yake imeandikwa kuanzia karne ya nne B.K. iliyokuwa na zote Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na za Agano Jipya la Kiyunani. Ni aina ya “Maandishi ya Kialekzandria.”
4. Kitabu cha miswada ya Kale cha Alekzandrianus, kijulikanacho kama “A” au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayo ilipatikana katika Alekzandria, Misri.
5. Kitabu cha miswada ya Kale cha Machapisho ya Kiyunani cha karne ya nne, kijulikanacho kama “B” au (03), iliyopatikana katika maktaba ya Vatikani katika Roma na imeandikiwa tarehe kuanzia katikati ya karne ya nne B.K. Ina zote Tafsiri za Kale za Kiebrania za Agano la Kale na Agano Jipya la Kiyunani. Yalikuwa aina ya “Maandishi ya Kialekzandria.”
6. Kitabu cha miswada ya kale cha Ephraemi, kijulikanacho kama “C” au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayokwa makusudi yaliaribiwa.
7. Kitabu cha miswada ya Kale cha Bazae, kijulikanacho kama “D” au (05), machapisho ya Kiyunani ya karne ya kwanza ya tano au sita. Ni mwakilishi mkuu wa kile kinachojulikana kama “Maandishi ya Magharibi.” Ina maongezeko mengi ulikuwa ushahidi mkuu wa tafsiri ya Mfalme James.
8. Agano Jipya la machapisho ya kale yanaweza kuwekwa katika makundi matatu, kadria nne, familia ambazo zimeshiriki sifa fulani.
  - a. Maandishi ya Kialekzandria kutoka Misri
    - (1) P<sup>75</sup>, P<sup>76</sup> ( yapata 200 B. K.), ambayo inachukua kumbukumbu ya Injili.
    - (2) P<sup>46</sup> (yapata 225 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya barua za Paulo
    - (3) P<sup>72</sup> (yapata 225-250 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya Petro na Yuda
    - (4) Kitabu cha miswada ya Kale B, kiitwacho Viticanus (mnamo 325 B. K), ambacho kimebeba Agano la Kale zima na Agano Jipya
    - (5) Origen alinukuu kutoka aina hii ya maandiko
    - (6) Machapisho ya kale mengine ambayo yanaonyesha aina hii ya maandishi ni  $\aleph$ , C, L, W, 33
  - b. Maandishi ya Magharibi kutoka Afrika ya Kaskazini
    - (1) alinukuu kutoka wakuu wa kanisa wa Afrika ya Kaskazini, Tertullian, Cyprian, na tafsiri za Kale za Kilatini
    - (2) yalinukuliwa kutoka Irenaeus
    - (3) ilinukuliwa kutoka Kilatini na tafsiri za kale za Kisiria
    - (4) Andiko D la Machapisho ya kale “Baze” ilifuata aina ya maandishi haya
  - c. Byzantine Mashariki kutoka Constantinople
    - (1) aina ya maandishi inaakisiwa katika 80% ya 5,300 MSS

- (2) ilinukuliwa na kanisa la mapadre wa Antiokia ya Silia, Cappadoceans, Chrisostom, natherodoret
- (3) Andiko A la machapisho ya kale, katika Injili tu
- (4) Andiko E la machapisho ya kale, (karne ya nane) ya Agano Jipya
- d. aina ya nne iwezekanayo ni ya “Kikaizari” kutoka Palestina
  - (1) kwanza inaonekana katika Mrko tu
  - (2) baadhi ya shuhuda zake ni P<sup>45</sup> na W

## II. Matatizo na nadharia ya “ukosoaji dhaifu.”

### A. Ni kwa namna gani tofauti zilitokea

1. isio angalifu au bila kukusudia (matukio mengi mno)
  - a. makosa madogo madogo ya macho katika kunakili kwa mkono ambapo ulisomwa mfano wa pili wa maneno yanayofanana na pale ambapo yanaondoa maneno yote katikati (mfanano wa maneno)
    - (1) makosa madogo madogo ya macho katika kuondoa maneno ya herufi jozi au vifungu (urudiaji wa maneno)
    - (2) makosa madogo madogo ya kumbukumbu katika kurudia kifungu au msitari wa maandishi ya Kiyunani (mshabaha ule ule)
  - b. makosa madogo madogo ya masikio katika kunakili maneno ya imla ambapo makosa ya kiuandishi hutokea (itacism). Mara nyingi makosa ya kiuandishi hudokeza au kutaja herufizenye mfanano wa sauti za maneno ya Kiyunani.
  - c. maandishi ya Kiyunani ya kale hayakuwa na sura au mgawanyo wa mistari, chache au alama za uandishi na hakuna mgawanyo kati ya maneno. Inawezekana kuzigawa herufi katika nafasi kuunda maneno tofauti.
2. makusudi
  - a. mabadiliko yalifanywa ili kufanikisha muundo wa kisarufi wa maandishi yaliyo nakiliwa
  - b. mabadiliko yalifanywa ili kuyaleta maandiko katika ulinganifu na maandiko mengine ya kibiblia (mlinganyosambamba)
  - c. mabadiliko yalifanywa kwa kuuunganisha masomo mawili au zaidi yaliyokuwa tofauti katika muungano mmoja wa maandishi marefu (conflation)
  - d. mabadiliko yalifanywa kusahihisha makosa yaliyotambuliwa katika maandishi ( cf. I Kor. 11-27 na I Yohana 5:7-8)
  - e. baadhi ya taarifa za nyongeza kama mpangilio wa kihistoria au ufafanuzi sahihi wa maandishi uliwekwa pembezoni kwa nakala moja lakini zilihamishiwa katika maandishi kwa kuzinakili mara ya pili ( Yohana 5:4)

### B. Mafundisho muhimu ya ukosoaji wa maandiko (mwongozo wa kimantiki ili kubainisha usomaji halisi wa maandishi wakati tofauti inapojitokeza)

1. maandishi ambayo hayakuwa na ustadi zaidi au ambayo hayakuwa muhimu kisarufi yamkini ni halisi
2. maandishi mafupi zaidi yamkini ni halisi
3. maandishi ya kale yamepewa uzito zaidi kwa sababu ya ukaribu wake kihistoria katika uhalisia, kila kitu kuwa sawa zaidi
4. Machapisho ya kale ni namna mbali mbali ya kijiografia mara nyingi yana usomaji halisi
5. Kimafundisho maandishi ya wanyonge, hasa yale yanayohusiana na majadiliano makuu ya kitheolojia ya kipindi cha mabadiliko ya machapisho kama Utatu katika Yohana 5:7-8, yanapaswa kupendelewa.
6. maandishi ambayo yanaweza kuelezea zaidiasili ya tofauti zingine
7. nukuu mbili ambazozinzaidia kuonyesha usawa katika tofauti zinazotaabisha
  - a. kitabu cha J. Harold Greenless, *Introduction to New Testament Textual Criticism*, “Hakuna mafundisho ya Kikristo yanayoning’inia juu ya maandishi yenye kujadiliwa; na mwanafunzi wa Agano wa Jipya anapaswa kuyatambua maandiko yake anayoyataka kuwa mwenye imani zaidi au kuwa mwenye nguvu kimafundisho kuliko msukumo asilia” (uk. 68).

- b. W. A. Criswell alimwambia Greg Garrison ya *The Birmingham News ambayo yeye* (Criswell) haamini kila neno katika Biblia ni la kutia moyo “angalau si kila neno ambalo limekwisha kutolewa kwa alaiki ya kisasa kwa karne za watafsiri.” Criswell alisema “Mimi ni mwamini sana katika ukosoaji wa maandishi. Kama vile, Nafikiri, nusu ya sura ya 16 ya Marko ni uasi: haitii moyo, imebuniwa...Unapolinganisha machapisho hayo kwa kurudi huko nyuma, hakukuwa na kitu kama hicho kama lilehitimisho la Kitabu cha Marko. Mtu fulani alikiongeza...” Mababa wa uzao wa SBC wasio wakoaji walidai kuwa “kutia maneno yasiokuwepo katika kitabu” pia ni dhahiri katika Yohana, uwajibikaji wa Yesu katika bwawa la Bethesda. Na alijadili tofauti mbili za uwajibikaji wa kujinyonga kwa Yuda (Mt. 27 na Matendo 1): “Ni maoni tofauti ya kujinyonga,” Criswell alisema “Kama iko katika Biblia, kuna maelezo yake. Na hatia mbili za kujinyonga kwa Yuda ziko katika Biblia.”Criswell aliongeza, “Ukosoaji wa Maandishi nisayansi ya ajabu ndani yake yenyewe. Si ya muda mfupi kupita, si isiyo husiana.Ni yenye nguvu na kuu...”

### III. Matatizo ya machapisho (ukosoaji wa maandishi)

#### A. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya kusoma zaidi

1. *Biblical Criticism, Historical, Literary and Textual*, na R. H. Harrison
2. *The Textual of the New Testmemt: Its Transmission, Corruption and Restoration*, na Bruce M. Metzger
3. *Introduction to New Testament Txtual Critism*, na J. H Greenlee

## KAULI YA KIMAFUNDISHO

Mimi siangalii hasa habari za imani au kanuni za imani. Napendelea kuthibitisha Biblia yenyewe. Ingawa, natambua kuwa habari ya imani itawaleta wale tusiojuana ili kupima mtizamo wa mafundisho yangu. Katika siku zetu za leo zenye makosa mengi ya kithiolojia na upotofu, natoa muhtsari mfupi wa thiolojia yangu kama ifuatavyo.

1. Biblia, yote katika Agano la Kale na Agano Jipya, ni neno la Mungu lililovuviwa, lenye uhakika, lenye uzima na lenye mamlaka. Ni ufunuo pekee wa Mungu ulioandikwa na watu chini ya uongozi wa nguvu za ajabu. Ni kiini pekee cha ukweli sahihi kuhusu Mungu na Kusudi Lake. Pia ni kiini pekee cha imani na utendaji wa kanisa lake.
2. Kuna Mungu mmoja tu wa uzima, muumbaji na mkombozi. Yeye ndiye muumbaji wa vitu vyote, vionekavyo na visivyo onekana. Amejidhilihisha mwenyewe kama Mungu wa upendo na anayejali ingawa pia ni Mungu asiye na upendeleo. Amejidhilihisha mwenyewe katika nafsi tatu tofauti: Baba, Mwana na Roho; haswa wanatengana lakini wanafanya kazi moja.
3. Muda wote Mungu yuko hai kuangalia ulimwengu huu. Kuna mpango wa milele kwa uumbaji wake usiobadilika na mtazamo wa kipekee unaomfanya binadamu kutenda mapenzi huru. Hakuna kinachoweza kutokea pasipo ruhusa na maarifa ya Mungu, bado anaruhusu uchaguzi kwa wote malaika na wanadamu. Yesu ni chaguo la Baba na wote kimanufaa wamechaguliwa katika Yeye. Ufahamu wa mbele wa Mungu kuhusu matukio hayampunguzii binadamu kubainisha maandiko yaliyoandikwa kabla. Wote tunahusika kwa mawazo yetu na matendo.
4. Binadamu, japo aliumbwa kwa sura ya Mungu na mbali na dhambi, aliamua kumwasi Mungu. Ingawa alijaribiwa na kitu chenye nguvu ya ziada. Adamu na Hawa waliwajibika kwa utashi wao wenyewe kuamua. Uasi wao umeathiri utu wa uumbaji. Watu wote tunahitaji rehema na huruma ya Mungu yote kwa hali ya ushirika katika Adamu na uasi binafsi wa hiari.
5. Mungu anatoa aina ya msamaha na urejesho kwa binadamu aliyeanguka. Yesu Kristo, Mwana pekee wa Mungu Baba, akawa mwanadamu, akaishi maisha yasio na dhambi, na kwa kifo chake mbadala, akalipa malipo ya dhambi ya mwanadamu. Ndiyo njia pekee ya kurejesha ushirika wetu na Mungu. Hakuna njia nyingine ya wokovu isipokuwa kupitia imani ya kazi yake aliyoimaliza.
6. Kila mmoja wetu binafsi yampasa kupokea ahadi ya msamaha na urejesho katika Kristo. Hilo linatimizwa kwa njia ya imani ya hiari katika ahadi za Mungu kupitia Kristo Yesu na kugeuka kwa mapenzi huru kwa dhambi inayojulikana.
7. Sisi sote tumesamehewa jumla na urejesho umelenga juu ya kuamini katika Kristo na toba toka dhambini. Ingawa, ushahidi wa mahusiano mapya unaonekana katika mabadiliko na badiliko endelevu. Dhumuni la Mungu kwa wanadamu sio tu kwenda mbinguni siku moja, lakini kufanana na Kristo kwa sasa. Wale wote ambao wanakombolewa kweli ingawa wakati mwingine wanatenda dhambi, wataendelea katika imani na toba siku zao zote za maisha.
8. Roho Mtakatifu ni “Yesu mwingine”. Yuko duniani kuwaongoza wale wote waliopotea katika Kristo na kujenga ufanano wa Kristo katika kuokolewa. Karama za rohoni zinapewa toka kwenye wokovu. Ni maisha na huduma ya Yesu yaliyogawiwa katika mwili wake, yaani kanisa. Vipawa 358 ambavyo kimsingi ndio mwelekeo na msukumo wa hitaji la Yesu likihamasishwa na tunda la Roho. Roho yu hai katika siku zetu kama alivyokuwa katika enzi za Biblia.
9. Baba amemfanya Yesu Kristo aliyefufuka kama mwamuzi w vitu vyote. Atarudi duniani kuhukumu wanadamu wote. Wale wote walioamini Yesu na majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo watapata mwili na utukufu ataporudi. Wataishi nae milele. Ingawa, wale wote walioikataa

kweli ya Mungu watatengwa milele toka katika furaha ya ushirika wa Mungu wa Utatu. Watahukumiwa pamoja na shetani na malaika zake.

Hii hakika haijaisha au kukamilika lakini natarajia itakupa ladha ya kithiolojia ya moyo wangu, nafurahia maelezo:

“Katika mambo ya msingi-umoja, mambo yaliyo ukingoni-uhuru, katika mambo yote-upendo.”